
USHINDI WA UPENDO
WA MUNGU
E.G. White

# USHINDI WA UPENDO

# WA

# MUNGU

*Ellen G. White*

1911

YALIYOMO


**WALIOFANIKISHA KAZI**

**Maneno Ya Wafanikishaji Wa Kazi Pamoja Na Ushauri Kwa Msomaji**

**MUHTASARI WA KITABU NJIA SALAMA (STEPS TO CHRIST)**

**DIBAJI**

**SURA YA 1**

**KUHARIBIWA KWA YERUSALEMU……………………………………………1**

**SURA YA 2**

**MATESO KATIKA KARNE ILE YA KWANZA………………………………18**

**SURA YA 3**

**ZAMA ZA GIZA LA KIROHO……………………………………………………27**

**SURA YA 4**

**WAWALDENSIA/WAVODWA…………………………………………………39**

**SURA YA 5**

**JOHN WYCLIFFE (1328-1415)…………………………………………………56**

**SURA YA 6**

**HUSS NA JEROME………………………………………………………………74**

**SURA YA 7**

**KUJITENGA KWA LUTHER KUTOKA RUMI………………………………95**

**SURA YA 8**

**LUTHER MBELE YA BARAZA………………………………………………120**

**SURA YA 9**

**MWANAMATENGENEZO WA USWISI……………………………………144**

**SURA YA 10**

**MAENDELEO YA MATENGENEZO UJERUMANI…………………………157**

**SURA YA 11**

**UPINZANI WA WAKUU WABADILI MWELEKEO………………………168**

**SURA YA 12**

**MATENGENEZO KULE UFARANSA…………………………………………182**

**SURA YA 13**

**UHOLANZI NA SCANDINAVIA………………………………………………208**

**SURA YA 14**

**WANAMATENGENEZO WA BAADAYE WA UINGEREZA………………216**

**SURA YA 15**
**BIBLIA NA MAPINDUZI YA UFARANSA……………………………………235**
**SURA YA 16**
**WASAFIRI WA IMANI WALIOTAFUTA UHURU KATIKA NCHI MPYA ……………………………………………………………………………………261**
**SURA YA 17**
**AHADI ZA MAREJEO YA KRISTO…………………………………………271**
**SURA YA 18**
**NURU MPYA KATIKA ULIMWENGU MPYA………………………………287**
**SURA YA 19**
**NURU KUPITIA GIZANI…………………………………………………312**
**SURA YA 20**
**UAMSHO MKUU WA KIDINI……………………………………………323**
**SURA YA 21**
**ONYO LAKATALIWA……………………………………………………342**
**SURA YA 22**
**UNABII WATIMIZWA……………………………………………………358**
**SURA YA 23**
**PATAKATIFU NI NINI?…………………………………………………374**
**SURA YA 24**
**NDANI YA PATAKATIFU PA PATAKATIFU………………………………387**
**SURA YA 25**
**SHERIA YA MUNGU ISIYOBADILIKA……………………………………396**
**SURA YA 26**
**WATETEZI WA ILE KWELI………………………………………………413**
**SURA YA 27**
**UAMSHO WA KISASA……………………………………………………423**
**SURA YA 28**
**KUKABILIANA NA KUMBUKUMBU YA MAISHA…………………………438**
**SURA YA 29**
**CHIMBUKO LA UOVU……………………………………………………450**
**SURA YA 30**
**UADUI KATI YA MWANADAMU NA SHETANI, UNABII WA KWANZA. ……………………………………………………………………………………462**

**SURA YA 31**
**UTENDAJI WA PEPO WABAYA……………………………………………468**
**SURA YA 32**
**MITEGO YA SHETANI…………………………………………………474**
**SURA YA 33**
**UDANGANYIFU WA KWANZA MKUBWA…………………………………487**
**SURA YA 34**
**JE! WATU WETU WALIOKUFA (WAFU) WANAWEZA KUSEMA NASI?506**
**SURA YA 35**
**UHURU WA DHAMIRI WATISHIWA………………………………………516**
**SURA YA 36**
**PAMBANO LINALOTARAJIWA HIVI KARIBU……………………………535**
**SURA YA 37**
**MAANDIKO NDIYO USALAMA WETU PEKEE……………………………546**
**SURA YA 38**
**(UJUMBE NA ONYO LA MWISHO)…………………………………………556**
**SURA YA 39**
**WAKATI WA TAABU…………………………………………………565**
**SURA YA 40**
**WATU WA MUNGU WAKOMBOLEWA…………………………………583**
**SURA YA 41**
**UKIWA WA DUNIA…………………………………………………599**
**SURA YA 42**
**MWISHO WA PAMBANO………………………………………………607**
**Kiambatanisho…………………………………………………………622**
**Hoja Muhimu Za Kitabu Cha Pambano Kuu…………………………………645**

# WALIOFANIKISHA KAZI HII

Wengi wamehusika kusaidia hii kazi, kwa maombi, Kutafsiri, kuhariri, kutia moyo, kusaidia mambo ya kiufundi n.k

Grace Momadi Masaka
Godfrey Herman Herra
John Mugane
Judi Mmari
Moses Ambonisye Mwalumbili
Gerard Makori Nyafanga
Mbusi Mpagalushu
Ibrahim Makamba
Shilagale Mloganzala
Nyang'oro Mahamba
Charles Sebastian
Emanuel Munisi
Jemima Nyafanga Kivunge
Onesmo Emmanuel
Mwl. Peter Marwa
Pendo Makori Momadi
Joyce Manka Mmari
Stefano Kasiri

Musa L Budodi
Isaac Kannuda Gama
Faustine Mkama
Joseph Mickey Marr
Daudi Jabez Masaka
Paulo Momadi Masaka
John Chilala Momadi
Gibson Wilson Mujuni
Robert Ndinayo
Rudy Harnisch
Paulina Bisieri Masaka
Elias Kasika
Dorothy Mokua Onyonka
Cindy Tutsch
Sandra Barron
Chuaro Shinywane Zuzo
Ron na Pat Goss.
Daniel Nyangaresi Masaka

# Maneno Ya Wafanikishaji Wa Kazi Pamoja Na Ushauri Kwa Msomaji

Kitabu hiki kimetafsiriwa kuwa majina mawili yaani **Pambano Kuu** au **Ushindi wa Upendo wa Mungu** kutoka katika toleo la Kiingereza la **The Great Controversy (GC)** au **God's Triumphant Love**. Badala ya kuishia tu kusema **Pambano Kuu (PK)**, imekuwa vyema pia kuonyesha kwamba ni kweli kuna Pambano Kuu lakini katikati ya Pambano hilo kuna upendo wa Mungu usio na kifani lakini pia katikati ya pigano hilo Mungu daima Ndiye Mshindi dhidi ya Adui Mkuu. Hivyo, kwa kila kichwa kikuu cha sura kuna kichwa kidogo chini yake kilicho ndani ya mabano. Mwanzoni mwa kila sura kuna muhtasari kuhusiana na sura hiyo. Baada tu ya sura ya mwisho ya kitabu hiki kunafuata maswali toka katika kila sura ambayo ni mwongozo wa kujifunzia (Study Guide). Tumefanya hivi kuongeza uelewa wa kitabu.

Katika toleo la Kiswahili la kitabu hiki, mpangilio wa namba za Aya uko hivi; ukiachana na maelezo mengine bali kwa kuanzia hasa kwenye sura zenyewe za kitabu, kila Sura ina idadi ya Aya ambapo mwishoni mwa kila Aya kuna mafungu mawili ya namba:

- Fungu la awali ni namba ya Aya kulingana na mpangilio wa Aya katika toleo la Kiingereza (**mfano; GC 132.3**) na
- Fungu la pili ni namba ya Aya kulingana na mfuatano wa Aya toka mwanzo wa Sura hadi mwisho wa Sura hiyo (**mfano; PK Aya ya 8**).

Hivyo, ukiwa unataka kunukuu aya yo yote, anza na jina la kitabu, inafuata sura ya kitabu ilipo aya hiyo na kisha anza kuhesabu aya zote toka mwanzoni mwa sura mpaka utakapoifikia aya unayotaka kuinukuu. Hii itarahisisha kuhifadhi kumbukumbu na itakuwa rahisi kumshirikisha mtu kuhusiana na aya hiyo.

Mpangilio huu ni tofauti na kunukuu kwa kufuata ukurasa kwani utafsiri hutofautiana kwa mtu mmoja na mwingine, lakini pia uongezeaji wa maelezo fulani hufanya yaliyomo kutofautiana katika kurasa yalipo.

Katika toleo hili, neno "volume" limetafsiriwa kama 'gombo," na wakati mwingine limetumika kwa kubadilishana na neno "juzuu"

**Vifupisho**

GC—Great Controversy
PK—Pambano Kuu
SG—Study Guide

SC—Steps to Christ

Vita ya muda mfupi kupita zote ilipiganwa kwetu hapa Zanzibar Mwaka 1896 kwa dakika 38 tu, kati ya Oman na Uingereza. Sultani wa Oman alijisalimisha na Waingereza wakakichukua kisiwa hicho. Vita kubwa na ya muda mrefu kupita zote ilianzia mbinguni ambapo Shetani alitaka kumpindua Mungu na achukue uongozi (Ufunuo 12). Alishindwa vita hivyo na akatupwa chini hapa, na yupo kibaruani zaidi ya miaka 6000 na bado hajajisalimisha mpaka leo. Nia yake ni kumfanya mwanadamu awe upande wake katika vita ili wapate adhabu naye, karamu ya adhabu yake ya mwisho aliandaliwa mwenyewe tu, hivyo hatuna haja kwenda kwenye karamu tusiyoalikwa (gatecrash). Silaha Saba za Waefeso sita ni lazima zivaliwe na kila anayetaka kushinda. Tunapenda Kumshukuru Mungu kwa Msaada Wake mkubwa wa kazi hii. Muhtasari wa Biblia ni maneno matatu tu-(Uumbaji, Maanguko, Ukombozi)-Uumbaji katika Mwanzo moja na mbili, Maanguko katika Mwanzo tatu na Ukombozi, ni kuanzia Mwanzo Nne Mpaka Ufunuo ishirini na mbili. Mungu analeta manabii nao wanapigwa vita mwishowe anamleta Mwanawe, Naye anazaliwa na kuishi na Kufa, na kupaa, na sasa anafanya kazi ya upatanishi, na kutuombea kutokana na kitabu cha Waebrania 8-10, na hivi karibuni atatokea kwenye Mawingu. Tunaona viashiria vingi vya Yeye kutokea hivi punde. Kitabu hiki ni cha kila binadamu kukisoma, hasa kwa wakati huu tunaoishi. Tuombeane. Tunakaribia nyumbani! MASIHI Anakuja upesi! Ukiwa na mashaka na Historia yoyote ya Biblia mfano Danieli, tafuta vitabu vya historia halisi kama vile vya mitaala ya shule au google mtandaoni ili uthibithishe mwenyewe! Historia ya Dunia kama falme zilizotawala dunia yote iliyojulikana n.k. Biblia inaendana na historia ya mwanadamu na ndicho kitabu cha dini pekee ambacho kinaendana na historia ya kweli ya mwanadamu. Mwanadamu, historia hii ni pungufu ya miaka 6000. Maana katika kila nchi watu huanza kusoma kuhusu Mesopotamia kama historia iliyothibithishwa, miaka 5000+ iliyopita, hawataji mwaka wa milioni moja nini kilitokea au 3,000,000 KK! Biblia ndiyo kitabu pekee cha Maandishi ya Kale chenye kukubalika na kuaminiwa zaidi, katika kusema Ukweli (the most authentic document in ancient writings-Luka na Matendo vilichukuliwa kuthibithisa jambo hili)

Ikiwa tuna muda wa kuomba, Mungu atatujibu. Maombi haya matatu yanakuja na baraka zote:

1. Roho Mtakatifu
2. Kujisalimisha kwa MUNGU na
3. Kuwa ndani Yake Mungu.

Basi mambo muhimu kwa Kila Mwanadamu ni haya saba tukimsubiri Masihi

1. Kumkiri Mungu na kutubu dhambi zetu
2. Kusali daima

3. Kusoma Neno Lake Mungu Kila siku
4. Kuishi mtindo wa maisha kutokana na Maandiko
5. Kuwaambia wengine habari Njema yaani Ukweli
6. Kuhudhuria ushirika unaofuata Maandiko
7. Huduma za Jamii

Ni shukrani kuu kufikia hatua hii ya kazi, kwani ni kitabu kigumu kilichochukua miaka kushughulikia! Ni matumaini yetu kuwa utakapokipata kitabu hiki utakisoma kwa bidii na kwa kweli utamaduni wa kujisomea/kujifunza unapaswa upaliliwe, hivyo fanya kila juhudi—Yohana 17:3! Shukrani kwa nakala za mtandaoni za Kingereza na Kiswahili zilizorahisishwa, hizi zilitusaidia sana kwani lugha ya kitabu hiki ni ya unabii na ya zamani na pia maneno mengi ambayo hayapo Kiswahili, na mengine ni ya kidini/kiroho na yasiyotumika mara nyingi. Mfano Holy see (Santa Sede) ambayo ni Serikali ya Kanisa la Rumi, hivi ni vile wanavyojiita wenyewe au utawala wa hierakia (hierachy). Pia maneno ya Kingereza mengi yalibidi yashikwe na maneno ya kiswahili kadhaa, mfano Debauchery na Despot na corruption n.k. Maneno haya yana maana tofauti tofauti Kingereza ila yanaelekea kusemwa kwa neno moja tu Kiswahili.

Maneno Ushirikina (Superstition) na Upagani leo yana maana tofauti kidogo na miaka ya zamani. Wapagani wa asili walikuwa wafuasi wa dini ya kale iliyoabudu miungu kadhaa (miungu mingi au Polytheism). Leo, upagani ni mpana zaidi—m hutumika kuelezea mtu ambaye haendi kwenye sinagogi, kanisa, au msikiti. Huenda ikawa wanaabudu miungu kadhaa kwa wakati mmoja, au hawapendezwi na mungu ye yote hata kidogo. Hii inaweza kuwa wale watu wa dunia ambao Kingereza tunasema Secular. Ushirikina ni zaidi ya kuamini hadithi za umizimu bali pia ni kuogopa laana/kulaaniwa, wachawi, au mapokeo na mila ambazo zinatisha watu ambao hawaamini nguvu za Yesu kuwakomboa kutoka kwa Shetani, au laana/kulaaniwa.

Tunashauri ukiwa na muda Kuangalia vitabu/video za Theodicy kuhusu Upendo na Haki ya Mungu mfano ni video/maandishi ya Mchungaji John Peckham kuhusiana na Pambano Kuu, Vita inaendelea na kuna sheria katika vita hii (Rules of engagement). Toka uumbaji, Maanguko ya binadamu na Wokovu wake vita hivi vinaonekana katika Biblia kwa uwazi kabisa. Tunakaribia nyumbani! “Roho na Bibi arusi waseme, “Njoo!” Kila mtu asikiaye hili, na aseme, “Njoo!” Aliye na kiu na aje; anayependa, na achukue maji ya uhai bila malipo. Naye anayetoa ushahidi Wake juu ya mambo haya asema: “Kweli Naja upesi.”Amina. Njoo Bwana Yesu! Nawatakieni nyote neema ya Bwana Yesu. Amina.”

Grace Momadi-Masaka na Daniel Masaka, Samaritan Laymen Ministries, New Jersey.

# **MUHTASARI WA KITABU NJIA SALAMA** (STEPS TO CHRIST)

Sehemu ya I

**Ninawezaje Kuja Kwa Kristo?**

Asili na ufunuo wa Mungu kwa wanadamu vyote kwa pamoja hushuhudia upendo wa Mungu. Ni uvunjaji (uasi) wa Sheria ya Mungu - Sheria ya upendo – ndio kwamba umeleta misiba na kifo. Lakini hata katikati ya mateso yanayotokana na dhambi, upendo wa Mungu unafunuliwa. “Mungu ni upendo” imeandikwa juu ya kila chipukizi, juu ya kila unyasi unaochipuka.

Yesu alikuja kuishi miongoni mwa wanadamu ili kudhihirisha upendo wa Mungu usio na kikomo. Upendo, rehema, na huruma zilikuwa zimefunuliwa katika kila tendo la maisha Yake; Moyo Wake ulikwenda kwa huruma nyororo kwa watoto wa wanadamu. Alichukua asili ya mwanadamu, ili Aweze kufikia matakwa ya mwanadamu. Maskini na wanyenyekevu zaidi hawakuogopa kumkaribia Yeye. Hiyo ndiyo tabia ya Kristo kama inavyofunuliwa katika maisha Yake. Hii ndiyo tabia ya Mungu.

Ilikuwa ni kwa ajili ya kutukomboa ambapo Yesu aliishi, aliteseka, na kufa. Alifanyika “Mtu wa Huzuni,” ili sisi tupate kufanywa washirika wa furaha ya milele. Lakini dhabihu hii kuu haikutolewa ili kuunda katika Moyo wa Baba upendo kwa mwanadamu, sio kumfanya awe tayari kutuokoa. Hapana, hapana! “Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa Mwanawe pekee.” Yohana 3:16. Baba anatupenda, si kwa sababu ya upatanisho mkuu, bali Alitoa upatanisho kwa sababu anatupenda. Hakuna mwingine ila Mwana wa Mungu Ndiye Ambaye angeweza kutimiza ukombozi wetu.

Hii inaweka thamani iliyoje kwa mwanadamu! Kupitia uasi, wana wa binadamu wanakuwa raia wa Shetani. Kupitia imani katika dhabihu ya upatanisho ya Kristo, wana wa Adamu wanaweza kuwa wana wa Mungu. Upendo usio na kifani wa Mungu kwa ulimwengu ambao haukumpenda! Mawazo yana nguvu ya kutiisha juu ya nafsi na huleta akili katika utumwa wa mapenzi ya Mungu.

Mwanadamu hapo awali alijaliwa uwezo wa kiungwana na akili iliyo na usawa mzuri. Alikuwa mkamilifu katika nafsi yake, na kupatana na Mungu. Mawazo yake

yalikuwa safi, malengo yake yalikuwa matakatifu. Lakini kwa kutokutii, nguvu zake zilipotoshwa, na ubinafsi ukachukua nafasi ya upendo. Asili yake ilidhoofika sana kupitia dhambi ambayo haikuwezekana kwake, kwa nguvu zake mwenyewe, kupinga nguvu za uovu.

Haiwezekani sisi, sisi wenyewe, kuepuka shimo la dhambi ambalo tumezama ndani yake. Mioyo yetu ni miovu, na hatuwezi kujibadilisha. Lazima kuwe na nguvu inayofanya kazi kutoka ndani, maisha mapya kutoka juu, kabla ya wanadamu kubadilishwa kutoka katika dhambi hadi utakatifu. Nguvu hiyo ni Kristo. Neema Yake pekee ndiyo inayoweza kuhuisha uwezo usio na uhai wa nafsi, na kuivuta kwa Mungu, kwa utakatifu. Kwa wote, kuna jibu moja tu, Tazama Mwana-Kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu." Yohana 1:29. Hebu na tuikubali njia hii iliyotolewa kwa ajili yetu ili tuweze kugeuzwa na kufanana Naye, na kurejeshwa katika ushirika na malaika wanaohudumia, kwa maelewano na ushirika na Baba na Mwana.

Mtu atakuwaje mwenye haki mbele za Mungu? Mwenye dhambi atafanywaje kuwa mwadilifu? Ni kwa njia ya Kristo pekee tunaweza kuletwa katika mapatano na Mungu, kwa utakatifu; lakini tunawezaje kumwendea Kristo?

Toba ni pamoja na huzuni kwa ajili ya dhambi na kuiacha. Hatutaacha dhambi mpaka tuone ubaya wake; mpaka tuiache kwa moyo, hakutakuwa na mabadiliko ya kweli katika maisha. Lakini moyo unapokubali kuongozwa na Roho wa Mungu, dhamiri itahuishwa, na mwenye dhambi atatambua jambo fulani la kina, na utakatifu wa Sheria takatifu ya Mungu, na msingi Wa serikali Yake mbinguni na duniani. Kisha usadikisho hushika akili na moyo.

Ombi la Daudi, baada ya anguko lake, linaonyesha asili ya huzuni ya kweli kwa ajili ya dhambi. Toba yake ilikuwa ya dhati na ya kina. Hakukuwa na jitihada za kutuliza hatia yake; hakuwa na hamu ya kutoroka hukumu inayomtishia ila aliongozwa katika maombi yake. Daudi aliona ukubwa wa kosa lake; aliona unajisi wa nafsi yake; yeye aliichukia dhambi yake. Haikuwa kwa ajili ya msamaha tu kwamba aliomba, lakini kwa ajili ya usafi wa moyo. Alitamani furaha ya utakatifu, kurejeshwa katika maelewano na ushirika na Mungu.Toba kama hii haiwezi kufikiwa na uwezo wetu wenyewe na kuikamilisha; bali hupatikana tu kutoka Kristo.

Kristo Yuko tayari kutuweka huru kutokana na dhambi, lakini halazimishi nia hiyo. Tukikataa anaweza kufanya nini zaidi? Jifunze Neno la Mungu kwa maombi. Unapoona ukubwa wa dhambi, kama unavyojiona jinsi ulivyo, usikate tamaa kwa kupoteza matumaini. Ni wenye dhambi ndio ambao Kristo alikuja kuwaokoa. Shetani anapokuja kukuambia kuwa wewe ni mwenye dhambi mkuu, mtazame Mkombozi wako na uongee juu ya wema Wake. Ikiri dhambi yako, lakini

mwambie adui kwamba “Kristo alikuja ulimwenguni kuwaokoa wenye dhambi” ili mimi nipate kuokolewa (1 Timotheo 1:15).

“Afichaye dhambi zake hatafanikiwa, bali yeye aziungamaye na kuziacha atapata rehema.” Mithali 28:13. Masharti ya kupata rehema ya Mungu ni rahisi na ya haki na busara. Ungameni dhambi zenu kwa Mungu, Ambaye peke Yake Ndiye anayeweza kuwasamehe, na msameheane makosa yenu ninyi kwa ninyi. Wale ambao hawajanyenyekesha nafsi zao mbele za Mungu, kwa kukiri hatia yao, bado hawajatimiza hatua ya kwanza ya kukubalika sharti tuwe tayari kunyenyekesha mioyo yetu na kufuata masharti ya Sheria ya Neno la Kweli. Kukiri ambako kumiminiwa kwa roho ya ndani hupata njia yake kwa Mungu wa huruma Asiye na kikomo. Kuungama kwa kweli siku zote huwa na tabia maalum, na hukubali dhambi fulani. Maungamo yote yanapaswa kuwa ya uhakika na ya kulenga jambo mahususi. Imeandikwa, “Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote.” 1John 1:9.

Ahadi ya Mungu ni, “Mtanitafuta na kuniona, mtakaponitafuta kwa mioyo yenu yote.” Yeremia 29:13. Moyo wote sharti utolewe, au mabadiliko hayawezi kamwe kufanywa ndani yetu ambayo kwayo tunapaswa kurejeshwa kwa mfano Wake.

Vita dhidi ya nafsi ni vita kubwa zaidi kuwahi kupiganwa. Kujitolea kwa nafsi, kusalimisha Mapenzi yetu yote kwa Mungu, inahitaji mapambano; lakini nafsi inapaswa kunyenyekea kwa Mungu kabla ya kufanywa upya katika utakatifu. Katika kujitoa kwa Mungu, ni lazima kuacha yote ambayo yangetutenganisha Naye. Kuna wale wanaodai kumtumikia Mungu huku wakitegemea juhudi zao wenyewe kutii Sheria Yake, ili kuunda tabia sahihi na kupata wokovu. Mioyo yao haiguswi na hisia yoyote ya kina ya upendo wa Kristo, lakini wanatafuta kutekeleza majukumu ya maisha ya Kikristo kama vile ambavyo Mungu anataka kutoka kwao ili kuipata mbingu. Dini kama hiyo haina thamani.

Kristo akikaa ndani ya moyo, roho itajawa na upendo Wake, na furaha ya kuungana Naye, kwamba roho itashikamana Naye; na katika kumfikiria Yeye, nafsi itasahauliwa. Upendo kwa Mwenyezi Mungu utakuwa chemchemi ya Kila wazo na tendo. Mambo hayo hayalengi viwango vya chini kabisa, bali hulenga kupatana kikamilifu na Mapenzi ya Mkombozi wao.

Je, unahisi kwamba ni dhabihu kubwa sana kutoa yote kwa Kristo? Jiulize swali, “Ni nini Kristo ametoa kwa ajili yangu?” Mwana wa Mungu alitoa maisha yake yote, kwa upendo na akapitia mateso kwa ajili ya ukombozi wetu. Je, sisi, tusiostahili, ambao ni walengwa wa upendo mkuu hivyo, tutazuia mioyo yetu Kwake? Je, Tunatoa nini zaidi wakati tunatoa yote? Ni Moyo uliochafuliwa na dhambi tu, ndiyo tunatoa na hakuna lingine la thamani tunalolitoa kwa Mungu,

tunautoa moyo huu, ili Yesu ausafishe, ausafishe kwa damu Yake Mwenyewe, na kutuokoa kwa upendo Wake usio na kifani. Na ajabu ni kwamba, bado watu wanafikiri ni vigumu kuacha yote! (na kumbe kile tunachokiacha ni moyo mchafu tu). Mungu hataki tutoe chochote ambacho ni cha manufaa kwetu ili tubaki salama. Katika yote anayofanya, Yeye ana maslahi ya watoto Wake katika mtazamo Wake.

Wengi wanauliza, “Nifanyeje kujisalimisha kikamilifu kwa Mungu?” Unatamani kujitoa Kwake, lakini u dhaifu katika uwezo wa kimaadili,una utumwa wa mashaka, na unatawaliwa na tabia za maisha ya dhambi. Ahadi na maazimio yako ni kama kamba za mchanga. Huwezi kudhibiti mawazo yako, misukumo yako, na mapenzi yako. Ujuzi ulio nao kuhusu ahadi zako zilizovunjwa na ahadi ulizopoteza hudhoofisha kujiamini kwako katika unyofu wako mwenyewe, na kukufanya uhisi kwamba Mungu hawezi kukukubali; lakini huna haja kukata tamaa.

Unachohitaji kuelewa ni nguvu ya kweli ya uthubutu (uchaguzi). Hii ndiyo nguvu inayotawala katika asili ya mtu, nguvu ya uamuzi, au ya kuchagua. Kila kitu kinategemea hatua sahihi ya uthubutu. Nguvu ya uhuru wa kuchagua ambao Mungu amewapa wanadamu; ni juu ya hii unapaswa kuifanyia mazoezi. Huwezi kubadilisha moyo wako, na huwezi kujibadili wewe mwenyewe, kwahiyo mpe Mungu mapenzi (matamanio) ya moyo wako; lakini unaweza kuchagua kumtumikia. Unaweza kumpa mapenzi yako; Naye Atafanya kazi ndani yako kutaka na kutenda sawasawa na mapenzi Yakemema. Kwa hivyo asili yako yote itaweza kuletwa chini ya udhibiti wa Roho wa Kristo; mapenzi yako yataelekezwa Kwake, mawazo yako yatakuwa sawa na Yeye.

Matamanio ya kuwa na wema na utakatifu ni sawa kadiri yanavyokwenda; lakini ukiishia hapa, hautafaidika kwa chochote. Wengi watapotea huku wakitumaini na kutamani kuwa Wakristo. Hawafikii hatua ya kuweka mapenzi yao kwa Mungu. Hawachagui sasa kuwa Wakristo.

Kupitia mazoezi sahihi ya uthubutu, mabadiliko yote yanaweza kufanywa katika maisha yako. Utakuwa na nguvu kutoka juu ili kukuweka imara, na hivyo kupitia kuendelea kujitoa daima kwa Mungu utawezeshwa kuishi maisha mapya, hata maisha ya imani.

Kwa vile dhamiri yako imehuishwa na Roho Mtakatifu, umeona kitu juu ya uovu/ubaya wa dhambi, na nguvu zake, hatia yake, na majanga yake; na sasa unaitazama dhambi kwa chuki. Ni amani ndiyo unayohitaji. Umeungama dhambi zako, na kuziweka mbali na moyo wako. Umeamua kujitoa kwa Mungu. Sasa nenda Kwake, na umwombe kwamba akuoshe dhambi zako na kukupa moyo mpya.

Basi amini kwamba Yeye Anafanya hivi kwa sababu ameahidi hivyo. Zawadi ambayo Mungu anatuahidi, ni sharti tuamini kwamba tunaipokea, na kwamba ni zetu. Wewe ni mwenye dhambi. Huwezi kulipia dhambi zako zilizopita; huwezi kuubadili moyo wako na kujifanya kuwa mtakatifu. Lakini Mungu anaahidi kufanya haya yote kwa ajili yako kupitia Kristo. Wewe amini tu ahadi hiyo. Tubu dhambi zako na kujitoa kwa Mungu. Utapenda kumtumikia. Vile vile unapofanya hivi, hakika Mungu atatimiza Neno Lake kwako. Ikiwa unaamini katika ahadi hiyo, Mungu anaitoa kwako kweli (kiuhalisia). Usisubiri mpaka uhisi kuwa umefanywa mzima, lakini sema, "Naamini; ni hivyo, si kwa sababu ninaihisi, bali kwa sababu Mungu "Aliahidi."

## Sehemu ya II

### Ninawezaje Kubaki Mkweli kwa Kristo?

Yesu anasema, "Yoyote myaombayo mkisali, amininini ya kwamba mnayapokea, nayo yatakuwa yenu." Marko 11:24. Kuna sharti kwa ahadi hii - kwamba tuombe sawasawa na Mapenzi ya Mungu. Lakini ni Mapenzi ya Mungu kutusafisha na dhambi zetu, kutufanya watoto Wake, na kutuwezesha kuishi maisha matakatifu. Hivyo tunaweza kuomba baraka hizi, na kuamini kwamba tunazipokea, na kumshukuru Mungu kwamba tumepokea ahadi hizo.

Tangu sasa ninyi si mali yenu wenyewe; mmenunuliwa kwa bei kubwa. Kupitia tendo hili rahisi la kumwamini Mungu, Roho Mtakatifu amezaa maisha mapya ndani ya moyo wako. Wewe ni mtoto aliyezaliwa katika familia ya Mungu, na Yeye anakupenda kama vile anavyompenda Mwanawe.

Sasa kwa kuwa umejitoa kwa Yesu, usirudi nyuma tena, usijiondoe Kwake, lakini siku baada ya siku sema, "Mimi ni wa Kristo, nimejitoa Kwake," na umwombe Akupe Roho Wake ili Akutunze kwa neema Yake. Kama ilivyo, unapojitoa kwa Mungu, na kumwamini, basi, unakuwa mtoto Wake, ndivyo na wewe wanapaswa kuishi ndani Yake.

Hapa ndipo maelfu wanaposhindwa; hawaamini kwamba Yesu anasamehe kila nafsi,yaani mtu mmoja mmoja. Hawamtilii maanani Mungu katika Neno Lake. Ni fursa ya wote wanaotii masharti kujua wenyewe kwamba msamaha unatolewa kwa kila dhambi. Ondoa shaka kwamba ahadi za Mungu hazikukusudiwa kwa ajili yako.Ahadi za Mungu zipo kwa ajili ya kila nafsi inayotubu. Inueni macho juu, ninyi wenye mashaka na kutetemeka; kwa maana Yesu Yu hai ili atuombee. Mshukuruni Mungu kwa ajili ya zawadi ya Mwanawe mpendwa.

"Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya, ya kale yamepita; tazama, mambo yote yamekuwa mpya." 2 Wakorintho 5:17. Huenda mtu asiweze kutaja wakati au mahali hasa, au kufuatilia mlolongo wote kwamba

mambo yalikuwaje katika huu mchakato wa uongofu; lakini hii haithibitishi kuwa wewe haujaongoka.

Mabadiliko yataonekana katika mwenendo, tabia, na utendaji wako. Tofauti itakuwa wazi na kuamuliwa kati ya vile ambavyo ulivyo sasa na ulivyokuwa. Nani ana moyo wako? Mawazo yetu yanamilikiwa na nani? Je, tunapenda kuzungumza juu ya nini au nani? Ni nani aliye na upendo wetu makini na nguvu zetu bora zaidi? Ikiwa sisi ni wa Kristo, mawazo yetu yapo pamoja Naye. Hakuna uthibitisho wa toba ya kweli isipokuwa inafanya kazi ya matengenezo.

Uzuri wa tabia ya Kristo utaonekana kwa wafuasi Wake. Ilikuwa furaha Yake Masihi kufanya Mapenzi ya Mungu. Kuna makosa mawili ambayo watoto wa Mungu hasa wanatakiwa kujilinda nayo: La kwanza ni lile la kujivunua kazi zao wenyewe, kujiamini kuwa wao wanaweza kufanya kitu fulani, ili kuweza kujileta wenyewe katika mapatano na Mungu. Yote ambayo mwanadamu anaweza kufanya bila Kristo yamechafuliwa na ubinafsi na dhambi. Ni neema ya Kristo pekee, kwa njia ya imani, ndiyo ambayo inaweza kutufanya watakatifu.

Kosa la pili lililo kinyume na la hatari ni kwamba watu huamini kwamba imani katika Kristo huwaachilia wanadamu kutoka katika kuishika Sheria ya Mungu; kwamba kwa kuwa na imani pekee tunakuwa washiriki wa neema ya Kristo, matendo yetu hayana la kufanya katika suala la ukombozi wetu.

Utii ni tunda la imani. Haki inafafanuliwa kwa kiwango cha Sheria takatifu ya Mungu, kama inavyoonyeshwa katika zile Amri kumi (Kutoka 20:3-20). Kile kinachoitwa imani katika Kristo ambacho kinadai kuachilia watu kutoka katika wajibu wa utii kwa Mungu, si imani, lakini ni kiburi na uelewa ulio na makosa. Sharti la uzima wa milele lilivyo sasa ndivyo lilivyokuwa siku zote - kama ilivyokuwa katika edeni (au paradiso) kabla ya anguko la wazazi wetu wa kwanza, sharti hilo ni Utii mkamilifu kwa Sheria ya Mungu, ambayo ndiyo uadilifu mkamilifu.

Ikiwa uzima wa milele ungetolewa kwa sharti lolote pungufu ya hili, basi furaha ya sayari zote na mbingu imo hatarini. Njia ingelifunguliwa wazi kwa ajili ya dhambi, pamoja na msururu wake wote wa misiba na taabu, hata kama watu hawafi.

Kristo anabadilisha moyo. Anakaa moyoni mwetu kwa imani. Tunapaswa kudumisha uhusiano huu na Kristo kwa imani na kujitoa daima kwa mapenzi yetu Kwake; na mradi unafanya hivi, Yeye atafanya kazi ndani yake kutaka na kutenda kulingana na mapenzi Yake mema.

Kadiri unavyomkaribia Masihi, ndivyo utakavyoona ulivyo na makosa zaidi machoni pako; maana maono yako yatakuwa wazi zaidi. Huu ni ushahidi kwamba udanganyifu wa Shetani unapoteza nguvu zake. Hakuna upendo wa kina kwa Yesu

unaoweza kukaa katika moyo ambao hautambui dhambi yake wenyewe. Nafsi inayogeuzwa kwa neema ya Kristo itapendezwa na tabia Yake Mungu. Mtazamo wa dhambi zetu unasukuma na Yeye anayeweza kusamehe; na wakati nafsi, inatambua unyonge wake, na kumfikia Kristo, Yeye atajidhihirisha kwa uwezo Wake. Kadri hisia za kumhitaji zinavyotusukuma Kwake na kwa Neno la Mungu, ndivyo tutakavyokuwa na mitazamo iliyotukuka zaidi juu ya tabia Yake, na kwa ukamilifu zaidi tutaiakisi sura Yake.

Badiliko la mioyo ambalo kwalo tunafanyika kuwa wana wa Mungu linapatikana katika Biblia kama kuzaliwa. Tena linalinganishwa na kuota kwa mbegu nzuri iliyopandwa na mkulima. Ni Mungu Ndiye anayeleta chipukizi la majani kutokea na kisha ua, na mwishowe matunda. Ni kwa uwezo Wake mbegu hukua. Kama vile Ua linavyoligeukia jua, ili miale yake angavu isaidie katika ukamilifu mzuri na ulinganifu wake; ndivyo sisi tutakiwavyo kuligeukia Jua la Haki, ili nuru ya mbinguni iangaze juu yetu, ili tabia zetu ziweze kukuzwa katika kufanana na Kristo.

Je, unauliza, “Ninawezaje kukaa ndani ya Kristo?” Kama jinsi ulivyompokea Kristo hapo kwanza. "Basi kama mlimpokea Kristo Yesu, Bwana, enendeni vivyo hivyo katika Yeye.” Wakolosai 2:6. Kwa imani wewe ukawa Wake Kristo; na kwa imani unapaswa kukua ndani Yake kwa kutoa na kupokea. Unapaswa kutoa yote, moyo wako, mapenzi yako, huduma yako, hebu jitoe Kwake ili kutii matakwa Yake yote; nawe sharti uvibebe vyote, yaani umchukue Kristo (Ambaye Ndiye vyote), Ambaye ni utimilifu wa baraka zote, Akae moyoni mwako, Awe nguvu yako, Awe haki yako, na Msaidizi wako wa milele wa kukupa uwezo wa kutii.

Jiweke wakfu kwa Mungu asubuhi; fanya hii iwe kazi yako ya kwanza kabisa. Ombi lako liwe, Nitwae, Ee Bwana, niweWako kabisa. Ninaweka mipango yangu yote miguuni Pako. Nitumie leo katika huduma Yako. Kaa nami, na kazi yangu yote na itimizwe ndani yako.” Niepushe kuyafanya yale ambayo sipaswi kuyafanya, na kuyafanya yale ambayo napaswa kufanya. Hili ni jambo la kila siku. Kila asubuhi jiweke wakfu kwa Mungu kwa ajili ya siku hiyo. Peleka mipango yako yote Kwake, ili itekelezwe au iache kutokana na majaliwa Yake yatakavyoonyesha. Hivyo siku baada ya siku unaweza kuwa unayatoa maisha yako mikononi mwa Mungu, na hivyo maisha yako yatafinyangwa zaidi na zaidi kufanana na maisha ya Kristo.

Maisha ndani ya Kristo ni maisha ya utulivu. Kunaweza kuwa hakuna furaha yenye mihemko ya hisia, lakini kunapaswa kuwa na uvumilivu wa kuendelea kudumu katika Imani yenye matumaini. Wakati akili inapokaa juu ya ubinafsi, inageuzwa mbali na Kristo, Aliye chanzo cha nguvu na uhai. Kwa hivyo, ni juhudi ya mara kwa mara ya Shetani kutoa usikivu kutoka kwa Mwokozi na hivyo kuzuia muungano na ushirika wa roho na Kristo.

Kristo alipotwaa asili ya mwanadamu juu Yake, Aliufungamanisha ubinadamu Kwake kwa kifungo cha upendo ambacho hakiwezi kamwe kuvunjwa na mamlaka yoyote, isipokuwa chaguo la mwanadamu mwenyewe. Shetani ataendelea kuweka vivutio vya kutushawishi kuvunja uhusiano huu yaani kuchagua kujitenga na Kristo. Lakini wacha tuendelee kuinua macho yetu kumtazama Kristo, Naye atatuhifadhi. Tukimtazama Masihi, tuko salama. Hakuna kinachoweza kutung'oa kutoka mkononi Mwake. Yote ambayo Kristo alikuwa kwa wanafunzi, anatamani yawe kwa watoto Wake leo.

Yesu alituombea, na aliomba kwamba tuwe na umoja Naye, kama vile Yeye alivyo mmoja na Baba. Huu ni muungano wa thamani kiasi gani! Hivyo, tukimpenda na kukaa ndani Yake, “tutakua hata tumfikie Yeye katika yote, Yeye Aliye kichwa, Kristo.” Waefeso 4:15.

Mungu Ndiye chanzo cha uhai na nuru na furaha kwa ulimwengu. Popote uzima wa Mungu unapokuwepo ndani ya mioyo ya watu, uzima huo utatiririka kwa wengine kwa upendo na baraka.

Furaha ya Mwokozi wetu ilikuwa katika kuinuliwa na ukombozi wa wanadamu walioanguka. Kwa hili hakuyahesabu maisha Yake kuwa ya thamani Kwake Yeye Mwenyewe, bali aliustahimili msalaba na kuidharau aibu. Wakati upendo wa Kristo umo ndani ya moyo, ni kama manukato au harufu nzuri isiyoweza kufichwa. Upendo kwa Yesu utadhihirika katika hamu ya kufanya kazi kama Yeye alivyofanya kazi kwa ajili ya baraka na kuinuliwa kwa ubinadamu. Upendo kwa Kristo huleta mwitikio wa upendo, rehema, na huruma yenye mguso kwa viumbe vyote ambavyo Baba yetu wa mbinguni Anavitunza. Wale walio washiriki wa neema ya Kristo watakuwa tayari kutoa dhabihu yoyote, ili wengine aliowafia wapate kushiriki zawadi ya mbinguni. Watafanya yote wawezayo kufanya duniani, ili dunia iwe mahali bora zaidi katika kukaa kwao humo. Roho hii ndiyo chanzo cha uhakika cha nafsi iliyoongoka kweli kweli. Mara tu mtu anapokuja kwa Kristo ndipo unazaliwa ndani ya moyo wake hamu ya kufanya ijulikane kwa wengine ni urafiki wa thamani gani ameupata kwa Yesu. Ikiwa tumeonja na kuona kwamba Bwana ni mwema, tutakuwa na kitu cha kusema. Tutajaribu kuwasilisha kwa wengine vivutio vya Kristo na mambo yasiyoonekana ya ulimwengu ujao. Kutakuwa na nguvu yenye matamanio makubwa katika kufuata njia ambayo Yesu aliipita.

Na jitihada za kuwabariki wengine zitaleta mwitikio wa baraka juu yetu wenyewe. Wale ambao wanakuwa washiriki katika kazi ya upendo, huletwa karibu zaidi na Muumba wao. Roho ya kufanya kazi bila ubinafsi kwa ajili ya wengine hutoa kina, uthabiti, na kuwa na tabia ya kupendeza kama Kristo kwa mhusika, na kisha huleta amani na furaha kwa mhusika(mtoaji). Nguvu huja kwa kujizoesha. Hatuhitaji kwenda katika nchi za kipagani, au hata kuacha mazingira ya nyumba zetu, ikiwa hapo ni pale ambapo wajibu wetu uko, ili kufanya kazi

kwa ajili ya Kristo. Kwa roho ya upendo tunaweza kufanya kazi kwa unyenyekevu katika maisha “kwa Bwana.” Wakolosai 3:23. Ikiwa upendo wa Mungu umo moyoni, utadhihirika katika maisha yetu. Haupaswi kungojea hafla nzuri au kutarajia uwezo wa ajabu kabla ya kwenda kufanya kazi kwa ajili ya Mungu. Wanafunzi wanyenyekevu na maskini zaidi wa Yesu wanaweza kuwa baraka kwa wengine wakati wote.

Kuna njia nyingi ambazo Mungu anatafuta kujitambulisha kwetu na kutuleta katika ushirika pamoja Naye. Ikiwa tutasikiliza tu, Asili huzungumza na hisia zetu bila kukoma. Kazi zilizoumbwa na Mungu zitatufundisha masomo ya thamani ya utii na uaminifu.

Hakuna machozi yanayotolewa ambayo Mungu hayatambui. Hakuna mwenendo asiyoutia alama. Kama tungeweza kumwamini kikamilifu, mahangaiko yote yasiyofaa yangetupiliwa mbali. Maisha yetu yasingejazwa na kukata tamaa kama ilivyo sasa; kwa maana kila kitu, kiwe kikubwa ama kidogo, kingeachwa mikononi mwa Mungu.

Mungu huzungumza nasi kupitia kazi Zake na majaliwa na kupitia ushawishi wa Roho Wake juu ya moyo yetu. Mungu anazungumza nasi katika Neno Lake. Hapa tunayomistari iliyo wazi zaidi ya ufunuo wa tabia Yake, kushughulika Kwake na wanadamu, na kazi kuu ya ukombozi. Jaza moyo wote kwa Neno la Mungu. Neno ni maji yaliyo hai, yakizima kiu yako iwakayo. Neno ni mkate wa uzima kutoka mbinguni.

Siri ya ukombozi ni jambo ambalo malaika wanatamani kuliangalia na kulijua ila ni fumbo na siri; ukombozi wa mwanadamu itakuwa ndiyo sayansi na wimbo wa waliokombolewa katika enzi zote zisizo na kikomo za milele. Kama ni hivyo, Je, haifai tufikirie sasa kwa makini na kujifunza leo hii? Tunapotafakari juu ya Mwokozi, kutakuwa na njaa na kiu ya nafsi ya kuwa kama Yeye Ambaye tunamwabudu.

Biblia iliandikwa kwa ajili ya watu wa kawaida. Kweli kuu zinazohitajika kwa wokovu zinafanywa wazi kama mchana. Hakuna kitu kinachohesabiwa kuimarisha akili kuliko kujifunza Maandiko Matakatifu. Lakini kuna faida kidogo inayopatikana kwa kusoma Biblia haraka-haraka. Fungu moja likisomwa kwa makini hadi tukagundua umuhimu kwa akili zetu na uhusiano wake, na mpango wa wokovu ukawa dhahiri, huu ndio usomaji wa thamani zaidi kuliko usomaji wa sura nyingi bila malengo dhahiri na hakuna maagizo chanya yaliyopatikana.

Weka Biblia yako pamoja nawe. Upatapo nafasi, isome; yaweke maandishi kwenye kumbukumbu yako. Hatuwezi kupata hekima bila uangalifu wa dhati na kujifunza kwa sala.

Kamwe Biblia haipaswi kusomwa bila maombi. Kabla ya kufungua kurasa Zake, tunapaswa kuomba nuru ya Roho Mtakatifu, nayo itatolewa. Malaika kutoka katika ulimwengu wa nuru watakuwa pamoja na wale ambao kwa unyenyekevu wa moyo wanatafuta mwongozo wa Mwenyezi Mungu. Je, ni kwa jinsi gani Mungu anawathaminiwanadamu? Yeye alimtoa Mwanawe ili afe kwa ajili yao na anamtuma Roho Wake Mtakatifu kuwa mwalimu wa mwanadamu, Naye ni kiongozi wa kudumu!

Kupitia asili na ufunuo, kupitia majaliwa Yake, na kwa ushawishi wa Roho Wake, Mungu anazungumza nasi. Lakini haya hayatoshi; tunahitaji pia kumimina mioyo yetu Kwake. Ili kuwasiliana na Mungu, sharti tuwe na kitu cha kumwambia kuhusu maisha yetu halisi, maisha ya kila siku. Maombi ni kufungua moyo kwa Mungu kama kwa rafiki. Sio kwamba ni sharti tumjulishe Mungu mambo yalivyo kwetu, bali ni ili Atuwezeshe kumpokea Yeye mioyoni mwetu. Maombi hayamshushi Mungu kwetu, lakini maombi hutupeleka juu Kwake.

Baba yetu wa mbinguni anasubiri kutupa utimilifu wa baraka Zake. Inashangaza kiasi gani kwamba sisi tunaomba kidogo sana! Mungu Yuko tayari kutubariki na Anawiwa kusikia maombi ya dhati ya watoto Wake walio wanyenyekevu zaidi. Malaika wa mbinguni wanashangaa wanapofikiria juu ya wanadamu maskini wasiojiweza, ambao wako chini ya majaribu, nao wanaomba kidogo sana na wana imani ndogo sana, wakati Moyo wa Mungu wenye upendo usio na kikomo una matamanio nao, Naye Yupo tayari kuwapa zaidi ya vile wanavyoweza kuomba au kufikiria.

Giza la mwovu linawafunika wale wanaopuuza kuomba. Majaribu ya kunong'ona ya adui huwashawishi wanadamu kutenda dhambi; na yote ni kwa sababu hawatumii fursa ya maombi. Walakini maombi ndio ufunguo katika mkono wa imani kufungua ghala ya mbinguni, ambapo rasilimali zisizo na kikomo za Mweza wa yote zinatunzwa.

Kuna masharti fulani ambayo kwayo tunaweza kutarajia kwamba Mungu atasikia na kujibu maombi yetu: Moja ni kwamba tunahisi hitaji letu la msaada kutoka Kwake. Tukiwaza maovu mioyoni mwetu, tukishikamana na dhambi yoyote tuijuayo; Bwana hatatusikia; lakini sala ya mtu aliyetubu na aliyeungama hukubaliwa daima. Wakati wote makosa yanayojulikana yanaposahihishwa, tunaweza kuamini kwamba Mungu atajibu maombi yetu.

Kipengele kingine cha maombi yenye nguvu ni imani. Wakati maombi yetu yanaonekana kutojibiwa, tunapaswa kushikilia kaw bidii ahadi Zake; kwani wakati wa kujibiwa utakuja hakika, na tutapokea baraka tunazozihitaji zaidi. Lakini kudai kwamba maombi daima yatajibiwa kwa namna tutakavyo na kila kitu tunachokitamani ni dhana za kufikirika.

Tunapokuja kwa Mungu katika maombi, tunapaswa kuwa na roho ya upendo na msamaha ndani ya mioyo yetu wenyewe. Kuendelea kudumu katika maombi kumefanywa kuwa sharti la kupokea majibu yetu. Sharti tuombe kila wakati ikiwa tunataka kukua katika imani na uzoefu.

Tunapaswa kuomba katika mzunguko wa familia, na zaidi ya yote hatupaswi kupuuza maombi ya siri, kwa maana haya ndiyo maisha ya kiroho. Sala ya familia au ya hadhara pekee yake haitoshi. Maombi ya siri yanasikika kwa Mungu Ajibuye maombi.

Hakuna wakati au mahali pasipofaa kutoa ombi kwa Mungu. Katika umati wa watu mtaani, katikati ya shughuli za kibiashara, tunaweza kutuma ombi kwa Mungu na kumsihi Mungu Atupe mwongozo wa Kiungu.

Hebu roho na ivutwe na kwenda juu, ili Mungu atupe pumzi ya anga la mbinguni. Sisi tunaweza kuwa karibu sana na Mungu kiasi kwamba katika kila jaribu lisilotarajiwa mawazo yetu yatamgeukia Yeye kwa ile kawaida ya ua linavyoligeukia jua. Weka mahitaji yako, furaha yako, huzuni zako, wasiwasi wako, na hofu zako mbele za Mungu.

Huwezi kumlemea; huwezi kumchosha. Yeye hachoshwi na matakwa ya watoto Wake.

Tunapata hasara tunapopuuza fursa ya kujumuika pamoja ili kuimarishana na kutiana moyo sisi kwa sisi katika utumishi kwa Mungu. Ikiwa Wakristo watashirikiana pamoja, wakisemezana kuhusu upendo wa Mungu na Kweli za thamani za ukombozi, mioyo yao wenyewe ingeburudishwa na wangeburudishana wao kwa wao.

Ni sharti tukusanyike pamoja kwa ajili ya msalaba. Kristo na Yeye aliyesulubiwa vinapaswa kuwa mada ya kutafakari, mada ya mazungumzo, na hisia zetu za furaha zaidi. Tunapaswa kuweka katika mawazo yetu kila baraka tunayoipokea kutoka kwa Mungu, na tunapotambua upendo Wake mkuu tunapaswa kuwa tayari kuamini kila kitu kilicho katika mikono ile iliyotundikwa msalabani kwa ajili yetu.

Nafsi inaweza kupaa karibu na mbingu kwa mbawa za sifa kwa Mungu. Tunapoonyesha shukrani zetu, ndivyo tukaribiavyo kuabudu na majeshi ya mbinguni. Wengi nyakati fulani wanatatizwa na mapendekezo ya kutilia shaka kuhusu Mungu. Mungu kamwe hatuambii tuamini bila kutoa uthibitisho wa kutosha wa kujenga imani yetu. Tunaweza kuficha uhalisia au ukweli Kwa namna tuwezavyo, ila sababu halisi ya shaka na kutokuamini, katika hali nyingi, ni kupenda dhambi. Ni sharti tuwe na nia ya dhati ya kujua Ukweli na utayari wa moyo kuitii.

Kabla ya kuingia kwa dhambi, Adamu alifurahia ushirika wa wazi na Muumba wake; lakini tangu mwanadamu alipojitenga yeye mwenyewe kutoka kwa Mungu kwa kutenda dhambi, jamii ya kibinadamu imekatiliwa mbali na upendeleo huu mkuu. Kwa mpango wa ukombozi, hata hivyo, njia imefunguliwa ambayo kwayo wakaaji wa dunia wanaweza bado kuwa na uhusiano na Mbingu. Mungu amewasiliana na wanadamu kwa Roho Wake, na nuru ya Bwana imekuwa ikipandikizwa ulimwenguni kwa mafunuo, kupitia watumishi Wake wateule. "Watu watakatifu wa Mungu walinena kama walivyokuwa wakiongozwa na Roho Mtakatifu." 2 Petro 1:21.

Wakati wa karne ishirini na tano za kwanza za historia ya mwanadamu, hapakuwa na ufunuo ulioandikwa (Musa aliishi miaka 2500 hivi baada ya Adamu kuumbwa, na ndiye mwandishi wa kwanza). Wale ambao walikuwa wamefundishwa na Mungu, waliwasilisha ujuzi wao kwa wengine, na maarifa haya yalipitishwa kutoka kwa baba kwenda kwa mwana, kupitia vizazi vilivyofuatana. Maandalizi ya Neno lililoandikwa yalianza wakati wa Musa.

Mafunuo yaliyovuviwa yalijumuishwa katika kitabu kilichovuviwa. Kazi hii iliendelea kwa muda mrefu kipindi cha miaka elfu na mia sita (1600), kutoka kwa Musa, mwanahistoria wa uumbaji na Sheria, hadi Yohana, mwandishi wa Kweli kuu za injili (takribani Kutoka 1500 KK hadi 100 BK).

Biblia inaelekeza kwa Mungu kama mwandishi Wake; lakini iliandikwa kwa mikono ya wanadamu; na kwa mtindo wake tofauti vitabu vyake mbalimbali vinawasilisha sifa za waandishi kadhaa. Kweli zilizofunuliwa zote "hutolewa kwa pumzi ya Mungu" (2 Timotheo 3:16); lakini zinaonyeshwa kwa maneno ya wanadamu, kwani si imla, ila walipewa njozi na ndoto na wakaandika kwa maneno yao. Roho Mtakatifu ametoa nuru katika akili na mioyo ya watumishi Wake. Amewapa ndoto na maono, alama na takwimu; na wale waliofunuliwa Kweli hizi, wameonyesha wenyewe mawazo hayo katika lugha ya kibinadamu.

Amri kumi zilinenwa na Mungu Mwenyewe, na ziliandikwa kwa mkono Wake Mwenyewe. Amri Kumi ni za Mungu Mwenyewe. Tunatakiwa tuwe waangalifu sana, kwani amri za mataifa yetu tunazitilia maanani, na tunapozivunja tunapata shida, sembuse Amri za Mwenyezi Mungu? Hakuna awezaye kushika sheria na kutembea na Mwenyezi Mungu isipokuwa amepata msaada kutoka Kwake, na Kila mwanadamu aombaye msaada huo, Mungu Yupo tayari kumpa.

# DIBAJI

Mpendwa Msomaji, kitabu hiki hakijachapishwa ili kutuambia kwamba kuna dhambi na ole na taabu katika ulimwengu huu. Tunajua haya yote vizuri sana. Kitabu hiki hakijachapishwa kutuambia kuwa kuna pambano kubwa lisilopatanishika kati ya giza na nuru, dhambi na haki, makosa na haki, kifo na uzima. Katika mioyo yetu tunalijua hilo, na tunafahamu kuwa sisi ni washiriki, watendaji, katika pambano hili. Kitabu hiki kimechapishwa ili kulitia nguvu tumaini letu lenye kina miongoni mwa matumaini yetu yote tunayoyapenda sana - yaani, suluhisho la mwisho na sahihi la mambo ya binadamu. Hakijachapishwa ili kutuambia sisi kwamba dhambi na huzuni na taabu vipo katika ulimwengu wetu huu. Hakijachapishwa ili kutuambia sisi kwamba pana pambano kuu kati ya giza na nuru, dhambi na haki, mauti na uzima. Ndani ya moyo wa mioyo yetu tunajua, na kuelewa ya kwamba sisi ni washiriki katika pambano hilo. Lakini wengi wanaogopa na kuchanganyikiwa. Hawana hakika kabisa kwamba upendo utashinda hatimaye dhidi ya nguvu hizo za uovu. Ndani ya kila moyo wa mwanadamu kuna shauku kubwa ya kutaka kujua zaidi juu ya pambano hilo) [PK iii.1]

Lakini kwa kila mmoja wetu wakati mwingine huja hamu ya kujua zaidi kuhusu pambano kuu. Je! Pambano hilo kati ya wema na uovu lilianzaje? Au lilikuwa hapa wakati wote? Je! Ni vipengele gani vinaingia katika nyanja zake ngumu? Je, mimi nina uhusiano gani na pambano hilo? Wajibu wangu ni upi? Ninajikuta katika ulimwengu huu bila hiari yangu mwenyewe. Je! Hiyo inamaanisha jema au baya kwangu? [PK iii.2].

Je! Ni kanuni gani kuu zinazohusika? Pambano hili litaendelea hadi lini? Mwisho wake utakuwa nini? Je! Dunia hii itazama kwenye kina kirefu cha usiku usio na jua, uliohifadhiwa milele kama wanasayansi wengine wanavyosema? Au kuna siku bora zijazo? [PK iii.3]

Swali linakuja karibu zaidi: Je! Pambano ndani ya moyo wangu mwenyewe, yaani pigano kati ya hali ya ubinafsi inayoingia na upendo unaotoka, vinatatuliwaje katika ushindi wa wema, na kusuluhishwaje milele? Je! Biblia

inasema nini? Je! Mungu ametufundisha nini juu ya swali hili muhimu milele zote? [PK iii.4]

Ni lengo la kitabu hiki kwako msomaji, kuisaidia roho yako inayofadhaika kupata suluhisho sahihi la shida hizi zote. Kitabu kimeandikwa na yule ambaye ameonja na kuona kuwa Mungu ni mwema, na ambaye amejifunza katika ushirika na Mungu na kusoma Neno Lake kwamba siri ya Bwana iko pamoja na wale wanaomcha, Naye atawaonyesha Agano Lake. [PK iii.5]

Ili tuweze kuelewa vizuri kanuni za pambano muhimu kabisa, ambalo maisha ya ulimwengu yanahusishwa, mwandishi ameliweka mbele yetu katika masomo makuu na madhubuti ya karne ishirini zilizopita. [PK iii.6]

Kitabu kinaanza na tukio la mwisho la kusikitisha la kisa cha Yerusalemu-mji wa wateule wa Mungu, baada ya kumkataa Mtu wa Kalvari, aliyekuja kuokoa. Kuendelea mbele kwenye barabara kuu ya mataifa, inatuelekeza katika mateso ya watoto wa Mungu kwenye karne za kwanza; uasi mkubwa uliofuata katika kanisa Lake; uamsho wa ulimwengu juu ya matengenezo, ambayo kanuni zingine kuu za pambano zinadhihirishwa wazi; somo la kutisha la kukataliwa kwa kanuni za haki na Ufaransa; uamsho na kuinuliwa kwa Maandiko, na mvuto Wake mzuri wa kuokoa maisha; mwamko wa kidini wa siku za mwisho; kufunuliwa kwa chemchemi inayong'aa ya Neno la Mungu, na ufunuo Wake mzuri wa nuru na maarifa kukutana na chipukizi la kutisha la kila udanganyifu wa giza. [PK iii.7]

Pambano la sasa linalokaribia, pamoja na kanuni muhimu zinazohusika, ambazo hakuna mtu anayeweza kukosa kuwa na upande wowote, limeelezewa kwa uwazi na kwa nguvu. [PK iv.1]

Mwishowe, tunaambiwa juu ya ushindi wa milele na utukufu wa mema juu ya mabaya, sahihi dhidi ya uovu, nuru dhidi ya giza, furaha dhidi ya huzuni, matumaini dhidi ya kukata tamaa, utukufu dhidi ya aibu, uhai dhidi ya kifo, na upendo wa milele, wenye uvumilivu dhidi ya kulipiza kisasi. [PK iv.2]

Kwa kuanza na toleo lake la kwanza la mwaka (1888), ikifuatiwa na marekebisho ya mwandishi ya mwaka (1911), kazi hii imara imefanikiwa kufikia ulimwengu wote kupitia matoleo na tafsiri nyingi. Msomaji atafahamu kuwa mwandishi ameandika kwa uwazi na kwa nguvu, akionyesha makosa na kupendekeza suluhisho kulingana na Neno la Mungu lisilokosea. Ingawa miongo michache iliyopita imeshuhudia mabadiliko na marekebisho katika ulimwengu wa dini, mpango mkuu na matukio yajayo yaliyowasilishwa katika kitabu hiki leo yanadumisha wakati kamili na kuvutia shauku. [PK iv.3]

Matoleo ya awali ya kitabu hiki yameleta roho nyingi kwa Mchungaji wa Kweli; ni maombi ya Mchapishaji kwamba toleo hili liweze kuzaa matunda zaidi ya mema ya milele. [PK iv.4]

Wachapishaji: Angalia Maneno na mafungu katika mabano ( ) au yameongezwa kwa ufafanuzi tu. Haya tumeona ni msaada kukamilisha maana ya sentensi inayohusika au

ufafanuzi unaohitajika. Yote yamewekwa kwa msomaji anayetaka kujifunza kwa kina. Kwa vile tumeona wapo wachache wataosoma bila kuelewa mambo mengine. Tunashauri uchukue muda kujisomea/kujifunza zaidi unabii wa Daniel na Ufunuo. Waweza kututafuta tukuelekeze au kukupa masomo ya unabii wa Daniel na Ufunuo pia. Maandiko yenye herufi za mlazo (*italics*) yamewekwa mahali pengine ili kukazia kipengele au pointi fulani. Alama * imewekwa kuelezea mada hiyo zaidi nawe unaweza kuwaandikia wachapishaji wa hiki kitabu na kuulizia zaidi kama sisi tulivyofanya wakati wa tafsiri.

## **Utangulizi**[v]

Kabla ya kuingia kwa dhambi duniani, Adamu alifurahia ushirika wa kuongea ana kwa ana na Muumba Wake; lakini toka pale mwanadamu alijitenga mwenyewe na Mungu kwa sababu ya uvunjaji wa sheria, jamii ya binadamu imezuiwa kuupata upendeleo huo wa hali ya juu. Hata hivyo Kwa mpango ule wa ukombozi, njia imefunguliwa ambayo kwayo wakazi wa dunia bado wanaweza kuwa na mahusiano na kuunganishwa na mbingu. Mungu amewasiliana na wanadamu kwa Roho Wake, na nuru ya Mungu imewasilishwa ulimwenguni kwa ufunuo aliowapa watumishi Wake wateule. “Bali wanadamu walinena yaliyotoka kwa Mungu, wakiongozwa na Roho Mtakatifu.” 2 Petro 1:21. [PK v.1]

Katika kipindi kile cha kwanza cha miaka elfu mbili na mia tano (2500) ya awali ya historia ya mwanadamu, hakukuwa na ufunuo uliokuwa kwenye Maandishi. Wale ambao walikuwa wamefundishwa na Mungu, walirithisha (waliwagawia) kwa watu wengine maarifa yao, nayo yalipasiwa/yalitolewa kutoka kwa baba na kwenda kwa mwana, kupitia vizazi vyote vilivyofuata. Utayarishaji wa Neno lililoandikwa ulianza wakati wa Musa. Baadaye mafunuo hayo yaliyovuviwa yalifumbatwa pamoja katika kitabu kimoja kilichovuviwa. Kazi hii iliendelea kwa kipindi kirefu cha miaka mia elfu moja na mia sita (1600), kutoka kwa Musa, mwanahistoria wa uumbaji na sheria/torati, hadi kufikia Yohana wa Ufunuo, mwandishi wa kumbukumbu tukufu na zilizovuviwa za Kweli ya injili. [PK v.2].

Biblia inamwonyesha Mungu kama mwandishi Wake; Lakini iliandikwa kwa mikono ya wanadamu; na kwa njia ya mtindo tofauti-tofauti ya uandishi wa vitabu Vyake, inaziwasilisha sifa za waandishi kadhaa (takribani 40). Kweli zote zilizofunuliwa humo “zimetolewa kwa uvuvio wa Pumzi ya Mungu” (2 Timotheo 3:16); lakini zimeelezwa kwa kutumia maneno ya wanadamu. Yeye Yule asiye na mwisho, yaani wa milele, kwa kupitia Roho Wake Mtakatifu ameimwaga nuru katika akili na mioyo ya watumishi Wake. Amewapa ndoto na maono, mfumo wa ishara, mifano, alama na maumbo; na wale ambao Ukweli ulifunuliwa kwao, wakalivika/wakaliweka wazo hilo walilopewa katika lugha ya wanadamu. [PK v.3]

Amri Kumi zilinenwa na Mungu Mwenyewe, na kuandikwa kwa mkono Wake Mwenyewe. Hizi zinatoka kwa Mungu Mwenyewe, wala hazijatungwa na mwanadamu yeyote. Lakini Biblia pamoja na Kweli zake zote zilizotolewa ambazo zimefafanuliwa kwa lugha ya wanadamu, huonyesha muungano wa Uungu na Ubinadamu. Muungano kama huo ulikuwepo katika asili Yake Kristo, Ambaye alikuwa Mwana wa Mungu na Mwana wa Adamu. Hivyo ndivyo ilivyo Kweli kuihusu Biblia, kama vile ilivyokuwa Kweli kumhusu Kristo, kwamba “Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu Yohana 1:14. [PK v.4]

Imeandikwa katika enzi tofauti (Vizazi mbalimbali), na watu ambao walitofautiana sana kwa vyeo vyao, hadhi, kazi na katika vipawa vya kiakili na kiroho, vitabu vya Biblia vinaonyesha tofauti pana katika mitindo yake ya uandishi, na vile vile utofauti katika aina ya masomo yaliyofunuliwa. Aina tofauti za kujieleza/usemi zimetumiwa na waandishi tofauti tofauti; mara nyingi Kweli ile ile moja imefanunuliwa katika namna ya kuvutia au msisitizo zaidi na mwandishi mmoja kuliko mwingine. Na kama waandishi hao kadhaa wanawasilisha mada katika nyanja/somo fulani chini ya mahusiano tofauti tofauti, kwa mtu anayesoma juujuu tu, asiyejali, au mwenye dhana ya chuki na ubaguzi bila sababu, kunaweza kukaonekana kuwepo kwa mashimo ya kujaza (dosari) au kukinzana, ambako kwa mwanafunzi mwenye kicho kwa Mungu, anayetafakari kwa utambuzi dhahiri, anabaini upatanifu uliopo katika somo hilo. [PK vi.1]

Kama Ukweli unavyowasilishwa kupitia kwa watu tofauti tofauti, Kweli hiyo inafunuliwa katika mitazamo inayotofautiana. Mwandishi mmoja huvutiwa zaidi na awamu moja ya mada hiyo; huchukua vidokezo/vipengele vile vinavyoendana na uzoefu wake wa maisha au na vile vinavyopatana na uwezo wake wa utambuzi na kufurahia kwake anapotathmini; mwingine hushikilia kwa awamu au upande ulio tofauti na ule wa mwingine, na kila mmoja, akiwa chini ya uongozi wa Roho Mtakatifu, anaelezea kile ambacho kimemgusa zaidi katika akili yake mwenyewe, katika picha mbalimbali za Kweli ile ile moja, lakini upatanifu mkamilifu na sahihi unapatikana kupitia kwa wote. Na kisha Kweli zilizofunuliwa huunganishwa na kuunda ukamilifu wote wa kitu kimoja kizima, kinachokidhi mahitaji ya wanadamu katika mazingira yao yote na uzoefu wao wote wa maisha. [PK vi.2]

Mungu amependezwa kuiwasilisha hii Kweli Yake ulimwenguni kwa kutumia mawakala wa kibinadamu, na kwa kupitia Kwake Yeye Mwenyewe kwa kumtumia Roho Wake Mtakatifu, aliwapa wanadamu sifa zinazostahili kuwapa uwezo wa kuifanya kazi hii. Aliziongoza akili zao katika uteuzi wa maneno ya kusema na kipi cha kuandika. Hazina hiyo iliwekwa katika vyombo vya udongo (wanadamu wanyonge), lakini, hata hivyo, Kweli hii bado imetoka Mbinguni. Ingawa

ushuhuda huo umetolewa kupitia usemi/maneno yasiyo makamilifu ya lugha ya mwanadamu, lakini huo bado ni ushuhuda utokao kwa Mungu; na mtoto wa Mungu mtiifu na mwaminifu, huona ndani Yake huo ushuhuda wa Maandiko, na utukufu wa uweza wa Bwana, ambao umejaa neema na Kweli. [PK vi.3]

Katika Neno Lake, Mungu amewakabidhi wanadamu maarifa muhimu kwa ajili ya wokovu wao. Hebu Maandiko hayo Matakatifu yapokelewe na kukubaliwa kama ufunuo wenye mamlaka, na usiokosea kamwe wa mapenzi Yake. Hayo ndiyo kiwango na kipimo cha tabia yetu, nayo hufunua mafundisho yote ya dini, tena hayo ndiyo kipimo cha kupimia uzoefu wetu wa maisha. "Kila Andiko, lenye pumzi ya Mungu, lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki; ili mtu wa Mungu awe kamili, amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema." 2 Timotheo 3:16, 17. [PKvii.1]

Walakini Ukweli huo kwamba Mungu ameyafunua mapenzi Yake kwa wanadamu kupitia kwa Neno Lake, haufanyi kutohitajika kwa uwepo wa uongozi wa Roho Mtakatifu. Kinyume chake, Roho aliahidiwa na Mwokozi wetu ili kuwafunulia Neno watumishi Wake, kuangaza na kuyatumia mafundisho Yake (katika maisha yao). Na kwa kuwa alikuwa ni Roho Mtakatifu wa Mungu aliyeivuvia Biblia, basi haiwezekani kabisa kwamba mafundisho ya Roho yawe kinyume na yale yaliyomo katika Neno hilo. [PK vii.2]

Roho huyo hakutolewa-- wala kamwe hawezi kutolewa kuwa mbadala au kuchukua mahali pa Biblia; kwa maana Maandiko yanasema wazi kwamba Neno la Mungu ni kipimo/kiwango ambacho kwa hicho mafundisho yote ya dini na uzoefu wote sharti yapimwe kwayo. Anasema mtume Yohana, "Wapenzi, msiiamini kila roho, bali zijaribuni hizo roho, kwamba zimetokana na Mungu; kwa sababu manabii wa uongo wengi wametokea duniani." 1 Yohana 4: 1. Na Isaya anatangaza, "Na waende kwa sheria na ushuhuda; ikiwa hawasemi sawasawa na Neno hili, bila shaka kwa hao hapana asubuhi." Isaya 8:20 (yaani wamo gizani, hawana nuru ni vipofu). [PK vii.3]

Shutuma kubwa imetupiwa juu ya kazi ya Roho Mtakatifu na mafundisho potofu ya kikundi kimoja ambacho kinadai kuangaziwa na nuru, na wakitangaza kuwa hakuna haja tena ya kuongozwa na Neno la Mungu. Wao wanaongozwa na hisia/mihemko ambayo wanaiona kama ndiyo sauti ya Mungu ndani ya mioyo yao. Lakini roho Yule anayewatawala/anayewadhibiti si Roho wa Mungu (Yn 8:47). Huku kuzifuata hisia za moyoni na kuyadharau Maandiko kunaweza kusababisha mkanganyiko/machafuko tu, kwa kuwapeleka katika udanganyifu na maangamizi. Jambo hilo linatumika tu kuendeleza ubunifu wa hila za yule mwovu. Kwani huduma ya Roho Mtakatifu ni ya muhimu sana kwa kanisa Lake Kristo, ni moja ya mbinu za Shetani, kupitia makosa ya wale wenye msimamo

mikali iliyopitiliza,* yaani mashabiki au watu shupavu wasio na busara, kudharau kazi ya Roho Mtakatifu na kusababisha watu wa Mungu kupuuza Chimbuko hili la nguvu zao ambalo Bwana wetu Mwenyewe ametupa *(Itikadi kali) [PKvii.4]

Kwa kupatana na Neno la Mungu, Roho Wake alipaswa kuendeleza kazi Yake katika kipindi chote cha kuhubiri kwa injili mpaka hapo itakapofungwa. Wakati wa zama za Maandiko ya Agano la Kale na Agano Jipya yalipokuwa yakitolewa, Roho Mtakatifu hakuacha kuwasilisha nuru katika akili za mtu mmoja mmoja, Mbali na mafunuo yale ambayo yalijumuishwa katika kanuni hii takatifu ya Maandiko (canon). Biblia yenyewe inaelezea jinsi kupitia Roho Mtakatifu, watu walivyopokea maonyo, makaripio, mashauri na maagizo/mafundisho, katika mambo mbalimbali ambayo kwa njia yoyote hayakuwa na uhusiano wowote na utoaji wa Maandiko yale. Na orodha imetolewa ya manabii katika enzi/vizazi tofauti, ambao matamshi yao hayakuwekwa katika kumbukumbu ya maandishi (Gad, Nathan, Hulda n.k). Vivyo hivyo, baada ya kufungwa kwa Kanuni ya juzuu hiyo ya Maandiko (Biblia), Roho Mtakatifu alikuwa bado akiendelea na kazi Yake ya kuwaangazia nuru Yake, kuwaonya, na kuwafariji watoto wa Mungu. [PK viii.1]

Yesu aliwaahidi wanafunzi Wake, akisema “Lakini huyo Msaidizi, huyo Roho Mtakatifu, ambaye Baba atampeleka kwa Jina Langu, atawafundisha yote, na kuwakumbusha yote niliyowaambia.” “Lakini Yeye atakapokuja, huyo Roho wa Kweli, atawaongoza awatie kwenye Kweli yote. Na mambo yajayo atawapasha habari Yake.” Yohana 14:26; 16:13. Maandiko yanafundisha wazi wazi kwamba ahadi hizi, licha ya kwamba zilitamkwa siku zile za mitume, zinalifikia kanisa la Kristo katika vizazi vyote. Mwokozi anawahakikishia wafuasi Wake, “Mimi Nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari.” Mat 28:20. Na Paulo anatangaza akitia mkazo kwenye fundisho la karama za Roho, na udhihirisho wa mafunuo ya Roho kwa kusema kuwa ziliwekwa kanisani “kwa kusudi la kuwakamilisha watakatifu, hata kazi ya huduma itendeke, hata mwili wa Kristo ujengwe, hata na sisi sote tutakapoufikia umoja wa imani na kumfahamu sana Mwana wa Mungu, hata kuwa mtu mkamilifu, hata kufika kwenye cheo cha kimo cha utimilifu wa Kristo;” Waefeso 4:12, 13. [PK viii.2]

Kwa waumini wa Efeso mtume aliomba, “Mungu wa Bwana wetu Yesu Kristo, Baba wa utukufu, awape ninyi roho ya hekima na ya ufunuo katika kumjua Yeye; macho ya mioyo yenu yatiwe nuru, mjue tumaini la mwito Wake jinsi lilivyo; na utajiri wa utukufu wa urithi Wake katika watakatifu jinsi ulivyo; na ubora wa ukuu wa uweza Wake ndani yetu tuaminio jinsi ulivyo; kwa kadiri ya utendaji wa nguvu za uweza Wake.” Waefeso 1: 17-19. Huduma ya Roho Mtakatifu katika kuangazia nuru ufahamu wetu na kutufunulia akilini mwetu mambo ya kina ya Neno takatifu la Mungu, ilikuwa ndiyo baraka ambayo Paulo alikuwa akiliombea kanisa la Efeso ipate. [PK ix.1]

Baada ya udhihirisho wa ajabu wa kumwagwa kwa Roho Mtakatifu katika Siku ile ya Pentekoste, Petro aliwahimiza watu kutubu na kubatizwa kwa Jina la Kristo, kwa ajili ya ondoleo la dhambi zao; na akasema: “nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu. Kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa watu wote walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie.” Matendo 2:38, 39. [PK ix.2]

Kwa kuhusiana matukio ya siku ile kuu ya Mungu, Bwana kwa kupitia kwa nabii Yoeli ameahidi utatokea udhihirisho (onyesho/miujiza) wa pekee wa Roho Wake. Yoeli 2:28. Unabii huu ulipata utimilifu kwa sehemu katika kumwagwa kwa Roho Mtakatifu ile Siku ya Pentekoste; lakini utafikia utimilifu wake kamili katika udhihirisho wa neema ya Mungu ambayo itatambatana katika kazi ya mwisho ya injili (kufungwa kazi). [PK ix.3]

Pambano kuu kati ya wema na ubaya litazidi kuongezeka makali yake hadi mwisho wa wakati. Katika nyakati zote ghadhabu ya Shetani imedhihirishwa dhidi ya kanisa la Kristo; na Mungu ametoa kwa watu Wake neema na Roho Wake ili kuwaimarisha kusimama dhidi ya nguvu za yule mwovu. Wakati mitume wa Kristo walivyotakiwa kuipeleka injili Yake ulimwenguni na kuiandika kwa ajili ya kumbukumbuku kwa nyakati (vizazi) zote zijazo, kwa njia ya pekee walipewa nuru na Roho Wake. Lakini wakati kanisa linapokaribia kile kilele cha ukombozi Wake, [x]

Shetani atafanya kazi kwa nguvu kubwa zaidi. Huyo ameshuka chini akiwa “mwenye ghadhabu nyingi, akijua ya kuwa ana wakati mchache tu.” Ufunuo 12:12. Atafanya kazi “kwa uwezo wote, na ishara na ajabu za uongo.” 2Wathesalonike 2: 9. Kwa miaka elfu sita, Mbunifu huyu mwerevu (shetani) ambaye zamani alikuwa na cheo cha juu kabisa kuliko malaika wote wa Mungu ameuweka mwelekeo wake wote kwenye kazi ya udanganyifu na maangamizi. Na kina chote cha ustadi wa kishetani na ujanja aliojipatia, na ukatili wote aliouendeleza, wakati wa mapambano haya ya vizazi vyote vilivyopita, atauleta dhidi ya watu wa Mungu katika pambano lake la mwisho. Na katika wakati huu wa hatari, wafuasi wa Kristo wanapaswa kupeleka onyo la ujio wa pili wa Bwana kwa ulimwenguni; na watu wanapaswa kuandaliwa wapate kusimama mbele Yake wakati wa kuja Kwake, bila “kuwa na mawaa wala aibu mbele Yake.” 2 Petro 3:14. Wakati huu wa majaliwa maalumu ya neema ya Mungu na nguvu unahitajika sana kwa kanisa kuliko siku zile za mitume. [PK ix.4]

Kupitia mwangaza wa nuru ya Roho Mtakatifu, matukio ya pambano hili lililoendelea kwa muda mrefu kati ya wema na uovu yamefunuliwa kwa mwandishi wa kurasa hizi (kwa njia ya maono Hes 12:6). Mara kwa mara mimi nimeruhusiwa kulitazama pambano hilo kuu katika vizazi mbalimbali, kati ya Kristo, Mfalme wa uzima, na Mwasisi wa wokovu wetu, na Shetani, mkuu wa

uovu, mwasisi wa dhambi, mwasi wa kwanza wa sheria takatifu ya Mungu katika zama zote (Kutoka 20). Uadui wa Shetani dhidi ya Kristo umedhihirika kwa kuwashambulia wafuasi Wake. Chuki ile ile ya kanuni za sheria ya Mungu (Amri Kumi), sera ile ile ya udanganyifu, ambayo mafundisho ya uongo hufanywa kuonekana kama Ukweli, ambayo sheria za wanadamu hufanywa kuwa mbadala wa sheria ya Mungu (zinachukua nafasi ya Sheria ya Mungu), na watu huongozwa kuabudu kiumbe au mwanadamu badala ya Muumbaji, inaweza kufuatiliwa na kuonekana katika historia yote iliyopita. Jitihada ya Shetani ya kuipotosha/kuielezea vibaya tabia ya Mungu, kusababisha watu kuthamini dhana ya uwongo kuhusu Muumba, na hivyo kuwafanya wamtazame kwa hofu na chuki badala ya kumwangalia kwa upendo; jitihada yake ya kuweka kando sheria ya Bwana (Amri Kumi), na kuwafanya watu wajione kuwa wako huru, kuwa hawafungwi dhidi ya matakwa Yake; na kuleta mateso yake kwa wale wanaothubutu kupinga udanganyifu wake, mambo hayo yamekuwa yakitendwa kwa uthabiti katika kila kizazi kilichopita. Mambo hayo yanaweza kufuatiliwa katika historia ya wazee, manabii, mitume, na wafia dini na wanamatengenezo wa kanisa. [PK x.1]

Katika pambano kuu lile la mwisho, Shetani atatumia sera hiyo hiyo, atadhihirisha roho yake mbaya ile ile, na kufanya kazi kwa lengo sawa na lile la enzi zilizopita. Yale ambayo yalikuwa, yatakuwako, isipokuwa kwamba pambano lile linalokuja litaweka historia kwa ukali wa kuogofya zaidi, kitu ambacho ulimwengu huu haujawahi kushuhudia. Udanganyifu wa Shetani utakuwa wa hila/werevu zaidi, mashambulizi yake yatadhamiriwa zaidi. Kama ingewezekana apate kuwadanganya yamkini, hata hao wateule. Marko 13:22, RV [PK xi.1]

Wakati Roho wa Mungu alipoifunua akili yangu Ukweli mkuu wa Neno Lake, na matukio yale yaliyopita zamani na yanayokuja baadaye, nimeagizwa kuwajulisha wengine kile ambacho kimefunuliwa kwangu kwa njia hiyo--, yaani kuandika historia ya mgogoro/pambano katika vizazi vile vilivyopita, na haswa ili kulielezea kwa namna ambayo itatoa nuru juu ya pambano linalokuja kwa haraka siku za usoni. Katika kutekeleza kusudi hili, nimejitahidi kuchagua na kuyapanga pamoja matukio katika historia ya kanisa kwa njia ambayo itasaidia kufuatilia Kweli hizi kuu zinazowapima wanadamu, na ambazo kwa nyakati tofauti zimetolewa kwa ulimwenguni huu, nazo zimechochea ghadhabu ya Shetani, na uadui kutoka kwa kanisa lile linaloupenda ulimwengu huu, na ambazo zimehifadhiwa kwa ushuhuda wa wale ambao “hawakupenda maisha yao hata kufa.” (Ufu. 12:11). [PK xi.2]

Katika rekodi hizi tunaweza kuona kielelezo cha pambano lililoko mbele yetu. Tukiziangalia Kweli hizi huru za Neno la Mungu, na kutiwa nuru na Roho Wake, tunaweza kuona kufichuliwa hila za yule mwovu, na hatari ambazo sharti

tuzikwepe kama tutakuwa wale ambao tutakutwa “bila mawaa” mbele Zake Bwana wakati wa kuja Kwake. [PK xi.3]

Matukio yale makuu yaliyoweka alama katika maendeleo ya matengenezo ya kanisa katika zama zile zilizopita, ni mambo ya historia, ambayo hujulikana vizuri na kutambuliwa kote katika ulimwengu wa Kiprotestanti; ni Ukweli ambao hakuna anayeweza kuupinga. Historia hii nimeiwasilisha kwa ufupi, kulingana na upeo (nafasi) wa kitabu, na ufupi ambao sharti uzingatiwe, licha ya kuminywa na kuwekwa pamoja katika nafasi ndogo kama yalivyoonekana kwa uthabiti, yanapatana na uelewa sahihi wa matumizi yake. Katika visa vingine ambapo mwanahistoria amekusanya pamoja matukio fulani ili kutoa picha au mtazamo mzima wa somo hilo kwa kifupi, maoni kamili (kinagaubaga) ya mada hiyo, au alivyotoa maelezo mafupi kwa njia rahisi, maneno yake yamenukuliwa; lakini katika namna nyingine hakuna sifa maalum zilizotolewa, kwani nukuu hazitolewi kwa madhumuni ya kumtaja mwandishi huyo kama ndiye mamlaka, lakini kwa sababu taarifa yake inasaidia kutoa maelezo yaliyoandaliwa tayari (na kurahisisha au kuleta nguvu katika mada hiyo). Katika kusimulia uzoefu na maoni ya wale wanaoendeleza kazi ya matengenezo ya kanisa katika siku zetu hizi, matumizi kama hayo katika kazi zao zilizochapishwa yametumika. [PK xi.4]

Lengo la kitabu hiki siyo kuwasilisha Ukweli mpya juu ya mapambano ya nyakati zile zilizopita, bali kuleta Ukweli pamoja na kanuni za muhimu ambazo zinahusiana na matukio yale yanayokuja. Walakini kikitazamwa kama sehemu ya pambano kati ya nguvu za nuru na zile za giza, basi rekodi hizi zote za zamani zitaonekana kuwa na maana mpya kwetu; na kupitia kwake nuru itamulikwa kwetu juu ya siku zijazo, ikiangazia njia za wale ambao, wataitwa kushuhudia kama walivyoitwa wanamatengenezo wale wa nyakati zilizopita, hata kwa gharama ya kuacha mema ya kidunia, na mali yao yote, kwa kutoa ushuhuda wao “kwa ajili ya Neno la Mungu, na kwa ushuhuda wa Yesu Kristo.” [PK xii.1]

**KUSUDI**: Kuyafunua matukio yanayohusika ya pambano kuu kati ya Ukweli na uongo; kuzifichua hila za Shetani, na njia za kuweza kumpinga kwa mafanikio kabisa; kutoa suluhisho la kuridhisha kwa janga kubwa la uovu, kwa kutoa nuru juu ya Chanzo/silika ya dhambi na jinsi hatimaye jinsi itakavyondolewa kwa kikamilifu kiasi cha kuweza kudhihirisha haki na fadhili Zake Mungu katika kushughulika Kwake kote na viumbe Vyake; na kuonyesha asili/tabia Yake takatifu, isiyobadilika ya Sheria Yake (Amri Kumi), ndiyo lengo la kitabu hiki (watu waokolewe). Ili kwa njia ya mvuto Wake watu wavutwe kutoka katika nguvu ya giza, na kuwa “washiriki wa urithi wa watakatifu katika nuru,” kwa sifa ya Yeye aliyetupenda, na kujitoa nafsi Yake Mwenyewe kwa ajili yetu, ndilo ombi la dhati la mwandishi huyu. [PK xii.2]

# SURA YA 1

## KUHARIBIWA KWA YERUSALEMU

### (Upendo Na Uvumilivu Wa Kristo)

Ufupisho: Hekalu la Yerusalemu lilikuwa la fahari kuliko mahekalu yote yaliyojulikana ulimwenguni. Jiji la Yerusalemu nalo lilikuwa na uzuri kati ya miji ya dunia, na majenerali wa Kirumi walitaka lisibomolewe kwa ajili ya fahari yake, ila liliungua mpaka kwenye msingi licha ya jitihada za watu kuliponya kwa sababu ya unabii alioutoa Yesu miaka 39 kabla. Wayahudi walikuwa wamefanya uasi kwa Rumi na Cestio alitoa majeshi yake mwaka 67 BK na kisha Tito akauhusuru mji mnamo Mei 70BK, na mji ukaangushwa Agosti.

"Laiti ungalijua, hata wewe katika siku hii, yapasayo amani! Lakini sasa yamefichwa machoni pako. Kwa kuwa siku zitakuja, adui zako watakapokujengea boma, likuzunguke; watakuzingira na kukuhusuru pande zote; watakuangusha chini wewe na watoto wako ndani yako, wasikuachie jiwe juu ya jiwe, kwa sababu hukutambua majira ya kujiliwa kwako." Luka19: 42-44. [GC 17.1; PK Aya ya 1]

Toka katika kilele kile cha mlima wa Mizeituni, Yesu aliutazama mji wa Yerusalemu. Mwonekano wake ulikuwa ni mzuri, shwari na wa amani mbele Yake. Yalikuwa ni majira ya Pasaka, na kutoka katika nchi mbalimbali, wana wa Yakobo walikuwa wamekusanyika hapo kusherehekea sikukuu hii kubwa ya kitaifa. Katikati ya bustani zile na mashamba ya mizabibu, na mteremko wa kijani iliyozingirwa na mahema ya mahujaji, viliinuka vilima vyenye matuta viliyofuatana, majumba mazuri ya kifalme (serikali), na ngome yenye kuta refu kwenye mji ule mkuu wa Israeli. Binti Sayuni alionekana katika kiburi chake akisema, mimi malkia huketi na sitaona huzuni; kwa kupendeza kisha hujiona kuwa yuko salama kwa kupendelewa na Mbingu, kama mwimbaji mashairi wa kifalme (Daudi) alivyoimba katika vizazi vilivyopita: "Kuinuka kwake ni mzuri sana. Ni furaha ya dunia yote. Mlima Sayuni ... Mji wa Mfalme mkuu...." Zaburi 48:2. Yakiwa yanaonekana kwa wazi kabisa, yalikuwa ni yale majengo mazuri ya hekalu. Miale ya jua lililokuwa linaelekea kuzama iliangaza weupe wa theluji ya kuta zake za marumaru na kung'aa kutoka katika lile lango la dhahabu na mnara ule mrefu na ncha yake. Likasimama katika "uzuri wake mkamilifu" yaani kama fahari na kiburi cha taifa la Kiyahudi. Ni mwana yupi wa Israeli ambaye angeweza kuangaza macho yake juu ya picha ya eneo hili bila kusisimka kwa furaha, kwa kuvutiwa na hali yake ya kustaajabia! Lakini Yesu alijawa na mawazo tofauti moyoni. "Alipofika karibu aliuona mji, akaulilia," Luka 19:41. Katikati ya shangwe ya watu wale wote na kuingia kwa ushindi na furaha, wakati

matawi ya mitende yakipeperushwa hewani, wakati furaha za hosana zilipoamsha miangwi kwenye vilima vile, na maelfu ya sauti zilimtangaza Yeye kuwa Mfalme, Mkombozi wa ulimwengu kwa ghafla alilemewa na huzuni na majonzi ya ajabu, na yasiyoelezeka. Yeye, Mwana wa Mungu aliyeahidiwa kwa Israeli, ambaye uweza Wake ulikuwa umeshinda kifo na kuwaita mateka Wake kutoka kaburini, alikuwa akibubujika machozi, si machozi ya huzuni ya kawaida, bali machozi ya maumivu makali sana yasiyozuilika, na yasiyoweza kuvumilika. [GC 17.2; PK Aya ya 2]

Machozi Yake hayakuwa kwa ajili Yake Mwenyewe, ingawa alijua vizuri kuwa miguu Yake ilikuwa ikielekea wapi. Mbele Yake kulikuwa na Gethsemane, eneo Lake la mateso na uchungu alilokuwa akilikaribia. Lango lile la kondoo pia lilikuwa likionekana mbele Yake, ambalo kwalo kwa karne nyingi waathiriwa/wahanga wa kafara walikuwa wakiongozwa, na ambalo lingefunguliwa kwa ajili Yake wakati wa kuletwa Kwake Yeye "Kama Mwana-Kondoo apelekwaye machinjoni." Isaya 53:7. Kalawari haikuwa mbali sana kutoka pale, yaani mahali pa kusulubiwa Kwake. Juu ya njia ambayo alikuwa sasa anaenda kuikanyaga si muda mrefu, hofu kuu ya giza ikamwangukia, punde atapaswa kuitoa nafsi Yake kama sadaka kwa ajili ya dhambi. Walakini haikuwa tafakari juu ya matukio haya ndiyo iliyomtia Yesu kivuli cha simanzi katika saa hii ya shamra-shamra. Hakuna hofu ya uchungu wa hali Yake ya kibinadamu uliohafifisha roho Yake isiyo ya ubinafsi. Alililia kwa sababu ya maelfu ya watu wa Yerusalemu waliokuwa wanaelekea kukutana na ole na kifo (kuangamia) -- kwa sababu ya upofu, kukataa kutubu, na ugumu wa mioyo ya wale ambao alikuja kwa ajili ya kuwabariki na kuwaokoa (kuwaletea heri/furaha). [GC 18.1; PK Aya ya 3]

**Upendo Wa Baba**

Historia ya zaidi ya miaka elfu moja ya upendeleo maalum wa Mungu pamoja na ulinzi Wake kwao kama wateule, vilikuwa vinaonekana wazi kwenye jicho Lake Yesu. Pale ulikuwa Mlima Moria, mahali ambapo mwana yule wa ahadi (Isaka), mhanga ambaye hakufanya upinzani kutolewa kafara, alikuwa amefungwa juu ya madhabahu ile -- akiwa ishara ya kafara ile ya Mwana wa Mungu. Pale ndipo Agano la baraka, yaani ahadi tukufu ya Masihi, ikawa imethibitishwa kwa yule baba wa wenye Imani (Ibrahimu). Mwanzo 22: 9, 16-18. Pale ndipo mahali ambapo ndimi za moto wa dhabihu zilipanda juu kuelekea mbinguni toka katika kiwanja kile cha kupuria cha Ornani/Arauna, na kugeuzia kando upanga wa malaika yule aharibuye 1 Mambo ya Nyakati 21 – Huo ulikuwa mfano stahiki kabisa wa kafara ya Mwokozi na upatanisho Wake kwa ajili ya wanadamu wenye dhambi/hatia. Yerusalemu ulikuwa umeinuliwa kwa heshima na Mungu juu ya dunia yote. Bwana alikuwa "Ameichagua Sayuni," Alikuwa

"Ametamani akae ndani Yake." Zaburi 132:13. Hapo ndipo mahali ambapo kwa miaka mingi manabii watakatifu walikuwa wametamka ujumbe wao wa onyo. Hapa ndiko makuhani walikuwa wamepepea vyetezo vyao, na wingu la moshi wa uvumba likapaa juu pamoja na maombi ya waabuduo, vyote vilipanda mbele za Mungu. Hapa ndipo ambapo kila siku damu ya wana-kondoo waliochinjwa ilitolewa, ikielekeza kwa Mwana-Kondoo wa Mungu ajaye. Pale ndipo Yehova alikuwa amefunua uwepo Wake katika wingu la utukufu juu ya Kiti cha Rehema. Mahali hapo ndipo iliposimikwa ncha ya ngazi ile ya ajabu inayounganisha dunia na mbingu Mwanzo 28:12; Yohana 1:51--Ngazi ile ambayo malaika wa Mungu walishuka na kupanda juu yake, na ambayo ilifungulia ulimwengu njia ya Patakatifu pa Patakatifu (Patakatifu mno). Endapo Israeli kama taifa lingedumisha uaminifu wake kwa Mbingu, Yerusalemu ingesimama milele kuwa mji mteule wa Mungu. Yeremia 17:21-25. Lakini historia ya watu hao waliopendelewa ilikuwa ni rekodi ya kurudi nyuma na kuasi. Walikuwa wameipinga neema ya Mbinguni, wakitumia vibaya fadhila yao, na wakachezea na kudharau fursa zao nzuri walizopewa. [GC 18.2; PK Aya ya 4]

**Maonyo Yadhihakiwa**

Ingawa Israeli ilikuwa "Imedhihaki wajumbe wa Mungu, na kuyadharau Maneno Yake, na kuwacheka manabii Wake" 2 Mambo ya Nyakati 36:16, bado Yeye aliendelea kujidhihirisha kwao, kama "Bwana, Mungu mwingi wa huruma, Mwenye fadhili, si mwepesi wa hasira, mwingi wa rehema na Kweli;" Kutoka 34: 6; licha ya wao kukataa tena na tena, rehema Yake ilikuwa imeendelea kuwasihi. Kwa upendo wa huruma na wenye sikitiko unaozidi ule wa baba kwa mtoto Wake, Mungu aka "tuma kwao mikono ya wajumbe Wake, akiondoka mapema, na kutuma; kwa sababu aliwahurumia watu Wake, na makao Yake." Wakati maonyo yenye mkazo, kusihi, na makaripio viliposhindwa, Aliwatumia zawadi kubwa na bora ya mbinguni; naam, Alimwaga mbingu yote kupitia Zawadi ile Moja (Mwanawe). [GC 19.1; PK Aya ya 5]

Mwana wa Mungu Mwenyewe alitumwa kuubembeleza ule mji uliokuwa hautaki kutubu au kuwa na majuto. Ni Kristo aliyewaleta Israeli kama mzabibu mzuri kutoka Misri. Zaburi 80: 8. Mkono Wake Mwenyewe ulikuwa umewafukuza mataifa kafiri mbele yao. Alikuwa ameupanda "Kilimani penye rutuba na kuzaa sana." Ulinzi Wake ukalijengea handaki (wigo) kulizunguka pande zote ili uwe salama. Watumishi Wake walikuwa wametumwa kulitunza. "Je! Ni kazi gani iliyoweza kutendeka ndani ya shamba Langu la mizabibu ambayo sijaifanya?" Isaya 5: 1-4. Ingawa Alitazamia kwamba litazaa zabibu, lakini likazaa zabibu mwitu, akiwa na shauku bado kwamba lizae matunda, Yeye alikuja Mwenyewe kushugulikia shamba Lake la mizabibu, yumkini huenda ukaokolewa, na usiharibiwe kabisa. Akalichimbia kulizunguka; kwa upendo Alilipogoa na

kuliendeleza. Hakuchoka katika juhudi Zake za kuokoa mzabibu huu alioupanda Mwenyewe. [GC 19.2; PK Aya ya 6]

Kwa miaka mitatu Bwana wa nuru na utukufu alikuwa akiingia na kutoka miongoni mwa watu Wake. Yeye "Akazunguka huko na huko, akitenda kazi njema na kuwaponya wote walioonewa na Ibilisi," Akiwaganga wote waliovunjika moyo, akiwatangazia wafungwa kufunguliwa kwao, akiwafanya vipofu wapate kuona, akiwafanya viwete waweze kutembea, akitakasa wenye ukoma, akifanya viziwi wasikie, akifufua wafu na kuhubiri kwa masikini habari njema. Matendo 10:38; Luka 4:18; Mathayo 11:5. Kwa watu wa matabaka yote vile vile mwito wa neema ulitolewa: "Njoni Kwangu, ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo, Nami nitawapumzisha." Mathayo 11:28. [GC 20.1; PK Aya ya 7]

Ingawa walimlipa mabaya badala ya mema, Na chuki badala ya upendo Wake. Zaburi 109: 5, Yeye aliendelea kutenda kwa bidii utume Wake wa rehema. Kamwe wale waliotafuta neema Yake, Yeye hakuwafukuza. Mtu asiye na mahali pa kuishi, akitanga-tanga, mwenye fedheha, shutuma na ufukara, Aliishi ili kuhudumia wahitaji na kuleta afueni penye maumivu, akiwasihi waipokee zawadi ile ya uzima. Mawimbi ya rehema, yaliyorudis nyuma na mioyo hiyo mikaidi, yalirudi kwao kama wimbi lenye nguvu zaidi la huruma na masikitiko, na upendo usioelezeka. Lakini Israeli alikuwa amemwacha mbali Rafiki yake wa karibu na Msaada Pekee. Kusihi Kwake kwa upendo kulidharauliwa, mashauri Yake yalipigwa teke kwa dharau, na maonyo Yake yalidhihakiwa. [GC 20.2; PK Aya ya 8]

Saa ya matumaini na msamaha ilikuwa ikiyoyoma kwa haraka; kikombe kile cha ghadhabu ya Mungu iliyoahirishwa kwa muda mrefu kilikuwa karibu kujaa. Wingu ambalo lilikuwa likikusanyika katika vizazi vile vyote vya ukafiri na uasi sasa likiwa jeusi na huzuni (misiba) ndani yake, lilikuwa karibu kupasuka juu ya watu wenye hatia; na Yeye peke Yake, ambaye Ndiye angeweza kuwaokoa kutoka katika hatima ya uangamivu inayokuja, walikuwa wamemdharau, wamemtukana, wamemnyanyasa, wamemkataa na kumkana, na si muda mrefu alikuwa anaenda kusulubiwa. Wakati Kristo alipokuwa anaangikwa juu ya msalaba wa Kalvari, ndipo siku ya Israeli kama taifa lililopendwa na kubarikiwa na Mungu ingekoma. Kupotea hata kwa roho moja tu, ni msiba unaozidi faida na hazina zote za ulimwengu huu; lakini Kristo alipoutazama Yerusalemu, uharibifu wa mji ule mzima, na taifa lote, ulikuwa mbele Yake,---Jiji lile, taifa lile, ambalo awali lilikuwa limechaguliwa na Mungu kuwa hazina Yake ya kipekee. [GC 20.3; PK Aya ya 9]

Manabii walikuwa wamelia machozi juu ya uasi wa Israeli na maangamizi na ukiwa wa kutisha ambavyo vilipatiliza dhambi zao. Yeremia alikuwa ametamani kwamba macho yake yangekuwa kama chemchemi ya machozi, ili alie mchana na

usiku kwa ajili ya binti za watu wake waliouawa na kwa ajili ya kundi la Bwana lililochukuliwa mateka. Yeremia 9: 1; 13:17. Je! Ni huzuni gani aliyokuwa nayo Yeye Yesu, ambaye jicho Lake la kinabii liliona mbele, si tu miaka mingi, bali vizazi vingi! Alimwona yule malaika anayeharibu akiwa na upanga ulioinuliwa juu ya mji huo ambao kwa muda mrefu ulikuwa makazi ya Yehova. Kutoka kwenye kilele cha mlima wa Mizeituni, mahali pale pale alipokuja kusimama Tito na jeshi lake (70 BK), Aliangalia ng'ambo ya bonde, juu ya nyua zile takatifu, pamoja na baraza zake zenye matao na nguzo, na kwa macho yakiwa hayaoni vizuri kwa machozi yaliyomlengalenga, aliona picha ya kutisha, kuta zile zikiwa zimezungukwa na majeshi ya kigeni. Alisikia vishindo vya miguu ya majeshi yaliyokuwa yanasonga kwa ajili ya vita. Alizisikia sauti za akina mama na watoto zikilia kwa kukosa mkate katika mji uliozingirwa. Aliiona nyumba Yake takatifu na nzuri (hekalu), majengo yake ya kifalme na minara yake, vyote vikiteketezwa kwa moto, na mahali hapo yaliposimama majengo mara ya kwanza, pakawa na rundo la mabaki ya vifusi vinavyofuka moshi. [GC 21.1; PK Aya ya 10]

### Kutawanywa Katika Kila Nchi

Akitazama matukio ya siku zijazo, aliwaona watu wa agano (Wayahudi) wakiwa wametawanyika katika kila nchi, "kama mabaki ya meli iliyovunjika katika mwambao wa jangwa." Katika kisasi kilichokuwa karibu kuwaangukia watoto wake, Aliona ladha ya kwanza kutoka katika kikombe hicho cha ghadhabu ambacho wakati wa hukumu ya mwisho ni sharti anywe mpaka matone yake ya mwisho. Huruma ya Mungu, upendo Wake wenye kujali, vilipata kutamkwa katika maneno haya yaliyojaa huzni n amaombolezo: "Ee Yerusalemu, Yerusalemu, uwauaye manabii, na kuwapiga kwa mawe wale waliotumwa kwako! Ni mara ngapi nimetaka kuwakusanya pamoja watoto wako, kama vile kuku avikusanyavyo pamoja vifaranga vyake chini ya mabawa yake, lakini hamkutaka!" Laiti ungalijua, wakati wa kujiliwa kwako, ee taifa liliopendwa zaidi ya mataifa yote, na yakupasayo amani! Nimemzuia malaika wa haki, nimekuita utubu, lakini bila mfanikio. Sio watumishi wa kawaida tu, wajumbe, na manabii, ambao umewakataa na kuwagomea, lakini umemkataa Mtakatifu wa Israeli, Mkombozi wako. Ukiangamizwa, ni wewe peke yako utawajibika kwa hilo. "Wala hamtaki kuja Kwangu mpate kuwa na uzima." Mathayo 23:37; Yohana 5:40. [GC 21.2; PK Aya ya 11]

Kristo aliona katika Yerusalemu ishara ya ulimwengu ulio sugu kwa kutokuwa na imani na kuasi na ambayo inaharakisha kukutana na hukumu za Mungu za kupatiliza. Maumivu ya jamii wanadamu iliyoanguka, ikaishinikiza nafsi Yake na kuilazimisha midomo kutoa kilio kizito cha uchungu. Aliona rekodi ya dhambi iliyoonyeshwa kama chanzo cha taabu, machozi, na damu za wanadamu; Moyo Wake ulisukumwa na huruma isiyo na kikomo kwa walimwengu waliotaabika na

kuteseka; Alitamani sana kuwaondolea wote maumivu yao. Lakini hata kama mkono Wake ungeweza kuzuia wimbi la misiba utakaowapata mwanadamu; ni wachache tu ambao wangetafuta Yule aliye Chanzo chao cha msaada. Yeye alikuwa tayari kutoa nafsi Yake hadi kifo, kuleta wokovu mahali pale ambapo wangeweza kuupata; lakini ni wachache tu ambao wangemwendea Yeye ili wapate uzima. [GC 22.1; PK Aya ya 12]

**Mwana Wa Mungu Atokwa Machozi**

Mkuu wa enzi ya mbinguni akidondokwa machozi! Mwana wa Mungu asiye na kikomo akitaabika moyoni, na kuinama chini kwa uchungu mkubwa! Tukio hilo liliijaza mbingu yote kwa mshangao. Tukio hilo linatufunulia sisi ukubwa wa hali ya uovu wa dhambi; linatuonyesha jinsi kazi ilivyo ngumu, hata Kwake Yeye Mwenye Nguvu isiyo na ukomo, kuwaokoa wenye dhambi kutokana na matokeo ya kukiuka Sheria ya Mungu. Yesu, akiangalia chini mpaka kizazi cha mwisho, aliona ulimwengu uliohusishwa katika udanganyifu sawa na ule uliosababisha uharibifu wa Yerusalemu. Dhambi kubwa ya Wayahudi ilikuwa ni kumkataa Kristo; dhambi kubwa ya ulimwengu wa Kikristo leo aliona ingekuwa ni kukataa kwao Sheria ya Mungu, msingi wa serikali Yake mbinguni na duniani. Amri za Yehova zingeweza kudharauliwa na kufutwa kama si kitu kwa watu. Mamilioni ya watu wako katika vifungo (utumwa) vya dhambi, ni watumwa wa Shetani, ambao watakumbwa na mateso ya mauti ya pili, wangeweza kusikiliza Maneno ya Ukweli katika siku ya kujiliwa kwao. Ni Upofu wa kutisha huo! Kupumbazikwa kwa ajabu jamani! [GC 22.2; PK Aya ya 13]

Siku mbili kabla ya Pasaka, wakati Kristo alipoondoka hekaluni kwa mara Yake ya mwisho, baada ya kukemea unafiki wa watawala wa Kiyahudi, alitoka tena na wanafunzi Wake kwenda kwenye Mlima wa Mizeituni na kuketi pamoja nao kwenye kilele cha mteremko wenye nyasi wakiutazama mji. Akaangalia tena kuta zake, minara yake, na majumba yake. Kwa mara nyingine tena aliliona hekalu katika uzuri wake wa kung'aa, taji ya uzuri ikiufunika mlima huo mtakatifu. [GC 23.1; PK Aya ya 14]

**Hekalu La Kifahari**

Miaka elfu moja kabla, mwimba Zaburi alielezea vizuri upendeleo wa Mungu kwa Israeli kwa kuifanya nyumba Yake takatifu kuwa makao Yake: “Kibanda Chake pia kiko Salemu, Na maskani Yake iko Sayuni.” Bali "aliichagua kabila ya Yuda, Mlima Sayuni alioupenda. Akajenga Patakatifu Pake kama vilele.” Zaburi 76: 2; 78:68, 69. Hekalu la kwanza lilikuwa limejengwa wakati wa mafanikio zaidi katika historia ya Israeli. Akiba kubwa ya hazina kwa kusudi la ujenzi wa hekalu ilikuwa imekusanywa na Mfalme Daudi, na mipango na ramani ya ujenzi wake ilichorwa kwa uongozi wa Mungu. 1 Mambo ya Nyakati 28:12, 19. Sulemani, mfalme mwenye hekima zaidi kati ya wafalme wa Israeli, ndiye aliyetekeleza

kazi hiyo. Hekalu hili lilikuwa jengo zuri sana ambalo ulimwengu haujapata kuona. Walakini Bwana alikuwa ametangaza hivi kupitia nabii Hagai, kuhusu hekalu hili la pili: "Utukufu wa mwisho wa nyumba hii utakuwa mkuu kuliko utukufu wake wa kwanza." ""Nami nitatikisa mataifa yote, na vitu vinavyotamaniwa na mataifa yote vitakuja; Nami nitaijaza nyumba hii utukufu, asema BWANA wa majeshi." Hagai 2:9, 7. [GC 23.2; PK Aya ya 15]

Baada ya Nebukadreza kuharibu hekalu hili, hekalu jipya lilijengwa kama miaka mia tano kabla ya kuzaliwa Kwake Kristo na watu ambao walikuwa wamerejea kama mateka katika nchi iliyoharibiwa na kukaribia kutelekezwa, wakitokea kwenye utumwa wa muda mrefu. Wakati huo walikuwemo wazee ambao walikuwa wameuona utukufu wa hekalu la Sulemani, na ambao walilia ulipowekwa msingi wa jengo jipya, wakisema hili la sasa, limekuwa na viwango duni sana kuliko lile la zamani. Hisia iliyokuwapo imeelezewa kwa msukumo na yule nabii aliposema: "Miongoni mwenu amebaki nani aliyeiona nyumba hii katika utukufu wake wa kwanza? Nanyi mnaionaje sasa? Je! Mbele ya macho yenu, siyo kama si kitu?" Hagai 2: 3; Ezra 3:12. Ndipo ikatolewa ahadi kwamba utukufu wa jengo hili la mwisho ungekuwa mkubwa kuliko ule wa nyumba ya kwanza. [GC 23.3; PK Aya ya 16]

Lakini hekalula pili halikupendeza kama lile la kwanza; wala halikutukuzwa na kwa viashiria vinavyoonekana vya uwepo wa Mungu ambavyo vilionekana katika hekalu la kwanza. Hakukuwa na udhihirisho wa uwezo usio wa kawaida kuashiria wakati wa kuwekwa kwake wakfu. Hakuna wingu la utukufu lililoonekana kujaza Patakatifu hapo palipojengwa baadaye upya. Hakuna moto ulioshuka kutoka mbinguni kuteketeza kafara juu ya madhabahu yake. Hapakuwa na nuru tukufu ya Shekina kati ya makerubi ndani ya Patakatifu pa Patakatifu; Sanduku la Agano, Kiti cha Rehema, na Mbao za Ushuhuda (Vipande viwili vya Mawe, vyenye Amri Kumi), havikuwamo ndani yake. Hakuna sauti iliyotoka mbinguni kumjibu kuhani alipouliza kujua mapenzi ya Yehova. [GC 24.1; PK Aya ya 17]

### Lapewa Heshima Kwa Kuwepo Kwake Kristo

Kwa karne nyingi Wayahudi walikuwa wamejaribu kutafuta bila mafanikio jinsi ahadi ya Mungu iliyotolewa na Hagai ilivyokuwa imetimizwa; ila kiburi na kutokuamini kwao vilipofusha akili zao kuelewa maana halisi ya Maneno ya nabii. Hekalu lile la pili halikuheshimiwa na wingu la utukufu wa Yehova, bali na uwepo halisi/mbashara wa Yule ambaye ndani Yake ulikaa utimilifu wa Uungu kimwili--ambaye alikuwa Mungu Mwenyewe aliyedhihirishwa katika mwili. Yeye aliyekuwa "Matamanio ya mataifa yote" hakika Alikuwa amekuja katika Hekalu, wakati Yule Mtu wa Nazareti alipofundisha na kuponya katika kumbi zake takatifu. Ni katika uwepo wa Kristo, na katika namna hiyo tu, ndiyo hekalu la pili lilizidi hekalu la kwanza kwa utukufu. Lakini Israeli imemsukuma mbali Yeye aliyekuwa

Zawadi ya mbinguni. Siku ile ambayo Mwalimu Yule mnyenyekevu alipopita na kutoka katika lango lake la dhahabu, utukufu ulikuwa umeondoka milele kutoka katika hekalu lile. Tayari Maneno ya Mwokozi yalikuwa yametimizwa: "nyumba yenu mmeachiwa hali ya ukiwa." Mathayo 23:38. [GC 24.2; PK Aya ya 18]

Wanafunzi walikuwa wamepigwa na butwaa juu ya utabiri wa Kristo juu ya kutekwa kwa hekalu, na walitamani kuelewa kikamilifu zaidi maana ya Maneno Yake. Mali, kazi, na ustadi wa kusanifu majengo, vilikuwa vimetumiwa kwa ukarimu mwingi kwa zaidi ya miaka arobaini ili kuongeza uzuri wake. Herode Mkuu alikuwa amewekeza utajiri wa Kirumi na hazina ya Kiyahudi, na hata mfalme wa himaya za ulimwengu wote unaojulikana, alikuwa amelitajirisha na zawadi zake. Vipande vikubwa sana vya matofali ya marumaru nyeupe, vyenye ukubwa wa kustaajabisha, vilisafirishwa kutoka Rumi kwa ujenzi huu, navyo vikawa sehemu ya jengo hili; na wanafunzi hao walivuta umakini wa Mwalimu wao kwenye majengo yale, kwa kusema: "tazama, yalivyo mawe na majengo haya!" Marko 13:1. [GC 24.3; PK Aya ya 19]

**Mambo Hayo Yatakuwa Lini**

Kuhusiana na maneno hayo, Yesu alitoa jibu zito na la kushtua: "Amin, nawaambieni, Halitasalia hapa jiwe juu ya jiwe ambalo halitabomoshwa." Mathayo 24: 2. [GC 25.1; PK Aya ya 20]

Wanafunzi waliusianisha utabiri wa kubomolewa kwa majengo ya Yerusalemu na matukio ya kuja kwa Kristo Mwenyewe kimwili na katika utukufu Wake na muda ule wa kuchukua kiti cha enzi cha ufalme wa ulimwengu, kuwaadhibu Wayahudi wasiotaka kutubu, na kuvunja kongwa la utumwa wa Kirumi kwa taifa lile. Bwana alikuwa amewaambia kwamba atakuja tena mara ya pili. Kwa hivyo wakati alipotaja hukumu juu ya Yerusalemu, akili zao zikaelekezwa katika kule kuja Kwake; na walipokuwa wamekusanyika karibu na Mwokozi juu ya Mlima wa Mizeituni, waliuliza: "Tuambie, mambo hayo yatakuwa lini? Nayo ni nini dalili ya kuja Kwako, na ya mwisho wa dunia?" Mstari wa 3. [GC 25.2; PK Aya ya 21]

Mambo ya wakati ujao yalifichwa machoni pa wanafunzi kwa ajili ya rehema Zake Bwana. Endapo wakati huo wangeelewa kikamilifu ukweli wa mambo haya mawili ya kutisha-- yaani mateso na kifo cha Mkombozi, na uharibifu wa mji wao pamoja na hekalu lao, wangezidiwa na hofu kuu. Kristo aliwasilisha mbele yao muhtasari wa matukio muhimu yatakayotendeka kabla ya mwisho wa wakati. Maneno Yake hayakueleweka kikamilifu wakati huo; lakini maana yake ingeendelea kufunuliwa kadri watu Wake walivyokuwa na matamanio na mafundisho yale yaliyotolewa humo. Unabii alioutamka ulikuwa na maana mbili; wakati ulikuwa unatabiri uharibifu wa Yerusalemu, ulifananishwa pia na utisho

mkuu wa siku kuu ya mwisho (siku ya hukumu ya binadamu wote). [GC 25.2; PK Aya ya 22]

Yesu aliwatangazia wanafunzi Wake waliosikiliza hukumu ambazo zinapaswa kuwaangukia Israeli walioasi, na haswa kisasi cha ghadhabu ambacho kingewajia kwa kumkataa kwao na kumsulubisha Masihi. Ishara zisizoweza kukosewa zingeweza kukitangulia kilele kile cha kutisha. Saa ile ya kutisha ingekuja kwa ghafla na haraka. Na Mwokozi aliwaonya wafuasi Wake: "Basi hapo mtakapoliona chukizo la uharibifu lile lililonenwa na nabii Danieli, limesimama katika Patakatifu (asomaye na afahamu), kisha wale walio katika Uyahudi wakimbilie milimani." Mathayo 24:15, 16; Luka 21:20, 21. Wakati ule ambapo viwango na taratibu za ibada ya sanamu za Warumi zingewekwa katika ardhi ile takatifu, iliyotandaa mamia ya mita za urefu nje ya kuta za mji ule, basi hapo ndiyo wafuasi wale wa Kristo wangepata usalama wao kwa kukimbia. Wakati ule ishara ya lile onyo inapoonekana, wale ambao walitaka kuokoa nafsi zao walipaswa kukimbia bila kuchelewa. Katika nchi yote ile ya Yuda, vile vile katika Yerusalemu yenyewe, dalili zile za onyo la kukimbia ni sharti zitiiwe mara moja. Yule aliyeko juu ya dari na asishuke kwenda nyumbani kwake, hata kama anataka kuokoa hazina zake alizozithamini zaidi. Wale ambao watakuwa wakifanya kazi katika mashambani au kwenye mimea yao ya mizabibu hawapaswi kurudi nyuma ili kufuata vazi la nje walililoliweka kando ya shamba wakati walipokuwa wakihenyeka na kazi kwenye joto la mchana. Walitakiwa wasisite-site hata kidogo, wasije wakajikuta wameingia katika maangamizi yale ya watu wote (jumla.) [GC 25.4; PK Aya ya 23]

Katika enzi ya utawala wa Herode, Yerusalemu haikuwa imependezeshwa vizuri tu, bali pia ilikuwa imejengwa kwa minara, kuta, na ngome, na kuongezea uimara katika asili yake pale ulipokaa, ulikuwa mji usioweza kuingilika kirahisi. Yeye ambaye kwa wakati huo angeweza kutabiri kuangamizwa kwake hadharani kama Nuhu katika siku zake, angeitwa mtoa tahadhari zilizotiwa chumvi, na mwendawazimu. Lakini Kristo alikuwa amesema: "Mbingu na nchi zitapita; lakini Maneno Yangu hayatapita kamwe." Mathayo 24:35. Kwa sababu ya dhambi zake, ghadhabu ilikuwa imeshatangazwa juu ya Yerusalemu, na ukaidi wake wa kutoamini, ulihakikisha uharibifu wake. [GC 26.1; PK Aya ya 24]

Bwana alikuwa ametangaza kupitia nabii Mika: "Sikieni haya, tafadhali, enyi vichwa vya nyumba ya Yakobo, mnaoitawala nyumba ya Israeli, mnaochukia hukumu, na kuipotosha adili. Wanaijenga Sayuni kwa damu, na Yerusalemu kwa uovu. Wakuu wake uhukumu ili wapate rushwa, na makuhani wake hufundisha ili wapate ijara, na manabii wake hubashiri ili wapate fedha; ila hata hivyo watamtegemea Bwana, na kusema, Je! Hayupo Bwana katikati yetu? Hapana neno baya lolote litakalotufikia." Mika 3: 9-11. [GC 26.2; PK Aya ya 25]

Maneno haya yalielezea kwa uaminifu kabisa ufisadi na kujihesabia haki kwa wakazi wa Yerusalemu. Wakati wakidai kutii kwa ushupavu maagizo ya sheria ya Mungu, walikuwa wakizivunja kanuni Zake zote. Walimchukia Kristo kwa sababu maisha Yake ya usafi na utakatifu yalifunua uovu wao; na wakamshutumu kuwa Yeye Ndiye sababu ya taabu zao zote zilizowapata kama matokeo ya dhambi zao. Ingawa walifahamu kuwa Yeye hana dhambi, walikuwa wametangaza kwamba kifo Chake ni sharti kitokee kwa usalama wa taifa lao. "Tukimwacha hivi" viongozi wa Kiyahudi walisema, "watu wote watamwamini; na Warumi watakuja, na watatuondolea mahali petu na taifa letu." Yohana 11:48. Kama Kristo angeuawa, yaani angetolewa kafara, basi wao wangeweza tena kuwa watu wenye nguvu na umoja zaidi. Hivyo ndivyo walivyowaza, na wakakubaliana na uamuzi wa kuhani wao mkuu, kwamba ni heri mtu mmoja afe kuliko taifa lote kuangamia. [GC 27.1; PK Aya ya 26]

Kwa hivyo viongozi wa Kiyahudi walikuwa wameijenga "Sayuni kwa damu, na Yerusalemu kwa uovu." Mika 3:10. Wakati walipomwua Mwokozi wao kwa sababu alikemea dhambi zao, bado walijihesabia haki (uadilifu) wao wenyewe kwa njia ya kushangaza na hata wakajiona kwamba ni watu waliopendelewa na Mungu na kutarajia Bwana atawaokoa kutoka kwa maadui zao. "Basi, kwa ajili yenu" akaendelea nabii, "Sayuni utalimwa kama shamba lilimwavyo, na Yerusalemu utakuwa magofu; na mlima wa nyumba utakuwa kama mahali palipoinuka msituni." Mstari wa 12. [GC 27.2; PK Aya ya 27]

### Uvumilivu Wa Mungu

Kwa karibu miaka ipatayo arobaini baada ya maangamizi ya Yerusalemu kutangazwa na Kristo Mwenyewe, Bwana alikawiza hukumu Zake juu ya mji na taifa hili. Ustahimilivu wa Mungu ulikuwa wa kushangaza kwa watu hawa waliokataa injili Yake na waliomuua Mwanawe. Mfano wa mti usiozaa matunda uliwakilisha jinsi Mungu alivyoshughulika na taifa la Kiyahudi. Amri hii ilikuwa imetolewa, "uukate, mbona hata nchi unaiharibu?" Luka 13: 7, lakini rehema ya Mungu ilikuwa imeiepusha adhabu kwa muda mrefu kidogo. Bado kulikuwa na watu wengi kati ya Wayahudi ambao walikuwa hawajui tabia na kazi ya Kristo. Na Watoto nao walikuwa hawajazifurahia zile fursa nzuri au kupokea nuru ile ambayo wazazi wao walikuwa wameipiga teke. Kupitia njia ya mahubiri ya mitume na wenzao, Mungu angefanya nuru ile iweze kuwaangazia; wangeruhusiwa kuona jinsi unabii unavyotimizwa, sio tu katika kuzaliwa kwa Kristo na maisha ya Yake, bali pia katika kifo Chake na ufufuo Wake. Watoto hawakuhukumiwa kwa ajili ya dhambi za wazazi wao; lakini wakati walipokuwa wamepokea ufahamu wa nuru ile yote iliyotolewa kwa wazazi wao Ezekiel 18:18-24, na watoto wale wakaikataa ile nuru ya ziada waliyopewa wao wenyewe, walifanywa kushiriki dhambi za wazazi wao, na kukijaza kikombe cha uovu wao. [GC 27.4; PK Aya ya 28]

**Hali Ya Kusikitisha Ya Taifa**

Ustahimilivu wa Mungu kwa mji wa Yerusalemu ulithibitisha tu ukaidi wa Wayahudi ambao hawakutaka kufanya toba ya maovu yao. Katika chuki yao na ukatili wao kwa wanafunzi wa Yesu walikuwa wameikataa nafasi yao ya mwisho ya rehema. Ndipo Mungu akaondoa ulinzi Wake kutoka kwao na akaondoa uweza Wake wa kumzuia Shetani na malaika zake, na taifa lile likaachwa katika utawala wa kiongozi waliyemchagua wenyewe. Watoto wake walikuwa wameikataa kwa madharau neema ya Kristo, ambayo ingewawezesha kushinda misukumo yao ya uovu, na hivyo ile misukumo mibaya ikashinda. Shetani alikuwa amewaamshia miskumo mikali iliyo mibaya na tamaa za mwili/roho za kutisha na zenye kudhalilisha (tamaa za dhambi za mwili, za macho na kiburi cha maisha). Hekima ikapotea kwa wanadamu, yaani utashi haukutumiwa vyema na akili zikaruka; walikuwa wamepoteza uwezo wa kufikiri na busara (akili zimepotea), wakiongozwa na mihemko na hasira za kijinga na kutisha, na hasira zenye upofu. Wakawa kama shetani mwenyewe au mapepo katika ukatili wao. Katika familia na katika taifa, kati ya tabaka la juu na la chini kabisa, kulikuwa na tuhuma za kutokuaminiana, wivu, chuki, ugomvi, uasi, na mauaji. Hakukuwa na usalama popote pale. Marafiki, ndugu na jamaa wa damu walisalitiana. Wazazi waliwachinja watoto wao, nao watoto wakawaua wazazi wao. Watawala wa watu (viongozi) hawakuwa na nguvu za kujitawala wenyewe. Tamaa, hasira na mihemko isiyodhibitiwa ikawafanya wawe jeuri, katili na madikteta. Wayahudi walikuwa wamekubali ushuhuda wa uwongo kumhukumu Mwana wa Mungu asiye na hatia. Sasa mashtaka yao yale ya uongo yakafanya maisha yao wenyewe kutokuwa na uhakika. Kwa matendo yao, na mitindo yao ya maisha walikuwa wameshasema kwa muda mrefu: "Mkomesheni Mtakatifu wa Israeli mbele yetu." Isaya 30:11. Sasa walipewa matakwa yao, kufanya lolote wanalotaka kulifanya bila kizuizi. Hofu na uchaji wa Mungu havikuwasumbua tena. Shetani akawa kiongozi au bosi wa taifa, na viongozi wa juu zaidi wa kiraia na dini walikuwa chini yake. [GC 28.1; PK Aya ya 29]

Viongozi wa vikundi pinzani wakati huo (marengo) waliungana kupora na kutesa wahanga wao walio masikini na wanyonge na wasioweza kujitetea, na tena vikosi vyao vikageukiana na kuchinjana kinyama bila huruma. Hata utakatifu wa hekalu haukuweza kuzuia ukatili wao wenye kutisha. Waliokuja kwenye ibada mle walichinjwa mbele ya madhabahu, na Patakatifu palichafuliwa kwa unajisi na maiti za wale waliouawa. Lakini bado wakiwa na dhana yao ya upofu na ya kufuru, wahamasishaji wa kazi hii ya kuzimu walitangaza hadharani kwamba hawakuwa na hofu kwamba Yerusalemu ingeangamizwa, kwani ulikuwa mji wa Mungu Mwenyewe. Ili kuimarisha nguvu zao kwa uthabiti zaidi, waliwahonga manabii wa uongo kutangaza kwamba watu wangojee ukombozi

utakaokuja kutoka kwa Mungu, hata wakati ule majeshi ya Kirumi yalipokuwa yamekwishalizingira lile hekalu. Mpaka mwisho, umati wa watu hao ulishikilia tumaini hilo la uongo kwamba Yeye Aliye juu angeingilia kati ili kuwashinda wapinzani wao. Lakini Israeli alikuwa ameukataa kwa dharau ulinzi wa Mungu, na sasa hakuwa na kinga yoyote. Yerusalemu iliyojaa huzuni jamani! Iliyoraruliwa-raruliwa vipande vipande na mafarakano ya ndani, damu ya watoto wake waliouana wenyewe kwa wenyewe sasa ikawa imepaka barabara rangi nyekundu mwote, wakati majeshi ya wageni yakibomoa ngome zake na kuua watu wake wa vita, yaani wanajeshi wake! [GC 29.1; PK Aya ya 30]

**Utabiri Wa Kristo Watimizwa**

Kila utabiri uliotolewa na Kristo juu ya uharibifu wa Yerusalemu sasa ulitimizwa kabisa Neno kwa Neno. Wayahudi walipata uzoefu kamili wa Ukweli wa Maneno Yake yale ya onyo: "na kipimo kile mpimiacho, ndicho mtakachopimiwa." Mathayo 7: 2. [GC 29.2; PK Aya ya 31]

Ishara na maajabu yalionekana, vikitishia majanga na maangamizi. Usiku wa manane nuru isiyo ya kawaida iliangaza juu ya hekalu na madhabahu. Juu ya mawingu wakati wa machweo ya jua, kulikuwa na picha za magari ya vita na wanajeshi waliokusanyika kwa ajili ya vita. Makuhani waliokuwa wakihudumu usiku katika Patakatifu walitishwa na sauti za kushangaza; kisha dunia ilitetemeka, na sauti nyingi zikasikika zikilia: "Jamani hebu tuondokeni humu haraka." Lango kubwa la mashariki, ambalo lilikuwa zito sana kiasi kwamba lilikuwa gumu kufungwa hata na wanaume ishirini hivi, na ambalo lilifungwa na bawaba kubwa sana za chuma zilizochimbiwa ndani ya zege ngumu, lilifunguka usiku wa manane, na yule aliyelifungua hakuonekana na mtu yoyote. — Milman, Historia ya Wayahudi, kitabu cha 13. [GC 29.3; PK Aya ya 32]

Kwa miaka saba mtu mmoja aliendelea kupanda na kushuka, akizunguka mitaa ya Yerusalemu na kuwatangazia majanga ambayo yangeujia mji huo. Mchana na usiku akiimba wimbo wa maombolezo kama mwendawazimu: "Sauti kutoka mashariki! Sauti kutoka magharibi! Sauti kutoka katika pepo nne! (Pande zote za dira), sauti dhidi ya Yerusalemu na dhidi ya hekalu! sauti dhidi ya bwana-arusi na bi-arusi! Sauti dhidi ya watu wote!"-Ibid. Kiumbe huyu wa ajabu alifungwa gerezani na kupigwa mijeledi, lakini hakuna malalamiko yoyote yaliyotoka kwenye midomo yake. Aliyajibu matusi, manyanyaso na jeuri kwa kusema tu: "Ole, ole kwa Yerusalemu!" "Ole, ole wao wakazi wakaao humo!" Kilio chake cha onyo hakikukoma hadi alipochinjwa katika mji huo uliokuwa katika harakati ya kuhusuriwa (kuzingirwa) kama alivyokuwa ametabiri. [GC 30.1; PK Aya ya 33]

**Wakristo Waokoka**

Hakuna Mkristo hata mmoja aliyeangamia katika uharibifu wa Yerusalemu. Kristo alikuwa amewapa wanafunzi Wake onyo, na wote walioyaaamini Maneno Yake waliingojea ile ishara waliyoahidiwa. “Lakini, hapo mtakapoona mji wa Yerusalemu umezungukwa na majeshi, Yesu alisema “ndipo jueni ya kwamba uharibifu wake umekaribia. Ndipo walio katika Uyahudi na wakimbilie milimani, na walio katikati yake wakimbilie nje.” Luka 21:20, 21. Baada ya Warumi kuuhusuru ule mji wakiongozwa na Cestus, ghafla waliacha kuuzingira ule mji pasipo watu kutarajia, wakati kila kitu kilionekana kuwa kinaenda vyema kufanikisha shambulio hilo la haraka. Waliozingirwa, wakiwa wamekata tamaa ya kuweza kumshinda mpinzani aliyewavamia, nao walikuwa kwenye hatua ya kujisalimisha, wakati jenerali huyo wa Kirumi alipoyaondoa majeshi yake na kurudi bila sababu ya kimsingi. Lakini uongozi wenye rehema wa Mungu ndiyo ulikuwa umeshikilia usukani kwenye matukio hayo kwa manufaa ya watu Wake Mwenyewe. Ishara ile iliyoahidiwa ilikuwa imekwisha kutolewa kwa wale Wakristo waliokuwa wanasubiri kufanya hivyo, na sasa nafasi ilitolewa kwa wote ambao walikuwa tayari kutii onyo la Mwokozi. Matukio yalikuwa yanaratibitiwa na majaliwa ya Mungu makubwa, kiasi kwamba Wayahudi na hata Warumi hawakuweza kuzuia kukimbia kwa Wakristo. Baada ya kurudi nyuma kwa Cestio, Jeshi la Kiyahudi, likajumuika pamoja kutoka Yerusalemu, wakilifuata jeshi hilo la Rumi lililokuwa linarudi nyuma; na wakati vikosi vyote viwili vinapambana kikamilifu ana kwa ana, Wakristo wakapata nafasi ya kutoroka kutoka katika mji huo. Kwa wakati huu maadui waliokuwa na uwezo wa kuwazuia walikuwa wameondolewa katika nchi. Wakati wa kuzingirwa, Wayahudi walikuwa wamekusanyika huko Yerusalemu kusherekea Sikukuu ya Vibanda, na hivyo Wakristo kote nchini waliweza kutoroka bila kusumbuliwa. Bila ya kuchelewa walikimbilia mahali salama-- katika jiji la Pella, katika nchi ya Perea, ng'ambo ya Yordani. [GC 30.2; PK Aya ya 34]

### Wayahudi Waendelea Kukataa Kusalimu Amri

Vikosi vya jeshi la Wayahudi, vikamfuata kwa nyuma Cestius na jeshi lake, nao wakaanguka nyuma yao kwa ukali kiasi cha kutishiwa kuangamizwa kabisa. Ilikuwa ni kwa shida sana kwamba Warumi walifanikiwa kurudisha nyuma majeshi yao. Wayahudi walitoroka bila hasara yoyote ya maana, wakarudi na nyara zao kwa ushindi na shangwe huko Yerusalemu. Hata hivyo mafanikio haya yaliyoonekana dhahiri yaliwaletea maovu tu. Yalichochea roho ya upinzani na ukaidi dhidi ya Warumi na kuleta haraka maafa (ole) yasiyoweza kutamkika juu ya mji uliokuwa unaendea maangamizi. [GC 31.1; PK Aya ya 35]

Majanga ya kutisha yaliuangukia Yerusalemu wakati jiji lile lilipozingirwa tena na Tito. Jiji lile lizingirwa wakati wa Pasaka, wakati ambapo mamilioni ya Wayahudi walipokuwa wamekusanyika ndani ya kuta zake. Hifadhi yao kwenye

maghala ya vyakula na vitu vingine vya kujikimu kimaisha, kwa kawaida inapotumiwa kwa uangalifu ingeweza kuwahudumia wenyeji wake kwa miaka mingi, ila hapo awali iliharibiwa kutokana na wivu na kulipiza kisasi kwa vikundi vinavyogombana, na sasa hofu ya kufa kwa njaa ilitapakaa kote. Kipimo cha ngano kiliuzwa kwa talanta moja. Maumivu ya njaa yalikuwa makali sana kiasi kwamba watu walitafuna ngozi za mikanda, viatu (makubasi) na ngozi zilizofunika ngao zao. Idadi kubwa ya watu walitoka usiku kisirisiri kukusanya mimea ya mwituni inayoota nje ya kuta za jiji, ingawa wengi walikamatwa na kuuawa kwa mateso makali, na mara nyingi wale waliorudi salama walikuwa wananyag'anywa na wenzao kile walichokuwa wamekikusanya katika hatari na shida kubwa. Mateso ya kikatili na kinyama mno yalisababishwa na wale walioko madarakani, kwa kuwapora wale wasio na kitu na masikini, akiba yao kidogo na ya mwisho ambayo wangeweza kuificha. Na ukatili huu mara kwa mara haukufanywa na watu ambao walikuwa na njaa, bali wale waliokuwa wamekula na kushiba vizuri, na ambao walikuwa wakitamani tu kujiwekea akiba ya chakula kwa siku zijazo. [GC 31.2; PK Aya ya 36]

Maelfu ya watu waliangamia kutokana na njaa, maradhi na tauni. Tabia ya asili ya mapenzi na huruma aliyopewa mwanadamu ilionekana imeharibiwa kabisa. Waume waliwapora wake zao, na wake pia wakawaibia waume zao. Watoto walionekana wakinyakua chakula kutoka vinywani mwa wazazi wao wazee kwa nguvu. Swali la nabii, "Je! Mwanamke aweza kumsahau mtoto wake anyonyaye, hata asimhurumie mwana wa tumbo lake?" lilipata jibu ndani ya kuta za mji huu uliokuwa umepatwa majanga: "Mikono ya wanawake wenye huruma Imewatokosa watoto wao wenyewe; Walikuwa ndio chakula chao Katika uharibifu wa binti ya watu wangu." Isaya 49:15; Maombolezo 4:10. Unabii huu wenye ilani, uliotolewa karne kumi na nne kabla, sasa ulitimia: "Mwanamke kati yenu aliye mwororo na laini, ambaye hangehatirisha kuweka wayo wa mguu wake nchi kwa umalidadi na ulaini, jicho lake huyu litakuwa ovu juu ya mume wa kifuani mwake, na juu ya mwanawe, na juu ya binti yake.... na juu ya wanawe atakaowazaa; kwa kuwa atawala kwa siri, kwa uhitaji wa vitu vyote; katika mazingirwa na mkazo utakaokazwa na adui yako katika malango yako." Kumbukumbu la Torati 28:56, 57. [GC 32.1; PK Aya ya 37]

**Maangamizi Kamili**

Viongozi wa wa Kirumi walijitahidi kuwapa kipigo cha hofu Wayahudi na hivyo kuwafanya wajisalimishe kwao. Mateka au wafungwa wale ambao waliowapinga wakati wa kuchukuliwa, walipigwa mijeledi, wakateswa, na kusulubiwa mbele ya ukuta wa jiji lile. Mamia waliuawa kila siku kwa njia kama hizi, na kazi ya kutisha iliendelea mpaka kando ya Bonde la Yehoshafati na huko Kalwari, misalaba iliwekwa kwa idadi kubwa sana kiasi kwamba kulikuwa hakuna nafasi ya

kupita katikati yake. Hivyo ndivyo walivyotembelewa kwa jinsi ya kutisha sana na laana iliyotamkwa mbele ya kiti cha hukumu cha Pilato: “Damu Yake na iwe juu yetu, na juu ya watoto wetu.” Mathayo 27:25. [GC 32.2; PK Aya ya 38]

Jemedari Tito alitaka kuahirisha matukio haya ya kutisha, na hivyo kuiepusha Yerusalemu kipimo chake kamili cha ghadhabu iliyomstahili. Alifadhaishwa mno alipoiona miili ya wafu ikiwa imelala katika marundo kwenye mabonde. Akiwa amevutiwa sana na uzuri wa hekalu, alilitazama kutoka kwenye kilele cha Mlima wa Mizeituni na akaamuru kwamba lisiguswe hata jiwe moja. Kabla ya kujaribu kumiliki hii ngome, alitoa wito wa dhati wa kuwasihi viongozi wa Kiyahudi wasije wakamlazimisha kupanajisi mahali patakatifu kwa damu. Kama wangekuja mbele kupigana mahali pengine popote (isipokuwa hekalu), kusingekuwa na Mrumi yoyote ambaye angeharibu utakatifu wa hekalu. Josephus mwenyewe (Kuhani, msomi, na mwanahistoria wa Kiyahudi), kwa wito wa ufasaha zaidi, aliwasihi Wayahudi wajisalimishe ili kujiokoa wao wenyewe, mji wao, na mahali pao pa ibada. Lakini maneno yake yalijibiwa kwa laana na matusi makali. Watu hawa walimshambulia kwa mishale yule mpatanishi wao wa mwisho wa kibinadamu, wakati akiendelea kusimama na kuwasihi. Wayahudi walikuwa wamekataa kule kusihi kwa Mwana wa Mungu, na sasa malalamiko na wito wa kuwasihi viliwafanya kudhamiria zaidi kupinga hadi mwisho. Jitihada za Tito kuokoa hekalu zilikuwa kazi bure. Yeye aliyekuwa Mkuu kuliko yeye alikuwa ameshatangaza kwamba hakuna jiwe ambalo litasalia juu ya lingine. [GC 32.3; PK Aya ya 39]

Ukaidi ule wa kijinga, wa viongozi wa Kiyahudi (vipofu), na uhalifu wa kuchukiza uliofanywa ndani ya mji uliokuwa umezingirwa, ulichochea hasira na ghadhabu ya Warumi, hatimaye Tito aliamua kulitwaa hekalu kwa mashambulizi makali. Alidhamiria kuwa hata hivyo kwa kadri inavyowezekana, lile hekalu lisitendewe uharibifu wowote. Lakini maagizo yake hayakuzingatiwa. Baada ya kurudi hemani kwake usiku ili kupumzika, Wayahudi waliokuwa ndani ya hekalu, wakaanza kuwashambulia askari wa Kirumi walioko nje. Katika mkiki huo, vijinga vya moto vilitupwa na askari kupitia eneo lilo wazi la ukumbi, na punde vyumba vilivyonakshiwa na mbao za mierezi katika nyumba hii takatifu vikawa vimewaka moto. Tito alikimbia kwenda mahali hapo, akifuatiwa na majenerali wake na wakuu wa majeshi ya Kirumi, na kuwaamuru askari wake wazime ule moto. Maneno yake hayakusikilizwa. Kwa ghadhabu yao, askari hawa wakatupa mienge ya moto ndani ya vyumba vilivyokuwa vimeunganishwa na hekalu lile, na kisha kwa panga zao wakawaua watu wengi waliokuwa wamejificha humo. Damu zilitiririka kwenye ngazi za hekalu kama maji. Maelfu kwa maelfu ya Wayahudi waliangamia. Mbali na sauti zile za mapigano, sauti zingine zilisikika zikipiga kelele: “Ikabodi!” –utukufu umeondoka. [GC 33.1; PK Aya ya 40]

**Tamasha La Kuogofya**

"Tito aligundua kwamba ilikuwa haiwezekani kwake kutuliza ghadhabu za wanajeshi; basi akaingia na maafisa wake ndani, ili kuchunguza mambo yahusuyo jengo lile 'takatifu' kwa ndani. Utukufu na fahari yake iliwajaza mshangao; na kwa kuwa moto ulikuwa bado haujaingia mahali pale Patakatifu, yeye akafanya juhudi za mwisho ili kuliokoa, naye akaruka kwenda mbele tena ili kuwasihi askari waendelee kuuzima moto. Akida aliyeitwa Liberalis alijitahidi kulazimisha utii kwa maofisa wake wanaomsaidia kazi; lakini hata ile heshima kwa mfalme wao hawakuweza kuitoa kwasababu ya uhasama mkali dhidi ya Wayahudi, na hicho kikawa kichocheo kikali cha vita, na tamaa ya kutotosheka na nyara. Askari waliona kila kitu karibu nao kikiwa kinang'aa kwa dhahabu ambayo iliangaza kwa mng'ao kwenye macho yao ikiwa ndani ya moto; waliona kwamba hazina zisizohesabika kwa thamani zilikuwa zimewekwa katika Patakatifu pale. Askari asiyefahamika, akarusha mwenge wake wa moto kati ya bawaba za mlango: kwa ghafla, jengo lote likawaka moto papo hapo. Moshi ukapofusha macho watu wasione vizuri, na moto ukawalazimisha wale maafisa kurudi nyuma, na jengo hilo zuri lililowaletea utukufu likaachwa katika hatima yake kuteketea. [GC 33.2; PK Aya ya 41]

"Lilikuwa tukio la kutisha kwa Mrumi – Je, kwa Myahudi je, ilikuwaje? Kilele chote kile cha kilima ambacho kilichokuwa kinaamrisha jiji lile (utawala), kiliwaka kama volkano. Majengo yaliangauka moja baada ya jingine, kwa kishindo kikubwa, na yakamezwa katika shimo lile la moto. Mapaa ya mwerezi yaliwaka kama karatasi za miali ya moto; minara ile mirefu iliyopakwa dhahabu ikangaa kama taa ya misumari miekundu; minara ya malango ilirusha juu mihimili mirefu ya moto na moshi. Milima ya jirani ilimulikwa kwa mwanga; na vikundi vyeusi vya watu vilionekana kwenye giza vikitazama kwa wasiwasi na kutishika na uharibifu huu uliokuwa unaendelea: kuta na nguzo za mji ulio mkuu zilijawa na nyuso nyingi za watu, zingine zikiwa zimegeuka rangi kwa uchungu na kukata tamaa, wengine wakawa wanasonya kwa hasira kwa kushindwa kulipiza kisasi. Kelele za majeshi ya Warumi walipokuwa wakikimbia kwenda huko na huko, na mayowe ya askari waasi (wayahudi) ambao walikuwa wakiangamia kwa moto, vikachanganyikana na ngurumo za moto na sauti ya mshindo kama wa radi kwa ajili ya mbao refu zilizokuwa zinadondoka. Mwangwi wa milima ile kutoka kwenye vilele vyake ulirudisha vilio vya uchungu mkali wa wale watu walioko juu ya mnara; kelele za mayowe na maombolezo zilisikika kila mahali kando ya kuta; watu ambao waliokuwa dhaifu na wakielekea kifoni kwa ajili ya njaa walikamua nguvu zao zilizobaki, walipokuwa wakitoa kilio cha uchungu, upweke na shida. [GC 34.1; PK Aya ya 42]

"Mauaji ya ndani yalikuwa ya kutisha zaidi kuliko wale waliokufa kwa tukio lile la nje. Wanaume kwa wanawake, wazee na vijana, askari waasi na

makuhani, wale waliopigana na wale walioomba rehema, walikatwa-katwa katika mauaji yasiyobagua. Idadi ya wale waliochinjwa ilizidi ile ya waliochinja. Wanajeshi wa Kirumi walilazimika kupenya juu ya yale marundo ya wafu ili kuendelea na kazi yao ya kuangamiza."- Milman, The History of the Jews, kitabu cha 16. [GC 35.1; PK Aya ya 43]

Punde baada ya uharibifu wa hekalu lile, mji wote ukaangukia mikononi mwa Warumi. Viongozi wa Kiyahudi wakatelekeza ngome/minara yao imara isiyoweza kuingiliwa kirahisi, na Tito akawakuta wameachwa ukiwa. Naye akawatazama kwa mshangao, na akatangaza kwamba ni Mungu Ndiye ambaye amewatia wayahudi mikononi mwake; kwani hakuna zana au injini zozote, hata zile zenye nguvu, ambazo zingeweza kupenya zile ngome na kushinda mapambano haya makali. Majengo ya jiji na hekalu vilibomolewa kutoka kwenye misingi yao, na ardhi ambayo juu yake nyumba takatifu ilikuwa imesimama "ikalimwa kama shamba lilimwavyo." Yeremia 26:18. Katika kuvamiwa kwa kuzingirwa na mauaji yaliyofuata, zaidi ya watu milioni moja waliangamia; walionusurika walichukuliwa mateka, wengine wakauzwa kama watumwa, wakaburutwa kwenda Rumi kwa maadhimisho na maonyesho yenye shangwe kwa mshindi aliyewateka, wengine walitupwa kwa wanyama-mwitu katika viwanja vya michezo ya maonyesho ya hadhara (colosseum), au walitawanyika kama wazururaji wasio na makazi kote kote ulimwenguni. [GC 35.2; PK Aya ya 44]

**Tunawiwa Kiasi Gani Na Kristo**

Wayahudi walikuwa wamejitengenezea pingu zao wenyewe; walikuwa wamejijazia kikombe chao cha kisasi. Katika uharibifu kamili uliowapata kama taifa, na katika majanga yaliyowafuata katika kutawanyika kwao, walikuwa wakivuna tu mazao ambayo waliyapanda kwa mikono yao wenyewe. Nabii anasema: "Ee Israeli, umejiangamiza mwenyewe;" "Kwa maana umeanguka kwa uovu wako." Hosea 13: 9; 14:1. Mateso yao mara nyingi huwakilishwa kama adhabu iliyowasibu kama maagizo ya moja kwa moja toka kwa Mungu (kupatilizwa). Hivyo ndivyo mdanganyifu yule mkubwa anavyotafuta kuficha kazi yake mwenyewe. Kwa kule kukataa kwao kwa ukaidi upendo na huruma za Mungu, Wayahudi walikuwa wamesababisha ulinzi wa Mungu kuondolewa kutoka kwao, na Shetani alikuwa ameruhusiwa kuwatawala jinsi apendavyo mwenyewe. Ukatili wa kutisha uliotekelezwa katika uharibifu wa Yerusalemu ni dhihirisho lenye nguvu la hasira ya kisasi aliyo nayo Shetani juu ya wale wanaojisalimisha kuutii utawala wake wa mabavu. [GC 35.3; PK Aya ya 45]

Sisi hatuwezi kujua ni kwa kiasi gani tunawiwa na Kristo kwa amani na ulinzi Wake ambao tunaufurahia leo. Ni nguvu ya Mungu iokoayo, ndio ambayo inawazuia wanadamu wasiende upande wa Shetani kudhibitiwa kikamilifu na utawala wake. Wale wasio watiifu na wale wasio na shukrani, wana sababu

kubwa ya kushukuru rehema ya Mungu na ustahimilivu Wake katika kudhibiti nguvu ya ukatili mbaya wa yule mwovu. Lakini wakati wanadamu wanapovuka mipaka ya uvumilivu wa Mungu, basi kinga hiyo huondolewa (Roho Mtakatifu). Mungu hasimami mbele ya mwenye dhambi (mwasi) kama mtekelezaji wa hukumu dhidi ya makosa; lakini huwaruhusu wale wakataao rehema Zake kufanya watakavyo, ili wajipatie mavuno ya kile walichokipanda. Kila mwale wa nuru uliokataliwa, kila onyo linalodharauliwa au lisilotiliwa maanani, kila tamaa mbaya iliyoendekezwa, kila uvunjaji wa sheria ya Mungu, ni mbegu iliyopandwa ambayo hakika itatoa mavuno yake. Roho wa Mungu, anayepingwa mara kwa mara, mwishowe huondolewa kutoka kwa mwenye dhambi, halafu hakuna nguvu ya kudhibiti tamaa mbaya zilizo moyoni mwake, na kisha hakuna kinga dhidi ya uovu na uadui wa Shetani. Uharibifu wa Yerusalemu ni onyo la kutisha na lenye uzito kwa wale wote wanaocheza-cheza na utolewaji wa neema ya Mungu na kupinga maombi Yake yanayosihi kwa huruma/rehema. Kamwe hakujapata kutolewa ushuhuda uliothibitika zaidi ya huo wa jinsi Mungu anavyoichukia dhambi na kuhusu adhabu yenye uhakika ambayo itawaangukia wale wenye hatia (waovu). [GC 36.1; PK Aya ya 46]

Unabii wa Mwokozi kuhusu Yerusalemu kujiliwa na hukumu, utakuwa na utimilifu mwingine tena, ambapo uharibifu ule wa kutisha utakuwa ni hafifu tu ya huu wa Yerusalemu, kwani utakuwa kama kivuli tu. Katika hatima ya mji ule mteule tunaweza kuona maangamizi ya ulimwengu ambao umekataa rehema ya Mungu na kuikanyaga kwa miguu yake Sheria Yake. Ni za giza jinsi gani, kumbukumbu zile za taabu za binadamu ambazo dunia hii imewahi kuzishuhudia wakati wa karne nyingi za uhalifu. Moyo huugua, na ubongo unadhoofika katika kutafakari haya. Matokeo ya kukataa mamlaka ya Mbingu yamekuwa ya kutisha. Lakini tukio lenye giza zaidi limewasilishwa katika ufunuo wa siku zijazo. Kumbukumbu za zamani---milolongo mirefu yenye kelele zenye machafuko, vita, na mapinduzi, “Maana silaha zote za mtu mwenye silaha... na mavazi yaliyovingirishwa katika damu.” Isaya 9: 5, --haya ni kitu gani ukilinganisha? Kwa kweli ni madogo sana ukilinganisha na vitisho vya siku ile wakati Roho wa Mungu anayezuia na kudhibiti ugaidi na uovu wa kuogofya atakapoondolewa kabisa kutoka kwa waovu, kutakuwa hakuna tena kizuizi cha dhoruba ya hasira ya mwanadamu itakapolipuka na jazba na ghadhabu ya kishetani! Hapo ndipo ulimwengu utaona, kuliko usivyopata kuona kamwe katika siku za nyuma, matokeo ya utawala wa Shetani. [GC 36.2; PK Aya ya 47]

Lakini katika siku hiyo, kama ilivyokuwa wakati wa uharibifu ule wa Yerusalemu, watu wa Mungu wataokolewa, kila mtu atakayeonekana ameandikwa miongoni mwa hao walio hai katika kitabu cha uzima. Isaya 4:3. Kristo ametangaza kwamba atakuja mara ya pili kuwakusanya waaminifu Wake Kwake: “ndipo mataifa yote ya ulimwengu watakapoomboleza, nao watamwona

Mwana wa Adamu akija juu ya mawingu ya mbinguni pamoja na nguvu na utukufu mwingi. Naye atawatuma malaika Zake pamoja na sauti kuu ya parapanda, nao watawakusanya wateule Wake toka pepo nne, toka mwisho huu wa mbingu mpaka mwisho huu. Mathayo 24:30, 31. Ndipo wale wasioitii injili watateketezwa kwa pumzi ya kinywa Chake, na kuangamizwa kwa ufunuo wa kuwapo Kwake; 2Wathesalonike 2:8. Kama ilivyokuwa ile Israeli ya zamani, waovu wanajiangamiza wenyewe; wanaanguka kwa uovu wao. Kwa maisha yao yale ya dhambi, wamejiweka wenyewe katika hali ya kutopatana na Mungu, tabia/asili yao imeharibiwa sana na uovu/ufisadi, kiasi kwamba kudhihirishwa kwa utukufu Wake kwao hao utakuwa moto ulao (unaoteketeza). [GC 37.1; PK Aya ya 48]

Hebu watu na wajihadhari wasije wakapuuzia somo hili walilopewa kwenye Maneno ya Kristo. Kama vile alivyowaonya wanafunzi Wake juu ya uharibifu wa Yerusalemu, akiwapa ishara ya uharibifu unaokaribia ili kwamba waweze kuponyoka au kutoroka; ndivyo hivyo ameuonya ulimwengu leo, juu ya siku ile ya uharibifu wa mwisho na amewapa vidokezo vya wakati huo unapokaribia, ili wote wenye nia, kwa kadri iwezekanavyo, waweze kukimbia ghadhabu inayokuja. Yesu anatangaza: "Tena, kutakuwa na ishara katika jua, na mwezi, na nyota; na katika nchi dhiki ya mataifa." Luka 21:25; Mathayo 24:29; Alama 13: 24-26; Ufunuo 6: 12-17. Wale wanaoziona dalili hizi za Mathayo 24:33. "Kesheni basi," ndiyo Maneno ya mawaidha na maonyo kwetu. Marko 13:35. Wale wanaotii onyo hili hawataachwa gizani, kiasi kwamba siku hiyo iwapate bila maandalizi. Lakini kwa wale ambao hawatakesha, "Yakini ya kuwa siku ya Bwana yaja kama vile mwivi ajavyo usiku." 1 Wathesalonike 5: 2-5. [GC 37.2; PK Aya ya 39]

Ulimwengu hauko tayari zaidi kupokea ujumbe wa wakati huu kuliko wayahudi walivyokuwa hawako tayari kupokea onyo la Mwokozi kuhusu Yerusalemu. Haijalishi itakavyokuja, ile Siku ya Mungu/Bwana kwa wale wasiomcha Yeye, itakuja kwa kushtukiza. Wakati maisha yanaendelea kama kawaida katika mzunguko (duru) wake usiobadilika na wa kila siku; wakati wanadamu wakiwa wametota au kubweteka katika anasa, katika biashara, katika kusafiri au mawasiliano, katika utengenezaji wa pesa; wakati viongozi wa dini wanapotukuza maendeleo ya kidunia, na kuangaziwa kielimu (teknolojia, sanaa, sayansi) na watu wakiwa wamelala kwa kupumbaa na usalama wa uongo—ndipo kama ilivyo kwa mwizi aibavyo usiku wa manane ndani ya yale makao yasiyo na mlinzi, ndivyo uharibifu wa ghafla utakavyowajia wale wasiojali na kumcha Mungu, "nao hawatakimbia." Mstari wa 3. [GC 38.1; PK Aya ya 50]

# SURA YA 2

# MATESO KATIKA KARNE ILE YA KWANZA

**(Wakristo Wa Kwanza Waaminifu Waliooshwa Na Kuwa Weupe Kama Theluji)**

Ufupisho: Matukio ya sura hii yalianza mnano 64 BK chini ya mfalme Nero wa himaya ya Rumi aliyeanza kuwatesa Wakristo na kuendelea baadaye hapa na pale mpaka karne ya saba, ila matukio ya mateso makubwa zaidi yalifanyika katika miaka ya 311-337.Tertulian mwanasheria (197-227) akimwandikia mfalme wa dola ya Rumi alisema 'Septimius Severus' -Akimaanisha Damu ya Wakristo ndiyo mbegu ya kueneza injili.Ghafla mnamo mwaka 311 mateso yalikoma chini ya Kaisari Constatino I. na Ukristo ukawa mashuhuri, makosa toka kwenye upagani wa Rumi yakaingia, Ukristo ukawa dini rasmi ya Himaya ya Rumi ila Maandiko yalipotoshwa. Utesaji wa huzuni wa wale wapagani walioongoka nusu nusu ukaanza na kuendelea kwa karne nyingi.

Wakati Yesu anawafunulia wanafunzi Wake hatima ya Yerusalemu na matukio ya ujio Wake wa mara ya pili, aliwaelezea pia uzoefu ambao watu Wake wangeupitia kuanzia kipindi atakapochukuliwa kutoka kwao hadi wakati wa kurudi Kwake katika nguvu na utukufu kwa ajili ya ukombozi. Kutoka kwenye mlima wa Mizeituni Mkombozi aliona dhoruba zilizokuwa karibu kulipiga lile kanisa la mitume; na akazama kwa kina juu ya utabiri wa wakati ujao, jicho Lake lilipenya kwenye tufani kali za majaribu ambazo zilikuwa zinaenda kuwapiga wafuasi Wake katika zama zijazo za giza na mateso. Kwa Maneno machache muhimu, na yenye kusikitisha, Alitabiri fungu ambalo watawala wa ulimwengu huu wangechangia kutenda kwa kanisa la Mungu. Mathayo 24:9, 21, 22. Iliwabidi wafuasi wa Kristo kupitia njia ile ile ya kudhalilishwa, kusumbuliwa, kushutumiwa, unyenyekevu na mateso ambayo Bwana wao aliyapitia. Uadui uliolipuka dhidi ya Mkombozi wa ulimwengu huu, ungedhihirishwa tena dhidi ya wote watakaoliamini Jina Lake. [GC 39.1; PK Aya ya 1]

Historia ya kanisa la awali ilishuhudia kutimizwa kwa Maneno ya Mkombozi. Nguvu za dunia na kuzimu zilijikusanya na kujipanga pamoja dhidi ya Kristo aliyewakilishwa kupitia wafuasi Wake. Upagani uliona kuwa ikiwa injili itashinda, mahekalu na madhabahu yake yangefagiliwa mbali; hivyo ukayaagiza majeshi yake kuja kwa mkutano wa dharura ili kupanga mipango ya kuuharibu Ukristo. Mioto ya mateso ikawashwa. Wakristo wakanyang'anywa mali zao walizomiliki na kufukuzwa kutoka katika makazi yao." Walistahimili vita na magomvi makubwa yenye maumivu." Wabrania 10:32. "Wengine walijaribiwa kwa dhihaka na mapigo naam, kwa vifungo, na kwa kutiwa gerezani." Waebrania 11:36. Idadi kubwa sana ikautia muhuri ushuhuda wao kwa damu zao. Mabwana na watumwa, tajiri na masikini, wasomi na wasiosoma, wakauawa bila huruma. [GC 39.2; PK Aya ya 2]

Mateso haya yaliyoanza chini ya utawala wa Nero wakati wa kuuawa kwa Paulo, yaliendelea kwa ghadhabu kubwa kwa karne nyingi ama kwa udogo au kwa ukubwa. Wakristo walituhumiwa kwa shutuma za uongo, kwa uhalifu wa kutisha sana na kutangazwa kuwa wao ndio wasababishaji wa majanga makubwa –yaani, ya njaa kali, magonjwa ya milipuko, pamoja na matetemeko ya ardhi. Kadiri walivyoonekana kuwa walengwa maarufu wa vielelezo vya chuki na kushukiwa, ndivyo jinsi watoa habari walivyojiweka tayari ili kupata manufaa kwa kuwasaliti watu hawa wasio na hatia. Walishitakiwa kama waasi dhidi ya himaya, kama maadui wa dini na watu waletao usumbufu na kero kwa jamii. Wengi sana walitupwa kwenye wanyama pori wakali au kuchomwa moto wakiwa hai kwenye viwanja vya maonyesho (kwenye halaiki za watu kwenye stadium zilizoitwa colosseum google historia). Baadhi yao walisulubiwa, wengine walifunikwa kwa ngozi za wanyama pori na kutupwa katika eneo la viwanja vyao vya michezo ili wararuliwe na mbwa wakali (arena). Adhabu yao mara nyingi ilifanywa kuwa burudani kuu kwenye sherehe za umma. Umati mkubwa wa watu ulikusanyika kufurahisha macho, kwa kufurahia maumivu yao kwa vicheko, shangwe na kupiga makofi. [GC 40.1; PK Aya ya 3]

Popote walipopata makimbilio yao, Wafuasi hawa wa Kristo walisakwa kama wanyama wawindwao. Walilazimika kutafuta maficho katika maeneo ya ukiwa, faragha na upweke. "Maskini hawa na wahitaji, waliosumbuliwa na kuteswa: (watu ambao ulimwengu haukustahili kuwa nao) walikuwa wakizunguka-zunguka nyikani na katika milima, mapango na katika mashimo ya nchi Mstari wa 37, 38. Mahandaki yaliyochongwa chini kuzikia watu yalikuwa ndiyo makazi kwa maelfu ya watu hawa. Chini ya milima iliyoko nje ya jiji la Roma, njia ndefu za chini kwa chini ardhini na kwenye miamba zilitengenezwa; njia zenye giza na mfumo wa kutatanisha zilisambaa kwa maili nyingi ng'ambo ya pili ya kuta za mji ule. Katika makimbilio na maficho haya ya chini ya ardhi, wafuasi wa Kristo waliwazika wafu wao; na humo pia, waliposhukiwa na kupigwa marufuku

walipata hifadhi ya makao hapa. Wakati Yule Mtoaji wa uzima atakapowaamsha wale waliopigana vita vile vizuri, wengi waliouwa kwa ajili ya Kristo watafufuliwa kutoka katika mashimo na mapango hayo ya giza. [GC 40.2; PK Aya ya 4]

**Imani Na Mashahidi Wa Mungu**

Chini ya yale mateso makali kupindukia, mashahidi hawa wa Yesu waliitunza imani yao safi ili isitiwe na mawaa. Ingawa walinyimwa kila aina ya faraja, na utulivu, wakifungiwa mbali na mwanga wa jua kwenye kiini cha ardhi, na hivyo kufanya kao lao ardhini kwenye giza, wala hawakutamka neno lolote la kulaumu. Kwa maneno yenye Imani, ustahimilivu na matumaini walitiana moyo wao kwa wao kuvumilia ufukara, mateso na fadhaa. Kupoteza kila mema au mbaraka wa kidunia hakukuwafanya kuikana imani yao kwa Kristo. Majaribu na mateso (maonjo) waliyoyapitia yalikuwa kwao kama hatua tu ya kuwaleta karibu na pumziko na thawabu yao. [GC 41.1; PK Aya ya 5]

Kama ilivyokuwa kwa watumishi wa Mungu wa zamani, wengi "waliteswa wasikubali ukombozi ili wapate ufufuo ulio bora." Mstari wa 35. Hili liliwakumbusha Maneno ya Bwana wao akilini mwao, kwamba watakapoteswa kwa ajili ya Kristo, wanapaswa kuwa na furaha inayozidi kipimo, kwani thawabu yao itakuwa kubwa kule mbinguni; na hivyo ndivyo manabii walivyoteswa mbele zao. Walifurahi kwa kuhesabiwa kuwa wanastahili kuteseka kwa ajili ya ile Kweli, na nyimbo za ushindi zilipanda juu kutoka katikati ya ile miale ya moto iliyokuwa inatoa sauti wakati nyama zilikuwa zinaungua. Wakitazama juu mbinguni kwa Imani, walimuona Kristo na malaika wakiwa wamesimama katika kuta za mbinguni wakiwatazama chini kwa shauku yenye kina na kuafikiana na msimamo wao kwa kupendezwa. Sauti ikaja kwao kutoka katika kile kiti cha enzi cha Mungu ikisema kwao: "Uwe mwaminifu hata kufa, Nami nitakupa taji ya uzima" Ufunuo 2:10 [GC 41.2; PK Aya ya 6]

Juhudi za Shetani kuliharibu kanisa la Kristo kwa ukatili na mabavu zilikuwa kazi bure. Pambano kuu ambalo kwalo wanafunzi wa Yesu waliyatoa maisha yao halikukoma wakati ambapo wabeba viwango hawa waliobeba bendera Yake kwa uaminifu walilala usingizi wa mauti katika nafasi zao za ulinzi. Kwa 'kushindwa' kwao walikuwa wameshinda. Watendakazi wa Mungu waliuawa kikatili lakini kazi Yake ilisonga mbele daima kwa uthabiti. Injili ikaendelea kuenea na idadi kubwa ya wafuasi walioyakumbatia mafundisho yake kwa nguvu ikazidi kuongezeka. Ilipenya katika maeneo yale ambayo haikuwa rahisi kufikiwa hata na wale tai wa Kirumi (askari). Alisema hivi Mkristo mmoja aliyekuwa akiwaeleza watawala wale wa kipagani waliokuwa wakitekeleza yale mateso, mnaweza: "kutuua sisi, kututesa na pia kutuhukumu... Udhalimu wenu ni uthibitisho fika kwamba sisi hatuna hatia....wala ukatili wenu.... hautawasaidia kitu" Ulikuwa ni mwaliko

imara wa kuwaleta wengine katika ushawishi wao "Kadiri mnavyotufyeka ndivyo ambavyo idadi yetu inavyozidi kuongezeka, damu ya Wakristo ni mbegu." -- Tertullian Apology,aya ya 50. [GC 41.3; PK Aya ya 7]

Maelfu walifungwa gerezani na wengine wakauawa, lakini wengine waliibuka ghafla kuja kujaza nafasi zao. Na wale waliokufa kishujaa kwa ajili ya Imani yao katika Kristo, wakahesabiwa pamoja Naye kuwa washindi. Walikuwa wamevipiga vita vile vizuri vya imani, nao wamestahili kuvaa taji ya utukufu wakati ule Kristo atakaporejea. Mateso yale waliyoyavumilia yaliwaunganisha kwa karibu wale Wakristo wao kwa wao, pamoja na Mkombozi wao. Vielelezo vyao hai, yaani maisha waliyoishi na ushuhuda wa kifo chao vilikuwa ushuhuda tosha na wa kudumu kwa ajili ya Ukweli; na mahali ambapo haikutarajiwa kabisa, watenda kazi wale wa Shetani waliacha huduma yao kwake na kujiandikisha kutumika chini ya bendera ya Kristo. [GC 42.1; PK Aya ya 8]

Kwa hivyo Shetani aliiweka mipango yake ya kupigana vita dhidi ya Mungu iwe na ufanisi zaidi kwa kupandikiza bendera yake katika kanisa la Kikristo. Endapo wafuasi wa Kristo wangeweza kundanganywa na hivyo kupelekea kumchukiza Mungu, basi nguvu, ujasiri na uimara wao ungeshindwa, nao kwa urahisi wangalianguka na kuwa mawindo rahisi ya adui. [GC 42.2; PK Aya ya 9]

Mpinzani huyu mkuu kwa sasa anajitahidi kwa hila kupata kile alichoshindwa kukipata kwa nguvu. Mateso yale yakakoma na badala yake kumekuwa na ulaghai wa hatari wa mafanikio ya muda (vivutio vya ustawi) na kupenda heshima ya dunia. Waabudu sanamu hawa wakashawishiwa waipokee sehemu tu ya Imani ya Kikristo, na huku wakivikataa vipengele vingine muhimu vya ile Kweli (mafundisho ya Biblia). Walikiri kumpokea Yesu Kristo kama Mwana wa Mungu na kuamini kifo Chake na ufufuo Wake, lakini hawakuguswa na usadikisho wa dhambi zao na wala hawakuona haja yoyote ya kutubu au kuwa na badiliko lolote katika mioyo yao. Pakafanyika makubaliano kwa baadhi ya vipengele kwa wale waabudu sanamu na kisha wakapendekeza kuwa Wakristo pia ni sharti wafanye maridhiano ya kupunguza mafundisho yao fulani, ili kwamba wote wapate kuungana pamoja katika jukwaa la kumwamini Kristo (Imani ya Yesu). [GC 42.3; PK Aya ya 10]

Sasa kanisa likawa katika hatari kubwa ya kutisha. Magereza, maumivu, mateso, moto na panga vilikuwa ni mibaraka ukilinganisha na njia waliyokuwa wanaelekea. Baadhi ya Wakristo waliendelea kusimama imara, na kutangaza kuwa wasingeweza kushusha viwango kwa maridhiano (au kulegeza masharti kwa kuchuja imani). Wengine walipendelea kuacha au kurekebisha kidogo baadhi ya vipengele vya imani zao (kutokana na msemo wao, kuviboresha kidogo ili visionekane kupitiliza-(modify) na kuungana na wale waliokubali sehemu tu ya Ukristo, wakidai kwamba hii ingekuwa njia yao ya kuwaelekeza kwenye wongofu

kamili. Hiki kilikuwa kipindi cha uchungu na maombolezo makali kwa wafuasi waaminifu wa Kristo. Chini ya vazi la Ukristo bandia Shetani alikuwa amejipenyeza mwenyewe na kuingia ndani ya kanisa ili kuchafua imani yao na kugeuza mawazo yao kutoka kwenye lile Neno la Ukweli. [GC 42.4; PK Aya ya 11]

Hatimaye Wakristo wengi walikubali kushusha chini viwango vyao vya imani na muunganiko ukatengenezwa na kuhitimishwa kati ya Ukristo na Upagani. Ijapokuwa waabudu sanamu walikiri wameongoka na kuungana na kanisa, bado walikuwa wanaendelea kung'ang'ania ibada ya miungu yao, walibadilisha tu vitu vya kuabudu, yaani picha au sanamu za kuabudu badala yake zikawa na taswira ya Yesu, na hata ya Mariamu na watakatifu. Uchafu wa chachu ile mbaya ya ibada ya sanamu ukaletwa kanisani na kuendeleza kazi yake ya uovu au isiyo na urafiki na Neno la Mungu. Mafundisho yasiyo sahihi, desturi na mila za ibada zenye ushirikina, sherehe na maadhimisho ya sikukuu za ibada ya sanamu yakaingizwa katika imani na ibada ya kanisa hili. Kadiri wafuasi wa Kristo walivyoungana na waabuduo sanamu, ndivyo jinsi dini ya Kikristo ilivyozidi kupotoka, na kanisa lilipoteza usafi na nguvu zake. Hata hivyo kulikuwa na wengine ambao hawakupotoshwa na udanganyifu na kuchanganyikiwa huku, hawa bado walidumisha uaminifu wao kwa Mwanzilishi wa ile Kweli na kumwabudu Mungu peke Yake (Mungu Pekee, Ndiye Asili ya Ukweli). [GC 43.1; PK Aya ya 12]

**Makundi Mawili Ndani Ya Kanisa**

Daima kumekuwa na matabaka mawili miongoni mwa watu wanaodai kuwa wafuasi wa Kristo. Wakati tabaka moja linajifunza maisha ya Mkombozi na kutafuta kwa dhati na bidii kurekebisha makosa yao ili kufanana na Kielelezo na Mfano wao (Kristo), kundi jingine lilikuwa linajitahidi kuzikwepa zile Kweli za wazi, zinazohushu maisha ya kivitendo ya kila siku, na ambazo zinafichua makosa yao. Hata katika kipindi chake cha ubora wa juu kabisa, sio watu wote waliokuwa safi, dhati, na wanyofu kwa ile Kweli. Mwokozi wetu alifundisha kuwa wale ambao kwa hiari yao wenyewe wanafanya kwa kusudi kuiendekeza na kuifurahia dhambi kwa makusudi, hawapaswi kupokelewa kanisani; ila Yeye alijiunganisha na watu wenye tabia mbaya na mapungufu, yaani dhambi na hivyo akawanufaisha kupitia mafundisho Yake na mifano, ili wapate fursa ya kuona makosa yao na kuyasahihisha. Miongoni mwa wale mitume kumi na wawili, mmoja wao alikuwa msaliti. Yuda alikubaliwa sio kwa sababu ya kasoro zake za tabia bali licha ya kasoro zile alizokuwa nazo. Alikuwa ameunganishwa na wanafunzi Wake, ili kwamba kupitia Mafundisho na Kielelezo Chake Kristo, basi na aweze kujifunza kile ambacho kinatengeneza tabia ya Kikristo, na hivyo kuongozwa kuziona dosari zake na kutubu na kisha kwa msaada wa neema ya Mungu kuitakasa nafsi yake "kwa kutii ile Kweli." Lakini Yuda hakutembea katika

nuru ambayo kwa neema iliruhusiwa kumulika mbele yake. Kwa kuendekeza kujifurahisha na dhambi alikaribisha majaribu ya Shetani. Mazoea maovu yakaendelea kushamiri na kutawala maisha yake. Aliusalimisha moyo na akili zake kulemewa na nguvu za giza, aliudhika wakati makosa yake yalipokemewa, na hivyo kupelekea kutenda uhalifu wa kutisha wa kumsaliti Bwana wake. Kadhalika, wale wote wanaofuga maovu mioyoni mwao, huku wakidai na kukiri kwamba huo ndio utauwa, na huku wanawachukia wale wote wanaowasumbua amani yao kwa kukemea mwenendo wao wa dhambi. Watakapopata fursa nzuri kama ilivyokuwa kwa Yuda, watawasaliti wale ambao waliwaonya ili wajirekebishe kwa ajili ya mwisho wao mwema (faida yao wenyewe). [GC 43.2; PK Aya ya 13]

Mitume walikumbana na wale ambao ndani ya kanisa walidai kuukiri utauwa na huku kwa kisirisiri walikuwa wameuthamini uovu mioyoni mwao. Anania na Saphira walikuwa sehemu ya utendaji au uigizaji (drama) huo wa udanganyifu kwa kujifanya kuwa wametoa dhabihu yote kwa Mungu, wakati kwa tamaa walikuwa wamezuia sehemu ya sadaka kwa ajili yao wenyewe. Roho Yule wa Kweli aliwafunulia mitume tabia halisi iliyofichwa na waigizaji hawa, na hukumu ya Mungu ikashughulika kulisafisha na kuliondoa doa hilo chafu lenye harufu mbaya kutoka kwenye kanisa Lake lililokuwa safi. Ushuhuda huu wa Roho wa Kristo anayeona na kufahamu mambo yote katika Kanisa ukawa tishio linaloleta kiwewe kwa wanafiki (watu feki kwa lugha ya leo) na watenda maovu. Wasingeweza kudumu kwa muda mrefu kuendelea kuwa na mahusiano na wale ambao kwa tabia na msimamo walikuwa wawakilishi wa kudumu wa Kristo; na majaribu na mateso yalivyokuja kwa wafuasi Wake, ni wale tu waliokuwa tayari kuacha yote kwa sababu ya Ukweli peke yake, ndio waliokuwa na matamanio kuwa wanafunzi Wake. Kwa hivyo kwa kadiri mateso yalivyoendelea, ndivyo jinsi kanisa lilivyokuwa linakaribia kufikia ule usafi kwa ukamilifu (moyo na mafundisho vilipelekana). Lakini mateso yalipokoma waongofu wasiojitoa wakfu kikamilifu au kuwa wanyofu waliendelea kuongezeka na njia ikafunguliwa kwa uwazi kwa ajili ya Shetani kupata pahali pa kukanyagia. [GC 44.1; PK Aya ya 14]

Lakini hakuna uhusiano kati ya Mfalme wa nuru na mfalme wa giza na vivyo hivyo hapawezi kuwepo na muungano kati ya wafuasi wao. Wakati Wakristo walipokubali kuungana na wale walioongoka nusu-nusu kutoka katika upagani (uvuguvugu), waliingia katika njia ambayo iliwapeleka mbali zaidi na Ukweli. Shetani alishangilia kwamba amefanikiwa kudanganya idadi kubwa ya wafuasi wa Kristo. Ndipo akashinikiza nguvu zake kuwa thabiti katika kuwatumia hawa 'waangofu wa nusu-nusu' na kuwachochea ili wawatese wale walioendelea kuwa waaminifu kwa Mungu. Hakuna watu waliobobea vyema katika kupinga Imani ya Kweli ya Kikristo kama wale waliowahi kuwa watetezi wa Kristo hapo awali; na Wakristo hawa walioasi wakiwa wameungana na wenzao waliokuwa nusu wapagani walielekeza upinzani wao dhidi ya viini muhimu zaidi vya mafundisho

muhimu ya Ukristo, yaani mafundisho ya Kristo. (Upagani ni kuwa na miungu mingi, na kwa kawaida inahusisha dini ya umizimu-spiritualism, au kuzungumza na watu waliokufa kwa njia za giza) [GC 45.1; PK Aya ya 15]

Ilihitaji mapambano yenye juhudi kali kwa wale ambao wangetaka kuwa waaminifu, kusimama imara dhidi ya udanganyifu na uasi uliofichwa katika vazi la kikuhani (makasisi) na kuingizwa ndani ya kanisa. Biblia haikukubalika kama kanuni/kiwango cha imani. Fundisho kuhusu uhuru wa dini liliitwa uzushi au uongo na waanzilishi wake walichukiwa na kupigwa marufuku. [GC 45.2; PK Aya ya 16]

**Umuhimu Wa Kutengana**

Baada ya pambano kali na la muda mrefu, wale waumini wachache waliokuwa waongofu wa kweli, waliamua kuuvunja muungano wa aina yoyote na kanisa lile lililokuwa limeasi ikiwa lingeendelea kukumbatia mafundisho ya uongo (ya mwanadamu) pamoja na ibada ya sanamu. Wakaona kwamba kujitenga nao ni jambo la muhimu na lisilokwepeka, ikiwa wangelitii Neno la Mungu. Hawakudiriki kuyavumilia makosa ya kufisha mioyo yao na kuweka mfano ambao ungehatarisha imani ya watoto wao, na watoto wa watoto wao. Ili kuilinda amani na umoja walikuwa tayari kufanya makubaliano yoyote yale yanayoendana sambamba na uaminifu wao kwa Mungu; lakini waliona ya kwamba, hata ile amani ingekuwa inanunuliwa kwa gharama kubwa sana, endapo wangetoa kafara kanuni za Mungu (Maagizo, Amri, Neno, Shuhuda, Sheria za Mungu). Endapo umoja ule ungeweza kulindwa tu kwa kuridhiana na kushusha viwango vya Ukweli na haki au kulegeza masharti, basi ni bora kuwe na tofauti kati yao au hata vita. [GC 45.3; PK Aya ya 17]

Ingekuwa bora na vyema kwa kanisa na ulimwengu huu, ikiwa kanuni zile ambazo ziliwachochea watu zingewaka moto tena mioyoni mwa watu wanaomkiri Mungu na kujiita wafuasi Wake. Kuna kutokujali kunakotisha juu ya mafundisho ambayo ni nguzo za imani ya Kikristo. Mtazamo huu unazidi kupata mashiko yenye nguvu, kwamba hata hivyo mafundisho hayo siyo ya maana au ya msingi. Anguko hili linaimarisha mikono ya mawakala wa Shetani, kiasi kwamba nadharia za uongo na udanganyifu unaotisha ambazo zilihatarisha maisha ya waaminifu katika zama zilizopita walipokuwa wakizipinga na kuzifichua, hivi sasa zinakubalika kwa upendeleo na maelfu ya wale ambao wanadai kuwa wafuasi wa Kristo. [GC 46.1; PK Aya ya 18]

Hakika Wakristo wa awali walikuwa ni watu wa kipekee sana. Mwenendo wao usio na dosari na Imani yao isiyoyumbayumba vilikuwa ni kemeo la nyakati zote, ambalo lilisumbua amani ya wenye dhambi. Japo walikuwa ni wachache tu kwa idadi yao, watu wasio na utajiri, fursa, vyeo vikubwa au nyadhifa, walikuwa tishio kwa watenda maovu popote pale ambapo tabia na mafundisho yao

yalijulikana. Kwa hivyo walichukiwa na waovu kama vile Habili alivyochukiwa na Kaini ambaye hakumcha Mungu. Ilikuwa ni sababu ile ile ambayo kwayo Kaini alimuua Habili, iliyofanya wale ambao walitaka kutupilia mbali vizuizi vya Roho Mtakatifu wawaue watu wa Mungu. Ilikuwa ni sababu hiyo hiyo iliyowafanya Wayahudi wamkatae na kumsulubisha Mwokozi—kwa sababu usafi na utakatifu wa tabia Yake, ulikuwa ni kemeo la kudumu kwa uchoyo, ubinafsi na ufisadi waliokuwa nao. Tangu siku zile za Kristo mpaka leo, wanafunzi Wake waaminifu wameamsha chuki na upinzani wa wale wanaopenda, na kuzifuata njia zile za dhambi. [GC 46.2; PK Aya ya 19]

Kwa namna gani basi injili inaweza kuitwa kuwa ni ujumbe wa amani? Wakati Isaya alipotabiri kuzaliwa kwa Masihi alimpa jina lijulikanalo kama “Mfalme wa Amani” Wale Malaika, waliwapowatangazia wachungaji kuwa Kristo amezaliwa, waliimba katika eneo la Bethlehemu kwa kusema “Atukuzwe Mungu mbinguni na Duniani iwe amani kwa watu aliowaridhia.” Luka 2:14. Kunaonekana kana kwamba kuna ukinzani kati ya Matamko ya unabii na Maneno haya ya Kristo “msidhani ya kuwa nimekuja kuleta amani duniani; La! Sikuja kuleta amani bali upanga.” Mathayo 10:34. Lakini ujumbe huu ukieleweka vyema, itajulikana kwamba vyote hivi viwili vinapatana kikamilifu. Injili ni ujumbe wa amani. Ukristo ni mfumo ambao mtu anapoukubali na kuutii, utasambaza amani, utulivu, umoja na furaha ulimwenguni kote. Dini Yake Kristo itawaunganisha katika umoja, na undugu wa karibu wale wote wanaoyakubali mafundisho Yake. Ulikuwa ni utume wa Yesu kuja kuwapatanisha wanadamu na Mungu na hivyo kumpatanisha mwanadamu na mwanadamu mwenzake. Lakini sehemu kubwa ya ulimwengu kwa ujumla inamilikiwa na Shetani, mpinzani yule mchungu (mkubwa na mwenye chuki) wa Kristo. Injili huwasilisha kwao kanuni za maisha ambazo zinakinzana na tabia na matamanio yao, na hivyo huamsha upinzani na kuleta uasi. Wanachukia usafi wa maisha ya wale ambao hufunua na kuzihukumu dhambi zao na kisha wanawatesa na kuwaangamiza wale ambao wanahimiza madai yake halali na matakatifu. Ni kwa mtazamo huu--Kwasababu ya Ukweli wake ulioinuliwa, injili huleta chuki kali, vurugu na malumbano— ndiyo maana injili huitwa upanga. [GC 46.3; PK Aya ya 20]

Majaliwa na uongozi Wake Mungu ni siri na fumbo kwetu katika kushugulika na waovu, jambo hili limeleta mashaka na utata kwa wengi walio dhaifu katika Imani. Wengine wako tayari hata kutupilia mbali tumaini lao kwa Mungu kwa sababu eti Yeye anaruhusu watu walio waovu, na wenye maadili ya chini wafanikiwe, ilihali watu wema na safi kabisa wanasumbuka, wanateseka na kuumizwa na utawala wao wa kikatili. Wanauliza, yawezekanaje basi, Yeye ambaye ni Mwenye haki na Mwenye rehema na ambaye uwezo Wake hauna kikomo, avumilie ukatili, dhuluma na uonevu huu ‘kwa watu Wake’? Hili ni swali ambalo sisi hatuna lolote la kufanya. Mungu ametupatia sisi ushahidi wa kutosha juu ya upendo Wake kwetu, na hatuna shaka juu ya fadhila Zake kwetu hata

kama hatuwezi kuelewa namna ya utendaji wa hekima Yake. Mwokozi aliyanena Maneno haya kwa wanafunzi Wake akiyaona mashaka yatakashinikiza roho zao katika siku za majaribu na giza “likumbukeni lile Neno nililowaambia mtumwa si mkubwa kuliko Bwana Wake ikiwa waliniudhi Mimi watawaudhi ninyi.” Yohana 15:20. Yesu alipata mateso kwa ajili yetu kuliko yoyote miongoni mwa wafuasi Wake anavyoweza kuteseka kwa ukatili wa watu waovu. Wale walioitwa kustahimili mateso makali na kuuawa kama wafia dini wanafuata nyayo za Mwana mpendwa wa Mungu. [GC 47.1; PK Aya ya 21]

“Bwana hakawii kuitimiza ahadi Yake 2 Petro 3:9. Yeye hawasahau wala kuwapuuza watoto Wake; Bali anawaruhusu waovu kuzidhihirisha tabia zao halisi, ili kwamba asiwepo yeyote anayetaka kufanya mapenzi Yake ambaye anaweza kudanganywa nao kuhusu walivyo haswa. Kadhalika, wenye haki huwekwa katika tanuru la mateso, ili wao wenyewe waweze kutakaswa; ili mfano wao uweze kuwasadikisha wengine juu ya uhalisi wa Imani yao na ucha Mungu; na pia ili mwenendo wao usiopinda uweze kuwahukumu wasiomcha Mungu na wale wasioamini. [GC 48.1; PK Aya ya 22]

Mungu huwaruhusu waovu kufanikiwa na kudhihirisha uadui wao dhidi Yake, ili watakapokuwa wamejaza kipimo chao cha uovu, wote wapate kuiona haki na rehema Yake na kustahili kwao kuangamizwa kabisa. Siku ile ya kulipiza kisasi inaharakisha, wakati wale wote waliokiuka sheria Yake, na kuwanyanyasa watu Wake watakapokutana na malipo ya stahiki ya matendo yao. Wakati ambapo vitendo vyote vya ukatili au visivyo vya haki kwa waaminifu wa Mungu vitaadhibiwa kana kwamba vilifanywa dhidi Yake Kristo Mwenyewe. [GC 48.2; PK Aya ya 23]

Kuna swali jingine la muhimu ambalo linapaswa kuvuta umakini wa makanisa yetu leo. Mtume Paulo anatangaza “Naam, na wote wapendao kuishi maisha ya utauwa katika Kristo wataudhiwa” 2 Timotheo 3:12. Kwa nini basi mateso yanaonekana kusinzia kwa kiasi kikubwa? (yamepoa). Jibu pekee ni kwamba kanisa limeafikiana na kiwango cha dunia na kwa hivyo, haliamshi upinzani wowote toka kwa adui. Dini iliyopo katika siku zetu leo sio yenye tabia safi na takatifu kama ilivyokuwa ile imani ya Kikristo katika siku za Kristo na mitume Wake. Ni kwa sababu tu ya kuwapo ile roho ya kuafikiana na dhambi, kwa sababu Kweli zile kuu za Neno la Mungu hazithaminiwi, kwa sababu kuna uhai mdogo wa utauwa ndani ya kanisa kiasi kwamba Ukristo unapendwa na kuwa mashuhuri ulimwenguni (mstari wa kutofautisha ni mgumu). Hebu kuwe na uamsho wa imani na nguvu ambazo lile kanisa la awali lilikuwa nazo, na hapo ndipo roho ya mateso itakapoamshwa na kisha ile mioto ya mateso itawashwa tena. [GC 48.3; PK Aya ya 24]

# SURA YA 3

# ZAMA ZA GIZA LA KIROHO

**(Kulikataa Neno la Mungu Na Kwenda Chini)**

Ufupisho: Kwa miaka 300 mateso makali yaliwabamiza Wakristo wa awali, na kisha ulipofika mwaka 311 BK kukawa na amani ghafla, kwa sababu za kisiasa, Kaisari Constatino alitaka kuwa rafiki wa kanisa (306-337), angalia mwaka 321 machi saba, tangazo la Mfalme Constatino na angalia Constatino Edict of Toleration 1211 BK, jambo lililofanya historia kubadilika kabisa, mwafaka/maridhiano ya amani yalifanywa na mateso yakaanza kutoka kwa ndugu waliojifanya kuwa Wakristo au Wakristo feki. Kanisa hilo aliloanza Constatino likawa dini rasmi ya himaya ya Rumi. Hapo ndipo mambo kama vile kuombea wafu, pugatori, Inkwizisheni (inquisition), uuzaji wa misamaha yaani indugensia na mengineyo yaliingizwa na kwa jumla hapa Daniel 7:25 na Ufunuo 13:5-7 ilianza kazi yake, katika ile miaka 1260 ya kutesa watakatifu wa Mungu—538-1798BK. Mwishowe kanisa likachukua hatua za kwenda chini, soma zaidi!

Mtume Paulo, katika barua yake ya pili kwa Wathesalonike, alitabiri uasi mkubwa ambao ungetokana na kuanzishwa kwa mamlaka ya upapa. Alitangaza kwamba siku ya Kristo isingekuja, "usipokuja kwanza ule ukengeufu; akafunuliwa yule mtu wa kuasi, mwana wa uharibifu; yule mpingamizi, ajiinuaye nafsi yake juu ya kila kiitwacho Mungu, akijionyesha nafsi yake kana kwamba yeye ndiye

Mungu.” Na zaidi ya hayo, mtume anawapa tahadhari ndugu zake kwamba “siri ya kuasi tayari inafanya kazi.” 2 Wathesalonike 2:3, 4, 7. Hivyo hata siku hizo za mwanzoni, mtume aliona uovu/makosa yakilinyemelea kanisa taratibu, nayo yangeandaa njia ya kuinuka na kukuza upapa ndani ya kanisa. [GC 49.1; PK Aya ya 1]

Kidogo kidogo, mwanzoni kwa siri na kimya kimya, kisha baadaye kwa uwazi zaidi, ilipoongezeka nguvu na kudhibiti akili za wanadamu, ile “siri ya uasi” ikaendeleza mbele kazi yake ya udanganyifu na makufuru. Taratibu, mapokeo na mila zile zikajikongoja bila kutambulika, lakini, desturi hizo za kipagani zikaingia katika kanisa la Kikristo kwa uhakika. Roho ile ya kuridhiana, au kulegeza maagizo ili kufanana na dunia ilikuwa imezuiliwa kwa muda na mateso makali ambayo kanisa lilistahimili chini ya upagani. Lakini mateso yalipokoma, na Ukristo ukaingia katika nyua na majumba ya kifalme, kanisa likaweka kando imani sahili na nyenyekevu ya Kristo na mitume Wake kwa fahari na kiburi cha mapadri na watawala wa kipagani; na kuweka nadharia na desturi za wanadamu badala ya amri za Mungu. Wongofu wa jina tu wa Constatine (Mtawala au Kaisari wa Himaya ya Rumi), mwanzoni mwa karne ile ya nne, ulisababisha shangwe kubwa; na ulimwengu (wa kipagani) ukiwa umevikwa joho la mfano wa haki ukatembea na kuingia kanisani. Basi kazi ile ya uharibifu/ufisadi ikasonga mbele kwa kasi. Upagani, japokuwa ulionekana kama vile unatokomezwa kabisa, ndio ulioshinda hatimaye. Roho yake ya kipagani ikalitawala kanisa. Mafundisho yake ya dini, maadhimisho, umizimu au ushirikina wake vikajumuishwa na kuingizwa katika imani na ibada na wale waliojidai kujiita wafuasi Wake Kristo. [GC 49.2; PK Aya ya 2]

Mapatano haya kati ya upagani na Ukristo yalileta na kukuza kwa “mtu wa dhambi (mwana wa uasi)” aliyetabiriwa katika unabii kama anayepinga na kujiinua juu ya Mungu. Mfumo huu mkubwa wa dini ya uongo ndio nyenzo yake kuu ya kilele cha uwezo wake Shetani-- ni udhihirisho wa juhudi zake za kujiketisha yeye mwenyewe juu ya kiti cha enzi ili kuitawala dunia hii kama apendavyo yeye mwenyewe. [GC 50.1; PK Aya ya 3]

Kuna siku ambayo Shetani alijaribu kufanya maridhiano na Kristo ili wawe timu moja. Alimwendea Mwana wa Mungu jangwani na kumwonyesha milki zote za ulimwengu na utukufu wake na kujitolea kumpatia vyote hivyo kama tu angekiri ukuu wa mfalme wa giza. Kristo alimkemea mjaribu mwenye kiburi na akamlazimisha aondoke. Lakini sasa Shetani anapata mafanikio makubwa anapoyaleta majaribu yale yale kwa mwanadamu. Ili kujipatia manufaa na heshima za ulimwengu huu, kanisa lile likaongozwa kutafuta upendeleo wa wanadamu na watu mashuhuri wa dunia hii; na kwa njia hiyo hiyo, likiwa limemkana Kristo, likashawishika kujitiisha kwa mwakilishi yule wa shetani---kwa askofu yule wa Rumi. [GC 50.2; PK Aya ya 4]

Moja ya mafundisho makuu ya dini ya Kirumi ni kwamba, papa ndiye kichwa kinachoonekana cha kanisa lote la Kristo ulimwenguni kote na kwamba amepewa mamlaka ya juu kabisa juu ya maaskofu, makasisi na wachungaji katika sehemu zote za dunia hii. Zaidi ya hayo, papa amepewa vyeo vile vya Uungu/Mungu. Ameitwa "Bwana Mungu Papa" (tazama Kiambatisho), na imetangazwa kuwa yeye hawezi kukosea kamwe. Anadai kwamba wanadamu wote wanapaswa kumsujudu yeye. Madai hayo hayo yaliletwa na Shetani katika jangwa la majaribu na ndio bado yanasisitizwa naye kwa kupitia Kanisa katoliki la Rumi na idadi kubwa ya watu iko tayari kumsujudu yeye.[GC 50.3; PK Aya ya 5]

Lakini wale wanaomcha na kumheshimu Mungu wanapambana kwa ujasiri mkuu kama Kristo alivyopambana na majaribu ya yule adui mwerevu: "Msujudie Bwana Mungu wako, na umwabudu Yeye peke Yake tu." Luka 4:8. Mungu hajawahi kutoa dokezo lolote katika Neno Lake kwamba amemteua mwanadamu fulani kuwa kichwa cha kanisa Lake. Fundisho la dini la ukuu wa papa usio na kifani linapingana moja kwa moja na mafundisho ya Maandiko. Papa hawezi kuwa na nguvu juu ya kanisa la Kristo isipokuwa kwa kupora/utapeli. [GC 51.1; PK Aya ya 6]

Dini ya Kirumi imeendelea kuleta lawama ambazo ni uzushi dhidi ya Waprotestanti kwamba wameamua kujitenga kwa makusudi na kanisa la kweli. Wao ndio walioishusha chini bendera ya Kristo na kuiacha "Imani waliyokabidhiwa watakatifu mara moja tu." Yuda 3. [GC 51.2; PK Aya ya 7]

**Hekima Na Uwezo Wa Neno**

Shetani alijua vyema kwamba Maandiko Matakatifu yangewawezesha watu kugundua madanganyo yake na kuupinga uwezo wake. Ilikuwa ni kwa njia ya Neno hilo tu, kwamba hata Mwokozi wa ulimwengu aliweza kuyapinga mashambulizi yake Shetani. Katika kila shambulio, Kristo aliwasilisha mbele ya Shetani ngao ya Ukweli wa milele akisema, "Imeandikwa." Kwa kila shauri lililotolewa na mpinzani, Alipinga kwa kutumia hekima na nguvu ya Neno. Ili Shetani apate kudumisha upotofu wake juu ya wanadamu, ni sharti asimamishe mamlaka ya unyang'anyi ya upapa (kupora kwa nguvu), ilikuwa sharti awafanye wanadamu wasiyafahamu Maandiko (ayafiche kwa kuleta ujinga wa kutojua Maandiko). Alifahamu kuwa Biblia ingemwinua na kumtukuza Mungu na kuwaweka wanadamu wenye ukomo katika nafasi yao wanayostahili hasa; kwa hivyo ilikuwa ni sharti zile Kweli Zake takatifu zifichwe kwa watu na kufutiliwa mbali (kwa kupigwa marufuku). Mantiki hiyo ilitumiwa na Kanisa Katoliki la Kirumi. Kwa mamia ya miaka usambazaji wa Biblia ukapigwa marufuku. Watu walikatazwa kuisoma au kuwa nayo majumbani mwao, mapadri na makasisi/maaskofu wakayafafanua mafundisho yake ili kudumisha udanganyifu

na unafiki wao. Hivyo ndivyo papa alivyokuja kutambuliwa na kukubaliwa karibu ulimwengu mzima kama kaimu wa Mungu hapa duniani au mwakilishi wa Mungu, ambaye amepewa mamlaka juu ya kanisa na serikali. [GC 51.3; PK Aya ya 8]

Baada ya kingamuzi/wa makosa (Biblia) au mafundisho potofu kuondolewa, Shetani alifanya kazi jinsi apendavyo. Unabii ulikuwa umetangaza kwamba upapa "utaazimu kubadilisha majira na sheria." Danieli 7:25. Kazi hii hakuchukua muda kuitekeleza. Ili kuwapa wongofu kutoka katika upagani mbadala wa ibada ya sanamu na njia hiyo kuhamasisha kuukublai Ukristo kwa jina tu kwamba wameupokea Ukristo, kuabudu sanamu, ibada ya wafu na vitu vyao vilivyosalia miongoni mwa hawa watakatifu wa zamani,* viliingizwa polepole, na hivyo mapokeo au itikadi za wanadamu, zikawa ndizo taratibu katika ibada ya Kikristo makanisani. Hatimaye amri ya baraza kuu ilianzisha mfumo huu wa ibada ya sanamu (tazama Kiambatisho). Ili kuikamilisha kazi hiyo ya makufuru, Kanisa la Rumi liliazimia kuifutilia mbali amri ya pili inayokataza ibada ya sanamu kutoka kwenye Sheria ya Mungu (Tazama Amri kumi katika Kutoka 20), na kuigawanya ile amri ya kumi, ili kuendelea kuwa na idadi ile ile ya amri kumi kama ilivyokuwa awali *(sanamu, picha, nguo za watakatifu au masalio yao fulani nk - relics). [GC 51.4; PK Aya ya 9]

Roho ya kuafikiana/maridhiano na upagani ikafungua njia ya kupuuza na kutojali zaidi na zaidi mamlaka ya Mbinguni. Shetani, akifanya kazi yake kwa kupitia viongozi wa kanisa lake ambao hawajajiwekwa wakfu kikamilifu, akaingia kunyumbua-nyumbua ile amri ya nne pia, naye akajaribu kuiweka kando ile Sabato ya mwanzo (Jumamosi), siku ambayo Mungu alikuwa ameibariki na kuitakasa (Mwanzo 2:2, 3) na badala yake aliinua sikukuu inayotukuzwa na wapagani kama siku ya kuheshimiwa "siku ya jua kutukuzwa." Mabadiliko haya hapo awali hayakufanywa waziwazi. Katika karne za mwanzo Sabato ya Kweli ilikuwa imetunzwa na Wakristo wote. Walikuwa na wivu kwa ajili ya heshima ya Mungu, na hawa, waliamini kwamba sheria Yake haibadiliki kamwe, basi kwa bidii walilinda utakatifu wa kanuni Zake. Lakini kwa ujanja mkubwa na siri Shetani alifanya kazi kupitia vibaraka wake kufanikisha lengo lake. Ili kuvuta umakini wa watu kuelekea Jumapili, siku hiyo ilifanywa kuwa sikukuu rasmi ya kuadhimisha ufufuo wa Kristo. Huduma za kidini zilifanyika siku hiyo; ila ilichukuliwa kama siku ya burudani, Sabato (Jumamosi) bado ikaendelea kutunzwa kwa utakatifu. [GC 52.1; PK Aya ya 10]

Ili kuandaa njia kwa ile kazi ambayo amekusudia kuikamilisha, Shetani alikuwa amewaongoza Wayahudi, kabla ya kuja kwa Kristo, kuiwekea Sabato kongwa zito na masharti makali na kufanya utunzwaji wake kuonekana kuwa mzigo mzito ulemeao. Sasa, akitumia nafasi hiyo hiyo ya nuru ya uongo ambayo alikuwa ameisababisha, aliituhumu Sabato ili watu waione kama ni taasisi ya Kiyahudi. Wakati Wakristo kwa ujumla waliendelea kuitunza Jumapili kama siku

ya sherehe ya furaha, akiwaongoza kuifanya Sabato kuwa siku ya kufunga (saumu), siku ya huzuni, kiza na majonzi ili kuonyesha chuki yao dhidi ya lile kanisa la Kiyahudi. [GC 52.2; PK Aya ya 11]

**Konstantino Atoa Amri**

Mwanzoni wa karne ya nne, Kaisari Konstantino (wa Rumi) alitoa amri ya kuifanya Jumapili kuwa siku ya sherehe ya umma katika Milki yake yote ya Rumi. (Tazama Kiambatisho). Siku hiyo ya jua (Jumapili) iliheshimiwa na raia wake wapagani na ikaheshimiwa na Wakristo; ilikuwa sera ya Mfalme huyu kuunganisha maslahi yale yanayopingana ya upagani na Ukristo (walichukua wanayopenda Wapagani na kuunganisha na Ukristo). Alishurutishwa kufanya hivyo na maaskofu wa kanisa, ambao, walikuwa wamesukumwa na tamaa ya ukuu na uchu wa madaraka, walikuwa wamegundua kwamba ikiwa siku ile ile moja ingetunzwa na kuadhimishwa na Wakristo na wapagani, basi, ingeweza kukubalika na kupokelewa kwa jina la Ukristo na wapagani na hivyo kuendeleza mbele mamlaka na utukufu wa kanisa. Lakini wakati wafuasi wa Kikristo wengi wanaomcha Mungu walipoongozwa pole pole kuiona Jumapili kama ina kiwango cha utakatifu, bado waliendelea kuishika na kuitunza Sabato ya Kweli kama takatifu kwa Bwana na tena wakaizingatia kwa kuitii amri ya nne. [GC 53.1; PK Aya ya 12]

Mdanganyifu mkuu akiwa bado hajaikamilisha kazi yake. Aliazimia kuukusanya ulimwengu wote wa Kikristo chini ya bendera yake na kutumia nguvu zake kupitia kwa kaimu wake, yaani, yule papa mwenye kiburi/anayejivuna ambaye alijidai kuwa ndiye mwakilishi wake Kristo. Kupitia wapagani wale walioongoka nusu-nusu, makasisi wenye tamaa ya ukuu na waumini wa kanisa wanaopenda ulimwengu, walitimiza kusudi lake. Vikao vya mabaraza makubwa vikafanyika mara kwa mara, kisha humo wakuu wa kanisa hilo walikusanyika kutoka ulimwenguni kote. Karibu katika kila baraza, Sabato ambayo Mungu alikuwa ameianzisha ilididimizwa chini kidogo zaidi na wakati huo huo Jumapili ikawa inainuliwa juu. Hivyo ndivyo jinsi ile siku kuu ya kipagani ilivyokuja kuheshimiwa hatimaye kama siku iliyoagizwa na Mungu kuadhimishwa, na wakati ule ule Sabato ile ya Biblia ilitangazwa kuwa ilikuwa ni desturi na mabaki tu ya dini ya Kiyahudi na waadhimishaji wake wakatangazwa kuwa wamelaaniwa. [GC 53.2; PK Aya ya 13]

Mdanganyifu huyo mkuu alikuwa amefanikiwa kujiinua mwenyewe "juu ya kila kiitwacho Mungu ama kuabudiwa." 2 Wathesalonike 2: 4. Alikuwa amethubutu kubadilisha amri ile ya pekee katika Sheria ya Mungu ambayo bila kukosea kabisa, inawaelekeza wanadamu wote kwa Mungu wa Kweli, aliye hai. Katika amri ya nne, Mungu anafunuliwa kabisa kwamba Ndiye Muumbaji wa mbingu na

dunia na kwa hali hiyo anatofautishwa na miungu yote ya uongo (Yeremia 10:10-16). Ilikuwa ni kwa ajili ya kumbukumbu ya kazi ya uumbaji, ndiyo siku ya saba ilitengwa kwa matumizi matakatifu (ilitakaswa) kama siku ya mapumziko kwa mwanadamu. Ilikusudiwa kuweka kumbukumbu katika mawazo ya mwanadamu daima kwamba Mungu aliye hai, Ndiye asili ya vyote, naam, uzima, Naye anastahili ibada na kicho. Shetani anapambana kuwageuza watu kutoka kwenye utii wao kwa Mungu na sheria Yake; na kwa hivyo huzielekeza juhudi zake kwa makini dhidi ya amri ile (Sabato) ambayo inamwonyesha Mungu kuwa Ndiye Muumbaji. [GC 53.3; PK Aya ya 14]

Waprotestanti siku hizi hudai kwamba ufufuo Wake Kristo katika siku ya Jumapili ndio uliifanya siku hiyo kuwa Sabato ya Wakristo. Lakini ushahidi wa Maandiko umekosekana, Kristo au mitume Wake hawakuitunza Jumapili kama siku ya Sabato. Uadhimishaji wa Jumapili kama taasisi au siku ya ibada ya Wakristo, asili yake ilitokana na ile “siri ya uasi” (2 Wathesalonike 2:7) ambayo, hata katika siku za Paulo ilikuwa imeanza kufanya kazi yake. Ni wapi basi na ni lini Bwana alipomuasili au kumpa idhini mtoto huyu aliyezaliwa na upapa? (Jumapili). Je, ni sababu gani ya msingi na halali inayoweza kutolewa kwa badiliko hilo ambalo halijaruhusiwa na Maandiko? [GC 54.1; PK Aya ya 15]

Katika karne ya sita, upapa ulikuwa umeimarika kabisa. Kiti chake cha enzi kilikuwa kimeimarika katika jiji na himaya na askofu wa Kanisa la Rumi alitangazwa kuwa ndiye mkuu juu ya kanisa lote. Upagani ulikuwa umeingiza upapa. Yule Joka alikuwa amempa huyo mnyama “nguvu zake na kiti chake cha enzi na mamlaka kuu.” Ufunuo 13:2. Na sasa ikaanza ile miaka 1260 ya ukandamizaji/mateso ya papa iliyotabiriwa katika unabii wa Danieli na Ufunuo. Danieli 7:25; Ufunuo 13:5-7. *(Tazama Kiambatanisho)* Wakristo wakalazimishwa kuchagua ama kutoa uadilifu wao na kuikubali taratibu na sherehe (mapokeo) ya kipapa pamoja na ibada yake au kuchakaza maisha yao katika gereza lilipo shimoni, au kifo kwa mti wa mateso au msumeno, au kuuwawa kwa kuchomwa na kuni au kuchinjwa kwa kutumia shoka. Hapa ndiyo Maneno ya Yesu yalitimia: “Mtasalitiwa na wazazi na ndugu, na jamaa, na marafiki; na baadhi yenu watauawa. Nanyi mtachukiwa na watu wote kwa ajili ya Jina Langu.” Luka 21:16, 17. Mateso yakafunguliwa kwa ghadhabu kubwa kwa waaminifu kuliko hapo awali, na kisha ulimwengu ukawa uwanja wa vita. Kwa mamia ya miaka kanisa la Kristo lilipata kimbilio katika maficho ya upweke. Ndiyo maana nabii anasema hivi: “Yule mwanamke alikimbilia nyikani, ambapo ana mahali palipotengenezwa na Mungu, ili wamlishe huko siku elfu na mia mbili na sitini.” Ufunuo 12:6. [GC 54.2; PK Aya ya 16]

Kule kuinuka kwa mamlaka ya Kanisa la Kirumi kukaashiria kuanza kwa Zama za Giza. Kadri nguvu zake zilivyozidi kuongezeka, ndivyo giza likazidi kuwa nene

(Ujinga wa Biblia, Sayansi, hata teknolojia). Imani ikahamishwa kutoka kwa Kristo, aliye msingi wa Kweli, na kwenda kwa papa wa Kanisa la Rumi. Badala ya kumtegemea Mwana wa Mungu kutoa msamaha wa dhambi na wokovu wa milele, watu wakamwangalia papa, mapadri na makasisi ambao aliwapatia mamlaka. Wakafundishwa kwamba papa alikuwa mwombezi na mpatanishi wa mwanadamu duniani na kwamba hakuna hata mmoja ambaye angeweza kumfikia au kumwendea Mungu pasipo kupitia kwa papa; na zaidi, kwamba alisimama badala ya Mungu kwao na kwa hivyo alipaswa kutiiwa kikamilifu bila swali lolote. Kwenda kinyume na matakwa yake ilikuwa sababu tosha ya adhabu kali sana kwenye miili na roho za wahalifu. Kwa hivyo akili za watu zikageuzwa kutoka kwa Mungu na kwenda kwa watu katili, wenye mapungufu, wanaoweza kuanguka dhambini (wasio wakamilifu), wenye kupotoka, naam, kwa yule mkuu wa giza mwenyewe, ambaye alikuwa akishinikiza nguvu zake kupitia kwa watu hao. Dhambi ikafichwa katika vazi la utakatifu. Wakati Maandiko yanakandamizwa yaani yanazuiwa kusomwa na mwanadamu anapojiona kuwa yeye ndiye yuko juu ya yote, kinachofuatiwa kuonekana kitakuwa udhalimu tu, utapeli, udanganyifu, uovu au maadili potofu yanayomdhalilisha mwanadamu. Katika kuinuliwa kwa sheria na mapokeo ya wanadamu sheria ya Mungu inawekwa kando, na ufisadi hudhihirika daima. [GC 55.1; PK Aya ya 17]

### Siku Za Hatari Katika Kanisa

Hizo zilikuwa ni siku za hatari kubwa kwa kanisa Lake Kristo. Waaminifu wale walioibeba bendera Yake walikuwa ni wachache mno. Ingawa ile Kweli haikuachwa bila kuwa na mashahidi au ushuhuda, lakini wakati mwingine ilionekana kuwa mafundisho yale ya uongo, upagani, umizimu na ushirikina yalikuwa yameshamiri na pengine hata dini ya Kweli ingetupiliwa mbali, duniani kote. Injili ikawa imesahauliwa, badala yake kawaida na mitindo ya dini ikaongezeka na watu wakalemewa na mizigo mizito waliyotwishwa pamoja masharti makali. [GC 55.2; PK Aya ya 18]

Wakafundishwa sio tu kumtazama papa kama mwombezi na mpatanishi wao, lakini pia kutegemea matendo yao wenyewe kama fidia ya ondoleo la dhambi zao. Safari ndefu za hija kwenda kuzuru ‘patakatifu’, kutenda matendo ya kitubio, kuabudu visanamu vilivyowakilisha wafu wa zamani au sehemu zao za mwili, au vitu vyao kama nguo, kujenga makanisa, kuabudu watakatifu waliokufa (dini ya umizimu) kwenye sehemu maalumu, kujenga makaburi ya watakatifu, kujenga altare za miungu na madhabahu za namna hiyo, kulipa fedha nyingi kwa kanisa—haya, pia na matendo mengine mengi yanayofanana na haya yaliamriwa ili kuituliza ghadhabu ya Mungu au kupata upendeleo Wake; kana kwamba Mungu

alikuwa kama wanadamu, kwamba angeweza kukasirishwa kwa mambo madogo madogo sana, yasiyo na maana, au kutulizwa kwa kupewa vijizawadi au matendo ya toba (kitubio)! [GC 55.3; PK Aya ya 19]

Licha ya ubaya au uovu wa jambo hilo, ushawishi wake uliendelea kushamiri na kuenea kwa uhakika kila mahali hata kati ya viongozi wa Kanisa la Kirumi. Karibu na mwisho wa ile karne ya nane, wafuasi wa papa waliweka madai kwamba katika enzi za kwanza za kanisa la Kikristo, maaskofu wa Kanisa la Rumi walikuwa wanayo mamlaka yale yale ya kiroho ambayo sasa walikuwa nayo. Ili kuridhisha watu kwa dai hilo, mbinu zingine zililazimika kutumika ili kulipatia dai hilo mamlaka yao; kasha njia ilipendekezwa kwa urahisi na baba wa uongo. Maandishi ya kale yaligushiwa na watawa (yakaigwa kwa kutumia udanganyifu). Matamko ya mabaraza yaliyokuwa hayajapata kusikiwa siku za nyuma yaligunduliwa, yakithibitisha ukuu wa papa usio na kifani ulimwenguni kote tangia nyakati zile za zamani. Na kanisa ambalo lililokuwa limekataa ile Kweli katakata kwa tamaa/uroho wake likakubali udanganyifu huu. (*Tazama Kiambatisho.*) [GC 56.1; PK Aya ya 20]

**Wasiotishwa Na Upinzani**

Waaminifu wachache waliojenga juu ya msingi ule wa Kweli (1 Wakorintho-3:10, 11) walifadhaishwa na kutatanishwa vibaya na kuzuiliwa kutenda kazi kwa zile takataka za yale mafundisho ya uongo (uchafu). Kama wajenzi wale wa kuta zile za Yerusalemu katika siku za Nehemia, wengine walikuwa tayari kusema: “Nguvu zao wachukua mizigo zimedhoofika, na kifusi tele kipo. Tusiweze kuujenga ukuta “ Nehemia 4:10. Kwa kuchoshwa na mapambano ambayo hayaishi dhidi ya mateso, ulaghai, uovu na kila kikwazo kinginecho chote ambacho Shetani angeweza kukibuni ili kuzuia maendeleo yao, wengine ambao walikuwa wajenzi waaminifu walivunjika moyo; na kwa ajili ya amani na usalama kwa mali zao na maisha yao, waliuacha msingi ule wa Kweli. Ila, wengine pasipo kuogopa upinzani ule wa maadui zao, walisema bila woga: “Msiwaogope: kumbukeni Bwana, aliye Mkuu na wa kutisha” (aya ya 14); na wakaendelea mbele na kazi yao, kila mtu akiwa amejifunga upanga wake kiunoni mwake. Waefeso 6:17. [GC 56.2; PK Aya ya 21]

Roho ile ile ya chuki na upinzani wa ile Kweli iliyosukuma maadui wa Mungu katika kila kizazi na ukeshaji wa uaminifu ule ule, vimekuwa vikihitajika miongoni mwa watumishi Wake Mungu hadi mwisho wa wakati. Maneno ya Kristo kwa wanafunzi Wake wa awali yanatumika kwa wafuasi Wake hadi mwisho wa wakati: “Ninachosema kwako nasema kwa wote, Tazama.” Marko 13:37. [GC 56.3; PK Aya ya 22]

Giza lile likaonekana kana kwamba linaongezeka zaidi. Ibada ya sanamu ikawa imezagaa kwa wingi zaidi, na kuwa jambo la kawaida. Mishumaa ikawashwa

mbele ya sanamu na sala zikafanywa kwa sanamu. Desturi zile za kipuuzi kabisa na za kishirikina na kimizimu zichukua hatamu. Akili za watu zikadhibitiwa kabisa na ujinga na mapokeo ya kishirikina na kufikiri kwenyewe kwa ubongo kukaonekana kupoteza nguvu zake. Kwa kuwa mapadri na maaskofu wenyewe walikuwa wapenda anasa za dunia, wenye tamaa za mwili (waasherati) na mafisadi, ilikuwa wazi basi kutarajia vile vile kwa watu wale waliotegemea uongozi wao kwamba nao wangezama katika ujinga na uovu. [GC 57.1; PK Aya ya 23]

Hatua nyingine katika dhana ya upapa ilichukuliwa, wakati, katika karne ya kumi na moja, Papa Gregory wa Saba alipotangaza kwamba Kanisa la Kirumi ni kamilifu. Miongoni mwa madai aliyotoa ilikuwa ni lile linalodai kwamba kanisa lile halijawahi kukosea, na wala lisingekosea kamwe, kulingana na Maandiko Matakatifu yasemavyo. Lakini kulingana na uthibitisho/ushuhuda wa Maandiko maneno hayo yaliyosemwa na mwanadamu hayakupatana na yale ya Mungu. Papa yule mwenye majivuno alidai pia kuwa na mamlaka ya kuwaondoa watawala wa dola katika kiti chao cha enzi na akatangaza kwamba hakuna maamuzi yeyote ambayo yeye ameyatangaza yanaweza kutenguliwa na mtu mwingine yeyote, ila kwamba yeye ndiye alikuwa na haki ya kuyabadili au kuyabatilisha maamuzi ya wengine wote. (*Tazama Kiambatanisho*) [GC 57.2; PK Aya ya 24]

**Henry Wa Nne (IV) Ajinyenyekeza**

Kielelezo halisi cha kushangaza cha tabia dhalimu (dikteta) ya wakili huyo wa fundisho la kwamba 'papa hakosei' kilionekana katika namna ile aliyomtendea mfalme Henry IV yule wa Ujerumani, Kwa ajili ya kutotambua kwake kwa makusudi, mamlaka ya papa, mfalme huyo alitangazwa kuwa ametengwa na ushirika wa kanisa na kuondolewa kwenye kiti chake cha madaraka ya ufalme (alitishiwa). Kwa hofu kubwa ya kutengwa na vitisho kutoka kwa wakuu wake mwenyewe, ambao walikuwa wametiwa moyo kufanya uasi dhidi yake yeye na agizo la papa, Henry aliona umuhimu wa kupatana na Rumi (kutafuta amani). Akiandamana na mkewe na mtumishi mwaminifu, walivuka safu za ile milima mirefu ya Alps wakati wa majira yale ya baridi kali na theluji, ili kujisalimisha na kujinyenyekeza mwenyewe mbele ya papa yule. Baada ya kufika kwenye kasri ambayo Gregory alikuwa amekwenda kupumzika, aliongozwa kwenda bila wapambe wake kwenye ua wa nje, kwenye baridi kali ya msimu huo wa theluji, huku kichwa chake kikiwa wazi bila kufunikwa, na pasipo kuvaa viatu na mavazi yanayomsitiri, alisubiri ruhusa ya kumwona papa ili aweze kukutana naye. Ni mpaka zilipopita siku tatu za kufunga na kuungama, ndipo papa yule alipojishusha na kumpa msamaha. Hata hivyo ilikuwa kwa sharti tu kwamba

mfalme huyu asubiri masharti/vizuizi fulani kutoka kwa papa kabla ya kuanza tena kutumia madaraka yake ya kifalme. Na Gregory, akiwa amejaa furaha kubwa kwa ushindi wake, alitamba kuwa ni jukumu lake kutiisha, na kushusha viburi vya wafalme. [GC 57.3; PK Aya ya 25]

Ni tofauti iliyoje, na ya kushangaza kati ya kiburi cha papa huyu aliyekuwa dikteka ukilinganisha na upole na unyenyekevu wa Kristo, ambaye anajiwasilisha Mwenyewe kama mtu anayebisha hodi mlangoni, akibembeleza kuingia ndani, ili atakapoingia alete msamaha na amani, tena Yule aliyewafundisha wanafunzi Wake, akisema: "Yeyote anayetaka kuwa mkuu kati yenu, na awe mtumwa wenu." Mathayo 20:27. [GC 58.1; PK Aya ya 26]

Karne zilizofuata mbele, zilishuhudia kuongezeka mara kwa mara kwa uongo katika mafundisho yaliyotolewa kutoka katika kanisa hilo la Rumi. Hata kabla ya kuanzishwa kwa upapa mafundisho ya wanafalsafa wa kimizimu na kipagani yalipewa umakini na kuzingatiwa na kanisa. Wengi ambao walidai kuongoka bado waling'ang'ania kanuni na falsafa zao za kipagani, nao sio tu waliendelea kujifunza falsafa hiyo wao wenyewe, bali waliwashurutisha watu wengine kuipokea kwamba, ndiyo ilikuwa njia ya kupanua ushawishi wao miongoni mwa wale makafiri. Makosa makubwa na ya kutisha yakaingizwa katika mafundisho ya imani ya Kikristo. Fundisho kuu kati ya hayo lililojitokeza sana lilikuwa ni lile la imani ya kwamba mtu hafi, yaani kutokufa kwa mwanadamu, kwamba mtu anapokufa bado ufahamu wake unaendelea kuwepo hata katika kifo. Fundisho hili liliweka msingi wa kanisa la Rumi kuanzisha sala kwa ajili ya watakatifu (waliokufa) na ibada ya Bikira Maria,* Kutokana fundisho hili pia kuliibuka uzushi wa mateso ya moto wa milele kwa yule ambaye hataweza hatimaye kutubu, fundisho ambalo lilingizwa mapema kabisa katika imani ya kipapa. ***(Ibada kwa wafu, au jitihada ya kuzungumza na watu waliokufa, huitwa pia dini ya umizimu)*** [GC 58.2; PK Aya ya 27]

Kisha njia ikaandaliwa kwa kuingizwa kwa uvumbuzi/ubunifu mwingine wa kipagani, ambao kanisa la Rumi liliupa jina la 'toharani' (Purgatori) (Yaani mahali pa ahera pa kutakasia dhambi ndogo) na fundisho hilo likatumiwa kuwaogofya, na kuwaridhisha watu waliopo kwenye makundi ya wasio na ufahamu, wanaodanywa kirahisi na washirikina (wajinga wa Maandiko). Kwa uongo huo wakathibitisha uwepo wa mahali pa mateso ambapo roho za wale ambao hawajastahili hukumu ya milele zitapaswa kuadhibiwa kwa ajili ya dhambi zao, na ya kwamba, baada ya hapo, zinawekwa huru mbali na uchafu wake, ndipo roho hizo hutoka toharani, na kuingizwa mbinguni ****(wanadai zinawekwa huru kwa njia ya maombezi ya viongozi wao wa dini). (Tazama Kiambatisho)*** [GC 58.3; PK Aya ya 28]

Bado uzushi mwingine ulihitajika ili kuiwezesha Rumi kufaidika kutokana na hofu hiyo ya watu, na maovu ya wafuasi wake. Uongo huo uliwezekana kwa kutumia fundisho la indulgensia (yaani ondoleo la dhambi au msamaha kwa wale wanaopenda kujifurahisha na anasa). Ondoleo kamili la dhambi za zamani, dhambi za sasa na dhambi za siku za baadaye, na kuachiliwa ili mtu asiweze kupatikana na maumivu au machungu yote pamoja na adhabu zote anazostahili (toharani), likawa limeahidiwa kwa wale wote ambao wangejiandikisha katika vita vya papa ili kupanua mipaka ya utawala wake wa kidunia, na ili kuwaadhibu maadui zake au kuwaangamiza kabisa wale ambao wangethubutu kupinga ukuu wake usio wa kifani wa kiroho. Watu hao pia wakafundishwa kwamba kwa kulipa pesa kwa kanisa wangeweza kujiweka huru kutoka katika dhambi na pia kuzifungua roho za marafiki zao waliokufa ambazo zilikuwa zimefungiwa katika shimo la moto wa mateso (pugatori). Kwa njia hizo kanisa hilo la Rumi likajaza makasha yake ya hazina na kudumisha fahari, anasa na uovu wa yule aliyejifanya kuwa mwakilishi bandia wa Yeye ambaye hakuwa na mahali pa kulaza kichwa Chake (Kristo). *(Tazama Kiambatanisho)* [GC 59.1; PK Aya ya 29]

Agizo la Maandiko kuhusu huduma ya Meza ya Bwana lilikuwa limeondolewa na badala yake ikawekwa ibada ya sanamu ya misa (ibada ya kimizimu). Makasisi wa kipapa, kwa kutamka maneno fulani ya kidini kwa minong'ono isiyofahamika (maneno yasiyo na maana au mummery), wakajidai kwamba wanaweza kubadilisha mkate na divai ya kawaida kuwa "mwili na damu halisi ya Kristo." -- Kardinali Wiseman, Uwepo halisi wa Mwili na Damu ya Bwana wetu Yesu Kristo katika Ekaristi iliyobarikiwa, Imethibitishwa Kutoka kwenye Maandiko, hotuba ya 8, seh. 3, kif. 26. Kwa Madai yao haya ya kukusudia na kufuru, walidai waziwazi kuwa na uwezo wa kumwuumba Mungu, Muumbaji wa vyote. Wakristo walitakiwa, kwa tishio la kuuwawa (kifo), kuikiri na kuidumisha imani yao katika udanganyifu huo unaotisha, wa kuitukana Mbingu. Watu wengi waliokataa kuafiki walichomwa moto. *(Tazama Kiambatanisho)* [GC 59.2; PK Aya ya 30]

Katika karne ile ya kumi na tatu kilianzishwa chombo kikuu cha kutisha mno cha uendeshaji wa upapa (injini ya upapa)---yaani Inkwizisheni (Inquistion) *(Taasisi ya Kimahakama au Baraza la kanisa la Rumi la kukomesha uasi, hasa katika karne ile ya 15 na 16; pia huitwa 'ofisi takatifu' kuhukumu Wazushi au wapingaji).* Mkuu wa giza alishirikiana na viongozi wa uongozi wa hierakia au ngazi zile za upapa (hierarchy). Katika mabaraza yao ya siri, Shetani na malaika zake walidhibiti mawazo ya watu wabaya na katikati yao alisimama malaika wa Mungu asiyeonekana, akichukua kumbukumbu ya kutisha ya amri zao zilizojaa uovu na kuandika historia ya matendo mabaya, ya kikatili, ya kuchukiza na ya kutisha mno, ambayo yasingeweza kuonekana kwenye macho ya mwanadamu. "Babeli mkuu" (Rumi) alikuwa "amelewa na damu za watakatifu" Ufunuo 17:5, 6. Mamilioni ya wafia dini ambao miili yao ilikuwa imeharibiwa vibaya walimlilia Mungu ili apate

kulipiza kisasi juu ya mamlaka hiyo ya uasi. *(Semi hii ni kama ya damu ya Habili inamlilia Mungu katika Mwanzo 4, Watakatifu walikatwa, walitumbuliwa, walipasuliwa, walisagwa, walinyumbuliwa hadi kufa)* [GC 59.3; PK Aya ya 31]

Upapa ukawa dikteta/dhalimu, ukatawala ulimwengu mzima. Wafalme na watawala wakuu wa dola, wakasujudia (wakapigia magoti) matamko ya papa, mkuu wa kanisa la Rumi. Hatima ya Maisha ya wanadamu kwa wakati huo na milele zote, ikaonekana kana kwamba ilikuwa chini ya udhibiti wake. Kwa mamia ya miaka mafundisho ya dini kutoka Rumi yalikuwa yamepokelewa na watu kwa mapana yote na bila maswali yoyote, taratibu zake za ibada zililendeshwa kwa kicho, sherehe zake zikatuzwa kwa ujumla na watu wote. Makasisi wake waliheshimiwa, walitukuzwa na kutendewa kwa ukarimu (walipewa mahitaji yao kwa wingi). Kamwe kanisa la Rumi halikuwahi kufikia heshima kuu, hadhi, ufahari, au mamlaka kuu kama wakati huo. [GC 60.1; PK Aya ya 32]

Lakini ule "mchana wa upapa ilikuwa ni usiku wa manane kwa ulimwengu mzima." - J. A. Wylie, Historia ya Uprotestanti,b. 1, Sura ya 4. Maandiko Matakatifu yalikuwa hayajulikani kwa kiasi kikubwa, si kwa watu wa kawaida tu, bali hata kwa mapadri (makasisi). Kama ilivyokuwa kwa Mafarisayo wa zamani, viongozi wa kipapa waliichukia ile nuru ambayo ingeweza kufunua dhambi zao. Sheria ya Mungu, ambayo ndiyo kipimo cha haki (kanuni ya haki), baada ya kuondolewa, waliyatumia mamlaka yao bila mipaka na kutenda uovu bila vizuizi vyovyote (hawakuthibitiwa). Ulaghai, tamaa ya mali, na ubadhirifu vilishamiri na kuenea kila pahali. Wanadamu hawakujiepusha na uhalifu wowote ambao kwao wangeweza kujipatia utajiri au cheo. Majumba ya mapapa na makasisi yalikuwa maonyesho ya ufisadi mbaya, kama uasherati, ulevi na uovu mwingine. Baadhi ya mapapa waliotawala walikuwa na hatia ya uhalifu wa kutisha, kiasi kwamba watawala wa serikali za dunia walinuia na kujitahidi kuwaondoa hawa viongozi wa kanisa wenye tabia za kizimwi (au zinazofanana na wanyama wakatili wa pori) ambao hawakuweza kuvumilika hata kidogo. Kwa karne nyingi Ulaya haikuweza kuendelea au kusonga mbele katika elimu, sanaa au ustaarabu. Kupooza kimaadili na kiakili kulikuwa kumeiangukia Jumuiya ya Wakristo ulimwenguni. [GC 60.2; PK Aya ya 33]

Hali ya ulimwengu chini ya mamlaka ya Rumi ilionyesha kutimiza kwa namna ya kutisha na kushangaza Maneno haya ya nabii Hosea: "Watu Wangu wameangamizwa kwa kukosa maarifa: kwa sababu umekataa maarifa, Nami pia nitakukataa:...Umesahau sheria ya Mungu wako, Nami pia nitawasahau watoto wako." "Hakuna Ukweli, wala rehema, wala kumjua Mungu katika nchi. Kwa kuapa, na kusema uongo, na kuua, na kuiba, na kufanya zinaa, huruka mpaka na damu hugusana na damu." Hosea 4:6, 1, 2. Hayo ndiyo yalikuwa matokeo ya kuliondolea mbali Neno la Mungu. [GC 60.3; PK Aya ya 34]

# SURA YA 4

# WAWALDENSIA/WAVODWA

**(Kuitetea Kweli Milimani Kwa Karibu Milenia Nzima—300-800 BK)**

Ufupisho: Miaka mingi iliyopita kule Ulaya ya kusini kati, wale waliompenda Mungu na Neno Lake, yaani Maandiko Matakatifu walisakwa na kuteswa kwa ajili ya imani yao. Columba alianza kituo cha utume Iona 563BK. Kutoka hapa wamishonari walitumwa sehemu mbali mbali na hadi huko Italia mwaka 614 BK. Ila Warumi waliingia Saxon 596 BK na kuwaletea watu hao dini yao ya upagani. Ni nini kilisababisha haya yote, na waliyastahimilije haya, Je, walipona kweli? Hakika sote tuwashukuru watu hawa, vizazi vijavyo haviwezi kujua haswa yale waliyosaidiwa na kuwepo kwao, sasa unaenda kusoma watu ambao historia ilitaka kuwafutilia mbali kwenye dunia, watu hawa waliteswa vikali walipoendelea kuitunza Sabato na amri za Mungu wakihubiria watu huko Afrika, Asia na Ulaya. Mwaka 1487 Ndipo papa Innocent alipoamuru wapondwe kama nyoka wa Sumu. Soma Historia ya Wawaldensia.

Katikati ya giza lile la utusitusi lililotanda duniani wakati wa kipindi kirefu cha hatamu za kipapa, nuru ya ile Kweli haikuweza kuzimwa kabisa. Katika kila kizazi walikuwepo mashahidi wa Mungu-- watu ambao waliitunza imani yao katika Kristo, kwamba Ndiye mpatanishi wa pekee kati ya Mungu na mwanadamu, watu ambao waliishikilia Biblia kama kanuni yao ya pekee ya maisha na ambao waliitakasa na kuitunza Sabato ya Kweli. Ni kwa kiasi gani ulimwengu huu unawiwa na waaminifu kama hawa, vizazi vile vijavyo havitaweza kuelewa hili kamwe. Walipewa jina baya la wapotoshaji, na waasi, dhamiri zao zilishutumiwa, tabia zao zilichafuliwa, maandishi yao yaliondolewa, yakawakilishwa visivyo au kuchanwa-chanwa. Ila walidumu kusimama imara na kutoka kizazi hadi kizazi wakadumisha imani yao katika hali ya usafi wake kama urithi mtakatifu kwa vizazi vijavyo. [GC 61.1; PK Aya ya 1]

Historia ya watu wa Mungu katika zama za giza zilizofuatiwa mara baada tu ya Rumi kushika hatamu zake za utawala, yote imeandikwa kule mbinguni, lakini ina sehemu ndogo mno katika rekodi zilizoandikwa na wanadamu. Kumbukumbu au viashiria vichache sana vinaweza kupatikana leo, isipokuwa tu zile za mashtaka ya watesi wao. Ilikuwa sera ya Rumi kufutilia mbali kila dokezo au mabaki yanayopinga mafundisho au maagizo yake. Kila kitu kilichohusu kile alichokiita ‘uzushi,’ iwe ni watu au maandishi, Rumi ilijaribu kukiharibu kabisa. Kuonyesha mashaka au kuhoji maswali juu ya mamlaka au mafundisho ya papa, kulitosha kuyaondolea mbali maisha ya watu waliohusika, iwe ni matajiri au maskini, wenye cheo au wenye hali ya chini. Rumi ilipania pia kuharibu kila rekodi ya ukatili wake, kwa wote walioipinga. Mabaraza ya Papa yaliagiza kwamba vitabu na maandishi yaliyo na rekodi kama hizo yanapaswa kuondoshwa kwa miale ya moto. Kabla ya ugunduzi wa uchapaji wa maandishi, vitabu vilikuwa vichache na katika mfumo au dutu ambayo ni ngumu kuhifadhiwa; kwa hivyo hakukuwa na ugumu kwa Warumi kutekeleza azma yao. [GC 61.2; PK Aya ya 2]

Hakuna kanisa lolote lililokuwa chini ya hatamu ya Kirumi lililoachwa kwa muda mrefu bila kufadhaishwa katika kufurahia uhuru wao wa dhamiri. Mara tu upapa ulipopata nguvu, ndipo uliponyoosha mikono yake ili kuwaponda-ponda wote waliokataa kuutambua utawala wake, na kanisa moja baada ya jingine, likajisalimisha chini ya mamlaka yake. [GC 62.1; PK Aya ya 3]

Huko Uingereza Ukristo ule wa asili na ulio sahili, na wa Kweli ulikuwa umeotesha mizizi yake mapema sana. Injili iliyopokelewa na Waingereza katika karne za kwanza ilikuwa kwa wakati huo isiyogoshiwa (haijachafuliwa) na uasi ule wa Kirumi. Mateso kutoka kwa falme kuu za kipagani, ambayo yalifikia hata fukwe za mbali, ndiyo zawadi pekee ambayo makanisa ya kwanza ya Uingereza yalipokea kutoka kwa Rumi. Wakristo wengi, walikimbia mateso huko Uingereza, kisha wakapata kimbilio huko Scotland; kutoka hapo Ukweli ulipelekwa katika

nchi ya Ireland na katika nchi hizi zote ulipokelewa kwa shangwe. [GC 62.2; PK Aya ya 4]

Wakati Wasaxon walipovamia Uingereza, imani yao ya upagani ilipata nguvu na kustawi sana. Washindi hawa wa vita walioteka wengine, waliona wapo juu sana kustahili kufundishwa na watumwa wao na ndipo wale Wakristo wakalazimishwa kurudi milimani, vichakani na nyikani. Hata hivyo, nuru ile iliyojificha kwa muda fulani, iliendelea kuangaza. Huko Scotland, karne moja baadaye, nuru hiyo iliangaza kwa mwanga uliofikia nchi za mbali. Kutoka Ireland alikuja mcha Mungu Columba na watendakazi wenzake, ambao walikusanya waumini waliotawanyika kwenye kisiwa chenye upweke cha Iona, walifanya sehemu hii kuwa kitovu cha kazi zao za umishenari. Miongoni mwa wainjilisti hawa alikuwepo mtunzaji wa Sabato ya Biblia, kwa hivyo kwa njia hiyo Ukweli huo ukaanza kutambulishwa miongoni mwa watu hawa. Shule ilianzishwa huko Iona, ambayo wamishenari walitoka kwenda nje, si tu Scotland na Uingereza, bali hadi kule Ujerumani, Uswizi na hata kule Italia. [GC 62.3' PK Aya ya 5]

**Tofauti Kubwa**

Lakini Rumi ilikuwa imekodolea macho yake kule Uingereza na ikaazimu kuileta Uingereza chini ya himaya yake. Katika karne ya sita wamishonari wake wakafanya kazi ya kuwaongoa Wasaxson wapagani (lugha za zamani zilisema washenzi). Hapa walipokelewa kwa upendeleo na hawa watu wasio wastarabu, yaani wapagani waliojaa majivuno, nao waliwashawishi maelfu mengi wakiri imani ya Kanisa la Kirumi. Kazi ilipoendelea mbele, viongozi wale wa papa na waongofu wao walikutana na Wakristo safi wa awali. Tofauti ya kushangaza ilionekana kati yao. Wale wa mwisho hawakuwa na mambo mengi, walikuwa watu wa kawaida, sahili na wanyenyekevu, na tena waliishi mtindo wa maisha unaoendana na Maandiko katika tabia, mafundisho na adabu, ambapo wale wa kwanza walidhihirisha tabia ya ushirikina, kutaka makuu (fahari), nao walikuwa na ubinafsi na majivuno ya upapa. Mjumbe wa Rumi alidai kwamba makanisa haya ya Kikristo yakubali au kutambua kwamba papa ni mfalme mkuu kuliko wote. Waingereza* walijibu kwa upole kwamba walitamani kuwapenda watu wote, lakini kwamba papa hakuwa na haki ya kuchukua mamlaka na kuwa mkuu wa kanisa na wangeweza kumpa yeye tu utii ule ambao unastahili kila mfuasi wa Kristo. Majaribio yalirudiwa kila mara ili kupata uaminifu wao kwa Rumi (walitii lile kanisa la Rumi); lakini Wakristo hawa wanyenyekevu, wakiwa wameshangazwa na kiburi kilichoonyeshwa na wajumbe hawa, walijibu kwa kusimama imara kwamba wao hawamjui Bwana mwingine zaidi ya Kristo. Sasa roho halisi ya upapa ikawa imefunuliwa. Kiongozi huyo wa Warumi akasema: "Ikiwa hamtawapokea ndugu hao wanaowaletea amani, ninyi mtawapokea maadui ambao watawaletea vita. Ikiwa hamtaungana nasi katika kuwaonyesha

Wasaxson njia ya maisha, basi mtapokea pigo la mauti kutoka kwao."- JH Merle D'Aubigne, Historia ya Matengenezo ya karne ya kumi na sita, b. sura ya 17.2. Hivyo havikuwa vitisho vya bure. Vita, fitina, madanganyo na hila vilitumika dhidi ya mashahidi hawa waliokuwa na imani ya Biblia, mpaka makanisa ya Uingereza yalipoharibiwa kabisa au kulazimishwa kuyatii mamlaka ya papa kwa kujisalimisha *(Britons ni watu wa visiwa vine-England, Wales, Scotland na Ireland ya Kusini). [GC 62.4; PK Aya ya 6]

Katika nchi zile zilizokuwa mbali na mamlaka ya Rumi kulikuwa na makundi ya Wakristo yaliyodumu kuwa huru kwa kiasi kikubwa kwa karne nyingi na ufisadi wa kipapa. Walikuwa wamezungukwa na ukafiri, na zama zile ziliposonga mbele, wakawa wameathiriwa na makosa yake (upagani); lakini waliendelea kuichukulia Biblia kama mwongozo/kanuni pekee ya imani na wakazingatia Kweli Zake nyingi. Wakristo hawa waliamini kudumu kwa Sheria ya Mungu na waliishika ile Sabato ya amri ya nne. Makanisa yale yaliyoshikilia imani hii na mazoea haya yalikuwako kule Afrika ya Kati (Ethiopia, Ghana n.k) na miongoni mwa Waarmenia wa Asia. [GC 63.1; PK Aya ya 7]

**Imani Ya Waldensia**

Lakini, miongoni mwa watu waliokataa katu kuingiliwa na mabavu ya papa walikuwa ni Wawaldensia, hawa walisimama imara katika mstari wa mbele ukilinganisha na wengine. Katika nchi ile ambayo upapa umesimika kiti chake, yaani makao yake makuu, hapo ndipo uongo wake na ufisadi ulipopingwa zaidi. Kwa karne nyingi makanisa yale ya Piedmont yaliendelea kuwa na uhuru wao; lakini hatimaye wakati ukafika ambapo Rumi ilipoyalazimisha kuitii. Baada ya mapambano yasiyo na matunda dhidi ya dhuluma (udikteta) yake, viongozi wa makanisa haya kwa shingo upande wakaikiri mamlaka ile kuwa ndiyo kuu kuliko zote ambayo ulimwengu wote ulionekana kana kwamba unaitambua na kuisujudu. Lakini hata hivyo, kulikuwa na wengine ambao walikataa kuitii mamlaka ya. Walikuwa wamedhamiria kudumisha utii wao kwa Mungu na kutunza usafi na unyenyekevu wa imani yao (Imani isiyo na mapambo katika desturi zake za ibada). Mafarakano yakatokea. Kwa hiyo wale ambao waliikumbatia imani ile ya zamani kikamilifu walijitenga na wengine, wakiiacha milima yao ile mirefu ya Alps, wakaiinua bendera ya Ukweli katika nchi za kigeni; wengine wakakimbilia kwenye mabonde membamba ya milima iliyokuwa na miamba (ngome) na huko walikojitenga waliudumisha uhuru wao wa kumwabudu Mungu. [GC 64.1; PK Aya ya 8]

Imani ambayo kwa karne nyingi ilishikiliwa na kufundishwa na Wakristo wa Wawaldensia ilikuwa tofauti kabisa na yale mafundisho ya uongo yaliyotolewa kutoka Rumi. Imani yao ya kidini ilijengwa juu ya msingi wa Neno la Mungu ambalo liliandikwa, walikuwa na mfumo sahihi, na wa Kweli wa Ukristo. Lakini

wakulima hawa wanyenyekevu, katika maficho yao, walikuwa wametengwa mbali na ulimwengu, na kulazimika kufanya kazi ngumu kama kuchunga mifugo na kushugulikia mashamba yao ya mizabibu kila siku, hawa walikuwa hawajaifikia Kweli hiyo wenyewe, yaani ule Ukweli ulio kinyume cha mfumo wa dini ya mazoea na uasi wa kanisa ili kuyapinga mafundisho yale ya upotovu na uongo (dogma) wa lile kanisa asi/kengeufu. Imani yao waliyoipokea haikuwa imani mpya. Imani yao ile ya kidini ilikuwa ni urithi wao kutoka kwa mababa zao. Walishindania imani ile ya kanisa lile la mitume, -- “imani ambayo walikabidhiwa watakatifu wa Mungu mara moja tu” Yuda 3. “Kanisa la nyikani,” wala si ule mfumo wa utawala wa msonge (hierachy) wenye majivuno mengi, ulioketi katika kiti cha enzi katika ule mji mkuu wa dunia, hili ndilo lilikuwa Kanisa la Kweli la Kristo, mlinzi wa hazina za Ukweli ambazo Mungu amewekeza kwa watu Wake ili waweze kuufikisha kwa ulimwengu. [GC 64.2; PK Aya ya 9]

Miongoni mwa sababu kuu zilizoleta kujitenga kwa Kanisa lile la Kweli kutoka Rumi ilikuwa ni ile chuki ya Rumi dhidi ya Sabato ya Biblia (Jumamosi). Kama ilivyotabiriwa katika unabii, mamlaka ile ya kipapa ikautupa Ukweli chini (Dan 8:12). Sheria ya Mungu (Amri kumi) ikakanyagwa katika mavumbi, ilhali mila na desturi za wanadamu zikainuliwa juu na kutukuzwa. Makanisa yale yaliyokuwa chini ya utawala wa kipapa yalilazimishwa mapema kuiheshimu Jumapili kama siku takatifu. Katikati ya mafundisho yenye makosa, uasi na ushirikina ulionea, wengi, hata miongoni mwa wale watu wakweli wa Mungu, walichanganyikiwa mno kiasi kwamba wakati walipokuwa wakiitunza Sabato (Jumamosi), waliacha kufanya kazi siku ile ya Jumapili pia. Lakini hili halikuwaridhisha wale viongozi wa upapa. Waliwashurutisha kwa nguvu wakisema, sio tu kwamba Jumapili itakaswe, bali kwamba Sabato (Jumamosi) itiwe unajisi (inajisiwe); wakawakemea kwa lugha kali hadharani wote waliodiriki kuiheshimu Sabato ya Kweli. Ilikuwa ni kwa kukimbia tu mbali na nguvu ile ya Rumi, ndiyo uwezekano ungelikuwapo wa kuitii Sheria ya Mungu kwa amani (Amri za Mungu). (Tazama Kiambatisho.) [GC 65.1; PK Aya ya 10]

Wawaldensia walikuwa miongoni mwa watu wa kwanza wa Ulaya kupata tafsiri ya Maandiko Matakatifu *(Tazama Kiambatisho)*. Mamia ya miaka kabla ya Matengenezo ya kanisa (Reformation) walikuwa na Biblia iliyonakiliwa kwa mkono katika maandishi (muswada), kwa lugha yao ya asili (lugha ya kuzaliwa au ya mama). Walikuwa na Kweli ile isiyogoshiwa (isiyochafuliwa na kuchanganywa na uongo) na jambo hilo liliwafanya wao wawe walengwa wa chuki na mateso makali. Wakalitangaza Kanisa la Rumi kuwa ni Babeli ulioanguka (waasi) wa kitabu kile cha Ufunuo, na kwa kuhatarisha maisha yao wakasimama kidete na kupinga ufisadi na udhalimu wake. Chini ya shinikizo la mateso ya muda mrefu, wengine walianza kutoisimamia imani yao ya awali, taratibu, yaani kidogo kidogo wakaanza kukubaliana na kanuni zake bainishi, ila wengine miongoni mwao

waliushikilia sana Ukweli. Muda wote walipokuwa wakipitia zama za giza na ukengeufu, kulikuwa na kundi la Wawaldensia waliokataa ukuu wa Rumi, ambao walikataa kuzisujudia sanamu yaani ibada ya sanamu na ambao waliishika Sabato ile ya Kweli (Jumamosi). Chini ya dhoruba kali za upinzani walidumisha imani yao. Japo mkuki ule wa Savoyard uliwatoboa na kuwatia majeraha makubwa, tena walichomwa kwa moto juu ya tita la kuni za Kirumi, bado walisimama bila kutetereka na kulitetea Neno la Mungu na heshima Yake. [GC 65.2; PK Aya ya 11]

Nyuma ya ngome zile ndefu za milima—ambazo zilikuwa kimbilio lao Wawaldensia waliteswa na kudhulumiwa katika vizazi vyote - - Hapo, Wawaldensia walipata mahali pao pa kujificha. Hapo ndipo nuru ile ya Kweli ilipotunzwa, nayo ikaendelea kuwaka katikati ya giza la Zama za Kati. Hapa ndipo, kwa miaka elfu, wale mashahidi wa ile Kweli walidumisha imani ya awali/zamani. [GC 65.3; PK Aya ya 12]

**Mungu Aliwafunga Kiunoni Mshipi Wa Nguvu**

Mungu alikuwa amewaandalia watu Wake mahali pa hifadhi na kimbilio penye uzuri wa kushangaza, pahali pa fahari kubwa, palipofaa kutunza zile Kweli zenye nguvu walizopewa kuzihifadhi kama amana. Kwa wakimbizi hao waaminifu waliokuwa wamefukuzwa mbali na kwao, milima ile ilikuwa nembo au ishara ya uadilifu wa Yehova usiobadilika uhamishoni. Waliwaelekeza watoto wao kwenye vile vilele virefu juu yao katika kuonyesha ukuu Wake usiobadilika-badilika na kunena nao juu Yake Yeye ambaye Kwake hakuna kubadilika- badilika, wala kivuli cha kugeuka-geuka, ambaye Neno Lake ni la kudumu kama vilima vile vya milele. Mungu alikuwa ameisimika kwa uimara milima ile na kuivika nguvu; hakuna mkono wowote ila ule wa Nguvu isiyo na kipimo peke yake ndiyo ambao ungeweza kuiondoa pale ilipowekwa. Kwa namna ileile, alikuwa ameiweka Sheria Yake kuwa msingi wa serikali Yake mbinguni na duniani. Mkono wa mwanadamu unaweza kuwafikia watu wenzake na kuyaharibu maisha yao; lakini kama vile ambavyo mkono huo wa binadamu usingeweza kuing'oa milima ile kwa urahisi kutoka kwenye misingi yake na kuitupa baharini, ndivyo vile vile ambavyo usingeweza kuibadili hata amri moja ya Sheria ya Yehova au kufutilia mbali mojawapo ya ahadi Zake kwa wale watendao mapenzi Yake. Katika uaminifu wao kwa sheria Yake, watumishi wa Mungu wanapaswa kusimama imara, na kutobadilika kama vilima visivyobadilika. [GC 66.1; PK Aya ya 13]

Milima ile iliyoyazunguka mabonde yale ya chini, ilikuwa ni mashahidi wa kudumu wa nguvu za uumbaji za Mungu, uhakikisho wa ulinzi Wake usioshindwa kamwe na utunzaji Wake. Wasafiri au mahujaji hao walijifunza kuzipenda alama zile za kimya za uwepo wa Yehova. Hawa hawakulalamika au kusononeka kwa sababu ya ugumu waliokuwa wakiupitia kimaisha; hawakuwahi kujihisi kuwa ni wapweke katikati ya milima ile iliyokuwa mbali na makazi ya watu huko nyikani.

Walimshukuru Mungu kwamba alikuwa amewapatia hifadhi mbali na ghadhabu na ukatili wa wanadamu. Wakaufurahia uhuru wao wa kuabudu mbele Zake Bwana. Mara nyingi walipokuwa wanafuatwa na maadui zao, nguvu za vilima hivi zilithibitisha ulinzi wa hakika kwao. Kutoka kwenye miamba ile mirefu waliziimba sifa Zake Mungu kwa shangwe na wala majeshi yale ya Rumi hayakuweza kuzinyamazisha nyimbo zao za shukrani kwa Mungu. [GC 66.2; PK Aya ya 14]

Wafuasi hawa wa Kristo walikuwa na uchaji Mungu (utawa) wenye usafi wa moyo, wema, usahili, na bidii. Walizithamini kanuni za ile Kweli zaidi ya majumba, ardhi, marafiki, jamaa na hata uhai wenyewe (Ufu 12:11). Walitafuta kwa bidii kuziweka mioyoni mwa vijana kanuni hizi. Tangu wakiwa watoto wachanga, vijana wao walilelewa kwa mafundisho ya Maandiko, wakifunzwa kuyachukua madai ya Sheria ya Mungu kuwa ni matakatifu. Nakala za Biblia zilikuwa haba mno; na kwa hiyo, Maneno Yake ya thamani yaliwekwa kwenye kumbukumbu za vichwa vyao- kwa kukaririwa. Wengi waliweza kukariri sehemu kubwa za Agano la Kale na Jipya. Mawazo yao juu ya Mungu yalihusishwa sawa na mandhari zile za juu zilizokuwa nzuri kwa asili, na baraka walizozipata katika maisha yao ya kila siku (miti, mimea, wanyama, mito, milima, na riziki). Watoto wadogo walijifunza kumtazama Mungu kwa shukrani kama mpaji/mtoaji wa kila neema, upendeleo, fadhili na faraja. [GC 67.1; PK Aya ya 15]

Wazazi, wakiwa wema, wanaojali na wenye mapenzi kama vile walivyokuwa hasa, waliwapenda watoto wao kwa hekima mno kiasi cha kutowazoesha kujifurahisha au kudekeshwa, na pia walilelewa kwa kujengewa uwezo kifikra ili watende na kujitegemea wenyewe (walikuza kujikana nafsi, yaani afya na kiasi). Mbele yao walikabiliwa na maisha magumu ya majaribu (maonjo) na shida, na pengine hata kifo cha mfia dini. Mapema kwenye utoto walifundishwa kuvumilia magumu, kukubali kuongozwa na wakati huo huo pia kufikiria na kutenda wao wenyewe binafsi (kujitegemea kifikra). Mapema sana walifundishwa kubeba majukumu yao, kuwa makini katika kulinda ndimi zao, na kuielewa hekima ya kukaa kimya. Neno moja lisilo la busara linaporuhusiwa kudondoka masikioni mwa maadui zao lingeweza kuhatarisha sio tu maisha ya mnenaji, bali pia maisha ya mamia ya ndugu zake; kwani kama vile mbwa mwitu wanavyowinda mawindo yao, ndivyo maadui wa ile Kweli walivyowawinda watu waliothubutu kudai uhuru wa imani ya dini. [GC 67.2; PK Aya ya 16]

Wawaldensia walikuwa wameyatoa kafara mafanikio yao ya ulimwengu huu na kuachana na utajiri wao wa kidunia kwa ajili ya ile Kweli na walifanya hili kwa uvumilivu usiochoka, walijitaabisha kwa kazi ngumu ili kujipatia riziki zao. Kila kipande cha ardhi kilichowezekana kulimika kati ya milima yao kiliboreshwa kwa uangalifu ili kiweze kutoa mavuno mengi; mabonde na mitelemko yenye rutuba kidogo iliboreshwa ili kutoa mazao mengi. Somo la uchumi, yaani kubana

matumizi, kutofuja pesa, na kukana nafsi viliunda sehemu ya elimu ambayo watoto hawa waliipata kama urithi wao wa pekee. Walifundishwa kwamba Mungu huyapanga maisha haya kuwa somo la kuwafundisha nidhamu ya kuikana nafsi, na kwamba mahitaji yao yangeweza kupatikana tu kwa njia ya kutoa jasho kwao binafsi, kwa kufikiria mipango ya mbele, kuwa waangalifu, kujali na kutunza imani. Mchakato huo ulikuwa mgumu, wenye kazi nzito zenye usumbufu na kuchosha, lakini huo ulikuwa mpango mkamilifu wa Mungu, jambo ambalo mwanadamu alilihitaji kwa hakika kukidhi hali yake ya anguko, hiyo ilikuwa shule ambayo Mungu alikuwa ameitoa kwa ajili ya mafunzo na maendeleo yake. Japokuwa vijana walikuwa wamezoezwa kuhenyeka na kazi ngumu na shida, uboreshaji wa akili haukupuuzwa. Walifundishwa kuwa uwezo na nguvu zao zote zilikuwa ni mali ya Mungu, na kwamba vyote vinapaswa kuboreshwa na kuendelezwa kwa huduma/utumishi Wake. [GC 67.3; PK Aya ya 17]

### Ari Ya Kimishonari Na Kujitolea Mhanga

Makanisa ya Wavaudois/Kivodwa (Wawaldensia wa Kiitaliano), katika usafi, usahili na unyenyekevu wake, yalifanana na kanisa la nyakati zile za mitume. Waliukataa kabisa ule utawala uliosema papa na maaskofu wake ndiyo wakuu zaidi kuliko mwingine yoyote, wakiishikilia Biblia kuwa ndiyo mamlaka ya juu kuliko yote, na isiyoweza kukosea. Wachungaji wao, walikuwa tofauti na wale mapadri wa Rumi waliotaka kuwa waheshimiwa wanaotumikiwa na kujaa kiburi, kwani wao walikifuata kielelezo cha Bwana wao, ambaye "hakuja kuhudumiwa au kutumikiwa, bali kutumika na kuhudumia." Walilisha kundi la Mungu, wakiliongoza kwenye malisho mabichi na chemchemi hai za Neno Lake Takatifu. Kinyume na zile sanamu za fahari na kiburi cha wanadamu na kujiinua, watu hao walikusanyika, sio katika makanisa ya kifahari au katika makanisa makubwa ya majimbo yaitwayo kathedro, bali chini ya vivuli vya milima, kwenye mabonde ya milima ile mirefu sana ya Alps kule Ulaya, au, nyakati za hatari, katika ngome mojawapo kwenye miamba, kusikiliza Maneno ya Ukweli kutoka kwa watumishi Wake Kristo. Wachungaji wao hawakuihubiri injili tu, bali walitembelea wagonjwa, wakiwafundisha Watoto kwa njia ya maswali na majibu, wakawaonya wakosaji (waliotenda dhambi) na kufanya bidii kusuluhisha magomvi na kuhamasisha maelewano na upendo kati ya ndugu. Nyakati za amani walitegemezwa na sadaka za matoleo ya hiari ya watu; lakini, kama Paulo mtengenezaji wa mahema, kila mmoja alijifunza biashara, stadi/fani au ufundi wa aina fulani ambao, ikiwa atalazimika kuutumia, basi angeweza kufanya vile ili aweze kujipatia riziki na kujikimu maisha yake mwenyewe. [GC 68.1; PK Aya ya 18]

Vijana walipokea mafundisho Kutoka kwa wachungaji wao. Japokuwa elimu ya maarifa ya matawi ya kawaida ilitiliwa umakini sana (mitaala katika mashule

yote yaani hesabu, lugha, historia, sayansi nk), Biblia ndiyo ilifanywa kuwa somo lao kuu. Injili za Mathayo na Yohana ziliwekwa kwenye kumbukumbu vichwani mwao, na Nyaraka nyingi za mitume katika Biblia zilikaririwa pia. Walitumika pia katika kunakili Maandiko. Miswada mingine ilikuwa na Biblia nzima (manuscript), ila nakala zingine zilikuwa na visehemu vifupi tu, ambavyo ufafanuzi sahili wa maandishi uliambatanishwa pamoja navyo na wale waliokuwa na uwezo wa kufafanua Maandiko. Basi kwa njia hiyo, hazina zile za Kweli ambazo kwa muda mrefu zilikuwa zimefichwa na wale ambao walitafuta kujiinua wenyewe juu ya Mungu ziliwekwa wazi. [GC 68.2; PK Aya ya 19]

Kwa kufanya kazi kwa uvumilivu, pasipo kuchoka, nyakati zingine wakiwa kwenye mapango yenye kina kirefu na giza, na kutumia mienge ya moto kama mwanga, Maandiko Matakatifu yaliandikwa, mstari kwa mstari, sura kwa sura. Hivyo ndivyo ambavyo kazi ilivyosonga mbele, na mapenzi ya Mungu yaliyofunuliwa mle yakawa yaking'aa kama dhahabu safi; ni wale tu waliokuwa wamehusika kuifanya kazi ile, ndiyo walioweza kutambua kwa udhahiri mng’ao ule ulivyokuwa mkali zaidi, dhahiri zaidi, na wenye nguvu kwa kiasi gani kutokana na majaribu (shida) waliyoyapitia kwa ajili ya kazi hii. Malaika kutoka mbinguni waliwazingira wale watendakazi waaminifu. [GC 69.1; PK Aya ya 20]

Shetani alikuwa amewasukuma mapadri na maaskofu wa kipapa kulizika Neno la Kweli chini ya mafundisho potofu yenye takataka na makosa, uzushi (uongo), na ushirikina wao; lakini kwa namna ya ajabu kabisa Biblia ilihifadhiwa bila kuchafuliwa kupitia katika kipindi cha zama zote za giza (vizazi vyote). Neno la Mungu halikubeba muhuri wa mwanadamu, bali chapa ya Mungu. Wanadamu walikuwa hawachoki katika juhudi zao za kuficha maana ya Maandiko iliyo wazi, na sahili, na kuyafanya yapingane na ushuhuda wake yenyewe; lakini kama Safina ilivyokuwa inaelea kwenye vilindi virefu vya mawimbi na tufani, ndivyo Neno la Mungu linavyoshinda katika dhoruba zinazolitishia na uharibifu. Kama vile mgodi ulivyo na visehemu vyenye utajiri wa dhahabu na fedha chini ya ardhi ili watu watu wanaotaka wafanye bidii kuchimba na kuzigundua stoo/ghala zake za thamani, kadhalika Maandiko Matakatifu yana hazina za ile Kweli ambazo hufunuliwa tu kwa yule mtafutaji wa dhati, aliye mnyenyekevu na mwenye bidii katika kujitoa wakfu na maombi. Mungu alikusudia kwamba Biblia iwe Kitabu cha mafunzo kwa wanadamu wote, katika umri wa utoto, ujana, na utu uzima, na kwamba kiwe kitabu cha kusomwa wakati wote (vipindi vyote). Yeye Alitoa Neno Lake kwa wanadamu kama ufunuo Wake Mwenyewe. Kila Kweli mpya inayoeleweka ni ufunuo mpya wa tabia ya Mwandishi/Mwasisi Wake. Kujifunza na Kuyachunguza Maandiko ndio njia iliyoamriwa na Mungu ya kuwaleta watu katika muungano wa karibu zaidi na Muumba wao na kuwapa uelewa wa wazi wa mapenzi Yake. Ni mfereji wa mawasiliano kati ya Mungu na mwanadamu. [GC 69.2; PK Aya ya 21]

Japokuwa Wawaldensia walikuwa wanatambua kuwa kumcha Bwana ndiyo chanzo cha hekima, watu hawa hawakuwa vipofu katika kutambua umuhimu wa kuwa na mawasiliano na ulimwengu huu, kuwafahamu wanadamu wengine na maisha na kazi zao za kila siku, ili kukuza akili zao na kuharakisha uelewa wa mambo. Baadhi ya vijana wao waliomaliza masomo kwenye shule zao kule milimani walipelekwa kwenye vyuo (taasisi) vya masomo katika miji ya Ufaransa au Italia ambapo kulikuwa na nyanja pana zaidi za masomo, fikra na uchunguzi kuliko katika milima yao ya Alps walikozaliwa. Vijana hao waliopelekwa huko, walikuwa karibu zaidi na majaribu, wakashuhudia uovu, na kukutana na mawakili wa Shetani, ambao waliwasihi wakubali uzushi wenye hila na udanganyifu wa hatari zaidi. Lakini malezi na elimu yao waliyoipata tangu utotoni yalikuwa ya tabia ile ya kuwaandaa kukabiliana na haya yote. [GC 69.3; PK Aya ya 22]

Katika shule walizokwenda kusomea, hawakupaswa kumfanya mtu yoyote kuwa msiri wao au kumweleza mambo yao ya ndani zaidi. Mavazi yao yalishonwa kwa namna ambayo ingesitiri hazina yao kuu—yaani maandishi ya mkono ya yale Maandiko ya thamani (muswada wa Maandiko). Hayo Maandiko, yalikuwa ni matunda ya miezi na miaka ya kazi ngumu, nao wakatembea pamoja nayo, na kila walipoweza kuwapa watu bila kuamsha shuku, walipandikiza kwa uangalifu sehemu fulani ya hizi Kweli katika njia za wale ambao mioyo yao ilionekana kana kwamba imefunguliwa wazi kupokea Kweli. Tangu walipopakatwa kwenye magoti ya mama zao, vijana hawa wa Kiwaldensia walikuwa wamefundishwa kusudi hilo kwenye fikra zao; walielewa kazi yao, na kwa uaminifu waliifanya. Waongofu wa imani ya Kweli walipatikana kutoka katika taasisi hizi za elimu na mara nyingi kanuni zake zilionekana zikipenya katika chuo au shule nzima na kusambaa-watu wakaongoka; pamoja na uchunguzi wa karibu Zaidi ukafanywa, viongozi wa papa hawakuweza kugundua chanzo cha kile walichokiita uzushi wenye kuharibu. [GC 70.1; PK Aya ya 23]

Roho ya Kristo ni roho ya kimishenari. Msukumo au hisia ya kwanza kabisa ya moyo uliofanywa upya ni kuwaleta wengine pia kwa Mwokozi. Hiyo ndiyo ilikuwa roho ya Wakristo wa Vaudois. Waliamini kwamba Mungu alihitaji kutoka kwao zaidi ya kuhifadhi tu Ukweli katika usafi wake katika makanisa yao wenyewe; kwamba wajibu mkubwa sana ulikuwa juu yao kuiruhusu nuru yao iangaze kwa wale ambao walikuwa gizani; kwa uwezo mkuu wa Neno la Mungu walitafuta kuvunjilia mbali vifungo vile ambavyo Rumi ilikuwa imeweka. Wachungaji wa Vaudois walifundishwa kuwa wamishenari, kila mtu ambaye alitarajia kuingia katika huduma ya kichungaji alihitajika kwanza kupata uzoefu wake wa kazi kama mwinjilisti. Kila mmoja alitakiwa kutumika kwa miaka mitatu katika eneo moja la utume kabla ya kukabidhiwa kuongoza kanisani nyumbani au nchini kwao (kanisa mahalia). Huduma hiyo, iliyohitaji kwanza kujikana nafsi, na kujitoa, ilikuwa utambulisho mzuri unaofaa kwa maisha ya mchungaji katika nyakati zile zilizojaribu kwa ukali roho za watu. Vijana waliowekewa mikono ya uchungaji ili

kufanya kazi katika ofisi takatifu ya huduma, hawakuona mbele yao yale matarajio ya kupata utajiri na utukufu wa dunia hii, bali maisha yaliyoambatana na kazi ngumu, usumbufu na hatari, na pengine hata kukabiliwa na ile hatima ya mfia dini. Wamishonari walikwenda wawili-wawili, kama vile Yesu alivyowatuma wanafunzi Wake. Kila kijana wa kiume kwa kawaida alikuwa akipewa mwanamume wa makamo na mzoefu, kisha kijana huyu akawa chini ya uongozi wa yule mwenzake ambaye aliwajibika na kumfundisha na ambaye alitakiwa kuyazingatia maagizo yake. Watendakazi hawa hawakuwa pamoja wakati wote, lakini mara nyingi walikutana kwa ajili ya maombi na kushauriana na hivyo kuimarishana katika imani. [GC 70.2; PK Aya ya 24]

Kitendo cha kujulikana lengo la utume wao kungehakikisha kushindwa kwake; kwa hivyo hawakuweka mwenendo wao halisi wazi, hapa ilibidi wawe waangalifu. Kila mchungaji/mhudumu alikuwa na ufahamu wa ujuzi fulani wa kazi, yaani stadi, au tasnia fulani, kisha wamishenari hawa walitekeleza wito wao wa utume chini ya mwavuli wa vibarua vya kawaida vya kidunia, yaani visivyohusiana na shuguli za utume au mambo ya kiroho (washona mahema-tent makers). Kwa kawaida walichagua njia ile ya mfanyabiashara wa jumla au mchuuzi reja reja (machinga wa nyumba kwa nyumba). "Walibeba vitambaa au nguo za hariri, vito vya mapambo au vitu vinginevyo, ambavyo kwa wakati ule havikuweza kununulika karibu kirahisi isipokuwa sehemu za mbali; na walikaribishwa kama wafanyabiashara katika maeneo ambayo vinginevyo wangelikataliwa katu ikiwa wangeenda kama wamishenari."- Wylie, b. 1, sura ya 7. Wakati wote huo, mioyo yao ilikuwa imeinuliwa juu kwa Mungu ili kupata hekima ya kuiwasilisha ile hazina yenye thamani zaidi kuliko dhahabu au vito vya thamani. Walibeba kwa siri sehemu au nakala nzima za Biblia, na wakati wowote fursa nzuri ilipojitokeza, waliyavuta mawazo ya wateja wao katika miswada hii (nakala za Maandiko zilizonakiliwa na mkono). Mara nyingi hamu ya kusoma Neno la Mungu iliamshwa, na hivyo wakawaachia kwa furaha wateja wao waliokuwa tayari kupokea Neno, au sehemu ya Maandiko haya Matakatifu. [GC 71.1; PK Aya ya 25]

### Kuzitawanya Mbegu Za Thamani Sana

Kazi ya wamishonari hawa ilianzia katika tambarare na mabonde yanayozunguka milima yao wenyewe, lakini ilipanuka na kwenda mbali zaidi ya mipaka hii. Wakiwa wanatembea bila viatu (peku) na mavazi yaliyochakaa na kuchafuka kwa safari kama yalivyokuwa yale ya Bwana wao, wakipita kwenye miji mikubwa na kupenya hadi nchi za mbali. Kila mahali wakisambaza mbegu hii ya thamani. Makanisa yalichipua katika njia yao, na damu ile ya wafia dini ikashuhudia ile Kweli. Siku ya Mungu itafunua mavuno mengi ya roho yaliyokusanywa ghalani kwasababu ya kazi za watu hawa waaminifu. Likiwa

limefunikwa na kimya kimya, Neno la Mungu liliendelea kusafiri na kupenya katika ulimwengu ule wa Kikristo na kupokelewa kwa furaha majumbani na mioyoni mwa watu (kabla ya mtandao Neno lilikwenda kasi, wakati wetu wa teknolojia au mtandao linabidi liende kwa kasi ya mwanga, fursa ni kubwa zaidi sasa). [GC 71.2; PK Aya ya 26]

Kwa wale Wawaldensia Maandiko hayakuwa kumbukumbu au historia tu ya jinsi Mungu alivyoshugulika na wanadamu katika kipindi kile cha zamani, na ufunuo wa wajibu na majukumu ya nyakati hizi, bali ulikuwa pia ni mafunuo ya hatari zile kubwa na utukufu wa siku za usoni. Waliamini kwamba mwisho wa mambo yote haukuwa mbali sana, na walipojifunza Biblia kwa maombi na machozi waliguswa zaidi mioyoni mwao na Maneno yake ya thamani na jukumu lao la kuwajulisha wengine ule Ukweli Wake uokoao. Waliona mpango wa wokovu ukiwa umefunuliwa wazi zaidi (dhahiri) katika kurasa zake takatifu, nao walipata faraja, matumaini na amani katika kumwamini Yesu. Nuru ilipoangazia uelewa wao na kuburudisha mioyo yao, walitamani kuimulika nuru hiyo kwa wale ambao walikuwa katika giza la makosa ya upapa. [GC 72.1; PK Aya ya 27]

Waliona kwamba chini ya mwongozo wa papa na mapadri wake, watu wengi walikuwa wakijitahidi kupata msamaha bila mafanikio kwa kuitesa miili yao kwa ajili ya dhambi za roho zao. Wakiwa wamefundishwa kutegemea matendo yao mema kuwaokoa, walikuwa wakijitazama wenyewe kila wakati, huku akili zao zikatafakari juu ya hali yao ya dhambi, nao wakajiona wameachwa peke yao kukabiliana na hasira ya Mungu, nao wakajitesa roho na mwili, lakini hawakupata afueni yoyote. Hivyo ndivyo roho za watu wale waliokuwa na dhamira iliyokuwa na uangalifu sana zilivyofungwa na mafundisho ya Rumi (binadamu anapaswa kuwa na dhamira ya uangalifu kwa Mungu kwanza na si kwa mwanadamu). Maelfu wakatelekeza marafiki na jamaa zao na kwenda kutumia maisha yao katika vyumba vidogo vya watawa. Kwa mifungo (saumu) iliyorudiwa mara kwa mara na kujichapa wenyewe kwa ukatili kabisa (mijeledi yenye misumari katika ncha zake), katika mikesha ya usiku wa manane, kwa kusujudu kifudifudi kwa masaa mengi ya kuchosha sana juu ya mawe baridi na yenye unyevunyevu yaliyokuwa makao yao yenye mwonekano unaotisha, kwa kufunga safari ndefu kwenda kuhiji, kwa toba zenye adhabu za kudhalilisha na suluba za mateso ya kutisha, maelfu walitafuta amani ya dhamiri zao bali ilikuwa ni kazi bure. Wakiwa wamelemewa na mateso ya hisia za dhambi zao, walisumbuliwa mara kwa mara na hofu ya ghadhabu ya Mungu ya kulipiza kisasi, wengi wao waliendelea kuteseka hadi hali yao ya uchovu ikajichokea na kifo kikaja, na bila ya kuwa na hata mwale mmoja wa nuru au tumaini wakazama na kuingia ndani ya makaburi. [GC 72.2; PK Aya ya 28]

### Kuwaelekeza Wenye Dhambi Kwa Kristo

Wawaldensia walitamani kuwamegea watu hawa wenye njaa mkate wa uzima, kuwafungulia watu ujumbe ule wa amani unaopatikana kutoka katika ahadi za Mungu na kuwaelekeza kwa Kristo ambaye ndiyo tumaini lao pekee la wokovu. Fundisho lao kuu la kwamba matendo yao mema yanaweza kulipia uvunjaji wa sheria ya Mungu lilishikiliwa na watu licha ya kuwa ni msingi uliojengwa juu ya uongo. Kutegemea haki au kazi ya binadamu kunapotosha uhalisia wa upendo wa Kristo usio na kipimo. Yesu alikufa kama dhabihu kwa mwanadamu kwa sababu wanadamu walioanguka hawawezi kufanya neno lolote liwezalo kuwapa sifa ya kukubalika na Mungu. Wema na sifa za Mwokozi aliyesulubiwa na kufufuka ndiyo msingi wa imani ya Kikristo. Tegemeo la roho kwa Kristo ni jambo halisi kabisa, na muunganiko Naye sharti uwe wa ukaribu sana kama ulivyo mkono au mguu na mwili au tawi lilivyo kwa mzabibu. [GC 73.1; PK Aya ya 29]

Mafundisho ya mapapa na makasisi yalikuwa yamewafanya watu waifikirie tabia ya Mungu, na hata ya Kristo, kama ni ya ukali sana, isiyo na upendo, isiyovutia, isiyo na huruma na yenye kuleta huzuni (mawingu), isiyo na urafiki na ya kuogofya mno. Mwokozi aliwakilishwa kama asiye na rehema kwa mwanadamu hata kidogo katika hali yake mwanadamu ya kuanguka, kiasi cha kuhitaji upatanisho wa mapadri na watakatifu. Wale ambao akili zao zilikuwa zimeangaziwa na Neno la Mungu walitamani kuzielekeza roho hizi kwa Yesu kama Mwokozi wao Mwenye huruma, Mwenye mapenzi/upendo, aliyesimama na mikono iliyonyoshwa, akiwaalika wote wamwendee Yeye na mizigo yao ya dhambi, masumbufu, na uchovu wao. Walitamani kuondoa vizuizi ambavyo Shetani alikuwa amevirundika ili watu wasizione ahadi Zake Bwana, na kuja moja kwa moja kwa Mungu, na kutubu Kwake dhambi zao na kupata msamaha na amani. [GC 73.2; PK Aya ya 30]

### Kuushambulia Ufalme Wa Shetani

Kwa shauku kubwa, mmishonari wa Kivodwa aliwafunulia wote waliohitaji kujua Kweli ya thamani ya injili. Kwa tahadhari aliwaonyesha sehemu za Maandiko Matakatifu zilizonakiliwa kwa mkono. Ilikuwa furaha yake kubwa kutoa tumaini kwa yule ambaye dhamiri yake imemchoma baada ya kugongwa na dhambi, yule ambaye alikuwa akimwona Mungu kama mlipiza kisasi tu, anayesubiri kumlipa mtu kwa haki yake. Kwa midomo iliyotetemeka na jicho lililojaa machozi, na mara nyingi akiwa magotini, aliwafungulia ndugu zake ahadi za Maandiko za thamani na tamu ambazo, humfunulia mwenye dhambi tumaini lake la pekee. Na hivyo ndivyo nuru ya Ukweli ilivyopenya kwenye mioyo mingi iliyotiwa giza, ikirudisha nyuma wingu la huzuni, mpaka Lile Jua la Haki (Kristo) lilipoangaza mioyoni mwao na miale Yake ya uponyaji. Ilikuwa kawaida kuisoma sehemu fulani ya Maandiko kwa kuirudia tena na tena, msikilizaji alitamani

irudiwe kana kwamba alitaka kujiridhisha kwa kujihakikishia kuwa amesikia kwa usahihi. Maneno haya ndiyo yaliyopendwa hasa na kurudiwa sana, kwani kurudiwa kwake kulitamaniwa sana na watu: “Damu ya Yesu Kristo Mwanawe hututakasa na dhambi zote.” 1 Yohana 1:7. “Kama vile Musa alivyoinua nyoka jangwani, vivyo hivyo sharti Mwana wa Adamu ainuliwe: ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.” Yohana 3:14, 15. [GC 73.3; PK Aya ya 31]

Watu wengi hawakudanganywa kwa madai ya Rumi. Waliona jinsi ule upatanisho wa mwanadamu au malaika kwa niaba ya mwenye dhambi ulivyokuwa kazi bure. Kadri nuru ya Ukweli ilipowazukia mioyoni mwao walisema kwa kupaza sauti ya shangwe: “Kristo Ndiye kuhani wangu; Damu Yake ni kafara yangu; Madhabahu Yake ndipo mahali pa toba/maungamo yangu.” Wakajisalimisha kikamilifu juu ya sifa Zake Yesu, wakirudia Maneno, “Pasipo imani haiwezekani kumpendeza Mungu.“ Waebrania 11:6. “Wala hakuna wokovu katika mwingine awaye yote, kwa maana hapana jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo.” |Matendo 4:12. [GC 74.1; PK Aya ya 32]

Hakikisho la upendo wa Mwokozi lilionekana kwao kwamba limepita upeo wao kueleweka kwa baadhi ya watu wale maskini waliotupwa huku na kule na dhoruba za mafundisho ya uongo. Maneno hayo yalileta ahueni na faraja kubwa, mafuriko ya nuru yalimwagwa juu yao, kiasi cha kuona kana kwamba walikuwa wamesafirishwa na kuwasili mbinguni. Mikono yao ilishikiliwa kwa ujasiri katika mkono ule wa Kristo; na miguu yao ilisimikwa juu ya ule Mwamba wa Zama zote. Hofu zote za kifo zikapotea. Sasa waliweza kulitamani gereza au kuchomwa moto na kuni zilizolundikwa pamoja, endapo kwa njia hiyo wangeweza kulitukuza Jina la Mkombozi wao. [GC 74.2; PK Aya ya 33]

Katika maeneo ya siri, Neno la Mungu lililetwa na kusomwa, wakati mwingine kwa mtu mmoja tu, nyakati zingine kwa kikundi kidogo kilichokuwa kikitamani sana kuipata nuru na ile Kweli. Mara nyingi usiku kucha ulitumiwa kwa njia kama hiyo. Wasikilizaji walitekewa mno na mshangao na matamanio jambo ambalo lilimfanya mbeba ujumbe wa rehema akatishe usomaji, mpaka wasikilizaji wake waelewe vyema habari njema ya wokovu. Mara nyingi maneno kama haya yalisemwa: “Hivi ni kweli Mungu anaweza kuikubali sadaka yangu? Je! Ataonyesha tabasamu Lake kwangu mimi? Je! Yeye atanisamehe mimi?” Jibu lilisomwa: "Njooni Kwangu, ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo, Nami nitawapumzisha.” Mathayo 11:28. [GC 74.3; PK Aya ya 34]

### Njia Ya Kweli Ya Maisha

Imani ikaishikilia ahadi hiyo na kisha jibu la furaha lilisikika: “Hakuna haja ya kufanya safari ndefu za kuhiji tena; hakuna haja ya kufanya safari za maumivu

kwenye maeneo matakatifu ya miungu wengine (holy shrines). Ninaweza kuja kwa Yesu vile nilivyo, mwenye dhambi na asiye mtakatifu (mchafu), Naye hatayapiga teke maombi yangu ya toba. “Umesamehewa dhambi zako. Zangu, hata zangu, zinaweza kusamehewa!” [GC 75.1’ PK Aya ya 35]

Wimbi la furaha takatifu liliujaza moyo, na Jina la Yesu lilikuzwa kwa sifa na shukrani zao. Roho hizo zenye furaha zilirudi majumbani mwao ili kusambaza nuru, kuurudia ujumbe ule kwa wengine, kwa kadri walivyoweza, yaani ule uzoefu wao mpya; kwamba sasa walikuwa wameipata ile Njia ya Kweli na uzima. Kulikuwa na nguvu ya ajabu na nzito katika Maneno ya Maandiko ambayo yalizungumza moja kwa moja na mioyo ya wale ambao walikuwa wana matamanio na Ukweli. Ilikuwa ni sauti ya Mungu, nayo ileleta usadikisho kwa kuchoma mioyo ya wale waliosikia. [GC 75.2; PK Aya ya 36]

Mjumbe wa Ukweli aliendelea na safari yake; lakini mwonekano wake wa unyenyekevu, ari na bidii yake ya kina na dhati, ilikuwa ni mada waliyoiongelea tena na tena. Katika matukio mengi wasikilizaji wake walikuwa hawajamuuliza alikotoka au anakokwenda. Walikuwa wametekewa kabisa, mwanzoni kwa mshangao na baadaye kwa shukrani na furaha, kiasi kwamba hawakuwaza kumhoji maswali yoyote. Walipokuwa wanamwomba kuandamana nao kwenda majumbani mwao, aliwajibu kwamba imempasa kuwatembelea kondoo wa kundi waliopotea. Je, pengine huyo alikuwa malaika kutoka mbinguni? Waliulizana wao kwa wao. [GC 75.3; PK Aya ya 37]

Mara nyingi yule mjumbe wa Ukweli hakuweza kuonekana tena. Alikuwa amesafiri kwenda kwenye nchi zingine, au alikuwa anamaliza maisha yake kwa kuteseka katika gereza lisilojulikana chini ya ardhi au labda mifupa yake ilikuwa inageuka kuwa miyeupe na kukauka mahali alipofia bila kuzikwa kama shahidi wa Ukweli. Lakini Maneno yale ambayo alikuwa ameyaacha nyuma yake hayakuweza kuharibiwa. Yalikuwa yanafanya kazi katika mioyo ya watu; matokeo yake yaliyobarikiwa, yatajulikana kwa ukamilifu tu katika siku ya hukumu. [GC 75.4; PK Aya ya 38]

Wamishonari wa Wawaldensia walikuwa wanauvamia ufalme wa Shetani, hapo ndipo nguvu za giza ziliamshwa kwa umakini zaidi. Kila jitihada ilivyofanywa katika kupeleka Ukweli ilitazamwa kwa umakini na yule mkuu wa uovu na ikahamasisha hofu kwa mawakala wake. Wale viongozi wa upapa waliiona ishara ya hatari kutoka katika kazi ya wasafiri wale wanyenyekevu, waliotembea kwa miguu. Endapo ile nuru ya Ukweli ingeruhusiwa kung'aa pasipo kipingamizi chochote, basi ingeyapukutisha mbali mawingu mazito ya mafundisho potofu ambayo yalikuwa yamegubika watu. Ingeelekeza akili za watu kwa Mungu peke yake na mwishowe ingeangamiza ukuu wa kanisa lile la Kirumi. [GC 76.1; PK Aya ya 39]

Ule tu uwepo wa watu hawa, walioishikilia imani ya kanisa lile la awali (la mitume), ulikuwa ushuhuda wa daima wa uasi wa Rumi na kwa hivyo jambo hilo lilichochea chuki kali na mateso machungu dhidi yao. Kukataa kwao kuyasalimisha Maandiko yao pia lilikuwa kosa ambalo Rumi isingeweza kulivumilia. Rumi ikaazimia kuwafutilia mbali kutoka duniani. Sasa vilianza vita vitakatifu vya kutisha (mashambulizi yaliyojulikana kama crusades au vita vya msalaba) dhidi ya wale watu wa Mungu katika makazi yao kule milimani. Wapelelezi na wakomeshaji wale wa uasi (inquisitors-watesi) waliwekwa kuzifuatilia njia zao wanazopita, na ndipo tukio lile la Habili asiye na hatia akianguka mbele ya Kaini mwuaji likarudiwa mara nyingi. [GC 76.2; PK Aya ya 40]

Tena na tena mashamba yao yenye rutuba yalibaki ukiwa, makazi yao, makanisa yao madogo (chapels) yakafagiliwa mbali, kiasi kwamba mahali pale ambapo palikuwa na mashamba yaliyostawi na nyumba za watu wasio na hatia, na wenye bidii, palibaki kuwa jangwa tupu. Kama mnyama yule mwenye njaa kali anavyozidi kuwa mkali zaidi akionja ladha ya damu, ndivyo hasira kali ya wafuasi wa upapa ilivyowashwa na kuwa kali zaidi walipoona maumivu ya waathiriwa wao (wahanga). Wengi kati ya hawa mashahidi wa Imani safi walikimbizwa kule milimani na kuwindwa bondeni walikokuwa wametafuta maficho, wakiwa wamekingwa na misitu iliyoshonana na vilele vya miamba. [GC 76.3; PK Aya ya 41]

Hakuna shitaka lolote lililoweza kuletwa dhidi ya tabia au uadilifu wa kundi hili lililopigwa marufuku. Hata wale maadui zao walitangaza kuwa hawa ni watu wenye amani, wasio na kelele, na wacha Mungu. Kosa lao kubwa ni kwamba hawakutaka kumwabudu Mungu kulingana na matakwa au mapenzi ya papa. Kwa uhalifu huu kila aina ya udhalilishaji, unyanyasaji, matusi na mateso ambayo wanadamu au mashetani wangeweza kuyabuni yalirundikwa juu yao. [GC 76.4; PK Aya ya 42]

### Vita Takatifu Dhidi Ya Mashahidi Wa Mungu

Wakati Rumi ilipoamua kuangamiza kabisa dhehebu lile lililochukiwa (Wawaldensia), amri ikatolewa na papa (tangazo la bulla),* akiwalaani kama wazushi (waongo kwasababu wanaifuata Biblia), na kuwapeleka kuchinjwa. *(Tazama Kiambatanisho)* Hawakushutumiwa kuwa ni wavivu wanaozurura au kwamba siyo waaminifu au watu wenye fujo; lakini ikatangazwa kwamba walikuwa na mwonekano wa ucha-Mungu na utakatifu uliowavutia wale “kondoo wa zizi la Kweli.” Kwa hivyo papa aliamuru “lile dhehebu au kikundi kibaya, kiovu na chenye kuchukiza, chenye watu wenye nia mbaya,” ikiwa “watakataa kukana imani yao kwa kiapo, wapondwe-pondwe kama nyoka wenye sumu kali.” --

Wylie, b. 16, sura ya 1. Je, mtawala huyu mwenye kiburi alitarajia kukutana na maneno hayo tena? Je! Alijua kwamba maneno haya yalikuwa yameandikwa katika vitabu vya mbinguni, na atakabiliana nayo siku ya hukumu? "Kwa kadri mlivyomtendea mmojawapo wa hao ndugu Zangu walio wadogo," Yesu alisema, "mlinitendea Mimi." Mathayo 25:40. *(Fahali wa papa ni amri anayoitoa kwa umma, hati miliki ya barua, au nyaraka inayotolewa na papa wa Kanisa Katoliki. Imepewa jina la muhuri (bulla kwa lugha yao ya Kiitaliano. Interdict Kingereza). [GC 77.1; PK Aya ya 43]

Tamko au amri hii ya papa iliwataka washiriki wote wa kanisa hilo wajiunge na vita vile vya msalaba au 'vitakatifu' (crusade au utesaji) dhidi ya 'wazushi' au waasi. Kama motisha ya kuwafanya washiriki katika kazi hii ya kikatili," Washiriki walioitii ile amri waliondolewa  maumivu na adhabu zote za kidini/kikanisa, kwa ujumla na mahsusi; Rumi iliwaachilia wale wote waliojiunga na vita (walivyoviita vitakatifu) na kuwafungua kutoka katika kiapo chochote ambacho walikuwa wamekichukua; ikiwapa hatimiliki kisheria ya mali yoyote ambayo walikuwa wameipata  isivyostahili huko nyuma; na kuahidi ondoleo la dhambi zao zote kwa wale ambao watamuua mpinzani wa mafundisho yao, ambaye walidai ni mzushi. Ilitangua mikataba yote iliyofanywa kwa manufaa au kwa niaba ya Wavodwa, ikaamuru watumishi wa majumbani mwao au wale walioishi nao, waachane nao kabisa, na watu wote walizuiliwa wasiwape msaada wowote, na ikawawezesha watu wote kutwaa na kumiliki mali zao."- Wylie, b. 16, ch. 1. Hati au nyaraka hii inafunua wazi roho kuu iliyo nyuma ya pazia (yule pepo mkuu). Ni mngurumo wa Joka lenyewe na wala sio sauti ya Kristo inayosikika ndani yake. [GC 77.2; PK Aya ya 44]

Viongozi wa upapa hawakujenga tabia zao kulingana na kiwango kile kikuu cha sheria ya Mungu, lakini badala yake waliweka kiwango au kanuni zinazowafaa wao wenyewe, nao wakadhamiria kuwalazimisha wote kufuata kiwango kile kwasababu tu Rumi Ilipenda iwe hivyo. Uovu wa kutisha sana ulitendwa. Mapadri na mapapa fisadi na wenye kukufuru walikuwa wakitenda kazi ambayo Shetani alikuwa amewateua waifanye. Rehema au huruma haikuwa na nafasi katika tabia zao. Roho ile ile iliyomsulubisha Kristo na kuwaua mitume, roho ile ile iliyomhamasisha Nero mwenye kiu ya damu dhidi ya wale waaminifu katika nyakati zake, ilikuwa kazini kuwatoa duniani wale wote wanaopendwa na Mungu (wapenzi wa Mungu). [GC 77.3; PK Aya ya 45]

Kwa muda wa karne nyingi mateso yale yaliendelea kuwatembelea hawa wacha-Mungu, nao kwa uthabiti, na uaminifu, wakayavumilia yote kwa kumheshimu Mkombozi wao. Licha ya zile vita zilizoitwa za msalaba dhidi yao (crusades) na mauaji ya kuchinjwa kinyama waliyofanyiwa, waliendelea kutuma wamishenari wao kusambaza Ukweli huo wa thamani. Waliwindwa hadi wakauwawa; lakini damu yao ilinyweshea ile mbegu iliyopandwa, nazo zile

mbegu hazikushindwa kuzaa matunda. Kwa hivyo Wawaldensia walishuhudia kwa ajili ya Mungu kwa karne nyingi kabla ya kuzaliwa kwa Luther. Wakiwa Wametawanyika katika nchi nyingi, walipanda mbegu za Matengenezo ambayo yalianza wakati wa Wycliffe, na hayo Matengenezo yakapanuka zaidi katika siku za Luther na kuongezeka kwa kina, yaani kuweka mizizi chini, na hayo yanapaswa kuendelezwa mbele hadi wakati wa mwisho kupitia kwa wale ambao wako tayari kuteseka katika mambo yote kwa ajili ya "Neno la Mungu, na kwa ajili ya ushuhuda wa Yesu Kristo." Ufunuo 1: 9. [GC 78.1; PK Aya ya 46]

# SURA YA 5

# JOHN WYCLIFFE (1328-1415)

**(Sauti Ya Mtu Aliaye Nyikani, Nyota Ya Kwanza Ya Matengenezo)**

(Nuru Yaangaza Kule Uingereza—1328-1415)

Ufupisho: Ulikuwepo wakati ambao watu wa kawaida hawakuwa na Maandiko Matakatifu, yaani Biblia. Hebu fikiria, hakuna Biblia kila nyumba unayoenda! Hawakuruhusiwa kuwa nazo. Ndipo akaja mtu ambaye aliazimia kuwapa watu

Biblia majumbani mwao. Naye akatafsiri. Biblia kwa lugha ya wakazi wa nchi yake ya Uingereza, yaani Kingereza (1482-1484) Soma kilichotokea alipofanikiwa kufanya hivyo, hii ni historia ya mtumishi wa Mungu ambaye hata leo tukiwa tumebarikiwa na mitandao yetu yote ya jamii tunapaswa kumwiga kwa kusambaza Maandiko Matakatifu kwa gharama ndogo kushinda wakati wake yeye! Anza leo kusambaza Biblia Pdf kwenye ulimwengu wetu wote wa Kiswahili au lugha yoyote ile ambayo unaweza kufanya hivyo, maana ndani humo mna uzima wa milele. Ikiwezekana itafsri kwa Lugha yako haraka basi!

Kabla ya matengenezo ya kanisa kufanyika, kulikuwa na nyakati fulani ambazo nakala chache sana za Biblia zilikuwepo, lakini Mungu hakuwa ameruhusu Neno Lake liharibiwe/liangamizwe kabisa. Kweli za Neno Lake zisingeweza kufichwa milele. Yeye Angeweza kuifungua minyonyoro iliyofunga Maneno ya uzima kwa urahisi kama alivyofungua malango ya chuma ya magereza ili kuwaacha huru watumishi Wake. Katika nchi tofauti za Ulaya watu walisukumwa na Roho wa Mungu kuutafuta Ukweli kama watu watafutavyo hazina iliyositirika. Wakiwa wameongozwa na majaliwa ya Mungu kwenye Maandiko Matakatifu, walifungua na kujifunza kurasa zake takatifu kwa matamanio makubwa. Walikuwa tayari kuikubali nuru kwa gharama yoyote kwa nafsi zao. Ingawa hawakuweza kuyaona mambo yote kwa uwazi, waliwezeshwa kuzielewa Kweli nyingi zilizokuwa zimezikwa kwa muda mrefu. Kama wajumbe waliotumwa na Mbingu, watu hawa wakatoka na kusonga mbele, wakirarua-rarua na kuvitenga vile vipande vya minyororo ya mafundisho ya uongo pamoja na ushirikina wake, na kuwaita wale waliokuwa wamefanywa watumwa kwa muda mrefu, kuamka na kusimama kidete ili kuutwaa uhuru wao.[GC 79.1; PK Aya ya 1]

Isipokuwa tu miongoni mwa Wawaldensia, Neno la Mungu lilikuwa limefungwa kwa zama nyingi katika zile lugha zilizoeleweka na wasomi peke yake tu ndio. Wawaldensia walikuwa na Biblia katika lugha yao ya asili au lugha mama, (wakati wengine walikuwa nayo katika Kilatini, Kiebrania na Kigiriki tu); lakini wakati ulikuwa umewasili wa Maandiko kutafsiriwa, na kugawiwa kwa watu wa nchi tofauti mbalimbali katika lugha zao za asili. Dunia ilikuwa imelipitia lile giza la usiku wa manane na kulimaliza. Saa za giza zilikuwa zinakwisha sasa na katika maeneo mengi zilionekana dalili za mapambazuko ya alfajiri yaliyokuwa yanakuja. [GC 79.2; PK Aya ya 2]

Katika karne ya kumi na nne, kule nchini Uingereza ilitokezea "Nyota ya alfajiri ya Matengenezo ya kanisa." John Wycliffe alikuwa Mwasisi au mpiga mbiu wa kwanza wa matengenezo ya kanisa si kwa ajili ya Uingereza peke yake, bali kwa ajili ya ulimwengu wote wa Ukristo. Ule upinzani wake mkuu aliowezeshwa kuutamka dhidi ya Rumi haungeweza kunyamazishwa kamwe. Upinzani huo ulianzisha pambano ambalo matokeo yake yangemweka huru mtu mmoja mmoja, makanisa, na kisha mataifa." [GC 80.1; PK Aya ya 3]

Wycliffe alipata elimu huria au pana (liberal),* na kwake kumcha Bwana kulikuwa ndiyo chanzo cha hekima. Alijulikana chuoni kwa tabia yake ya kumcha Mungu kwa bidii (utauwa), hali kadhalika pia, kwa talanta zake zenye kushangaza na uwezo wake wa elimu. Kwasababu ya kiu yake ya maarifa, alitafuta kupata ujuzi katika taaluma/fani mbalimbali za elimu. Alikuwa amesomea masomo ya falsafa ya ualimu, historia, teolojia, kanuni au sheria za kanisa na sheria za kiraia, hususani zile za taifa lake. Katika kazi zake za baadaye, ile thamani ya mafunzo aliyopata awali, ilionekana dhahiri. Ule uelewa wake wa kina katika falsafa za nadharia za kubaini mambo kwenye kipindi chake, ulimwezesha kuyafichua makosa yaliyomo ndani yake (speculative philosophy); na kule kusomea kwake sheria ya kitaifa na ya kanisa kulikuwa kumemwandaa tayari kujihusisha katika mapambano makubwa ya kupigania uhuru wa kiraia na wa kidini. Wakati akiwa na uwezo wa kutumia silaha kutoka kwenye Neno la Mungu, alikuwa pia amejipatia uwezo wa kiakili upatikanao na nidhamu ya shule, naye alielewa mbinu za wasomi wa vyuo vikuu (wanazuoni). Uwezo uliotokana na vipaji vyake vya akili nyingi au uwezo wa kuelewa mambo kwa wepesi, kipaji cha uwezo wa fikra, na stadi  (genius) na upeo mpana na mkamilifu wa maarifa au elimu yake, vilimfanya aheshimiwe na marafiki, na maadui zake. Wale waliomuunga mkono walitazama kwa kuridhika kwamba mshindani na shujaa wao alisimama mstari wa mbele kati ya akili zinazoongoza na kutegemewa kwenye taifa; na maadui zake walizuiliwa kutupa dharau au lawama kwa kazi ile ya matengenezo ya kanisa kwamba inaendeshwa kwa ujinga au udhaifu wa  kielimu wa yule msaidizi wake anayeiunga mkono. [GC 80.2; PK Aya ya 4]

(Je, imani za elimu huria ni zipi? 'liberal Education': "elimu ya kiliberali huzalisha watu walio na akili iliyofunguka yaani iliyo wazi, ni watu wasio na upendeleo wa maeneo fulani, au mafundisho ya kidini fulani, au dhana ya awali, au kubagua itikadi fulani; hawa huwa wanajali maoni na maamuzi yao; matendo yao;…Jambo hili ni zuri kama mtu anaongozwa na Roho wa Mungu kama Wilberforce alivyopinga utumwa kwenye serikali ya Uingereza au watu weusi walivyodai kuwa na haki za kibinadamu, ila kama haongozwi na Bwana, anaweza akatua mahali pabaya na kukinzana na maagizo ya Mungu, mfano wa siku za leo itakuwa ni kama kuwa na dhana huru katika kufikiria kuwa unaweza kubadilisha jinsia yako, unaweza kutoa mimba n.k

## Ujuzi Wa Maandiko Aliokuwa Nao Wycliffe

Wycliffe akiwa bado chuoni, alianza kusoma Maandiko Matakatifu. Katika nyakati hizo za zamani, Biblia ikiwa katika lugha za awali tu (Kiebrania, Kigiriki, Kilatini), wasomi wa Biblia ndio walioweza kupata njia ya kuifikia chemchemi ya Ukweli ambayo ilikuwa imefungwa kwa matabaka ya watu wasio na kisomo. Hivyo njia ilikuwa imeshaandaliwa tayari kwa ajili ya kazi ya mbeleni ya Wycliffe, kama Mwanamatengenezo wa kanisa. Watu wenye kisomo walikuwa tayari wamejifunza Neno la Mungu na walikuwa wameipata humo ile Kweli kuu ya neema Yake Bwana iliyofunuliwa mle bure. Katika mafundisho yao walikuwa

wameeneza ujuzi wa Ukweli huu na walikuwa wamewaongoza watu wengine kuyageukia yale Mausia (oracles) ya Mungu yaliyo hai. [GC 80.3; PK Aya ya 5]

Wakati umakini wa Wycliffe ulikuwa umeelekezwa katika kuchunguza Maandiko, alijiingiza katika uchunguzi wa bidii na ukamilifu uleule uliomwezesha kubobea yale masomo ya shuleni/taaluma. Kabla ya hapa alikuwa amehisi hitaji kubwa ambalo halikuweza kutoshelezwa kwa masomo yake ya chuoni, au kwa mafundisho ya kanisa lake. Katika Neno la Mungu alikipata kile alichojitahidi kutafuta pasipo kupata mafanikio. Mle aliuona mpango wa wokovu ukiwa umefunuliwa na Kristo alidhihirishwa kama Ndiye Mwombezi na Mtetezi Pekee wa mwanadamu. Aliamua kujitoa kikamilifu kwa ajili kufanya huduma ya Kristo na kudhamiria kuzitangaza zile Kweli alizokuwa amezigundua. [GC 81.1; PK Aya ya 6]

Kama ilivyokuwa kwa Wanamatengenezo wa kanisa wa siku za baada yake, mwanzoni mwa kazi yake Wycliffe hakuweza kuona ni wapi ile kazi yake ingempeleka. Yeye hakuwa na makusudi ya kupingana na Rumi. Lakini kujitoa kwake katika kuupenda Ukweli kusingemwepusha kuingia katika mgogoro dhidi ya yale mafundisho ya uongo. Kadiri alivyobainisha waziwazi mafundisho yale potofu ya upapa ndivyo alivyozidi kufundisha kwa bidii zaidi yale mafundisho ya Biblia. Aliona kwamba Rumi ilikuwa imeliacha Neno la Mungu na mahali pake kushikilia mapokeo ya wanadamu au hadithi za binadamu tu; bila woga wowote aliwashutumu mapadri kwa kuyapiga marufuku Maandiko, na kutaka kwamba Biblia irejeshwe kwa watu na kwamba mamlaka yake ikubaliwe na kuimarishwa tena ndani ya kanisa. Alikuwa ni mwalimu hodari, mwenye umbuji, mwenye uwezo na bidii, na kisha mtindo wa maisha yake ya kila siku yalikuwa kielelezo cha Ukweli aliouhubiri. Ujuzi wake wa Maandiko, uwezo wake katika kujenga hoja, usafi wa maisha yake, na ujasiri wake usioweza kuyumba au kulegezwa pamoja na uadilifu wake thabiti vilimpatia heshima na kukubalika na watu wengi. Wengi miongoni mwa watu waliokuwa hawajaridhika na Imani yao ya awali walipoona uovu uliotawala ndani ya kanisa la Rumi, walishangilia kwa furaha isiyofichika katika kuzipokea zile Kweli alizowafunulia Wycliffe; lakini viongozi wa Upapa walijazwa na ghadhabu kali walipogundua kuwa Mwanamatengenezo yule alikuwa akiendelea kupata heshima na ushawishi mkubwa zaidi kuliko ule waliokuwa nao wao. [GC 81.2; PK Aya ya 7]

### Alikuwa Makini Sana Kugundua Makosa

Wyciffe alikuwa mgunduzi makini katika kubaini makosa, naye alikosoa bila woga mambo mengi yaliyoidhinishwa vibaya kwenye Maandiko na mamlaka ya Rumi. Wakati alipotumika kama kasisi wa mfalme alichukua msimamo mkali dhidi ya ushuru uliotozwa na papa kutoka kwa mfalme wa Kingereza na tena alionyesha kwamba ile dhana ya papa katika kujitwalia mamlaka juu ya

watawala wa serikali za kiraia, ilikuwa kinyume na busara ya kawaida na mafunuo ya Neno la Mungu. Madai ya upapa yalikuwa yameamsha chuki kubwa, na mafundisho ya Wycliffe yalichochea mvuto wenye nguvu katika akili za wale wanaoongoza katika taifa. Mfalme huyo wa Uingereza na wasaidizi wake waliungana katika kukataa madai ya papa yaliyosema kwamba yeye alikuwa na mamlaka ya kiraia, na kisha wakakataa kulipa kodi. Hivyo pigo madhubuti lilikuwa limetolewa dhidi ya mamlaka na ukuu wa upapa katika nchi ya Uingereza. [GC 82.1; PK Aya ya 8]

Uovu mwingine ambao Mwanamatengenezo huyo alipambana nao vikali kwa muda mrefu na kwa kudhamiria ulikuwa ni ule wa uanzishaji wa mfumo au taasisi ya vyama vya watawa-ombaomba.* Watawa hawa walizagaa katika nchi ya Uingereza, wakiweka kashfa mbaya juu ya ukuu na mafanikio ya taifa lile. Bidii ya kazi katika fani mbalimbali, ujasiliamali, uzalishaji, stadi, elimu na maadili yote viliathiriwa na ushawishi huu wa kunyongonyesha. Maisha ya uvivu ya watawa na ombaomba hawa, yalikuwa si mzigo mzito tu uliozikausha rasilimali na hazina za watu, bali pia zilifanya kazi yoyote ya manufaa kudharauliwa. Vijana walikatishwa tamaa, wakapotoshwa na kuharibiwa. Vijana wengi kwa ushawishi wa watawa walidanganywa kuingia katika makazi ya watawa na kutumia mle maisha yao yote kama watawa pasipo kujua wanachokifanya wala kuridhia kwa wazazi wao au hata bila ya wao kutumia utashi wao wenyewe, na kinyume kabisa cha mapenzi yao wenyewe. Mmoja wa mababa wa awali wa Kanisa la Kirumi alisisitiza na kuhamasisha watu kwamba madai yale ya kuwa mtawa yalipita jukumu la wanandugu wa damu, naye akatangaza hivi: “Hata kama baba yako atalala mbele ya mlango wako akilia na kuomboleza, na mama yako akionyesha uchi wake uliokuzaa na maziwa uliyonyonya, hakikisha ya kwamba unawakanyaga chini ya miguu yako, na kwenda zako moja kwa moja kwa Kristo.” Kwa njia ya huo “ufedhuli wa kinyama au kizimwi” ambao Luther baadaye aliuelezea kuwa “ulinukia harufu ya mbwa mwitu na dikteta kuliko Mkristo na mwanadamu mwenye utu.” Na hivyo mioyo ya watoto ikafanywa kuwa migumu kama chuma dhidi ya wazazi wao.--Barnas sears, The life of Luther, ukurasa 69, 70. Hivyo ndivyo viongozi wale wa papa walivyofanya, kama mafarisayo wale wa zamani walivyofanya, walitangua amri ya Mungu zisiwe na umuhimu au maana, ukilinganisha na mapokeo yao. Kwa hivyo nyumba zao zikafanywa hali ya ukiwa na wazazi wakawa wamenyimwa kuwa na ushirika kwenye jamii za wana na binti zao zao. *[Watawa wa chama au shirika la Mendicant walikuwa ni kundi la watawa walioweka nadhiri au kiapo cha usafi wa maisha na ufukara. Walijikimu mahitaji yao kwa kuomba omba- (Mendicant friars were an order of monks who took on vows of chastity and poverty. They supported themselves by begging.)] [GC 82.2; PK Aya ya 9]

**Walielekezwa Kwenye Chimbuko La Ile Kweli**

Hata wanafunzi wa vyuo vikuu walidanganyika na uwasilishaji wa mifano ile ya uongo iliyoonyeshwa na watawa, nao wakavutwa kujiunga katika vyama hivyo vya kitawa. Wengi baadaye walijutia hatua ile waliyoichukua, wakiona kuwa wameyaharibu maisha yao wenyewe na kuwaletea huzuni wazazi wao, lakini walipokuwa wamenaswa barabara katika mtego ule, haikuwezekana kujinasua ili kupata uhuru wao. Wazazi wengi wakiuogopa ushawishi wa watawa hao, waligoma kuwapeleka watoto wao katika vyuo vikuu nchini. Kulikuwa na kupungua mahudhurio kulikoonekana dhahiri katika idadi ya wanafunzi waliojisajili katika vituo vikuu vya elimu. Shule zilizidididimia na ujinga ukastawi. [GC 83.1; PK Aya ya 10]

Papa alikuwa amewatunukia watawa mamlaka au idhini ya kusikia na kupokea maungamo ya watu na kutoa msamaha wa dhambi. Jambo hili likawa chanzo cha maovu makuu. Wakiwa wamejielekeza katika kunufaika wao, watawa hawa waliokula kiapo cha kuwa masikini 'friars' walikuwa tayari kabisa kutoa msamaha wa dhambi kwa wahalifu wote wa kila namna waliokuja kwao, na matokeo yake yalikuwa ni uovu mwingi kuongezeka katika jamii kwa haraka. Wagonjwa na maskini waliachwa wakiteseka na kuhangaika, wakati zawadi au sadaka ambazo zilipaswa kuwapunguzia shida zao kama wahitaji zilipelekwa kwa watawa ambao kwa kutumia vitisho walidai wapewe misaada au sadaka zilizotolewa na watu, wakiwashutumu kwa kukosa ucha-Mungu na kuwashambulia wale walioshindwa kufuata maelekezo ya kuchangia sadaka kwenye mifumo (vyama) yao. Licha ya madai ya watawa hawa ya kula kiapo cha kuwa masikini, utajiri wao ulikuwa ukiendelea kuongezeka kila wakati, na majengo yao makubwa ya kifahari pamoja na meza za zilizojaa vyakula vya anasa, vilifilisi waziwazi taifa lao na kuongeza umasikini. Na wakati walipokuwa wakiutumia muda wao katika anasa na kujifurahisha na starehe zao, waliwatuma watu kwa niaba yao wasiojua kitu au waliokuwa wajinga, ambao waliishia tu kusimulia hadithi, hekaya za jadi zinazofurahisha, na kufanya mizaha ili watu wacheke na kutekewa na hivyo kuwa watulivu, basi watu hawa wakafanywa waonekane kama mabaradhuli wa watawa wale. Licha ya haya yote, watawa hawa walidumu kuyashikilia makutano haya makubwa yaliyojawa na ushirikina na kuwafanya wasadiki kwamba wajibu wao wote wa kidini ulikuwa katika kuukiri ukuu wa papa, kuabudu na kushabikia watakatifu waliokufa, pamoja na kutoa zawadi/sadaka kwa 'watawa ombaomba', na kwamba jambo hilo lilitosha kabisa kuwaandalia makazi kule juu mbinguni. [GC 83.2; PK Aya ya 11]

Watu waliokuwa wasomi na wacha Mungu walikuwa wamefanya kazi bila mafanikio katika kuleta matengenezo kwenye vyama hivi vya kitawa; lakini Wycliffe alikuwa amevuviwa na mtazamo ulio wazi na safi zaidi, yeye alishambulia kwenye mizizi ya uovu ule, akitangaza kwamba mfumo wote ulikuwa ni wa uongo (feki) na ya kwamba unapaswa kupigwa marufuku

(kukomeshwa). Mijadala na maswali yalizuka. Wakati watawa walipokuwa wakizunguka huku na kule katika nchi, wakiuza msamaha wa papa, watu wengi waliongozwa kutilia shaka uwezekano wa kununua msamaha kwa fedha, nao walijihoji wenyewe kwanini haiwapasi kutafuta msamaha kutoka kwa Mungu badala ya kutoka kwa papa wa Rumi *(Tazama Kiambatanisho cha Sura ya 3 Aya ya 28, 29 na 30).* Sio wachache walioshtuka kuiona tamaa hii kubwa ya fedha waliyokuwa nayo watawa juu ya mali ambao uchu wao ulionekana kana kwamba hauwezi kutoshelezwa. Nao wakatamka kwa kusema "Watawa na mapadri wa Rumi wanatutafuna kama saratani (kansa). Mungu ni sharti atuokoe la sivyo sisi walei tutaangamia" D'Aubigne,b.17, ch.17. Ili kuficha tamaa yao ya mali, watawa wale ombaomba walidai kwamba walikuwa wakifuata kielelezo cha Mwokozi, nao wakatangaza kwamba Yesu na wanafunzi Wake walikuwa walitegemezwa na misaada ya watu. Madai haya yalipelekea madhara katika kazi yao, kwani yaliwafanya wengi kuelekezwa katika Biblia ili kujifunza Ukweli --- Jambo ambalo halikupendwa sana na Rumi. Akili za watu zilielekezwa kwenye kile Chanzo cha Ukweli, jambo ambalo Rumi ilitaka lifichwe. [GC 84.1; PK Aya ya 12]

Wycliffe alianza kuandika na kuchapa vijuzuu ili kuyapinga madai ya watawa wa chama cha 'ombaomba', nia yake haikuwa kutafuta kuingia katika malumbano nao, bali kuyaelekeza mawazo ya watu katika mafundisho ya Biblia na Mtunzi Wake. Alitangaza kwamba mamlaka hiyo ya kutoa msamaha au kumtenga mtu ushirika na kanisa inayomilikiwa na papa haina kiwango chochote cha juu kuliko ile inayomilikiwa na mapadri wa kawaida na kwamba hakuna mtu anayeweza kutengwa usharika wake kiuhalisia isipokuwa yeye mwenyewe amejiletea hukumu (laana) ya Mungu juu yake. Hakuna njia yoyote iliyo na mafanikio ambayo Wycliffe angeweza kuichukua ili kuliangusha lile vazi kubwa la utawala ule wa kiroho na wa kiraia uliowafunika watu, na ambao papa alikuwa ameujenga, na ambao ndani yake roho na miili ya mamilioni ya watu ilikuwa imeshikiliwa mateka. [GC 84.2; PK Aya ya 13]

**Mwanamatengenezo Huyo Atumwa**

Kwa mara nyingine Wycllife aliitwa kuitetea haki za taji ya ufalme wa Uingereza iliyovamiwa na ukandamizaji wa Rumi; naye akiwa ameteuliwa kuwa balozi wa mfalme, alitumia miaka miwili Uholanzi katika mikutano mbalimbali pamoja na wawakilishi wa papa. Hapa aliweza kukutana na kuwasiliana na viongozi wa dini kutoka Ufaransa, Italia na Uhispania, hapa tena alikuwa na nafasi ya kuangalia nyuma ya pazia matukio yale na kujipatia maarifa ya mambo mengi ambayo yangeendelea kufichwa kwake kama bado angekuwa katika nchi ya Uingereza. Alijifunza mengi ambayo yalimsaidia kuwa na mashiko katika kazi yake aliyoenda kuifanya katika siku za usoni. Kazi ya wawakilishi hawa kutoka katika nyua ya upapa ilimpa kitabu cha kusoma tabia halisi na malengo ya

utawala ule wa kipapa (hierakia) na mfumo wake kwa jumla. Alirejea nchini kwake Uingereza na kurudia mafunzo yake ya awali kwa uwazi zaidi na kwa bidii/usongo mwingi zaidi na akatangaza kuwa tamaa ya mali, choyo, kiburi na udanganyifu vilikuwa miungu ya Rumi. [GC 84.3; PK Aya ya 14]

Akizungumza juu ya papa na wakusanya ushuru wake katika mojawapo ya ya vitini vyake, alisema "Wanachotaka kutoka katika nchi yetu ni vipato/riziki vya watu masikini na maelfu mengi ya fedha za Kijerumani (deutschemark) kila mwaka kutoka katika hazina ya fedha za mfalme wetu, na kutumia kwa ajili ya sakramenti na mambo ya kiroho, huo ni uzushi wa mafundisho ya uongo, yaletayo laana na kupora watu kwa kufanya biashara ya kuuza mambo matakatifu ya dini (waliuza msamaha wa dhambi) kwa jinsi hii, na kuulazimisha ulimwengu wote wa Kikristo ukubaliane na kudumisha uzushi huu. Na kwa hakika ingawa ufalme wetu ulikuwa na kilima kikubwa cha dhahabu na hakika hakuna mtu mwingine aliyekichukua kilima hicho popote isipokuwa yule mkusanyaji wa ushuru wa kasisi aliyejaa udunia na majivuno mengi (papa), kwa mchakato huo kilima hiki chote kimekwisha, kwani yeye huchukua pesa kila wakati kutoka katika nchi yetu na kuitoa nje bila kurudisha chochote kwetu isipokuwa laana ya Mungu itokanayo na hali ya biashara yake ya ununuzi au uuzaji wa misamaha ya dhambi au rushwa ya kanisa." John Lewis, History of life and sufferings of J. Wycliffe, ukurasa 37. [GC 85.1; PK Aya ya 15]

Muda mfupi baada ya kurejea kwake Uingereza, Wycliffe aliteuliwa na Mfalme kuwa paroko wa chuo cha Lutterworth ambacho kilimilikiwa na kanisa la Uingereza. Huo ulikuwa ni uthibitisho kwamba mfalme hakuchukizwa na kusema kwake waziwazi mambo bila kuficha (kutoboa siri). Ushawishi wa Wycliffe ulionekana katika muundo mzuri wa utendaji wa mahakama, hata kurekebisha imani na itikadi ya taifa zima. [GC 85.2; PK Aya ya 16]

Punde si punde radi za papa zikamngurumia kwa nguvu dhidhi yake. Barua tatu za papa (bulla) zikapelekwa katika nchi ile ya Uingereza, - -kwenda kwenye chuo kikuu, kwa mfalme na kwa maaskofu-- zote zilikuwa zikiwaamuru kuchukua hatua za haraka na za mwisho zenye makusudio ya kumnyamazisha mwalimu wa uongo. (Augusts Neande, General History of the Christian Religion and Church, period 6, sec.2, pt.1, par.8. *(Tazama pia Kiambatanisho).* Kabla ya kuwasili kwa hati zile za papa, maaskofu kwa ari yao walikuwa wamemwita Wycliffe mbele yao kwa ajili ya mashtaka, lakini watu wawili wenye mamlaka na cheo katika ufalme waliongozana naye kwenda katika lile baraza la hukumu, kisha watu wakalizingira jengo na kukimbia kuingia ndani, majaji walishikwa na hofu kiasi kwamba hukumu iliahirishwa kwa muda fulani, na hivyo aliruhusiwa kuondoka zake kwa amani. Baadaye kidogo Mfalme Edward III, ambaye katika siku za awali alitumiwa na makasisi dhidi ya Mwanamatengenezo alifariki, hatimaye yule

mtetezi, na mlinzi wa zamani wa Wycliffe akawa mrithi wa ufalme. [GC 85.3; PK Aya ya 16]

Lakini kule kuwasili kwa hati zenye amri ya papa kuliiweka nchi yote ya Uingereza katika amri kali ya dharura na isiyopingwa, kwamba 'mzushi' huyu apate kukamatwa na kufungwa gerezani. Hatua hizi zilielekeza moja kwa moja katika kifo cha kwenye nguzo ile ya kuchomea watu moto. Ilionekana hakika, ndani ya muda mfupi, Wycliffe sharti aanguke kwani alikuwa ni windo la kisasi cha Rumi. Lakini Yeye aliyetangaza kwa mtu mmoja wa zamani na kumwambia, "Usiogope, Mimi ni ngao yako" "(Mwanzo 15:1), Akaunyoosha mkono Wake tena ili kumlinda huyu mtumishi Wake. Mauti ikaja lakini haikuwa ya Mwanamatengenezo bali papa aliyekuwa ametoa amri ile ya kuangamizwa kwake Wycliffe. Papa Gregory wa XI akafa na wale makasisi walioongoza kanisa, waliokuwa wamekusanyika kwa ajili ya kumshtaki na kumhukumu Wycliffe walisambaratika. [GC 86.1; PK Aya ya 17]

Uongozi wa Mungu bado ukaendelea kubatilisha matuko mengi, ili kutoa fursa ya kukua kwa kazi ya matengenezo. Kifo cha Gregory kilifuatiwa na uchaguzi wa mapapa wawili waliokuwa hawapatani na hivyo wakashindana. Watawala hawa wawili walilumbana, kila mmoja akidai kuwa hana dhambi, yaani hawezi kukosea kamwe na kudai kwamba watu wamtii na kumheshimu. (Tazama Kiambatisho ukurasa 50 na 85.) Kila mmoja aliwataka wale walio waaminifu kwake kumsaidia afanye vita juu ya upande ule mwingine wa mpinzani wake (papa mwingine) na huku akishinikiza nguvu madai yake kwa kuwatishia kutamka laana za kuogofya mno dhidi ya maadui zake, na kutoa ahadi ya zawadi za mbinguni kwa wafuasi wake wanaomwunga mkono. Tukio lile likayadhoofisha sana mamlaka ya upapa. Kambi hizi mbili za upinzani zilikuwa na mambo tosha kushambuliana wao kwa wao wenyewe, na yote ambayo wangeweza kuyafanya katika kushambuliana, na ndivyo Wycliffe alivyopata afueni kwa mapumziko. Maapizo ya laana, vurugu, kulaumiana na mashambulizi yaliruka kutoka kwa papa mmoja kwenda kwa papa mwingine, na mito ya damu za watu ikabubujika kwa ajili ya kuunga mkono madai yao yanayopingana. Uhalifu na kashfa vikaligharikisha kanisa ndani. Wakati ule Mwanamatengenezo huyu, alikuwa katika mapumziko yake kwa muda mrefu kwenye parokia yake ya Lutterworth, naye aliendelea kufanya kazi yake kwa bidii na utulivu ili kuwaelekeza wanadamu kutoka kwa mapapa waliokuwa wakipigana na kwenda kwa Yesu, Mfalme wa Amani. [GC 86.2; PK Aya ya 18]

Mgawanyiko ule pamoja na vita hii yote na ufisadi uliokuwa umesababishwa nao, uliandaa njia ya Matengenezo ya kanisa kwa kuwawezesha watu kujionea wenyewe uhalisia wa upapa. Katika Kipeperushi ambacho alikichapisha chenye kichwa kinachosema, On the Schism of the popes (Kuhusu Mfarakano wa Mapapa), Wycliffe aliwaalika watu kufikiria kwa makini sana ikiwa mapapa wale wawili walikuwa hawasemi ukweli katika kutupiana maneno ya laana wao kwa

wao kwa kusemana kwamba mwenzake ni mpinga Kristo. Alisema “Mungu asingeweza kuendelea tena kumruhusu pepo huyo au Shetani huyo kutawala ndani ya kasisi (papa) mmoja tu kama huyo, bali ... amefanya mfarakano uwepo kati ya hao wawili, ili wanadamu katika Jina Lake Yesu Kristo, waweze kuwashinda wote wawili kwa urahisi.” “R. Vaughan, Life and opinions of John Wycliffe, vol. 2, p. 6 [GC 86.3; PK Aya ya 19]

Wycliffe alihubiri injili kwa maskini, kama alivyofanya Bwana Wake. Akiwa hajaridhika na kule kuieneza nuru katika nyumba zao za kimaskini katika parokia yake ya Lutterworth, aliazimu kwamba injili ingepaswa kupelekwa katika kila sehemu ya nchi ya Uingereza. Ili kutekeleza jambo hili alifanya mpango wa kuunda kikundi cha wahubiri, watu sahili tu, wanyenyekevu, wacha Mungu, waliojitoa, walioipenda ile Kweli na ambao hawakutaka kitu kingine chochote zaidi ya kuisambaza nuru. Watu wale walienda kila mahali na kufundisha, katika maeneo ya sokoni, mitaani, katika miji mikuu, na katika vichochoro vilivyokuwa kule mashambani. Waliwatafuta wazee, wagonjwa, na maskini, na kuwafunulia habari njema za neema Yake Mungu. [GC 87.1; PK Aya ya 20]

**Apatwa Na Ugonjwa Wa Hatari**

Akiwa profesa wa theolojia huko Oxford, Wycliffe alihubiri Neno la Mungu pale, katika ukumbi wa chuo kikuu. Kwa uaminifu kabisa aliwasilisha Ukweli kwa wanafunzi ambao walikuwa chini ya mafunzo yake. Hata akapokea jina la “Daktari wa Injili.” Lakini kazi kubwa kuliko zote maishani mwake ambayo angeifanya ilikuwa ni ile ya kuyatafsiri Maandiko katika lugha ya Kiingereza. Katika kazi iitwayo, On the truth and Meaning of Scripture (kitabu kiitwacho-Kuhusu Ukweli na Maana ya Maandiko), Alielezea nia yake ya kuitafsiri Biblia- ili kusudi kila mtu katika nchi ile ya Uingereza apate kusoma matendo makuu na ya ajabu ya Mungu katika lugha yake ya kuzaliwa (lugha ya mama). [GC 87.2; PK Aya ya 21]

Lakini kwa ghafla kazi yake ilikatizwa. Ingawa alikuwa bado hajafikisha umri wa miaka sitini, kwani kule kufanya kazi ngumu bila kukoma, kujifunza, kusoma na kushambuliwa na maadui zake, kulimchosha na kumpunguzia nguvu zake na kumzeesha mapema kabla ya wakati wake. Alishambuliwa na ugonjwa wa hatari. Habari hizo ziliwafanya wale watawa waliokuwa omba omba washangilie. Basi, hawa walidhani ya kwamba yeye atajuta sana, na kutubia uovu wake aliokuwa amelifanyia kanisa (la Rumi), nao wakaharakisha kwenda kwenye chumbani mwake kusikiliza jinsi anavyoungama dhambi yake. Wawakilishi kutoka katika vyama vinne vya watawa wa kidini pamoja na maafisa wanne wa serikali ya kiraia walikusanyika kwa mtu aliyedhaniwa kwamba anakufa na kusema “kifo kimo kinywani mwako, hebu na uguswe na makosa yako, na kukanusha mbele yetu yote uliyosema ili kutujeruhi sisi.” Yule Mwanamatengenezo aliwasikiliza

akiwa kimya; Kisha akamwambia mhudumu wake amwinue kitandani mwake, naye, akiwa amewakodolea macho bila kuyapepesa walipokuwa wamesimama na kungojea ili apate kuikana imani yake, alisema kwa sauti imara, yenye nguvu, ambayo mara nyingi ilikuwa imewasababisha watetemeke: “Sitakufa, bali nitaishi; na nitayatangaza tena matendo maovu ya watawa.” -D`Aubigne, b. 17, sura ya 7. Wakiwa wamepigwa na butwaa na kuaibishwa vibaya, watawa hawa walitimua mbio, ili kuharakisha kutoka ndani ya chumba kile. [GC 87.3; PK Aya ya 22]

Maneno ya Wyclife yalitimizwa. Aliendelea kuishi mpaka alipoweka mikononi mwa raia wa nchi yake silaha yenye nguvu kuliko silaha zote dhidi ya Rumi---yaani aliwapa Biblia, wakala aliyeteuliwa na mbingu ili kuwaweka watu huru, kuwaangazia nuru na kuwapa watu injili. Vilikuwako vikwazo vingi na vikubwa vya kuvishinda katika kuifanikisha kazi hii. Wycliffe (Wiklifu) alilemewa na maradhi mengi; alijua kwamba alikuwa amebakiwa na miaka michache tu ya kazi; aliziona changamoto za upinzani ambazo alikuwa hana budi kupambana nazo; lakini, yeye alikuwa alijipa moyo kwa ahadi zilizomo katika Neno la Mungu, naye akasonga mbele bila hofu ya kitu chochote. Akiwa na nguvu kamili kiakili, na uzoefu mwingi, alikuwa amelindwa, amehifadhiwa na kutayarishwa kwa uongozi wa majaliwa ya pekee ya Mwenyezi Mungu kwa ajili hii kazi, yaani, kazi yake kuu kuliko zote alizowahi kufanya. Wakati Ulimwengu wote wa Kikristo ulikuwa umejazwa na machafuko na ghasia, Mwanamatengenezo huyu alikuwa katika kazi yake ya ukasisi kwenye parokia ya Lutterworth, bila kutilia maanani dhoruba ile iliyokuwa ikiendelea kuvuma huko nje, alitumia nguvu zake zote kufanya kazi yake aliyokuwa amechaguliwa kuifanya. [GC 88.1; PK Aya ya 23]

Hatimaye kazi ikakamilika—tafsiri ya kwanza kabisa ya Biblia kwa lugha ya Kiingereza ilikuwa imekamilika. Neno la Mungu likawa limefunguliwa wazi katika nchi ya Uingereza. Mwanamatengenezo huyu sasa hakuogopa gereza wala nguzo ya kuchomea watu moto, alikuwa ameweka mikononi mwa watu wa Uingereza nuru ambayo isingeweza kuzimwa kamwe. Kwa kuwapatia Biblia raia wenzake, alikuwa amefanya mengi zaidi katika kuzivunjilia mbali zile pingu za ujinga, madanganyo na uovu, hakika, alikuwa amefanya mengi zaidi katika kuikomboa na kuiinua nchi yake kuliko mafanikio yoyote yaliyowahi kupatikana kwa ushindi mahiri wa akili katika kwenye viwanja ya vita. [GC 88.2; PK Aya ya 24]

Sanaa ya uchapaji wa vitabu ilikuwa bado haijajulikana, hivyo kulikuwa na ugumu katika uzalishaji wa nakala za Biblia, hakika kazi hiyo ilikuwa yenye kuchosha, na inayoenda taratibu tu. Hamu ya kukipata hiki Kitabu Kikuu ilikuwa kubwa mno hivi kwamba watu wengi walishiriki kufanya kazi ya kunakili Neno kwa mikono yao wenyewe na kwa hiari moyo, lakini kulikuwa bado na ugumu mkubwa kwa wale waliolinakili katika kutosheleza mahitaji ya kila mmoja. Baadhi ya wanunuzi waliokuwa matajiri walitamani kujipatia angalau nakala

moja yenye vitabu vyote vya Biblia. Wengine walinunua sehemu tu. Pahali pengi familia kadhaa ziliungana ili kuweza kununua Biblia moja. Ni kwa njia hiyo ndiyo nakala za Biblia ya Wycliffe zilivyoweza kupata njia ya kufika majumbani mwa watu. [GC 88.3; PK Aya ya 25]

Kule kuwasihi watu kutumia busara au fikra zao kukawa kumeamsha watu kutoka katika hali yao ya kuyatii mafundisho ya kipapa bila kufanya chochote kama vile kuwauliza maswali. Basi, Wycliffe sasa akafundisha Mafundisho Makuu na bainishi ya dini ya Uprotestanti (ambayo yalikuwa tofauti- doctrines) - wokovu kwa njia ya imani katika Kristo, na kwamba Maandiko pekee ndiyo hayawezi kukosea kamwe. Wahubiri aliokuwa amewatuma nje waliisambaza Biblia pamoja na maandishi yake mwenyewe Mwanamatengenezo, kazi hii ilifanywa kwa mafanikio makubwa yaliyoifanya Imani hii mpya kupokelewa na karibu nusu ya watu wa nchi ya Uingereza. (palikuwa na nafasi kwa kipindi fulani ya kulieneza Neno la Mungu). [GC 89.1; PK Aya ya 26]

Kuonekana kwa Maandiko (Biblia) kulileta mshtuko wa hofu kwa mamlaka ya kanisa la Rumi. Sasa ilibidi wakutane na wakala mwenye nguvu kuliko Wycliffe—yaani wakala ambaye silaha zao dhidhi yake zisingefua dafu hata kidogo. Wakati ule hapakuwa na sheria huko Uingereza iliyoipiga marufuku Biblia kwani ilikuwa haijawahi kuchapishwa kamwe kwa lugha ya watu wa nchi hiyo. Sheria kama hizo baadaye zilitungwa na kutekelezwa kwa ukali na nguvu. Wakati huo licha ya juhudi za makasisi kupinga kulikuwa na msimu fulani wa fursa ya kulisambaza Neno hilo la Mungu.T [GC 89.2; PK Aya ya 27]

**Wycliffe Apelekewa Hati Ya Kuitwa Kesini**

Kwa mara nyingine viongozi wa upapa wakala njama kunyamazisha sauti ya Mwanamatengenezo yule. Aliitwa mbele ya mabaraza (mahakama) matatu ya hukumu kwa mfululizo ili kujibu mashtaka, lakini bila mafanikio yoyote. Kwanza Sinodi ya maaskofu iliyatangaza Maandiko yake kuwa ni uzushi na wakafanikiwa kumshawishi mfalme kijana Richard II, kuwa upande wao, kisha wakapata amri ya mfalme iliyoamuru kuwapeleka gerezani wale wote ambao wangeendelea kuyashikilia mafundisho yale waliyoyalaani kwa kuyapiga marufuku. [GC 89.3; PK Aya ya 28]

Wycliffe akakata rufaa kutoka kwa kamati/sinodi ile kwenda Bungeni, bila woga kwa kuushtaki mfumo ule wa uongozi wa kanisa wa hierakia mbele ya baraza la kitaifa na kudai matengenezo yafanywe kuhusu desturi nyingi za unyanyasaji mkubwa zilizoidhinishwa na kanisa (la Rumi). Kwa uwezo ulio na mashiko na unaoweza kuwashawishi watu, alionyesha mamlaka hiyo livyojinyakulia mamlaka isivyo halali na ufisadi wa serikali ya upapa inayojiita see (angalia kwenye google ‘holy see’ au sancta sedes).* Maadui zake

wakachanganyikiwa vibaya. Marafiki na wafuasi wa Wycliffe walikuwa wamelazimishwa kuitii ile amri, tena waliamini na kutarajia kwamba Mwanamatengenezo mwenyewe katika uzee wake, akiwa katika upweke, na bila rafiki, basi angelisalimu amri kwa mamlaka ile ya muungano wa kofia ya kifalme na ile ya kiaskofu. Lakini badala yake wafuasi wa upapa walijikuta wameshindwa. Bunge, likiwa limezinduka na miito iliyowasisimua kutoka kwa Wycliffe, likasitisha ile amri ya mateho, na Mwanamatengenezo huyu akaachiwa huru tena. [GC 89.4; PK Aya ya 29]

Kwa mara yake ya tatu aliletwa mbele ya mahakama tena kuhojiwa, kwa wakati ule, hilo lilikuwa baraza la juu kabisa la kanisa katika ufalme huo. Katika baraza lile hakuna upendeleo au huruma yoyote ambayo ingeweza kuonyeshwa kwa uzushi. Mle ndiyo hatimaye Rumi ingeshinda, na kazi ya Mwanamatengenezo huyu ingekomeshwa. Hivyo ndivyo walivyodhani viongozi na wafuasi wa upapa. Endapo wangeweza tu kutimiza kusudi lao, basi, Wycliffe angelazimishwa kuyakana mafundisho yake, au angetoka mbele ya baraza lile na kwenda kuchomwa moto tu. [GC 90.1; PK Aya ya 30]

**Wyclife Akataa Katakata Kuikana Imani Yake**

Lakini Wycliffe hakukana imani yake; hakutaka kuificha nia yake. Bila hofu yoyote aliyatetea mafundisho yake na kuyapinga mashtaka ya watesi wake. Akijisahau nafsi yake mwenyewe, cheo chake, na tukio lile lenyewe, aliwaita wasikilizaji wake kufika mbele ya mahakama ya Bwana, kuyapima maneno yao ya uongo na udanganyifu katika mizani ya Ukweli wa milele. Nguvu ya Roho Mtakatifu ilidhihirika katika chumba cha baraza. Uwepo wa Mungu ulikuwa juu ya wasikilizaji wale. Walionekana kana kwamba hawana nguvu yoyote ya kuondoka mahali pale. Kama mishale toka katika podo la Bwana, ndivyo maneno ya Mwanamatengenezo yule yalivyoichoma mioyo yao. Shitaka la uzushi walilokuwa wamelileta dhidi yake, kwa uwezo ule unaogusa na kusadikisha moyo, yeye aliwatupia wao wenyewe. Kwanini, akataka kujua, walithubutu kueneza mafundisho yao ya uongo? Je, ni kwa ajili ya kujipatia faida, yaani, kufanya biashara ya neema ya Mungu? [GC 90.2; PK Aya ya 31]

Mwishowe aliwaambia “Hivi ninyi Mnafikiri mnashindana na nani? Je, mnapambana na mtu yule aliye kizee anayekaribia kuingia kaburini? Hapana! Ninyi mnapambana na ile Kweli—kweli ile ambayo ina nguvu kuwashinda ninyi, nayo itawashinda.” - Wylie, kitabu cha 2, sura ya 13. Akisha kusema hayo, akatoka mbele ya ule mkutano, na wala hakuna hata mmoja miongoni mwa wale maadui zake aliyejaribu kumzuia. -Wylie, b. 2, sura ya 13. [GC 90.3; PK Aya ya 32]

Kazi ya Wycliffe ilikuwa karibu kumalizika; bendera ya Ukweli ambayo alikuwa ameibeba kwa muda mrefu ilikuwa inakaribia sana kudondoka kutoka katika

mkono wake; lakini kwa mara nyingine tena alipaswa kushuhudia Injili. Kweli ile ilipaswa kutangazwa kuanzia katika ngome halisi ya ufalme ule wa uongo/makosa (yaani, toka Rumi kwenyewe). Wycliffe aliitwa kwa mashitaka mbele ya mahakama ya papa kule Rumi, ambayo mara nyingi ilikuwa imemwaga damu ya watakatifu (Ufu. 17:6). Yeye hakuwa kipofu kwa ile hatari iliyomtishia, hata hivyo angekuwa ameitii amri hiyo ya kwenda barazani kama shambulio lile kali la mshtuko wa kupooza/kiharusi lisingefanya iwe vigumu kwake kufanya safari hiyo. Lakini ijapokuwa sauti yake ilikuwa haiwezi kusikika kule mjini Rumi, aliweza kuzungumza kwa njia ya barua, na jambo hilo alidhamiria kulifanya. Kutoka katika parokia yake, Mwanamatengenezo huyu alimwandikia papa barua, ambayo, ingawa ilikuwa ladha ya heshima kwa maneno yake na roho ya Kikristo, ilikemea vikali na kwa umakini fahari na kiburi cha taasisi au serikali ile ya see ya upapa **(Jimbo la Papa linaitwa 'holy see' au 'Kiti kitakatifu' au kilatini 'Sancta Sedes')*. [GC 90.4; PK Aya ya 33]

"Hakika nina furaha," akasema, "kumfunulia na kumtangazia kila mtu imani ile niliyo nayo, na hususani kwa askofu wa Rumi: imani ambayo, kwa kadiri mimi ninavyoamini ni sahihi na ya Kweli, naye atakuwa tayari kabisa kuithibitisha imani yangu hiyo niliyoitaja, la kama ina makosa, aifanyie marekebisho ili iwe bora. [GC 91.1; PK Aya ya 34]

"Kwanza, mimi nadhani kwamba Injili Yake Kristo ndio mwili yaani kiini cha Sheria Yake yote Mungu.... Mimi namwajibisha askofu wa Rumi kama mwakalishi wa Mungu hapa duniani, kwamba yeye amefungwa kabisa na sheria hiyo ya Injili kuliko wanadamu wengine wote, kwa kuwa yeye ni badala ya Kristo hapa duniani. Kwa maana ule ukubwa miongoni mwa wanafunzi wa Kristo haukutokana kwa hadhi kubwa ya ulimwengu huu au katika kujikweza na heshima zake, bali katika ukaribu na usahihi wa kumfuata Kristo katika maisha Yake na mwenendo (tabia) Wake.... Kristo, katika kipindi cha safari Yake humu duniani, alikuwa ni mtu maskini (hohehahe), alikubali kujishusha na kuwa mtu aliye duni, akikataa utawala wote wa dunia hii pamoja na heshima na utukufu wake.....[GC 91.2; PK Aya ya 35]

### Usalama Peke Yake Ni Kumfuata Kristo

"Hakuna mtu mwaminifu anayepaswa kumfuata papa mwenyewe au mtu yeyote miongoni mwa watu wale walio watakatifu (ambao walikufa zamani), isipokuwa tu wale ambao katika mambo yote wamemfuata Bwana Yesu Kristo; kwa maana Petro na wana wa Zebedayo, wakiwa wanatamani heshima ya kidunia, kinyume na kuzifuata nyayo Zake Kristo, walifanya kosa, na kwa hiyo kwa makosa hayo hawapaswi kufuatwa.... [GC 91.3; PK Aya ya 36]

“Papa anapaswa kuachana na mamlaka ya serikali za dunia hii na himaya na utawala wote kilimwengu (usio wa kiroho au kidini), na katika mambo hayo kuwashawishi na kuwapa ujasiri kwa kuwatia moyo na kuwasaidia kwa ufanisi makasisi wake wote kusonga mbele katika njia hiyo njema; kwa kuwa hivyo ndivyo alivyofanya Kristo, na Mitume Wake. Kwa sababu hiyo, kama nimekosa katika kipengele chochote katika hoja hizo, najisalimisha kwa unyenyekevu kabisa na kukubali kusahihishwa/kukosolewa, hata ikibidi kwa kufa ikiwa itanilazimu kufanya hivyo: na kama itahitajika mambo yawe hivyo; na kama mimi ningeweza kufanya kazi kulingana na mapenzi yangu au matamanio yangu katika utu wangu binafsi, kwa hakika ningeweza kujitokeza mbele ya askofu wa Rumi, lakini kinyume chake Bwana ameongea nami kwa njia nyingine, Naye amenifundisha kumtii Mungu kuliko wanadamu.” [GC 91.4; PK Aya ya 37]

Kwa kuhitimisha aliweza kusema hivi: “Hebu na tumwombe Mungu wetu kwamba atamshtua Papa wetu Urbano wa VI kama alivyoanza, ili yeye pamoja na makasisi wake wapate kumfuata Bwana Yesu Kristo katika maisha yao na mwenendo wao; na ya kwamba wapate kuwafundisha watu ipasavyo, na wao vile vile wapate kuwafuata katika mambo yayo hayo.” John Foxe Acts and Monuments,Vol.3, pp.49, 50. [GC 92.1; PK Aya ya 38]

Hivyo ndivyo Wycliffe alivyoonyesha kwa papa na makadinali wake ule upole na unyenyekevu wa moyo aliokuwa nao Kristo, akidhihirisha si kwao tu, bali na kwa Ulimwengu wote wa Kikristo tofauti iliyopo kati yao na Bwana wao ambaye wao walijidai kuwa ni wawakilishi Wake. [GC 92.3; PK Aya ya 39]

Wycliffe alitarajia kabisa kwamba maisha yake yangekuwa ndiyo gharama ya uadilifu na msimamo wake. Mfalme, papa, pamoja na maaskofu waliungana pamoja ili kufanikisha maangamizi yake, tena ilionekana kana kwamba ilikuwa ni dhahiri kwamba miezi michache ijayo ingemfikisha kwenye nguzo ya kuchomea watu moto. Lakini ule ujasiri wake ulikuwa haujatikiswa. Alisema “Kwa nini ninyi mnazungumza juu ya kuitafuta mbali sana taji ile ya mfia dini? Hubirini Injili Yake Kristo kwa maaskofu hao wenye majivuno makubwa, nanyi hamtakosa kupata hicho kifo cha mfia dini. Mnasema nini! Mimi niishi na kukaa kimya?... Kamwe! Hebu pigo na liniangukie basi, nangojea linijie”-D’Aubigne, b.17,sura ya 8. [GC 92.4; PK Aya ya 40]

Lakini majaliwa ya Mungu bado yaliendelea kumlinda mtumishi Wake. Mtu yule ambaye katika maisha yake yote alisimama kwa ujasiri kuitetea ile Kweli, kila siku akiwa katika hatari ya kupoteza maisha yake, hakupaswa kuanguka kama mhanga wa chuki za maadui zake. Wycliffe hakuwahi kamwe kutafuta namna ya kujihami au kujilinda yeye mwenyewe, ila Bwana alikuwa Ndiye mlinzi wake; na hata pale maadui zake walipojisikia kwamba wanayo hakika ya kupata mawindo yao, mkono Wake Mungu ulimwondolea mbali mahali ambapo wao wasingeweza kupafikia. Katika kanisa lake pale Lutterworth, alipokuwa anataka

kuendesha Huduma ya Meza ya Bwana (Ushirika Mtakatifu au Komunio), alianguka chini, naye akawa amepooza (kiharusi), na baada ya muda alisalimisha maisha yake kwa kifo. [GC 92.4; PK Aya ya 41]

Mungu alikuwa amemteua Wycliffe kwa ajili ya kazi yake. Alikuwa ameliweka Neno Lake la Kweli katika kinywa chake na kuweka ulinzi kumzunguka ili Neno Lake lipate kuwafikia watu. Maisha yake yalilindwa, na kazi zake zikarefushwa mpaka hapo msingi wa kazi ile kubwa ya Matengenezo ya Kanisa ulipokuwa umewekwa. [GC 92.5; PK Aya ya 42]

Wycliffe aliibuka katika utusitusi wa Zama zile za Giza. Hapakuwa na watu wowote waliomtangulia ambao kutokana na kazi zao, yeye angeweza kujenga mfumo wake wa matengenezo ya kanisa. Akiwa amelelewa na kuinuliwa kama yule Yohana Mbatizaji ili apate kufanya kazi mahsusi ya utume, alikuwa ni mjumbe na mpiga mbiu wa kizazi kile kipya. Pamoja na hayo, ule mfumo wa ile Kweli aliyoihubiri kulikuwepo na umoja na ukamilifu ambao Wanamatengenezo waliomfuata baadaye hawakuweza kuupita, na ambao wengine hawakuweza kuufikia hata miaka mia moja baadaye. Msingi ulikuwa umejengwa kwa upana na kina kirefu mno, muundo ulikuwa imara na wa Kweli, hata ikawa hapana haja ya kuujenga upya tena kwa wale waliofuata baada yake. [GC 93.1; PK Aya ya 43]

**Mto Wa Mibaraka**

Harakati hii endelevu ambayo Wyclife aliizindua, ambayo ilikusudiwa kuiweka huru dhamiri na akili ya mtu, na kisha kuyakomboa mataifa yaliyokuwa yamefungwa kwa kipindi kirefu kwenye gari lile la ushindi wa Rumi, chemchemi yake ilitoka kwenye Biblia. Humo ndimo ulimotoka ule mfereji wa mibaraka, ambao, maji yake ya uzima, yamebubujika na kushuka chini na kuja kwetu hadi kwenye vizazi vyote tangu karne ya kumi na nne. Wycliffe aliyakubali Maandiko Matakatifu kwa imani isiyotikisika kama ndio ufunuo uliovuviwa wa mapenzi ya Mungu, yaani, kanuni toshelevu ya imani na utendaji. Alikuwa amelelewa katika mazingira ya kulifikiria Kanisa la Rumi kama ndiyo mamlaka ya Kimungu isiyoweza kukosea kamwe, na kuyakubali kwa kicho, bila kuyahoji mafundisho na desturi ambazo zilikuwa zimejengwa kwa miaka elfu moja; lakini aliyapa kisogo yote hayo ili kulisikiliza Neno Takatifu la Mungu. Hiyo ndiyo mamlaka aliyowasisitizia watu kuikubali. Badala ya kanisa kuzungumza kupitia kwa papa, yeye aliwatangazia ya kwamba mamlaka pekee ya Kweli ni sauti ya Mungu inayozungumza nasi kupitia katika Neno Lake. Tena hakufundisha tu kwamba Biblia ni ufunuo kamili wa mapenzi ya Mungu, bali kwamba Roho Mtakatifu Ndiye mtafsiri peke yake wa Biblia, na ya kwamba kila mtu anapaswa kujifunza mafundisho yake (hiyo Biblia), na yeye mwenyewe kujifunza humo wajibu wake umpasao. Kwa njia hiyo aligeuza bongo za watu kutoka kwa papa na Kanisa la Rumi na kuzielekeza kwenda kwenye Neno la Mungu. [GC 93.2; PK Aya ya 44]

Wycliffe alikuwa ni mmoja wa wanamatengenezo wakuu sana. Kwa upeo mpana wa akili yake, katika uwazi wa fikra zake, kwa msimamo wake katika kuudumisha Ukweli, na kwa ujasiri wake katika kuilinda ile Kweli, aliweza kulinganishwa na wachache mno waliofuata baada yake. Usafi wa maisha yake, bidii yake isiyojua kuchoka katika kujifunza na kutenda kazi yake, uadilifu usiochafuliwa, msimamo wake thabiti usio na ufisadi, na upendo wake unaofanana na ule wa Kristo, pamoja na uaminifu wake katika kutoa huduma yake, vilikuwa ndiyo sifa za mwanamatengenezo huyu wa kwanza (morning star reformer). Na haya yote yaliwezekana licha ya kuwapo giza la kiakili/kielimu na ufisadi wa kimaadili, katika zama au kizazi kile alichoibuka. [GC 94.1; PK Aya ya 45]

Tabia ya Wycliffe ni ushuhuda wa nguvu za Maandiko Matakatifu yanayoielimisha, na kuibadilisha tabia. Biblia ndiyo iliyomfanya kuwa kama vile alivyokuwa. Juhudi za kutaka kuzishikilia zile Kweli kuu za mafunuo ya Mungu huvipa upya na nguvu vitivo vingine vyote. Biblia Huipanua akili, na kunoa uwezo wa ufahamu wa kupambanua mambo, na kuukomaza uwezo wa maamuzi ya mambo. Kujifunza Biblia kutaiadilisha kila fikra, hisia, na matamanio yoyote kuifikia hali ya juu katika mambo ya kiroho kuliko somo jingine lolote liwezavyo kufanya. Biblia inatoa imara wa nia/mapenzi ya mtu, ustahimilivu ujasiri, na ushupavu; inaboresha na inalainisha tabia na kuitakasa nafsi. Kujifunza Maandiko kwa dhati na kicho, ambako kunayaleta mawazo ya mwanafunzi mahali yanapoweza kugusana/kukutana na mawazo ya Mungu yasiyo na kikomo, kungeweza kuupatia ulimwengu huu watu wenye akili yenye nguvu na uhai na utendaji wa hali ya zaidi, wenye kanuni bora, kuliko ilivyopata kutokea kwa njia ya mafunzo yanayofaa kabisa ambayo falsafa ya kibinadamu inaweza kutoa. “Kufafanusha Maneno Yako” Anaimba Mtunzi wa Zaburi, “kwatia nuru na kumfahamisha mjinga.” Zaburi 119:130. [GC 94.2; PK Aya ya 46]

Mafundisho makuu ya imani/dini (doctrines) yaliyokuwa yamefundishwa na Wycliffe yaliendelea kuenea kwa muda mrefu; wafuasi wake, waliojulikana kama Wawiklifu (Wycliffites) na Walaladi (Lollards), sio tu kwamba walitawanyika katika nchi yote ya Uingereza tu, bali pia walienda katika nchi zingine, wakichukua maarifa ya Injili ya milele. Kwa vile sasa kiongozi wao alikuwa ameondolewa, wahubiri hawa walifanya kazi yao kwa bidii sana kuliko hapo awali, na watu wengi walimiminika ili kuyasikiliza mafundisho yao. Baadhi ya wakuu mashuhuri, waungwana na hata mke wa mfalme, wakawa miongoni mwa wale waongofu. Pahali pengi matengenezo yalionekana dhahiri katika tabia za watu, na zile viashiria/nembo za ibada ya sanamu ya Urumi zikaondolewa katika makanisa yao. Lakini mara hiyo dhoruba ya mateso isiyokuwa na huruma ikapasuka kwa mshindo juu ya wale waliothubutu kuikubali Biblia kama kiongozi wao. Wafalme wa Kiingereza, wakiwa na shauku kubwa ya kuimarisha mamlaka

yao kwa kujipatia msaada kutoka Rumi, hawakusita kuwatoa kafara Wanamatengenezo wake. Kwa mara ya kwanza katika historia ya nchi ile ya Uingereza nguzo ya kuchomea watu moto ikasimikwa kwa amri dhidi ya wafuasi wale wa injili. Mauaji ya wafia dini yakafuatiwa na mauaji mengine ya wafia dini. Watetezi wa ile Kweli waliokuwa wamepigwa marufuku na kuteswa, waliweza tu kumwaga machozi na kilio chao, ili kipate kusikiwa na sikio la Yule Bwana wa majeshi tu. (Ufu. 6:9- 11). Wakiwa wanasakwa kama maadui wa kanisa na wasaliti wa ufalme, waliendelea kuhubiri mahali kwa siri, wakipata mahali pa kujihifadhi kwa kadiri walivyoweza katika nyumba duni za maskini, na mara nyingi wakiwa wanajificha mbali, naam, katika mapango ya wanyama na mashimo kwenye milima na miamba [GC 94.3; PK Aya ya 48]

Licha ya hasira, na misukosuko ya mateso yale, ukinzani uliofanywa kwa njia kwa utulivu bila kelele kwa kujitoa kwa dhati, na uvumilivu mwingi, uliendelea kutolewa dhidi ya upotovu ule wa imani ya dini uliokuwapo kwa karne nyingi. Wakati wa kipindi kile cha awali, Wakristo wale waliokuwa na ujuzi wa Ukweli kwa sehemu tu, lakini wakiwa wamejifunza kulipenda na kulitii Neno la Mungu, tena kwa ustahimilivu, waliteswa kwa ajili Yake Bwana. (Ufu. 12:11). Kama walivyofanya wanafunzi wa siku za Mitume, wengi wao walitoa mali yao yote ya kidunia kuwa kafara kwa ajili ya kazi Yake Kristo. Wale waliSoruhusiwa kuishi katika nyumba zao, kwa furaha wakawa wanawahifadhi ndugu zao waliofukuzwa kwao, na wao pia walipofukuzwa walikubali kwa furaha kuishi maisha kama ya mtu aliyetengwa na jamii yake (maisha ya mkimbizi uhamishoni). Ni kweli kwamba maelfu, wakiwa wameingiwa na hofu kuu kutokana na ghadhabu dhidi yao waliyokuwa nayo watesi wao, walinunua uhuru wao kwa gharama ya kupoteza imani yao, kisha wakatolewa magerezani wakiwa wamevikwa mavazi ya ‘toba’ kuonesha kwamba wameikana imani yao. Walakini idadi yao haikuwa ndogo --tena miongoni mwao walikuwamo watu wa hadhi za juu wa koo za kifalme pamoja na watu wa kawaida na watu fukara - ndiyo idadi ya wale walioishuhudia ile Kweli bila hofu ndani ya seli za magereza yale yaliyo chini ya ardhi, na katika ile “Minara ya Lollards” (wafuasi wa Wycliffe), na katikati ya mateso makali na ndimi za moto, walikuwa wakifurahia kwamba walikuwa wamehesabiwa kustahili kujua maana ya “kushiriki mateso Yake (Kristo).” [GC 95.1; PK Aya ya 49]

Wafuasi wa papa walikuwa wameshindwa kutenda vile walivyotaka dhidi ya Wycliffe wakati wa uhai wake, tena ile chuki yao haikuweza kuridhishwa wakati mwili wake ulipokuwa umepumzika kwa utulivu kaburini. Kwa amri ya Baraza la Constance, lililofanyika zaidi ya miaka arobaini baada ya kifo chake, mifupa yake ilifukuliwa na kutolewa na kisha kuchomwa moto hadharani, na majivu yake yakatupwa katika kijito kilichokuwa jirani na mahali pale. Mwandishi wa zamani alisema maneno haya “Kijito hichi kimeyasafirisha majivu yake Wycliffe na

kuyapeleka katika mto Avon, na kutoka Avon hadi kuingia katika mto Severn, na Severn ukayachukua hadi katika bahari nyembamba, na kutoka kule kuingia katika bahari ile kubwa. Na kwa njia hiyo majivu ya Wycliffe ni ishara (nembo) ya mafundisho yake, ambayo hivi sasa yametawanywa na hivyo kusambaa ulimwenguni kote." -T, Fuller, Church History of Britain, b. 4, kipengele 2, aya. 54. Masikini! Wale maadui zake hawakutambua kwamba kitendo chao cha hiana kilikuwa ndiyo faida kwa mwanamatengenezo huyu na injili pia![GC 95.1; PK Aya ya 50]

Ni kwa kupitia maandishi yake Wycliffe, John Huss (Jan Hus) wa Bohemia, aliongozwa kuyakataa mafundisho mengi ya makosa/uongo ya Urumi na kuingia kuanza kazi hii ya Matengenezo ya Kanisa. Hivyo ndivyo ilivyopandwa mbegu ya Ukweli katika nchi hizo mbili zilizokuwa zimetengana kwa umbali mkubwa. Kutoka kule Bohemia kazi ile ikazidi kuenea katika nchi zingine. Mawazo ya watu yakielekezwa kwenye Neno la Mungu lililokuwa limesahauliwa kwa kipindi kirefu sana. Mkono wa Mungu ulikuwa unaiandaa njia kwa ajili ya Matengenezo Makuu ya Kanisa. [GC 96.1; PK Aya ya 51]

# SURA YA 6

# HUSS NA JEROME

**(Kukaribia kwa Mapambazuko:** Mashujaa Wawili wakabili kifo 1396-1428 BK—vita vitakatifu/vya msalaba/Crusade/Krusedi—ni kitu kimoja)

Ufupisho: Mtu ambaye hakuweza kusimamishwa na gereza au migogoro mikali. Mtu aliyetikisa Ulaya na kuleta injili safi ya Biblia miaka 100 kabla ya Martin Luther, na kuweka msingi wa Matengenezo yale makuu. Watu kadhaa walikuwa

wamezungumza kuhusu ufisadi wa kanisa kule Bohemia miaka ya 1360-1390BK. Huss alipata kazi ya Paroko mwaka 1392 Lutterworth. Baraza la Constance lilikuwa mnano Novemba 1414 mpaka Aprili 1418) nalo liliitwa na mmoja wa mapapa waliokinzana. Huss alichomwa moto 1415 na Jerome 1416, na Wahusi waliendelea vita mpaka mnamo mwaka 1438. Soma Historia!

Injili ilikuwa imeshapandwa katika nchi ya Bohemia mwanzoni mwa karne ya tisa. Biblia ilikuwa imetafsiriwa na ibada za hadhara kufanyika kwa kutumia lugha za wenyeji (lugha ya asili). Lakini kadiri nguvu ya papa ilivyozidi kuongezeka, ndivyo Neno la Mungu lilivyozidi kufichwa na kuwekewa vikwazo kwa kugubikwa mawingu. Gregory VII, ambaye, yeye mwenyewe alijichukulia jukumu la kuvishusha viburi vya wafalme, alidhamiria kuwafanya watu kuwa watumwa wake, basi wakati huo huo amri ya papa, yaani tamko rasmi (bulla-fahali) likatolewa ili kupiga marufuku kufanyika kwa ibada za hadhara kwa lugha ya Bohemia. Papa alitangaza kuwa "ilikuwa inampendeza sana Mwenyezi Mungu, kuwa ibada Yake iendeshwe kwa kutumia lugha isiyoeleweka, na kwamba maovu pamoja na uzushi mwingi vimeinuka kwa kutokuzingatia sheria hii."— Wylie, b. 3, sura ya 1. Hivyo Rumi ikatangaza amri ya nuru ya lile Neno la Mungu ipate kuzimwa kabisa, na watu walipaswa kuendelea kufungiwa gizani. Lakini mbingu ilitoa mbadala mwingine, njia kwa ajili ya kulihifadhi na kulilinda kanisa. Wawaldensia (Waldenses) na Walbigensia (Albigenses) wengi, waliofukuzwa na yale mateso waliyoyapata nyumbani kwao Ufaransa na Italia, walikuja katika nchi ya Bohemia (vipande vya Chekoslovakia/Chek, Ujerumani na Uswiz). Ingawa hawakuthubutu kufundisha hadharani, walifanya kazi kwa bidii na sirini. Hivyo ndivyo Imani hii ya Kweli ilivyohifadhiwa kutoka karne moja mpaka karne nyingine. [GC 97.1; PK Aya ya 1]

Kabla ya siku za Huss kulikuwa na watu Bohemia ambao waliinuka na kukemea ufisadi wa kanisa waziwazi, na uasherati, ubaradhifu na ukosefu wa maadili kwa jumla miongoni mwa watu. Jitihada zao zilichochea shauku kubwa iliyosambaa kwa upana. Hofu ya mamlaka ya kanisa la Rumi ya hierakia au ngazi (hierarchy) ikaongezeka, na mateso yakaanza dhidi ya wanafunzi wa injili. Wakiwa wamefukuzwa, walilazimika kuabudu misituni na milimani, waliwindwa na askari, na wengi wao waliuwawa. Baada ya muda ilitangazwa kwamba wote wale waliojitenga na ibada ya Kiroma walipaswa kuchomwa moto. Lakini wakati Wakristo wakiyatoa maisha yao, walitazamia ushindi wa kazi yao siku za usoni. Mmoja wa wale Wakristo "aliyefundisha kwamba wokovu unaweza kupatikana kwa Imani tu kupitia kwa Mwokozi aliyesulubiwa," alisema hivi alipokuwa akifa: "Hasira ya maadui wa Ukweli imetushinda kwa sasa, lakini haitakuwa hivyo milele; atainuka mtu miongoni mwa watu wa kawaida, asiye na upanga wala mamlaka, na watakapompinga mtu huyo, hawataweza kumshinda."—Ibid., b. 3, ch. 1. Wakati wa Luther ulikuwa mbali bado; lakini tayari mtu alikuwa akiinuka,

ambaye ushuhuda wake dhidi ya Rumi uliyakoroga-koroga mataifa. [GC 97.2; PK Aya ya 2]

John Huss (Jina lake kamili kwa lugha yao- Jan Hus inatamkwa Yan Hus) alizaliwa katika mazingira duni na akiwa mdogo aliachwa yatima kwa kifo cha baba yake. Mama yake mcha Mungu, alichukulia elimu na kumcha Mungu kama mali za thamani zaidi, akatafuta namna ya kuutunza urithi huu kwa ajili ya mwanae. Huss alisoma shule katika jimbo lao kisha akaenda katika chuo kikuu huko Prague, akidahiliwa kwa kufadhiliwa. Alisindikizwa na mama yake katika safari ya kuelekea Prague; mama huyu mjane na maskini, hakuwa na zawadi za utajiri wa kidunia za kumpatia mwanae, lakini walivyolikaribia jiji lile kubwa, alipiga magoti pembeni ya kijana yule asiye na baba na kumwombea mibaraka kutoka kwa Baba yao aliye mbinguni. Yule mama hakujua hata kidogo namna ambavyo ombi lake lingejibiwa. [GC 98.1; PK Aya ya 3]

Akiwa huko chuo kikuu, haikuchukua muda kwa Huss kujitofautisha na wengine kwa kuwa na bidii isiyokoma na maendeleo ya kasi, huku maisha yake yasiyo na mawaa na tabia njema ya upole, vikimsaidia kuheshimika kwa watu wote. Alikuwa muumini mwaminifu wa Kanisa la Rumi na mtafutaji thabiti wa mibaraka ya kiroho ambayo kanisa hilo lilidai kwamba linatoa kwa watu wake. Wakati wa maadhimisho ya Jubilee/Yubile, Huss alikwenda kuungama, na kisha akalipa sarafu zake chache za mwisho kutoka katika akiba yake ndogo, na kujiunga katika msafara wa maandamano ili apate kushiriki katika msamaha ulioahidiwa. Baada ya kumaliza mafunzo yake ya chuo kikuu, alijiunga katika kazi ya upadre, naye akaanza kuwa maarufu, na punde alihikamanishwa na utumishi kwenye kasiri la mfalme. Huss Alifanywa kuwa profesa na baadaye paroko katika chuo kikuu ambacho alijipatia elimu yake. Kwa miaka michache mwanafunzi huyu maskini aliyefadhiliwa katika masomo, akawa mtu mwenye kuiletea nchi yake sifa, na jina lake likajulikana Ulaya yote. [GC 98.2; PK Aya ya 4]

### Kazi Ya Matengenezo Ya Kanisa Yaanza

Lakini ilikuwa ni katika uwanja mwingine ndiyo Huss alianza kufanya matengenezo. Miaka kadhaa baada ya kupokea majukumu ya upadirisho aliteuliwa kuwa mhubiri wa kanisa dogo la Bethlehemu (chapel). Mwasisi wa kanisa hili alikuwa ameshauri watu kuzingatia kama suala la umuhimu mkubwa, kuhubiri maandiko kwa kutumia lugha ya wenyeji. Licha ya upinzani wa Rumi dhidi ya desturi hii ya kuhubiri kwa kutumia Biblia, jambo hilo halikuwa limezuiwa kabisa mahali pote katika nchi ya Bohemia. Lakini palikuwa na ujinga mkubwa wa kutokuijua Biblia, na maovu mabaya kabisa yalishamiri miongoni mwa watu wa kila tabaka. Huss aliyakemea maovu haya bila kubakiza kitu,

akilinukuu Neno la Mungu ili kuimarisha kanuni za ile Kweli na usafi wa maisha aliousisitiza. [GC 99.1; PK Aya ya 5]

Mkazi wa Prague, Jerome, ambaye hapo baadaye alishirikiana kwa ukaribu sana na Huss, alikuwa anarudi kutoka Uingereza, aliyaleta Maandiko ya Wycliffe. Malkia wa Uingereza ambaye alikuwa ameongolewa kupitia maandiko ya Wycliffe, alikuwa ni binti wa mfalme wa Bohemia, na kupitia mvuto wake pia, kazi za Mwanamatengenezo zilisambazwa zaidi katika nchi yake (Bohemia). Huss aliyasoma maandishi haya kwa shauku; aliamini kuwa mwandishi wake alikuwa Mkristo mwadilifu na aliyejizatiti katika kuyatilia maanani matengenezo aliyoyahubiri. Japokuwa hakutambua, Huss tayari alikuwa ameingia katika njia ambayo ingempeleka mbali sana na Rumi. [GC 99.2; PK Aya ya 6]

**Picha Mbili Zaugusa Moyo Wa Huss**

Karibu na wakati huu, wageni wawili kutoka Uingereza waliwasili jijini Prague, watu wasomi ambao walikuwa wameipokea nuru ya injili, nao walikuja kusambaza katika nchi hii ya mbali. Wakaanza kwa kuushambulia ukuu wa papa hadharani, nao wakanyamazishwa mara moja na mamlaka; lakini wakiwa hawajaafiki kuliacha lengo lao, nao wakiwa wanasanaa na wahubiri, walikuwa na mbadala mwingine wa kuutumia ule ujuzi wao. Walichora picha mbili katika eneo la wazi. Picha moja ilionesha kuingia kwa Yesu Yerusalemu akiwa "mnyenyekevu, Naye amepanda mwanapunda" (Mathayo 21:5), na akifuatiwa na wanafunzi Wake katika mavazi yaliyochakaa kwa safari na wakiwa miguu peku (bila viatu). Picha nyingine ilionesha msafara wa papa-- papa akiwa amejivika majoho yake ya kitajiri na taji tatu kichwani (tiara), akiwa amepanda farasi aliyepambwa kwa gharama na fahari, akitanguliwa na wapiga tarumbeta na kufuatiwa na makadinali na maaskofu wakiwa katika mpangilio wa kuvutia na wakimetameta (vito walivyojiwekea). [GC 99.3; PK Aya ya 7]

Hapa kukawa na hubiri ambalo lilivuta umakini wa watu wa matabaka yote. Makundi yakaja kuangaza macho yao kwenye ile michoro. Hakuna mtu aliyeshindwa kuelewa maana ya somo lile la kimaadili na wengi walivutiwa na tofauti kati ya upole na unyenyekevu wa Kristo ambaye Ndiye Bwana na kiburi na majivuno ya papa, aliyedai kuwa mtumishi Wake Kristo. Kulikuwa taharuki kubwa mjini Prague, na ndipo wageni baada ya muda waligundua kuwa ilikuwa ni muhimu kwa ajili ya usalama wao kuondoka. Lakini somo walilolifundisha lilikuwa siyo la kusahaulika. Picha zile ziligusa kwa kina akili za Huss na kumpelekea kujifunza Biblia na Maandiko ya Wycliffe kiundani. Japokuwa bado alikuwa hajajiandaa, yaani, alikuwa bado hajayakubali matengenezo yote yaliyoshauriwa na Wycliffe, aliona ameona kwa uwazi zaidi tabia halisi ya upapa na kwa ari kubwa akapinga kiburi, fahari, tamaa ya makuu na ufisadi wa utawala wa mfumo wa upapa, utawala wa hierakia (hierarchy). [GC 100.1; PK Aya ya 8]

Nuru ikasambaa kutoka Bohemia mpaka Ujerumani, kwasababu ya yale machafuko ndani ya Chuo Kikuu cha Prague,nayo yalipelekea mamia ya wanafunzi wa Ujerumani kuondoka na kurudi makwao. Wengi miongoni mwao walikuwa wamefundishwa mafundisho ya awali ya Biblia na Huss na waliporejea makwao walisambaza injili katika nchi za mababa zao. [GC 100.2; PK Aya ya 9]

Habari ya kazi iliyofanyika Prague zilipelekwa Roma, na mara tu Huss aliitwa mbele ya papa. Kutii wito huo ingekuwa ni kujipeleka kwenye kifo cha hakika. Mfalme na malkia wa Bohemia, chuo kikuu, watu wa ngazi za juu, na maofisa wa serikali waliungana kumsihi papa kwamba Huss aruhusiwe kubaki Prague na ajibu mashitaka yake kupitia kaimu wake huko Rumi. Badala ya kulikubali ombi hili, papa aliliendeleza shauri na shitaka dhidi ya Huss na huku akimlaani kwa kutoa hukumu, na kisha aliutangaza mji wa Prague kuwa kizuizini yaani utengwe pamoja na watu wake na ibada zake (interdiction). [GC 100.3; PK Aya ya 10]

**Kutaharuki Katika Mji Wa Prague**

Katika zama zile hukumu ya namna hii ilipokuwa ikitangazwa tu, ilileta kutanda kwa hofu na mshtuko kwa wengi. Taratibu zilizoambatana na hukumu hii zilikusudiwa kuwatengenezea watu hofu, watu waliosadiki kuwa papa ndiye mwakilishi wa Mungu Mwenyewe, aliyezishika funguo za mbinguni na kuzimu, na mwenye mamlaka ya kutoa hukumu ya hapa duniani na za kiroho. Iliaminika kwamba malango ya mbinguni yalifungwa dhidi ya mji ambao ulihukumiwa kwa kuwekwa kizuizini; mpaka pale ambapo itakapompendeza papa kuuondolea kifungo hicho, basi wale waliokufa walikuwa wamefungiwa nje kutoka katika makao yale ya raha kamili na shangwe. Kama ishara ya janga hili kubwa, huduma zote za kidini zilisitishwa kwa muda. Makanisa yalifungwa. Ndoa zikafungwa kwenye uwanja wa nje ya kanisa. Wafu wakazuiliwa kuzikwa katika maeneo maalumu yaliyowekwa wakfu, nao wakazikwa bila huduma au taratibu za ibada za mazishi makaburini, kwenye makorongo, mitaro au mashambani. Hivyo kwa kutumia njia ambazo ziliiteka fikra, Rumi ilifanikiwa katika kuzitawala dhamiri za watu. [GC 101.1; PK Aya ya 11]

Jiji la Prague lilijazwa na machafuko. Watu wengi walimlaumu Huss kama sababu ya majanga yao yote na walidai kwamba akabidhiwe kwenye mamlaka ya Rumi ili ilipize kisasi. Ili kutuliza dhoruba, Mwanamatengenezo Huss aliondoka kwa muda kwenda kijijini kwao alikozaliwa. Akiwaandikia marafiki zake aliowaacha kule Prague, alisema: "Kama mimi nimetoweka miongoni mwenu, ni ili kufuata kielelezo na mfano wa Yesu Kristo, ili nisitoe nafasi kwa watu wenye nia mbaya kujisababishia wenyewe hukumu ya milele, na ili nisiwe sababu ya chanzo cha taabu na mateso kuwapata watu wacha Mungu. Nimeondoka kwenda kupumzika kwa hofu kwamba makuhani waovu wasiendelee kuzuia kuhubiriwa kwa Neno la Mungu miongoni mwenu kwa kipindi kirefu zaidi; lakini sikuondoka

ili niukane Ukweli mtakatifu, ambao kwa msaada wa Mungu, niko tayari kufa."—Bonnechose, The Reformers Before the Reformation, juzuu ya kwanza, uk. 87. Huss hakukoma utendaji wa kazi zake, lakini alizunguka kwenye nchi za jirani akihubiria halaiki zilizokuwa na shauku. Kwahiyo njia ambazo papa alichagua kutumia kuikandamiza injili zilikuwa zikiiwezesha isambae zaidi. "Maana hatuwezi kutenda neno lolote kinyume cha Kweli, bali kwa ajili ya Kweli." 2 Wakorintho 13:8 [GC 101.2; PK Aya ya 12]

Akili ya Huss, katika hatua hii ya kazi yake, ilionekana kama uwanja wa migogoro iliyomletea maumivu mengi. Ingawa kanisa lilikuwa linatafuta namna ya kumuumiza kwa radi za vitisho, yeye alikuwa hajayakana mamlaka yake. Kwa Huss Kanisa la Rumi lilibaki kuwa bibi harusi wa Kristo, na papa alikuwa mwakilishi na mtumishi wa Mungu. Huss alikuwa anapinga matumizi yao mabaya ya mamlaka, na sio kanuni yenyewe. Jambo hili likaleta mgogoro wa kutisha kati ya kile alichosadiki kwa uelewa wake, na madai ya dhamiri yake. Ikiwa mamlaka ile ilikuwa ya haki na isiyokosea kama alivyoamini, inakuwaje basi ajisikie anasukumwa kutoitii? Aliona kulitii ni kutenda dhambi; lakini kwanini utii kwa kanisa takatifu lisilokosea ipelekee suala kama hilo? Hili lilikuwa ni tatizo ambalo alishindwa kulitatua; mashaka hayo yalimtesa saa hadi saa. Suluhisho lililokuwa karibu sana naye, ambalo aliweza kutoa lilikuwa ni kwamba jambo lile lilikuwa limerudiwa tena, kama ilivyokuwa kipindi cha Mwokozi, makuhani/makasisi wa kanisa walikuwa wamegeuka na kuwa watu waovu, tena walikuwa wakitumia mamlaka yao halali kwa makusudi ambayo hayakuwa halali. Waz0 lile akalifanya kuwa mwongozo wake, kisha aliwahubiria wengine Neno la hekima ili liwe mwongozo wao, na kwamba kanuni za Maandiko, zikiingia katika uelewa wa mtu, ni sharti ziitawale dhamiri yake; kwa maneno mengine, ni kwamba usikivu uwe kwa Mungu anenapo kupitia Biblia, na wala sio kanisa linasema nini kupitia upapa, Maana Yeye pekee Ndiye Mwongozo pekee usioweza kukosea kamwe."—Wylie, b. 3, ch. 2. [GC 102.1; PK Aya ya 13]

Mara baada ya ghasia kupungua Prague, Huss alirejea kwenye kanisa lake dogo la Bethlehem (chapel), na kuendelea kwa juhudi kubwa na moyo kulihubiri Neno la Mungu. Maadui zake walikuwa hai na wenye nguvu, lakini malkia na baadhi ya watu wa ngazi za juu walikuwa marafiki zake, na idadi kubwa ya watu ilikuwa upande wake. Watu walikuwa wakilinganisha mafundisho yake safi yaliyogusa moyo, dhidi ya mafundisho yanayopotosha, nayo yaliwatia matumaini pamoja na maisha yake matakatifu ukilinganisha na yale waliyohubiri wafuasi wa Rumi, kisha kwa ulafi na uchu wao wa mali pamoja na ulevi, uasherati na uovu mwingine walioufanya, wengi waliona ni fahari au heshima kuwa upande wake [GC 102.2; PK Aya ya 14]

Mpaka wakati ule Huss alikuwa amesimama mwenyewe katika taaluma na kazi yake; lakini sasa Jerome aliingia pichani, huyu alipokuwa Uingereza alikuwa

ameyakubali Maandiko ya Wycliffe, ksha akajiunga kwenye kazi ya matengenezo ya kanisa. Tangu hapo hawa wawili waliunganishwa katika maisha yao, na hata katika kifo hawakutenganishwa. Karama za ubora wa akili, ufasaha mzuri wa kuongea na kujifunza, na kipaji cha kushawishi na kupendwa na umma--zilimilikiwa na Jerome kwa kiwango kikubwa ukilinganisha na mwenzake; lakini katika sifa zile zinazoipa tabia nguvu yake kwa uhalisi, Huss alimzidi. Hekima yake iliyotulia ilitumika kutuliza roho yenye papara ya Jerome katika maamuzi ambayo yaliyopaswa yafanywe kwa taratibu, naye Jerome kwa unyenyekevu wa kweli, alitambua thamani yake, na kuyatii mashauri ya mwenzake Huss. Chini ya muunganiko wa kazi yao, matengenezo ya kanisa yakasambaa kwa haraka zaidi (Kumb 32:20). [GC 102.3; PK Aya ya 15]

Mungu aliruhusu nuru kubwa iangaze kwenye mioyo ya watu hawa aliowachagua, akiwafunulia mafundisho mengi yenye makosa ya kanisa la Rumi; lakini wao hawakupokea nuru yote ambayo ilipaswa kutolewa ulimwenguni. Kupitia hawa watumishi Wake, Mungu alikuwa anawaongoza watu kutoka katika giza la Urumi; lakini kulikuwa na vipingamizi vingi na vikubwa walivyopaswa kukutana navyo Naye aliwaongoza hatua kwa hatua, kwa kadiri walivyoweza kustahimili. Walikuwa hawajajiandaa kupokea nuru yote kwa mkupuo yaani kwa mara moja. Kama vile ulivyo mng'ao kamili wa jua la mchana kwa wale ambao wameishi gizani kwa muda mrefu, nuru ile, endapo ingewasilishwa yote kwao, ingeweza kusababisha wageuke na kwenda zao au kukimbia. Kwahiyo aliwafunulia viongozi kidogo-kidogo, kadri ya vile watu walivyoweza kuipokea. Toka karne hata karne, watendakazi wengine waminifu walitazamiwa kuifuata nuru hii na hivyo kuwaongoza watu zaidi kwenye njia hii ya matengenezo ya kanisa (Protestant Reformation). [GC 103.1; PK Aya ya 16]

Mpasuko ndani ya kanisa bado ukaendelea. Sasa mapapa watatu wakawa wanagombania madaraka na ugomvi wao ukajaza uhalifu na fujo kwenye ulimwengu wa Kikristo. Kwa kutotosheka na kutupiana laana na kwa machafuko yaliyokuwa yakiongezeka, waliamua kutumia silaha za kidunia. Kila kundi likajielekeza kununua silaha na kujipatia wanajeshi. Kimsingi pesa zilikuwa zinahitajika kutimiza lengo hilo; na ili kuzipata, sadaka, zawadi, baraka, ofisi za na mali zote za kanisa zikapigwa mnada. *(Tazama Dokezo la kiambatanisho cha sura ya 3 Aaya 28, 29 na 30).* Mapadri pia, huku wakiwaiga wakuu wao, waliamua kufanya kazi kwa faida binafsi kwa kushurutisha watu kununua huduma za kichungaji au kanisa na kufanya vita, nao wakawanyenyekesha wapinzani wao ili kuimarisha nguvu zao. Kwa ujasiri wake ulioongezeka kila siku Huss alinguruma dhidi ya machukizo ambayo yalivumiliwa katika jina la dini; na watu wakawalaumu viongozi wa Urumi waziwazi kuwa walikuwa chimbuko la machungu yaliyokuwa yanaugharikisha ulimwengu wa Kikristo. [GC 103.2; PK Aya ya 17]

Kwa mara nyingine jiji la Prague likaonekana kukaribia ukingo wa mlipuko wa pambano ambalo lingemwaga damu. Kama ilivyokuwa katika vizazi vya zamani, mtumishi huyu wa Mungu alishitakiwa kuwa “mtaabishaji wa Israeli” 1 Wafalme 18:17. Mji uliwekwa chini ya uangalizi, na kutengwa tena, naye Huss aliondoka na kurejea kijijini kwao tena. Ushuhuda uliobebwa kwa uaminifu na kanisa lake alilolipenda la Bethlehem ulikomeshwa. Alikuwa anakwenda kuzungumza kutoka kwenye jukwaa pana zaidi sasa, kwenye ulimwengu wote wa Kikristo, akiwa kwenye jukwaa pana zaidi kabla ya kuuawa kwake kama shahidi mwaminifu wa ile Kweli (mfia dini). [GC 104.1; PK Aya ya 18]

Ili kuweza Kuyaponya maovu yote yaliyokuwa yanaleta machafuko na kuchukua usikivu wa watu wa Ulaya, baraza kuu likaitishwa kule mjini Constance. Baraza liliitishwa kwa matakwa ya mtawala Sigismund, kupitia mmoja wa mapapa watatu waliokinzana, John XXIII. Hitaji la kuwepo kwa baraza halikuafikiwa na Papa John, ambaye tabia na sera yake visingestahimili kufanyiwa uchunguzi, kwani hata maaskofu wake hawakuwa na maadili yaliyokuwa tofauti na washiriki au walei wa kipindi kile. Hata hivyo, hakuthubutu, kuyapinga matakwa ya Sigismund. *(Tazama Kiambatanisho)* [GC 104.2; PK Aya ya 19]

Malengo makuu yaliyopaswa kutimizwa katika baraza hili yalikuwa ni kuondoa mafarakano na kuung’oa mzizi wa uzushi ndani ya kanisa. Kwa hiyo wale mapapa wawili waliopingana waliitwa mbele ya baraza, na yule msambazaji mkuu aliyebuni yale maoni mapya, John Huss. Wale wawili wa kwanza (mapapa), kwa kuhofia usalama wao wenyewe, hawakuhudhuria wao binafsi, bali waliwakilishwa na wajumbe wao. Ingawa papa John alikuwa ndiye aliyeitisha baraza, alikuja katika baraza akiwa na mashaka mengi, akishuku lengo la siri la mfalme kumwondoa kwenye madaraka, na akiogopa kuhukumiwa kwa uovu ambao ulikuwa umeidhalilisha mamlaka ya upapa (tiara), pamoja na makosa ya jinai aliyofanya ili kuipata taji hiyo (uhalifu). Hata hivyo aliingia katika jiji lile la Constance kwa mbwembwe (fahari) kubwa, akiandamana na watumishi wa vyeo vya juu kabisa na kufuatiwa na msururu wa watumishi wa ofisi ya mfalme. Makasisi au viongozi wa dini, na waheshimiwa ndani ya jiji, pamoja umati mkubwa wa raia walitoka kwenda kumlaki. Juu ya kichwa chake kulikuwa na dari ya dhahabu, kama mwavuli hivi, iliyoshikiliwa na majaji wakuu wanne. Jeshi kubwa lilitangulia mbele yake, Mkate ule mtakatifu wa komunio yaani hostia, ulibebwa mbele yake na mavazi ya kitajiri ya makadinali na watu wa ngazi ya juu yaliwavutia watu kwa maonyesho makubwa sana. [GC 104.3; PK Aya ya 20]

Wakati ule ule, msafiri mwingine alikuwa akikaribia Jiji la Constance. Huss alizitambua hatari zilizotishia maisha yake. Aliagana na marafiki zake kana kwamba hataweza kuonana nao tena uso kwa uso, na akaendelea na safari yake akihisi kwamba ilikuwa inampeleka kwenye ile nguzo ya kuchomea moto watu.

Ijapokuwa alikuwa amepata waraka wa kumhakikishia ulinzi kutoka kwa mfalme wa Bohemia, na waraka mwingine kutoka kwa mtawala Sigismund wakati akiwa kwenye safari yake, lakini alifanya mipango yake yote huku akitazamia uwezekano wa kifo chake. [GC 104.4; PK Aya ya 21]

### Cheti Cha Kumruhusu Kusafiri Salama Toka Kwa Mfalme

Katika barua aliyowaandikia marafiki zake wa Prague alisema: "Ndugu zangu, ……naondoka nikiwa na cheti kutoka kwa mfalme cha kunihakikishia kusafiri salama, ili nikutane na maadui zangu wengi wenye ukomo, yaani binadamu wawezao kufa……Ninaweka tumaini langu lote kwa Mungu Mwenye nguvu zote, Mwokozi wangu; ninaamini atayasikiliza maombi yenu ya dhati na bidii, na kwamba ataweka busara ya kubainisha mambo na hekima Yake kinywani mwangu, ili niweze kuwapinga; na kwamba atanipa Roho Wake Mtakatifu kunitia nguvu katika Ukweli Wake, ili niweze kukabiliana kwa ujasiri majaribu, gereza na ikilazimika kifo kile cha kikatili. Yesu Kristo aliteseka kwa ajili ya wale aliowapenda; je, kwanini tustaajabu basi, kwamba kwanini Yeye ametuachia mfano Wake, ili nasi tuweze kuvumilia katika mambo yote kwa ajili ya wokovu wetu wenyewe? Yeye ni Mungu, na sisi tu viumbe Vyake; Yeye Ndiye Bwana, na sisi ni watumishi Wake; Yeye Ndiye Bwana wa ulimwengu, na sisi ni wanadamu tunaochukiza na tunaokufa tu— na bado Yeye Aliteseka! Kwanini basi, sisi tusiteseke pia ikiwa mateso hayo ni kwa ajili ya utakaso wetu? Kwahiyo, wapendwa, ikiwa kifo changu kitachangia utukufu Wake, niombeeni kwamba kije haraka, Naye aniwezeshe kuyakubali majanga yangu yote kwa uadilifu, bila kuterereka. Lakini ikiwa ni vyema nirudi kati yenu, basi tumuombe Mungu ili nirudi bila doa — ikimaanisha kwamba, nisije nikaukandamiza Ukweli au kuingia kwenye maridhiano hata chembe moja ya ile Kweli ya injili, ili niweze kuwaachia ndugu zangu kielelezo bora cha kufuata. Huenda hamtauona uso wangu huko Prague; lakini kama mapenzi ya Mungu Mwenye nguvu zote yakijaribu kunirudisha kwenu, hebu basi na tuendelee kwa moyo imara zaidi katika maarifa na upendo wa sheria Yake."- Bonnechose, vol. 1, uk.147, 148. [GC 105.1; PK Aya ya 22]

Katika barua yake nyingine kwa kasisi ambaye alikuwa amegeuka na kuwa mwanafunzi wake wa injili, Huss aliongea kwa unyenyekevu mkubwa juu ya makosa yake mwenyewe, akijilaumu mwenyewe "kwa kujisikia raha wakati wa kuvaa kwake mavazi ya fahari/kitajiri na kupoteza masaa katika kazi za kijinga au mambo ya kipuuzi na yasiyokuwa na maana." Kisha akaongeza maonyo haya ya kugusa moyo: "Hebu utukufu wa Mungu na wokovu wa roho za watu uijaze akili yako, na si milki ya mali, maslahi ya kikasisi, majumba, mashamba na faida zingine. Jihadhari na tabia ya kupamba nyumba yako kuzidi roho yako; na juu ya yote, jitoe kwa makusudi ya kujenga mionjo ya kiroho kuliko kitu kingine. Uwe

mcha Mungu, mwadilifu, mnyenyekevu na maskini, usiwe mbaradhifu wa mali zako kwa karamu. Unapaswa kurekebisha maisha yako na kujiepusha na mambo yale yanayozidi kiasi, au ufujaji wa aina yoyote, wasiwasi wangu ni kwamba usipotengeneza maisha yako, utaadhibiwa kwa kuwajibishwa vikali sana, kama mimi mwenyewe nilivyo……wewe unayajua mafundisho yangu, kwani umeyapokea maagizo yangu tangu utoto wako; kwa hivyo haina maana kwangu kukuandikia zaidi ya haya. Lakini nakuasa kwa rehema ya Bwana wetu, usiniige katika majivuno au ubatili wowote ulioniona nimetumbukia kwa huo. "Juu ya bahasha ya barua hiyo aliongezea maneno haya: "Ninakusihi, rafiki yangu, usifungue barua hii mpaka utakapopata uthibitisho kwamba nimekufa." - Ibid., Vol. 1, uk. 148, 149. [GC 105.2; PK Aya ya 23]

**Mwanamatengenezo Huyo Atiwa Mbaroni**

Katika safari yake hii, Huss aliona viashiria vya kuenea na kupendwa kwa mafundisho yake kila mahali na namna ambavyo kazi yake ilikubaliwa. Watu walifurika wakitaka kukutana naye, na katika miji mingine mahakimu walijitokeza kumsindikiza alipopita kwenye mitaa yao. [GC 106.1; PK Aya ya 24]

Baada ya kufika jiji la Constance, Huss alipewa uhuru kamili. Pamoja na waraka wa kibali cha kumlinda cha mfalme, alihakikishwa ulinzi binafsi na papa pia. Lakini, kinyume na matamko haya mazito ya ahadi za kupewa usalama na yaliyorudiwa tena na tena kwake, Mwanamatengenezo huyu alikamatwa baada ya muda mfupi tu kwa amri ya papa na makadinali na kutupwa kwenye gereza chafu la kuchukiza, chini ya ardhi. Baadaye alihamishiwa kwenye ngome imara huko Rhine na huko aliwekwa kama mfungwa. Papa, alinufaika kidogo kwa udanganyifu wake kwa Huss, kwani naye alipelekwa kwenye gereza hilo muda si mfupi baadaye. Ibid., vol. 1, uk. 247. Alikuwa ameshutumiwa na kuthibitishwa mbele ya baraza kuwa na makosa ya jinai makubwa zaidi, ambayo yalikuwa mzizi wa uhalifu, mbali na yale ya mauaji, kujitengenezea faida binafsi kupitia mambo ya kiroho (indulgensia), kula hongo, na uzinzi, "zilikuwa ni dhambi ambazo haziskutahili kutajwa mbele za watu." Kwa hivyo baraza lenyewe lilitangaza, na mwishowe alinyang'anywa taji ya upapa (kofia iitwayo tiara) na kutupwa gerezani. Mapapa wale wawili waliopingana, wote waliondolewa, na papa mpya akachaguliwa. [GC 106.2; PK Aya ya 25]

Ingawa papa mwenyewe alikuwa na mashitaka makubwa ya uhalifu kuliko ambayo Huss alivyokuwa amewashutumu mapadre ambao alidai wafanye matengenezo, hata hivyo baraza lile lile lililomdhalilisha na kumshusha papa liliendelea kumsagasaga Mwanamatengenezo huyu. Kufungwa kwa Huss kuliamsha ghadhabu kubwa huko Bohemia. Watu waungwana na mashuhuri wa ngazi za juu waliwasilisha upinzani wa dhati juu ya jambo hili. Mfalme, ambaye alichukia kwa kuruhusu ukiukwaji wa kibali cha usalama alichompa Huss, alipinga

mwenendo wa baraza dhidi ya Huss. Lakini maadui wa Mwanamatengenezo walikuwa wakatili na waliodhamiria uovu. Walitaka mfalme awaonyeshe upendeleo, wakamtia hofu na kumwambia awe na shauku upande wa kanisa. Wakaleta hoja zao ndefu sana kuthibitisha kwamba "imani isishikwe pamoja na wazushi au mtu anayeshukiwa uasi, hata kama anapewa vyeti vya kusafiri salama na mfalme wa dola pamoja na wafalme wao." - Jacques Lenfant, History of the Council of Constance, vol. 1, uk. 516. Hatimaye walishinda. [GC 107.1; PK Aya ya 26]

Akiwa amedhoofika sana kwa ugonjwa na kifungo,-- kwa sababu ya hewa chafu ya unyevunyevu kwenye gereza la ardhini, ambalo lilimsababishia homa ambayo ilibaki kidogo kuyamaliza maisha yake--- mwishowe Huss alifikishwa mbele ya baraza. Akiwa amefungwa na minyororo mingi mizito, naye akasimama mbele ya mfalme wa dola ambaye kwa heshima na nia yake njema alikuwa ameahidi kumlinda kwa kumpa hati ya usalama. Wakati wa kesi yake ndefu alidumisha kuitetea ile Kweli mbele ya viongozi mashuhuri wa kanisa na serikali, alitamka maneno adhimu na yenye uaminifu katika kupinga ufisadi wa uongozi ule wa ngazi wa kanisa (hierakia). Alipohitajika kuchagua ikiwa atayakana mafundisho yake au kufa, aliikubali hatima ya mfia dini (shujaa kwa kumfia Kristo). [GC 107.2; PK Aya ya 27]

### Ategemezwa Kwa Neema Ya Mungu

Neema ya Mungu ilimshikilia. Katika zile wiki za mateso zilizotangulia kabla ya hukumu yake ya mwisho, amani ya mbinguni iliujaza moyo wake. "Ninaandika barua hii," alimwambia rafiki, "nikiwa ndani ya gereza langu, na kwa kutumia mkono wangu uliofungwa pingu na minyororo, nikiitarajia hukumu yangu ya kifo kesho-- ikiwa kwa msaada wa Yesu Kristo, tutakapokutana tena katika amani ile tamu ya maisha yale ya baadaye, utafahamu jinsi Mungu alivyojidhihirisha kwangu kuwa Mwenye rehema nyingi, jinsi alivyonitegemeza katikati ya majaribu na mateso yangu."- Bonnechose, vol. 2, uk. 67. [GC 107.3; PK Aya ya 28]

### Huss Akataa Kuikana Imani Yake

Katika upweke wa giza kwenye gereza lake la chini ya ardhi aliuona mbele ushindi wa imani ile ya Kweli. Akirejelea ndoto zake za kanisa la Prague ambapo alikokuwa ameihubiri injili, alimwona papa na maaskofu wake wakizifuta picha za Kristo ambazo alikuwa amezichora kwenye kuta zake. "Ndoto hii ilimfadhaisha: lakini siku iliyofuata aliwaona wachoraji wengi wakishughulika kurejesha michoro hii kwa idadi kubwa na kwa rangi zinazong'aa zaidi. Mara tu kazi yao ilipomalizika, wachoraji ambao walikuwa wamezungukwa na umati mkubwa walipiga kelele wakisema, "hebu sasa na waje wale mapapa na maaskofu; kamwe hawataweza kuzifuta tena!'" Mwanamatengenezo alisema,

alipokuwa akisimulia ndoto yake: “Ninaamini hili kwa hakika, kwamba sura ya Kristo haitafutwa kamwe. Wametamani kuiharibu kabisa, walakini itachorwa upya tena katika mioyo yote, tena kupitia wahubiri bora zaidi kuliko mimi mwenyewe.”- D’Aubigne, b. 1, sura ya. 6. [GC 108.1; PK Aya ya 29]

Kwa mara ya mwisho, Huss aliletwa mbele ya baraza. Ulikuwa mkutano mkubwa sana, wa watu wengi mahiri na wenye vipaji na taaluma tofauti ---mfalme yule wa dola, wakuu ambao wana damu ya kifalme, viongozi wa ufalme, manaibu wa kifalme, makadinali, maaskofu na makasisi na umati mkubwa waliojihudhurisha kama watazamaji wa matukio ya siku hiyo. Kutoka katika sehemu zote za ulimwengu ule wa Ukristo walikuwa wamekusanyika kama mashahidi wa kafara hii kubwa ya kwanza katika safari refu ya mapambano makubwa ambayo uhuru wa dhamiri ungeweza kupatikana. [GC 108.2; PK Aya ya 30]

Alipoitwa kwa ajili ya kutoa uamuzi wake wa mwisho, Huss alitamka kukataa kwake kukana msimamo wake kwa kiapo na akakaza macho yake kwa yule mfalme ambaye ahadi za maneno yake zilikuwa zimekiukwa bila aibu, akasema “Niliazimia kwa hiari yangu mwenyewe, kufika mbele ya baraza hili, chini ya ulinzi wa serikali na imani ya mfalme huyu wa dola aliyepo hapa.”- Bonnechose, vol. 2, uk. 84. Uso wa Sigismund ulibadilika na kuwa mwekundu sana kwa aibu, na macho ya watu wote katika mkutano yakigeukia kumtazama. [GC 108.3; PK Aya ya 31]

Baada ya hukumu kutangazwa, sherehe ya kumshusha hadhi au kumdhalisha ikaanza. Maaskofu walimvika mfungwa wao mavazi ya kipadre na alipovaa joho la kipadre alisema: “Bwana wetu Yesu Kristo alivikwa vazi jeupe, kwa dhihaka na matusi wakati Herode alipompeleka mbele ya Pilato.”- Ibid., Vol. 2, uk. 86. Alipoambiwa tena kujisalimisha, alijibu, akiwageukia watu: “hivi mimi nitaiangalia mbingu kwa uso gani? Je, Nitautazamaje umati wa watu ambao nimewahubiria injili safi? Hapana; Nathamini wokovu wao kuliko mwili huu dhaifu, ambao sasa umehukumiwa kuuawa.” Mavazi hayo yaliondolewa moja baada ya jingine, na kila askofu akitamka laana wakati anafanya sehemu yake ya sherehe. Hatimaye “walimwekea kichwani kofia au kilemba cha karatasi kilichokuwa na umbo la msonge/piramidi, ambalo juu yake kulikuwa na taswira za kutisha za mashetani/mapepo na neno 'Mkuu wa uzushi/uasi' lilionekana mbele yake. Huss akasema 'Nina furaha zaidi, nitavaa taji hii ya aibu kwa ajili Yako, Ee Yesu, ambaye ulivaa taji ya miiba kwa ajili yangu.” [GC 108.4; PK Aya ya 32]

Alipovikwa hivi, “maaskofu wakasema, ‘Sasa tunaitoa roho yako wakfu kwa mwovu/shetani.’ ‘Na mimi,’ alisema John Huss, akiinua macho yake kuelekea mbinguni, ‘naweka roho yangu mikononi Mwako, Ee Bwana Yesu, kwa kuwa Wewe Ulinikomboa.’” —Wylie, b. 3, sura ya 7. [GC 109.1; PK Aya ya 33]

### Huss Afa Kwa Kuchomwa Katika Nguzo Ya Kuchomea

Sasa alikabidhiwa katika mamlaka ya kidunia na kupelekwa mahali pale pa kuulia watu. Msafara mkubwa sana ulifuata nyuma yake, mamia ya watu wakiwa wamebeba silaha, mapadri na maaskofu wakiwa wamevalia mavazi yao ya gharama kubwa na wakazi wa Constance. Alipofungwa kwenye nguzo ya mti wa kuchomea watu, na moto ukiwa tayari kuwashwa, mfia dini huyu aliulizwa kwa mara nyingine kujiokoa nafsi yake mwenyewe kwa kuyakiri makosa yake au kukanusha imani yake. Huss aliuliza, “Ni makosa gani ni sharti niyakane? Ninajua mwenyewe kuwa sina hatia yoyote. Ninamwita Mungu ashuhudie ya kwamba yote niliyoandika na kuhubiri yalikuwa ni kwa lengo la kuokoa roho kutoka kwenye dhambi na uangamivu; na kwa hivyo, kwa furaha kubwa nitathibitisha kwa damu yangu Ukweli huo ambao nimeandika na kuuhubiri.”—Ibid., b. 3, sura ya 7. Wakati moto ulipokuwa umewashwa kumzunguka, alianza kuimba, “Yesu, Mwana wa Daudi, unirehemu,” na aliendelea kuimba mpaka sauti yake iliponyamazishwa milele katika dunia hii (ila siku ya ufufuo itazungumza tena!). [GC 109.2; PK Aya ya 34]

Hata maadui zake walipigwa na butwaa kwa ushujaa wake wa pekee. Mfuasi wa upapa na mkereketwa mwenye usongo akielezea kuuawa kwa Huss na kwa Jerome, aliyekufa mara baada ya hapo, alisema: “Wote wawili walikuwa na msimamo thabiti wakati saa yao ya mwisho ilipokaribia. Walijiandaa kukabili moto kana kwamba walikuwa wakienda kwenye sherehe ya arusi. Hawakutoa sauti au kilio chochote cha maumivu. Wakati ndimi za moto zilipopanda juu, walianza kuimba nyimbo; na ukali wa moto haukuweza kuzuia ari yao ya kuimba.” —Ibid., b. 3, sura ya 7. [GC 109.3; PK Aya ya 35]

Wakati mwili wa Huss ulipoteketezwa kabisa, majivu yake pamoja na udongo ambao majivu yalikaa juu yake, vilikusanywa na kutupwa ndani ya mto Rhine huko ulaya, na kwa njia hiyo yakachukuliwa kupelekwa baharini. Watesi wake walijidanganya kwamba wameing’oa mizizi ya zile Kweli alizokuwa akizihubiri. Hawakudhani hata kidogo katika siku ile kwamba majivu yalipopelekwa baharini yangekuwa kama mbegu iliyotawanyika katika mataifa yote ya dunia; kwamba katika nchi ambazo hazijulikani bado yangechipuka matunda tele ya mashahidi wa Ukweli. Sauti ile ambayo ilinena katika ukumbi wa baraza la Constance ilikuwa imeweka hai miangwi ambayo ingesikika kwa vizazi vyote vijavyo. Huss alikuwa hayupo tena, lakini Ukweli ule ambao alioufia usingeweza kuangamia kamwe. Kielelezo chake cha imani na msimamo thabiti vingeweza kuwatia moyo watu wengi kusimama kwa uthabiti kwa ajili ya Ukweli, mbele ya mateso na kifo. Kuuawa kwake kuliuonyesha ulimwengu wote ukatili wa kutisha na hila za Rumi. Maadui wa Ukweli, ingawa hawakujua, walikuwa wanaunga mkono na

kuiendeleza mbele kazi ya Mungu ambayo walidhani wanaiharibu, ila hawakufanikiwa. [GC 110.1; PK Aya ya 36]

**Jerome Afika Kule Constance**

Hata hivyo nguzo nyingine ya kuchomea watu ilikuwa inaandaliwa katika jiji la Costance. Damu ya shahidi mwingine ilipaswa tena kushuhudia ile Kweli. Jerome, baada ya kuagana na Huss wakati alipokuwa anaondoka kuelekea katika baraza, alikuwa amemsihi kuwa jasiri na uthabiti, akimhakikishia kwamba ikiwa angekuwa katika hatari yoyote, basi yeye mwenyewe angeenda kumsaidia mara moja. Aliposikia kuwa Mwanamatengenezo huyo amefungwa, mwanafunzi huyo mwaminifu alijiandaa mara moja ili kutimiza ile ahadi yake. Bila kibali cha uhakikisho wa usalama, Jerome alielekea Costance na rafiki mmoja. Alipofika pale, alitambua kwamba alikuwa amejiingiza mwenyewe hatarini, naye hakuwa na uwezo wa kufanya chochote ili kumwokoa Huss. Alikimbia kutoka katika mji ule, lakini alikamatwa akiwa safarini kurudi nyumbani na kurudishwa akiwa amefungwa minyororo mingi mizito akiwa chini ya ulinzi wa kikosi cha maaskari/wanajeshi. Alipotokea kwa mara ya kwanza katika baraza, jitihada zake za kujibu tuhuma zilizoletwa dhidi yake zilikumbwa na kelele, "Atupwe motoni pamoja naye! Motoni!"- Bonnechose, vol. 1, uk. 234. Alipotupwa gereza la chini ya ardhi, alifungwa kwa minyororo kwa jinsi ambayo ilimsababishia mateso makubwa sana, na alilishwa mkate na maji tu. Baada ya miezi kadhaa ya mateso na kifungo chake, Jerome alipatwa na ugonjwa uliotishia uhai wake, na maadui zake waliogopa kwamba angeweza kuwatoka yaani kufa, nao wakapunguza makali kidogo, ingawa aliendelea kukaa gerezani kwa mwaka mmoja. [GC 110.2; PK Aya ya 37]

**Jerome Akubali Kulitii Baraza**

Kifo cha Huss hakikuleta matokeo yale ambayo wafuasi wa papa waliyatarajia. Ule ukiukwaji wa hati usalama uliamsha dhoruba ya hasira na kama njia salama, baraza liliamua, badala ya kumteketeza kwa moto Jerome, limlazimishe, ikiwa inawezekana, akanushe imani yake badala ya kumchoma moto. Ndipo Jerome, akaletwa mbele ya baraza na akapewa nafasi ya kukana imani yake kwa kutangua maneno yake, au kufa katika nguzo ya kuchomea watu. Mwanzoni mwa kifungo chake, kifo kingekuwa rehema kwake ikilinganishwa na mateso mabaya aliyoyapitia; lakini sasa, alikuwa na udhaifu kwa maradhi, na hali mbaya ya chumba chake cha gereza na mateso ya wasiwasi, mfadhaiko, mashaka ya kutengwa na marafiki zake, na kuvunjika moyo kwa kifo cha Huss, ujasiri wa Jerome uliyumba na alikubali kujisalimisha kwa baraza. Aliahidi kufuata imani ya Kikatoliki na akakubali hatua ya baraza hilo kulaani baadhi ya mafundisho ya Wycliffe na Huss, licha ya, "Kweli zile takatifu" walizokuwa wamezifundisha. Ibid, vol. 2, uk. 141. [GC 111.1; PK Aya ya 38]

Kwa uamuzi huu Jerome alinuia kuinyamazisha sauti ya dhamiri yake ili kuepukana na maafa yatakayompata. Lakini katika upweke wa gereza la ardhini, aling'amua kwa wazi zaidi kile ambacho alichokuwa amekifanya. Aliufikiria ujasiri na uaminifu wa Huss na kwa kulinganisha akatafakari juu ya kukana kwake Ukweli. Alimtafakari Mwalimu Yule mtakatifu wa mbinguni, ambaye alikuwa amejitolea kumtumikia na ambaye kwa ajili Yake alivumilia kifo cha msalaba. Kabla ya kuikana imani yake alikuwa amepata faraja katikati ya mateso yake yote katika uhakikisho wa wema wa Mungu; lakini sasa majuto na mashaka yaliitesa roho yake vikali. Alijua fika kwamba bado angetakiwa kukana zaidi imani yake, ili kufikia kwenye maridhiano ya amani na Rumi. Njia ile ambayo alikuwa akiichagua ilikuwa inaishia tu kwenye uasi kamili kwa Mungu. Azimio lake lilifanyika: Asingependa kumkana Bwana wake ili kuepuka kipindi hiki kifupi cha mateso ya kitambo. [GC 111.2; PK Aya ya 39]

Baadaye kidogo akaletwa tena mbele ya baraza lile. Akakubali kujisalimisha kwake, jambo ambalo halikuwaridhisha mahakimu wake. Kiu yao ya damu, iliyosababishwa na kifo cha Huss, ilihitaji wahanga wapya. Ni kwa kuikana wazi imani hii tu, kwa kuitupilia mbali mambo yote, ndiyo Jerome angeweza kuyaokoa maisha yake. Lakini yeye alikuwa ameamua kudhihirisha imani yake na kumfuata ndugu yake mfia dini, kwenda kuchomwa motoni. [GC 112.1; PK Aya ya 40]

Jerome akaukataa katakata uamuzi wake wa kuikana imani yake kama alivyofanya awali na kama mtu anayeelekea kwenda kufa, aliomba sana fursa ya kujitetea. Kwa kuogopa ushawishi wa maneno yake, wale maaskofu walisisitiza kwamba yeye sharti tu akubali au akane (atangue) Ukweli wa mashtaka aliyoshtakiwa. Jerome alipinga ukatili na dhuluma ya namna hiyo. "Mmeniweka kifungoni siku mia tatu na arobaini ndani ya gereza la kutisha," alisema, "katikati ya uchafu, giza, makelele, uvundo, kinyaa na uhaba wa mahitaji ya lazima; kisha mnanileta mbele yenu na mnawasikiliza maadui zangu wauaji ambao wanakufa, na mnakataa kunisikiliza mimi……Ikiwa ninyi ni watu wenye busara kweli, na mmekuwa nuru ya ulimwengu, jihadharini msitende dhambi dhidi ya haki. Mimi kama mimi, ni mwanadamu aliye dhaifu tu, mwenye mwili unaokufa; maisha yangu hayana umuhimu sana; na ninapowasihi msitoe hukumu isiyo ya haki, naongea kwa faida yenu ninyi kuliko yangu mimi mwenyewe."- Ibid., vol. 2, ukurasa wa 146, 147. [GC 112.2; PK Aya ya 41]

**Utetezi wa Kijasiri wa Jerome**

Hatimaye ombi lake lilikubaliwa. Mbele ya waamuzi wake, Jerome alipiga magoti na kuomba ili Roho wa Mungu aweze kudhibiti mawazo na maneno yake, kwamba asizungumze chochote kilicho kinyume na Ukweli au lolote lisilompendeza Mwalimu wake. Kwake siku hiyo ilitimizwa ahadi ya Mungu kwa

wanafunzi Wake wale wa kwanza: “Nanyi mtachukuliwa mbele ya watawala na wafalme kwa ajili Yangu, kuwa ushuhuda kwao na kwa mataifa. Lakini hapo watakapowapeleka, msifikirifikiri jinsi mtakavyosema; maana mtapewa saa ile mtakayosema. Kwa kuwa si ninyi msemao, bali ni Roho wa Baba yenu asemaye ndani yenu.” Mathayo 10:18-20. [GC 112.3; PK Aya ya 42]

Maneno ya Jerome yaliamsha mshangao na mvuto hata kwa maadui zake. Kwa mwaka mzima alikuwa kifungoni ndani ya gereza la ardhini, naye hakuweza kusoma au hata kuona kwa ajili ya mateso makubwa ya mwili na mfadhaiko wa kiakili. Licha ya hayo, hoja zake ziliwasilisha kwa uwazi na uthabiti kana kwamba alikuwa hakuwa na masumbufu au changamoto za kujifunza mle kifungoni. Aliwaorodheshea wasikilizaji wake mlolongo mrefu wa watakatifu ambao walikuwa wamehukumiwa na majaji walio dhalimu. Karibu katika kila kizazi kulikuwepo na wale ambao wakati wanatafuta namna ya kuwafahamisha watu wakati wao kwa kuwainua, walidhihakiwa na kutupwa nje, ila katika nyakati za baadaye walionekana kuwa wanastahili heshima. Kristo Mwenyewe alihukumiwa kama mtenda mkosaji/mhalifu katika mahakama isiyo ya haki. [GC 112.4; PK Aya ya 43]

Wakati wa awali alipoikana imani, Jerome alikuwa amekubaliana na hukumu ya Huss kuwa ya haki; ila sasa alitangaza toba yake na kushuhudia kutokuwa na hatia kwake, na utakatifu wa mfia dini Huss. “Nilimjua tangu utoto wake,” alisema. “Alikuwa mtu mwema sana, mwenye haki na mtakatifu; alihukumiwa, ingawa hakuwa na hatia. Mimi pia, niko tayari kufa: sitarudi nyuma kwasababu ya mateso ambayo yameandaliwa kwa ajili yangu na maadui zangu na mashahidi wa uongo ambao siku moja watalazimika kutoa hesabu ya uovu wao mbele ya Mungu mkuu, ambaye Yeye hawezi kudanganywa na chochote.”—Bonnechose, vol. 2, uk. 151. [GC 113.1; PK Aya ya 44]

Kwa kujilaumu mwenyewe kwa kuukana Ukweli, Jerome aliendelea: “Miongoni mwa dhambi zote ambazo nimezifanya tangu ujana wangu, hakuna hata moja inayolemea akili yangu uzito mkubwa na kunisababishia majuto ya kusikitisha kama ile niliyofanya mahali hapa pa mauaji, Nilipoidhinisha hukumu ya uongo iliyotolewa dhidi ya Wycliffe, na dhidi ya shahidi mfia dini yule mtakatifu John Huss, bwana wangu na rafiki yangu. Ndio! Ninaiungama dhambi yangu kwa dhati kutoka moyoni mwangu na ninatangaza kwamba niliteteteka kwa sababu ya hofu ya kifo kile kilichonikabili, nikalaani mafundisho yao. Kwa hivyo ninaomba---- Mungu Mweza wa Yote anihurumie na akubali kunisamehe dhambi zangu, na hasa dhambi hii moja iliyo mbaya zaidi ya zote.” Akisonda kidole kwa majaji wake, alisema kwa kukazia: “Mliwahukumu Wycliffe na John Huss, si kwa sababu ya kutikisa mafundisho ya kanisa, bali kwa sababu tu walipinga tabia za aibu na ufisadi zinazoendelea kwa makasisi-- yaani majivuno yao (kujigamba), kujikweza kwao na maovu yote ya maaskofu na mapadre.

Mambo ambayo waliyathibitisha na ambayo hayawezi kukanushwa, mimi pia ninafikiri na kusema hivi kama hao wenzangu walivyofanya.” [GC 113.2; PK Aya ya 45]

Maneno yake yalikatizwa. Maaskofu hao wakitetemeka kwa ghadhabu kali, walipiga kelele wakisema: “Kuna haja gani ya ushahidi zaidi? Kwa macho yetu tunaona mzushi aliye mkaidi, na sugu zaidi ya wote!” [GC 114.1; PK Aya ya 46]

Bila kushtushwa na shambulio hilo, Jerome alisema: “Je! Mnafikiri kwamba ninaogopa kufa? Mmenifungia kwa mwaka mzima kwenye gereza la kuogofya chini ya ardhi, ambalo ni la kutisha zaidi kuliko kifo chenyewe. Mmenitendea kwa unyama zaidi kuliko Mturuki, Myahudi au mpagani na nyama za mwili wangu zimeoza na zinakuwa kama zinatoka kwenye mifupa ningali hai; na bado silalamiki, kwani kulalamika na kuomboleza si fungu la mtu jasiri na mwenye imani; lakini siwezi kujizuia kuacha kuelezea mshtuko wangu wa unyama huo mkubwa mnaoufanya dhidi ya Mkristo.”- Ibid., vol. 2, uk. 151-153. [GC 114.2; PK Aya ya 47]

**Apewa Kifungo Na Kungojea Kuuawa**

Ghadhabu ya hasira ikalipuka tena, na Jerome akafurumushwa na kupelekwa haraka gerezani. Lakini kulikuwa na wengine katika mkutano ambao maneno yake yalikuwa yamewagusa sana na ambao walitamani kuokoa maisha yake. Alitembelewa na wakuu wa kanisa na akahimizwa ajisalimishe kwenye baraza lile. Ahadi za zawadi nzuri sana zilitolewa kwake kama tuzo ya kuukana upinzani wake kwa Rumi. Lakini kama ilivyokuwa kwa Bwana Wake alipopewa utukufu wa ulimwengu na shetani akakataa, Jerome alibaki kuwa imara. [GC 114.3; PK Aya ya 48]

“Nithibitishie kutoka kwenye Maandiko Matakatifu kuwa nina makosa,” akasema, “nami nitatoa kiapo cha kuyakana.” [GC 114.4; PK Aya ya 49]

“Maandiko Matakatifu!” mmoja wa wale waliomjaribu alimshangaa, “Hivi Kila kitu kinatakiwa kupimwa kwa hayo? Ni nani basi anayeweza kuyaelewa hayo isipokuwa kanisa limeyatafsri?” [GC 114.5; PK Aya ya 50]

“Je! Mapokeo ya wanadamu yana thamani na yanapaswa kuaminiwa katika imani kuliko injili ya Mwokozi wetu?” alihoji Jerome. “Paulo hakuhimiza wale ambao aliwaandikia wasikilize mapokeo ya wanadamu, bali alisema, “Yachunguzeni Maandiko.” [GC 114.6; PK Aya ya 51]

“Mzushi wee!” akazomewa, “Ninajuta kwa kukubembeleza muda mrefu wewe. Ninaona kwamba unasukumwa na yule mwovu.”- Wylie, b. 3, [GC 114.7; PK Aya ya 52]

Baada ya muda usio mrefu hukumu yake ilitangazwa. Naye akaongozwa nje kwenda mahali palepale ambapo Huss alikuwa ameyatoa maisha yake. Alienda akiimba njiani, sura yake ikiwa imeng'aa kwa furaha na amani. Macho yake yalikazwa kwa Kristo, na kwake kifo kilikuwa kimepoteza utisho wake. Wakati muuaji alipokaribia kuwasha rundo la kuni za kumchomeeа moto, alisimama nyuma yake, mfia dini huyu alisema: “Njoo mbele kwa ujasiri; washa moto mbele ya uso wangu. Endapo ningekuwa naogopa, nisingekuwa hapa.” [GC 114.8; PK Aya ya 53]

Maneno yake ya mwisho, aliyosema wakati moto ukipanda juu yake, yalikuwa ni ombi. “Bwana, Baba Mwenyezi,” akalia, “unihurumie, na unisamehe dhambi zangu; kwa kuwa unajua kuwa nimeipenda Kweli Yako siku zote.”- Bonnechose, vol. 2, uk. 168. Sauti yake ikakoma, lakini midomo yake iliendelea kujongea kwa maombi. Wakati moto ulipomaliza kazi yake, majivu ya yule shahidi mfia dini, pamoja na udongo ambao ulikuwa umekaa juu yake, vilikusanywa kama vile alivyofanyiwa Huss, na kutupwa ndani ya mto Rhine. [GC 115.1; PK Aya ya 54]

Hivyo ndivyo wale wabeba nuru waaminifu wa Mungu walivyoangamia. Lakini nuru ya Ukweli ambao waliutangaza-- nuru iliyotokana na mfano wao wa kishujaa--isingeweza kuzimwa. Kama vile watu wasivyoweza kulirudisha jua nyuma katika mwendo wake ili kuzuia machweo ya siku hiyo, ndivyo ambavyo hata wakati ule hawakuweza kuzuia mapambazuko ya siku ile ambayo yalikuwa yakitokea kwenye ulimwengu. [GC 115.2; PK Aya ya 55]

### Vita Katika Nchi Ya Bohemia

Kuuwawa kwake Huss kulikuwa kumewasha mwali wa moto wa ghadabu kali na utisho mkubwa huko Bohemia. Jambo likaugusa moyo wa taifa lote kwamba alikuwa ameangukia kifo kwasababu ya hila na chuki za mapadre pamoja na usaliti wa yule mfalme aliyekuwa madarakani. Alitangazwa kuwa alikuwa mwalimu mwaminifu wa Ukweli na baraza ambalo lililoamuru kifo chake likashtakiwa kwa hatia ya mauaji. Mafundisho yake sasa yalivutia watu zaidi kuliko hapo awali. Kwa amri ya papa maandishi ya Wycliffe yalipaswa kuchomwa moto. Lakini yale maandishi ambayo yalikuwa yameponea chupuchupu kuharibiwa, sasa yalitolewa mafichoni mwao na wakajifunza kuyasoma wakiyahusianisha na Biblia, au sehemu zake ambazo watu wangeweza kuzipata na kwa hivyo wengi waliongozwa kukubali imani iliyofanyiwa matengenezo. [GC 115.3; PK Aya ya 56]

Wauaji wale wa Huss hawakuweza kukaa kimya na kushuhudia ushindi wa kazi yake. Papa na mfalme yule wa dola waliungana kuzima harakati hizo na majeshi ya Sigismund yalipelekwa Bohemia. [GC 115.4; PK Aya ya 57]

Lakini mkombozi wao aliinuliwa. Ziska, ambaye mara tu baada ya kuanza kwa vita ile alipofuka macho kabisa, alikuwa mmoja wa majenerali hodari wa enzi zake, naye ndiye alikuwa kiongozi wa Wabohemia. Akiutegemea msaada wa Mungu na kusudi lao la haki ya kazi yao, watu hawa waliweza kuyapinga majeshi yenye nguvu ambayo yaliletwa dhidi yao. Tena na tena mfalme aliandaa majeshi mapya kuivamia Bohemia, lakini yakawa yakirudishwa nyuma na kushindwa kwa aibu kubwa. Wafuasi wa Huss (Wahuss) waliinuliwa juu kuishinda hofu ya kifo, na hakuna chochote kilichoweza kusimama dhidi yao. Miaka michache baada ya kuanza kwa vita, jasiri Ziska alifariki; lakini nafasi yake ilijazwa na Procopius, ambaye alikuwa jenerali jasiri na mwenye stadi na ujuzi wa vita sawa na ule wa Ziska, na kwa vipengele fulani, alikuwa kiongozi shupavu na mwenye stadi zaidi. [GC 116.1; PK Aya ya 58]

Maadui wale wa Wabohemia, wakijua fika kuwa shujaa kipofu wa vita amekufa, waliona wamepata fursa hiyo kuwa nafasi nzuri ya kurejesha yote waliyoyapoteza huko nyuma. Papa alitangaza vita 'takatifu au vita vya msalaba' dhidi ya Wahuss (krusedi) na kisha nguvu kubwa ya kijeshi ikaelekezwa Bohemia, lakini walishindwa vibaya sana. Vita nyingine takatifu ikatangazwa. Wanaume, pesa na vifaa vya vita vilichangishwa Katika nchi zote zilizokuwa chini ya upapa za Ulaya. Umati wa watu ulimiminika kwa idadi kubwa, upande wa bendera ile ya papa, naye akawahakikishia kukomeshwa kwa wale wazushi wa Huss, akisema muda ulikuwa umewadia. Wakiwa na ujasiri na imani ya kupata ushindi, kikosi cha jeshi kubwa kiliingia Bohemia. Watu wa Bohemia wakashonana ili kuwafukuza warudi nyuma. Majeshi hayo mawili yakazidi kusogeleana hadi pale ambapo mto tu ndio uliokuwa unawatenganisha. "Jeshi la watesi au askari wa msalaba (krusedi) lilikuwa kubwa na lenye nguvu zaidi, lakini badala ya kwenda mbio ili kuvuka ule mto, na kuanza kupigana dhidi ya Wahuss ambao walitoka mbali sana ili kukutana nao, walisimama kimya wakiwaangazia macho yao wale wapiganaji." - Wylie, b. 3, sura ya 17. Hapo ndipo kwa ghafla hofu kuu ya kushangaza ikaliangukia jeshi lile la wapiganaji wa msalaba (crusade). Bila kupata kipigo chochote, lile jeshi kubwa lilisambaratika na kutawanyika kana kwamba lilikuwa linafukuzwa na nguvu isiyoonekana kwa macho. Idadi kubwa ya wanajeshi wao wakauwawa na jeshi la Wahuss, ambao waliwafukuza mateka, na nyara nyingi zikaangukia mikononi mwa washindi hawa, badala ya vita ile kuwaletea umaskini, iliwatajirisha Wabohemia. [GC 116.2; PK Aya ya 59]

Miaka michache baadaye, chini ya papa mwingine mpya, vita vingine vitakatifu au vya msalaba (Krusedi), vikaanza tena. Kama ilivyokuwa awali, watu pamoja na mali vilikusanywa kutoka katika nchi zote za kipapa za Ulaya. Zawadi na vivutio vingi vikaahidiwa kwa wale ambao wangeshiriki katika shughuli ya uhalifu huu wa hatari. Msamaha kamili wa uhalifu huu wa kuogofya zaidi ulihakikishwa kwa kila mpiganaji wa krusedi au vita vya msalaba. Wote waliokufa

vitani waliahidiwa thawabu kubwa kule mbinguni na wale walionusurika waliahidiwa kuvuna heshima na utajiri kutoka katika uwanja wa vita. Jeshi kubwa liliandaliwa tena na wakavuka mpaka wakaingia Bohemia. Vikosi vile vya Wahuss vikarudi nyuma yao, ili kwa njia hiyo wapate kuwavuta wavamizi wale kuingia zaidi na zaidi ndani ya nchi, na kuwafanya waone kuwa ushindi wao umekwisha kupatikana. Mwishowe jeshi la Procopius likasimama na kuwageukia maadui zao ili kupigana nao. Basi wale wapiganaji watesi (wanakrusedi) walipogundua makosa yao, walirejea kujificha katika kambi lao wakisubiri mashambulizi tena. Wakati mvumo wa sauti ya nguvu ya majeshi ilivyokuwa inakaribia na kusikika hata kabla ya wafuasi wa Huss kuonekana, hofu ikawashika tena (panik) wale wanajeshi wanaopigana vita vya msalaba, Wakuu au wana wa wafalme, makamanda/majenerali, na askari wa kawaida, walitupa silaha zao, kisha wakakimbia kila upande. Jitihada za kiongozi wa uvamizi ambaye alikuwa mwakilishi wa papa, zikawa ni kazi bure katika kukusanya majeshi yake yaliyojaa hofu na yaliyosambaratika. Licha ya juhudi yake kubwa, yeye mwenyewe alifagiliwa mbali na wimbi la wakimbizi. Maangamizi yale yakawa yamekamilika, na kwa safari nyingine tena ushindi mkubwa ulikuwa mikononi mwa Wabohemia. [GC 116.3; PK Aya ya 60]

Hivyo kwa mara ya pili jeshi kubwa sana, lililotumwa na mataifa yenye nguvu zaidi huko Ulaya, majeshi yenye watu mashujaa, watu walio wazoefu wa vita, waliopewa mafunzo kwa kuandaliwa vyema na kuwa na vifaa vya vita vyenye uwezo, wakakimbia bila hata kupata kipigo kimoja mbele ya watetezi wa taifa lile dogo na dhaifu. Hapo kulikuwa na udhihirisho wa uweza wa Mungu. Wavamizi hao walipatwa na hofu isiyomithilika kibinadamu. Yeye aliyeyachapa na kuyashinda majeshi ya Farao katika Bahari ya Shamu, Yeye aliyeyakimbiza majeshi ya Midiani mbele ya Gideoni na watu wake mia tatu, Yeye ambaye kwa usiku mmoja aliyanyenyekeza majeshi ya Waashuri waliojiamini, sasa alikuwa ameunyosha tena mkono Wake ili kunyausha nguvu za udhalimu. "Hapo waliingiwa na hofu pasipokuwapo hofu, Maana Mungu ameitawanya mifupa yake aliyekuhusuru. Umewatia aibu, Kwa sababu MUNGU amewadharau." Zaburi 53:5. [GC 117.1; PK Aya ya 61]

**Watumia Mbinu Za Diplomasia**

Hatimaye viongozi wa upapa, wakiwa wamekata tamaa ya kushinda kwa kutumia nguvu za majeshi, waliamua kutumia diplomasia *(werevu wa kufikia mahusiano mazuri ili kufanikisha ajenda yao—maridhiano)*. Maafikiano yakafanywa, wakiwa katika mapatano, wakajidai kana kwamba wanawapa wale watu wa Wabohemia uhuru wa dhamiri zao (wakawaambia wanaweza kumwabudu Mungu wapendavyo), na kumbe kiuhalisia walikuwa wakiwasaliti na kuwaweka chini ya mamlaka ya Rumi. Wabohemia waliweka mambo manne kama masharti ambayo

walikuwa wameyabainisha katika kufanya amani na Rumi: uhuru wa kuihubiri Biblia; haki ya kanisa lote kushiriki mkate na kunywa divai wakati wa ushirika mtakatifu (komunio), na matumizi ya lugha ya kuzaliwa katika kuendesha huduma ya ibada; kuwaondoa viongozi wote wa kanisa kutoka kwenye vyeo vya kiraia (serikali za kidunia); na panapotokea kesi za uhalifu yaani makosa ya jinai, mahakama za kiraia ndiyo ziwe mamlaka ya juu kwa viongozi wa kidini na walei bila ya kubagua. Hatimaye mamlaka ya upapa "Iliafikiana na vile vipengele vinne vya Wahuss vikubaliwe, ila haki ya kuvifafanua, yaani, kuamua utekekelezaji na maana yake halisi ni nini, ingebaki mikononi mwa baraza hili - kwa maneno mengine, ingebaki mikononi mwa papa na mfalme wa dola."- Wylie, b. 3, sura ya 18. Kwa msingi huo mapatano yakafikiwa, na mkataba ukawekwa na kanisa la Rumi likafanikiwa kwa njia hiyo ya unafiki (kujifanya) na udanganyifu, kupata kile ambacho ilishindwa kukipata kwa njia ya mapambano; kwani, kwa Rumi kuweka tafsiri yake mwenyewe juu ya kanuni zile za wafuasi wa Huss, kama ilivyokuwa kwenye Biblia, Rumi ingeweza kupotosha maana yake halisi ili kukidhi makusudi yao mwenyewe. [GC 118.1; PK Aya ya 62]

Kundi kubwa la watu huko Bohemia, lilipoona wazi kusalitiwa huko kwa uhuru wao kutokana na mapatano yale, halikukubali kuafikiana na mkataba ule. Mabishano, upinzani na mafarakano yalitokea, na kusababisha ugomvi ulioleta vita vya umwagaji damu miongoni mwao wenyewe kwa wenyewe. Katika migogoro hii, Procopius shujaa bora alianguka na uhuru wa Bohemia uliangamia. [GC 118.2; PK Aya ya 63]

Sigismund, msaliti wa Huss na Jerome sasa alikuwa mfalme wa Bohemia, na licha ya kiapo chake alichotoa cha kuunga mkono haki za Wabohemia, akaendelea kuimarisha upapa. Lakini alinufaika kidogo tu kwa kujisalimisha kwake kwa Rumi. Kwa miaka ishirini, maisha yake yalikuwa yamejaa kazi ngumu, mahangaiko, hatari na majanga mengi. Vikosi vyake vya jeshi vilikuwa vimedhoofika na hazina zake zikakaushwa katika mapambano ya muda mrefu na yasiyo na matunda; na sasa, baada ya kutawala mwaka mmoja, alikufa, akiachia ufalme wake kwenye ukingo wa vita vya wenyewe kwa wenyewe na akirithisha kizazi kijacho jina lile lililotiwa jina baya. [GC 118.3; PK Aya ya 64]

Ghasia, migogoro, na umwagaji damu viliendelea kwa muda mrefu. Majeshi ya kigeni yakavamia tena Bohemia na mafarakano/upinzani wa ndani ukazidi kulisumbua taifa lile. Wale walioendelea kuwa waaminifu kwa injili waliteswa kwa mateso yaliyosababisha umwagaji wa damu. [GC 118.4; PK Aya ya 65]

### Kanisa Tofauti Likaanzishwa

Kama ilivyokuwa kwa ndugu zao wa awali, waliingia katika muungano na kanisa la Rumi, walipoyapokea makosa yao na kuyahifadhi, ndipo wale walioshikilia imani ya zamani (ya mitume) wakawa wamejitenga na kwenda

kuunda kanisa tofauti linalojitegemea, wakitumia jina la “Umoja wa Ndugu au Ndugu pamoja- United brethren.” Kitendo hiki kilikaribisha laana kutoka tabaka zote za watu kujongea kwao. Lakini msimamo wao haukumangamanga huku na kule. Pale walipolazimika kutafuta kimbilio katika misitu na mapango, bado waliendelea kukusanyika na kusoma Neno la Mungu na kuungana katika ibada kwa Mungu. [GC 119.1; PK Aya ya 66]

Kupitia wajumbe wao waliotumwa kwa siri katika nchi mbalimbali, waligundua kwamba hapa na pale kulikuwa na wale watu “walioikiri ile Kweli wakiwa wamekaa mahali pa upweke na palipojitenga, wachache katika jiji hili na wachache katika jiji lile, wakiwa walengwa wa mateso kama wao; na kwamba katikati ya milima ya Alps (Uswisi) kulikuwa na kanisa la zamani, lililokuwa limejengwa juu ya msingi wa Maandiko nalo lilipinga ufisadi na upotofu wa ibada ya sanamu ya kanisa la Rumi.” Wylie, b. 3, sura ya 19. Upelelezi ule ukapokelewa kwa furaha kubwa na mawasiliano yakaanzishwa na Wakristo wa Kiwaldensia. [GC 119.2; PK Aya ya 67]

**Kungojea Mapambazuko**

Wakiwa wamesimama imara katika injili, Wabohemia wale wakangoja katika usiku wao wa mateso, katika wakati ule wa giza nene sana, waligeuza macho yao mawinguni kama watu wanaokesha wakiingojea asubuhi. “Sehemu yao iliwaangukia katika siku ile mbaya ya uovu, lakini ….. waliyakumbuka maneno yaliyotamkwa hapo awali na Huss, na kurudiwa na Jerome, kwamba karne ile ilikuwa haina budi kupita kabla ya kupambazuka kwa ule usiku. Maneno hayo kwa wale Watabori (Wahuss) kama maneno ya Yusufu yalivyokuwa kwa makabila ya Israeli katika nyumba ya utumwa: “Mimi ninakaribia kufa. Lakini kwa hakika Mungu atawasaidia na kuwachukueni kutoka nchi hii”—Ibid., B. 3, sura ya 19. “Kipindi cha mwisho cha karne ya kumi na tano kilishuhudia ongezeko la polepole lakini la uhakika la makanisa ya umoja wa Ndugu (Churches of the Brethren). Ingawa hawakukosa kusumbuliwa, bado walifurahia utulivu linganifu. Mwanzoni mwa karne ya kumi na sita makanisa yao yalifika mia mbili huko Bohemia na Moravia.”- Ezra Hall Gillett, Life and Times of John Huss, vol. 2, p. 570. “kukawa na idadi nzuri ya ‘masalio’, nao wakiwa wamenusurika maangamizi makali ya moto na upanga, walijaliwa kuyaona mapambazuko ya siku ile ambayo Huss alikuwa ameitabiri.” - Wylie, b. 3, sura ya 19. [GC 119.3; PK Aya ya 68

# SURA YA 7

# KUJITENGA KWA LUTHER KUTOKA RUMI

## (Mtu Aliyekuja Kwa Wakati Wake Kusaidia Kuongeza Uelewa Wa Maarifa Ya Mungu Katika Giza Lililokuwepo 1483-1521BK)

Ufupisho: Shujaa aliyekuwa mbele katika kuliongoza kanisa kwenye matengenezo alikuwa si mwingine ila Martin Luther, Mtu mnyenyekevu ila asiye na hofu ya vitisho. Aliingia utawa 1505, na kuwekewa mikono ya upadre mwaka 1507 naye akaanza kufundisha Chuo Kikuu cha Wittenberg mwaka uliofuatia. Oktoba 31, 1517 aliweka yale matamako au hoja 95 mashuhuri zihusuzo Indulgensia kwenye malango ya kanisa la Wittenburg, Ujerumani. Walikutana na Rafiki yake Melachthon Tangazo liitwalo Bulla la Papa Leo X la kusema ni mzushi lilitamkwa 1521.

Miongoni mwa wale walioitwa na aliyekuwa maarufu zaidi ya wote katika kuliongoza kanisa kutoka katika giza lile la upapa ili kulielekeza kwenye nuru ya imani safi zaidi, alikuwa Martin Luther. Akiwa mtu mwenye bidii na ari/usongo na aliyejitoa wakfu, huyu hakuwa na hofu yoyote isipokuwa hofu ya kumcha Mungu, naye hakukubaliana na msingi mwingine wowote wa imani ya kidini isipokuwa ule uliojengwa juu ya Maandiko Matakatifu peke yake. Luther alikuwa ni mtu wa pekee wa wakati wake; kupitia kwake yeye, Mungu alikamilisha kazi kubwa kwa ajili ya matengenezo ya kanisa na kutoa nuru kwenye ulimwengu mzima. [GC 120.1; PK Aya ya 1]

Kama watangazaji injili wa awali, Luther alichipuka kutoka kwenye safu ya familia iliyokuwa maskini. Miaka yake ya awali ilitumika katika nyumba ya kimaskini/nyenyekevu ya mkulima mdogo wa Kijerumani. Kwa kuhenyeka na kazi ngumu kila siku kama kibarua katika machimbo ya madini, baba yake aliweza kujipatia fedha kwa ajili ya elimu yake. Alinuia mwanawe awe mwanasheria; lakini Mungu alikusudia kumfanya awe mjenzi wa hekalu kuu ambalo lilikuwa likiinuka juu polepole kupitia vipindi vya karne zote. Ugumu wa maisha, ufukara na nidhamu kali ndivyo vilikuwa shule ambayo ndani yake ile Hekima Isiyo na ukomo ilimwandaa Luther kwa ajili ya utume muhimu katika maisha yake. [GC 120.2; PK Aya ya 2]

Baba yake Luther alikuwa mwenye akili nyingi (uelewa mkubwa) na inayofanya kazi kwa utendaji bora, uadilifu mkubwa wa tabia, uaminifu, msimamo imara, ushupavu na unyofu wa moyo. Alikuwa mtu aliyesimamia kile

alichosadiki kwenye dhamiri yake kuhusiana na majukumu bila kujalisha kwamba matokeo yangekuwaje. Busara yake nzuri ilimwongoza kuuangalia ule mfumo wa watawa kwa mashaka. Alichukizwa sana wakati Luther alipoingia kwenye utawa bila idhini yake; na ilichukua miaka miwili baadaye kabla baba yake kupatanishwa na mwanaye na hata wakati huo maoni yake yalibaki vile vile. [GC 120.3; PK Aya ya 3]

Wazazi wa Luther waliweka umakini mkubwa sana juu ya elimu na mafunzo ya watoto wao. Walijibidisha katika kuwafundisha kujua Neno la Mungu na kanuni za maisha ya Kikristo. Sala za baba zilipanda juu daima kwa Bwana nazo zikisikika kwa mwana wake huyu kwamba alikumbuke Jina la Bwana na siku moja awe msaada katika kuiendeleza Kweli Yake. Kila fursa kwenye malezi/makuzi ya kimaadili au kiakili ambayo maisha yao ya mahangaiko magumu yaliwaruhusu kufurahia, iliboreshwa vyema na wazazi hawa. Jitihada zao zilikuwa za dhati na zenye ustahimilivu ili kuwaandaa watoto wao kwa ajili ya maisha ya uchaji Mungu, manufaa maishani. Pamoja na uimara wao na uadilifu wa tabia, walitumia ukali mwingi kupita kiasi; Japokuwa Mwanamatengenezo mwenyewe alitambua kwamba katika matukio fulani wazazi wake walikosea, aliona mengi ya kukubalina nayo na kuenzi kuliko ya kulaumu katika malezi yao. [GC 121.1; PK Aya ya 4]

Alipelekwa shuleni akiwa na umri mdogo. Luther alitendewa kwa ukali, na mabavu na hata kwa ukatili wakati mwingine. Umaskini wa wazazi wake ulikuwa mkubwa sana kiasi kwamba akiwa anatoka nyumbani kwenda shule iliyopo mji mwingine kuna wakati alilazimika kuimba kutoka nyumba moja hadi nyingine ili kupata chakula kama wanavyofanya 'ombaomba' na mara nyingi alishinda na njaa. Mawazo yaliyojaa huzuni na yaliyo na ushirikina na upotofu yalikuwa yakitawala wakati ule, nayo yalimjaza hofu. Mara nyingi alilala usiku akiwa na moyo uliosononeka, akitazamia siku zijazo zenye giza kwa kutetemeka kwa sababu ya wakati ujao wa giza na kuwa katika hofu wakati wote kwa wazo kwamba Mungu ni hakimu mkali, asiye na huruma, na dikteta katili, badala ya kumwona kama Baba Yake wa mbinguni, Mwenye huruma. [GC 121.2; PK Aya ya 5]

Licha ya kuwa chini ya mambo mengi na makubwa yanayovunja moyo, Luther alisonga mbele kwa msimamo thabiti kuelekea mbele kwenye kiwango cha juu cha ubora wa kimaadili na kiakili jambo ambalo liliuvutia sana moyo wake. Alikuwa na kiu ya maarifa, unyofu na utendaji wa tabia wa akili yake, navyo vikamwongoza kuyatamani mambo yale yaliyokuwa imara na yenye manufaa kuliko yale ya kujionyesha tu, na ya juu juu. [GC 121.3; PK Aya ya 6]

Wakati akiwa na umri wa miaka kumi na nane, alijiunga na Chuo Kikuu cha Erfurt, hali yake ilikuwa ya kuridhisha zaidi, na matarajio yake ya siku zijazo yakawa angavu na bora zaidi kuliko miaka yake ya awali. Wazazi wake

waangalifu katika kubana matumizi na kuchapa kazi, walijipatia uwezo wa kumpa msaada wote aliouhitaji. Kisha mvuto wa marafiki zake wenye busara ulikuwa umepunguza makali kwa kiasi fulani matokeo ya kuhuzunisha ya mafunzo yake yale ya kwanza. Alijituma kwa nguvu nyingi kujifunza mambo yaliyoandikwa na waandishi bora, kwa bidii aliiweka hazina ya mawazo yao mazito moyoni mwake, na kuifanya hekima ya wale wenye hekima kuwa yake mwenyewe. Pamoja na nidhamu ile kali ya malezi ya wakufunzi wake wa awali, alikuwa ameonyesha mapema tumaini la kujipatia sifa kubwa, na chini ya mivuto ifaayo iliyokuwa imemzunguka, akili yake ilikua kwa haraka sana. Uwezo wake wa kukumbuka mambo, kuelewa upesi, na kutafakari na kufikiria yale asiyoweza kuyaona kwa macho na ubunifu (imagination), nguvu kubwa za kupembua mambo na kuhoji, na kuyashugulikia hayo yote kiutendaji bila kuchoka vilimweka katika ngazi ya juu miongoni mwa wenzake. Nidhamu yake ya kiakili ikakomaza uelewa wake na ufahamu wake na kuamsha utendaji wa akili yake kwa ule umakini ulionolewa katika kuelewa mambo, jambo ambalo lilimwandaa kwa ajili ya migogoro ya maisha yake. [GC 121; PK Aya ya 7]

Hofu ya Bwana, yaani uchaji wa Mungu ulikaa ndani ya moyo wa Luther, ukimuwezesha kudumisha uimara wa kusudi lake na kumwongoza kwenye kusudi lake la kumfanya awe mnyenyekevu sana mbele za Mungu. Daima alihisi upungufu ndani yake, hivyo akamtegemea Mungu kuwa msaada wake, naye hakukosa kuianza siku yake bila sala, wakati moyo wake ulikuwa ukipumua dua kila wakati ili apate mwongozo na msaada. “Kuomba vizuri,” alisema mara nyingi, “ndiyo nusu bora ya somo” (1/2 kuomba, 1/2 kusoma kwa kuichunguza Biblia na umakini ndiyo hufanya kitu kizima).” D'Aubigne, b. 2, sura ya 2. [GC 122.1; PK Aya ya 8]

Siku moja alipokuwa anasoma kwa umakini vitabu vya maktaba ya chuo kikuu, Luther aliigundua Biblia ya Kilatini. Kitabu kama kile alikuwa hajapata kukiona kabla ya hapo. Alikuwa hajui kama kitabu kama hicho kipo duniani. Alikuwa amesikia sehemu za Injili na Nyaraka ambazo zilisomwa kwa watu kwenye ibada ya hadhara na alidhani kwamba hizo ndizo Biblia nzima (yote). Sasa, kwa mara yake ya kwanza, alikuwa analitazama Neno lote la Mungu. Kwa kicho, butwaa na mshangao, alizifungua kurasa zake takatifu; wakati mapigo ya moyo yakienda kwa kasi, na kudunda- dunda kwa nguvu, akajisomea kwa macho yake mwenyewe Maneno ya uzima, akipumzika hapa na pale na kusema kwa sauti ya mshangao: “Laiti kama Mungu angenipa kitabu kama hiki kwa ajili yangu mwenyewe!” Ibid., b. 2, sura ya 2. Malaika wa mbinguni walikuwa kando yake na miale ya nuru kutoka katika kiti cha enzi cha Mungu ilimfunulia hazina ya ile Kweli ili aweze kuelewa. Daima yeye alikuwa mwoga kumkosea Mungu, lakini sasa aliguswa ndani ya moyo wake kwa usadikisho wa kina ambao hajapata kuwa

nao kabla ya wakati ule kuhusu hali yake halisi ilivyo, naye akaamini fika kwamba yeye alikuwa ni mwenye dhambi. [GC 122.2; PK Aya ya 9]

**Kuwa Na Amani Na Mungu**

Shauku ya dhati ya kutaka kuwa huru na dhambi, na kupata amani mbele za Mungu vilimwongoza kuingia katika nyumba ya watawa na kutoa maisha yake wakfu ili aishi maisha ya kitawa. Mle alilazimika kufanya kazi duni na ngumu sana, zenye kuchosha, na kuwa ombaomba aendaye nyumba kwa nyumba. Alikuwa amefikia umri ule ambao kwa kawaida watu hutamani sana heshima, kuthaminiwa na kukubalika kwa hamu kubwa, na sasa shughuli zile za kudhalilisha, yaani zisizokuwa na cheo au hadhi kubwa, zilikuwa zinaumiza sana hisia zake za moyo wa asili; lakini kwa saburi alistahimili ile fedheha yake, akiamini kwamba ilikuwa sharti apitie njia hiyo kwa sababu ya dhambi zake. [GC 123.1; PK Aya ya 10]

Kila muda alioweza kujipatia baada ya majukumu yake ya kila siku aliutumia katika kusoma, akijinyima usingizi na hata akaona kijicho kwa ule muda alioutumia katika kula chakula chake kile kidogo. Alifurahia kujifunza Neno la Mungu zaidi ya mambo mengine yote. Alikuwa ameiona Biblia iliyofungwa kwa minyororo kwenye ukuta wa nyumba ya watawa, na mara kwa mara alienda kupumzika hapo. Kwa kadri hisia zake zilivyomshawishi kuwa yeye ni mwenye dhambi, ndivyo alivyozidi kutafuta kwa matendo yake mwenyewe kupata msamaha wa dhambi na amani. Aliishi maisha magumu ya kujitesa sana, akijitahidi kudhibiti uovu uliokuwa katika silika yake kwa njia ya kufunga, kukesha kwa kuwa macho usiku kucha, na kujichapa mijeledi kuitawala asili yake ya uovu, na haya yote hayakumletea nafuu yoyote katika maisha yake ya kitawa. Hakupiga chenga au kuepa kujitoa mhanga kwa njia yoyote ile ambayo kwayo angeweza kujipatia usafi wa moyo ambao ungemwezesha kupata kibali cha kusimama mbele za Mungu. "Hakika mimi nilikuwa mtawa mcha Mungu," alisema baadaye, "tena nilifuata taratibu na kanuni za mtawa kwa ukali na umakini sana kuliko niwezavyo kueleza. Endapo mtawa angeweza kuipata mbingu kwa kazi au matendo yake ya kitawa, basi, hakika mimi ningekuwa na haki ya kuipata mbingu ……Ikiwa ningeendelea nayo maisha yale kwa muda mrefu zaidi, basi, ningekuwa nimeutesa vibaya mno mwili wangu hata kufikia hatua ya kujiua mimi mwenyewe." bid., b. 2, sura ya 3. Kama matokeo ya nidhamu hiyo iliyomletea maumivu mengi alipoteza nguvu ya mwili na alipata shida ya mishtuko ya kuzimia wakati mwingine, jambo ambalo lilimletea madhara ambayo hayakuweza kupona kikamilifu. Lakini pamoja na juhudi zake zote, moyo wake uliokuwa umelemewa na mzigo mzito wa dhambi zake, haukuweza kupata afueni yoyote. Hatimaye aliufikia ukingo wa kukata tamaa. [GC 123.2; PK Aya ya 11]

Pale ilipoonekana kwa Luther kana kwamba amepoteza kila kitu au mambo yote yamekwenda kombo, Mungu alimwinua rafiki na msaidizi kwa ajili yake. Mcha Mungu Staupitz alilifunua Neno la Mungu Luther kwenye akili ya Luther kama lilivyo na kumwagiza asijiangalie mwenyewe, bali atazame mbali na nafsi yake, na kisha aache kabisa kutafakari juu ya adhabu ya milele kwa kuivunja sheria ya Mungu (Amri kumi) na amwangalie Yesu Mwokozi wake anayesamehe dhambi. “Badala ya wewe kujitesa mwenyewe kwa ajili ya dhambi zako, jidondoshe kabisa mikononi mwa Mkombozi. Mtumainie Yeye, itegemee haki ya maisha Yake, tegemea upatanisho wa kifo Chake.... Msikilize Mwana wa Mungu. Alifanyika mwanadamu (mwili) ili apate kukupa wewe uhakika wa kupata upendeleo wa Mungu.” “Mpende Yeye aliyekupenda wewe kwanza.” Ibid., kitabu cha 2, sura ya 4. Hivyo ndivyo alivyonena yule mjumbe wa rehema. Maneno yake yaliugusa sana ubongo wa Luther. Baada ya kufanya mapambano yake mengi dhidi ya makosa yake yaliyojengeka akili mwake kwa muda mrefu sana alikuwa amewezeshwa kushikilia na kuelewa Ukweli, na ndipo amani ikaingia katika roho yake iliyokuwa ikisumbuka sana. [GC 123.3; PK Aya ya 12]

**Apewa Uprofesa Pale Wittenberg**

Luther aliwekewa mikono ya upadirisho na akaitwa atoke kwenye nyumba ya kitawa ili awe profesa katika Chuo Kikuu cha Wittenberg. Hapa alijikita kwa nguvu zake zote kwenye kusoma Maandiko katika lugha zile za asili za Biblia (Kiebrania, Kiaramaiki na kigiriki). Akaanza kutoa mihadhara ya Biblia; na ndipo vitabu vya Zaburi, Injili, na Nyaraka viklifunguliwa na kufafanuliwa kwenye ufahamu wa makundi makubwa yaliyokuwa na shauku. Staupitz, rafiki yake na bosi wake, alimsihi sana apande kwenye mimbari na ahubiri Neno la Mungu. Luther akawa anasita-sita, akijiona hakustahili kuzungumza na watu kwa niaba Yake Kristo. Ilikuwa baada ya mvutano wa muda mrefu ndipo alipokubali ushawishi wa marafiki zake. Tayari yeye alikuwa na umahiri mkubwa katika Maandiko, na neema ya Mungu ilikuwa juu yake. Ufasaha wake wa kuzungumza uliwafanya wasikilizaji wake watekewe, na kisha uwazi na uwezo wake ambao kwa huo aliwasilisha Ukweli vilishawishi watu uelewa wao na ari (usongo) yake iligusa mioyo yao. [GC 124.1; PK Aya ya 13]

Luther bado alikuwa mtoto mwaminifu wa kanisa la upapa na wala hakuwa na wazo kwamba angekuwa kitu kingine tofauti. Kwa maongozi ya Mungu alikwenda kutembelea Rumi. Alishika njia yake na kuanza safari yake kwa miguu, akiwa analala kwenye nyumba za kitawa njiani. Alipofika katika nyumba moja ya watawa huko Italia alijawa na mshangao kwa utajiri, fahari na anasa alizozishuhudia. Wakiwa wamepewa mapato ya juu kama wafalme, watawa walikaa katika nyumba za fahari, wakijivika nguo za kitajiri na majoho ya gharama kubwa, nao walikula karamu ya vyakula vya gharama vya kila aina. Kwa

uchungu mkubwa, Luther alilinganisha eneo na mandhari hii na kujikana, na ugumu wa maisha yake mwenyewe. Akiwa ameingiwa na mashaka yaliyomtia uchungu moyo, Luther alilinganisha mandhari hii na ile na maisha yake mwenyewe ya kujikana nafsi na yenye ugumu. Alianza kupata mfadhaiko na kuchanganyikiwa katika mawazo yake. [GC 124.2; PK Aya ya 14]

Hatimaye akiwa mbali aliuona mji wenye vilima saba. Kwa hisia ya furaha, alijitupa kifudifudi kwenye ardhi na kisha akapiga kelele kwa mshangao: “Mji mtakatifu wa Roma, nakusalimu!” Ibid., b. 2, sura ya 6. Aliungia mji na kuyatembelea makanisa, akasikiliza hekaya za ajabu zilizotungwa na kurudiwa tena na tena na makasisi pamoja na watawa, wakitekeleza taratibu na maadhimisho yote yaliyohitajika. Kila mahali aliona matukio ambayo yalimjaza mshangao na hofu. Aliona uovu miongoni mwa tabaka zote za uongozi wa kanisa-makasisi nk. Alisikia mizaha ya aibu na michafu kutoka kwa maaskofu, naye akajazwa na hofu kuu kusikia matusi na makufuru yao ya kuogofya sana, hata wakati wa kuendesha Misa. Alipojichanganya na watawa na raia wa pale, alikutana na ulafi, kutokuwa na kiasi, ubaradhifu, ulevi, uasherati na kila aina ya ufisadi. Popote alipoweza kugeuka katika matembezi yake pale pahali patakatifu aliona kufuru tu. “Hakuna anayeweza kufikiri au kutia mawazoni mwake,” aliandika, “dhambi na matendo maovu sana yanayotendwa huku Rumi; ni sharti mtu ajionee kwa macho yake mwenyewe na kusikia kwa masikio yake mwenyewe ili aweze kusadiki. Hivyo wanao msemo uliozoeleka unaosema, ‘ikiwa kama kuna Jehanum, basi, Rumi imejengwa juu yake: huyo (Rumi) ni shimo la kuzimu itokako kila aina ya dhambi’ Ibid., b. 2, sura ya 6. [GC 124.3; PK Aya ya 15]

### Juu Ya Ngazi Ya Pilato

Kwa njia ya amri ya papa iliyokuwa imetolewa kwenye nyaraka hivi karibuni (decretalis), cheti cha msamaha wa dhambi kilikuwa kimeahidiwa na papa kwa wote ambao wangeweza kupanda kwa magoti yao “Ngazi ya Pilato,” ambayo ilisemekana kwamba Mwokozi alitelemkia juu yake alipotoka katika Ukumbi wa mahakama ya Kirumi (Praitorio), na ya kwamba kimiujiza ilisafirishwa kutoka Yerusalemu kwenda kule Rumi. Siku moja wakati Luther alipokuwa anaipanda ngazi ile kwa kicho na unyofu, sauti ya mngurumo kama wa radi ilisikika kwake kwa ghafla, alisikia kana kwamba inamwambia maneno haya: “Mwenye haki ataishi kwa imani.” Warumi 1:17. Mara hiyo hiyo alisimama mara moja na kuondoka kwa haraka, aibu na hofu kuu. Aya hii huu, haikupoteza nguvu yake moyoni mwake. Kuanzia wakati huu alielewa kwa wazi sana kuliko kabla ya hapo kosa na udanganyifu wa kutegemea matendo ya kibinadamu kujipatia wokovu, na umuhimu wa kuwa na imani thabiti katika wema (sifa) Wake Kristo. Macho yake yakawa yamefumbuliwa, nayo kamwe yasingeweza kufungwa tena katika kubaini madanganyo ya upapa. Alipougeuza uso wake kuelekea mbali na Roma, alikuwa

amegeuza moyo wake hivyo hivyo mbali na Roma, na kuanzia wakati ule ufa (mtengano) ukaendelea kuwa mkubwa zaidi na zaidi, mpaka hapo alipokata kabisa mambo yote yaliyomwunganisha na kanisa la kipapa. [GC 125.1; PK Aya ya 16]

Baada ya kurejea kwake kutoka Rumi, Luther alipata shahada ya uzamivu katika fani ya theolojia kutoka katika Chuo Kikuu cha Wittenberg *(Udaktari wa masomo ya theolojia ya Kikristo yaani Biblia, Mungu, na Huduma—Doctor of Divinity).* Sasa akawa huru kutumia muda wake kusoma Maandiko yale aliyoyapenda, jambo ambalo alikuwa hajapata kulifanya kabla ya hapo. Alikuwa ameweka nadhiri ya kitawa kujifunza kwa uangalifu na kulihubiri kwa uaminifu Neno la Mungu, siyo matamko tu au maneno na mafundisho ya mapapa, siku zote za maisha yake. Sasa yeye hakuwa mtawa wa kawaida tu au profesa, bali mpiga mbiu, yaani mjumbe aliyepewa mamlaka kuitangaza Biblia (kutangaza Neno la Mungu). Alikuwa amepewa wito kama mchungaji kulilisha kundi la Mungu ambalo lilikuwa na njaa na kiu ya Ukweli. Alitangaza kwa mkazo kwamba Wakristo hawapaswi kupokea mafundisho mengine yoyote isipokuwa yale ambayo yanajengwa kwenye msingi wa mamlaka ya Maandiko Matakatifu. Maneno hayo yaliugonga msingi wa ukuu wa upapa. Yalikuwa na kanuni kuu za Matengenezo ya kanisa. [GC 125.2; PK Aya ya 17]

Aliwasilisha ujumbe wa thamani mbele ya umati wa watu wenye shauku, nao walisikiliza kwa makini, na kuyakumbatia maneno yale. Kamwe mafundisho kama hayo hayakuwahi kuanguka kwenye masikio yao. Habari njema ya upendo wa Mwokozi, uhakika wa kupewa msamaha na amani kwa njia ya damu Yake ya upatanisho, vilifurahisha mioyo yao na kuamsha ndani yao tumaini la kupata uzima wa milele. Nuru ilikuwa imewashwa kule Wittenberg, ambayo miale yake ingeenea hadi sehemu zote za miisho ya dunia na ambayo ukali wa mng’ao wake ungeongezeka mpaka kufikia mwisho wa wakati. [GC 126.2; PK Aya ya 18]

Lakini nuru na giza haviwezi kupatana. Kati ya mafundisho ya Ukweli na ya makosa kuna mgogoro usioweza kusuluhishika. Kuunga mkono na kukitetea kimoja kati ya hivi ni kukishambulia na kukipindua chini kingine. Mwokozi wetu Mwenyewe alitangaza akisema: “Sikuja kuleta amani bali upanga.” Mathayo 10:34. Miaka michache baada ya kuanza kwa Matengenezo ya kanisa. Luther alisema hivi: “Mungu haniongozi tu, bali ananisukuma kwenda mbele. Ananibeba na kunipeleka mbali. Mimi siyo bosi wangu mwenyewe (Mimi sijitawali nafsi yangu mwenyewe). Natamani sana kuishi kwa amani/utulivu; lakini natupwa katikati ya vurugu na mapinduzi.” -- D'Aubigne, b. 5, sura ya 2. Kwa sasa alikuwa karibu kuingizwa katika pambano lile. [GC 126.3; PK Aya ya 19]

### Tetzel Na Vyeti Vya Msamaha Wa Dhambi (Indulgensia)

Kanisa la Kirumi liliifanyia biashara neema ya Mungu (waliuza neema). Meza za wanaobadilisha pesa ziliwekwa kando ya altare (madhabahu) zake na hewa yake ikajazwa na kelele za wanunuzi na wauzaji (Mathayo 21:12). Kwa madai ya kusihi kufanya harambee ya uchangiaji wa pesa kwa ajili ya ujenzi wa Kanisa la Mtakatifu Petro kule Rumi, vyeti vya msamaha wa dhambi vilitolewa na kuuzwa hadharani kwa idhini ya papa. Kwa kutumia malipo ya uhalifu, walikusudia kulijenga hekalu kwa ajili ya kumwabudu Mungu-- jiwe kuu la pembeni liliwekwa kwa mashahara/mapato yale ya uovu! Lakini mali ile ile iliyotumika kwa kuitukuza Rumi, ilisababisha kipigo cha kufisha kwenye mamlaka na ukuu wake. Ni jambo hili, ndilo lilichochea maadui wa upapa waliokuwa wameazimia kuung'oa kabisa na ambao walifanikiwa, kusababisha vita ambayo vilitikisa kiti cha enzi cha upapa na kuipiga kikumbo ile taji yake yenye ngazi tatu (tiara) iliyokuwa juu ya kichwa cha papa. [GC au PK 127.1]

Afisa yule aliyeteuliwa kuendesha uuzaji wa vyeti vya msamaha kule Ujerumani---aliyeitwa Tetzel kwa jina-- alikuwa ameshitakiwa kwa makosa ya uhalifu mkubwa kwa jamii na dhidi ya sheria ya Mungu; lakini baada ya kuikwepa adhabu aliyoistahili kwa uhalifu wake, alitumiwa kuendeleza miradi ya umamluki na ufisadi, yaani alinunuliwa ili kuiendeleza miradi ya upapa ya kupata faida kwa kutumia njia zisizo na maadili mema. Naye bila soni usoni, na kwa hila kubwa, aliirudia tena na tena kusema maneno yaliyojaa uongo mtupu na kusimulia hekaya za ajabu kwa madhumuni ya kuwadanganya watu waliokuwa wajinga, wepesi wa kuamini kila jambo, na washirikina. Laiti kama wangekuwa wanalo Neno la Mungu mioyoni mwao, wasingekuwa wamedanganywa kwa jinsi ile. Ilikuwa ni kwa kusudi la kuwaweka chini ya udhibiti wa papa; ili kujiongezea mamlaka na utajiri wa viongozi wake wenye uchu wa madaraka, na mali, ndiyo maana Biblia ilikuwa imefichwa ili wasiweze kuiona kwa macho. (Tazama John CL Gieseler, A Compendium of Ecclesiastical History, kwa. 4, sec. 1, kif. 5.) [GC 127.2; PK Aya ya 20]

Kabla Tetzel hajaingia katika mji fulani, mjumbe alitangulia mbele yake, akitoa tangazo hili: "Neema ya Mungu na ya baba mtakatifu ipo malangoni penu."- D'Aubigne, b. 3, sura ya 1. Na watu wakamkaribisha mtu huyu mwenye makufuru aliyejifanya au kuigiza (drama au jambo feki) kana kwamba ndiye Mungu Mwenyewe aliyeshuka kutoka mbinguni na kuja majumbani mwao. Biashara hii ya aibu na haramu ilianzishwa na kuwekwa ndani ya kanisa, na Tetzel, alipanda mimbarani, akisifia ile mali iliyokusanywa ya indulgensia, yaani iliyopatika kwa kuuza misamaha wa dhambi kwamba ndiyo thawabu kubwa mno kuliko zingine zote kutoka kwa Mungu. Alitangaza kwamba nguvu ya vyeti vile vya msamaha wa dhambi zote, ambazo mnunuzi wa vyeti angeweza baadaye kutamani kuzitenda angesamehewa, na ya kwamba, "wala hakuwa na haja ya kuzitubia tena." - Ibid., b. 3, sura ya 1. Zaidi ya hili, aliwahakikishia wasikilizaji

wake kwamba vyeti hivi vya msamaha, havikuwa tu na uwezo wa kuwaokoa wale walio hai, bali hata wafu; kwamba wakati ule ule ile pesa inapotoa mlio inapodondoka kwenye chombo cha matoleo, roho ya yule ambaye fedha ilikuwa imetolewa kwa ajili yake ingetoka mara moja huko purgatori na kuanza kwenda juu mbinguni (ingetoka katika moto ule wa utakaso-purgatory na kuelekewa moja kwa moja mbinguni). (Tazama K. R. Hagenbach, History of the Reformation, vol. 1, uk. 96.) [GC 127.3; PK Aya ya 21]

**Maelfu Wavipokea Vyeti Vilivyotolewa Na Tetzel**

Wakati Simoni Magusi yule Mchawi alipotaka kununua kutoka kwa mitume nguvu ya kutenda miujiza Petro alimjibu: "Fedha yako na ipotelee mbali pamoja nawe, kwa kuwa umedhania ya kuwa karama ya Mungu yapatikana kwa mali.." Matendo 8:20. Lakini biashara/ofa ya Tetzel ilikumbatiwa kwa nguvu na maelfu ya watu kwa shauku kubwa. Dhahabu na fedha vilitiririka na kuingia ndani ya hazina yake. Wokovu uliopatikana kwa kununuliwa na fedha ulipatikana kirahisi sana ukilinganisha na wokovu unaohitaji toba, imani, na juhudi kubwa ya kuipinga na kuishinda dhambi *(Tazama Kiambatisho).* [GC 128.1; PK Aya ya 22]

Fundisho hilo la vyeti vya msamaha wa dhambi (indulgensia) limekuwa likipingwa na watu wenye elimu na wacha Mungu waliokuwa katika Kanisa la Rumi, tena kulikuwa na wengi waliokuwa hawana imani na maigizo na unafiki ule, yaani mambo yaliyokuwa bandia (feki au drama) yaliyokwenda kinyume kabisa na busara ya mafunuo ya Neno la Mungu. Hakuna askofu aliyethubutu kuinua sauti yake dhidi ya biashara hii ya uovu; lakini mawazo ya watu yalikuwa yanaanza kusumbuliwa na wasiwasi uliwaingia, na kisha wengi kwa shauku waliuliza iwapo Mungu asingeweza kutumia kufanya kazi Yake kupitia chombo fulani (au kupitia mjumbe) ili kulisafisha kanisa Lake. [GC 128.2; PK Aya ya 23]

Japokuwa Luther alikuwa bado mfuasi wa papa mwaminifu kabisa na mwenye aina fulani ya unyofu, yeye alijazwa na hofu kuu alipoyasikia madai yenye kufuru yaliyotamkwa na wafanya biashara wenye tamaa ya pesa waliouza vyeti vya msamaha wa dhambi. Wengi katika ushirika wake mwenyewe walikuwa wamekwisha kujinunulia vyeti hivi vya msamaha wa dhambi, na punde wakaanza kuja kwa mchungaji wao, wakiziungama dhambi zao za aina mbalimbali tena, wakitazamia kupewa ondoleo la dhambi zao, si kwa sababu wao walikuwa na nia ya kutubu na kutaka kujirekebisha kwa kufanya matengenezo katika maisha yao, bali kwa msingi wa vyeti vya msamaha wa dhambi. Luther aliwanyima utakaso au ondoleo la dhambi zao, kisha akawaonya kwamba ikiwa hawatatubu na kunuia kuyatengeneza maisha yao, hawana budi kufa katika dhambi zao. Wakiwa wamechanganyikiwa vibaya, walirudi tena kwa Tetzel wakilalamika kwamba yule anayepokea maungamo yao (Padri mwuungamishaji) alikuwa amevikataa vyeti vya msamaha vya Tetzel; na wengine kwa ujasiri walidai warudishiwe fedha zao.

Mtawa huyu alijawa na ghadhabu kali. Akatamka laana za kuogofya mno, akaagiza mioto iwashwe mahali sehemu za wazi ambazo watu hukutania mijini (public Squares), na kutangaza kwamba “Alikuwa amepokea agizo kutoka kwa papa kuwachoma moto wazushi wote waliodiriki kuvipinga vyeti vyake vitakatifu sana vya msamaha wa dhambi.” D'Aubigne, b. 3, sura ya 4. [GC 128.3; PK Aya ya 24]

**Luther Mtetezi Wa Kweli**

Sasa Luther alianza kazi yake kwa ujasiri kama mtetezi wa Ukweli. Sauti yake thabiti ilisikika kutoka kwenye mimbari kwa onyo la dhati na zito. Aliweka mbele ya watu uhalisi wa jinsi dhambi inavyochukiza na kuwafundisha kwamba haiwezekani kwa mwanadamu, kwa matendo yake mwenyewe, kupunguza hatia yake au kukwepa adhabu ya dhambi yake. Hakuna kitu chochote, isipokuwa toba kwa Mungu na imani katika Kristo, ndiyo ambayo ingeweza kumwokoa mwenye dhambi. Neema Yake Kristo haiwezi kununuliwa; ni zawadi inayotolewa bure. Aliwashauri watu wasinunue vyeti vile vya msamaha wa dhambi, bali wamtazame kwa imani Mkombozi wao aliyesulibiwa. Akasimulia uzoefu wa kisa chake mwenyewe kilichomletea maumivu makali alipotaka kujitesa bure, kujidhili na kufanya kitubio ili kujipatia wokovu, tena aliwahakikishia wasikilizaji wake ya kwamba ilikuwa ni kwa njia ya kutojiangalia nafsi yake mwenyewe na kumwamini Kristo ndipo yeye alipopata amani na furaha. [GC 129.1; PK Aya ya 25]

Kwa kadri Tetzel alivyoendelea na biashara na unafiki wake uliokuwa umejaa makufuru (maigizo feki yasiyo na kicho), Luther aliamua kuchukua hatua ya ufanisi zaidi, ambayo ingeleta matokeo mazuri dhidi ya vilio vilivyosababishwa na uonevu wa kutisha. Haikuchukua muda kwa fursa kujitokeza. Katika kanisa kubwa la Wittenberg (Vitenbergi) kulikuwa na masalia ya vitu vya watakatifu kama vile mifupa, nguo za watakatifu, na vitu vingine vya wale waliokufa zamani ambavyo kanisa lilikuwa linaviabudu *(relics)*, na katika siku fulani takatifu vitu hivi vilikuwa vinaonyeshwa kwa watu, na kisha msamaha kamili wa dhambi ulikuwa unatolewa kwa wote waliotembelea kanisani na kuungama. Basi, katika siku zile idadi kubwa sana ya watu ilikwenda pale. Mojawapo la matukio hayo makubwa sana, yaani, ile Sikukuu ya Watakatifu Wote na ilikuwa inakaribia (All Saints Day). Siku moja kabla ya siku hii ya Watakatifu, Luther, aliungana na umati mkubwa wa vikundi vya watu ambao walikuwa tayari wanatembea kuelekea lile kanisa, ndipo alibandika mlangoni karatasi lenye hoja au matamko tisini na tano *(95 Thesis)* dhidi ya fundisho la vyeti vya msamaha wa dhambi *(Doctrine of Indulgunce)*. Alitangaza kwamba yeye atakuwa tayari kutetea matamko yake haya aliyoyaandika siku iliyofuata katika kile Chuo Kikuu, dhidi ya watu wote ambao waliona ni vyema kuyashambulia. [GC 129.2; PK Aya ya 26]

Matamko yake yalivuta usikivu wa watu wote. Yalisomwa tena na tena, na kurudiwa kuzungumzwa tena na tena kila pande yalikokwenda. Msisimko mkubwa ukatokea katika Chuo kikuu na katika jiji lote. Kwa njia ya Matamko au hoja zile (95) zilizoandikwa, watu waliona kwamba uwezo wa kutoa msamaha wa dhambi au kuidhinisha adhabu kwa mdhambi ulikuwa haujapata kamwe kukabidhiwa kwa papa au kwa mwanadamu mwingine yoyote. Mpango ule wote ulikuwa ni maigizo na upuzi mtupu, --- yaani, ulikuwa ni ujanja au utapeli wa kujipatia fedha kwa nguvu kwa kucheza na imani za kishirikina walizokuwa nazo watu - ilikuwa ni mbinu au chombo cha Shetani, kuziangamiza roho za wale wote ambao wangeyatumainia maigizo yake ya uongo. Pia ilionyeshwa wazi kwamba Injili Yake Kristo ndiyo hazina ya kanisa yenye thamani kupita zote, na ya kwamba neema ya Mungu, iliyofunuliwa katika Injili hiyo, hutolewa bure kwa wale wote wanaoitafuta kwa njia ya toba na imani. [GC 130.1; PK Aya ya 27]

**Ujerumani Yote Yatikiswa Na Mapendekezo Yale**

Matakamko ya Luther yalileta changamoto na kuchochea mjadala (mdahalo); lakini hakuna mtu aliyethubutu kuitikia changamoto hiyo. Maswali yale ambayo alikuwa amependekeza yalikuwa yameenea katika Ujerumani yote baada ya siku chache na baada ya majuma machache yalikuwa yamesikika katika ulimwengu wote wa Kikristo. Wafuasi wengi wa Rumi waliokuwa wacha Mungu, na ambao walikuwa wameona na kuomboleza kwa ajili ya uovu wa kutisha uliokuwamo ndani ya kanisa lao, lakini walikuwa hawajui jinsi ya kuyazuia mambo yale yasiendelee, walisoma mapendekezo yale kwa furaha kubwa, nao wakaitambua sauti ya Mungu ndani ya maandishi haya. Waliona kwamba Bwana kwa neema Yake alikuwa ameweka mkono Wake kulizuia wimbi lile la ufisadi lililokuwa linaumuka kwa haraka sana ambalo lilikuwa linatoka katika serikali ya Holy see huko Rumi (Holy See inatazamwa kama serikali kuu ya Kanisa Katoliki na kiti kitakatifu). Wafalme na mahakimu walishangilia kwa siri kwamba udhibiti ulikuwa umewekwa dhidi ya mamlaka yenye kiburi na ufidhuli ambayo ilikuwa imekataa haki ya kukata rufaa dhidi ya maamuzi yake. [GC 130.2; PK Aya ya 28]

Lakini umati wa watu walioipenda sana dhambi na kuwa na imani ya ushirikina, uliingiwa na hofu kubwa sana kwa kuona madanganyo yale yaliyokuwa yamezituliza hofu zao yakifagiliwa mbali na matamko ya Luther. Makasisi wajanja walioliongoza kanisa, walipoona wanaingiliwa katika kazi yao ya kuhalalisha uhalifu, na kwa kuona kwamba mapato yao yalikuwa hatarini, walighadhabika mno, nao waliljikusanya tena na kuungana ili kuutetea ule ulaghai (maisha ya bandia). Mwanamatengenezo alikabiliwa na washtaki wakali sana. Wengine miongoni mwao wakamshitaki kuwa alitenda mambo yake kwa papara na kufanya kazi kwa mihemko bila kufikiri kwa busara. Wengine walimshtaki kuwa ana majivuno, wakitangaza kwamba alikuwa hajaongozwa na Mungu, bali alikuwa akitenda kwa kiburi, 'kimbelembele' na kujionyesha. "Ni

nani asiyejua” alijibu, “kwamba ni nadra mno kwa mtu kutoa wazo jipya bila kuwa na mwonekano fulani wa kiburi, na bila kushitakiwa ya kuwa anaanzisha migogoro/malumbano?..…” akajibu. Kwa nini Kristo na mashujaa wa imani au wafia dini wote waliuawa? Kwa sababu walionekana kana kwamba walikuwa na kiburi na kuidharau hekima au maamuzi ya wakati ule, na kwa vile waliendeleza mawazo mapya bila kuweka umakini katika kunyenyekea kwanza kwa kupata mashauri yenye uzoefu wa hekima, historia na maoni ya watu wale wa zamani. [GC 130.3; PK Aya ya 29]

Tena alisema: “Chochote nachofanya kitafanyika, si kwa hekima za wanadamu, bali kwa hekima na ushauri wa Mungu. Ikiwa kazi hii ni ya Mungu, ni nani atakayeisimisha? Kama si Yake, ni nani atakayeiendeleza mbele? Siyo kwa mapenzi yangu, wala si kwa mapenzi yao, wala si kwa mapenzi yetu sisi; bali ni kwa mapenzi Yako, Ee Baba Mtakatifu uliye mbinguni.”- Ibid., b. 3, sura ya 6. [GC 131.1; PK Aya ya 30]

**Mapambano Makali Sana**

Ingawa Luther alikuwa amesukumwa na Roho wa Mungu kuanza kazi yake hii, yeye Asingeweza kuiendeleza mbele bila kukabiliwa na migogoro mikali. Kugombezwa na maadui zake, maelezo yenye kupotosha makusudi yake, na kusingiziwa kusiko haki na kuliojaa kijicho chenye kunuia kuleta madhara kuhusu tabia na nia yake katika mambo yale aliyoyatenda, vikamwangukia kama mafuriko ya maji yaliyomlemea; nayo hayakukosa kuleta madhara. Alikuwa amesadiki kwamba viongozi wa watu katika makanisa, na mashuleni, kwa furaha wangeungana naye katika juhudi zake za kufanya matengenezo. Maneno ya kutia faraja kutoka kwa wale waliokuwa katika nyadhifa za juu yalikuwa yamemhuisha kwa furaha na matumaini. Katika matarajio yake tayari alikuwa amekwishaiona siku ile njema ikianza kupambazuka kwenye kanisa. Walakini kutiwa moyo huku kukageuka na kukawa kuabishwa na kulaumiwa. Wakuu wengi wa kanisa na serikali, walipata kushawishiwa na Kweli za matamko aliyoyaweka; lakini walitambua mara moja kwamba kuzikubali Kweli zile kungeleta mabadiliko mengi makubwa kwao. Zaidi ya hayo, kule kuwaelimisha kwa kuwapa mwangaza na kuwafanyia matengenezo watu, kungeidhoofisha kabisa mamlaka ya Rumi, na kungezuia maelfu ya mito ya fedha iliyokuwa ikitiririka na kuingia katika hazina yake, na hivyo kungepunguza sana ubadhirifu na anasa za viongozi wa upapa. Zaidi ya hayo, kule kuwafundisha watu kufikiri na kutenda kama nafsi zinazowajibika, wakimtazama Kristo peke Yake kwa ajili ya wokovu wao, kungekipindua kiti cha enzi cha papa na hatimaye kuiangamiza mamlaka yao wenyewe. Kwa sababu hiyo waliyakataa maarifa ya ujumbe waliopewa na Mungu, nao wakajipanga wenyewe dhidi ya Kristo naUkweli kwa kumpinga mtu yule aliyemtuma kuwaangazia nuru. [GC 131.2; PK Aya ya 31]

Luther alitetemeka kwa hofu alipojitazama mwenyewe --- alijiona kuwa alikuwa ni mtu mmoja tu, anayesimama kupigana na mamlaka za dunia zenye uwezo mkubwa. Wakati mwingine aliingiwa na mashaka na kujiuliza kama ni kweli alikuwa ameongozwa na Mungu kujiweka mwenyewe dhidi ya mamlaka ya kanisa. "Mimi nilikuwa nani," aliandika, "kupinga Ukuu wa papa, yeye ambaye anatetemekewa na wafalme wa dunia na ulimwengu mzima?... Hakuna hata mtu mmoja awezaye kujua jinsi moyo wangu ulivyoteseka katika miaka hii miwili ya kwanza, wala kujua ni katika hali gani ya kufa moyo nimekuwamo, au niseme nini katika hali ya kukatishwa tamaa ambayo nilikuwa nimezama ndani yake." Ibid., b. 3, sura ya 6. - kitabu cha 3, sura ya 6. Lakini, hakuachwa akate tamaa kabisa. Wakati msaada wa kibinadamu ulipofeli au kukosekana, alimwangalia Mungu peke Yake na kujifunza kwamba angeweza kuuegemea kwa usalama kabisa kwenye ule mkono Wenye uweza wote. [GC 132.1; PK Aya ya 32]

**Biblia Peke Yake**

Luther Akimwandikia rafiki yake Mwatengenezo wa kanisa alisema: "Hatuwezi kuufikia uelewa wa Maandiko ama kwa kujifunza kwetu, au usomi wetu au kwa akili zetu wenyewe. Wajibu wako wa kwanza ni kuanza kwa sala. Umsihi sana Bwana akupatie wewe, kutoka katika rehema Zake kuu, uelewa sahihi wa Neno Lake. Hakuna mwingine yeyote awezaye kulifasiri Neno la Mungu zaidi ya Mwasisi wa Neno hilo, kama vile alivyosema Yeye Mwenyewe (Yoh 6:45), 'Wote watafundishwa na Mungu.' Usitumainie kupata kitu chochote kutokana na juhudi zako mwenyewe, kutokana na uelewa wako mwenyewe: mtumainie Mungu peke Yake, na katika mvuto wa Roho Wake. Amini haya kwa Neno la mtu yule (Luther) aliyeupata uzoefu huo." Ibid., b. 3, sura ya 7. Hapa lipo somo lenye umuhimu mkubwa kwa wale wanaohisi kwamba Mungu amewaita ili kuwasilisha kwa wengine Ukweli wa wakati huu (Ukweli wa leo). Kweli hizi zitaamsha uadui wa Shetani na wa watu wake wanaozipenda sana hekaya za uongo alizozibuni yeye mwenyewe. Katika kupambana na nguvu zile za uovu kunahitajika kitu fulani kimoja ambacho ni muhimu zaidi ya kuwa na nguvu za akili na hekima ya kibinadamu. [GC 132.2; PK Aya ya 33]

Wakati adui walipotumia desturi na mapokeo yao, au madai na mamlaka ya papa, Luther alikabiliana nao kwa kutumia Biblia na Biblia pekee (Sola Scriptura kwa kilatini). Hapo zilikuwamo hoja ambazo wasingeweza kuzijibu; kwa hiyo, watumwa wale wa kufuata desturi za kidini na ushirikina wakapiga makelele wakiitaka damu Yake, kama vile Wayahudi walivyopiga makelele wapoitaka damu Yake Kristo. "Huyu ni mzushi" (mwongo kwao ni mtu afundishaye mafundisho ya Kweli za Biblia kinyume na cha yale ya Rumi), wakapiga makelele wale mashabiki wa Rumi. "Ni uhaini wa hali ya juu dhidi ya kanisa kumwacha

mzushi huyo wa kuchukiza mno kuishi hata saa moja zaidi. Hebu na kijengwe mara moja jukwaa/kiunzi cha kumnyongea!" - Ibid., b. 3, sura ya 9. Lakini Luther hakuangukia mkononi mwao kama mawindo kutokana na ghadhabu yao. Mungu alikuwa na kazi kwa ajili yake ya kuifanya, na malaika wa mbinguni walitumwa kwake kumlinda. Hata hivyo, wengi waliokuwa wameipokea nuru ile ya thamani kutoka kwa Luther walikuwa ndio walengwa wa ghadhabu ya Shetani na kwa ajili yaUkweli waliteswa vibaya na kuuawa pasipo kuwa na woga. [GC 132.3; PK Aya ya 34]

Mafundisho yale ya Luther yalivuta utashi wa watu waliokuwa wanatafakari mambo kwa umakini katika nchi yote ya Ujerumani. Kutoka kwenye mahubiri na maandiko yake, mishale ya nuru ilitoka ambayo iliwazindua akili na kuwatia nuru maelfu ya watu. Imani iliyokuwa hai ilikuwa inachukua mahali pa desturi na taratibu mfu (mazoea mfu au kaida) ambazo zilikuwa zimelishikilia sana kanisa kwa muda mrefu sana. Kila kukicha watu walikuwa wanapoteza imani kutokana na ushirikina ule wa Kirumi (imani potofu). Vizuizi vya ubaguzi vilivyokuwapo, ambavyo viliwafanya watu kuchukia au kupendelea upande fulani bila hekima, vilikuwa vinabomolewa. Neno la Mungu ambalo kwa hilo Luther alilipima kila fundisho la dini na kila dai, nako lilikuwa kama upanga ukatao kuwili, likikata na kupenya mpaka ndani ya mioyo ya watu. Kila mahali palikuwa na uamsho ulioleta matamanio makubwa ya kupata maendeleo ya kiroho. Kila mahali kulikuwa na njaa kubwa na kiu ya kuitafuta haki kama ambavyo haijapata kujulikana kwa vizazi vingi vilivyotangulia. Macho ya watu ambayo kwa kipindi kirefu yalikuwa yameelekezwa kwenye taratibu za ibada zilizowekwa na wanadamu na kwenye wapatanishi wa kidunia, sasa yakawa yanageukia toba na imani ili kumtazama Kristo Yule Aliyesulibiwa. [GC 133.1; PK Aya ya 35]

### Apewa Hati Ya Kuitwa Hukumuni Rumi

Shauku iliyokuwa imeenea mahali pengi, iliibua hofu nyingi zaidi kwenye mamlaka ya upapa. Luther akapokea hati ya mahakama, ikimwita kwenda kujibu mashitaka katika kesi ya uzushi Rumi. Amri hii iliwajaza hofu kuu rafiki zake. Walijua fika hatari iliyomkabili katika mji huu uliojaa ufisadi, ambao tayari ulikuwa umelewa damu ya wafia dini yaani mashahidi wa Yesu. Walipinga kwenda kwake Rumi na kuomba kwamba ahojiwe katika nchi yao ya Ujerumani. [GC 133.2; PK Aya ya 36]

Hatimaye mpango huu ulitekelezwa, na mwakilishi wa papa aliteuliwa kusikiliza kesi hii. Katika maelekezo yaliyotolewa na papa kwa afisa wake, ilielezwa kwamba Luther alikuwa ametangazwa kuwa ni mzushi tayari. Kwa hiyo, mwakilishi wa Papa, alikuwa ameagizwa "kumfungulia mashtaka kisheria na kumweka kizuizini bila kuchelewa." Ikiwa angeendelea kuwa imara kwenye msimamo wake, na huyu balozi akashindwa kumkamata, basi, alipewa uwezo wa

“kumpiga marufuku asionekane katika sehemu yoyote ya Ujerumani; kumfukuza mbali na nchi yao, kumlaani, na kuwafuta ushirika watu wote wanaoshikamana naye.”- Ibid., b. 4, sura ya 2. Tena, zaidi ya hayo, papa alimwagiza mwakilishi wake huyo, kwamba, ili kuung’oa kabisa uzushi ule uliokuwa kama tauni au ugonjwa wa kuambukiza, yafaa awatenge watu na ushirika wa kanisa, wale wote wenye hadhi yoyote kanisani au serikalini, isipokuwa mfalme wa dola (emperor) peke yake, ambaye watamwacha ili amkamate Luther pamoja na wafuasi wake, na kuwasalimisha kwa Rumi ili Rumi ipate kulipiza kisasi [GC 133.3; PK Aya ya 37]

Hapa ndipo roho halisi ya upapa inapodhihirishwa waziwazi. Hakuna chembe ya mwonekano wa kanuni ya Kikristo ndani ya roho hiyo au hata haki za kawaida za wanadamu wote ambayo inaonekana katika mchakato wote (au hati ile nzima). Luther alikuwa ametengwa kwa umbali mkubwa na Rumi; alikuwa hajawai kupata fursa ya kujielezea au kutetea msimamo wake; lakini hata kabla ya kesi yake kufanyiwa upelelezi, alikuwa amekwisha kuhukumiwa kama mzushi na siku hiyo hiyo, akashauriwa, akashtakiwa na kuhukumiwa kwa kupatikana na hatia; na yote hayo yalifanywa na yule aliyejipachika mwenyewe kuwa ni baba mtakatifu kwa staili yake, na kwamba ndiye pekee aliye na mamlaka ya juu kabisa isiyoweza kukosea hata kidogo katika kanisa au katika serikali/himaya! [GC 134.1; PK Aya ya 38]

### Melanchthon

Wakati huu ambapo Luther alihitaji sana kupata faraja, huruma na ushauri kutoka kwa rafiki aliye wa kweli, majaliwa ya neema ya Mungu yalimtuma Melanchthon huko Wittenberg. Yeye akiwa kijana kwa umri, alikuwa mwenye haya, mwenye kiasi, mtulivu, mwenye mvuto wa umbuji, mwenye tabia ya unyofu, mwenye ufahamu mpana, usafi wa moyo, upole, unyenyekevu, mkimya, asiyependa kujitanguliza, na mwoga kwa tabia yake, Melanchthon alipendwa na watu wote na kuheshimiwa kutokana na maamuzi yake mazuri, elimu yake pana, na ufasaha wake uliowavutia watu, mambo hayo yalikuwa yamechanganyika pamoja na usafi wake wa maisha na unyofu wa tabia yake. Talanta zake mahiri hazikuonekana sana ukilinganisha na ile tabia yake ya upole na uungwana. Punde akawa mwanafunzi wa injili mwenye bidii, na rafiki mwaninifu wa Luther na mtu wa thamani aliyemwunga mkono; upole na uungwana wake, kuchukua kwake tahadhari, na usahihi wake vikachangia katika kuukamilisha ujasiri na utendaji wake Luther (alibalansi kwa namna fulani tabia ya Luther aliyekuwa mkali kidogo!) Muungano wao katika kazi ukaongeza nguvu kwenye matengenezo ya kanisa na kwa Luther ukawa chanzo cha kumhamasisha sana moyo wake. [GC 134.2; PK Aya ya 39]

Mji wa Augsburg ukatengwa kuwa ndiyo mahakama ya kusikiliza kesi yake, Mwanamatengenezo huyu akaanza safari yake kwa mguu kuelekea huko. Wenzake walikuwa na hofu kubwa kwa ajili yake. Vitisho vilikuwa vimeshatolewa waziwazi kwamba atakamatwa na kuuawa akiwa njiani, ndipo marafiki zake wakamsihi sana asithubutu kwenda huko. Hata walimsihi sana aondoke pale Wittenberg kwa muda na kutafuta hifadhi kwa kukaa pamoja na wale ambao wangekuwa na furaha kabisa kumlinda. Lakini yeye hakuweza kuondoka mahali pale ambapo Mungu alikuwa amemweka. Ilikuwa ni sharti aendelee kwa uaminifu kuitetea na kuidumisha ile Kweli, licha ya dhoruba zilizokuwa zikimchapa. Lugha yake ilikuwa ni hii: "Mimi ni kama Yeremia, mtu wa migogoro na malumbano; lakini kadri vitisho vyao vinavyozidi kuongezeka, ndivyo furaha yangu inavyozidi kuwa nyingi zaidi.... Tayari wamekwishanivunjia heshima yangu na kuniharibia sifa yangu. Jambo moja tu sasa limebaki; ni huu mwili wangu dhaifu; basi, waacheni wauchukue; kwa njia hiyo watafupisha maisha yangu kwa saa chache tu. Lakini kwa habari ya roho yangu, hiyo hawawezi kuitwaa. Yeye anayetaka kulitangaza Neno la Kristo kwa ulimwengu huu, ni lazima atarajie kifo kila wakati." - Ibid., b. 4, sura ya 4. [GC 134.3; PK Aya ya 40]

Habari za kuwasili kwake Luther pale Augusburg zikampendeza sana balozi wa papa. Mzushi yule msumbufu, aliyeleta matata, na kuamsha usikivu wa ulimwengu mzima, alionekana sasa kuwa yumo katika mamlaka ya Rumi,na yule mjumbe wa papa alidhamiria kuwa asiweze kutoroka. Mwanamatengenezo alikuwa ameshindwa kupata hati ya kumhakikishia kusafiri kwa usalama. Rafiki zake walimsihi sana asijitokeze mbele ya balozi yule wa papa bila kuwa na hati hiyo ya uhakikisho wa usalama, na wao wenyewe wakachukua jukumu la kuipata kutoka kwa mfalme wa dola (emperor). Mwakilishi wa papa alikusudia ikiwezekana, amlazimishe Luther kuikana imani yake, la sivyo, kama angeshindwa kukanusha, basi, angeweza kumchukua mpaka Rumi kwenda kushiriki hatima kama ile waliyokutana nayo Huss (Jan Hus) na Jerome. Kwa hiyo, kupitia mawakala wake, alimshawishi Luther kusafiri bila kuwa na hati maalum inayomhakikisha usalama, kwamba aziamini tu hisani za yule balozi. Jambo hilo Mwanamatengenezo huyu alikataa katakata kulifanya. Hakuweza kujitokeza mbele ya balozi wa papa mpaka alipopokea hati iliyomwahidi ulinzi kutoka kwa mfalme wa dola. [GC 135.1; PK Aya ya 41]

Kama ilivyopaswa kutendwa kisera (au hila), Warumi waliamua kumshawishi Luther kwa njia ya kumwonyesha sura ya uungwana na upole. Mjumbe yule wa papa, katika mahojiano yake naye, alijionyesha kuwa na roho ya kirafiki sana; lakini alitaka Luther ajisalimishe kabisa katika kila kipengele kwenye mamlaka ya kanisa, na kutupilia mbali kila hoja aliyokuwa nayo bila kubishana naye au kuwa na swali lolote. Alikuwa hajaipima na kuitambua vizuri tabia ya mtu yule aliyekuwa anataka kushughulika naye. Kwa kujibu, Luther alieleza jinsi

anavyoliheshimu kanisa, matamanio yake kwa ajili ya Ukweli, utayari wake wa kujibu ukinzani wote kwa yale aliyokuwa ameyafundisha, na kuwasilisha mafundisho yake ili yapimwe na baadhi ya vyuo vikuu vinavyoongoza kwa umashuhuri (vyenye sifa za taaluma hiyo). Lakini kwa wakati ule ule alipinga njia aliyoitumia kadinali huyu ya kumtaka yeye akanushe mafundisho yake (akubali kushindwa) bila kumthibithishia makosa yake yako wapi. [GC 135.2; PK Aya ya 42]

**Mwanamatengenezo Huyo Aombwa Kuikana Imani Yake**

Jibu lake pekee lilikuwa ni hili: "Kana, tangua (Kubali kushindwa)!" Mwanamatengenezo alionyesha kuwa msimamo wake uliungwa mkono na Maandiko, na kujengwa kwenye msingi wa Maandiko, naye akasema kwa mkazo kuwa asingeweza kuukana Ukweli. Yule balozi wa papa, akiwa ameshindwa kuzijibu hoja za Luther, alimkandika kwa dhoruba za makaripio/magombezo, kebehi, kumzomea, dharau, kushushua, matusi, na sifa za kinafiki, akichanganya na madondoo toka katika mapokeo na semi za mababa, (viongozi wa kanisa), pasipo kumpa Mwanamatengenezo nafasi ya kusema. Luther akaona kama huu mkutano ungeendelea kwa namna hiyo, basi, yote yangekuwa ni kazi bure, yaani yasingeleta tija, Luther hatimaye alikubali kwa shingo upande kutoa jibu lake kwa maandishi. [GC 136.1; PK Aya ya 43]

Kwa kufanya hivyo," akasema, alimwandikia rafiki yake, "wale wanyonge wanaokandamizwa wanapata faida maradufu; kwanza, kila kilichoandikwa kinaweza kutolewa ili kipate kuchunguzwa na hivyo kupata maamuzi ya watu wengine; na pili, mtu anakuwa na nafasi nzuri ya kuishughulikia hofu yake, sio katika dhamiri ya dikteta huyo, yaani, mtawala huyo dhalimu, jeuri, na mpayukaji, ambaye vinginevyo angeweza kumshinda kwa lugha yake yenye kuamuru, isiyo na haki, yenye majivuno, na ya kutumia nguvu." - Martyn, The Life and Times of Luther, ukurasa wa 271, 272. [GC 136.2; PK Aya ya 44]

Katika mahojiano yaliyofuata, Luther alitoa maelezo yaliyo wazi, mafupi, na yenye nguvu juu ya maoni yake, yakiungwa mkono kikamilifu na dondoo nyingi za Maandiko. Barua hii ya kujieleza, baada ya yeye kuisoma kwa sauti, alimkabidhi kadinali yule, ambaye kwa dharau aliitupa kando, akisema kwamba ilijaa maneno mengi ya kipuuzi (sifuri tu) na dondoo zisizohusiana na hoja ile. Luther, akiwa amechachamaa kabisa sasa, akapambana na askofu yule mwenye dharau katika uwanja wake mwenyewe - yaani, uwanja wa mapokeo na mafundisho ya kanisa – na kuzivunjilia mbali dhana na madai yake. [GC 136.3; PK Aya ya 45]

Kadinali (mwakilishi) alipoona kwamba sababu zile za hekima alizozitoa Luther zilikuwa haziwezi kujibiwa, alishindwa kabisa kujizuia, na kwa ghadhabu kali akapiga makelele, akisema: "Kanusha mafundisho yako! (ondoa hoja zako

hapa au zinakushe) La sivyo nitakupeleka Rumi ukaonekane kule mbele ya mahakimu wale waliopewa maagizo la kuisikiliza kesi yako. Nitakuondoa katika ushirika wa kanisa, wewe pamoja na wafuasi wako wote, mashabiki, na wale wote ambao kwa wakati wowote ule wanakupa upendeleo, wewe pamoja na hao nitawatupa nyote nje ya kanisa." Na mwishowe, akatangaza kwa sauti ya kiburi na ya hasira: "Kanusha au usirudi." - D'Aubigne, London ed., B. 4, sura ya 8. [GC 136.4; PK Aya ya 46]

### Atoroshwa Kwenda Augusburg (Mwanamatengenezo)

Mwanamatengenezo aliondoka mara moja pamoja na rafiki zake, hiyo ilitangaza waziwazi kuwa kitendo cha kukanusha kisingeweza kutarajiwa kutoka kwake. Jambo hili halikuwa kama alivyokusudia yule kadinali. Alikuwa amejitapa kwa kujidanganya mwenyewe kwamba kwa kutumia nguvu angemtia hofu kuu Luther na kumfanya akubali. Sasa, akiwa ameachwa peke yake pamoja na wafuasi wake waliomuunga mkono, alimwangalia huyu huku na yule kule, akiwa ameudhika vibaya na kujaa aibu kwa kushindwa kusikotarajiwa kwa hila zake. [GC 137.1; PK Aya ya 47]

Jitihada za Luther katika tukio hili hazikukosa kuwa na matunda mazuri. Mkutano mkubwa uliohudhuria pale ulipata nafasi ya kuwalinganisha watu hao wawili, na kuamua wao wenyewe kuhusu ile roho iliyodhihirishwa mbele yao, pamoja na nguvu na Ukweli wa misimamo yao. Tofauti zao zilikuwa dhahiri na kubwa! Mwanamatengenezo, alikuwa mtu wa kawaida tu. Alikuwa mtu sahili, mnyenyekevu, jasiri, mtulivu, na alisimama katika nguvu za Mungu akiwa na Ukweli upande wake; mwakilishi wa papa, mwenye kujiona mwenyewe kwamba ni wa muhimu, mwenye majivuno, mwenye jeuri, mwenye kutamani makuu, na asiyetumia busara, alikuwa hana hata hoja moja kutoka katika Maandiko, lakini alipiga makelele kwa nguvu na hasira, akisema: "Kanusha" (tangua), la sivyo upelekwe Rumi kuadhibiwa." [GC 137.2' PK Aya ya 48]

Pamoja na kwamba Luther alijipatia cheti cha ulinzi cha kumruhusu kusafiri salama, Warumi walikuwa wanafanya njama yao kwa siri ili kumkamata na kumtia gerezani. Rafiki zake walisisitiza kwamba ilikuwa haina tija kwake kurefusha kukaa kwake pale, kwamba angepaswa kurudi Wittenberg bila kuchelewa, na tahadhari kubwa sana ilipaswa kuchukuliwa ili kuficha mipango yake. Kwa kuzingatia hayo, aliondoka kwa farasi pale Augusburg kabla ya mapambazuko, akiwa amesindikizwa na mwongoza njia aliyepewa na hakimu. Akitarajia kukutana na mambo mengi mabaya mbele ya safari yake, aliondoka kwa wasiwasi na kwa siri katika mitaa yenye giza na kimya cha mji. Maadui zake, wakiwa macho na wakatili, walikuwa wamekula njama ili kumwangamiza. Je! angeweza kuikwepa ile mitego waliyokuwa wameitega? Kwake zile zilikuwa ni nyakati za mfadhaiko na maombi ya dhati na bidii. Alifika kwenye mlango mdogo

wa ukuta wa mji. Mlango ukafunguliwa kwa ajili yake, kisha yeye na mwongozaji wake wakapita bila kukutana na kikwazo chochote. Mara tu walipojiona kuwa wako salama nje ya mji ule, wakimbizi hawa waliharakisha kukimbia kwao mapema, na kabla balozi wa papa hajajua habari za kuondoka kwa Luther, alikuwa amekwenda mbali sana, mahali asikoweza kufikiwa na watesaji wake. Shetani na vibaraka wake  wakawa wameshindwa. Mtu ambaye walifikiri kwamba alikuwa katika mamlaka yao alikuwa amekwenda zake, ameponyoka kama ndege anavyoponyoka kutoka katika mtego wa mwindaji. [GC 137.3; PK Aya ya 49]

Baada ya kupokea habari ya kutoroka kwake Luther, balozi wa papa alipigwa butwaa na kukasirika mno. Alikuwa ametazamia kupokea heshima kubwa kwa hekima na ushupavu wake katika kumshughulikia yule mwenye kulisumbua na kulivuruga kanisa; lakini matumaini yake hayakuambulia kitu. Aliidhihirisha hasira yake kali katika barua aliyomwandikia Frederick, mtawala wa Saxony, mwenye haki ya kumteua mfalme, akimshutumu Luther kwa ukali sana na akimwamuru Frederick ampeleke Mwanamatengenezo kule Rumi au kumfukuzilia mbali kutoka jimbo la Saxony. [GC 138.1; PK Aya ya 50]

Katika kujitetea kwake, Luther alisisitiza kwamba mwakilishi wa papa, au papa mwenyewe amwonyeshe makosa yake kutoka kwenye Maandiko, na kutoa ahadi yake kwa njia ya kiapo kitakatifu kwamba atayakana mafundisho yake ya dini kama angeweza kuonyeshwa kuwa yalikuwa yakipingana na Neno la Mungu. Akaonyesha shukrani yake kwa Mungu kwa kuwa alikuwa amehesabiwa kuwa anastahili kuteswa kwa ajili ya kazi takatifu sana kama ile. [GC 138.2; PK Aya ya 51]

Mtawala  mwenye haki ya kumteua mfalme (Elector), mpaka hapo, alikuwa ana ufahamu mdogo mno wa yale mafundisho ya matengenezo, lakini aliguswa na kuvutiwa sana moyoni mwake kwa maneno yale ya Luther yenye unyofu usiopendelea upande wowote, yenye nguvu, na yaliyo wazi; na mpaka pale Mwanamatengenezo atakapoonekana kuwa ana makosa, Frederick aliazimu kusimama kama mlinzi wake. Katika jibu lake kwa madai ya balozi yule wa papa aliandika hivi: "'Kwa vile Dk. Martin amekuja mbele yako huko Augusburg, wewe ungekuwa umeridhishwa. Hatukutarajia kwamba wewe ungejaribu kumlazimisha kukana mafundisho yake au ashindwe bila ya wewe kumsadikisha makosa yake. Hakuna hata mmoja miongoni mwa wasomi katika eneo letu hili, aliyenipasha habari mimi kuwa mafundisho ya dini ya Martin yanamkufuru Mungu, yako kinyume na Ukristo, au yana uzushi ndani yake (yanapotosha).' Zaidi ya hayo, Elekta huyo wa Saxony alikataa kumpeleka Luther kule Rumi, au kumfukuza katika majimbo ya utawala wake." - D'Aubigne, b. 4, sura ya 10. [GC 138.3; PK Aya ya 52]

Elekta aliona kwamba palikuwa na ukiukwaji mkubwa wa kimaadili kwa jumla katika jamii ile. Kazi kubwa ya matengenezo ilihitajika. Mikakati migumu na

yenye gharama nyingi iliyokuwapo ya kuzuia na kutoa adhabu kwa uhalifu isingekuwa ya lazima kama watu wangeyakubali na kuyatii matakwa ya Mungu na msukumo wa dhamiri yao iliyoelimishwa. Aliona kwamba Luther alikuwa anajitahidi kulifikia lengo lile, naye kwa siri alishangilia kwamba mvuto ulio bora zaidi, ulikuwa unaingia na kusikika ndani ya kanisa. [GC 138.4; PK Aya ya 53]

### Hamu Mpya Ya Kusoma Maandiko Matakatifu

Aliona Pia Luther katika nafasi kama profesa katika Chuo Kikuu, alikuwa amepata mafanikio makubwa. Ni mwaka mmoja tu uliokuwa umepita tangu Mwanamatengenezo alipokuwa amebandika matamko yake kwenye mlango wa kanisa, hata hivyo palishakuwa na upungufu wa idadi kubwa ya mahujaji waliolitembelea kanisa katika Sikukuu ile ya Watakatifu Wote. Rumi ilikuwa imenyang'anywa watu wanaoabudu na matoleo yake ya sadaka, lakini nafasi yao ilijazwa na kundi jingine ambalo lilikuja Wittenberg, si kama mahujaji waliokuja kuabudu mifupa na vitu vya kale vya watakatifu waliokufa wa kanisa hilo, bali wanafunzi walijaza kumbi zake za kujifunzia. Maandishi ya Luther yalikuwa yamechochea kila mahali hamu mpya ya kusoma Maandiko Matakatifu, wala siyo tu kutoka katika sehemu zote za Ujerumani, bali kutoka katika nchi mbalimbali nyinginezo; wanafunzi walimiminika katika Chuo Kikuu Vijana wa kiume walipoiona Wittenberg kwa mara yao ya kwanza, "walinyanyua mikono yao kuelekea juu mbinguni wakimsifu Mungu kwa kuifanya nuru ya Ukweli iweze kuangaza kutoka katika jiji lile, kama kutoka Sayuni katika nyakati zile za zamani, na kutoka pale ilienea hata kufika katika nchi za mbali sana." - Ibid., b. 4, sura ya 10. [GC 139.1; PK Aya ya 54]

Mpaka pale Luther alikuwa ameongolewa nusu tu kutoka katika mafundisho yenye makosa ya Uroma. Lakini alipoendelea kuyalinganisha Maneno Matakatifu ya Mungu na amri zilizowekwa na papa pamoja na katiba za upapa, alijawa na mshangao mkubwa. "Ninaendelea kuzisoma," alisema, "amri zile zilizotolewa na mapapa, nami ... sielewi kama papa ndiye Mpinga Kristo mwenyewe haswa, au mtume wake tu, kwa kuwa Kristo amewakilishwa vibaya mno na kusulibiwa katika amri zao hizo." - Ibid., b. 5, sura ya 1. Hata hivyo, mpaka wakati ule Luther alikuwa bado anaendelea kuliunga mkono Kanisa la Rumi, wala hakuingiwa na wazo kwamba angekuja kujitenga kutoka katika ushirika wake. [GC 139.2; PK Aya ya 55]

Maandishi ya Mwanamatengenezo pamoja na mafundisho yake ya dini yalikuwa yakienezwa katika kila taifa kwenye Ulimwengu wa Kikristo. Kazi yake ilienea hadi huko Uswisi na Uholanzi. Nakala za maandiko yake zilifika hadi Ufaransa na Uhispania. Kule Uingereza maandishi yake yalipokelewa kama Maneno ya uzima. Ukweli ulikuwa umefika na kuenea pia kule Ubelgiji na Italia. Maelfu walikuwa wanaamka kutoka katika usingizi wao mzito unaofanana na kifo

cha kiroho na kuingia katika furaha na matumaini ya kuishi maisha ya imani. [GC 139.3; PK Aya ya 56]

Rumi ilizidi kuudhiwa zaidi na zaidi kwa mashambulio ya Luther, tena ilitangazwa na baadhi ya wapinzani wake waliokereketwa, yaani watu shupavu waliopitiliza (fans), hata na madaktari wa falsafa katika vyuo vikuu vya kikatoliki, ya kwamba yeyote ambaye angemwua mtawa huyo mwasi angekuwa hana dhambi yoyote. Siku moja mgeni mmoja, akiwa ameificha bastola yake katika joho lake, alimkaribia Mwanamatengenezo na kumwuliza kwa nini alitembea njiani akiwa peke yake namna ile. "Mimi niko mikononi mwa Mungu," alijibu yule Luther. "Yeye Ndiye nguvu zangu na ngao yangu. Mwanadamu anaweza kunitenda nini?" - Ibid., b. 6, sura ya 2. Baada ya kusikia maneno yale, uso wa mgeni yule uligeuka rangi na kuwa kama chokaa, naye akatimua mbio kwenda zake, kana kwamba alikuwa ameona uwepo wa malaika wa mbinguni. [GC 140.1; PK Aya ya 57]

Rumi ikawa imejielekeza kumwangamiza Luther; lakini Mungu alikuwa Ndiye mlinzi wake. Mafundisho yake ya dini yalisikika kila mahali - "katika nyumba ndogo za mashambani na katika nyumba za watawa,... katika ngome za watawala, katika vyuo vikuu, na katika majumba ya wafalme;" na watu mashuhuri na waungwana wakawa wakijitokeza kila upande kuunga mkono na kudumisha juhudi zake." - Ibid., b. 6, sura ya 2. [GC 140.2; PK Aya ya 58]

Ilikuwa ni karibu na wakati huu, alipokuwa akisoma vitabu vya Huss, ndipo Luther alipogundua Ukweli mkuu wa kuhesabiwa haki kwa njia ya imani, ambayo yeye mwenyewe alikuwa anajaribu kuitetea, kuipigania na kuifundisha, nayo ilikuwa imepata kushikwa na Mwanamatengenezo huyu wa Bohemia. "Sisi sote," alisema Luther, "Paulo, Augustine, na mimi mwenyewe, tumekuwa wafuasi wa Huss (Wahusi) tukitafuta Ukweli pasipo kujua!" "Hakika Mungu atauwajibisha ulimwengu kwa ujumbe huu," aliendelea kusema, "kwa kuwa Ukweli huu umehubiriwa katika ulimwengu tangia karne moja iliyopita, na kuchomwa moto! (kupigwa vita)" - Wylie, b. 6, sura ya 1. [GC 140.3; PK Aya ya 59]

Katika wito wake kwa mfalme wa dola na wakuu wa Ujerumani kwa niaba ya kutetea matengenezo ya Ukristo, Luther aliandika hivi kumhusu papa: "Ni jambo la kutisha sana kumwangalia mwanadamu huyo anayejiita mwenyewe kuwa ni 'Badala ya Kristo', akionyesha fahari ambayo hakuna mtawala yeyote wa dola anaweza kufanana naye. Je! Huku ndiko kufanana na Yesu maskini, au Petro mnyenyekevu? Kama wasemavyo watu, yeye ni bwana wa ulimwengu huu! Lakini Kristo, ambaye yeye anajigamba kuwa anamwakilisha, amesema hivi, 'Ufalme Wangu sio wa ulimwengu huu.' Je! Eneo la ufalme wa yule mwakilishi Wake, linaweza kuenea na kuvuka mipaka ya huyo Mkuu wake?" (Yesu anatawala mbinguni, siyo ulimwenguni; imekuwa-kuwaje, basi, ya kwamba papa amevuka

mipaka na kuutawala ulimwengu huu?)" - D'Aubigne, b. 6, sura ya 3. [GC 140.4; PK Aya ya 60]

Aliandika maneno haya kwa vyuo vikuu: "Mimi naogopa sana kwamba vyuo vikuu vinaweza kuwa malango makuu ya kuingilia jehanum, visipofanya kazi kwa bidii ya kuyafafanua Maandiko Matakatifu, na kisha kuyakazia, kwa kuyanakshi katika mioyo ya vijana. Simshauri mtu yeyote kumpeleka mtoto wake kule ambako Maandiko hayapewi kipaumbele au kushika nafasi kubwa. Kila taasisi ambayo ndani yake watu hawajishugulishi kujifunza Neno la Mungu bila kukoma ni lazima tu itapotoka na kuwa na ufisadi."- Ibid., b. 6, sura ya 3. [GC 140.5; PK Aya ya 61]

Wito huo ulisambazwa kwa haraka sana katika Ujerumani yote na kuwa na ushawishi wenye nguvu juu ya watu. Taifa zima lilitaharuki na kuamka usingizini, na watu wengi wakawa wameamshwa na kuunga mkono bendera ya Matengenezo ya Kanisa. Wapinzani wa Luther, wakiwa na msukumo wa kulipiza kisasi ndani ya mioyo yao, walimsihi sana papa kuchukua hatua kali na zenye kudhamiria dhidi yake. Amri ikatolewa iliyosema kwamba mafundisho yake yalaaniwe na kupigwa marufuku mara moja. Mwanamatengenezo pamoja na wafuasi wake walipewa siku sitini, baada ya siku hizo kupita kama wangekuwa hawajayakana mafundisho yao, basi, wote wangepaswa kuondolewa katika ushirika wa kanisa. [GC 141.1; PK Aya ya 62]

### Hali Ya Kutisha

Hilo lilikuwa janga la dharura na kutisha kwa Matengenezo ya Kanisa. Kwa karne nyingi ile hukumu iliyotolewa na Rumi ya kutengwa na kanisa iliwatia hofu kuu wafalme wenye nguvu; dola zenye nguvu zilikuwa zimejazwa na misiba na maangamizi na ukiwa. Wale waliokumbwa na hukumu hii walitazamwa na watu kwa woga, mshtuko na huzuni kuu; walitengwa wasiweze kuongea na wenzao, tena walitendewa kama vile ni maharamia waliopaswa kusakwa na kuangamizwa kabisa. Luther hakuwa kipofu kwa tufani iliyokuwa karibu kumpasukia; ila alisimama imara, akimtegemea Kristo kama Ndiye msaada na ngao yake. Akiwa anayo imani ya mfia dini na ujasiri, aliandika, akisema: "Kile kinachokaribia kutokea mimi sikijui, na wala sitaki kujishugulisha nacho kwamba nikijue.... Liache pigo hilo lianguke liwezapo kuanguka na kuangaza, mimi sina woga wowote. Hakuna hata jani linaloweza kuanguka chini bila ya mapenzi ya Baba yetu. Ni kwa hakika ilioje basi, kwamba Yeye anatujali sisi! Ni jambo jepesi kabisa kufa kwa ajili ya Neno, kwa sababu Yule Neno aliyefanyika mwili Yeye Mwenyewe alikufa. Tukifa pamoja Naye, basi tutaishi pamoja Yeye; na kwa kupitia pale ambapo Yeye amepita kabla yetu, tutakuwa mahali pale alipo na kuishi na Yeye milele zote." - Ibid., 3d London ed., Walther, 1840, b. 6, sura ya 9. [GC 141.2; PK Aya ya 63]

Amri ya papa (bulla-fahali) ilipomfikia Luther, alisema hivi: “Mimi naidharau kabisa na kuishambulia kwa kuwa hiyo ni barua ovu na ya uongo.... Ni Kristo hasa Ndiye anayeshutumiwa ndani humo.... Nafurahi sana kuweza kustahimili maumivu kama hayo kwa ajili ya kazi hii iliyo bora kuliko zote. Tayari nimekwisha kusikia ndani ya moyo wangu uhuru mkubwa; kwa maana hatimaye mimi nimejua kwamba papa ndiye Mpinga Kristo, na ya kwamba kiti chake cha enzi ni kile cha Shetani mwenyewe.” - D'Aubigne, b. 6, sura ya 9. [GC 141.3; PK Aya ya 64]

Hata hivyo, amri toka Rumi haikupita bure bila madhara yake. Gereza, mateso, na upanga zilikuwa ndizo silaha zake zenye nguvu zilizoshinikiza utii kwake (Dan. 11:32-35). Wale waliokuwa dhaifu na wenye imani za kishirikina walitetemeka mbele ya amri hii ya papa; na ijapokuwa watu wengi walimwonea huruma Luther, wengi waliona kwamba maisha yao yalikuwa ni ya thamani mno kwao kuweza kujitia hatarini katika kazi hii ya harakati ya Matengenezo ya Kanisa. Kila kitu kilikuwa kinaashiria kana kwamba kazi ya Mwanamatengenezo huyu ilikuwa inakaribia kufungwa. [GC 142.1; PK Aya ya 65]

Lakini Luther bado alikuwa hana hofu yoyote. Rumi ilikuwa imemwaga radi ya laana zake, na ulimwengu ukawa unaangalia kile kilichokuwa kinaendelea, nao haukutazamia jambo lolote isipokuwa kuangamizwa kwake au kulazimishwa kujisalimisha na  kuwatii kwa kutangua. Lakini kwa  nguvu za kutisha, alirudisha (Rumi) laana ile ile na kutangaza hadharani azimio lake la kuachana naye milele. Mbele ya kundi la wanafunzi, madaktari wa falsafa wa theolojia (wa dini), na wakazi wa matabaka yote, Luther aliichoma barua ile ya papa, iliyokuwa na kanuni za kanisa lile, na mkusanyiko wa amri za upapa (decretals), na maandishi fulani yaliyowezesha  mamlaka hii ya kipapa kuendelea. “Maadui zangu, wameweza kwa kuvichoma vitabu vyangu,” alisema, “kujeruhi kazi hii ya ‘Ukweli’ katika mawazo ya watu wote, na kuziangamiza roho zao; kwa sababu hiyo, mimi nami nilivichoma moto vitabu vyao kulipiza kisasi. Mgogoro mkubwa ulikuwa umeanza. Mpaka sasa nilikuwa nachezacheza tu na papa. Nilianza kazi hii katika Jina la Mungu; nayo itakwisha bila ya mimi, na kwa uwezo Wake Yeye.” - Ibid., b. 6, sura ya 10. [GC 142.2; PK Aya ya 66]

**Neno La Mungu**

Kuhusu makaripio yaliyotoka kwa maadui zake waliokuwa wakimkejeli ili wamuudhi kwa kusema kazi yake ni dhaifu, Luther alijibu, akisema: “Ni nani ajuaye kama Mungu hajanichagua mimi na kuniita, na ya kuwa watu wangepaswa kuogopa kwamba, kwa kule kunidhihaki na kunidharau mimi, basi wanamdhihaki Mungu Mwenyewe? Musa alikuwa peke yake alipotoka Misri; Eliya alikuwa peke yake katika enzi ya utawala wa hububujika mfalme Ahabu; Isaya alikuwa peke

yake kule Yerusalemu; Ezekieli alikuwa peke yake kule Babeli.... Kamwe Mungu hakupata kumchagua kama nabii kuhani mkuu, ama mtu mwingine awaye yoyote aliye mashuhuri au nwenye cheo kikubwa; bali kwa kawaida aliwachagua watu wa hali ya chini, waliokuwa wanadharauliwa, kuna wakati alimchagua hata mchungaji wa kondoo, Amosi. Katika kila zama, watakatifu wa Bwana walilazimika kuwakosoa wakuu, wafalme, watawala, makuhani, na wenye hekima, kwa kuhatarisha maisha yao.... Sisemi kwamba mimi ni nabii; ila nasema kwamba inawapasa wao kuogopa sana, kwa sababu mimi niko peke yangu na wao wapo wengi. Nina uhakika na jambo hili, kwamba Neno la Mungu liko ndani yangu, na ya kwamba Neno hilo haliko pamoja nao." - Ibid., b. 6, sura ya 10. [GC 142.3; PK Aya ya 67]

Hata hivyo, haikuwa bila mashindano makali ya kutisha ndani ya moyo wake mwenyewe, na ndipo Luther alipotoa uamuzi wa kujitenga kabisa na kanisa la Rumi. Ilikuwa ni katika wakati kama huu ndipo alipoandika na kusema: "kila siku iendayo kwa Mungu, nahisi zaidi na zaidi ugumu wa kutupilia kando uelewa ambao mtu amejifunza tokea utotoni. Jamani! Ni mateso makali kiasi gani niliyokwisha kuyapata kutokana na uhalisia huo, ingawa nilikuwa na Maandiko upande wangu kunihakikishia mimi kuwa inanipasa kuthubutu kusimama peke yangu kinyume na papa, na kumfichua hadharani kuwa yeye ndiye Mpinga Kristo! Mateso ya moyo wangu yamekuwa makubwa kiasi gani? Ni mara ngapi nimejiuliza mwenyewe kwa uchungu maswali yale ambayo mara kwa mara yalikuwa vinywani mwa wafuasi wa papa: 'Je! Ni wewe peke yako ndiwe uliye na busara? Je! kila mtu anaweza kuwa amekosea isipokuwa wewe? Je, Itakuwaje basi, ikiwa hata hivyo, ni wewe ndiwe hauko sahihi na ndiye ambaye unawajumuisha watu wengine katika makosa yako, na hatimaye watu hawa waangamie milele?' Hivyo ndivyo mimi nilivyopigana na nafsi yangu mwenyewe, na Shetani, mpaka Kristo kwa Neno Lake lisiloweza kukosea kamwe, alipouimarisha moyo wangu dhidi ya mashaka niliyokuwa nayo." - Martyn, ukurasa wa 372, 373. [GC 143.1; PK Aya ya 68]

**Pambano Kuu**

Papa alikuwa amemtishia Luther kumfuta ushirika wa kanisa endapo angekuwa hajayakanusha mafundisho yake, na tishio hilo sasa likawa limetekelezwa. Amri mpya ya papa ikaonekana (bulla-fahali), ikitangaza kutengwa kabisa kwa Mwanamatengenezo na Kanisa la Rumi, akimshutumu kuwa alikuwa amelaaniwa na mbingu, na katika hukumu yake aliwajumuisha wale wote watakaoyapokea mafundisho yake ya dini. Pambano kubwa likawa limekwishaingiwa kikamilifu. [GC 143.2; PK Aya ya 69]

Kukabiliwa na upinzani ni fungu linalowakabili wote wanaotumiwa na Mungu kuzihubiri Kweli mahsusi ambazo zinahusika na kufaa hasa kwa ajili ya wakati

wao. (Mithali 4:18). Palikuwa na Ukweli wa Leo katika siku za Luther, - Ukweli ambao ulikuwa na umuhimu maalum kwa wakati huo; Na siku zetu hizi pia, upo Ukweli wa leo kwa ajili ya kanisa la nyakati hizi. Yeyote Yule atendaye mambo yote kulingana na mashauri na mapenzi Yake Mungu ambaye amependezwa kuwaweka watu katika hali mbali mbali na kuwaagiza wafanye majukumu maalumu kwa nyakati wanazoishi pamoja na mazingira ambayo wamewekwa. Kama wangeweza kuithamini nuru ile waliyopewa, mitazamo mipana ya Ukweli ingeendelea kufunuliwa mbele yao. Lakini basi, ile Kweli huwa haipendwi sana na watu wengi siku hizi kuliko vile ilivyokuwa inapendwa na wafuasi wa upapa waliompinga Luther. Kuna mwelekeo ule ule wa kupokea nadharia na mapokeo ya wanadamu badala ya Neno la Mungu kama ilivyokuwa mnamo zama za kale. Wale wanaowakilisha Ukweli kwa ajili ya wakati huu wasitegemee kupokelewa na watu kwa furaha au upendeleo mkubwa kuliko walivyopokewa Wanamatengenezo wa zama zilizopita. Pambano kuu kati ya Ukweli na makosa, kati ya Kristo na Shetani, litazidi kuongezeka katika ukali na kasi yake hadi kufungwa kwa historia ya ulimwengu huu (mwisho wa dunia). [GC 143.3; PK Aya ya 70]

Yesu akawaambia wanafunzi Wake Maneno haya: “Kama mngekuwa wa ulimwengu, ulimwengu ungewapenda walio wake; lakini kwa kuwa ninyi si wa ulimwengu, bali Mimi naliwachagua katika ulimwengu, kwa sababu hiyo ulimwengu huwachukia. Likumbukeni lile Neno nililowaambia, Mtumwa si mkubwa kuliko bwana wake. Ikiwa waliniudhi (walinitesa) Mimi, watawaudhi ninyi; ikiwa walilishika Neno Langu watalishika na lenu.” Yohana 15:19, 20. Na kwa upande mwingine Bwana wetu alitangaza waziwazi, alisema: “Ole wenu ninyi watu wote watakapowasifu, kwa kuwa baba zao waliwatenda manabii wa uongo mambo kama hayo.” Luka 6:26. Roho ya ulimwengu huu haipatani au amani sana na roho ya Kristo hivi leo kama ilivyokuwa katika nyakati zile za awali, tena wale wanaolihubiri sasa Neno la Mungu katika usafi Wake, hawawezi kupokelewa kwa upendeleo mkubwa sasa kuliko wakati ule. Miundo ya upinzani dhidi ya Ukweli huenda inaweza kubadilika yaani, uadui huo unaweza kuwa haujionyeshi kwa wazi sana kwa sababu umefichwa chini-chini sana kwa hila; lakini uhasama ule ule bado upo, nao utaendelea kudhihirika hadi mwisho wa wakati. [GC 144.1; PK Aya ya 71]

# SURA YA 8

# LUTHER MBELE YA BARAZA

## (Mtetezi Mkuu Wa Kweli Mbele Ya Baraza Liitwalo Diet Kijerumani Kule Worms)

Ufupisho: Charles V (1500-1558) alionekana kana kwamba ni mtu aliyekuja kwa wakati wake akiwa na umri wa miaka 21: Mfalme huyu wa Dola ya Ujerumani alikutana na Martin Luther, na hapo changamoto zake zikaanza, alikuwa na migogoro katika maisha yake yote, na mwishowe hakushinda. Luther hapa anatetea Neno la Mungu mbele ya watu mashuhuri duniani, japo alikuwa katika hatari kubwa ya kifo. Baraza lilifanyika Nov 1520 na Luther alifika pale kwenye baraza April 17, 1521 na kutoa maelezo yake siku iliyofuata. Alipotoroshwa kwenye Kasiri la Wartburg, alianza kutafsiri Biblia kwa Kijerumani Desemba 1521, na ikachapwa Septemba, 1522. Wakati huo Johannes Guternberg alikuwa amevumbua mashine ya kuchapa mwaka 1456. Kisa hiki unapaswa kukisoma mwenyewe.

Mfalme mkuu mpya, Charles wa V, alikuwa ndiyo tu amesimikwa rasmi ili kukalia kiti cha enzi huko Ujerumani na ndipo wawakilishi wa kanisa la Rumi walipoharakisha kumpa salaam zao za pongezi na kumshawishi mfalme kutumia

madaraka kusitisha matengenezo ya kanisa. Kwa upande mwingine, Elekta wa Saxony, mwenye haki ya kumteua mfalme, ambaye kwake Charles aliwiwa sana kwa kuchangia kumweka madarakani, alimsihi asichukue hatua yoyote dhidi ya Luther hadi hapo atakapompa nafasi ya kumsikiliza. Kwahiyo mfalme huyo akajikuta katika hali ya mtanziko na aibu kubwa. Wafuasi wa papa wasingetosheka na chochote pungufu ya amri ya kifalme ya kumhukumu Luther kifo (kuuawa). Elekta alikuwa ametangaza kwa ujasiri kwamba "Mfalme mwenyewe, au wasaidizi wake, au mtu mwingine yeyote hawakuona mahali ambapo maandishi ya Luther yalikuwa yamekanushwa;" hivyo aliomba "kwamba Dk. Luther apewe hati ya kumhakikisha kusafiri salama ili aweze kufika mbele ya mahakama ya majaji wasomi, wacha Mungu, na wasio na upendeleo."- D'Aubigne, b. 6, sura ya 11. [GC 145.1; PK Aya ya 1]

Macho na umakini wa watu wote sasa vilielekezwa kwa wale waliokusanyika kwenye baraza la majimbo kule Worms (voms) Ujerumani mara tu baada ya Charles kuingia madarakani kwenye dola hiyo. Yalikuweko masuala na hoja muhimu za kisiasa zilizokusudiwa kujadiliwa na baraza hili kuu la taifa; kwa mara yao ya kwanza watawala hawa wa Ujerumani walitakiwa kukutana na mfalme wao kijana katika mkutano wa kujadiliana hoja mbalimbali. Kutoka kwenye sehemu zote za nchi ya mababa zao walikuja viongozi wa kanisa na serikali. Mabwana au wakuu wa serikali, watu waliozaliwa kwenye koo za vyeo vya juu, watu wenye mamlaka makubwa na wenye wivu katika kutetea madaraka yao na nafasi walizorithishwa; viongozi wa juu wa kanisa, wakionyesha utambuzi vyeo na mamlaka yao; wakuu wanaosimamia sheria za nchi na walinzi wao wenye silaha; na mabalozi toka nchi za kigeni na za mbali,-- wote walikusanyika huko Worms (Voms). Ila katika mkutano huo mkubwa, mada ambayo iliibua shauku kubwa miongoni mwa watu ilikuwa kazi ya Mwanamatengezo wa Saxony. [GC 145.2; PK Aya ya 2]

Hapo awali Charles alikuwa amemwemwagiza kiongozi wa jimbo la Saxony ampeleke Luther kwenye baraza, akimhakikishia ulinzi wake, na kuahidi kuwa na mjadala huru pamoja na watu wenye sifa za ujuzi wa zile hoja zilizokuwa zinabishaniwa. Luther alikuwa na shauku ya kufika mbele za mfalme wa dola. Afya yake wakati huu ilikuwa imezorota na kuwa hafifu sana; ila bado alimwandikia Kiongozi wa Saxony: "Ikiwa mimi sitaweza kwenda huko Worms nikiwa na afya njema, basi nitabebwa kwenda huko, nikiwa mgonjwa kama nilivyo. Kwa maana ikiwa Mfalme ananiita, siwezi kuwa na mashaka kuwa huo ni wito wa Mungu Mwenyewe. Ikiwa wanatamani kutumia ukatili dhidi yangu, na hilo linawezekana kabisa (maana hawakuniamuru kufika kule kwa mapenzi yao wenyewe), mimi ninaweka jambo hilo mikononi mwa Bwana. Kwani Yeye bado Yu hai, na tena bado anatawala, ni Yeye Ndiye aliyewaokoa vijana watatu katika tanuru lililokuwa linawaka moto. Hata kama hataniokoa mimi, maisha yangu

hayana maana sana. Hebu sisi tuepushe tu injili isiwekwe mahali ambapo itadharauliwa na waovu, na hebu damu yetu imwagike kwa ajili ya injili, ili tusitoe nafasi ya wao kushinda. Si juu yangu mimi kuamua kama kuishi kwangu au kifo changu ndiyo kitatoa mchango wangu mkubwa kwa wokovu wa wote..... Unaweza kutarajia yote kutoka kwangu-- isipokuwa kukimbia na kukana Imani. Kutimua mbio mimi siwezi, na bado siwezi kukana au kutangua nilichosema naamini."- Ibid., b 7, sura ya 1. [GC 146.1; PK Aya ya 3]

Habari ziliposambazwa pale Worms kwamba Luther anatazamiwa kuhudhuria mbele ya Baraza kuu la taifa, watu wote walitaharuki. Aleander, mwakilishi wa Papa ambaye alikabidhiwa dhamana maalumu ya kesi hiyo, alishtushwa na kughadhabika. Aliona kuwa matokeo yangekuwa mabaya katika kazi ya upapa. Kuanzisha uchunguzi juu ya kesi ambayo Papa alikuwa ameshatangaza tayari hukumu ya kulaani ingekuwa ni kuidharau mamlaka papa mkuu. Kwa kuongezea, alikuwa na hofu kuwa hoja zile zenye nguvu, ufasaha na uimara za mtu huyu lazima zingeweza kuwafanya wakuu wengi kuyapa kisogo madai na maslahi ya Upapa. Kwa hivyo, kwa njia ya mkazo na kuonyesha jambo hili ni la dharura, alimsihi Charles asimlete Luther huko Worms. Karibu na wakati huo huo, barua yenye amri ya papa (bulla) iliyotangaza kuwa Luther ameshatengwa ilichapishwa; na hili likijumuishwa pamoja na mawasilisho ya mwakilishi wa papa, vilimshawishi mfalme wa dola kukubali. Alimwandikia kiongozi wa Saxony kwamba kama Luther hawezi kukana mafundisho yake, basi inampasa abakie huko-huko Wittenberg. [GC 146.2; PK Aya ya 4]

Akiwa hajaridhishwa bado na ushindi huu, Aleander alijitahidi kufanya kazi kwa nguvu zote na hila zote alizoweza ili Luther aweze kupata adhabu. Kwa kung'ang'ania kunakopaswa kufanywa kwa mambo yaliyo mema kuliko hayo, alishinikiza kwamba jambo hilo lipate kufikiriwa na watawala wa serikali, maaskofu, na wajumbe wengine wa baraza kuu la taifa, akamshtaki Mwanamatengenezo kwa kuwachochea watu kuiasi serikali, kupinga uongozi hadharani, kuishi maisha ya dhambi, na kufuru." Lakini ukali na harara aliyoidhihirisha mwakilishi ikaifunua kwa wazi mno ile roho iliyokuwa inamsukuma ndani yake. "Anasukumwa na chuki na kulipiza kisasi," ulikuwa ndiyo mtazamo wa watu wengi kwa jumla, "zaidi kuliko ari ya upendo na ucha Mungu."- Ibid., b. 7, sura ya 1. Watu wengi waliokuwa Barazani wakavutiwa na kazi aliyokuwa anaifanya Luther zaidi, nayo ikapata upendeleo kuliko huko nyuma. (Diet of Worms au Baraza la Worms) [GC 147.1; PK Aya ya 5]

Kwa juhudi iliyoongezwa maradufu, Aleander alimsisitizia mfalme wa dola kwamba wajibu ulikuwa kutekeleza amri za papa. Lakini kwa mujibu wa sheria za Ujerumani jambo hili lisingeweza kufanywa bila watawala wengine kuridhika nalo; mwishowe akiwa amelemewa na usumbufu wa mwakilishi huyu wa papa, Charles alimwamuru awasilishe kesi yake mbele za Baraza kuu la taifa *(Diet kwa*

*kijerumani).* "Ilikuwa siku ya kujivunia kwa mjumbe huyo wa papa (nuncio). Baraza lilikuwa kubwa na hoja ile ilikuwa ni kubwa zaidi. Aleander alipaswa kuitetea Rumi,……mama na kimada mwenye mamlaka kwa makanisa yote." Alitakiwa kuutetea na kuuthibithisha ukuu wa Petro mbele ya baraza la wakuu katika ulimwengu wa Kikristo. "Alikuwa na kipawa cha ufasaha, naye alikuwa amejiandaa vya kutosha kulingana na tukio, na akafanya jambo linalopaswa kushinda magumu yaliyojitokeza. Uongozi wa Mungu (majaliwa Yake) ulikuwa umeamuru kuwa Rumi ianze kujitetea kwanza kupitia kwa mmoja wa wanenaji wake mahiri, na wenye uwezo mkubwa, mbele ya Baraza la majaji linaloheshimiwa kupita mabaraza yote kabla ya kushutumiwa kwake."- Wylie, b. 6, sura ya 4. Wale waliopendelea kazi ya Mwanamatengenezo, wakiwa hawajafurahia jambo hilo ila hawakuwa na jinsi ya kuliepuka, walisubiri waone matokeo ya hotuba ya Aleander. Kiongozi wa Saxony mwenye haki ya kumteua mfalme hakuwepo pale (Elekta wa Saxony Frederick III), lakini kwa maelekezo yake baadhi ya wajumbe wake walihudhuria ili kuandika maelezo ya hotuba ya mwakilishi huyo wa papa. *(hapa ndiyo tunapata jina mashuhuri kwenye matengenezo -Diet of Worms-Baraza lililokutana kwenye mji wa Worms kushugulika na kesi ya Luther) [GC 147.2; PK Aya ya 6]

**Ashtakiwa Kwa Uzushi**

Kwa uwezo wake wote unaolingana na usomi na ufasaha wake, Aleandar alijizatiti kuupindua ile Ukweli. Shitaka baada ya shtaka lilirushwa dhidi ya Luther kuonyesha kwamba yeye ni adui wa kanisa na serikali, adui wa walio hai na wafu, adui viongozi wa kanisa waliowekewa mkono na walei, adui wa mabaraza mbalimbali na Wakristo wanaojitegemea au wenye huduma binafsi (self supporting). "katika makosa ya Luther," akatangaza "ni mambo tosha kabisa," yanayowastahilisha adhabu ya kuchomwa moto "wazushi wapatao laki moja" [GC 148.1; PK Aya ya 7]

Katika kuhitimsha hotuba yake alijaribu kuonyesha dharau kwa wafuasi wa imani ya matengenezo, akisema: "Hivi hawa Walutheri ni kitu gani kweli? Hawa ni waalimu waasi, makasisi wafisadi, watawa waovu, wanasheria wajinga, na waungwana na wakuu walioshushwa hadhi yao, wakijumuisha watu wa kawaida ambao wamewapotosha na kuwaharibu. Kundi la wakatoliki linawazidi hawa kwa mbali kiasi gani basi kwa idadi, uwezo, na nguvu kuliko wao! Amri itakayotolewa kwa kauli moja kutoka katika mkutano huu itawatia nuru hao wajinga, na kuwaonya wale wasiokuwa na busara, na kuwafanya wale wanaomangamanga kwa kutokuwa na msimamo wakate shauri, na kuwapa nguvu wale walio dhaifu." - D'Aubigne, kitabu cha 7, sura ya 3. [GC 148.2; PK Aya ya 8]

Watetezi wa Ukweli wamekuwa wakishambuliwa katika kila zama, kwa silaha kama hizo. Hoja hizo hizo bado zinatumika dhidi ya wote ambao wanathubutu kuwasilisha mafundisho yaliyo wazi, na yenye unyofu wa Neno la Mungu, kinyume na mafundisho ya wanadamu, yenye makosa/uongo uliojiimarisha. “Hawa wanaohubiri mafundisho hayo mageni/mapya ni akina nani?” wanasema kwa mshangao wale wanaotaka dini mashuhuri, inayopendwa na watu wengi. “ni watu wasio na kisomo, ni wachache kwa idadi, na tena wanatoka katika tabaka la watu maskini sana. Na bado wanadai kwamba wanao Ukweli, na ya kwamba wao ndio watu waliochaguliwa na Mungu. Hao ni wajinga, tena wamedanganyika. Kwa idadi ya watu kanisa letu ni bora zaidi na tena lina mvuto mkubwa zaidi kwa kiasi gani basi! Ni watu wangapi ambao wana elimu ya juu miongoni mwetu! Upande wetu una nguvu kubwa iliyoje” Hizo ndizo hoja za kubishania, na zilizo na mvuto mkubwa katika ulimwengu wetu huu; lakini hoja hizi peke yake hazitoshi kabisa kuhitimisha mambo kama ilivyokuwa katika siku zile za Mwanamatengenezo Luther. [GC 148.3; PK Aya ya 9]

Matengenezo ya Kanisa hayakuishia kwa Luther kama wengi wanavyodhani. Yataendelea hadi mwisho wa historia ya ulimwengu huu (haijalishi). Luther alikuwa na kazi kubwa ya kufanya katika kuwaakisia wengine nuru ile ambayo Mungu alikuwa ameruhusu imwangazie; hata hivyo hakupokea nuru yote ambayo ulimwengu ulipaswa kupewa. Tangu wakati huo hadi sasa, nuru mpya imekuwa ikiendelea kuangaza kutoka katika Maandiko daima, na Kweli mpya zimekuwa zikiendelea kufunuliwa. (Mithali 4:18). [GC 148.4; PK Aya ya 10]

**Ushindi Dhahiri**

Hotuba ya mwakilishi wa papa ilikuwa na mguso mkubwa kwa wajumbe wa Baraza kuu la taifa (Diet). Luther, ambaye ndiye alikuwa na ule Ukweli wa wazi na unaoshawishi wa Neno la Mungu ili kumzima mtetezi shujaa wa papa hakuwepo pale mkutanoni. Hakuna aliyejaribu kufanya jitihada yoyote kumtetea Mwanamatengenezo huyu. Mioyo ya wengi ilijidhihirisha pale, sio tu katika kutaka kumshutumu Luther pamoja na mafundisho aliyoyafundisha, bali pia, kama ingewezekana, kuung’oa kabisa uzushi ule. Rumi ilikuwa imefaidi kuipata fursa nzuri mno ya kuyatetea madai yake. Yale yote iliyoweza kusema katika kujitetea au kujilinda yenyewe (na kulipiza kisasi) yalikuwa yamekwisha kusemwa. Lakini ule mwonekano wa ushindi kwa kanisa uliashiria kushindwa kwake. Tangu pale tofauti kati ya Ukweli na uongo ikaanza kuwa wazi kabisa, maana sasa walikuwa wanaenda kuingia nje, kwenye uwanja mkubwa na kupambana waziwazi na kila mtu angelishuhudia. Kamwe Rumi isingeweza kusimama kwa usalama tena kutoka siku hiyo kama ambavyo ilikuwa imesimama kabla ya hapo. [GC 149.1; PK Aya ya 11]

Wakati ambapo wengi miongoni mwa wajumbe wa Baraza wasingesita kumtoa Luther ili apate adhabu ya kisasi cha Rumi, sasa wengi wao waliona kupindapinda kwa maadili na kushtuka, na hivyo wakalaumu uovu uliokuwepo ndani ya kanisa hili la Rumi na wakatamani kukomeshwa kwa mateso/uonevu waliokuwa wametendewa Wajerumani kama matokeo ya ufisadi na uchu wa uongozi wa hierakia wa kanisa (hierarchy). Yule balozi alikuwa ameuwasilisha utawala wa papa kwa nuru ya kuupendelea kwa hali ya juu. Sasa Bwana alimsukuma mjumbe mmoja wa Baraza lile kutoa picha sahihi ya matokeo ya ukatili wa papa. Kwa uthabiti mzuri wa kiungwana, George, mwana wa mfalme wa Saxony alisimama katika ukumbi huo wa watawala na kutaja kwa kinagaubaga na usahihi wa kutisha, udanganyifu na machukizo ya upapa na matokeo yake mabaya. Wakati akifunga alisema hivi: [GC 149.2; PK Aya ya 12]

"Hizi ni baadhi ya dhuluma ambazo zinapiga kelele dhidi ya Rumi. Aibu yote imewekwa kwenye kona pembeni na lengo lao pekee ni pesa, pesa, pesa,…… kiasi kwamba hata wale wahubiri ambao wanapaswa kufundisha Ukweli, wasiseme chochote zaidi ya uongo mtupu, na sio tu kwamba wanavumiliwa, lakini pia wanazawadiwa, kwa sababu kadiri uongo wao unavyokuwa mkubwa zaidi, ndivyo mapato yao yanavyozidi kuwa makubwa zaidi. Ni kutoka katika chemchemi hiyo ya maji-taka yanayonuka, ndiyo maji haya machafu na yaliyo na uvundo hutiririka. Ubaradhifu, uasherati na ulevi unayosha mkono wake kwa ile tamaa kubwa ya kujipatia mali nyingi .... Uwii! Hiyo ni kashfa inayosababishwa na hao viongozi wa kidini waliowekewa mkono, ambayo inazirusha roho za watu wengi masikini katika hukumu ya milele. Ni sharti Matengenezo makubwa yafanyike"- Ibid., Kitabu cha. 7, sura ya 4. [GC 149.3; PK Aya ya 13]

Ukosoaji wenye uwezo na nguvu zaidi wa manyanyaso ya upapa usingeweza kuwasilishwa na Luther mwenyewe vyema zaidi kama vile ilivyokuwa; na ule ukweli kwamba mzungumzaji huyu alikuwa ni adui aliyedhamiria na mkubwa zaidi wa mwanamatengenezo, uliyapa ushawishi mkubwa zaidi maneno yake. [GC 150.1; PK Aya ya 14]

Endapo macho ya wajumbe wa mkutano ule yangekuwa yamefumbuliwa, wangeweza kuwaona malaika wa Mungu katikati yao wakimulika miale ya nuru ili kupukutisha giza la mafundisho ya uongo (makosa) na kuzifungua akili na mioyo ili wapokee Ukweli. Ulikuwa ni uweza wa Mungu wa Ukweli na hekima Yake, uliwaongoza hata maadui wa Matengenezo, na hivyo kutayarisha njia kwa ajili ya kazi kubwa iliyokuwa karibu kufanyika. Martin Luther hakuwapo pale; lakini sauti ya Yule aliye Mkuu kuliko Luther ilikuwa imesikika katika mkutano ule. [GC 150.2; PK Aya ya 15]

**Apewa Hati Ya Kuitwa Mbele ya Baraza**

Kamati ikaundwa mara moja na Baraza ili kuandaa orodha ya manyanyaso ya upapa ambayo yaliwalemea sana watu wa Ujerumani kwa ukandamizaji/uonevu wake. Orodha hii, iliyokuwa na vipengele mahsusi mia moja na moja, iliwasilishwa kwa mfalme wa dola pamoja na ombi kuwa achukue hatua za haraka ili kuondoa unyanyasaji ule. "Ni hasara kubwa kiasi gani kwa kupoteza roho za Wakristo," wakasema wale waliokuwa wanasihi "ni uporaji ulioje huo, ni utozaji wa fedha kwa mabavu ulioje, unaowakabili watu kwasababu ya kashfa zinazomzunguka yule aliye kiongozi wa kiroho wa jamii ya Wakristo duniani! Ni wajibu wetu kuzuia maangamizi na mambo haya yanayowadhalilisha watu wetu. Kwa sababu hiyo, kwa unyenyekevu mkubwa, lakini kwa msisitizo mkubwa kwa kuwa jambo hili ni la dharura, tunakuomba kwa heshima, utoe amri ya kufanya marekebisho/matengenezo makubwa katika nyanja zote, na uhakikishe utekelezaji wake (yakamilishwe)." Ibid., kitabu cha 7, sura ya 4. [GC 150.3; PK Aya ya 16]

Sasa baraza sasa likadai Mwanamatengenezo ajiwasilishe mbele yao. Licha ya kusihi, mapingamizi na vitisho vya Aleander, mwisho wake mfalme alikubali na Luther akapelekewa hati ya kumwamuru aje mbele ya Baraza. Pamoja na wito huo wa kuja mbele ya baraza kwa maandishi, alipewa pia cheti cha uhakikisho wa kusafiri kwa usalama kwenda huko, na akahakikishiwa tena kuwa atarejea kwake akiwa salama. Nyaraka hizo zilipelekwa Wittenberg na mjumbe, aliyekuwa ameagizwa kumleta katika jiji la Worms. [GC 150.4; PK Aya ya 17]

Marafiki zake Luther waliingia hofu na fadhaa. Wakiwa wanaitambua chuki na uadui uliokuwapo dhidi yake, waliogopa kwamba hata cheti chake cha kumhakikishia usalama kisingeweza kuheshimiwa, nao wakamsihi sana asihatarishe maisha yake. Yeye Alijibu hivi: "Wafuasi wa papa hawatamani nije huko Worms, bali wanataka nihukumiwe, na kuuawa. Hilo siyo tatizo kwangu, msitoe sala kwa ajili yangu, bali kwa ajili ya Neno la Mungu.....Kristo atanipa Roho Wake kushinda wahudumu wa uovu/makosa. Mimi, katika maisha yangu, nimechukizwa nao, nao nitawashinda kabisa kwa kifo changu. Wanajishughulisha sana kule Worms ili kunilazimisha mimi nitangue mafundisho yangu; na huku kutakuwa ndiko kukana kwangu: nilisema awali kwamba papa alikuwa ni mwakilishi wa Kristo; ila sasa ninasisitiza kwamba yeye ni mpinzani mkubwa wa Bwana wetu na mtume wa Shetani."- Ibid., b. 7, sura ya 6. [GC 150.5; PK Aya ya 18]

### Matarajio Ya Kukutana Na Mambo Mazito

Luther hakupaswa kuifanya safari yake ya kuhatarisha peke yake. Kando na mjumbe wa serikali ya kifalme, marafiki zake watatu wa karibu waliamua kumsindikiza. Melanchthon alitamani sana kwa moyo wake wote kujiunga nao. Moyo wake ulikuwa umeshikamana na ule wa Luther kwa ukaribu sana, naye

alitamani kujiunga nao na ikiwa itabidi gerezani au hata mautini. Lakini matakwa yake yalikataliwa. Endapo Luther angeangamia, basi matumaini ya Matengenezo ya kanisa sharti yangebaki kwa huyu mtendakazi mwenzake kijana. Mwanamatengenezo wakati akiagana na Melanchthon alimwambia maneno haya: “Kama sitarejea na maadui zangu wakaniua, wewe endelea kufundisha na simama imara katika Ukweli. Fanya kazi hiyo badala yangu..... Ikiwa wewe upo hai bado, kifo changu kitakuwa na athari/madhara madogo sana.” Ibid., kitabu cha 7, sura ya 7. Wanafunzi na raia ambao walikuwa wamekusanyika kushuhudia kuondoka kwake Luther waliguswa sana. Umati mkubwa ambao mioyo yao ilikuwa imeguswa na injili, walimuaga huku wakilia (buriani pengine!) Hivyo ndivyo Mwanamatengenezo na wasindikizaji wenzake walivyosafiri kutoka Wittenberg. [GC 151.1; PK Aya ya 19]

Wakiwa safarini waliona kuwa akili na mioyo ya watu yalikuwa yamelemewa na hisia nyingi za huzuni, kukata tamaa na hofu. Katika baadhi ya miji huwakuonyeshwa heshima yoyote. Waliposimama usiku ili wapate kupumzika na kulala, kasisi mmoja aliyekuwa rafiki yake Luther alionyesha hofu yake kwa kushikilia picha ya mwanamatengenezo wa Italia ambaye alikuwa ameuawa kwa ajili ya kutetea imani yake. Siku iliyofuata waligundua kwamba maandishi ya Luther yalikuwa yamepigwa marufuku kule jijini Worms. Wajumbe wa mfalme walikuwa wakitangaza amri ya mfalme wa dola na kutoa wito kwa watu kuleta mbele za mahakimu kazi hizo zilizopigwa marufuku (maandishi ya mafundisho ya matengenezo aliyoyaandika Luther). Mjumbe aliyekuwa msindikizaji, kwa kuhofia usalama wa Luther barazani, na kufikiria kuwa huenda azimio lake linaweza kutikiswa, aliuliza ikiwa bado alitaka kuendelea na safari. Alijibu: “Ingawa nimepigwa marufuku katika kila mji lakini nitaendelea mbele na safari.” Ibid., kitabu cha 7, sura ya 7. [GC 151.2; PK Aya ya 20]

### Kuhubiri Kule Erfurt

Huko mjini Erfurt, Luther alipokelewa kwa heshima. Akizungukwa na umati wa watu waliompenda, alipita katika mitaa ambayo alikuwa amepita mara nyingi na mkoba wake alipokuwa ‘mtawa ombaomba’. Akakitembelea chumba chake katika nyumba ya watawa, kisha akafikiria juu ya ule mgogoro mzito ambao kwa huo nuru sasa inafurika Ujerumani yote kwa wakati ule, nayo pia ilikuwa imeangaza moyoni mwake (kutoka chumba kile!). Aliombwa ahubiri pale. Hili lilikuwa jambo ambalo alikuwa amekatazwa kulifanya, lakini yule mpiga mbiu wa mfalme (mjumbe) alimpa ruhusa, ndipo yule mtawa, ambaye zamani alitumika kwa kazi duni na za kuchosha katika nyumba ile ya watawa, sasa alipanda mimbarani kuhubiri. [GC 152.1; PK Aya ya 21]

Kwenye mkutano uliokuwa umejaa watu wengi, Luther alinena nao maneno ya Kristo, “Amani na iwe kwenu.” “Wanafalsafa, wasomi, madaktari na waandishi,”

akasema, “wamejitahidi sana kuwafundisha watu njia ya kupata uzima wa milele, wala hawajafanikiwa…….. Sasa mimi nitawaelezea njia hiyo, Mungu amemfufua Mtu Mmoja kutoka kwa wafu, Bwana Yesu Kristo, ili apate kuiharibu mauti, kuikomesha kabisa dhambi na kufunga milango ya kuzimu. Hii ndio kazi ya wokovu.... Kristo ameshinda kabisa! Hii ndio habari njema yenye kuleta furaha; na sisi tunaokolewa kwa kazi Yake aliyoifanya na sio kutokana na kazi yetu wenyewe.... Bwana wetu Yesu Kristo alisema, ‘Amani iwe nanyi; tazameni Mikono Yangu;’ hiyo ni kusema, Tazama, Ee mwanadamu! ni Mimi, Mimi peke Yangu, ambaye nimechukua na kuziondoa dhambi zako na kukukomboa wewe; na sasa wewe unayo amani, Asema Bwana.” [GC 152.2; PK Aya ya 22]

Akaendelea, kuwaonyesha kwamba imani ya Kweli itadhihirishwa katika maisha matakatifu. “Kwa kuwa Mungu ametuokoa sisi, hebu na tupange kazi zetu, ili ziweke kukubalika Kwake. Je! Wewe ni tajiri? Basi hebu mali zako zishughulikie mahitaji ya maskini. Je! Wewe ni maskini? Hebu huduma yako na ikubalike mbele ya matajiri. Ikiwa kazi zako zinakubalika kwako wewe peke yako, huduma hiyo unayojifanya unamfanyia Mungu ni ya uongo.”-Ibid., kitabu cha. 7, sura ya 7. [GC 152.3; PK Aya ya 23]

Watu walisikiliza kwa butwaa (walitekewa). Mkate wa uzima ulikuwa ukimegwa kwa ajili ya watu wale waliokuwa na njaa. Kristo aliinuliwa mbele yao juu ya mapapa, mabalozi wa papa, watawala na wafalme wa himaya. Luther hakugusia chochote kuhusiana na hatari iliyomkabili mwenyewe. Hakutafuta wamfikirie yeye binafsi au kuwafanya wamwonee huruma. Katika kumtafakari Kristo alikuwa amesahau kujitazama mwenyewe. Alijificha nyuma ya Yule Mtu wa Kalvari, akitafuta tu kumwasilisha na kumhubiri Yesu kama Mkombozi pekee wa wenye dhambi. [GC 152.4; PK Aya ya 24]

### Ujasiri Wa Mfia Dini

Wakati Mwanamatengenezo akiendelea na safari yake, alitupiwa macho kila mahali kwa shauku kubwa. Umati wa watu wenye shauku ukamsonga na kumzunguka pande zote na sauti za marafiki zilimwonya juu ya kusudi la viongozi wa kanisa la Kirumi. “Watakuchoma moto,” wengine walisema, “na kuunguza mwili wako ubaki majivu, kama walivyofanya kwa John Huss.” Luther alijibu, “Hata kama wangewasha moto kutoka jiji la Worms hadi jiji la Wittenberg, na ndimi za moto zikafika mbinguni, nitapita katikati ya huo moto kwa Jina la Bwana, na kutokea mbele yao; nitaingia kupitia kinywa cha huyu mnyama wa kutisha kama behemoth* na kuyavunja meno yake, huku nikimkiri Bwana Yesu Kristo mbele yao.” - Ibid., kitabu cha 7, sura ya 7 **(pengine kiboko Dinosaur)* [GC 153.1; PK Aya ya 25]

Habari juu ya kukaribia kwake Worms ilisababisha umati mkubwa kuwa na ghasia. Marafiki zake wakatetemeka kuhofia usalama wake, maadui zake waliogopa kufanikiwa kwa mipango yao. Jitihada za nguvu zilifanywa ili kumshawishi asiingie mjini. Kwa msukumo wa watetezi wa papa aliombwa aende kupumzika nje ya mji kwenye kasri ya rafiki aliyekuwa askari wa nyumba ya mfalme ambaye alikuwa ni mtu mwema (knight), ambapo, ilitangazwa kwamba matatizo yote yangeweza kusuluhishwa kwa njia ya kirafiki. Marafiki zake walijitahidi kuchochea hofu yake kwa kuelezea hatari ambazo zingeweza kumkabili. Jitihada zao zote zilishindwa. Luther, bila kutetereka alitangaza: "Hata kuwe na mashetani wengi jijini Worms kama vigae kwenye paa la nyumba, bado mimi nitaingia tu humo." -Ibid., kitabu cha 7, sura ya 7. [GC 153.2; PK Aya ya 26]

**Kufika Worms**

Alipofika mjini Worms, umati mkubwa wa watu ulimiminika malangoni kumkaribisha. Kusanyiko kubwa kama lile halikuwahi kutokea hata wakati wa kumlaki mfalme mwenyewe. Msisimko ulikuwa mkubwa na kutoka katikati ya umati huu sauti ya kusikitisha iliimba wimbo wa maombolezo ya mazishi kama onyo kwa Luther juu ya hatima iliyokuwa inamsubiri. "Mungu atakuwa ngome yangu," alisema, huku akishuka kutoka kwenye gari lake la kukokotwa na farasi. [GC 153.3; PK Aya ya 27]

Watetezi wa upapa hawakuamini macho yao kwamba Luther angeweza kuthubutu kuonekana kule jijini Worms, na kufika kwake kukawajaza hisia tofauti-tofauti za woga, mshangao na fadhaa kubwa. Mfalme mara moja aliitisha baraza la viongozi wake ili kujadili hatua gani zichukuliwe. Mmoja wa maaskofu, mtetezi wa upapa mwenye msimamo mkali, alitangaza "Tumekuwa tukishauriana sana juu ya jambo hili kwa muda mrefu. Hebu mfalme wetu uliye mkuu, mwangamize mtu huyu mara moja. Je! Sigismund hakuwezesha John Huss kuchomwa moto? Sisi hatufungwi ama kutoa au kulinda cheti cha usalama cha mzushi huyu kusafiri salama." "Hapana," Mfalme yule alsema, "lazima tutunze ahadi yetu.", Ibid., kitabu cha. 7, sura ya 8. Basi ikaamuliwa kuwa Mwanamatengenezo asikilizwe. [GC 153.4; PK Aya ya 28]

Jiji zima lilikuwa na shauku ya kumwona mtu huyu maarufu na wa kushangaza, na kwa muda mfupi msongamano wa wageni ukajaza hoteli yake, yaani nyumba ya wageni y akulala. Luther akiwa bado hajapona vizuri ugonjwa wake uliomshika hivi karibuni; alikuwa amechoshwa na safari ambayo ilimchukua wiki mbili kamili, ilikuwa ni sharti ajitayarishe kukutana na matukio muhimu keshoye na alihitaji utulivu na mapumziko. Lakini ile hamu ya kumwona ilikuwa kubwa zaidi kiasi kwamba aliweza kupata masaa machache tu ya kupumzika wakati waheshimiwa, wakuu, maaskari wa mfalme, makasisi na raia

walipokusanyika kwa hamu kumzingira yeye. Miongoni mwa hawa walikuwa waheshimiwa ambao kwa ujasiri walimwomba Mfalme afanye matengenezo yahusianayo na unyanyasaji unaofanywa na kanisa na ambao, Luther alisema, “waliokuwa wamewekwa huru kwa injili yangu.”,--Martyn, ukurasa 393. Maadui, pia na marafiki, walikuja kumtazama mtawa huyo asiye na woga; lakini yeye akawapokea kwa utulivu mkubwa usiotikisika, akiwajibu wote kwa heshima na hekima. Mwonekano wake ulikuwa wenye uimara, na ujasiri. Uso wake uliokonda na kugeuka rangi kwa kupauka, ulikuwa na dalili za uchovu wa kazi na kuugua, ila ulikuwa na mwonekano wa wema, upole na furaha. Uzito na udhati wa kina wa maneno yake ulimpa nguvu ambayo hata maadui zake hawakuweza kabisa kuistahimili. Marafiki na maadui kwa pamoja walijawa na mshangao mkubwa. Baadhi walishawishika kuamini kuwa uwezo wa Mungu ulimzingira, wengine walinena kama vile Mafarisayo walivyofanya kwa Kristo: “Ana pepo.” [GC 154.1; PK Aya ya 29]

Siku iliyofuata Luther aliagizwa kufika mbele ya Baraza (Diet). Afisa wa jumba la kifalme aliteuliwa kumleta kwenye ukumbi wa hadhara; hata hivyo, alipafikia mahali hapo kwa shida sana. Kila mtaa ulikuwa umejaa watazamaji waliokuwa na hamu kubwa ya kumwona huyu mtawa ambaye alithubutu kupinga mamlaka ya upapa. [GC 154.2; PK Aya ya 30]

Alipokaribia kuingia mbele ya uwepo wa majaji wake, jenerali mmoja mkongwe, shujaa wa vita vingi, alimwambia kwa upole: “Maskini mtawa wee! Maskini mtawa wee! Sasa wewe unakwenda kuweka msimamo ulio bora kuliko wangu au kuliko kapteni mwingine yeyote aliopata kuutoa katika vita zetu zilizojaa umwagaji wa damu nyingi zaidi. Lakini kama kazi yako ni ya haki, na tena wewe una uhakika nayo, basi, songa mbele katika Jina la Mungu, na wala usiogope kitu. Mungu hatakuacha.” - D’Aubigne, kitabu cha 7, sura ya 8. [GC 154.3; PK Aya ya 31]

### Mbele Ya Baraza

Hatimaye Luther akasimama mbele ya baraza. Mfalme aliketi katika kiti chake cha enzi. Alikuwa amezungukwa na watu maarufu na wenye vyeo vya juu katika himaya yake. Kamwe haikuwahi kutokea mtu yeyote kusimama katika baraza la kuvutia kama lile ambalo Martin Luther alitakiwa kutetea imani yake. “Kule kuonekana kwake tu pale kwenyewe, kulikuwa ni ishara ya ushindi wake mkuu dhidi ya upapa. Papa alikuwa amekwishamhukumu na kumlaani na kumtenga mtu huyu na sasa alikuwa amesimama mbele ya mahakama ambayo, kwa tendo hili pekee yake, ilikuwa imejiweka juu ya papa. Papa alikuwa amemweka Luther chini ya amri na kumtenga mbali na jamii yote ya wanadamu; ila bado yeye aliitwa kuja shaurini kwa lugha ya heshima na akapokelewa mbele ya mkutano mkuu kabisa ulimwenguni. Papa alikuwa amemhukumu na kumkatilia mbali, ila

sasa alikaribia kuzungumza mbele ya maelfu ya wasikilizaji makini waliokusanyika pamoja kutoka sehemu za mbali zaidi za Jumuiya ya ulimwengu wa Kikristo wa wakati huo. Hakika mapinduzi makubwa yalikuwa yamefanywa kutokana na kazi ya Luther. Tayari Rumi ilikuwa inashuka kutoka kwenye kigoda chake cha enzi na tena ilikuwa ni sauti ya mtawa yule, ndiyo iliyomshusha na kumletea aibu." Ibid., kitabu cha. 7, sura ya 8. [GC 155.1; PK Aya ya 32]

Mbele ya baraza lenye watu wenye nguvu, sifa na vyeo vya heshima, Mwanamatengenezo huyo aliyezaliwa katika hali duni, alionekana kuingiwa na mshtuko na kutahayari. Baadhi ya wakuu, walipogundua hisia za moyo wake, walimwendea na mmoja wao alinong'ona: "Usiwaogope hao wauao mwili, lakini wasiweze kuiua roho." Mwingine akasema: "Watakapowapeleka mbele ya watawala na wafalme kwa ajili Yangu, mtapewa na Roho wa Baba yenu mtakayosema." Hivyo ndivyo Maneno Yake Kristo yalivyoletwa kwa njia ya wakuu wa ulimwengu ili kumtia nguvu mtumishi Wake katika saa ile ya kujaribiwa na kuhukumiwa kwake. [GC 155.2; PK Aya ya 33]

Luther aliongozwa mbele ili akae kwenye kiti kinachotazamana moja kwa moja na kiti cha enzi cha mfalme. Ukimya mrefu ukatanda kwenye baraza lile lililoshonana. Kisha afisa wa mfalme akainuka na kunyoshea kidole chake mkusanyo wa maandishi ya Luther, akimtaka Mwanamatengenezo huyo ajibu maswali mawili--- ikiwa aliyakubali kuwa ni maandishi yake na ikiwa alipanga kuyakanusha maoni yaliyomo humo ambayo amekuwa akiyaendeleza. Baada ya majina ya vitabu vile kusomwa, Luther alijibu kuwa kwa swali la kwanza alikiri kuwa vitabu vile vilikuwa ni vyake. "Kuhusu swali la pili," alisema, "Kwa kuwa ni swali ambalo linalohusu imani na wokovu wa roho na ndani yake mna Neno la Mungu, ile hazina kuu na ya thamani sana kuliko zote Mbinguni au duniani, ningetenda pasipo busara ikiwa ningejibu haraka bila kutafakari. Kuna uwezekano wa mimi kuthibithisha kidogo kuliko hali halisi inavyodai, au nikajibu zaidi ya vile Ukweli unavyotaka, na hivyo nikatenda dhambi dhidi ya tamko hili la Kristo: 'Bali mtu yeyote atakayenikana mbele ya watu, Nami nitamkana mbele za Baba Yangu aliye mbinguni.' (Mathayo 10:33) Kwa sababu hiyo ninakusihi mtukufu mfalme, kwa unyenyekevu wote, unipatie muda, ili nitoe jibu bila kulikosea Neno la Mungu." D'Aubigne, kitabu cha 7, sura ya 8. [GC 155.3; PK Aya ya 34]

Kwa kutoa ombi hili, Luther alienenda kwa hekima. Njia yake aliyoitumia ililishawishi baraza kwamba hakutenda mambo kwa jazba au kukurupuka kwa mihemko. Utulivu wa namna ile na kujitawala nafsi, vilionekana bila kutarajiwa kwa yule ambaye alikuwa amejionyesha jasiri na asiyetaka maridhiano au kuyumbishwa, jambo hilo likaongezea nguvu kwenye upande wake na kumwezesha baadaye kujibu kwa busara, hekima, heshima, na kuhitimisha maamuzi vyema, jambo ambalo liliwashangaza na kuwakatisha tamaa maadui

zake na kuukemea ujeuri, ukosefu wao wa nidhamu pamoja na kiburi chao. [GC 156.1; PK Aya ya 35]

**Kupigana Mweleka Na Mungu**

Siku ile iliyofuata alipaswa aje kutoa jibu lake la mwisho. Kwa muda fulani moyo wake ulinyong'onyea alipofikiria majeshi yale ambayo yalikuwa yameungana pamoja kuipinga ile Kweli. Imani yake ikayumba; woga na kutetemeka vikamjia na hofu na kutetemeka vikamlemea. Hatari zilizidi kuongezeka mbele yake, maadui zake walionekana kushangilia kwa ushindi na nguvu za giza kutawala. Mawingu yalijikusanya juu yake na kumzunguka kana kwamba yanamtenga na Mungu. Alitamani sana kupata uhakikisho kuwa Bwana wa majeshi atakuwa pamoja naye. Kwa uchungu wa roho alijitupa chini kifudifudi juu ya ardhi na kumwaga kilio cha uchungu wa moyo uliopondeka na kuvunjika, ambacho hakuna mtu yeyote bali Mungu peke yake Ndiye angeweza kukielewa kikamilifu. [GC 156.2; PK Aya ya 36]

"Ee Mungu Mwenyezi wa milele," aliomba, "ulimwengu huu unatisha kama nini! Tazama, unafunua kinywa chake ili unimeze, nami tumaini langu Kwako ni dogo mno.... Ikiwa mimi napaswa kuliweka tegemeo langu juu ya nguvu ya ulimwengu huu peke yake, basi, huu ndiyo mwisho wangu.... Saa yangu ya mwisho imefika, hukumu yangu imekwisha kutangazwa... Ee Mungu, unisaidie mimi dhidi ya hekima ya ulimwengu huu. Na ufanye hivyo,... Wewe peke Yako;... maana hii siyo kazi yangu, bali ni Yako Wewe,... nayo ni kazi ya haki na ya milele. Ee Bwana, unisaidie! Mungu uliye mwaminifu, usiyebadilika, mimi sina mtu mwingine yoyote ninayemtumaini....Chochote kinachotokana na mwanadamu hakina uhakika wowote; yote yatokayo kwa mwanadamu yanaangushwa chini.... Ni Wewe Ndiye uliyenichagua kwa kazi hii.... Simama kando yangu, kwa ajili ya mpendwa Wako Yesu Kristo, ambaye Ndiye ngome yangu, ngao yangu, na mlinzi wangu imara." Ibid., kitabu cha 7, sura ya 8. [GC 156.3; PK Aya ya 37]

Uongozi wa wenye hekima yote, ulikuwa amemruhusu Luther kutambua hatari iliyomkabili, ili asitegemee nguvu zake mwenyewe na kujiingiza kwa haraka kwa kiburi cha kukusudia katika hatari ile. Walakini haikuwa hofu ya kuogopa mateso yake binafsi, wala woga wa kuteswa hadi kifo ambacho kilionekana kama kinamkaribia punde, la! Hayo hayakumsumbua kwa vitisho vyake. Alikuwa amekifikia kilele cha mgogoro, naye alijisikia kuwa hana utoshelevu ndani yake mwenyewe, kukabiliana nao. Kupitia udhaifu wake, kazi ya ile Kweli ingeweza kupata hasara. Si kwa usalama wake mwenyewe, bali kwa ajili ya ushindi wa injili, alipigana mweleka na Mungu. Kama ilivyokuwa kwa Israeli katika pambano lile la usiku kando ya kijito cha upweke, huo ndio ulikuwa utungu na mapambano ya nafsi yake. Kama ilivyokuwa kwa Israeli, yeye pia naye

alimshinda Mungu! Katika hali yake ya kutokuwa na msaada wowote kabisa, imani yake ilimng'ang'ania Kristo, Mkombozi Mwenye uwezo mkuu. Aliimarishwa kwa uhakikisho kuwa asingekwenda mbele ya mkutano akiwa peke yake. Amani ikamrudia moyoni mwake, naye akafurahi kwamba alikuwa ameruhusiwa kuliinua juu Neno la Mungu mbele ya watawala wa mataifa. [GC 157.1; PK Aya ya 38]

Akili yake ikiwa imetulizwa kwa Mungu, Luther alijitayarisha kwa ajili ya mapambano yaliyokuwa mbele yake. Alifikiria juu ya mpangilio wa jibu lake, akachunguza aya katika maandishi yake mwenyewe na kutafuta kutoka kwenye Maandiko Matakatifu uthibitisho unaofaa kutetea misimamo yake. Kisha alipoweka mkono wake wa kushoto kwenye Gombo Takatifu (Biblia), ambalo lilikuwa wazi mbele yake, alinyanyua mkono wake wa kuume kuelekea Mbinguni na kuapa "kubaki kuwa mwaminifu kwa injili na kukiri imani yake kwa uhuru, hata ikiwa ingemlazimu kutia muhuri ushuhuda wake kwa damu yake.", Ibid., kitabu cha. 7, sura ya 8. [GC 157.2; PK Aya ya 39]

**Mbele Ya Baraza Lile Tena**

Alipoletwa tena mbele ya Baraza, uso wake haukuonesha hofu wala aibu. Akiwa mwenye utulivu na amani, lakini jasiri na mwuungwana sana, alisimama kama shahidi wa Mungu kati ya watu wakuu kabisa wa dunia hii. Yule Afisa wa mfalme wa dola sasa akamtaka atoe uamuzi wake ikiwa alikusudia kuyakana mafundisho yake. Luther alitoa jibu lake kwa sauti ya utulivu na unyenyekevu, bila vurugu au mhemko wa jazba. Mwonekano wake ulikuwa sio wa kujiona au kudharau watu, bali wenye adabu na staha, na bado alionyesha ujasiri, kuamini asemayo na furaha ambayo iliushangaza mkutano ule. [GC 158.1; PK Aya ya 40]

"Mfalme mtulivu sana, waheshimiwa wakuu na wana wa wafalme, na mabwana wahashamu/wakarimu" alisema Luther, "mimi nimekuja mbele yenu leo hii, kutimiza amri niliyopewa jana, na kwa rehema Zake Mungu, nakuomba sana mtukufu mfalme pamoja na wakuu wako wenye taadhima kuusikiliza kwa neema utetezi wangu wa kazi ambayo mimi nina uhakika kuwa ni ya haki na ya Kweli. Kama, kwa kutokujua, nitakiuka taratibu na itifaki za mahakama, nawasihi mnisamehe, kwa kuwa sikukulia katika majumba ya kifalme, bali katika nyumba pweke ya watawa." Ibid., kitabu cha 7, ch. 8. [GC 158.2; PK Aya ya 41]

Kisha, akaendelea kwa kujibu swali, alisema kwamba vitabu vyake havikuwa na sifa ya aina moja. Katika baadhi ya kazi alielezea juu ya imani na matendo mema na hata maadui zake walizungumzia kuhusu hivyo, kwamba sio tu havikuwa na madhara yoyote, bali vilikuwa na manufaa. Kuvikana vitabu hivi itakuwa kuuzuia Ukweli ambao pande zote zimekiri kukubaliana. Kundi la pili la vitabu lilikuwa na maandishi yanayofichua ufisadi na matumizi mabaya ya madaraka ya upapa. Kutangua vitabu hivi kungeutia nguvu utawala katili wa Rumi na kuachia mlango wazi zaidi kwa makufuru mengi na makubwa. Katika

kundi la tatu la vitabu vyake alikuwa amewashambulia watu binafsi ambao walikuwa wanatetea maovu yaliyokuwapo. Kuhusiana na hivi aliungama kwa hiari kwamba alikuwa ametumia lugha kali zaidi kuliko ilivyotakiwa. Hakudai kuwa hakuwa na makosa kabisa, lakini hata vitabu hivi hakuweza kuvibatilisha, kwa sababu kwa kufanya hivyo angewapa ujasiri maadui wa ile Kweli na wangechukua tukio hilo kuwa fursa ya kuwasagasaga watu wa Mungu kwa ukatili mkubwa zaidi. [GC 158.3; PK Aya ya 42]

"Hata hivyo mimi ni mwanadamu tu, na sio Mungu," aliendelea; "kwa hiyo, mimi nitajitetea mwenyewe kama Kristo alivyofanya. 'Kama mimi nimesema mabaya, basi, unishuhudie juu ya mabaya hayo.'... Kwa rehema Zake Mungu, ninakuomba sana, Ee mfalme mtulivu sana, waheshimiwa wakuu na wana wa wafalme, na watu wote wa kila tabaka, naomba mnithibithishie kutoka katika Maandiko ya manabii na mitume pale nilipokosea mimi. Na mara nitakaposhawishiwa au kusadikishwa kwamba vina makosa, nitatangua na kuungama kuhusu kila kosa nililoandika, na nitakuwa wa kwanza kuvishika vitabu vyangu na kuvitupa motoni. [GC 159.1; PK Aya ya 43]

**Si Amani, Bali Upanga**

"Niliyokwisha kusema punde yanaonesha wazi, ninatumaini kuwa nimepima kwa uangalifu na kuzingatia hatari ambazo ninajiweka wazi kwazo; lakini licha ya kufadhaika, ninafurahi kuona kuwa injili kwa sasa, kama ilivyokuwa nyakati za zamani ni chanzo cha taabu na mifarakano. Hii ndiyo tabia, naam, hii ndio hatima ya Neno la Mungu. 'Sikuja Kuleta amani duniani, bali upanga,' alisema Yesu Kristo. Mungu ni wa ajabu na wa kutisha katika mashauri Yake, jihadharini, msije kwa kudhania mnaepuka mipasuko, kumbe mnalitesa Neno takatifu la Mungu na mkajisababishia gharika ya kutisha ya hatari zisizokoma, majanga ya sasa, uangamivu, na ukiwa wa milele.... ninaweza kunukuu mifano mingi kutoka kwenye Maneno ya Mungu. Ninaweza kusema juu ya Mafarao, wafalme wa Babeli na wale wa Israeli, ambao kazi yao ilichangia zaidi kujiangamiza kwao wakati walipotafuta ushauri kwa wote walioonekana wenye busara zaidi, ili kuimarisha utawala wao. "Mungu huondosha milima, nao hawalijui hilo", Ibid., kitabu cha. 7, sura ya 8. [GC 159.2; PK Aya ya 44]

Luther alikuwa ameongea kwa lugha ya Kijerumani na sasa aliombwa kurudia maneno yale yale kwa Kilatini. Ijapokuwa alichoka kwa shughuli ya hapo awali, alitii na akawasilisha tena hotuba yake, kwa uwazi sawa na nguvu kama ile ya awali. Uongozi wa Mungu ulielekeza jambo hili. Akili za wakuu wengi zilikuwa zimepofushwa mno kwa makosa na ushirikina kiasi kwamba wakati wa hotuba yake ya kwanza hawakuweza kuiona ile nguvu ya hoja za Luther; lakini kule kurudia kuliwawezesha kutambua wazi zile hoja zilizowasilishwa. [GC 159.3; PK Aya ya 45]

Wale ambao kwa ukaidi wa mioyo walifumba macho yao kwa nuru na wakanuia kutoshawishika na Ukweli, walikasirishwa na nguvu ya maneno ya Luther. Alipomaliza kuongea, msemaji wa Baraza alisema kwa hasira: "Hukujibu swali uliloulizwa. "Wewe unahitajika kutoa jibu la wazi, dhahiri na fupi……Je, unatangua au hautangui?" ("Je, uko tayari au hauko tayari, kukana mafundisho uliyofundisha?" [GC 160.1; PK Aya ya 46]

Mwanamatengenezo yule akajibu kwa kusema: "Kwa vile mfalme mtulivu na waheshimiwa viongozi wote mnataka kwangu jibu lililo wazi, rahisi, na fupi, basi, nitawapa moja, nalo ni hili: Mimi siwezi kuikana au kuisalimisha imani yangu ama kwa papa, au kwa baraza, kwa sababu imekuwa dhahiri kama vile ulivyo mchana ya kuwa mara nyingi mapapa wamekosea na kupingana wao kwa wao katika maoni mara kwa mara. Kwa hiyo, isipokuwa tu pale mimi nimethibithishiwa vinginevyo kwa njia ya ushuhuda wa Maandiko, au kwa sababu ya hoja zilizo wazi kabisa, nisiposhawishiwa kwa njia ya aya zile nilizokwisha kuzinukuu, tena kwa njia hiyo ni lazima ziifungamanishe dhamiri yangu na Neno la Mungu, basi siwezi na sitoweza kupindisha, Mimi siwezi, na wala sitaweza kuikana imani yangu kamwe, kwani siyo salama kwa Mkristo, kusema lolote kinyume na dhamiri yake. Nasimamia kwa hilo tu, siwezi kufanya jingine lolote kabisa; Namuomba Mungu anisaidie. Amina." Ibid., kitabu cha 7, sura ya 8. [GC 160.2; PK Aya ya 47]

Hivi ndivyo mtu huyu mwenye haki alivyosimama kidete juu ya msingi wa hakika wa Neno la Mungu. Nuru ya mbinguni iliuangazia uso wake. Ukuu wake na usafi wa tabia, amani na furaha yake ya moyoni, ndiyo mambo yaliyojionyesha waziwazi mbele ya wote aliposhuhudia dhidi ya nguvu ya makosa/uongo ya Rumi nao watu wakashuhudia nguvu ya imani ile iushindayo ulimwengu (1 Yohana 5:4]). [GC 160.3; PK Aya ya 48]

Mkutano wote ukapigwa bumbuwazi, na kuduwaa kimya kwa muda. Wakati akijibu swali lake la kwanza Luther alizungumza kwa sauti ya chini na yenye heshima, na alikuwa kama amejisalimisha kwao. Watetezi wa kanisa la Rumi waliutafsiri mwelekeo ule kama ushahidi ulioonyesha kwamba ujasiri wake ulikuwa unaanza kushindwa. Walilichukulia ombi lake la kuchelewesha jibu kama ndio utangulizi tu, wa yeye kuikana imani yake. Charles mwenyewe, akizingatia, ila pia akiliangalia, nusu kwa dharau, umbile dhaifu la mtawa, nguo zake za kimasikini, na usahili wa hotuba yake, alikuwa ametangaza kwa kusema "Mtawa huyo hataweza kunifanya mimi kuwa mzushi kamwe." Ujasiri na uimara ambao aliouonyesha sasa, pamoja na nguvu na uwazi wa hoja zake alizozitoa, viliduwaza makundi yote kwa mshangao mkubwa. Mfalme wa dola, akiwa amevutiwa na kuguswa sana, kiasi cha kuweza kumstahi, alisema kwa mshangao na furaha, "Mtawa huyu anaongea kwa moyo mkuu usiotishika na kwa ushujaa usioyumbayumba." Wengi miongoni mwa watawala wale wa Kijerumani

wakamwangalia kwa kujivunia (fahari) kwa ajili yake na furaha, kwani alikuwa mwakilishi wa taifa lao. [GC 160.4; PK Aya ya 49]

Wafuasi shupavu wa Rumi wakawa wameshindwa vibaya kabisa; hoja yao ilionekana katika nuru isiyofaa kabisa kwao na dhaifu. Walikuwa wamejitahidi sana kuyadumisha mamlaka yao, sio kwa kutumia Maandiko, bali kwa kujielekeza kwenye kutumia vitisho, hiyo ndiyo hoja ya Rumi isiyoshindwa. Akasema hivi mnenaji mkuu wa Baraza: "Kama wewe usipokanusha, basi, mfalme wa dola na serikali za himaya zote watajadiliana pamoja ili kutafuta njia gani waitumie dhidi ya mzushi sugu asiyerekebishika." (au kama wewe hukani msimamo wako wa kuyafuata Maandiko- hukani imani yako…) [GC 161.1; PK Aya ya 50]

Rafiki yake Luther, aliyekuwa amesikiliza kwa furaha utetezi wake bora na wa kiungwana, alitetemeshwa sana alipoyasikia maneno haya; lakini daktari mwenyewe alisema kwa utulivu: "Eh Mungu uwe msaada wangu, kwasababu siwezi kukana chochote (katika imani yangu)." Ibid., Kitabu cha 7, sura ya 8. [GC 161.2; PK Aya ya 51]

**Mgogoro Mkubwa**

Aliamriwa kuondoka kwenye ukumbi wa Baraza wakati wakuu wakishauriana pamoja jambo la kufanya. Ilionekana kuwa hali ya hatari na dharua ilikuwa imefika. Kukataa kwa daima kwa Luther kujisalimisha kungeweza kuathiri historia ya kanisa la Rumi kwa vizazi vingi. Ikaamuliwa kwamba apewe nafasi moja zaidi ili akanushe. Kwa mara ya mwisho aliletwa tena ndani ya baraza lile. Swali liliulizwa tena, ikiwa atakana mafundisho yake. "Sina jibu lingine lolote la kutoa," alisema "zaidi ya hilo nililokwisha kulitoa." alisema, Ilikuwa dhahiri kwamba asingeshawishiwa, ama kwa ahadi au vitisho, kujisalimisha kwa ile mamlaka ya Rumi. [GC 161.3; PK Aya ya 52]

Viongozi wa kipapa walichukizwa sana kwamba mamlaka yao iliyowafanya wafalme na wakuu watetemeke, na sasa ipate kudharauliwa na kudhihakiwa hivi na mtawa masikini; walitamani apate kuonja ukali wa ghadhabu yao kwa kumtesa sana hadi apoteze maisha yake. Lakini, Luther alikuwa ameing'amua hatari ile iliyomkabili mapema, naye akanena na wote kwa heshima na utulivu wa Kikristo. Maneno yake hayakuwa na kiburi, harara, au chochote cha kupotosha watu kwa kuwasilishwa isivyo. Alikuwa amejisahau nafsi yake mwenyewe, na wale wakuu waliokuwa wamemzunguka pale, naye alihisi tu ya kuwa alikuwa katika uwepo wa Yule Mmoja aliye Mkuu kuliko mapapa, maaskofu, wafalme wa wa nchi, au wafalme wa himaya kubwa. Kristo alikuwa amezungumza kupitia ushuhuda wa Luther kwa nguvu na utukufu ambao kwa wakati huo uliwavutia marafiki na maadui zake wote kwa hofu na mshangao. Roho wa Mungu alikuwepo ndani ya baraza hilo, akiigusa mioyo ya wakuu wale

wa dola. Baadhi ya wakuu na wana wa wafalme walikiri kwamba madai ya Luther yalikuwa ya halali na haki. Wengi walishawishiwa kwa wazi na Ukweli. Wengi waliisadiki ile Kweli; lakini wengine ushawishi ule walioupokea haukuwa wa muda mrefu. Palikuwapo na kundi jingine la watu ambao wakati ule hawakusadiki mioyoni mwao, lakini, ambao baada ya wao wenyewe kuyachunguza Maandiko siku za usoni waligeuka na kuwa waungaji mkono wasioogopa kitu wa Matengenezo ya Kanisa. [GC 161.4; PK Aya ya 53]

Elekta Frederick, mtawala yule aliyekuwa na haki ya kumteua mfalme, alikuwa ametarajia kwa shauku kubwa sana kwamba Luther angejitokeza mbele ya Baraza lile, na kusisimka sana moyoni mwake alipoisikiliza hotuba yake. Kwa furaha na kuona fahari alishuhudia na kuuona ujasiri, uimara, na kujitawala nafsi kwake yule daktari, ndipo akadhamiria kusimama kwa imara zaidi katika kumtetea. Akazilinganisha pande zilizohusika katika pambano lile, na kubainisha kwamba hekima ya mapapa, wafalme, na maaskofu ilikuwa si kitu (ni sifuri) mbele ya ile nguvu ya Ukweli wa Neno la Mungu. Upapa ulipata anguko na kushindwa vibaya, kipingo hiki kingehisiwa miongoni mwa mataifa yote na katika zama zote. [GC 162.1; PK Aya ya 54]

Wakati mjumbe wa papa alipogundua madhara yaliyotokana na hotuba ya Luther, aliingiwa na hofu kuu ambayo kamwe hakuwa nayo awali kwa ajili ya usalama wa nguvu ile ya Kirumi, na akaazimu kutumia kila njia iliyokuwa katika uwezo wake kukamilisha zoezi la kumpindua Mwanamatengenezo. Kwa kutumia ufasaha wote na ustadi wa kidiplomasia pamoja na stadi ambazo alijulikana kuwa mashuhuri kwazo, alimweleza mfalme kijana (wa Ujerumani) upumbavu na hatari ya kuvunja urafiki na kupoteza mkono wa msaada wa Kiongozi wa serikali ya kipapa au serikali ya ***see**** yenye nguvu ya Rumi kwa ajili ya madai ya mtawa (mafundisho) asiyejulikana au asiye na maana. [GC 162.2; PK Aya ya 55]

Maneno yake hayakukosa kuwa na madhara. Siku iliyofuata baada ya Luther kutoa jibu lile, Charles aliagiza ujumbe uwasilishwe kwenye Baraza kuu la taifa, ukitangaza uamuzi wake wa kutekeleza sera ya watangulizi wake katika kudumisha na kulinda dini ya Kikatoliki. Kwa vile Luther alikuwa amekataa kuyakana makosa yake, hatua kali mno zinapaswa kuchukuliwa dhidi yake na uzushi ule alioufundisha. “Mtawa mmoja tu, anayepotoshwa na upumbavu wake mwenyewe, ameinuka dhidi ya imani ya Kikristo. Ili kuthibiti kufuru hii, nitakuwa tayari kuacha falme zangu, hazina zangu, marafiki zangu, mwili wangu, damu yangu, roho yangu na maisha yangu. Ninakaribia kumfukuzilia mbali Luther, mtawa wa chama cha Augustine (Mwagustino), kumpigia marufuku kabisa ili asisababishe vurugu hata kidogo miongoni mwa watu; Ndipo nitaenda dhidi yake na wafuasi wake ambao ni wazushi sugu wanaofanya mambo kwa makusudi, na kuwatenga na kanisa, kuwapiga marufuku wao pamoja na ibada zao, na kwa kila njia au gharama inayoweza kuwaangamiza. Natoa wito kwa wajumbe wa serikali

za majimbo yote kuenenda kama Wakristo waaminifu” Ibid., kitabu cha 7, sura ya 9. Hata hivyo mfalme wa dola alitangaza kwamba cheti cha uhakikisho wa usalama cha Luther kinapaswa kuheshimiwa na hivyo kabla ya hatua yoyote ile kuchukuliwa dhidi yake, lazima aruhusiwe kufika nyumbani kwake salama. [GC 162.3; PK Aya ya 56].

**Kung’ang’ania Desturi Na Mapokeo**

Mitazamo miwili inayopingana sasa ilitolewa kwa kusisitizwa na wajumbe wa Baraza. Wajumbe na wawakilishi wa papa walidai tena kwamba hati ya kusafiri salama ya Mwanamatengenezo inapaswa kupuuzwa. “Mto Rhine,” walisema, “unapaswa kupokea majivu yake, kama ulivyopokea yale majivu ya John Huss karne moja iliyopita.”-Ibid., kitabu cha 7, sura ya 9. Lakini viongozi wakuu wa ufalme wa Ujerumani hawakuafikiana ingawa wao wenyewe walikuwa ni wafuasi wa papa na maadui wa wazi wa Luther, walipinga ukiukwaji wa hadharani wa uaminifu wao kwa umma/raia, kwamba jambo hilo litatia doa kwa heshima ya taifa. Walirejelea maafa yaliyofuata baada ya kifo cha Huss, kisha wakatangaza kwamba wasingethubutu kukaribisha majanga hayo ya kutisha kuangukia Ujerumani, wala juu ya kichwa cha mfalme wao kijana, yaani, wasingependa kuyarudia tena maovu yale ya kutisha. [GC 163.1; PK Aya ya 57]

Charles mwenyewe akitoa jibu lake juu ya pendekezo hilo baya, alisema: "Ijapokuwa heshima na imani vinapaswa kupigwa marufuku ulimwenguni kote, mambo hayo mawili yanapaswa yapate kimbilio ndani ya mioyo ya watawala wetu.” Ibid., kitabu cha 7, sura ya 9. Alizidi kusihiwa zaidi na mmojawapo wa wale maadui wakuu wa Luther ambao walikuwa wafuasi wa upapa ili apate kumshughulikia Mwanamatengenezo yule kama vile Sigismund alivyomshughulikia Huss—yaani amwache mikononi mwa rehema za kanisa nao wamshugulikie; lakini kwa kukumbuka tukio lililompata Huss akiwa katika mkutano wa hadhara alipoonyesha minyororo yake na kumkumbusha mfalme juu ya ahadi yake aliyoitoa kwa imani njema, Charles V alisema: “Mimi sitaki kuaibika kama Sigismund na kisha uso wangu ubadilike kuwa rangi nyekundu ukionyesha kuumbuka huko.”, Lenfant, juz. 1, uk. 422. [GC 163.2; PK Aya ya 58]

Hata hivyo, Charles alikuwa amezikataa kwa makusudi zile Kweli zilizowasilishwa na Luther. “Nimeazimia kwa nguvu zangu zote kuiga mfano wa mababu zangu” aliandika mfalme huyo. D'Aubigne, b. Kitabu cha 7, sura ya 9. Alikuwa ameamua kwamba asingeweza kuondoa mguu wake katika njia ya mazoea, mila na desturi na kutembea katika njia za Kweli na haki. Kwa kuwa baba zake walifanya vile, basi, yeye alitaka kuendelea kuutetea upapa, licha ya ukatili wake wote na ufisadi. Hivyo ndivyo alivyouchagua msimamo wake, akikataa katakata kuipokea nuru yoyote zaidi ya ile waliyoipokea baba zake, au kufanya wajibu wowote ule ambao wao hawakuufanya. [GC 163.3; PK Aya ya 59]

Kuna wengi hata katika siku za leo wanaong'ang'ania desturi na mapokeo ya baba zao. Wakati Bwana anapowatumia nuru ya nyongeza (bonasi), wao wanakataa kabisa kuipokea, kwa kuwa haikutolewa kwa baba zao basi hata wao wasingeipokea. Sisi hatuwekwi katika nafasi baba zetu walikuwa; matokeo yake, wajibu na majukumu hayafanani na yao. Sisi hatutaweza kukubaliwa na Mungu kwa kuangalia mfano wa mababa zetu katika kuamua wajibu wetu, badala ya sisi wenyewe kulichunguza Neno la Ukweli sisi wenyewe. Wajibu wetu ni mkubwa zaidi kuliko ule wa mababu zetu. Sisi tunawajibika kwa nuru ile waliyoipokea wao na ambayo ililetwa kwetu kama urithi, na kisha tunawajibika pia kwa nuru ya nyongeza ambayo sasa hivi inang'aa juu yetu kutoka kwenye Neno la Mungu (Mithali 4:18). [GC 164.1; PK Aya ya 60]

**Kuungwa Mkono Na Wakuu**

Kristo alisema hivi juu ya Wayahudi wasioamini: "Kama nisingalikuja na kusema nao, wasingalikuwa na dhambi; lakini sasa hawana udhuru kwa dhambi yao." Yohana 15:22. Nguvu na mamlaka ile ile ya mbinguni ilikuwa imezungumza na mfalme wa dola na watawala wale wa Ujerumani kupitia kwa Luther. Na kama nuru inalivyomulika kutoka katika Neno la Mungu, Roho Wake Mungu aliwasihi watu wengi katika mkutano ule kwa mara ya mwisho. Kama Pilato, karne nyingi zilizopita, aliruhusu kiburi na umaarufu wake na kupendwa na watu vifunge moyo wake dhidi ya Mkombozi wa ulimwengu; kama vile Feliki aliyekuwa akitetemeka alivyomuaga yule mjumbe wa Ukweli, akisema "Sasa enenda zako, nami nikipata nafasi nitakuita;" kama vile Agripa mwenye kiburi alivyokiri kwa kusema, "Kwa maneno machache wadhani kunifanya mimi kuwa Mkristo."(Matendo 24:25; 26:28), lakini akaupa kisogo na kuukataa ujumbe uliotumwa na Mbingu,-- ndivyo alivyofanya Charles V, alikubali kutawaliwa na kiburi cha ulimwengu huu pamoja na siasa/sera zake, akaamua kuikataa nuru ya Ukweli. [GC 164.2; PK Aya ya 61]

Umbeya juu ya njama dhidi ya Luther ulienezwa sana, na kusababisha taharuki kubwa katika jiji lote. Mwanamatengenezo alikuwa amejitengenezea marafiki wengi ambao walijua fika ukatili wa hila ya Rumi juu ya wote waliothubutu kufichua ufisadi wake, nao wakaamua kwamba Luther hatatolewa kafara. Mamia ya wakuu wenye vyeo wakatoa ahadi ya kumlinda. Hawakuwa wachache, walioupinga ujumbe wa mfalme uliodhihirisha udhaifu wake kwa kujisalimisha kwake chini ya udhibiti wa mamlaka ya Rumi. Katika milango mikubwa ya nyumba pamoja na maeneo watu wakakusanyika au sehemu za hadhara zinazotembelewa na watu wengi, mabango ya matangazo yakatundikwa, mengine yakilaani na mengine yakiungana na Luther. Katika mojawapo la mabango yale yaliandikwa maneno haya ya maana ya mtu mwenye hekima: "Ole wako, nchi, akiwa mfalme wako ni kijana." Mhubiri 10:16. Ari ya watu wengi kwa Luther katika nchi yote ya Ujerumani ilimthibitishia mfalme yule dola

pamoja na Baraza la taifa kwamba dhuluma yoyote itakayotendwa dhidi yake, ingeweza kuhatirisha amani ya dola nzima na hata uimara wa kiti cha enzi. [GC 164.3; PK Aya ya 62]

**Juhudi Za Kufanya Maridhiano**

Mfalme Frederick wa Saxony alitulia kimya na kwa uangalifu alificha hisia zake halisi kuhusu Mwanamatengenezo, lakini wakati huohuo akaendelea kumlinda kwa umakini bila kuchoka, akiangalia harakati zake kwa umakini, kule alipokwenda na pia akiangalia mienendo ya maadui zake wote. Lakini kulikuwa na wengi ambao hawakujaribu kuficha huruma zao kwa Luther. Yeye alitembelewa na watawala, watoto wa wafalme, wasaidizi wa mfalme (counts), wafanya biashara, wanasheria, malodi na watu wengine wa hadhi za juu wakiwemo walei na watenda kazi wa kanisa. “Chumba kidogo cha daktari," aliandika Spalatin, "hakikuweza kuwatosha wageni wote walioenda kumtembelea.”-- Martyn 1: 404. Watu walimkodolea macho kana kwamba alikuwa zaidi ya mwanadamu. Hata wale ambao hawakuwa na imani na mafundisho yake hawakuweza kujizuia kuhusudu au kushabikia uadilifu wake mkubwa na ushujaa wa hali ya juu ambao ulimwezesha kuthubutu kukabiliana na kifo kuliko kwenda kinyume na dhamiri yake. [GC 165.1; PK Aya ya 63]

Jitihada kubwa ilifanywa ili Luther aridhie kufikia mapatano na Rumi. Waheshimiwa, wakuu na wana wa kifalme walimweleza kwamba kama angeendelea kung’ang’ania uamuzi wake dhidi ya ule wa kanisa na baraza, basi, muda si mrefu angefukuzwa katika ufalme ule na aishi bila ulinzi wowote. Kwa wito huo ambao ulikuwa ni tishio, Luther alijibu hivi: “Injili yake Kristo haiwezi kuhubiriwa bila kuamsha chuki.... Kwa nini basi hofu au woga wa hatari unitenge mimi mbali na Bwana, na mbali na Neno la Mungu ambalo peke yake ndilo Ukweli? Hapana; mimi bora niutoe mhanga mwili wangu, damu yangu, na uhai wangu.” - D’Aubigne, kitabu cha 7, sura ya 10. [GC 165.2; PK Aya ya 64]

Alisihiwa kwa mara nyingine tena ajisalimishe kwa hukumu ya mfalme na ndipo baada ya hapo asingekuwa na lolote la kuogopa. "Ninakubali," alisema kwa kujibu, "kwa moyo wangu wote, kwamba mfalme, wana wa wafalme, wakuu na hata Mkristo mwenye roho mbaya sana, anapaswa kuzipima na kuzichunguza kazi zangu, ili kutoa maamuzi, lakini kwa sharti moja, kwamba wachukue Neno la Mungu kama kiwango/kipimo chao. Wanadamu hawana chaguo jingine lolote ila kulitii Neno la Mungu. Usiiumize dhamiri yangu kwa kuitendea ukatili, kwani imefungwa kwa kuzungushiwa minyororo na Maandiko Matakatifu.”-Ibid.,b.7, sura ya 10. [GC 166.1; PK Aya ya 65]

Kwa kusihiwa kwingine ambako pia ilikuwa kama tishio lililotolewa kwake, yeye alisema hivi: “Mimi nakubali kukitupilia mbali cheti changu cha kunihakikishia kusafiri salama. Naweka nafsi yangu na uhai wangu mikononi mwa

mfalme wa dola, lakini Neno la Mungu - kamwe!” Ibid., b. 7, sura ya 10. Alieleza utayari wake wa kujikabidhi kwenye maamuzi ya baraza kuu, lakini kwa sharti tu kwamba baraza linatakiwa kuamua kulingana na Maandiko. “Katika masuala yahusuyo Neno la Mungu na imani, "aliongeza," kila Mkristo ni jaji mzuri kama alivyo papa, hata kama yeye anaungwa mkono na mabaraza milioni moja, hayo mabaraza pia yanaweza kuwa kwa ajili yake.” (Kasisi hana ujuzi wa pekee kuliko mkristo mwingine)- Martyn gombo la 1: 410. Marafiki na pia maadui walisadiki mwishowe kuwa juhudi zaidi za upatanisho zingegonga mwamba tu (zisingetoboa). [GC 166.2; PK Aya ya 66]

**Uthabiti Usioyumba Kamwe**

Endapo yule mwanamatengenezo angekuwa amejisalimisha au kukubaliana nao katika pointi moja tu, Shetani na majeshi yake wangekuwa wamejipatia ushindi. Lakini uimara wake usioyumba ulikuwa ndiyo njia ya kulikomboa kanisa, na kuanzisha zama mpya, na bora zaidi (kuachana na udhalimu, kuwa na ibada ya kweli ya Ufunuo 12). Mvuto wa mtu yule mmoja, ambaye alidiriki kufikiri na kutenda tofauti na wengine katika mambo ya dini/kiroho, ulibadili kanisa na ulimwengu mzima, siyo tu katika wakati wake tu, lakini pia katika vizazi vyote vya baadaye. Uimara na uaminifu wake ungewaimarisha wote ambao wangepitia katika uzoefu unaofanana na huo hadi mwisho wa wakati. Nguvu na utukufu wa Mungu vilisimama juu ya mashauri ya wanadamu, na juu ya uweza wa nguvu kali za Shetani. [GC 166.3; PK Aya ya 67]

Punde Luther aliamriwa na mamlaka ya Mfalme arudi nyumbani kwake, naye akajua kwamba taarifa ile ingefuatiwa upesi na hukumu yake. Mawingu ya vitisho yalitanda juu ya njia yake; lakini wakati alipokuwa akiondoka kutoka pale Worms, moyo wake ulijaa furaha na sifa. “Ibilisi mwenyewe,” akasema, “ndiye aliyeilinda ngome ya papa; lakini Kristo ameipasua na kuacha ufa mpana ndani yake, naye Shetani amelazimishwa kukiri ya kwamba Bwana ndiyo ana nguvu zaidi kuliko yeye.” D'Aubigne, b. 7, sura ya 11. [GC 166.4; PK Aya ya 68]

Baada ya kuondoka kwake, bado alitamani kwamba ushupavu/ujasiri wake ule usitafsiriwe kuwa ni uasi, Luther alimwandikia mfalme wa dola. “Mungu, ambaye Mchunguzi wa mioyo, ni shahidi wangu,” akasema, “kuwa mimi niko tayari, kwa dhati na juhudi kabisa kukutii wewe mfalme wangu mtukufu, katika heshima au katika aibu, katika uzima au mauti, na pasipo kubagua lolote, isipokuwa tu Neno la Mungu, ambalo kwalo mwanadamu huishi. Katika mambo yote yahusuyo maisha haya ya sasa, uaminifu wangu hautalegalega, kwa maana kupoteza au kupata hapa siyo suala la msingi kwa wokovu. Lakini katika masuala ya umilele, mapenzi ya Mungu ni kwamba mwanadamu yeyote asijikabidhi chini ya mwanadamu mwenzake. Kwa maana kujisalimisha huko katika masuala ya kiroho

ni ibada halisi (ya Kweli), na ibada inapaswa kufanywa/kutolewa kwa Muumbaji peke Yake" Ibid., b. 7, sura ya 11. [GC 167.1; PK Aya ya 69]

Kwenye safari akiwa njiani kutoka Worms, mapokezi ya Luther yalikuwa ya kupendeza zaidi kuliko hata wakati alipokuwa akienda huko. Viongozi wakuu wa kanisa wa ngazi za juu walimkaribisha mtawa aliyekuwa ametengwa, na watawala wa serikali ya kiraia walimheshimu mtu ambaye Mfalme alikuwa amemhukumu kwa kumtenga na kanisa. Alisihiwa kuhubiri, na licha ya zuio/marufuku ya kifalme, aliingia tena kibwetani. "Sikuwahi kuahidi kulifunga mnyororo Neno la Mungu," alisema, "wala sitafanya hivyo." - Martyn 1: 420. [GC 167.2; PK Aya ya 70]

**Akamatwa Na Kufungwa**

Haikuchukua muda mrefu baada ya Luther kutoka kule Worms, wafuasi wa papa walimzidi nguvu mfalme wa dola, naye akatoa amri dhidi yake Luther. Katika amri ile Luther alishutumiwa kuwa y "yeye ndiye Shetani mwenyewe hasa katika umbile la mwanadamu, aliyevaa vazi la kitawa." - D'Aubigne, kitabu cha 7, sura ya 11. Amri ilitolewa ikisema kwamba mara tu muda wa cheti chake cha uhakikisho wa kusafiri salama kitakapoisha muda wake, basi hatua zichukuliwe kuikomesha kazi yake. Watu wote walikatazwa kumpa hifadhi majumbani mwao, kumpa chakula au kinywaji, au kwa neno au kwa tendo, hadharani au faraghani, kumsaidia au kushirikiana naye. Alipaswa kukamatwa popote pale ambapo angepatikana, na kukabidhiwa kwa wenye mamlaka ya serikali. Wafuasi wake pia walitakiwa kufungwa gerezani na mali zao kutaifishwa (kuchukuliwa na serikali). Maandiko yake yalipaswa kuteketezwa, na, hatimaye wale wote ambao wangethubutu kufanya kinyume cha ile amri wangejumuishwa katika hukumu ile. Elekta wa Saxony, mwenye haki ya kumteua mfalme, pamoja na watawala waliokuwa marafiki wa Luther walikuwa wameondoka kule Worms mara tu baada ya yeye kuondoka, na ile amri ya mfalme wa dola ilikuwa imepata idhini ya Baraza kuu. Basi, wafuasi wa Rumi wakafurahi na kushangilia. Walidhani hatima ya Matengenezo ya Kanisa ilikuwa imetiwa muhuri. [GC 167.3; PK Aya ya 71]

Mungu alikuwa ameandaa mpenyo wa kutokea mtumishi Wake katika saa hii ya hatari. Jicho Lile Lisilosinzia lilikuwa limefuatilia kila Luther alipojongea, na moyo ule mkweli, bora, na mwema ulikuwa umeamua kumwokoa. Ilikuwa wazi kwamba Rumi isingeridhika na kitu chochote isipokuwa kifo chake, ni kwa kumficha tu ndipo angeweza kuokolewa na makanwa ya simba. Mungu akampa hekima Frederick wa Saxony kubuni mpango wa kumhifadhi Mwanamatengenezo. Kwa ushirikiano wa marafiki wa kweli kusudi la Elekta Fredrick lilitekelezwa, na Luther alifichwa kwa ufanisi kwani marafiki na hata maadui hawakuweza kumfikia. Alipokuwa akielekea kurudi nyumbani alikamatwa ghafla, na kutengwa na wahudumu wake na kupitishwa haraka msituni hadi kasri la Wartburg, ngome

iliyo katika milima iliyojitenga. Kukamatwa kwake na kufichwa kwake kulifanywa kwa siri mno kiasi Frederick mwenyewe kwa muda mrefu hakujua ni wapi alikopelekwa. Kutokujua huko hakukuwa bahati mbaya; kwa kadiri ambavyo asingeweza kujua chochote kuhusu mahali alipo Luther, ndivyo ambavyo asingeweza kufichua siri yoyote. Alijifariji mwenyewe kujua kwamba Mwanamatengenezo alikuwa salama, na kujua kwake hilo, kulimfanya aridhike. [GC 168.1; PK Aya ya 72]

Majira ya kuchipua, majira ya joto, na majira ya kupukutisha yakapita na msimu wa baridi yenye theluji ukaja na Luther bado alibaki kuwa mfungwa. Aleander na wafuasi wake walifurahi kwani nuru ya injili ilionekana kana kwamba karibu kuzimwa. Lakini badala yake, Mwanamatengenezo alikuwa akijaza taa yake mafuta kutoka kwenye ghala la Ukweli, na nuru yake ilikuwa inaenda kuangaza kote kwa mng'ao mkubwa zaidi. [GC 168.2; PK Aya ya 73]

Akiwa katika usalama wa kirafiki wa ngome ya Wartburg, Luther alifurahia kwa muda kutolewa kwake kutoka kwenye joto la mapambano na vurugu la vita. Lakini hakuridhika kuishi kwa muda katika ukimya na mapumziko. Akiwa amezoea maisha ya shughuli na migogoro mikali, hakuweza kuvumilia kukaa tu. Katika siku hizo za kukaa peke yake, hali ya kanisa iliingia kwenye mawazo yake, na alilia kwa kukata tamaa. “Jamani! Hivi kweli hakuna hata mtu katika siku hizi za mwisho za hasira Yake, wa kusimama kama ukuta mbele za Bwana, na aokoe Israeli!”- Ibid., B. 9, sura ya 2. Kwa mara nyingine mawazo yake yalimrudia tena, naye aliingia na hofu ya kulaumiwa kwa woga na kwa kuepa mapambano. Kisha akajikosoa mwenyewe kwa uvivu na kuendekeza kwake kufurahisha nafsi yake. Lakini wakati huohuo alikuwa akikamilisha mengi kila siku, zaidi ya yale yanayoweza kufanywa na mtu mmoja. Kalamu yake kamwe haikukaa bila shuguli. Wakati maadui zake wakijidanganya kwamba amenyamazishwa, walishangaa na kuchanganyikiwa na ushahidi dhahiri kwamba alikuwa bado anafanya kazi. Vijuzuu vingi vilivyotolewa kutoka kwenye kalamu yake, vilisambazwa kote katika nchi ya Ujerumani. Alifanya pia huduma muhimu kupita zote kwa watu wa nchi yake kwa kutafsiri Agano Jipya katika Lugha ya Kijerumani. Kutoka kwenye kifungo chake hiki kama cha Patmo kule miambani, aliendelea kwa karibu mwaka mzima kutangaza injili na kukemea dhambi na mafundisho yenye makosa ya wakati wake. [GC 168.3; PK Aya ya 74]

Lakini haikuwa tu kwa ajili ya kumhifadhi Luther dhidi ya ghadhabu za maadui zake, wala hata kumpatia msimu wa utulivu kufanya kazi hizi muhimu, kwamba ndiyo zilikuwa sababu pekee za Mungu kumwondoa mtumishi Wake kutoka kwenye jukwaa hili la maisha ya hadharani. Kulikuweko na matokeo mengine ya thamani zaidi ya haya ambayo yalikuwa yapatikane. Katika upweke, mapumziko na maficho yake kwenye milima, Luther alikuwa ametengwa na misaada ya kidunia na alifungiwa mbali na sifa za wanadamu. Kwa hivyo aliokolewa kutoka

katika hatari ya kiburi na kujituamini mwenyewe, mambo ambayo mara nyingi husababishwa na mafanikio. Kwa mateso na kudhalilishwa vile, alikuwa ameandaliwa kutembea tena salama katika vilele vile vya juu sana, ambavyo husababisha kizunguzungu baada ya kuinuliwa juu kwa ghafula mno. [GC 169.1; PK Aya ya 75]

Kadri ambavyo watu wanafurahia uhuru ule ambao Injili au Ukweli huwaletea, ndivyo wanavyokuwa na mwelekeo wa kuwasifu wale ambao Mungu amewaweka kuvunja minyororo ya makosa na ushirikina. Shetani anajitahidi kuyageuza mawazo na mapenzi ya watu kutoka kwa Mungu, na kuyaelekeza kwa mawakala wa kibinadamu, anawaongoza watu kukiheshimu chombo hichi tu na kupuuza mkono Ule unaoongoza matukio yote ya uongozi wa Mungu (majaliwa Yake). Mara nyingi viongozi wa dini ambao husifiwa na kuheshimiwa hupoteza hitaji lao la kumtegemea Mungu na kuongozwa kujitumainia wenyewe. Matokeo yake wanatafuta kutawala akili na dhamiri za watu ambao wana mwelekeo wa kuwatazama wao kama mwongozo badala ya kulitegemea Neno la Mungu. Kazi ya matengenezo mara nyingi hurudishwa nyuma kwasababu ya roho hii inayoendekezwa na wafuasi wanaounga mkono matengenezo. Mungu anailinda kazi ya Matengenezo kutokana na hatari hii. Alitamani kazi hiyo isipokee muhuri wa mwanadamu, bali chapa ya Mungu. Macho ya wanadamu yalikuwa yamemgeukia Luther kama ndiye mfafanuzi mwenye uwezo wa kuelezea ile Kweli, sasa alikuwa ameondolewa kwao ili macho yote yaelekezwe kwa Mwasisi wa milele wa Ukweli. [GC au PK 169.2]

*'Holy See' au Sencta sedes kilatini maana yake ni kiti kitakatifu, yaani cha utawala wa Serikali ya kanisa la Rumi. Neno hilo linarejelea jiji-jimbo la Vatikani, eneo ambalo Papa anakaa. Ni neno linalotumiwa na Serikali yenyewe ya Kanisa Katoliki la Roma. Angalia zaidi kwenye vitabu vya historia au tovuti.

# SURA YA 9

# MWANAMATENGENEZO WA USWISI

**(Nuru Yawashwa Kule Uswisi Na Watu Hawakutikiswa Kama Milima Yao Kule Alps)**

Ufupisho: Matengenezo ya Kanisa yalianza karne ya 16 Kule Ujerumani chini ya uongozi wa Martin Luther, na wakati huo huo Zwingli aliyezaliwa wiki chache baada ya Luther, aliongoza matengenezo kule Switzerland. Huyu hakuwa tayari

kuacha kazi ya Kutetea Neno la Mungu. Matukio kwenye sura hii yalitokea kati ya 1484-1528. Zwingli alimwamini Kristo mwaka 1506 na kuanza huduma ya ukasisi kwenye Zurich Kathedro baada ya chuo mwaka 1519. mwaka uliofuata alipinga uuzaji wa misamaha na kuitwa mzushi 1522, na 1528 alimsaidia Oecolampadius kufanya mdahalo kule Bern.

Katika mchakato wa uchaguzi wa watu wa kufanya Matengenezo ya Kanisa, unaonekana mpango wa Mungu ule ule kama alioutumia katika kulianzisha Kanisa Lake. Mwalimu wa Mbinguni aliwapita wakuu wa nchi, wenye vyeo, na utajiri, waliokuwa wamezoea kupokea sifa na heshima kama viongozi wa watu. Hawa walikuwa na kiburi mno, tena walijitumainia/walijitegemea, na kujiamini mno katika ukuu wao, nao walijigamba na hata haikuwezekana kuuumbwa upya (kufinyangwa) tabia zao tena ili wapate kuwa wenye huruma na hivyo kushirikiana na wanadamu wenzao kwa kuwa watendakazi-wenzi pamoja na Yule Mtu Mnyenyekevu wa Nazareti. Kwa wavuvi wa samaki wa Galilaya, wasio na kisomo, ambao walikuwa wakifanya kazi ngumu, mwito huu ulitolewa kwao: Nifuateni, Nami nitawafanya ninyi wavuvi wa watu." Mathayo 4:19. Wanafunzi hawa walikuwa wanyenyekevu na wanaoufundishika. Kadiri walivyokuwa wameathiriwa kidogo na mafundisho ya uongo ya wakati wao, ndivyo ilivyokuwa rahisi zaidi kwa Kristo kufanikiwa kuwaelekeza, kuwaandaa na kuwafundisha juu ya kufanya huduma Yake. Hivyo ndivyo ilivyokuwa katika siku zile Matengenezo Makuu ya Kanisa. Wanamatengenezo wakuu walikuwa ni watu waliotoka katika maisha ya chini—watu waliokuwa hawajaathiriwa na kiburi cha madaraka, wala ushawishi wa itikadi zilizopitiliza, ushupavu, chuki ubaguzi na hila walizokuwa nazo makasisi. Ni mpango Wake Mungu kuvitumia vyombo (wajumbe) vinyenyekevu na dhaifu ili kuleta matokeo makubwa. Hapo ndipo utukufu hautatolewa kwa wanadamu, bali Kwake Yeye afanyaye kazi ndani yao na kupitia kwao na kutenda kwao ili kulitimiza mapenzi Yake mema (Wafilipi 2:13). [GC 171.1; PK Aya ya 1]

Majuma machache baada ya kuzaliwa kwa Luther kwenye kibanda kidogo cha mchimba madini huko Saxony, Ulric Zwingli akazaliwa katika kibanda kidogo cha mbao cha mchunga mifugo huko Milima ya Alps. Mazingira ya Zwingli utotoni, malezi na mafunzo yake ya mapema yalikuwa yale ambayo yangeweza kumpa maandalizi kwa ajili ya utume wake wa baadaye. Alilelewa katikati ya mandhari yenye kuvutia, na yenye utukufu wa asili, uzuri wa ajabu na kustaajabisha (misitu, milima, maua, mito, bahari n.k), akili yake iliguswa mapema na hisia ya utukufu, uwezo, nguvu na ukuu wa Mungu. Historia ya matendo ujasiri iliyotendeka juu ya milima ile ya kwao ilichochea joto la matarajio mema katika ujana wake. Naye akiwa kando ya bibi yake mcha Mungu alivisikiliza visa vichache vya Biblia ambavyo nyanya huyu alikuwa amevikusanya kwa shida kutoka miongoni mwa hadithi za wahenga na kutoka mapokeo ya kanisa. Kwa

shauku kubwa alisikiliza habari za matendo makuu ya wazee na manabii, habari za wachungaji wale waliochunga mifugo yao katika vilima vile vya Palestina ambako malaika walizungumza nao, na habari za Mtoto yule Mchanga wa Bethlehemu na Yule Mtu wa Kalvari. [GC 171.2; PK Aya ya 2]

Kama John Luther, babaye Zwingli, alitamani mwanawe apate elimu na hivyo huyo kijana alipelekwa mapema kutoka bonde lake la asili, kule alikozaliwa kuhudhuria shule. Akili yake ikakua haraka, na si muda mrefu, swali likawa limejitokeza kwamba watawapata wapi waalimu wanaofaa kumfundisha. Akiwa ana umri wa miaka kumi na mitatu aliendа Bern, mahali ambapo wakati ule palikuwa na shule iliyojulikana sana kwa ubora kitaaluma kuliko zote katika nchi ile ya Uswisi (Switzerland). Lakini pale hatari ikatokea ambayo iliweka ukungu kwenye matumaini ya maisha yake. Jitihada zilizodhamiriwa zilifanywa na watawa ili kumshawishi kuingia utawa. Watawa wa Dominican (Wadominika) na wa Franciscan (Wafransiska) wakawa wanashindana katika kupata umaarufu na kupendwa na watu wengi. Walijitahidi kufikia lengo hili kwa kuyapamba makanisa yao yawe ya kuvutia, na kuzifanya sherehe zao kuwa za fahari, na kuweka vivutio vya mifupa ya watakatifu waliokufa zamani (au vitu-relics), ambayo ilikuwa maarufu sana, pamoja na sanamu zilizodaiwa kutenda miujiza. [GC 172.1; PK Aya ya 3]

Wadominika wa Bern waliona kuwa kama wangeweza kumpata msomi yule kijana mwenye karama zilizosheheni, basi, wangejipatia utajiri na heshima. Ujana wake, ushupavu, uwezo wake wa kuzaliwa wa kuhutubu, uandishi na umahiri wake wa muziki na mashairi, hivyo vingewaletea mafanikio makubwa zaidi kuliko urembo, vito, maonyesho, na kujionyesha kwao katika kuwavuta watu kuja kwenye ibada zao na kuongeza mapato ya shirika lao la watawa. Kwa kutumia udanganyifu, sifa zenye kutiwa chumvi, walijitahidi sana kumshawishi Zwingli kuingia katika chama chao cha watawa. Luther, alipokuwa mwanafunzi shuleni, alijifungia mwenyewe katika chumba kidogo cha nyumba ya watawa, naye asingeonekana au kujulikana ulimwenguni kama majaliwa ya Mungu yasingeingilia kati na kumweka huru. Zwingli hakuachwa pale kupambana na hatari inayofanana na hiyo. Kwa uongozi Wake Mungu, baba yake alipokea taarifa ya hila za watawa. Hakuwa na kusudi la kumwacha mwanawe kufuata maisha yale ya kivivu na yasiyofaa na thamani. Aliona kwamba utumishi wake utakaokuwa na msaada katika maisha ya baadaye ulikuwa hatarini, naye akamwagiza kurudi nyumbani bila kuchelewa [GC 172.2; PK Aya ya 4]

*Relics ni Masalia ya zamani ya watakatifu, yanaweza kuwa mabaki yanayodaiwa kuwa, au halisi ya kimwili ya watakatifu, kama vile mifupa, vipande vya nguo, au baadhi ya vitu vinavyohusishwa na watakatifu, hivi watu wa madhehebu mengine wamefundishwa kuviabudu.

## Zwingli Aigundua Ile Kweli

Agizo lile alilitii; lakini kijana hakuweza kuridhika kukaa katika bonde alilozaliwa kwa muda mrefu, na haikupita muda, naye alirudi tena masomoni kwa kwenda mji wa Basel baada ya kupita muda fulani. Ni mahali Hapa ndipo Zwingli alisikia kwa mara ya kwanza habari ya injili ya neema ya Mungu itolewayo bure. Wittembach, mwalimu wa lugha za kale, alipokuwa akijifunza Kigiriki (Kiyunani) na Kiebrania, aliongozwa kwenye Maandiko Matakatifu, na kwa njia hiyo mionzi ya nuru ya mbinguni iliangaza ndani ya mioyo ya wanafunzi waliokuwa chini yake. Akawatangazia kwamba palikuwa na Ukweli wa zamani zaidi, na wenye thamani kubwa sana kuliko nadharia zile zilizofundishwa na waalimu wa shule pamoja na wanafalsafa. Ukweli huu wa zamani ulisema kwamba kifo Chake Kristo kilikuwa ndiyo fidia pekee ya mwenye dhambi. Kwa Zwingli maneno haya yalikuwa kama mwale wa kwanza wa nuru inayotangulia mapambazuko. [GC 173.1; PK Aya ya 5]

Muda si mrefu Zwingli aliitwa kutoka Basel kuanza kazi yake ya maisha. Eneo lake la kwanza la kazi lilikuwa katika parishi ya Milimani Alps, hapa hapakuwa mbali na bonde alilozaliwa. Akiisha kuwekewa mikono ya ukasisi, alijitoa wakfu kwa moyo wake wote kuitafuta ile Kweli ya Mungu; kwa kuwa alikuwa na utambuzi mzuri," alisema Mwanamatengenezo mwenzake, "Yule aliyekabidhiwa kundi la Kristo anapaswa awe na maarifa kwa kiasi kikubwa." - Wylie, kitabu cha 8, sura ya 5. Kwa kadiri alivyozidi kuyachunguza Maandiko, ndivyo alivyozidi kuona tofauti dhahiri kati ya Kweli Zake Mungu na uongo wa Rumi. Akajisalimisha mwenyewe kwa Biblia kama Neno la Mungu, kanuni ya pekee inayojitosheleza, na isiyoweza kukosea kamwe. Aling'amua sharti Maandiko yajitafsri yenyewe. Yeye hakuthubutu kuyafafanua Maandiko ili kuunga mkono nadharia, ubunifu, Fundisho au ufafanuzi fulani uliofanywa na watu siku za huko nyuma, bali alichukua kuwa jukumu lake kujifunza mafundisho yaliyo dhahiri na wazi (kwamba yanafundisha nini kwa usahili). Alijitahidi kupata kila msaada alioweza kuupata ili kuweza kupata uelewa sahihi wa maana yake, na aliomba msaada wa Roho Mtakatifu, ambaye angemsaidia kuyaelezea, na kuyafunua kwa wote waliotafuta kwa unyofu wa moyo na maombi. [GC 173.2; PK Aya ya 6]

"Maandiko," alisema Zwingli, "yanatoka kwa Mungu, sio kwa mwanadamu, na hivyo Yule Mungu anayeangazia, atakupa ufahamu kwamba Maneno hayo yanatoka kwa Mungu. Neno la Mungu ... haliwezi kushindwa au kuanguka; linang'aa, linajifundisha lenyewe, linajifunua lenyewe, linaitia nuru nafsi kwa kuipa wokovu wote na neema, na kufariji katika Mungu, linanyenyekesha moyo kiasi kwamba moyo unajiachia na kujikana wenyewe (ubinafsi unakufa), na kumkumbatia Mungu." Ukweli wa maneno yale ulithibitishwa na Zwingli mwenyewe. Aliongea juu ya uzoefu wake wa maisha kwa wakati ule, na baadaye aliandika, akisema: "Wakati mimi ... nilipojitoa kikamilifu kwa Maandiko

Matakatifu, falsafa na theolojia (elimu Chuoni) daima vilipendekeza migogoro kwangu. Mwishowe nikafikia msimamo huu, nikafikiri hivi, 'Yakupasa kuacha uongo wote, na kujifunza Neno la Mungu peke yake kutoka katika Neno lake lililo sahili.' Ndipo nikaanza kumwomba Mungu anipe nuru yake, ndipo Maandiko yakaanza kuwa rahisi zaidi kwangu." – Ibid kitabu cha 8, sura ya 6. [GC 174.1; PK Aya ya 7]

**Afundisha Mafundisho Ya Yesu**

Fundisho la imani alilolihubiri Zwingli halikutoka kwa Luther. Lilikuwa ni Fundisho la Kristo. "Kama Luther anamhubiri Kristo," alisema yule Mwanamatengenezo wa Kiswisi (Switzerland), "basi, anafanya kile ninachofanya mimi. Wale ambao amewaleta kwa Kristo ni wengi zaidi kuliko wale niliowaongoza mimi. Lakini hii haijalishi. Mimi sibebi jina jingine lolote isipokuwa lile la Kristo, ambaye mimi ni askari Wake, na ambaye Yeye peke yake Ndiye Mkuu wangu. Sijawahi kabisa kumwandikia Luther hata neno moja, wala Luther hajawahi kuniandikia mimi. Na kwa nini? ... ili ipate kuonekana kwamba Roho Mungu ni Yule Yule mmoja (Mungu hapingani na Mungu), kwa sababu, sisi sote wawili, bila kufanya njama au mapatano yoyote ya siri, tunafundisha fundisho la Kristo kwa usawa unaolingana." D`Aubigne, 8, sura ya 9. [GC 174.2; PK Aya ya 8]

Mnamo mwaka wa 1516, Zwingli alialikwa kuwa mhubiri katika nyumba ya watawa huko Einsiedeln. Hapa angepata nafasi ya kujionea mwenyewe kwa karibu zaidi ufisadi wa kanisa la Rumi, na alikuwa anakwenda kuweka mvuto wenye nguvu kama Mwanamatengenezo ambao ungeonekana na kuvuka mipaka ya kijijini kwao pale Alps alikozaliwa. Miongoni mwa vivutio vikuu vya jiji la Einsiedeln ilikuwa ni ile sanamu ya Bikira ambayo ilisemekana kwamba ilikuwa na nguvu ya kufanya miujiza. Juu ya lango kubwa la kuingilia kwenye nyumba ya watawa palikuwa na maandishi haya, "Hapo ondoleo kamili la dhambi zote linaweza kupatikana." -Ibid., b. 8, sura ya 5.8. Mahujaji walikwenda misimu yote kwenye sehemu hii takatifu ya Bikira (waliona ni mahali patakatifu au madhabahu); lakini wakati wa sherehe kubwa ya kuwekwa wakfu kila mwaka, watu wengi walikuja pale kutoka katika sehemu zote za nchi ya Uswisi, na hata kutoka Ufaransa na Ujerumani. Zwingli, akiwa ameumia na kusumbuliwa sana kwa kuiona sanamu ile, alichukua fursa kuwatangazia uhuru watumwa hawa wa ushirikina, uhuru upatikanao kwa njia ya injili. [GC 174.3; PK Aya ya 9]

"Msidhani kwamba," akasema, "Mungu Yu katika hekalu hili zaidi sehemu nyingine yoyote ya uumbaji Wake. Haidhuru nchi mnayokaa iwe ni nchi gani, Nchi yoyote unayokaa, Mungu Yuko pamoja nawe, na anakusikia Je, ….inawezekana kazi zisizoleta manufaa yoyote, safari ndefu za kuhiji, sadaka,

sanamu zinazoabudiwa, dua zenu kwa Bikira au watakatifu zinaweza kuwahakikisha ninyi kupata neema ya Mungu?... Kuna faida gani kuwa na maneno mengi ya kupamba sala zetu? Je! Ni mafanikio gani yanayopatikana kwa kuvaa kofia kubwa inayopendeza yenye kola ya kikuhani shingoni (cowl), na kichwa laini kilichonyolewa upara na kung'aa, na joho refu linalopepea huku na huko, au kuvaa malapa yaliyotariziwa kwa dhahabu?... Mungu anauangalia moyo, na mioyo yetu iko mbali Naye." "Kristo," alisema, "ambaye alitolewa mara moja pale msalabani, Yeye Ndiye kafara na Kondoo wa Kafara (mhanga), aliyekuwa na ufumbuzi uliotosheleza dhambi kwa wote waaminio milele zote." --Ibid., b. 8, sura ya 5. [GC 175.1; PK Aya ya 10]

Kwa wasikilizaji wengi waliokuwa pale mafundisho hayo hayakupendwa wala kukaribishwa. Lilikuwa ni jambo chungu sana na lililowakatisha tamaa kuambiwa kwamba safari zao ngumu na kuchosha za hija walizokuwa wamezifanya zilikuwa ni kazi bure kabisa. Msamaha ule utolewao bure ndani ya Kristo hawakuweza kuuelewa. Waliridhika na njia ya zamani ya kwenda mbinguni ambayo Rumi ilikuwa imewawekea alama za kupita. Walijiepusha na fedheha ya kutafuta kitu chochote bora. Walikuwa wametosheka na njia ile ya zamani ya kwenda mbinguni ambayo Rumi alikuwa imewawekea alama kwa ajili yao. Walisita kujiingiza katika utata na mahangaiko ya kutafuta njia nyingine iliyokuwa bora zaidi. Ilikuwa rahisi zaidi kwao kuwatumaini makuhani, na kuwawajibisha kubeba jukumu la wokovu wao na papa kuliko kutafuta usafi wa moyo. [GC 175.2; PK Aya ya 11]

Lakini tabaka jingine likazipokea kwa furaha habari zile za wokovu kupitia kwa Kristo. Maadhimisho (taratibu) yale yaliyokuwa yameamriwa na Rumi yalikuwa yameshindwa kabisa kuwaletea amani moyoni mwao, nao kwa imani wakaikubali damu Yake Mwokozi kama ndiyo upatanisho wao. Hawa walirudi nyumbani kwao kuwafunulia wengine nuru ile ya thamani waliyokuwa wameipokea. Kwa njia hiyo, Ukweli ukabebwa kutoka kijiji hata kijiji, toka mji hata mji, na idadi ya mahujaji wa kumbukumbu ya Bikira ilipungua sana. Matoleo yao sadaka yakapungua, na matokeo yake mshahara wa Zwingli uliotokana na kipato hicho, ukapungua pia. Lakini jambo lile likamletea furaha tu kwake alipoona kwamba nguvu ya unafiki pamoja na ushirikina ilikuwa ukivunjwa. [GC 175.3; PK Aya ya 12]

Mamlaka ya kanisa haikuwa kipofu kuhusu kazi aliyokuwa akiifanya Zwingli; lakini kwa muda huu walistahimili wasiweze kuingilia kati. Wakitumainia kumvuta awe upande wa kusudi lao, walijitahidi kumshawishi kwa kumsifia kwa udanganyifu; na wakati huo huo Ukweli ulikuwa unaendelea kushikilia mioyo ya watu kwa nguvu. [GC 176.1; PK Aya ya 13]

**Ahubiri Katika Kanisa Kuu La Jimbo Pale Zurich.**

Kazi za Zwingli huko Einsiedeln zilimwandaa kufanya kazi katika eneo pana zaidi, naye alikuwa karibu kuanza kazi hiyo muda mfupi toka pale. Baada ya kukaa miaka mitatu pale, alipewa wito wa kazi ya mhubiri katika kanisa kuu la jimbo la Zurich (Cathedral). Wakati ule ulikuwa ni mji muhimu katika Muungano wa shirikisho la Uswisi kuliko miji yote, na mvuto wenye nguvu ambao ulitolewa hapa, uliweza kugusa eneo kubwa. Japo viongozi wa kanisa ndio waliompa mwaliko kwenda Zurich, hata hivyo, walitaka kuzuia ubunifu wowote au mambo mapya, na kwa ajili hiyo, walichukua hatua ya kumfundisha majukumu yake yalivyopaswa kuwa. [GC 176.2; PK Aya ya 14]

"Utatumia kila juhudi" walisema, "kukusanya mapato ya kanisa mahalia, bila kuacha hata pato dogo kabisa. Utawahimiza walio waaminifu, kutoka katika mimbari na katika chumba cha kitubio, ili walipe zaka zao pamoja na kodi zote, na kuwafanya waonyeshe kwa sadaka zao upendo walio nao kwa kanisa hili. Utafanya bidii kuongeza mapato yatokayo kwa wagonjwa, yanayotokana na misa na kwa jumla kutokana na kila huduma au hafla ya kanisa." "Kuhusu huduma ya sakramenti, mahubiri, na kulilisha kundi hili," waliongeza kusema wakufunzi wake, "haya pia ni majukumu ya kiongozi wa kiroho au chapleini (chaplensia). Lakini kwa haya unaweza kutumia mtu mbadala, na hususani katika kuhubiri. Usimpe sakramenti mtu yoyote, isipokuwa watu mashururi au muhimu tu, na kwa wakati ule unapoalikwa tu; unakatazwa kufanya hivyo bila ya kuwatofautisha watu." -Ibid., b. 8, sura ya 6. [GC 176.3; PK Aya ya 15]

**Kristo Kiini Cha Mahubiri Yake**

Zwingli alisikiliza maelekezo akiwa kimya, na kwa kujibu, na akatoa shukrani yake kwa heshima ya wito ule wa kuja kwenye kituo kile cha muhimu, akaendelea kuwaeleza njia aliyokuwa anapendekeza kuitumia. "Maisha Yake Kristo," akasema, "yamefichwa mbali na watu kwa muda mrefu mno. Nitahubiri kitabu chote cha Injili ya Mtakatifu Mathayo,...nikichota kutoka katika chemchemi/visima vya Maandiko peke yake, nikizama kwenda chini kabisa, nikilinganisha fungu moja la Maandiko na jingine, na kutafuta ufahamu kwa njia ya maombi ya dhati, na bidii daima. Ni kwa ajili ya utukufu wa Mungu, kwa ajili ya sifa za Mwanawe wa pekee, kwa ajili ya wokovu halisi wa roho za watu, na kwa ajili ya kuwajenga katika imani ya Ukweli, ndiyo mimi nitajitoa wakfu kufanya huduma hii."- Ibid., b. 8, sura ya 6. Ingawa baadhi ya viongozi wa kanisa hawakukubali mpango wake, na walijaribu kumshawishi aachane nao, Zwingli alisimama kidete. Alisema kwamba alikuwa haleti mbinu yoyote mpya, bali mapito yale ya zamani yaliyotumiwa na kanisa la awali na nyakati safi. [GC 176.4; PK Aya ya 16]

Tayari shauku ilikuwa imeamshwa katika Kweli zile alizozifundisha; na watu wengi wakamiminika kwa idadi kubwa kuja kusikiliza mahubiri yake. Watu wengi

ambao kwa muda mrefu walikuwa wameacha kuhudhuria ibada wakawa miongoni mwa wasikilizaji wake. Alianza huduma yake kwa kuwafunulia vitabu vya Injili, akiwasomea na kuwaeleza wasikilizaji wake kisa kile cha maisha ambayo yalikuwa yamevuviwa, yaani mafundisho, na kifo Chake Kristo. Hapa, kama ilivyokuwa kule Einsiedeln, aliwasilisha Neno la Mungu kuwa peke yake ndilo lenye mamlaka isiyoweza kukosea kamwe, na ya kwamba kifo Chake Kristo ndiyo dhabihu/kafara pekee kamilifu. “Ni Kwake Kristo,” alisema, “mimi ninatamani kuwaongoza ninyi - kwa Kristo, Chanzo cha Kweli cha wokovu.”—Ibid. b. 8, sura ya 6. Mhubiri huyu alizungukwa na watu waliosheheni wa matabaka yote, kuanzia viongozi wa serikali, wasomi, mafundi na hata wakulima wadogo. Kwa hamu kubwa sana waliyasikiliza maneno yake. Yeye hakutangaza tu kutolewa kwa wokovu bure, bali pia, bila woga wowote aliyakemea maovu na ufisadi wa nyakati zile. Wengi walirudi kwao toka kwenye kanisa lile kuu wakimsifu Mungu. “Mtu huyu,” walisema, “ni mhubiri wa ile Kweli. Atakuwa Musa wetu kutuongoza sisi kutoka katika giza hili la Kimisri.” -Ibid., b. 8, sura ya 6. [GC 177.1; PK Aya ya 17]

Ingawa mwanzoni kazi zake zilipokelewa kwa furaha na shauku kubwa, baada ya muda upinzani uliibuka, Watawa wakanuia kujipanga pamoja ili kuipinga kazi yake, na kuyalaani mafundisho yake. Wengi walimshambulia kwa matusi, kejeli, na kumkenulia meno yao (kumng’onga); wengine wakatumia jeuri, matusi, kumkosea adabu na vitisho. Lakini Zwingli alichukuliana na yote, akisema: “Kama tunataka kuwaleta waovu kwa Yesu Kristo, basi, ni lazima tufumbe macho yetu dhidi ya mambo mengi.” - Ibid., b. 8, sura ya 6. [GC 177.2; PK Aya ya 18]

Karibu na wakati huu, mtendakazi mwingine mpya alijitokeza wa kuiendeleza kazi ile ya Matengenezo ya Kanisa. Mtu mmoja kutoka mji wa Lucerne alitumwa kutoka Zurich na rafiki wa Mwanamatengenezo aliyeishi mji wa Basel akiwa na baadhi ya machapisho ya Luther, alishauri kwamba uuzaji wa vitabu hivi vya Luther ungekuwa njia yenye nguvu ya kuitawanya nuru ile. “Jihakikishie mwenyewe,” akamwandikia Zwingli, “kama mtu huyo ana busara ya kutosha pamoja na ujuzi wa kutosha; kama ndiyo hivyo, basi, mruhusu kuvipeleka toka mji hadi mji, kutoka kijiji hadi kijiji na hata nyumba kwa nyumba, miongoni mwa Waswisi, kazi hizo za Luther (vitabu au maandishi), na hasa maelezo yake ya ufafanuzi juu ya Sala ya Bwana, ambayo yameandikwa kwa ajili ya walei (waumini wa kawaida). Kadiri watu watakavyozidi kuyajua haya, ndivyo wanunuzi watakavyozidi watazidi kuongozeka.” –-Ibid., b. 8, sura ya 6. Hivyo ndivyo nuru ilivyopata njia ya kuingia. [GC 178.1; PK Aya ya 19]

Wakati Mungu anapoandaa mkakati wa kuvunja pingu za ujinga na ushirikina, ndipo wakati Shetani anapofanya kazi yake kwa nguvu zake zote kuwafunga wanadamu hao katika giza na kuwafunga pingu na kuzikaza kwa uthabiti zaidi. Watu walipokuwa wanajitokeza katika nchi mbalimbali kuhubiri kwa watu

msamaha na kuhesabiwa haki kwa njia ya damu Yake Kristo, Rumi ilikuwa inasonga mbele kwa nguvu mpya kufungua masoko yake katika Ulimwengu wote wa Kikristo, ikiuza misamaha kwa fedha. [GC 178.2; PK Aya ya 20]

Kila dhambi ilikuwa na bei yake, na watu walipewa leseni ya bure ya uhalifu (ruksa ya dhambi) alimradi tu hazina ya kanisa ilikuwa ikiendelea kujazwa vizuri daima. Kwa hivyo, harakati hizo mbili ziliendelea (makundi mawili), -- Kundi moja likitoa msamaha wa dhambi kwa malipo ya fedha, na jingine msamaha wa bure kupitia njia ya Kristo,-- Rumi ikitoa liseni ya kutenda dhambi na kufanya iwe ndicho chanzo chake cha mapato; Wanamatengenezo wakishutumu dhambi na kuwaelekeza watu kwa Kristo kuwa Ndiye mpatanishi wao na Mkombozi wao. [GC 178.3; PK Aya ya 21]

**Mauzo Ya Vyeti Vya Msamaha Wa Dhambi Kule Uswisi**

Katika nchi ya Ujerumani kazi hiyo ya uuzaji wa vyeti vya msamaha wa dhambi ilikabidhiwa kwa watawa wa Dominican (Wadominikani), na ikaendeshwa na mtu mwenye sifa mbaya za ukorofi, Tetzel. Katika nchi ile Uswisi biashara ile ilikabidhiwa mikononi mwa watawa wa Franciscan (Wafransiskani), chini ya uongozi wa Samsoni, mtawa wa Kiitaliano. Samsoni tayari alikuwa amekwisha kufanya kazi nzuri kwa ajili ya kanisa, huyu akajipatia fedha nyingi sana kutoka Ujerumani na Uswisi na kujaza hazina ya papa. Sasa akasafiri katika nchi ya Uswisi, akiyavuta makundi makubwa ya watu, na kuwanyang'anya wakulima maskini mapato yao haba, na kudai kwa nguvu kupewa zawadi nono kutoka kwa tabaka ya matajiri. Lakini ushawishi wa yale Matengenezo ya Kanisa tayari ulikuwa umesikika kiasi cha kuipunguza, japokuwa si kuikomesha kabisa, biashara ile. Zwingli alikuwa bado angali pale Einsiedeln, mara Samsoni alipoingia katika nchi ya Uswisi, alifika na biashara yake katika mji wa jirani. Akiwa amearifiwa juu ya utume wake ule, yule Mwanamatengenezo alianza mara moja kumpinga. Watu hao wawili hawakukutana, lakini hayo yalikuwa ndiyo mafanikio ya Zwingli katika kuuweka peupe unafiki (feki) wa mtawa Samson hata akalazimika kwenda mahali pengine. [GC 178.4; PK Aya ya 22]

Akiwa Zurich, Zwingli alihubiri kwa bidii dhidi ya wafanya biashara wa misamaha ya dhambi wenye tamaa ya fedha; na Samsoni alipokaribia mji ule, alikutana na mjumbe kutoka kwenye baraza aliyekuwa na taarifa iliyosema kwamba alitarajiwa kupitiliza hapo na kuendelea mbele na safari yake. Hata hivyo Samson aliweza kuingia pale kwa kutumia hila, lakini akalikuzwa bila kuuza hata msamaha wa dhambi mmoja, na muda mfupi baada ya hapo akaondoka katika nchi ya Uswisi. [GC 179.1; PK Aya ya 23]

Msukumo wenye nguvu ulikuja kusaidia harakati za Matengenezo ya Kanisa lilipotokea pigo la tauni (plague), au Mauti Kuu (Great Death), gonjwa hili lilifagia nchi yote ya Uswisi katika mwaka 1519. Watu wengi walipokabiliwa uso

kwa uso na ugonjwa unaoua, wengi waliona jinsi vyeti vya msamaha wa dhambi vilivyokuwa ni ubatili mtupu na visivyo na thamani kabisa, vyeti ambavyo walikuwa wametoka kuvinunua karibuni tu; nao wakatamani kuupata msingi imara (nanga) kwa ajili ya imani yao. Zwingli akiwa Zurich alipata pigo kali la tauni; alikuwa mahututi sana, na matumaini yote ya kupona kwake yalipotea, na habari ikasambazwa kila mahali kwamba alikuwa amekufa. Katika saa ile ya kujaribiwa sana, tumaini na ujasiri wake havikutetereka. Kwa imani aliutazama ule msalaba wa Kalvari, akiutegemea upatanisho kamili, utoshao kwa dhambi zake. Aliporudi kutoka karibu na malango ya mauti, ilikuwa ni kwa kusudi la kuihubiri injili kwa bidii nyingi zaidi kuliko hapo awali; na yale maneno yake yakawa na nguvu kubwa isiyo ya kawaida. Watu walimkaribisha kwa furaha mchungaji wao mpendwa aliyerudishwa kwao toka kwenye ukingo wa kaburi. Wao wenyewe walikuwa wametoka kuwahudumia wagonjwa pamoja na wale waliokuwa wanakufa, nao wakahisi mioyoni mwao, kuliko huko nyuma, faida ya injili. [GC 179.2; PK Aya ya 24]

Zwingli alikuwa amefikia uelewa ulio wazi zaidi wa Ukweli wa injili, tena kwa ukamilifu zaidi alikuwa ameuonja uzoefu mkamilifu katika utu wake wa ndani, nguvu ya injili inayobadilisha na kumfanya mtu awe kiumbe kipya. Anguko la mwanadamu dhambini pamoja na mpango wa ukombozi yalikuwa ndiyo masomo aliyokita zaidi kufundisha. “Ndani ya Adamu,” alisema, “sisi sote tumekufa, tumezama katika ufisadi na laana ya kuhukumiwa.” -- Wylie, b. 8, sura ya 9. “Kristo ... amenunua kwa ajili yetu sisi ukombozi usiokwisha....Shauku Yake… ndiyo kafara Yake ya milele, ambayo ina uwezo wa usiokoma kuponya na kuokoa; inakidhi haki ya Mungu milele kwa ajili ya wale wote wanaoitegemea kwa imani thabiti, isiyotikisika.” Hata hivyo, alifundisha wazi kabisa kwamba wanadamu, kwa sababu ya neema hiyo ya Kristo, hawako huru, kuendelea kuishi katika dhambi. “Mahali popote palipo na imani kwa Mungu, hapo Yupo Mungu; na popote Mungu alipo, hapo ndipo ilipo juhudi inayosihi na kuwasukuma watu kutenda matendo mema.” - D’Aubigne b, kitabu cha 8, sura ya 9. [GC 180.1; PK Aya ya 25]

Hiyo ndiyo shauku waliyokuwa nayo watu kwa mahubiri ya Zwingli hata Kanisa lile kuu likawa likijaa na kufurika kwa makundi ya watu waliokuja kumsikiliza. Kidogo-kidogo kadiri walivyoweza kuelewa na kucheua, alifunua Ukweli zaidi kwa wasikilizaji wake. Alikuwa mwangalifu kutoleta mwanzoni vipengele vile ambavyo vingewashtua sana na kuamsha chuki na upinzani. Kazi yake ilikuwa ni ile ya kuiongoa mioyo yao ili ipate kuyapokea mafundisho ya Kristo, kuilainisha kwa kuwaonyesha upendo Wake, na kuweka mbele yao mfano Wake; na kadiri ambavyo wangeendelea kuzipokea kanuni za injili, basi, imani zao za kishirikina pamoja na mapokeo yao au desturi vingepinduliwa chini. [GC 180.2; PK Aya ya 26]

Hatua kwa hatua Matengenezo ya Kanisa yalisonga mbele katika jiji lile la Zurich. Kwa tahadhari, adui zake wakaamka na kufanya upinzani wenye nguvu. Mwaka mmoja kabla ya mtawa wa Wittenberg, Luther kutamka 'Hapana' yake kwa papa na kwa mfalme wa dola kule Worms, na sasa kila kitu kilionyesha kana kwamba mashambulizi yale yalikuwa yanarudiwa kule Zurich kwa madai ya upapa. Mashambulio ya mara kwa mara yalifanyika dhidi ya Zwingli. Katika yale majimbo au maeneo ya papa, mara kwa mara, wanafunzi wake wa injili waliletwa kwenye mti wa kuchomea watu na kuchomwa moto, lakini hili halikutosha; mwalimu wa uzushi (yaani, Zwingli) alipaswa kunyamazishwa. Kwa hiyo, askofu wa Constance aliwatuma wajumbe watatu kwenye Baraza la Zurich kumshtaki Zwingli akisema kwamba alikuwa akiwafundisha watu kuziasi amri za kanisa, na kwa njia ile kuhatarisha amani na kuleta vurugu. Endapo mamlaka ya kanisa ingeweza kuwekwa kando, alisisitiza, basi maasi ya watu wote dhidi ya serikali zote yangetokea. Zwingli alijibu kwa kusema kwamba kwa miaka minne alikuwa akihubiri injili katika jiji la Zurich, "ambao ulikuwa shwari na wenye amani kuliko mji mwingine wowote katika shirikisho." "Hivi" akasema, "Je, Ukristo sio kinga bora kuliko zote ya usalama wa watu wote?" -- Wylie, b. 8, sura ya 11. [GC 180.3; PK Aya ya 27]

Manaibu walikuwa wamewapa ushauri madiwani wa baraza waliokuwa pale kuendelea kukaa ndani ya kanisa la Rumi kwa vile nje ya kanisa lile walisema kwamba hakuna wokovu. Zwingli akajibu: "Hebu mashtaka haya yasiwafanye mtikisike. Msingi wa Kanisa ni Mwamba ule ule, yaani, Kristo Yule Yule ambaye alimpa Petro jina Lake kwa sababu alimkiri Yeye kwa uaminifu (Mt.16:16-18]. Katika kila taifa yeyote amwaminiye Bwana kwa moyo wake wote hukubaliwa na Mungu (Mdo 10:34,35). Hapa, kusema kweli, ni kanisa ambamo, hakuna hata mmoja awezaye kuokolewa." - D'Aubigne, London ed., B. 8, sura ya 11. Matokeo yake, mmojawapo wa manaibu wa askofu aliipokea imani ya Matengenezo. [GC 181.1; PK Aya ya 28]

Baraza lilikataa kuchukua hatua yoyote dhidi ya Zwingli, ndipo Rumi ikajiandaa upya kufanya shambulio jipya. Mwanamatengenezo alipopewa taarifa ya njama za maadui zake, alisema kwa nguvu: "Acheni waje; mimi nawaogopa kama vile mwamba ulio mrefu ulio pembezoni mwa bahari unavyoyaogopa mawimbi yanayolipiga na kunguruma miguuni pake." - Wylie, kitabu cha 8, sura ya 11. Jitihada za viongozi wa kanisa zilisaidia kusukuma mbele kazi waliyotaka kuiangusha. Ukweli ukaendelea kuenea. Kule Ujerumani wafuasi wa ile Kweli, wakiwa wamegubikwa na huzuni kwa kutoweka kwa Luther, walitiwa moyo tena walipoyaona maendeleo ya Injili katika nchi ya Uswisi. Wylie, b. 8, sura ya 11. [GC 181.2; PK Aya ya 29]

Matengenezo ya Kanisa yalipojiimarisha katika jiji la Zurich, matunda yake yalionekana kikamilifu zaidi katika kupungua kwa maovu, utaratibu na amani.

“Amani imefanya maskani yake hapa katika mji wetu,” aliandika Zwingli; “hakuna magomvi, hakuna unafiki, hakuna wivu, wala migogoro. Je! Ni wapi muungano kama huu unaweza kupatikana kama siyo kwa Bwana peke yake, pamoja na haya mafundisho yetu ya dini ambayo hutujaza sisi kwa matunda ya amani na utauwa?” -- Ibid., b. 8, sura ya 15. [GC 181.3; PK Aya ya 30]

Ushindi ambao wanamatengenezo wa Kanisa waliupata yaliwachochea Warumi kufanya juhudi nyingi zaidi zilizodhamiriwa kabisa ili kuyavunjilia mbali. Walipoona jinsi walivyopata mafanikio kidogo tu kwa kutumia mateso na kuikandamiza kazi ya Luther kule Ujerumani, waliamua kupambana na Matengenezo ya Kanisa kwa kutumia silaha zake. Waliamua kufanya mdahalo (debate) na Zwingli, na kwasababu wao ndio walipanga mambo hayo, wangehakikisha kwamba wanapata ushindi kwa kuchagua wenyewe, sio tu mahali pa majadiliano yale, bali pia majaji ambao wangeamua kati yao na upande ule wa Zwingli. Na kama wangeweza kumshika Zwingli mara moja tu na kumweka chini ya mamlaka yao, basi, wangehakikisha kwamba hawaponyoki. Ikiwa kiongozi huyu angenyamazishwa, basi, kundi lile lingevunjwa-vunjwa kwa haraka sana. Kusudi lile, hata hivyo, lilikuwa limefichwa kwa uangalifu sana [GC 181.4; PK Aya ya 31]

Mdahalo ule ulipangwa kufanyika mji wa Baden; lakini Zwingli hakuhudhuria. Baraza la Zurich, likishuku mipango ya hila ya wafuasi wa upapa, tena likiwa limepata onyo la marundo ya kuni yaliyowashwa katika majimbo ya papa dhidi ya wafuasi wa injili, walimkataza mchungaji wao asijipeleke katika hatari ile. Pale Zurich alikuwa tayari kukutana na wafuasi shupavu wa papa ambao angeweza, angewatuma pale; lakini kwenda kule Baden, ambako damu ya wafia dini kwa ajili ya ile Kweli ilikuwa imetoka kumwagwa siku za karibuni, ingekuwa ni kujipeleka kwenye kifo cha uhakika. Oecolampadius na Haller walichaguliwa kuwawakilisha Wanamatengenezo, wakati Dr. Eck, mtu mashuhuri, akisaidiwa na kundi kubwa la madaktari wengi wasomi wa falsafa wa theolojia, pamoja na maaskofu, alikuwa ndiye mtetezi hodari wa Rumi. [GC 182.1; PK Aya ya 32]

Ijapokuwa Zwingli hakuwapo kwenye mdahalo, ushawishi wake uliweza kusikika kule. Makatibu muhtasi wote walichaguliwa na wafuasi wa papa, watu wengine walikatazwa kuchukua kuandika ripoti ya yale yanayosemwa kwa tishio la kifo. Licha ya hayo yote, Zwingli alipokea taarifa ya kuaminika ya yote yaliyosemwa pale Baden kila siku. Mwanafunzi fulani aliyehudhuria kwenye mdahalo ule kila jioni aliandika kumbukumbu ya hoja zilizowasilishwa siku ile. Karatasi zile wanafunzi wengine wawili walichukua jukumu la kuzipeleka kule Zurich, pamoja na barua za kila siku za Oecolampadius zilizoandikwa kwa Zwingli huko Zurich. Mwanamatengenezo Zwingli alijibu na kutoa ushauri na mapendekezo yake. Barua zake ziliandikwa usiku, kisha wanafunzi wale walirudi nazo Baden asubuhi. Ili kukwepa macho ya udadisi ya mlinzi aliyewekwa kwenye

malango ya mji ule, wajumbe wale walijitwika vikapu vilivyokuwa na kuku ndani yake, nao waliruhusiwa kupita bila kipingamizi chochote. [GC 182.2; PK Aya ya 33]

Hivyo ndivyo Zwingli alivyoendeleza vita dhidi ya wapinzani wake wajanja. “Amefanya kazi zaidi,” alisema Myconius, “kwa kutafakari kwake, kukesha mara nyingi usiku, na kwa ushauri wake alioutuma kule Baden kuliko vile ambavyo angefanya kwa kujadiliana mbashara na maadui zake.” - D'Aubigne, b. 11, sura ya 13. [GC 183.1; PK Aya ya 34]

Wafuasi wa Rumi, wakiwa na moto wa furaha tele kwa matarajio yao ya kupata ushindi, walikuwa wamekuja Baden wakiwa wamevalia majoho ya ghali sana, yaliyomeremeta kwa vito vya thamani. Meza zao za anasa zilisheheni vyakula vitamu vya gharama kubwa sana, na mvinyo maarufu unaopendwa na wengi. Mzigo wa kazi majukumu yao ya kikanisa ulipunguzwa na wakajiona wepesi wa moyo walipojihusisha na shamrashamra, makelele na vifijo vya sherehe na unywaji kwenye sherehe zao. Kwa tofauti iliyoonekana wazi, Wanamatengenezo walikuwa tofauti kabisa, kwani walionekana kama watu fukara, au karibia kufanana na kundi la ombaomba, chakula chao kidogo na cha kimasikini, kiliwaweka mezani kwa muda mfupi tu. Mwenye nyumba aliyopangisha Oecolampadius, alichukua muda fulani kumchungulia chumbani mwake, na kila wakati alimkuta akijishughulisha na kusoma au kusali, na kwa mshangao sana aliripoti kwamba angalau mzushi huyo alikuwa "mchaji Mungu sana". [GC 183.2; PK Aya ya 35]

Katika mdahalo ule, Eck alipanda kwa madaha kwenda juu kwenye mimbari iliyopambwa kifahari, wakati masikini Oecolampadius alikuwa amevaa nguo za kimaskini, naye alilazimika kukaa juu ya kigoda kilichochongwa hovyo ovyo (rafu) tu mbele ya mpinzani wake.” -- Ibid., b. 11, sura ya 13. Sauti yake Eck yenye mamlaka ilisikika mbali, naye alikuwa na kujiamini kusiko na mipaka ambako hakukuwahi kumwangusha kamwe. Juhudi yake ile ilichochewa na tumaini la kupewa utajiri/dhahabu na umaarufu; kwa kuwa huyu mtetezi wa imani ya Rumi alipaswa kuzawadiwa kwa malipo mazuri. Wakati hoja zake nzuri au zenye mashiko ziliposhindwa, aliamua atatumia matusi, kashfa na hata kutoa laana. [GC 183.3; PK Aya ya 36]

Oecolampadius,mtu aliyejistahi, mwenye kiasi na asiyejitumainia mwenyewe, alikuwa amejikunja kwa woga wa pambano, naye aliingia katika pambano akikiri kwa kiapo na kicho kwa kusema: “Sitambui kiwango kingine chochote cha maamuzi zaidi ya Neno la Mungu.” - Ibid.,b. 11, sura ya 13, Ingawa alikuwa mpole, mwungwana na mwenye adabu katika mwenendo wake, alionekana kuwa anao uwezo na msimamo usioyumbayumba, au kuzimia. Wakati wafuasi wa Rumi kulingana na mazoea yao, walitaja mamlaka ile itokanayo na desturi za kanisa, Mwanamatengenezo huyu alishikilia kikamilifu Maandiko Matakatifu. “Desturi,”

alisema, “hazina nguvu katika nchi yetu ya Uswisi, ila tu kama zitaendana na Katiba ya nchi yetu; basi, katika masuala ya imani, Biblia ndiyo katiba yetu.” - Ibid., b. 11, sura ya 13. [GC 183.4; PK Aya ya 37]

Tofauti iliyoonekana kati ya washindani wale wawili wa mdahalo haikukosa kuwa na matokeo yake. Hoja za mwanamatengenezo zilizotolewa kwa kueleweka wazi, utulivu, upole na uungwana, zilivuta akili za watu waliochukizwa na maneno ya majigambo yaliyokuwa hayajahakikishwa, ambayo Eck aliyatoa kwa kujigamba na makelele mengi. [GC 184.1; PK Aya ya 38]

Mdahalo ule uliendelea kwa siku kumi na nane. Wakati wa kufungwa kwake, wafuasi wa upapa kwa kujiamini, wakadai kwamba wamepata ushindi. Wengi miongoni mwa manaibu walisimama upande wa Rumi, ndipo Baraza lilipotangaza kwamba Wanamatengenezo walikuwa wamemalizwa vibaya sana, tena wakatangaza kwamba, wao pamoja na Zwingli kiongozi wao walikuwa wametengwa na Kanisa. Lakini matunda ya mdahalo ule yalidhihirisha ni upande gani hasa ulionufaika kutokana na mdahalo huo. Shindano lile lilileta usongo/msukumo wenye nguvu kwa kazi ya Waprotestanti, tena haikupita muda mrefu baadaye na miji muhimu ya Bern na Basel ilijitangaza kuwa inaunga mkono Matengenezo. [GC 184.2; PK Aya ya 39]

# SURA YA 10

# MAENDELEO YA MATENGENEZO UJERUMANI

**(Kusonga mbele licha ya matatizo)**

Ufupisho: Mfalme Charles V wa Ujerumani alitangaza kwamba Martin Luther alipaswa kuuawa, na kisha Luther akapotea, hivi ni nani alimchukua? Je, matengenezo makubwa yaliyoanza sasa yalipaswa kusitishwa? Angalia jinsi uongozi wa Mungu ulivyoingilia kati, si tu kwa kumwokoa Luther, bali pia kuwapa watu wa Ujerumani kwa mara ya kwanza Biblia kwa Lugha yao. Luther alitolewa kwenye kasiri ya Wartburg March 1521 kwa ajili ya mashabiki walioleta vurugu. Matukio katika Sura hii ni ya Aprili 1521 mpaka Septemba 1522.

Kule kutoweka kwa Luther kwa siri na ajabu, kulifadhaisha watu na kuleta mshtuko Ujerumani nzima. Maswali kumhusu yeye yalisikika kila mahali. Umbeya mbaya zaidi ulisambazwa na wengi waliamini kwamba alikuwa ameuawa. Kulikuwa na maombolezo makubwa, sio tu kwa marafiki zake wa karibu, bali kwa maelfu ambao hawakuwa wameonesha msimamo wao wa wazi upande wa Matengenezo yale. Wengi wakala kiapo kizito kulipiza kisasi kwa ajili ya kifo chake. [GC 185.1; PK Aya ya 1]

Viongozi wa Rumi waliogopa ghadhabu za watu zilizoinuka dhidi yao. Ingawa mwanzoni walikuwa wamefurahia  kifo cha 'kudhaniwa' cha Luther, haukupita muda, nao walitamani kujificha mbali na ghadhabu ya watu. Maadui zake hawakuwa wametaabishwa na matendo yake ya kijasiri wakati alipokuwa miongoni mwao kama alipokuwa ameondolewa kati yao. Wale ambao katika ghadhabu yao walitaka kumwangamiza yule Mwanamatengenezo hodari sasa walijawa na hofu wakati alipokuwa  mfungwa asiye na msaada wowote. "Njia pekee iliyobaki ya sisi kujiokoa," mtu mmoja alisema, "Ni kuwasha mienge ya moto na kumsaka Luther ulimwenguni kote, na kumrudisha kwenye taifa hili linalomwita." D'Aubigne, b. 9, sura ya 1. Amri ya mfalme ilionekana haina nguvu. Wawakilishi wa papa walijawa na ghadhabu walipoona kwamba walikuwa na mvuto mdogo  sana ukilinganisha na janga lililompata Luther. [GC 185.2; PK Aya ya 2]

Habari zilizosema kwamba Luther alikuwa salama, ijapokuwa alikuwa mfungwa, zilituliza hofu ya watu, ingawa zilizidisha shauku yao juu yake. Maandishi yake yalisomwa kwa shauku kubwa zaidi kuliko hapo awali. Idadi kubwa ya watu ilijiunga kwenye harakati za mtu yule shujaa, ambaye katika mazingira yale ya hatari sana, alilitetea Neno la Mungu mpaka mwisho. Matengenezo yalikuwa yakizidi kupata nguvu kila wakati. Mbegu ambayo Luther alikuwa ameipanda ilichipuka kila mahali. Kutokuwepo kwake kulitimiza kazi ambayo uwepo wake ungeshindwa kuifanya. Watenda kazi wengine walihisi wajibu mpya, kwa kuzingatia kwamba sasa kiongozi wao mkuu alikuwa ameondolewa. Kwa imani na usongo mpya walisonga mbele wakifanya yote yaliyokuwa ndani ya uwezo wao, ili kazi ile iliyokuwa imeanzishwa vizuri sana isikwame. [GC 185.3; PK Aya ya 3]

Lakini Shetani hakuzembea. Sasa alijaribu kukifanya kile ambacho amekuwa akikifanya katika kila harakati za matengenezo--yaani kuwadanganya na kuwaangamiza watu kwa kupandikiza uongo kwa kuleta mbadala bandia kwenye kazi ya Kweli. Kama vile kulivyokuwa na makristo wa uongo katika karne ile ya kwanza ya kanisa la Kikristo, kadhalika waliinuka manabii wa uongo katika karne ile ya kumi na sita. [GC 186.1; PK Aya ya 4]

Watu wachache, walioathiriwa kiundani na msisimko uliokuwepo katika ulimwengu ule wa kidini, walifikiri kuwa wamepokea ufunuo maalumu kutoka Mbinguni na kudai kuwa wameagizwa na Mungu kuyaendeleza matengenezo ya kanisa hadi yatakapokamilika. Matengenezo ambayo, wao walidai, yalikuwa yameanzishwa kwa udhaifu tu na Luther. Kusema kweli, hawa walikuwa wakitengua kazi ile aliyokuwa ameikamilisha. Waliikataa kanuni kuu ambayo ilikuwa msingi halisi wa Matengenezo ya kanisa, kwamba Neno la Mungu ndiyo kanuni inayojitosheleza ya imani na matendo; na badala ya mwongozo huo usiokosea waliweka mbadala usio imara, unaobadilika, usiokuwa na viwango hakika uliotokana na hisia na fikra zao wenyewe. Kwa kitendo hiki cha kumweka kando mgunduzi yule mkubwa wa makosa na uongo (Biblia) mpenyo ukawa ukawa umefunguliwa kwa Shetani kuitawala akili na moyo kama apendavyo mwenyewe. [GC 186.2; PK Aya ya 5]

Mmojawapo wa manabii wale akadai kuwa aliagizwa na malaika Gabrieli. Mwanafunzi aliyeungana naye aliacha masomo yake, akitangaza kwamba Mungu mwenyewe alimpa hekima ya kulifafanua Neno Lake. Wengine ambao kwa hulka yao walikuwa wamejielekeza kwenye ushabiki wa kidini usiotumia hekima na unaopitiliza, waliungana nao. Shuguli ya mashabiki hawa hazikusababisha msisimko mdogo. Mahubiri ya Luther yalikuwa yamewaamsha watu kila mahali kuhisi umuhimu wa kufanya matengenezo na sasa baadhi ya watu waadilifu wa kweli walipotoshwa na uongo wa manabii wale wapya [GC 186.3; PK Aya ya 6]

Viongozi wa harakati hii walienda hadi Wittenberg na kusisitiza madai yao kwa Melanchthon na wafanyakazi wenzake. Wakasema: "Sisi tumetumwa na Mungu kuwafundisha watu. Tumekuwa tukifanya maongezi ya ukaribu sana na Bwana; Sisi tunajua mambo yanayokuja; kwa kifupi, sisi ni mitume na manabii nasi tunatoa wito kwa Dkt. Luther." -- Ibid., b. 9, sura ya 7. [GC 187.1; PK Aya ya 7]

### Mashabiki Wa Dini Wasiotumia Hekima Waleta Kipingamizi

Wanamatengenezo walishtushwa na kupata mkanganyiko. Hili lilikuwa jambo ambalo hawakuwahi kukutana nalo huko nyuma na wala hawakujua wachukue njia gani kulikabili. Melanchthon akasema: "Hakika kuna roho za kustaajabisha ndani ya watu hawa; lakini ni roho za aina gani hizo?..... Upande mmoja, tunapaswa kuchukua tahadhari tusimzimishe Roho wa Mungu na kwa upande

mwingine, inatupasa tuchukue tahadhari tusipotoshwe na roho wa Shetani." -- Ibid., b. 9, sura ya 7. [GC 187.2; PK Aya ya 8]

Tunda la mafundisho mapya likaanza kuonekana waziwazi baada ya muda mfupi. Watu waliongozwa kuipuuza Biblia au kuitupa kando kabisa. Shule zikaingizwa katika vurugu. Wanafunzi, walivikataa vizuizi vyote (makatazo), wakayaacha masomo yao na kujiondoa katika chuo kikuu. Watu ambao walijidhania wenyewe kuwa wana uwezo wa kufanya uamsho wa kiroho na kuongoza kazi ya Matengenezo walifanikiwa tu kuifikisha kazi ukingoni mwa uharibifu. Wafuasi wa dini ya Uroma sasa walipata ujasiri, nao wakashangilia kwa nguvu wakisema: "Limebakia pambano moja tu la mwisho na wote watakuwa upande wetu."-- Ibid., b. 9, sura ya 7. [[GC 187.3; PK Aya ya 9]

Luther akiwa pale Wartburg, alisikia juu ya kile kilichotokea, akasema kwa masikitiko makubwa: "Mimi sikuzote nilitarajia kwamba Shetani angetutumia pigo hili la tauni."-- Ibid., b. 9, sura ya 7. Aliitambua tabia halisi ya manabii wale waongo na kuiona hatari ambayo sasa ilitishia harakati ya kazi ile ya Ukweli. Upinzani wa papa na mfalme wa dola haukumsababishia mfadhaiko mkubwa na dhiki kama ile aliyoihisi sasa. Kutoka kwa wale marafiki waliojidai kujitoa kwa Matengenezo, waliibuka maadui wake wakuu zaidi. Kweli zile zile zilizokuwa zimemletea furaha kubwa na faraja, sasa zilitumiwa kuchochea malumbano na kusababisha machafuko kanisani. [[GC 187.4; PK Aya ya 10]

**Vita Kwa Ajili Ya Kuitetea Ile Kweli**

Katika kazi ya matengenezo ya kanisa, Luther alikuwa amesukumwa na Roho wa Mungu na alikuwa amebebwa na kupelekwa mbele zaidi ya uwezo wake mwenyewe au alivyofikiria inawezekana. Alikuwa hajanuia kuchukua misimamo kama ile aliyoifanya au kufanya mabadiliko makubwa sana. Lakini yeye alikuwa ni chombo tu mikononi mwa nguvu ya Yeye asiye na kikomo (Yule wa milele). Hata hivyo mara nyingi alitetemeka kuyaona matokeo ya kazi yake. Alikuwa amepata kusema: "kama ningejua kwamba fundisho langu limemjeruhi mtu mmoja, mtu mmoja tu, haidhuru awe mtu wa hali ya chini na asiyejulikana kwa kiasi gani,--jambo ambalo haliwezi kufanyika kwa kuwa ni injili yenyewe, ingelikuwa ni heri kwangu kufa mara kumi kuliko kuikana."- Ibid., b. 9, sura ya 7. [GC 188.1; PK Aya ya 11]

Na sasa mji wa Wittenberg wenyewe, kitovu chenyewe halisi cha Matengenezo ya kanisa, ulikuwa unaanguka kwa haraka chini ya nguvu ya misimano ya itikadi kali isiyotumia busara na maasi. Hali hii ya kutisha haikutokana na mafundisho ya Luther; lakini Ujerumani nzima maadui zake walikuwa wakimshutumu yeye kwa hali hii ya machafuko. Kwa uchungu mkubwa wa moyo, wakati mwingine aliuliza: "Je! Huu basi,unaweza kuwa ndiyo mwisho wa kazi hii kubwa ya Matengenezo?"-

Ibid., b. 9, sura ya 7. Kisha kadri alipoendelea kupigana mieleka na Mungu katika maombi yake, amani ilibubujika moyoni mwake. “Kazi si yangu, bali ni Yako Wewe Mwenyewe,” alisema; “Wewe hutairuhusu iharibiwe na ushirikina au ushabiki wa kidini usiotumia busara au kupitiliza.” Lakini wazo la kukaa kwa muda mrefu zaidi mbali na ule mgogoro katika kipindi hicho cha machafuko lilishindwa kuungwa mkono naye. Naye akakusudia kurejea Wittenberg. [GC 188.2; PK Aya ya 12]

Bila kuchelewa akaanza safari yake ya hatari. Alikuwa chini ya kizuizi cha himaya (marufuku). Maadui walikuwa na uhuru wa kuutoa uhai wake; marafiki zake walikatazwa kumsaidia au kumhifadhi. Serikali ile ya kifalme ilikuwa ikichukua hatua kali zaidi dhidi ya wafuasi wake. Lakini yeye aliona kazi ya injili ilikuwa hatarini na kwa Jina la Bwana aliondoka na kwenda vitani bila hofu yoyote ili kuipigania ile Kweli. [GC 188.3; PK Aya ya 13]

Katika barua aliyoiandika kwa Elekta, baada ya kuelezea kusudi lake la kuondoka Wartburg, Luther alisema: “Ninakujulisha mfalme mkuu, ya kuwa mimi ninakwenda Wittenberg chini ya ulinzi ulio wa hali ya juu sana kuliko ule wa wakuu na maelekta. Mimi sifikirii kuomba msaada toka kwako mheshimiwa na licha ya kutoona ulazima wa kupata ulinzi kutoka kwako, ni heri mimi nikulinde wewe. Kama ningejua kama wewe mheshimiwa unaweza kunilinda mimi, basi nisingeenda kabisa kule Wittenberg. Hakuna upanga wowote unaoweza kuiendeleza kazi hii mbele. Ni Mungu peke Yake anapaswa kufanya kila kitu, bila msaada au kuingia ubia na mwanadamu. Yeye aliye na imani kubwa kupita wote, ndiye aliye na uwezo mkubwa kuwalinda wengine. Ibid., b. 9, sura ya 8. [GC 188.4; PK Aya ya 14]

Katika barua yake ya pili, iliyoandikwa akiwa njiani kuelekea Wittenberg, Luther aliongezea kwa kusema: “Mimi niko tayari kukabiliwa na hasira yako Ee mkuu na hasira ya ulimwengu wote. Je! Wakazi wa Witternberg si kondoo wangu? Je! Mungu hakuwakabidhi katika utunzaji wangu? Je! Sipaswi mimi ikiwa ni lazima, kujianika kwenye hatari ya kifo kwa ajili yao? Zaidi ya hayo, ninaogopa kuona mlipuko mbaya wa ugonjwa katika nchi ya Ujerumani, ambao kwa huo Mungu ataliadhibu taifa letu.”- Ibid., b. 9, sura ya 7. [GC 189.1; PK Aya ya 15]

**Uwezo Wa Neno**

Kwa tahadhari kubwa na unyenyekevu, lakini kwa uamuzi sahihi na msimamo imara, akaingia kwenye kazi yake. “Kwa Neno,” alisema, “lazima tukiangushe na kukiharibu kile kilichosimamishwa kwa kutumia ukatili. Mimi sitatumia nguvu dhidi ya washirikina uongo na wale wasioamini.... Hakuna anayepaswa kulazimishwa. Uhuru ndio kiini hasa cha imani.”- Ibid., b. 9, sura ya 8. [GC 189.2; PK Aya ya 16]

Punde zilienea habari kwa mshindo kule Wittenberg, kuwa Luther alikuwa amerudi na angehubiri. Watu walimiminika kutoka pande zote na kanisa likajaa na kufurika. Alipanda kwenye mimbari, na kwa kutumia hekima na upole mwingi akafundisha, akashauri, akaonya na kukemea. Akigusia njia za baadhi waliokuwa wameanza kutumia njia za mabavu kukomesha misa, akisema: [GC 189.3; PK Aya ya 17]

"Misa ni jambo baya; Mungu anaipinga; inapaswa kukomeshwa; nami ningependa kwamba ulimwenguni pote ibadilishwe na badala yake kiweke chakula cha jioni cha injili au meza ya Bwana ya injili. Lakini hebu mtu yeyote asiachanishwe nayo nayo kwa nguvu. Lazima tuliache hili jambo mikononi mwa Mungu. Neno Lake sharti litende na siyo sisi. Na kwa nini iwe hivyo? Ninyi mtauliza. Kwa sababu sishikilii mioyo ya watu mikononi mwangu, kama vile mfinyanzi anavyoshikilia udongo. Tunayo haki ya kusema: hatuna haki ya kutenda. Wacha sisi tuhubiri; yaliyobaki mengine ni ya Mungu. Kama ningetumia nguvu, ningefaidika na nini? Kukunja uso kwa ndita za maumivu, kung'ang'ania desturi au urasmi, maigizo au mambo feki ya usanii, unafiki na kanuni za kibinadamu.... Lakini hakutakuwa na unyofu wa moyo ulio wa dhati, wala imani, wala upendo. Ambapo haya matatu yanapokosekana, yote hukosekana nami siwezi kutoa hata kijiti kimoja cha mti wa matunda ya mpea kupata matokeo kama hayo (sina haja ya kuhenyeka na kile kisicho na tija). Mungu hutenda zaidi kwa Neno Lake peke Yake kuliko wewe, na mimi na ulimwengu wote kwa kuunganisha nguvu zetu. Mungu anaushika moyo; na moyo unapochukuliwa Naye, basi ushindi wa vyote umepatikana... [GC 189.4; PK Aya ya 18]

"Mimi nitahubiri, nitajadili na kuandika; lakini sitamlazimisha mtu yeyote, kwa maana imani ni tendo la hiari. Tazameni nilichokifanya. Nilisimama dede dhidi ya upapa, vyeti vya msamaha wa dhambi vya kulipia na wafuasi wa upapa, lakini bila kuleta fujo au ghasia. Nililiweka mbele ya watu Neno la Mungu; Nikahubiri na kuandika, haya ndiyo yote niliyofanya mimi. Na bado wakati nilipokuwa nimesinzia,-- lile Neno ambalo nilikuwa nimehubiri likaushinda/likaupindua upapa, kiasi kwamba hakuna mkuu wala mfalme wa dola aliyelidhuru Neno vibaya. Na bado mimi sikufanya kitu chochote; Neno la Mungu peke yake lilifanya yote hayo. Ikiwa ningekuwa nimetaka kutumia nguvu, pengine nchi yote ya Ujerumani ingekuwa imefurika damu. Lakini matokeo yake yangekuwa ni nini? Maangamizi na ukiwa wa mwili pamoja na roho. Kwa hiyo mimi nilinyamaza kimya na kuliacha Neno kukimbia ulimwenguni kote lenyewe."-Ibid., b. 9, sura ya 8. [GC 190.1; PK Aya ya 19]

Siku baada ya siku, kwa wiki nzima, Luther aliendelea kuhubiria makundi yenye shauku. Neno la Mungu likazivunja hirizi za mihemko ya ushabiki wa kidini usio na busara. Nguvu ya injili kawarudisha watu waliokuwa wamepotoshwa katika njia ile ya Kweli. [GC 190.2; PK Aya ya 20]

Luther hakuwa na hamu ya kukutana na mashabiki wale waliopitiliza kwa kutotumia busara na ambao njia waliyoitumia ilikuwa imezalisha maovu makubwa sana. Aliwajua kuwa ni watu waliopungukiwa na maamuzi ya busara na wenye mihemko isiyo na nidhamu, nao, walipokuwa wakidai kuangaziwa na nuru maalumu kutoka mbinguni, hawakuweza kustahimili changamoto hata kidogo za kukanushwa au karipio au ushauri mzuri. Wakiwa wamejitwalia bila haki mamlaka makubwa, walimtaka kila mtu kukubali madai yao bila maswali yoyote. Lakini, walipotaka mahojiano naye, alikubali kukutana nao; naye akafanikiwa sana kuzifichua hila zao, hata wanafiki (watu feki) wale wakaondoka Wittenberg mara moja. [GC 190.3; PK Aya ya 21]

**Waalimu Washupavu Wa Dini Walidharau Neno**

Ushupavu wa kidini usiotumia akili ulisitishwa kwa muda; lakini miaka kadhaa baadaye ulilipuka tena ukiwa na ukatili mwingi zaidi na matokeo ya kutisha zaidi. Luther alisema, kuhusu viongozi wa harakati hii: "Kwao Maandiko Matakatifu yalikuwa barua iliyokufa tu, yaani isiyo na uwezo na wote walianza kupiga kelele kwa kugumia, 'Roho! Roho!' Lakini hakika mimi sitafuata kule anakowaongoza huyo roho wao. Mungu kwa rehema Zake na anitunze mimi katika kanisa ambalo hakuna watu wa aina nyingine isipokuwa watakatifu tu. Mimi natamani kukaa pamoja na wanyenyekevu, walio dhaifu, wagonjwa, wanaozijua na kuzihisi dhambi zao na ambao mioyo yao inaugua na kumlilia Mungu daima kutoka ndani kabisa ya mioyo yao kwa dhati ili kupata faraja na msaada Wake."- Ibid., b. 10, sura ya 10. [GC 190.4; PK Aya ya 22]

Thomas Munzer shabiki mwenye bidii zaidi miongoni mwa wale wenye itikadi kali za dini zilizopitiliza, alikuwa mtu mwenye uwezo mkubwa, ambao kama ungeelekezwa kwa usahihi, ungemwezesha kufanya mema; lakini yeye hakuwa amejifunza kanuni za kwanza za dini ya Kweli. "Alikuwa na tamaa ya kuufanyia ulimwengu matengenezo au kuugeuza ulimwengu, na kisha akasahau kama wote wenye itikadi kali za kidini zilizopitiliza wanavyofanya, kwamba matengenezo yalipaswa kuanzia kwake mwenyewe.", Ibid., b. 9, sura ya 8. Alikuwa na tamaa ya kupata cheo na umaarufu na hakuwa tayari kuwa namba mbili, hata kwa Luther. Alitangaza kwamba kwa Wanamatengenezo kuyapatia mamlaka Maandiko Matakatifu badala ya yale ya papa, walikuwa wakianzisha tu mfumo mwingine tofauti wa upapa. Yeye mwenyewe, alidai, kuwa ametumwa" na Mungu kuanzisha matengenezo ya Kweli. " Yule anayemiliki roho hii," alisema Munzer, "anayo imani ya Kweli, hata kama asingeweza kamwe kuyaona hayo Maandiko Matakatifu katika maisha yake yote."- Ibid., b. 10, sura ya 10. [GC 191.1; PK Aya ya 23]

Walimu wa ushabiki wa kidini usiotumia busara walijiachia kutawaliwa na hisia zao, kwa kuchukua kila wazo na msukumo wa moyoni kuwa ndiyo sauti ya

Mungu; mwishowe wakafika mahali pa kupitiliza na kuvuka mipaka sana. Wengine hata walidiriki kuchoma moto Bibilia zao wakipaza sauti zao na kusema: "Andiko huua, bali Roho huhuisha." (2 Kor 3:6) Mafundisho ya Munzer yalivuta shauku ya kuona maajabu na kuamsha kiburi chao kwa kuweka maoni na mawazo yao ya kibinadamu juu ya Neno la Mungu. Mafundisho yake ya kidini yalipokelewa na maelfu. Haikupita muda naye akanza kukemea utaratibu wa aina yoyote uliotumika katika ibada ya hadhara na alitangaza kuwa kutii wakuu na watawala wa serikali kulikuwa ni kujaribu kumtumikia Mungu na Beliali (Shetani) kwa wakati mmoja. [GC 191.2; PK Aya ya 24].

Akili na mioyo ya watu vikiwa tayari kuanza kulivua kongwa la upapa, zikawa pia zinakosa uvumilivu wa kuwa chini ya makatazo ya mamlaka ya serikali ya kiraia. Mafundisho ya kimapinduzi ya Munzer, yakidai kwamba yana idhini ya Mungu, yaliwaongoza watu wajitenge na mamlaka yote na kujiachilia kufanya mambo yale waliyopenda kwa hamasa na tamaa zao za mwili. Mandhari za kutisha za uchochezi wa maasi dhidi ya serikali pamoja na ugomvi wenye chuki yalifuata na viwanja vya Ujerumani vikaloweshwa na damu. [GC 191.3; PK Aya ya 25]

### Luther Apata Uchungu Kutokana Na Mambo Yalivyogeuka

Uchungu mkubwa wa moyo ambao Luther aliwahi kuupata huko Erfurt kwa muda mrefu sasa ukawa umemlemea kwa nguvu maradufu alipoyaona matokeo ya shutuma za wale wenye itikadi za kidini wakisababisha mashataka dhidi ya Matengenezo. Viongozi wa upapa wakatangaza—na wengi walikuwa tayari kuuunga mkono matamko yao-- kwamba maasi yale yalikuwa tunda dhahiri na halali la mafundisho ya Luther. Ijapokuwa shitaka hili halikuwa na msingi wowote kabisa, bado liliweza kumsababishia dhiki kubwa tu yule Mwanamatengenezo. Kwamba kazi ya Ukweli ilifedheheshwa vile kwa kuwekwa kwenye kikapu kimoja na ushabiki ule wa kidini usiotumia busara na uliokuwa mbaya kabisa, lilionekana kuwa ni jambo lililozidi uwezo wake kustahimili. Kwa upande mwingine, viongozi wa maasi walimchukia Luther kwa sababu hakuwa tu anayapinga mafundisho yao na kuyakataa madai yao ya kuwa na uvuvio kutoka kwa Mungu, bali pia aliwaita kuwa ni waasi dhidi ya serikali ya kiraia. Kwa kulipiza kisasi wakamshutumu kuwa alikuwa mwigizaji mkuu wa uovu. Ilionekana kana kwamba alikuwa amejitengenezea uadui mwenyewe upande wa wakuu wa nchi, pamoja na wananchi wa kawaida. [GC 192.1; PK Aya ya 26]

Warumi walishangilia, wakitarajia kushuhudia anguko la haraka la Matengenezo ya kanisa; na walimlaumu Luther hata kwa yale makosa ambayo alikuwa akijitahidi sana kuyasahihisha. Kundi lile la ushabiki wa kidini usio na busara, kwa kutoa madai yao ya uongo kuwa walikuwa wamefanyiwa dhuluma kubwa, walifanikiwa kupata huruma za kundi kubwa la watu na kama ilivyo mara

nyingi, kwa wale ambao wanasimama upande usiofaa wenye makosa, walikuja kuonekana kana kwamba wao ndiyo wafia dini. Kwa hivyo wale ambao walikuwa wakijitahidi kwa nguvu zote kupingana na Matengenezo walihurumiwa na kupongezwa kwamba wao ndio walikuwa wahanga wa ukatili na uonevu. Hii ilikuwa ni kazi ya Shetani, akichochewa na roho ile ile ya uasi ambayo iliyoonyeshwa kwanza kule mbinguni. [GC 192.2; PK Aya ya 27]

**Hiyo Ni Kazi Ya Shetani**

Daima Shetani hutafuta kila namna ya kuwadanganya watu na kuwaongoza kuiita dhambi ndiyo haki na haki ndiyo dhambi. Kazi yake imefanikiwa kwa jinsi ya ajabu sana! Ni mara ngapi watumishi waaminifu wa Mungu wamekosolewa na kuaibishwa kwa sababu wao wanasimama bila hofu kuitetea ile Kweli! Watu ambao ni mawakala wa Shetani kiuhalisia ndiyo hutukuzwa na kusifiwa na hata kutazamwa kama wao ndiyo wafia dini, wakati wale ambao wangestahili kuheshimiwa na kusaidiwa kudumisha uaminifu wao kwa Mungu, wanaachwa kusimama peke yao, wakishukiwa vibaya na kutoaminiwa. [GC 192.3; PK Aya ya 28]

Utakatifu bandia, utakaso wa uongo/feki, bado unafanya kazi yake ya udanganyifu. Kwa maumbo au mifumo mbalimbali unadhihirisha roho ile ile kama siku za Luther, ukiondoa akili za watu kutoka kwenye Maandiko na kuwaongoza watu kufuata hisia zao na maoni yao wenyewe badala ya kusalimisha utii wao kwa Sheria ya Mungu. Hii ni mojawapo ya mbinu iliyofanikiwa zaidi ya Shetani, kuaibisha Ukweli na usafi wa maisha. [GC 193.1; PK Aya ya 29]

Bila hofu Luther aliitetea injili dhidi ya mashambulizi ambayo yalikuja kutoka kila sehemu. Neno la Mungu lilijidhihirisha lenyewe kuwa ndiyo silaha yenye nguvu katika kila mgogoro uliotokea. Akiwa na Neno hilo alipigana dhidi ya mamlaka aliyoipora papa isivyo halali na dhidi ya falsafa za urazimu ya wakufunzi wa vyuo vikuu (rationalistic philosophy) wakati akisimama imara kama mwamba dhidi ya itikadi kali za kidini ambazo zilifanya mambo kwa kupitiliza na ambazo wafuasi wake sasa walitafuta kujifungamanisha na Matengenezo ya kanisa. [GC 193.2; PK Aya ya 30]

Kila moja ya kundi lililoleta upinzani lilikuwa likiyaweka kando Maandiko Matakatifu kwa namna yake na kuinua hekima ya kibinadamu kama chanzo cha Ukweli na maarifa ya kidini. Nadharia ya urazini huiabudu fikra kama ndiyo mungu na kuifanya iwe kigezo/kipimo cha dini. Uroma ukidai kwa ajili ya kiongozi wao mkuu uvuvio ulioshuka chini katika mstari usiokatika toka kwa mitume kuja kwao, ambao nyakati zote haubadiliki, unatoa fursa ya kutosha kwa kila aina ya ubadhirifu na ufisadi/uhalifu kufichwa chini ya utakatifu wa mitume. Uvuvio uliodaiwa na Munzer na wenzake haukutoka kwenye chanzo chochote cha juu zaidi ya dhana ya kufikirika na nguvu yake ikachochea maasi dhidi ya

mamlaka zote, zile za kibinadamu au ya Mungu. Ukristo wa Kweli hulipokea Neno la Mungu kama nyumba kuu ya hazina, Ukweli uliovuviwa na kipimo cha uvuvio wote. [GC 193.3; PK Aya ya 31]

Baada ya kurejea kutoka Wartburg, Luther alimaliza tafsiri yake ya Agano Jipya na muda mfupi tu baada ya hapo injili ile ilitolewa kwa watu wa Ujerumani kwa lugha yao wenyewe. Tafsiri hiyo ilipokelewa kwa shangwe kuu na wote waliopenda Ukweli; lakini ilikataliwa kwa dharau na wale waliochagua kufuata mapokeo na maagizo ya wanadamu. [GC 193.4; PK Aya ya 32]

Makasisi waliingiwa na hofu kwa dhana kwamba sasa watu wa kawaida wangeweza kujadiliana nao juu ya maagizo na kanuni za Neno la Mungu na kwamba ujinga waliokuwa nao wenyewe ungeweza kufichuliwa (kutojua Maandiko). Silaha za mawazo yao ya kimwili zilikuwa hazina nguvu dhidi ya ule upanga wa Roho. Rumi ikatumia mamlaka yake yote kuzuia usambazaji wa Maandiko; lakini amri, vitisho, laana, na mateso yake vilikuwa kazi bure. Kadiri ilivyoilaani na kuipiga marufuku Biblia, ndivyo shauku ya watu ilivyokuwa kubwa zaidi kutaka kujua ni nini hasa Biblia ilifundisha. Wale wote ambao waliweza kusoma walikuwa na hamu ya kujifunza Neno la Mungu wenyewe. Waliibeba kila mahali walipokwenda na waliisoma na kuisoma tena na hawakuweza kuridhika mpaka walipoweka sehemu yake kubwa kwenye kumbukumbu zao- walikariri. Alipoona jinsi Agano Jipya lilivyopokelewa na kupendwa, mara moja Luther alianza kulitafsiri Agano la Kale na kuchapa sehemu ndogo ndogo kwa haraka kwa kadri alivyokamilisha kutafsiri sehemu zile. [GC 194.1; PK Aya ya 33]

Maandishi ya Luther yalikaribishwa kwa shauku ile ile mjini na vijijini. “Kilichoandaliwa na Luther na marafiki zake, wengine walisambaza. Watawa, wakiwa wameshawishiwa juu ya uharamu wa maisha ya kitawa, walitamani kubadilisha maisha yaliyojawa na uvivu kwa muda mrefu ili waishi maisha ya kutoa jasho kwa bidii ya kazi, lakini walikuwa na ujinga wa kulihubiri Neno la Mungu, walisafiri kwa kupita majimbo mbalimbali, wakitembelea vijiji na nyumba ndogo za kule mashambani wakiuza vitabu vya Luther na marafiki zake. Punde Ujerumani nzima ilifurika na hawa wainjilisti wa vitabu jasiri.” - Ibid., b. 9, sura ya 11. [GC 194.2; PK Aya ya 34]

**Matokeo Ya Kusoma Maandiko**

Maandishi haya yalisomwa na kuchunguzwa kwa hamu kubwa sana na matajiri na maskini, wenye elimu kubwa ya shuleni na wale ambao hawakwenda shule. Usiku walimu wa shule za vijijini walivisomea vikundi vidogo vilivyokusanyika kando ya moto majumbani kwa sauti ya juu. Kwa kila juhudi iliyofanywa roho zingine ziliamini Ukweli na baada ya kulipokea Neno kwa furaha, ikawa zamu yao pia kuwaambia wengine habari zile njema. [GC 194.3; PK Aya ya 35]

Maneno yale ya Uvuvio yakawa yamethibithishwa: “Kufafanusha Maneno Yako kwatia nuru, na kumfahamisha mjinga.” Zaburi 119: 130. Kujifunza Maandiko Matakatifu kukaleta mabadiliko makubwa katika akili na mioyo ya watu. Utawala wa kipapa ulikuwa umewawekea raia wake nira nzito ya chuma ambayo iliwafunga kwenye ujinga na kuwafanya washuke chini kimaisha. Uzingatiaji wa taratibu za kishirikina ulikuwa umesimamiwa kwa uangalifu sana; lakini katika ibada yao ile yote moyo na akili vilikuwa na sehemu ndogo sana ya kufanya. Mahubiri ya Luther, yaliyowasilisha wazi Kweli za Neno la Mungu na kisha Neno lenyewe, lililowekwa mikononi mwa watu wa kawaida, lilikuwa limeamsha nguvu zao za akili zilizokuwa zimelala, siyo tu kwa madhumuni ya kuutakasa na kuuboresha mwenendo wao wa kiroho, bali pia kuleta nguvu mpya na uhai kwenye akili yao. [GC 195.1; PK Aya ya 36]

Watu wa matabaka yote walionekana wakiwa na Biblia  mikononi mwao, wakilinda na kuyatetea mafundisho ya Matengenezo. Wafuasi wa upapa (walei) ambao walikuwa wamewaachia mapadri na watawa kujifunza Maandiko Matakatifu, sasa waliwataka waje na kuyakanusha haya mafundisho mapya. Lakini, wao kwa kutoyajua yale Maandiko Matakatifu na uweza wa Mungu, viongozi wa upapa walishindwa kabisa na wale ambao walikuwa wamewashutumu kuwa wajinga na wazushi. Mwandishi mmoja Mkatoliki alisema: “kwa masikitiko,” “Luther alikuwa ameshawishi wafuasi wake wasiamini kanuni yoyote zaidi ya Maandiko Matakatifu.” D'Aubigne, b. 9, sura ya 11. Makundi ya watu yalikusanyika ili kusikia Ukweli uliotetewa na watu wenye elimu ndogo na hata walipojadiliana na wanatheolojia  hodari na wenye ufasaha. Ujinga wa kuabisha wa watu hawa wakuu ulidhihirishwa wakati hoja zao zilipojibiwa na mafundisho sahili ya Neno la Mungu. Vibarua, wanajeshi, wanawake na hata watoto, waliyajua  mafundisho ya Biblia vizuri zaidi kuliko mapadri na madaktari wazamivu wa theolojia. [GC 195.2; PK Aya ya 37]

Tofauti iliyokuwapo kati ya wanafunzi wale wa injili na watetezi wa ushirikina wa kipapa haikuonekana kupungua katika safu za wasomi wa Biblia na miongoni mwa watu wa kawaida. “Tofauti na mabingwa wa zamani wa upapa, viongozi wa hierakia, ambao walikuwa wamepuuzia kujifunza lugha na kukuza uelewa kwenye fani ya fasihi, walikuwepo vijana wema na wenye nidhamu, waliojitolea kujifunza kwa umakini, wakichunguza Maandiko na kujishugulisha na kazi za maandishi ya kale ya watu mashuhuri (antiquity). Wakiwa na akili ya utendaji, roho iliyoadilishwa na kuinuliwa na mioyo ya ujasiri, kwa muda mfupi vijana hawa walikuwa wamejipatia maarifa ambayo kwa muda mrefu hapakuwa na watu walioweza kushindana nao.... na hapo ndipo hawa watetezi vijana wa Matengenezo walipokutana na madaktari wa falsafa wa Kiroma katika kusanyiko lolote, waliwashambulia kwa urahisi na kwa ujasiri kiasi kwamba hawa wasiojua

Maandiko walisita, walibabaika, waliudhika, na waliaibishwa na kudharaulika mbele ya watazamaji wote.” Ibid., b. 9, sura ya 11. [GC 195.3; PK Aya ya 38]

Mapadri wa Kiroma walipoona makutano yao yakipungua, waliomba msaada wa mahakimu na kwa kila njia kwa nguvu zao walijitahidi kuwarudisha wasikilizaji wao. Lakini watu walikuwa wamepata katika mafundisho mapya, kile ambacho ndicho kilikidhi mahitaji ya roho zao na waliachana na wale ambao kwa muda mrefu waliwalisha pumba zisizofaa za taratibu za ibada zenye ushirikina na mapokeo ya wanadamu. [GC 196.1; PK Aya ya 39]

Ikawa kazi bure kabisa kuwaomba viongozi wa kanisa na serikali kukomesha mbali ‘uzushi’ ule. Bila mafanikio walitumia vifungo magerezani, mateso, kuchomwa moto na upanga. Maelfu ya waumini waliigonga muhuri imani yao kwa damu yao na bado hata hivyo kazi iliendelea mbele. Mateso yalitumika tu kama kichocheo cha kuenea Ukweli, na unafiki wa kidini ambao Shetani alijitahidi kujiunga nao uliishia katika kufafanua kwa udhahiri zaidi, tofauti kati ya kazi ya Shetani na kazi ya Mungu. [GC 196.3; PK Aya ya 40]

# SURA YA 11

# UPINZANI WA WAKUU WABADILI MWELEKEO

## (Wakuu Wa Nchi Wapinga Feb 1529 - Jun 1530)

Ufupisho: Upinzani wa wakuu wa Ujerumani waliokuwa Wakristo mwaka 1529. Wengi Ulaya walijiweka pamoja ili kupinga Uprotestanti, lakini Mashujaa hawa wa Kikristo walisimama imara. Upinzani au kupinga kwao katika Baraza la Spires kumetupa sisi jina la Uprotestanti. Hapa utajifunza kuhusu mababa wa Uprotestanti, na urithi waliouacha duniani. Luther alikuwa na miaka 47 sasa, na Alipokufa Elekta Frederick, kakaye John alimlinda Luther kwa neema za Mungu.

Mojawapo ya shuhuda bora na za kujivunia kabisa zilizowahi kutolewa katika kuyaunga mkono Matengenezo ulikuwa ni ule wa upinzani ('Protest') uliotolewa na watawala Wakristo wa nchi ya Ujerumani katika Baraza lililofanyika kule Spires mwaka 1529. Ujasiri, imani, na uimara wa wale watu wa Mungu ulivipatia vizazi vilivyofuata uhuru wa fikra na dhamiri. Kupinga huko (protesting) ndiko kulikoliletea kanisa la Matengenezo jina la Protestanti; kanuni zake ndizo zilianzisha "msingi halisi wa Uprotestanti." - D'Aubigne, b. 13, sura ya 6. [GC 197.1; PK Aya ya 1]

Siku ya giza na ya kuogofya ilikuwa imefika kwa Matengenezo ya Kanisa. Licha ya lile 'tamko la hukumu' lilitolewa pale Worms, lililomtangaza Luther kuwa ni haramia na kuyapiga marufuku mafundisho yake ya dini na kuwapiga marufuku watu kuyaamini, mpaka wakati huu uvumilivu wa mafundisho ya dini ulikuwa unaendelea kuwepo bado kwenye dola. Majaliwa Yake Mungu yalikuwa yameyazuia majeshi yaliyopinga Ukweli. Charles wa V ameazimia kuwa upande wa kuyasagasaga Matengenezo, lakini mara nyingi aliponyanyua mkono wake juu ili kuupa kipigo kikali na kuyafanya yakome, alilazimishwa kugeuza pigo lake pembeni. Tena na tena maangamizi ya mara moja ya wale wote waliodiriki kuipinga Roma yalionekana kuwa yalikuwa karibu sana kufanikiwa; lakini dakika chache kabla ya utekelezaji wake, majeshi ya Waturuki yalitokea kwenye mpaka wa upande wa mashariki, au mfalme wa Ufaransa, au hata papa mwenyewe, kwasababu ya wivu wa ukuu wa mfalme wa dola uliokuwa unazidi kuongezeka, walifanya vita dhidi yake; na hivyo katikati ya migogoro na machafuko ya mataifa, Matengenezo ya Kanisa yalikuwa yameachwa kuimarika na kuenea. [GC 197.2; PK Aya ya 2]

Hatimaye, hata hivyo, mamlaka ya upapa ilikomesha uhasama na magomvi kati yao, ili wapate kushikana pamoja na kupambana na Wanamatengenezo kwa nguvu kubwa zaidi. Baraza la mji wa Spires la kwanza, lililokuwa mwaka 1526 liliwapa kila jimbo uhuru kamili katika masuala ya kidini mpaka mkutano wake mkuu unaojumuisha wote, yaani Baraza Kuu. Lakini haukupita muda baada ya

hatari zilizosababisha kuidhinisha uhuru na upatanisho huo, mfalme akaita baraza la pili kukusanyika huko Spiers mnamo 1529 kwa kusudi la kukomesha uzushi. Wakuu wa majimbo walipaswa kushawishiwa kwa njia ya amani ikiwa ingewezekana, ili wapate kusimama kinyume cha Matengenezo; lakini ikiwa njia hizi zingeshindwa, basi Charles alikuwa tayari kutumia upanga. [GC 197.3; PK Aya ya 3]

Wafuasi wa upapa walishangilia sana. Wakajitokeza kule Spiers kwa idadi kubwa, nao wakadhihirisha waziwazi chuki na uadui wao dhidi ya Wanamatengenezo na wale wote waliowaunga mkono. Melanchthon alitamka ya kwamba: “Sisi ni kama laana na takataka za ulimwengu huu; lakini Kristo atawaangalia watu Wake wahitaji na wanyenyekevu, na kuwahifadhi.” - Ibid., b. 13, sura ya 5. Wakuu wa nchi na wana wa wafalme ambao walikuwa wafuasi wa injili (evangelicals princes) ambao walihudhuria katika Baraza lile walikatazwa kuruhusu injili kuhubiriwa hata katika maskani yao wenyewe. Lakini watu wale wa Spires walikuwa na kiu ya Neno la Mungu, na licha ya kupigwa marufuku injili, maelfu walimiminika kwenda kwenye ibada iliyoendeshwa katika kanisa dogo (chapel) la yule Elekta wa Saxony. [GC 198.1; PK Aya ya 4]

Jambo hili liliharakisha hali ya hatari kuwasili. Ujumbe wa kifalme ulilitangazia Baraza lile kwamba kwa kuwa azimio lililotoa uhuru wa dhamiri lilikuwa limeleta machafuko makubwa na kutofuata utaratibu, mfalme wa dola alitaka libatilishwe. Kitendo kile cha kidikteta kiliamsha hasira, hofu na tahadhari kwa Wakristo waaminio injili. Mmoja wao alisema: “Kristo ameangukia tena mikononi mwa Kayafa na Pilato.” Wafuasi wa Roma walianza tena ukatili. Mfuasi wa upapa mwenye itikadi kali alitangaza, akisema, “Waturuki ni bora kuliko Walutheri; kwa maana Waturuki wanaadhimisha siku za swaumu/mfungo, na Walutheri wanazivunja. Endapo tutalazimika kuchagua Maandiko Matakatifu ya Mungu na mafundisho ya uongo ya zamani ya kanisa, sisi tunapaswa kuyaacha Maandiko Matakatifu.” Melanchthon akasema: “Kila siku, mkutano unapokuwa umejaa watu, Faber amekuwa akitutupia sisi wanainjili jiwe jipya” (wahubiri wa injili).” --Ibid., b. 13, sura ya 5. [GC 198.2; PK Aya ya 5]

Uvumilivu wa kidini kwa imani ya wengine ulipitishwa kisheria, na majimbo yale yaliyoamini injili yakaazimu kupinga ukiukwaji wa haki zao. Luther, akiwa angali bado chini ya kizuizi au katazo lililotamkwa kule Worms, hakuruhusiwa kuhudhuria pale Spiers; lakini mahali pake pakajazwa na watendakazi wenzake na wakuu wa nchi ambao Mungu alikuwa amewainua kuitetea kazi yake katika nyakati ile ya dharura na hatari. Mheshimiwa Frederick wa Saxony, mlinzi wa awali wa Luther, alikuwa ameondolewa kwa kifo; lakini mwana wa mfalme, Duke John, kaka na mrithi wake, alikuwa ameyakaribisha Matengenezo ya Kanisa kwa furaha, na yeye akiwa rafiki mpenda amani, alionyesha juhudi kubwa na ujasiri

mwingi katika maslahi yote yaliyohusiana na maslahi ya imani. [GC 198.3; PK Aya ya 6]

**Kukabiliwa Na Hatari Kubwa Kule Spiers**

Makasisi wakadai kwamba majimbo yale yaliyokuwa yamekubali Matengenezo ya Kanisa yajisalimishe bila maswali kwa utawala wa Roma. Wanamatengenezo, kwa upande mwingine, walidai waendelee kupewa uhuru uliokuwa umetolewa awali. Hawakuweza kukubali kuwa Roma iyatawale tena majimbo yale yaliyokuwa yamelipokea Neno la Mungu kwa furaha nyingi mno. [GC 199.1; PK Aya ya 7]

**Upinzani Wa Viongozi**

Kama njia ya kufikia maridhiano au mwafaka mwishowe ikapendekezwa kwamba mahali pale ambapo Matengenezo ya Kanisa yalikuwa hayajaanzishwa, Tamko lile la hukumu la Worms litekelezwe kikamilifu na kwa umakini sana; na ya kwamba "katika maeneo ambako watu walikuwa wameacha kulifuata tamko hilo la hukumu, na kule ambako watu wasingeweza kuliheshimu bila hatari ya maasi, basi angalau watu wasiingize matengenezo yoyote mengine mapya, wasiguse vipengele vyovyote vinavyobishaniwa, wasipinge uadhimishaji wa sherehe ya Misa, na wasimruhusu mfuasi Mromani Katoliki awaye yote kupokea imani ya Ulutheri." -Ibid., b. 13, sura ya 5. Kigezo hicho cha sheria kilichopendekezwa kilipitishwa na Baraza, na kuwaridhisha mno makasisi na maaskofu wa upapa. [GC 199.2; PK Aya ya 8]

Ikiwa amri hii ingetekelezwa, basi, "Matengenezo ya Kanisa yasingeweza kuenezwa mbali……mahali kule ambako yalikuwa bado hayajulikani, wala yasingeweza kuijengwa juu ya misingi imara ... pale ambapo tayari yalikuwepo." - Ibid., b. 13, sura ya 5. Uhuru wa kusema ungekuwa umepigwa marufuku. Wongofu wa roho mpya wa aina yoyote ile usingeruhusiwa. Na marafiki wa Matengenezo ya Kanisa walitakiwa kutii masharti na makatazo haya mara moja. Matumaini ya ulimwengu yalionekana kana kwamba yalikuwa karibu sana kuzimwa. "Kurudishwa tena kwa utawala wa upapa wa ngazi uitwao hierakia…… kungerejesha bila kukosea maovu na mateso ya zamani;" na fursa ingeweza kupatikana kwa urahisi ya "kukamilisha uharibifu wa kazi ile ambayo tayari ilikuwa imetikiswa vibaya" na hali ya uwepo wa itikadi kali za kidini zisizotumia busara pamoja na mifarakano. -Ibid., b. 13, sura ya 5. [GC 199.3; PK Aya ya 9]

**Mambo Makuu Yako Hatarini**

Wakati Kundi la wafuasi wa injili lilipokutana kwa ajili ya kushauriana, kila mmoja alimwangalia mwenzake katika hali ya kuduwaa na mfadhaiko bila kutamka neno lolote. Swali likapita kutoka kwa mmoja na kwenda kwa mwingine: "Jambo gani lifanyike?" Masuala mazito ya ulimwengu mzima

yalikuwa hatarini. “Je! viongozi wa Matengenezo ya Kanisa sasa wajisalimishe na kukubali kupokea tamko la hukumu hiyo? Ni rahisi kiasi gani, wakati huu wa hatari, ambayo kusema kweli ilikuwa kubwa sana, kujenga hoja itakayowapeleka katika njia isiyo sahihi! Ni visingizio vingapi vyenye mashiko vilivyoweza kutolewa na sababu nzuri zenye haki na zilizokubalika ambazo wangeweza kuzitoa ili wajisalimishe. Viongozi wa Kilutheri walipewa uhakikisho wa nchi wa uhuru wa kuendelea na dini yao. Upendeleo wa baraka ile ile ulitolewa kwa wote waliokuwa raia zao, ambao kabla ya kupitishwa kwa sheria ile iliyokuwa imependekezwa, walikuwa wameamini mtazamo wa Kimatengenezo. Je! Jambo hili halitoshi kuwafanya waridhike? Ni hatari ngapi ambazo wangejiepusha nazo kwa kujisalimisha! Ni hatari ngapi na migogoro ambayo upinzani wao ungeweza kusababisha? Ni nani ajuaye ni fursa gani nzuri ambazo siku za baadaye wangeweza kuzipata? Hebu tukumbatie amani na tulinyakue kwa ari jani la mzeituni* ambalo Roma inanyosha mkono wake kutupa sisi, na kuyafunga majeraha ya nchi hii ya Ujerumani; Kwa hoja kama hizi, wanamatengenezo wangeweza kuhalalisha njia ambayo kwa hakika ingeiangamiza kazi yao katika muda usiokuwa mrefu *(Jani la mzeituni ni nembo ya amani na matumaini kama katika Safina -Mwanzo 8:11). [GC 199.4; PK Aya ya 10]

“Kwa furaha, waliichunguza kanuni ambayo kwayo msingi wa mwafaka/maridhiano ulikuwa umejengwa juu yake, nao walitenda kwa imani. Je, kanuni hiyo ilikuwa ni ipi? Ilikuwa ni haki ya Roma kutumia nguvu katika kuilazimisha dhamiri ya mtu (yaani, kumkataza mtu kumwabudu Mungu kama apendavyo mwenyewe) na kumkataza mtu kuweza kuuliza maswali kwa uhuru. (kuchunguza au kuuliza yale yahusianayo na imani). Lakini, je! Haikuwa haki yao wenyewe pamoja na raia zao Waprotestanti kuwa na uhuru wa kufurahia dini yao? Ndiyo, walikuwa nao uhuru, kama fadhila maalum iliyotamkwa haswa katika mpango huu, na wala sio kama haki yao. Lakini kwa wale wote waliokuwa nje ya mwafaka ule, kanuni hiyo kuu ya mamlaka ilikuwa itawale; dhamiri ya mtu ilikuwa nje ya uwezo wa mahakama. Roma ndiye alikuwa jaji asiyeweza kukosea hata kidogo, tena ilikuwa ni sharti atiiwe. Kuukubali mwafaka ule uliopendekezwa ingelikuwa ni kukubali kwa dhahiri kabisa kwamba uhuru wao wa dini ungepaswa kuwa ndani tu ya mipaka ya jimbo lile la Saxony lililopokea imani ile ya Matengenezo; na kuhusu mahali ambapo Matengenezo yalikuwa yamekubaliwa na wengine katika ulimwengu wa Kikristo uliosalia)* huko, uhuru wa mtu kuuliza habari yoyote katika kujifunza hii imani na kuingia katika imani hiyo ya Matengenezo ingekuwa ni uhalifu mkubwa wa jinai, na lazima mtu huyo angepatilizwa kwa kufungwa katika gereza la chini ya ardhi, na kuunguzwa kwa moto kwa kufungwa kwenye mti wa kuchomea watu. Je! Waridhike na kuruhusu uhuru wa dhamiri uwe katika eneo moja tu? (Saxony). Yaani sasa itangazwe kwamba imani ya Matengenezo ya Kanisa ilikuwa imejipatia mwongofu wake wa mwisho? Kwamba yalikuwa yamejipatia ekari yake ya mwisho ya utawala?

(yashindwe kusonga mbele yakiwa katika ekari yake ya mwisho yaani Saxony tu?) Na ya kwamba popote pale ambapo Rumi ilikuwa inatawala katika wakati ule, basi ufalme wake uendelee kubaki hivyo milele zote? Je! wale Wanamatengenezo wangeweza kujitetea kwa watu na kuwafanya wawasadiki kwamba wao hawakuwa na hatia ya damu ya mamia na maelfu ambao kwa kutekelezwa kwa mwafaka huo, wangelazimika kuyatoa maisha yao mhanga katika nchi za upapa? Kufanya jambo hili katika saa hii muhimu na nyeti, ingelikuwa kusaliti kazi ya injili pamoja na uhuru wa Ulimwengu wote wa Kikristo." - Wylie, b. 9, sura ya 15. Mwishowe waliona ingelikuwa ni heri kwao "kutoa kafara kila kitu, hata yale majimbo yao, taji zao, pamoja na maisha yao." – D'Aubgne, b, 13, ch 5. [GC 200.1; PK Aya ya 11]

"Hebu sisi na tuikatae amri hii," walisema wakuu wale wa majimbo ya nchi ya Ujerumani. "Katika mambo yale yanayohusu dhamiri* ya mtu kanuni ya wengi wape haina uwezo wowote." Manaibu wale walitangaza, wakisema: "Ni amri ya mwaka 1526, ndiyo ambayo imetuwezesha sisi kufurahia amani katika dola hii: basi, kule kuifutilia mbali kungeweza kuijaza nchi nzima ya Ujerumani na taabu na migawanyiko. Baraza hili la sheria (Diet) halina uwezo wowote kabisa wa kufanya zaidi ya kuhifadhi uhuru wa dini mpaka hapo Baraza kuu litakapokutana." -Ibid., b. 13, sura ya 5. Kuulinda uhuru wa dhamiri ya mtu ndio wajibu wa dola, na huo ndio mpaka wa mamlaka yake katika masuala ya dini. Kila serikali yoyote ya kidunia inayojaribu kurekebisha, kutunga, kutekeleza au kulazimisha maadhimisho fulani ya kidini kwa kutumia mamlaka ya kiraia, inaiua kanuni ile ile haswa ambayo Mkristo Mwinjilisti (mwenezaji wa Injili) ameipambania kwa heshima na gharama kubwa.*(uamuzi wa mtu wa kuchagua kumwabudu Mungu kama apendavyo mwenyewe) [GC 201.1; PK Aya ya 12]

**Upinzani Wa Wakuu**

Wafuasi wa papa walidhamiria kuangusha kile walichokiita "ukaidi usio na hofu." Wakaanza kwa kujaribu kuongeza jitihada ili kuleta migawanyiko miongoni mwa wale waliounga mkono Matengenezo ya Kanisa na kuwatisha mno wale wote waliokuwa hawajatangaza waziwazi upendo wao kwa Matengenezo. Wawakilishi wa miji iliyo huru mwishowe waliitwa mbele ya Baraza Kuu na kutakiwa kutangaza iwapo walikubaliana na mapendekezo ya mwafaka. Wakaomba wapewe muda kidogo, lakini ombi lao halikukubaliwa. Walipoletwa kuhojiwa mbele ya Baraza, karibu nusu ya idadi yao walikuwa upande wa Wanamatengenezo. Wale ambao walikataa kukiuka uhuru wao wa dhamiri ya mtu na haki ya kila mtu kuamua mambo yake, walijua fika ya kwamba msimamo wao ule ungewaweka kuwa lengo dhahiri la kukosolewa katika siku za usoni, kushutumiwa na kuteswa. Mjumbe mmoja alisema maneno haya: " Inatupasa Ama tulikane Neno la Mungu, au - tuchomwe moto." – Ibid., b, 13, sura ya 5. [GC 201.2; PK Aya ya 13]

Mfalme Ferdinand, mwakilishi wa mfalme wa dola katika Baraza Kuu, aliona kwamba amri ile ingesababisha mgawanyiko mkubwa sana ikiwa wakuu wa nchi wasingeweza kushawishiwa kuikubali kwa kuiunga mkono na kuiwezesha. Kwa hiyo, alijaribu kutumia sanaa ya ushawishi, akijua fika ya kwamba kutumia nguvu kwa watu kama wale kungewafanya tu kuwa washupavu na kunuia zaidi. Yeye "akawasihi sana wakuu wa nchi kuikubali amri ile, akiwahakikishia kwamba mfalme wa dola angependezwa sana nao." Lakini wanaume wale waaminifu walikiri tu mamlaka ile iliyokuwa juu ya watawala wa kidunia, nao wakajibu kwa utulivu, wakisema: "Sisi tutamtii mfalme wa dola katika kila jambo linaloweza kuchangia kudumisha amani pamoja na heshima ya Mungu." - Ibid., b. 13 ch 5. [GC 201.3; PK Aya ya 14]

Hatimaye mbele ya Baraza Kuu mfalme alitangaza kwa Elekta na marafiki zake kwamba amri "ilikuwa karibu inaenda kuandikwa katika mfumo wa amri ya kifalme," na ya kwamba "njia pekee iliyobaki kwao ilikuwa ni kujisalimisha upande wa wengi." Baada ya kusema maneno hayo, aliondoka katika mkutano ule, na hakuwapatia Wanamatengenezo nafasi yoyote ya kujadili, kutafakari au kujibu. "hata hivyo walimtuma mjumbe na ikawa kazi bure kumsihi mfalme huyu arudi." Jibu lake kwa malalamiko yao lilikuwa: "Ni jambo lililokwisha kuamuliwa tayari; kujisalimisha kwa yote sasa, ndiyo jambo lililobaki." - Ibid., b. 13, sura ya 5. [GC 202.1; PK Aya ya 15]

Kikosi cha mfalme wa dola kilisadiki kwamba wale Wakuu wa nchi wa Kikristo wangeng'ang'ania Maandiko Matakatifu kuwa ndiyo bora kuliko mafundisho ya wanadamu na matakwa yao; tena walijua kwamba mahali popote pale ambapo kanuni ile ilikubalika hivyo, upapa hatimaye uliangushwa kabisa. Lakini, kama maelfu walioishi kuanzia siku zao, wao waliangalia tu mambo yale "yanayoonekana kwa macho," wakajigamba kwa kujidanganya kwamba kusudi la mfalme wa dola na papa lilikuwa na nguvu, na upande wa Wanamatengenezo ulikuwa dhaifu. Endapo Wanamatengenezo wangekuwa wameutegemea msaada wa mwanadamu peke yake, wangekuwa hawana uwezo wowote kama walivyofikiri wafuasi wa papa. Ingawa walikuwa dhaifu kwa idadi yao, tena walikuwa wanatofautiana na Rumi (kiimani), walikuwa na nguvu yao. Walitoa rufaa yao "ambayo haikutokana na taarifa za Baraza lile kuu, na kwenda kwenye Neno la Mungu, na kutoka kwa mfalme wa dola Charles kwenda kwa Yesu Kristo, Mfalme wa wafalme na Bwana wa mabwana." - "Ibid.,b. 13, sura ya 6. [GC 202.2; PK Aya ya 16]

Kwa kuwa mfalme Ferdinand alikuwa amekataa kuheshimu msimamo wao wa imani na dhamiri zao, wakuu wa Kikristo waliamua wasijali kule kutokuwepo kwake, bali walete upinzani* mbele ya mkutano wa taifa bila kuchelewa. Hivyo basi, tamko rasmi lenye maneno haya mazito likatayarishwa na kupelekwa mbele ya Baraza lile *(Protest): [GC 202.3; PK Aya ya 17]

“Sisi, kwa njia ya hati hii, tunapinga mbele za Mungu, Muumbaji wetu pekee, Mtunzaji, Mlinzi, Mwokozi na Mkombozi wetu ambaye siku moja atakuwa mhukumu wetu, kwamba sisi tunapinga mbele ya wanadamu wote pamoja na viumbe vyote, kwamba sisi, kwa niaba yetu na kwa niaba ya watu wetu, hatukubaliani, wala hatuitii kwa namna yoyote ile amri hiyo iliyopendekezwa na jambo lolote lile ambalo ni kinyume na Mungu kinyume na Neno Lake Takatifu, kinyume na haki ya dhamiri yetu, na kinyume na wokovu wa roho zetu [GC 202.4; PK Aya ya 18]

“Nini! Tuthibithishe amri hii!* Tunatoa dai letu kwamba Mwenyezi Mungu anapomwita mwanadamu ili apate kushiriki ujuzi Wake, mtu huyu hata hivyo hawezi kupokea ujuzi wa Mungu!” “Hakuna fundisho la dini la hakika ila lile ambalo linapatana na Neno la Mungu.... Bwana anakataza kufundisha Fundisho jingine lolote.... Maandiko Matakatifu yanapaswa kufafanuliwa au kuelezwa kwa kutumia aya zingine zinazoeleweka kwa uwazi zaidi,.... Kitabu hiki Kitakatifu, miongoni mwa mambo yote yaliyo ya muhimu kwa Mkristo, ni rahisi kueleweka, nacho kimekusudiwa kusambaratisha giza. Sisi tumedhamiria, kwa neema Yake Mungu, kudumisha kuhubiri Neno Lake tu lililo safi na pekee, kama lilivyo katika vitabu vya Biblia vya Agano la Kale na Agano Jipya, pasipo kuongeza kitu chochote humo ambacho kinaweza kuwa kinyume chake. Neno hili ndiyo Ukweli peke yake; ni kanuni ya hakika ya kupimia mafundisho yote ya dini pamoja na maisha yote, wala haliwezi kamwe kutuangusha, kushindwa na wala kutudanganya. Yule ajengaye juu ya msingi huu atasimama imara dhidi ya nguvu zote za kuzimu (jehanamu), wakati ubatili au majivuno yote ya kibinadamu yanapopangwa dhidi ya Neno la Mungu, yataanguka mbele ya uso wa Mungu. *(Sisi tukubaliane na tamko hili!). [GC 203.1; PK Aya ya 19]

“kwa ajili ya sababu hiyo, tunaikataa katakata nira iliyowekwa juu yetu.” “Wakati huo huo sisi tunatarajia kwamba mfalme wetu mkuu atatutendea kama kiongozi Mkristo anayempenda Mungu zaidi kuliko kitu kingine chochote; na sisi tunawaahidi kuwa tuko tayari kumpa yeye, pamoja na ninyi mabwana waheshimiwa, upendo wetu wote pamoja na utii ambao ndio wajibu wetu wa haki na halali kutoa.” -Ibid., b. 13, sura ya 6. [GC 203.2; PK Aya ya 20]

Mguso wa kushangaza na wenye kina ulihisiwa kwenye Baraza Kuu (Diet). Wengi wao walijawa na mshangao na tahadhari kuona ujasiri wa wale wapinzani (waprotestanti). Siku zao za usoni zilionekana kuwa zina dhoruba na zisizo na uhakika wowote. Migawanyiko, migogoro, vita, na umwagaji damu vilionekana kana kwamba havikuweza kuepukika. Lakini wale Wanamatengenezo, baada ya kuhakikishiwa kuwa msimamo na madai yao yalikuwa ni ya haki, tena wakiutegemea mkono wa Mungu Mwenye Uweza wote, walikuwa “wamejawa na ujasiri pamoja na msimamo ulio thabiti.” [GC 203.3; PK Aya ya 21]

“Kanuni zilizomo ndani ya Hati hii maarufu ya upinzani unaosherekewa (Uprotestanti) ... ndizo zinazojenga msingi na kiini hasa cha Uprotestanti. Sasa, upinzani huu hupinga dhuluma inayofanywa dhidi ya mwanadamu katika masuala ya imani: dhuluma ya kwanza, ni ile ya uingiliaji wa mahakama za kiraia, na dhuluma ya pili ni ile mamlaka ya kiholela na kidikteta ya kanisa (au mamlaka ya imla). Badala ya maovu hayo Uprotestanti huweka nguvu ya dhamiri ya mtu juu kuliko hakimu, na mamlaka ya Neno la Mungu juu zaidi kuliko mamlaka ya kanisa linaloonekana kwa macho ya kibinadamu. Katika nafasi ya kwanza kabisa, (uprotestanti) unakataa katakata mamlaka ya kiraia kuingilia mambo yamhusuyo Mungu, tena inaungana pamoja na manabii na mitume na kusema, “Imetupasa kumtii Mungu kuliko wanadamu” (Mdo. 5:29). Juu zaidi ya taji ya mfalme wa dola Charles wa Tano, (Hati hii ya uprotestanti) inaiinua juu zaidi taji ya Yesu Kristo. Lakini Hati hii ya uprotestanti, inaendelea mbele zaidi kwa kusema zaidi ya hayo; inaweka msingi wa kanuni isemayo kwamba mafundisho yote ya wanadamu ni lazima yawe chini ya uthibiti wa Maneno aliyosema Mungu.” -Ibid., b. 13, sura ya 6. Zaidi ya hayo, Wapinzani/Waprotestanti walikuwa wameithibitisha haki yao ya kuzungumza kwa uhuru kabisa waliyoamini kuhusu Ukweli. Kwamba hawangeamini na kulitii tu, bali wangefundisha kile inachoeleza kuhusu Neno la Mungu, tena walipinga haki ya kasisi au hakimu kuingilia kati. Upinzani/uprotestanti ule wa Spiers, ulikuwa ni ushuhuda mzito dhidi ya ile roho ya kukosa uvumilivu wa dini za wengine)* na kutoa dai la haki za binadamu wote kumwabudu Mungu kulingana na matakwa ya dhamiri zao wenyewe *(uvumilivu wa kidini-religious intolerance)* [GC 203.4; PK Aya ya 22]

**Kuikubali Hati Ile Ya Kupinga/Upinzani**

Tayari tamko lilikuwa limekwisha kutolewa. Lilikuwa limeandikwa katika kumbukumbu za maelfu ya watu na kusajiliwa katika vitabu vya mbinguni, mahali ambako hakuna juhudi yoyote ya mwanadamu ambayo ingeweza kulifuta. Ujerumani yote iliyoikuwa imeipokea injili, ilipokea Tamko hili la upinzani/uprotestanti kama ndio tamko au kaulimbiu yao ya imani. Kila mahali watu waliona katika tamko hili kama ahadi ya enzi mpya iliyo bora zaidi. Mmojawapo wa Wakuu wa nchi aliwaambia Waprotestanti wa Spiers/Spayas: “Mwenyezi Mungu, aliyewapa ninyi neema ya kumkiri kwa nguvu, kwa uhuru, na bila hofu, na awatunze ninyi katika huo msimamo imara wa Kikristo mpaka siku ile ya umilele.” -Ibid., b. 13, sura ya 6. [GC 204.1; PK Aya ya 23]

Kama Matengenezo ya uprotestanti, baada ya kupata kiasi fulani cha mafanikio, yangekubali kukawiza-kawiza muda ili kupata upendeleo wa ulimwengu, yangekosa uaminifu wa kweli kwa Mungu na kwa matengenezo yenyewe, na kwa njia hiyo yangejihakikishia kifo chake yenyewe. Uzoefu uliowapata Wanamatengenezo mashuhuri wenye vyeo ni somo kwa zama zote

zilizofuata. Namna ya Shetani anavyofanya kazi yake dhidi ya Mungu na Neno Lake haijabadilika; yeye bado hata leo anayapinga Maandiko ili yasipate kufanywa kuwa mwongozo wa maisha ya watu kama alivyofanya katika karne ile ya kumi na sita. Katika wakati wetu kuna ukengeufu mkubwa toka kwenye mafundisho na kanuni za Maandiko, tena kuna hitaji la kurudi kwenye kanuni zile kuu za Uprotestanti - Biblia, na Biblia peke yake, kama kanuni ya imani na wajibu. Shetani angali bado anafanya kazi kwa kila njia awezayo kutawala ili kuharibu uhuru wa dhamiri/dini. Nguvu ya upinzani dhidi ya Ukristo ambayo Waprotestanti wa Spiers waliikataa katakata, hivi sasa kwa nguvu mpya, inatafuta kurudisha utawala ilioupoteza. Kuling'ang'ania Neno la Mungu kule kule na utii imara usioyumbayumba kwa Neno la Mungu ulioonyeshwa wakati wa hatari na migogoro ya Matengenezo, ndilo tumaini la pekee kwa Matengenezo ya Kanisa leo. [GC 204.2; PK Aya ya 24]

Ishara za hatari zilijitokeza kwa Waprotestanti; kulikuwa na ishara pia, zilizoonyesha kuwa mkono wa Mungu ulikuwa umenyoshwa kuwalinda waaminifu. Ilikuwa ni karibu na wakati huu "Melanchthon alipompitisha rafiki yake Simon Grynaeus kwa haraka katika mitaa ya mji ule wa Spiers kuelekea kwenye mto Rhine, akimshurutisha avuke mto. Huyu wa pili yaani Grynaeus, alishangaa kuiona haraka ya namna ile. 'Mtu mmoja mzee sana na aliyeonekana makini na mwenye mambo mazito, lakini ambaye mimi sikumjua,' akasema Melanchthon, 'alijitokeza mbele yangu na kusema, Ndani ya muda wa dakika moja tu Maafisa wa sheria watatumwa na Ferdinand kumkamata na kumweka mahabusu Grynaeus." [GC 205.1; PK Aya ya 25]

**Kuponea Chupuchupu**

Wakati wote wa mchana, Grynaeus alikuwa amesemewa kwa kashfa na Faber, daktari wa theolojia, msomi na mfuasi wa papa, katika mahubiri yake; na katika kuyafunga mahubiri yake, alimshutumu kwa sababu ya kutetea "mafundisho fulani potofu ya kuchukiza sana." "Faber aliificha hasira yake, lakini mara tu baada ya pale alimwendea mfalme, ambapo kutoka kwake alipata amri dhidi ya Profesa msumbufu wa Heidelberg, asiyechoka kukazia mambo yake. Melanchthon hakutilia shaka hata kidogo kwamba Mungu alikuwa amemwokoa rafiki yake kwa kumtuma mmoja wa malaika Zake watakatifu kumuonya mapema dhidi ya hatari iliyomkabili. [GC 205.2; PK Aya ya 26]

"Akiwa amesimama bila ya kujongea kwenye kingo zile za mto Rhine, alingoja hadi maji ya mto ule yalipokuwa yamemwokoa Grynaeus dhidi ya watesi wake. 'Hatimaye," alipiga kelele Melanchthon, alipomwona mwenzake upande wa pili, 'hatimaye ametenganishwa na taya lililojaa ukatili wa watu waliojaa kiu ya kumwaga damu isiyo na hatia' Aliporudi nyumbani kwake, Melanchthon alipewa taarifa kwamba maafisa waliokuwa wanamtafuta Grynaeus, walikuwa

wameipekua sana nyumba yake yote toka juu hadi chini.” -Ibid., b. 13, sura ya 6. [GC 205.3; PK Aya ya 27]

**Baraza Pale Augsburg**

Sasa ilikuwa Matengenezo ya Kanisa yaletwe mahali ambapo yangeweza kujulikana sana, mbele ya viongozi wenye nguvu wa dunia hii. Wale Wakuu wa nchi Wainjilisti walikuwa wamenyimwa nafasi ya kusikilizwa na mfalme Ferdnand; lakini walikuwa wapewe fursa ya kuwasilisha madai yao mbele ya mfalme wa dola na waheshimiwa wa kanisa na serikali waliokusanyika. Ili kuyanyamazisha migawanyiko iliyoivuruga dola, Katika mwaka ule uliofuata baada ya upinzani wa Spier, Charles wa V, aliitisha kikao cha Baraza pale Augsburg, ambapo alitangaza kwamba yeye binafsi ana nia ya kuwa mwenyekiti wa kikao hicho. Viongozi wa Uprotestanti walipewa hati kuitwa shaurini pale. [GC 205.4; PK Aya ya 28]

Hatari kubwa zikayakabili Matengenezo ya Kanisa; lakini watetezi wake bado walimtegemea Mungu awasaidie kwa kazi yao, na waliahidi watakuwa imara kwa injili. Elekta wa Saxony, alisihiwa na wajumbe wake wa Baraza asihudhurie lile Baraza kuu. Mfalme wa dola, walisema, aliwataka wakuu wa nchi wahudhurie ili kuwavuta na kuwaingiza kwenye mtego. “Je! siyo kuhatirisha kila kitu kwenda na kujifungia mwenyewe ndani ya kuta za jiji huku ukiwa na adui yako mwenye nguvu?” Lakini wengine walielezea kwa uungwana au namna bora, wakisema: “Hebu wakuu wa majimbo tujivike ujasiri, na kazi ya Mungu itaokolewa.” “Mungu ni Mwaminifu; hatatutelekeza,” akasema Luther.” —Ibid., b. 14, sura ya 2. Elekta Saxony aliondoka pamoja na msafara wake kwenda kule Augsburg. Wote walizielewa hatari zilizomtishia, na wengi walikwenda mbele wakiwa na nyuso zenye huzuni na mioyo iliyojaa fadhaa. Lakini Luther aliyewasindikiza hadi Coburg, aliifufua imani yao iliyokuwa karibu kuzama kwa kuimba wimbo ulioandikwa wakati wa safari ile, uliosema, “Mungu wetu Ndiye Ngome (A Mighty Fotress is Our God- Zaburi 46 angalia wimbo huu kwenye tovuti na tafakari maneno yake).” Hofu nyingi za kutazamia mabaya mbeleni ziliwekwa kando na wengi, mioyo mingi mizito iliburudishwa waliposikia sauti ya wimbo ule uliovuviwa na vyombo vya ala vya nyuzi vya muziki. [GC 206.1; PK Aya ya 29]

Wakuu wa nchi walioyapokea Matengenezo ya Kanisa walikuwa wamedhamiria kuandika tamko la pamoja la maoni yao katika mfumo ulio na mpangilio mzuri, likiwa na uthibithisho kutoka katika Maandiko ili kuwasilisha mbele ya Baraza; na kazi ya kuyaandaa ilikabidhiwa kwa Luther, Melanchthon, na washirika wenzao. Ungamo hili lilikubaliwa na Waprotestanti kama ndiyo muhtasari wa ufafanuzi wa imani yao, nao wakajikusanya pamoja ili kuweka majina yao, yaani sahihi zao

katika hati ile ya muhimu. Ulikuwa ni wakati wa muhimu sana lakini wenye majaribu mengi. Wanamatengenezo walikuwa waangalifu sana kuona kwamba kusudi lao lisichanganywe na hoja za kisiasa; walihisi kuwa Matengenezo ya Kanisa yasingepaswa kutumia mvuto mwingine wowote zaidi ya ule unaotoka katika Neno la Mungu. [GC 206.2; PK Aya ya 30]

Wakati wakuu wa nchi Wakristo walipotaka kuendelea mbele kutia sahihi zao katika ungamo lile, Melanchthon, aliingilia kati,na kusema: "Ni kazi ya wanatheolojia na wachungaji kupendekeza mambo haya; hebu na tuache mambo mengine mikononi mwa mamlaka za wakuu wenye nguvu wa dunia." "Hasha, haiwezekani hata kidogo," alijibu John wa Saxony, "kwamba wewe unitenge mimi. Nimeamua kufanya lile lililo haki na sahihi, wala sijali taji yangu. Shauku yangu ni kumkiri Bwana wangu. Kofia yangu niliyoteuliwa kwayo, pamoja na joho langu hili la kicheche ambalo ni vazi la jimbo, havina thamani kubwa mno kwangu kama ulivyo msalaba wa Yesu Kristo." Baada ya kusema hayo, aliandika jina lake. Mwingine miongoni mwa wakuu wale wa nchi alisema hivi alipoishika kalamu: "ikiwa heshima ya Bwana Wangu Yesu Kristo inataka hivyo katika jambo hili, basi, mimi niko kuacha nyuma mali yangu pamoja na maisha yangu." "Ni heri mimi niwaache raia zangu na majimbo yangu, niiache nchi ya mababa zangu nikiwa na fimbo tu mkononi mwangu," aliendelea kusema, "kuliko nipokee fundisho jingine lolote tofauti na lile lililo katika Ungamo hili." -—Ibid., b. 14, ch. 6. Hiyo ndiyo ilikuwa imani na ujasiri wa watu wale wa Mungu. [GC 206.3; PK Aya ya 31]

### Siku Kuu Kuliko Zote Katika Matengenezo Ya Kanisa

Wakati mwafaka uliwadia wa kwenda mbele ya mfalme mkuu wa dola. Charles wa V, akiwa ameketi katika kiti chake cha enzi, akiwa amezungukwa na maelekta pamoja na wakuu wa nchi, alitoa nafasi ya kuwasikiliza Wanamatengenezo wale wa Kiprotestanti. Ungamo la Imani yao lilisomwa. Katika mkutano huo mkubwa wenye hadhi, Kweli za injili zilielezwa waziwazi, na makosa ya kanisa la papa yalianikwa waziwazi. Naam, na katika siku hiyo ilitangazwa vema kuwa ndiyo "siku kuu zaidi kuliko zote za Matengenezo, na siku yenye utukufu mwingi zaidi kuliko zote katika historia ya Ukristo na wanadamu." -Ibid., b. 14, sura ya 7. [GC 207.1; PK Aya ya 32]

Lakini miaka michache tu ilikuwa imepita tangu mtawa wa Wittenberg aliposimama peke yake katika jiji la Worms mbele ya baraza la kitaifa. Sasa mahali pake walisimama viongozi wenye heshima kubwa na nguvu nyingi katika dola. Luther alikuwa amekataliwa kuonekana huko Augsburg, lakini alikuwepo kwa njia ya maneno na maombi yake. "Nimefurahi kupita kiasi," aliandika, "kuishi mpaka wakati huu, ambapo Kristo ameinuliwa hadharani na waumini mashuhuri kama hawa." - Ibid., b. 14, sura ya 7. Kwa njia hiyo yakatimizwa

Maandiko yanayosema: "Nitazungumza juu ya shuhuda zako ... mbele ya wafalme." Zaburi 119: 46. [GC 207.2; PK Aya ya 33]

Katika siku za Paulo, injili ambayo kwayo alifungwa gerezani, ilifikishwa kwa njia hiyo hiyo mbele ya wakuu na waheshimiwa wa jiji la kifalme. Kwa hiyo katika tukio hili, kile ambacho mfalme wa dola alikuwa amepiga marufuku kisihubiriwe kutoka mimbarani kilihubiriwa katika nyumba ya mfalme; yaani, kile wengi walichodhani kwamba kilikuwa hakifai kusikilizwa hata na watumishi, kikawa kinasikilizwa na mabwana na malodi wa dola ile kwa mshangao mkubwa. Wafalme na wakuu wale walikuwa ndio wasikilizaji, wakuu wa nchi wenye taji za kifalme walikuwa ndio wahubiri, na hubiri lenyewe lilikuwa ni ile Kweli ya kifalme ya Mungu. “Tangu enzi zile za Mitume,” akasema mwandishi mmoja, “hakujapata kuweko kazi kubwa zaidi au ungamo bora sana kuliko hilo.” - D’Aubigne, kitabu cha 14, sura ya 7. [GC 208.1; PK Aya ya 34]

“Yote ambayo Walutheri wamesema ni ya Kweli; hatuwezi kuyakana,” alisema askofu mmoja wa kipapa. “Je, mnaweza kupata sababu nzuri za kukanusha kwa kutoa sababu za msingi Ungamo hilo lililofanywa na Elekta pamoja na wenzake?” akauliza mwingine kwa Dk. Eck. “kwa kutumia Maandishi ya Mitume na Manabii - hapana!” Likawa ndilo jibu lake; “Lakini kwa kutumia maandishi ya Mababa na ya mabaraza - naam!” “Ninaelewa,” alisema aliyeuliza swali. “Walutheri, kulingana na maelezo yako, wapo ndani ya Maandiko, na sisi tuko nje.” Ibid., b. 14, sura ya 8. [GC 208.2; PK Aya ya 35]

Baadhi ya wakuu wa nchi ya Ujerumani waliongoka na kujiunga na imani ya Matengenezo ya Kanisa. Mfalme wa dola mwenyewe akatangaza kwamba zile kanuni za imani ya Waprotestanti zilikuwa ni Kweli tupu. Tamko/Ungamo lile lilitafsiriwa katika lugha mbalimbali na kutawanywa katika nchi zote za Ulaya, nalo likakubaliwa na mamilioni katika vizazi vilivyofuata kuwa ndilo linatoa muhtasari wa tamko la imani yao. [GC 208.3; PK Aya ya 36]

Watumishi waaminifu wa Mungu walikuwa hawafanyi kazi hii ngumu wakiwa peke yao. Wakati falme na nguvu na pepo wachafu (mashetani) katika ulimwengu wa roho walipokuwa wameungana dhidi yao, Bwana hakuwaacha watu Wake. Kama macho yao yangekuwa yamefunguliwa, wangekuwa wameuona ushahidi dhahiri wa uwepo Wake Mungu pamoja na msaada Wake kama ulivyotolewa kwa nabii wa kale. Mtumishi wa Elisha alipomwonyesha bwana wake jeshi la maadui lililokuwa limewazingira na kuzuia uwezekano wote wa kutoroka kwao, yule nabii aliomba, kwa kusema: "Bwana, nakuomba, fungua macho yake, ili apate kuona." 2 Wafalme 6:17. Na, tazama, mlima wote ulikuwa umejaa magari ya vita na farasi wa moto, jeshi la mbinguni liliwekwa pale kumlinda mtu yule wa Mungu. Hivyo ndivyo malaika walivyowalinda watendakazi katika kazi yao ya Matengenezo ya Kanisa. [GC 208.4; PK Aya ya 37]

Mojawapo ya kanuni zile ambazo Luther alikuwa amezishikilia kwa nguvu sana ni ile iliyosema kwamba pasiwepo na haja yoyote ya kuiendea mamlaka ya kidunia na kuiomba msaada wa kuyaunga mkono Matengenezo ya Kanisa, ama kuomba au kutumia silaha kuyatetea matengenezo. Alifurahi sana kwamba injili ilikuwa imekiriwa na wakuu wale wa nchi wa dola ile; lakini walipotoa mapendekezo yao ili kuungana naye katika umoja wa kujihami, alitangaza kwamba "fundisho lile la injili linapaswa kulindwa na Mungu peke yake.... Kwa kadiri mwanadamu asivyojiingiza sana katika kazi ile, ndivyo Mungu angejihusisha kwa udhahiri zaidi kwa ajili ya kazi Yake. Tahadhari zile zote za kisiasa zilizopendekezwa, kwa maoni yake yeye, zilitokana na hofu isiyostahili kuwapo pamoja na yale mashaka yatokanayo na dhambi." - D'Aubigne, London, ed., 10, ch 14. [GC 209.1; PK Aya ya 38]

Wakati Maadui wenye nguvu walipokuwa wanaungana ili kuiangamiza imani ile ya Matengenezo, ndipo tena ilipoonekana kana kwamba maelfu ya mapanga yanaenda kuchomolewa ili kufutilia mbali matengenezo, Luther aliandika, akisema: "Shetani anaonyesha ghadhabu yake; maaskofu wasiomcha Mungu wanakula njama mbaya pamoja; na sisi tunatishiwa vita. Waonyeni watu ili wapate kushindana kwa ushujaa mbele ya kiti cha enzi cha Bwana, kwa imani na maombi, ili maadui zetu, wakiwa wamenyamazishwa kabisa kwa njia ya Roho wa Mungu, waweze kushurutishwa kuishi kwa amani. Hitaji letu kuu, kazi yetu kuu, ni maombi; hebu watu na wajue kwamba wamekabiliwa na ncha ya upanga na ghadhabu ya Shetani, hebu na waombe." - D'Aubigne, b. 10, sura ya 14. [GC 209.2; PK Aya ya 39]

Tena, katika tarehe fulani za baadaye, akiutaja muungano ule uliofikiriwa na wakuu wa nchi kati yao na Matengenezo yale ya Kanisa, Luther alisema kwa nguvu kuwa silaha peke yake itakayotumika katika vita ile ingekuwa ni ule "upanga wa Roho." Akamwandikia yule mtawala wa Saxony, na kusema: "Kwa dhamiri yetu hatuwezi kuunga mkono muungano huo unaopendekezwa. Ni afadhali tufe mara kumi kuliko kuona injili yetu ikisababisha hata tone moja la damu kumwagika. Sehemu yetu sisi ni kuwa kama wanakondoo wanaokwenda kuchinjwa. Msalaba Wake Kristo ni sharti tuubebe. Hebu mheshimiwa usiogope. Tutafanya mengi sana kwa maombi yetu kuliko kule kujitapa au kujigamba kwingi kwa maadui zetu wote. Ila jambo muhimu ni kwamba tu wewe usiruhusu mikono yako kutiwa doa la damu ya ndugu zako. Kama mfalme wa dola anataka sisi tukabidhiwe katika mahakama zake, basi, sisi tuko tayari kwenda. Wewe huwezi kuitetea au kuilinda imani yetu: kila mmoja wetu anapaswa kuamini, kwa kuwa tayari kujipatia hasara na maangamizi ya maisha yake mwenyewe." - Ibid., b. 14, sura ya 1. [GC 209.3; PK Aya ya 40]

Kutoka katika chumba cha siri cha maombi ndiko ilipotoka nguvu iliyoutikisa ulimwengu mzima katika yale Matengenezo Makuu ya Kanisa. Pale, wakiwa na

utulivu mtakatifu, watumishi wa Bwana walisimika miguu yao juu ya Mwamba wa ahadi Zake. Wakati ule wa mieleka na patashika yao iliyofanywa mjini Augsburg, Luther “hakuacha siku ipite bila kutumia angalau masaa matatu katika sala, nayo yalikuwa ni masaa yaliyokuwa yamechaguliwa miongoni mwa yale yaliyofaa sana kwa ajili ya kujifunza Maandiko.” Katika faragha ya chumba chake alisikika akiimimina roho yake mbele za Mungu kwa maneno “yaliyojaa sifa, kicho, na tumaini, sawa na rafiki anayezungumza na rafiki yake.” “Mimi ninajua kwamba Wewe ni Baba yetu na Mungu wetu,” alisema, “na ya kwamba wewe utawasambaratisha watesi wa watoto Wako; kwa kuwa Wewe Mwenyewe uko hatarini pamoja na sisi. Jambo lote hili ni lako Wewe, na ni kwa kutubidisha Wewe ndiyo maana sisi tumeweka mikono yetu juu yake. Tulinde na tulinde basi, Ee Baba!” -Ibid., b. 14, sura ya 6. [GC 210.1; PK Aya ya 41]

Kwa Melanchthon, aliyekuwa amekandamizwa chini ya mzigo mzito wa wasiwasi na hofu, alimwandikia, akasema: “Neema na amani katika Kristo - mimi nasema, katika Kristo, na wala si katika ulimwengu huu, Amina. Nachukia kwa chuki inayopita kiasi mifadhaiko na masumbufu yale yanayokulemea na kukutafuna kupita kiasi. Kama kazi hii si ya haki, basi, achana nayo; ila kama hoja hii ni ya haki, kwa nini, basi, sisi tuseme uongo kwa zile ahadi Zake Yeye ambaye ametuamuru kulala usingizi bila hofu yoyote?... Kristo hatatupungukia katika kazi hii ya haki na Ukweli. Yeye Yu hai, Naye anatawala; basi, sisi tuwe na hofu gani tena?” -Ibid., b. 14, sura ya 6. [GC 210.2; PK Aya ya 42]

Mungu alisikia kilio cha waja Wake. Aliwapa wale wakuu wa nchi na wachungaji neema Yake na ujasiri wa kutetea Ukweli dhidi ya watawala wale wa giza la ulimwengu huu. Asema hivi Bwana: "Tazama, ninaweka Sayuni jiwe kuu la pembeni, teule, la thamani; na Yeye amwaminiye hatatahayarika." 1 Petro 2: 6. Wanamatengenezo Waprotestanti walikuwa wamejenga juu ya Kristo, na malango yale ya kuzimu hayakuweza kuwashinda (Mathayo 16:18; 7:24-27). [GC 210.3; PK Aya ya 43]

# SURA YA 12

# MATENGENEZO KULE UFARANSA

**(Mapambazuko Kule Ufaransa Na Watu Waliokuwa Tayari Kufa Kwa ajili Ya Neno La Mungu)**

Ufupisho: Louis Berquin alikuwa mmoja wa wakuu mashuhuri kule Ufaransa, naye alipompata Kristo alikuwa tayari kufa kwa ajili ya imani yake. Soma uone jinsi maisha ya Berquin yalivyokuwa na changamoto katika kutetea haki, wakati ambapo wengi walitaka kujilinda wenyewe. Soma watu waliofanya naye kazi ya matengenezo kule Ufaransa. Matukio ya Historia hapa ni mengi, mfano Charles V aliuacha ufalme wake 1554. Zwingli alikufa kwenye vita ya Cappel mwaka 1531. Berquin alichomwa mwaka 1529, Calvin aliingia kwenye Uprotestanti 1534, huu pia ulikuwa mwaka ambao Feret aliweka mabango. January 21, 1793 Mfalme wa Ufaransa Louis XVI alikatwa kichwa. Geneva ilikuwa na dini ya Uprotestanti 1536. John Knox alipokea imani 1542, naye alizungumza na Malkia Mary 1551 na kufanya kazi Scotland miaka ya 1559.

Upinzani uliofanyika pale Spiers na Ungamo la pale Augsburg (kukiri)* ndiyo matukio ambayo yaliweka alama ya ushindi wa Matengenezo kule Ujerumani, yalifuatiwa na miaka ya mapambano na giza. Baada ya kudhoofishwa kwa migawanyiko miongoni mwa wafuasi wake waliouunga mkono, na kushambuliwa na maadui zake wenye nguvu, Uprotestanti ulionekana kana kwamba unaelekea kuangamizwa kabisa. Maelfu walitia muhuri ushuhuda wao kwa damu yao. Vita ya wenyewe kwa wenyewe ndani ya nchi vikazuka; Mmojawapo wa wafuasi wake wakuu aliisaliti kazi ya Uprotestanti; na watu wema kuliko wote miongoni mwa wale wakuu bora wa nchi waliokuwa wameyapokea Matengenezo yale ya Kanisa, wakaangukia katika mikono ya mfalme wa dola na kuburuzwa kama mateka toka mji hata mji. Lakini katika dakika ile ushindi wake ulipokuwa unaonekana kana kwamba ni dhahiri, mfalme alipigwa na kushindwa. Alishuhudia mawindo yake yakipokonywa kwa nguvu toka katika mkono wake, naye hatimaye akalazimika kutoa ruhusa ya kustahimili mafundisho yale ambayo katika maisha yake alikuwa amepania kuyaangamiza. Alikuwa ameuhatirisha ufalme wake, hazina zake, na maisha yake ili tu ausagesage kabisa uzushi. Sasa alishuhudia majeshi yake

yakimalizwa katika vita, hazina zake zikikauka, falme nyingi alizozitawala zikitishiwa na uasi, wakati kila mahali imani ile aliyokuwa amefanya kazi bure kabisa kuizima na kuikandamiza ilikuwa ikienea mahali pengi. Charles V alikuwa anapambana na mamlaka ya Mungu yenye nguvu kubwa kuliko zote. Mungu alisema, "na Iwepo nuru," bali yule mfalme wa dola alikuwa akipambana ili giza lisiondoke. Makusudi yake yakashindwa; na uzee ukamjia mapema kuliko wakati wake kwani mapambano ya muda mrefu yalimdhofisha, naye akajiuzulu na kung'atuka kwenye kiti chake cha enzi na kwenda kujificha katika nyumba ya watawa (The Augsburg Confession (Source: https://bookofconcord.org/augsburg-confession/)). [GC 211.1; PK Aya ya 1]

Katika nchi ya Uswisi, kama ilivyokuwa katika nchi ya Ujerumani, kulikuja siku za giza kwenye Matengenezo. Ingawa mikoa mingi iliipokea imani ya Matengenezo, mingine iling'ang'ania itikadi ya Rumi kwa upofu. Mateso yao dhidi ya wale waliokuwa na matamanio ya kuupokea Ukweli hatimaye yalisababisha vita ya wenyewe kwa wenyewe. Zwingli na wengi waliokuwa wamejiunga naye katika Matengenezo ya Kanisa walianguka katika uwanja wa damu wa Cappel. Oecolampadius, akiwa ametindikiwa kabisa moyoni na majanga haya ya kutisha, alikufa mara tu baada ya pale. Roma ilishinda na kushangilia, na kwenye maeneo mengi, ilionekana kana kwamba karibu itayarejesha yote iliyokuwa imepoteza. Lakini Yeye Yule ambaye mashauri Yake ni ya tangu milele, hakuwa ameiacha kazi Yake wala watu Wake. Mkono Wake ulikuwa unaenda kuwaletea ukombozi. Katika nchi zingine alikuwa amewainua watendakazi wa kuyaendeleza mbele Matengenezo. [GC 211.2; PK Aya ya 2]

Katika nchi ya Ufaransa, kabla jina la Luther halijasikika kama Mwanamatengenezo, siku ilikuwa tayari imeshaanza kupambazuka. Mmoja miongoni mwa watu wa awali kupokea nuru hiyo alikuwa ni yule mzee Lefevre, mtu aliyekuwa amesoma kwa mapana sana, profesa katika Chuo Kikuu cha Paris, na mfuasi wa dhati wa papa na mtu mwenye jitihada kubwa. Katika utafiti wake alioufanya katika Maandiko yale ya kale, umakini wake ulivutwa kuelekea kwenye Biblia, naye akaanzisha mafunzo ya Biblia miongoni mwa wanafunzi wake. [GC 212.1; PK Aya ya 3]

Lefevre alikuwa shabiki kipenzi wa ibada ya watakatifu waliokufa zamani, naye alijielekeza katika kazi ya kutayarisha historia ya watakatifu na wafia dini kama ilivyosimuliwa katika mapokeo ya kanisa. Hii ilikuwa ni kazi iliyohitaji nguvu nyingi; lakini yeye alikuwa tayari ameendelea mbele vya kutosha katika kazi hii, wakati alipodhania kwamba angeweza kupata msaada wenye kumnufaisha kutoka katika Biblia, alianza kuisoma Biblia ile akiwa na kusudi hilo moyoni mwake. Ni kweli aliwakuta watakatifu katika Biblia, lakini si kama vile walivyoelezewa katika kalenda ya Kiroma. Mafuriko ya nuru ya Mungu yalimwagika akilini mwake. Kwa mshangao na kuchukizwa, aligeuka na kuiacha

kazi yake ile aliyokuwa amejipangia mwenyewe (uchunguzi wa watakatifu) na kutumia muda wake wote kujifunza Neno la Mungu kwa makini. Kweli zile za thamani alizozigundua humo, alianza kuzifundisha mara moja. [GC 212.2; PK Aya ya 4]

### Lefevre Na Farel Waanza Kazi

Mnamo mwaka ule wa 1512, kabla ya Matengenezo ya Kanisa waliyofanya Luther na Zwingli, Lefevre aliandika, akisema: “Ni Mungu anayetupatia sisi, kwa imani, uadilifu ambao ni kwa neema peke yake tu tunatuhesabiwa haki na kwa ajili ya uzima wa milele.” — Wylie. b. 13, sura ya 1. Akiwa anatafakari sana juu ya siri na mafumbo yale za ukombozi, alishangilia, akasema: “Loo! ni ukuu usioelezeka wa kubadilishana huko! - Yeye Asiyekuwa na Hatia Anahukumiwa kufa, na yeye aliye na hatia anaachwa huru; Mbaraka (Kristo) unabeba laana, na yule aliyelaaniwa anapata mbaraka; Yule aliye Uzima Anakufa, na mfu anaishi; Utukufu Unafichwa kabisa katika giza, na yeye asiyejua chochote isipokuwa uso wa aibu uliochanganyikiwa, anavikwa utukufu.” (The great exchange!) - D’Aubigne, b. 12, sura 2. [GC 212.3; PK Aya ya 5]

Na wakati akifundisha kwamba utukufu wa wokovu ni wa Mungu pekee, pia alisema kwamba wajibu wa utii ni wa mwanadamu. “Ikiwa wewe ni mshiriki wa kanisa Lake Kristo,” alisema, “basi, wewe ni kiungo cha mwili Wake; na ikiwa wewe ni wa mwili Wake, basi, wewe umesheheni utimilifu wa tabia Yake Mungu.... Lo! Laiti wanadamu wangeweza kupata ufahamu wa upendeleo huu, ni kwa kiasi gani wangeishi maisha matakatifu, ya haki, na yenye usafi wa moyo basi, halafu wangeweza kuuona utukufu wa ulimwengu huu kuwa ni wa kuchukiza jinsi gani ukilinganishwa na utukufu ule uliomo ndani yao, - Ule utukufu ambao jicho la kimwili haliwezi kuuona-ikiwa tu wangefikiria utukufu wote wa ulimwengu huu.” – Ibid., b. 12, sura 2. [GC 213.1; PK Aya ya 6]

Walikuwemo miongoni mwa wanafunzi wa Lefevre waliosikiliza maneno yake kwa hamu kubwa, na ambao muda mrefu baada ya sauti ya mwalimu wao kunyamazishwa, wangeendelea kuutangaza Ukweli. William Farel ni mfano kati ya hao. Mwana wa wazazi wacha Mungu, tena aliyeelimisha na kulelewa katika mafundisho ya kanisa kwa imani isiyo na swali, naye angeweza kuungana pamoja na Paulo kwa kusema maneno haya kwa nguvu kuhusu habari zake mwenyewe: “Wakinijua sana tangu mwanzo, kama wakipenda kushuhudia, ya kwamba nalikuwa Farisayo kwa kuifuata madhehebu ya dini yetu iliyo sahihi kabisa.” Matendo 26:5. kama Mroma madhubuti, aliwaka moto kwa ari ya kutaka kuwaangamiza wote ambao waliothubutu kulipinga kanisa. “Nilisaga meno yangu kama mbwa-mwitu mwenye hasira kali,” alisema baadaye, akirejelea kipindi hiki cha maisha yake, “nilipomsikia mtu yeyote akisema neno lolote dhidi ya papa.” - Wylie, kitabu cha 2. 13, sura Ya 2. Alikuwa hachoki kuwaabudu watakatifu waliokufa zamani alipokuwa pamoja na Lefevre katika mizunguko yao kuyazuru

makanisa ya Paris, wakiabudu kwenye altare (madhababu) na kuyapamba maeneo haya matakatifu kwa zawadi zao. Lakini maadhimisho haya ya ibada hayakuweza kuleta amani rohoni mwao. Hatia ya dhambi ilimbana moyoni kwa nguvu, na hatia hii haikuweza kuondolewa moyoni hata kwa matendo yake yote ya toba aliyofanya. Kama ile sauti iliyotoka mbinguni alisikia maneno ya Mwanamatengenezo yaliyosema: "Wokovu ni kwa neema." "Yeye Asiye na hatia Amehukumiwa kufa, na mhalifu ameachiliwa huru." "Ni msalaba wa Kristo peke yake unaofungua malango ya mbinguni, na kufunga malango ya kuzimu." -Ibid., b. 13, sura ya 2. [GC 213.2; PK Aya ya 7]

Farel alipokea Ukweli kwa furaha. Kwa uongofu kama ule wa Paulo aligeuka na kuupa kisogo utumwa wa mapokeo na kuingia katika uhuru wa wana wa Mungu. "Badala ya kuwa na roho yake ile ya kurarua na kuua iliyokuwa kama ya mbwa-mwitu mwenye njaa kali," akageuka, kama alivyosema yeye mwenyewe, "akawa mkimya kama mwana-kondoo mpole asiye na madhara yoyote, moyo wake ukiwa umehamishwa kabisa kutoka kwa papa, na kukabidhiwa kwa Yesu Kristo." - D'Aubigne, b.12, sura ya 3. [GC 214.1; PK Aya ya 8]

### Injili Yapokelewa Pengi

Pale Lefevre alipoendelea kuieneza nuru miongoni mwa wanafunzi wake, Farel, akiwa na bidii ile ile katika kazi ya Kristo kama aliyokuwa nayo katika kazi ya papa, alitoka kwenda kuitangaza ile Kweli hadharani. Mhashamu wa kanisa hilo, askofu wa Meaux, muda mfupi tu baada ya pale alijiunga nao. Na waalimu wengine waliokuwa na sifa zenye umaarufu kulingana na uwezo na kisomo chao kikubwa, wakajiunga katika kuitangaza injili, nayo injili ikajipatia wafuasi miongoni mwa tabaka zote za watu, kuanzia katika nyumba za mafundi stadi na wakulima hadi katika ikulu ya mfalme. Dada yake Francis wa I, ambaye kwa wakati ule alikuwa ndiye mfalme anayetawala, aliipokea imani ile ya matengenezo. Mfalme mwenyewe anayetawala, na mama wa malkia, walionekana kwa muda, kana kwamba wanapendezwa nayo injili na kuiunga mkono, na kwa matumaini makubwa Wanamatengenezo walitarajia wakati ule ambapo Ufaransa ingeongolewa na kuiamini injili. [GC 214.2; PK Aya ya 9]

Lakini matumaini yao hayakutimia. Majaribu na mateso yaliwasubiri wanafunzi wa Kristo. Hata hivyo, rehema za Mungu lilificha hili, nalo halikuonekana machoni pao. Kipindi cha amani kiliingia kati, ili waweze kujenga ujasiri wa kukabiliana na dhoruba iliyokuwa inakuja; na Matengenezo yalisonga mbele kwa haraka. Askofu wa Meaux alifanya kazi kwa bidii nyingi katika dayosisi yake kuwafundisha mapadri na walei au watu wa kawaida. Maaskofu wasio na elimu na waovu wakaondolewa, na, kwa kadiri ilivyowezekana, nafasi yao ilijazwa na watu wenye elimu na wacha Mungu (watauwa wa kweli). Askofu huyu alitamani sana kwamba watu wake walipate lile Neno la Mungu wao wenyewe, na jambo

lile likatekelezwa upesi. Lefevre alichukua jukumu la kutafsiri Agano Jipya Kifaransa; wakati ule ule Biblia ya Luther ya Kijerumani ilikuwa inatoka kwenye mitambo ya uchapishaji vitabu kule Wittenberg, na Agano Jipya la Kifaransa lilichapishwa pale jijini Meaux. Askofu hakukwepa kutumia nguvu au mali yake katika kazi hii ya kulitawanya Neno katika parishi zake, na haukupita muda mrefu kwa wakulima wadogo wa Meaux kuwa na Maandiko Matakatifu. [GC 214.3; PK Aya ya 10]

Kama vile walivyo wasafiri wanaokaribia kuangamia kutokana na kiu wanavyoikaribisha kwa shangwe chemchemi ya maji yaliyo hai, ndivyo roho hizi zilivyoupokea ujumbe ule kutoka mbinguni. Vibarua wa mashambani, mafundi stadi katika karakana zao, walichangamshwa na kazi yao ngumu ya kila siku wakizungumza juu ya Kweli zile za Biblia zenye thamani. Wakati wa jioni, badala ya kukimbilia kwenye maduka ya mvinyo, walikusanyika katika nyumba ya kila mmoja wao,kwa zamu, ili kulisoma Neno la Mungu na kujiunga katika maombi na kumsifu Mungu. Badiliko kubwa likaonekana upesi katika jumuia hizi. Ingawa zilikuwa ni jumuia za tabaka ya chini kabisa za wakulima wasio na kisomo na vibarua wa kazi za sulubu au mitulinga, nguvu inayobadilisha tabia na kuinua ya neema ya Mungu ilionekana katika maisha yao. Wakiwa ni wanyenyekevu, walio na upendo, na watakatifu, walisimama kama mashahidi wa kile ambacho injili inaweza kutimiza kwa wale wanaoipokea kwa moyo dhati. [GC 215.1; PK Aya ya 11]

Nuru iliyowashwa pale Meaux ilitupa miale yake ya mwanga mbali. Kila siku idadi ya waongofu ilikuwa ikiongezeka. Ghadhabu ya viongozi wa kanisa wa hierakia katika kanisa la Roma kwa muda fulani walikuwawa medhibitiwa na mfalme, ambaye alidharau ubinafsi na ubaguzi ulio na ufinyu wa mawazo, waliokuwa nao wale watawa; lakini viongozi wa kipapa hatimaye walifaulu. Basi, ule mti wa kuchomea watu moto ukasimikwa. Askofu yule wa Meaux, akalazimishwa kuchagua kati ya moto na kuikana imani yake, akakubali njia ile rahisi yaani kukana; ila, licha ya kuanguka kwa kiongozi yule, kundi lake liliendelea kusimama kidete. Wengi walitoa ushuhuda wao kwa ajili ya ile Kweli wakiwa katikati ya ndimi za moto, Kwa ujasiri na uadilifu wao wakiwa katika mti wa mateso na moto, Wakristo hawa wanyenyekevu walihubiri injili kwa maelfu ya watu ambao katika siku zile za amani hawakuwa wamewahi kusikia ushuhuda wao kabla ya hapo. [GC 215.2; PK Aya ya 12]

### Mtu Wa Ukoo Wa Kuheshimika Aupokea Mwenge Wa Injili

Hawakuwa watu wa hali ya chini na maskini tu ambao katikati ya mateso na dharau walidiriki kushuhudia kwa ajili ya Kristo. Katika majumba ya makubwa ya matajiri na waheshimiwa wenye vyeo vya juu, na kwenye majumba ya kifalme walikuwako watu wa koo za kifalme walioithamini ile Kweli zaidi kuliko utajiri au

cheo ama hata maisha yao yenyewe. Mavazi ya kifalme ya vita yalificha roho ya juu, na imara zaidi kuliko joho na kofia ya kiaskofu. Louis de Berquin alizaliwa katika ukoo bora ulioheshimika wa kilodi (Lords). Alikuwa shujaa na mwenye cheo kinachohusiana na kutoa mashauri na ulinzi katika jumba lile la kifalme, alikuwa anapenda kutumia muda wake mwingi katika kujifunza, mwenendo wake uling'aa na tabia za kiungwana, na maadili yake yalikuwa hayana lawama. "Yeye alikuwa," mwandishi mmoja alisema, "mfuasi mkuu wa mambo yote yanayohusiana na taasisi za kipapa kama vile kanuni au katiba zake, na msikilizaji mkubwa wa Misa pamoja na mahubiri;... na sifa zake nyingine zote alizifunika kwa kuuangalia Ulutheri kwa chuki kubwa na maalum." Lakini kama wengine wengi, aliongozwa na majaliwa ya Mungu kuielekea Biblia, alishangaa kukuta humo, "hakuna mafundisho ya Rumi, bali mafundisho ya Luther." - Wylie, Wylie, b. 13, sura. 9. Kuanzia pale na kuendelea mbele alijiweka wakfu kabisa kwa kazi ya injili. [GC 215.3; PK Aya ya 13]

"Yeye alikuwa msomi zaidi miongoni mwa watu wa tabaka la juu na waungwana wa Ufaransa," Alikuwa mwenye akili nyingi (genius) na mwenye uwezo wa kuongea kwa ufasaha, ujasiri wake usiotaka kushindwa na juhudi zake za kishujaa, na mvuto wake katika jumba la kifalme, -- naye alipendwa na mfalme, -- vilimfanya kuchukuliwa na wengi kwamba alikuwa amechaguliwa na Mungu awe Mwanamatengenezo wa nchi yake. Alisema hivi Beza: "Berquin angeweza kuwa Luther wa pili, kama angekuwa amepata ndani ya Francis wa I, mtawala mwenye haki wa pili, roho ya Elekta Frederick." "Ni mbaya kuliko Luther," walipiga makelele wafuasi wa upapa." - Ibid, b. 13, sura. 9. Waroma wa Ufaransa walipatwa utisho kwa mwenendo wake. Wakamtupa gerezani kama mzushi, lakini akaachiwa huru na mfalme. Kwa miaka mingi mgogoro ule ukawa ukiendelea. Francis, akawa akiyumbayumba kati ya Roma na Matengenezo ya Kanisa, wakati fulani aliweza kuzistahimili juhudi kali za watawa, na wakati mwingine aliweza kuzizuia. Mara tatu Berquin alifungwa gerezani na mamlaka za kipapa, na kuweza kufunguliwa tu na yule mfalme, ambaye, kwa kuvutiwa na kipaji chake cha akili, pamoja na tabia yake nzuri ya kiuungwana, alikataa kumtoa kafara mikononi mwa uovu ule mbaya wa mamlaka ya hierakia ya kanisa uliokuwa umenuia kumdhuru. [GC 216.1; PK Aya ya 14]

Berquin alionywa mara kwa mara dhidi ya hatari iliyokuwa inamtishia nchini Ufaransa, na kuombwa kwa kuhimizwa kwamba, kwa hiari yake mwenyewe, afuate nyayo za wale waliokuwa wamepata usalama wao kwa kwenda uhamishoni kama wakimbizi. Erasmus, mtu mwoga, mwenye kujipendekeza na mtumishi wa maslahi ya muda mfupi, ambaye pamoja na fahari ya usomi mwingi alikosa kuwa na ukuu wa kimaadili unaoyashikilia maisha na heshima na kufanya tamaa zake zichukue nafasi ya kupenda Ukweli, alimwandikia Berquin, akisema: "Omba upate kupelekwa kama balozi kwenye nchi fulani ya kigeni; nenda na

kusafiri katika nchi ya Ujerumani. Wewe unamjua Beda, na mtu kama yule alivyo – yeye ni zimwi kubwa lenye vichwa elfu moja, atemaye sumu yake kali kila upande. Maadui zako ni wengi sana wao huitwa jeshi. Kama kazi yako ingekuwa bora kuliko ile ya Yesu Kristo, wasingeweza kukuacha uende zako mpaka wawe wamekuangamiza vibaya. Usiutumainie sana ulinzi wa mfalme. Katika hali yoyote ile, usinitie mimi hatarini kwa kunijumuisha pamoja na kitivo hicho cha theolojia." - Ibid., b. 13, sura. 9. [GC 216.2; PK Aya ya 15]

**Hatari Zazidi Kuongezeka**

Lakini kadiri hatari zilivyozidi kuongezeka na kuwa kubwa zaidi, ndivyo juhudi (usongo) ya Berquin ilivyozidi kuimarika nguvu yake. Licha ya kukataa kufuata ushauri wa kisiasa na ushauri uliomnufaisha Erasmus mwenyewe, alidhamiria kuzichukua hatua nyingine za kijasiri zaidi. Sio tu kwamba angesimama na kuitetea ile Kweli tu, bali pia angeyashambulia makosa. Shtaka la uzushi ambalo viongozi wa Roma walikuwa wanajitahidi sana kumpakazia, yeye alilielekeza kwao. Wapinzani wake wenye bidii na wenye uchungu mkubwa sana dhidi yake walikuwa ni wale madaktari wa falsafa wasomi pamoja na watawa wasomi wa idara ya theolojia katika Chuo Kikuu mashuhuri pale Paris, mojawapo ya mamlaka ya juu zaidi kabisa ya kidini katika jiji na taifa la Ufaransa. Kutokana na maandishi ya madaktari hawa wa falsafa alichota vipengele kumi na mbili ambavyo alitangaza hadharani kuwa "vililikuwa vinapingana na Biblia, tena vilikuwa ni uzushi/uongo;" naye alimwomba mfalme awe mwamuzi katika mapambano/mabishano yao. [GC 216.3; PK Aya ya 16]

Mfalme hakuona tatizo la kuzikutanisha pande hizi mbili zinazokinzana za wasomi waliobobea fani zao, alifurahia kupata nafasi ya kukinyenyekesha kiburi cha watawawenye majivuno, aliwaagiza viongozi wa Kiroma kutetea msimano wao kwa kutumia Biblia. Silaha hii, wao walijua fika, ingewanufaisha kwa udogo sana. Silaha walizojua kuzitumia vizuri wao, zilikuwa kifungo, mateso, na mti wa kuchomea watu moto (Dan. 11:32-35). Sasa meza zikawa zimepinduliwa, nao wakajiona wenyewe kuwa walikuwa karibu kutumbukia kwenye shimo walilokuwa wametumainia kumtumbukiza Berquin. Wakiwa wamepigwa na bumbuazi, walitafuta njia ya kutorokea. [GC 217.1; PK Aya ya 17]

"Karibu na wakati huo sanamu ya Bikira iliyokuwa kwenye kona ya mtaa mmojawapo ilikuwa imeharibiwa vibaya." Kulikuwa na taharuki kubwa jijini mle. Umati wa watu ulimiminika na kusongamana kwenda mahali pale, wakiwa na nyuso za maombolezo na ghadhabu. Mfalme naye akaguswa sana. Hapo ndipo fursa ilijitokeza ambayo watawa hawa wangeweza kuitumia kujenga hoja kwa manufaa yao, nao walikuwa wepesi kuiboresha fursa hiyo haraka. "Haya ni matunda ya mafundisho ya Berquin," walipiga makelele. "kila kitu sasa

kinakwenda kupinduliwa - dini, sheria, na kiti cha enzi chenyewe - kwa hila hii ya Kilutherani." -Ibid., b. 13, sura 9. [GC 217.2; PK Aya ya 18]

Berquin (Beke) alikamatwa na kufungwa tena. Mfalme aliondoka Paris, na kwa njia hiyo watawa wakawa huru kufanya mapenzi yao wenyewe. Mwanamatengenezo alishitakiwa na kuhukumiwa adhabu ya kifo, na ili Francis asije akaingilia kati hata wakati ule kumwokoa,hukumu yake ilitekelezwa siku hiyo hiyo ilipotamkwa. Wakati wa mchana Berquin alipelekwa mahali pa kifo chake. Umati mkubwa wa watu kubwa ulisongamana kushuhudia tukio hili, na walikuwepo wengi walioangalia kwa mshangao na mashaka moyoni mwao kuwa mhanga yule alikuwa amechaguliwa miongoni mwa familia zile bora, za watu wema, jasiri na waungwana zaidi nchini Ufaransa (Lords), Mshangao, hasira, uchungu, dharau, na chuki kali, vilitia giza nyuso za kundi kubwa lililokuwa limezagaa pale; ila kwenye uso mmoja peke yake hapakuwa na kivuli chochote kilichoonekana. Mawazo ya mfia dini yalikuwa mbali na vurugu za tukio lile; yeye alihisi uwepo wa Bwana Wake tu. [GC 217.3; PK Aya ya 19]

**Berquin Anyamazishwa**

Mkokoteni mbovu alioupanda, nyuso zilizokunjamana kwa hasira za watesi wake, kifo cha kutisha sana ambacho kilikuwa kinamsubiri -- mambo yale yote yeye hakuyajali kabisa; Yule Aliye hai, ambaye alikuwa amekufa, na ambaye Yu hai milele hata milele, tena anazo funguo za mauti na kuzimu (kaburi – Ufu. 1:18), alikuwa kando yake. Uso wa Berquin ulikuwa unang'aa kwa nuru na amani itokayo mbinguni. Alikuwa amevaa mavazi mazuri, ikiwemo "joho la kitambaa laini cha velvet, nusu koti la kitambaa cha hariri na pamba, lenye urembo uliofumwa, na suruali ya rangi ya dhahabu."-D'Aubigne, History of the Reformation in Europe in the Time of Calvin, b. 2, sura. Alikuwa anakaribia kutoa ushuhuda wake kwa ajili ya imani yake mbele Zake Yule Mfalme wa wafalme na mbele ya malimwengu yaliyokuwa yakishuhudia, na hakuna ishara yoyote ya majonzi ambayo ilipasa kuficha furaha yake. [GC 218.1; PK Aya ya 20]

Maandamano yalipokuwa yakisogea mbele polepole kupitia katika mitaa iliyofurika watu, watu waligundua kwa mshangao jinsi amani yake isivyokuwa na mawingu yoyote, alionyesha ushindi wenye furaha kwenye mwonekano na mwenendo wake. "Yeye" watu walisema "anaonekana kama mtu aketiye katika hekalu, na anatafakari mambo matakatifu." - Wylie, b., 13, sura. 9. [GC 218.2; PK Aya ya 21]

Akiwa amefungwa kwenye mti wa mateso ili kuchomwa moto, Berquin alijaribu kusema maneno machache kwa watu; lakini watawa wakihofia matokeo yake, walianza kupiga makelele, na askari wakaamriwa kuzigonganisha silaha zao, na kishindo cha makelele yao kikameza sauti ya mfia dini hata isiweze kusikika. Hivyo ndivyo, katika mwaka ule wa 1529, mamlaka ya juu kabisa ya

kistaarabu, ya kikanisa na kisomi Paris, “iliwekea umma mwaka huo wa 1793 msingi wa mfano mbaya wa kuyazima Maneno matakatifu ya watu waliokuwa wanakufa kwenye jukwaa la kunyongea wahalifu.” - Ibid., b. 13, sura. 9. [GC 218.3; PK Aya ya 22]

Berquin alinyongwa, na mwili wake ukateketezwa kwa ndimi za moto. Habari za kifo chake zilileta huzuni kwa marafiki wa matengenezo nchini kote Ufaransa. Lakini mfano wake haukupotea bure. “Sisi, pia, tuko tayari,” walisema mashahidi wa Ukweli, “kukabiliana na kifo kwa furaha, tulikodoa macho yetu kwenye maisha yale yajao.” - D’Aubigne, History of the Reformation in Europe in the Time of Calvin, b. 2, sura 16. [GC 218.4; PK Aya ya 23]

Wakati wa kipindi cha mateso pale Meaux, waalimu wa imaniya Matengenezo ya Kanisa walinyimwa leseni za kuhubiri, ndipo wakaenda kwenye maeneo mengine. Lefevre baada ya muda fulani alikwenda zake Ujerumani. Farel alirudi kwenye mji alikozaliwa, mashariki ya Ufaransa, ili kuieneza nuru ile nyumbani kwao alipokulia utotoni. Tayari habari zilikuwa zimesikika kuhusu kile kilichokuwa kikiendelea mjini Meaux, na kuhusu ile Kweli aliyoifundisha kule kwa juhudi yake isiyojua woga, aliwapata wasikilizaji. Baada ya muda mfupi wenye mamlaka walishtuka na kutaka kumnyamazisha, naye alifukuzwa kutoka katika mji ule. Ingawa hakuweza tena kufanya kazi yake hadharani, alipita katika nyika na katika vijiji, akifundisha katika makao ya watu binafsi na katika mabonde ya majani, katika sehemu pweke, tena alipata maficho misituni na miongoni mwa mapango ya majabali aliyokuwa akiyatembelea mara kwa mara wakati wa ujana wake. Mungu alikuwa akimwandaa kwa ajili ya majaribu makubwa zaidi mbeleni. “Misalaba, mateso, na nyenzo za Shetani, mambo ambayo mimi nilikuwa nimetahadharishwa nayo mapema, havijapungua,” alisema; “ni vikali sana kuliko ambavyo mimi mwenyewe ningeweza kustahimili, lakini Mungu Ndiye Baba yangu; Amenitunza kwa majaliwa Yake na daima atanipatia nguvu ninazohitaji.”- D'Aubigne, History of the Reformation in Europe in the Time of Calvin, b. 12, sura 9. [GC 219.1; PK Aya ya 24]

Kama ilivyokuwa katika siku za mitume, mateso yalikuwa “yametokea zaidi kwa kuiendeleza injili.” Wafilipi 1:12. Walipofukuzwa kule Paris na Meaux, “wale waliotawanyika wakaenda kila mahali wakilihubiri Neno.” Matendo 8:4. Na kwa njia ile nuru ikapata kupenya katika majimbo mengi ya mbali ya Ufaransa. [GC 219.2; PK Aya ya 25]

### Mungu Awatayarisha Watenda Kazi Wake

Mungu alikuwa bado akiwaandaa watendakazi Wake kuipanua kazi Yake. Katika mojawapo ya shule za mjini Paris, alikuwamo kijana mmoja mwenye kutafakari kwingi kwa kina, mkimya, ambaye tayari alionyesha matumaini ya kuwa na akili yenye nguvu, na inayopenya, na ambaye alijulikana kwa

umashuhuri wa maisha yake yasiyo na lawama kama alivyojulikana kwa uwezo wa akili na bidii katika kujitoa wakfu kumwabudu Mungu. Kipaji chake cha akili nyingi zisizokuwa za kawaida (genius) pamoja na jinsi alivyozitumia kikamfanya awe fahari ya Chuoni pale, na kwa imani ilitarajiwa kwamba John Calvin angekuwa mtetezi mmojawapo wa kanisa mwenye uwezo mkubwa na heshima nyingi kabisa. Lakini mwonzi wa nuru ya Mungu ukapenya hata ndani ya kuta za falsafa za uanazuoni na ushirikina ambao ulikuwa umemfunga Calvin. Alisikia habari za mafundisho mapya ya dini kwa kutetemeka, naye hakutilia shaka kwamba wazushi walistahili moto ambao walichomwa nao. Lakini, bila ya yeye kukusudia, alijikuta anakabiliana ana kwa ana na uzushi ule na kulazimika kuupima uwezo wa theolojia ile ya Kiroma ili kuweza kukabiliana na mafundisho ya Kiprotestanti. [GC 219.3; PK Aya ya 26]

Binamu yake Calvin ambaye alikuwa amejiunga na Wanamatengenezo, alikuwa jijini Paris. Ndugu hawa wawili walikutana mara kwa mara na kujadiliana pamoja mambo yaliyokuwa yasumbua Ulimwengu wa Kikristo. “Kuna dini mbili tu ulimwenguni,” alisema yule Olivetan Mprotestanti. “Kundi la kwanza la dini ni lile ambayo wanadamu wenyewe wamejibunia/wameivumbua wenyewe, katika hiyo, mwanadamu hujiokoa mwenyewe kwa njia ya kufuata maadhimisho ya dini na matendo mema; dini nyingine ni ile ambayo imefunuliwa katika Biblia, ambayo inamfundisha mwanadamu kutafuta wokovu wake kwa njia ya neema ya Mungu pekee yake, ambayo hutolewa bure.” [GC 220.1; PK Aya ya 27]

“Sitaki kusikia hata moja ya mafundisho yako hayo mapya,” Calvin alijibu kwa sauti ya juu; “hivi wewe unafikiri kwamba mimi nimeishi katika makosa siku zangu zote?” - Wylie, kitabu cha 13, sura ya 7. [GC 220.2; PK Aya ya 28]

### Chini Ya Shinikizo La Ile Kweli

Lakini fikra zake zilikuwa zimeamshwa akilini mwake, ambazo hakuweza kuziondoa kama apendavyo. Akiwa peke yake katika chumba chake, aliyatafakari maneno ya binamu yake. Hatia ya dhambi zake ilimlemea, naye akajiona mwenyewe akiwa bila mwombezi mbele ya Jaji mtakatifu na Mwenye haki. Upatanishi kwa njia ya maombezi ya watakatifu waliokufa zamani, matendo mema, taratibu na sherehe za kanisa, vyote hivi havikuwa na uwezo kabisa wa kulipia fidia hatia ya dhambi zake. Hakuweza kukiona kitu chochote mbele yake zaidi ya giza la kukata tamaa milele. Ikawa ni bure kabisa kwa madaktari wale wa falsafa, ambao walikuwa wasomi wa kanisa, kujaribu kuondoa maumivu yake moyoni. Alijitahidi kufanya maungamo na kitubio bila mafanikio yoyote; mambo yale hayakuweza kuipatanisha nafsi yake na Mungu. [GC 220.3; PK Aya ya 29]

Akiwa angali anajishughulisha na mapambano haya yasiyokuwa na matunda, Calvin, siku moja alibahatika bila kupanga kuzuru mojawapo ya viwanja vya

umma, naye akaona watu wengi waliokusanyika pale, na kisha akashuhudia kuchomwa moto kwa mzushi mmoja. Alijawa na mshangao kwa kuona amani iliyokuwa katika uso wa mfia dini. Akiwa katikati ya mateso makali ya kifo cha kutisha, na chini ya hukumu ya kanisa ya kuogofya sana, alionyesha imani na ujasiri, ambao kijana huyu mwanafunzi Calvin, aliyatofautisha na uchungu mkali na kule kukata tamaa kwake mwenyewe, pamoja na giza alilokuwa nalo moyoni mwake, wakati akiishi kwa utii kamili kwa kanisa lake. Alijua kuwa, 'wazushi' walitegemeza imani yao katika Biblia. Aliazimu kujifunza Biblia, ili ikiwezekana agundue siri ya furaha yao. [GC 220.4; PK Aya ya 30]

Katika Biblia alimpata Kristo. "Ee Baba," akalia, "Dhabihu Yake imeipoza ghadhabu Yako kwangu, na damu Yake imeuosha uchafu wangu; msalaba Wake umeibeba laana yangu; kifo Chake kimenilipia mimi fidia na kunipatanisha na Mungu. Sisi tulikuwa tumebuni upumbavu mwingi usiokuwa na faida kwetu wenyewe, lakini Wewe umeliweka Neno lako mbele yangu mimi kama tochi, tena umenigusa moyo wangu, ili niyachukie mambo yote mengine isipokuwa yale tu yenye sifa za Yesu." - Martyn, gombo la 1, vol. 3, sura 13. [GC 221.1; PK Aya ya 31]

Calvin alisomea upadre. Wakati akiwa ana umri wa miaka kumi na miwili tu, aliteuliwa kuwa msaidizi wa kanisa dogo (chapleini), na kichwa chake kilikuwa kimenyolewa upara na askofu kulingana na kanuni ya kanisa. Hakufanyiwa upadirisho, wala hakutekeleza majukumu ya kasisi, ila alihesabiwa kuwa mmojawapo wa makasisi, akishikilia cheo kile cha kazi yake, na kupokea posho kwa ajili ya kazi hii. [GC 221.2; PK Aya ya 32]

Sasa alihisi kuwa hatakuwa padre kamwe, kwa kipindi fulani aligeukia fani ya sheria, lakini hatimaye aliliacha kusudi lake hilo na kudhamiria kuyatumia maisha yake yote kuhubiri Injili. Lakini alisita kuwa mwalimu wa hadhara. Kwa tabia yake ya asili alikuwa ni mwoga na tena alilemewa na hisia ya jukumu zito kuhusu cheo hicho, na bado alitamani kutoa muda wake wote kwa ajili ya kujifunza na kusoma. Lakini hatimaye ushauri wa dhati wa rafiki zake ulifanikiwa kupata ridhaa yake. "Ni ajabu sana," alisema, "ya kwamba mtu mwenye maisha ya hali ya chini kama mimi aweze kuinuliwa na kupewa cheo kama hiki." - Wylie, b. 13, sura 9. [GC 221.3; PK Aya ya 33]

Calvin alianza kazi yake kimya kimya, na maneno yake yalikuwa kama matone ya umande udondokao chini na kuiburudisha ardhi. Alikuwa ameondoka Paris, na sasa alikuwa katika mji wa jimbo chini ya ulinzi wa binti mfalme aitwaye Margaret, ambaye, kwa kuipenda injili, alipanua wigo wake wa ulinzi kwa wanafunzi wa injili. Calvin bado alikuwa ni kijana tu, mpole, asiyetaka makuu na pia asiyependa tabia ya kujifanya (feki). Kazi yake ikaanza kwa kuwatembelea watu majumbani mwao. Wakati alipokuwa amezungukwa na watu waliomo mle nyumbani, aliwasomea Biblia na kuzifunua Kweli za wokovu. Wale waliousikia

ujumbe ule walizipeleka habari zile njema kwa wengine, na muda si mrefu mwalimu huyu akawa amekwenda mbali na mji ule na kuingia kwenye vitongoji na vijiji. Katika majumba makubwa na katika vibanda vilivyojengwa kwa makuti na magogo alikaribishwa, kisha alisonga mbele, akiweka msingi wa makanisa yaliyoweza kutoa ushuhuda wake bila hofu kwa ajili yaUkweli [GC 221.4; PK Aya ya 34]

Baada ya miezi michache alirudi tena huko mjini Paris. Pakawa na msukosuko usio wa kawaida katika makundi ya wenye elimu na wasomi. Kujifunza lugha za kale kulikuwa kumewaongoza watu kwenye Biblia (Kiebrania, kigiriki na Kilatini), na wengi ambao mioyo yao ilikuwa haijaguswa na Ukweli wake walikuwa wakiujadili kwa hamu kubwa na hata kupambana na mabingwa wa Uroma. Calvin, ingawa alikuwa mpiganaji Hodari mwenye uwezo katika nyanja za mabishano ya hoja za kitheolojia, alikuwa na utume (misheni) wa hali ya juu sana aliopaswa kuutekeleza kuliko makelele ya wanazuoni. Mioyo na akili za watu zikawa zimetibuliwatibuliwa, na sasa wakati ukawa umewadia wa kufungua malango ya Ukweli. Wakati kumbi za vyuo vikuu zilipojaa makelele ya malumbano ya kitheolojia, Calvin yeye alikuwa akitembea nyumba kwa nyumba, kuwafungulia watu Biblia, na kuzungumza kwao habari za Kristo Yule aliyesulubishwa. [GC 222.1; PK Aya ya 35]

**Nuru Yaangaza Paris**

Kwa uongozi Wake Mungu, mji wa Paris ulikuwa unakwenda kupokea mwito mwingine wa kuipokea injili. Wito wa Lefevre na Farel ulikuwa umekataliwa, lakini tena ujumbe ule ulipaswa kusikiwa na watu wa tabaka zote katika jiji hili kubwa. Mfalme, akishawishiwa na mambo ya kisiasa, alikuwa bado hajaamua kuunga mkono Roma kikamilifu ili kuyapinga Matengenezo ya Kanisa. Margaret alikuwa angali anashikilia tumaini kwamba Uprotestanti hauna budi kushinda katika nchi ya Ufaransa. Aliazimia kwamba imani ya matengenezo inapasa kuhubiriwa huko mjini Paris. Mfalme alipokuwa hayupo, alimwamuru mchungaji wa Kiprotestanti kuhubiri katika makanisa ya mji. Jambo lile lilipokuwa limekataliwa na wakuu ya upapa, binti mfalme huyu alifungua milango wazi katika jumba la kifalme kwa Matengenezo. Chumba kikaandaliwa kitumike kama kanisa dogo (chapel), na tangazo likatolewa kwamba kila siku, kwa saa maalum iliyopanga, hubiri la Neno la Mungu lingetolewa, na watu wa kila hadhi, tabaka na kazi, walialikwa kuhudhuria. Makundi ya watu yalifurika kwenda kwenye ibada. Sio tu ndani ya kanisa lile dogo watu walijaa, bali na vyumba vyake vya kuingilia katika ukumbi mkuu pamoja na kumbi za kusubira watu kulikuwa na msongamano wa watu. Kila siku maelfu ya watu walikusanyika pale – watu mashuhuri, waungwana (malodi), wakuu wa serikali, wanasheria, wafanya biashara, na mafundi stadi. Mfalme badala ya kupiga marufuku mikutano ile, aliamuru makanisa mawili ya mjini Paris yafunguliwe. Kamwe mji huo

haukuwahi kusukwasukwa kwa Neno la Mungu kwa jinsi hiyo. Yule Roho wa Uzima toka mbinguni alionekana kana kwamba amewavuvia watu. Kuwa na kiasi, usafi wa maisha, bidii ya kufanya kazi au stadi, utaratibu na mipangilio, vilichukua nafasi ya ulevi, anasa za tamaa ya mwili, ubaradhifu, malumbano na uvivu. [GC 222.2; PK Aya ya 36]

Lakini mamlaka ya hierakia ya kanisa hayakubung'aa. Mfalme bado alikataa kuingilia kati ili kuzuia mahubiri, na mamlaka ya Kiroma yakawakakawageukia wanachi. Hapakuwa na njia ambayo iliachwa kutumiwa ili kuchochea hofu, chuki, na ushabiki wa dini usiotumia akili miongoni mwa halaiki ile iliyojaa ujinga na ushirikina. Kwa upofu, wakilisalimisha kwa waalimu wake wa uongo, mji wa Paris, kama Yerusalemu ya zamani, haukujua majira ya kujiliwa kwake, wala haukujua mambo iliyopasa kujua ili kudumisha amani yake. Kwa miaka miwili Neno la Mungu lilihubiriwa katika mji mkuu; lakini wakati wakiwapo wengi walioipokea injili, watu walio wengi miongoni mwa watu waliikataa. Francis alikuwa amejifanya kuonyesha moyo wa kuwa na uvumilivu wa dini zingine kwa kulinda tu maslahi yake mwenyewe, ndipo wafuasi wa papa walifanikiwa kujirudishia tena mamlaka yao. Makanisa yakafungwa tena, na mti wa kuchomea watu moto ukasimikwa. [GC 223.1; PK Aya ya 37]

Calvin alikuwa bado angali mjini Paris, akijiandaa kwa kusoma, kusali, kuchunguza na kutafakari kwa ajili ya kazi yake ya wakati ujao, na huku akiendelea kueneza nuru. Hatimaye hata hivyo, walimshuku. Mamlaka ya kanisa ikadhamiria kumleta kwenye ndimi za moto. Yeye, alijidhania kuwa yu salama katika maficho yake, hakuwa amefikiria hata kidogo juu ya hatari iliyokuwa imemkabili, wakati marafiki zake walipokuja kwa haraka katika chumba chake walileta habari kwamba maafisa walikuwa njiani kuja kumkamata na kumtia mbaroni. Dakika ile ile walisikia kishindo cha mlango wa nje ukigongwa kwa nguvu. Hapakuwa na muda wa kupoteza. Baadhi ya marafiki zake waliweza kuwacheleweshe maafisa pale mlangoni, wakati marafiki wengine wakimsaidia Mwanamatengenezo kutoroka kwa kumshusha chini kupitia dirishani, naye alipofika chini, alitembea kwa haraka sana na kutoka nje ya viunga vya mji. Baada ya kupata hifadhi yake katika kibanda cha kibarua mmoja aliyekuwa rafiki na muumini wa matengenezo, alijigeuza kwa kuvaa nguo za mwenyeji wake, kisha, akiwa amelibeba jembe lake begani, alianza safari yake. Alisafiri kuelekea upande wa kusini, na akapata tena kimbilio katika maeneo ya utawala wa Margaret. (Angalia D'Aubigne, History of the Reformation in Europe in the Timeof Calvin b. 2, sura ya 30) [GC 223.2; PK Aya ya 38]

### Chini Ya Ulinzi Wa Rafiki Zake

Alibaki hapa kwa miezi michache, akiwa salama chini ya ulinzi wa marafiki wenye nguvu, naye akaendelea kujishughulisha kujifunza kama hapo awali.

Lakini moyo wake ulikuwa umekita kwenye kuhubiri injili katika nchi ya Ufaransa, wala yeye hakuweza kutulia kwa muda mrefu. Muda mfupi baada ya dhoruba kutulia kwa kiasi fulani, alitafuta shamba jipya la kufanya kazi ya Bwana kule Poitiers, mahali palipokuwa na Chuo Kikuu, na ambako mawazo mapya yalikuwa yamepata upendeleo kwa watu. Watu wa matabaka yote waliisikiliza injili kwa furaha. Hapakuwa na mahubiri ya hadhara, bali katika nyumba ya hakimu mkuu, yaani, katika makazi yake ya muda mfupi, na wakati mwingine katika bustani ya Umma, Calvin aliyafungua maneno ya uzima kwa wale waliopenda kuyasikia. Baada ya muda fulani kupita, idadi ya wasikilizaji ilipozidi kuongezeka, ilifikiriwa kwamba ilikuwa ni salama zaidi kwao kukusanyika nje ya jiji. Pango moja lililokuwa kwenye ukingo wa korongo jembamba lenye kina lililokuwa limejitenga katikati ya milima, mahali ambapo miti na miamba iliinamia na kuyafanya mazingara kukamilika zaidi kama mahali pa maficho, basi hapa palichaguliwa kuwa ndipo mahali pa kukutania. Makundi madogo madogo, yaliyokuwa yakitoka mjini kwa njia tofauti, yalielekea kule. Katika sehemu hii tulivu na ya faragha, Biblia ilisomwa kwa sauti kubwa na kufafanuliwa. Hapa Meza ya Bwana iliadhimishwa na Waprotestanti wa Ufaransa kwa mara yao ya kwanza. Kutokana na kanisa hili dogo wainjilisti/wamishonari kadhaa waaminifu walitumwa kwenda nje kwenye maeneo mengine. [GC 224.1; PK Aya ya 39]

Kwa mara nyingine Calvin alirudi tena mjini Paris. Bado yeye alikuwa hajapoteza tumaini mawazoni mwake kwamba Ufaransa kama taifa itayapokea Matengenezo. Lakini aligundua kuwa karibu kila mlango wa kufanya kazi kule umefungwa. Kufundisha injili ilikuwa ni kupita katika barabara iliyoelekea moja kwa moja kwenda kwenye nguzo ya kuchomea watu moto, ndipo hatimaye alidhamiria kuondoka na kwenda Ujerumani. Mara tu alipokuwa ameondoka Ufaransa, dhoruba kali ya mateso iliwapasukia Waprotestanti, kiasi kwamba kama angeendelea kubaki hapo, lazima angeingizwa katika maangamizi ya jumla. [GC 224.2; PK Aya ya 40]

Wanamatengenezo Wafaransa, wakiwa na matamanio ya kuiona nchi yao ikienda sambamba kwa kasi na nchi ya Ujerumani na Uswisi, waliazimia kutoa kipigo chao kikali dhidi ya ushirikina wa Rumi kwa ujasiri, jambo ambalo lingeliamsha taifa zima. Basi, mabango yaliyoishambulia Misa yalibandikwa kwa usiku mmoja katika nchi yote ya Ufaransa. Badala ya kuyaendeleza Matengenezo ya Kanisa, hatua hii yenye mori lakini ambayo iliyoamuliwa vibaya kwa kutokuwa na busara, ilileta madhara, sio tu kwa walioitekeleza, bali pia marafiki wa imani ya matengenezo katika nchi nzima ya Ufaransa. Iliwapa viongozi wa Roma kile walichokitamani kwa muda mrefu -- kisingizio cha kutoa madai yao kwamba wazushi wale waangamizwe kabisa kama watu walio hatari kwa uimara wa kiti cha enzi cha mfalme na amani ya taifa zima. [GC 224.3; PK Aya ya 41]

Kwa njia ya mkono wa siri usiojulikana - iwe wa rafiki asiye na tahadhari au adui mwenye hila haikuweza kujulikana kamwe—mojawapo ya mabango lilitundikwa kwenye chumba cha faragha cha mfalme. Mfalme aliingiwa na hofu kuu. Kwenye karatasi la bango hilo, mambo ya kishirikina yaliyokuwa yamepewa heshima kwa zama nyingi yalikuwa yameshambuliwa bila kubakisha kitu. Na huu ujasiri usio na mfano wa kudiriki kuandika maneno yale ya wazi ulishtua na kuamsha ghadhabu ya mfalme. Katika kustaajabu kwake alisimama kwa muda mfupi akitetemeka kwa hofu na kukosa maneno ya kusema. Hatimaye ghadhabu ilimfanya kutamka maneno haya ya kutisha: "Na wakamatwe wale wote wanaoshukiwa kuwa na imani ya Kilutheri bila kumwacha mtu. Mimi nitawaangamiza wote." - Ibid., b. 4, sura. 10. Kulikuwa hakuna kurudi nyuma sasa. Mfalme yule alikuwa amekata shauri kujiambatanisha kabisa na upande wa Roma. [GC 225.1; PK Aya ya 42]

**Utawala Wa Vitisho**

Hatua zilichukuliwa mara moja kumkamata kila mfuasi wa Luther aliyekuwa katika mji wa Paris. Fundi stadi mmoja masikini, mfuasi wa imani ya Matengenezo, ambaye alikuwa na mazoea ya kuwaita waumini kwenda kwenye mikutano yao ya siri, alikamatwa, naye, akiwa ametishiwa kuchomwa moto moja kwa moja kwenye mti wa kuchomea watu moto, aliamriwa kumwongoza wapelelezi wa papa kwenda naye kwenye nyumba ya kila Mprotestanti katika jiji. Alijikunyata kwa hofu kukubali pendekezo baya, lakini hatimaye hofu ya ndimi za moto ilimlemea, naye akakubali kuwa msaliti wa ndugu zake. Mbele yake ikatangulia hostia (Mkate Mtakatifu), halafu akafuata Morin mpelelezi wa mfalme, akiwa pamoja na yule msaliti, akiwa amezungukwa na maandamano ya mapadri, wabeba vyetezo vya kufukiza uvumba, watawa, na askari, polepole na kimya-kimya wakapita katika mitaa ya jiji. Maandamano yalionekana kama vile yalikuwa ya kuiheshimu fahari ya "sakramenti takatifu," kitendo cha kulipa fidia kwa tusi lililokuwa limetolewa dhidi ya Misa na wapinzani. Lakini chini ya tamasha hilo la gwaride, kusudi la mauaji lilikuwa limefichwa. Walipofika karibu na nyumba ya mfuasi wa Luther, msaliti alitoa ishara yake, lakini bila kutamka neno lolote. Msafara ulisimama, na nyumba ile iliingiwa, na wanafamilia ile wakaburutwa nje na kufungwa kwa minyororo, halafu kikundi cha kuogofya kilisonga mbele kutafuta wahanga wapya. Maandamano haya "hayakuiacha hata nyumba moja, kubwa au ndogo, hata katika vitivo vililivyokuwa katika Chuo Kikuu cha Paris.... Morin aliufanya mji mzima utetemeke .... Ulikuwa ni utawala wa vitisho." - Ibid., b. 4, sura 10. [GC 225.2; PK Aya ya 43]

Wahanga waliuawa kwa maumivu ya kikatili mno, hali hiyo ilikuwa mbaya zaidi kwa vile iliamuriwa kuwa moto upunguzwe ili kurefusha muda wa maumivu yao. Lakini watu hawa walikufa kama washindi (Ufu. 12:11). Msimamo wao thabiti haukutetereka, amani yao haikutiwa wingu la giza. Watesi wao, kwa vile

walikuwa hawana uwezo kabisa wa kuuvunja uthabiti wao usionyumbulika, walijiona wameshindwa. “Chanja za kuchomea watu moto zikatawanywa sehemu zote za mji wa Paris, kisha uchomaji wa watu moto ukaendelea siku zilizofuata mfululizo, lengo likiwa ni kueneza hofu kuu dhidi ya uzushi ule kwa kueneza kila mahali mauaji (unyongaji, au ukataji vichwa). Lakini, hatimaye faida ya kitendo kile ilibaki upande wainjili. Mji mzima wa Paris uliwezeshwa kujionea wenyewe ni aina gani ya watu ambao mawazo mapya yaliweza kuzalisha. Hapakuwa na mimbari ya mahubiri kwao iliyokuwa bora zaidi ya rundo la maiti za wafia dini. Furaha yenye amani iliyoangaza katika nyuso za hawa watu walipokuwa wakipita ... wakielekea mahali pa kunyongewa, ujasiri na ushujaa wao waliposimama katikati ya ndimi kali za moto zenye uchungu, upole, msamaha wao wa unyenyekevu kwa wale waliowaumiza kiasi kile, ni mambo ambayo yaliwabadilisha wengi, mara nyingi, hasira iligeuka na kuwa huruma, chuki kuwa upendo, na kitendo kile kikawasihi wajitoe na kusimama upande wa injili kwa ufasaha usioweza kupingika.” - Wylie, b. 13, sura. 20. [GC 226.1; PK Aya ya 44]

Makasisi wakiwa wamejielekeza kudumisha ghadhabu katika vilele vyake vya juu kama walivyozoea, walisambaza mashtaka ya kutisha dhidi ya Waprotestanti. Walishtakiwa Waprotestanti kwamba walikuwa wamekula njama ya kuwaua Wakatoliki wengi kwa jeuri, kuipindua serikali, na kumwua mfalme. Hapakuwa hata na chembe ya ushahidi ulioweza kutolewa ili kuunga madai yao. Hata hivyo, utabiri ule wa kutokea kwa maovu yale ulifikia utimilifu wake baadaye; lakini chini ya mazingira tofauti kabisa, na kutokana na sababu zilizo na sura tofauti kabisa. Mambo ya ukatili yaliyofanywa na Wakatoliki dhidi ya Waprotestanti wasiokuwa na hatia yoyote yalizidi kurundikana kwa ukali wake na kuzidi kuwa mzigo wa kisasi, na baada ya karne nyingi zilizofuata, yalileta majanga yale yale ambayo walikuwa wametabiri kwamba yangekuja kutokea, dhidi ya mfalme, serikali yake, na raia wake; lakini yaliletwa na watu makafiri wasiomjua Mungu, na wafuasi wa upapa wenyewe. Ilikuwa siyo ustawishaji au uimarishaji wa Uprotestanti bali ule ukandamizaji na ukomeshaji wa Uprotestanti, ndio ambao ulileta maafa yale ya kutisha katika nchini ya Ufaransa miaka mia tatu baadaye. [GC 226.2; PK Aya ya 45]

Kushuku wengine, kutoaminiana, hofu na ugaidi vilienea miongoni mwa matabaka yote ya jamii. Katikati ya taharuki ya jumla iliyowapata watu wote ilionekana dhahiri jinsi ambavyo mafundisho ya Luther yalivyopata mashiko ndani ya mioyo ya watu waliokuwa na elimu ya juu, mvuto, na uzuri wa tabia. Nafasi za amana na heshima zikabaki tupu kwa ghafla. Mafundi stadi, wachapaji vitabu, wasomi, maprofesa katika vyuo vikuu, waandishi wa vitabu na hata watumishi wa mfalme walitoweka. Mamia ya watu walilikimbia jiji la Paris, walikuwa wakimbizi kwa hiari yao wenyewe kwa kutoka nchi waliyozaliwa na kwenda katika nchi nyingine, na katika mifano hiyo mingi walitoa dokezo kwamba wao

walikuwa wanaipenda imani ya Matengenezo. Viongozi wa upapa waliwaangalia kwa mshangao watu hao na kufikiria kwamba palikuwa na wazushi miongoni mwao ambao walikuwa bado hawajawashuku. Hasira yao ikaelekezwa kwenye makundi ya wahanga fukara waliokuwa ndani ya uwezo wao. Magereza yalijaa wafungwa, na hewa yenyewe ikaonekana kana kwamba imetiwa giza na moshi wa rundo la watu waliokuwa wanachomwa moto kwa kuikiri injili. [GC 227.1; PK Aya ya 46]

**Kulipia Fidia Kwa Kosa La Kumwaga Damu**

Francis I aliona fahari kuwa kiongozi katika vuguvugu kubwa ya kufufua elimu ambayo iliashiria mwanzo wa karne ya kumi na sita. Alikuwa amefurahia sana kuwakusanya watu katika jumba lake la kifalme, watu wenye elimu kutoka katika kila nchi. Kupenda kwake elimu na dharau yake dhidi ya ujinga na ushirikina waliokuwa nao watawa vilichangia walau kwa kiwango fulani, uvumilivu aliouonyesha kwa Matengenezo ya Kanisa. Lakini alipochochewa na juhudi ya kuukomesha uzushi wote, mlezi huyu wa elimu alitoa amri iliyotangaza kwamba uchapishaji wa vitabu ulikuwa umekomeshwa katika nchi yote ya Ufaransa! Francis I alikuwa ni mfano mmoja miongoni mwa mifano mingi iliyorekodiwa katika kumbukumbu inayoonyesha kwamba kukuza utamaduni wa kiakili si tiba dhidi ya chuki za kidini na kutesa watu (religious intolerance). [GC 227.2; PK Aya ya 47]

Ufaransa kwa kufanya sherehe adhimu na ya hadhara, ilikuwa imejitoa kikamilifu kabisa kuuangamiza Uprotestanti. Makasisi walidai kwamba dharau na matusi yaliyotolewa dhidi ya Mbingu za juu kwa kupiga marufuku Misa ilipaswa kupatanishwa kwa njia ya damu, na kwamba mfalme kwa niaba ya watu wake, alitakiwa abariki kazi ile ya kutisha sana, kwa kutangaza hadharani ili ifanyike. [GC 227.3; PK Aya ya 48]

Tarehe 21 Januari, 1535 ilipangwa kwa ajili ya sherehe hiyo ya kutisha. Hofu za za kishirikina pamoja na chuki kali zisizokuwa na sababu ziliamshwa katika taifa zima. Jiji la Paris lilishonana kwa umati wa watu wa kutoka katika maeneo yote ya mashambani yaliyouzunguka mji, na watu wakawa wamejaa mitaani. Siku ile ilikuwa haina budi kukaribishwa kwa maandamano makubwa yenye fahari. "Vitambaa vya maombolezo au matanga vilitundikwa katika nyumba zote zilizokuwa kandokando ya njia yalikopita mandamano, na altare (madhabahu) zilijengwa huko kila baada ya umbali fulani." Mbele ya kila mlango palikuwa na mwenge uliowashwa kwa heshima ya "sakramenti takatifu." Kabla ya mapambazuko, waandamanaji walijipanga karibu na jumba la mfalme. Mbele zilitangulia bendera pamoja na misalaba ya parokia kadhaa; kisha wakafuata

raia, wakitembea wawili wawili, na wakibeba mienge mikononi mwao." Mashirika manne ya watawa yakafuata nyuma yao, kila shirika likiwa katika mavazi yake ya tofauti na ya kipekee. Kisha likaja kundi kubwa la watu waliobeba mifupa mingi na vitu vya watakatifu waliokufa zamani ambavyo vilikuwa vimekusanywa na kuhifadhiwa (relics). Halafu wakaja waheshimiwa viongozi wa dini matajiri katika mavazi yao ya rangi ya zambarau na majoho mekundu na mapambo ya vito, wakiwa wamepanda juu ya farasi, safu zao zilizopendeza sana na kumetameta zilijipanga. [GC 228.1; PK Aya ya 49]

"Hostia au mkate wa komunio ulibebwa na askofu wa Paris chini ya mwavuli wa kifalme uonekanao kama dari au kipaa cha juu kilicho maridadi sana,... akisaidiwa na wakuu wa nchi wanne wa damu.... baada ya hostia ile alifuata mfalme.... Francis wa Kwanza siku ile hakuvaa taji yake ya kifalme, wala joho lake lake la kitaifa." Akiwa na "kichwa wazi, kisichofunikwa kitu, macho yake yakiangalia chini, na mkononi mwake akiwa ameshikilia mshumaa mwembamba unaowaka moto," mfalme wa Ufaransa alionekana "katika sura ya mtu mwenye kutubu." - Ibid. b. 13, sura 21. Kwenye kila altare/madhabahu, aliinama chini kwa kujidhili, siyo kwa ajili ya uovu ulioinajisi nafsi yake, wala si kwa ajili ya damu isiyokuwa na hatia aliyoimwaga, na ambayo ilitia waa mikono yake, bali kwa ajili ya dhambi ya mauti iliyotendwa na raia zake waliodiriki kuipinga Misa. Nyuma yake alifuata malkia na wakuu wa taifa, nao wakiwa wanatembea wawili wawili, kila mmoja akiwa na mwenge uliowashwa. [GC 228.2; PK Aya ya 50]

Kama sehemu ya huduma ya siku ile, mfalme mwenyewe alihutubia maafisa wa ngazi za juu wa ufalme wake katika ukumbi mkubwa wa ikulu ya maaskofu. Akiwa na uso uliojaa huzuni, alitokea mbele yao, na kwa maneno ya ufasaha na yenye mguso kwa watu, aliomboleza kwa ajili ya "uhalifu, kufuru, siku ya huzuni na aibu," ambayo ilikuwa imekuja juu ya taifa la Ufaransa. Naye akamwamuru kila raia aliye mtiifu na mwema kusaidia katika kukomesha kabisa gonjwa lile la uzushi mbaya lililoitishia kuangamiza nchi ya Ufaransa. "Mabwana, kwa hakika, mimi hapa mfalme wenu," akasema, "ikiwa ningejua mojawapo ya mkono au mguu wangu ulikuwa na doa au umeambukizwa na uozo huo unaochukiza mno, basi, ningewapa ili muukate.... Na zaidi ya hayo, kama ningemwona mmojawapo wa watoto wangu achafuliwa nao, basi, nisingeweza kumwacha hai.... Na ningemtoa mimi mwenyewe kafara kwa Mungu." Machozi yalikatiza hotuba yake naye akashindwa kutamka maneno yake, na mkutano wote ukaangua kilio, na kwa kauli moja wakapiga kelele kwa nguvu wakisema: "Sisi tutaishi na kufa kwa ajili ya dini ya Kikatoliki!" - D'Aubigne, History of the Reformation in Europe in the Time of Calvin b. 4, sura 12. [GC 228.3; PK Aya ya 51]

Giza la kutisha lilikuwa limekuja katika taifa ambalo lilikuwa limeikataa katakata nuru ya Ukweli. Neema "iletayo wokovu" ilikuwa imefunuliwa kwao; lakini, baada ya kuangalia nguvu yake na utakatifu wake, baada ya maelfu

kuvutwa na uzuri wake usio na kifani wa kimbingu, baada ya miji na vitongoji kutiwa nuru kwa mng'ao wake, Ufaransa iligeuka na kuipa nuru kisogo, na ikachagua giza badala ya nuru. Walikuwa wameitupa mbali zawadi ya mbinguni ambayo ilikuwa imetolewa kwao. Walikuwa wameuita uovu kuwa ndio wema, na wema uovu, mpaka wakawa wamegeuka na kuwa wahanga wa kujitakia na kujidanganya wenyewe kimakusudi kabisa. Japo mioyoni mwao walisadiki kabisa ya kwamba walikuwa wanamfanyia Mungu huduma kwa kuwatesa watu Wake, hata hivyo, kuamini kwa dhati hivyo mioyoni mwao hakukuwafanya wasiwe na hatia. Nuru ile ambayo ingeweza kuwaokoa kutoka katika udanganyifu, kutoka katika kuchafua roho zao kwa hatia ya kumwaga damu, walikuwa wameikataa kwa kuchagua kwao wenyewe. [GC 229.1; PK Aya ya 52]

Kiapo kizito cha kidini cha kuung'oa uzushi kabisa kilitolewa katika Kanisa Kuu la Jimbo, ambamo takribani karne tatu hivi baadaye, Mungu mke wa mantiki (Goddess of Reason) alitawazwa kwenye kiti cha enzi na taifa hilo lililokuwa limemsahau Mungu aliye hai. Maandamano yakajipanga kwa mara nyingine tena, na wawakilishi wa nchi ya Ufaransa walijipanga kwenda kuanza kazi ile waliyokuwa wameapa kuifanya. "Majukwaa ya kunyongea watu yakasimikwa kwa umbali wa karibu karibu, nayo juu yake Wakristo fulani wa Kiprotestanti walikusudiwa kuchomwa na kuni za moto wakiwa hai, tena ilikuwa imepangwa kwamba malundo yale ya kuni yawashwe wakati mfalme anapokaribia pale, na ya kwamba msafara usimame pale kushuhudia mhanga akifa." - Wylie, kitabu cha. 13, sura. 21. Maelezo ya kinagaubaga ya mateso makali waliyoyastahimili hawa mashahidi kwa ajili Yake Kristo yanatia uchungu na kutisha moyo kiasi kwamba hayafai kusimuliwa tena; lakini hapakuwa na kutetereka kokote kwa wahanga. Waliposhurutishwa kuikana imani yao, mmoja wao alijibu hivi: "Mimi naamini tu kile walichohubiri manabii na mitume awali, pamoja na yale ambayo kundi lote la watakatifu waliamini. Imani yangu ina uhakika kwa Mungu ambaye atazipinga nguvu zote za kuzimu." - D'Aubigne, History of the Reformation in Europe in the Time of Calvin, kitabu cha 4, sura ya 12. [GC 229.2; PK Aya ya 53]

Tena na tena msafara ule ulisimamishwa mahali pa mateso. Walipofika mahali pale walipoanzia katika ikulu ya mfalme, kundililitawanyika, na mfalme na maaskofu waliondoka, wakiwa wameridhika sana na shuguli zilizofanyika siku ile, huku wakijipongeza wenyewe na kusema kwamba kazi ile waliyoianza ingeendelea mpaka uzushi utakapoteketezwa kabisa. [GC 230.1; PK Aya ya 54]

**Injili Yang'olewa Kabisa**

Injili ya amani ambayo Ufaransa ilikuwa imeikataa hakika ilingolewa kabisa, lakini matokeo yake yangekuwa ni ya kutisha mno baadaye. Tarehe 21 Januari, 1793, miaka mia mbili hamsini na minane (258) tangu siku ile ambayo Ufaransa ilijitoa rasmi katika kutesa Wanamatengenezo, na yalitokea maandamano

mengine, yenye madhumuni tofauti kabisa na yale, yakapita katika mitaa ile ile ya Paris. “Mfalme safari hii pia alikuwa mhusika mkuu; pakawa na vurugu na makelele tena; safari hii tena kikasikika kilio cha kutaka wahanga wengi zaidi waletwe; kulikuwa tena na majukwaa meusi ya kunyongea watu; na matukio ya siku ile yakafungwa tena kwa mauaji mabaya sana; Louis wa Kumi na Sita, akipambana mkono kwa mkono na askari wa gereza waliokuwa wanaenda kumnyonga, alikokotwa na kuwekwa juu ya jukwaa au kiunzi cha kukatia vichwa, na kushikiliwa pale kwa nguvu nyingi mpaka shoka liliposhuka chini, na kichwa chake kilichotenganishwa kiwiliwili kikabingirika juu ya jukwa la kunyongea watu.” - Wylie, kitabu cha. 13, sura. 21. Wala mfalme hakuwa mhanga peke yake; karibu na mahali pale pale watu elfu mbili na mia nane waliuawa kwa mashine yenye kisu cha kukatia vichwa (guillotine) katika kipindi hiki cha umwagaji damu kilichofanywa na utawala wa vitisho. (Reign of Terror). [GC 230.2; PK Aya ya 55].

Matengenezo ya Kanisa yalikuwa yameupatia ulimwengu Biblia iliyo wazi, yakifunua kanuni za Sheria ya Mungu (Amri Kumi), na kuhimiza madai yake katika dhamiri za watu. Upendo wa Mungu usio na kikomo ulikuwa umewafunulia wanadamu amri na kanuni zile za mbinguni. Mungu alikuwa amesema: “Zishikeni basi, mkazitende, maana hii ndiyo hekima yenu na akili zenu, machoni pa mataifa watakaozisikia amri hizi zote, nao watasema, Hakika taifa hili kubwa ni watu wenye hekima na akili.” Kumbukumbu la Torati 4:6. Wakati Ufaransa ilipotupilia mbali zawadi ya mbinguni, ilikuwa imepanda mbegu za machafuko, uasi na uharibifu dhidi ya serikali; ndipo utendaji kazi usioepukika wa asili na athari ukazalisha Mapinduzi na ule Utawala wa hofu na udikteta [GC 230.3; PK Aya ya 56]

### Farel Kule Uswisi

Muda mrefu kabla ya mateso yaliyochochewa na mabango, Farel, mtu yule jasiri na mwenye ari kubwa, alikuwa amelazimika kukimbia kutoka katika nchi yake aliyozaliwa. Alihamia Uswisi, na kwa njia ya kazi yake, akaiunga mkono kazi ile ya Zwingli, huyu alisaidia kuigeuza mizani kuelekea kwenye kupokelewa vyema kwa Matengenezo. Miaka yake ya baadaye ilitumiwa hapa, lakini aliendelea kutoa mvuto wake wenye nguvu uliokuwa umedhamiriwa katika upande wa Matengenezo kule Ufaransa. Katika miaka yake ya mwanzo ya kuishi kwake uhamishoni kama mkimbizi, juhudi zake zilielekezwa hasa katika kuieneza Injili katika nchi yake alikozaliwa. Alitumia wakati wake mwingi kuhubiri miongoni mwa watu wa nchi yake waliokuwa mpakani, ambako kwa juhudi zisizojua kuchoka alifuatilia mgogoro na kusaidia kwa maneno yake ya kutia moyo pamoja na mashauri yake. Kwa msaada wa wakimbizi wengine, vitabu vya Wanamatengenezo wa Kijerumani vilitafsiriwa katika lugha ya Kifaransa, na, pamoja na Biblia ya Kifaransa, vikachapishwa kwa wingi. Kwa njia ya wainjilisti

wa vitabu, kazi zile za vitabu zikauzwa katika eneo kubwa la nchi ya Ufaransa. Vitabu vilitolewa kwa wainjilisti wa vitabu kwa bei ya chini, ili faida inayopatikana kutokana na kazi ile, iwawezeshe kuiendeleza kazi hiyo. [GC 231.1; PK Aya ya 57]

Farel alianza kazi yake katika nchi ya Uswisi katika vazi la unyenyekevu la ualimu, akiwa mkuu wa shule wa kawaida. Alienda kwenye parokia iliyokuwa imejificha, aliutumia muda wake mwingi katika kuwafundisha watoto wadogo. Kando ya fani za kawaida za elimu zilizo kwenye mtaala husika, kwa tahadhari alizipenyeza Kweli za Biblia kwa tahadhari sana, akitumainia kwamba kwa kupitia watoto angeweza kuwafikia wazazi wao. Walikuwapo baadhi yao walioamini, lakini makasisi na mapadri walijitokeza ili wapate kuizuia kazi hiyo, kisha wananchi wa mashambani waliokuwa wamejaa ushirikina walichochewa ili wapate kuipinga kazi yake. “hiyo haiwezi kuwa Injili ya Yesu Kristo,” walisisitiza mapadri, “kwa vile kuihubiri kwake hakuleti amani, bali vita.” - Wylie, kitabu cha 14, sura. 3. Kama ilivyokuwa kwa wanafunzi wa kwanza, alipoteswa katika jiji moja alikimbilia jingine. Toka kijiji hata kijiji, toka mji hata mji, alikwenda akisafiri kwa miguu yake, akistahimili njaa, baridi, na uchovu mwingi, na kila mahali akiyahatirisha maisha yake. Alihubiri sokoni, makanisani, na wakati mwingine katika mimbari za makanisa makubwa. Mara nyingine alikuta kanisa likiwa tupu, bila wasikilizaji; nyakati nyingine mahubiri yake yalikatizwa kwa makelele, kuzomewa na kuchekwa; halikadhalika aliwahi kuburuzwa kikatili kutoka katika kibweta. Zaidi ya mara moja alishambuliwa kwa kufanyiwa njama na wahuni au wanasiasa na kupigwa hadi karibu ya kufa. Lakini hata hivyo, yeye alisonga mbele. Ingawa mara nyingi alifukuzwa, ila kwa ustahimilivu wake usiochoka alirudi tena kwenye uwanja wa mashambulizi yale; na, kwenye mji mmoja baada ya mwingine, alishuhudia miji midogo na miji mikubwa, ambayo ilikuwa ngome ya upapa, ikifungua malango yake na kuipokea injili. Parokia yake ndogo aliyokuwa ametumika hapo awali, muda si mrefu iliipokea imani ile ya Matengenezo. Miji mikuu ya Morat na Neuchatel nayo pia ikaachana na mapokeo/taratibu ya dini ya Kiroma na kuziondoa sanamu zilizoabudiwa kutoka katika makanisa yao. [GC 231.2; PK Aya ya 58]

Kwa muda mrefu Farel alikuwa ametamani kusimika bendera ya Uprotestanti katika mji wa Geneva. Ikiwa jiji lile lingeweza kuongolewa, basi, lingekuwa kitovu Matengenezo ya Kanisa kwa nchi za Ufaransa, Uswisi, na Italia. Akiwa na azimio hili kwenye moyo wake, aliendelea kufanya kazi yake hadi miji mingi na vitongoji vilivyozunguka vilipoongolewa. Kisha akiwa na mwenzake mmoja, aliingia jiji la Geneva. Lakini aliruhusiwa kuhubiri mahubiri mawili tu. Makasisi baada ya kushindwa kufanikiwa kupata hukumu ya kumnyonga kutoka kwa mamlaka ya kiraia, walimwita mbele ya baraza la kikanisa, hapo walikuja wakiwa wamezificha silaha ndani ya majoho yao, wakiwa wamedhamiria kuutoa

uhai wake. Nje ya ukumbi, kundi la watu wenye hasira, wakiwa na marungu na mapanga, lilijikusanya kuhakikisha kifo chake endapo angefanikiwa na kulitoroka baraza. Lakini ule uwepo wa mahakimu na maaskari wenye silaha ulimwokoa. Mapema asubuhi iliyofuata, yeye pamoja na yule mwenzi wake, waliongozwa kulivuka ziwa hadi mahali pa usalama. Hivyo ndivyo juhudi yake ya kwanza ya kuihubiri Injili mji wa Geneva ilivyoishia. [GC 232.1; PK Aya ya 59]

### Chombo Duni Chateuliwa

kwa ajili ya jaribio la pili, mjumbe wa hali ya chini zaidi alichaguliwa - yaani, mwanaume mmoja kijana, ambaye sura yake ilionekana kuwa ni ya unyenyekevu sana, kiasi kwamba alitendewa kwa ubaridi na dharau hata na marafiki zake waliodai kuyapenda Matengenezo. Lakini, je! mtu kama huyo angeweza kufanya nini mahali ambapo Farel alikuwa amekataliwa?” Inawazekanaje basi, mtu mwenye ujasiri na uzoefu mdogo aweze kuipinga tufani ambayo watu wenye nguvu na hodari kabisa walikuwa wamelazimika kuikimbia? "Si kwa nguvu, wala si kwa uwezo, bali kwa Roho Wangu, asema Bwana wa majeshi." Zakaria 4:6. “Mungu alivichagua vitu dhaifu vya dunia ili aviaibishe vyenye nguvu; sababu upumbavu wa Mungu una hekima zaidi ya wanadamu, na udhaifu wa Mungu una nguvu zaidi ya wanadamu.1 Wakorintho 1:27, 25. [GC 232.2; PK Aya ya 60]

Froment alianza kazi yake kama mwalimu mkuu wa shule. Kweli zile alizowafundisha watoto wadogo shuleni, watoto nao walizirudia kuzifundisha nyumbani kwao. Muda si mrefu wazazi wao wakaja kuisikiliza Biblia ikifafanuliwa shuleni, hadi chumba cha darasa kikajazwa na wasikilizaji makini. Nakala za Agano Jipya pamoja na vijizuu vilisambazwa bure, navyo viliweza kuwafikia wengi ambao wasingediriki kuja pale hadharani kuyasikiliza yale mafundisho mapya. Baada ya muda mfupi kupita, huyu mtendakazi alilazimika kukimbia pia; lakini Ukweli alioufundisha ulikuwa umeotesha mizizi katika mioyo ya watu. Mbegu ya matengenezo ilikuwa imepandwa pale, nayo iliendelea kuimarika kwa nguvu na kuenea. Wahubiri walirudi tena pale, na hatimaye kupitia kazi zao ibada ya Kiprotestanti ilianzishwa katika jiji lile la Geneva. [GC 232.3; PK Aya ya 61]

Jiji lilikuwa tayari limeshatangaza kuunga mkono Matengenezo baada ya kutangatanga kwake kwingi na kujipatia mikasa iliyoleta mabaliko mbalimbali, ndipo Calvin alipoingia katika milango yake. Akirudi kutoka katika ziara yake ya mwisho kutoka kule alikozaliwa, alikuwa njiani kuelekea Basel, wakati, alipogundua kuwa barabara ile ya moja kwa moja ilikuwa inatumiwa na majeshi ya Charles V, naye alilazimika kuchukua njia ya mzunguko kupitia Geneva. [GC 233.1; PK Aya ya 62]

Katika ziara hii Farel aliutambua mkono wa Mungu. Ingawa Geneva ilikuwa imeipokea imani ya matengenezo, bado kazi kubwa ilitakiwa kufanyika pale. Ni

mtu mmoja mmoja tu, ndiye ambaye huongolewa kwa Mungu na wala si jumuiya; kazi ya kuzaliwa upya haina budi kufanyika moyoni na katika dhamiri kwa uwezo wa Roho Mtakatifu, siyo kwa amri zinazotolewa na mabaraza. Watu wa Geneva walipokuwa wameitupilia mbali mamlaka ile ya Roma, walikuwa hawajawa tayari sana kuachana na uovu ambao ulikuwa umeshamiri chini ya utawala wa Roma. Kuziimarisha kanuni safi za injili mahali hapa na kuwatayarisha watu kuwa na stahiki za kuzijaza nafasi ambazo majaliwa ya Mungu yalikuwa yanawaita kuzijaza, haikuwa kazi nyepesi. [GC 233.2; PK Aya ya 63]

Farel alikuwa na uhakika kwamba kwa kumpata Calvin, alikuwa amempata mtu ambaye angeweza kushirikiana naye katika kazi hii. Katika jina la Mungu, alimwapisha kwa kiapo kikuu mwinjilisti kijana ili apate kubaki na kufanya kazi pale. Calvin alirudi nyuma kwa tahadhari. Akiwa mtu mwoga na mpenda amani, alisita kukutana na roho yenye ujasiri, huru na hata ya kutumia nguvu na ujeuri ya mkazi wa Geneva. Udhaifu uliotokana na afya yake na kukosa ujasiri, pamoja na mazoea yake ya kupenda kujisomea Neno la Mungu kwa bidii, vilimsukuma kutafuta mahali pa faragha, ambapo hapana ghasia. Akiamini kuwa kwa njia ya kalamu yake angeweza kuisaidia kuendeleza kazi ya Matengenezo ya Kanisa, alitamani kupata mahali pa faragha, na penye utulivu, kwa ajili ya kujifunza kwake, na pale, kwa njia ya machapisho, apate kuyafundisha na kuyaimarisha makanisa. Lakini shauri lile zito lililotoka kwa Farel lilimjia kama wito kutoka Mbinguni, naye hakuthubutu kukataa. Ilionekana kwake, alisema mwenyewe, “ni kama mkono wa Mungu ulikuwa umenyoshwa kuelekea chini toka mbinguni, hata ulimshika, na kumweka mahali ambapo daima hakuwa na papara tena kuondoka.”- D’Aubigne, History of the Reformation in Europe in theTime of Calvin, b. 9, sura ya 17. [GC 233.3; PK Aya ya 64]

**Kutishwa Na Maadui Wa Kuogofya**

Wakati huu hatari kubwa sana zikawa zimeizingira kazi ya Matengenezo ya Kanisa. Laana alizozitamka papa zilinguruma kama radi dhidi ya mji wa Geneva, na mataifa yenye nguvu na kutishia kuuangamiza. Ni kwa jinsi gani jiji hili dogo lingeweza kuupinga utawala wa ngazi wa upapa, wenye nguvu nyingi, ambao mara kwa nyingi ulikuwa umewalazimisha wafalme wadogo pamoja na wafalme wa himaya kubwa kuutii? Ni kwa jinsi gani ungeweza kusimama dhidi ya majeshi ya washindi wakuu wa dunia? [GC 234.1; PK Aya ya 65]

Katika Ulimwengu wote wa Ukristo, Uprotestanti ulihatarishwa na maadui zake wa kutisha na wenye kufadhaisha. Ushindi wa kwanza wa Matengenezo ukiwa umekwisha kupita, Roma ilikusanya nguvu mpya, ikitarajia kuangamiza kabisa Uprotestanti. Wakati huu chama au shirika la Majesuiti* likawa limeundwa, shirika katili mno, fidhuli, na likawa shirika lenye nguvu kuliko mabingwa watetezi wote wa upapa. Wakiwa wamejitenga na mshikamano

wowote na dunia au mapenzi na maslahi ya wanadamu, walikuwa hawana urafiki na mtu, akili na dhamiri zao vikiwa vimenyamazishwa kabisa kwa mapenzi ya asili aliyoumbwa nayo kila binadamu ili ayaonyeshe kwa mwanadamu mwezake (natural affection), hawa hawakujua kanuni nyingine yoyote, nao hawakuwa na mahusiano na mtu yoyote isipokuwa na shirika lao tu, na tena hawakutaka kuwa na wajibu mwingine bali ule wa kueneza na kupanua mamlaka yake. *(Tazama kiambatanisho)* Injili yake Kristo ilikuwa imewawezesha wafuasi wake kukabiliana na hatari ile na kustahimili mateso, kukatishwa tamaa, na baridi kali, njaa, uchovu, na umaskini, ili kuiinua juu bendera ya ile ya Kweli, huku wakikabiliana ana kwa ana na kitanda cha kutesea watu (rack), gereza la chini ya ardhi, na nguzo ya kuchomea watu moto. Ili kupambana na majeshi ya Wanamatengenezo na kuyashinda, Ujesuiti uliwahamasisha wafuasi wake ili wawe na ushabiki, yaani ushikiliaji sana wa mambo, usiotumia akili uliowawezesha kustahimili hatari kama hizo, na kuipinga nguvu ya Ukweli kwa kutumia silaha zote za madanganyo. Hakukuwa na uhalifu wowote kwao uliokuwa mkubwa mno kuufanya, hapakuwa na uongo wowote mbaya ambao wasingeweza kuusema, wala uigizaji wowote ambao wasingeweza kuufanya. Wakiwa wameapa kuishi maisha ya kimasikini, na unyenyekevu daima, lengo lao lililokusudiwa kabisa lilikuwa n kujipatia utajiri na madaraka, kujitolea kutumia muda wao wote kuuangusha Uprotestanti, na kuurejesha tena upya ukuu wa upapa duniani. **(Order of the Jesuits or Society of Jesus tafsiri yake ni Chama cha Yesu)* [GC 234.2; PK Aya ya 66]

Walipoonekana kama wanachama wa shirika hilo la Ujesuiti (Jesuit order), walivaa vazi la utakatifu, wakitembelea magereza na hospitali, wakiwahudimia wagonjwa na masikini, wakitangaza kwa ulimwengu kwamba wao wameiacha dunia, na kulibeba Jina takatifu la Yesu, ambaye alikwenda kila mahali akitenda wema. Lakini wakati wamelivaa vazi lile la nje lisilokuwa na lawama yoyote, makusudi yao ya moyoni ya liuhalifu na kimauaji mara nyingi yalikuwa yamefichwa sana kwa watu chini ya mwonekano huu wa unaopendeza kwa nje. Ilikuwa ni kanuni ya msingi ya shirika hilo kuwa mwisho (matokeo) unahalalisha njia zilizotumika. Kwa kanuni yao hiyo, matendo ya uongo, wizi, viapo vya udanganyifu, mauaji ya siri, hayakuwa mambo ya kusamehewa tu bali ya kusifiwa ikiwa yalilinda maslahi au ajenda ya kanisa. Chini ya vificho mbalimbali Majesuiti walijipenyeza katika ofisi za serikali, wakipanda vyeo hadi kuwa washauri wa wafalme (au Marais), na kuzipanga sera za mataifa. Walijigeuza na kuwa watumishi ili wafanye kazi ya upelelezi dhidi ya mabwana zao. Walianzisha vyuo kwa ajili ya watoto wa kiume wa wana wa wafalme, wakuu wa nchi na matajiri (malodi), na shule kwa ajili ya watu wa kawaida; na watoto wa wazazi wa Kiprotestanti walitekwa mawazoni kuziadhimisha taratibu/mapokeo ya kipapa. Utukufu wote wa nje na maonyesho ya ibada ya Kiroma yalitumika ili kuwafanya watu wachanganyikiwe, waduwazwe na kushikwa akili zao na ndipo wayanase mawazo ya watu hawa (watekewe), na kwa hivyo uhuru ambao wazazi

wao waliteseka sana ili kuupata kwa kumwaga damu yao, ulisalitiwa na wana wao. Majesuiti kwa muda mfupi walijitandaza katika bara lote la Ulaya, na kokote walipokwenda, palifuatiwa na uamsho au kufufuliwa kwa upapa (fuatilia historia). [GC 235.1; PK Aya ya 67]

Ili kuwapa nguvu kubwa zaidi, amri ya papa (bulla) ilitolewa ili kuanzisha tena Mahakama ya uchunguzi.* *(Tazama Kiambatisho)* Licha ya mahakama hiyo kuchukiwa na watu wengi kwa jumla, hata katika nchi za Kikatoliki, mahakama hiyo ya kuogofya sana [Inkwizisheni] ilianzishwa tena na watawala wa kipapa, na ukatili wa kuogofya sana usioweza kuvumilika ukaoneshwa wazi wakati wa mchana ulirudiwa tena katika magereza yake ya siri yaliyo chini ya ardhi. Katika nchi nyingi, maelfu kwa maelfu miongoni mwa maua ya taifa, wenye maisha safi na waungwana kabisa, wenye akili nyingi sana na wasomi mahiri, wachungaji wacha Mungu, waliojitoa wakfu kumtumikia Mungu, raia wenye bidii na stadi nyingi katika kufanya kazi na wazalendo, wanazuoni wenye akili nyingi sana, wanasanaa wenye talanta, mafundi wenye stadi za juu, walichinjwa au kulazimika kukimbia kwenda katika nchi zingine. [Inquisition or Holy Office = uchunguzi au Ofisi Takatifu]* [GC 235.2; PK Aya ya 68]

Hizo ndizo njia ambazo Roma ilikuwa imezitumia ili kuizima nuru ya Matengenezo, kuziondoa Biblia kutoka kwa watu, na kuurejesha ujinga na ushirikina wa Zama zile za Giza. Lakini chini ya mbaraka wa Mungu na kazi za watu wakuu na bora, ambao Mungu alikuwa amewainua kuchukua nafasi iliyoachwa na Luther, Uprotestanti haukuweza kuangushwa chini. Nguvu zake hazikupatikana kutokana na upendeleo wa wakuu wa nchi au silaha walizokuwa nazo. Nchi zile zilizokuwa ndogo kabisa, mataifa yaliyokuwa masikini na dhaifu kabisa, ndiyo yalikuwa ngome imara ya matengenezo. Ilikuwa ni jiji la Geneva ndogo katikati ya maadui wenye nguvu nyingi waliokuwa wanapanga mkakati wa kuangamiza; ilikuwa nchi ndogo ya Uholanzi, kwenye pwani ya mchanga katika bahari ya kaskazini, iliyopambana mieleka kwa nguvu dhidi ya udikteta wa Uhispania, ambao kwa wakati ule ulikuwa ufalme wenye maarufu na wenye utajiri mwingi sana; ilikuwa ni Sweden, nchi ndogo isiyo na rutuba yenye ukiwa na ukame, ambayo ilipata ushindi kwa ajili ya Matengenezo. [GC 235.3; PK Aya ya 69]

Kwa karibu miaka thelathini hivi Calvin alifanya kazi yake pale jijini Geneva, kwanza, alianzisha kanisa linalosimamia maadili ya Biblia, na baadaye aliyaendeleza Matengenezo ya Kanisa katika bara lote la Ulaya. Mwenendo wake kama kiongozi wa umma haukukosa kuwa na dosari, na mafundisho yake ya dini hayakukosa kuwa na makosa. Lakini yeye alikuwa ni chombo kilichotumika kutangazia zile Kweli ambazo zilikuwa na umuhimu wa pekee katika wakati wake, katika kudumisha kanuni za Uprotestanti dhidi ya lile wimbi la upapa lililokuwa linarudi tena kwa kasi, na katika kuhamasisha kwake juu ya kuishi

maisha ya sahili, yaliyo ya kawaida na yenye usafi, badala ya kuwa na kiburi na ufisadi vilivyokuwa vimejengwa chini ya mafundisho ya Kiroma. [GC 236.1; PK Aya ya 70]

Kutoka pale Geneva, machapisho na walimu walitoka nje kueneza mafundisho ya Matengenezo ya Kanisa. Mpaka hivi leo mahali pale ndipo wale wanaoteswa wa nchi zote wanakuja kupata mafundisho, mausia, na kutiwa moyo (amnesty- Mahakama na Koti kuu za haki za Binadamu zipo hapa). Jiji la Calvin likawa kimbilio la Wanamatengenezo waliokuwa wakisakwa katika Ulaya yote ya Magharibi. Wakikimbia kwenda mbali kwa ajili ya dhoruba za kutisha zilizoendelea kwa karne nyingi, wakimbizi hawa walikuja kwenye malango ya Geneva. Wakiwa wanakufa kwa njaa, wakiwa wamejeruhiwa, wakiwa wamepoteza nyumba zao pamoja na ndugu zao, walikaribishwa vizuri na kutunzwa kwa upendo; nao walipopata makazi yao hapa, walililetea jiji lililowapokea mibaraka kwa stadi zao, elimu yao, na uchaji Mungu wao. Wengi waliotafuta hifadhi pale walirudi katika nchi zao na kuendelea kuupinga ukatili wa Roma. John Knox, Mwanamatengenezo jasiri wa Scotland, Wapyuritani wa Kiingereza ambao hawakuwa wachache, Waprotestanti wa Uholanzi na wale wa Spain, Waprotestanti wa Ufaransa waitwao Huguenots, waliuchukua mwenge wa ile Kweli toka Geneva na kwenda nao kuangaza katika giza la nchi zao walikozaliwa [GC 236.2; PK Aya ya 71]

*Hierakia ni Uongozi wa Msururu wa amri uliobainishwa wazi kutoka ngazi za chini hadi za juu- Hierarchy

*(Mteule (elector) wa Kwanza ni yule kiongozi wa Ujerumani aliyemsaidia Luther na kumlinda kwenye matengenezo-Frederick)

*Ufafanuzi wa uchunguzi (inquisition)- ni mfululizo wa maswali au mahojiano haswa na chanzo rasmi. Mfano wa mahakama ya kuhukumu wazushi ulikuwa wakati kati ya 1232 na 1820, Angalia Historia kwa ufafanuzi wa ziada.

# SURA YA 13

# UHOLANZI NA SCANDINAVIA.

**(Mashujaa Wa Ile Kweli Kule Uholanzi Na Skandinavia Waleta Moto Wa Injili Ulioteketeza Makapi)**

Ufupisho: Wakati Martin Luther akifanya kazi ya Matengenezo Ujerumani, nuru iliaanza kuangaza Ulaya yote, na ndipo Matengenezo makuu yalianza. Menno Simmons aliipata injili kwa kushuhudia mtu kuuawa naye alikuwa mwanzilishi wa makanisa ya Mennonite na Amish (1531-1536), William Orange alisaidia nchi ya Uholanzi kumwabudu Mungu kwa Uhuru na Tausen, mwaka wa 1530 alisaidia kuleta Matengenezo Denmark. Olaf na Laurentius Petri walimpelekea mfalme wa Sweden injili na taifa zima likapokea Matengenezo mwaka 1527.

Katika nchi ya Uholanzi (Netherlands) ukatili na uonevu wa kipapa ulipelekea upinzani mkali mapema kabisa. Miaka mia saba kabla ya wakati wa Luther, Kiongozi wa kanisa la Kiroma alishtakiwa ili kuondolewa ofisini na maaskofu wawili bila kumwogopa, ambao, walipotumwa kule Rumi kama mabalozi, walikuwa wamepata habari za tabia halisi ya serikali ya Vatican la "holy see"* yaani mamlaka takatifu na wakampasha maneno haya: Mungu "amemweka malkia na mwenzi wake, yaani, kanisa lake, kuwa ruzuku bora, ya kutosha, na ya milele kwa familia Yake, kwa kutoa mahari Yake ambayo, wala haiharibiki au kupunguka, na kumpatia taji na fimbo ya kifalme ya milele;... mambo hayo yote ambayo hutenda kazi kukunufaisha wewe kama mtego wa mnyang'anyi. Unajiweka mwenyewe katika hekalu la Mungu; badala ya kuwa mchungaji, wewe umegeuka kuwa mbwa-mwitu kwa kondoo;..... unataka kutufanya sisi tuamini kwamba wewe ni askofu mkuu kuliko wote, lakini mwenendo wako ni ni wa katili mwonevu. Wakati ambapo wewe ulipaswa kuwa mtumishi wa watumishi, kama unavyojiita mwenyewe, wewe unapambana kuwa bwana wa mabwana.... Wewe ndiwe unazidharau za Mungu na unazifanya amri [kumi] za

Mungu zipate kudharauliwa na wengine.... Roho Mtakatifu Ndiye mjenzi wa makanisa yote kadiri ya upeo na miisho ya dunia.... Jiji la Mungu wetu, ambao sisi ni raia Wake, linapanuka na kufikia maeneo yote ya mbinguni; tena ni kubwa zaidi kuliko jiji, ambalo manabii watakatifu waliliita kuwa ni Babeli, ambalo hujifanyia maigizo kuwa ni mtakatifu au wa Kimungu, nao hujitapa wenyewe hadi kwenye Mbingu, na kujigamba eti hekima yake ni ya milele; na kwa kumalizia, ingawa pasipo sababu yoyote ya msingi, wewe unadai kwamba haujapata kukosea, na wala hauwezi kukosea kamwe." - Gerard Brandt, History of the Reformation in and About the Low Countries 1:6. [GC 237.1; PK Aya ya 1]

Wengine waliinuka toka karne hata karne na wakiurudia mwangi wa upinzani huu. Na waalimu wale wa awali, ambao walitembelea katika nchi mbali mbali, na wakijulikana kwa majina mbalimbali, walikuwa na tabia ya Wamishonari wa Vaudois (Kivodwa) au Wawaldensis, wakisambaza kila mahali maarifa ya injili, walipenya mpaka Uholanzi. Mafundisho yao ya dini yalienea kwa haraka sana. Biblia ya Kiwaldensia waliitafsiri kwa mtindo unaofanana kila fungu katika lugha ya Kidachi. Wakatangaza kwamba kulikuwa na manufaa makubwa yapatikanayo ndani yake; kwamba ilikuwa haina mizaha/futuhi, haina hadithi za uongo au hekaya, haina upuuzi, haina udanganyifu au hila bali ilikuwa ina Maneno ya Kweli; na ya kwamba, kwa kusema kweli ya moyoni, hapa na pale palikuwa na ganda gumu kutafuna, yaani mambo magumu kuyaelewa, lakini, iko hivyo ili kwamba mafuta yaliyomo ndani ya mifupa pamoja na utamu wa kile kilichokuwa chema, laini na kitakatifu vipate kugunduliwa kwa urahisi ndani yake." - Ibid. 1:14. Hivyo ndivyo walivyoandika marafiki wa imani ile ya kale katika karne ya kumi na mbili. [GC 238.1; PK Aya ya 2]

Sasa ndipo yalianza mateso ya Kiroma; lakini katikati ya yale matita ya kuni za kuchomea watu moto na mateso, waumini walizidi kuongezeka bila kutetereka, wakitangaza kwa ujasiri kwamba Biblia peke yake ndiyo mamlaka ya dini isiyokosea kamwe, na ya kwamba "mtu awaye yote asilazimishwe kuamini kwa kutumia nguvu, bali aweze kuongolewa kwa njia ya kuhubiriwa." - Martyn 2:87., gombo la 2, p. 87. [GC 238.2; PK Aya ya 3]

**Uholanzi Na Scandinavia**

Mafundisho ya Luther yalipata udongo mzuri unaofaa kule Uholanzi, na watu walio dhati na waaminifu waliinuka kule kuihubiri injili. Kutoka katika mojawapo ya majimbo ya Uholanzi alitokea Menno Simons. Akiwa ameelimishwa na kanisa la Katolikii la Roma, na kuwekwa wakfu kwa upadirisho, alikuwa mjinga kabisa kuhusu Biblia (hakujua lolote kuhusu Biblia), wala hakutaka kuisoma kwa kuogopa kushawishika na kuingia katika uzushi. Wakati mashaka yalipokuja juu yake kwa nguvu juu ya fundisho lile lisemalo kwamba mkate na mvinyo wa meza ya Bwana au Sakramenti hugeuka kabisa na kuwa mwili na damu ya Kristo halisi

(transubstantiation), alilichukulia kuwa ni jaribu lililotoka kwa Shetani, na kwa sala na toba alitafuta jinsi ya kuachana nalo kabisa mawazoni mwake; lakini bila mafanikio. Alijitahidi kunyamazisha sauti ya dhamiri iliyokuwa ikimshitaki ndani, kwa kujichanganya katika matukio ya uovu wa vileo, ubaradhifu na ngono pasipo kupata ahueni yoyote. Baada ya kupita muda fulani alivutwa kujifunza Agano Jipya, na hili, pamoja na mafundisho ya Luther, vilimfanya aikubali imani ya matengenezo. Muda mfupi tu baada ya hapo, alishuhudia mtu akikatwa kichwa na kuuawa kwa ajili ya kubatizwa mara ya pili katika kijiji jirani. Jambo hili lilimfanya aisome Biblia ili kujifunza juu ya ubatizo wa watoto wachanga. Hakuweza kupata ushahidi wowote wa ubatizo huo katika Maandiko, ila yeye aliona kwamba toba na imani kila mahali inatakiwa kama sharti la kupokea ubatizo. [GC 238.3; PK Aya ya 4]

Menno aliachana na Kanisa la Kiroma na kujitolea maisha yake yote kwa kuzifundisha zile Kweli alizokuwa amezipokea. Katika nchi zote mbili, Ujerumani na Uholanzi, kikundi cha mashabiki wa dini au itikadi kali isiyotumia busara walikuwa wamejitokeza, wakawa wanahubiri mafundisho ya kipuuzi na yenye kuwachochea watu kuiasi serikali, kutenda maovu ya ukatili, na kuvuruga amani na heshima, na kuchukua hatua za kutumia nguvu na kufanya maasi dhidi ya serikali. Menno aliona matokeo ya kutisha na yasiyoepukika ambayo vuguvugu zile zingeweza kuwahamasisha watu kufikia, naye kwa bidii nyingi alichukua hatua madhubuti kupinga mafundisho potofu pamoja na mipango ya hovyo, iliyojaa fujo na hila za watu wenye itikadi kali za kidini zisizotumia busara. Lakini, walikuwapo wengi waliokuwa wamepotoshwa na mashupavu hawa wa dini, ambao baadaye walikuwa wameyaacha mafundisho yao potofu yenye kuleta madhara; tena masalia wengi wa Wakristo wa zamani walikuwepo bado (vitukuu), matunda ya mafundisho ya Wawaldensia. Menno alifanya kazi miongoni mwa matabaka haya, kwa bidii kubwa (usongo) na mafanikio makubwa. [GC 239.1; PK Aya ya 5]

Kwa miaka ishirini na mitano alisafiri pamoja na mkewe na watoto wao, akistahimili shida nyingi na ufukara na kujinyima, na mara kwa mara, alihatirisha maisha yake. Alizunguka katika nchi ya Uholanzi na Ujerumani kaskazini, akifanya kazi yake kwa sehemu kubwa miongoni mwa matabaka ya watu wa hali ya chini, lakini akiwa na mvuto wenye nguvu miongoni mwa watu wengi wa sehemu mbalimbali. Akiwa na uwezo wa asili wa kuongea kwa ufasaha, ingawa alikuwa na elimu ndogo, alikuwa ni mtu mwenye uadilifu usioyumba, mwenye roho ya unyenyekevu, uungwana, na mpole kwa tabia, na mwenye utauwa wa dhati utokao moyoni, akionyesha kupitia maisha yake mwenyewe kanuni zile alizozifundisha jambo ambalo lilivuta usikivu na kuaminiwa na watu. Wafuasi wake walitawanywa, na kunyanyaswa. Walipata mateso mengi sana kwa kukutana na changamoto za usumbufu kutoka kwenye kikundi cha watu wenye itikadi kali zisizo na busara ambao walikuwa ni wafuasi wa Munsterites. Hata

hivyo wengi wao waliongolewa chini ya utendaji wake wa kazi. [GC 239.2; PK Aya ya 6]

Hakuna mahali ambako mafundisho ya Matengenezo ya Kanisa yalipokelewa kwa furaha kwa jumla na watu wengi zaidi kuliko katika nchi ya Uholanzi. Ni katika nchi chache ndiyo ambapo wafuasi wa mafundisho ya Matengenezo walistahimili mateso ya kutisha zaidi kuliko katika nchi ya Uholanzi. Katika nchi ya Ujerumani, Charles V alikuwa ameyapiga marufuku Matengenezo ya Kanisa, tena angefurahi sana kuwaleta wafuasi wake wote kwenye mti wa kuchomea watu moto; lakini wakuu wa nchi walisimama kidete kama kizuizi dhidi ya ukatili wake. Katika nchi ya Uholanzi mfalme alikuwa na nguvu zaidi, na amri zake za kuwatesa Wanamatengenezo zilitolewa kwa kufuatana, moja baada ya nyingine kwa haraka haraka. Kusoma Biblia, kuisikiliza au kuihubiri, au hata kuizungumzia, ilikuwa ni kujitakia adhabu ya kifo kwa kuchomwa moto kwenye mti wa kuchomea watu. Kumwomba Mungu faraghani/sirini, kukataa kuisujudu sanamu, au kuimba Zaburi, adhabu yake ilikuwa kifo. Hata wale waliokana makosa yao kwa kiapo, endapo walikuwa wanaume, walihukumiwa kufa kwa upanga; endapo walikuwa wanawake, walizikwa wakiwa hai. Maelfu wakaangamia chini ya utawala wa Charles na Philip wa pili (II) [GC 239.3; PK Aya ya 7]

Wakati mmoja familia nzima ililetwa mbele ya waendesha Mahakama ya uchunguzi ya Majesuiti (Inquisitors), wakishitakiwa kwa kutohudhuria Misa na kuabudu nyumbani mwao. Mwana wao mdogo kabisa alipohojiwa kuhudu ibada zao za faraghani alijibu hivi: "Tunapiga magoti, na kuomba kwamba Mungu aangazie akili (mioyo) zetu na kutusamehe dhambi zetu; tunamwombea mfalme wetu ili utawala wake upate kufanikiwa na maisha yake yapate kuwa na furaha; tunawaombea mahakimu wetu ili Mungu apate kuwalinda na kuwatunza." - Wylie, b. 18, sura ya 6. Baadhi ya majaji waliguswa sana moyoni mwao, lakini, hata hivyo, baba na mmojawapo wa watoto wake walihukumiwa kuchomwa moto kwenye mti wa kuchomea. [GC 240.1; PK Aya ya 8]

**Imani Ya Wafia Dini**

Ghadhabu ya watesi ililingana na imani ya wafia dini. Si wanaume tu, bali na wanawake, pamoja na wasichana wadogo dhaifu, hawa walionyesha ujasiri wao usiotetereka au kuchoka. "Wake walisimama kando ya mti wa kuwachomea moto waume zao, na wakati mume alikuwa akiungua moto waliweza kunong'ona maneno ya faraja au kuimba Zaburi ili kumtia moyo." "Mabinti wadogo waliweza kulala katika makaburi yao wakiwa hai kana kwamba walikuwa wakiingia katika vyumba vyao vya kulala kwa usingizi wa kila usiku, au walikwenda kwenye kiunzi cha kunyongea na kwenye moto, wakiwa wamevalia nguo zao nzuri kabisa, kana

kwamba walikuwa wanaenda kwenye harusi zao." -Ibid., b. 18, sura ya 6. [GC 240.2; PK Aya ya 9]

Kama ilivyokuwa katika siku ambazo upagani ulipamba moto na kujaribu kuiangamiza injili, damu ya Wakristo ilikuwa mbegu. (Angalia Tertullian, Apology, Ibara ya 50.) Mateso yalichochea ongezeko la idadi ya mashahidi kwa ajili ya Ukweli. Mwaka baada ya mwaka mfalme, aling'atwa na wenda wazimu kwa uchungu aliokuwa nao kwa kuona msimamo usioyumba au usiokubali kushindwa wa watu wake, naye alihimiza kazi yake ile ya ukatili iendelee; lakini ikawa ni kazi bure tu. Chini ya mkuu (Lord) William of Orange, hatimaye Mapinduzi yalileta uhuru wa kumwabudu Mungu katika Uholanzi. [GC 240.3; PK Aya ya 10]

Katika milima ile ya Piedmont, katika tambarare za Ufaransa na katika sehemu za pwani za Uholanzi, maendeleo ya injili yalitiwa alama ya damu ya wanafunzi wake. Lakini katika nchi za kaskazini iliingia kwa amani. Wanafunzi pale Wittenberg, walipokuwa wakirudi majumbani mwao, walibeba imani ya matengenezo kule Scandinavia.* Machapisho ya maandishi ya Luther pia yalieneza nuru. Watu sahili wa kaskazini, wazoefu wa kazi ngumu na taabu, waliachana na ufisadi, ushirikina na majivuno ya kanisa la Roma, nao kwa furaha wakazikaribisha zile Kweli safi, nyenyekevu, na sahili zenye kubadilisha maisha na kuleta uzima kutoka katika Biblia *(Sweden, Norway, Denmark, Finland, Greenland na Iceland). [GC 240.4; PK Aya ya 11]

**Mwanamatengenezo Wa Denmark**

Tausen, "Mwanamatengenezo wa Denmark," alikuwa mtoto wa kiume wa mkulima mdogo. Kijana huyu alionyesha mapema kuwa na akili mahiri, yenye utendaji wenye nguvu; alikuwa na kiu ya elimu; lakini jambo hili halikuwezekana kutokana na hali ya wazazi wake, hivyo, aliingia katika nyumba ya watawa. Hapa usafi wa maisha yake, Pamoja uadilifu na bidii yake katika kazi vilimfanya kupendwa na wakuu wake. Mtihani ulionyesha kuwa ana talanta zinazoashiria kuwa siku za usoni angeweza kulinufaisha kanisa kwa utumishi wake. Iliazimiwa kuwa apewe elimu katika mojawapo ya vyuo vikuu vya Ujerumani au Uholanzi. Mwanafunzi huyu kijana aliruhusiwa kujichagulia mwenyewe shule aliyoipenda kwa sharti moja, kuwa ni lazima asiende kule kusoma kule Wittenberg. Msomi huyu wa kanisa hakupaswa kuhatarishwa na sumu ya uzushi. Hivyo ndivyo watawa walivyosema. [GC 241.1; PK Aya ya 12]

Tausen alikwenda Cologne, Ujerumani, mahali ambapo nyakati hizo, kama ilivyo sasa, ni ngome mojawapo imara na kubwa ya Uroma (Romanism). Punde akawa amechukizwa na mafundisho ya sri na mafumbo yasiyoeleweka ya walimu wa chuo kile (mysticisms). Karibu na wakati huo huo aliyapata maandishi ya Luther. Aliyasoma kwa mshangao na furaha, na kutamani kuyafaidi zaidi mafunzo

ya Mwanamatengenezo Luther mbashara. Lakini ili kufanya hivyo ilibidi ahatarishe stahiki yake ya kufadhiliwa masomo (sponsa), kwani jambo hilo lingemchukiza mkuu wake wa nyumba ya watawa. Alifanya uamuzi wake punde baada ya pale, na alisajiliwa kama mwanafunzi katika chuo kikuu cha Wittenberg. [GC 241.2; PK Aya ya 13]

Aliporudi kule Denmark, alikwenda tena kwenye nyumba yake ya watawa. Hakuna hata mmoja Mpaka wakati huu aliyekuwa amemshuku kuwa sasa ni mtu wa Imani ya Kilutheri; naye hakuifichua siri yake kwao, bali alijitahidi kuwaongoza katika imani safi zaidi na maisha matakatifu zaidi bila ya kuamsha chuki kutoka kwa wenzake. Aliifungua Biblia na kueleza maana yake ya kweli, na hatimaye aliwahubiri Kristo kuwa Ndiye njia ya kuhesabiwa haki kwa mwenye dhambi na tumaini pekee la wokovu. Ghadhabu ya mkuu wake katika nyumba ya watawa ilikuwa kali sana, kwani alikuwa amejenga matumaini makubwa sana juu yake, kuwa atakuwa mlinzi na mtetezi shujaa wa Roma. Aliondolewa mara moja katika nyumba ya watawa na kupelekwa kwingine, kisha akafungiwa katika gereza la chumba kidogo cha peke yake, chini ya usimamizi mkali. [GC 241.3; PK Aya ya 14]

Walezi na walinzi wake wapya walipatwa na hofu, kwa kuwa watawa kadhaa walijitangaza wenyewe kuwa wameongoka na kuwa walikuwa wameupokea Uprotestanti. Kupitia katika zile nondo za chumba chake kidogo cha gereza, Tausen alikuwa amefanya mawasiliano na wenzake mafundisho ya Ukweli. Kama wale mababa wa Kidenishi (Denmark) wangekuwa wamezijua mbinu za kanisa la Roma za kuushughulikia uzushi, basi, sauti ya Tausen isingeweza kusikika tena kamwe; lakini badala ya wao kumfungia kaburini katika mojawapo ya magereza ya chini ya ardhi, walimfukuza kutoka katika nyumba ya watawa peke yake. Basi sasa wakawa hawana uwezo wowote juu yake. Amri ya mfalme, iliyokuwa imetolewa hivi karibuni, ilitoa ulinzi kwa waalimu wa mafundisho yale mapya ya Matengenezo. Tausen akaanza kuhubiri. Makanisa yakafungua milango yake kumkaribisha, na watu walifurika kumsikiliza. Wengine walikuwa wakihubiri Neno la Mungu pia. Agano Jipya, ambalo lilikuwa limetafsiriwa katika lugha ya Kidenish lilisambazwa sana mahali pengi. Jitihada iliyofanywa na watetezi wa papa kutaka kuipindulia mbali kazi ile zikasababisha kupanuliwa kwake na kuieneza, na muda si mrefu baada ya pale, Denmark ilitangaza kuwa ilikuwa imekubali kuipokea imani ya Matengenezo. [GC 242.1; PK Aya ya 15]

**Maendeleo Kule Sweden**

Katika nchi ya Sweden pia, vijana wa kiume ambao walikuwa wamekunywa maji kutoka kwenye chemchemi ya maji ya uzima ya Mungu kutoka Wittenberg walibeba maji ya uzima na kuwapelekea watu wa nchi yao hayo. Viongozi wawili wa Kiswidi katika yale Matengenezo walikuwa Olaf and Laurentius Petri, wana

wa mhunzi mmoja aliyeishi Orebro, walijifunza chini ya Luther na Melanchthon, na zile Kweli walizojifunza wakawa wanawafundisha wengine kwa bidii. Kama Mwanamatengenezo mkuu Luther, Olaf aliwagusa mioyo watu kwa bidii na ufasaha wake, wakati Laurentius kama Melanchthon, alikuwa mtu mtulivu, mkimya, msomi, mwenye kutafakari, na kucheua mambo. Wote wawili walikuwa wacha Mungu wa dhati na motomoto, nao walikuwa na uwezo mkubwa katika taaluma ya kitheolojia, wenye ujasiri usioterereka au kuwa na woga katika kuieneza Ukweli. Upinzani wa wafuasi wa papa haukukosekana kuwapo. Kasisi mmoja wa Kikatoliki aliwachochea watu waliokuwa wajinga na washirikina. Olaf Petri mara kwa mara alishambuliwa na kundi la watu hao wabaya, na katika matukio mbalimbali kadhaa aliponea chupuchupu kupoteza maisha yake. Walakini, Wanamatengenezo hawa wawili walipata upendeleo na ulinzi kutoka kwa mfalme wao. [GC 242.2; PK Aya ya 16]

Chini ya utawala wa Kanisa la Roma, watu walikuwa wamezamishwa katika lindi la umaskini na kukanyagwa-kanyagwa chini kwa kuonewa. Walikuwa maskini wa kukosa Maandiko, nao wakiwa na dini ya ishara na sherehe tu, ambayo haikupelekea nuru yoyote akilini mwao, walikuwa wakirudi kwenye imani zao za kishirikina na desturi zao za kipagani/kishenzi walizozipata kutoka kwa mababu zao makafiri na waabudu mizimu. Taifa likagawanyika katika makundi yanayoshindana, na migogoro yao ya daima iliongeza matatizo na huzuni kwa wote. Mfalme alidhamiria kuleta matengenezo serikalini na kanisani, naye aliwakaribisha wasaidizi wake hawa wenye uwezo katika vita yake dhidi ya Roma. [GC 243.1; PK Aya ya 17]

Akiwa mbele ya mfalme na viongozi wa ngazi za juu wa Uswidi, Olaf Petri kwa uwezo mkubwa aliyatetea mafundisho ya imani ya matengenezo dhidi watetezi bingwa wa Roma. Alitangaza kwamba mafundisho ya mapadri, yanapaswa kupokelewa pale tu yanapopatana au kukubaliana na Maandiko, akasisitiza kwamba mafundisho muhimu ya imani yametolewa katika Biblia kwa njia iliyo wazi na sahili, ili watu wote waweze kuyaelewa. Kristo alisema, "Mafunzo Yangu si Yangu Mimi, ila ni Yake Yeye aliyenituma." (Yohana 7:16); na Paulo alitangaza kuwa kama “sisi au malaika wa mbinguni atawahubiri ninyi injili yoyote isipokuwa hiyo tuliyowahubiri, na alaaniwe. (Wagalatia 1: 8). "Je, iweje basi!" alisema Mwanamatengenezo huyo, "watu wengine wajipe mamlaka ya kutunga sheria zao kama wapendavyo na kuwalazimisha wengine kuzitii kama mambo muhimu kwa ajili ya wokovu?" - Wylie, b. 10, sura ya 4. Alionyesha kuwa amri zile zinazotolewa na kanisa hazina mamlaka yoyote ikiwa zinapingana na amri za Mungu, kisha akaitetea ile kanuni kuu ya Uprotestanti isemayo kwamba “Biblia na Biblia peke yake” ndiyo kanuni ya imani na matendo (Sola Scriptura). [GC 243.2; PK Aya ya 18]

Shindano hili, ingawa lilifanyika juu ya jukwaa lililojificha kabisa, kwa kiasi fulani, linatuonyesha sisi "aina ya watu waliojiunga kuwa askari katika jeshi la Wanamatengenezo. Hawakuwa wajinga tu, yaani watu wasiojua kusoma na kuandika, watu wapendao kujiundia madhehebu yao na kubagua wengine, wabishi na wapiga mdomo au makelele mengi tu - hasha, walikuwa tofauti kabisa na kitu kama hicho; hawa walikuwa watu waliokuwa wamejifunza Neno la Mungu, na kujua jinsi ya kutumia vizuri silaha ambazo Biblia, kama ghala ya silaha inaweza kutoa. Kwa habari ya elimu au ujuzi wao, walikuwa wamekwenda mbele sana kuliko Zama zao. Sisi tunapoelekeza umakini wetu wote kwenye vituo vile vilivyong'aa vya taaluma vya Wittenberg na Zurich, na vya majina mashuhuri yenye nyadhifa kama ya akina Luther na Melanchthon, Zwingli na Oecolampadius (Okolampadio), tunajikuta tuko tayari kuambiwa kwamba hao ndio walikuwa viongozi wa vuguvugu za Matengenezo ya Kanisa, nasi tungetarajia kuona uwezo na mafanikio makubwa waliyopata; lakini watu husema kwamba wale waliokuwa chini yao hawakuwa na uwezo kama wao. Ndipo sisi tunageukia kule Sweden, maeneo ambayo yalikuwa hayajulikani, ila ambako yalitokea mambo makuu, na majina yale madogo ya Olaf na Laurentius Petri yanaletwa - kutoka kwa walimu kwenda kwa wanafunzi wao - Je, tunakuta nini?……Wasomi na wanatheolojia; watu walioumudu na kuulewa kabisa mfumo mzima wa Ukweli wa injili, na ambao wanawashinda kirahisi wanafalsafa wa dhana mbalimbali danganyifu na waheshimiwa wa Roma." -Ibid., b. 10, sura ya 4. [GC 243.3; PK Aya ya 19]

### Sweden Yajitangaza Kuwa Imepokea Matengenezo Ya Kanisa

Kama matokeo ya mdahalo huu, mfalme wa Uswidi aliipokea imani ya Matengenezo, na muda si mrefu baada ya pale Bunge lilitoa tangazo kuunga mkono imani ya Matengenezo. Agano Jipya lilikuwa limetafsiriwa na Olaf Petri katika lugha ya Kiswidi, na kwa matamanio ya mfalme, ndugu hawa wawili walipewa jukumu la kuitafsiri Biblia nzima. Hivyo kwa mara ya kwanza watu wa Sweden walilipokea Neno la Mungu katika lugha yao wenyewe. Baraza Kuu la Taifa liliamuru kwamba katika ufalme wote, wachungaji wayafafanue Maandiko na watoto mashuleni wafundishwe kuisoma Biblia. [GC 244.1; PK Aya ya 20]

Taratibu, lakini kwa uhakika, nuru ile yenye baraka ya injili ikalifukuzilia mbali lile giza la ujinga na ushirikina. Likiwa limekombolewa kutoka katika udikteta na unyanyasaji wa Kiroma, taifa hili likajipatia nguvu nyingi na utukufu, ambao lilikuwa halijaupata kamwe katika siku zake za nyuma. Sweden ikawa ni ngome mojawapo kuu ya Uprotestanti. Karne moja baadaye, katika wakati wa hatari kubwa mno kuliko wakati mwingine wowote, nchi hii ndogo na ambayo mpaka wakati ule ilikuwa haina nguvu - yaani, taifa peke yake kule Ulaya lililothubutu kutoa msaada - lilikuja kuikomboa Ujerumani katika pambano lake la kutisha sana la Vita yake ya Miaka Thelathini (Thirty Years War). Ulaya yote ya

kaskazini ilionekana kana kwamba ilikuwa karibu sana kuletwa chini ya udikteta na ukatili wa Roma. Yalikuwa ni majeshi ya Sweden yaliyoiwezesha Ujerumani kugeuzia mbali mkondo wa mafanikio ya upapa, na kuzishawishi dini zingine kuivumilia imani ile ya Waprotestanti, - yaani, ya Wakalvini (Calvinists) na Walutheri, - na kurudisha uhuru wa dhamiri katika nchi zile zilizokuwa zimeyapokea Matengenezo yale ya Kanisa (uhuru wa mtu kuweza kumwabudu Mungu kama dhamiri yake itakavyo). [GC 244.2; PK Aya ya 21]

*Holy see au Kiti Kitakatifu-Holy See ni jina walilojipa serikali ya Kanisa Katoliki la Roma, ambalo linaongozwa na papa kama askofu wa Roma. Mamlaka ya Holy See inaenea juu ya Wakatoliki ulimwenguni kote. Tangu 1929 mamlaka hiyo imekuwa ikiishi katika Jiji la Vatikani.

# SURA YA 14

# WANAMATENGENEZO WA BAADAYE WA UINGEREZA

**(Kweli Yasonga Mbele Katika Visiwa Vya Uingereza Na Wingu La Mashahidi)**

Ufupisho: Siku moja Tyndale alimwambia kiongozi wa kanisa la Roma "Ikiwa Mungu atayanusuru maisha yangu, nitahakikisha hata yule kijana mdogo anayelima kwa jembe la plau anajua Maandiko kuliko wewe Kiongozi wa Kiroho" Hili lilifanikiwa, na alichapisha Biblia ya kwanza ya Kingereza, iitwayo Tyndale Bible 1536, ijapokuwa alisalitiwa na rafikiye na kuchomwa moto mwaka huo huo. King James Bible ina asilimia 90% ya kazi yake. Mwaka 1531 Januari Mfalme Henry VIII aliachana na Roma, japo mateso yaliendelea kwa kiasi fulani. Mwaka 1660-1675 John Bunyan aliandika kitabu chake mashuhuri cha Pilgrims Progress au Safari ya Mkristo akiwa gerezani, ni kitabu cha pili kwa kuuzika kando na Biblia nacho kina filamu yake mtandaoni. Wanamatengenezo wengine ni George Whitfield wa mwaka 1735 aliyehubiri kwa watu laki moja bila kipaza sauti, John na Charles Wesley walihubiri miaka ya 1738. Charles aliandika Tenzi 6000, na John alitembea kwa farasi maili 250,000 kupeleka injili, wazazi wao walikuwa na watoto 19 waliojihusisha na injili. John Knox mtu shujaa wa Scotland, alifanya maombezi haya "Bwana nipe Scotland au Nife." Aliishi kuona nchi yake ikipokea

Imani ya Matengenezo, japo wengi waliuawa kabla yake na viongozi, mwishowe Mary malkia wa Scotland akawa mfuasi wa Matengenezo.

Wakati Luther alipokuwa akiifungua wazi Biblia iliyokuwa imefungwa kwa watu wa Ujerumani, Tyndale alikuwa amesukumwa na Roho wa Mungu kufanya jambo hilo hilo katika nchi ya Uingereza. Biblia ya Wycliffe ilikuwa imetafsiriwa kutoka katika tafsiri ya maandishi ya Kilatini, ambayo ilikuwa na makosa mengi. Biblia hii ilikuwa haijapata kuchapishwa kamwe na bei ya nakala za muswada, zilizokuwa zimeandikwa kwa mkono (manuscript) na gharama yake ilikuwa kubwa mno kiasi kwamba watu wachache sana, yaani matajiri au wakuu pekee, ndiyo walioweza kuinunua na zaidi ya hayo, kwasababu ya kanisa kuipiga marufuku kwa zuio kali, usambazaji wa Biblia hiyo ulikuwa finyu sana. Katika mwaka 1516, kabla ya kuonekana kwa hoja za Luther (Hoja 95), Erasmus alikuwa amechapisha toleo lake la Kigiriki/Kiyunani na la Kilatini la Agano Jipya. Sasa, kwa mara ya kwanza Neno la Mungu likawa limechapishwa Katika lugha ya asili (Agano Jipya liliandikwa kwa Kigiriki). Katika kazi hii makosa mengi ya matoleo ya nyuma yalirekebishwa, na maana yake ya kimantiki ilitolewa kwa wazi zaidi. Jambo hili likafanya wengi miongoni mwa matabaka ya wasomi kuwa na uelewa bora zaidi wa Ukweli na kuipa hamasa mpya kazi ya matengenezo. Lakini watu wa kawaida kwa kiasi kikubwa bado walikuwa wamenyimwa kupata Neno la Mungu. Tyndale ndiye aliyekamilisha kazi ya Wycliffe katika kuwapatia wananchi wenzake Biblia. [GC 245.1; PK Aya ya 1]

Akiwa mwanafunzi mwenye bidii katika kuutafuta Ukweli kwa dhati, alikuwa ameipokea Injili kutoka katika Agano Jipya la Kigiriki la Erasmus. Alihubiri ushuhuda wa imani yake bila hofu, alisisitiza kwamba, mafundisho yote ya dini sharti yapimwe kwa Maandiko. Na kuhusu dai la upapa kwamba kanisa lao ndio lilikuwa limepewa Biblia na kwamba kanisa lao pekee ndilo lina mamlaka ya kuifafanua, Tyndale alijibu:"Je, wewe wamjua ni nani aliyewafundisha tai kutafuta mawindo yao? Naam, Mungu Yule Yule huwafundisha watoto Wake wenye njaa kumpata Baba yao katika Neno Lake. Mbali na ninyi kutotupatia sisi hayo Maandiko, ninyi ndiyo mlioyaficha Maandiko ili sisi tusiyaone; Ni ninyi mnaowachoma moto wale wanayoyafundisha Maandiko, na kama mngelikuwa na uwezo, mngeweza kuyachoma moto Maandiko yenyewe"-D'aubigne, History of the Reformation of the Sixteenth Century, b.18, sur.4. [GC 245.2; PK Aya ya 2]

Mahubiri ya Tyndale yaliamsha hamu kubwa ndani ya watu wengi; wengi Waliukubali Ukweli lakini mapadri walikuwa macho, na mara tu alipokuwa akiondoka kwenye eneo moja, waliingia pale na kwa vitisho vyao na taarifa zao za uongo walijitahidi kuiharibu kazi yake. Mara nyingi waliweza kufanikiwa. "Ni nini cha kufanya? "Alisema. "Wakati Mimi ninapokuwa nikipanda katika sehemu moja, adui zangu wanalipa kisasi kwa kuharibu shamba nililoacha, mimi siwezi kuwa kila mahali, Oh jamani! Kama Wakristo wangepata Maandiko Matakatifu

katika lugha yao wenyewe, wangeweza wao wenyewe kuwakabili hawa waalimu wa uongo. Bila Biblia haiwezekani kuwaimarisha washiriki wa kawaida, yaani walei katika Ukweli, "-Ibid.,b.18,sur.4. [GC 246.1; PK Aya ya 3]

Kusudi jipya likawa akilini mwake, “ilikuwa ni katika lugha ile ya Israeli." alisema, "Zile Zaburi ziliwezwa kuimbwa kwenye Hekalu la Yehova; na Je, Agano Jipya halipaswi kuzungumza nasi katika lugha ya Kingereza miongoni mwetu?.....Je, kanisa linapaswa kuwa na nuru pungufu mchana kuliko wakati ule wa mapambazuko?... Ni lazima Wakristo wasome Agano Jipya katika Lugha zao za asili (waliyozaliwa nayo). "Madaktari wa falsafa na Walimu wa Kanisa walikuwa hawakubaliani miongoni mwao wenyewe. Ni kwa njia ya Biblia pekee wanadamu wangeweza kuujua Ukweli. "Mmoja anamwunga mkono daktari huyu wa falsafa, mwingine yule, yaani mmoja anamfuata msomi huyu wa theolojia, mwingine anamfuata msomi yule..... Sasa, kila mwandishi miongoni mwa hao humpinga yule mwingine. Twawezaje basi, kujua ni nani asemaye Ukweli na yule asemaye uongo?.... Kwa njia gani?... hakika ni kwa njia ya Neno la Mungu.”- Ibid.,b.18, sur. 4. [GC 246.2; PK Aya ya 4]

Haikuchukua muda mrefu baada ya pale ambapo msomi mmoja wa kikatoliki, daktari wa falsafa (theolojia), alipoanza mahojiano naye kwa kusema kwa nguvu: "Ni heri kwetu sisi kutokuwa na amri za Mungu kuliko kutokuwa na zile za papa." Tyndale alijibu: " Siafikiani na papa na sheria zake zote; na ikiwa Mungu atayahifadhi maisha yangu, kabla ya miaka mingi kupita nitamfanya mvulana anayelima kwa jembe la plau la kukokotwa na ng’ombe ayajue Maandiko kuliko wewe unavyojua.”- Anderson, Annals of the English Bible, ukurasa wa 19. [GC 246.3; PK Aya ya 5]

**Agano Jipya La Kingereza Lakamilika**

Kusudi lile ambalo alikuwa ameanza kulithamini na kulifikiria, la kuwapatia watu Maandiko ya Agano Jipya katika lugha yao wenyewe, likawa limethibithika sasa, na mara moja alijituma kwa kuanza kuifanya ile kazi yeye mwenyewe. Akiwa amefukuzwa kutoka nyumbani kwake kwasababu ya mateso, alikwenda hadi jijini London na huko kwa muda fulani aliendelea na kazi yake bila usumbufu. Lakini kwa mara nyingine vurumai na ukatili wa watetezi wa upapa vilimlazimisha kukimbia tena. Uingereza yote ikaonekana kana kwamba imefunga mlango dhidi yake naye, naye akaazimu kutafuta hifadhi kule Ujerumani. Hapa alianza kuchapisha Agano Jipya la Kiingereza. Kazi yake ilisimamishwa mara mbili kazi; lakini alipozuiliwa kuchapisha katika jiji moja, alienda katika mji mwingine. Hatimaye aliweza kuelekea Worms, ambapo miaka michache kabla, Luther alikuwa ameitetea injili mbele ya Baraza Kuu la kitaifa (Diet of Worms). Katika mji huo wa zamani kulikuwa na marafiki wengi wa Matengenezo na Tyndale aliendelea na kazi yake pale bila kizuizi. Muda si mrefu, nakala elfu tatu

za Agano Jipya zikawa zimekwisha kuchapishwa na toleo jingine lilifuata ndani ya mwaka ule ule. [GC 246.4; PK Aya ya 6]

Kwa moyo mkuu na ustahimilivu mkubwa aliendelea na kazi yake. Licha ya mamlaka ya Kiingereza kuzilinda vikali sana bandari zao. Neno la Mungu kwa njia mbalimbali lilisafirishwa kwa siri hadi jijini London na kutoka pale likaenezwa katika nchi nzima. Wafuasi wa papa walijaribu kuizuia ile Kweli, lakini hawakupata mafanikio. Askofu wa Durham wakati mmoja alinunua Biblia zote kutoka kwa duka la muuza vitabu, aliyekuwa rafiki yake Tyndale kwa kusudi la kuziteketeza, akidhani kwamba jambo hilo lingesaidia kuizuia kazi hiyo. Lakini Kinyume chake, fedha iliyopatikana kwa njia hiyo, zilitumiwa kwa ajili ya kununua malighafi kwa ajili ya toleo jipya na bora zaidi, ambalo, kama isingelikuwa tukio lile isingewezakana. Wakati Tyndale baadaye alipokamatwa na kuwa mfungwa gerezani, alipewa fursa ya kuachiliwa huru kwa sharti la kuwajulisha majina ya wale waliomsaidia kupata fedha za kuchapisha Biblia zake. Alijibu kuwa askofu wa Durham alikuwa ametoa msaada mkubwa zaidi kuliko mtu mwingine yeyote; maana kwa kumlipa pesa nyingi kwa ajili ya vitabu vilivyokuwa vimebaki mkononi, alikuwa amemwezesha kuendelea mbele kwa ujasiri mkubwa zaidi. [GC 247.1; PK Aya ya 7]

Tyndale alisalitiwa na kuingia mikononi mwa adui zake, na kwa kipindi kimoja aliteseka gerezani kwa kifungo cha miezi mingi. Hatimaye akashuhudia Imani yake kwa kifo cha mfia dini; lakini silaha zile ambazo alizokuwa ameziandaa tayari ziliwawezesha askari wengine kupigana vita katika karne zote hata kuufikia wakati wetu tulio nao sasa. [GC 247.2; PK Aya ya 8]

**Viongozi Wenye Bidii Na Utauwa Wajitokeza**

Latimer alihubiri kutoka mimbarini kwamba Biblia inapaswa kusomwa katika lugha za watu. Mwasisi wa Maandiko Matakatifu, alisema ni "Yeye Mungu Mwenyewe; na "Maandiko haya yanashiriki nguvu na umilele ule ule alio nao Mwasisi Wake. Hakuna mfalme yoyote, mkuu wa dola, Hakimu wala Mtawala…..ambaye asiyehusika katika kulitii.... Wote wanawajibika kulitii Neno Lake Takatifu". "Hebu, sisi tusitembee kando katika njia zetu ndogo ndogo za pembeni bali tuliruhusu Neno la Mungu lituongoze sisi: Hebu na tuache kuifuata--mienendo ya mababu zetu waliotangulia, wala tusiyafuate yale waliyofanya wao, bali tuyaangalie yale waliyopaswa kuyatenda."-- Hugh Latimer," Hubiri la Kwanza Lililohubiriwa Mbele ya Mfalme Edward wa VI." [GC 248.1; PK Aya ya 9]

Barnes na Frith, marafiki waaminifu wa Tyndale, waliinuka ili kuutetea Ukweli. Ridleys na Cranmer walifuata. Viongozi hawa katika Matengenezo ya Uingereza walikuwa ni watu wasomi sana na wengi wao walikuwa wamepewa heshima ya juu sana kwa juhudi na uchaji wa Mungu wao miongoni mwa wanajumuiya wa Kiroma. Upinzani wao kwa upapa ulikuwa matokeo ya ugunduzi

wa makosa yaliyofanywa na lile jimbo takatifu liitwalo “holy see."* Kuzifahamu kwao siri za Babeli kuliwapa mamlaka kubwa walipotoa ushuhuda dhidi yake. [GC 248.2; PK Aya ya 10]

**Swali La Ajabu**

"Sasa ningependa kuuliza swali la ajabu," alisema Latimer. "Ni Askofu gani au kasisi yupi aliye mwenye bidii zaidi katika nchi nzima ya Uingereza ..... Ninaona ninyi mnasikiliza kwa hamu kubwa na kungojea kusikika mimi nikimtaja...... Nitawaambia: ni Ibilisi. Yeye kamwe hajawahi kutoka nje ya Jimbo lake; mwiteni wakati wowote mnapomtaka, yeye daima yupo nyumbani mwake;... daima anaendesha jembe lake la kukokotwa na ng’ombe.... Kamwe hamuwezi kumkuta akikaa kivivu bila kazi, mimi nawahakikishieni hilo.... Mahali pale akaapo huyo Ibilisi,... pale hakuna vitabu na badala yake kuna mishumaa iliyoinuliwa juu; Biblia zimeondolewa mbali, badala yake kuna shanga (watu hutumia kusalia); nuru ya injili imeondolewa mbali, badala yake kuna nuru ya mishumaa, naam, nyakati za mchana; Msalaba wa Kristo umewekwa chini:..... pochi ya kukusanyia fedha za toharani/purgatori ipo juu;... hakuna kuwavika nguo walio uchi, maskini, na wasiojiweza wowote, badala yake kuna kuabudu sanamu zilizosheheni mapambo, shea za hisa na vito kwa uchangamfu, vitu visivyokuwa na uhai; mapokeo na sheria ya mwanadamu vimeinuliwa juu, mapokeo na Neno Lake Mungu takatifu sana vimeshushwa chini.... Laiti kama maaskofu wetu wangekuwa na bidii nyingi katika kupanda mbegu ya nafaka njema ya mafundisho ya dini mema kama vile Shetani alivyo na bidii katika kupanda magugu na aina fulani za majani yanayofanana na nafaka, ila ni magugu tu miongoni mwa ngano!”– Ibid., “Sermon of the Plough.” [GC 248.3; PK Aya ya 11]

Kanuni kuu iliyoshikiliwa na kutetewa na Wanamatengenezo hawa - ni ile ile iliyokuwa ilimeshikiliwa na Wawaldensia, na Wycliffe, na John Huss, na Luther, Zwingli, pamoja na wale walioungana nao - ilikuwa mamlaka isiyokosea kamwe ya Maandiko Matakatifu, kama ndiyo kanuni ya imani na matendo. Walitupilia mbali haki za mapapa, mabaraza, Mababa, na wafalme kuitawala dhamiri katika masuala ya dini. Biblia ndiyo iliyokuwa mamlaka yao, na walipima mafundisho yote mafundisho yote na madai yote kwa mafundisho yake. Imani katika Mungu na Neno lake iliwashikilia watu hawa watakatifu walipoyasalimisha maisha yao kwenye nguzo za kuchomea watu moto. “Na muwe na faraja na amani nyingi kidogo,” Latimer mfia dini aliwaambia wenzake kwa sauti kuu wakati ndimi za moto zilipokuwa karibu kuzinyamazisha sauti zao, “siku hii ya leo, kwa neema Zake Mungu sisi tunauwasha mshumaa kama huu katika nchi hii ya Uingereza ambao, naamini, hautaweza kuzimwa kamwe.” - Works of Hugh Latimer, gombo la 1, ukurasa wa xiii. [GC 249.1; PK Aya ya 12]

Katika nchi ya  Scotland mbegu za Ukweli zilizotawanywa na Columba na watenda kazi wenzake hazikuweza kuharibiwa kabisa. Kwa mamia ya miaka baada ya Makanisa ya Uingereza kujisalimisha kwa Roma, makanisa ya Scotland yalidumisha uhuru wao. Hata hivyo, katika karne ya kumi na mbili, utawala wa Roma ulianzishwa tena hapa, nao ukawa umezishika barabara hatamu zake za utawala hapo kuliko katika nchi nyingine yoyote. Hakuna mahali pengine palipokuwa na giza lenye nene zaidi kuliko lililokuwepo katika nchi hii. Ila bado ilikuja miale ya nuru iliyolipenya giza lile nene, na kutoa ahadi ya mchana unaokuja. Waloladi, waliokuja kutoka Uingereza wakiwa na Biblia na mafundisho ya Wycliffe, walifanya kazi kubwa ya kuhifadhi Ukweli wa Injili na kila karne ilikuwa na mashahidi na wafia dini. [GC 249.2; PK Aya ya 13]

Maandishi ya Luther yalikuja yakiambatana na ufunguzi wa Matengenezo yale Makubwa (Great Reformation), na kisha Agano jipya la Kiingereza la Tyndale. Bila kutambuliwa na uongozi wa hierakia wa kanisa la Roma, wajumbe hawa walivuka milima na mabonde kimyakimya, wakiuwasha upya ule mwenge wa Ukweli uliokuwa karibu kuzimwa kabisa katika nchi  ya Scotland na kusahihisha makosa kwa kuibomoa ile kazi iliyokuwa imefanywa na Rumi kwa karne nne za ukandamizaji wake. [GC 249.3; PK Aya ya 14]

**Msukumo Mpya Wa Harakati**

Ndipo damu ya wafia dini ilileta msukumo mpya kwenye vuguvugu ya matengenezo, viongozi wa upapa walipoamka kwa ghafla walibaini kuhusu hatari iliyotishia kazi yao, waliwaleta pamoja wazaliwa wa Scotland mashuhuri na walioheshimiwa ili kuwachoma moto katika mti wa kuunguzia watu. Wakajenga jukwaa kubwa kwa ajili ya kuwachoma moto, na hapo maneno ya mashahidi waliokuwa wanakufa yalisikika katika nchi zima, yakisisimua roho za watu kwa kusudi la kutokukata tamaa, na hilo likawapa motisha wa kujivua minyonyoro ya Roma. [GC 249.4; PK Aya ya 15]

Hamilton na Wishart, watu wema katika tabia, na wana wa kifalme kwa urithi, walikuwa miongoni mwa msururu mrefu wa wanafunzi wanyenyekevu waliotoa maisha yao kwa kuchomwa moto kwenye mti ule wa kuchomea watu. Lakini kutoka kwenye  rundo la kuni la Wishart lililokuwa linawaka moto. Alitokea mmoja ambaye miali ya moto haikuweza kumpa tishio, huyu akiwa chini ya usimamizi wa Mungu aliupa kipigo kikali upapa kule Scotland, kilichotoa sauti ya kengele ya kifo kwa upapa kwenye nchi hii. [GC 250.1; PK Aya ya 16]

John Knox alikuwa ameachana na mapokeo na imani za kishirikina ya kanisa na kujilisha Kweli ya Neno la Mungu na mafundisho ya Wishart yalikuwa

yamethibitisha azimio lake la kuacha ushirika wa Rumi na kujiunga na Wanamatengenezo waliokuwa wakiteswa. [GC 250.2; PK Aya ya 17]

Aliposhauriwa sana na wenzake afanye kazi ya kuhubiri, alijikunyata kwa kutetemeka kutokana na jukumu hilo zito, na ilikuwa tu baada ya siku za kuwa na faragha na migogoro ya nafsi iliyomletea maumivu mwenyewe ndipo alikubali. Lakini mara tu baada ya kuikubali kazi hiyo, alisonga mbele kwa nia isiyobadilika na ujasiri usio na hofu kadiri alivyodumu kuwa na uzima. Mwanamatengenezo huyu mwenye moyo wa dhati, hakuogopa uso wa mtu, au mioto ya kuunguza wafia dini iliyokuwa ikiwaka kumzunguka kila upande wake, haya yalimsukuma tu kuharakisha bidii yake kwa ukali zaidi. Alipotishiwa kuwa shoka la mtesi katili litainuliwa juu ya kichwa chake, alisimama kidete, akitoa vipigo vikali kwenye mkono wa kulia na upande wa kushoto akivunjavunja ibada ya sanamu. [GC 250.3; PK Aya ya 18]

**Ana Kwa Ana Na Malkia**

Alipoletwa mbele ya malkia wa Scotland uso kwa uso, mama ambaye juhudi ya viongozi wengi  Waprotestanti ilikuwa imepata tishio na kunywea, John Knox alitoa ushuhuda usioyumba kwa ajili ya Ukweli. Hakuweza kushindwa kwa kubembelezwa au kupakwa mafuta kwa chupa ya mgongo, hakujikunyata mbele ya vitisho. Malkia alimshtaki kwa kosa la uzushi. Alikuwa akiwafundisha watu kupokea dini iliyopigwa marufuku na serikali, ndipo malkia akasema kwasababu hiyo Knox alikuwa amevunja amri ya Mungu inayowataka raia kuwatii wakuu wao wa serikali. Knox alijibu hivi kwa ujasiri: [GC 250.4; PK Aya ya 19]

“Kwa kuwa dini ya Kweli haipokei nguvu zake za asili wala mamlaka kutoka kwa wakuu wa ulimwengu, bali hutoka kwa Mungu wa milele pekee, kadhalika raia hawapaswi kujenga maisha yao ya imani au dini kulingana na ladha au matakwa ya wakuu wao. Kwa maana mara nyingi  wakuu wa kidunia ni wajinga (hawana ujuzi) ukilinganisha na watu wengine wote kuhusiana na dini ya Kweli ya Mungu. Ikiwa wazao wote wa Ibrahimu wangekuwa katika dini ya Farao, ambao walikuwa raia wake kwa muda mrefu, nakuuliza mama, kungekuwa na dini gani ulimwenguni? Au kama watu wote katika siku za mitume walikuwa na dini ya Makaisari wa Kirumi, ni dini gani ingekuwepo kwenye uso wa dunia? Na kwa hivyo, Bibie/mama, unaweza kung’amua kuwa raia hawafungwi na dini ya wakuu wao, ingawa wameamrishwa kuwatii." [GC 250.5; PK Aya ya 20]

Malkia Mary akasema hivi: “Wewe unayafafanua Maandiko hayo kwa njia moja, na wao (waalimu Wakatoliki wa Roma) wanayafafanua kwa njia nyingine; ninamwamini nani, naye ni nani atakayekuwa mwamuzi?" [GC 251.1; PK Aya ya 21]

"Mwaminini Mungu azungumzaye wazi kupitia Neno Lake," akajibu Mwanamatengenezo huyu; "na zaidi ya kile Neno linachowafundisha, msimwamini huyu wala yule, Neno la Mungu liko wazi lenyewe; na kunapotokea giza lolote au kutoeleweka mahali pamoja, Roho Mtakatifu, ambaye kamwe hawezi kujipinga Mwenyewe, hufafanua sehemu hiyo kwa uwazi zaidi katika sehemu zingine, ili kwamba kusiwe na mashaka yoyote yanayoweza kubaki, isipokuwa kwa wale ambao kwa ukaidi wa moyo hubaki kuwa wajinga." David Laing, The Collected Works of John Knox, juz. 2, uk. 281, 284. [GC 251.2; PK Aya ya 22]

Hizo ndizo Kweli ambazo Mwanamatengenezo asiye na woga, kwa kuhatarisha maisha yake, alizungumza kwenye sikio la malkia. Kwa ujasiri huo huo usiotetereka, alishikamana na kusudi lake, akiomba na kupigana vita vya Bwana, mpaka Uskochi ilipoachana kabisa na upapa. [GC 251.3; PK Aya ya 23]

Katika nchi ya Uingereza ustawishaji wa Uprotestanti kama dini ya kitaifa kulipunguza, lakini hakukomesha kabisa mateso. Wakati mengi ya mafundisho ya Kirumi yalikuwa yameachwa, taratibu zake za ibada zisizokuwa chache zilibakizwa. Ukuu wa papa ulikataliwa, lakini mahali pake mfalme alitawazwa kama kiongozi mkuu wa kanisa. Ibada za kanisa bado zilikuwa zinapishana na usafi wa maisha na usahili wa injili. Kanuni kuu ya uhuru wa kidini ilikuwa bado haijaeleweka. Ingawa mambo ya kutisha na kikatili ambayo Roma iliyatumia dhidi ya uzushi yalitumiwa kwa nadra sana na watawala wa Kiprotestanti, bado haki ya kila mtu kumwabudu Mungu kulingana na uchaguzi wa dhamiri yake mwenyewe haikuzingatiwa. Wote walitakiwa kuyakubali mafundisho na kuzingatia sera za ibada zilizoamriwa na kanisa lililotambuliwa na serikali. Wale ambao walienda kinyume cha kanisa waliteswa, kwa kiwango kikubwa au kidogo, kwa mamia ya miaka. [GC 251.4; PK Aya ya 24]

Katika karne ya kumi na saba, maelfu ya wachungaji walifukuzwa kutoka kwenye kazi zao. Watu walikatazwa kwa tishio la faini kubwa, kufungwa gerezani, kufukuzwa nchini, watu walikatazwa kuhudhuria mikutano yoyote ya kidini isipokuwa ile iliyoidhinishwa na kanisa. Wale watu waaminifu ambao hawangeweza kuacha kukusanyika ili kumwabudu Mungu walilazimika kukutana katika vichochoro vyenye giza, kwenye vipenu vilivyojificha darini, na nyakati fulani msituni katika usiku wa manane. Katikati ya maficho ya msitu mnene, hekalu lile lililojengwa na Mungu Mwenyewe, watoto wa Bwana waliokuwa wametawanywa na kuteswa walikusanyika ili kumimina roho zao kwa njia ya sala na sifa. Lakini licha ya tahadhari zao zote, wengi waliteseka kwa ajili ya imani yao. Magereza yalijaa watu, familia zilivunjika, na wengi walifukuzwa kutoka nchi zao na kukimbilia katika nchi za kigeni. Hata hivyo Mungu alikuwa pamoja na watu Wake na wala yale mateso hayakufaulu kunyamazisha ushuhuda wao. Wengi walifukuzwa katika nchi yao na kulazimika kuvuka bahari hadi Amerika na

hapa waliweka misingi ya uhuru wa kiraia na wa kidini ambao umekuwa nguzo na utukufu wa nchi hii ya Marekani. [GC 252.1; PK Aya ya 25]

Kwa mara nyingine, kama ilivyokuwa katika siku za mitume, badala ya mateso kukomesha kazi ya injili, yaligeuka na kuwa njia ya kusambaa kwake. Katika gereza la chini ya ardhi lenye uvundo na kuchukiza, kulikuwa na msongamano wa watu wenye maadili machafu na wauaji, John Bunyan alivuta hewa ya mbinguni na humo ndimo aliandika kisa kile chenye fumbo la ajabu la Maendeleo ya msafiri kutoka katika nchi ya uharibifu hadi kwenye mji mtakatifu. Kwa zaidi ya miaka mia mbili sauti ile kutoka gereza la Bedford imezungumza kwa nguvu inayosisimua kwenye mioyo ya wanadamu. Vitabu hivi vya Bunyan Pilgrims Progress (Maendeleo ya Msafiri au mhujaji) na Grace Abounding to the Chief of Sinners (Neema tele kwa mkuu wa wenye dhambi) vimeongoza miguu ya wengi kwenye njia ya uzima. *(Pilgrims Progress ni kitabu cha pili kuuzika duniani-best seller, kinafuatia Biblia, na cha tatu kikiwa Kuruani, na cha nne ni Kitabu chekundu cha ukomunisti cha China) [GC 252.2; PK Aya ya 26]

Baxter, Flavel, Alleine, na watu wengine wenye talanta, elimu, na uzoefu wa kina wa maisha ya Ukristo walisimama kishujaa kuitetea imani ambayo ilikabidhiwa kwa watakatifu mara moja tu. Kazi iliyofanywa na watu hawa, iliyokuwa imepigwa marufuku na kuharamishwa na watawala wa ulimwengu huu, haiwezi kamwe kuangamia. Vitabu vya Flavel viitwavyo Fountain of Life (Chemchemi ya Uhai) na Method of Grace (Mbinu ya neema) vimewafundisha maelfu jinsi ya kuzisalimisha roho zao kwa Kristo. Kitabu cha Baxter kiitwacho Reformed Pastor (Mchungaji Mwanatengenezo) kimekuwa mbaraka kwa wengi wanaotamani kuifufua kazi ya Mungu na kitabu chake kingine kiitwacho Saints' Everlasting Rest (Pumziko la Milele la Watakatifu) kimefanya kazi yake katika kuongoza watu kwenye "pumziko" ambalo limesalia kwa watu wa Mungu. [GC 252.3; PK Aya ya 27]

### Whitefield Na Wesley

Miaka mia moja baadaye, katika siku ya giza nene la kiroho, Whitefield na wafuasi wa Wesley walijitokeza kama wabeba nuru kwa ajili ya Mungu. Chini ya utawala wa kanisa la kitaifa lililoanzishwa na watu wa Uingereza, walikuwa wamerudi nyuma na kuzama katika hali ya mporomoko wa maadili ya kidini kiasi kwamba hawakutofautiana na Wapagani/kafiri. Dini ya asili, iliyofuata desturi ndiyo ilikuwa somo lao lililopendwa zaidi na wachungaji, na lilijumuisha pia sehemu kubwa ya theolojia yao. Watu wa matabaka ya juu walidharau uchaji Mungu wao, na kujivunia kuwa wao walikuwa juu ya kile walichokiita ushabiki wa kidini usiotumia akili, watu wa tabaka la chini walikuwa wajinga kupita kiasi na walijiingiza kutenda maovu bila mipaka, wakati kanisa lilikuwa halina ujasiri

wala imani tena ya kuunga mkono kazi ya Ukweli-injili, iliyokuwa imeanguka chini. [GC 253.1; PK Aya ya 28]

Fundisho kuu la kuhesabiwa haki kwa imani, lililofundishwa kwa uwazi sana na Luther, lilikuwa limesahaulika kwa kiasi kikubwa machoni pao. Na ile kanuni ya Kirumi ya kutegemea matendo mema kwa ajili ya wokovu, ilikuwa imechukua nafasi yake. Whitefield na akina Wesley, ambao walikuwa ni washiriki wa kanisa la taifa lililostawi tayari, walikuwa watafutaji wa dhati wa mapenzi ya Mungu na kwa hili walikuwa wamefundishwa kuwa mapenzi ya Mungu yalikuwa yanapatikana katika kuishi maisha ya uadilifu na kushika sheria za dini. [GC 253.2; PK Aya ya 29]

Wakati Fulani Charles Wesley alipougua na kuona kwamba kifo chake kilikuwa kinakaribia, aliulizwa swali kuwa tumaini lake la uzima wa milele limejengwa kwenye nini. Jibu lake lilikuwa: “Nimetumia juhudi zangu zote kumtumikia Mungu.” Wakati rafiki yake aliyemwuliza swali hilo alipoonekana kutoridhika kabisa na jibu lake, Wesley aliwaza: “Je! juhudi zangu si msingi unaotosha kujenga tumaini langu juu yake?" Je, wewe anaweza kunipora juhudi zangu? Basi, mimi sina kitu kingine zaidi cha kutumainia.”- John Whitefield, Life of the Rev. Charles Wesley, ukurasa wa 102. Hilo ndilo giza nene lililokuwa katika kanisa, lililouficha upatanisho, na kumnyang’anya Kristo utukufu Wake, na kugeuza mawazo ya wanadamu kutoka katika tumaini lao pekee la wokovu--yaani katika damu ya Mkombozi aliyesulubiwa. [GC 253.3; PK Aya ya 30]

**‘Lakini Mtu Huwaje Mwenye Haki Mbele Za Mungu’**

Wesley na washirika wake waliongozwa kuona kwamba dini ya kweli inakaa moyoni, na kwamba sheria ya Mungu inapanuka na kuhusisha hadi mawazo, maneno na matendo. Wakiwa wamesadikishwa juu ya umuhimu wa kuwa na utakatifu wa moyo, pamoja na usahihi wa mwenendo unaoonekana nje; walianza kujielekeza kwa dhati na bidii kuishi maisha haya mapya. Kwa uadilifu wenye bidii na kwa maombi walijitahidi kuyadhibiti maovu ya moyo wa asili. Waliishi maisha ya kujinyima, ukarimu, upendo, na unyenyekevu, wakishika kwa ukali na kwa usahihi kila kigezo ambacho walidhani kingeweza kuwasaidia katika kukipata kile walichokuwa wakikitamani zaidi---- utakatifu ule ambao ungewawezesha kupata upendeleo wa Mungu, lakini hawakufikia lengo walilokuwa wanalitafuta. Juhudi zao za kujiweka huru kutokana na hukumu ya dhambi au kuvunja nguvu zake zilikuwa kazi bure. Lilikuwa ni pambano lile lile ambalo Luther alikuwa amelipitia akiwa chumbani mwake pale Erfurt. Lilikuwa swali lile lile ambalo lilikuwa limeitesa nafsi yake “Lakini mtu huwaje mwenye haki mbele za Mungu?” Ayubu 9:2. [GC 254.1; PK Aya ya 31]

Mioto ya Ukweli wa Mungu, ambayo ilikuwa karibu kuzimika juu ya madhabahu ya Uprotestanti, ilipaswa kuwashwa tena upya kwa kutumia mwenge

ule wa zamani uliorithishwa katika Zama zote na kushuka chini katika vizazi vya Wakristo wa kule Bohemia. Baada ya Matengenezo ya Kanisa, Uprotestanti katika Bohemia ulikuwa umekanyagwa chini na genge la waumini wa Roma na kutoweka. Wote waliokataa kuukana Ukweli walilazimika kukimbia. Baadhi ya hawa, walijipatia hifadhi huko Saxony, na walidumisha imani ya zamani. Ilikuwa ni kutoka kwa vitukuu Wakristo hawa ambapo nuru ilikuja kwa Wesley na wenzake. [GC 254.2; PK Aya ya 32]

John na Charles Wesley, baada ya kuwekewa mikono ya uchungaji kwa huduma, walitumwa kama wamishenari huko Marekani. Ndani ya meli waliyopanda, mlikuwemo kundi la Wamoravian. Katika safari walikumbana na dhoruba kali na John Wesley, alipokabiliwa uso kwa uso na kifo, alijisikia moyoni mwake kuwa hakuwa na uhakika wa amani kati yake na Mungu. Wajerumani kinyume chake, walionyesha utulivu na tumaini ambalo lilikuwa geni kwake, kwani hakuwa na uzoefu nalo. [GC 254.3; PK Aya ya 33]

“kwa muda mrefu huko nyuma,” alisema, “nilikuwa nimeichunguza tabia yao ya kuchukulia mambo kwa umakini, isiyokuwa na mambo ya mizaha-mizaha, kwa unyenyekevu wao ambao ulikuwa umedhihirishwa kwa watu daima, kwa kuzifanya kazi za hali ya chini kama watumwa kwa ajili ya abiria wengine ambazo hakuna hata mtu mmoja miongoni mwa Waingereza ambaye angeweza kuzifanya; hizi walipenda kuzifanya kwa moyo, na japo walistahili malipo, hawakukubali kupokea malipo yoyote, walisema ni vyema kwa mioyo yao yenye kiburi, na kwamba Mwokozi wao mwenye upendo alikuwa amewafanyia wao zaidi ya yale. Na kwamba kila siku Mwokozi alikuwa amewapa fursa ya kuonyesha unyenyekevu ambao usingeweza kuathiriwa na shida ya aina yoyote. Endapo wao walisukumwa au kupigwa na kutupwa chini huku na kule katika meli, waliinuka tena na kwenda zao lakini hakukuwa na malalamiko yoyote yaliyopatikana vinywani mwao. Basi, kulikuwa na fursa iliyojitokeza, ya kuwapima iwapo walikuwa wamekombolewa kutokana na roho ya hofu, kiburi, hasira, na kulipiza kisasi. Katikati ya kuimba Zaburi ambayo ilitumika kuanzisha ibada yao, bahari ilichafuka ghafla, dhoruba ikapasua tanga vipande-vipande na kumimina maji kwenye Sitaha kana kwamba kina kikuu cha bahari kilikuwa tayari kimeshatumeza. Mayowe ya kutisha yalianza kumiminika miongoni mwa Waingereza. Wajerumani wao waliendelea kuimba tu Zaburi kwa utulivu, nilimuuliza mmoja wao baadaye, ‘Je, wewe hukuogopa?’ Alijibu, ‘Namshukuru Mungu, hapana.’ Nikauliza, ‘Lakini je, wanawake na watoto wenu hawakuogopa?’ Alijibu kwa upole, ‘Hapana. Wake zetu na watoto wetu hawaogopi kifo.’”— Whitehead, Life of the Rev. John Wesley, ukurasa wa 10. [GC 255.1; PK Aya ya 34]

Baada ya kufika Savannah kule Marekani, Wesley alikaa kwa muda mfupi pamoja na Wamoraviani, naye alivutiwa sana na haiba yao ya Kikristo. Kuhusu

mojawapo ya ibada zao, zilizotofautiana kabisa na utaratibu wa ibada za kimfumo zisizo na uhai za Kanisa la Uingereza, aliandika hivi: “Usahili mkubwa, pamoja na kicho chao kwa Mungu katika ibada yao yote, vilinifanya mimi nikaribie kusahau kabisa ile miaka elfu moja na mia saba iliyokuwa imepita, na kunifanya nipate kujifikiria mwenyewe ya kuwa nilikuwa katika mmojawapo ya mikutano ile ambamo mfumo na serikali ya kanisa havikuwamo; bali Paulo mtengeneza mahema, au Petro mvuvi wa samaki, ndio waliokuwa wakiongoza ibada; na udhihirisho wa Roho na uweza” -Ibid., ukurasa wa 11, 12. [GC 255.2; PK Aya ya 35]

**Ni Kristo Peke Yake**

Aliporudi Uingereza, Wesley, kutokana na mafundisho ya mhubiri wa Kimoraviani, aliweza kufikia uelewa mzuri zaidi wa imani ya Biblia, alikuwa amesadiki kabisa kwamba ni lazima aachane na kutegemea matendo yake mema kwa ajili ya wokovu na ilimpasa sasa kumtumaini kabisa “Mwana-Kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu.” katika mkutano wa chama cha Moravian huko London kauli ilisomwa kutoka kwa Luther, inayoelezea badiliko lile ambalo Roho wa Mungu hulileta ndani ya moyo wa mtu yule aaminiye. Wesley alipokuwa akisikiliza, imani iliwashwa ndani ya moyo wake "Nilihisi moyo wangu ukitiwa joto kwa namna ya ajabu." akasema “Nilihisi kwamba mimi ninamtumaini Kristo, Kristo pekee, kwa ajili ya wokovu wangu na uhakikisho ulitolewa kwangu, kwamba Yeye alikuwa amezichukua dhambi zangu, ndiyo dhambi zangu mimi zote, na kuniokoa kabisa kutoka katika sheria ya dhambi na mauti.”—Ibid., 52. [GC 255.3; PK Aya ya 36]

Katika muda mrefu wa mahangaiko ya kuchosha, na yasiyoniletea raha yoyote--miaka ya kujikana nafsi kwa ukali, kujinyima sana, kujidhili na kujinyenyekesha, Wesley alikuwa alimejibidisha daima kutekeleza kusudi lake moja tu, la kumtafuta Mungu. Sasa akawa amempata, naye akagundua kuwa neema ambayo alijiyosumbuka sana ili aipate kwa sala na kufunga/swaumu, kwa matendo ya ukarimu kama kutoa sadaka kwa masikini na kujikana nafsi, ilikuwa ni zawadi, “isiyo na fedha wala bei.” [GC 256.1; PK Aya ya 37]

Alipokwisha kuimarishwa katika imani ya Kristo, moyo wake wote uliwaka na matamanio ya kueneza kila mahali maarifa haya ya injili yenye utukufu ya neema ya bure ya Mungu “Nautazama ulimwengu wote kama parokia yangu,” alisema “katika sehemu yoyote ile nilipo, ninaona kuwa panastahili, tena ni haki, na wajibu wangu uliowekwa na unaonifunga, kuwatangazia watu wote ambao wako tayari kusikia, habari njema za furaha na wokovu.”—Ibid., ukurasa wa 74. [GC 256.2; PK Aya ya 38]

Aliendelea maisha madhubuti ya nidhamu kali na kujikana nafsi yake, siyo sasa kama msingi, bali matokeo ya imani, sio kama mzizi, bali kama tunda la

utakatifu. Neema ya Mungu iliyo katika Kristo ndiyo msingi wa tumaini la Mkristo, na neema hiyo inadhihirika katika utii. Maisha ya Wesley yaliwekwa wakfu kwa kuhubiri Kweli kuu alizokuwa amezipokea—yaani kuhesabiwa haki kwa njia ya imani katika damu ya upatanisho ya Kristo na uweza ule unaoumba upya moyo, nguvu ya Roho Mtakatifu juu ya moyo wa mtu, uikizaa tunda katika maisha linalopatana na mfano Wake Kristo. [GC 256.3; PK Aya ya 39]

Whitefield na Wesley walikuwa wameandaliwa kwa ajili ya kazi yao, kila mmoja akiwa amesadikishwa binafsi kwa muda mrefu kutambua hali yake ya kupotea; na kwamba wangeweza kustahimili ugumu wa maisha kama askari wema wa Kristo, walikuwa wamewekwa chini ya moto wa majaribu makali ya dharau, dhihaka na mateso katika chuo kikuu na walipokuwa wakiingia katika huduma ya kichungaji. Wao pamoja na wenzao wachache waliowaunga mkono waliwaita kwa dhihaka Wamethodisti na wanafunzi wenzao wasiomcha Mungu--Jina ambalo kwa sasa hivi linaheshimiwa na ni mojawapo ya madhehebu makubwa zaidi nchini Uingereza na Marekani. [GC 256.4; PK Aya ya 40]

Kama washiriki wa Kanisa la Uingereza (Anglikana) walikuwa wamefungamanishwa sana na desturi zake za ibada, lakini Bwana alikuwa amewasilisha mbele yao katika Neno Lake, kiwango cha juu zaidi. Roho Mtakatifu, aliwaagiza wamhubiri Kristo na Yeye aliyesulubiwa. Nguvu za Yeye aliye Juu Zaidi ziliandamana na kazi zao, maelfu waliamini na kuongolewa kikamilifu. Ilikuwa ni lazima kwamba kondoo wale walindwe dhidi ya mbwa-mwitu wakali. Wesley hakuwa na wazo la kuanzisha dhehebu jipya, lakini aliwasimamia chini ya mwavuli wa kile kilichoitwa "Mshikamano wa Kimethodist au Muungano wa Kimethodist" "Methodist Connection." [GC 257.1; PK Aya ya 41]

Wahubiri hawa walipata upinzani na usumbufu wa ajabu kutoka katika kanisa la kitaifa, na usumbufu huu ulikuwa kama fumbo kwao, lakini Mungu kwa hekima Yake, aliingilia kati na kufanya matukio hayo kuanzisha Matengenezo ndani ya kanisa lenyewe. Ikiwa Matengenezo yangekuja kutokea nje peke yake, basi yasingaliweza kupenya na kuingia mahali yalipohitajika sana. Lakini kwa vile wahubiri hawa walikuwa na uamsho na walikuwa watu wa kanisa, popote pale walipoweza kupata fursa, Ukweli ulipata kuingia hapo, ambapo vinginevyo milango ingeweza kubaki imefungwa. Baadhi ya wachungaji waliamshwa kutoka katika usingizi na ugoigoi wa kimaadili na wakawa wahubiri waliochemka katika parishi zao wenyewe Makanisa ambayo yalikuwa yamegubikwa na mifumo ya desturi na taratibu za kanisa za ibada za kurudia-rudia maneno au vitendo bila moyo au akili kuhusika yalihuishwa haraka na kuwa hai tena. [GC 257.2; PK Aya ya 42]

Wakati wa Wesley, kama ilivyokuwa katika nyakati zote za historia ya kanisa, watu wenye karama mbalimbali walitenda kazi walizopangiwa kuzifanya. Hawakuafikiana katika kila kipengele cha fundisho lao la Biblia, bali wote

waliongozwa na kusukumwa na Roho wa Mungu, na kuunganishwa katika kusudi moja lililovuta mioyo yao, nalo ni kuleta roho kwa Kristo. Tofauti zilizokuwepo kati ya Whitefield na Wesley wakati fulani zilitishia kuleta mafarakano; lakini kwa kadri walivyojifunza upole na unyenyekevu katika shule ya Kristo, na kuvumiliana, pamoja na upendo pande zote mbili, walipatana na kuvumiliana kwa ukarimu. Hakika hawakuwa na muda wa kulumbana, wakati mafundisho ya uongo, potofu na yenye uovu yalikuwa Yanaendelea kushamiri kila mahali, na wenye dhambi walikuwa wakiteremka chini na kuelekea kwenye shimo la uangamivu. [GC 257.3; PK Aya ya 43]

**Wesley Anusurika**

Watumishi wa Mungu walipita katika njia yenye mikwaruzo-rafurafu. Watu wenye mvuto wa elimu kubwa walitumia uwezo wao dhidi yao. Baada ya muda fulani, wengi miongoni mwa wachungaji walionesha uhasama ulionuiwa waziwazi, na milango ya makanisa ilifungwa dhidi ya imani safi na wale walioitangaza. Hatua iliyotumiwa na wachungaji ya kuwashutumu na kuwapiga marufuku kutoka kwenye mimbari zao ilihamasisha mbegu za giza, ujinga, na uovu. Tena na tena. John Wesley aliponea chupu chupu kuuawa kwa miujiza ya rehema Zake Mungu. Ghadhabu ya umati ilipochochewa juu yake, na ikaonekana hapakuwa na njia ya kuponyokea, malaika katika umbo la kibinadamu alikuja na kusimama kando yake, na kundi lenye ghasia likarudi nyuma, na mtumishi wa Kristo alipita salama na kuondoka mahali pale penye hatari. [GC 258.1; PK Aya ya 44]

Kuhusiana na kuokolewa kwake kutoka katika umati wenye ghadhabu katika moja ya matukio hayo, Wesley alisema haya: “Wengi walijaribu sana kuniangusha chini tulipokuwa tukitelemka mlimani kwenye njia inayoteleza kuelekea mjini; walikuwa wamefikiria kwamba ikitokea mara moja nikaanguka chini, basi ingeniwia vigumu kuinuka tena, lakini mimi sikujikwaa hata kidogo, wala hata kuteleza kidogo, mpaka nilipoponyoka, na kuwa huru, mbali kabisa na mikono yao-- Japokuwa wengi walijitahidi kushika upindo wa shati langu shingoni au mavazi yangu, ili kunivuta chini na kuniangusha chini, hawakuweza kushika hata kidogo: ni mmoja tu ndiye aliyefanikiwa kushika pindo la nusukoti langu, ambacho muda si mrefu kushika nusukoti, hili lilibaki mkononi mwake; kipande kingine ambacho kilikuwa na mfuko, kilibaki, na ndani yake ilikuwemo noti moja, ..... Mtu mmoja aliyekuwa mwenye hasira na nguvu karibu na mgongo wangu, alinipiga mara kadhaa kwa fimbo kubwa ya mti wa mwaloni ambayo kama angenipiga nayo mara moja kwenye sehemu ya nyuma ya kichwa changu (kisogoni) ingeweza kumwondolea udhia na matatizo yote kwani angeniua. Lakini kila aliponipa kipigo, pigo lake liligeuzwa kando, sijui jambo hilo lilitokeaje, kwa maana mimi sikuweza kusogea upande wa kulia au wa kushoto... Mwingine alikuja akitimua mbio kupitia katika msongamano wa watu na kunyanyua mkono

wake ili anipige, kwa ghafla aliushusha chini mkono wake na kukipapasa tu kichwa changu, akisema, ‘Loh, huyu mtu ana nywele laini kama nini!’...... Watu wa kwanza kabisa ambao mioyo yao iligeuzwa na injili ndio waliokuwa mashujaa wa mji huo, viongozi wa makundi ya wahuni au wapiganaji walioleta ghasia katika nyakati zote, mmoja wao akiwa mpiganaji wa ngumi na alishawahi kupata tuzo la masumbwi katika Bustani za Dubu ...... [GC 258.2; PK Aya ya 45]

“Ni kwa hatua ya upole lakini za hakika, Mungu anatuandaa sisi kwa ajili ya kutenda mapenzi Yake! Miaka miwili iliyopita, kipande cha tofali la kuchomwa kilinikwangua kidogo mabegani, ilikuwa ni mwaka mmoja baadaye ambapo jiwe liliponigonga katikati ya macho yangu. Mwezi uliopita nilipokea kipigo kimoja, na jioni hii viwili, kimoja kabla hatujafika mjini humu, na kingine baada ya sisi kuondoka nje ya mji. Lakini vyote viwili vilikuwa kama si kitu; maana ijapokuwa mtu mmoja alinipiga kifuani kwa nguvu zake zote, na mwingine mdomoni kwa nguvu hata ikafanya damu damu itoke papo hapo, sikuhisi maumivu yoyote makali zaidi kuliko yale ambayo ningeyapata kama wangenigusa kwa unyasi mkavu wa ngano." John Wesley, Works, juz. 3, uk. 297, 298. [GC 259.1; PK Aya ya 46]

**Wamethodisti Wadhihakiwa Na Kuteswa**

Wamethodisti wa siku zile za awali--- Watu na wahubiri wao, walivumilia dhihaka na mateso ya aina moja kutoka kwa washiriki wa kanisa na kutoka kwa watu waliojionyesha kutokuwa na dini waziwaziwi, nao walikasirishwa kwa mambo ambayo yalikuwa yamewasilishwa visivyo kuhusu wao. Walishitakiwa mbele ya mahakama za haki--kwa jina kama zilivyoitwa, kwa maana haki ilikuwa nadra sana katika mahakama za wakati huo. Mara nyingi waliteswa na kufanyiwa ukatili na watesi wao. Makundi ya watu yalitembea nyumba kwa nyumba, yakiharibu samani na mali zingine, yakipora chochote walichokichagua, na kuwanajisi kikatili wanaume, wanawake, na watoto. Katika matukio fulani, matangazo ya hadhara yalibandikwa, yakitoa wito kwa wale ambao walipenda kusaidia kuvunja madirisha na kupora mali kutoka katika nyumba za Wamethodisti, wakusanyike saa fulani na mahali palipochaguliwa. Ukiukwaji huo wa wazi wa sheria za mwanadamu na ya Mungu uliruhusiwa kupita bila hata kemeo. Utesaji uliopangwa uliendelea dhidi ya watu ambao kosa lao pekee lilikuwa ni kutafuta kugeuza miguu ya wenye dhambi kutoka kwenye njia ya uharibifu na kuielekeza katika njia ya utakatifu. [GC 259.2; PK Aya ya 47]

Alisema John Wesley, akirejelea mashtaka dhidi yake mwenyewe na wenzake: “Wengi wao hudai kwamba mafundisho ya watu hawa ni ya uongo, yana makosa, na yana usongo unaopitiliza; kwamba ni mapya na hawajawahi kuyasikika hadi hivi majuzi; kwamba wao ni dhehebu lile la Quakers* lenye imani ya kutokwenda vitani n.k, na kwamba wana ushabiki wa dini usiotumia busara, na ni watetezi

wa upapa. Maigizo yote haya tayari yameshakatwa mpaka kwenye mizizi yake sasa, baada ya kuonyeshwa kwa ujumla na wazi kila kipengele cha mafundisho haya ya dini ni mafundisho yaliyo wazi kabisa kama yalivyotafsiriwa na kanisa letu wenyewe. Kwa hiyo hayawezi kuwa ya uwongo au yenye makosa, mradi tu Maandiko Matakatifu yawe ya Kweli." "Wengine wanadai, 'Mafundisho yao ni makali nayo yanawafinya na kuwabana sana watu; wao huifanya njia ya kwenda mbinguni kuwa finyu sana.' Na dai hilo kwa kweli ndilo lilikuwa pingamizi la awali,* na kwa siri ndiyo msingi wa vipingamizi vingine elfu na zaidi, vinavyojitokeza katika sura mbalimbali. lakini Je, vinaifanya njia ya mbinguni kuwa nyembamba kuliko vile Bwana wetu na Mitume Wake walivyoifanya? Je,kuna fundisho gumu au kali linalowabana watu kuliko lile la Biblia? Hebu fikiria aya chache tu zilizo wazi: 'Mpende Bwana, Mungu wako, kwa moyo wako wote, na kwa akili zako zote, na kwa roho yako yote, na kwa nguvu zako zote. 'Kwa kila neno lisilo maana, watakalolinena wanadamu, watatoa hesabu siku ya hukumu.' 'Basi mlapo, au mnywapo, au mtendapo neno lo lote, fanyeni yote kwa utukufu wa Mungu.' *(Quakers ni dini iliyo sehemu za Marekani, nchi zingine inaitwa Friends) *(kwa kuwa dai hilo ndiyo lililokuwa kipingamizi pekee yake kwa muda fulani) [GC 259.3; PK Aya ya 48]

"Ikiwa fundisho lao ni kali au linambana mtu kuliko hili, basi walaumiwe; lakini wewe unajua katika dhamiri yako kuwa sivyo ilivyo. Na ni yupi anayeweza kupunguza ukali hata wa yodi moja, pasipo kuliharibu au kulighushi Neno la Mungu? Je wakili wa siri Zake Mungu za ajabu anawezaje kuonekana kuwa ni mwaminifu endapo anabadilisha sehemu yoyote ya amana ile takatifu aliyokabidhiwa? Hapana. Hawezi kupunguza chochote, hawezi kulilainisha fundisho; analazimika kuwatangazia watu wote, 'Mimi siwezi kuyashusha Maandiko matakatifu chini ili kukidhi ladha au matakwa yako, lazima wewe ndiyo upande juu na kuja Biblia ilipo au uangamie milele. Huu ndio msingi halisi wa kile kilio kingine maarufu kinachosema 'kukosa ukarimu na upendo kwa watu hawa.' Je, ni kweli hawana hisani na upendo? Katika mambo gani basi? Je, hawawapi chakula wenye njaa na kuwavika nguo walio uchi? 'Hapana; hilo siyo kweli: wao hawana upungufu katika jambo hilo: lakini hawana ukarimu katika kuwahukumu watu wengine! Wanadhania kwamba hakuna mtu anayeweza kuokolewa isipokuwa wale watu tu wanaofuata njia yao."- Ibid., juz. 3, uk. 152, 153. [GC 260.1; PK Aya ya 49]

Kuporomoka kwa hali ya kiroho kulikoonekana waziwazi katika Uingereza muda mfupi tu kabla ya wakati wa Wesley kwa sehemu kubwa kulitokana na matokeo ya mafundisho yapingayo Sheria ya amri za Mungu kwa kusema tumeokolewa kwa neema na hivyo sheria haina mashiko, na hivyo Wakristo hawana wajibu wa kuitii Sheria (antinomian). Wengi waliamini kwamba Kristo alikuwa ameifuta sheria ya maadili na hivyo Wakristo hawalazimiki kuifuata

tena; kwamba muumini amewekwa huru kutoka katika “utumwa wa matendo mema.” wengine, japo walikiri uendelevu wa sheria ya Mungu, walitangaza kwamba ilikuwa lazima kwa wachungaji kuwahimiza watu kuzitii amri Zake, kwa kuwa wale ambao Mungu aliwachagua waokolewe, wangeweza “kwa msukumo usiozuilika wa neema ya Mungu, kusukumwa kuishi maisha ya utauwa na kutenda matendo mema”- (automatik),” wakati wale waliopangiwa laana ya kupotea milele “hawakuwa na uwezo wa kutii sheria ya Mungu (Amri Kumi). [GC 260.2; PK Aya ya 50]

Wengine, wakishikilia pia kuwa “wale walioteuliwa au kuchaguliwa, hawawezi kuanguka kutoka kwenye neema, na wala hawawezi kunyimwa fadhila ya Mungu,” hawa walifikia mkataa wa kutisha na kuchukiza zaidi kwamba “matendo maovu wanayofanya, kwa kweli, si dhambi kabisa, wala hayapaswi kuhesabiwa kuwa uvunjaji wa sheria ya Mungu, na kwa sababu hiyo, hawana haja ya kuungama dhambi au kuachana nazo kwa njia ya toba." McClintock na Strong, Cyclopedia Art  Antinomians. "Antinomia au waumini wanaozikataa Amri za Mungu." Kwa hiyo, walifundisha kwamba hata mojawapo ya dhambi iliyo ya kutisha kabisa  zaidi, “inayochukuliwa na wanadamu wote kuwa ni uvunjaji mkubwa sana wa sheria ya Mungu, siyo dhambi machoni Pake Mungu,” ikiwa tu imetendwa na mmoja wa wateule, “kwa sababu ni mojawapo wa tabia muhimu na bainifu, yaani zinazowatofautisha wateule na watu wengine, kwamba hawawezi kufanya jambo lolote lisilompendeza Mungu au ambalo limekatazwa na sheria.” [GC 261.1; PK Aya ya 51]

Mafundisho haya potofu  na ya kutisha kama zimwi, kimsingi yanafanana kabisa na lile fundisho la baadaye ya waelimishaji maarufu na wanatheolojia mashuhuri-- kuwa hakuna sheria yoyote ya Mungu isiyobadilika-badilika na iliyo kiwango  cha haki, kwamba kiwango cha uadilifu kinaonyeshwa na jamii yenyewe, na kinakabiliwa na uwezekano wa kubadilika daima. Mawazo haya yote yamevuviwa na roho ile ile kuu (Ibilisi) --yaani yule ambaye, hata miongoni mwa wakazi wa mbinguni wasio na dhambi, alianza kazi yake ya kutafuta kuvunjilia mbali viwango vya haki vya sheria ya Mungu. [GC 261.2; PK Aya ya 52].

Fundisho la maagizo ya Kiungu, yanayoifunga tabia ya wanadamu na kuifanya isiyobadilika, limefanya watu wengi hatimaye kuikataa kabisa sheria ya Mungu. Kwa juhudi kubwa, Wesley aliendelea kuyapinga kwa uimara makosa ya walimu wa antinomian* na kuonyesha kwamba fundisho hili liliwaongoza watu kuona neema inawafanya wafuasi wa Kristo wasihitaji sheria ya Mungu. "Neema ya Mungu iwaokoayo wanadamu wote imefunuliwa." "Hili ni zuri, nalo lakubalika mbele za Mungu Mwokozi wetu; ambaye hutaka watu wote waokolewe, na kupata kujua yaliyo Kweli. Kwa sababu Mungu ni mmoja, na mpatanishi kati ya Mungu na wanadamu ni mmoja, mwanadamu Kristo Yesu; ambaye alijitoa Mwenyewe kuwa ukombozi kwa ajili ya wote, utakaoshuhudiwa kwa majira

yake." Tito 2:11; 1 Timotheo 2:3-6. Roho wa Mungu hutolewa kwa wingi na bure ili kumwezesha kila mtu kushikilia njia ya wokovu. Hivyo ndivyo alivyo Kristo ambaye, “Nuru ya Kweli-Nuru halisi,” “humtia nuru kila mtu ajaye ulimwenguni.” Yohana 1:9. Wanadamu hukosa wokovu kwa kukataa kwao kwa hiari zawadi ya uzima. *(Walimu wa Antinomian walifundisha kuwa neema inawafanya wafuasi wa Kristo wasiwe na hitaji la Sheria ya Mungu, jambo ambalo ni Kinyume cha Maandiko) [GC 261.3; PK Aya ya 53]

**Kuitetea Sheria Ya Maadili (Amri Kumi)**

Katika kujibu dai linalosema kwamba wakati wa kifo cha Kristo kanuni za amri kumi yaani Dekalojia zilifutwa pamoja na sheria ile ya sherehe (ceremonial law), Wesley alisema hivi: “Sheria ya Uadilifu, iliyomo katika Amri Kumi na ambayo manabii walisimamia utekelezaji wake, Kristo Hakuifuta au kuiondoa. Ujio Wake haukuwa na lengo la kuitangua au kuifuta sehemu yake yoyote ile. Hii ni sheria ambayo kamwe haiwezi kuvunjwa, nayo ‘husimama imara kama shahidi mwaminifu mbinguni.’... Hii ilikuwa hivyo tangu mwanzo wa ulimwengu, ‘ikiwa bado haijandikwa kwenye mbao za mawe,’ ilikuwa katika mioyo ya wanadamu wote walipotoka mikononi mwa Muumbaji wao. Na japokuwa herufi zile zilizoandikwa kwa kidole cha Mungu, zimehafifishwa na kuharibiwa na dhambi kwa kiwango kikubwa, bado hazijafutika katu, maadamu bado tuna ufahamu mioyoni mwetu wa mema na mabaya. Kila kipengele cha Sheria hii ya Mungu (Amri Kumi) lazima kibaki kuwa na nguvu juu ya wanadamu wote, na katika Zama zote, kwa kuwa sheria ya Mungu haitegemei ama wakati au mahali, au hali nyingine yoyote inayoweza kubadilikabadilika, bali juu ya asili ya Mungu, na asili ya mwanadamu, na uhusiano kati yao usiobadilikabadilika kwa kila mmoja. [GC 262.1; PK Aya ya 54]

“Sikuja kutangua, bali kutimiliza.’..... Bila shaka au bila swali, maana yake katika sehemu hii ni (ukirejelea bila kubadili yote yaliyotangulia kabla na yanayofuata baada ya hapo)-- nimekuja kulithibitisha katika ukamilifu wake, licha ya tafsiri zote zenye kumetameta za ubunifu wa mwanadamu: nimekuja kuweka mwonekano wake kamili na ulio wazi katika kila kilichokuwa giza au ambacho kilikuwa hakionekani; Nimekuja kutangaza umuhimu wa kweli na kamili wa kila kipengele chake; ili kuwaonyesha urefu na upana, pamoja na ukamilifu wake wote, wa kila amri iliyomo ndani yake, na kimo na kina, na usafi wake upitao ufahamu wetu pamoja na kiini chake cha kiroho katika matawi yake yote.”— Wesley, hotuba ya 25. [GC 262.2; PK Aya ya 55]

Wesley alifundisha upatanifu mkamilifu kati ya sheria na injili. “Kwa hiyo, kuna uhusiano wa karibu mno unaoweza kueleweka, kati ya sheria na injili; kwa upande mmoja, sheria daima hutengeneza njia kwa ajili ya kutuelekeza kwenye injili, na kwa upande mwingine, injili daima hutuongoza kwenye utekelezaji

mkamilifu wa sheria hiyo. Sheria, kwa mfano, inatutaka sisi tumpende Mungu, tumpende jirani, tuwe wapole, tuwe wanyenyekevu, na tuwe watakatifu. Sisi tunajisikia kwamba hatuna utoshelevu kutenda mambo haya, hilo ni hakika, 'kwa mwanadamu hilo haliwezekani;' lakini tunaona ahadi ya Mungu ya kutupatia upendo huo, na kutufanya tuwe wanyenyekevu, wapole, na watakatifu. Basi sisi tunaishikilia hii injili, na habari hizi njema ziletazo furaha; kisha tunapewa kadri ya imani yetu na ile 'haki ya sheria inatimizwa ndani yetu' kupitia njia ya imani iliyo ndani ya Kristo Yesu. .... [GC 263.1; PK Aya ya 56]

"Miongoni mwa maadui wakubwa zaidi wa injili ya Kristo," Wesley alisema, "ni wale wanaoihukumu sheria yenyewe kwa waziwazi na moja kwa moja, na 'kuisema vibaya sheria;' ambao wanawafundisha watu kuvunja sheria (Kwa kuikosoa sheria, Kuifutilia mbali, kulegeza masharti yake, na kuvifungua vifungo vya uwajibikaji wake) Siyo tu amri moja peke yake, iwe ile ndogo sana au kubwa zaidi, bali amri zote (kumi) kwa mpigo.......Jambo la kushangaza zaidi kuliko yote yanayoambatana na udanganyifu huu mkubwa, ambao ni kama ugonjwa wa akili wenye udanganyifu na nguvu, ni kwamba wale ambao wametawaliwa kwa udanganyifu huu kikamilifu, wanaamini kabisa kuwa wao wanamheshimu Kristo kwa kuiangusha sheria Yake, na kwamba wanaitukuza ofisi Yake na huku wanaliharibu fundisho Lake! Naam, wanamheshimu tu kama vile Yuda Iskariote alivyomheshimu kwa kusema, 'Salamu, Rabi na kumbusu.' Naye Bwana anaweza kuzungumza kwa haki kabisa na kila mmoja wao, 'Je, wamsaliti Mwana wa Adamu kwa kumbusu?' Si jambo jingine bali ni kumsaliti Yeye kwa busu, kuzungumzia juu ya damu Yake, na kumnyang'anya taji Yake; kukirahisisha kipengele chochote cha sheria Yake (Amri Kumi), kwa kujifanya kuwa wanafiki kwa kusema tunaieneza injili Yake. Kusema kweli, hakuna yoyote mwenye mwili awezaye kukwepa shitaka hili, ambaye ahubiriye imani kwa namna yoyote ambayo ama moja kwa moja au kwa kuzunguka-zungunguka, ana mwelekeo wa kukiweka kando kipengele chochote kinachohusu utii: anayemhubiri Kristo na huku anafuta au kuhafifisha kwa namna yoyote ile, amri za Mungu zilizo ndogo kabisa."—Ibid. [GC 263.2; PK Aya ya 57]

Kwa wale waliohimiza kwamba "kuihubiri injili hujibu miisho yote ya sheria," Wesley alijibu: "Wazo hili tunalikataa kabisa, kuhubiri haitoi jibu hata kuhusu ule mwisho wa kwanza kabisa wa sheria, maana yake, haiwezi kumsadikisha mtu hatia ya dhambi zake, kuwaamsha wale ambao bado wamelala usingizi ukingoni mwa kuzimu." Mtume Paulo anatangaza kwamba "kwa maana kutambua dhambi huja kwa ajili ya ujuzi wa sheria;" tena ni mpaka hapo tu mwanadamu atakaposhawishika kuwa ni mwenye dhambi, ndipo ataweza kuhisi kweli kweli hitaji lake la damu ya upatanisho ya Kristo……'Wale walio wazima,' kama Bwana wetu Mwenyewe alivyosema, 'hawahitaji tabibu, bali walio wagonjwa.' Kwa hiyo, ni kichekesho kuwaletea tabibu wale ambao ni wazima, au angalau watu

wanaojidhania wenyewe kuwa si wagonjwa. Ni lazima wewe uwaaminishe kwanza kwamba wao wanaumwa vinginevyo hawatakushukuru kwa kazi yako. Kadhalika, ni upuuzi kuwapelekea watu Kristo, ambao mioyo yao ni mizima, watu ambao bado hawajavunjikavunjika (roho haijapondeka bado)."—Ibid., Hotuba ya 35. [GC 264.1; PK Aya ya 58]

Hivyo wakati akiihubiri ile injili ya neema ya Mungu, Wesley, kama Bwana na Mwalimu Wake, alitafuta "kuikuza Sheria, na kuifanya iheshimiwe." Kwa uaminifu aliifanya na kuikamilisha kazi ile, na alijaliwa na Mungu kuyaona matokeo yenye utukufu mzuri. Mwishoni mwa maisha yake marefu yaliyopata miaka themanini-- zaidi ya nusu karne ilitumiwa katika safari za huduma ya kichungaji-- wafuasi wake waliojitokeza wazi wazi walikuwa zaidi ya watu nusu milioni (500,000). Lakini umati ambao kupitia taabu zake, walikuwa wameinuliwa kutoka kwenye uharibifu na kudharauliwa kunakosababishwa na dhambi na kwenda hadi maisha ya  juu na safi zaidi, pamoja na idadi ya watu ambao kwa njia ya mafundisho yake walisaidika kufikia uzoefu wa kina, ulio bora na mkubwa zaidi kiroho, hawa hawatajulikana kamwe mpaka familia nzima ya wale waliokombolewa itakapokusanywa katika ufalme wa Mungu. Maisha yake yanatoa somo la thamani isiyopimika kwa kila Mkristo. Hebu imani hii na unyenyekevu, na juhudi zisizochoka, kujisalimisha kikamilifu na kumcha Mungu alikokuwa nako mtumishi huyu wa Kristo kuakisiwe katika makanisa ya leo! [GC 264.2; PK Aya ya 59]

*Holy see au Kiti Kitakatifu-Holy See ni jina ililojipa serikali ya Kanisa Katoliki la Roma, ambalo inaongozwa na papa kama askofu wa Roma. Kwa hivyo, mamlaka ya Holy See inaenea juu ya Wakatoliki kote ulimwenguni. Tangu 1929 imekuwa ikiishi katika Jiji la Vatikani. Soma zaidi kwenye Historia mtandaoni au Encyclopedia.

# SURA YA 15

## BIBLIA NA MAPINDUZI YA UFARANSA

### (Utawala Wa Hofu Na Ugaidi Na Ulipizaji Kisasi Kule Ufaransa)

Ufupisho: Mapinduzi ya Ufaransa yalifanyika mwaka 1790, nayo yalikuwa matokeo ya nchi hiyo kushindana na Biblia kwa miaka 200. Historia ina mengi ya

kujifunza kwetu ili tusirudie makosa yale yale. Taifa hili lilimkana Mungu waziwazi na matokeo yake yalikuwa ya kutisha. Wahuguenots ambao walikuwa Waprotestant wa Ufaransa, walikuwa kama 400,000 kwa namba, nao walishambuliwa na kuuawa na kanisa la Roma wakitumia kikundi chao cha Majesuit mwaka 1562-1570 BK. Nchi ya Ufaransa ilifilisika mwaka 1789. Utawala wa vitisho au Ugaidi ulikuwa kati ya 1789-1794. na raia 300,000 waliuawa. Sherehe ya mungu wa Mantiki ilifanyika Novemba 1793. Voltaire aliyetajwa humu hatimaye nyumba yake ilitumiwa kuhifadhi Biblia na Chama cha Biblia.

Katika karne ya kumi na sita, Matengenezo ya kanisa yakiwasilisha kwa watu Biblia iliyofunguliwa, yaani iliyo wazi, nayo yalitaka kuingizwa katika nchi zote za Ulaya. Baadhi ya mataifa yaliikaribisha kwa furaha kama mjumbe kutoka Mbinguni. Katika nchi nyingine upapa ulifanikiwa kwa kiwango kikubwa kuzuia kuingia kwake; na nuru ile ya maarifa ya Biblia pamoja na mivuto yake inayoinua ilikuwa karibu kuondolewa kabisa. Katika nchi moja, ingawa nuru ilipata kuingia mle, haikukuweza kutambuliwa kwasababu ya giza lililokuwa humo. Kwa karne nyingi, Ukweli na makosa vilishindania utawala, yaani kimoja kikitaka kutawala kingine. Mwishowe uovu ulishinda, na Ukweli wa Mbinguni ulipigwa teke nje kwa nguvu. "Hii ndiyo hukumu, ya kuwa nuru imekuja ulimwenguni, na watu wakapenda giza kuliko nuru." Yohana 3:19. Taifa liliachwa livune matokeo ya uchaguzi wa njia ambayo ilitaka kupitia. Kizuizi cha Roho Mtakatifu wa Mungu kiliondolewa kutoka kwa watu ambao walidharau kipawa cha neema Yake. Uovu uliruhusiwa kufika hatua ya kukomaa. Na ulimwengu wote ukaona tunda la kuikataa nuru kwa makusudi. [GC 265.1; PK Aya ya 1]

Vita dhidi ya Biblia, iliyoendelea kwa karne nyingi katika nchi Ufaransa, iliishia katika matukio yaliyoleta Mapinduzi. Mpasuko huo wa kutisha ulikuwa matokeo halali tu ya ukandamizaji wa Maandiko wa Rumi. (Tazama kiambatisho.) Uliwasilisha kielelezo cha wazi kuliko vyote ambavyo ulimwengu umewahi kushuhudia katika utekelezaji kazi wa sera ya upapa-- kielelezo cha matokeo ambayo kwa zaidi ya miaka elfu moja ya mafundisho ya Kanisa la Roma yalikuwa yamejielekeza kwayo. [GC 265.2; PK Aya ya 2]

Ukandamizaji wa Maandiko wakati wa kipindi cha utawala wa upapa ulitabiriwa na manabii; na Yohana Mwandishi wa Kitabu cha Ufunuo pia unatuelekeza kwenye matokeo ya kutisha ambayo yangetokea hususani katika nchi hiyo ya Ufaransa kutoka kwa utawala wa mabavu wa yule "mtu wa dhambi" 2 Thes 2:3, 4 [GC 266.1; PK Aya ya 3]

Malaika wa Bwana alisema hivi: “Nao wataukanyaga mji mtakatifu miezi arobaini na miwili..... Nami nitawaruhusu mashahidi Wangu wawili, nao watatoa unabii siku elfu na mia mbili na sitini (1260), hali wamevikwa magunia…… Hata watakapoumaliza ushuhuda wao, Yule mnyama atokaye katika kuzimu atafanya vita nao, naye atawashinda na kuwaua. Na mizoga yao itakuwa katika njia ya mji

ule mkuu, uitwao kwa jinsi ya roho Sodoma, na Misri, tena na hapo Bwana wao aliposulubiwa. Nao wakaao juu ya nchi wafurahi juu yao na kushangilia. Nao watapelekeana zawadi wao kwa wao, kwa kuwa manabii hao wawili waliwatesa wao wakaao juu ya nchi. Na baada ya siku hizo tatu u nusu, roho ya uhai itokayo kwa Mungu ikawaingia, wakasimama juu ya miguu yao; na hofu kuu ikawaangukia watu waliowatazama". Ufunuo 11: 2-11. [GC 266.2; PK Aya ya 4]

Vipindi vilivyotajwa hapo juu -- "miezi arobaini na miwili," na "siku elfu na mia mbili na sitini" - vinakwenda sambamba, yaani vinahusu kipindi kile kile, na vyote kwa pamoja vinawakilisha kipindi cha muda ambacho Kanisa la Kristo lilipaswa kupata mateso kutoka Rumi. Miaka 1260 ya utawala wa kipapa ilianza mnamo 538 BK, na kwa hivyo ingemalizika mnamo 1798 BK. (Tazama Kiambatisho.) Wakati huo jeshi la Kifaransa liliingia Rumi na kumkamata papa na kumweka kifungoni, na alikufa akiwa uhamishoni*. Ingawa papa mpya alichaguliwa baada ya mfupi, utawala wa upapa ulikuwa kamwe haujawahi kuwa na nguvu kama uliokuwa nayo kabla au kutumia silaha tangu wakati huo. *(Soma historia zaidi ya Jenerali Bethier chini ya Napoleon, na yalimtokea papa Pius wa Sita) [GC 266.3; PK Aya ya 5]

**Walitoa Unabii Wao Wakiwa Wamevikwa Magunia**

Mateso ya kanisa hayakuendelea kwa kipindi chote cha miaka 1260. Rehema Zake Mungu kwa watu Wake zilikifupisha kipindi kile cha majaribu yao makali. Alipokuwa akitabiri mapema ile "dhiki kuu au taabu kuu" ambayo ingelipata kanisa Lake, Mkombozi alisema: "Na kama siku hizo zisingalifupizwa, asingeokoka mtu yeyote; lakini kwa ajili ya wateule zitafupizwa siku hizo” Mathayo 24:22. Kutokana na nguvu ya Matengenezo yale ya kanisa, mateso yale yalikomeshwa kabla ya 1798. [GC 266.4; PK Aya ya 6]

Kuhusiana na mashahidi wale wawili: nabii huyo anatangaza tena akisema: "Hao ndio ile mizeituni miwili na vile vinara viwili visimamavyo mbele za Bwana wa nchi." "Neno Lako," Anasema Mwandishi wa Zaburi, "ni taa ya miguu yangu, na mwanga wa njia yangu." Ufunuo11:4; Zaburi 119:105. Mashahidi hawa wawili wanawakilisha Maandiko ya Agano la Kale na Agano Jipya. Maagano hayo mawili ni ushuhuda muhimu wa maana kuhusu Chanzo na uendelevu wa Sheria ya Mungu (inadumu milele). Yote mawili pia ni mashahidi kwa ajili ya mpango wa wokovu. Mifano (vivuli), kafara, na unabii wa Agano la Kale huelekeza mbele kwa Mkombozi anayekuja. Injili na Nyaraka za Agano Jipya huelezea juu ya Mwokozi aliyekuja kwa namna ile sahihi kabisa iliyotabiriwa katika mifano na unabii. [GC 267.1; PK Aya ya 7]

"Watatoa unabii kwa siku elfu moja mia mbili na sitini, wakiwa wamevaa nguo za magunia." Katika sehemu kubwa ya kipindi hiki, mashahidi wa Mungu walibaki katika hali ya kufichwafichwa. Mamlaka ya kipapa yalijitahidi kuwaficha watu

Neno la Kweli na kuweka mbele yao mashahidi wa uwongo ili wapinge ushuhuda wake. (Tazama kiambatisho.) Wakati Biblia ilipopigwa marufuku na mamlaka ya kidini na ya kiraia; wakati ushuhuda wake ulipopindishwa na kila juhudi ikafanywa ili watu na mapepo waweze kubuni njia ya kugeuza mawazo ya watu mbali na hiyo Biblia: wakati ambapo watu waliothubutu kutangaza Kweli Zake takatifu walisakwa, walisalitiwa, waliteswa, walizikwa katika magereza madogo chini ya ardhi, waliuawa kwasababu ya imani yao (wafia dini), au kulazimishwa kukimbilia kwenye vifungo vya milima, na kwenye mashimo na mapango ya dunia - hapo ndipo mashahidi waaminifu walipotoa unabii wao na kushuhudia wakiwa wamevaa nguo za magunia. Lakini waliendeleza ushuhuda wao kwa kipindi chote cha miaka 1260. Katika nyakati za giza kulikuwa na watu waaminifu ambao walipenda Neno la Mungu na walikuwa na wivu kwa ajili ya heshima Yake. Hawa watumishi waaminifu walipewa hekima, nguvu, na mamlaka ya kutangaza Ukweli Wake Mungu katika kipindi chote cha wakati huu. [GC 267.2; PK Aya ya 8]

"Na mtu akitaka kuwadhuru, moto hutoka katika vinywa vyao na kuwala adui zao. Na mtu akitaka kuwadhuru, hivyo ndivyo impasavyo kuuawa." Ufunuo 11:5. Wanadamu hawawezi kulikanyaga Neno la Mungu chini ya miguu yao bila ya kupata madhara au adhabu. Maana ya onyo hili la kutisha imefafanuliwa katika sura ya mwisho ya kitabu cha Ufunuo: "Namshuhudia kila mtu ayasikiaye Maneno ya unabii wa kitabu hiki, Mtu yeyote akiyaongeza, Mungu atamwongezea hayo mapigo yaliyoandikwa katika kitabu hiki. Na mtu ye yote akiondoa lolote katika Maneno ya unabii wa kitabu hiki, Mungu atamwondolea sehemu yake katika ule mti wa uzima, na katika ule mji mtakatifu (Ufu 21), ambao habari zake zimeandikwa katika kitabu hiki." Ufunuo 22:18, 19. [GC 268.1; PK Aya ya 9]

**Matokeo Ya Uasi Dhidi Ya Mungu**

Hayo ndiyo maonyo ambayo Mwenyezi Mungu ametoa ili kuwalinda watu wasibadilishe kwa namna yoyote ile, kile ambacho amekifunua au kukiamuru. Hukumu hizi nzito zinawahusu wale wote ambao kwa mvuto wao, huwaongoza watu wengine kuichukulia sheria ya Mungu kirahisi au kuidharau. Hukumu hizi lazima ziwasababishe watu wanaotangaza kwa mzaha kuogopa na kutetemeka, wale wanaotangaza kwa purukushani yao kwamba kutii au kutotii Sheria ya Mungu ni jambo lisilo na madhara au ni dogo tu (Amri Kumi). Wale wote ambao huinua maoni yao juu ya ufunuo wa Mungu, wote ambao hubadilisha maana iliyo wazi ya Maandiko kwa ajili ya manufaa yao, au kwa ajili ya kufanana na ulimwengu, wanajitwika wajibu wa kutisha. Neno lililoandikwa, sheria ya Mungu, litaipima tabia ya kila mtu na kuwahukumu wote ambao kipimo hichi ambacho kamwe hakijawahi kukosea, kitawatangaza kuwa wamepungua. [GC 268.2; PK Aya ya 10]

"Watakapokuwa wamemaliza au wanamaliza ushuhuda wao." Kipindi ambacho mashahidi wawili walipaswa kutoa unabii wao wakiwa wamevaa nguo za magunia, kilimalizika mwaka 1798. Walipokuwa wanakaribia kumaliza kazi yao mafichoni, vita ilipaswa kupigwana dhidi yao na mamlaka ile iliyowakilishwa na "mnyama atokaye katika kuzimu." Katika mataifa mengi ya Ulaya mamlaka zilizotawala kanisani na serikalini kwa karne nyingi zilikuwa zinaongozwa na Shetani kupitia kile chombo chake cha upapa. Lakini, hapa unaleta mwonekano mpya wa udhihirisho wa nguvu ya kishetani. (Ufunuo 13:1, 2, 7 na ufunuo 17:12, 13) [GC 268.3; PK Aya ya 11]

Ilikuwa ni sera ya Rumi, chini ya madai yake kuwa inaiheshimu Biblia, kuifungia au kuitunza katika lugha isiyojulikana (Kilatini) na kuificha mbali ili isionwe na watu. Chini ya utawala wake mashahidi walitoa unabii wao huku "wamevaa nguo za magunia." Lakini mamlaka nyingine-- yule mnyama atokaye shimo la kuzimu (Dan7:17) alipaswa ainuke ili kufanya vita vya wazi wazi dhidi ya Neno la Mungu. [GC 269.1; PK Aya ya 12]

"Mji mkuu" ambao katikati ya barabara zake mashahidi wameuawa, na ambamo mizoga yao imelala ni Misri kwa jinsi ya kiroho". Kati ya mataifa yote yaliyosimuliwa katika historia ya Biblia, Misri ndiyo ilikuwa na ujasiri mkubwa zaidi na kupinga amri Zake. Hakuna mfalme yeyote aliyediriki kufanya maasi ya waziwazi na kuonyesha ujeuri na kiburi dhidi ya mamlaka ya Mbinguni kama alivyofanya Farao wa Misri. Wakati ujumbe ulipoletwa kwake na Musa, katika jina la Bwana, Farao alijibu kwa kiburi akisema: “BWANA ni nani, hata niisikilize sauti Yake, na kuwapa Israeli ruhusa waende zao? Mimi simjui BWANA, wala sitawapa Israeli ruhusa waende zao.” Kutoka 5:2. Huu ni ukafiri yaani kukana kuwa hakuna Mungu, na taifa hilo linalowakilishwa hapo na Misri lingetoa sauti kama ile na madai yanayofanana na yale yale na kukana kwamba hakuna Mungu aliye hai, tena lingeonyesha roho inayofanana na ile ya kutokuamini na ukaidi wa kudhamiria kabisa. “Mji ule mkuu” pia umelinganishwa na Sodoma “kwa jinsi ya kiroho.” Ufisadi wa Sodoma kwa kuvunja amri za Mungu (Amri Kumi) ulionekana hasa katika dhambi za uchafu wa ngono. Na dhambi hii ilikuwa ni sifa kuu ya taifa ambalo lingetimiza vipengele vya Andiko hili. [GC 269.2; PK Aya ya 13]

Kwa mujibu wa Maneno ya nabii huyo, muda mfupi kabla ya mwaka wa 1798, mamlaka fulani ambaye mwasisi wake ni Shetani ingeinuka na kufanya vita dhidi ya Biblia. Na katika sehemu au nchi hiyo ambapo ushuhuda wa mashahidi hawa wawili wa Mungu ungenyamazishwa kwa njia hiyo, kungejionyesha ukafiri, (kumkana Mungu), tabia ya kumkana Mungu ingeonekana waziwazi kama alivyofanya Farao na tamaa za mwili za uchafu wa ngono wa Sodoma [GC 269.3; PK Aya ya 14]

**Utimilizo Wa Kuvutia Sana Wa Unabii Huo**

Unabii huu ulitimizwa kikamilifu na kwa namna ya kushangaza katika historia ya Ufaransa. Wakati wa Mapinduzi, ya mwaka 1793, “Ulimwengu, kwa mara ya kwanza ulisikia habari la mkusanyiko wa watu, waliozaliwa na kuelimishwa katika ustaarabu, wakijitwalia haki ya kulitawala mojawapo la mataifa bora sana ya Ulaya, wakiinua sauti zao kwa pamoja na kuikataa Kweli ile muhimu na takatifu sana ambayo roho ya mwanadamu hupokea, na kukana kwa kauli yenye umoja wa imani na ibada ya Mungu.” - Sir Walter Scott, Maisha ya Napoleon, juzuu. 1, sura ya 17. "Ufaransa ni taifa pekee ulimwenguni ambalo rekodi yake halisi iliyoandikwa inaendelea kuishi, ya kwamba kama taifa iliinua mkono wake kufanya uasi wa wazi dhidi ya Muumbaji wa ulimwengu (Mwenyezi Mungu). Waliomkufuru au kumtukana Mungu ni wengi, makafiri au wanaomkana Mungu ni wengi, wamekuwepo na bado wataendelea kuwepo katika nchi ya Uingereza, Ujerumani, Uhispania, na kwingineko; lakini taifa la Ufaransa linasimama peke yake kama taifa moja pekee ulimwenguni ambalo serikali yake, kwa amri ya Bunge lake ilitangaza kuwa hakuna Mungu, na ambalo watu wake waliokuwako katika mji mkuu, na idadi kubwa ya raia wa mahali pengine, wanawake na wanaume, walicheza dansi na kuimba kwa furaha wakikubaliana na tangazo hilo.” -Jarida la Blackwood, Novemba, 1870. [GC 269.4; PK Aya ya 15]

Ufaransa pia ilistawisha tabia ile iliyoitambulisha Sodoma kwa namna ya pekee. Wakati wa Mapinduzi kulikuwa na mwonekano wa wazi wa kuporomoka kwa maadili na ufisadi ambao ulifanana na ule uliosababisha kuharibiwa kwa miji ile ya uwandani (Mwa 13:12 Sodoma, Gomora, Adma, Zoar na Zeboim). Na mwanahistoria anawasilisha pamoja, tabia ya kumkana Mungu (ukafiri) na ile ya uhuru wa kujibwaga kwenye dhambi za ngono kiholela, na tamaa zingine za mwili iliyofanywa na Ufaransa,* kama ilivyotabiriwa katika unabii huu: “Kwa mshikamano wa karibu sana na sheria hizi zinazoiathiri dini, ilikuwa ni amri ile iliyodhoofisha mshikamano wa ndoa - yaani, kifungo kile kitakatifu sana ambacho wanadamu wanaweza kuwa nacho, na ambacho kudumu kwake kuna mwelekeo wa nguvu sana katika kuiunganisha na kuiimarisha jamii nzima - nao waliifanya ndoa kuwa mkataba tu wa kiserikali, ambao ulikuwa na wa mpito tu, na ambao watu wote wawili wanaweza kuufanya kwa kufunga ndoa na kuachana wanapopenda, kulingana na starehe yao.... Ikiwa mapepo wenyewe walikuwa wamepania kuanza kufanya kazi ya kuvumbua mfumo wa kuharibu kabisa kitu chochote kilichokuwa kinaheshimika, kizuri, au kinachoendelea kudumu katika maisha ya nyumbani, na wakati ule ule kujipatia uhakika kwamba madhara yale mabaya ambayo lilikuwa ni lengo lao kuyasababisha yangeweza kuendelezwa toka kizazi kimoja hadi kizazi kingine, basi, wasingekuwa wamevumbua mbinu iliyo na uwezo wa kufanikisha mambo zaidi kuliko ile ya kuishusha hadhi ya ndoa.... Sophie Arnoult, mwanasanaa wa michezo ya kuigiza wa kike (drama), aliyejulikana sana kwa maneno na misemo yake ya busara na kuchekesha, aliieleza ndoa ile ya Kiserikali kama ‘Sakramenti ya uzinzi.’” (soma zaidi kuhusu

dhambi hizi za ngono Kingereza* Licentiousness)- Scott, gombo la 1, sura ya 17..... [GC 270.1; PK Aya ya 16]

"Mahali pia ambapo Bwana wetu alisulubiwa." Ufafanuzi wa kipengele hichi cha unabii pia kilitimizwa na nchi ya Ufaransa. Hakuna nchi nyingine yoyote ambayo ndani yake roho ya uadui dhidi ya Kristo ilijionyesha kwa namna ya kushangaza zaidi. Hakuna nchi nyingine yoyote ambayo ndani yake Kweli ilikuwa imekabiliana na upinzani mkali na wa kikatili sana kuliko nchi ya Ufaransa. Katika mateso ambayo Ufaransa iliwapatiliza wale walioikiri Injili, ilikuwa imemsulibisha Kristo katika umbile la wale wanafunzi Wake [GC 271.1; PK Aya ya 17]

Karne baada ya karne damu za watakatifu zilimwagwa. Wakati ule ule Wawaldensia walipokuwa wakipoteza maisha yao juu ya milima ya Piedmont kwa ajili ya “Neno la Mungu, na ushuhuda wa Yesu Kristo,” ushuhuda kama ule ule kwa ajili ya Ukweli ulikuwa ukitolewa na ndugu zao Waalbigensi wa Ufaransa. Katika siku za Matengenezo za kanisa wafuasi Wake waliuawa kwa mateso yenye maumivu ya kutisha. Mfalme na wasaidizi wake, wanawake na wajakazi wa nyumba ya mfalme, koo za vyeo vya juu, maamiri na maaskari wa mfalme, waliyafurahisha macho yao kwa kuyaangalia mateso yaliyoleta maumivu makali kwa mashahidi wa Yesu [wafia dini]. Wahuguenoti jasiri, wakipigania haki zao za msingi, ambazo moyo wa mwanadamu unazichukulia kama takatifu sana, walikuwa wamemwaga damu yao katika viwanja vingi vya vita katika mapambano makali. Waprotestanti walihesabiwa kama wahalifu/maharamia, bei ilipangwa kwa ajili ya vichwa vyao, na waliwindwa kama wanyama wa porini. [GC 271.2; PK Aya ya 18]

"Kanisa Jangwani," wazaliwa wachache wa Wakristo wa zamani ambao bado walikuwa huko Ufaransa katika karne ya kumi na nane, wakiwa wamejificha kwenye milima ya kusini, bado waliendelea kudumisha imani ya baba zao. Walipothubutu kukutana usiku kando ya milima au kwenye bonde mojawapo lililojificha nyikani, walifukuzwa na askari wapanda farasi na kukokotwa kwenda kuwa watumwa katika majahazi, maisha yao yote. Wale waliokuwa na maisha safi kabisa, watu wema, waungwana sana, na wenye akili nyingi sana miongoni mwa Wafaransa, walifungwa kwa minyororo, na kupata mateso ya kutisha sana, nao wakafungwa pamoja na majambazi na watu waliokodishwa kufanya mauaji ya siri. (Angalia Wylie, kitabu cha 22, sura ya 6.) Wengine waliotendewa kwa huruma kuliko wengine, walipigwa risasi na kufa kwa njia ya kikatili, wakiwa hawana silaha wala msaada wowote, walipokuwa wamepiga magoti yao wakiomba. Mamia ya wanaume wenye umri mkubwa, kwenye bonde mojawapo la upweke kule nyikani, walifukuzwa na askari wapanda farasi na kuburutwa kwenda kutumika kama watumwa katika majahazi yenye matanga kwa maisha

yao yote. (Angalia Wylie, kitabu cha 22, sura ya 6.) Mamia ya wanaume wenye umri mkubwa, wanawake wasio na ulinzi pamoja na watoto wasio na hatia yoyote waliachwa wakiwa wamekufa juu ya ardhi katika maeneo yao ya mikutano. Katika kuzunguka milima au misitu, mahali ambapo walikuwa wamezoea kukutana, halikuwa jambo la ajabu kukuta "kila hatua nne, maiti zikiwa zimezagaa kwa wingi katika nyasi, na zingine zikiwa zimening'inia juu ya miti." Nchi yao, ikiwa imeachwa ukiwa kwa panga, shoka, na kuni, "iligeuzwa na kuwa nyika kubwa yenye huzuni." "Ukatili na uovu huu haukutekelezwa katika kipindi cha giza, lakini katika Enzi nzuri hizo za Mwangaza au maendeleo za Mfalme Louis wa XVI. Sayansi ya wakati huo ilikuwa imekua vyema, wasomi, maandishi, na waandishi vilisheheni, wanafalsafa, wanatheolojia kwenye nyua mbalimbali za mji mkuu walikuwa na elimu za juu na umbuji nao walionekana kana kwamba wanazo zile tabia njema za upole, huruma na upendo.” -Ibid., b. 22, sura ya 7. [GC 271.3; PK Aya ya 19]

**Uhalifu Mbaya Mno**

Lakini tendo baya mno na la kutisha katika orodha ya maovu yote (blackest catalogue), yaani uovu wa wa kutisha mno kati ya matendo ya kishetani ya karne zote yenye kutisha, ilikuwa ni yale mauaji ya yaliyotokea eneo la Mtakatifu Bartholomayo (St. Bartholomew Massacre). Ulimwengu bado unayakumbuka kwa kutetemeka na kuchukizwa sana, matukio hayo ya kuwashambulia watu kwa ghafula, kitendo ambacho ni cha kisaliti na kinyama. Mfalme wa Ufaransa akiwa ameshinikizwa na mapadre wa Kiroma, pamoja na maaskofu wao, alitoa kibali cha kazi hiyo ya kinyama ipate kufanyika. Mlio wa Kengele usiku wa manane, ilikuwa ndiyo ishara ya uchinjaji huo. Maelfu ya Waprotestanti wakiwa wamesinzia kimya katika nyumba zao, wakiitumainia ahadi [ya ulinzi] iliyotolewa kwa heshima ya mfalme, waliburutwa nje bila kupewa onyo lolote na kuuawa kwa njia ya kikatili sana. [GC 272.1; PK Aya ya 20]

Kama vile Kristo alivyokuwa kiongozi Asiyeonekana kwa macho na watu Wake kutoka katika utumwa wa Misri, kadhalika Shetani alikuwa kiongozi asiyeonekana wa raia zake waliofanya kazi ile ya kutisha ya kuzidisha idadi ya wafia dini. Kwa siku saba mfululizo mauaji hayo ya kinyama ya maelfu yaliendelea katika jiji la Paris, katika siku tatu za kwanza kwa hasira kali isiyoelezeka. Na mauaji hayakuwa mjini peke yake, lakini kwa amri maalum ya mfalme yalienezwa katika majimbo na miji yote ambayo Waprotestanti walipatikana. Kulikuwa hakuna kujali umri au jinsia. Hata mtoto mchanga asiyekuwa na hatia yoyote hakuachwa, wala mzee mkongwe mwenye mvi. Mwuungwana na mkulima, mzee na kijana, mama na mtoto, walikatwa-katwa vipande vipande kwa pamoja. Katika Ufaransa nzima ‘chinja-chinja’ iliendelea kwa miezi miwili. Elfu sabini ya maua ya taifa hilo yaliangamia (Watu 70,000 bora wa taifa waliangamizwa). [GC 272.2; PK Aya ya 21]

**Mandhari Za Furaha Na Kujisifu Mno**

"Taarifa za mauaji hayo ya kinyama ya maelfu ya watoto, wanaume na wanawake zilipofika Rumi, shangwe na vifijo miongoni mwa mapadre na maaskofu haikuwa na mipaka. Kardinali wa Lorraine alimzawadia mjumbe aliyeleta ripoti fedha za kifaransa elfu moja (crowns); Mizinga ya Mtakatifu Angelo ilinguruma saluti ya furaha; na kengele zilipigwa kutoka kila mnara; mioto mikubwa ya kusherekea tukio, iligeuza usiku kuwa mchana; na papa Gregory wa XIII, akisindikizwa na makadinali na viongozi wa kanisa walioheshimiwa, walikwenda kwa maandamano marefu katika kanisa la Mtakatifu Louis, ambapo kardinali wa Lorraine aliimba wimbo wa shukrani na sifa kwa Mwenyezi Mungu 'Te Deum -tunakusifu Ee Mungu' - Medali ikatengenezwa na kuwekwa ukutani ili kuwa kumbukizi ya mauaji makuu ya kinyama ya maelfu, na ndani ya Vatican bado zinaweza kuonekana ukutani picha tatu za kuchorwa na Vasari,* nazo zinaelezea shambulio la  jemedari wa jeshi la wanamaji na manowari, mfalme akiwa katika kikao cha baraza wakipanga mauaji, na mauaji yenyewe ya kinyama kwa wanaume, wanawake, na watoto yakitekelezwa. Papa Gregori akamtumia mfalme Charles Ua la Waridi la Dhahabu; na miezi minne baada ya mauaji yale ya kinyama,... alisikiliza na kuridhika kwa furaha, hubiri lililotolewa na padre mmoja wa Kifaransa,... ambaye aliongelea habari za "siku ile iliyojaa furaha nyingi mno na nderemo, wakati baba mtakatifu sana, alipozipokea taarifa na kwenda kwa kicho kutoa shukrani kwa Mungu na kwa Mtakatifu Louis."- Henry White, The Massacre of St. Bartholomew, sura ya 14, aya ya 34. *(zilichorwa mbichi zikakauka-google frescoes of Vasari) [GC 272.3; PK Aya ya 22]

Yule roho mbaya, yaani pepo mkuu aliyehamasisha mauaji ya kinyama ya Mtakatifu Bartholomayo aliongoza pia katika matukio ya Mapinduzi. Yesu Kristo alihukumiwa kuwa Yeye ni mlaghai na kelele zilizopigwa na mkusanyiko ule wa makafiri wa Kifaransa zilikuwa zinasema hivi: "Mponde Kabisa Mtu Huyo Mwovu Sana," wakimaanisha Kristo. Makufuru yale yaliyofanywa kwa ushupavu dhidi ya Mbingu na uovu  wa kuchukiza sana, vilienda sambamba, na ukatili na uovu wa kupindukia miongoni mwa wanadamu waliofanana na mazimwi, na hao ndio walioheshimiwa na kutukuzwa sana, yaani, majitu yaliyokuwa na unyama na ukatili  yaliachwa tu kufanya ukatili na uovu wao. Katika mambo haya yote, walimsujudu Shetani, kwa kumpa heshima; wakati Kristo, katika sifa ya tabia Yake ya Ukweli, usafi wa maisha, na upendo usio na ubinafsi ndani yake, alisulibiwa. [GC 273.1; PK Aya ya 23]

"Yule mnyama atokaye kuzimu atafanya vita nao, naye atawashinda na kuwaua." Mamlaka ya kikanisa iliyotawala katika nchi ya Ufaransa wakati wa Mapinduzi na utawala wa Kigaidi na hofu ambao haukuamini kwamba kuna Mungu, ilifanya vita dhidi ya Mungu na Neno Lake takatifu kwa namna ambayo

ulimwengu haujawahi kushuhudia. Ibada ya Mungu ilipigwa marufuku kwa amri ya Bunge la taifa. Biblia zilikusanywa na kuchomwa moto hadharani kwa kila aina ya dhihaka na dharau inayowezekana kuonyeshwa. Sheria ya Mungu ilikanyagwa-kanyagwa chini ya miguu yao. Taasisi zote za Biblia au Mambo yaliyowekwa katika Biblia ili yapate kutendwa yalifutiliwa mbali. Siku ya mapumziko ya kila juma iliwekwa kando na badala yake kila siku ya kumi ilitumiwa dhidi ya Mungu, watu walisherekea mapumziko haya kwa ulevi, ulafi, ngono na pia kejeli na kufuru dhidi ya Mungu. Ubatizo na Ushirika Mtakatifu (Meza ya Bwana) vilipigwa marufuku. Na matangazo yalibandikwa wazi katika maeneo ya makaburi yenye maneno yasemayo kuwa kifo kilikuwa ni usingizi wa milele. [GC 273.2; PK Aya ya 24]

Hofu ya Mungu yaani kumcha Mungu kulisemwa kuwa mbali sana na mwanzo wa hekima, wakaendelea kusema kwa dharau na kufuru kwamba 'kumcha Mungu ndiyo chanzo cha upumbavu.' Aina zote za ibada za kidini zilipigwa marufuku isipokuwa ibada za uhuru na za nchi. "Askofu wa Paris aliyewekwa kikatiba aliletwa hadharani ili atende jukumu kubwa katika upuuzi huu wa kifidhuli kabisa na wa kashfa mbaya sana uliowahi kufanyika mbele ya wawakilishi wa kitaifa... Aliletwa mbele ya maandamano kamili, akiwa na wasaidizi wake ili aje kutangaza kwenye mkutano ule kwamba dini ile aliyokuwa ameifundisha kwa miaka mingi, kwa kila hali zake zote, ilikuwa ni ujanja na uongo mtupu wa kipadri, ambao haukuwa na msingi wowote katika historia na katika Ukweli mtakatifu. Alikanusha waziwazi kwa maneno mazito yanayoeleweka kabisa, uwepo wa Mungu ambaye mtumishi huyu alikuwa ameyatoa maisha yake wakfu kumwabudu, na aliamua kujitoa kutumia muda wake wote wa siku za usoni kuabudu uhuru, usawa, mambo mema, na uadilifu. Kisha aliweka mezani mapambo yake ya kiaskofu, na kupokea kumbatio la kindugu kutoka kwa mwenyekiti wa kongamano lile. Baadhi ya mapadri walioasi imani walifuata mfano wa kiongozi huyu wa kiroho." - Scott, juz. 1, sura ya 17. [GC 274.1; PK Aya ya 25]

"Nao wakaao juu ya nchi wafurahi juu yao na kushangilia. Nao watapelekeana zawadi wao kwa wao, kwa kuwa manabii hao wawili waliwatesa wao wakaao juu ya nchi." Ufaransa hii ya kikafiri, iliyomkataa Mungu, ilikuwa imenyamazisha sauti inayotoa maonyo ya mashahidi wawili wa Mungu. Neno la Ukweli likalala likiwa limekufa katika mitaa yake, na wale ambao walichukia makatazo na masharti ya sheria ya Mungu walishangilia sana. Watu wakamtukana na kumkana Mfalme wa mbinguni hadharani. Kama wenye dhambi wa zamani walivyofanya, walipiga kelele: "Mungu ajuaje? Yako maarifa Kwake aliye juu? Zaburi 73:11. [GC 274.2; PK Aya ya 26]

**Ushupavu Uliojaa Uhuru**

Kwa ujasiri uliojaa kufuru na matusi kuliko inavyoweza kuaminika, mmojawapo wa mapadri wa mfumo mpya wa utawala, alisema hivi: “Mungu, kama kweli upo, basi, lipiza kisasi kwa ajili ya Jina Lako ambalo sifa Zake zimejeruhiwa. Nakutangazia kwa jeuri nawe hebu thubutu kufanya kitu basi.* Wewe unakaa kimya tu; Je, huthubutu kuzituma radi Zako. Ni nani baada ya tukio hili atakayeamini uwepo Wako?” - Lacretelle, History, gombo la 11, uk. 309; ni gombo la 1, sura ya 10, katika kitabu cha Sir Archibald Alison, History of Europe. Huu ni mwangwi wa dai lile la Farao huko Misri aliposema: “BWANA ni nani, hata niisikilize sauti Yake?” “Mimi simjui BWANA!” *(Maneno haya yasemwapo kwa Mungu maana yake halisi ni Mungu, mimi ninakutukana Wewe! Ila kwa mwanadamu inamaanisha, sitakutii kamwe) [GC 274.3; PK Aya ya 27]

"Mpumbavu amesema moyoni, Hakuna Mungu." Zaburi 14:1. Naye Bwana anatangaza hivi kuhusu wapotoshaji wa Ukweli Wake: "Upumbavu wao utakuwa dhahiri kwa watu wote." 2 Timotheo 3: 9. Baada ya Ufaransa kupiga marufuku ibada ya Mungu aliye hai, “Yeye Aliye juu, aliyetukuka, na akaaye milele,” “haikuchukua muda mrefu Ufaransa kuporomoka chini hadi kusujudia sanamu kwa namna ya kufedhehesha sana, kwa kumwabudu mungu mke wa mantiki/fikra (Goddess of Reason), katika utu wa mwanamke mwovu na kahaba. Na jambo hili lilifanywa kwenye mkutano wa wawakilishi wa taifa, na wale wenye mamlaka ya juu kabisa serikalini na Bungeni! Anasema mwanahistoria: “Moja ya sherehe za wakati huu wa wendawazimu, ni upuuzi uliounganishwa na kukosa kicho mbele za Mungu mbele za umma. Milango ya mkutano ilifunguliwa wazi kukiruhusu kikundi cha bendi cha wanamuziki, mbele yao wakiwa wametanguliwa na viongozi wakuu wa jiji, waliingia kwa maandamano makubwa na ya kicho, wakiimba tenzi ya kuusifu uhuru, na kumsindikiza mtu aliyefunikwa kilemba, ambaye ndiye wangemwabudu siku za usoni, huyu alikuwa mwanamke waliyemwita Mungu mke wa Mantiki/fikra. Alipoletwa ndani ya Baraza, alifunuliwa akiwa katika hali nzuri, na yenye utayari, kwa maonyesho na kupokea ibada ya watu, aliketishwa mkono wa kuume wa mwenyekiti wa mkutano, ndipo alitambuliwa na watu wote kuwa ni binti mchezaji wa muziki unaohusisha masimulizi na sanaa ya uigizaji (opera music drama).... Binti huyu kama mwakilishi stahiki wa Mungu hoja wanayemwabudu (uasherati), Mkutano ule wa kitaifa wa Ufaransa ulifanya ibada hadharani kwa ajili yake. [PK 275.1; PK Aya ya 28]

"Mchezo huu wa kuigiza wa kipagani, na kipuuzi, uliofanywa mtindo wa vitendo bila kusema neno lolote,* ulimkufuru Mungu; na usimikaji huu wa mungu wa kike wa Mantiki ulirudiwa upya kuigizwa tena kwa taifa zima na kuigwa na watu wote kwenye taifa katika maeneo ambayo wakazi wake walitamani kujionyesha kwa watu kuwa walikuwa wanaafikiana kabisa na hatua hii ya vilele

vya juu vya Mapinduzi." *(mummery)- Scott, gombo la 1, sura ya 17. [GC 275.2; PK Aya ya 29]

Msemaji aliyetambulisha ibada ya Mantiki alisema: "Enyi watunga sheria! Ushabiki wa kushikilia mambo bila ya kutumia akili umeondoka na nafasi yake imechukuliwa na Mantiki. Macho yake yasiyoona vizuri hayakuweza kustahimili mwangaza mkali wa nuru. Siku hii mkutano mkubwa umekusanyika chini ya paa hili la nakshi ya mawe na chuma lililojengwa na Wagothiki, ambalo, kwa mara ya kwanza limerudisha mwangi wa ukweli. Pale Wafaransa wamesherehekea ibada ya pekee ya kweli, -- Ibada ya uhuru, Ibada ya Mantiki. Hapa tumetoa maombi yetu kwa ajili ya ustawi wa majeshi ya Jamhuri hii. Hapa tumezitupa mbali sanamu zisizokuwa na uhai ndani yake na kupata Mungu wa Mantiki, yaani, sanamu hii iliyo hai ya mwanamke huyu anayewakilisha ibada hii ya sanamu, kiumbe huyu ni kazi bora kabisa ya maumbile na asili"* (Kol 3:5,6) *(Ameumbika vizuri sana) - M. A. Thiers, History of the French Revolution, gombo la 2, ukurasa wa 370 na 371. [GC 275.3; PK Aya ya 30]

Wakati mungu huyu wa kike alipoletwa kwenye ukumbi wa mkutano wa kitaifa, msemaji yule alimshika mkono, na akiugeukia umati alisema: "Ee wanadamu wenye maisha mafupi, mnaokufa, acheni kutetemeka mbele ya radi za Mungu zisizokuwa na nguvu ila ni hofu zenu tu zimeumba hiyo nguvu. Tangu sasa na kuendelea msimtambue mungu yoyote zaidi ya huyu Mantiki. Naweka mbele yenu sanamu yake iliyo tukufu na safi kabisa; kama ni lazima ninyi muwe na sanamu za kuabudu, basi, toeni kafara zenu kwa mungu huyu peke yake.... Angukeni chini ya Baraza hili tukufu la Uhuru la Agosti, Ee kifuniko cha Mantiki!" [GC 276.1; PK Aya ya 31]

"Yule mungu wa kike, baada ya kukumbatiwa na mwenyekiti wa mkutano wa wawakilishi, alipandishwa juu ya gari zuri la kifahari, na kupitishwa katikati ya umati mkubwa sana wa watu na kwenda kwenye kanisa kuu la Notre Dame (mama yetu-Bikira Maria), kuchukua nafasi ya Mungu. Alipofika kule alipandishwa juu ya madhabahu ya juu (altare ndefu), na alipokea hapo ibada ya wote waliohudhuria." - Alison, vol. 1, sura ya 10. [GC 276.2; PK Aya ya 32]

Muda si mrefu baadaye, tukio hili lilifuatiwa na kuchomwa kwa Biblia hadharani. Katika tukio moja wanachama wa "Chama kinachopendwa na Maarufu cha Jumba la Makumbusho" waliingia katika ukumbi wa manispaa, wakipiga kelele, "Vive la Raison!" (Idumu Mantiki/Uishi milele Mungu Fikra) na juu ya mlingoti mrefu walikuwa wamebeba masalio ya vitabu kadhaa vilivyoungunzwa nusu kwa moto, miongoni mwake vikiwemo vitabu vya taratibu za sala na ibada za kila sikuza Kirumi (breviales), Misale, na Agano la Kale pamoja na Agano Jipya, ambavyo "vimelipizwa kisasi katika moto ule mkubwa," alisema mwenyekiti, "upumbavu wote walioubuni wamewaongoza wanadamu kuutenda." - Journal of Paris, 1793, Na. 318. Jarida hilo limenukuliwa katika

kitabu cha Buchez-Roux [Bushe Ruu], Collection of Parliamentary History, gombo la 30, ukurasa wa 200 na 201. [GC 276.3; PK Aya ya 33]

**Ufaransa Dhidi Ya Matengenezo Ya Kanisa**

Upapa ndio ambao ulikuwa umeanzisha kazi ya kumkana Mungu yaani ukafiri, nao ulikuwa ukikamilishwa sasa na hii nchi. Sera za Rumi zilikuwa zimeumba hali ya hewa ya kijamii, kisiasa, na kidini, na hali hiyo ilikuwa inaiharakisha Ufaransa kudumbukia kwenye maangamizi yake. Waandishi, wakirejelea mambo ya kutisha yaliyofanywa na Mapinduzi, wanasema kuwa lawama ya mashtaka haya ya kuvuka mipaka kwa aina hii inapaswa kuwekwa juu ya kiti cha enzi na Kanisa (Angalia Nyongeza 12 mwisho). Kwa maana halisi ya kutenda haki kabisa, mashtaka haya yanapaswa kutwishwa juu ya kichwa cha Kanisa. Upapa ulikuwa umeweka sumu kwenye akili za wafalme dhidi ya Matengenezo, kama adui wa ufalme, wazo ambalo lingeweza kuleta malumbano ambayo yangesababisha hatari ya kuondoa amani na umoja wa taifa. Ilikuwa ni hila za Rumi ndio ambazo zilichochea ukatili wa kutisha mno na ukandamizaji ulioleta usumbufu mkubwa sana toka kwenye kiti cha enzi cha mfalme wa nchi. [GC 276.4; PK Aya ya 34]

Roho ya uhuru iliondoka pamoja na Biblia. Popote pale injili ilipopokelewa, mafikra ya watu yaliamshwa. Walianza kutupilia mbali minyonyoro ambayo ilikuwa imewafunga katika ujinga, uovu, na ushirikina. Na walianza kufikiria na kutenda kama watu, yaani walitumia akili zao wenyewe. Wafalme waliona na kuanza kutetemeka kwa ukandamizaji wao. [GC 277.1; PK Aya ya 35]

Rumi haikucheleweseha kuchochea hofu zao zilizojaa wivu. Papa mmoja alimwambia hivi balozi wa Ufaransa mwaka 1525: "Wazimu huu [Uprotestanti] sio tu utashinda na kuharibu dini, bali pia utashinda na kuharibu tawala zote, yaani falme zote, utashinda na kuangamiza uungwana, sheria, utaratibu, mamlaka zote, na majeshi yote”- G. de Felice, History of the Protestants of France, kitabu cha 1, sura ya 2, aya ya 8. Miaka michache baadaye mjumbe wa papa alimwonya mfalme akisema: “Mheshimiwa usidanganyike. Waprotestanti watavuruga utaratibu wote wa kiraia pamoja na ule wa kidini...Kiti chako chako cha enzi pamoja na altare yote kwa pamoja viko hatarini,...Uanzishaji wa dini mpya ni lazima uanzishe serikali mpya!” - D’Aubigne, History of the Reformation in Europe in the Time of Calvin, b. 2, sura ya 36. Na wanatheolojia waliamsha chuki walizokuwa nazo kwa kutangaza kuwa mafundisho ya dini ya Kiprotestanti "yanawashawishi watu kushika mambo mapya ya kipumbavu; yanamrubuni mfalme upendo na utii wa raia zake, na kuliangamiza kanisa pamoja na serikali.” Hivyo ndivyo Roma ilivyofanikiwa kuipanga Ufaransa kusimama dhidi ya Matengenezo ya Kanisa. "Ilikuwa ni kwa kusudi la kudumisha kiti cha enzi, kulinda watu mashuhuri wenye vyeo, na kudumisha sheria zilizokuwapo, ndiyo maana upanga wa mateso ulichomolewa kutoka katika ala yake kwa mara ya

kwanza katika nchi ya Ufaransa.” - Wylie, kitabu cha 13, sura ya 4." - Wylie, b. 13, sura ya 4. [GC 277.2; PK Aya ya 36]

### Sera Ya Kufisha

Watawala wa nchi hawakuweza kuona hata kidogo matokeo ya sera hizo zenye hatari. Mafundisho ya Biblia yangekuwa yamepandikiza kwenye akili na mioyo ya watu kanuni za kutenda haki, kiasi, Ukweli, usawa, na ukarimu ambazo ndizo jiwe kuu la pembeni hasa katika usitawi na mafanikio ya taifa lolote. "Haki huinua taifa." Kwa hivyo “kiti cha enzi huthibitika kwa haki.” Mithali 14:34; 16:12. "Kazi ya haki itakuwa amani;” na matokeo yake yatakuwa, “utulivu na matumaini daima.” Isaya 32:17. Mtu anayetii sheria ya Mungu ataziheshimu na kuzitii kikamilifu sheria za nchi yake. Mtu anayemcha Mungu atamheshimu mfalme katika utekelezaji mamlaka yake yote ya haki na halali (Rumi 13:1-7). Lakini Ufaransa yenye huzuni, iliipiga marufuku Biblia na kuwapiga marufuku nchini wafuasi wake (kuwafukuza). Karne baada ya karne, watu wanaofuata kanuni na wenye msimamo thabiti kwa uadilifu, watu wenye vipaji vya akili mahiri na nguvu za kimaadili, waliokuwa na ujasiri wa kuikiri imani yao na kusimamia kile walichokiamini kiasi cha kupata mateso kwa ajili ya Ukweli - kwa karne nyingi watu hawa walifanya kazi ngumu kama watumwa katika majahazi, waliuawa kwa kuchomwa moto kwenye mti wa kuchomea watu, au kuoza katika seli za magereza yaliyokuwa chini ya ardhi. Maelfu kwa maelfu walipata usalama wao kwa kukimbia na kwenda uhamishoni; na hali ile iliendelea kwa miaka mia mbili na hamsini baada ya kuanzishwa kwa Matengenezo ya Kanisa [GC 277.3; PK Aya ya 37]

### Kukimbia Kwa Raia Bora Wa Ufaransa

“Kwa mara chache sana kulikuwepo kizazi cha watu wa Ufaransa wakati wa kipindi kirefu ambacho hakikushuhudia wanafunzi wa injili wakikimbia mbele ya hasira za mwenda wazimu mtesaji, na wakiondoka na akili, ujuzi, sanaa, tasnia zao, bidii na utaratibu, ambavyo, kama kanuni, walikuwa wamefanikiwa kwa stadi hizi kwa viwango vya juu sana, nao wakaenda kuzitajirisha nchi nyingine walikopata hifadhi kwa vipawa vyao. Na kwa uwiano ule ule ambao walizijaza nchi nyingine kwa vipawa hivi, ndivyo walivyoondoa karama hizo kutoka nchi ya Ufaransa. Endapo wale wote ambao walifukuzwa mbali ya nchi wangekuwa wamebaki katika nchi hii ya Ufaransa; ikiwa katika kipindi hiki cha miaka mia tatu, stadi za utendaji-kazi za wakimbizi zingetumika katika kuilima ardhi yake; ikiwa katika miaka hii mia tatu, ujuzi wao wa sanaa ungekuwa ukitumiwa katika uzalishaji wa vitu mbalimbali nchini mwao; ikiwa katika miaka hii mia tatu, kipaji chao cha akili zenye ubunifu na uwezo wao wa kudadavua mambo ungetumiwa katika kuboresha fasihi yake na kuiendeleza sayansi yake; ikiwa hekima yake ingetumika kuyaongoza mabaraza yake, kama mashujaa wake

wangetumika katika kupigana vita vyao, kama ufahamu wao kuhusu haki ungetumika katika kutunga sheria zao, na dini ya Biblia ingekuwa ikiimarisha akili na kuiongoza dhamiri ya watu wake, ni utukufu mwingi kiasi gani ungeifunika nchi nzima ya Ufaransa siku hii ya leo! Ni kwa jinsi gani ingekuwa nchi kuu, mashuhuri, tajiri, na ya furaha ----kielelezo cha kuigwa - na mataifa mengine yote! [GC 278.1; PK Aya ya 38]

"Lakini, chuki ya kijinga na yenye upofu na isiyoepukika, ilimfukuza kutoka katika ardhi yake kila mwalimu aliyewafundisha watu kuwa na maisha mema na tabia safi, kila mpiganaji shujaa aliyetetea utaratibu, kila mlinzi mwaminifu wa kiti cha enzi; iliwaambia maneno haya watu ambao wangeifanya nchi yao kuwa na 'sifa njema na itukuke' katika ulimwengu huu, chagua unachotaka, kuchomwa moto kwenye mti wa kuchomea watu au nenda ukawe mkimbizi katika nchi nyingine (hama!). Hatimaye uharibifu wa taifa la Ufaransa ulikamilika; haikubaki dhamiri ya kupigwa marufuku; hapakuwa na dini ile tena ya kuwaburuta wafuasi wake na kuwapeleka kwenye mti wa kuchomea moto; hapakuwa na uzalendo tena wa kuwafukuzilia watu mbali kwenda nchi zingine." - Wylie, kitabu cha 13, sura ya 20. Na Mapinduzi, pamoja na mambo yake ya kutisha, yalikuwa ndiyo matokeo yake ya kutisha na yenye giza nene. [GC 279.1; PK Aya ya 39]

**Kile Ambacho Kingalikuwa**

"Kitendo cha kuikimbia nchi cha Wahuguenoti (waprotestanti kama wale wa Waldensia), kulipelekea hali ya uchumi kurudi nyuma na uharibifu wa jumla katika sekta zote. Miji iliyostawi viwanda vya uzalishaji viliyoshamiri iliporomoka katika uozo; ardhi zenye rutuba zilirudi kwenye nyika kama hapo awali; udumavu wa akili na anguko la uadilifu vilifuatia kipindi cha maendeleo makubwa yaliyokuwa si ya kawaida. Jiji la Paris liligeuka na kuwa nyumba moja kubwa ya omba omba, na inakadiriwa kuwa wakati wa kuzuka kwa Mapinduzi maskini laki mbili walikuwa wanatafuta misaada kutoka mikononi mwa mfalme. Wajesuiti peke yake ndiyo walionawiri na kustawi katika taifa lililokuwa linaendelea kuoza na kutawaliwa kwa ukatili wa kutisha katika makanisa, mashule, magereza na majahazi ya vita. [GC 279.2; PK Aya ya 40]

Injili ingekuwa imeiletea Ufaransa suluhisho la shida zake za kisiasa na kijamii, ambazo ziliwaacha mdomo wazi viongozi wa kidini, mfalme wake, na watunga sheria wake, kwani walikoswa mbinu za kuleta mwafaka, na hatimaye walilitumbukiza taifa hili katika kutokuwa na serikali au uongozi unaoweza kutawalika na uasi mkubwa ukalifikisha taifa katika maangamizi yake. Lakini chini ya utawala huu wa kidikteta wa Rumi, watu walikuwa wamepoteza mafundisho ya Mwokozi yenye mibaraka juu ya kujikana nafsi, kujitoa mhanga na kuwa na upendo usio na ubinafsi au choyo. Walikuwa wamepotoshwa na kwenda mbali na roho ya kujinyima au kujikana nafsi kwa faida ya wengine. Matajiri

hawakupata karipio lolote kwa kuwaonea maskini, maskini hawakupata msaada wowote kwa utumishi wao na uonevu waliofanyiwa. Uchoyo wa matajiri na wenye mamlaka ulizidi kuonekana wazi zaidi na zaidi kwa kuwakandamiza wanyonge. Kwa karne nyingi uchoyo, tamaa ya mali na ubadhirifu wa 'mabwana wakubwa' wale uliendelea ukiwa na matokeo ya kuwadhulumu vibaya wakulima wadogo kwa kuwatoza ushuru mkubwa, kwa nguvu. Wale matajiri, mabwanyenye/makabaila waliendelea kuwatendea uonevu mwingi maskini, na maskini nao wakawachukia sana matajiri. [GC 279.3; PK Aya ya 41]

Katika majimbo mengi ardhi kubwa ilimilikiwa na 'mabwana wakubwa' au watu matajiri (malodi), na wale waliokuwa katika tabaka la wafanyakazi au vibarua, walikuwa ni wapangaji au watwana walionyenyekea tu na kuchukuliana na madai ya wale mabwana; waliwatii mabwana zao waliowapangisha mashamba yale, tena walilazimishwa kutekeleza madai yao mengi. Mzigo wa kulisaidia kanisa pamoja na serikali ulilianguki tabaka la kati na la chini, ambao walitozwa malipo makubwa na wenye mamlaka serikalini pamoja na viongozi wa kanisa. "Anasa au starehe za 'waheshimiwa' hawa zilifikiriwa kuwa ndiyo sheria kuu kuliko zote; wakulima wakubwa kwa wadogo wangeweza kufa kwa njaa, jambo ambalo wanyanyasaji wao hawakulijali kabisa.... Kila wakati wananchi wale walilazimika kushughulikia tu maslahi yale yaliyompendeza mmiliki wa ardhi au majumba. Maisha ya vibarua waliokuwa wanashughulika na kilimo yalikuwa ni maisha ya kufanya kazi ngumu isiyokoma nao walibeba mzigo wa taabu usioweza kutuliwa chini; malalamiko yao, ikiwa waliweza kudiriki kulalamika, yalishughulikiwa kwa dharau ya kifidhuli. Mahakama za sheria sikuzote zilimsikiliza yule mwenye uwezo na siyo mkulima mdogo; rushwa ilikuwa inapokelewa sana na majaji wale walioshughulikia matakwa madogo kabisa ya watawala wa koo zile zilizokuwa bora, nayo yakawa na nguvu ya sheria (yakawa ndiyo sheria yenyewe), kutokana na mfumo ule uliokuwa umeenea kote wa rushwa (ufisadi). Kwa habari ya zile kodi zilizokamuliwa na matajiri waliokuwa wakuu wa serikali, kwa upande mmoja, kutoka kwa watu wa kawaida (masikini) na kwa upande mwingine, kutoka kwa mapadri na maaskofu, hata nusu yake haikuingia katika hazina ya mfalme au katika ile ya kanisa; fedha iliyobaki ilitapanywa katika kujifurahisha nafsi zao kwa ubaradhifu wa anasa za tamaa ya matendo ya mwili. Na wale watu waliowafanya wananchi wenzao kuwa maskini, wao wenyewe walikuwa wamesamehewa kulipa kodi, tena walipewa haki kisheria au kwa kufuata desturi iliyokuwapo ya kuweza kuteuliwa na serikali kupata kazi za aina yo yote ile. Tabaka zilizopata upendeleo ule zilifikia idadi ya watu mia moja na hamsini elfu, na kwa ajili ya kutosheleza matakwa yao, mamilioni ya wananchi waliadhibiwa kwa kuwafanya waishi maisha duni kabisa, na yasiyokuwa na matumaini." *(Tazama kiambatanisho)* [GC 279.4; PK Aya ya 42]

### Anasa Na Uovu Wa Utawala Wa Makabaila

Nyua ya mfalme ilisheheni anasa, ubaradhifu, na rushwa. Palikuwa na kuaminiana kudogo sana kati ya wananchi na watawala wao. Hatua zote zilizochukuliwa na serikali zilishukiwa na kusemwa kwamba zilikuwa ni njama za kubuni za ubinafsi na uchoyo wao. Kwa zaidi ya nusu karne (miaka 50) kabla ya kipindi cha Mapinduzi, kiti cha enzi kilikuwa kimekaliwa na Mfalme Louis XV, ambaye, hata katika nyakati zile za uovu, alijulikana kama ni mfalme mzembe, juha au mpuuzi, na anayetawaliwa na tamaa za mwili, hasa uasherati sugu. Akiwa na watawala makabaila wa koo bora zilizomomonyoka kimaadili na kuwa wakatili, pamoja na tabaka la chini la wananchi waliofanywa kuwa maskini na wajinga, serikali ilikuwa imefilisika na kufedheheka, na wananchi wakiwa wamechukizwa sana, na hivyo hapakuhitajika jicho la nabii kuweza kuona mapema yale mambo ya kutisha yaliyokuwa yanakuja mbele dhidi ya serikali ile. Kwa maonyo yaliyotolewa kwake na washauri wake, mfalme alikuwa na tabia ya kujibu hivi: "najitahidi sana kuyafanya mambo yapate kuendelea mbele kwa kadiri mimi ninavyoendelea kuishi; baada ya kifo changu, mambo na yawe kama yatakavyokuwa." Ilikuwa ni bure kabisa kusisitiza kwake umuhimu wa kufanya matengenezo. Aliyaona maovu, lakini hakuwa na ujasiri wowote, uwezo au nguvu za kukabiliana na hayo. Maangamizi yaliyoingojea Ufaransa, yalielezwa kwa lugha ya picha halisi ilijionyesha tu katika jibu lake hili la kivivu na lililojaa ubinafsi: "Baada yangu mimi, gharika!" [GC 280.1; PK Aya ya 43]

Kwa kucheza na wivu wa mfalme pamoja na tabaka la watawala, Rumi ilikuwa imepata mamlaka ya kuwafanya watu kuwa watumwa wao. Rumi akijua fika ya kwamba kwa njia ile serikali hiyo ingeweza kudhoofika, alikusudia kwa njia hiyo kupata wepesi wa kuwafunga watawala na wananchi chini ya kongwa lake la utumwa. Akiwa na sera yake iliyona mbali sana, alitambua kwamba ili kuwaweka wananchi katika utumwa kikamilifu, na kuleta matokeo yaliyokusudiwa, ilikuwa ni lazima kuzifunga roho zao kwa pingu; na ya kwamba njia ya hakika ya kuwazuia wasiweze kuponyoka katika utumwa wao ule, ilikuwa ni kuwafanya wasiweze kuwa huru. Jambo lililokuwa la kutisha zaidi mara elfu kuliko mateso yale ya mwili ilikuwa ni ule mmomonyoko wa maadili, yaani kutokuwa na uadilifu, kulikotokana na sera yake. Wakiwa wamenyang'anywa Biblia, na kuachwa na mafundisho yenye chuki na ubinafsi na kugubikwa na ujinga na ushirikina, wananchi hawa wakawa wametota katika uovu, kiasi kwamba walijikuta hawana uwezo kabisa wa kujitawala nafsi zao wenyewe. [GC 281.1; PK Aya ya 44]

Lakini matokeo ya mambo haya yalikuwa tofauti sana na kile ambacho Rumi alikuwa imekilenga ili ikipate. Badala ya kuushikilia umma katika hali ya kutii

kwa upofu tu mafundisho yake ya dini bila kuyahoji (dogma), kazi hiyo ilileta matokeo ya kuwafanya watu kuwa makafiri na wanamapinduzi. Waliudhihaki Urumi kama ni hila au usanii tu wa mapadri. Waliwaona viongozi wa kidini kama chama kinachowakandamiza. Mungu pekee waliyemjua wao alikuwa ni mungu wa Roma (2 The.2:3,4); mafundisho ya kanisa la Roma ndiyo yalikuwa dini yao ya pekee. Walichukulia ulafi na ukatili wake kama tunda halali la Biblia, nao hawakutamani kabisa kuwa na dini kama ile hata kidogo. [GC 282.2; PK Aya ya 45]

**Matokeo Yalivunwa Kwa Damu**

Rumi ilikuwa imeiwakilisha vibaya tabia ya Mungu na kuyapotosha maagizo Yake, na sasa wananchi walikataa yote mawili, yaani, Biblia na Mwasisi Wake (Mungu). Kanisa lilikuwa limetaka watu wawe na imani ya kijinga au iliyo na upofu, isiyohoji mafundisho yake ya dini, chini ya idhini au kisingizio kwamba Maandiko yalikuwa yanaunga mkono mafundisho yao. Katika mwitikio wao kwa hilo, Voltaire na wenzake walilitupilia mbali Neno la Mungu na kusambaza kila mahali sumu ya ukafiri (kumkana Mungu). Rumi ilikuwa imewaponda-ponda watu chini ya kisigino chake chenye nyayo za chuma; na sasa umma wa watu waliodhalilishwa na kutendewa kwa ukatili mkubwa, katika kushtuka kwao na kujibu mapigo ya  mtesaji wao katili, walitupilia mbali kila kizuizi. Wakiwa wamekasirika vibaya kutokana na udanganyifu uliokuwa unaonekana waziwazi sana, na ambao kwa muda mrefu wamekuwa wakiuabudu, walikataa katakata ile Kweli pamoja na uongo kwa pamoja; nao wakidhani kwamba ule uvunjaji wa sheria au kujifanyia lolote watakalo ndio uhuru, watumwa hawa wa uovu walishangilia uhuru wao wa kufikirika. [GC 281.3; PK Aya ya 46]

Wakati wa mwanzo wa mapinduzi, kwa idhini ya mfalme, wananchi wa kawaida walipewa uwakilishi (serikalini) unaozidi ule wa wakuu na matajiri (lords) na viongozi wa dini wakiwekwa pamoja. Kwa njia hiyo, uzito wa madaraka ulikwemda mikononi mwa wananchi, lakini hawakuwa wameandaliwa kuyatumia mamlaka hayo kwa hekima na kiasi. Wakiwa na shauku ya kulipiza kisasi kwa maovu ambayo waliyotendewa, waliazimia kuijenga upya jamii. Raia walioudhiwa, ambao akili zao zilijazwa na kumbukumbu zenye uchungu wa muda mrefu, kwa kutendewa hiana, waliazimia kuleta mapinduzi katika hali yao ya mateso ambayo yalikuwa yamefikia kipimo cha kutovumilika na kujilipiza kisasi kwa wale ambao walidhani kuwa ni waasisi wa mateso yao. Wale waliokuwa wamepitia udhalimu mkubwa, walitumia somo walilokuwa wamejifunza kutoka kwenye ukatili wa Roma, nao waligeuka na kuwa wakandamizaji dhidi ya wale waliokuwa wamewakandamiza. [GC 282.1; PK Aya ya 47]

Maskini! Ufaransa yenye huzuni ilivuna damu kama mavuno ya mbegu walizopanda. Matokeo ya kutii kwake na kutawaliwa na mamlaka ya Rumi

yakawa ni ya kutosha sana. Wakati Ufaransa ilipokuwa chini ya usimamizi wa dini ya Kirumi, ilisimika nguzo ya kwanza ya kuchomea watu moto, mwanzoni mwa Matengenezo ya Kanisa, hapa ndipo Mapinduzi yalijenga mashine yake ya kwanza ya kisu cha kukatia vichwa watu (angalia guillotine mtandaoni). Mahali pale pale ambao wafia dini wa kwanza wenye imani ya Kiprotestanti walichomwa moto katika karne ya kumi na sita, wahanga wa kwanza wa mapinduzi walikatwa vichwa vyao kwa mashine katika karne ya kumi na nane. Katika kitendo cha kuipinga injili isiende mbele, ambayo ingeleta uponyaji katika nchi yao, Ufaransa, ikawa imefungua mlango wa kuruhusu kumkana Mungu na uangamivu uingie ndani ya nchi. Mara baada ya vizuizi vya Sheria ya Mungu kutupwa kando, ilionekana wazi kuwa sheria za mwanadamu zilikuwa hazitoshi kuyazuia mawimbi yenye nguvu za mihemko mikali ya wanadamu; ndipo taifa lile liliswagwa na kupelekwa katika uasi na machafuko ya kisiasa. Vita dhidi ya Biblia ilizindua Zama ambazo husimama katika historia ya ulimwengu kama Utawala wa Hofu (Reign of Terror). Amani na furaha zilifukuzwa kutoka majumbani na mioyoni mwa watu. Hakuna mtu yeyote aliyekuwa salama. Yule aliyesherekea ushindi leo, kesho yake alishukiwa, na kuhukumiwa. Ukatili wa kutumia nguvu na tamaa za mwili vikawa vimetawala kabisa bila mpinzani. [GC 282.2; PK Aya ya 48]

Mfalme, viongozi wa kanisa, waheshimiwa na wakuu walilazimika kujisalimisha chini ya ukatili wa wananchi waliokuwa wamekasirika sana na kuwa kama wenda wazimu. Kiu yao ya kutaka kulipiza kisasi ilikuwa imeamshwa mara tu baada ya mauaji ya mfalme wao; na watu ambao walikuwa wameamuru auwawe, muda si mrefu walimfuata kwenye jukwaa la kunyongea watu. Mauaji ya jumla yakawa yamepangwa kwa wale walioshukiwa kuwa walikuwa wapinzani wa Mapinduzi. Magereza yalifurika watu, wakati mmoja kulikuwa na wafungwa zaidi ya laki mbili. Miji mikubwa ya ufalme ilijaa matukio ya kutisha. Kikundi kimoja cha Wanamapinduzi kilipigana na kikundi kingine, na nchi ya Ufaransa ikageuka kuwa uwanja mpana wa makundi makubwa yanayopigana, wakiongozwa na hasira za mihemko yao. Katika jiji la Paris msukosuko mmoja ulifuata baada ya mwingine, na raia walikuwa wamegawanyika katika vikundi vingi vinavyopigana na kuleta fujo tu, ambavyo vilionekana kana kwamba vilikuwa havina kusudi jingine lolote ila kumalizana vyenyewe kwa vyenyewe." Na kwa kuongezea matatizo ya jumla ya taifa, Ufaransa ilijiingiza katika vita ya muda mrefu na yenye uharibifu mwingi dhidi ya mataifa makubwa ya Ulaya na kuleta uharibifu mwingi. "Nchi ilikuwa karibu kufilisika kabisa, na wanajeshi walikuwa wakidai kwa nguvu malipo ya nyuma ya mishahara yao. Wakazi wa jiji la Paris walikuwa wana njaa kali ambayo ingewaletea kifo wakati wowote, majimbo yakawa yameachwa bila kitu kutokana na magenge ya wanyang'anyi, na ustaarabu ulikaribia kutoweka kabisa kwa sababu ya nchi kutotawalika na uhalifu uliokuwa unatendwa kwa uhuru mkubwa, kila mtu alifanya lolote alitakalo bila ya kujali serikali." [GC 283.1; PK Aya ya 50]

Wananchi walikuwa wakijifunza vizuri mafunzo yaliyotokana na ukatili na utesaji ambao Rumi ilikuwa imewafundisha kwa juhudi nyingi. Siku ya kupatilizwa kwake zilikuwa zimefika hatimaye. Safari hii hawakuwa wafuasi wa Yesu waliotupwa katika magereza ya chini ya ardhi na kuburuzwa kwenda kuchomwa moto kwenye nguzo ya mti wa kuchomea watu. Watu hao walikuwa wameangamizwa muda mrefu au kufukuzwa na kwenda kuishi uhamishoni kama wakimbizi katika nchi zingine. Roma isiyojua huruma kwa mtu, sasa ilihisi nguvu ya mauaji ya wale iliyokuwa imewafundisha kufurahia matendo ya umwagaji damu. "Mfumo wa utesaji, ambao maaskofu na viongozi wa Ufaransa walikuwa wameuonyesha kwa zama nyingi, sasa uliwarudia wao wenyewe kwa nguvu nyingi zaidi. Majukwaa ya kunyongea watu yakawa mekundu kwa damu ya mapadri iliyokuwa ikitiririka. Majahazi yenye matanga na magereza, ambayo awali yalijaa msongamano wa Wahuguenots au Waprotestanti wa Kifaransa, sasa yakawa yamejaa watesaji wao. Wakiwa wamefungwa minyororo kwenye benchi na kufanya kazi ngumu ya kutoa jasho na kupiga makasia, viongozi la Roman Catholic walipata uzoefu wa mateso ambayo kanisa lao lilifanya sana dhidi ya wazushi wapole." *(Tazama Kiambatisho Sura ya 15, Aya ya 50)* [GC 283.2; PK Aya ya 51]

"Ndipo zilikuja siku zile ambazo sheria ya kishenzi au kinyama kabisa kuliko zote ilitekelezwa na mahakama katili kuliko mahakama zote; wakati ambapo mtu hakuruhusiwa kuwasalimu majirani zake au kufanya sala zake binafsi ..... bila kuwa katika hatari ya kutenda kosa linaloadhibiwa na kifo; wakati wapelelezi walipokuwa wakijibanza katika kila kona; wakati mashine yenye kisu cha kuchinjia vichwa vya watu yaani 'chinja-chinja' ilipokuwa inaendelea kufanya kazi yake ngumu kuanzia kila asubuhi na kuendelea kwa muda mrefu* (bamba la guillotine); wakati magereza yalipokuwa yamesongamana kama vyumba vya meli za watumwa zilivyokuwa zinajaza watu; wakati mifereji ya maji ilipokuwa ikijaa damu iliyotoa povu na kutiririka kuelekea mto Seine.... Wakati magari yaliyokokotwa na farasi yalipokuwa yamejaa wahanga na kupita mitaa ya Paris kila siku kuelekea mahali pa kuuliwa, wawakilishi wa kamati ya mfalme katika idara mbalimbali, walifanya karamu kubwa kusherekea ukatili mbaya uliokuwa haujawahi kuonekana katika mji mkuu kwa kucheza dansi, kunywa vileo na kula chakula. Waliona kisu cha mashine ya kukata vichwa vya watu kikiinuka na kushuka taratibu sana ili kutimiza kazi yao mbaya ya kuwachinja watu. Foleni refu za wafungwa zilifyekwa chini kwa risasi ndogondogo zilizofungwa pamoja kama vichale vya zabibu (grapeshot). Matundu yalitobolewa katika sakafu ya mashua zilizojaa watu mtoni. Mji wa Lyons uligeuka na kuwa jangwa. Katika mji wa Arras watu walinyimwa hata ile rehema ya kikatili ya kifo cha haraka. Maeneo yote hadi chini ya mto Loire, tangu Saumur kwenda baharini, makundi makubwa ya kunguru na mwewe walikula karamu ya maiti zilizokuwa uchi, zilizokuwa zimejisokota pamoja kama kamba, watu wakiwa

wamekumbatiana kwa namna ya kuchukiza au isiyofaa kutazamwa. Hakuna huruma iliyoonyeshwa kwa jinsia au umri. Idadi ya vijana wadogo wa kiume na wa kike wa miaka kumi na saba waliouawa na serikali hii inayotisha, inaweza kukadiriwa kuwa mamia mengi. Watoto wachanga waliopokonywa kwa nguvu kutoka kwenye matiti ya mama zao walitupwa kutoka mkuki hata mkuki kando ya safu za 'Jacobin' kule Ufaransa (Tazama kiambatisho.) Katika kipindi hiki kifupi cha miaka kumi, umati mkubwa wa wanadamu uliangamizwa. [GC 284.1; PK Aya ya 52]

Yote hayo yalitendeka kulingana na matakwa ya Shetani. Haya ndiyo amekuwa akiyafanyia kazi kwa zama nyingi ili aweze kuyatimiza. Sera yake ni ile ya kutumia udanganyifu toka mwanzo mpaka mwisho (Yn. 8:44), na kusudi lake thabiti ni kuleta maumivu na maafa kwa wanadamu, kuharibu sura ya Mungu na kuchafua kazi ya uumbaji Wake na malengo ya Mungu ya ukarimu na upendo, na kwa njia hiyo alete huzuni kubwa kule mbinguni. Hivyo kwa ufundi wake wa sanaa za uongo, anapofusha akili za wanadamu, na kuwaongoza watu wamtupie lawama Mungu kwa kazi ambazo anayehusika kuzifanya ni Shetani, kana kwamba misiba hiyo yote ni matokeo ya mpango wa Muumbaji. Kwa jinsi hiyo hiyo, wakati watu ambao wamedhalilishwa na kutendewa kinyama na kuumizwa vibaya kwa sababu ya nguvu zake za kikatili wanapopata uhuru wao, anawasukumiza kupita kiasi ili waende mbali zaidi katika kuwatendea mambo ya kikatili watesi wao. Ndipo picha ya uovu huo usio na mipaka inatumiwa na watu wakatili na watesaji kufanya mabaya bila kizuizi na kusondwa kidole na watawala wa kidikteta na wakandamizaji kuwa hicho ndicho kielelezo cha matokeo ya uhuru. [GC 284.2; PK Aya ya 53]

Wakati kosa linagunduliwa katika sura moja, Shetani huvalisha barakoa kosa hilo hilo katika sura nyingine tofauti, na watu wengi hulipokea kwa shauku kubwa kama walivyopokea kosa hilo katika sura ya kwanza. Wakati watu walipogundua kwamba dini ya Kirumi ni dini ya udanganyifu mtupu, na Shetani alipotambua kuwa asingeweza kupitia taasisi hii kuwaongoza watu kwenye ukiukaji wa sheria ya Mungu, basi, aliwachochea kuona dini zote ni ulaghai, na Biblia kama hekaya za uongo; nao, walipokuwa wamezitupilia mbali amri takatifu za Mungu, walijiachia na kujiingiza katika kufanya maovu bila kujizuia [GC 285.1; PK Aya ya 54]

Kosa la kubwa la kufisha ambalo lilileta madhara makubwa kwa wananchi wa Ufaransa lilikuwa ni lile la kupuuza Kweli hii moja kuu: kwamba uhuru wa Kweli umo ndani ya mipaka ya kuyatii kwa dhati makatazo yaliyomo katika Amri za Mungu. "Laiti ungalisikiliza amri Zangu! ndipo amani yako ingalikuwa kama mto wa maji, na haki yako kama mawimbi ya bahari." "Hapana amani kwa wabaya, asema Bwana." "Bali kila anisikilizaye atakaa salama, na naye atatulia bila kuogopa mabaya." Isaya 48:18, 22; Mithali 1:33. [GC 285.2; PK Aya ya 55]

Wanaokana kwamba Mungu hayupo, makafiri,* na wale wanaokufuru, huipinga na kuishutumu sheria ya Mungu; lakini matokeo ya ushawishi wao yanathibitisha kwamba ustawi wa mwanadamu unafungamana mno na utii wao kwa zile Amri za Mungu (Zaburi 119:165). Wale ambao hawajifunza somo kutoka katika kitabu cha Mungu wanaagizwa kujifunza katika historia ya mataifa.*(atheist au wakana-Mungu). [GC 285.3; PK Aya ya 56]

**Chimbuko La Misiba**

Wakati Shetani alipotenda kazi kupitia Kanisa la Kirumi, kuwapeleka watu kwenda mbali na utii, mbinu yake ilifichwa na kazi yake ilikuwa imefunikwa sana kiasi kwamba udhalilishaji wa watu, pamoja na misiba waliyoipata havikuonekana kama ni matunda ya kuiasi hiyo Sheria ya Mungu (Amri Kumi). Na nguvu yake Shetani kwa kiasi kikubwa ilithibitiwa sana na utendaji wa Roho wa Mungu kiasi kwamba matunda ya makusudi yake yalizuiwa kukomaa na hivyo hayakufikia utimilifu uliotarajiwa. Watu hawakuweza kuunganisha madhara na chanzo chake na matokeo yake ni kuwa, hawakuweza kugundua chanzo cha misiba au taabu yao. Lakini katika Mapinduzi, Sheria ya Mungu (Amri Kumi) iliwekwa pembeni waziwazi na Baraza kuu la Taifa, linalotunga sheria. Na katika kipindi hiki cha Utawala wa kigaidi au Hofu kilichofuatia, utendaji kazi wa chanzo na madhara viliweza kuonekana wazi na wote (cause and effect). [GC 285.4; PK Aya ya 57]

Wakati Ufaransa ilipomkataa Mungu kama serikali hadharani na kuiweka kando Biblia, watu waovu na pepo wabaya wa giza, walishangilia kwa kulifikia lengo lao walilokuwa wamelitamani kwa muda mrefu sana -- kupata ufalme ulio huru, usiothibitiwa na Sheria ya Mungu (Hawataki makatazo ya Mungu). Kwasababu hukumu dhidi ya kazi mbaya haikutekelezwa haraka, kwa hivyo mioyo ya wana wa watu ilikuwa "imethibitishwa ndani yao ili kutenda uovu." Mhubiri 8:11. Lakini ukiukwaji wa sheria hiyo ya haki na takatifu bila shaka utaleta taabu na maangamizi. Ingawa haukupatilizwa kwa hukumu mara moja, hata hivyo, uovu wa watu ulikuwa unafanya kazi yake kwa hakika kuwaletea maangamizi yao. Karne nyingi za uasi wa imani na uhalifu ulikuwa zikidunduliza akiba ya ghadhabu dhidi ya siku ya kupatilizwa; na maovu yao yalipokijaza kikombe chao, wale waliokuwa wakimdhihaki Mungu waling'amua wakiwa wamechelewa mno, kwamba ni jambo la kutisha kuuchosha uvumilivu wa Mungu. Roho wa Mungu anayedhibiti, na ambaye anaweka kizuizi Chake dhidi ya nguvu za kikatili za Shetani, alikuwa ameondolewa kwao kwa kiwango kikubwa, na yule adui ambaye furaha yake pekee ni kufurahia taabu inayowapata wanadamu, aliruhusiwa kufanya mapenzi yake kwao. Wale waliokuwa wamechagua, huduma ya uasi, waliachwa wavune matunda ya uasi mpaka pale nchi ilipokuwa imejaa uhalifu wa kuogofya mno kiasi ambacho hata kalamu haiwezi kuandika habari zake. Kutoka

katika majimbo yaliyokuwa yamefanywa ukiwa na miji iliyovunjwavunjwa na kuwa magofu, kilio cha kutisha kilisikika,-- kilio cha uchungu mkali mno. Ufaransa ilitikiswa vibaya kama tetemeko la ardhi linavyotikisa nchi, dini, sheria, utulivu wa kijamii, familia, serikali, na kanisa—vyote hivyo vilibamizwa chini na mikono ya watu wasiomcha Mungu ambayo ilikuwa imeinuliwa dhidi ya sheria ya Mungu. Mtu mwenye hekima alikuwa amesema Ukweli: "Mtu mwovu ataanguka kwa uovu wake." "Ajapokuwa mwenye dhambi amefanya maovu mara mia, akazidisha siku zake; lakini hata hivyo najua hakika ya kwamba itakuwa heri kwao wamchao Mungu, wenye kicho mbele Zake; walakini haitakuwa heri kwa mwovu." Mithali 11: 5; Mhubiri8:12, 13. Kwa kuwa "Walichukia maarifa, wala hawakuchagua kumcha Bwana;" "Kwa hiyo watakula matunda ya njia yao, watashiba mashauri yao wenyewe." Mithali 129; 31. [GC 286.1; PK Aya ya 58]

**Biblia Yarejeshwa Ufaransa**

Mashahidi wale waaminifu wa Mungu, waliochinjwa na mamlaka yenye makufuru "itokayo katika kuzimu," hawakunyamaza kwa muda mrefu. "Na baada ya siku hizo tatu u nusu, roho ya uhai itokayo kwa Mungu ikawaingia, wakasimama juu ya miguu yao; na hofu kuu ikawaangukia watu waliowatazama." Ufunuo 11:11. Ilikuwa mwaka 1793 ambapo Bunge la Kifaransa liliweka sheria ambazo ziliifutilia mbali dini ya Kikristo na kuiweka Biblia kando. Miaka mitatu u nusu baadaye azimio lililozitangua sheria hizi, lilipitishwa na Bunge lile lile likitoa ruhusa ya kuyastahimili Maandiko. Ulimwengu ulisimama mdomo wazi kuuona uovu huu mkubwa wa kutisha, uliotokana na kuyakataa Mausia Matakatifu, na wanadamu wakatambua umuhimu wa kuwa na imani katika Mungu na katika Neno Lake kama msingi wa wema na maadili. Bwana anasema hivi: "Ni nani uliyemshutumu na kumtukana? Umeinua sauti yako juu ya nani, na kuinua macho yako juu? Juu ya Mtakatifu wa Israeli." Isaya 37:23. "Basi, tazama, nitawajulisha, mara moja hii nitawajulisha, mkono Wangu, na nguvu Zangu; nao watajua ya kuwa Jina Langu ni YEHOVA." Yeremia 16:21. [GC 287.1; PK Aya ya 59]

Kuhusiana na mashahidi wawili nabii anaelezea zaidi: "wakasikia sauti kuu kutoka mbinguni ikiwaambia, Pandeni hata huku. Wakapanda mbinguni katika wingu, adui zao wakiwatazama." Ufunuo 11:12. Tangu Ufaransa ilipofanya vita yake dhidi ya mashahidi hao wa Mungu wawili, mashahidi hao wameheshimiwa kwa hali ya juu mno kuliko kabla ya hapo. Mnano mwaka ule wa 1804 Chama cha Biblia cha Uingereza -British and Foreign Bible Society kilianzishwa. Vyama vingine vinavyofanana na hicho vilianzishwa, na vikawa na matawi mengi sana katika bara la Ulaya. Mnamo mwaka 1816 Chama cha Biblia cha Marekani-American Bible Society kiliundwa. Wakati Chama cha Uingereza yaani British Bible Society kilipoanzishwa,* Biblia ilikuwa imechapishwa na kusambazwa

mahali pengi kwa lugha hamsini. Tangu wakati ule imetafsiriwa katika maelfu mengi ya lugha na lahaja zake (tofauti za matamko ya lugha moja katika maeneo mbalimbali-mifano itakuwa kama kisukuma na kinyamwezi-dialects). Tazama Kiambatisho.) [GC 287.2; PK Aya ya 60]

Miaka hamsini iliyotangulia kabla ya mwaka 1792, palikuwa na umakini na jitihada ndogo kuhusiana na kazi ya umishenari katika nchi za kigeni. Hakuna vyama vipya vilivyoundwa, tena palikuwa na makanisa machache sana yaliyofanya juhudi ya aina yoyote ili kueneza Ukristo katika nchi za kipagani. Lakini kuelekea mwisho wa karne ya kumi na nane mabadiliko makubwa yalitokea. Watu hawakuridhika kutegemea tu matokeo ya kuyatazama mambo kwa kutumia falsafa ya mantiki peke yake,* tena waligundua umuhimu wa kuwa na mafunuo ya Mungu na dini halisi, ambayo ambayo ina vitendo. Tangu wakati huo kazi ya misheni za kigeni ilifikia ukuaji mkubwa kwa namna isivyopata kufikiwa kabla ya hapo *(Rationalism-kutumia hekima ya kibinadamu peke yake). (Tazama Kiambatisho) [GC 287.3; PK Aya ya 61]

Maboresho katika kazi ya Uchapaji yametoa msukumo katika kazi ya kusambaza Biblia. Ongezeko la njia za miundo-mbinu ya mawasiliano kati ya nchi mbalimbali, kuondolewa kwa vipingamizi vya zamani vya chuki na ubaguzi kati ya taifa moja na jingine; na upotezaji wa nguvu za kiserikali za kiongozi mkuu wa kanisa la Roma vimefungua njia kwa ajili ya Neno la Mungu kusambaa. Kwa miaka kadhaa Biblia imekuwa ikiuzwa bila vipingamizi vyovyote katika mitaa ya Roma, na sasa imepelekwa katika kila sehemu ya dunia hii inayokaliwa na watu.* Angalia mwisho wa Sura hii kwa habari zaidi za Biblia. [GC 288.1; PK Aya ya 62]

Mtu aliyemkana Mungu ufaransa aitwaye Voltaire aliwahi kujigamba kwa kusema: "Nimechoshwa sana kusikia watu wakisema kwa kurudia-rudia kwamba wanaume wale kumi na wawili walianzisha dini ya Kikristo. Mimi Nitathibithisha kwamba mtu mmoja tu anatosha kuweza kuipindua. “Vizazi na vizazi vimepita tangu kifo chake huyu mtu. Mamilioni wamejiunga katika kupigana vita kwa ajili ya Biblia. Lakini dini ya Kikristo siyo tu kuwa haijaangamzwa, badala yake pahali pale ambapo palikuwa na Biblia mia moja katika wakati ule wa Voltaire, sasa zipo nakala laki moja za kitabu hiki cha Mungu. Katika maneno ya Mwanamatengenezo wa awali kuhusu Kanisa la Kikristo,: “Biblia ni fuawe ambayo imezichakaza vibaya nyundo nyingi.” Bwana asema: “Kila silaha itakayofanyika juu yako haitafanikiwa, na kila ulimi utakaoinuka juu yako katika hukumu utauhukumu kuwa mkosa.” Isaya 54:17)* [GC 288.2; PK Aya ya 63]

"Neno la Mungu wetu litasimama milele." “Maagizo Yake yote ni amini. Yamethibitika milele na milele, yamefanywa katika Kweli na adili.” “Majani yakauka, ua lanyauka; Bali Neno la Mungu wetu litasimama milele”. Isaya 40:8;”Matendo ya mikono Yake ni Kweli na hukumu, Maagizo Yake yote ni amini,

Yamethibitika milele na milele, Yamefanywa katika Kweli na adili." Zaburi 111: 7, 8. Kitu chochote kilichojengwa juu ya mamlaka ya mwanadamu kitaangushwa na kushindwa; lakini kile kilichojengwa juu ya mwamba wa Neno la Mungu lisilobadilika kamwe litadumu milele. [GC 288.3; PK Aya ya 64]

**Kuhusiana na miaka 1260 soma zaidi kwenye unabii wa Biblia. Akasema hivi yule malaika wa Bwana: "Nao wataukanyaga mji mtakatifu (watawatesa na kuwaua watakatifu) miezi arobaini na miwili [42 x 30 = miaka 1260]. Nami nitawaruhusu mashahidi wangu wawili [Agano la Kale na Agano Jipya], nao watatoa unabii siku elfu na mia mbili na sitini [miaka 1260], hali wamevikwa magunia [Neno la Mungu lilihubiriwa kwa siri].... Hata watakapoumaliza ushuhuda wao, yule mnyama [mfalme – Dan. 7:17]*

**(Biblia ndiyo kitabu cha kwanza kwa mauzo duniani toka kianze kunakiliwa kwa mkono miaka elfu tatu iliyopita na kuchapwa kwenye mtambo wa kwanza wa uchapaji kule Ujerumani mwaka 1456 na Johannes Gutenberg, yaani best seller, cha pili ni Pilgrim Progress, cha tatu ni Kuruani na cha nne ni kitabu chekundu ya Ukomunisti cha China. Martin Luther ndiye alikuwa mtafsiri wa hiyo Biblia ya kwanza ya Kijerumani)*

**BIBLIA YA KISWAHILI ILITUFIKIAJE? (HOW DID WE GET SWAHILI BIBLE?)*

*Kulingana na utafiti, kwa sasa kuna lugha 7,106 duniani. Kufikia 2020 Biblia nzima ilikuwa imetafsiriwa katika lugha 704. Agano Jipya limetafsiriwa katika lugha 1,551 na sehemu za Biblia zimetafsiriwa katika lugha 1,160 za ziada. Fanya hesabu Kuhusu Lugha ambazo zinabidi kufikiwa. Chama cha Biblia chaWycliffe, kinaweza Kutupa taarifa zaidi.*

*Mary Jones alizaliwa kijiji cha Llanfihangely Pennant, katika kisiwa cha Wales (UK) tarehe 16 Desemba,1784. Alilipenda sana Neno la Mungu na alitamani sana awe na Biblia yake mwenyewe lakini alikuwa masikini. Akiwa na umri wa miaka 16, tayari alikuwa ametunza pesa ili aweze kununua Biblia yake mwenyewe, Alipata taarifa kuwa katika kanisa fulani, angeweza kununua Biblia, kwa hivyo, alitembea Km 40 kwenda kwenye kanisa ambapo alikutana na mchungaji Thomas Charles. Mchungaji alimweleza kuwa Biblia zote zilikwisha nunuliwa na haikusalia hata moja. Mary alimsimulia mchungaji Thomas kisa chake na jambo hili lilimsisimua mchungaji kiasi cha kuamua kumuuzia Biblia ambayo ilikwishalipiwa na mtu mwingine ila alichelewa kuichukua Biblia yake. Mchungaji huyu, alipata msukumo moyoni kufanya mpango ili watu wote wa kawaida wapate Biblia zao na wajisomee kwa kuzingatia ule usemi usemao, "Uzima wa Milele ndiyo huu, Kumjua Mungu Mmoja wa Pekee na Yesu Kristo Aliyemtuma". Mchungaji Thomas alifanya mkutano na viongozi wa Religious Tract Society mwaka 1802, na katika mazungumzo waliafikiana kuisaidia Wales kupata Biblia. Baada ya maamuzi hayo, akatokea bwana mmoja aitwaye Joseph Hughes na kuhoji: "Yaani kwa Wales tu? Je, nchi zingine?" Hoja yake ilipelekea kuundwa kwa chama kilichojulikana kama, British and Foreign Bible Society, mnamo March 7, 1804. Kwa pamoja walianzisha mitambo ya kuchapa; ni kutokana na chama hiki vimezaliwa*

*vyama vingi duniani vya Biblia vikiwemo kile cha Kenya Bible society, Bible Society of Tanzania na American Bible Society. Vyama hivi vimesaidia sana kueneza Biblia kwa wingi wakiruzuku mauzo Yake na wakati mwingine hupata wafadhili. Mary Jones aliishi miaka 80 na alifanikiwa kushuhudia na kufurahia matunda ya njozi yake Mara nyingi tunadhani kuwa, mtu anaweza tu kuleta tofauti katika jamii iwapo ana pesa au mamlaka. Hapa tumeona kwamba hili si kweli, njozi inaleta malengo, madhumuni na hatimaye, yaweza kuhamisha milima mingi katika maisha ya mwanadamu. Johannes Ludwig Krapf alizaliwa nchini Ujerumani (1810-1881). Alihitimu shahada ya Theolojia katika chuo kikuu cha Tubingen mnamo mwaka 1874. Alisafiri kwenda Misri na huko alioa na kupata mtoto; Baadae, yeye na familia yake, walihamia kule Rabai, Mombasa ambapo mkewe na mtoto walifariki kwa malaria. Krapf alikuwa na talanta ya lugha iliyomwezesha kufahamu Kigiriki, Kilatini, Kiebrania, kifaransa, na Kiitaliano. Krapf alikuwa Mlutheri na Mwaka 1844 alifanya umishonari katika nchi za Afrika Mashariki. Mara alipowasili, mwaka 1844, alianza kujifunza Kiswahili cha kimvita. Aliandika Kamusi ya Kwanza ya Kiswahili na Sarufi ya Lugha ya Kiswahili. Alianza pia kuandika kitabu cha Mwanzo cha Biblia ila lugha Yake haikuwa na mpangilio mzuri (Tazama mfano wa nakala za kwanza mtandaoni-Angalia Johann Krapf's 1847 tafsiri ya Mwanzo 1:1-3 into Swahili). Krapf aliona kwamba kuna hitaji kubwa la kueneza Neno la Mungu kwa watu kwa kusoma Biblia ya Kiswahili. Hata hivyo, jaribio hilo lilishindwa kwa sababu yeye mwenyewe alijifunza tu Kiswahili cha mawasiliano rahisi, ila hakuwa mtumiaji*.

*Krapf alifanya kazi na Jaji wa Kiislamu aitwaye Ali Bin Modehin, kutafsiri kitabu cha Mwanzo. Mwishowe, alimaliza Agano Jipya la kimvita japo hakuchapa nakala nyingi. Kazi yake ilikuja kutumiwa baadae katika kuandika Biblia ya Kiswahili "Southern Version" aliyoshughulikia Steer. Huyu katika mwaka wa 1868 alimaliza Agano Jipya na Mwaka 1879 Biblia yote ilikamilika, yaani, Agano la Kale na Agano Jipya. Waandishi wengine walikuja na kujiunga naye wakisaidiana kukamilisha uandishi Agano la Kale nao ni Johannes Rebmann, na Rabai Krapf. Majina ya wengine ni Wiliam Taylor, Harry Bins, Edward Steere, Franciss Hodgson, na Arthur Madan. Hadi kufikia mwaka 1895 Biblia yote ya Kiswahili iliweza kupatikana. Kamusi ya Krapf pia ilisaidia wengi katika kazi za kutafsiri. Krapf alitafsiri Biblia pia kikamba, na lugha ya Oromo ya Ethiopia. Edward Steer (1928), Mwanglikani kutoka nchini Uingereza, aliwekewa mikono ya Uchungaji mwaka 1850. Alifika kufanya kazi Zanzibar mwaka 1864. na mwaka 1869 akiwa na Chapa ya Krapf alimaliza kutafsiri Agano jipya. Alikuwa amesaidiana na wananchi wa. Hawa walifadhiliwa na chama cha Biblia nao wakafanikiwa kutafsiri Biblia kwa lugha ya Kiswahili. Steer alikufa mwaka 1882. Tafsiri aliyoianzisha Krapf iliendelea kuboreshwa na watu mbalimbali kwa kadri Mungu Alivyowatumia hadi mwaka 1950. Kamusi yake ilisaidia katika kutafsiri Biblia kwa Mchungaji Steer na wenzake na pia kwa tafsiri za makabila mengine ya kibantu kama Luganda. Chapa ya kwanza ya Biblia ya Kiswahili (tunayoitumia leo) ilitolewa rasmi mwaka 1952, hata hivyo kulingana na taratibu za mabadiliko na kukua kwa lugha, ni jambo la kawaida kuhakiki kitabu kila baada ya miaka 50. Wapo watu wengine wa Zanzibar ambao*

*walisaidia kupata lugha sahihi, hasa watunga mashairi kama vile Mwajuma, Shaban Robert na Mathias Mnyampala. Mchango wao ni tunu kwa watumiaji wa lugha ya Kiswahili. Kwa mantiki hiyo, Biblia yetu hii, ina umri wa miaka takribani 75, hatutashangaa iwapo siku moja tutapata Biblia fafanuzi, au Kronolojia, au Biblia ya Kesha (Paraphrase/Devotional Bible). Tumeanza kuandika kitabu cha Warumi kwa ufafanuzi/Kesha (paraphrase/devotional). Hebu Mungu Atusaidie na kututumia ili kazi ikamilike mapema. Tunatamani maombi yenu. Tunaomba mtukumbuke katika utume. Marekebisho ya mwaka 1950 yalizingatia umuhimu wa kuwa na "Standardized Bible" ya Kiswahili katika Afrika Mashariki ndipo ikazaliwa tafsiri ambayo tunayo mpaka leo (Swahili Union Version). Makanisa mengine yameshiriki kutoa tafsiri ya Biblia ya lugha zingine za Afrika*

*Mashariki za makabila ya Afrika Mashariki, baadhi yake ni Mazumo (Zaburi) kwa lugha ya Chasu (Kipare) kilichochapiswa na Max Poenig Msabato mwaka 1919, Agano Jipya kwa Kipare mwaka 1912 na miaka iliyofuatia. Vingine vilivyofuata ni*

*Agano la Kale na Agano Jipya (Ilagano lya Kale na Ilagano Ipya) kwa Kisukuma kilichotafsiriwa na Wamisionari Wasabato wa Kipare huko Usukuma wakati wa vita ya kwanza na kuchapishwa huko Kendu Bay (Kenya). Pia Mmisionari Rudolph*

*Reider aliyekuwa Majita na Ibrahimu Maradufu walitafsiri Agano Jipya kwa lugha ya Kijita liitwalo Indagano Inyaaya baada ya vita ya kwanza.*

*Hapa kwetu barani Afrika, Chama cha Biblia kilifika nchini Kenya na Ethiopia kwanza, na wakati huo Tanzania tulihudumiwa kutokea Kenya mpaka mwaka 1978 chama hicho kilipoanzishwa hapa Tanzania huko Iringa. Kati ya 1979-1980*

*ndipo kilihamishiwa mjini Dodoma ambapo kimestawi hadi leo na kinaendelea kuhudumia jamii kubwa duniani, yenye hitaji la Neno la Mungu kwa kiswahili (hasa ilipoonekana kwamba kuna uhitaji mkubwa).*

*Kuna haja ya kuwa na tafasiri zingine za Biblia kama lugha zingine zilivyo, mfano Kingereza kina tafsiri zaidi ya 100. Sasa hivi kuna tafsiri ya Biblia ya Kiswahili cha Kisasa ambayo tumeshaizoea!*

*(Tumehoji vyama vya Biblia pia, ila kazi ya binadamu mara nyingi inakuwa na makosa, ila nia yetu ni kushiriki nanyi habari hizi njema hivyo kama kuna masahihisho yoyote tafadhali tusaidieni. Tunapenda kubarikiwa nanyi kwa maombi, mashauri na masahihisho, Asante). Ombi zito sana ambalo limesheheni ni hili, nawe jiombee na liishi kisha utapata mafunuo ya kuweza kulielewa Neno na siku moja tuwe mbinguni pamoja NAYE milele zote, Raha hiyo ya rohoni ni amana ya pumziko ambalo limewekwa juu kikomo cha masukumbuko!*

*Efeso 3:14-20-Kwa sababu hiyo, nampigia magoti Baba, 15 Aliye asili ya jamaa zote duniani na mbinguni. 16Namwomba Mungu, kadiri ya utajiri wa utukufu Wake, awajalieni kwa uwezo wa Roho Wake, nguvu ya kuwa imara ndani yenu, 17 Naye Kristo akae mioyoni mwenu kwa imani. Namwomba mpate kuwa na mzizi na msingi katika mapendo 18kusudi muweze kufahamu*

*pamoja na watu wote wa Mungu jinsi upendo wa Kristo ueneavyo kwa mapana na marefu, kwa kimo na kina. 19Naam, mpate kujua upendo wa Kristo upitao elimu yote, mjazwe kabisa utimilifu wote wa Mungu. 20Kwake Yeye ambaye kwa nguvu Yake ifanyayo kazi ndani yetu aweza kufanya mambo makuu zaidi ya yale tuwezayo kuomba au kufikiria; 21Kwake Mungu uwe utukufu katika kanisa na katika Kristo Yesu, nyakati zote, milele na milele! Amina.*
*EFES0 3:14-21*

Grace Momadi-Masaka, David Bunga Dettu, Bariki Kangalu Elineema, na Daniel Nyangaresi

Masaka 2012.

# SURA YA 16

# WASAFIRI WA IMANI WALIOTAFUTA UHURU KATIKA NCHI MPYA

**(Wazee Mahujaji)**

Ufupisho: Miaka mingi iliyopita kulikuwa na watu ambao hawakuweza kumwabudu Mungu katika nchi zao kufuatana na dhamiri zao, kwasababu sheria nchi zilipiga marufuku jambo hilo. Hawa waliziacha nchi zao na kwenda kuishi uhamishoni kama wakimbizi katika nchi mpya-America na Australia. Jimbo la Rhode Island, ndiyo lilikuwa mahali palipojulikana kama mahali pa uhuru wa dini. Mwanzilishi wake Roger Williams alitaka kuanzisha serikali ya kiraia ambayo inatoa uhuru wa dhamiri, yaani mtu kumwabudu Mungu wake kama anavyotaka. Biblia ya King James Version ilichapwa mwaka 1611. Puritans walitoka Ulaya mwaka 1606. John Robinson alienda Amsterdam 1618. Roger Williams alifika 1631 na kuchunga kanisa la Salem, New England. Hawa walijulikana kama makasisi wasafiri, kwa meli ya MayFlower na kufika Marekani November 21, 1629.

Wanamatengenezo wa Uingereza, wakati walipokuwa wakiyakataa mafundisho ya dini ya Kirumi, walikuwa wamebakiza desturi na mifumo yake mingi. Hivyo, ingawa mamlaka na itikadi ya dini ya Rumi ilikataliwa, lakini bado mila, desturi na tararibu zake nyingi za ibada ziliingizwa katika ibada ya Kanisa la Uingereza (Anglikana church of England). Ilidaiwa kwamba mambo haya hayakuwa na uhusiano wowote wa dhamiri (mema au mabaya); kwamba, japo yalikuwa hayajaagizwa katika Maandiko, na kwa ajili hiyo yalikuwa si ya maana, lakini yalikuwa hayajakatazwa, yaani, hayakuwa na uovu kwa asili yake. Kule kuyaadhimisha kulikuwa na mwelekeo wa kuufanya ufa ulioyatenganisha makanisa ya Matengenezo na Rumi kuwa mdogo, tena ilisisitizwa kwamba

yangekuza imani ya Kiprotestanti kuweza kukubaliwa na Rumi. [GC 289.1; PK Aya ya 1]

Kwa wale wahafidhina, wasiopenda kubadilika au kuyumbiswa kirahisi (conservative) na wale wapenda maafikiano kirahisi, hoja hizo zilionekana kana kwamba zina nguvu na zinaenda kuleta hitimisho. Lakini palikuwepo na tabaka jingine ambalo halikuwa na mtazamo wa jinsi hiyo. Ukweli kuwa desturi hizi "zilikuwa na mwelekeo wa kujenga daraja kwenye ufa mkubwa kati ya Rumi na Matengenezo ya Kanisa - yaani kupunguza tofauti zao" (Martyn, gombo la 5, ukurasa wa 22) katika mtazamo wao, hiyo ikawa ni hoja yenye nguvu, katika mawazo yao, ya kuhitimisha azma yao ya kutobaki nazo. Waliziona kama ni alama za utumwa wao ambao walikuwa wamekwishakombolewa nao, na ambao hawakuwa tayari kuurudia. Walifikiria kwamba Mungu alikuwa ameweka maagizo katika Neno Lake yaliyoongoza taratibu na kanuni za ibada Yake, na ya kwamba wanadamu hawana uhuru wa kuziongeza zingine zaidi ya zile zilizopo au kuzipunguza zilizopo. Mwanzo wenyewe hasa wa uasi huu mkuu ilikuwa katika kutafuta kuongeza mamlaka ya kanisa kwa mamlaka ya Mungu. Rumi ilianza kwa kuongeza kile ambacho Mungu alikuwa hajakikataza, na iliishia kwa kukataza kile Mungu alichokuwa amekiagiza waziwazi. [GC 289.2; PK Aya ya 2]

Wengi wao walikuwa na matamanio ya dhati ya kuurudia usafi na usahili,* ambao ulikuwa ni sifa kuu iliyolitambulisha kanisa la awali. Walizichukulia desturi nyingi zilizozoeleka na Kanisa la Uingereza/Kianglikani kama kumbukumbu za ibada ya sanamu, nao kufuatana na dhamiri zao wasingeweza kuungana nalo katika ibada zake. Lakini kanisa lile, likiungwa mkono na wenye mamlaka serikalini, halikutaka kufanya tofauti zozote katika desturi zake za ibada. Mahudhurio katika ibada zake yalitakiwa kwa mujibu wa sheria ya nchi, na mikutano ya ibada isiyoidhinishwa ilipigwa marufuku chini ya adhabu ya kifungo, kufukuzwa nchini (uhamisho), na kuuawa *(taratibu rahisi za ibada zisizokuwa na mapambo).[GC 290.1; PK Aya ya 3]

Mwanzoni mwa karne ya kumi na saba, mfalme aliyekuwa ametawazwa katika kiti cha enzi cha Uingereza alitangaza nia yake ya kuwafanya wafuasi wa imani ya Puritans/Wapyuritani* "Wakubaliane nao katika kuziweka desturi za ibada walizotaka, au vinginevyo...wateswe na kunyanyaswa mara kwa mara hadi waikimbie nchi yao, au vinginevyo wapatwe na mambo mabaya zaidi."- George Bancroft, History of the United States of America, sehemu ya 1, sura ya 12, aya ya 6. Wakiwindwa, wakiteswa, na wakifungwa magerezani, hawakuweza kuona ahadi yoyote ya kuleta hali bora zaidi kwenye siku zao za usoni, na wengi wao waliamini kwamba, kwa wale ambao wangetaka kumtumikia Mungu kulingana na msukumo wa dhamiri zao,"Uingereza ilikuwa inapungua daima kuwa mahali salama, pa kukaa watu kama hao." - J. G. Palfrey, History of New England, sura ya 3, aya ya 43. Baadhi hatimaye walidhamiria kutafuta kimbilio kule Uholanzi.

Dhiki, hasara, na vifungo viliwakumba. Makusudi yao yalizimwa, kisha wakasalitiwa na kutiwa katika mikono ya adui zao. Lakini uvumilivu wao imara hatimaye ukashinda, nao wakapata hifadhi yao kwenye pwani rafiki za Jamhuri ya Kidachi. **Puritans maana yake ni wasafi, hawa walikuwa Waprotestanti wasiotaka mila na ibada ya Kanisa la Kikatoliki ziingizwe katika Kanisa la Uingereza*). [GC 290.2; PK Aya ya 4]

Katika kukimbia kwao Puritans walikuwa wameziacha nyumba zao, mali zao, na njia za kujipatia riziki zao kila siku. Walikuwa wageni katika nchi ya kigeni, miongoni mwa watu wa lugha na mila tofauti. Walilazimika kujifunza stadi mpya za kazi na ambazo hapo awali walikuwa hawajazijaribu ili tu kujipatia mkate wao. Watu wenye umri wa kati, waliokuwa wametumia sehemu kubwa ya maisha yao kuilima ardhi, sasa iliwabidi kujifunza kazi za ufundi. Lakini walikubaliana na hali hiyo kwa moyo mkunjufu na hawakupoteza muda katika uvivu au kulalamika kuhusu shida yao. Ingawa mara nyingi waliteseka kwa kubanwa na ufukara, walimshukuru Mungu kwa mibaraka iliyokuwa bado inaendelea kutolewa kwao na kupata furaha yao katika ushirika wao wa kiroho usio masumbufu au kero. "Walijua kwamba wao walikuwa ni wasafiri, wala hawakuyaangalia sana mambo hayo, bali waliyainua macho yao juu mbinguni, kwenye nchi yao nzuri, waliyoipenda, na mioyo yao ilitulizwa." - Bancroft, seh 1, sura 12, aya ya 15. [GC 290.3; PK Aya ya 5]

**Upendo Na Imani Vyazidi Kuwa Na Nguvu**

Katikati ya hali yao ya ukimbizi na shida, upendo na imani yao vilizidi kuimarika nguvu. Walizitumainia ahadi Zake Bwana, Naye hakuwaangusha wakati wa uhitaji. Malaika Zake walikuwa kando yao, kuwatia moyo na kuwategemeza. Na mkono wa Mungu ulipoonekana kana kwamba unawaelekeza kuvuka ng'ambo ya bahari  na kwenda kwenye nchi ambayo wangeweza kuunda serikali yao wenyewe, na kuwaachia watoto wao urithi wa thamani wa uhuru wa dini, walisonga mbele bila kuwa na hofu yoyote katika njia waliyoongozwa na Mungu katika kuipitia. [GC 291.1; PK Aya ya 6]

**Wazee Wa Imani Na Wasafiri/Mahujaji**

Mungu alikuwa ameyaruhusu majaribu yawajie watu Wake ili kuwaandaa kulitimiza kusudi Lake la neema kwa ajili yao (Yer. 29:11-14). Kanisa lilikuwa limedhalilishwa ili lipate kuinuliwa juu. Mungu alikuwa karibu sana kuuonyesha uweza Wake kwa ajili ya kanisa, ili kuuonesha ulimwengu ushahidi mwingine kwamba hawezi kuwatupa wale wanaomtumainia (Ebr. 13:5, 6). Mungu alikuwa ameyageuza matukio  kwa kuifanya ghadhabu ya Shetani na njama  za watu waovu ipate kutangaza utukufu Wake na kuwaleta watu Wake hadi mahali palipo na usalama. Mateso yao na kufukuzwa uhamishoni mbali na kwao vilifungua njia ya kuelekea kwenye uhuru. [GC 291.2; PK Aya ya 7]

Walipolazimika kwa mara yao ya kwanza kujitenga na Kanisa la Kingereza yaani Anglikana, Wapyuritani walikuwa wameungana kwa pamoja kwa kiapo thabiti cha kidini, kama watu wa Mungu walio huru, "kutembea pamoja katika njia Zake zote zilizofunuliwa kwao na Mungu au zile ambazo angewafunulia." - J. Brown, The Pilgrim Fathers, ukurasa wa 74. Hapo ndipo ilipokuwapo roho ya Kweli ya Matengenezo ya Kanisa, kanuni ya msingi ya Uprotestanti. Ilikuwa ni kwa ajili ya kusudi hilo Wasafiri waliondoka Uholanzi na kwenda kutafuta makazi yao katika Ulimwengu Mpya (Marekani na Australia ni uliovumbuliwa baadaye). John Robinson, mchungaji wao, ambaye kwa uongozi Wake Mungu alizuiwa asiweze kuandamana nao, katika hotuba yake ya kuagana na wakimbizi, alisema hivi: [GC 291.3; PK Aya ya 8]

"Ndugu zangu, tunakaribia kutengana kwa muda mrefu, Bwana anajua ikiwa mimi nitakuwa hai na kuweza kuziona nyuso zenu tena au la. Lakini ikiwa Bwana amepanga tuonane tena au ataona vyema tusionane tena, ninawaagiza, mbele Zake Mungu na mbele ya malaika Zake waliobarikiwa, mnifuate mimi kwa kiwango kile tu ambacho nimemfuata Kristo. Endapo Mungu atawafunulia jambo lingine lolote kupitia chombo kingine chochote kile, iweni tayari kulipokea kama ambavyo mlikuwa tayari kuupokea Ukweli wowote uliotokana na huduma yangu; kwa maana mimi nina uhakika kwamba Bwana anao Ukweli na nuru zaidi ambavyo bado vinapaswa kugunduliwa katika Neno Lake takafitu." - Martyn, gombo la 5, ukurasa wa 570. [GC 291.4; PK Aya ya 9]

**Ahadi Ya Kupokea Nuru**

"Kwa upande wangu, siwezi kuonyesha masikitiko yangu kiasi cha kutosha kwa ajili ya hali ya makanisa yaliyofanya matengenezo ambayo sasa yamefika kwenye kikomo au kituo, na hivyo hayawezi kwenda mbali zaidi kuliko yale mafundisho ya Wanamatengenezo waliyo nayo sasa. Walutheri hawawezi kuvutwa kwenda mbele zaidi ya kile alichokiona Luther;... na Wakalvini (Calvinists), kama mnavyoona, wanang'ang'ania tu mahali pale walipoachwa na yule mtu wa Mungu, ambaye hata hivyo alikuwa bado hajayaona mambo yote. Huu ni msiba mkubwa unaopaswa kuombolezwa sana; maana, kwa kuwa wao walikuwa taa zilizowaka na kuangaza katika wakati wao, lakini bado walikuwa hawajapenya na kuyajua mausia na mashauri yote ya Mungu, walakini, kama wangekuwa wangali hai sasa, wangekuwa tayari kuipokea nuru zaidi kama walivyoipokea ile ya kwanza." - D. Neal, History of the Puritans, gombo la 1, uk. 269. [GC 292.1; PK Aya ya 10]

"Likumbukeni lile agano la kanisa lenu, mlilokubali, kwamba mtatembea na Bwana katika njia Zake zote ambazo mmejulishwa au ambazo mtajulishwa. Kumbukeni ahadi na agano lenu mlilotoa kwa Mungu na kwa kila mmoja kwa

mwenzake, kuipokea nuru yoyote ya Ukweli itakayojulishwa kwenu kutoka katika Neno Lake lililoandikwa; lakini hata hilo jihadharini, nawasihi sana, kile mnachokipokea kama Ukweli, na mkilinganishe na kukipima na Maandiko mengine ya Ukweli kabla ya kukikubali; kwa maana haiwezekani kabisa kwamba Ulimwengu huu wa Kikristo uliotoka hivi karibuni katika giza nene kama hilo la Mpinga Kristo, uweze kuufikia ujuzi mkamilifu kwa mara moja." - Martyn, gombo la 5, uk. 70,71. [GC 292.2; PK Aya ya 11]

Ilikuwa ni ile shauku ya kupata uhuru wa dhamiri (yaani, uhuru wa kumwabudu Mungu kama apendavyo mtu mwenyewe) ndiyo ambayo iliwasukuma Wasafiri kukabiliana kishujaa na hatari za safari ndefu kuvuka ng'ambo ya bahari, kustahimili shida na hatari za nyikani, na kwa mibaraka ya Mungu kujenga, kando ya pwani ya Amerika, msingi wa taifa lenye nguvu. Pamoja na Wasafiri kuwa wanyofu wa moyo na wacha Mungu kama vile walivyokuwa, wasafiri na wapitaji hawa, walikuwa bado hawajaielewa vyema kanuni ile kuu ya uhuru wa dini. Uhuru waliojitolea mhanga ili kuupata kwa ajili yao wenyewe, wao hawakuwa radhi kuwapa wengine usawa kama ule. "Wachache sana, hata miongoni mwa watu wenye fikra pevu na wafundishaji wa maadili wa karne ya kumi na saba, waliokuwa na hata dhana ndogo na sahihi juu ya kanuni hiyo kuu, iliyochipuka kutoka katika Agano Jipya, ambayo inamkiri Mungu kama Ndiye mhukumu pekee wa imani ya mwanadamu." – Ibid., gombo la 5, uk. 297. Fundisho lile lisemalo kwamba Mungu amelikabidhi kanisa haki ya kuitawala dhamiri (kumlazimisha muumini kuamini kile linachoamuru na kumpa adhabu asipofanya vile), pamoja na kufafanua na kuadhibu uzushi, ni mojawapo ya makosa ya kipapa, nalo limezamisha mizizi yake chini sana. Wanamatengenezo wa Kanisa walipoikataa itikadi ya Rumi, haina maana kuwa walikuwa huru kabisa na roho yake ya kutoivumilia imani ya wengine iliyo tofauti na yao (intolerance). Giza nene sana, ambalo kwalo, katika zama nyingi za utawala wake, lilikuwa limeufunika Ulimwengu wote wa Kikristo, lilikuwa bado halijapukutishwa kabisa. Alisema hivi mmojawapo wa wachungaji wao mashuhuri katika koloni la Ghuba ya Massachusetts: "Kuvumiliana ndiko kuliufanya ulimwengu uwe kinyume na Kristo; wala kanisa halijawahi kupata madhara yoyote kamwe kwa kuwaadhibu wazushi." Ibid., gombo la 5, uk. 335. Sheria ilitungwa na wakoloni nayo ilisema kuwa ni washiriki wa kanisa pekee ndio ambao wangekuwa na sauti katika serikali ya kiraia. Aina fulani ya kanisa linaloongozwa na serikali iliundwa, na watu wote walilazimika kuwategemeza wachungaji na mahakimu waliokuwa wamepewa mamlaka ya kudhibiti uzushi. Kwa njia ile nguvu ya serikali ikawa mikononi mwa kanisa. Haukuchukua muda mrefu kupita kabla ya hatua hizo kuleta matokeo yake yasiyoepukika - yaani, mateso. [GC 292.3; PK Aya ya 12]

**Roger Williams**

Miaka kumi na moja baada ya kuanzishwa koloni la kwanza U.S.A, Roger Williams alienda katika Ulimwengu Mpya*-Marekani. Kama walivyokuwa wasafiri wa awali alikwenda kwa ajili ya kufurahia uhuru wa kidini; lakini, akiwa amehitilafiana nao, kwani yeye aliona -- kile ambacho wachache mno katika wakati wake walikuwa wamepata kukiona -- kwamba uhuru huu ulikuwa ni haki ya watu wote isiyoweza kuachanishwa na mtu (mtu hawezi kuuondoa au kumpa mwingine), bila ya kujali kwamba wao wana itikadi au imani ya aina gani. Alikuwa ni mtafutaji wa dhati na bidii wa Ukweli (mwenye kiu), yeye pamoja na Robinson, walishikilia kwamba haiwezekani kabisa kwamba nuru yote kutoka katika Neno la Mungu iwe imekwisha kupokelewa tayari. Wiliams "Alikuwa mtu wa kwanza katika Ulimwengu mpya wa Kikristo kuanzisha serikali ya kiraia kwa kuzingatia msingi wa fundisho la uhuru wa dhamiri, usawa wa mawazo, mbele ya sheria ya nchi" -- Bancroft, sehemu ya 1, sura ya 15, aya ya 16. Alisema kuwa ilikuwa ni wajibu wa hakimu kudhibiti uhalifu, lakini kamwe siyo kutawala dhamiri. "Umma au mahakimu wanaweza kuamua," alisema, "Kipi ni wajibu kati ya mtu mmoja na mwingine, lakini wanapojaribu kumpangia mwanadamu majukumu yake kwa Mungu, wanakuwa wametoka nje ya mstari, na wala hakuwezi kuwa na usalama wowote hapo; kwa kuwa ni wazi kwamba kama hakimu anayo mamlaka, basi, anaweza kuamuru leo seti moja ya maoni au imani, na kesho mwingine akatangaza zingine kesho; kama ambavyo imefanyika katika nchi ya Uingereza na wafalme na malkia mbalimbali, na mapapa pamoja na mabaraza mbalimbali katika Kanisa la Roma; kiasi cha kuifanya imani kuwa lundo la machafuko." *(Marekani na Australia, yalikuwa mabara ya watu wachache sana na hivyo kuitwa nchi mpya na wale waliohamia huko. Watu walianza kuishi karibu na Edeni kwanza, yaani Mashariki ya Kati, na Marekani na Australia mwishoni) - Martyn, gombo la 5, uk. 340.[GC 293.1; PK Aya ya 13]

**Wazee Wasafiri/Mahujaji**

Kushiriki katika ibada za kanisa rasmi la serikali ilikuwa lazima kwa tishio la kutozwa faini au kufungwa. "Wiliams aliikataa hiyo sheria; amri mbaya kuliko zote katika Sheria za Kiingereza ilikuwa ni ile ya kuwalazimisha watu kuhudhuria katika kanisa la parokia. Alichukulia tendo la kuwalazimisha watu kuungana na watu wa itikadi tofauti, kuwa ni ukiukaji wa wazi wa haki zao za asili; kuwakokota watu wasiokuwa na dini wasiopenda kwenda kuabudu, ilionekana kana kwamba ni kutaka kuendeleza au kulazimisha watu wawe na unafiki tu..… 'Hakuna mtu yoyote anayepaswa kulazimishwa kuabudu kwa lazima, au,' aliongeza kusema, 'kuendelea kuabudu kinyume na mapenzi yake mwenyewe.' 'Nini!' wakasema kwa nguvu wapinzani wake kwa mshangao na itikadi zake, na kusema 'Je! Mtendakazi anastahili kupata ujira kwa ajili ya kazi yake?' 'ndiyo,' yeye alijibu, kutoka kwa wale waliomwajiri.'" - Bancroft, sehemu ya 1, sura ya 15, aya ya 2. [GC 294.1; PK Aya ya 14]

Roger Wiliams aliheshimiwa na kupendwa kama mchungaji mwaminifu, mtu mwenye vipaji ambavyo watu wengi hawana, mwenye msimamo na uadilifu usiopinda na ukarimu wa kweli; hata hivyo upinzani usiotetereka dhidi ya mahakimu wa serikali ya kuwa  mamlaka ya kanisa, pamoja na madai yake ya kutaka uwepo uhuru wa dini, havikuweza kuvumiliwa. Matumizi ya fundisho hili jipya, ilisisitizwa sana kuwa, "yangeupindua msingi wa dola pamoja na serikali ya nchi." – Ibid., sehemu ya 1, sura ya 10. Alihukumiwa kufukuzwa kutoka katika makoloni, na, hatimaye, ili kukwepa kukamatwa, alilazimika kukimbia, katikati ya majira ya baridi kali na dhoruba, na kuingia katika msitu ulioshikamana bila vinjia mpaka mbali sana. [GC 294.2; PK Aya ya 15]

"Kwa majuma kumi na manne," anasema, "niliteseka vibaya katika majira yenye uchungu sana, sukujua mkate au kitanda ni nini." Lakini "kunguru walinilisha mimi nyikani," na mara nyingi mti wenye uwazi kwenye shina ndiyo ulikuwa mahali pangu pa kujihifadhi. - Martyn, gombo la 5, uk. 349,350. Hivyo ndivyo alivyoendelea na ukimbizi wake uliomletea maumivu mengi katikati ya theluji na msitu usiokuwa na njia, mpaka alipopata hifadhi yake kwa kabila moja la Wahindi wekundu* ambalo lilimwamini na kumpenda kwa juhudi zake za kuendelea kuwafundisha Kweli za injili *(wazalendo wa Marekani waliokuwa huko mamia ya miaka kabla watu wa Ulaya kufika kule). [GC 294.3; PK Aya ya 16]

Hatimaye, baada ya miezi mingi ya mabadiliko ya hali ya hewa na mizunguko ya kutangatanga kwake, alifika katika pwani za Ghuba ya Narragansett, hapa ndipo alijenga msingi wa jimbo la kwanza la siku hizi ambalo, kwa maana yake kamili, lilitambua haki ya uhuru wa kidini. Kanuni ya msingi ya koloni la Roger Wiliams ilikuwa "kila mtu anatakiwa awe na uhuru wa kumwabudu Mungu kulingana na nuru ambayo inaangaza katika dhamiri yake mwenyewe." - Ibid., gombo la 5, uk.354. Jimbo lake ndilo dogo sana Marekani hata leo, nalo linaitwa Rhode Island, hili likawa hifadhi ya watu walioonewa, nalo likazidi kukua na kufanikiwa mpaka kanuni zake za msingi- - yaani, uhuru wa kiraia na uhuru wa dini - zikawa mawe makuu  jiwe la msingi la pembeni la Jamhuri ya Marekani. [GC 295.1; PK Aya ya 17]

**Hati Kuu Ya Zamani Ya Uhuru**

Katika Hati Kuu ya Zamani ya Uhuru ambayo waasisi wa taifa la Marekani waliitangaza kuwa ndiyo muswada wao wa Haki za Binadamu --- yaani, Tamko lao la Uhuru* —walitangaza hivi: "Tunachukulia kuwa Kweli hizi zina ushahidi ulio wazi, kuwa wanadamu wote wameumbwa wakiwa sawa; kuwa wamepewa na Muumbaji wao haki kadhaa zisizoweza kuachanishwa;* kwamba miongoni mwa hizi haki ni Uhai, Uhuru na utafutaji wa furaha." Tena, Katiba yao ya Nchi inatoa uhakikisho ulio wa kuuheshimu uhuru wa dhamiri ya mtu kwa maneno haya yanayoeleweka wazi kabisa katika kutokiukwa kwa dhamiri: "Hakuna kigezo

chochote cha kidini kitakachotakiwa kama sifa ya kuajiriwa au kufanya kazi katika ofisi yeyote au cheo chochote chenye dhamana ya Umma katika nchi hii ya Marekani (U.S.A).” “Bunge la Marekani, yaani Congress, halitatunga sheria yoyote inayohusika na uanzishaji wa dini, au kupiga marufuku watu kujihusisha na dini kwa uhuru *(zisizoachika, zisizotenganishwa, hati hii inaitwa Declaration of Independence). [GC 295.2; PK Aya ya 18]

**Haki Za Dhamiri Zisizoweza Kuondolewa Kamwe**

“Waandishi wa Katiba ya Nchi walikuwa wameitambua kanuni ya milele isemayo kwamba uhusiano wa mwanadamu na Mungu wake uko juu ya sheria zote iliyotungwa na wanadamu, na haki zake za dhamiri haziwezi kuondolewa kamwe. Mtu hakuhitajika kutumia fikra nyingi ili kuielewa hii Kweli; kwani sote tunaijua hii kutoka ndani ya mioyo yetu. Ni utambuzi huu ndio ambao, katika kushindana kwake na sheria za kibinadamu, umewatia nguvu wafia dini wengi mno katika mateso yao makali kwenye ndimi za moto. Walihisi kwamba wajibu wao kwa Mungu ulikuwa wa hali ya juu sana kuliko amri zilizotungwa na wanadamu (Mdo. 5:29), na ya kwamba mwanadamu asingepaswa kuwa na uwezo wa kutumia mamlaka yake yoyote juu ya dhamiri zao. Ni kanuni tunayozaliwa nayo ambayo hakuna kitu chochote kinaweza kuifuta au kuiondoa.”- Congressional documents (U.S.A.) (Hati za Bunge la Marekani), Serial namba 200, hati Na. 271 [GC 295.3; PK Aya ya 19]

Habari zilipoenea katika nchi za Ulaya, kuhusu nchi ambayo ndani yake kila mtu anaweza kufurahia matunda ya kazi yake na kutii imani ya dhamiri yake mwenyewe, maelfu walifurika kwenda kwenye fukwe za Ulimwengu Mpya [Marekani na Australia]. Makoloni yaliongezeka kwa kasi sana. Massachusetts, kwa sheria maalum, ilitoa ukaribisho na msaada wa bure, kwa gharama ya serikali, kwa Wakristo wa taifa lolote ambao wangekimbia na kuivuka bahari ya Atlantiki ili ‘kukwepa vita au njaa, au uonevu kutoka kwa watesi wao.’ Kwa njia hiyo wakimbizi na wale waliokanyagwa chini au kutendewa vibaya walipokelewa kama wageni rasmi wa dola kwa mujibu wa sheria.” - Martyn, gombo la 5, uk. 417. Kwa kipindi cha miaka ishirini tangu walipotia nanga mara ya kwanza kule Plymouth, maelfu mengi ya Wasafiri walikuja kufanya makazi yao katika jimbo la New England (Uingereza Mpya). [GC 296.1; PK Aya ya 20]

Ili kukidhi lengo lililowaleta, “waliridhika kupata kipato kidogo kilichokidhi maisha yao na wakajinyima kwa kubana matumizi na huku wakifanya kazi ngumu, zenye kutoa jasho. Hawakutafuta chochote kutoka ardhini zaidi ya mapato yanayolingana na kazi yao. Hakuna njozi ya dhahabu iliyotupa kivuli cha kuwahadaa katika njia yao. Waliridhishwa na maendeleo ya polepole lakini yenye uhakika ya serikali zao za kijamii. Walivumilia kwa subira umasikini wa nyika, wakiumwagilia mti wa uhuru kwa machozi yao na kwa jasho la nyuso zao, hadi

ulipostawi kikamilifu na kuweka mizizi mirefu ndani ya ardhi." [GC 296.2; PK Aya ya 21]

Biblia ilichukuliwa kuwa msingi wa imani yao, chanzo cha hekima, na mwongozo wa uhuru. Kanuni zake zilifundishwa kwa bidii majumbani, shuleni na kanisani na matunda yake yalionekana waziwazi katika njia, katika kubana matumizi, kuweka akiba, uwezo mkubwa wa akili, usafi na kiasi. Mtu angeweza akaishi kwa miaka mingi katika makazi ya Wapuritan au Wasafi, "na asimwone mlevi, asisikie kiapo, au asikutane na mtu ombaomba." Bancroft, p. 1, sura. 19, kifungu. 25. Ilionyeshwa kwamba kanuni za Biblia ndiyo ulinzi wenye uhakika wa ukuu wa taifa. Makoloni yaliyo dhaifu na yaliyotawanyika huku na huko, yalikua na kuunda muungano wa majimbo yenye nguvu na ulimwengu ulishikwa na butwaa ulipoona amani na mafanikio ya "kanisa lisilokuwa na papa dola isiyokuwa na mfalme." [GC 296.3; PK Aya ya 22]

Idadi kubwa ya watu iliendelea kufurika, ikivutiwa na fukwe za Amerika, ila walisukumwa na nia tofauti kabisa na ile ya Wasafiri wa kwanza. Ingawa imani ya awali na usafi ziliendelea kutoa mvuto ulioenea na nguvu inayoumba mwenendo, lakini mvuto wake uliendelea kupungua kwa kadiri idadi ya wale waliokuja kutafuta faida ya kidunia ilivyoongezeka. [GC 296.4; PK Aya ya 23]

Kanuni iliyopitishwa na wakoloni wa awali, ya kuruhusu washiriki wa kanisa pekee kupiga kura au kushika nyadhifa katika serikali ya kiraia, ilileta matokeo mabaya zaidi. Hatua hii ilikuwa imekubaliwa kama njia ya kuhifadhi usafi wa serikali, lakini Ilisababisha ufisadi ndani ya kanisa. Mtu kuwa na dini ilipofanywa kuwa stahiki au kigezo cha kupiga kura na kushika ofisi katika serikali ya kiraia, watu wengi kwa kusukumwa tu na nia ya mafanikio ya kidunia, walijiunga na kanisa bila badiliko la moyo. Hivyo makanisa yalijikuta yakiwa na idadi kubwa ya watu ambao hawajaongoka; na hata katika huduma ya kichungaji, kulikuwa na wale ambao si tu walishikilia mafundisho yenye makosa, bali pia hawakuwa na uzoefu wa nguvu za Roho Mtakatifu zinazoumba upya moyo. Kwahiyo yalidhihirishwa tena matokeo mabaya yaliyoshuhudiwa mara kwa mara katika historia ya kanisa tangu siku za Konstantino hadi sasa ya kujaribu kulijenga kanisa kwa msaada wa serikali, kwa kuomba mamlaka ya kidunia kuunga mkono Injili Yake Yeye aliyesema: "Ufalme wangu si wa ulimwengu huu." Yohana 18:36. Muungano wa kanisa na serikali hata uwe wa kiwango ambacho ni kidogo sana, ilhali unaweza kuonekana kama unaweza kuuleta ulimwengu karibu na kanisa, unaweza katika uhalisia kulileta kanisa karibu na ulimwengu. [GC 297.1; PK Aya ya 24]

**Kusimamisha Matengenezo Ya Kanisa**

Kanuni kuu iliyowekewa mkazo kwa ubora na kutetewa na Robinson pamoja na Roger Williams, ilikuwa ile inayosema Ukweli ni endelevu, kwamba inawapasa

Wakristo kusimama tayari kupokea nuru yote inayoweza kuangaza kutoka katika Neno takatifu la Mungu, (Mithali 4:18), dhana kwamba Wakristo wanapaswa kuwa tayari kuipokea nuru yote inayoweza kuangaza toka katika Neno takatifu la Mungu, ilikuwa imepotezwa na wazao wao. Makanisa ya Kiprotestanti ya Amerika, - na yale ya Ulaya pia, -- yaliyopendelewa mno kupokea mibaraka ya Matengenezo ya Kanisa, yalishindwa kusonga mbele katika njia ile ya Matengenezo ya Kanisa. Ingawa watu wachache waaminifu walijitokeza, kutoka wakati hata wakati, kutangaza Ukweli huu mpya na kuyafichua makosa yaliyoshikiliwa kwa muda mrefu, watu wengi, kama Wayahudi katika siku Zake Kristo au mapapa katika wakati ule wa Luther, waliridhika kuamini kama mababa zao walivyokuwa wameamini, na kuishi kama vile baba zao walivyoishi. Kwa hiyo, dini ilipotoka tena na kugeuka kuwa desturi na mapokeo ya kawaida tu; na mafundisho yenye makosa, pamoja na ushirikina, yaani, mambo yale ambayo yangekuwa yametupiliwa kando kama kanisa lingekuwa limeendelea kutembea katika nuru ya Neno la Mungu, yaliendelea kushikiliwa na kuhifadhiwa. Hivyo roho ile iliyochochea Matengenezo ikafa taratibu, mpaka ikawapo haja kubwa sana ya kufanya matengenezo ndani ya makanisa haya ya Kiprotestanti kama ilivyokuwapo haja ya kufanya katika Kanisa la Rumi wakati ule wa Luther. Hali ile ile ya kuipenda dunia au Udunia, na usingizi mzito wa kiroho vilikuwamo ndani ya makanisa, aina ile ile ya kuyaheshimu mawazo ya wanadamu na kuweka nadharia za kibinadamu badala ya mafundisho ya Neno la Mungu. [GC 297.2; PK Aya ya 25]

Usambazaji mkubwa wa Biblia mwanzoni mwa karne ya kumi na tisa, na nuru ile kubwa iliyokuwa imeuangazia ulimwengu, haikufuatiwa na ukuaji wa maarifa ya Ukweli yaliyokwisha kufunuliwa, au mitindo ya maisha iliyobadilishwa na dini-dini ya vitendo. Shetani hakuweza kulizuia au kulificha Neno la Mungu kuwafikia watu kama alivyofanya katika vizazi vile vilivyokuwa vimepita; lilikuwa limewekwa mahali pa karibu kwa wote, pale ambapo wote wangeweza kulipata; lakini ili kuendelea kulitimiza kusudi lake, aliwafanya wengi kulithamini kidogo, na kulichukulia kwa wepesi. Watu walipuuzia kuyachunguza Maandiko, na hivyo waliendelea kuzikubali tafsiri za uongo au potofu, na kuyashikilia mafundisho ya dini ambayo hayakuwa na msingi katika Biblia. [GC 298.1; PK Aya ya 26]

Shetani alipoona kuwa juhudi zake zimeshindwa kuangamiza Ukweli kwa kutumia mbinu ya mateso, aliutumia tena mpango wa kufanya maridhiano ya kulegeza masharti, jambo ambalo lilisababisha uasi mkuu na uundwaji wa Kanisa la Roma. Aliwashawishi Wakristo waungane, wenyewe kwa wenyewe, sasa siyo na upagani, bali na wale ambao, katika kujiingiza kwao sana na mambo ya ulimwengu huu, walikuwa wamejionyesha wenyewe kwenda mbali kiasi kwamba walishakuwa waabudu sanamu halisi, sawa na wale waabudu sanamu za kuchongwa. Na matokeo ya muungano huu yalikuwa mabaya zaidi sasa kuliko

katika zama zilizokuwa zimepita; kiburi na ubaradhifu vilijitokeza chini ya vazi la unafiki wa dini, na makanisa yakaanza kuharibikiwa kwa ufisadi. Shetani aliendelea kupotosha mafundisho ya Biblia, na desturi na mila ambazo zingeharibu mamilioni ya watu zilikuwa zikiotesha mizizi yake mirefu kwenda chini sana. Kanisa lilikuwa likishikilia na kutetea tamaduni hizi, badala ya kuishindania "imani waliyokabidhiwa watakatifu mara moja tu." Kwa njia hiyo, kanuni zile ambazo kwa ajili yake Wanamatengenezo wa awali walikuwa wamezifanyia kazi na kupata mateso mengi zilishushwa chini. [GC 298.2; PK Aya ya 27]

*(Katika vitabu vya Roho ya Unabii kwa kawaida anaposema Sheria, Kanuni, Maagizo au Amri za Mungu ana maana zile Sheria za AMRI KUMI zilizotolewa Sinai-Kutoka 20, Kumbukumbu La Torati 5, Mathayo 5. Kuhusu Ukweli wa Mungu, Nasi pia tunapaswa kuwa na uelewa kama wa Roger Williams, yaani Mungu angali ana hazina katika Neno Lake ambazo anaendelea kuwafunulia wale walio tayari kusikia au wenye shauku kujifunza, daima Ukweli ni endelevu, ni Mungu tu Ndiye ana Ukweli wote, sisi tutaendelea kujifunza milele zote na kukua, katika Neno lake kuna ahadi 8110 katika Biblia hebu na tuzichunguze na kuzidai hizo.)*

## SURA YA 17

## AHADI ZA MAREJEO YA KRISTO

### (Wajumbe wa Mapambazuko/Wapiga Mbiu za Mapambazuko)

Ufupisho: Ujio wa Yesu Katika aya za Biblia 31,102 umetajwa mara 2000 hivi. Jambo hili ni la uhakika kabisa. Hata hivyo wengi hawaujui Ukweli huu.Tazama Maandiko na kuyabainisha mafungu hayo ili moyo upate kuwaka furaha na tumaini kuu na la ajabu kupita yote!

Mojawapo kati ya zile Kweli makini na zenye utukufu mno, zilizofunuliwa katika Biblia ni ile inayohusu kuja Kwake Kristo kwa mara ya pili ili kuitekeleza/kuikamilisha kazi Yake kuu ya ukombozi. Kwa watu wa Mungu walio wasafiri, ambao wamekwisha kuondoka muda mrefu sana uliopita na kwenda katika "nchi ya uvuli wa mauti," tumaini la baraka lenye thamani na linaloamsha furaha ndani ya mioyo yao, limetolewa tena katika ahadi ya kutokea Kwake, Yeye aliye "ufufuo na uzima," ili apate "kuwarudisha nyumbani tena watu Wake waliofukuzwa." Fundisho hilo la ujio wa Kristo kwa mara ya pili ndio ufunguo muhimu haswa wa Maandiko Matakatifu. Tangu siku ambayo wale wanandoa wawili kwa kwanza walipogeuza hatua zao kwa huzuni na kuondoka katika bustani ya Edeni, watoto wa imani wameendelea kungojea kuja Kwake Yeye Aliyeahidiwa kuja kuzivunjilia mbali nguvu za yule mharibifu na kuwarudisha tena kwenye Paradiso iliyopotea. Watakatifu wa zamani walitazamia kuja Kwake

Masihi katika utukufu Wake, kama ndilo utimilifu na kilele cha tumaini lao. Henoko, mtu wa saba tu katika mfululizo wa uzao wa wale walioishi katika bustani ya Edeni, mtu ambaye kwa karne tatu akiwa duniani, alitembea na Mungu wake, aliruhusiwa kumwona tokea mbali Mkombozi anayekuja. “Tazama,” alitangaza, “Bwana anakuja na maelfu ya watakatifu Wake, ili afanye hukumu juu ya wote.” Yuda 14, 15. Mzee wa imani Ayubu katika usiku ule wa mateso yake alisema maneno haya kwa nguvu na tumaini lisilotikisika: “Lakini mimi najua ya kuwa Mteteaji wangu Yu hai, na ya kuwa hatimaye atasimama juu ya nchi: ... pasipokuwa na mwili wangu nitamwona Mungu; Nami nitamwona mimi nafsi yangu, Na macho yangu yatamtazama, wala si mwingine.” Ayubu 19:25-27 [GC 299.1; PK Aya ya 1]

Ujio Wake Kristo kuleta utawala wa haki uliwahamasisha waandishi wa Maandiko Matakatifu kuandika maneno mazito, bora, yenye nguvu, na yanayogusa na kuleta joto moyoni. Waandishi wa mashairi na manabii wa Biblia wamedumu katika hii ahadi kwa Maneno yanayong’aa kwa moto wa utukufu wa mbinguni. Mwandishi wa Zaburi aliimba kuhusu nguvu na ukuu wa Mfalme wa Israeli: “Tokea Sayuni, ukamilifu wa uzuri, Mungu amemulika. Mungu wetu atakuja wala hatanyamaza....Ataziita mbingu zilizo juu, Na nchi pia awahukumu watu Wake.” Zaburi 50:2-4. “Mbingu na zifurahi, nchi na ishangilie ... mbele za Bwana, kwa maana Anakuja. Kwa maana Anakuja Aihukumu nchi. Atauhukumu ulimwengu kwa haki, Na mataifa kwa uaminifu Wake.” Zaburi 96:11-13 [GC 300.1; PK Aya ya 2]

Alisema hivi nabii Isaya: “Amkeni, kaimbeni, ninyi mnaokaa mavumbini, kwa maana umande wako ni kama umande wa mimea, nayo ardhi itawatoa waliokufa.” "Wafu wako wataishi, maiti Zangu zitafufuka.” “Amemeza mauti hata milele; na Bwana Mungu atafuta machozi katika nyuso zote; na aibu ya watu Wake ataiondoa katika dunia yote; maana Bwana amenena hayo. Katika siku hiyo itasemwa, Tazama, Huyu Ndiye Mungu wetu, Ndiye tuliyemngoja atusaidie; Huyu Ndiye Bwana tuliyemngoja, Na tufurahi na kuushangilia wokovu Wake.” Isaya 26:19; 25:8, 9. [GC 300.2; PK Aya ya 3]

Naye Habakuki, akiwa amezidiwa nguvu na kustaajabishwa na njozi takatifu, aliuona ujio Wake. “Mungu alikuja kutoka Temani, Yeye aliye Mtakatifu kutoka Mlima Parani. Utukufu Wake ukazifunika mbingu, nayo dunia ikajaa sifa Yake. Mwangaza Wake ulikuwa kama nuru.” “Akasimama, akaitetemesha dunia; Akatazama, akawasitusha mataifa; Na milima ya zamani ikatawanyika, vilima vya kale vikainama; Miendo Yake ilikuwa kama siku za kale.” “Hata ukapanda farasi Zako, katika magari Yako ya wokovu.” “Milima ilikuona, ikaogopa; vilindi vikatoa sauti yake, vikainua juu ya mikono yake. Jua na mwezi vikasimama makaoni mwao; mbele ya nuru mishale yako itakapotapakaa mbele ya mwangaza wa mkuki Wako umeremetao.” “Ukatokea kwa ajili ya wokovu wa watu Wako, kwa

ajili ya wokovu wa Masihi wako." Habakuki 3:3, 4, 6, 8, 10, 11, 13. [GC 300.3; PK Aya ya 4]

Wakati Mwokozi alipokuwa karibu kutengana na wanafunzi Wake, aliwafariji katika huzuni yao kwa ahadi kwamba angerudi tena: "Msifadhaike mioyoni mwenu. Nyumbani mwa Baba Yangu mna makao mengi.... maana naenda kuwaandalia mahali. Basi Mimi nikienda na kuwaandalia mahali, nitakuja tena niwakaribishe Kwangu." Yohana 14:1-3. "Hapo atakapokuja Mwana wa Adamu atakuja katika utukufu Wake, na malaika watakatifu wote pamoja Naye." "Ndipo atakapoketi katika kiti cha utukufu Wake; na mataifa yote watakusanyika mbele Zake." Mathayo 25:31, 32. [GC 301.1; PK Aya ya 5]

Malaika waliochelewa-chelewa kuondoka pale juu ya mlima Mizeituni baada ya kupaa kwa Kristo waliirudia ahadi ile ya kurudi Kwake kwa wanafunzi: "Huyu Yesu aliyechukuliwa kutoka kwenu kwenda juu mbinguni, atakuja jinsi hiyo hiyo mlivyomwona akienda Zake mbinguni." Matendo 1: 11. Naye Mtume Paulo, akisema kwa njia ya Uvuvio wa Roho, alishuhudia akasema: "Kwa sababu Bwana Mwenyewe atashuka kutoka mbinguni pamoja na mwaliko, na sauti ya Malaika Mkuu, na parapanda ya Mungu." 1 Wathesalonike 4:16, 17. Anasema nabii katika kisiwa cha Patmo: "Tazama, Yuaja na mawingu; na kila jicho litamwona." Ufunuo 1:7. [GC 301.2; PK Aya ya 6]

Marejeo Yake yamezungukwa na utukufu wa "kufanywa upya vitu vyote, zilizonenwa na Mungu kwa kinywa cha manabii Wake watakatifu tokea mwanzo wa ulimwengu." Matendo 3:21. Ndipo utawala wa uovu ambao umedumu kwa muda mrefu utavunjwa; "Falme za ulimwengu huu" zitakuwa "falme za Bwana wetu, na za Kristo Wake; Naye atatawala milele na milele." Ufunuo 11:15. "Na utukufu wa Bwana utafunuliwa, na wote wenye mwili watauona pamoja." "Ndivyo Bwana Mungu atakavyootesha haki na sifa mbele ya mataifa yote." Atakuwa "ni taji ya fahari, na kilemba cha uzuri, kwa mabaki ya watu Wake." Isaya 40:5; 61:11; Isaya 28:5. [GC 301.3; PK Aya ya 7]

Wakati ule ndipo ufalme wa amani wa Masihi, uliotamaniwa kwa muda mrefu, utakapoanzishwa chini ya mbingu hii yote. "Bwana ataufariji Sayuni; atapafariji mahali Pake palipokuwa ukiwa; atafanya jangwa lake kuwa kama bustani ya Edeni, na nyika yake kama bustani ya Bwana.." "Litapewa uzuri wa Lebanoni, utukufu wa Karmeli na Sharoni." "Hutaitwa tena Aliyeachwa, wala nchi yako haitaitwa tena, Ukiwa; bali utaitwa Hefsiba (Namfurahia Bwana); na nchi yako Beula (Ameolewa)." "Kama vile bwana arusi amfurahiavyo bibi arusi, ndivyo Mungu wako atakavyokufurahia wewe." Isaya 51:3; 35:2; 62:4, 5,pambizo. [GC 302.1; PK Aya ya 8]

Marejeo Yake Bwana yamekuwa tumaini la wafuasi Wake wote wa kweli katika enzi zote. Ujio wa Bwana umekuwa tumaini la wafuasi Wake wa kweli

katika zama zote. Ahadi ya Mwokozi wakati akiagana na wanafunzi Wake juu ya mlima wa Mizeituni, kuwa angelirudi tena, iliwaangazia na kuwaletea wanafunzi Wake matumaini ya wakati ujao, iliijaza mioyo yao furaha na tumaini ambalo huzuni isingeweza kulizima wala majaribu kulihafifisha. Katikati ya mateso,ugumu wa maisha, maumivu na mahangaiko, "kutokea kwa Mungu mkuu na Mwokozi wetu Yesu Kristo" kulikuwa ni "tumaini lenye baraka." Wakristo wa Thesalonike walijawa na huzuni walipokuwa wakizika wapendwa wao, ambao walikuwa wametumaini kuishi na kushuhudia ujio wa Bwana, Paulo, mwalimu wao, aliwaelezea juu ya ufufuo utakaotokea wakati wa kuja Kwake Mwokozi kwa mara ya pili. Ndipo wale waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza, na kwa pamoja na walio hai tutanyakuliwa ili kumlaki Bwana hewani. "Na hivyo," alisema, "tutakuwa pamoja na Bwana milele. basi tufarijiane kwa Maneno haya." 1 Wathesalonike 4:16-18. [GC 302.2; PK Aya ya 9]

Kwenye kisiwa cha Patmo chenye miamba, mwanafunzi huyo mpendwa alisikia ahadi, "Naam, Naja upesi,"* na mwitikio wake unatoa ombi lenye matamanio la kanisa katika safari yake yote, "Amina; na uje, Bwana Yesu." Ufunuo 22:20 *(fungu zima linasema Yeye Mwenye kuyashuhudia haya asema, Naam, Naja upesi." [GC 302.3; PK Aya ya 10]

Kutoka katika gereza la chini ya ardhi, kutoka katika mti wa kuchomea watu moto, kutoka katika jukwaa la kutesea watu, ambapo watakatifu na wafia dini walitoa ushuhuda kwa ajili ya Ukweli, inakuja baada ya karne nyingi sauti ya imani na tumaini lao "ikiwa vimehakikishiwa juu ya ufufuo Wake binafsi na hatimaye ufufuo wao wakati wa ujio Wake, kwa ajili ya kusudi hilo," alisema mmoja wa Wakristo hao, "waliidhihaki mauti, na wakaonekana kuwa juu ya mauti."- Daniel T. Taylor; The Reign of Christ on Earth: or, The Voice of the Church in All Ages, ukurasa wa 33. Walikuwa tayari kushuka makaburini mwao, ili wapate 'kufufuka wakiwa huru.'-Ibid., ukurasa wa 54. Walitarajia kumwona "Bwana akishuka kutoka mbinguni katika mawingu pamoja na utukufu wa Baba Yake," "kuwaletea wenye haki nyakati za ufalme." Wawaldensia pia walidumisha imani hiyo hiyo.- Ibid., ukurasa wa 129-132. Wycliffe alitazamia kwa hamu kutokea kwa Mkombozi kama ndiyo tumaini lenye baraka la kanisa.- Ibid., ukurasa wa 132-134. [GC 302.4; PK Aya ya 11]

Luther alitangaza hivi: "Naishawishi nafsi yangu kuamini kwa hakika kwamba, siku ya hukumu haitakosa kuja ndani ya miaka mia tatu kamili. Mungu hawezi, wala hataweza, kuuacha ulimwengu huu ulio mwovu kwa muda mrefu zaidi." "Siku ile kuu inakaribia ambayo katika hiyo ufalme huo wa machukizo utapinduliwa."- Ibid., ukurasa wa 158, 134. [GC 303.1; PK Aya ya 12]

"Ulimwengu huu uliozeeka hauko mbali na mwisho wake," alisema Melanchthon. Calvin anawaasa Wakristo "wasisite, kutarajia kwa matamanio na bidii siku ya kuja kwa Kristo kama tukio lililo na heri na mafanikio kuliko matukio

mengine yote; na alitangaza kwamba “familia nzima ya waaminifu itadumu kuitarajia siku hiyo mawazoni mwake.” “Yatupasa kuwa na njaa ya kumtafuta Kristo, tunapaswa kutafuta, tunapaswa kutafakari,” alisema, “mpaka mapambazuko ya siku ile kuu, ambapo Bwana ataonyesha kikamilifu utukufu wa ufalme Wake.”- Ibid., ukurasa wa 158, 134. [GC 303.2; PK Aya ya 13]

“Je, Bwana wetu Yesu Kristo hajakwenda nayo juu mbinguni miili yetu?” Knox, Mwanamatengenezo wa Scotland alisema, “tena, si atarudi tena? Sisi twajua kwamba atarudi, na tena upesi na atasindikizwa katika safari Yake, na msafara wenye makusudi maalumu.” Ridley na Latimer, ambao waliyasalimisha maisha yao kwa ajili ya Ukweli, walitazamia kwa imani kwa ajili ya ujio wa Bwana. Ridley aliandika: “Ulimwengu, bila shaka lolote nazungumza haya - jambo hilo mimi naliamini, na kwa hiyo ninalisema - ulimwengu huu unakaribia mwisho wake. Hebu sisi pamoja na Yohana, mtumishi wa Mungu, na tupige kelele mioyoni mwetu na kumlilia Mwokozi wetu Kristo, tukisema, Na uje, Bwana Yesu, njoo.”- Ibid., ukurasa wa 151, 145. [GC 303.3; PK Aya ya 14]

Baxter alisema, “Mawazo juu ya ujio wa Bwana,” “ni matamu zaidi kuliko mawazo mengine yoyote, na yananiletea furaha kubwa sana.”, Richard Baxter, Works, juzuu ya 17, uk. 555. “Ni kazi ya imani na tabia ya watakatifu Wake kupenda marejeo Yake na kulitazamia lile tumaini lenye baraka.” “Ikiwa mauti ndiye adui wa mwisho kuangamizwa wakati ule wa ufufuo, basi, tunaweza kujifunza kwa bidii jinsi waumini wanavyopaswa kutamani na kuombea kwa ajili ya ujio wa pili wa Kristo, wakati ushindi huu mkamilifu na wa mwisho utakapopatikana.”- Ibid., juz. ya 17, uk. 500. “Hii ndiyo siku ambayo waumini wote wanapaswa kuitamani sana, kuitumainia na kuingoja, kama ukamilifu wa kazi yote ya ukombozi wao na shauku na juhudi zote za roho zao.” “ Harakisha Ee Bwana, siku hii yenye baraka!”- Ibid., juz. ya 17, uk. 182, 183. Hilo ndilo lilikuwa tumaini la kanisa la mitume, la “kanisa nyikani,” na kanisa la Wanamatengenezo. [GC 303.4; PK Aya ya 15]

Unabii hauelezei tu namna Kristo atakavyokuja na kusudi la kuja Kwake, bali huelezea ishara ambazo kupitia hizo, wanadamu wataweza kujua kukaribia kwa ujio Wake. Alisema hivi Yesu: “Kutakuwa na ishara katika jua, na mwezi, na nyota.” Luka 21:25. “Jua litatiwa giza, na mwezi hautatoa mwanga wake, na nyota za mbinguni zitakuwa zikianguka, na nguvu zilizo mbinguni zitatikisika. Hapo ndipo watakapomwona Mwana wa Adamu akija mawinguni kwa nguvu nyingi na utukufu.” Marko 13:24-26. Hivyo ndivyo mwandishi wa ufunuo anavyoelezea ishara za kwanza zinazotangulia ujio Wake wa pili: “Palikuwa na tetemeko kuu la nchi; jua likawa jeusi kama gunia la singa, na mwezi ukawa kama damu. Ufunuo 6:12. [GC 304.1; PK Aya ya 16]

**Maangamizi Ya Lisbon**

Ishara hizi zilishuhudiwa kabla ya mwanzo wa karne ya kumi na tisa. Katika utimizo wa unabii huu, mnamo mwaka wa 1755, kulitokea tetemeko la ardhi la kutisha sana kuliko yote yaliyowahi kutokea na kuwekwa kwenye rekodi. Ingawa kwa kawaida linajulikana kama tetemeko la ardhi la Lisbon, lilienea na kufika hadi kwenye eneo kubwa la Ulaya, Afrika, na America. Lilifika huko Greenland, huko Kwenye visiwa vya West Indies au Carribean (kama nchi ya Martinique), kisiwa cha Madeira, Norway na Sweden, Uingereza na Ireland. Lilienea na kusikika kiasi cha eneo lisilopungua maili za mraba milioni nne. Barani Afrika mtikisiko ulikuwa mkubwa kama ulivyokuwa Ulaya. Sehemu kubwa ya Algiers iliharibiwa; na umbali mfupi kutoka Morocco, kijiji kilichokuwa na wakazi kati ya elfu nane na elfu kumi kilimezwa chote. Wimbi kubwa lilifagia mwambao wa Uhispania na Afrika na kumeza miji na kusababisha uharibifu mkubwa sana. [GC 304.2; PK Aya ya 17]

Ilikuwa katika nchi ya Uhispania na Ureno ambapo mtikisiko huo ulisababisha uharibifu wake mkubwa kuliko maeneo mengine. Huko katika maeneo ya Cadiz wimbi, lililopita hapo, lilisemekana lilikuwa limeinuka urefu wa futi sitini kwenda juu. “Baadhi ya milima mirefu sana nchini Ureno ilitikiswa sana, kana kwamba, ilikuwa itoke kwenye misingi yake na baadhi yao ilifunguka kwenye vilele vyake, ikapasuka na kugawanyika na kisha kuvunjikavunjika kwa namna ya ajabu sana, mabonge makubwa ya vipande vyake yakitupwa chini kwenye mabonde yaliyo karibu. Inasimuliwa kwamba Ndimi za moto zilitoka na kuonekana kutoka kwenye mipasuko ya milima hii.”- Sir Charles Lyell, Principles of Geology ukurasa wa 495. [GC 304.3; PK Aya ya 18]

Huko katika jiji la Lisbon “sauti ya radi ilisikika chini ya ardhi, na muda mfupi baadaye mtikisiko na mshtuko mkubwa ukaangusha sehemu kubwa zaidi ya jiji lile. Katika muda wa takribani dakika sita watu elfu sitini waliangamia. Kwanza, bahari ilirudi nyuma, na kuufanya ukanda ule mwembamba wa sakafu ya bahari kuwa mkavu; halafu bahari ikarudi tena, ikiwa imeinuka juu ya usawa wake wa kawaida kwa kiasi cha futi hamsini au zaidi.” (tsunami) “Miongoni mwa matukio mengine yasiyo ya kawaida yaliyosimuliwa kutoka pale Lisbon wakati wa wa janga hilo kuu ni lile la kudidimia kwa gati jipya,* lililokuwa limejengwa kwa marumaru tupu, kwa gharama kubwa sana. Umati mkubwa wa watu ulikuwa umejikusanya pale kwa usalama wao, pakiwa ni mahali ambapo wangekuwa mbali na yale majumba yaliyokuwa yakianguka chini; lakini kwa ghafula gati lile likazama chini pamoja na watu wote waliokuwa juu yake, wala hakuna hata mwili mmoja, miongoni mwa miili ya maiti zile, ulioelea juu ya uso wa bahari ile.”- Ibid., ukurasa wa 495 *(gati ni mahali pa kupakia na kupakua mizigo na kuziegesha meli kwa kuzifunga). [GC 305.1; PK Aya ya 19]

“Kishindo kikubwa cha mtikiso” wa tetemeko la ardhi “Kilifuatwa mara moja na kuanguka kwa kila kanisa na nyumba ya watawa, karibia majengo yote

makubwa ya umma na zaidi ya robo ya nyumba zote za makazi ya watu. Katika muda wa saa mbili baada ya mtikiso huo, mioto ililipuka katika maeneo tofauti tofauti na ukaendelea kwa hasira na kasi hiyo kwa muda wa takribani siku tatu mfululizo, kiasi kwamba jiji lote lilitelekezwa kabisa. Tetemeko hili lilitokea katika siku yao takatifu ya ibada, wakati ambapo makanisa na nyumba za watawa zilikuwa zimejaa watu, wachache tu, ndio waliweza kuokoka." - Encyclopedia Americana, art. "Lisbon," note (ed. 1831). "Hofu iliyowashika watu ilikuwa zaidi ya maelezo. Hakuna mtu aliyeweza kulia; tukio hili lilikuwa lilikuwa zito kiasi kwamba hata machozi yalikauka. Walikimbia huku na huko, wakijawa wamechanganyikiwa kwa mshtuko, wakijipiga nyuso zao na vifua, wakilia, 'Miseri-cordia! Tuhurumie ulimwengu umefikia mwisho wake!'Akina mama waliwasahau watoto wao, na kukimbia huku na huko wakiwa wamebeba mizigo mizito ya sanamu za Yesu aliyeangikwa msalabani. Kwa bahati mbaya, wengi walikimbilia makanisani ili kupata ulinzi; lakini ilikuwa ni kazi bure, hawakupata msaada wowote, na ibada za sakramenti zilifichuliwa na kuumbuka; viumbe hawa maskini walizikumbatia altare au mimbari; sanamu, mapadri pamoja na watu wakazikwa chini ya gofu moja katika maangamizi ya pamoja." Imekisiwa kwamba watu wapatao tisini elfu walipoteza maisha yao katika siku ile ya maafa mazito. [GC 305.2; PK Aya ya 20]

**Jua Na Mwezi Kuitiwa Giza**

Miaka ishirini na tano baadaye ilitokea ishara ya pili iliyotajwa kwenye unabii-- kutiwa giza kwa jua na mwezi. Kilichopelekea hili kushangaza watu zaidi ilikuwa ni ukweli kuwa wakati wa kutimizwa kwake ulikuwa umebainishwa waziwazi. Katika maongezi ya Mwokozi na wanafunzi Wake katika mlima wa Mizeituni, baada ya kuelezea kipindi kirefu cha kujaribiwa kwa Kanisa, -- miaka 1260 ya mateso ya upapa, ambayo kwayo alikuwa ameahidi kwamba mateso yangelifupishwa,-aliyataja kwa njia hiyo matukio kadhaa ambayo yangetangulia kabla ya marejeo Yake, na kuweka wakati maalumu ambapo moja ya ishara hizi ingeshuhudiwa: "Lakini siku zile, baada ya dhiki hiyo, jua litatiwa giza, na mwezi hautatoa mwanga wake." Marko 13:24. Siku au miaka 1260, iliishia mnamo mwaka 1798. Robo karne kabla, mateso yalikuwa karibu yamekoma kwa kiwango kikubwa. Baada ya mateso haya, kulingana na maneno Yake Kristo, jua lilipaswa kutiwa giza. Siku ya tarehe 19 Mei, 1780, unabii huu ulitimizwa. [GC 306.1; PK Aya ya 21]

"Karibu sana, kama sio tukio la pekee kabisa, laweza kuwa kile kioja cha siri na ajabu mno kuliko vyote, cha aina yake kabisa, ambacho mpaka sasa hakijapatiwa maelezo yoyote,... ni siku hii ya giza ya Mei 19, 1780, - Kutiwa giza kwa ajabu, kusikoelezeka kwa mbingu zote zilizokuwa zinaonekana kwa macho pamoja na anga-hewa yake katika jimbo lile la Massachusets, Marekani linaloitwa

Uingereza Mpya (New England).” - R. M. Devens, Our First Century, uk. wa 89. [GC 306.2; PK Aya ya 22]

Shahidi mmoja aliyeliona tukio hili mbashara, akiwa anaishi Massachusetts alilieleza tukio hili kama ifuatavyo: “Asubuhi jua lilichomoza vyema bila kuwa na mawingu, lakini ghafla lilifunikwa. Mawingu yaliteremka chini na ndani yake yalitoa tahadhari ya giza la kutisha, tena yakiwa ya kuogofya, na baada ya muda mfupi tu umeme wa radi ulimulika ghafula, ngurumo ya radi ikapiga na mvua za rasharasha zikanyesha. Kufikia saa tatu asubuhi, mawingu yale yakawa mepesi zaidi na yakawa na sura ya shaba au msasa, mawe, miti, majengo, maji na watu walibadilishwa na mwanga huu wa ajabu, usiokuwa wa dunia hii. Dakika chache baadaye, wingu zito jeusi lilitanda anga nzima isipokuwa katika ukingo mwembamba kwenye upeo wa macho na kulikuwa na giza ambalo kwa kawaida hutokea saa tatu usiku wakati wa majira ya joto (Summer).... [GC 306.3; PK Aya ya 23]

“Hofu, wasiwasi, kicho na woga pole pole vilianza kuzijaza akili ya watu. Wanawake walisimama milangoni, wakitazama nje mandhari ya giza lililofunika; wanaume walirejea kutoka katika kazi zao za mashambani; seremala aliziacha zana zake, mhunzi aliiacha oveni/kalibu yake ya kuoka chuma, mfanyabiashara aliiacha meza yake ya biashara. Wanafunzi shuleni wakapewa ruhusa kwenda zao, na watoto waliokuwa wakitetemeka, walitimua mbio kuelekea majumbani mwao. Wasafiri walikatisha safari zao na kutafuta hifadhi katika nyumba ya wakulima iliyokuwa karibu. ‘Ni nini kinakuja?’ kila kinywa na kila moyo ulijiuliza. Ilionekana kana kwamba kimbunga kilikuwa karibu kupita kwa kasi juu ya nchi nzima, au kana kwamba ilikuwa siku ya kilele cha mambo yote. [GC 306.4; PK Aya ya 24]

Mishumaa ilitumika; na mioto ya nyumbani ikang'aa sana kama usiku usiokuwa na mbalamwezi katika majira ya kupukutisha majani unavyokuwa. Kuku walirudi kwenye mabanda yao kulala usingizi, ng’ombe walijikusanyika kwenye ugo wa vyombo vya malisho, mazizini mwao na kutoa sauti, vyura walichungulia kinachoendelea, ndege waliimba nyimbo zao za jioni na popo waliruka huku na kule. Lakini binadamu walijua kuwa usiku ulikuwa haujawadia bado...…. [GC 307.1; PK Aya ya 25]

“Dk. Nathanael Whittaker, mchungaji wa kanisa la Tabernacle huko Salem, aliendesha ibada za kidini katika jumba la mikutano na alihubiri mahubiri ambayo alisisitiza kwa kuelezea kwamba giza lile halikuwa la kawaida, na pengine ulikuwa ni muujiza. Waumini wa makanisa walikusanyika pamoja katika sehemu nyingine pia. Mafungu yaliyotumika kwa hotuba za papo kwa hapo, yaani bila kuandaliwa, yalikuwa hayatofautiana sana, yote yalikuwa ni yale yaliyoonekana kuonyesha kwamba giza lile lililapatana na unabii wa Maandiko....Giza liliongezeka na kuwa nene sana muda mfupi tu baada ya saa

tano asubuhi.” The Essex Antiquarian, Aprili, 1899, juz. ya 3, Na. 4, uk. wa 53, 54. “Katika sehemu nyingi za nchi lilikuwa nene sana wakati wa mchana, kiasi cha watu kutokuweza kuzisoma saa saa zao za mikononi, au saa za mezani, au kuweza kula chakula chao, au wala kuendesha shughuli zao za nyumbani bila kutumia mwanga wa mishumaa....[GC 307.2; PK Aya ya 26]

“Eneo la ukubwa wa giza hili lilikuwa ni la ajabu. Kwani lilienda mbali hadi mashariki, mpaka sehemu za Falmouth. Upande wa magharibi lilifika hadi sehemu ya mbali zaidi ya Connecticut na Albany. Kwa upande wa kusini, lilionekana katika fukwe za bahari; na upande wa kaskazini lilifikia eneo lote la makazi ya watu wa Amerika.” William Gordon, History of the Rise, Progress, and Establishment of the Independence of the U.S.A., juzuu ya 3, uk. 57. [GC 307.3; PK Aya ya 27]

**Ushahidi Wa Historia**

Giza nene la mchana liliendelea, mpaka saa moja au mbili kabla ya jioni, na anga lisilokuwa na mawingu kiasi na jua lilitokea na kuonekana, ingawa bado lilikuwa limefunikwa na ukungu mweusi, mzito. “Baada ya jua kutua, mawingu yakaja tena juu na giza likaingia tena kwa kasi.” “Wala hakukuwahi kuwa na giza la usiku lisilo la kawaida na la kutisha kuliko lile la siku ile; ijapokuwa kulikuwa na mbalamwezi iliyokuwa inang'aa na kukaribia upevu, kulikuwa hakuna kitu kilichoweza kutambuliwa au kuonekana bila msaada wa nuru ya bandia kama mshumaa au chanzo kingine kilichotengenezwa na mwanadamu, nuru hiyo ilipoonekana kutoka nyumba za jirani na maeneo mengine kwa mbali, ilionekana mithili ya giza la Misri ambalo lilionekana kutopenyeka miale ya nuru.”, Isaiah Thomas, Massachusetts Spy; or, American Oracle of Liberty, juz. ya 10, Na. 472 (Mei 25, 1780). Shahidi aliyejionea tukio hilo alisema hivi: “nilishindwa kujizuia kuelewa wakati huo, kuwa endapo kila kitu chenye uwezo wa kutoa mwanga huko angani ulimwenguni kingekuwa kimefunikwa katika kivuli kisichoweza kupenyeka na nuru au kisichoweza kuondosheka kabisa, basi giza ambalo lingetokea lisingeweza kuwa kamilifu zaidi ya lile.”, Letter by Dr. Samuel Tenney, of Exeter, New Hampshire, December, 1785 (in Massachusetts Historical Society Collections, 1792, mfululizo wa 1, juz. 1, uk. 97). Ijapokuwa mnamo saa tatu ya usiku mwezi ulijitokeza wote na kuonekana vizuri kabisa “haukuwa na uwezo wowote wa kuviondoa vivuli hivyo vya giza vilivyokuwa kama hofu ya kifo.” Baada ya sasa sita usiku, giza lilitoweka na mwezi, ulipoonekana mara ya kwanza, ulikuwa na mwonekano wa damu. [GC 307.4; PK Aya ya 28]

Mei 19, 1780, inabaki katika historia kama “Siku ya Giza.” Tangu wakati wa Musa hakuna kipindi chochote kilichokuwa na giza lenye uzito, kwa kiwango na muda sawa na hilo, ambacho kimewahi kuandika kwenye kumbukumbuku. Maelezo ya tukio lile, kama yalivyotolewa na mashahidi waliojionea mambo haya

mbashara, ni mwangwi tu wa yale Maneno ya Bwana, yaliyoandikwa na nabii Yoeli, miaka elfu mbili na mia tano kabla ya kutimiza kwake: “Jua litageuzwa kuwa giza, na mwezi kuwa damu, kabla haijaja hiyo siku ya Bwana iliyo kuu na itishayo.” Yoeli 2:31. [GC 308.1; PK Aya ya 29]

**Ishara Zaidi Za Marejeo Ya Kristo**

Kristo alikuwa amewaeleza watu Wake waziangalie ishara au dalili za kuja Kwake na kufurahi wanapoviona viashiria vya ujio wa Mfalme wao. “Basi mambo hayo yaanzapo kutokea,” Alisema, “changamkeni, mkaviinue vichwa vyenu, kwa kuwa ukombozi wenu umekaribia.” Akawaelekeza wafuasi Wake kwenye miti Iliyokuwa inachipuka wakati wa majira ya Kuchipua na kusema: “Wakati iishapo kuchipuka, mwaona na kutambua wenyewe ya kwamba majira ya mavuno yamekwisha kuwa karibu. Nanyi kadhalika, mwonapo mambo hayo yanaanza kutokea, tambueni ya kwamba ufalme wa Mungu u karibu.” Luka 21:28, 30, 31. [GC 308.2; PK Aya ya 30]

Lakini jinsi ile roho ya unyenyekevu na ya uchaji ndani ya kanisa ilivyozidi kutoweka na kutoa nafasi ya kiburi, ibada ya mapokeo, upendo kwa Kristo na imani katika kurejea Kwake vilikuwa vimepoa. Wakiwa wamemezwa na kuipenda dunia na kutafuta anasa, wale waliodai kuwa watu wa Mungu walipofushwa hata wakashindwa kukumbuka maagizo ya Mwokozi kuhusu ishara za ujio Wake. Fundisho la ujio wa pili lilikuwa limepuuzwa; Mafundisho yanayolihusu yalifichwa na tafsiri zao potovu, mpaka likapuuzwa kwa kiasi kikubwa na hatimaye kusahauliwa. Jambo hilo hasa lilitokea katika makanisa yale ya Amerika. Uhuru na raha zinazofurahiwa na tabaka zote za jamii ile, tamaa yao kuu ya kujipatia mali na kuishi maisha ya anasa, ilikuwa ndiyo matokeo ya kuwafanya watumie muda wao mwingi katika kujipatia fedha, kukimbilia kutafuta umaarufu na madaraka, jambo ambalo lilionekana kufikiwa na watu wote kwa urahisi, na kuwafanya watu kuweka umakini wao katika mambo ya dunia hii wanayoyachangamkia, maslahi na matumaini yao katika mambo ya maisha haya, na kuisukuma katika wakati ujao, siku ile adhimu ya kutisha wakati mambo ya wakati huu yatakapokuwa yamepita na kutoweka. [GC 309.1; PK Aya ya 31]

Wakati Mwokozi alipowaonyesha wafuasi Wake ishara za kurudi Kwake, alitabiri hali ya kurudi nyuma ambayo ingekuwepo kabla tu ya ujio Wake wa pili. Kungekuwa, kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, shuguli, na pilikapilika za biashara za mambo ya kidunia na kutafuta anasa,---kununua, kuuza, kupanda, kujenga, kuoa na kuolewa, -- pamoja na kumsahau Mungu na maisha ya wakati ujao. Kwa wale watakaoishi wakati huu, maonyo na maelekezo ya Kristo ni haya: “Basi, jiangalieni, mioyo yenu isije ikalemewa na ulafi, na ulevi, na masumbufu ya maisha haya; siku ile ikawajia ghafula, kama mtego unasavyo.” “Basi, kesheni

ninyi kila wakati, mkiomba, ili mpate kuokoka katika haya yote yatakayotokea, na kusimama mbele za Mwana wa Adamu.” Luka 21:34, 36. [GC 309.2; PK Aya ya 32]

Hali ya kanisa kwa wakati huu imeelezwa katika Maneno ya Mwokozi katika Ufunuo: “Una jina la kuwa hai, nawe umekufa." Na kwa wale wanaokataa kuamka kutoka usingizi wa usalama wa kufikirika, onyo zito linaelekezwa kwao: “Walakini usipokesha, nitakuja kama mwivi, wala hutaijua saa nitakayokuja kwako.” Ufunuo 3:1, 3. [GC 309.3; PK Aya ya 33]

Ilikuwa ni muhimu kwamba watu waamshwe na kujulishwa hatari inayowakabili; waamshwe ili wajiandae kukabiliana na matukio mazito yanayohusiana na kufungwa kwa mlango wa rehema. Nabii wa Mungu anatangaza hivi: “Kwa kuwa siku ya Bwana ni kuu, yenye kitisho sana; Naye ni nani awezaye kuistahimili?” Ni nani atakayesimama atakapotokea Yeye aliye “Mwenye macho safi hata asiweze kuangalia uovu,” na hawezi “kutazama ukaidi”? Yoeli 2:11; Habakuki 1:13. Kwa wale watu Wangu waliao, watalia “Mungu wangu, sisi Israeli tunakujua,” lakini wamelihalifu agano Langu, wameiasi sheria Y, wameharakisha kumfuata mungu mwingine, huku wakiwa wameficha uovu mioyoni mwao na wakipenda njia za uasi--, kwa watu hawa siku ya Bwana ni “giza, wala si nuru, naam, yenye giza sana, wala haina mwanga.” Hosea 8:2, 1; Zaburi 16:4; Amosi 5:20. “Kisha itakuwa wakati ule, asema Bwana, nitauchunguza Yerusalemu kwa taa; Nami nitawaadhibu watu walioganda juu ya sira zao; wasemao katika mioyo yao, Bwana hatatenda mema, wala hatatenda mabaya.” Sefania 1:12. “Nami nitaadhibu ulimwengu kwa sababu ya ubaya wake, na wenye dhambi kwa sababu ya hatia yao; Nami nitaikomesha fahari yao wenye kiburi; Nami nitayaangusha chini majivuno yao walio wakali.” Isaya 13:11. “Fedha yao wala dhahabu yao havitaweza kuwaokoa;” “Na huko utajiri wao utakuwa mateka, na nyumba zao zitakuwa ukiwa.” Sefania 1:18, 13. [GC 310.1; PK Aya ya 34]

**Wito Wa Kuamka**

Nabii Yeremia, akiangalia mbele wakati huo wenye kuogopesha, alisema hivi: “Naumwa katika moyo wangu wa ndani……Siwezi kunyamaza, kwa sababu umesikia, Ee nafsi yangu, sauti ya tarumbeta, mshindo wa vita. Uangamivu baada ya uangamivu umetangazwa.” Yeremia 4:19, 20. [GC 310.2; PK Aya ya 35]

“Siku ile ni siku ya ghadhabu, Siku ya fadhaa na dhiki, Siku ya uharibifu na ukiwa, Siku ya giza na utusitusi, Siku ya mawingu na giza kuu, Siku ya tarumbeta na ya kamsa.”Sefania 1:15, 16. “Tazama, siku ya Bwana inakuja, ...ili iifanye nchi kuwa ukiwa, na kuwaharibu watu wake, wenye dhambi, wasikae ndani yake.” Isaya 13:9. [GC 310.3; PK Aya ya 36]

Kwa kuzingatia siku hiyo kuu Neno la Mungu, katika lugha makini na yenye mguso, anatoa wito kwa watu Wake waamke kutoka katika ulegevu wao wa kiroho na kuutafuta uso Wake kwa toba na unyenyekevu: "Pigeni tarumbeta katika Sayuni, Pigeni na kelele katika mlima Wangu mtakatifu; Wenyeji wote wa nchi na watetemeke; Kwa maana siku ya Bwana inakuja. Kwa sababu inakaribia." Takaseni saumu, kusanyeni kusanyiko kuu; Kusanyeni watu, litakaseni kusanyiko, Kusanyeni wazee, kusanyeni watoto: ...Bwana arusi na atoke chumbani mwake, Na bibi arusi katika hema yake. Hao makuhani, wahudumu wa Bwana, na walie Kati ya Patakatifu na madhabahu." "Nirudieni Mimi kwa mioyo yenu yote, na kwa kufunga, na kwa kulia, na kwa kuombolea; rarueni mioyo yenu, wala si mavazi yenu, mkamrudie Bwana, Mungu wenu; kwa maana Yeye Ndiye Mwenye neema, amejaa huruma; si mwepesi wa hasira, ni mwingi wa rehema." Yoeli 2:1, 15-17, 12, 13. [GC 311.1; PK Aya ya 37]

Ili kuwaandaa watu kusimama katika siku ya Mungu, kazi kubwa ya matengenezo inapaswa kufanyika. Mungu aliona kwamba wengi wa wale wanaodai kuwa watu Wake walikuwa hawajengi kwa ajili ya umilele na kwa rehema Zake alikuwa karibu kutuma ujumbe wa onyo ili kuwaamsha kutoka katika usingizi wao unaowazubaisha na kuwaongoza katika maandalizi ya kuja kwa Bwana. [GC 311.2; PK Aya ya 38]

Onyo hili limetolewa katika Ufunuo 14. Hapa kuna ujumbe wenye sehemu tatu unaowakilishwa na kutangazwa na viumbe wale wa mbinguni na kufuatiwa kwa haraka na ujio wa Mwana wa Adamu kukusanya "mavuno ya nchi." La kwanza katika maonyo haya linatangaza hukumu inayokaribia. Nabii huyo alimwona malaika akiruka "Kisha nikaona malaika mwingine, akiruka katikati ya mbingu, mwenye Injili ya milele, awahubiri hao wakaao juu ya nchi, na kila taifa na kabila na lugha na jamaa, akasema kwa sauti kuu, Mcheni Mungu, na kumtukuza, kwa maana saa ya hukumu Yake imekuja. Msujudieni Yeye aliyezifanya mbingu na nchi na bahari na chemchemi za maji." Ufunuo 14:6, 7. [GC 311.3; PK Aya ya 39]

Ujumbe huu unatangazwa kuwa ni sehemu ya "injili ya milele." Kazi ya kuihubiri injili haijakabidhiwa kwa malaika, bali imewekwa kama dhamana kwa wanadamu. Malaika watakatifu wamekwa ili kuiongoza kazi hii, wanasimamia harakati zote kubwa kwa ajili ya wokovu wa wanadamu; lakini utangazaji halisi wa injili, hufanywa na watumishi Wake Kristo duniani. [GC 312.1; PK Aya ya 40]

Watu waaminifu, ambao walikuwa wanatii misukumo ya Roho wa Mungu na mafundisho ya Neno Lake, walipaswa kutangaza onyo hili kwa ulimwengu. Walikuwa ni wale waliokuwa wamelisikia na kulizingatia "Neno la unabii lililo imara zaidi," ambalo ni "taa ing'aayo mahali penye giza, mpaka kutakapopambazuka, na nyota ya asubuhi kuzuka." 2 Petro 1: 19. Walikuwa wakitafuta ujuzi wa Mungu zaidi ya hazina zote zilizositirika, wakiamini kwamba

kumjua Mungu ni "bora kuliko biashara ya fedha, Na faida yake ni nyingi kuliko dhahabu safi." Mithali 3:14. Na Bwana aliwafunulia mambo makuu ya ufalme. "Siri ya Bwana iko kwao wamchao, Naye atawajulisha Agano Lake." Zaburi 25:14. [GC 312.2; PK Aya ya 41]

**Ujumbe Uliotangazwa Na Watu Waliokuwa Duni Zaidi**

Sio wanatheolojia wasomi ambao walikuwa na ufahamu wa Ukweli huu na ambao walishiriki katika utangazaji wake. Endapo watu hawa wangekuwa walinzi waaminifu, na wenye kukesha, wakiyachunguza Maandiko kwa bidii kubwa na kwa maombi mengi; unabii huu ungekuwa umewafunulia matukio yale yaliyokuwa karibu kutokea. Lakini hawakuchangamkia fursa hiyo, na ujumbe ule ukatolewa na watu kawaida na wanyenyekevu. Yesu alisema: "Enendeni maadamu mnayo nuru hiyo, giza lisije likawaweza maana aendaye gizani hajui aendako." Yohana 12:35. Wale wanaogeuka na kuipa kisogo nuru hiyo ambayo Mungu amewapa au wanaopuuza kuitafuta wakati inapatikana karibu na wao, huachwa gizani. Lakini Mwokozi wetu anatangaza: "Yeye anifuataye hatakwenda gizani kamwe, bali atakuwa na nuru ya uzima." Yohana 8:12. Yeyote aliye na kusudi moja tu, la dhati na nyofu kutaka kufanya mapenzi ya Mungu, akiifuata kwa bidii nuru ambayo tayari imetolewa kwake, huyo atapokea nuru kubwa zaidi; na kwa mtu kama huyo, nyota yenye nuru ya mbinguni itatumwa kumwongoza katika Ukweli wote. [GC 312.3; PK Aya ya 42]

Wakati ule wa ujio wa kwanza wa Kristo makuhani na waandishi wa Mji Mtakatifu, ambao walikabidhiwa dhamana ya maagizo ya Mungu, wangeweza kutambua dalili za nyakati na kutangaza ujio Wake Yule Aliyeahidiwa. Unabii wa Mika ulitangaza mahali halisi ambapo angezaliwa; Danieli alisema wakati mahsusi wa ujio Wake. Mika 5:2; Danieli 9:25. Mungu aliwakabidhi unabii huu kwa viongozi wa Kiyahudi; hawakuwa na udhuru wa kutojua na kutangaza kwa watu kwamba ujio wa Masihi ulikuwa umekaribia. Kutojua kwao kulikuwa matokeo ya dhambi ya kupuuzia. Wayahudi walikuwa wakijenga minara mikubwa ya makaburi kwa ajili ya kumbukumbu ya manabii wa Mungu waliouawa, wasijue kwamba katika kujishugulisha kutoa heshima yao kwa watu mashuhuri wa dunia walikuwa wakitoa heshima kwa watumishi wa Shetani. Wakiwa wamezama katika mapambano na tamaa zao kwa ajili ya vyeo na mamlaka miongoni mwa watu, walishindwa kabisa kutambua fadhila na heshima bora sana walizopewa na Mfalme Yule wa mbinguni. [GC 313.1; PK Aya ya 43]

Kwa shauku kubwa na kicho, wale wazee wa Israeli walipaswa kujifunza na kuelewa habari zilizohusu mahali, wakati, na muktadha wa tukio kuu kabisa katika historia ya ulimwengu huu—Ujio wa Mwana wa Mungu kukamilisha ukombozi wa mwanadamu. Watu wote walipaswa kukesha na kungojea ili wawe miongoni mwa watu wa kwanza kumpokea Mkombozi wa ulimwengu. Lakini,

kumbe, pale Bethlehemu wasafiri wawili waliochoka kutoka katika vilima vya Nazareti walitembea umbali wote wa barabara nyembamba hadi mwisho wa mashariki ya mji, wakitafuta bila mafanikio mahali pa kupumzika na mahali pa kujihifadhi wakati wa usiku. Hakuna milango iliyokuwa imefunguliwa, tayari kuwapokea. Hatimaye walipata hifadhi katika banda bovu lililojengwa kwa ajili ya ng'ombe, katika hili kimbilio, ndiyo mahali ambapo Mwokozi wa ulimwengu alizaliwa humo. [GC 313.2; PK Aya ya 44]

**Habari Njema**

Malaika wa mbinguni walikuwa wameuona utukufu ambao Mwana wa Mungu alishiriki pamoja na Baba kabla ya ulimwengu kuwepo na walikuwa wamengojea kwa hamu kubwa kuonekana Kwake duniani kuwa liwe tukio ambalo lingeleta furaha kubwa zaidi kwa watu wote. Malaika walichaguliwa rasmi, kupeleka habari njema za furaha kwa wale waliokuwa tayari kuzipokea na ambao wangeitangaza kwa furaha wangeitangaza kwa wakazi wa dunia. Kristo alikuwa amejishusha kuchukua juu Yake asili ya mwanadamu; Alitarajiwa kubeba uzito usio na kipimo wa huzuni  na taabu (ole) kwa kutoa nafsi Yake kuwa dhabihu kwa ajili ya dhambi; lakini malaika walitamani hata katika unyenyekevu Wake, Mwana Yeye Aliye Juu zaidi kuliko wote, apate kutokea mbele ya watu akiwa na angalau heshima na utukufu unaolingana na hadhi Yake. Je, watu wakuu wa dunia wangekusanyika katika mji mkuu wa Israeli kukaribisha ujio Wake? Je, majeshi ya malaika yangemtambulisha kwa umati mkubwa wa watu waliomtarajia kwa shauku kubwa? [GC 313.3; PK Aya ya 45]

Malaika mmoja aliizuru dunia ili kuona ni akina nani waliojiandaa tayari kumkaribisha Yesu. Lakini hakuweza kuona dalili zozote za maandalizi ya kumpokea. Hakusikia sauti yoyote ya sifa na shangwe iliyoonyesha kwamba kipindi cha kuja kwa Masihi kimekaribia. Malaika anaambaa hewani kwa muda juu ya mji ule uliochaguliwa na katika hekalu ambapo uwepo mtakatifu wa Mungu ulikuwa ukidhihirika kwa zama nyingi. Lakini hata kwenye mji huu kuna Kutojali kule kule. Makuhani, katika fahari na majivuno yao, walikuwa wakitoa dhabihu zilizo najisi hekaluni. Mafarisayo walikuwa wakiwahutubia watu kwa sauti kubwa au kufanya sala za majigambo katika kona za mitaa. Katika ikulu za wafalme, katika mikusanyiko ya wanafalsafa, katika shule za marabi, wote kwa pamoja hawakuwa na wazo lolote kuhusu Ukweli wa ajabu ambao ulikuwa umeijaza mbingu yote kwa furaha na sifa-- kwamba Mkombozi wa wanadamu alikuwa karibu kutokea duniani. [GC 314.1; PK Aya ya 46]

Hakukuwa na ushahidi wowote unaonyesha kwamba Kristo alitarajiwa kutokea, hakukuwa na  matayarisho kwa ajili ya huyo Mkuu wa uzima. Kwa mshangao, mjumbe wa mbinguni alikuwa karibu kurudi mbinguni akiwa na taarifa mbaya na yenye aibu, ndipo anagundua kundi la wachungaji waliokuwa

wakichunga makundi ya mifugo yao usiku na hao walipokuwa wanaangaza macho yao katika mbingu yenye nyota, wakiutafakari unabii wa Masihi aliyetarajiwa kuja duniani na wakitamani ujio wa Mkombozi wa ulimwengu. Hapa palikuwa na kikundi kilichojiandaa tayari kupokea ujumbe wa mbinguni. Na kwa ghafla malaika wa Bwana aliwatokea, akitangaza habari njema yenye furaha kuu. Utukufu wa mbinguni ulifurika pande zote za uwanda, kundi la malaika wasioweza kuhesabika lilifunuliwa, kana kwamba furaha ile ilikuwa kubwa mno kwao kiasi kwamba malaika mmoja hakutosha kuleta ujumbe mzito kama huo kutoka mbinguni, sauti nyingi zinapasuka na kuwa wimbo wa sifa kwa Mungu, ambao mataifa yote ya waliookolewa watauimba siku moja "Atukuzwe Mungu juu mbinguni, Na duniani iwe amani kwa watu aliowaridhia." Luka 2:14. [GC 314.2; PK Aya ya 47]

Loo! Kisa hiki cha ajabu kilichotokea kule Bethlehemu! Hili ni somo la ajabu kiasi gani. Ni kwa uzito kiasi gani jambo hili hukemea kukosa imani kwetu, kiburi chetu, na kujitosheleza kwetu. Kisa hiki kinatuonya sisi kwa umakini kujihadhari na kukesha, isije ikawa kwa kupuuzia kwetu, ambako ni uhalifu mkubwa, tushindwe kuzitambua dalili za nyakati kwa makosa yetu na kwa hivyo tushindwe kujua siku ya kujiliwa kwetu. [GC 315.1; PK Aya ya 48]

Haikuwa tu juu ya milima Yuda pekee, sio tu miongoni mwa wachungaji wa hali ya chini peke yao, ambapo malaika waliwakuta wakeshaji waliosubiri ujio Wake Masihi. Katika nchi za kipagani, pia walikuwepo watu waliomtazamia kwamba atakuja; walikuwa ni watu wenye hekima, matajiri, waungwana, wakuu, na wanafalsafa wa Mashariki. Wakiwa wanafunzi wa maumbile na vitu vya asili, Mamajusi walikuwa wamemwona Mungu katika kazi za mikono Yake. Kutoka katika Maandiko ya Kiebrania walikuwa wamejifunza kwamba Nyota itatokea katika Yakobo (Hes 24:17) na kwa hamu kubwa walingojea ujio Wake, Yeye ambaye angekuwa siyo tu "Faraja ya Israeli," bali pia "Nuru ya kuwa mwangazia Mataifa," na "kwa ajili ya wokovu wa miisho ya dunia." Luka 2:25, 32; Matendo 13:47. Walikuwa watafutaji wa nuru, na nuru kutoka kwenye kiti cha enzi cha Mungu iliwaangazia njia kwa ajili ya nyayo zao. Wakati makuhani na marabi wa Yerusalemu, yaani wale watunzaji na wafafanuzi wa Ukweli, waliochaguliwa na Mungu, walikuwa wamegubikwa katika giza, nyota iliyotumwa kutoka Mbinguni iliwaongoza wageni hawa waliotoka katika mataifa ya nje ya Uyahudi hadi kufika mahali ambapo mtoto huyu mchanga, aliye Mfalme, ndiyo tu alikuwa amezaliwa. [GC 315.2; PK Aya ya 48]

**Ni Kwa Hao Wamtazamia**

Ni "kwa wale wamtazamiao" ndiyo Kristo "atatokea mara ya pili, pasipo dhambi, kwa hao wamtazamiao kwa wokovu." Waebrania 9:28. Kama vile habari za kuzaliwa kwa Mwokozi zilivyokuwa, ujumbe wa ujio Wake wa mara ya pili

haujakabidhiwa mikononi mwa viongozi wa dini wanaowaongoza watu. Walikuwa wameshindwa kudumisha uhusiano wao na Mungu na walikuwa wamekataa nuru ile iliyotoka mbinguni; kwa hiyo hawakuwemo miongoni mwa ile hesabu iliyoelezwa na mtume Paulo: "Bali ninyi, ndugu, hammo gizani, hata siku ile iwapate kama mwivi. Kwa kuwa ninyi nyote mmekuwa wana wa nuru, na wana wa mchana; sisi si wa usiku, wala wa giza." 1 Wathesalonike 5:4, 5. [GC 315.3; PK Aya ya 49]

**Watu Wamelala Usingizi**

Walinzi walio juu ya kuta za Sayuni walipaswa kuwa wa kwanza kupata habari za ujio Wake Mwokozi, wangekuwa wa kwanza kuinua sauti zao na kutangaza ukaribu Wake, wangekuwa wa kwanza kuwaonya watu wajiandae kwa ajili ya Ujio Wake. Lakini walikuwa wamestarehe na kujiziuka, wakiota ndoto za amani na usalama, huku wakiwa wamelala usingizi katika dhambi zao. Yesu aliliona kanisa Lake, kama mtini usiozaa matunda, ukiwa umejaa majani ya udanganyifu, lakini bila matunda ya thamani. Palikuwa na kujigamba kwingi kwamba wao wanazingatia mifumo yote ya kidini, wakati roho ya unyenyekevu, toba, na imani ya Kweli - mambo pekee ambayo yangeweza kuifanya ibada na huduma yao ipate kukubalika kwa Mungu - vilikosekana. Badala ya neema za Roho kilionekana kiburi, kushikilia taratibu zinazojirudia-rudia za kidini, mapokeo ya kale, kujigamba bure, ubinafsi, na ukandamizaji. Kanisa lililokuwa likirudi nyuma lilifumba macho yake lisizione dalili za nyakati. Mungu hakuwaacha, wala kuruhusu watu Wake waaminifu washindwe; lakini wao walimwacha, na kujitenga mbali na upendo Wake. Kwa kukataa kutii masharti, ahadi Zake Mungu kwao hazikutimizwa. [GC 315.4; PK Aya ya 50]

Hayo ndiyo matokeo ya hakika ya kutojali, kutothamini na kutoiboresha nuru na fursa atoazo Mungu. Kanisa lisipofuatilia milango ya uongozi Wake Mungu inayofunguliwa au kufungwa kwao, lisipoukubali kila mwale wa nuru, lisipotekeleza kila jukumu linaloweza kufunuliwa kwao, basi, dini yao bila shaka itadidimia hadhi yake na kurudi katika uadhimishaji tu wa taratibu za dini (mapokeo), kisha ile roho ya uchaji wa kweli itatoweka. Ukweli huo umerudiwa tena na tena kuelezwa kwa mifano katika historia ya kanisa. Mungu anataka kutoka kwa watu Wake kazi na matendo yatokanayo na imani na utii unaolingana na mibaraka na fursa Zake alizozitoa (upendeleo Wake). Utii unahitaji kafara na unahusisha kubeba msalaba; hii ndiyo sababu watu wengi mno miongoni mwa wale wanaojiita wafuasi Wake Kristo walikataa kuipokea ile nuru iliyotoka mbinguni, tena, kama ilivyokuwa kwa Wayahudi wa zamani, hawakujua majira ya kujiliwa kwao. Luka 19:44. Kwa sababu ya kiburi chao na kutokuamini kwao, Bwana aliwapita kando yao na kufunua Ukweli Wake kwa wale ambao, kama wachungaji wale wa kondoo wa Bethlehemu na Mamajusi wa Mashariki, walikuwa

wameitii/wameizingatia nuru yote waliyokuwa wameipokea. [GC 316.1; PK Aya ya 51]

# SURA YA 18

# NURU MPYA KATIKA ULIMWENGU MPYA

## (Mwanamatengenezo Wa Marekani Afungua Unabii)

Ufupisho: Ni nini kitatokea wakati watu wanaamua kuyafungua Maandiko Matakatifu na kuanza kujifunza kwa uangalifu kwa miaka kadhaa? Kuna nguvu na utajiri katika Neno la Mungu na unabii ulioandikwa humo, utayabadilisha maisha yako hakika. Biblia iliyofunguliwa ndiyo chanzo na msingi wa matengenezo na uamsho katika kila kizazi kilichoishi hapa duniani. Biblia si kitabu cha habari tu, bali ni kitabu kinachobadilisha maisha yetu na kututayarisha kuishi mbinguni, Yn 17:3 (The Bible is not the book of information, but transformation). William Miller aliishi kutoka mwaka 1782-1849 kule Massachusets, Marekani.

Mkulima mwadilifu, mwenye moyo mnyofu, ambaye alikuwa ameongozwa kutilia mashaka mamlaka ya Mungu iliyomo katika Maandiko, lakini ambaye kwa dhati alitamani sana kuujua Ukweli, alikuwa ndiye mtu aliyechaguliwa na Mungu kwa njia ya pekee ili kuongoza katika kutangaza habari ya kuja kwa Kristo mara

ya pili. Kama wanamatengenezo wengine wengi, William Miller katika maisha yake ya awali alikuwa amepambana na umaskini na hivyo alikuwa amejifunza masomo makubwa ya kufanya kazi kwa bidii na kujikana nafsi. Watu waliozaliwa katika familia ambayo alitoka, walikuwa na sifa ya kupenda kujitegemea, roho ya kupenda uhuru, uwezo wa kustahimili, na uzalendo wa hali ya juu—Sifa ambazo pia zilikuwa zimejulikana katika maisha yake. Baba yake alikuwa Kapteni katika jeshi la Mapinduzi lilopigana kwa ajili ya uhuru wa nchi ya Marekani, na kwa kujitolea mhanga kwake katika mapambano na mateso ya kipindi kile cha dhoruba kuliweza kuonekana katika mazingira yale magumu ya maisha ya Miller ya awali. [GC 317.1; PK Aya ya 1]

Alikuwa na mwili wenye afya njema, na hata katika utoto wake alionyesha uwezo wake wa nguvu za akili zisizokuwa za kawaida. Kadiri alivyoendelea kukua, jambo hilo lilizidi kujionyesha dhahiri. Akili yake ilikuwa kazini na ilikuwa mahiri, na alikuwa na kiu kikubwa cha kupata maarifa. Ingawa hakupata fursa ya kunufaika na elimu ya chuo kikuu, kupenda kwake kusoma na tabia ya kutafakari kwa makini na uchambuzi wa mambo kwa kina, ikiwemo na ukosoaji unaofaa kulimfanya awe mtu wa maamuzi mazuri na mawazo mapana. Alikuwa na tabia njema kimaadili, isiyo na lawama na sifa ya kutamanika, akiheshimiwa kwa ujumla kwa uadilifu, uangalifu wake wa kutumia mali, na ukarimu. Kwasababu ya bidii yake katika kazi za mikono, aliweza kubobea mapema stadi za maisha, ingawa tabia zake za kujifunza bado ziliendelea kudumishwa. Alifanya kazi katika nyadhifa mbalimbali za kiraia na za kijeshi, kwa mafanikio na kusifiwa, mifereji ya kujipatia mali na heshima ilifunguliwa kwake. [GC 317.2; PK Aya ya 2]

Mama yake alikuwa ni mwanamke mcha Mungu haswa, hivyo Miller alipata mivuto ya kidini chini ya mamaye utotoni mwake. Katika miaka ya mwanzoni mwa utu uzima wake, alitupwa katika jamii ya watu ambao walikuwa wakiamini Mungu Yupo, lakini walikataa ushugulikaji wa Mungu na viumbe vyake baada ya Uumbaji (imani ya Deist),* ambao ushawishi wao ulikuwa na nguvu nyingi zaidi kwake kutokana na ukweli kwamba walikuwa ni raia wema sana, na watu wenye tabia yenye utu, huruma, mwelekeo wa ukarimu na fadhila. Wakiishi, kama vile walivyoishi, katikati ya taasisi na mazingira ya Kikristo, tabia zao kwa kiwango fulani zilikuwa zimefanana na mazingira yao. Uzuri wao uliowapatia heshima na imani kwa watu, ulitokana na Biblia (bila ya wao kujua); na bado vipawa vile vizuri vilitumiwa vibaya sana kiasi cha kuweza kutoa ushawishi wake wenye nguvu dhidi ya Neno la Mungu. Kwa kushirikiana na watu hawa, Miller alishawishiwa kuiga fikra zao. Tafsiri za Maandiko zilizokuwapo wakati ule zilileta matatizo yaliyoonekana kwake kuwa ni makubwa sana; lakini imani yake ile mpya, japo ilikuwa inaiweka Biblia kando, haikutoa chochote kilicho bora kuchukua mahali pake, kwani hakuweza kuridhika kabisa moyoni mwake. Hata hivyo aliendelea kuyashikilia maoni haya kwa miaka kumi na miwili takribani.

Lakini alipofikia umri wa miaka thelathini na minne, Roho Mtakatifu aliugusa moyo wake na kumpa hisia ya kuielewa hali yake kama mtu mwenye dhambi. Katika imani yake ile ya kwanza ya Deist,* ambayo haikumpa uhakika wowote wa furaha ng'ambo ya kaburi. Mambo ya wakati ujao kwake yakaonekana kuwa giza na huzuni tu. Miaka ya baadaye alipotafakari hisia alizokuwa nazo kwa wakati ule, alisema: [GC 318.1; PK Aya ya 3]

"Kuangamia au kupotea milele lilikuwa ni wazo linaloleta ubaridi wa hofu mwilini, udhaifu na kufa moyo, na uwajibikaji ungekuwa uharibifu kwa wote. Mbingu zilikuwa kama shaba juu ya kichwa changu, na dunia kama chuma chini ya miguu yangu. Umilele - maana yake ni nini? Na kifo - kwa nini kilikuwapo? Kwa kadiri nilivyozidi kutafakari zaidi na kutafuta sababu ndivyo nilivyozidi kukaa katika nchi ya kufikirika. Nilivyozidi kufikiria zaidi ndivyo mahitimisho yangu yalivyozidi kusambaratika zaidi. Nikajaribu kuacha kufikiria, lakini mawazo yangu hayakuweza kutawaliwa, nilikuwa wa kusikitikiwa kweli, ila mimi sikujua chanzo chake ni nini. Nilinung'unika na kulalamika, lakini sikujua nilimnung'unikia au kumlalamikia nani? Nilijua kwamba palikuwa na mambo ambayo siyo sahihi, lakini sikujua kwa jinsi gani au wapi ninaweza kupata jambo lililo sahihi. Niliomboleza, bila kuwa na tumaini." [GC 318.2; PK Aya ya 4]

**Miller Ampata Rafiki**

Aliendelea kuwa katika hali ile kwa miezi kadhaa. "Ghafula," alisema yeye, "tabia ya Mwokozi ilifunuliwa waziwazi akilini mwangu. Ilionekana kana kwamba ni lazima kutakuwa na Mwenye uhai Mmoja aliyekuwa Mwema na Mwenye huruma nyingi kiasi cha Yeye Mwenyewe kuweza kujipatanisha kwa ajili ya makosa yetu (kulipa fidia ya dhambi zetu), na kwa njia hiyo kutuokoa sisi toka katika mateso na adhabu ya dhambi zetu. Kwa ghalfa nilihisi jinsi huyo Mwenye uhai alivyokuwa mwema sana, tena niliwaza kwamba mimi mwenyewe ningeweza kujitupa mikononi Mwake huyo na kutumainia rehema Zake. Lakini swali lilizuka, Yawezekanaje kuthibitisha kama nafsi ya namna hiyo au huyo Mmoja Yupo? Kando ya Biblia niliona kwamba sikuweza kupata ushahidi wowote wa uwepo Wake Mwokozi kama huyo, au hata uwepo wa hali njema ya wakati ujao...[GC 319.1; PK Aya ya 5]

"Niliona kwamba Biblia ikichora picha ya Mwokozi ambaye nilimhitaji mbele yangu; nami nikafadhaika kwa utata, kwamba kwa jinsi gani basi kitabu kisichovuviwa na pumzi ya Mungu kiweze kujenga kanuni zinazokidhi kikamilifu mahitaji ya ulimwengu ulioanguka dhambini? Nililazimika kukubali kwamba Maandiko lazima yawe ni ufunuo kutoka kwa Mungu. Maandiko yakaja kuwa chanzo cha furaha yangu; na ndani ya Yesu nilimpata rafiki. Mwokozi akaja kuwa kwangu mkuu na bora miongoni mwa kumi elfu, na Maandiko ya Biblia, ambayo zamani yalikuwa giza kwangu na yanayokinzana yenyewe, sasa yalikuwa taa ya

miguu yangu na mwanga wa njia yangu. Moyo wangu ukatulia na kutosheka/kuridhika. Nikamwona Bwana Mungu kuwa ni Mwamba katikati ya bahari ya maisha. Biblia sasa ikawa ndiyo somo langu kuu la kujifunza, nami naweza kusema kwa hakika kwamba nilikichunguza kwa furaha kubwa. Hatimaye nikagundua kwamba nusu yake ilikuwa haijapata kusimuliwa kwangu kamwe. Nilistaajabu na kujiuliza kwa nini sikuwa nimeuona uzuri na utukufu wake kabla ya wakati huo, nami nilishangaa sana kwamba kwanini hata mimi nilijaribiwa kuikataa. Niligundua kuwa kila kitu ambacho moyo wangu ulikitamani kilikuwa kimefunuliwa humo, na tiba kwa kila ugonjwa wa moyo ilipatikana humo. Nilipoteza ladha ya kusoma vitabu au mandishi mengine, na kuuelekeza moyo wangu kujipatia hekima itokayo kwa Mungu." - S. Bliss, Kumbukumbu za William Miller (Memoirs of Wm Miller), ukurasa wa 65-67. [GC 319.2; PK Aya ya 6]

Miller alikiri imani yake hadharani katika dini ile aliyokuwa ameidharau na kuidhihaki. Lakini rafiki zake makafiri hawazubaa katika kuleta mbele yake hoja zote ambazo yeye mwenyewe mara nyingi alikuwa akizitumia dhidi ya mamlaka ya Mungu katika Maandiko. Wakati huo hakuwa tayari kuzijibu; lakini alieleza kwamba ikiwa Biblia ni ufunuo utokao kwa Mungu, basi, ni lazima isijipinge, yaani lazima ipatane na yenyewe; na ya kwamba kwa kuwa ilitolewa kwa mafundisho kwa ajili ya mwanadamu, basi, ni lazima iendane kwa kadri ya uelewa wake. Alidhamiria kujifunza Maandiko yeye mwenyewe na kujiridhisha ikiwa kila kupingana kunaodhaniwa kuwepo, kunaweza kusuluhishwa na kuwa na upatanifu. [GC 319.3; PK Aya ya 7]

**Ufahamu Wake Unakuwa Safi**

Alijitahidi kuweka kando maoni yote potovu aliyokuwa nayo siku za nyuma, akiacha pembeni vitabu au magombo ya ufafanuzi wa Biblia (Biblia Commentaries) akalinganisha Maandiko na Maandiko kwa msaada wa mafungu ya rejea yaliyo pembeni mwa kurasa za Biblia yaani pambizo na kwa kutumia kitabu chenye orodha ya maneno yaliyo mengi na yaliyopangiliwa kialfabeti katika Biblia (concordance). Alipanga uchunguzi wake wa kujifunza Biblia kwa njia ya kudumu, yaani kwa kupanga muda maalumu kila siku na kwa kutumia mfumo au mbinu iliyojengwa juu ya utaratibu maalum hivyo alipanga kuisoma Biblia kwa muda maalumu ule ule;* alianza kusoma kitabu cha Mwanzo, na alisoma fungu kwa fungu, na hakuendelea kwa kasi zaidi kuliko uwezo wake wa kuelewa maana ya vifungu hivyo kadhaa vilivyofunuliwa na kueleweka kwake ili kumwondolea dukuduku moyoni, pamoja na aibu yote (ambayo ingeweza kumpata kutoka kwa marafiki, au wanaopinga Neno). Alipogundua fungu lolote lililokuwa na giza kwa kutolielewa kwake, ilikuwa ni desturi yake kulilinganisha na kila fungu jingine lililoonekana linarejelewa au kugusiwa kwa njia yoyote na jambo lililokuwa linafikiriwa na kuchunguzwa kwa muktadha ule. Kila neno liliruhusiwa kuwa na

uzito wake unaostahili kuchangia katika somo la kufafanua fungu lile, na ikiwa wazo la hilo fungu liliafikia na kila kifungu kilichoongelea jambo lile lile, basi, kwake tatizo lile lilikuwa limekoma kuwa na ugumu tena. Hivyo kila alipokutana na fungu lililokuwa gumu kwake kulielewa alipata maelezo yake katika sehemu nyingine ya Maandiko. Alipokuwa akiendelea kujifunza kwa bidii na maombi ya dhati ili kuangaziwa na nuru kutoka kwa Bwana, kile kilichoonekana kwake kuwa ni giza katika ufahamu wake mwanzoni, kikawa kinaeleweka wazi vizuri kabisa. Akauonja uzoefu wa Ukweli wa maneno haya ya Mwandishi wa Zaburi:" kufafanusha Maneno Yako kwatia nuru, na kumfahamisha mjinga.Zaburi 119:130 *(regular, and methodically). [GC 320.1; PK Aya ya 8]

Kwa hamu kubwa sana alijifunza vitabu vya Danieli na Ufunuo, akizitumia kanuni zile zile za kutafsiri alizozitumia kwa Maandiko mengineyo, na, kwa furaha kubwa aligundua kwamba mifano ya kiunabii iliyotumika iliweza kueleweka. Aliona kwamba sehemu mbalimbali za unabii, zilikuwa zimetimizwa, katika ulimwengu unaoonekana, Neno kwa Neno (hakikisho halisi kabisa); kwamba matumizi ya vielelezo vyote mbalimbali, maneno au mafumbo, sitiari, visa kwa njia ya vielelezo, mahesabu au michoro mbalimbali, hadithi zenye mafundisho, mifano, nk, mambo hayo yaliweza kufanunuliwa kwa kulinganisha muktadha ulio karibu, yaani maneno yale yaliyokuwa karibu sana na hayo, au maneno ya ile lugha ya mafumbo yaliyotumika kuelezea yalikuwa yamefafanuliwa katika Maandiko mengine, na ikiwa yalifasiliwa hivyo katika sehemu zingine za maandiko na kufafanuliwa hivyo, basi yalipaswa kueleweka moja kwa moja kwa maana yake halisi kama yalivyo. "Hivyo kwa njia hiyo mimi niliridhika," alisema, "Biblia ni mfumo wa Ukweli uliofunuliwa waziwazi mno na kwa usahili, kiasi kwamba msafiri, hata kama angekuwa mjinga kiasi gani, hana haja ya kupotea au kushindwa kuelewa kile Maandiko yanachosema." - Bliss, ukurasa wa 70. Kukipata kiunganishi baada ya kiunganishi cha mnyororo wa Ukweli ikawa ndiyo baraka na zawadi ya juhudi zake, kwani kwa kadri alivyofuatilia hatua kwa hatua mistari ya matukio makubwa ya unabii. Malaika wa mbinguni walikuwa wakiyaongoza mawazo yake na kumfunulia ili aweze kuyaelewa Maandiko. [GC 320.2; PK Aya ya 9]

**Ngano Na Magugu**

Alizingatia jinsi unabii mwingi ulivyokuwa umetimizwa katika siku mbali mbali huko nyuma kama kigezo ambacho kwacho angeweza kupima unabii wa mambo yajayo ambayo bado yalikuwa hayajatokea ila, hakika yalikuwa yanakuja mbeleni, aliridhika kwamba maoni yaliyopendwa na watu wengi kuhusu utawala wa kiroho wa Kristo - - milenia ya wakati mfupi hapa duniani kabla ya mwisho wa dunia hii - hayakuungwa mkono na Neno la Mungu. Fundisho hili, lililoyaelekeza macho ya watu kwenye kipindi kile cha miaka elfu moja ya haki na amani kabla ya ujio binafsi Bwana, lilifanya ule utisho wa siku ile kuu ya Mungu kuonekana

kwamba iko mbali sana. Lakini, japokuwa linaweza kuwa linapendeza sana, kama vile lilivyo, liko kinyume na mafundisho Yake Kristo pamoja na yale ya Mitume Wake, waliotangaza kwamba ngano na magugu vinapaswa kukua pamoja mpaka wakati wa mavuno, mwisho wa dunia; kwamba "watu wabaya na wadanganyaji wataendelea, na kuzidi kuwa waovu," kwamba katika "siku za mwisho kutakuwako nyakati za hatari"; na ya kuwa ufalme wa giza utaendelea kuwako mpaka wakati wa kuja Kwake Bwana, nao utakomeshwa kwa roho ya kinywa Chake, na kuangamizwa kwa mng'ao wa kuja Kwake. Mathayo 13:30, 38-41; 2 Timotheo 3:13, 1; 2 Wathesalonike 2:8. [GC 321.1; PK Aya ya 10]

**Fundisho Ambalo Halikushikwa Na Kanisa La Mitume**

Fundisho la kuongolewa kwa ulimwengu mzima pamoja na utawala wa kiroho wa Kristo halikufundishwi na Kanisa la Mitume. Kwa ujumla halikukubaliwa na Wakristo mpaka karibu na mwanzoni mwa karne ya kumi na nane. Kama inavyokuwa fundisho jingine lolote la uongo, matokeo yake yalikuwa mabaya. Liliwafundisha watu kuyatazamia marejeo Yake Bwana katika siku za mbali sana huko mbeleni, na liliwazuia wasiweze kuzizingatia dalili za zilizoashiria vilivyokuwa vinatangaza ujio wa Yesu ulikokuwa unakaribia. Lilichochea hisia za kujiamini wenyewe na kujiona wako salama, jambo hili halikuwa na msingi mzuri, tena lilipelekea wengi kupuuzia kufanya maandalizi muhimu ili kumlaki Bwana wao. [GC 321.2; PK Aya ya 11]

Miller aligundua kwamba kuja Kwake Kristo kimwili, yaani ujio halisi au binafsi ulifundishwa waziwazi katika Maandiko (Yn. 5:25-28). Asema hivi Paulo: "Kwa sababu Bwana Mwenyewe atashuka kutoka mbinguni pamoja na mwaliko, na sauti ya malaika mkuu, na parapanda ya Mungu." 1 Wathesalonike 4:16. Na Mwokozi anatangaza hivi: "Nao watamwona Mwana wa Adamu akija katika mawingu ya mbinguni akiwa na nguvu na utukufu mwingi." maana, kama vile umeme uangazavyo toka mashariki hadi magharibi, ndivyo kutakavyokuwa kuja Kwake Mwana wa Adamu. Mathayo 24:30, 27. Ataandamana na majeshi yote ya mbinguni. "hapo Atakapokuja Mwana wa Adam katika utukufu Wake, na malaika watakatifu wote pamoja Naye." Mathayo 25:31. "Naye atawatuma malaika Zake pamoja na sauti kuu ya tarumbeta, nao watawakusanya wateule Wake." | Mathayo 24:31. [GC 321.3; PK Aya ya 12]

Wakati wa kuja Kwake, wale wenye haki waliokufa watafufuliwa, na wenye haki walio hai watabadilishwa. "Hatutalala sote -Hatutakufa sote," asema Paulo, "lakini sote tutabadilika, kwa dakika moja, kufumba na kufumbua, wakati wa parapanda ya mwisho; maana parapanda italia, na wafu watafufuliwa, wasiwe na uharibifu, nasi tutabadilika. Maana sharti huu uharibikao uvae kutokuharibika, nao huu wa kufa uvae kutokufa." 1 Wakorintho 15:51-53. Kisha katika Waraka wake kwa Wathesalonike, baada ya kueleza habari za marejeo ya Bwana,

anasema hivi: “Nao Waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza; kisha sisi tulio hai, tuliosalia, tutanyakuliwa pamoja nao katika mawingu, ili kumlaki Bwana angani: na hivyo tutakuwa pamoja na Bwana milele.” |1 Wathesalonike 4:16, 17. [GC 322.1; PK Aya ya 13]

Ni mpaka wakati wa ujio wa Kristo Mwenyewe ndipo watu Wake watakapoupokea ufalme. Mwokozi alisema: “Hapo atakapokuja Mwana wa Adamu katika utukufu Wake, na malaika watakatifu wote pamoja Naye, ndipo atakapoketi katika kiti cha utukufu Wake; na mataifa yote watakusanyika mbele Zake; naye atawabagua kama vile mchungaji abaguavyo kondoo na mbuzi; atawaweka kondoo mkono Wake wa kuume, na mbuzi mkono Wake wa kushoto. Kisha Mfalme atawaambia wale walioko mkono Wake wa kuume, Njoni, mliobarikiwa na Baba Yangu, urithini ufalme mliowekewa tayari tangu kuumbwa ulimwengu.” Mathayo 25:31-34. Tumeona katika Maandiko yaliyokwisha kutolewa punde kwamba Mwana wa Adamu atakapokuja, wafu watafufuliwa na kuwa na hali ya kutokufa tena, na wale walio hai watabadilishwa. Kwa badiliko hilo kubwa wanaandaliwa kuupokea ufalme, kwa maana Paulo asema hivi: “Mwili na damu hauwezi kuurithi ufalme wa Mungu; wala uharibifu kurithi kutokuharibika.” 1 Wakorintho 15:50. Mwanadamu katika hali yake ya sasa, ana hali ya kufa, ana mwili unaoharibika; lakini ufalme wa Mungu utakuwa usioharibika, yaani, unaodumu milele. Kwa hiyo, mwanadamu katika hali yake ya sasa hawezi kuingia katika ufalme wa Mungu. Lakini hapo Yesu atakapokuja atawatunukia watu Wake kutokufa; kisha atawaita kuurithi ufalme ambao tangu wakati huo utakuwa ni urithi wao wanaostahili. [GC 322.2; PK Aya ya 14]

**Ushahidi Wa Aina Nyingine**

Maandiko haya, pamoja na Maandiko mengine yalimthibithishia Miller wazi mawazoni mwake kuwa matukio yaliyokuwa yakitarajiwa kutokea na watu wote kwa jumla kabla ya kuja Kwake Kristo, kama vile utawala wa amani wa ulimwengu mzima na kuuanzisha ufalme wa Mungu hapa duniani, yangetokea baada ya ujio wa pili wa Kristo. Zaidi ya hayo, dalili zote za nyakati na hali ya ulimwengu vililandana na maelezo ya kiunabii ya siku za mwisho. Alilazimika kufikia hitimisho, kwa kujifunza Maandiko peke yake, kwamba kipindi kilichotolewa cha kuendelea kuwako kwa dunia hii katika hali yake ya sasa, kilikuwa kinakaribia kwisha (kufikia mwisho wake). [GC 323.1; PK Aya ya 15]

“Aina nyingine ya ushahidi iliyoathiri sana mawazo yangu,” alisema, “Ilikuwa ni lile jambo la kronologia* kwenye maandiko, yaani mpangilio wa matukio kufuatana na muda yalipotokea katika Maandiko .... Nilikuta kwamba matukio ambayo yalikuwa yametabiriwa katika unabii, na ambayo yalikuwa yametimizwa katika siku za nyuma, mara nyingi yalitokea katika muda ule ule husika ulioamuriwa. Miaka mia moja na ishirini hadi wakati wa gharika (Mwanzo 6:3);

siku saba ambazo zilitangulia kabla ya gharika pamoja na siku arobaini za mvua iliyotabiriwa kunyesha (Mwanzo 7:4); miaka mia nne ya kukaa ugenini kwa uzao wa Ibrahimu (Mwanzo 15:13); siku tatu za ndoto ya Mnyweshaji na mwoka mikate (Mwanzo 40:12-20); miaka saba inayomhusu Farao (Mwanzo 41:28-54); miaka arobaini jangwani (Hesabu 14:34); miaka mitatu na nusu ya njaa (1 Wafalme 17:1) (tazama Luka 4:25) miaka sabini ya kukaa kama mateka (Yeremia 25:11); Nyakati saba za Nebukadneza kuwa kama mnyama. (Danieli 4:13-16); na majuma saba, majuma sitini na mawili, na juma moja, ambayo jumla yake ni majuma sabini, yaliyoamriwa juu ya Wayahudi (Danieli 9:24-27),— matukio ambayo yalihusisha nyakati hizi, hapo zamani yalikuwa ni unabii tu, nayo yalitimizwa kulingana na utabiri husika." - Bliss, ukurasa wa 74 na 75 *(Wendo, matukio kutokana na mfulilizo wa tarehe). [GC 323.2; PK Aya ya 16]

Wakati alipogundua katika kujifunza kwake Biblia, wendo au kronologia ya Maandiko, yaani mpangilio wa matukio ya Biblia kulingana jinsi yalivyofuatana kutokana kwa uelewa wake wa matukio hayo, aliweza kuyaona tu kama ni zile "nyakati zilizoteuliwa mapema," ambazo Mungu alikuwa amewafunulia watumishi Wake; "Mambo ya siri," asema Musa, "ni ya BWANA, Mungu wetu; lakini mambo yaliyofunuliwa ni yetu sisi na watoto wetu milele; " Naye Bwana anatangaza kwa njia ya nabii Amosi, kuwa Yeye "hatafanya Neno lolote, bila kuwafunulia watumishi Wake manabii siri Yake." Kumbukumbu la Torati 29:29; Amosi 3:7. Basi, wanafunzi wa Neno la Mungu wanaweza kutarajia kwa matumaini na ujasiri kuliona tukio lile kuu kuliko yote yatakayotokea katika historia ya wanadamu, na ambalo limeelezwa waziwazi katika Maandiko hayo ya Ukweli. [GC 324.1; PK Aya ya 17]

**Maandiko Yote Yafaa**

"Kwa kuwa nilikuwa nimesadiki kikamilifu," asema Miller, kwamba "kila andiko, lenye pumzi ya Mungu, lafaa kwa mafundisho 2 Timotheo 3:16, kwamba halikuja wakati wowote kwa mapenzi ya mwanadamu, bali liliandikwa na wanadamu watakatifu, walioongozwa na Roho Mtakatifu 2 Petro 1:21, tena kwamba liliandikwa 'ili kutufundisha sisi, ili kwa saburi na faraja ya Maandiko tupate kuwa na tumaini' Warumi 15:4, mimi niliweza kuziona sehemu za Biblia zilizoandikwa kwa mpangilio wa matukio kulingana na muda yalipotokea kuwa zilikuwa ni sehemu za Neno la Mungu, na ya kwamba zilistahili kutiliwa maani, kama sehemu zingine zozote tu ya Maandiko. Kwa hiyo, mimi niliona kwamba katika kujitahidi kwangu kufahamu kile ambacho Mungu kwa rehema Zake alikuwa ameona inafaa kutufunulia sisi, mimi sikuwa na haki yoyote ya kuviruka vile vipindi vya unabii." - Bliss, ukurasa wa 75. [GC 324.2; PK Aya ya 18]

Unabii ulioonekana kuwa wazi zaidi katika kufunua wakati ule wa kuja Kwake Bwana kwa mara ya pili ulikuwa ni ule wa Danieli 8:14: "Hata siku elfu mbili na

mia tatu; ndipo Patakatifu patakapotakaswa.”. Akifuata kanuni yake ya kuyafanya Maandiko yajifasiri yenyewe, Miller aligundua kwamba siku moja katika unabii wa mifano inawakilisha mwaka mmoja, (Hesabu 14:34; Ezekieli 4:6); aliona kwamba kipindi hiki cha siku 2300 za kiunabii, ama miaka halisi 2300, kingeenda mbele zaidi hadi kuvuka kufungwa kwa kipindi cha Wayahudi kuwa taifa takatifu, na hivyo kisingeweza kurejelea hekalu la kipindi kile cha Wayahudi kama taifa teule na takatifu. Miller aliukubali mtazamo uliokuwepo kwa jumla miongoni mwa watu wengi katika zama za Ukristo, kwamba dunia hii ndiyo Patakatifu, na, kwa hiyo, alielewa kwamba kutakaswa kwa Patakatifu kulikotabiriwa katika Danieli 8:14 kuliwakilisha kutakaswa kwa dunia hii kwa moto wakati wa ujio wa Kristo wa mara ya pili. Basi, ikiwa mahali sahihi pa kuanzia zile siku 2300 pangeweza kujulikana- mambo yangekuwa rahisi, hivyo alihitimisha kwa uamuzi kwamba wakati wa kuja Kwake Kristo mara ya pili hakika ungeweza kuthibithishwa kwa urahisi. Hivyo wakati wa mwisho ule mkuu wa mambo yote ungeweza kujulikana, wakati ule ambapo hali ya mambo ilivyo sasa, pamoja na “kiburi, uovu, majivuno, nguvu, kujionyesha, upuuzi, na ubatili vingefikia mwisho wake; wakati ambapo laana “ingeondolewa duniani, kifo kingeangamizwa, thawabu ingetolewa kwa watumishi wa Mungu, manabii na watakatifu, pamoja na wale wanaolicha Jina Lake, na wale wanaoiharibu dunia kuangamizwa” (Ufu. 11:18) - Bliss, ukurasa wa 76. [GC 324.3; PK Aya ya 19]

### Danieli 8:14

Kwa jitihada mpya na yenye kina, Miller aliendelea kuuchunguza unabii huo, usiku na mchana ulitumika kujifunza kile kilichoonekana kabisa kwake, kuwa kina umuhimu wa ajabu mno, na ambacho kilivuta umakini wake wote kukifuatilia. Katika sura ya nane ya Danieli hakuweza kupata kidokezo chochote ambacho kingemsaidia kujua mwanzo wa kipindi cha siku 2300; malaika Gabrieli, ingawa aliagizwa kumsaidia Danieli aelewe njozi, alimpa sehemu tu ya maelezo yake. Mateso ya kutisha yatakayoliangukia kanisa yalipofunuliwa katika maono ya nabii Danieli, nguvu zake za mwili zilimtoweka. Hakuweza kustahimili zaidi; malaika akamwacha kwa muda fulani. Danieli “alizimia na akawa mgonjwa kwa siku kadha wa kadha.” “Nami naliyastaajabia yale maono,” anasema, “ila hakuna aliyeyaelewa” (Dan. 8:16-27). [GC 325.1; PK Aya ya 20]

### Kufanya Mahesabu Ya Ratiba Ya Unabii

Walakini Mungu alikuwa amemwagiza mjumbe Wake, akisema: “Mfahamishe mtu huyu maono haya.” Agizo hilo lilikuwa halina budi kutekelezwa. Kwa kulitii agizo hilo, malaika muda fulani baadaye, alimrudia Danieli, na kumwambia akisema: “Sasa nimetokea ili nikupe akili upate kufahamu.; “Basi lifahamu jambo hili, ukatafakari maono hayo.” Danieli 8:27, 16; 9:22, 23, 25-27. Palikuwa

na jambo moja la muhimu katika maono ya sura ya nane ambalo lilikuwa limeachwa bila kutolewa maelezo ya ufafanuzi, yaani, lile linalohusiana na wakati - kipindi kile cha siku 2300; basi, malaika kwa kurudi na kuendelea tena katika maelezo yake, anashuglikia sana juu ya mada hiyo ya wakati: [GC 325.2; PK Aya ya 21]

"Muda wa majuma sabini umeamriwa/umetengwa juu ya watu wako (Wayahudi), na juu ya Mji wako Mtakatifu.... Basi ujue na kufahamu, ya kuwa tangu kuwekwa amri ya kutengeneza na kuujenga upya Yerusalemu hata zamani zake Masihi aliye Mkuu; kutakuwa na majuma saba; na katika majuma sitini na mawili utajengwa tena pamoja na njia kuu zake na handaki, naam, katika nyakati za taabu. Na baada ya yale majuma sitini na mawili, Masihi atakatiliwa mbali, Naye atakuwa hana kitu.... Naye atafanya agano thabiti na watu wengi kwa muda wa juma moja; na kwa nusu ya juma hiyo ataikomesha sadaka na dhabihu." (Mt. 27:50,51; 1 Kor. 5:7; Ebr. 10:14,18). [GC 326.1; PK Aya ya 22]

**Malaika Alitumwa Kwa Danieli**

Malaika alikuwa ametumwa kwa Danieli kwa kusudi maalum la kumweleza jambo lile alilokuwa ameshindwa kulielewa katika njozi ya sura ya nane, yaani, jambo lile lililohusiana na wakati - "Hata nyakati za jioni na asubuhi elfu mbili na mia tatu; ndipo Patakatifu patakapotakaswa." Baada ya kumwagiza Danieli "atafakari habari hii na kuyafahamu maono haya," Maneno ya kwanza kabisa ya malaika yule ni haya: "Muda wa majuma sabini umeamriwa juu ya watu wako, na juu ya mji wako Mtakatifu." Neno lililotafsiriwa hapa "umeamriwa" maana yake ikichukuliwa neno kwa neno ni hii "umeondolewa kwa kukatwa" (au "umetengwa"). Majuma hayo sabini yaiwakilishayo ile miaka 490 (70 x 7 = siku/miaka 490, Eze. 4:6), yalitangazwa na malaika kuwa yametengwa, yaani, yanawahusu hasa Wayahudi. Lakini, Je! Yalitengwa au kukatwa kutoka katika kipindi gani au kutoka wapi? Kwa vile siku 2300 ndicho kipindi pekee cha wakati kilichotajwa katika sura ya 8, basi, lazima kiwe ndicho kipindi ambacho kutokana nacho majuma hayo sabini yaliondolewa kwa kukatwa (kutengwa); kwa hiyo, majuma hayo sabini ni lazima yawe sehemu ya siku zile 2300, na vipindi vyote viwili lazima vianze kwa pamoja. Majuma hayo sabini yalitangazwa na yule malaika kwamba yataanza kuhesabiwa tangu kuwekwa amri ya kuurejesha na kuujenga upya Yerusalemu. Endapo tarehe ya amri ile ingeweza kupatikana, basi, tarehe ya kuanza kipindi hicho kikuu cha siku 2300 ingeweza kujulikana kwa hakika. [GC 326.2; PK Aya ya 23]

Katika sura ya saba ya Ezra, ndiyo amri hiyo inapatikana. Fungu la 12 hadi la 26. Katika ukamilifu wake wote, ilitolewa na Artashasta, mfalme wa Uajemi, mwaka ule wa 457 K.K. Lakini katika Ezra 6:14 nyumba ya Bwana kule Yerusalemu inasemekana kuwa ilikuwa imejengwa "kwa amri ya ["agizo la,"

Koreshi, na Dario, na Artashasta mfalme wa Uajemi.” Wafalme hawa watatu, katika kuanzisha, kukazia tena, na kuikamilisha amri ile, waliitekeleza katika ukamilifu wake kama ilivyotakiwa na unabii kuonyesha mwanzo wa miaka ile 2300. Tukiuchukua mwaka wa 457 K.K., yaani, wakati amri ile ilipotekelezwa kikamilifu, kama ndiyo tarehe rasmi ya kutolewa kwa amri, basi, kila kipengele cha unabii unaohusu majuma sabini kinaonekana kuwa kimeshatimizwa kikamilifu. *(Kuanzisha [537/536 K.K.], kuithibitisha tena [karibu na 519 K.K.], na kuitekeleza amri ile [457 K.K.], waliifikisha katika ukamilifu wake uliotakiwa) [GC 326.3; PK Aya ya 24]

“Tangu kuwekwa amri ya kutengeneza na kuujenga upya Yerusalemu hata zamani zake Masihi aliye mkuu; kutakuwa na majuma saba; na katika majuma sitini na mawili…..” - yaani, jumla ya majuma sitini na mbili na majuma saba. Amri ile ya Artashasta ilianza kutekelezwa katika majira ya kupukutisha majani Septemba hadi Novemba ya mwaka 457 K.K. Kuanzia mwaka huo ile miaka 483 ilifika hadi majira ya kupukutisha majani ya mwaka 27 B.K. (Tazama kiambatisho Mwisho) Wakati huo unabii huu ulitimizwa. Neno “Masihi” linamaanisha “Mpakwa-Mafuta.” Katika majira ya kupukutisha majani Mwaka 27 B.K Kristo alibatizwa na Yohana na kupokea upako wa Roho Mtakatifu. Mtume Petro anashuhudia kwamba “Mungu alimtia mafuta Yesu wa Nazareti kwa Roho Mtakatifu na nguvu.” Mtume Petro anashuhudia kwamba “Mungu alimtia mafuta Yesu wa Nazareti kwa Roho Mtakatifu na kwa nguvu.” Matendo 10:38. Na Mwokozi Mwenyewe alisema: “Roho wa Bwana yu juu Yangu, kwa maana amenitia mafuta kuwahubiri maskini Injili. Luka 4:18. Baada ya ubatizo Wake alienda Galilaya, “akihubiri Injili ya ufalme wa Mungu, akisema, wakati umetimia/umewadia.” Marko 1:14, 15 *(majuma 7 + majuma 62 = majuma 69, Majuma 69 ni siku 483 au miaka 483 kiunabii). [GC 327.1; PK Aya ya 25]

**Injili Yatangazwa Ulimwenguni Kote**

Naye atafanya agano thabiti na watu wengi kwa muda wa juma moja.” “Juma moja”* linalotajwa hapo ni juma lile la mwisho katika ya yale majuma sabini; ni miaka ile saba ya mwisho wa kipindi cha miaka iliyotengwa mahsusi kwa ajili ya Wayahudi. Katika kipindi hichi kinachoanzia mwaka wa 27 B.K. mpaka mwaka wa 34 B.K., Kristo, mwanzoni akiwapo duniani Yeye Mwenyewe ana kwa ana na watu, na baadaye kwa njia ya wanafunzi Wake, alipeleka rasmi mwaliko Wake wa injili kwa Wayahudi kama walengwa haswa. Wanafunzi Wake walipotoka na kwenda kutangaza Habari Njema za ufalme, maagizo ya Mwokozi kwao yalikuwa ni haya: “Msiende katika njia ya Mataifa, wala katika mji wowote wa Wasamaria msiingie; Afadhali shikeni njia kuwaendea kondoo waliopotea wa nyumba ya Israeli.” Mathayo 10:5, 6. [GC 327.2; PK Aya ya 26]

“Na kwa nusu ya juma hiyo ataikomesha sadaka na dhabihu.” Mnamo mwaka wa 31 B.K., yaani, miaka mitatu na nusu baada ya ubatizo Wake, Bwana wetu alisulibiwa. Kwa kafara ile kuu iliyotolewa juu ya Kalvari, aliukomesha ule mfumo wa sadaka ambao kwa miaka elfu nne (tangu Edeni) ulikuwa umesonda kidole chake mbele kwa Mwana -Kondoo wa Mungu. Kivuli au mfano, ulikutana na kitu halisi, ndipo sadaka na dhabihu zote za mfumo ule wa kaida, wa kutoa kafara ya wanyama ulikomea hapo (ceremonial system au sherehe-kafara za wanyama ndiyo mfano na Mwana-Kondoo wa Mungu ndiyo kitu halisi – Yn. 1:29)) (Efe. 2:11-18; Kol. 2:9-17; Zab. 85:10; Mt. 27:50,51). [GC 327.3; PK Aya ya 27]

Majuma yale sabini, au miaka ile 490, mahsusi waliyopewa Wayahudi, ikawa imeishia hapa, kama tulivyokwisha kuona, katika mwaka wa 34 B.K. Katika wakati huo, kupitia kwa tendo la Baraza Kuu la Wayahudi, yaani Sanhedrin, taifa lile lile lilitia muhuri wake kuikataa Injili kwa kumwua Stefano na kuwatesa wafuasi Wake Kristo. Tangu hapo, ujumbe wa wokovu ambao kwanza ulikuwa kwa wateule pekee, sasa ulitolewa kwa ulimwengu mzima, nao haukuweza kuwekewa mipaka tena (Mdo. 13:42-48). Wanafunzi Wake Bwana, walilazimishwa kuikimbia Yerusalemu kutokana na mateso, “walienda kila mahali wakilihubiri Neno.” “Filipo akatelemka akaingia mji wa Samaria akawahubiri Kristo.” Petro, akiongozwa na Mungu, alimfunulia injili akida wa Kaisaria, yaani, yule Kornelio, mcha Mungu sana; na Paulo aliyekuwa motomoto, ambaye alikuwa ameongolewa katika imani ile ya Kristo, alipewa agizo kuipeleka Habari Njema yenye furaha “mbali kwa watu wa Mataifa.” “mbali kwa Mataifa.” Matendo 8:4, 5; 22:21. [GC 328.1; PK Aya ya 28]

Kufikia hapo, kila elezo bayana la unabii huo limetimizwa kikamilifu kwa namna ya kushangaza mno, na ule mwanzo wa majuma sabini ukathibitika kuwa ni mwaka ule wa 457 K.K kiasi cha kutokuwapo na swali lolote kuhusiana nalo na kuishia katika mwaka wa 34 B.K. Kutokana na maelezo hayo, hakuna ugumu wowote wa kujua mwisho wa kipindi cha siku zile 2300. Majuma yale sabini - yaani, siku zile 490 - yakiwa yameondolewa kwa kukatwa kutoka katika siku zile 2300, pakawa na siku 1810 zilizosalia (2300-490 = 1810 siku/miaka). Baada ya mwisho wa siku zile 490, siku 1810 zilikuwa bado kutimizwa. Tangu ule mwaka wa 34 B.K. miaka ile 1810 ilifika hadi mwaka ule wa 1844 (34 + 1810 = 1844). Kwa hiyo, siku zile 2300 za Danieli 8:14 zinaishia mwaka wa 1844. Mwishoni mwa hichi kipindi kikuu cha kiunabii, kwa ushuhuda wa yule malaika wa Mungu, “ndipo Patakatifu patakapotakaswa.” Hivyo wakati wa kutakaswa Patakatifu --- uliaminiwa karibu na watu wote kuwa ungetokea wakati wa kuja Kwake Kristo mara ya pili - Ulikuwa umebainishwa kikamilifu. [GC 328.2; PK Aya ya 29]

**Ushahidi Ulio Wazi Na Wenye Nguvu**

Miller na wenzake mwanzoni, waliamini kwamba siku zile 2300 zingekoma/ zingeishia katika majira yale ya kuchipua majani (Spring – Machi hadi Mei) ya mwaka wa 1844, ambapo unabii huo huelekeza kwenye yale majira ya kupukutisha majani (Autumn – Septemba hadi Novemba) ya mwaka ule (Tazama kiambatisho.) Kutokulielewa vizuri jambo hilo kulisababisha kuvunjika moyo na mfadhaiko mkubwa kwa wale waliokuwa wameweka tarehe ya mapema zaidi kuwa ndio wakati wa marejeo Yake Bwana. Lakini hilo halikuathiri hata kidogo nguvu ya hoja hiyo iliyoonyesha kwamba siku zile 2300 ziliishika katika mwaka wa 1844, na ya kwamba tukio kuu lililowakilishwa na utakaso wa Patakatifu lazima lingetokea. [GC 328.3; PK Aya ya 30]

Alipokuwa ameingia katika kujifunza Maandiko, kama alivyokuwa akifanya kwa lengo la kuthibitisha kwamba yalikuwa ni ufunuo uliotoka kwa Mungu, Miller, mwanzoni, hakuwa na matarajio hata kidogo ya kufikia mkataa ule ambao alikuwa ameufikia sasa. Yeye mwenyewe aliona vigumu sana kuuamini utafiti wake kirahisi. Lakini ushahidi wa Maandiko ulikuwa wazi mno na wenye nguvu kiasi kwamba hakuweza kuusukumwa kando. [GC 329.1; PK Aya ya 31]

Alikuwa amejitoa kikamilifu kwa miaka miwili kwa ajili ya kujifunza Biblia, naye katika mwaka 1818 alisadikishwa kwa uzito kabisa kwamba ndani ya kipindi cha miaka ishirini na tano kuanzia wakati ule Kristo angetokea kuwakomboa watu Wake. "Sihitaji kusema," Miller alisema, "kuhusu habari ya shangwe iliyoujaza moyo wangu kwa sababu ya matazamio ya kuchangamsha moyo sana, na shauku yenye joto ndani ya moyo wangu kwa kuweza kushiriki katika shangwe ya waliokombolewa. Kwangu, Biblia sasa ilikuwa ni kitabu kipya. Maneno yake yakawa karamu ya fikra zangu; kila jambo lililokuwa la giza, siri, mafumbo au lisiloeleweka kwangu katika mafundisho yake, lilipukutishwa nje ya moyo wangu mbele ya nuru iliyokuwa wazi ambayo sasa ilikuwa imeanza kupambazuka kutoka katika kurasa zake takatifu; tena, Loo! Ukweli ulikuwa uking'aa kwa mwangaza na utukufu mwingi. Mambo yote yaliyoonekana awali kama yanakinzana na kutopatana yenyewe kwa yenyewe, ambayo nilikutana nayo hapo awali katika Neno yakawa yametoweka; na ingawa kulikuwa na maeneo mengi ambayo sikuridhika nayo kwamba nilikuwa na uelewa kamili, hata hivyo nuru kubwa ilimwagwa kutoka katika Maandiko na kuniangazia akili yangu, nami nikapata kuelewa maana yake, na bado nuru nyingi iliangazia katika sehemu hizo na kuipa akili yangu iliyokuwa gizani kabla yake nuru, hata nikafurahi kujifunza Maandiko, ambayo hapo awali sikudhani kwamba ningeweza kuipata katika mafundisho yake." - Bliss, ukurasa wa 76 na 77. [GC 329.2; PK Aya ya 32]

"Baada ya kusadikishwa kwa dhati kuhusu matukio hayo ya makuu sana ambayo yalikuwa yametabiriwa katika Maandiko na yalitarajiwa kutimizwa katika muda mfupi mno kama huo, swali likaja karibu na moyo wangu kwa nguvu kuhusiana na wajibu wangu kwa ulimwengu, kutokana na ushahidi huo ambao

ulikuwa umeugusa moyo wangu.” Ibid 81. Hakuweza kuepuka kuhisi kwamba ilikuwa ni wajibu wake kuwasilisha kwa wengine nuru ambayo alikuwa ameipokea. Alitarajia kukutana na upinzani kutoka kwa wale wasiomcha Mungu, ila alikuwa na uhakika kwamba Wakristo wote wangeweza kufurahia tumaini la kukutana na Mwokozi wao ambaye wadai kuwa wanampenda. Hofu yake ilikuwa tu kwamba katika shangwe yao kubwa ya kutazamia ukombozi wao wenye utukufu, ambao ulikuwa tayari kukamilika upesi sana, wengi wao wangelipokea fundisho lile pasipo kuyachunguza Maandiko kwa kiasi cha kutosha katika kudhihirisha Kweli Yake. Basi, alisitasitasita kuuwasilisha ujumbe huo, isije ikawa pengine amekosea na hivyo kuwa sababu ya kuwapoteza wengine. Hivyo alishawishiwa kuupitia tena ushahidi wote ambao uliunga mkono hitimisho alilokuwa amelifikia, na kutafakari kwa makini kila tatizo lilillokuwa limejitokeza lenyewe mawazoni mwake. Aliona kuwa vipingamizi vyote viliyeyuka mbele ya nuru ya Neno la Mungu kama ukungu unavyoyeyuka mbele ya miale ya jua. Miaka mitano iliyotumika kwa njia hiyo ilimwacha akiwa ameshawishika kabisa kuhusu usahihi wa msimamo wake. [GC 329.3; PK Aya ya 33]

### “Nenda Kautangazie Ulimwengu”

Na sasa wajibu wa kuhakisha kwamba wengine wanajulishwa juu ya kile alichokiamini kuwa kilifundishwa kwa uwazi sana katika Maandiko, ulimsukuma kwa nguvu. “Nilipokuwa nafanya shughuli zangu,” alisema, “daima kengele ilikuwa ikiendelea kusikika masikioni mwangu, ikisema, ‘Nenda ukauambie ulimwengu hatari yao inayowakabili.’ Fungu hili lilikuwa likinijia kila mara: 'Nimwambiapo mtu mbaya, Ewe mtu mbaya, hakika utakufa; kama husemi ili kumwonya mtu mbaya aiache njia yake, mtu mbaya huyo atakufa katika uovu wake; lakini damu yake nitaitaka mkononi mwako. Lakini, ukimwonya mtu mbaya juu ya njia yake, na kuiacha; asipoiacha njia yake, atakufa katika uovu wake; lakini umejiokoa nafsi yako.” Ezekieli 33:8, 9. Nilihisi kwamba ikiwa watu waovu wangeweza kuonywa kikamilifu kwa njia iletayo mabadiliko, wengi wao wangetubu; na kwamba ikiwa wasingeonywa, damu yao ingedaiwa mkononi mwangu.”— Bliss, ukurasa wa 92. [GC 330.1; PK Aya ya 34]

Alianza kuwasilisha maoni yake faraghani kwa mtu mmoja mmoja, kwa kadiri alivyoweza kupata fursa, akiombea kwamba mchungaji fulani angeweza kuguswa na nguvu ya mafundisho yale na kujitolea muda wake kuyatangaza. Lakini hakuweza kuondoa usadikisho kwamba alikuwa na wajibu binafsi wa kutekeleza katika kulitoa onyo hilo. Maneno haya yalikuwa yanakuja tena na tena akilini mwake: “Nenda kauambie ulimwengu; damu yao nitaitaka mkononi mwako.” Alisubiri kwa miaka tisa, mzigo huo ukazidi kuilemea nafsi yake, mpaka katika mwaka ule wa 1831 kwa mara yake ya kwanza aliwasilisha hadharani sababu za imani yake. [GC 330.2; PK Aya ya 35]

### Aitwa Kuliacha Jembe Lake La Kukokotwa Na Ng'ombe

Kama vile Elisha alivyoitwa kuacha kufuatana na ng'ombe zake wanaokokota jembe la plau shambani, na kulipokea joho la wakfu kwa ajili ya kazi ya kinabii, kadhalika Wiliam Miller aliitwa na kuliacha jembe lake la kukokotwa na ng'ombe na kuwafunulia watu siri na mafumbo ya ufalme wa Mungu. Akiwa katika hali ya kutetemeka aliingia kuianza kazi yake, akiwaongoza wasikilizaji wake, hatua kwa hatua, katika vipindi vile vya unabii hadi kwenye ujio wa pili wa Kristo. Kwa kila juhudi aliyoifanya, alipata nguvu na ujasiri alipoona shauku iliyokuwa imeamshwa ikisambaa kote kutokana na maneno yake. [GC 331.1; PK Aya ya 36]

Ilikuwa kwa njia ya kuombwa sana na ndugu na dada zake, ndipo kupitia maneno yao alisikia wito wa Mungu, Miller alikubali kuwasilisha mitazamo yake hadharani. Sasa alikuwa amefikia umri wa miaka hamsini, akiwa mtu asiye na uzoefu wa kuongea hadharani, tena alilemewa na hisia ya kutofaa kwake kwa kazi ile iliyokuwa mbele yake. Lakini kuanzia mwanzo wa juhudi zake, kazi yake ilibarikiwa kwa namna ya ajabu sana kwa ajili ya wokovu wa roho. Hotuba yake ya kwanza ilifuatiwa na mwamko wa kidini ambao familia zipatazo kumi na tatu, isipokuwa watu wawili, ziliongoka. Haikupita muda, naye akaombwa kwenda kuhubiri katika maeneo mengine, na karibu katika kila mahali kazi yake ilileta uamsho wa kazi ya Mungu. Wenye dhambi waliongolewa, Wakristo walihamasishwa kujitoa wakfu kikamilifu zaidi, na waumini wasiokubali ufunuo wa Mungu pamoja na makafiri waliongozwa kukubali Ukweli wa Biblia na dini ya Kikristo. Ushuhuda wa wale ambao miongoni mwao aliwafanyia kazi ulikuwa ni huu: "Tabaka fulani la akili limefikiwa naye ambalo halikuwa limeshawishiwa na mtu mwingine kabla ya hapo." - Ibid., ukurasa wa 138. Mahubiri yake yalikusudiwa kuamsha watu ili wapate kutambua mambo ya thamani yaliyo katika dini au mambo ya kiroho na kuithibiti hali ya udunia ambayo ilikuwa inazidi kuongezeka pamoja na kuzipenda anasa za tamaa za mwili za kizazi kile. [GC 331.2; PK Aya ya 37]

Karibu katika kila mji kulikuwepo na makundi ya watu, wengine wakiwa katika mamia waliongoka kama matokeo ya mahubiri yake. Mahali pengi karibu makanisa yote ya Kiprotestanti ya madhehebu yote yaliacha milango yake wazi kwa ajili yake, na mwaliko wa kufanya kazi kwa kawaida ulitoka kwa wachungaji wa makanisa tofauti tofauti. Ilikuwa ni kanuni yake isiyobadilika kutohubiri mahali pale alipokuwa hajaalikwa, baada ya muda mfupi baadaye, alijikuta hawezi kutimiza nusu ya maombi yaliyomiminika kuja kwake. Wengi ambao hawakuyakubali maoni yake kuhusu wakati mahsusi wa ujio Wake Kristo kwa mara ya pili walishawishika juu ya uhakika na ukaribu wa marejeo Yake Kristo na kuliona hitaji lao la kujiandaa tayari. Katika baadhi ya miji mikubwa, kazi yake iliwagusa sana watu. Wauzaji wa vileo waliacha biashara yao na kuvigeuza vilabu

vyao vya pombe kuwa vyumba vya mikutano; maficho ya kuchezea kamari yakavunjiliwa mbali; wasiomwamini Mungu, na wale wanaomwamini Mungu bila kukubali Maandiko Yake au kujishugulisha Kwake na viumbe Wake (Deists), na wenye falsafa inayoamini kwamba ulimwengu wote hatimaye utaongolewa (Universalist), na hata waovu wa kutupwa waliokatiwa tamaa waliongolewa na kupata matengenezo ya tabia, wengine miongoni mwao walikuwa hawajapata kukanyaga katika nyumba ya ibada kwa miaka mingi. Mikutano ya maombi ilianzishwa na madhehebu mbalimbali (interdenominational) katika sehemu mbalimbali, karibu kila saa, wafanya biashara walikuwa wakikutana wakati wa mchanga kwa ajili ya maombi na kumsifu Mungu. Hapakuwa na misisimko iliyopitiliza au ya bandia, badala yake palikuwa na kuchukulia ibada kwa uzito kulioenea kote katika mioyo ya watu. Kazi yake Miller, kama ilivyokuwa kazi ya Wanamatengenezo wa mwanzo, ilikuwa na mwelekeo wa kuushawishi ufahamu na kuiamsha dhamiri kuliko kuchochea mihemko ya moyoni peke yake. [GC 331.3; PK Aya ya 38]

### Cheti Cha Kumruhusu Kuhubiri

Mnamo mwaka wa 1833 Miller alipokea leseni/kibali cha kuhubiri toka kwa Kanisa la Kibaptisti, ambalo yeye alikuwa mshiriki wake. Idadi kubwa ya wachungaji wa dhehebu lake pia waliiunga mkono kazi yake, tena ilikuwa ni kwa kibali chao rasmi, hivyo aliweza kuendelea na kazi yake. Alisafiri na kuhubiri bila kupumzika, ingawa kazi zake kwa kawaida ziliwekewa mipaka zisitoke nje ya eneo lile la New England yaani Massachusets na Majimbo yale ya Kati ya Marekani. Kwa miaka kadhaa gharama zake zote zilitoka katika mfuko wake binafsi, na baadaye hakuweza kupata kiasi cha fedha za kutosha kumwezesha kulipia gharama zake ya kusafiri ili aende kila mahali alipoalikwa. Hivyo kazi zake kwa umma, mbali na kutomletea fedha, zilikugeuka kuwa mzigo mzito kiuchumi kwake, kwa kuwa hakuwa na kipato kikubwa na hivyo fedha zake ziliendelea kupungua taratibu katika kipindi hiki chote cha maisha yake. Alikuwa baba wa familia kubwa, lakini kwa vile wote walijua kubana matumizi vizuri, tena walikuwa wenye bidii katika kufanya kazi, basi, shamba lake lilitosha kukidhi mahitaji yao pamoja na kusaidia katika kazi zake za kuhubiri injili. [GC 332.1; PK Aya ya 39]

### “Nyota Zitaanguka Mbinguni”

Mnamo mwaka wa 1833, miaka miwili baada ya Miller kuwasilisha hadharani ushahidi wa kuja kwa Kristo, dalili ya mwisho miongoni mwa ishara zilizoahidiwa na Mwokozi kama ishara ya ujio wa haraka wa Kristo kwa mara ya pili zilionekana. Alisema hivi Yesu: “Nyota zitaanguka kutoka mbinguni.” Mathayo 24:29. Naye Yohana katika kitabu cha Ufunuo, alipoona katika maono yake matukio yale ambayo yangeashiria siku ya Mungu, alitangaza kwa kusema: “Nazo

nyota za mbingu zikaanguka juu ya ardhi kama matunda ya mtini yasiyokomaa yaangukavyo wakati mti wake unapotikiswa na upepo mkali.” Ufunuo 6:13. Unabii huo ulitimizwa kwa namna ya kustaajabisha, na kikamilifu, vimwondo vya kuvutia sana vilidondoka chini kama manyunyu ya mvua tarehe 13 Novemba, 1833. Hilo lilikuwa ni onyesho lililoshuhudiwa katika eneo kubwa duniani, nyota zilianguka kwa namna ya ajabu sana ambayo imepata kutokea na kurekodiwa katika kumbukumbu kabla ya hapo; “anga lote juu ya nchi yote ya Marekani (U.S.A) ambalo kwa wakati ule lilionekana kana kwamba liko katika ghasia kubwa na mwanga uliotokana na milipuko ile ya moto! Hakuna tukio au kioja cha mbinguni kilichopata kutokea katika nchi hii tangu ilipokaliwa na watu kwa mara ya kwanza, kitu ambacho kiliangaliwa kwa shauku na mshangao mkubwa na tabaka moja la jumuia ile, au kwa hofu kubwa mno na taharuki kubwa na tabaka jingine la watu (makundi mawili hisia tofauti). “Fahari yake na uzuri wake wa kuogopesha,bado ungali mawazoni mwa watu wengi waliokuwa bado wanaishi.… kamwe hakuna Mvua yoyote iliyopata kunyesha kwa wingi kuliko vile vimwondo vilivyokuwa vikidondoka chini kuelekea katika nchi; mashariki, magharibi, kaskazini, na kusini, mambo yalikuwa ni yale yale. Kwa kifupi, mbingu zote zilionekana kana kwamba zilikuwa zikijongea, yaani zikitembea.... onesho hilo, kama lilivyoelezwa katika Jarida la Profesa Silimani (Silliman’s Journal), lilionekana juu ya nchi yote ya Amerika Kaskazini.... Tangu saa nane usiku hadi mchana, anga likiwa utulivu mkamilifu, na lisilo na mawingu, nuru iliyocheza-cheza kwa mfululizo kutoka kwenye mianga ile iliyong’aa sana iliendelea kumulika katika mbingu zote.” - RM Devens, Maendeleo ya Marekani; au, Matukio Makuu ya Karne Kubwa Zaidi, sura 28, kifungu 1-5. [GC 333.1; PK Aya ya 40]

“Kwa kweli, hakuna lugha inayotosheleza kuelezea uzuri wa utukufu wa maonyesho hayo ya kushangaza, pamoja na fahari yake.... Hakuna hata mmoja aliyelishuhudia awezaye kuwa na dhana inayotosheleza kuelezea ule utukufu wa tukio lile. Ilionekana kana kwamba mbingu yote yenye nyota ilikuwa imejikusanya mahali pamoja karibu na anga yetu na kufanya kilele, na wakati huo huo zilikuwa zikifyatua vimwondo kwa kasi ya mwanga kwenda katika kila sehemu ya upeo wa macho; na wala hazikuchoka kamwe - maelfu nyota vipande vile vya nyota vikafuata katika njia zile zile za maelfu yaliyotangulia kana kwamba viliumbwa kwa tukio lile.” - F. Reed, katika Wakili wa Kikristo na Jarida, Des. “Video iliyokuwa sahihi zaidi ya mtini unaopukutisha mapooza yake unapotikiswa na upepo wenye nguvu, ilikuwa ni vigumu kuiona kuliko ile.” “Mwananchi Kizee wa Shamba (The Old Countryman)” katika gazeti la Mtangazaji wa jioni wa Portland, Novemba 26, 1833. [GC 333.2; PK Aya ya 41]

Katika Jarida la biashara, New York Journal of Commerce la Novemba 14, 1833, makala ndefu iliandikwa kuhusu kioja au tukio lile la ajabu, ikiwa na maneno haya: “Nadhani hakuna mwanafalsafa au mwanazuoni yeyote aliyewahi

kusimulia au kurekodi vizuri habari za tukio kama lile la jana asubuhi. Nabii alitabiri kwa kusimulia vizuri kuhusu tukio hili miaka elfu moja na mia nane iliyopita, na endapo sisi tutapata shida kuelewa kuwa maana ya kuanguka kwa nyota inamaanisha kuanguka kwa nyota,... katika maana yake ya pekee, iliyo kweli, na ambayo ni halisi na wazi." [GC 334.1; PK Aya ya 42]

Hivyo ndivyo ilivyoonekana ishara ya mwisho miongoni mwa dalili zote za marejeo Yake Kristo, ambazo Yesu aliwaasa wanafunzi Wake, akisema: "Nanyi kadhalika, myaonapo hayo yote, tambueni ya kuwa Yu mlangoni." Mathayo 24:33. Baada ya dalili hizo, Yohana aliona, tukio kuu lililofuata baada ya hili na ambalo lilitarajiwa kuja wakati wa karibu sana, mbingu zikiondolewa kama ukurasa uliokunjwa, wakati dunia ikitetemeka vibaya, milima na visiwa vikiondolewa mahali pake, na waovu kwa hofu kuu wakijaribu kutimua mbio kwenda mbali na uwepo wa uso Wake Mwana wa Adamu. Ufunuo 6:12- 17. [GC 334.2; PK Aya ya 43]

**Mbiu Ya Hukumu**

Wengi walioshuhudia kuanguka kwa nyota, waliziangalia kama ni mbiu inayotangaza hukumu iliyokuwa inakuja, "kiashiria cha kutisha, mtangulizi wa hakika, ishara ya rehema ya siku ile kuu na ya kuogofya sana." - "The Old Country- Man" katika gazeti la Portland Evening Advertiser, la Nov. 26, 1833. Hivyo ndivyo usikivu wa watu ulivyoelekezwa kwenye utimilifu wa unabii huu, na wengi wao walishawishiwa kuzingatia onyo lililokuwa linatolewa la Ujio wa pili wa Yesu. [GC 334.3; PK Aya ya 44]

Mnamo mwaka wa 1840 utimizo mwingine wa ajabu wa unabii ulisisimua shauku kubwa mahali pengi. Miaka miwili kabla yake, Josiah Litch, mmojawapo wa wachungaji mashuhuri waliohubiri habari ya ujio wa pili wa Kristo, alichapisha ufafanuzi wa Ufunuo 9, akitabiri anguko la Himaya ya Ottoman au Uturuki (Ottoman Empire). Kwa mujibu wa kukokotoa kwake, utawala huu ulikuwa lazima upinduliwe "katika mwaka wa 1840 B.K., muda fulani katika mwezi wa Agosti;" tena, siku chache tu kabla ya utekelezaji wake, aliandika hivi: "Tukiruhusu kipindi kile cha kwanza, yaani, miaka ile 150 (Julai 27, 1449 – Julai 26, 1499, B.K. = miaka 150), kuwa ilitimizwa kikamilifu kabla Deacoses hajapewa ufalme kwa kibali cha Waturuki, na ya kwamba miaka 391, na siku 15, ilianza mwisho wa kipindi kile cha kwanza, nacho kingeishia tarehe 11 Agosti, 1840, wakati Mamlaka ya Ottoman juu ya Contantinople ilitarajiwa kuvunjiliwa mbali. Na jambo hilo, mimi naamini, litatokea hivyo hivyo." - Josiah Litch, katika Signs of the Times, and Expositor of Prophecy, la Agosti 1, 1840. (Tafsiri- Gazeti la Ishara za Nyakati, na Mfafanuzi wa Unabii, Agosti 1, 1840.) *(Ufu. 9:15 – saa = siku 15; siku 1 = mwaka 1; mwezi 1 = siku/miaka 30; mwaka 1 =

siku/miaka 360. Julai 27, 1499 – Agosti 11, 1840 = miaka 391 na siku 15). [GC 334.4; PK Aya ya 45]

Kwa wakati ule ule hasa uliotajwa, Uturuki, kupitia kwa mabalozi wake ilikubali kuwa chini ya ulinzi wa mamlaka ya umoja wa mataifa ya Ulaya, na hivyo ilijiweka yenyewe chini ya udhibiti wa Mataifa ya Kikristo. Tukio hili likawa limetimiza kikamilifu utabiri. (Tazama kiambatisho) Jambo hilo lilipoeleweka vizuri, watu wengi sana walishawishika kuamini usahihi wa kanuni za kutafsiri unabii ambazo alizitumia Miller na wenzake, na msukumo wenye nguvu ya ajabu ulitolewa kwa vuguvugu la Uadventista, yaani watu wanaongojea ujio wa pili wa Yesu. Watu wenye elimu na vyeo waliungana na Miller, katika mambo yote mawili, yaani, kuhubiri na kuchapisha mafundisho yake, na kuanzia mwaka wa 1840 hadi 1844 kazi hii ilipanuka kwa haraka sana. [GC 335.1; PK Aya ya 46]

**Biblia Na Biblia Peke Yake**

William Miller alijaliwa na uwezo mkubwa wa akili iliyonidhamishwa na tafakari na kujifunza kwake Maandiko; juu ya hayo, aliongezea hekima ya mbinguni kwa kujiunganisha na Chanzo cha Hekima (Mungu Mith 1:7). Alikuwa mtu wa thamani kwa ajili ya uadilifu wake, na watu hawakusita kumpa heshima na sifa mahali popote pale ambapo unyofu wa tabia na ubora wa maadili vilithaminiwa. Alichanganya ukarimu na wema wa kweli utokao moyoni pamoja na unyenyekevu wa Kikristo na nguvu ya kujitawala nafsi, alikuwa msikivu na mwenye moyo wa kirafiki kwa wote, pia alikuwa tayari kusikiliza maoni ya wengine na kuzipima hoja zao. Bila hasira wala mihemko alizipima nadharia zote, na mafundisho yote ya dini kwa kutumia Neno la Mungu, na mpangilio wake mzuri wa hoja, pamoja na ujuzi wake mkubwa wa Maandiko vilimwezesha kuyapinga mafundisho yenye makosa na kuufichua uongo. [GC 335.2; PK Aya ya 47]

Hata hivyo, yeye hakufanya kazi yake bila kukabiliwa na upinzani mkali. Kama ilivyokuwa kwa wale Wanamatengenezo wa mwanzo waliotangulia, Kweli zile alizozihubiri hazikupokewa kwa upendeleo na waalimu wa dini maarufu na waliopendwa na watu wengi. Kwa kuwa watu hawa hawakuweza kutetea msimamo wao kwa kutumia Maandiko, walilazimika kutumia misemo na mafundisho ya dini yaliyotolewa na wanadamu kwa njia ya mapokeo ya Mababa au viongozi waliopita. Lakini Neno la Mungu lilikuwa ndio ushuhuda pekee uliokubaliwa na wahubiri wa Ukweli wa marejeo Yake Kristo. "Biblia, na Biblia peke yake," ilikuwa ndiyo kanuni na kaulimbiu yao. Kukosekana hoja zilizojengwa juu ya Maandiko kwa upande wa wapinzani wao kulifidiwa na dhihaka na dharau zao. Muda, mali na talanta vilitumiwa katika kuwachafua kwa kuwasema vibaya wale ambao kosa lao pekee lilikuwa ni kutazamia kwa furaha marejeo ya Bwana wao, tena walikuwa wakijitahidi kuishi maisha matakatifu na

kuwahimiza wengine ili wapate kujiandaa kwa ajili ya ujio Wake. [GC 335.3; PK Aya ya 48]

Juhudi kubwa zilitumiwa katika kuigeuzia mbali mioyo ya watu kuhusu fundisho lile la ujio wa mara ya pili. Hila zikafanywa ionekane kana kwamba kujifunza unabii uliohusiana na marejeo Yake Kristo na mwisho wa dunia ni dhambi, yaani, jambo ambalo watu wanapaswa kulionea haya. Hivyo ndivyo huduma ya wachungaji waliopendwa na watu wengi ilivyoihafifisha imani ya watu katika Neno la Mungu. Mafundisho yao yaliwafanya wanadamu wawe wapagani, na wengi wao walijipatia leseni ya kujiachia huru kuzifuata tamaa zao mbaya za mwili zinazopingana na Mungu. Kisha waasisi wa uovu ule waliwatupia lawama yote Waadventista (wale waliokuwa wanahubiri marejeo ya Bwana) kuwa ndio waliotenda maovu waliyoyaanzisha wao. [GC 336.1; PK Aya ya 49]

Ijapokuwa alikuwa akiwavuta wasikilizaji makini na wenye akili, na kuzijaza nyumba za mikutano, jina la Miller kwa nadra sana lilitajwa na vyombo vya habari vya kidini, isipokuwa kwa kusudi la kumdhihaki au kumpinga. Wasiojali na wasiomcha Mungu wakiwa wametiwa moyo na misimamo ya mafundisho ya waalimu wao wa dini, walitumia majina ya matusi ili kumdhihaki, misemo michafu ya kuchekesha, kumng’ong’a kwa dhihaka zenye makufuru, na juhudi za kumrundikia yeye pamoja na kazi yake ufidhuli. Mtu mzee mwenye mvi, aliyekuwa ameiacha nyumba yake nzuri yenye starehe na kusafiri kwa gharama zake mwenyewe kutoka jiji hadi jiji, kutoka mji hadi mji, akifanya kazi ngumu bila kupumzika, ili kutoa onyo zito la hukumu ya ulimwengu iliyokuwa imekaribia, wakamkenulia meno kwa kumng’ong’a na kumshutumu kama mtu aliye shupavu katika mambo ya dini isiyotumia akili na aliyepitiliza, mnafiki, tapeli na baradhuli mwenye kukisia-kisia tu mambo. [GC 336.2; PK Aya ya 50]

**Hamu Yazidi Kuongezeka**

Maneno ya dhihaka, uongo, na matusi yaliyorundikwa juu yake yalialika chuki na matamko makali kutoka katika vyombo vya habari visivyokuwa vya kidini. “Kulishughulikia fundisho hilo nyeti lenye utukufu mkuu mno kama huo na lenye matokeo ya kutisha,” kwa njia hiyo ya dharau na matusi kulitangazwa na watu wa kidunia kuwa sio tu “kuchezea hisia za wahubiri na watetezi wake,” bali “ni kuidhihaki siku ya hukumu yenyewe, ni kumdhihaki na kumdharau Mungu Mwenyewe, na kubeza utisho wa hukumu Yake.” - Bliss ukurasa wa 183. [GC 336.3; PK Aya ya 51]

Mwasisi na mchochezi wa maovu yote alitafuta, sio tu kufuta matokeo ya ujumbe ule wa marejeo Yake Kristo, bali kumwangamiza mjumbe mwenyewe. Miller alihubiri Ukweli wa Maandiko katika mioyo ya wasikilizaji wake, akizikemea dhambi zao na kusumbua kuridhika kwao, kwa kujiona kwamba wamejitosheleza, na maneno yake yaliyokata moja kwa moja, yaliamsha uadui

wao kwake. Upinzani ulioonyeshwa na washiriki wa kanisa dhidi ya ujumbe wake ulichochea ujasiri wa magenge ya wale wasiomcha Mungu kwenda mbali zaidi katika uovu wao; na wale maadui zake wakala njama ya kuyaondoa maisha yake mara tu atakapoondoka mahali pa mkutano. Lakini malaika watakatifu walikuwa katikati ya msongamano wa watu, na mmoja wao, akiwa katika umbile la mwanadamu, aliushika mkono wa mtumishi huyu wa Bwana na kumpeleka mahali pa usalama mbali na genge la watu wabaya, lenye hasira. Kazi yake ilikuwa bado haijamalizika, na Shetani pamoja na wajumbe wake walifadhaishwa katika kusudi lao. [GC 336.4; PK Aya ya 52]

Licha ya upinzani wote, shauku kubwa ya watu katika vuguvugu la Waadventista, yaani ujio wa Yesu kwa mara ya pili, iliendelea kuongezeka. Kutoka kwa makumi ya watu na kwenda kwenye mamia ya watu, makanisa yalikua kiasi cha kufikia maelfu mengi. Makundi makubwa ya watu yalikuwa yamefikiwa mara nyingi, na kuchukua msimamo wa kuunga harakati hizi, lakini baada ya muda fulani roho ya upinzani ilidhihirishwa hata dhidi ya waongofu hawa wapya, na makanisa yalianza kuchukua hatua za kinidhamu dhidi ya wale waliokuwa wameyapokea mafundisho ya Miller. Kitendo hiki kilisababisha Miller kujibu kwa njia ya kalamu yake, na akiwasiliana na Wakristo wa madhehebu yote, alisisitiza kwamba, kama mafundisho yake yalikuwa ya uongo, basi, anapaswa kuonyeshwa kosa lake kutoka katika Maandiko. [GC 337.1; PK Aya ya 53]

“Ni nini tunachokiamini sisi,” alisema, “ambacho hatukuagizwa au kuamriwa katika Neno la Mungu, Neno ambalo ninyi wenyewe mnakubali na kukiri kuwa ndiyo kanuni, na kanuni peke yake ya imani na matendo yetu? Ni kitu gani tumefanya ambacho mnatushambulia kwa shutuma kali kama hizo kutoka mimbarani na vyombo vya habari, na kuwapa haki ya kutuondoa sisi wahubiri wa ujio wa pili wa Yesu (Waadventista) katika makanisa yenu na ushirika wenu?” “Ikiwa sisi tumekosea, basi tunaomba mtuonyeshe kosa letu liko wapi. Tuonyesheni kutoka katika Neno la Mungu mahali ambapo sisi tumekosea; tumetukanwa vya kutosha; jambo hilo haliwezi kamwe kututhibitishia sisi kuwa tumekosea; Neno la Mungu pekee ndiyo linaweza kubadilisha mtazamo wetu. Hitimisho letu kwa jumla limefikiwa kwa tafakari na uangalifu mkubwa, pamoja na maombi ya dhati, kadri tulivyouona ushahidi katika Maandiko.” — Yoh.Ibid., ukurasa wa 250, 252. [GC 337.2; PK Aya ya 54]

### Kutokuamini Na Ukafiri

Tangu zama hadi zama (kizazi hadi kizazi), maonyo ambayo Mungu ameyatuma duniani kwa njia ya waja wake yamekutana na moyo mgumu,

mashaka na kutoamini. Wakati uovu wa watu wale walioishi kabla ya gharika ulipomfanya Mungu alete gharika ya maji juu ya dunia hii, kwanza aliwajulisha watu kusudi Lake, ili wapate fursa ya kugeuka na kuziacha njia zao mbaya. Kwa miaka mia moja na ishirini, sauti ya onyo la kuwataka watubu ilivuma masikioni mwao, ili ghadhabu ya Mungu isije ikadhihirishwa na kuwaletea maangamizi yao. Lakini ujumbe huo kwao ulionekana kama hekaya ya kufikirika, nao wala hawakuuamini. Wakiwa wamepata ujasiri katika uovu wao, walimdhihaki mjumbe wa Mungu, wakayadharau miito yake ya toba kwao, naam, hata wakamshtaki kwa kiburi chake cha makusudi au Imani bandia.* Inawezekanaje mtu mmoja kusimama kinyume na wote wenye mamlaka dunia nzima? Ikiwa ujumbe wa Nuhu ungekuwa wa kweli, kwa nini ulimwengu wote haukuuona, wala kuuamini? Yaani madai ya mtu mmoja yawe dhidi ya hekima ya maelfu! Hawakulitilia maanani onyo lile, wala hawakutaka kutafuta hifadhi ndani ya safina *(presumption). [GC 337.3; PK Aya ya 55]

Watu wenye dhihaka walisonda vidole vyao kuelekea mambo yanayoonekana kwenye maumbile ya asili, - yaani, kufuatana kusikobalika kwa misimu au majira, anga la kibluu ambalo lilikuwa halijapata kamwe kudondosha mvua, mimea yote ya kijani kibichi iliyoburudishwa na umande laini wa usiku, - kisha walipiga kelele kwa kusema: “Je, huyu hasemi kwa mafumbo kweli?” Kwa dharau walimtangaza mhubiri yule wa haki kuwa alikuwa mkereketwa wa dini isiyo na hekima na iliyopitiliza; kisha kwa hamu kubwa zaidi waliendelea kutafuta anasa zao, wakinuia kwenda katika njia za uovu zaidi kuliko hapo awali. Lakini kule kutokuamini kwao hakukuzuia tukio lililotabiriwa. Mungu aliwavumilia kwa muda mrefu kwa uovu wao, akiwapa nafasi ya kutosha kutubu; lakini, basi, kwa wakati ule ule uliopangwa hukumu Zake zilitekelezwa juu yao wale walioikataa rehema Yake. [GC 338.1; PK Aya ya 56]

### Mwisho Utakuja Ghafula

Kristo alisema kwamba kutakuwa na kutokuamini kama huko, kuhusiana na habari ya kuja Kwake mara ya pili. Kama vile watu wa siku za Nuhu ambao “hawatambua hata Gharika ikaja, ikawachukua wote; ndivyo,” kwa maneno Yake Mwokozi wetu, “kutakavyokuwa pia kuja Kwake Mwana wa Adamu.” Mathayo 24:39. Wakati wale wanaojiita watu wa Mungu watakapojichanganya na ulimwengu huu, na kuishi kama walimwengu wanavyoishi, na kujiunga nao katika anasa zile zilizokatazwa; wakati anasa za ulimwengu huu zinapokuwa ndiyo anasa za kanisa; wakati kengele za arusi zinapolia, na watu wote wanatarajia kuwa na miaka mingi ya mafanikio au ustawi wa ulimwengu huu katika siku zao mbeleni -- hapo ndipo, kwa ghafula kama vile umeme wa radi unavyomulika kutoka mbinguni, ndivyo utakavyokuja mwisho wa ndoto zao nzuri na matumaini yao yenye kuhadaa ndani yake. [GC 338.2; PK Aya ya 57]

Kama vile Mungu alivyomtuma mtumishi Wake kuuonya ulimwengu juu ya Gharika iliyokuwa inakuja, ndivyo alivyowatuma wajumbe Wake aliowachagua, kuwajulisha watu juu ya kukaribia kwa ile hukumu ya mwisho. Na kama vile watu walioishi kipindi kimoja na Nuhu walivyocheka na kudhihaki utabiri wa mhubiri yule wa haki, kadhalika katika siku zake Miller wengi, hata miongoni mwa watu waliodai kuwa watu wa Mungu, waliyadharau maneno ya onyo. [GC 339.1; PK Aya ya 58]

Na kwa nini mafundisho na mahubiri juu ya marejeo ya pili ya Kristo hayakupokelewa kwa furaha katika makanisa? Wakati marejeo Yake Bwana yanapoleta maafa na kilio kwa waovu, kwa wenye haki huleta shangwe na tumaini ndani yake. Ukweli huo mkuu umekuwa faraja kwa waaminifu wa Mungu katika zama zote; mbona basi ulikuja kama Mwasisi Wake, na kuwa "Jiwe likwazalo" na "mwamba uchukizao" kwa wale wanaodai kuwa watu Wake? Ni Mwokozi wetu Mwenye huruma, Ndiye aliyewaahidi wanafunzi Wake kwa kusema: "Nikienda na kuwaandalia mahali, nitakuja tena niwakaribishe Kwangu." Yohana 14:3. Alikuwa ni Mwokozi wetu Mwenye huruma, ambaye, akitarajia upweke na huzuni ya wafuasi Wake, aliwatuma malaika Zake wawafariji kwa kuwapa uhakikisho kwamba Yeye Mwenyewe atakuja tena (kimwili), naam, vilevile walivyomwona akienda mbinguni. Wanafunzi Wake walipokuwa wamesimama na kukaza macho yao kwa makini juu ili kumwona anavyotoweka Yule ambaye walimpenda, usikivu wao ulivutwa kwa maneno haya: "Enyi watu wa Galilaya, mbona mmesimama mkitazama mbinguni? Huyu Yesu aliyechukuliwa kutoka kwenu kwenda juu mbinguni, atakuja jinsi iyo hiyo mlivyomwona akienda Zake mbinguni." Matendo 1:1. Tumaini lao liliamshwa upya kwa ujumbe ule wa malaika. Wanafunzi "wakarudi Yerusalemu wenye furaha kuu. Nao walikuwa daima ndani ya hekalu, wakimsifu Mungu." Luka 24:52, 53. Hawakuwa wamefurahi kwa sababu Yesu alikuwa ametengwa mbali nao na kuwaacha wapambane na vishawishi na majaribu ya ulimwengu huu, bali walifurahi sababu ya uhakikisho uliotolewa kwao na malaika kwamba angerudi tena. [GC 339.2; PK Aya ya 59]

Utangazaji wa ujio wa Kristo unapaswa kuwa sasa, kama ulivyokuwa unafanywa na malaika kwa wachungaji wa kondoo wa Bethlehemu, habari njema ya furaha kuu. Wale wanaompenda Mwokozi kwa dhati, hawawezi kukosa kutulia au kushangilia kwa furaha tangazo hili lililojengwa juu ya msingi wa Neno la Mungu, lisemalo kuwa Yule ambaye Kwake matumaini yao ya uzima wa milele yanapatikana, anakuja tena, sio kuja kutukanwa, kudharauliwa,na kukataliwa na watu, kama alivyokuja mara Yake ya kwanza, bali katika uweza na utukufu kuwakomboa watu Wake. Ni wale wasiompenda Mwokozi, ndio ambao wanataka Yeye aendelee kubaki mbali nao, au asije, wala hapawezi kuwapo na ushahidi unaohitimisha mambo zaidi zaidi ya huu, kuwa makanisa yamemwacha Mungu

kuliko maudhi na uadui wao unaoamshwa na ujumbe huu uliotumwa kutoka mbinguni. [GC 339.3; PK Aya ya 60]

Watu waliolipokea fundisho lile la marejeo ya Kristo, waliamshwa na kuona umuhimu wa kuwa na toba na unyenyekevu mbele Zake Mungu. Wengi, kwa muda mrefu, walikuwa wakimanga-manga kati ya Kristo na ulimwengu; sasa walihisi kwamba wakati ulikuwa umewadia wa kuwa na msimamo wao. "Masuala ya umilele yakajitokeza kwao kwa namna isiyokuwa ya kawaida na kuwa mambo yenye uhakika na uhalisia usio na kifani. Mbingu ikajisogeza karibu nao, nao wakajisikia kwamba walikuwa na hatia mbele Zake Mungu." - Bliss, ukurasa wa 146. Wakristo walihuishwa na kuishi maisha mapya kiroho. Wakaongozwa kuona kwamba muda ulikuwa mfupi, kwamba kile walichopaswa kukifanya kwa ajili ya wanadamu wenzao kilikuwa hakina budi kifanyike haraka. Dunia ilitokomea machoni pao, umilele ulionekana kana kwamba unafunguka mbele yao na mioyoni mwao, pamoja na yale yote yaliyohusu umilele wake (mema) na (mabaya), mambo hayo yalionekana kuwa yamefunika kila mambo ya kidunia. Roho wa Mungu alitua juu yao na kuyapa uwezo maneno yao walipotoa miito ya bidii kwa ndugu zao, na kwa wenye dhambi, ili wapate kujiandaa kwa siku ile ya Mungu. Ushuhuda wa kimya wa maisha yao ukawa ni kemeo la kudumu kwa washiriki wa kanisa waliofuata mazoea tu na ambao walikuwa hawajajiweka wakfu. Hao hawakutaka kusumbuliwa katika pilikapilika zao za kuzitafuta anasa, kutumia muda wao wote katika kutafuta fedha, na tamaa yao kuu ya kupata heshima ya ulimwengu. Kwa sababu hiyo uadui na upinzani wao uliamshwa dhidi ya imani ile ya marejeo ya Kristo na wale waliotangaza imani hiyo. [GC 340.1; PK Aya ya 61]

Kwa kadri hoja zilizotolewa kuhusu vipindi vya kiunabii zilivyoonekana kuwa haziwezi kupingwa, wapinzani walijitahidi kuwavunja watu moyo ili wasiendelee kulichunguza somo hili, kwa kuwaambia watu kwamba masomo haya ya unabii yalikuwa yametiwa muhuri (yamefungwa). Hivyo ndivyo Waprotestanti walivyofuata katika nyayo za Waroma. Wakati Kanisa la kipapa lilikuwa linazuia Biblia isisomwe na watu (tazama kiambatisho) Makanisa ya Kiprotestanti yalitoa madai yao kwamba sehemu ya muhimu ya Neno Takatifu - Hususani Ukweli wa wakati wetu-- isingeweza kueleweka. [GC 340.2; PK Aya ya 62]

Wachungaji pamoja na walei wakatangaza kwamba unabii wa Danieli na Ufunuo ulikuwa na mafumbo na siri zisizoweza kueleweka. Lakini Kristo aliwaelekeza wanafunzi wake kwenye Maneno ya nabii Danieli kuhusu matukio yale ambayo yangetokea katika nyakati wao akisema: "Asomaye na afahamu." Mathayo 24:15. Na yale madai yao kwamba kitabu hicho cha Ufunuo ni siri au mafumbo, yaani, hakiwezi kueleweka, yanapingwa na kichwa chenyewe hasa cha kitabu hicho, kisemacho: "Ufunuo wa Yesu Kristo, aliopewa na Mungu awaonyeshe watumwa Wake mambo ambayo kwamba hayana budi kuwako

upesi.... Heri asomaye na wao wayasikiao maneno ya unabii huu, na kuyashika yaliyoandikwa humo; kwa maana wakati u karibu." Ufunuo 1:1-3. [GC 341.1; PK Aya ya 63]

**Kitabu Kilichofunuliwa**

Asema hivi huyo nabii: "Heri asomaye" - wako wale ambao hawatasoma, mbaraka huo si kwa ajili yao; (haiwahusu wasiosoma). "Na wao wasikiao" - wako baadhi pia wanaokataa kusikiliza chochote kinachohusiana na unabii huo; mbaraka huo haujakusudiwa kwa ajili ya tabaka hilo. "Na kuyashika yaliyoandikwa humo" - wengi wanakataa kuyasikia maonyo na mafundisho yaliyomo katika kitabu hicho cha Ufunuo; hakuna hata mmoja miongoni mwao awezaye kudai mbaraka huo ulioahidiwa. Wale wote wanaodhihaki mafundisho haya ya unabii na kuicheka mifano iliyotolewa humo na Mungu, yaani, wote wanaokataa kufanya matengenezo ya mitindo yao ya maisha na kujiandaa kwa ajili ya marejeo ya Mwana wa Adamu, hawatabarikiwa. [GC 341.2; PK Aya ya 64]

Katika kuzingatia ushuhuda huo wa Maandiko ya uvuvio, watu wanathubutuje basi, kufundisha kuwa kitabu cha Ufunuo ni mafumbo ya siri yasiyoweza kueleweka kwa wanadamu? Kitabu cha Ufunuo ni siri ambayo imefunuliwa (ni wazi), hicho ni kitabu ambacho kimefunuliwa, yaani kinapaswa kueleweka. Mafundisho ya kitabu cha Ufunuo huelekeza mawazo kwenye unabii wa Danieli, na vitabu vyote viwili huleta mafundisho ya muhimu sana ambayo Mungu amewapa binadamu kuhusu matukio yale yatakayotokea karibu na kufungwa kwa historia ya ulimwengu huu. [GC 341.3; PK Aya ya 65]

Yohana alifunuliwa mandhari ya kina na kusisimua mno kuhusu habari zinazohusu uzoefu utakaoilapata kanisa. Aliona hali ile itakayowakabili, hatari, mapambano, na ukombozi wa mwisho wa watu wa Mungu katika picha za matukio haya aliyoonyeshwa. (Ufu. 12:17,11; 13:7, 15-17; Dan. 7:21, 22, 25-28). Aliandika ujumbe wa kufungia utakaosaidia kukomaza mavuno ya nchi, ama kama miganda ya nafaka safi itakayowekwa ndani ya ghala la mbinguni, ama kama matita ya vijiti vitakavyokuwa tayari kuchomwa katika mioto ile ya maangamizi. Masomo ya muhimu sana yalifunuliwa kwake, hasa kwa ajili ya kanisa la mwisho, na kuwa wale ambao walitakiwa kuacha makosa na na kuushikilia Ukweli kwa bidii wafundishwe kuhusu hatari zile kubwa pamoja na migogoro iliyo mbele yao. Hakuna hata mtu mmoja ambaye anatakiwa kuwa gizani kuhusu kile kinachoujia ulimwengu huu. [GC 341.4; PK Aya ya 66]

Kwa nini, basi, uwepo ujinga huo ulioenea kote kuhusu sehemu hiyo muhimu ya Maandiko Matakatifu? Mbona watu wengi wanasitasita na kuwa wazito kuyachunguza mafundisho yake? Hakika hayo ndiyo matokeo ya juhudi kubwa ya yule mkuu wa giza, aliyoyafanyia utafiti na kuyafanya kwa makusudi ili awafiche wanadamu kile kinachoyaweka madanganyo yake peupe. Kwa sababu hiyo,

Kristo, Mwenye huo Ufunuo, yaani mfunuaji, alipoona mapema vita ile ambayo itakayopiganwa dhidi ya mafundisho ya kitabu hicho cha Ufunuo, alitamka mbaraka wake juu ya watu wote wanaokisoma, wanaokisikia, wanaokichunguza na kuyatenda maneno ya unabii wa kitabu cha Ufunuo (Ufunuo 1:3). [GC 342.1; PK Aya ya 67]

*Imani za kimsingi za theolojia zote za Deist ni kwamba Mungu Yupo na aliumba ulimwengu, lakini akauacha ili ujiendeshe wenyewe, kwamba hana shauku nao sana, Biblia kwao si mafunuo ya Mungu muhimu na siyo chanzo cha mafundisho ya dini.

*Biblia ni Ramani: Biblia ina mawazo ya Mungu, hali ya mwanadamu, njia ya wokovu, adhabu ya wenye dhambi, na furaha ya waumini. Mafundisho yake ni matakatifu, maagizo yake ni ya lazima, historia yake ni Kweli, na maamuzi yake hayabadiliki. Isome ili uwe na hekima, iamini uwe salama, na uifanye kuwa takatifu.

Ina mwanga wa kukuelekeza, chakula cha kukusaidia, na faraja ya kukuchangamsha. Ni ramani ya msafiri, fimbo ya msafiri, dira ya rubani, upanga wa askari na hati ya Mkristo. Hapa pia, Mbingu inafunguliwa na milango ya Kuzimu yanafichuliwa. Kristo Ndiye somo lake kuu, akili ya mwanadamu inakuwa na karamu kuu ya kuyafaidi Maandiko na kudai ahadi zaidi ya 3500. Kitabu hiki kinatusadia kumpa Mungu utukufu unaomstahili. Biblia inapaswa kujaza kumbukumbu, kutawala moyo, na kuongoza miguu. Isome polepole, kila siku, ukiimungunya kwa sala. Ni mgodi wa mali, paradiso ya utukufu, na mto wa raha. Umepewa maishani, itafunguliwa kwenye hukumu, na itakumbukwa na kujifunzwa milele. Inahusisha wajibu wa juu zaidi, huthawabisha kazi kubwa zaidi, na itawashutumu wale wote wanaocheza na yaliyo matakatifu humo. Ni kitabu cha kutubadilisha maisha, na kutusaidia tuweze kuwa mbinguni Yohana 17:3.

# SURA YA 19

# NURU KUPITIA GIZANI

## (Usiku Wenye Huzuni)

Ufupisho: Mara nyingi kuna kilio wakati wa giza au shida ila asubuhi inakuja. Kwa wale wanaogundua Fundisho kuu la Marejeo ya Bwana, watapata changamoto za kukatishwa tamaa, ila fungeni mkanda, asubuhi inakuja, hebu tupeane moyo kwa Maneno ya Yohana 14:1-3.

Kazi ya Mungu duniani humu, kutoka zama/kizazi hadi zama/kizazi, Ina mfanano wa kushangaza sana katika kila matengenezo makubwa au vuguguvu za mafanikio ya kiroho/kidini. Kanuni za jinsi Mungu anavyoshughulika na wanadamu daima ni zile zile. Matukio muhimu ya yanafana na matukio yaliyofanyika wakati uliopita, na uzoefu wa kanisa zama zilizopita una masomo yenye thamani kubwa kwa wakati wetu wa sasa. [GC 343.1; PK Aya ya 1]

Hakuna Ukweli ambao umefundishwa kwa uwazi zaidi katika Biblia kuliko ule usemao, Mungu kwa njia ya Roho Wake Mtakatifu, anawaongoza watumishi Wake duniani kwa njia ya kipekee, kuhusika katika vuguvugu kubwa la kupeleka mbele kazi ya wokovu. Wanadamu ni vyombo vilivyo mkononi Mwake Mungu, ambavyo hutumiwa Naye ili kutimiza makusudi Yake ya neema na rehema. Kila mmoja ana sehemu yake ya kutenda; Kila mmoja amepewa kiasi fulani ya kipimo cha nuru, kinachokidhi mahitaji ya wakati wake anaoishi, na ambacho kinatosha kumwezesha kufanya kazi ambayo Mungu amempa aifanye. Lakini hakuna mtu, hata kama awe amepewa na mbingu heshima kubwa kiasi gani, ambaye amewahi kupata uelewa kamili wa Mpango Mkuu wa Ukombozi, au hata kulithamani kusudi la Mungu kwa ukamilifu katika kazi kwa wakati wake wote mwenyewe kwa kipindi anachoishi. Wanadamu hawaelewi kikamilifu kile ambacho Mungu angetimiza kupitia kazi ambayo amewapatia kuifanya; hawaelewi kwa kinagaubaga yote yahusishayo ujumbe ule ambao wanautangaza kwa Jina Lake. [GC 343.2; PK Aya ya 2]

"Je! Wewe waweza kuuvumbua ukuu wa Mungu? Je, waweza kuufikilia upeo wa huyo Mwenyezi- kwa kufanya utafiti?" "Maana mawazo Yangu si mawazo yenu, wala njia zenu si njia Zangu; asema Bwana. Kwa maana kama vile mbingu zilivyo juu sana kuliko nchi, kadhalika njia Zangu zi juu sana kuliko njia zenu, na mawazo Yangu kuliko mawazo yenu." "Mimi ni Mungu, wala hapana aliye kama Mimi; nitangazaye mwisho tangu mwanzo, na tangu zamani za kale mambo yasiyotendeka bado." Ayubu 11:7; Isaya 55:8, 9; 46:9, 10. [GC 343.3; PK Aya ya 3]

Hata wale manabii ambao walipata upendeleo  wa  kwa kupewa nuru ya pekee ya Roho, hawakuelewa  kikamilifu maana yote, ya mafunuo yaliyotolewa kwao. Maana ya ujumbe wao, ulikusudiwa kufunuliwa kutoka kizazi hadi kizazi, kwa kadri ambavyo watu wa Mungu wanahitaji yale mafundisho yaliyomo katika ujumbe huo. [GC 344.1; PK Aya ya 4]

Petro, akiandika Habari ya wokovu  uliofunuliwa kwa njia kupitia nuru ya injili, anasema: Kuhusu habari ya wokovu huo "manabii walitafuta-tafuta na kuchunguza-chunguza, ambao walitabiri habari za neema itakayowafikia ninyi. Wakatafuta ni wakati upi, na wakati wa namna gani ulioonywa na Roho wa Kristo aliyekuwa ndani yao, ambaye alitangulia kuyashuhudia mateso yatakayompata Kristo, na utukufu utakaokuwako baada ya hayo.Wakafunuliwa ya kuwa si kwa ajili yao wenyewe, bali kwa ajili yetu walihudumu katika mambo hayo." 1 Petro 1:10-12. [GC 344.2; PK Aya ya 5]

Hata hivyo ingawa manabii hawakupewa uwezo wa kuelewa kikamilifu kila kitu kilichofunuliwa kwao, walitafuta-tafuta na kuchunguza-chunguza kwa bidii kupata nuru yote ambayo Mungu alipenda kuwafunulia. "Walichunguza na kutafakari kwa bidii," "Walitafuta ni wakati upi, au ni aina gani ya kipindi, Roho wa Kristo aliyekuwa ndani yao aliridhia." Ni somo kubwa kiasi gani, kwa watu wa Mungu wa kizazi cha Kikristo, ambao kwa faida yao unabii huu ulitolewa kwa ajili ya watumishi Wake! "Wakafunuliwa ya kuwa si kwa ajili yao wenyewe, bali walihudumu kwa mambo hayo kwa ajili yetu." Shuhudia basi, jinsi watu hao watakatifu wa Mungu "walipouliza-uliza na kuchunguza-chunguza kwa bidii" kuhusiana na mafunuo yale waliyopewa kwa ajili ya vizazi ambavyo vilikuwa bado havijazaliwa. Hebu linganisha bidii yao takatifu na uzembe au kupuuzia kabisa, ambako watu waliopendelewa wa vizazi vya baada ya hapo wanachukulia karama hii ya Mbinguni. Karipio kubwa kiasi gani kwa kutojali na kwa watu wanaopenda starehe, wanaopenda ulimwengu, ambao wanaridhika kusema kuwa unabii huo hauwezi kueleweka! [GC 344.3; PK Aya ya 6]

### Kukata Tamaa Kwa Wanafunzi Wake

Ingawa akili finyu za wanadamu hazikidhi kuingia katika mashauri ya Yule Asiye na kikomo, au kuelewa kikamilifu utendaji-kazi wa makusudi Yake, lakini mara nyingi ni kwa sababu kuna makosa fulani au kupuuzia kwa upande wao wenyewe, kiasi kwamba wanashindwa kuuelewa vizuri ujumbe huo utokao Mbinguni. Siyo mara chache akili za wanadamu, na hata za watumishi wa Mungu, hupofushwa mno kwa maoni, mapokeo na mafundisho ya uongo ya wanadamu, kiasi kwamba wanaweza kuyaelewa kwa sehemu ndogo tu mambo hayo makuu ambayo Mungu ameyafunua katika Neno Lake. Hivyo ndivyo walivyokuwa wanafunzi Wake Kristo, hata wakati ule Mwokozi alipokuwa pamoja nao ana kwa ana yaani kimwili. Mawazo yao yalikuwa yamegubikwa na dhana maarufu

zilizopendwa na watu wengi kumhusu Masihi kwamba angekuwa mfalme wa dunia hii ya muda mfupi, ambaye angeiinua Israeli juu na kuwaketisha kwenye kiti cha himaya ya ulimwengu wote, wala hawakuweza kuielewa maana ya Maneno Yake yaliyotabiri habari ya mateso na kifo Chake. [GC 344.4; PK Aya ya 7]

Kristo Mwenyewe alikuwa amewatuma wakatangaze ujumbe huu: “Wakati umetimia, na ufalme wa Mungu umekaribia; tubuni, na kuiamini Injili.” Marko 1:15. Ujumbe huu ulikuwa umejengwa juu ya unabii wa Danieli 9. Majuma sitini na tisa yalitangazwa na malaika kuwa yangeishia wakati wa “Masihi aliye Mfalme mkuu,” na kwa matumaini makubwa na matarajio yaliyojaa furaha wanafunzi walingojea kuanzishwa kwa ufalme wa Masihi pale katika jiji la Yerusalemu ili kuitawala dunia yote. [GC 345.1; PK Aya ya 8]

Walihubiri ujumbe ambao Masihi alikuwa amewakabidhi, ingawa hata wao wenyewe hawakuelewa maana ya ujumbe waliouhubiri. Wakati hubiri lao lilikuwa na msingi wake katika Danieli 9:25, hawakuweza kuona mstari ule unaofuata wa sura hiyo hiyo, kwamba huyo Masihi angekatiliwa mbali (angeuawa kikatili). Tangu kuzaliwa kwao mioyo yao ilikuwa imeelekezwa juu ya utukufu uliotazamiwa wa ufalme wa dunia hii, na matarajio hayo yalipofusha ufahamu wao kwa namna ile ile moja kuhusu maelezo bayana ya unabii pamoja na Maneno Yake Kristo. [GC 345.2; PK Aya ya 9]

Walitekeleza majukumu yao ya kulitangazia taifa la Wayahudi mwaliko wa rehema, na ndipo, wakati ule ule hasa waliotarajia kumwona Bwana wao akitawazwa ili kukikalia kiti cha enzi cha Daudi, walimwona akikamatwa kwa nguvu kama mhalifu, akipigwa kwa mijeledi, akidhihakiwa, na kuhukumiwa kuuawa, na kuning’inizwa juu ya msalaba wa Kalwari. Ni kukata tamaa na uchungu mkubwa kiasi gani ulinyonga mioyo ya wanafunzi wale katika kipindi cha siku tatu wakati Bwana wao alipokuwa amelala kaburini! [GC 345.3; PK Aya ya 10]

Kristo alikuwa amekuja wakati mahsusi na kwa njia iliyotabiriwa na unabii. Ushuhuda wa Maandiko ulikuwa umetimizwa katika kila kipengele cha huduma Yake. Alikuwa ameuhubiri ujumbe wa wokovu, na “Neno Lake lilikuwa na mamlaka.” Mioyo ya wasikilizaji Wake ilikuwa imeshuhudia kwamba ujumbe Wake ulikuwa umetoka mbinguni. Utume wa Kiungu wa Kristo ulithibithishwa na Neno pamoja na Roho wa Mungu. [GC 346.1; PK Aya ya 11]

### Kutokuwa Na Hakika Na Mashaka

Wanafunzi walidumu kumng’ang’ania Bwana wao mpendwa kwa upendo usio na kifani. Lakini mawazo yao yaligubikwa na kutokuwa na uhakika na mashaka. Katika uchungu wao uliowapata wakati ule hawakuweza kuyakumbuka Maneno

Yake Kristo yaliyoelekeza mbele kwenye mateso na kifo Chake. Ikiwa Yesu wa Nazareti alikuwa Ndiye Masihi kweli, wanafunzi Wake wangekuwa wametumbukia katika majonzi na kukatishwa tamaa kwa kiwango kile? Hilo ndilo swali hasa lililoitesa mioyo yao wakati Mwokozi wao alipokuwa amelala kaburini Mwake katika saa zisizokuwa na matumaini za Sabato iliyoingia katikati ya kifo Chake na kufufuka Kwake. [GC 346.2; PK Aya ya 12]

Ingawa usiku wa huzuni yao, ulikusanya giza, nalo likawazunguka pande zote wafuasi hawa wa Yesu, hata hivyo hawakuwa wametelekezwa. Nabii anasema: “Nikaapo gizani Bwana atakuwa nuru kwangu. Atanileta nje kwenye nuru, nami nitaiona haki Yake”. “Giza nalo halikufichi kitu, Bali usiku huangaza kama mchana; Giza na mwanga Kwako ni sawasawa.” Mungu amenena hivi: “Nuru huwazukia wenye adili gizani” “Nitawaleta vipofu katika njia wasiyoijua; katika mapito wasiyoyajua nitawaongoza; nitafanya giza kuwa nuru mbele yao, na mahali palipopotoka kuwa pamenyooka. Haya nitatenda, wala sitawaacha.” Mika 7:8, 9; Zaburi 139:12; 112:4; Isaya 42:16. [GC 346.3; PK Aya ya 13]

Tangazo la injili lililokuwa limetolewa na wanafunzi katika Jina la Bwana lilikuwa sahihi, na hata kwa vipengele vyote vya matukio ambavyo vilisonda kidole kwenye tangazo lile, hata wakati huo yalikuwa yakitendekea. “Wakati umetimia, ufalme wa Mungu umekaribia,” ulikuwa ndio ujumbe wao. Mwishoni mwa “wakati huo”,majuma sitini na tisa ya Danieli 9, ambayo yangeishia wakati wa Masihi, “Mpakwa- Mafuta”, Kristo alipokea upako wa Roho baada ya kubatizwa Kwake na Yohana katika Yordani. Na “ufalme wa Mungu” ambao waliokuwa wametangaza kuwa umekaribia ulianzishwa na kifo cha Kristo. Ufalme huu haukuwa, kama walivyofundishwa kuamini, milki ya kidunia. Wala haukuwa ufalme ule wa milele wa baadaye ambao hautasimikwa mpaka wakati ambapo “ufalme na mamlaka, na ukuu wa ufalme, chini ya mbingu zote, watapewa watu wa watakatifu Wake Aliye juu; ufalme Wake ni ufalme wa milele, ambamo “mamlaka zote zitamtumikia na kumtii.” Danieli 7:27. Kama ulivyotumika katika Biblia, usemi huu “ufalme wa Mungu” unatumika kuonyesha falme zote mbili, yaani, ufalme wa neema na ufalme wa utukufu. Ufalme wa neema unaonyeshwa na Paulo katika Waraka wake kwa Waebrania. Baada ya kuelekeza kwa Kristo, mwombezi Mwenye huruma ambaye “anaguswa na hisia za udhaifu wetu,” mtume anasema hivi: “Basi na tukikaribie kiti cha neema kwa ujasiri, ili tupewe rehema, na kupata neema.” Waebrania 4:15, 16. Kiti cha Neema huwakilisha ufalme wa neema; maana kule kuwako kwa kiti cha enzi kunamaanisha kuwako kwa ufalme. Katika mifano Yake mingi, Kristo anatumia usemi huu “ufalme wa mbinguni” kuonyesha kazi ya neema ya Mungu katika mioyo ya wanadamu. [GC 346.4; PK Aya ya 14]

Kwa hiyo kiti cha enzi cha utukufu huwakilisha ufalme wa utukufu; na ufalme huu unarejelewa katika Maneno ya Mwokozi: “Hapo atakapokuja Mwana wa

Adamu katika utukufu Wake, na malaika watakatifu wote pamoja Naye, ndipo atakapoketi katika kiti cha utukufu Wake; na mataifa yote yatakusanywa mbele Zake." Mathayo 25:31, 32. Ufalme huu bado ni wa wakati ujao, upo mbeleni. Hauwezi kusimikwa mpaka hapo Kristo atakapokuja mara ya pili. [GC 347.1; PK Aya ya 15]

**Nuru Kupitia Giza**

Ufalme wa neema ulianzishwa mara tu baada ya anguko la mwanadamu, wakati mpango wa wokovu ulipobuniwa kwa ajili ya kumkomboa mwanadamu mwenye hatia. Tangu hapo, mpango huo uliendelea kuwepo katika kusudi na ahadi Yake Mungu (Mwanzo 3:15); na kwa njia ya imani, jamii ya wanadamu waliweza kuwa raia wa ufalme huo. Hata hivyo, mpango wenyewe wa neema haukuanzishwa mpaka baada ya kifo Chake Kristo. Hata baada ya Yeye kuanza utume Wake hapa duniani, Mwokozi akiwa amechoshwa na ukaidi na utovu wa shukrani wa wanadamu, angeweza kurudi nyuma, yaani kujiondoa asiweze kuitoa kafara Yake pale Kalvari. Akiwa katika bustani ya Gethsemane, kikombe cha huzuni na mateso mengi kilitetemeka mkononi Mwake. Hata wakati huo angeweza kupangusa jasho Lake la damu kutoka katika kipaji cha uso Wake na kuiacha jamii ya wanadamu wenye hatia ipate kuangamia katia uovu wake. Kama angalikuwa amefanya hivyo, basi, kusingekuwako ukombozi wowote wa wanadamu walioanguka dhambini. Lakini Mwokozi aliposalimisha uhai Wake, na kuvuta pumzi Yake ya mwisho, na kukata roho, alipolia kwa sauti kuu akisema, "Imekwisha," (Tetelestai!) hapo ndipo utimilifu wa mpango wa ukombozi ulipokuwa umethibitika kikamilifu. Ahadi ya wokovu (Mwa. 3:15) iliyotolewa kwa jozi ya kwanza ya wanadamu (wenzi), mume na mkewe waliokuwa wadhambi katika bustani ya Edeni, ilikuwa imethibitishwa. Ufalme wa neema, ambao kabla ya hapo ulikuwepo kwa njia ya ahadi ya Mungu, ukawa umesimikwa rasmi tangu wakati ule wa kifo Chake. [GC 347.2; PK Aya ya 16]

Hivyo basi, Kifo Chake Kristo--tukio lile ambalo wanafunzi walikuwa wameliona kama mwisho wa tumaini lao --ndilo lililofanya tumaini lao kuwa la hakika milele. Ingawa lilikuwa limewakatisha tamaa kwa uchungu na kwa ukatili, lilikuwa kilele cha uthibitisho ulioonyesha kwamba imani yao ilikuwa sahihi. Tukio lile ambalo lilikuwa limewajaza huzuni/maombolezo na kukata tamaa, ndilo lililoufungua mlango wa matumaini kwa kila mtoto wa Adamu, na hilo ndilo kitovu cha maisha ya baadaye pamoja na furaha ya milele ya watu wa Mungu walio waaminifu katika vizazi vyote. [GC 348.1; PK Aya ya 17]

Makusudi ya rehema isiyo na kikomo, yaani ya milele, yalikuwa yamefikia utimilifu wake, naam, licha ya kukatishwa tamaa kwa wanafunzi Wake. Pamoja na mioyo kuwa imeongolewa na neema ya Mungu na nguvu ya mafundisho Yake, Yeye ambaye "alinena kwa namna ambayo kamwe mtu yeyote hakuwahi kuongea

kama Yeye," Lakini, dhahabu safi ya upendo wao kwa Yesu, ilichanganyika pamoja na madini hafifu yenye thamani ndogo na yasiyo safi ya kiburi chao na uchoyo wao wa kutaka makuu. Hata katika chumba kile walicholia Pasaka, wakati wa saa ile muhimu na ya kutisha, wakati Mwokozi alipokuwa tayari kuingia katika kivuli cha Gethsemane, palitokea "na mashindano miongoni mwao, juu ya nani miongoni mwao alikuwa mkuu kuliko wote." Luka 22:24. Maono yao yalisheheni kiti cha enzi, taji, na utukufu, huku mbele yao walikabiliwa na aibu na uchungu wa bustanini Gethsemane, ukumbi wa hukumu, msalaba wa Kalvari. Ni kiburi kilichokuwa ndani ya mioyo yao, yaani, kiu ya kutaka kuwa na utukufu wa dunia hii, ndivyo vilivyowafanya kuyakumbatia mno mafundisho yale ya uongo, ya wakati wao, na kushindwa kuyazingatia Maneno aliyosema Mwokozi, akiwaonyesha jinsi ufalme Wake katika uhalisia wake hasa, na kuwaelekeza mbele kwenye mateso Yake makali na kifo Chake. Na makosa haya yaliwasababishia majaribu yao-- makali ila yaliyokuwa na ulazima--ambayo yaliruhusiwa kuwapata ili wapate kujisahihisha. Ingawa wanafunzi walikuwa wamekosea kuelewa maana ya ujumbe wao, tena walikuwa wameshindwa kuyatambua matarajio yao, hata hivyo, walikuwa wamelihubiri lile onyo walilopewa na Mungu, na Bwana aliwazawadia thawabu kwa imani yao, Naye aliheshimu utii wao. Kwao ilikabidhiwa kazi ya kuitangaza kwa mataifa yote injili tukufu ya Bwana wao aliyefufuka. Ilikuwa ni kusudi la kuwaandaa katika kazi hii, ndiyo maana uzoefu huu uliruhusiwa kuwapata, jambo ambalo kwao lilionekana kuwa chungu mno. [GC 348.2; PK Aya ya 19]

### Imani Iliyojengwa Juu Ya Akili

Baada ya Ufufuo Wake, Yesu aliwatokea wakiwa njiani kwenda Emau, Naye "akianza kutoka Musa na manabii wote, aliwaeleza katika Maandiko yote mambo yaliyomhusu Yeye Mwenyewe." "Luka 24:27 Mioyo ya wanafunzi iliwaka moto ndani yao. Imani imani yao iliwashwa moto upya tena. Wakawa "Wamezaliwa upya tena katika tumaini lenye uzima" (1 Pet. 1:3) hata kabla ya Yesu kujidhihirisha kwao. Ilikuwa kusudi Lake kuangazia ufahamu wao na kuimarisha imani yao juu ya "Neno la hakika la unabii." Alitamani kwamba Ukweli upate kuotesha chini mizizi yake imara ndani ya mioyo yao, sio tu kwa sababu uliungwa mkono kwa ushuhuda Wake binafsi alioutoa, bali kwa sababu ya ushahidi usio na maswali; ulioonyeshwa kwa mifano na vivuli vya ile Sheria ya Kafara/kaida* na kwa njia ya unabii wa Agano la Kale. Ilikuwapo haja kwa wafuasi Wake Kristo ya kuwa na imani iliyojengwa juu ya akili, imani iliyoelimisha, na sio kwa ajili yao wenyewe tu, bali kwamba waweze kupeleka elimu hii ya injili ya kumjua Kristo kwa ulimwengu mzima. Na kama hatua ya kwanza kabisa ya kutoa maarifa haya, Yesu aliwaelekeza wanafunzi kwa "Musa na manabii wote" (Agano la Kale lote). Huo ulikuwa ndio ushuhuda uliotolewa na Mwokozi Yule aliyefufuka kuonyesha

faida, thamani na umuhimu wa Maandik ya Agano la Kale. *(Typical or Ceremonial Law) [GC 349.1; PK Aya ya 20]

**Mashaka Yageuka Kuwa Hakika**

Ni badiliko kubwa kiasi gani lililotokea mioyoni mwa wanafunzi walipoutazama tena kwa mara nyingine, uso mpendwa wa Bwana wao! Luka 24:32. Kwa maana sahihi na kamilifu zaidi kuliko hapo awali walikuwa "wamemwona Yeye, ambaye Musa katika torati na manabii, waliandika habari Zake." Kutokuwa na uhakika kwa ajili ya mashaka yao, uchungu, kukata tamaa kwao viligeuka na badala yake uhakika kamili, na imani isiyo na mawingu, vilitawala. Hakuna cha ajabu kuona kwamba baada ya kupaa Kwake "walidumu ndani ya hekalu sikuzote, wakimsifu na kumtukuza Mungu." Watu, wakijua tu kifo cha aibu na kutisha cha Mwokozi, walitazamia kuona katika nyuso zao, dalili za huzuni, kuchanganyikiwa na kushindwa; Lakini waliona uchangamfu, shangwe na ushindi. Wanafunzi hao walikuwa wamepokea maandalizi makubwa kiasi gani waliyopewa wanafunzi hawa ajili ya kazi iliyo mbele yao! Walikuwa wamepita katika maumivu na majaribu makali mno yaliyowezekana kwao kuyaonja, nao walikuwa wameona jinsi Neno la Mungu lilivyokuwa limetekelezwa kwa ushindi mkuu, ambapo, kwa macho ya kibinadamu, wakati ule mambo yote yalionekana kuwa yameshindikana. Kuanzia wakati ule kwenda mbele ni kitu gani kingeweza kuiyumbisha imani yao au kupooza usongo wa upendo wao kwa Bwana? Katika huzuni kubwa zaidi walikuwa na "faraja iliyo imara," tumaini ambalo lilikuwa kama "nanga ya roho, yenye salama, yenye nguvu." Waebrania 6:18,19. Walikuwa wamekuwa mashahidi wa hekima na uweza Wake Mungu, nao walikuwa "Wamekwisha kujua kwa hakika ya kwamba, wala malaika, wala wenye mamlaka, wala yaliyopo, wala yatakayokuwapo, wala wenye uwezo, wala yaliyo juu, wala yaliyo chini, wala kiumbe kinginecho chote, hakitaweza kuwatenga mbali na "upendo wa Mungu ulio katika Kristo Yesu Bwana wetu." "Lakini katika mambo hayo yote," walisema, "tunashinda, na zaidi ya kushinda, kwa Yeye aliyetupenda." "Katika mambo hayo yote," walisema, "Sisi ni zaidi ya washindi katika Yeye aliyetupenda." Warumi 8:38, 39, 37. "Bali Neno la Bwana hudumu milele." 1 Petro 1:25. Na "ni nani atakayewahukumia adhabu? Kristo Ndiye aliyekufa, naam na zaidi ya hayo amefufuka katika wafu, Naye Yuko mkono wa kuume wa Mungu, tena Ndiye anayetuombea (anatutetea)." Warumi 8:34. [GC 349.2; PK Aya ya 21]

Asema hivi Bwana: "Watu Wangu hawatatahayari kamwe." Yoeli 2:26. "Kilio huja kukaa usiku, Lakini asubuhi huwa furaha." Zaburi 30:5. Wanafunzi walipokutana na Mwokozi wao siku ya ufufuo Wake, na mioyo yao ilipowaka ndani yao walipokuwa wakiyasikiliza maneno Yake; walipotazama kichwa, mikono na nyayo Zake zilizokuwa zimejeruhiwa kwa ajili yao; Yesu, wakati, wa

kabla ya kupaa Kwake, alipokuwa amewaongoza na kwenda nao hadi Bethania, na kuinua mikono Yake juu ili kuwabariki, na akiwaagiza, akisema, “Enendeni ulimwenguni kote, mkaihubiri Injili,” na kuongeza kwa kusema, “Tazama! Mimi Nipo pamoja nanyi hata ukamilifu wa dahari” (Marko 16:15; Mathayo 28:20); Wakati wa siku ya Pentekoste Mfariji aliyeahidiwa aliposhuka na nguvu kutoka juu ikatolewa kwao na roho za walioamini zikasisimka sana kutambua Uwepo halisi wa Bwana wao aliyekuwa amepaa – wakati huu, hata kama njia yao, kama ile Yake, ingewapitisha katika kutoa kafara maisha yao na kufa kifo cha wafia dini, je, wangekuwa wamebadilisha huduma ya Injili ya neema Yake Bwana, ambayo kwayo wangeweza kupokea ile “taji ya haki” itakayopokelewa wakati wa marejeo Yake Bwana? Je, unadhani wangekubali kubadilishana taji hii na utukufu wa kiti cha enzi cha hapa duniani, ambacho ndicho kilikuwa tumaini la awali katika uanafunzi wao? Yeye ambaye “awezaye kufanya mambo ya ajabu mno kuliko yote tuyaombayo au tuyawazayo” alikuwa amewajalia, pamoja na kushiriki mateso Yake- - ushirika wa furaha Yake, “furaha ya kuwaleta watoto wengi kwenye utukufu “furaha isiyoneneka, uzito wa milele wa utukufu” ambayo, Paulo anaielezea akisema, “dhiki yetu nyepesi, iliyo ya muda wa kitambo tu,” “haifai kulinganishwa.” (Si kitu ikilinganishwa na huo) [GC 350.1; PK Aya ya 22]

Uzoefu wa wanafunzi walioihubiri “injili ya ufalme” wakati wa ujio wa kwanza wa Kristo, ulikuwa unafanana na kielelezo cha uzoefu wa maisha ya wale waliotangaza ujumbe wa kuja Kwake mara ya pili. Kama vile wanafunzi wa Kristo walivyotoka na kwenda kuhubiri, “Wakati umetimia, ufalme wa Mungu umekaribia,” ndivyo Miller na wenzake walivyotangaza kwamba kile kipindi cha unabii kilichokuwa kirefu kuliko vyote na cha mwisho kimefunuliwa katika Biblia, ambacho kilikuwa kinakaribia sana kwisha, kwamba hukumu ilikuwa imekuja, na ufalme ule wa milele umekaribia kufika. Mahubiri ya wanafunzi kuhusiana na wakati yalijengwa juu majuma sabini ya Danieli 9. Ujumbe uliohubiriwa na Miller na wenzake ulitangaza kukoma kwa siku 2300 za Danieli 8:14, ambazo yale majuma sabini ni sehemu yake. Mahubiri ya kila mmoja yalijengwa juu ya utimizwaji wa sehemu mbalimbali za kipindi kile kile kirefu na kimoja cha kiunabii. [GC 351.1; PK Aya ya 23]

Kama ilivyokuwa kwa wanafunzi wa Kristo, William Miller na wenzake, wenyewe nao hawakuelewa kikamilifu maana ya ujumbe ule walioubeba na kuupeleka kwa watu. Mafundisho yenye makosa yaliyokuwa yameotesha mizizi kwa muda mrefu ndani ya kanisa yaliwazuia wasiweze kuifikia tafsiri sahihi ya pointi ile ya maana iliyokuwamo katika unabii huu. Kwa hiyo, ingawa walitangaza ujumbe ule waliokuwa wamekabidhiwa na Mungu ili kuupeleka kwa ulimwengu mzima, lakini, kwa kutouelewa maana yake vizuri kuliwapelekea kupata uzoefu wa kukatishwa kwa uchungu mwingi. [GC 351.2; PK Aya ya 24]

Katika ufafanuzi wake wa kuelezea Danieli 8:14, "Hata siku elfu mbili na mia tatu; ndipo Patakatifu patakapotakaswa," Miller, kama ilivyokwisha kusemwa huko nyuma, alijenga mtazamo tafsiri yake juu ya mtazamo uliokuwa umeshikiliwa na watu wengi katika wakati wake, ambao ulisema kuwa dunia hii ndiyo ilikuwa Patakatifu, naye aliamini kwamba kutakaswa kwa Patakatifu kuliwakilisha kuisafisha dunia hii kwa moto wakati wa ujio Wake Bwana. Basi, yeye alipogundua kwamba mwisho wa siku zile 2300 ulikuwa umebainishwa waziwazi kabisa katika unabii, alifikia hitimisho lake kuwa unabii ulitaja wakati mahsusi wa kuja mara ya pili kwa Kristo. Kosa lake lilitokana na kuamini mtazamo ule maarufu, uliopendwa na watu wengi ambao ulifafanua kwamba Patakatifu palikuwa ni nini hasa. [GC 352.1; PK Aya ya 25]

Katika mfumo wa mifano, ambayo ulikuwa ni kivuli cha kafara na ukuhani Wake Kristo, utakaso wa Patakatifu ulikuwa ni huduma ya mwisho iliyofanywa na kuhani mkuu katika mzunguko wa huduma ya mwaka mzima. Ilikuwa ndiyo kazi ya mwisho ya upatanisho ya kufungia mwaka -- Uondoshaji wa dhambi mbali na Israeli-(Kuiweka dhambi mbali). Ilikuwa ni mfano wa kazi ya mwisho katika huduma ya Kristo Kuhani wetu Mkuu mbinguni, katika kuziondoa au kuzifuta dhambi za watu Wake ambazo zimeandikwa katika kumbukumbu zilizoko mbinguni (Mdo.3:19-21). Huduma hii inahusu kazi ya upelelezi/uchunguzi, kazi ambayo ni ya hukumu; nayo inatangulia kabla tu ya marejeo Yake Kristo katika mawingu ya mbinguni, akiwa na nguvu na utukufu mwingi; kwa maana Yeye anapokuja, kesi ya kila mtu duniani, itakuwa imeamriwa. Asema hivi Yesu: "Ujira Wangu u pamoja Nami, kumlipa kila mtu kama kazi yake ilivyo. Ufunuo 22:12. Ni kazi hii ya hukumu, ndiyo inayotangulia muda mfupi kabla ya ujio wa pili, ndiyo ambayo inatangazwa katika ujumbe wa malaika wa kwanza wa Ufunuo 14:7: "Mcheni Mungu na kumtukuza; kwa maana saa ya hukumu Yake imekuja." [GC 352.2; PK Aya ya 26]

Wale waliolitangaza onyo hili walitoa ujumbe sahihi kwa wakati sahihi. Lakini kama wanafunzi wa awali walivyotangaza ujumbe ule uliojengwa juu ya msingi wa unabii wa Daniel 9, wakisema, "Wakati umewadia, na ufalme wa Mungu umekaribia," wa kati walishindwa kutambua kwamba kifo cha Masihi kilikuwa kimetabiriwa katika Andiko hilo hilo, kadhalika ndivyo Miller na wenzake walihubiri ujumbe ule uliojengwa katika msingi wa Danieli 8:14 na Ufunuo 14:7 na walishindwa kuona kuwa bado kulikuwa na ujumbe mwingine uliotolewa wazi katika Ufunuo 14, ambao pia ulipaswa kutolewa kabla ya marejeo Yake Bwana. Kama vile wanafunzi walivyokosea kuhusu ufalme ule uliotazamiwa na uliopaswa kusimikwa mwishoni mwa majuma sabini, ndivyo Waadventista hawa walivyokosea kuhusu tukio lilipaswa kutokea mwishoni mwa siku 2300. Katika matukio yote mawili palikuwa na hali ya kuyakubali au kuyang'ang'ania sana mafundisho yale yenye makosa na mashuhuri, na yaliyopendwa na watu wengi

wakati huo, haya yalizipofusha akili kiasi cha kushindwa kuutamba Ukweli. Makundi yote mawili yalitimiza mapenzi ya Mungu kwa kuhubiri ujumbe ule ambao Yeye alitaka ufikie watu, na makundi yote mawili, kwa kutouelewa vizuri ujumbe wao, walipatwa na uchungu na kukatishwa tamaa vibaya. [GC 352.3; PK Aya ya 27]

Hata hivyo Mungu alitimiza kusudi Lake lenye tija la kuruhusu onyo la hukumu litolewe kama lilivyokuwa. Siku ile kuu ilikuwa imekaribia, na katika uongozi Wake Mungu watu walileta kwenye mtihani wa wakati mahsusi, ili kuwafunulia kile kilichokuwa mioyoni mwao. Ujumbe ulikusudiwa kwa ajili ya kulipima na kulitakasa kanisa. Ilikuwa ni lazima waongozwe kuona kama mapenzi yao yaliwekwa juu ya ulimwengu huu au juu ya Kristo aliyeko mbinguni. Walikiri kwa midomo yao kumpenda Mwokozi; na sasa iliwapasa kuthibitisha upendo wao. Je, walikuwa tayari kuachana na matumaini na matamanio yao ya ukuu wa kidunia, na kukaribisha kwa furaha ujio wa Bwana wao? Ujumbe huo ulikusudiwa kuwawezesha kutambua hali yao ya halisi ya kiroho; ulitumwa kwa rehema ili kuwaamsha kumtafuta Bwana kwa toba na kujinyenyekeza. [GC 353.2; PK Aya ya 28]

Kule kukatishwa tamaa kwao pia, japokuwa kulisababishwa na wao wenyewe kutokuelewa vizuri ujumbe ambao waliouhubiri, kulikusudiwa kugeuzwa na kutumika na Mungu katika kuwaletea jambo jema. Kungeipima mioyo ya wale waliodai kuwa wamelipokea onyo. Wakiwa wanakabiliana uso kwa uso na kukatishwa tamaa, je, wangefanya mambo kwa mihemko na kutupilia mbali uzoefu wao wa maisha waliokuwa wameupata kwa haraka na kuiondoa mani yao katika Neno la Mungu? Ama, kwa njia ya maombi na unyenyekevu wao wangeweza kujitahidi kutafuta ili wagundue ni wapi walikuwa wameshindwa kuelewa maana ya unabii ule? Ni wangapi walikuwa wamesukumwa kwa hofu tu, au kutenda mambo bila kufikiri, au mhemuko na msisimko? Ni wangapi walikuwa wamejitoa nusu-nusu na wasioamini? Watu wengi sana walikiri kwamba wanapenda kuja Kwake Bwana. Walipotakiwa kustahimili dhihaka na shutuma za ulimwengu, pamoja na ule mtihani wa mambo kuchelewa na kule kukatishwa tamaa kwao, je! wangeikana imani yao? Kwa vile wao hawakuweza kuelewa mara moja jinsi Mungu alivyokuwa anashugulika nao, je! wangeutupapembeni Ukweli unaotegemezwa na ushuhuda ulio dhahiri kabisa wa Neno Lake Mungu? [GC 353.2; PK Aya ya 29]

Mtihani na jaribu, vingedhihirisha nguvu walizokuwa nazo wale ambao kwa imani ya kweli walikuwa wametii kile walichoamini kuwa ni mafundisho ya Neno na Roho wa Mungu. Hili lingewafundisha, kwa namna ambayo ni uzoefu kama huo walioupitia peke yake katika tukio lile ungeweza kuwafundisha, hatari ya kupokea nadharia na tafsiri za wanadamu, badala ya kuifanya Biblia ijitafsiri yenyewe. Kwa watoto wa imani kuchanganyikiwa na huzuni yao iliyotokana na

kosa lao kungeweza kuleta masahihisho yaliyotakiwa. Wangeongozwa kwenye uchunguzi wa makini wa Neno la kiunabii. Wangejifunza kuchunguza kwa uangalifu zaidi msingi wa imani yao na kukataa kila kitu ambacho hakikujengwa juu ya msingi wa Maandiko ya Kweli, hata kama kinakubaliwa na wengi katika Ulimwengu wa Kikristo, basi nao wakikatae kwa vile hakikujengwa juu ya Maandiko ya Ukweli. [GC 354.1; PK Aya ya 30]

Kwa hawa waumini, kama ilivyokuwa kwa wanafunzi wa awalil, kile ambacho katika saa ya majaribu kilionekana kana kwamba ni giza kwa ufahamu wao baadaye kingeweza kueleweka wazi. Wakati ambapo wangeuona ule "mwisho wa Bwana au lengo la Mwenyezi Mungu" wangejua kuwa, licha ya kuwa lile jaribu lilitokana na makosa yao, makusudi Yake ya upendo kwao yalikuwa yakienda kutimia kwa taratibu na uhakika kwao. Wangejifunza kwa uzoefu uliopata mibaraka ndani Yake kwamba Yeye ni "Mwenye huruma sana na rehema tele;" kwamba njia Zake zote ni "rehema na Kweli kwao walishikao Agano Lake na shuhuda Zake." [GC au PK 354.2]

## SURA YA 20

## UAMSHO MKUU WA KIDINI

### (Mwamko Mkuu Wa Kidini Katika Ulimwengu Mzima)

Ufupisho: Malaika wa kwanza wa ufunuo 14:6-7, ni onyo zito katika historia yote. Onyo hili lilianza kutangazwa wakati wa mwamko wa kidini wa ulimwengu mzima kama ambavyo tutaona kwenye sura hii.

Mwamko Mkuu wa Kidini, wakati wa utangazaji wa kuja upesi kwa Kristo, umetabiriwa katika unabii wa Ujumbe wa Malaika wa Kwanza wa Ufunuo 14. Malaika anaonekana akiruka "katikati ya mbingu, mwenye Injili ya milele, awahubiri hao wakaao juu ya nchi, na kila taifa na kabila na lugha na jamaa" anatangaza huu ujumbe kwa sauti kuu: "Mcheni Mungu na kumtukuza, kwa maana saa ya hukumu Yake imekuja. Msujudieni Yeye aliyezifanya mbingu na nchi na bahari na chemchemi za maji" Mstari wa 6, 7. [GC 355.1; PK Aya ya 1]

Ukweli kwamba malaika huyo anatajwa kuwa ndiye mpiga mbiu ya onyo hilo ni wa kutilia maanani sana. Kwa usafi wa maisha, utukufu na nguvu ya mjumbe huyo wa mbinguni, Mungu Mwenye hekima amependezwa kuiwakilisha tabia iliyoinuliwa ya kazi iliyopaswa kutekelezwa kwa huo ujumbe na nguvu na utukufu ulioambatana nao. Na ule urukaji wa malaika huyo "katikati ya mbingu," na ile "sauti kuu" ambayo kwayo onyo hilo linatolewa, na kutangazwa kwake waziwazi kwa hao wote "wakaao juu ya nchi," - hutupa sisi ushahidi wa kasi na ueneaji wa vuguvugu hilo ulimwenguni kote.* [GC 355.2; PK Aya ya 2]

Ujumbe wenyewe unatupa sisi fununu kuhusu wakati mahsusi ambapo vuguvugu hizi hufanyika. Unaelezwa kuwa umekuwa sehemu ya "Injili ya milele;" na unatangaza kuanza kwa hukumu. Ujumbe wa wokovu umehubiriwa katika zama zote; lakini ujumbe huu ni sehemu ya Injili, ambayo inahubiriwa tu wakati wa siku za mwisho, kwani ni kweli kwamba ni wakati huu tu ndiyo unaendana na tamko la 'saa ya hukumu imewadia'. Unabii huo unaonyesha mfululizo wa matukio yanayoongozana hadi kutufikisha kwenye kufunguliwa kwa hukumu. Hii ni Kweli hasa kuhusiana na kitabu cha Danieli. Lakini sehemu ile ya unabii wake unaohusiana na siku zile za mwisho, Danieli aliagizwa kuufunga na

kuutia muhuri “hata wakati wa mwisho.” Ujumbe huo uliohusu hukumu, ambao ulijengwa juu ya msingi wa utimizwaji wa unabii huu, usingeweza kutangazwa mpaka hapo tutakapoufikia wakati huo. Lakini katika siku zile za mwisho, asema nabii huyo, “wengi wataenda mbio huko na huko, na maarifa yataongezeka” Danieli 12:4. [GC 355.3; PK Aya ya 3]

Mtume Paulo alilionya kanisa lisitazamie Ujio Wake Kristo katika siku zao. “Maana haiji (siku ile), anasema, “usipokuja kwanza ule ukengeufu; akafunuliwa yule mtu wa kuasi, mwana wa uharibifu;” 2 Wathesalonike 2:3. Ni mpaka baada ya ule uasi mkuu, na kipindi kirefu cha utawala wa yule “mtu wa dhambi au mtu wa uasi,” ndipo hapo sisi tutaweza kutazamia marejeo ya Bwana wetu. Yule “mtu wa dhambi,” ambaye pia huitwa “siri ya kuasi,” “mwana wa uharibifu,” na “yule mwasi, au huyo mwovu” anauwakilisha upapa, ambao, kama ulivyotabiriwa katika unabii, ulipaswa kuendelea kushika hatamu zake za utawala wa dunia kwa miaka 1260. Kipindi hicho kilikoma katika mwaka wa 1798. Marejeo Yake Kristo yasingaliweza kutokea kabla ya wakati huo. Paulo kwa tahadhari anaelezea kipindi chote cha Ukristo toka wakati wake, akishuka chini kuja kwetu mpaka mwaka ule wa 1798. Ni upande huu wa wakati huo ambapo ujumbe wa ujio wa mara ya pili wa Kristo unapasa kuhubiriwa. [GC 356.1; PK Aya ya 4]

Hakuna ujumbe kama huo uliopata kutolewa katika zama zilizopita. Paulo, kama vile tulivyokwisha kuona, hakuuhubiri ujumbe huo; yeye aliwaelekeza ndugu zake kutazama kwa wakati ujao uliokuwa bado mbali zaidi na kile kipindi chao kwa ajili ya kuja Kwake Bwana. Wanamatengenezo hawakuhubiri ujumbe huo. Martin Luther aliiweka siku ya hukumu kama miaka mia tatu mbele ya wakati wake. Lakini tangu mwaka wa 1798 kitabu cha Danieli kimefunguliwa (Ufu. 10:1-7; Dan. 12:4,5-10), maarifa ya kuujua unabii mbalimbali yameongezeka, na wengi wameutangaza ujumbe huo mzito wa hukumu iliyokaribia. [GC 356.2; PK Aya ya 5]

**Joseph Wolff Mmishonari Wa Ulimwengu**

Kama yalivyokuwa yale Matengenezo Makuu ya Kanisa ya karne ya kumi na sita, ndivyo vuguvugu za ujio wa pili wa Kristo lilivyoonekana katika nchi mbalimbali za Ulimwengu wa Kikristo kwa wakati ule ule mmoja (Waliitwa Waadventista au Watu wanaongojea kuja kwa Kristo). Katika mabara yote mawili, yaani, Ulaya na Amerika, watu wenye imani na maombi waliongozwa kujifunza unabii mbalimbali, nao, wakifuatilia katika kumbukumbu za Maandiko zilizovuviwa, waliona ushahidi wa kuridhisha uliowashawishi kwamba mwisho wa mambo yote ulikuwa umekaribia. Katika nchi mbalimbali kulikuwa na makundi ya Wakristo waliokaa katika sehemu zilizojitenga ambapo, kwa kujifunza Maandiko peke yake, walifikia mahali ambapo walijenga imani kwamba marejeo Yake Mwokozi yalikuwa karibu. [GC 357.1; PK Aya ya 6]

Mnamo mwaka wa 1821, miaka mitatu baada ya Miller kufikia ufafanuzi wake wa unabii mbalimbali uliokuwa uliosonda kidole chake kwenye wakati wa hukumu. Daktari Joseph Wolff, “mmishonari kwa ulimwengu,” alianza kutangaza habari za kuja upesi kwa Bwana. Wolff alizaliwa katika nchi ya Ujerumani, wazazi wake wakiwa ni Wayahudi, baba yake akiwa ni rabi yaani mwalimu wa Kiyahudi. Akiwa bado mdogo, aliuamini Ukweli wa dini ya Kikristo. Akiwa mwenye akili inayojishugulisha sana, yenye udadisi wa mambo, alikuwa msikilizaji mwenye shauku wa maongezi yaliyofanyika ndani ya nyumba ya baba yao kama Waebrania wacha Mungu walivyokutanika kusimulia matumaini na matarajio ya taifa lao, utukufu wa Masihi aliyekuwa anakuja, na urejeshwaji wa Israeli. Siku moja alisikia Yesu wa Nazareti akitajwa, basi, yule mvulana aliuliza kwamba huyu Yesu wa Nazareti alikuwa ni nani. “Myahudi mwenye talanta za juu sana,” likawa ndilo jibu lake; “lakini alipojifanya kuwa ni Masihi, Mahakama ya kimataifa ya Kiyahudi ilimhukumu kuwa anastahili kuuawa.” “Kwa nini, basi,” muulizaji alidakia, “Yerusalemu umeangamizwa, na kwa nini sisi tuko utumwani?” “Ole! ole!” akajibu baba yake, “kwa sababu Wayahudi waliwaua manabii.” Mara moja wazo hili lilijengeka ndani ya yule mtoto: “Huenda Yesu pia alikuwa ni nabii, na Wayahudi walimwua alipokuwa hana hatia yoyote.” -Travels and Adventures of the Rev. Joseph Wolff, toleo la 1, uk. 6. Hisia hiyo ilikuwa yenye nguvu mno kiasi kwamba, ingawa alikatazwa kuingia katika kanisa lolote la Kikristo, mara kwa mara yeye alikaa nje ya kanisa kusikiliza mahubiri [GC 357.2; PK Aya ya 7]

Alipokuwa na umri wa miaka saba tu, alikuwa akijigamba kwa jirani yake aliyekuwa mzee wa Kikristo kuhusu ushindi wa Israeli katika siku za usoni atakapokuja Masihi, wakati yule mwanaume mzee alipomwambia hivi kwa upole na wema: “Kijana Mpendwa, mimi nitakuambia Masihi wa Kweli ni nani: Ni Yesu wa Nazareti,……ambaye mababu zenu walimsulibisha, kama walivyowafanya manabii wa zamani. Nenda nyumbani kwenu ukasome sura ya hamsini na tatu ya Isaya, nawe utasadiki ya kwamba Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu.” -- Ibid., juzuu ya 1, uk. Imani mara ile ikajengeka moyoni na kumshika kwa nguvu ndani yake. Akaenda nyumbani kwao na kusoma Maandiko yale, akastaajabu kuona jinsi yalivyokuwa yametimia kikamilifu ndani ya Yesu Yule wa Nazareti. Je, inawezekana kwamba maneno ya Mkristo yule yalikuwa ya kweli? Kijana alimwuliza baba yake ampatie ufafanuzi wa unabii ule, lakini alikutana na ukimya mkali mno kiasi kwamba hakuthubutu kurudia somo lile tena. Walakini jambo lile hata hivyo liliongeza tu hamu yake ya kutaka kujua zaidi kuhusu dini ya Kikristo. [GC 357.3; PK Aya ya 8]

**Ashtakiwa Kwa uzushi**

Maarifa aliyokuwa akiyatafuta kwa makini yalifichwa kwa makini katika nyumba yake ya Kiyahudi; lakini, alipokuwa na miaka kumi na moja tu, aliondoka nyumbani kwa baba yake na kwenda ulimwenguni kujipatia elimu yake, kujichagulia dini yake mwenyewe, na kazi yake ya maisha. Alipata maskani yake ya muda nyumbani kwa jamaa zake wa karibu, lakini alifukuzwa mara moja kutoka kwao kama mtu mwasi, naye alipokuwa mpweke, bila fedha, alilazimika kuishi maisha yake miongoni mwa watu baki asiowajua kabisa. Alitangatanga kutoka mahali hadi mahali, akijifunza masomo yake kwa bidii na kujipatia riziki yake kwa kufundisha Kiebrania. Kwa ushauri wa mwalimu mmoja Mkatoliki alishawishiwa kuipokea imani ya Kirumi na kuwa na wazo la kuwa mmishenari kwa watu wake. Akiwa na kusudi lile, miaka michache baadaye, alikwenda kuchukua masomo yake katika Chuo cha Propaganda cha Rumi. Hapa tabia yake ya kuwa na fikra huru na kusema kweli ilimletea sifa mbaya ya uzushi. Alishambulia waziwazi matendo mabaya ya unyanyasaji wa kanisa na kusisitiza umuhimu wa kufanya Matengenezo. Ingawa mwanzoni alitendewa kwa upendeleo na viongozi wa kipapa, baada ya muda fulani alifukuzwa Rumi. Akiwa chini ya jicho la kanisa, alienda mahali hata mahali mpaka ilipodhihirika kwamba asingeweza kufikia kwenye uamuzi wa kutii hali ya kuwa mtumwa wa Urumi. Alitangazwa kuwa alikuwa ni mtu asiyeweza kurekebishwa, kufundishika au kuwekwa chini ya nidhamu, naye akaachwa huru kwenda kokote alikopenda. Sasa alifunga safari kuelekea Uingereza, na huko akiwa anaikiri imani ya Kiprotestanti, alijiunga na Kanisa la Kiingereza yaani Anglikana. Baada ya mafunzo yake ya miaka miwili alitoka kwenda kutekeleza azimio lake la umishenari katika mwaka wa 1821. [GC 358.1; PK Aya ya 9]

Wakati Wolff alipokuwa ameikubali ile Kweli kuu ya ujio wa Kristo kwa mara ya kwanza kama "Mtu wa huzuni nyingi, ajuaye sikitiko," aliona ya kwamba unabii huu ulifunua kwa uwazi unaolingana na ule unaohusiana na kuja Kwake Kristo mara ya pili kwa nguvu na utukufu. Wakati alipokuwa anatafuta namna ya kuwaongoza watu wake kwa Yesu wa Nazareti kama Ndiye Yule Aliyeahidiwa, na kuwaonyesha kwenye Ujio Wake wa mara ya kwanza katika hali ya unyenyekevu na fedheha kama kafara ya dhambi za wanadamu, pia aliwafundisha juu ya Ujio Wake wa mara ya pili kama Mfalme na Mkombozi. [GC 358.2; PK Aya ya 10]

**Mfalme Wa Dunia Yote**

"Yesu wa Nazareti, Masihi wa Kweli," akasema, "ambaye mikono na nyayo Zake zilitobolewa, ambaye alipelekwa kama Mwana-Kondoo apelekwavyo machinjioni, Yeye ambaye alikuwa ni Mtu wa huzuni nyingi, ajuaye sikitiko, ambaye baada ya fimbo ya ufalme ilipoondolewa katika Yuda na mamlaka Yake ya utungaji wa sheria kuondolewa kutoka katikati ya miguu Yake, alikuja kwa mara ile ya kwanza; na kisha atakuja tena mara ya pili katika mawingu ya

mbinguni, na kwa tarumbeta ya Malaika Yule Mkuu," (Joseph Wolff, Researches and Missionary Labors, ukurasa wa 62). "Naye atasimama juu ya ule Mlima wa Mizeituni; hapo ndipo utawala ule uliokabidhiwa kwa Adamu wakati wa uumbaji, na kupotezwa naye (Mwanzo 1:26; 3:17), utakapokabidhiwa kwa Yesu. Atakuwa Mfalme wa ulimwengu mzima. Maumivu na maombolezo ya viumbe yatakoma; ila nyimbo za sifa na shukrani zitasikika……Yesu ajapo katika utukufu wa Baba, pamoja na malaika Zake watakatifu,... waumini waliokufa watafufuliwa kwanza. 1 Wathesalonike 4:16; 1 Wakorintho 15:23. Huu ndio ambao sisi Wakristo tunauita ufufuo wa kwanza. Ndipo ufalme wa wanyama utabadilisha silika yake (Isaya 11:6-9), na kutiishwa chini ya Yesu. Zaburi 8. Amani itatawala na kuenea kwenye Malimwengu yote." Journal of Rev. Joseph Wolff, ukurasa wa 378, 379. "Bwana ataangalia tena chini duniani; na kusema, 'Tazama, ni njema sana.'" - Ibid., ukurasa wa 294. [GC 359.1; PK Aya ya 11]

**Kuja Kwake Kristo Mara Ya pili**

Wolff alisadiki kwamba kuja Kwake Bwana kulikuwa kumekaribia, tafsiri yake ya vipindi vya kiunabii ikiweka hitimisho kuu ndani ya miaka michache tu ukilinganisha na jinsi alivyoonyesha Miller. Kwa wale waliotumia Maandiko na kudai kwamba "Habari ya siku ile na saa ile hakuna aijuaye," wakisema kwamba wanadamu hawapaswi kujua chochote kuhusu ukaribu wa ujio Wake Bwana, Wolff aliwajibu hivi: "Je, hivi Bwana wetu alisema kwamba siku na saa ile isingeweza kujulikana kamwe? Je, Yeye hakutupa dalili za nyakati ili angalau zitusaidie kujua ukaribu wa kuja Kwake kama mtu anavyojua kiangazi kinapokaribia kwa kuuangalia mtini unapopukutisha majani yake? Mathayo 24:32. Je, sisi hatupaswi kamwe kujua kuwa kipindi hicho, ambapo Yeye Mwenyewe alituonya sisi, sio tu kwa kusoma habari za Danieli nabii, bali kukielewa pia? Na katika kitabu hicho hicho cha Danieli, kuna mahali panaposema kwamba Maneno yake yalifungwa *na kutiwa muhuri mpaka wakati wa mwisho (jambo hilo ufungwaji lilikuwa katika siku zake), na ya kwamba, "wengi wataenda mbio huko na huko' (usemi wa Kiebrania unaoonyesha kuchunguza na kutafakari wakati), 'na maarifa' (kuhusu huo wakati) 'yataongezeka.' Danieli 12:4. Kando ya hili, Bwana wetu hakusudii kusema kwa kauli hii, kwamba kule kukaribia kwa wakati hakutajulikana, bali kwamba 'siku na saa' ile ile mahsusi'hakuna aijuaye.' Inatosha, Yeye alisema kuwa itajulikana kwa dalili za nyakati, kutushawishi sisi kujiandaa kwa ajili ya marejeo Yake, kama ilivyokuwa kwa Nuhu alipoitayarisha safina." - Wolff. Researches and Missionary Labors, ukurasa wa 404, 405. [GC 359.2; PK Aya ya 12]

Kuhusu mfumo mashuhuri uliopendwa na watu katika kutafsiri inavyotakiwa au kufasiri vibaya Maandiko, Wolff aliandika hivi: "Sehemu kubwa sana ya Kanisa la Kikristo imekengeuka kwa maana wazi ya Maandiko, nao wameugeukia mtindo

wa kuwazia tu mawazo yasiyo ya Kweli ya kufikirika na ndoto za mchana ambazo Wabudha wanazo, hawa wanaamini kwamba furaha ya baadaye ya wanadamu itakuwa ni kuambaa-ambaa hewani, au kujongea kwa kuranda-randa hewani, nao wanadhani kwamba wanaposoma neno hili Wayahudi, basi, wao wanapaswa pia kuelewa kuhusu watu wa Mataifa; na wanaposoma Yerusalemu, wao wanapaswa kuelewa kuwa hilo ni kanisa; na kama inasemwa nchi basi hiyo inamaanisha anga; na kwa habari ya marejeo ya Bwana wao wanapaswa kufahamu kuwa hayo ni maendeleo ya vyama vya Kimishenari; na kule kupanda kwenda kwenye mlima wa nyumba ya Bwana, kuwa humaanisha kutano kuu la tabaka la Wamethodisti." - Journal of the Rev Joseph Wolff, ukurasa wa 96. [GC 360.1; PK Aya ya 13]

Katika kipindi cha miaka ishirini na minne kuanzia 1821 hadi 1845, Wolff alisafiri sana: Katika bara la Afrika alizizuru nchi za Misri na Uhabeshi (Abyssinia/Ethiopia); katika Asia akipita katika nchi ya Palestina, Syria, Uajemi, Bokhara, na Uhindi (India). Alitembelea pia nchi ya Marekani (U.S.A), alipokuwa akisafiri kwenda kule, alihubiri katika kisiwa cha Mtakatifu Helena, California. Aliwasili New York katika mwezi wa Agosti, 1837; na baada ya kuhubiri katika mji huo, alihubiri kule Philadelphia na Baltimore, na hatimaye aliendelea mbele na safari yake kwenda Washington. Kule, yeye alisema hivi, " kwa njia ya hoja iliyoletwa na Rais mstaafu, John Quincy Adams, katika mojawapo ya vikao vya Bunge la Marekani-Kongresi, Bunge lilipitisha kwa kauli moja kunipa mimi ruhusa ya kuutumia mmojawapo wa kumbi za Bunge kwa ajili ya kutoa mhadhara, ambao niliutoa katika siku ya Jumamosi, nikipewa heshima ya kuwapo kwa wajumbe wote wa Bunge lile, pia pamoja na askofu wa Virginia na uwepo wa viongozi wa dini wachungaji na maaskofu na wakazi wa jiji la Washington. Heshima hiyo hiyo nilipewa na wajumbe wa serikali ya New Jersey na Pennsylvania, ambao katika uwepo wao niliwasilisha hotuba zilizotokana na utafiti wangu kule katika bara Asia, pamoja na zile zilizokuwa zimejengwa juu ya utawala wa Yesu Kristo Mwenyewe." - Ibid., ukurasa wa 398, 399. [GC 360.2; PK Aya ya 14]

### Uwezo Umo Ndani Ya Kitabu Hicho

Dk. Wolff alisafiri katika nchi za kishenzi au zenye ukatili wa kinyama pasipo kupewa ulinzi wa serikali yoyote ya Ulaya, akistahimili magumu mengi na kuzungukwa na hatari nyingi zisizokuwa na idadi. Aliteswa kwa kucharazwa viboko kwenye nyayo za miguu na kushindishwa na njaa, aliuzwa kama mtumwa, na mara tatu alihukumiwa kifo. Alishambuliwa na majambazi na wakati mwingine alikuwa karibu kufa kwa kiu. Mara moja aliporwa kila kitu alichokuwa nacho na kuachwa kutembea kwa miguu bila viatu, akapekua kwa mamia ya maili kupitia katika vilima, theluji ikimpiga usoni na kwenye miguu yake

isiyokuwa na viatu, mpaka miguu ikafa ganzi kwa kugusana na ardhi iliyoganda kwa barafu. [GC 361.1; PK Aya ya 15]

Alipopewa onyo dhidi ya kutembea bila kuwa na silaha miongoni mwa makabila yale yasiyostaarabika, makatili, yenye hasira, na yanayoua watu, alitangaza mwenyewe kuwa "alipewa silaha" - yaani, "maombi yake, ari yake kwa ajili ya Kristo, na imani yake katika msaada Wake Kristo." "Mimi pia," alisema "nimepewa upendo kwa Mungu na kwa jirani yangu ndani ya moyo wangu, na Biblia i mkononi mwangu." W.H.D Adams, In Perils Oft, uk. 192. Alibeba Biblia katika lugha ya Kiebrania na Kiingereza popote kule alipokwenda. Kuhusu mojawapo ya safari zake alizofanya baadaye, anasema hivi: "Mimi ... nilikuwa na Biblia iliyofunguliwa mkononi mwangu daima. Niliona kwamba nguvu zangu zilikuwa katika hiki Kitabu, na ya kwamba nguvu ya Kitabu ingeweza kunitegemeza mimi kwa kunipa nguvu za kusonga mbele.." - Ibid., ukurasa wa 201. [GC 361.2; PK Aya ya 16]

Hivyo ndivyo alivyoweza kudumu katika kazi zake mpaka pale ujumbe wa hukumu ulipokuwa umepelekwa katika sehemu kubwa inayokaliwa na watu wa ulimwenguni wa wakati huo. Miongoni mwa Wayahudi, Waturuki, Wafarsi/Waajemi, Wahindu, na mataifa mengi na jamii aligawa lile Neno la Mungu katika lugha hizo mbalimbali na kila mahali alipiga mbiu ya kutangaza ukaribu wa utawala wa Masihi. [GC 361.3; PK Aya ya 17]

Katika safari zake kule Bokhara alikuta fundisho la Ujio wa karibuni wa Bwana ambalo lilishikiliwa na watu waliokaa katika sehemu zilizokuwa zimejitenga mbali na watu na za upweke. Waarabu wa Yemeni, alisema, "wanacho kitabu kiitwacho Seera, ambacho kinatoa tangazo la kuja kwa Kristo mara ya pili na utawala Wake wa utukufu; nao wanatarajia kuona matukio makubwa katika mwaka wa 1840." - Journal of the Rev. Joseph Wolff, ukurasa wa 377. "Katika nchi ya Yemeni,... nilitumia siku sita na wana wa Rekabu. Hawanywi mvinyo, hawalimi mizabibu, hawapandi mbegu, nao wanaishi katika mahema, tena wanamkumbuka Yonadabu, mzee yule mwema, mwana wa Rekabu (Yeremia 35); na katika miongoni mwao niliwakuta wana wa Israeli, wa kabila la Dani,... ambao wanatazamia, pamoja na wana wa Rekabu, ujio wa haraka wa Masihi katika mawingu ya mbinguni." - Ibid., 389. Journal of the Rev. Joseph Wolff. [GC 361.4; PK Aya ya 18]

Imani kama hiyo aliiona kwa mmishenari mmoja kule Tatary (Sehemu za Urusi iliyosambaratika). Padri wa Kitatari alimtupia swali mmishenari huyu kuhusiana na lini Kristo angerudi mara ya pili. Mmishenari alipojibu kwamba alikuwa hajui chochote juu ya habari ile, padri alionekana ameshangazwa sana kwa ujinga kama ule kwa yule aliyejidai kuwa ni mwalimu wa Biblia, naye alieleza imani aliyokuwa nayo binafsi, iliyojengwa juu ya unabii, kwamba Kristo angekuja takribani mwaka 1844. [GC 362.1; PK Aya ya 19]

## Ujumbe Wa Marejeo Ya Kristo Kule Uingereza

Mapema kama mwaka wa 1826, ujumbe wa Ujio wa pili wa Yesu (ujumbe wa Kiadventista) ulianza kuhubiriwa Uingereza. Vuguvugu hapa hazikuchukua sura inayojionyesha kama kule Amerika; wakati mahsusi wa ujio Wake kwa ujumla haukufundishwa, ila Ukweli mkuu wa kuja kwa Kristo haraka katika nguvu na utukufu ulitangazwa maeneo mengi sana. Tena jambo hilo halikuwa tu kwa wale waliokataa kukubaliana na imani ya Kanisa ya Anglikana au wale ambao hawakuzikubali kawaida nyinginezo za ibada za kanisa lile tu (nonconformists). Mourant Brock, mwandishi wa Kiingereza, anaeleza kwamba karibu wachungaji wapatao mia saba wa Kanisa la Kingereza yaani Anglikana, walijishughulisha katika kuihubiri hiyo “habari njema ya ufalme.” Ujumbe ulioutaja mwaka 1844 kama ndio wakati wa kuja Kwake Bwana ulitolewa pia katika Jumuiya ile kuu ya ufalme ulioungana wa Uingereza, yaani United Kingdom (Scotland, Wales, Ireland na Uingereza yenyewe).... Machapisho ya Kiadventista (ya ujio wa Bwana) toka Marekani, yalisambazwa mahali pengi sana. Vitabu pamoja na majarida ya magazeti vilichapishwa tena katika nchi ya Uingereza. Na katika mwaka wa 1842, Robert Winter, Mwingereza kwa kuzaliwa, aliyekuwa ameipokea imani ya Kiadventista (marejeo ya Bwana) kule Amerika, alirudi katika nchi yake alikozaliwa na kupiga mbiu ya marejeo Yake Bwana. Wengi waliungana naye katika kazi hii, na ujumbe huu wa hukumu ulitangazwa katika sehemu mbalimbali za Uingereza. [GC 362.2; PK Aya ya 20]

## Mjesuiti Na Mlutheri Watoa Ushuhuda Wao

Kule Amerika ya Kusini, katikati ya kutostarabika kulikosheheni yaani ukafiri, na matendo mengine ya kishenzi kama ukatili, na ujanja yaani hila za mapadre, Lacunza, Mhispania na Mjesuiti aliipata njia yake kwa kujifunza Maandiko na kwa njia hiyo aliupokea Ukweli wa kuja kwa Kristo haraka. Akiwa anasukumwa kutoa onyo, lakini akitamani kukwepa makaripio ya Rumi, alichapisha mawazo yake chini ya jina tofauti na lake au bandia “Rabi Ben-Ezra,” akijifanya kama Myahudi aliyeongoka. Lacunza aliishi katika karne ya kumi na nane, lakini ilikuwa ni karibu na mwaka wa 1825 kitabu chake kilipofanikiwa kuingia London, kilitafsiriwa katika lugha ya Kiingereza. Kuchapishwa kwake kulisaidia kuufanya ushawishi na shauku viwe na kina zaidi kwenye moyo unaopenda kujua ambao tayari ulikuwa umeamshwa katika nchi ya Uingereza kuhusu mada ya kuja Kwake Kristo mara ya pili. [GC 362.3; PK Aya ya 21]

Katika nchi ya Ujerumani fundisho hilo lilikuwa limefundishwa na Bengel katika karne ya kumi na nane, mchungaji wa Kanisa la Lutherani na Msomi maarufu wa Biblia na mkosoaji wake (mdadavuaji). Alipohitimu elimu yake, Bengel alikuwa “ameutumia muda wake mwingi sana kujifunza theolojia; huyu

kutokana na akili yake iliyokuwa na umakini sana na yenye mwelekeo wa kidini, aliongezewa kina kutokana na mafunzo na nidhamu aliyopata mapema; basi yote hayo yakamfanya awe na mwelekeo ule unaopatana na tabia yake. Kama vijana wengine wenye tabia ya kutafakari kwa kina, kabla yake na tangu hapo, alilazimika kupambana na mashaka pamoja na matatizo ya asili ya kidini, na kwa hisia zake zenye kina, anataja kwa juu juu tu habari za ile 'mishale mingi iliyouchoma moyo wake mnyonge, na kuufanya ujana wake kuwa mgumu kustahimili." Akiwa mjumbe wa Baraza lililowekwa na papa la Wurttemberg, aliitetea hoja ya uhuru wa dini. "Huku akidumisha kutetea haki na fursa za kanisa, pia alikuwa ni mtetezi wa uhuru ulio na busara au uhuru wa msingi, kwamba uweze kutolewa kwa wale wote waliohisi kuwa wamefungwa, kwa misingi ya dhamiri zao, ili wapate kujiondoa katika ushirika wake." — Encyclopaedia Britannica, Toleo la 9, "Bengel." Athari chanya za sera hii bado zinaonekana katika jimbo lake alikozaliwa. [GC 363.2; PK Aya ya 22]

Ilikuwa ni wakati alipokuwa anaandaa hubiri lake kutoka katika Ufunuo 21 kwa ajili ya Jumapili ya Adventi (majilio), ambapo nuru iliangaza katika moyo wa Bengel kuhusu kuja Kwake Kristo kwa mara ya pili. Unabii wa Ufunuo ukafunuliwa katika ufahamu wake usivyopata kamwe kufunuliwa kwake katika siku za awali. Akiwa amelemewa na hisia za umuhimu mkubwa mno na utukufu usio na kifani wa matukio yaliyowasilisha picha kichwani mwake ambayo yaliyotolewa na nabii, alilazimika kwa muda fulani kuacha kutafakari mada hiyo. Alipokuwa mimbarani tukio la ujio wa Kristo likamjia tena kwa uwazi na nguvu zake zote. Tangu wakati ule alitumia muda wake mwingi sana kujifunza unabii wa Ufunuo yaani apokalipse, unabii wa matukio ya siku za mwisho (Ufunuo na Danieli ni vitabu vya Apocalypse), na mara imani ikamjia kwamba unabii ule ulikuwa ukisonda kidole chake na kuelekeza kwamba kuja Kwake Kristo kulikuwa kumekaribia. Tarehe ambayo aliiweka kama wakati wa marejeo Yake Kristo ilikuwa ndani ya miaka michache sana baada ya ile iliyowekwa baadaye na Miller. [GC 363.3; PK Aya ya 23]

Maandishi ya Bengel yalisambazwa katika Ulimwengu wote wa Kikristo. Mawazo yake juu ya unabii yalipokewa kwa ujumla na watu wengi sana katika jimbo lake la Wurttemberg, na kwa kiasi fulani katika sehemu zingine za Ujerumani. Na harakati hii iliendelea kuwapo hata baada ya kifo chake, na ujumbe wa marejeo ulisikika katika nchi ya Ujerumani kwa wakati ule ule mmoja ulipokuwa unapata mvuto na umakini wa watu wengi katika nchi nyinginezo. Katika tarehe za mwanzoni, baadhi ya waumini walikwenda Urusi na kuanzisha kule makoloni yao, na ujumbe wa imani hii ya kuja upesi kwa Kristo mpaka sasa (mwaka 1888), bado unashikiliwa na makanisa ya Kijerumani katika nchini humo. [GC 364.1; PK Aya ya 24]

**Nuru Yaangaza Ufaransa Na Kule Uswisi**

Nuru ile iliangaza pia katika nchi ya Ufaransa na Uswisi. Pale Geneva ambapo Farel na Calvin walikuwa wameeneza Ukweli wa Matengenezo ya Kanisa, Gaussen alihubiri ujumbe wa kuja kwa Kristo mara ya pili. Alipokuwa angali mwanafunzi shuleni, Gaussen alikuwa amepambana na roho ile ya falsafa ya urazini* (rationalism) iliyotumika katika kuyafafanua Maandiko kwa kufuata akili za wanadamu, ambayo ilikuwa imeenea kote Ulaya katika kipindi cha mwisho cha karne ya kumi na nane; naye alipojiunga na uchungaji hakuwa ni mjinga tu wa imani ya Kweli, bali alikuwa na mwelekeo wa kuifuata nadharia ile ya kuyaonea mashaka Maandiko (skepticism). Katika ujana wake alikuwa na moyo wa kupenda sana kujifunza unabii. Baada ya kukisoma kitabu cha Rolin cha Ancient History (Historia ya Kale), umakini wake ulivutwa kuelekea kwenye sura ya pili ya Danieli, naye alishtushwa kuona usahihi wa ajabu wa jinsi ambavyo unabii huo ulikuwa umetimizwa, kama inavyoonekana katika kumbukumbu za kihistoria. Hapa ukawa upo ushahidi wa uvuvio wa Maandiko, ambao ulikuwa kama nanga kwake katikati ya zile hatari kubwa za miaka ya baadaye. Hakuweza kutosheka na mafundisho ya ile falsafa ya kufikirika ya urazini, na katika kujifunza kwake Biblia na kutafuta nuru iliyo wazi zaidi, baada ya muda fulani kupita, aliongozwa kujenga imani hai na chanya. [GC 364.2; PK Aya ya 25]

**Watoto Wadogo Waelewa**

Kadiri alivyoendelea na utafiti wake wa unabii, alifika mahali pa kuamini kwamba ujio Wake Bwana ulikuwa umekaribia. Akiwa ameguswa na uzito, utufuku na umuhimu rd Ukweli huu mkuu, alitamani kuuleta mbele ya watu; lakini imani iliyozoeleka na watu wengi iliyosema kuwa unabii wa Danieli ulikuwa ni mafumbo na siri na kwamba hauwezi kueleweka ikawa ni kikwazo kikubwa katika njia yake. Hatimaye aliazimia - kama Farel alivyokuwa amefanya kabla yake katika kuihubiri Geneva - yaani kuanza na watoto, ambao kupitia kwao alitumainia kwamba ataweza kuamsha shauku ya wazazi wao. [GC 364.3; PK Aya ya 26]

"Natamani jambo hili lieleweke," alisema baadaye, akiongelea juu ya lengo lake katika shughuli ya kazi hii, "si kwa sababu ya umuhimu wake mdogo, lakini kinyume chake ni kwa sababu ya thamani yake kuu, ya kwamba mimi nilitaka kuutoa katika mfumo wake uliozoeleka na unaoelewekaa kirahisi, nami niliuwasilisha kwa watoto. Nilitamani mnisikilize, nami niliogopa kwamba nisingefanikiwa kusikilizwa kama ningezungumza na watu wazima kwanza." "Basi, mimi niliazimu kuwaendea wadogo kabisa. Nilikusanya wasikilizaji ambao ni watoto wadogo; kama kundi hilo linaongezeka, na kama inaonekana kwamba wanasikiliza, wana shauku na kufurahishwa, kwamba wanaelewa mada na kuweza kuelezea somo kwa wengine, basi nina uhakika kuwa na mduara wa kundi la pili hivi karibuni, na katika zamu yao, watu wazima nao watatambua

kwamba kuna thamani ya kutoa muda wao kidogo na kuketi chini na kujifunza. Jambo hilo likitendeka, basi ushindi unakuwa umepatikana (dhumuni limefikiwa)." - "L. Gaussen, Daniel the Prophet, juzuu ya 2, Dibaji. [GC 365.1; PK Aya ya 27]

Jitihada hiyo ilifanikiwa. Alipozungumza na watoto, watu wazima walikuja kusikiliza. Korido ndefu  za kanisa lake zilijaa wasikilizaji makini. Miongoni mwao walikuwamo watu wenye vyeo na wasomi na watu wasiofahamika na wageni kutoka nchi za nje waliokuwa wanazuru Geneva; na kwa njia ile ujumbe ukachukuliwa na kupelekwa sehemu zingine. [GC 365.2; PK Aya ya 28]

Akiwa ametiwa moyo kwa mafanikio haya, Gaussen alichapisha mafundisho yake (lessons) akiwa na matumaini ya kuendeleza tabia yenye kukuza moyo wa kujifunza vitabu vya unabii katika makanisa ya watu waliokuwa wakizungumza lugha ya Kifaransa. "Kuchapisha mafundisho haya yaliyotolewa kwa watoto," asema Gausen, "ni kuzungumza na watu wazima ambao mara nyingi mno hudharau au kupuuza vitabu kama hivyo chini ya madai ya uongo kuwa havieleweki, 'Vinawezaje kuwa havieleweki na wakati watoto wenu wanavielewa?" "Mimi nilikuwa na shauku kubwa," aliongeza kusema, "ya kuyafanya maarifa ya unabii yapate kupendwa na kuwa maarufu katika makundi yetu, kwa kadiri iwezekanavyo." "Naam, hakuna ujifunzaji unaokidhi vizuri zaidi mahitaji ya wakati huu kuliko huo." "Ni kwa sababu ya jambo hili, sisi tunatakiwa kujiandaa kwa mateso yaliyo mlangoni, na kukesha kumngojea Yesu Kristo." [GC 365.3; PK Aya ya 29]

Ingawa yeye alikuwa ni mmojawapo wa wahubiri mashuhuri na waliopendwa sana wa lugha ya Kifaransa, Gaussen, baada ya muda fulani alisimamishwa kazi yake ya uchungaji, kosa lake kubwa likiwa kwamba badala ya kutumia katekisimu ya kanisa, kama kitabu cha mwongozo wa taratibu usio mkali au kuchoma kama vile mnyama wa kufugwa (cha upole sana) na chenye falsafa ile ya razini, ambacho ndani yake kilikuwa kinakaribia kukosa hata imani chanya ndogo, yeye alikuwa anatumia Biblia kutoa mafunzo yake kwa wale vijana (Biblia ni kali kama mnyama wa porini, angetumia katekismu ambayo imepoa makali kama mnyama wa kufugwa). Baadaye akawa mwalimu katika shule ya theolojia, wakati ule ule aliendelea na kazi yake kama Katekista siku ya Jumapili, akizungumza na watoto na kuwafundisha Maandiko. Kazi zake kuhusu unabii zilipendwa, nazo zilisisimua usikivu ndani ya mioyo ya watu wale. Kutoka kwenye kiti chake cha Uprofesa wa chuo kikuu, kupitia katika mtambo wa kuchapisha vitabu (au hata vyombo vya habari), na katika kazi yake aliyoipenda zaidi kama mwalimu wa watoto, kwa miaka mingi alishinikiza ushawishi mkubwa, nao ukaenea pahali pengi, naye akahamasisha watu wengi kuyageuza mawazo yao kuelekea katika kujifunza unabii ulioonyesha kwamba kuja Kwake Bwana kulikuwa kumekaribia. [GC 366.1; PK Aya ya 30]

**Watoto Wadogo- Wahubiri Wa Skandinavia**

Pia katika nchi za Skandinavia, yaani Sweden, Norway, Denmark, Iceland na Finland, ujumbe ule wa marejeo ulihubiriwa. Wengi waliamshwa kutoka katika uzembe wao wa kujiona kwamba wako salama, wakaungama na kuziacha dhambi zao, na kutafuta msamaha katika Jina Lake Kristo. Lakini viongozi wa kanisa lililokuwa likiongozwa na serikali, walizipinga vuguvugu hizi, na kwa njia ya ushawishi wao baadhi ya wale waliouhubiri ujumbe huu walitupwa gerezani. Mahali pengi wahubiri wa habari ya ujio wa haraka wa Bwana walinyamazishwa kwa njia hiyo. Mungu alipendezwa kuutuma ujumbe kwa njia ya mwujiza, kupitia kwa watoto wadogo. Kwa vile walikuwa na umri mdogo, sheria ya nchi haikuweza kuwabana, na hivyo waliepuka hukumu, na kuruhusiwa kuzungumza bila ya kusumbuliwa au kunyanyaswa. [GC 366.2; PK Aya ya 31]

Vuguvugu hii kwa sehemu kubwa ilikuwa miongoni mwa watu wa tabaka la chini, tena ilikuwa ni katika makazi duni ya vibarua ambamo watu walikusanyika kulisikia onyo. Wahubiri watoto wenyewe kwa sehemu kubwa walitoka katika vibanda vile vya kimaskini. Wengine miongoni mwao hawakuzidi umri wa miaka sita au nane hivi; na wakati maisha yao yalithibitisha kwamba walikuwa wanampenda Mwokozi, walikuwa wanajitahidi kuishi maisha ya utii, kulingana na kanuni takatifu za Mungu, kwa kawaida walionyesha akili na uwezo wa kawaida unaoonekana kwa watoto wa umri huo. Lakini basi, waliposimama mbele ya watu, ilikuwa ni dhahiri kwamba walisukumwa na uwezo uliopita upeo wa vipawa vyao walivyozaliwa navyo. Mwelekeo, sauti na tabia yao vilibadilika, na kwa uwezo wa ajabu na mkuu walitoa onyo la hukumu, wakitumia Maneno mahsusi ya Maandiko, wakisema: “Mcheni Mungu, na kumtukuza, kwa maana saa ya hukumu Yake, imekuja.” Walizikemea dhambi za watu, sio tu kwa kushutumu upotofu wa maadili kama vile uasherati, ulafi, ulevi na maovu, bali waliikemea roho ile ya kuipenda dunia, pamoja na kurudi nyuma kwao kiroho, na kuwaonya wasikilizaji wao ili wapate kuikimbia kwa haraka ghadhabu ile iliyokuwa inakuja. [GC 366.3; PK Aya ya 32]

**Mkono Wa Mungu Ulikuwepo Kwenye Vuguvugu Zile**

Watu walisikiliza, huku wakitetemeka. Roho wa Mungu anayetusadikishia uovu wa dhambi zetu, aliichoma mioyo yao. Wengi waliongozwa kuanza kuyachunguza Maandiko kwa shauku mpya na kina zaidi, wasio na kiasi kama walevi kupindukia na waasherati, na wasio waadilifu walifanya matengenezo katika maisha yao na hivyo kurekebishwa kwa matengenezo, wengine waliyatupilia mbali mazoea yao ya dhuluma na kazi kubwa ilikuwa imefanyika ambayo ilionekana kwa dhahiri kabisa, kiasi kwamba hata wachungaji wa kanisa linaloongozwa na serikali

walilazimika kukiri kwamba mkono wa Mungu ulikuwa pamoja na vuguvugu hilo. [GC 367.1; PK Aya ya 33]

Ilikuwa ni mapenzi ya Mungu kwamba habari za kuja Kwake Mwokozi zipate kutolewa katika nchi zile za Skandinavia; na sauti za watumishi Wake ziliponyamazishwa, Bwana aliweka Roho Wake juu ya watoto, ili kazi Yake ipate kutekelezwa. Yesu alipokaribia Yerusalemu, akikaribishwa na makundi ya watu waliokuwa wakishangilia, ambao walipiga kelele za shangwe na ushindi na kupeperusha matawi ya mitende, walimtangaza Yeye kama Mwana wa Daudi, Mafarisayo wenye wivu walimwita wakimwagiza awanyamazishe; lakini Yesu alijibu kwamba yote hayo yalifanyika ili kutimiza unabii, na ikiwa hao wangenyamaza, basi, mawe yenyewe yangepiga kelele. Watu wakiwa wamepatwa na hofu nyingi kutokana na vitisho vya makuhani na watawala, walisitisha utangazaji wao wa shangwe walipoyaingia malango ya Yerusalemu; lakini watoto waliokuwa katika nyua za hekalu, baadaye walidakia pambio, nao, wakiyatikisa matawi yao ya mitende, walipiga kelele, wakisema: "Hosana, Mwana wa Daudi!" Mathayo 21:8-16. Mafarisayo wakiwa wamechukizwa sana, walimwambia Yesu, "Wasikia hawa wasemavyo?" Yesu aliwaambia, "Naam, hamkupata kusoma, Kwamba kwa vinywa vya watoto wachanga na wanyonyao umekamilisha sifa?" Kama vile Mungu alivyofanya kupitia kwa watoto wakati ule wa ujio wa Kristo kwa mara ya kwanza, kadhalika alitenda kupitia watoto katika kuutoa ujumbe wa marejeo Yake. Neno la Mungu ni lazima litimizwe, kwamba, tangazo la kuja Kwake Mwokozi linapaswa kutolewa kwa watu wote, lugha zote, kila jamaa na mataifa yote. [GC 367.2; PK Aya ya 34]

William Miller na watendakazi wenzake walipewa kulihubiri onyo huko Amerika. Nchi hii ikawa kitovu cha vuguvugu kuu za Waadventista (Marejeo ya Yesu). Hapa ndipo unabii wa malaika wa kwanza ulitimizwa moja kwa moja (Ufunuo 14). Maandiko ya Miller na washirika wake yalibebwa hadi nchi za mbali. Popote pale wamishenari walipokuwa wamepenya katika ulimwengu wote, habari njema za kurudi upesi sana kwa Kristo zilipelekewa. Maeneo ya mbali na katika upana wake, ujumbe wa Injili ya Milele ulienda, ukisema: "Mcheni Mungu, na kumtukuza, kwa maana saa ya hukumu Yake imekuja." [GC 368.1; PK Aya ya 35]

Ushuhuda wa unabii ambao ulionekana kana kwamba unaonyesha kuja Kwake Kristo kutatokea katika majira ya kuchipua (Machi hadi Mei) ya mwaka wa 1844, uliwagusa watu sana akilini mwao. Ujumbe ulipokwenda jimbo hata jimbo, kila mahali palikuwa na mwamko mkubwa wa kupenda kuijua habari hii. Wengi walisadiki kwamba hoja zile zilizotolewa kutokana na vipindi vya kiunabii zilikuwa sahihi, nao, wakajitolea kutupilia mbali kiburi cha maoni yao, kwa furaha nyingi walipokea Ukweli. Wachungaji wengine waliweka pembeni maoni

yao na hisia zao za kimadhehebu, waliiacha mishahara yao, na makanisa yao na kujiunga katika kutangaza marejeo ya Yesu. Walakini, kwa ulinganifu, walikuwepo wachungaji wachache mno ambao walikuwa tayari kuupokea ujumbe Marejeo; hivyo, kwa sehemu kubwa uliachiwa zaidi kwa walei duni na wanyenyekevu. Wakulima waliyaacha mashamba yao, mafundi wa aina mbalimbali waliziacha zana zao, wafanya biashara waliacha bidhaa zao, wanataaluma waliziacha nyadhifa zao; na, hata hivyo, idadi ya watendakazi ilikuwa ndogo ikilinganishwa na kazi iliyopaswa kukamilishwa. Hali ya kanisa lisilomcha Mungu na ulimwengu uliokuwa umelala katika uovu wake, mambo hayo yaliilemea mioyo ya walinzi wa kweli na waaminifu, nao kwa hiari yao wenyewe, walijinyima kwa kufanya kazi ngumu, umaskini, na mateso, ili wapate kuwaita watu watubu na kupata wokovu. Ingawa walipingwa na Shetani, kazi ile ilisonga mbele kwa mafanikio na uhakika, na Ukweli wa marejeo ulipokewa na maelfu mengi ya watu. [GC 368.2; PK Aya ya 36]

### Shinikizo La Kuwasadikisha

Kila mahali ushuhuda unaopenya mpaka ndani ya moyo na kuuchunguza ulisikika, ukiwaonya wenye dhambi wa aina mbili, yaani wale walioipenda dunia hii na kisha wale waliokuwa makanisani kama washiriki, kusudi wapate kuikimbia hasira inayokuja. Kama alivyokuwa Yohana Mbatizaji, mtangulizi wa Kristo, wahubiri waliweka shoka penye shina la mti na kuwasihi wote ili wazae matunda yaletayo toba. Miito yao iliyowatingisha sana wasikilizaji, ilikuwa na tofauti kubwa ukilinganisha na kuwahakikisha watu matumaini ya amani na usalama, mambo ambayo yalisikika yakihubiriwa katika mimbari mashuhuru walizozipenda watu wengi; na kila mahali ujumbe ulipotolewa, uliwagusa watu mioyoni. Ushuhuda sahili na wa moja kwa moja wa Maandiko, ulioingia mpaka ndani ya mioyo yaani mahali palipostahili, ulieleweka kwa uweza wa Roho Mtakatifu, nao ulileta shinikizo la usadikisho kwa watu kuhusu hatia yao, na ni wachache sana waliweza kuupinga kabisa. Maprofesa wa dini walizinduliwa kutoka katika usalama wao wa uongo. Watu walitambua kurudi nyuma kwao, udunia wao, na kutokuamini kwao, kiburi chao na ubinafsi wao. Wengi wao walimtafuta Bwana kwa toba na kujinyenyekesha. Mapenzi yao yaliyokuwa yameving'ang'ania vitu vya ulimwengu huu kwa muda mrefu sana sasa waliyaelekeza kule mbinguni. Roho wa Mungu alikaa juu yao, na kwa mioyo yao iliyolainishwa na kutiishwa, waliungana na kupiga kelele, wakisema: "Mcheni Mungu, na kumtukuza, kwa maana ya hukumu Yake imekuja." [GC 369.1; PK Aya ya 37]

Wenye dhambi wakauliza kwa machozi: "Nifanye nini ili nipate kuokoka?" Wale ambao Maisha yao yalikuwa yamesifiwa kwa mawaa ya udanganyifu, walikuwa na shauku ya kuweka mambo sawa kwa kufidia walichochukua kwa udanganyifu. Wale wote waliopata Amani yao ndani ya Kristo walitamani sana kuwaona wengine wakiupata mbaraka huo pia. Mioyo ya wazazi ikawarudia

watoto wao, na mioyo ya watoto iliwaelekea wazazi wao. Vizuizi vya kiburi na ubaridi wa kutoonyesha moyo wa urafiki vilifagiliwa mbali. Maungamo ya dhati kutoka moyoni yalifanywa, na watu waliokuwamo nyumbani walifanya kazi kwa ajili ya kuwaletea wokovu watu walioishi nao karibu na wapendwa wao. Mara kwa mara ilisikika sauti ya maombezi yaliyotolewa kwa dhati na bidii. Kila mahali watu walijaa utungu wakimsihi sana Mungu. Wengi walipambana mieleka usiku kucha katika maombi ili wapate uhakikisho kwamba dhambi zao wenyewe zilikuwa zimesamehewa au kwa ajili ya kuongoka kwa jamaa zao au majirani (kama Yakobo, Mwanzo 32). [GC 369.2; PK Aya ya 38]

Watu wa matabaka yote walifurika kwenye mikutano ya Waadventista, watu ambao walikuwa wanahubiri marejeo ya Kristo. Matajiri kwa maskini, wakubwa kwa wadogo, wenye vyeo kwa wanyonge, kutoka katika nyanja zao mbalimbali walikuwa na matamanio ya kulisikia wenyewe fundisho la kuja Kwake Kristo kwa mara ya pili. Bwana akaizuia roho ya upinzani wakati watumishi Wake walipokuwa wakifafanua sababu za imani. Wakati mwingine mjumbe au chombo kilichotumiwa kilikuwa kinyonge; lakini Roho wa Mungu alitoa nguvu kwa ajili ya Ukweli Wake. Uwepo wa malaika watakatifu ulihisiwa katika mikutano hii, na wengi kila siku walikuwa wakiongezeka katika idadi ya waumini. Ushahidi wa kuja upesi kwa Kristo ulipokuwa unarudiwa tena na tena, makundi makubwa sana ya watu yalisikiliza maneno yale mazito yakiwa kimya hata hukuweza kusikia sauti ya mtu akipumua. Mbingu na Dunia zilionekana kama zinakaribiana sana. Uweza wa Mungu ulihisiwa ndani ya wazee na vijana na watu wa umri wa kati. Watu walizirudia nyumba zao huku sifa zikiwa vinywani mwao, na sauti ya shangwe ilivuma hewani katika usiku mtulivu. Hakuna hata mmoja aliyehudhuria mikutano hiyo awezaye kusahau picha zile za matukio mawazoni, zilizoamsha moyo wa kupenda sana kujifunza. [GC 369.3; PK Aya ya 39]

### Upinzani Mkubwa Wa Ujumbe Ule

Utangazaji wa wakati mahsusi wa ujio wa Kristo uliamsha upinzani mkali toka kwa watu wa tabaka zote, tangu kwa mchungaji mimbarani na kushuka chini mpaka kwa yule mwenye dhambi asiyejali kabisa, anayeitukana Mbingu. Maneno ya unabii yalitimizwa: "Katika siku za mwisho watakuja na dhihaka zao watu wenye kudhihaki, wafuatao tamaa zao wenyewe, na kusema, Iko wapi ahadi ile ya kuja Kwake? Kwa maana, tangu hapo babu zetu walipolala, vitu vyote vinakaa hali iyo hiyo, tangu mwanzo wa kuumbwa." 2 Petro 3:3, 4. Wengi waliodai kwamba wanampenda Mwokozi walitangaza kwamba wao hawakuwa na upinzani wowote dhidi ya fundisho lile la marejeo ya Kristo; ila walipinga tu kule kuweka tarehe halisi. Lakini jicho la Mungu linaloona mambo yote likaisoma mioyo yao. Watu hawa hawakupenda kuisikia habari ya kuja Kwake Kristo kuuhukumu ulimwengu huu katika haki. Walikuwa watumishi wasio waaminifu, matendo yao yasingestahimili ukaguzi wa Mungu anayeuchunguza mioyo, na waliogopa

kukutana na Bwana wao uso kwa uso. (Yer. 17:9, 10), Sio tu walikataa kusikiliza hoja zilizo wazi kutoka katika Biblia, bali pia waliwadhihaki watu waliokuwa wakimtarajia Bwana. Shetani na malaika zake walishangilia na kutupa dhihaka mbele ya Kristo na malaika watakatifu kwamba wale wanaodai kuwa watu Wake Mungu, walikuwa na upendo mdogo sana Kwake kiasi kwamba hawakutamani majilio Yake, nao waliogopa kukutana na Bwana wao. [GC 370.1; PK Aya ya 40]

"Hakuna aijuaye siku ile na saa ile" ilikuwa ndiyo hoja yao iliyoletwa mara nyingi na wale walioikataa imani ya marejeo Yake Kristo. Maandiko ni haya: "Walakini habari ya siku ile na saa ile hakuna ajuaye, hata malaika walio mbinguni, wala Mwana ila Baba peke Yake." Mathayo 24:36. Maelezo ya wazi na yenye kuafikiana na Andiko hili yalitolewa na wale waliokuwa wakimtarajia Bwana na matumizi yake mabaya yaliyofanywa na wapinzani wao yalifichuliwa wazi. Maneno hayo yalisemwa na Kristo katika maongezi Yake yanayostahili kukumbukwa, ambayo yalifanywa kati yake na wanafunzi Wake juu ya Mlima wa Mizeituni alipokuwa ametoka hekaluni kwa mara Yake ya mwisho. Wanafunzi Wake walikuwa wameuliza swali hili: "Nayo ni nini dalili ya kuja Kwako, na ya mwisho wa dunia?" Yesu aliwapa dalili nyingi, na kusema: "Myaonapo hayo yote, tambueni ya kuwa Yu karibu, milangoni. Aya ya 3,33. Kauli moja ya Kristo haipaswi kutumiwa ili kuiharibu kauli Yake nyingine. Ingawa hakuna mtu yeyote aijuaye siku, wala saa ya Ujio Wake, tumeelekezwa, tumefundishwa na tumetakiwa kujua wakati unapokaribia. Tunafunzwa pia kwamba kulidharau onyo Lake hilo na kukataa au kupuuza kujua ukaribu wa ujio Wake, kutaleta ajali ya kuangamia kwetu kama ilivyokuwa kwa wale walioishi katika siku za Nuhu kwa kukataa kujua ni wakati gani gharika ilikuwa inakuja. Tena, mfano ulio katika sura hiyo hiyo (Mathayo 24), unaonyesha matokeo tofauti kati ya mtumishi aliye mwaminifu na asiye mwaminifu, na kutangaza ajali ya yule aliyesema moyoni mwake, "Bwana Wangu anakawia," huonyesha kwa nuru gani Kristo atawachukulia na kuwazawadia wale atakaowakuta wakimngojea, na kufundisha habari za ujio Wake, na kwa wale wanaoukataa ujumbe huo. "Kesheni basi," anasema. "Heri mtumwa yule, ambaye Bwana Wake ajapo atamkuta akifanya hivyo." Mstari wa 42, 46. Usipokesha, Nitakuja kama mwivi, wala hutaijua saa Nitakayokuja kwako. " Ufunuo 3:3. [GC 370.2; PK Aya ya 41]

Paulo anazungumza habari za tabaka ambalo kwao marejeo ya Bwana yatakuwa jambo la kushtukiza, yaani litakuwa ghafla kama vile mwivi ajavyo usiku. Wakati wasemapo, Kuna amani na salama, ndipo uharibifu uwajiapo kwa ghafula,... wala hakika hawataokolewa." Lakini anaongezea kusema hivi kwa wale watakaokuwa wamelitii onyo la Mwokozi wao: "Bali ninyi, ndugu, hammo gizani, hata siku ile iwapate kama mwivi. Kwa kuwa ninyi nyote mmekuwa wana wa nuru, na wana wa mchana; sisi si wa usiku, wala wa giza." 1 Wathesalonike 5:2-5. [GC 371.1; PK Aya ya 42]

Hivyo ilionyeshwa kwamba Maandiko hayawapi idhini wanadamu kubaki katika ujinga kuhusu ukaribu wa ujio wa Kristo. Walakini wale waliotamani tu kutoa kisingizio cha kuukataa Ukweli na kisha wakaziba masikio yao wasisikie ufafanuzi huu na maelezo yanayosema, "Hakuna aijuaye siku ile na saa ile" yaliendelea kurudiwa kama mwangwi na watu jasiri kwa dhihaka na hata kutoka kwa watu waliodai kuwa wachungaji wa Kikristo. Watu walipoamshwa, na kuanza kudadisi kwa maswali ili waijue njia ile ya wokovu, waalimu wao wa dini walisimama kati yao na Ukweli, wakijitahidi kunyamazisha hofu zao kwa tafsiri za uongo za Neno la Mungu. Walinzi waliokosa uaminifu walijiunga kufanya kazi ya yule laghai mkuu (Shetani), wakipiga makelele, na kusema, Amani, amani, wakati Mungu alikuwa hajasema amani. Kama Mafarisayo katika siku Zake Kristo, wengi walikataa wenyewe kuingia katika ufalme wa mbinguni, na wale waliokuwa wakiingia wakawazuia. Damu ya roho hizi itatakiwa mikononi mwao. [GC 372.1; PK Aya ya 43]

Kwa kawaida, wale waliokuwa wanyenyekevu na wacha Mungu sana ndani ya makanisa ndiyo walikuwa wa kwanza kuupokea ujumbe. Wale waliojisomea Biblia wenyewe waliweza kuona maoni yaliyokuwa hayaambatani na Maandiko juu ya unabii ambao watu wengi walipendezwa na hiyo tafsiri wakati wahubiri mashuhuri wanaiwasilisha; na popote pale ambapo watu hawakutawaliwa na mvuto wa viongozi wa makanisa yao, yaani, popote pale walipolichunguza Neno la Mungu wao wenyewe, fundisho lile la marejeo lilihitaji tu kulinganishwa na Maandiko ili kuweza kulithibitisha kwamba mamlaka yake ilitoka kwa Mungu. [GC 372.2; PK Aya ya 44]

Watu wengi waliteswa na ndugu zao wasioamini. Ili kuweza kuvilinda vyeo vyao kanisani, wengine walikubali kunyamaza kimya kuhusu tumaini walilokuwa nalo; lakini wengine waliona kwamba utiifu wao kwa Mungu uliwakataza kabisa kuzificha zile Kweli alizokuwa amewakabidhi kama dhamana kwao. Si wachache walioondolewa kabisa katika ushirika wa kanisa, sio kwa sababu nyingine isipokuwa tu ile ya kueleza imani yao kuhusu marejeo Yake Kristo. Yalikuwa ni ya thamani sana kwao Maneno haya aliyosema nabii kwa wale waliostahimili kupimwa imani yao: "Ndugu zenu wawachukia ninyi, waliowatupa kwa ajili ya Jina Langu, wamesema. Na atukuzwe BWANA, tupate kuiona furaha yenu; lakini watatahayarika." Isaya 66:5. [GC 372.3; PK Aya ya 45]

Malaika wa Mungu walikuwa wakiangalia kwa shauku kubwa mno kuona matokeo ya onyo. Wakati ujumbe ulipokuwa umekataliwa na makanisa yote, malaika waligeuka na kwenda zao kwa huzuni. Lakini palikuwa na watu wengi ambao walikuwa bado hawajaribiwa juu ya Ukweli wa marejeo ya Masihi kwa mara ya pili. Wengi walipotoshwa na waume zao, wake zao, wazazi wao, au watoto wao, kisha wakashawishiwa kuamini ya kwamba ilikuwa ni dhambi hata kusikiliza tu uzushi ule kama ulivyokuwa ukifundishwa na Waadventisa. Malaika

waliagizwa kuwalinda kwa uaminifu watu, kwa maana nuru nyingine kutoka katika kiti cha enzi cha Mungu ilikuwa njiani ili iwaangazie juu yao. [GC 372.4; PK Aya ya 46]

Kwa shauku kubwa isiyoweza kuelezeka, wale waliokuwa wameupokea ujumbe, walikesha kwa ajili ya kuja Kwake Mwokozi wao. Wakati waliotazamia kumlaki ulikuwa umekaribia. Walikaribia saa hii kwa kicho na utulivu. Wakitulia na kuendelea na mawasiliano yao matamu na Mungu wao, na kuwa na juhudi na shauku ya kuipata amani ambayo ingekuwa yao katika maisha yale maangavu ya baadaye, ambayo walifikiria kwamba yalikaribia sana kufika. Hakuna hata mmoja miongoni mwa wale waliokuwa wamepata uzoefu wa tumaini na imani hiyo ambaye anaweza kuzisahau saa zile za thamani za kumngojea Bwana. Kwa majuma mengi kabla ya wakati ule, shughuli za kidunia, kwa sehemu kubwa sana, ziliwekwa kando. Waumini wanyofu wa moyo walichunguza kila wazo na mihemko ya mioyo yao kwa umakini sana kana kwamba wapo vitandani mwao wakingojea kifo chao na kisha baada ya saa chache waweze kufumba macho yao na kutoziona mandhari za dunia hii tena. Kulikuwa hakuna ushonaji wowote wa "majoho ya kupalia juu mbinguni au mavazi ya kupaa juu" *(Tazama Kiambatanisho)*; lakini wote waliona hitaji la kuwa na ushahidi utokao ndani yao, kuonyesha kwamba walikuwa wamejiandaa kukutana na Mwokozi; majoho yao meupe yalikuwa ni usafi wa moyo --tabia zao zolizotakaswa dhambi, kwa damu ya upatanisho ya Kristo. Laiti kama bado ingalikuwamo ndani ya wale wanaojiita watu wa Mungu leo, roho ile ile ya kujichunguza moyo, na imani ile ile ya dhati, iliyodhamiria, na isiyoyumbayumba! Kama wangekuwa wameendelea kujinyenyekesha wenyewe kwa njia kama hiyo mbele za Bwana na kuzipeleka dua zao kwa bidii mbele za kile kiti cha rehema (Ebr. 4:14-16), wangalikuwa na uzoefu wa hali ya juu zaidi kuliko walio nao sasa. Kuna sala chache sana, kuna kushawishiwa/kusadikishwa kudogo sana kwa kweli kuhusiana na hatia ya dhambi, na kule kukosekana kwa imani ile iliyo hai, huwaacha wengi wakiwa wamepungukiwa na ile neema iliyotolewa kwao kwa wingi sana na Mkombozi wetu. [GC 373.1; PK Aya ya 47]

Mungu alikuwa amekusudia kuwahakiki watu Wake. Mkono Wake ulifunika kosa katika ukokotoaji wa vipindi vya unabii. Waadventista wale hawakugundua kosa, wala halikugunduliwa na wasomi wa hali ya juu miongoni mwa wapinzani wao. Hao wapinzani wasomi walisema hivi:: "Ukokotoaji wenu wa nyakati za unabii ni sahihi. Tukio fulani kubwa linakaribia kutokea; lakini siyo kama hilo ambalo Ndugu Miller analitabiri; ni uongofu wa ulimwengu mzima na wala sio ujio wa pili wa Kristo." *(Tazama Kiambatanisho)*. [GC 373.2; PK Aya ya 48]

**Kukata Tamaa Kuchungu Sana**

Wakati walioungojea yaani wa matarajio ukapita, wala Kristo hakutokea kuwakomboa watu Wake. Wale ambao kwa imani na upendo wao wa dhati walikuwa wametarajia kumwona Mwokozi wao, walipata uchungu na kukatishwa tamaa mno. Lakini makusudi ya Mungu yalikuwa yametimizwa. Alikuwa akiipima mioyo ya wale waliojidai kuwa wanangojea kuja Kwake. Miongoni mwao kulikuwa na wengi ambao walikuwa hawajachochewa na nia kubwa zaidi ya vihofu. Kutangaza imani yao kulikuwa hakujabadilisha mioyo yao au maisha yao. Wakati tukio walilolitarajia lilipokosa kutokea, watu hawa walitangaza kwamba wao walikuwa hawajaumizwa au kutatishwa tamaa; kwamba hata hivyo, wao hawakuwahi kuamini kabisa ya kwamba Kristo angeweza kuja. Hawa wakawa miongoni mwa watu wa kwanza kuzomea huzuni waliyokuwa nayo waumini wa dhati. [GC 374.1; PK Aya ya 49]

Lakini Yesu na jeshi lote la mbinguni waliwaangalia kwa upendo na huruma wale waliokuwa wamejaribiwa na kuonekana kuwa ni waaminifu ambao bado walikuwa wamekatishwa tamaa. Laiti kama pazia linaloutenganisha ulimwengu huu unaoonekana kwa macho lingekuwa limekunjwa na kusogezwa nyuma, basi, malaika wangeweza kuonekana wakija karibu na watu hawa waaminifu na imara na kuwakinga dhidi ya mishale ya Shetani. [GC 374.2; PK Aya ya 50]

*Kuruka kwa malaika watatu angani, hakumaanishi kwamba tutaona malaika wakiruka siku moja juu angani wakituhubiri, bali sisi binadamu ndiyo wajumbe wa kuhubiri ujumbe huo kwamba Tumche Bwana na kumsujudu Yeye aliye Muumbaji kwa maana saa Yake ya hukumu inakuja, Na kwamba kutomcha na kumsujudu kuna matokeo mabaya. Kisha mafundisho yote ya uongo ndiyo Babeli nao watoayo mafundisho hayo wataanguka, ndio ujumbe wa malaika wa pili na malaika yule wa tatu anasema wale wenye mafundisho ya uongo watapokea ghadhabu nzito isiyochanganywa na huruma. *Rationalism au urazini, ni falsafa ya Magharibi, ni mtazamo unaozingatia sababu kama chanzo kikuu na mtihani wa maarifa. Mfano wa urazini ni kutoamini mambo ambayo yapo nje ya uwezo wetu kama miujiza. (falsafa) Nadharia yasemna kwamba msingi wa ujuzi ni sababu, badala ya uzoefu au ufunuo wa Mungu. Hili linapingana na Imani.

# SURA YA 21

# ONYO LAKATALIWA

**(Kuvuna Tufani)**

Ufupisho: Ni masikitiko kwamba wengi hawataki kujifunza Biblia kuhusu ujio wa Yesu wa mara ya pili. Malaika wa kwanza wa Ufunuo 14:6-7 anafuatiwa na malaika wa pili katika Ufunuo 14:8, ambaye anaelezea adhabu endapo onyo la malaika wa kwanza halitatiiwa. Ujumbe huu tunapaswa kwa hakika kuuhubiri leo kuliko wakati uliozungumzwa hapa.

Katika kuhulibiri fundisho la ujio wa mara ya pili wa Kristo, William Miller na wenzake walikuwa wamefanya kazi kwa kusudi moja tu la kuwaamsha watu wapate kujiandaa kwa ajili ya hukumu. Walikuwa wamejitahidi kuwaamsha wale waliodai kuwa wanayo dini wapate kuliona tumaini la Kweli la kanisa na hitaji lao la kuwa na uzoefu wenye kina katika maisha ya Ukristo, pia walijitahidi kuwaamsha wale waliokuwa hawajaoongoka kuhusu wajibu wao wa kutubu mara moja na kuongolewa na Mungu. "Hawakujaribu kuwaongoa watu wajiunge na dhehebu au kundi lolote la dini. Kwa hiyo walifanya kazi miongoni mwa vyama,

vikundi na madhehebu yote bila kuingilia taratibu au kanuni au nidhamu yao." [GC 375.1; PK Aya ya 1]

"Katika kazi zangu yote," alisema Miller, "sikuwahi kabisa kuwa na shauku au wazo la kuanzisha dhehebu jingine tofauti na kujitenga na madhehebu yaliyokuwepo, au kulinufaisha kanisa moja kwa hasara ya jingine. Nilikusudia kuyanufaisha makanisa yote. Nilidhani kuwaWakristo wote wangeweza kushangilia katika tarajio la marejeo Yake Kristo, na ya kwamba wale ambao wasingeweza kuona kama mimi nilivyoona, wasingekosa kuwapenda wale ambao wangelipokea fundisho hili, sikufikiri kwamba kungekuwa na ulazima wowote wa kuwa na mikutano ya ibada tofauti. Lengo langu zima lilikuwa ni ile shauku yangu ya kutaka watu waongolewe na wamwelekee Mungu, kuujulisha ulimwengu huu habari ya hukumu iliyokuwa inakuja, na kuwashawishi wanadamu wenzangu wafanye matayarisho ya moyo ambayo yangewawezesha kukutana na Mungu wao kwa amani. Wengi wa wale waliokuwa wameongolewa kupitia kazi yangu walijiunga na makanisa mbalimbali yaliyokuwepo." - Bliss, uk. 328. [GC 375.2; PK Aya ya 2]

Kwa vile kazi yake ilikuwa na matokeo ya kuyaboresha makanisa kwa kuongeza idadi ya washiriki na mambo ya kiroho, kwa muda fulani kazi hii ilikubalika machoni pa watu. Lakini, kwa kuwa wachungaji na viongozi wa dini waliamua kuyapinga mafundisho ya marejeo ya pili ya Yesu yaliyohitimishwa kipindi hiki, na kutaka kuzuia ghasia zilizoibuka kote juu ya fundisho hili la marejeo, si tu kwamba waliyapinga mafundisho hayo kutoka katika mimbari zao, bali pia waliwanyima washiriki wao fursa ya kuhudhuria kwenye mahubiri yanayohusiana na kuja kwa Kristo mara ya pili, au waliwanyima hata kule kuongea tu juu ya lile tumaini lao katika mikutano ile ya kijamii ya kanisa. Hivyo watu walioamini walijikuta wako katika hali ya kujaribiwa sana na mfadhaiko. Waliyapenda makanisa yao, nao walichukia kujitenga nayo; lakini walipoendelea kuuona ushuhuda wa Neno la Mungu ukikandamizwa, na haki yao ya kuuchunguza unabii ikikataliwa, basi, waliona kuwa utii wao kwa Mungu uliwakataza wasijisalimishe kwa viongozi hao. Wale waliojitahidi kuufungia nje ushuhuda wa Neno la Mungu, waliwaona kama sio sehemu inayounda Kanisa la Kristo, ambalo ni "nguzo na msingi wa Ukweli." Kuanzia pale na kuendelea walijiona kwamba wanayo haki ya kujitenga mbali na ule uhusiano wao wa makanisa ya awali. Katika kipindi cha majira ya joto ya mwaka 1844, watu karibu elfu hamsini walijiondoa kutoka katika makanisa yao ya awali. [GC 376.1; PK Aya ya 3]

Karibu na wakati huu, badiliko kubwa lilionekana wazi ndani ya makanisa yaliyo mengi Marekani kote (U.SA). Kwa miaka mingi palikuwa na hali ya kuongezeka kwa uhakika, tabia ya kufanana na mwenendo, mazoea na desturi za kidunia iliyoendelea kuongezeka taratibu, ila kwa uhakika, na wakati ule ule kuporomoka kwa kiwango cha maisha halisi ya kiroho; lakini katika mwaka ule

palikuwapo na ushahidi mwingi wa mmomonyoko wa ghafula, ulioonekana waziwazi karibu kwa makanisa yote katika nchi ya Marekani. Ingawa hakuna mtu aliyeweza kueleza sababu ya anguko hilo, ukweli wenyewe ulibainishwa wazi na ulitolewa ufafanuzi na vyombo vya habari na wahubiri mimbarani. [GC 376.2; PK Aya ya 4]

Katika mkutano wa Baraza la Presbyterian huko Philadelphia,* Bwana Barnes, mwandishi wa kitabu cha ufafanuzi wa Biblia (Biblia commentary) kilichokuwa kikitumika na watu wengi, na ambaye alikuwa mmojawapo wa wachungaji wa makanisa makuu katika mji ule "alisema kwamba yeye alikuwa katika kazi ya uchungaji kwa miaka ishirini, na ya kwamba mpaka wakati wa Huduma ya Meza ya Bwana ya mwisho, alikuwa hajapata kamwe kuiendesha huduma hii bila ya kuwapokea kanisani watu wapya wa idadi fulani, ambao walitaka kujifunza zaidi kuhusu wokovu, na kujiunga, ila sasa amekuwa hapokei hata mtu mmoja. Lakini sasa hakukuwa na uamsho wowote, hakukuwa na waongofu wapya, hakuna ukuaji katika neema unaoonekana, wala hakuna mtu anayekuja ofisini mwake kufundishwa na kuzungumza naye juu ya wokovu wa roho yake. Pamoja na ongezeko la shuguli nyingi, na matarajio mazuri ya biashara kati ya mataifa na uzalishaji wa bidhaa viwandani, lipo ongezeko kubwa la kuipenda dunia, yaani udunia unayajaza mafikara ya washiriki. Hivyo ndivyo hali ya mambo ilivyo kwa madhehebu yote." – Congregational Journal, Mei 23, 1844 *(Kanisa la kwanza katika mji huu uliokuwa makao makuu ya kwanza ya nchi ya Marekani). [GC 376.3; PK Aya ya 5]

**Makanisa Yashukua Chini Kiroho**

Katika mwezi wa Februari mwaka ule ule, Profesa Finney wa Chuo Kikuu cha Oberlin alisema: "Tumekuwa nao ukweli ndani ya akili zetu, kwamba, kwa jumla, Makanisa ya Kiprotestanti katika nchi yetu, kama hivi yalivyo, ama yamekuwa hayakujali, au yalikuwa yana chuki kabisa dhidi ya matengenezo yote ya kimaadili ya kizazi hiki. Kuna makanisa machache ambayo kwa kiasi fulani yana unafuu, lakini tofauti hii kwa ujumla haitoshi kuufanya uhalisia wa ukweli huo kuwa na mtazamo mwingine. Tunao pia ukweli mwingine unaothibitisha ushahidi wa hoja hii: Kule kukaribia kutoweka kabisa kwa ushawishi wa uamsho wa kiroho ndani ya makanisa hayo yote. Hali ya kutojali mambo ya kiroho imeenea karibu kila mahali, tena ni ya kina kirefu cha kutisha; hivyo vyombo vya habari vya kidini vya nchi nzima, kama vile magazeti vinatoa ushuhuda kuhusu jambo hili……Mahali pengi sana, washiriki wa kanisa kwa jumla wanatumia muda wao wote katika ibada ya mitindo (fasheni), -wanashikana mikono na watu wasiomcha Mungu katika hafla zao, kucheza densi, na katika tamasha za anasa nk.... Lakini hatuna haja ya kulielezea sana somo hili lillilo chungu sana. Inatosha tu kusema kwamba ushahidi unazidi kuwa mzito sana, na unaotuminya sana kama mzigo mzito, na kubiringika kwetu kwa kutuonyesha kwamba

makanisa kwa jumla yanazidi kuzorota kwa kuporomoka kimaadili kwa namna ya kusikitisha sana. Yamekwenda mbali sana na Bwana, Naye amejiondoa kutoka katika makanisa hayo." [GC 377.1; PK Aya ya 6]

Na mwandishi wa jarida la Religious Telesope (Darubini ya Kiroho) anashuhudia hivi; "Kamwe hatujapata kushuhudia kurudi nyuma kukubwa kwa ujumla kwa mambo ya kidini kama inavyoonekana wakati huu wa sasa. Kwa kweli, kanisa linapaswa kuamka na kuchunguza chanzo cha ugonjwa huo; kwa maana tatizo hili ni dhiki kubwa ambayo kila mtu aipendaye Sayuni hana budi kulitazama hivyo. Tunapokumbuka kesi za waongofu wa kweli "jinsi walivyo wachache mno, tena mmoja yuko hapa na mwingine kulee, na kuona hali ambayo karibu kabisa haina dawa ya wenye dhambi wasiotaka toba, wajeuri, wasio na kicho tena wenye mioyo migumu mno, karibu tunashangaa kabisa, nasi bila kupenda kwetu, tunajikuta tunapaza sauti kwa kushangaa, 'Je, Mungu amesahau kuwa mwenye rehema kwetu? Au, mlango wa rehema umefungwa kwetu?' [GC 377.2; PK Aya ya 7]

Hali kama hiyo haiwezi kuwapo kamwe bila kuwapo na chanzo katika kanisa lenyewe. Giza la kiroho linaloyaangukia mataifa, makanisa, na watu binafsi, lipo, sio kwa sababu ya kuondolewa kiholela kwa misaada ya neema ya Mungu bila sababu maalum kwa upande wa Mungu, bali kwa sababu ya kutoijali, kuipuuza au kuikataa nuru ya Mungu kwa upande wa wanadamu. Mfano mzuri wa kuvutia sana kuhusu kweli hiyo umewasilishwa katika historia ya Wayahudi katika nyakati za Masihi. Kwa kujitolea kikamilifu kutumia maisha yao yote katika mambo ya ulimwengu huu na kumsahau Mungu na Neno Lake, ufahamu wao ulitiwa giza, mioyo yao ikawa na mwelekeo wa kidunia na kujaa tamaa mbaya za mwili hasa zihusuzo ngono. Hivyo ndivyo walivyopata ujinga wao (kuwa mbumbumbu) wa kutokutambua kuja Kwake Masihi, na katika kiburi chao na kutokuamini kwao wakamkataa Mkombozi wao. Hata wakati ule Mungu hakulizuia taifa hilo la Kiyahudi lisipate maarifa ya wokovu au lisishiriki fursa ya mibaraka yake. Lakini wale walioikataa ile Kweli walipoteza hamu yao yote ya kuitamani Zawadi ya Mbinguni. Walikuwa "wameliweka giza kuwa nuru, na nuru kuwa giza," mpaka nuru iliyokuwamo ndani yao ilipogeuka na kuwa giza, na giza hilo lilikuwa kubwa sana! [GC 377.3; PK Aya ya 8]

Inapatana na sera zake Shetani kuwaona wanadamu wakiendelea kubaki na mwonekano tu wa dini wakati roho ya utauwa hai inakuwa haipo kwao. Baada ya wao kuikataa injili, Wayahudi kwa juhudi na ari kubwa waliendelea kuzidumisha na kuzitetea taratibu/desturi zao za zamani za ibada, kwa bidii/usongo walitunza sana kujitenga kwao na mataifa (upekee wao), wakati wao wenyewe hawakuweza kukiri kwamba uwepo Wake Mungu ulikuwa hauonekani tena miongoni mwao. Unabii wa Danieli ulioonyesha pasipo kukosea wakati wa kuja Kwake Masihi, na kwa wazi kabisa ulitabiri juu ya kifo Chake, kiasi kwamba wao

waliwakatisha tamaa watu wasijifunze unabii ule, na mwishowe marabi wakawatamkia laana wale wote ambao wangejaribu kukokotoa wakati huo. Katika upofu na moyo usiokuwa na toba, watu wa Israeli katika kipindi cha karne zilizofuata walikuwa hawajali fursa za neema ya wokovu zilizotolewa kwao kwa wingi, hawakuzingatia ile mibaraka ya injili, wala onyo lile zito na la kuogofya, na hatari ya kuikataa nuru ile itokayo mbinguni. [GC 378.1; PK Aya ya 9]

Mahali po pote pale panapokuwapo na kisababishi, matokeo yale yale hufuata. Yule ambaye kwa makusudi kabisa anaizima sauti ya ushawishi iliyo ndani yake ambayo inamhakikishia kuhusu wajibu wake umpasao, ati kwa kuwa inaingilia mapenzi yake, hatimaye atapoteza uwezo wake wa kupambanua kati ya Ukweli na uongo. Ufahamu wake utajazwa giza, dhamiri yake hupata sugu (hufa ganzi), moyo wake huwa mgumu, na roho yake itatengwa mbali na Mungu. Mahali pale ambapo ujumbe wa Ukweli unapigwa teke au kudharauliwa, kanisa hapo litafunikwa na giza; imani na upendo wao utapoa, yaani utauwa utakuwa baridi kabisa, na mafarakano na malumbano yataingia. Washiriki wa kanisa huweka maslahi na nguvu zao katika kutafuta mambo ya dunia hii, na wenye dhambi wanakuwa wagumu katika hali yao ya uovu na kukataa kutubu. [GC 378.2; PK Aya ya 10]

**Onyo Kwa Kanisa**

Ujumbe wa malaika wa kwanza wa Ufunuo 14, ulioitangaza saa ya hukumu ya Mungu na kuwaita wanadamu wamche Mungu na kumwabudu, ulikuwa umekusudiwa kuwatenga watu wa Mungu ambao walimkiri Yeye, mbali na mivuto ipotoshayo ya ulimwengu huu, na kuwaamsha ili wapate kuiona hali yao halisi ya kuipenda dunia hii na kurudi nyuma kwao. Katika ujumbe huo, Mungu amelitumia onyo kanisa, ambao kama ungekubaliwa na kupokelewa, basi, kanisa lingekuwa limesahihisha maovu yao yaliyokuwa yanalitenga mbali nan Yeye. Laiti kama wangeupokea ujumbe ule kutoka mbinguni, na kuinyenyekesha mioyo yao mbele za Bwana na kwa unyofu wa moyo wajitahidi kufanya matayarisho ili waweze kusimama mbele Zake, Roho na uweza wa Mungu ungekuwa umejidhihirisha wazi miongoni mwao. Kanisa lingekuwa limefikia tena hali ile nzuri sana ya umoja, imani, na upendo, mambo ambayo yalikuwako katika siku zile za Mitume, waumini hawa walipokuwa na moyo mmoja na roho moja," na "Kulinena Neno la Mungu kwa ujasiri," wakati Bwana alipoliongeza kanisa kila siku kwa wale waliokuwa wakiokolewa." Matendo 4:32, 31; 2:47. [GC 379.1; PK Aya ya 11]

Ikiwa wale wanaojiita watu wa Mungu wangeipokea nuru kama inavyoangaza juu yao kutoka katika Neno Lake, basi, wangeweza kuufikia ule umoja ambao Kristo aliuombea, mshikamano ambao Mtume anaueleza kuwa ni "umoja wa Roho katika kifungo cha amani." Yeye asema kuna "Mwili mmoja, na Roho Mmoja, kama na mlivyoitwa katika tumaini moja la wito wenu. Bwana Mmoja, imani

moja, ubatizo mmoja.” Waefeso 4:3-5 (Kanisa ni mwili wa Kristo -Kol. 1:18). [GC 379.2; PK Aya ya 12]

Hayo yalikuwa ndiyo matokeo mazuri yenye baraka waliyopata wale walioukubali ujumbe wa marejeo Yake Kristo. Watu walitoka katika madhehebu mbalimbali; na vikwazo vya madhehebu yao vilitupwa chini kwa nguvu; itikadi au imani zao za dini (creeds) zilizokuwa zikikinzana zikavunjwa- vunjwa kabisa na kuwa na udogo wa atomi; tumaini lile lisilotokana na Biblia la milenia yaani miaka elfu moja ya muda mfupi hapa duniani likaachwa kabisa, maoni ya uongo juu ya ujio wa mara ya pili wa Kristo yalisahihishwa, kiburi chao na kufanana kwao na ulimwengu, vilifagiliwambali; makosa waliyotendeana wenyewe kwa wenyewe yaliungamwa; mioyo yao ilifungamanishwa katika ushirika mtamu sana kuliko wote, na upendo na furaha vikatawala kwa hali ya juu kabisa. Endapo fundisho hili liliwafanyia hivi watu hawa wachache waliolipokea, basi, lingeweza kutenda jambo hilo hilo kwa wote ambao wangelipokea. [GC 379.3; PK Aya ya 13]

Lakini kwa ujumla, makanisa, wachungaji au wahudumu wao hawakulipokea onyo hilo, na hawa kama walinzi “katika kuta za nyumba ya Israeli,” wangepaswa kuwa wa kwanza kuzitambua ishara za ujio Wake Yesu kwa mara ya pili, ila walikuwa wameshindwa kujifunza Ukweli kutoka katika ushuhuda wa manabii au kutokana na ishara za nyakati. Kwa kadri matumaini ya kidunia na matamanio ya kutafuta makuu yalipoujaza moyo wao, upendo wao kwa Mungu na imani yao katika Neno Lake vikawa vimepoa; na lile fundisho la marejeo Yake Kristo lilipoletwa kwao, likaamsha tu moyo wa chuki isiyokuwa na sababu na kutokuamini. Ule ukweli kwamba, kwa sehemu kubwa, ujumbe ule ulihubiriwa na walei ulisisitizwa kama ndiyo zana ya kuupinga. Kama ilivyokuwa katika siku za zamani, ushuhuda wazi wa Neno la Mungu ulikutana na swali hili: “Ni nani katika wakuu amwaminiye, au katika Mafarisayo?” Nao waligundua kwamba ilikuwa ni kazi ngumu kuzikanusha hoja zilizotolewa kutokana na vipindi vya kiunabii, wengi wao waliwakatisha watu tamaa ili wasipate kujifunza unabii huu, wakawa wakifundisha kwamba vitabu vile vya kiunabii vilikuwa vimetiwa muhuri na visingeweza kueleweka (Daniel na Ufunuo). Watu wengi sana, kwa kuwatumainia wachungaji wao kabisa, walikataa kabisa kulisikia onyo lile; na wengine, ijapokuwa wengine walishawishiwa na kuuamini Ukweli, hawakuthubutu kuikiri mbele ya watu, wasije “wakatengwa au kutupwa nje na sinagogi.” Ujumbe ambao Mungu aliutuma kwa madhumuni ya kulipima na kulitakasa/kulisafisha kanisa Lake, ulidhihirisha wazi kwamba idadi kubwa ya watu ilikuwa imeweka mapenzi yao katika ulimwengu huu badala ya kuyaweka kwa Kristo. Vifungo vile vilivyowafunga na ulimwengu huu vilikuwa na nguvu kuliko vivutio vilivyowaelekeza mbinguni. Walichagua kuisikiliza sauti ya hekima ya ulimwengu

huu na kuupa kisogo ujumbe wa Ukweli (kukengeuka), ambao uliuchunguza na kuuhoji moyo wao. [GC 380.1; PK Aya ya 14]

Kwa kulikataa onyo la malaika wa kwanza, walikuwa wameikataa njia iliyokuwa imewekwa na Mbingu kwa ajili ya kuponywa kwao (ukombozi au urejeshwaji wao). Wakampiga teke yule mjumbe mkarimu na mwenye neema, ambaye angeweza kuyasahihisha maovu yao yaliyowatenga mbali na Mungu, na kwa shauku kubwa zaidi waligeuka na kuanza kutafuta urafiki na ulimwengu Hiki ndicho kilikuwa chanzo cha hali yao ya kutisha ya kuipenda sana dunia hii, kurudi nyuma, na kifo cha kiroho kilichokuwamo ndani ya makanisa katika mwaka 1844. [GC 380.2; PK Aya ya 15]

Katika Ufunuo 14 malaika wa kwanza anafuatwa na malaka wa pili anayetangaza: "Umeanguka, umeanguka Babeli, mji ule mkubwa, ambao ndio uliowanywesha mataifa yote mvinyo ya ghadhabu ya uasherati wake." Ufunuo 14:8. "Babeli" limetokana na neno "Babel," na linamaanisha machafuko au mkanganyiko. Linatumika katika Maandiko kuonyesha mifumo mbalimbali ya dini za uongo au dini zilizomwasi Mungu. Katika Ufunuo 17, Babeli imewasilishwa kama mwananamke-Kielelezo kinachotumiwa katika Biblia kama alama ya kanisa, mwanamke safi, huwakilisha kanisa safi, na mwanamke kahaba huwakilisha kanisa lililomwasi Mungu. [GC 381.1; PK Aya ya 16]

Katika Biblia, tabia takatifu inayodumisha uhusiano uliopo kati ya Kristo na Kanisa Lake huwakilishwa kwa njia ya muungano wa ndoa (Efe. 5:25- 27,32). Bwana amewaunganisha watu Wake na Yeye Mwenyewe, kwa njia ya agano takatifu na zito, Yeye akiahidi kuwa Mungu wao, na wao Wanatoa kiapo wenyewe Kwake kwa ahadi ya kuwa watu Wake na Wake Yeye peke yake. Yeye anatangaza, akisema: "Nami nitakuposa uwe Wangu kwa milele; naam, nitakuposa kwa haki, na kwa hukumu, na kwa ufadhili, na kwa rehema."Hosea 2:19. Na tena anasema "Kwa kuwa Mimi ni mume wenu," Yeremia 3:14. Naye Paulo anatumia mfano uo huo katika Agano Jipya anaposema: "Nimewaposea Mume mmoja, ili nimletee Kristo bikira safi." 2 Wakorintho 11:2. [GC 381.2; PK Aya ya 17]

Kukosa uaminifu (uzinzi) kwa kanisa dhidi ya Kristo kwa njia ya kuruhusu imani na mapenzi yake kugeuzwa kutoka Kwake (mbali na Yeye), na kuruhusu kuyapenda mambo ya dunia hii kuujaza moyo wake, ni sawa na kukivunja nadhiri ya (kiapo). Dhambi ya Israeli kwa kumwacha Bwana inawakilishwa kwa kielelezo hiki hiki; na upendo wa ajabu wa Mungu walioudharau kwa njia ile umeonyeshwa kwa picha hiyo inayogusa moyo: "Nalikuapia, nikafanya agano nawe, aseme Bwana MUNGU, ukawa Wangu." "Nawe ulikuwa mzuri mno, ukafanikiwa hata kufikilia hali ya kifalme. Sifa zako zikaenea kati ya mataifa kwa sababu ya uzuri wako; kwa maana ulikuwa mkamilifu, kwa sababu ya utukufu Wangu niliokuwekea,... Lakini uliutumainia uzuri wako, ukafanya mambo ya kikahaba

kwa sababu ya sifa zako." "Kama vile mke amwachavyo mumewe kwa hiana, ndivyo ninyi mmetenda kwa hila Mimi, Ee nyumba ya Israeli, asema Bwana; "kama mke aziniye, akaribishaye wageni badala ya mumewe!" Ezekiel 16:8, 13-15, 32; Yeremia 3:20. [GC 381.3; PK Aya ya 18]

Katika Agano Jipya, lugha inayofanana sana na hiyo imetumiwa kwa wale wajiitao Wakristo, ambao hutafuta kuwa na urafiki na dunia hii kuliko kutafuta kukubaliwa na Mungu. Asema hivi Mtume Yakobo: "Enyi wazinzi, hamjui ya kwamba kuwa rafiki wa dunia ni kuwa adui wa Mungu? Basi kila yoyote atakaye kuwa rafiki wa dunia hujifanya kuwa adui wa Mungu" (Yak. 4:4). [GC 382.1; PK Aya ya 19]

### Mwanamke Wa Fumbo La Ufunuo

Mwanamke (Babeli) wa Ufunuo 17 anaelezwa kuwa "amevikwa nguo za rangi ya zambarau na nyekundu, aliyepambwa kwa dhahabu na vito vya thamani na lulu, naye alikuwa na kikombe cha dhahabu mkononi mwake, kilichojaa machukizo na uchafu:...na katika paji la uso wake limeandikwa jina; Siri, Babeli Mkubwa, mama wa makahaba." Nabii asema hivi: "Nikamwona yule mwanamke amelewa kwa damu ya watakatifu, na kwa damu ya mashahidi wa Yesu." Babeli anatangazwa tena kuwa ni "mji ule mkubwa wenye ufalme juu ya wafalme wa nchi." Ufunuo 17:4-6, 18. Mamlaka ile ambayo ilidumisha kwa karne nyingi utawala wake wa kidhalimu au kidikteta juu ya wafalme wa ulimwengu ule wa Jumuiya ya Wakristo ilikuwa Rumi. Rangi ya zambarau na nyekundu, dhahabu na vito vya thamani na lulu, huchora waziwazi picha ya utukufu wake na fahari yake iliyozidi ile ya ukuu wa kifalme (angalia pia mavazi na mapambo ya viongozi kwenye historia-vitabuni na mtandaoni), mambo ambayo jimbo lile la see la Rumi* lenye majivuno makuu, lilijigamba kuwa nayo. Wala hakuna mamlaka au serikali nyingine ambayo kiuhalisia ingeweza kutangazwa kuwa ilikuwa "Imelewa kwa damu ya watakatifu," kama kanisa ambalo limewatesa wafuasi wa Kristo kwa ukatili sana. Babeli anashtakiwa pia kwa dhambi ya kuungana isivyo halali (kuzini) na "wafalme wa nchi." Ilikuwa ni kwa njia ya kujitenga mbali na Bwana, na kuungana na wapagani/makafiri, ndipo kanisa la Kiyahudi liligeuka na kuwa kahaba (Ezekieli 23); naye Rumi (kama kanisa), akifanya ukahaba na kujinajisi kwa namna iyo hiyo kabisa, kwa kutafuta kuungwa mkono (au msaada) kutoka kwa mamlaka za kidunia, anapokea hukumu iyo hiyo. [GC 382.2; PK Aya ya 20]

### Anguko La Babeli

Babeli unasemwa kuwa ni "Mama wa Makahaba." Kule kusema anao binti zake ni lazima uwe ni mfano unaowaklisha makanisa yale yanayoyang'ang'ania mafundisho yake pamoja na mapokeo yake, na kufuata mfano wake katika kutupilia mbali Ukweli pamoja na kukubaliwa/upendeleo wa Mungu kwa

madhumuni ya kufanya muungano usio halali (haramu) na ulimwengu huu. Ujumbe wa Ufunuo 14, unaotangaza anguko la Babeli hauna budi kuyahusu yale mashirika ya kidini (makanisa) ambayo zamani yalikuwa safi na sasa yamegeuka na kuwa maovu. Kwa kuwa ujumbe huo unafuata baada ya onyo hilo la hukumu (fungu la 6,7), basi, hauna budi kutolewa katika siku hizi za mwisho; kwa hiyo hauwezi kurejelea Kanisa la Rumi peke yake kwa kuwa kanisa hilo limekuwa katika hali yake hiyo ya kuanguka kwa karne nyingi. Zaidi ya hapo, katika sura ile ya kumi na nane ya Ufunuo, watu wa Mungu wanaitwa ili watoke Babeli. Kulingana na andiko hilo, watu wa Mungu wengi ni lazima bado wamo Babeli. Naam, ni katika mashirika gani ya kidini ambamo sehemu kubwa zaidi ya wafuasi wa Kristo wanapatikana hivi sasa? Bila shaka, ni katika makanisa mbalimbali yanayoikiri imani ya Kiprotestanti. Wakati ule wa kuzaliwa kwake makanisa haya mwanzoni, yalichukua msimamo bora sana wa kumtetea Mungu na Ukweli Wake, na baraka Zake zilikuwa pamoja nao. Hata ulimwengu usioamini ulibidishwa kukiri matokeo yenye kunufaisha yaliyoandamana na kuzikubali kanuni zile za injili. Kwa kutumia Maneno haya aliyosema nabii huyo kwa Israeli: "Sifa zako zikaenea kati ya mataifa kwa sababu ya uzuri wako; kwa maana ulikuwa mkamilifu, kwa sababu ya utukufu Wangu niliokutia, asema Bwana MUNGU." Lakini (Waprotestanti hao) walianguka kwa tamaa ile ile ambayo ilikuwa imeleta laana na maangamizi kwa Israeli—shauku ya kuiga desturi za wale wasiomcha Mungu na kuwaposa (kuwatongoza) na kufanya urafiki nao. "Lakini uliutumainia uzuri wako, ukafanya mambo ya kahaba kwa sababu ya sifa yako." Ezekieli 16:14, 15. [GC 382.3; PK Aya ya 21]

**Onyo Kuungana Na Ulimwengu**

Makanisa mengi ya Kiprotestanti yanafuata nyayo za Rumi kwa kujifungamanisha kwa njia haramu pamoja na "wafalme wa dunia" - yaani, makanisa hayo yanayoongozwa na serikali au makanisa ya dola, yakiwa na uhusiano wa karibu na serikali za kiraia; yakijumuishwa na madhehebu mengine, kwa njia ya kutafuta kukubaliwa na ulimwengu huu. Tena neno hili "Babeli"- yaani, machafuko - linaweza kufaa kutumika kwa madhehebu hayo ya dini kwa usahihi kabisa, yote yakidai kwamba yanapata mafundisho yao ya dini kutoka katika Biblia, lakini huku wakiwa wamegawanyika takribani katika madhehebu au makundi yasiyo na idadi, yaliyo na itikadi na nadharia (Creeds) ambazo zinatofautiana na kupingana sana. [GC 383.1; PK Aya ya 22]

Pamoja na muungano huo wa dhambi na haramu na ulimwengu huu, makanisa hayo yaliyojitenga na Rumi yanaonyesha baadhi ya sifa/tabia zake Rumi. [GC 383.2; PK Aya ya 23]

Kitabu cha Kanisa Katoliki la Rumi kinatoa hoja yake isemayo hivi: "Ikiwa Kanisa la Rumi lilipata kuwa na hatia ya kuwa na ibada ya sanamu kuhusiana na

watakatifu (waliokufa zamani), basi, binti yake, yaani, Kanisa la Anglikana (Church of England), anasimama akiwa na hatia ile ile, kwani ana makanisa kumi yaliyowekwa wakfu kwa ajili ya Maria, na kanisa moja tu ndilo limewekwa wakfu kwa Kristo." —Richard Challoner, The Catholic Christian, instructed, Dibaji, ukurasa wa 21, 22. [GC 384.1; PK Aya ya 24]

Naye Dkt. Hopkins katika "A Treatise on the Millenium," anatangaza akisema: "Hakuna sababu ya kufikiri roho ya Mpinga Kristo na desturi zake zimefungamanishwa peke yake tu na kanisa ambalo kwa sasa linaitwa Kanisa la Roma. Makanisa ya Kiprotestanti yanacho kiwango kikubwa cha roho ya Mpinga Kristo ndani yake, nayo yako mbali sana na kufanyiwa matengenezo kamili kutokana na ...... ufisadi na maovu yake." - Samuel Hopkins, Kazi, juzuu ya 2, uk. 328. [GC 384.2; PK Aya ya 25]

Kuhusiana na habari za utengano kati ya Kanisa la Presbyterian kutoka Roma, Dkt. Guthrie anaandika hivi: "Miaka mia tatu iliyopita, kanisa letu, likiwa na Biblia iliyofunguliwa wazi juu ya bendera yake, na tamko lake la kauli mbiu ya hamasa yenye maneno haya, 'Yachunguzeni Maandiko,' kwenye hati-kunjo yake, lilitembea kijeshi na kutoka nje ya malango makubwa ya Rumi." Kisha anauliza swali hili la muhimu: "Je! walitoka Babeli wakiwa safi?"-Thomas Guthrie, The Gospel in Ezekiel, ukurasa wa 237. [GC 384.3; PK Aya ya 26]

"Kanisa la Uingereza au Kianglikana," asema Spurgeon, "linaonekana kana kwamba limedonolewa donolewa na kuliwa kabisa kwa kuzishika Sakramenti; lakini hata ule Ukristo wao usiozikubali baadhi ya kanuni za Kanisa hilo, unaonekana kama karibu umetobolewa vibaya sana na falsafa za ukafiri/upagani. Wale tuliowatarajia kwamba wana mambo mazuri zaidi, wanakengeuka na kwenda kando, mmoja baada ya mwingine, na kuiacha misingi halisi ya imani. Mimi naamini kabisa kwamba moyo halisi wa Uingereza umetobolewa-tobolewa na matundu kama sega la asali kwa ukafiri mbaya sana ambao bado unathubutu kwenda hata mimbarani na kujiita ni Ukristo bado." [GC 384.4; PK Aya ya 27]

Lakini chanzo cha huu ukengeufu mkuu ilikuwa ni kitu gani hsa? Kanisa liliachaje usahili wa injili kwa mara yake ya kwanza? Ni kwa njia ya kuiga desturi au mazoea ya upagani, ili kuwawezesha Wapagani waukubali Ukristo kwa urahisi. Hata katika siku zake, Mtume Paulo alisesema, "Maana Siri ya kuasi sasa hivi inatenda kazi." 2Wathesalonike 2:7, Wakati wa kipindi walichoishi mitume kanisa liliendelea kuwa safi ukilinganisha na nyakati zingine. Lakini "kuelekea mwishoni mwa karne ya pili, karibu makanisa yote yalikuwa yamejenga muundo na tabia mpya; lakini usahili wa kwanza ulikuwa umetoweka (taratibu rahisi za ibada zilitoweka); tena, bila kutambua, wanafunzi wa zamani walipoendelea kupumzika makaburini mwao, watoto wao pamoja na waongofu wapya,... walijitokeza na kusuka mwelekeo mpya kwenye kazi ya Mungu." — Robert Robinson, Ecclesiastical Researches, ch. 6, kifungu. 17, uk. 51. Ili kujipatia

waongofu wapya, kanuni ile yenye kiwango cha juu cha imani ya Kikristo ilishushwa chini, na matokeo yake "mafuriko ya upagani, yakawa yakitiririka na kuelekea ndani ya kanisa, na yakibeba mle pamoja na desturi zake, taratibu zake za ibada, matendo na sanamu zake." — Gavazzi Lecturers, ukurasa wa 278. Dini ya Kikristo ilipojipatia ukubali na msaada wa kuungwa mkono na watawala wa kidunia, ilipokewa kwa jina tu na watu wengi sana; wakati kwa mwonekano wa nje walikuwa wanaonekana ni Wakristo, wengi "kwa tabia yao ya ndani waliendelea kubaki wapagani, wakiendelea kuziabudu zile sanamu zao kwa siri." -[GC 384.5; PK Aya ya 28]

**Njia Ile Ile Yarudiwa**

Je, mchakato huo huo haujarudiwa tena karibu na kila kanisa linalojiita ni la Kiprotestanti? Kama Waanzilishi wake, yaani, wale waliokuwa na roho ya dhati ya kufanya matengenezo, wanapokufa, watoto wao hujitokeza na "kuunda upya mwelekeo wa kazi au sera ya kazi ya Mungu." Huku kwa upofu wao wanashikilia imani ya baba zao (creed) na kukataa kabisa kuipokea nuru au Kweli nyingine endelevu zaidi ya ile waliyoiona (baba zao), watoto hao wa Wanamatengenezo wanajitenga mbali sana na kielelezo kile cha unyenyekevu, kujikana nafsi, na kukana na kuachana na ulimwengu huu kwa njia hiyo "taratibu sahili za ibada ya kwanza hutoweka." Mafuriko yenye mwelekeo wa kidunia, yanayobubujika kuelekea ndani ya kanisa, kisha hubeba pamoja nalo "desturi zake, matendo yake, taratibu zake za ibada, na sanamu zake." [GC 385.1; PK Aya ya 29]

Ole! Kwa kile kiwango cha kutisha cha urafiki na dunia hii, ambao "uadui na Mungu" unaopaliliwa na kudumishwa miongoni mwa wale wanaodai kuwa ni wafuasi Wake Kristo! Ni kwa umbali gani makanisa yale mashuhuri yanayopendwa na watu wengi yamekengeuka kutoka katika kanuni na kiwango cha cha Biblia unyenyekevu, kujikana nafsi, taratibu za ibada sahili na zisizokuwa na mapambo, na utauwa! Alisema hivi John Wesley, alipozungumiza juu ya matumizi sahihi ya fedha: "Usitumie vibaya sehemu yoyote ya talanta hiyo ya thamani nyingi mno kwa ajili tu ya kuridhisha tamaa zenu za macho, kwa mavazi yanayozidi kiasi katika kupendeza au yenye gharama kubwa, au kwa mapambo yasiyokuwa ya lazima. Msitapanye sehemu yoyote ya talanta kwa kuzipamba nyumba zenu kwa mitindo ya ajabu, isiyo ya kawaida; kwa samani (fanicha) isiyozingatia tabia ya kiasi au yenye gharama kubwa; au kwa mapambo (madoido) yenye gharama nyingi, na picha za rangi zilizochorwa, au kupakwa dhahabu iliyo katika mada ya kimiminika juu yake (gold coated).... Usianike chochote nje kwa kujionyesha ili kukidhi kiburi cha uzima, ili kujitafutia kupendwa sana au kupongezwa au kuonekana wa maana zaidi mbele za watu.... 'ili mradi unatenda mema kwa jinsi unavyoona mwenyewe, watu watakusema vizuri kuhusu wewe. "Maadamu wewe unaendelea kuvaa 'nguo za zambarau na kitani safi', na kuendelea kula chakula cha fahari na ghali na kuishi maisha ya gharama kujionyesha na anasa zako kila

siku,' bila shaka wengi watakupigia makofi kwa umaridadi na madaha yako, na ladha ya mtindo wako wa maisha yenye fahari. Lakini usihenyeke au usitoke jasho kununua sifa zao ili wakupigie wewe makofi kwa hiyo gharama kubwa mno. Ni bora wewe ukatosheka na heshima ile itokayo kwa Mungu." - Wesley, Works, Hotuba ya 50, "The use of money/Matumizi ya Fedha." Lakini katika makanisa mengi ya wakati wetu mafundisho kama haya hawayajali, hakika yanapuuzwa. [GC 385.2; PK Aya ya 30]

**Mfano Wa Utauwa**

Tabia ya watu kukiri kufuata dini ni jambo mashuhuri na kwa kawaida linapendwa na walimwengu. Watawala, wanasiasa, wanasheria, madaktari wa falsafa, na wafanya biashara, hujiunga na kanisa kama njia ya kujipatia heshima na kuaminiwa na jamii yao, na kuendelea kupata maslahi yao wayapendayo ya kidunia. Hivyo wanajaribu kuzifunika shughuli zao zote zilizojaa dhuluma chini ya kifuniko cha kujidai wanao Ukristo. Mashirika mbalimbali ya kidini, yanayoimarishwa kwa utajiri na ushawishi wa watu hao wanaoupenda ulimwengu waliobatizwa, bado yanafanya jitihada kubwa sana kuwania kiwango cha juu zaidi ili kujipatia umaarufu na kupendwa na watu wengi na kuungwa mkono na wadhamini wao hao (sponsa). Makanisa ya kifahari, yaliyopambwa kwa njia ya umaridadi na ubadhirifu kwa kupitiliza mno hujengwa katika mitaa mashuhuri inayopendwa na watu wengi. Waabuduo humo hujivika kwa namna fulani mavazi ya gharama nyingi na mitindo ya kisasa. Mshahara mkubwa unatolewa kwa mchungaji mwenye talanta ya kuwatumbuiza, na kuwavutia watu. Mahubiri yake hayatakiwi kuzigusa dhambi zile maarufu na zinazopendwa na watu wengi, lakini yanapaswa kufanywa laini na yanayopendeza kwa masikio ya mtindo wa kisasa (yaani, yasiyopenda dhambi zao ziguswe). Hivyo ndivyo wenye dhambi hao wa mtindo wa kisasa wanavyoandikishwa majina yao katika kumbukumbu za kanisa, na dhambi zao hizo za mtindo wa kisasa hufichwa kwenye vazi la unafiki wao, kwa kisingizo kwamba wao ni wacha Mungu. [GC 386.1; PK Aya ya 31]

Akitoa maoni yake juu ya mtazamo wa siku hizi wa wale wanaojiita Wakristo kuelekea ulimwengu huu, Mwandishi wa habari wa jarida moja maarufu la kidunia alisema hivi: "Bila kutambua, kanisa limesalimu amri na kupokea roho ya kizazi hiki, na taratibu zake za ibada zinaendana ili kukidhi matakwa ya kileo." "Naam, mambo yale yote yanayosaidia kuifanya dini iwavutie watu, kanisa linayatumia sasa kama nyenzo zake." Na mwandishi mmoja katika gazeti la New York Independent anasema hivi kuhusu Umethodisti kama ulivyo sasa: "Mstari unaowatenga wacha Mungu na wale wasio na dini unazidi kufifia na kuwa kama kivuli chepesi (penumbra), na watu wale walio na bidii au motomoto pande zote mbili wanafanya kazi nzito inayowatoa jasho, wakijaribu kufutilia mbali tofauti zote zilizopo kati mitindo ya utendaji wao wa kazi na starehe zao." "Ule umashuhuri na kupendwa sana kwa dini na watu wengi una mwelekeo mkubwa

sana wa kuongeza idadi ya wale ambao wangependa kujipatia manufaa yake pasipo kutekeleza majukumu yake kikamilifu.” [GC 386.2; PK Aya ya 32]

Asema hivi Howard Crosby: “Ni jambo la kuhangaisha moyo sana, kwamba tunalikuta kanisa Lake Kristo likitekeleza kwa udogo sana mikakati aliyokusudia Bwana wake. Kama vile Wayahudi wa kale walivyoruhusu mahusiano au mwingiliano wao wa kawaida kati yao na mataifa yale yaliyoabudu sanamu kiasi cha kuipora mioyo yao toka kwa Mungu,... ndivyo lilivyo kanisa la Yesu sasa, kwa kufanya mapatano ya uongo au kinafiki na ulimwengu usioamini, linaziacha mbinu na njia za Mungu za maisha yale manyofu ya Kweli, na kujisalimisha lenyewe chini ya mazoea yenye maafa au madhara yanayonyemelea taratibu ambayo mara nyingi huonekana yana busara, ila yanaliletea kanisa vishawishi kutoka kwa jamii hiyo isiyo na Kristo, likitumia hoja zake na kufikia mahitimisho ambayo ni mageni kabisa na mafunuo matakatifu ya Neno la Mungu (Maandiko), nayo hupingana moja kwa moja na ukuaji katika neema wa aina yoyote ile.” - The Healthy Christian: an Appeal to the Church, uk. 141 na 142.” [GC 387.1; PK Aya ya 33]

**Kujikana Nafsi Kwa Ajili Ya Kristo Kumetoweka**

Katika wimbi hilo la kuipenda dunia na kujitafutia anasa, mambo ya kujikana nafsi na kujitolea binafsi kwa ajili Yake Kristo karibu yatoweke kabisa. “Baadhi ya wanaume na wanawake walio na uwezo wa kufanya kazi katika makanisa yetu, walipewa mafunzo yao ya kujinyima walipokuwa watoto wadogo, ili kuweza kutoa chochote au kufanya kitu fulani kwa ajili Yake Kristo.” Lakini “endapo fedha zinatakiwa sasa, hakuna mtu yeyote anayepaswa kuitwa ili atoe...La, Hapana! Hebu itisha tamasha, maigizo, maonyesho ya picha (video au sinema) ili fedha zipatikane bila ya sisi kutoa kitu, tuwe na siku kuu, michezo ya kuigiza, tuwe na chakula cha jioni kwa ajili ya maonyesho ya vitu vya kale au mitumba, au kitu chochote cha kula - yaani, kitu cho chote kile cha kuwatumbuiza au kuwachekesha watu.”* [GC 387.2; PK Aya ya 34]

Gavana Washburn wa Wisconsin katika ujumbe wake wa kila mwaka, Januari 9, 1873, alitangaza hivi:“Sheria ya aina fulani inaonekana kuhitajika kutungwa ili kuzivunja shule zile zinazowatayarisha watoto kuwa wacheza kamari. Shule hizo ziko kila mahali. Hata ndani ya kanisa (pasipo lenyewe kutilia maanani au kujua) wakati mwingine linakutwa likifanya kazi ya Shetani. Burudani za tamasha la muziki (concert) ambapo zawadi zinatolewa, na kuna biashara zinazotoa zawadi pamoja na kuuza vitu kwa kutumia kanuni za michezo ya bahati nasibu (raffles), wakati mwingine yanatoa msaada kwa malengo ya kidini au ya hisani lakini mara nyingi kwa madhumuni yasiyofaa ya bahati nasibu, vifurushi vya zawadi, n.k. Zote hizo ni juhudi za kujipatia pesa za changizo bila ya watu kutoa jasho au kurudisha thamani ya kile wanachopokea. Hakuna kitu kinachoharibu tabia

vibaya au kulevya mno hasa kwa vijana, kama kujipatia fedha au mali bila kuifanyia kazi. Kwamba watu wanaoheshimiwa ambao hujishughulisha katika biashara za pata potea au bahati nasibu, na kuzituliza dhamiri zao kwa kuona kwamba fedha hiyo inaenda kutekeleza lengo zuri, Siyo ajabu basi tena kwamba hilo limekuwa jambo la hakika kwa vijana wa taifa hili mara kwa mara huweza kujikuta wakiangukia katika tabia zile zinazochochewa na michezo hiyo ya hatari." [GC 387.3; PK Aya ya 35]

Roho ya maridhiano au kupatana na ulimwengu huu inayavamia makanisa katika Ulimwengu wote wa Kikristo. Robert Atkins, katika hotuba yake aliyoitoa mjini London, anachora picha ya kusikitisha ya kuporomoka kwa hali ya kiroho iliyozagaa katika nchi ya Uingereza akisema: "Wacha-Mungu wa kweli wanapungua duniani, wala hakuna anayeliweka hili moyoni mwake. Wale wanaojidai kukiri kuwa wanayo dini katika kila kanisa, ambao wanaishi ziku hizi, wanaipenda dunia hii, wanafanana nayo, wanapatana nayo, wanapenda faraja, starehe na ustawi wa kiumbe, kama vile chakula na malazi ya fahari ya wanadamu, tena wanatamani kupewa heshima. Wameitwa ili kuteseka pamoja na Kristo, lakini wanajikunyata hata pale wanapoonywa, au wanapogombezwa au kuaibishwa kidogo tu....GC 387.4; PK Aya ya 36]

Uasi, ukengeufu, uasi, maneno hayo yamechorwa mbele kabisa ya kila kanisa; na laiti wangelijua hilo, na laiti wangelihisi kwamba wako hivyo, basi, lingalikuwapo tumaini; lakini, basi, ole wao! Wanapiga makelele wakisema, 'Sisi tu matajiri, tumejitajirisha, wala hatuna haja ya kitu."— Second Advent Library, trakti Na 39. [GC 388.1; PK Aya ya 37]

Dhambi kubwa iliyoshtakiwa dhidi ya Babeli ni kwamba 'aliyafanya mataifa yote kunywa mvinyo ya ghadhabu ya uasherati wake." Kikombe hiki cha kileo anachowasilisha kwa ulimwengu kinawakilisha mafundisho ya uwongo ambayo ameyakubali kama matokeo ya uhusiano wake haramu na wakuu wa dunia. Urafiki wa ulimwengu na kanisa huipotosha imani yake, na kwa upande wake kanisa hutoa mvuto mbaya unaounajisi ulimwengu kwa kufundisha mafundisho ambayo yanakinzana kabisa na Mafundisho yaliyo wazi kabisa ya Maandiko Matakatifu. [GC 388.2; PK Aya ya 38]

Rumi iliwanyima watu Biblia kwa kuificha na kuwataka watu wote wakubali mafundisho yake badala Biblia. Ilikuwa ni kazi ya Matengenezo ya Kanisa kuwarejeshea wanadamu Neno la Mungu; lakini je, si kweli kwamba katika makanisa ya wakati wetu wanadamu wanafundishwa kuweka imani yao kwenye matamko yao ya imani na mafundisho ya kanisa lao badala ya Maandiko? Charles Beecher alisema hivi kuhusu makanisa ya Kiprotestanti: "Watu huchukia wakati neno lolote baya au lenye ujeuri lilipotamkwa dhidi ya kanuni au imani yao kwa hisia zile zile kali za chuki au kukwepa, ambazo mababa watakatifu walionyesha wakati neno linalokosoa lilipotamkwa dhidi ya ibada yao kwa watakatifu

waliokufa na wafia-dini ambao walikuwa wakiikuza.... Madhehebu ya Waprotestanti yameifunga mikono ya wenzao, na wenzao wakaifunga ya kwao na kisha wakaifunga mikono yao na wenzao pamoja, kiasi kwamba, kati ya hao wote, mtu hawezi kuwa mhubiri hata kidogo mahali popote, asipokubali vitabu vingine vilivyo kando na Biblia (wameshikamana mno na mafundisho yao hata yale ambayo si ya kutoka kwenye Maandiko).... Hakuna kitu cha kufikirika katika matamko ya imani kwamba nguvu ya mfumo wa imani sasa inaanza kukataza/kuzuia Biblia kama vile Rumi ilivyofanya, ingawa kwa njia nyeti na ya hila zaidi."—Sermon On "The Bible a Sufficient Creed," lililotolewa huko Fort Wayne, Indiana, Februari 22, 1846. [GC 388.3; PK Aya ya 39]

Wakati walimu waaminifu wanapoeleza Neno la Mungu, wanainuka watu wenye visomo, wachungaji wanaojidai kuyaelewa Maandiko, Wanaokataa na kuyashutumu mafundisho sahihi kama ndiyo uzushi, na hivyo kuwakatisha waulizaji ili wasiutafute Ukweli. Kama ulimwengu ungekuwa haujaleweshwa na matumaini ya mvinyo wa Babeli, watuumati wa ungechomwa moyo dhamiri zao na kuongoka kwa Maneno yaliyo wazi, yenyeUkweli unaokata wa Neno la Mungu. Lakini imani ya kidini inaonekana kuchanganyikiwa mno na kupingana kiasi kwamba watu hawajui ni fundisho gani la kuamini kama ndiyo Ukweli. Dhambi ya kutotubu ya ulimwengu inlala kwenye mlango wa kanisa. [GC 389.1; PK Aya ya 40]

Ujumbe wa malaika wa pili wa Ufunuo 14 ulihubiriwa kwa mara ya kwanza mnamo mwaka 1844, na wakati ule ulihusu matumizi ya moja kwa moja zaidi kwa makanisa ya Marekani, ambako onyo la hukumu lilikuwa limehubiriwa sana na kukataliwa kwa ujumla zaidi kwenye maeneo mengi, na mahali ambapo kurudi nyuma kwa makanisa kulikuwa kumeenea kwa haraka zaidi. Lakini ujumbe wa malaika wa pili haukufikia utimizwaji wake kikamilifu katika 1844. Kisha makanisa yalipata anguko la uadilifu, kwa matokeo ya kukataa kwao nuru ya ujumbe wa marejeo ya Masihi; lakini anguko hilo halikuwa kamili. Na kwa kadri yalivyoendelea kukataa Ukweli maalum kwa ajili ya wakati huu, yameendelea kuanguka chini na chini zaidi. Hata hivyo, bado haiwezi kusemwa kwamba "Umeanguka Babeli,... kwa maana ndiyo umeyafanya mataifa yote kunywa mvinyo ya ghadhabu ya uasherati wake." Bado Babeli hajayafanya mataifa yote kufanya hivyo. Roho ya ulimwengu ya maridhiano na ulimwengu na kupuuza Ukweli unaopima wa wakati wetu ipo na imekuwa ikipata mashiko na kuota mizizi katika makanisa ya imani ya Kiprotestanti katika nchi zote za Kikristo; na makanisa haya yamejumuishwa katika onyo zito na la kutisha ya malaika wa pili. Lakini kazi ya uasi bado haijafikia kipeo chake. [GC 389.2; PK Aya ya 41]

Biblia inatangaza kwamba kabla ya kuja kwa Bwana, Shetani atatendakazi "na nguvu na ishara na maajabu ya uongo, na madanganyo yote ya udhalimu; na wale ambao "hawakukubali kuipenda ile Kweli, wapate kuokolewa," wataachwa

wapokee “udanganyifu wenye nguvu, wauamini uwongo.” 2 Wathesalonike 2:9-11. Ni mpaka hali hii itakapofikiwa, na muungano wa kanisa na ulimwengu utakapofikia ukamilifu wake katika ulimwengu wote wa Ukristo, ndipo anguko la Babeli litakapokamilika. Mabadiliko ni endelevu yaani yanaendelea kutokea, hatua kwa hatua hadi kuufikia utimilifu kamili wa Ufunuo 14:8 bado ni wa siku za usoni. (haya yalisemwa mwaka, imepita miaka 110). [GC 388.3; PK Aya ya 42]

Licha ya giza la kiroho na utengano na Mungu katika makanisa yanayounda Babeli, kundi kubwa la wafuasi wa Kweli wa Kristo bado linaweza kupatikana katika ushirika wao. Kuna wengi wa hawa ambao hawajawahi kuona Ukweli maalum wa wakati huu. Siyo wachache ambao hawajaridhika na hali yao ya sasa na wanatamani kupata nuru iliyo wazi zaidi. Wanatazama-tazama ili wapate kuiona sura ya Kristo katika makanisa ambayo wameunganishwa nayo bila mafanikio (wanatoka bure). Madhehebu hayo yanapozidi kwenda mbali zaidi na zaidi kutoka katika Ukweli zaidi, na kujifungamanisha kwa karibu zaidi na ulimwengu, tofauti kati ya makundi hayo mawili itaongezeka na kuwa kubwa zaidi, na hatimaye itasababisha kutengana. Wakati utafika ambao wale wanaompenda Mungu kwa mioyo yao yote hawataweza tena kuendelea kushirikiana na wale “wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu; wenye mfano wa utauwa, lakini wakikana nguvu zake." [GC 390.1; PK Aya ya 43]

Ufunuo 18 huelezea wakati ambapo, kama matokeo ya kukataa onyo lenye Sehemu Tatu zilizofungamanishwa katika Ufunuo 14:6-12, kanisa litakuwa limefikia kikamilifu hali iliyotabiriwa na malaika wa pili, na watu wa Mungu ambao watakuwa bado wako katika Babeli, wataitwa kujitenga na ushirika wake. Ujumbe huu ni wa mwisho utakaotolewa kwa ulimwengu; nao utakamilisha kazi yake. Wakati wale ambao “Hawakuiamini Kweli, bali walikuwa wakijifurahisha katika udhalimu” (2 Wathesalonike 2:12), wataachwa wapokee udangayifu wenye nguvu zaidi na kuamini uongo, ndipo nuru ya Ukweli itawaangazia wote ambao mioyo yao iko wazi kuupokea, na watoto wote wa Bwana waliosalia katika Babeli watatii wito unasema: “Tokeni kwake, Enyi watu Wangu” (Ufunuo 18:4). [GC 390.2; PK Aya ya 44]

*Holy See ni serikali ya Kanisa Katoliki na inafanya kazi kutoka Jimbo la Vatican City, eneo linalojitawala, na kujitegemea. Papa ndiye mtawala wa Jimbo la Vatican City na Holy See. Holy See, kama chombo kikuu cha serikali ya Kanisa Katoliki, ni chombo huru cha kisheria chini ya sheria za kimataifa. Marekani na Holy See hufanya kazi pamoja katika vipaumbele vya pamoja, kama vile kukuza uhuru wa kidini na kupiga vita biashara haramu ya binadamu.

*Haya yote ni maswala ya kijamii ambayo wahusika walitoza ada ya kiingilio na kutumia mapato kwa shughuli zao za hisani, mfano kujenga kanisa, au kumsomesha mchungaji shule au kumlipa posho mlei. Roho ya unabii inasema aina

hizi za burudani zisiwe msingi wa utoaji wetu--tunapaswa tu kutoa kutoka moyoni badala ya kulipa ili kutumbuizwa. Pia tunapaswa kuwa na mpango wa kutoa Sadaka, na si kwa kushtukizwa, kulazimishwa au kutumbuizwa, kisha ndiyo tutoe. Kisha, tusizoee kupenda kutoa kitu ambacho hakitugharimu au ambacho kijasho.

# SURA YA 22

# UNABII WATIMIZWA

## (Kilio Cha Usiku Wa Manane, Kuvunjwa Matumaini Na Kuendelea Kuwa Waaminifu)

Ufupisho: Miaka ya usiku wa manane ilifanya ujumbe uende kwa nguvu kamawimbi la Tsunami katika nchi kavu. Uharaka huo  ulisababisha maamuzi ya kuupenda ujumbe huo au kuukataa. Matokeo yake ilikuwa mioyo mingi ilifichuliwa. Kwa bahati mbaya wengi waliupenda ulimwengu kuliko walivyompenda Kristo.

Muda uliotarajiwa kuja Kwake Bwana ulipopita, - katika majira ya kuchipua (Machi-Mei) ya mwaka wa 1844, - wale waliokuwa wametazamia kwa imani kuja Kwake Bwana, kwa kipindi fulani waliingiwa na mashaka na kutokuwa na hakika. Wakati ulimwengu ulipokuwa umewaona kama watu waliokuwa wameshindwa vibaya na kuthibitika kuwa ni watu wanaofuata Imani zisizo na uhalisia kwa kuchanganyikiwa na akili. Chanzo cha faraja yao bado kilikuwa ni Neno la Mungu. Wengi waliendelea kuyachunguza Maandiko, wakipima upya ushahidi wa imani yao na kujifunza unabii kwa umakini zaidi ili wapate nuru zaidi. Ushuhuda wa Biblia uliounga mkono msimamo wao ulionekana kuwa wazi kabisa na wenye kuhitimisha. Dalili ambazo zisingeweza kukosewa zilielekeza kidole chake kwenye ujio wa Kristo, kwa kuonyesha kwamba ilikuwa ni karibu. Mbaraka wa pekee wa Bwana katika uongofu wa wenye dhambi na uamsho wa maisha ya kiroho miongoni mwa Wakristo, ulikuwa ni ushuhuda kwamba ujumbe huu ulikuwa ni wa Mbinguni. Na ingawa waaminio hawakuweza kueleza sababu ya kukatishwa tamaa kwa matarajio yao, walihisi kuwa na matumaini kwamba Mungu Ndiye aliyekuwa amewaongoza katika uzoefu wao uliokuwa umepita. [GC 391.1; PK Aya ya 1]

Mafundisho yaliyochukuliwa yalikuwa ni yale yenye aya zenye unabii ambazo waliamini zilihusiana na wakati wa marejeo ya Bwana, nayo yalikuwa na mambo mahsusi yaliyochukuliana hasa na hali yao ya kutokuwa na uhakika na kujawa na mashaka, na mafundisho haya yaliwatia moyo kusubiri kwa uvumilivu na imani kuwa kile ambacho kilikuwa giza sasa katika ufahamu wao kingeweza kueleweka wazi kwa wakati wake unaostahili. [GC 391.2; PK Aya ya 2]

Miongoni mwa aya hizo za unabii ni ile ya Habakuki 2:1-4: “Mimi nitasimama katika zamu yangu, nitajiweka juu ya mnara, nitaangalia ili nione atakaloniambia, na jinsi nitakavyojibu katika habari ya kulalamika kwangu. Bwana akanijibu, akasema, Iandike njozi hii, ukaifanye iwe wazi sana katika vibao, ili aisomaye apate kuisoma kama maji. Maana njozi hii bado ni kwa wakati ulioamriwa, inafanya haraka ili kuufikilia mwisho wake, wala haitasema uongo; kwa kuwa haina budi kuja, haitakawia. Tazama, roho yake hujivuna, haina unyofu ndani yake; lakini mwenye haki ataishi kwa imani yake.” [GC 392.1; PK Aya ya 3]

Mwanzoni mwa mwaka 1842 agizo lilitolewa katika unabii huu kuwa “Iandike njozi, na kuifanya iwe wazi juu ya mbao, ili asomaye apate kusoma kama maji,” haya yalikuwa yamempendekezea Charles Fitch, mchoro wa chati ya kinabii ili kuelezea maono ya Danieli na Ufunuo. Uchapaji wa chati hii ulichukuliwa kama utimizaji wa agizo lile lililotolewa na Habakuki. Hata hivyo, hakuna hata mtu mmoja aliyeng’amua kuchelewa kulikokuwa dhahiri katika kutimizwa kwa njozi hii -- yaani, kipindi cha kusubiri kukawia Kwake - kilikuwa kimeelezwa katika

unabii ule ule. Baada ya kukatishwa tamaa, Andiko hili lilionekana kuwa la maana sana kwao: “Maana njozi hii bado ni kwa wakati ulioamriwa, inafanya haraka ili kuufikilia mwisho wake, wala haitasema uongo; ijapokawia, ingojee; kwa kuwa haina budi kuja, haitakawia.... Mwenye haki ataishi kwa imani yake. [GC 392.2; PK Aya ya 4]

Sehemu fulani ya unabii wa Ezekieli pia ilikuwa ni chimbuko la nguvu na faraja kwa walioamini: “Neno la Bwana likanijia, kusema, Mwanadamu, ni mithali gani hii mliyo nayo katika nchi ya Israeli, mkisema, Siku hizo zinakawia na maono yote hayatimizwi. Basi uwaambie, Bwana MUNGU asema hivi. Nitaikomesha mithali hii, wasiitumie tena kama mithali katika Israeli; lakini uwaambie siku hizo ni utimilizo wa maono yote. Kwa maana hayatakuwapo tena maono yoyote ya ubatili, wala ubashiri wa kujipendekeza, katika nyumba ya Israeli. Kwa maana Mimi ni Bwana; Mimi nitanena, na Neno lile nitakalolinena litatimizwa; wala halitakawilishwa tena; maana katika siku zenu. Ewe nyumba iliyoasi, nitalinena Neno hilo na kulitimiliza, asema Bwana MUNGU. Mwanadamu tazama, hao wa nyumba ya Israeli husema, maono hayo ayaonayo ni ya siku nyingi zijazo, naye anatabiri habari ya nyakati zilizo mbali sana. Basi uwaambie, Bwana Mungu asema hivi; Maneno Yangu hayatakawilishwa tena hata moja, bali Neno nitakalolinena litatimizwa, asema Bwana MUNGU.” Ezekieli 12:21-25, 27, 28. [GC 392.3; PK Aya ya 5]

**Unabii Uliotimizwa**

Wale waliokuwa wakingojea walifurahi sana, wakiamini kwamba Yeye aujuaye mwisho kutoka mwanzo alikuwa ametazama kupitia zama zote, Naye akiwa amekuona mapema kukatishwa tamaa kwao zama za nyuma, alikuwa amewapa maneno ya kuwatia ujasiri na matumaini. Kama isingelikuwa sehemu kama zile katika Maandiko zilizowausia kungojea kwa uvumilivu na kuishikilia imani yao kwa uthabiti katika Neno la Mungu, basi, imani yao ingekuwa imeshindwa katika saa ile ya kujaribiwa kwao.[GC 393.1; PK Aya ya 6]

**Wanawali Kumi**

Mfano wa wanawali kumi katika Mathayo 25 pia huonyesha kielelezo cha uzoefu wa Waadventista. Katika Mathayo 24, akijibu swali la wanafunzi Wake kuhusu dalili ya ujio Wake na ya mwisho wa dunia, Kristo alionyesha baadhi ya matukio muhimu sana katika historia ya ulimwengu huu na ya kanisa tangu ujio Wake wa mara ya kwanza hadi kuja Kwake mara ya pili; ambayo ni, kuharibiwa kwa Yerusalemu, ile dhiki kuu ya kanisa chini ya mateso ya kipagani na ya kipapa, kutiwa giza kwa jua na mwezi, na kuanguka kwa nyota mbinguni (Mt.

24). Baada ya hayo alizungumzia juu ya kuja Kwake katika ufalme Wake, na kusimulia mfano ule ulioyaeleza makundi yale mawili ya watumishi wanaotazamia marejeo Yake. Sura ya 25 huanza kwa Maneno haya: “Ndipo ufalme wa mbinguni utakapofanana na wanawali kumi.” Hapa tumeletwa kulitazama kanisa linaloishi katika siku za mwisho, lile lile lililodokezwa mwisho wa sura ya 24. Katika mfano huu uzoefu wa maisha yao unaelezwa kwa njia ya kielelezo cha matukio yanayoambatana na ndoa ya nchi ya Mashariki. [GC 393.2; PK Aya ya 7]

"Wakati huo, Ufalme wa mbinguni utafanana na wanawali kumi waliochukua taa zao, wakaenda kumlaki bwana arusi. Watano miongoni mwao walikuwa wapumbavu na watano walikuwa wenye busara. Wale waliokuwa wapumbavu walizitwaa taa zao, wasichukue mafuta pamoja nao; lakini wale wenye busara walichukua mafuta katika vyombo vyao pamoja na taa zao. Kwa kuwa bwana arusi alikawia kuja, wale wanawali wote walisinzia, wakalala. Usiku wa manane kukawa na kelele: Haya, haya! Bwana arusi Yuaja; nendeni kumlaki.” [GC 393.3; PK Aya ya 8]

### Bwana Arusi Alichelewa

Ujio Wake Kristo, kama unavyotangazwa na Ujumbe wa Malaika wa Kwanza,ulieleweka kuwakilishwa ujio wa bwana arusi. Matengenezo yaliyofanyika katika maisha ya watu ambayo yalikuwa yameenea mahali pengi chini ya tangazo la kuja Kwake upesi, yalifananishwa na kule kutoka kwa wanawali kumi. Katika mfano huo, kama ulivyo ule wa Mathayo 24, makundi mawili watu yamewakilishwa. Wote walikuwa wamezitwaa taa zao, yaani, Biblia (Zab. 119:105), na kwa njia ya nuru Yake waliondoka kwenda kumlaki Bwana arusi. Lakini wakati ambapo “wale waliokuwa wapumbavu walizitwaa taa zao, wasichukue mafuta pamoja nao,” “wale wenye busara walitwaa mafuta katika vyombo vyao pamoja na taa zao.” Kundi lile la pili lilikuwa limeipokea neema ya Mungu, yaani, uweza wa Roho Mtakatifu unaoumba upya, na kumtia mtu nuru, ambao unalifanya Neno Lake kuwa taa ya miguu na mwanga wa njia yetu. Katika kicho cha Mungu, walikuwa wamejifunza Maandiko ili kuujua Ukweli, na walikuwa wametafuta kwa bidii nyingi usafi wa moyo na usafi wa maisha yao. Hawa walikuwa na uzoefu binafsi katika maisha yao, walikuwa na imani kwa Mungu na katika Neno Lake, ambalo lisingeweza kushindwa kukabiliana na kukata tamaa kwao kule pamoja na kuchelewa Kwake. Wengine “walizitwaa taa zao, wasitwae na mafuta pamoja nao.” Hawa walikuwa wamesukumwa na mihemko yao tu. Hofu zao zilikuwa zimeamshwa kutokana na ujumbe ule mzito na wa kutisha, lakini wao walikuwa wakitegemea imani ya ndugu zao, walitosheka na mwali wa utambi wa mihemko mizuri uliokuwa unawaka ukiyumbayumba na kufifia bila ya wao kuwa na ufahamu kamili wa ile Kweli au kutambua kazi halisi inafanywa na neema ndani ya mioyo yao. Hawa walitoka

kwenda kumlaki Bwana, wakiwa wamejawa na tumaini la kupokea thawabu yao papo hapo (haraka), lakini hawakuwa wamejiandaa kukabiliana na kuchelewa Kwake pamoja na kule kukatishwa tamaa kwao. Majaribu yalipokuja, imani yao ilishindwa, na nuru ya taa yao ikafifia. [GC 393.4; PK Aya ya 9]

"Hata Bwana arusi alipokawia wale wanawali wote walisinzia, wakalala." Kule kukawia kwa bwana arusi kunawakilishwa na kupita kwa wakati ule ambapo Bwana alikuwa ametarajiwa kuja, kukatishwa tamaa kwao, na mwonekano uliojitokeza wa kukawia. Katika wakati ule wa mashaka, shauku ya wale waliokuwa na imani ya juu juu tu, pamoja na wale walioamini nusu nusu, punde walianza kuyumbishwa, nao wakalegeza juhudi zao; lakini wale ambao imani yao ilijengwa juu ya msingi wa ujuzi wao binafsi wa Biblia, walikuwa na mwamba imara chini ya nyayo zao, mawimbi yale ya kukata tamaa hayakuweza kuwafagilia mbali. "Wote wakasinzia wakalala usingizi;" kundi moja likiwa katika hali ya kutojali au wasiswasi, tena likiwa limeitupilia mbali imani yake, na kundi jingine likiwa linangojea mpaka nuru iliyo wazi zaidi itakapotolewa. Lakini katika usiku ule wa kujaribiwa, wale wa kwanza walionekana kana kwamba wamepoteza kwa kiasi fulani juhudi na kujitoa wakfu kwao. Wale waliojitoa nusu nusu (vuguvugu) na wale waliokuwa na imani ya juu juu tu hawakuweza kuitegemea tena imani ya ndugu zao. Kila mmoja alipaswa kusimama au kuanguka kwa nafsi yake mwenyewe. [GC 394.1; PK Aya ya 10]

Ushabiki wa dini usiotumia akili ulianza kujitokeza karibu na wakati huu. Baadhi ya wale waliojidai kuwa waumini wenye ari na bidii wa ujumbe wa marejeo, walilikana Neno la Mungu wakisema lilikuwa sio mwongozo wa pekee usiokosea, nao wakiwa wanadai kuwa wanaongozwa na Roho, walijiachia kutawaliwa na hisia, mihemko, maono, na fikra zao wenyewe. Walikuwapo baadhi yao walioonyesha juhudi iliyo na upofu na kung'ang'ania mawazo yao binafsi kupita kiasi, wakiwalaumu wale wote ambao hawakukubaliana na mwenendo wao. Mawazo yao ya ushabiki na matendo yao hayakuungwa mkono kabisa na sehemu kubwa ya Waadventista; hata hivyo walichangia katika kutoa shutuma na aibu juu ya kazi ya Ukweli. [GC 395.1; PK Aya ya 11]

Shetani alikuwa akitafuta kutumia njia hii ili kuipinga na kuiharibu kazi ya Mungu. Watu walikuwa wamepata uamsho mkubwa sana kutokana na vuguvugu la Marejeo (Waadventista), maelfu ya wenye dhambi walikuwa wameongoka, na watu waliokuwa waaminifu walikuwa wanajitoa wenyewe kufanya kazi ya kutangaza Ukweli, hata katika wakati huu wa kujaribiwa kwa kukawia Kwake. Mkuu wa uovu alikuwa akiwapoteza raia wake; naye, ili kuleta fedheha na shutuma juu ya kazi hii ya Mungu, alijitahidi kuwahadaa baadhi ya watu walioikiri imani na kuwapelekea wafanye mambo yao kwa kupitiliza, kwa kuwa na misimamo mikali ya kidini. Ndipo mawakala wake walisimama na kuwa tayari kutumia kila kosa lao, kila kushindwa kwao, kila tendo lao lisilofaa au la

kipuuuzi, na kulionyesha mbele ya watu katika nuru iliyotiwa chumvi sana, ili kuwafanya Waadventista, pamoja na imani yao kuwa jambo la machukizo kwa watu. Hivyo Shetani alijaribu kupata mrundiko wa watu wengi kadri awezavyo kukiri imani katika ujio wa mara ya pili huku uwezo wake ukitawala mioyo yao, na ndivyo angeweza kunufaika zaidi kwa kuyavuta mawazo ya watu na kuyaelekeza kwao, kwa kuwaonyesha kama hawa ndio wawakilishi wa kundi zima la waaaminiWakristo. [GC 395.2; PK Aya ya 12]

Shetani ni "mshitaki wa ndugu zetu," tena ni roho yake inayowachochea moyo watu kuchunguza makosa na mapungufu waliyo nayo watu wa Bwana, na kuyaonyesha mbele ya watu ili wayatilie umakini mapungufu haya, na huku matendo yao mazuri yanapita bila kutajwa. Yeye sikuzote yuko kazini, naye ana bidii nyingi wakati Mungu anapotenda kazi yake kwa ajili ya wokovu wa watu. Wakati wana wa Mungu wanapokuja kujihudhurisha mbele za Bwana, Shetani anakuja pia miongoni mwao. Katika kila uamsho yuko tayari kuwaingiza wale wote ambao mioyo yao haijatakaswa, na wale walio na akili zilizochanganyikiwa na zisizo na msawaziko mzuri (hisia hazina balansi). Hao wanapokubali baadhi ya vipengele vya Ukweli, na kujipatia nafasi miongoni mwa waaminio, hapo ndipo yeye anapofanya kazi yake kupitia kwao ili kuingiza nadharia zitakazowapotosha wale wasio na tahadhari. Hakuna mtu yeyote anayethibitishwa ya kuwa ni Mkristo wa kweli ati kwa sababu tu yeye anaonekana miongoni wa kundi la wana wa Mungu, hata katika nyumba ya ibada na kuzunguka Meza ya Bwana. Mara kwa mara Shetani yupo kwenye matukio muhimu katika umbile la wale anaoweza kuwatumia kama vibaraka wake wakati wa matukio hayo matakatifu. [GC 395.3; PK Aya ya 13]

**Uwanja Unaogombaniwa**

Mfalme huyo wa uovu anapigana vita, akigombania kila sentimita ya ardhi ambayo juu yake watu wa Mungu wanasonga mbele katika safari yao ya kwenda kwenye mji wa mbinguni. Katika historia yote ya kanisa hakuna Matengenezo ya Kanisa yaliyoendelezwa mbele bila kukumbana na vikwazo vya kutisha. Hivyo ndivyo ilivyokuwa katika siku zake Paulo. Popote pale ambapo mtu alijenga kanisa, palikuwa na wengine waliojidai kwamba wanaipokea hiyo imani, lakini waliingiza mafundisho ya uongo uzushi ndani ya kanisa, ambao, kama ungepokelewa, basi, hatimaye ungeweza kufutilia mbali upendo wote kwa ile Kweli. Luther pia alihangaishwa sana na kuwa na mfadhaiko mkubwa na udhia kutokana na mwenendo wa watu wa aina hii ambao walikuwa mashabiki wa dini pasipo kutumia busara, ambao walidai kwamba Mungu alikuwa amezungumza nao moja kwa moja, na ambao waliyaweka mawazo na maoni yao wenyewe juu zaidi ya ushuhuda wa Maandiko. Wengi waliokuwa na upungufu katika imani yao na uzoefu wao wa maisha ya imani, lakini waliokuwa kwa kiasi fulani

wamejitosheleza na kujitumainia wenyewe, tena walipenda kusikia na kusimulia mambo fulani mapya, walidanganywa na maigizo au unafiki wa waalimu wapya (walimu feki), nao wakajiunga na mawakala wa Shetani katika kazi yao ya kubomoa kile ambacho Mungu alikuwa amemwongoza Luther kukijenga. Tena, akina Wesley, na wengineo waliouletea ulimwengu mibaraka kwa ushawishi wao na imani yao, kwa kila hatua waliyosonga mbele walikumbana na hila za watu ambao Shetani alikuwa amewasukuma katika ushabiki wa dini usiotumia akili wa kila kiwango wale wote waliokuwa motomoto kupita kiasi (wenye bidii), waliokuwa hawana ulinganifu mzuri wa akili (hawana balansi), na wale waliokuwa hawajatakaswa. [GC 396.1; PK Aya ya 14]

William Miller hakuonyesha huruma kwa mivuto iliyosababishwa na ushabiki wa kidini usiotumia busara hata kidogo. Yeye, pamoja na Luther, walitangaza kwamba kila roho ni lazima ipimwe kwa Neno la Mungu (1 Yoh. 4:1-3). "Ibilisi," alisema Miller, "ana uwezo mkubwa juu ya mioyo ya baadhi ya watu katika siku zetu hizi. Na tutajuaje ni roho ya namna gani waliyo nayo? Biblia inajibu hivi: 'Kwa matunda yao mtawatambua...... Kuna roho nyingi zilizokwenda katika ulimwengu wote; na sisi tumepewa agizo la kuzipima roho hizo. Roho ile isiyotuongoza sisi tuishi maisha ya kiasi, haki, na utauwa, katika ulimwengu huu wa sasa, si Roho Wake Kristo. Mimi nasadiki zaidi na zaidi kwamba Shetani ana sehemu kubwa anayofanya katika harakati za vurugu na wenda wazimu......Wengi miongoni mwetu wanaojifanya kuwa wametakaswa kikamilifu (feki), wanafuata mapokeo ya wanadamu, tena inaonekana dhahiri ni wajinga wa Ukweli, sawa tu na wengine wasiofanya maigizo (wasiokuwa feki)"- Bliss, ukurasa wa 236, 237. "Roho wa uongo anatuongoza mbali kutoka katika Ukweli; na Roho wa Mungu atatuongoza katika Ukweli (Yn.17:17;119:142). Lakini unaweza kusema, mtu anaweza kuwa katika makosa, na bado akafikiri kwamba yeye anao Ukweli, kwamba yuko sahihi kabisa. Sasa hii inakuwaje basi? Sisi twajibu hivi, Roho wa Mungu na Neno hukubaliana. Kama mwanadamu anajihukumu mwenyewe kwa Neno la Mungu, hebu basi, na apate upatanifu kamili katika Neno la uzima lote, yeye anapaswa kuamini kwamba anao Ukweli; ila kama akiona roho ile inayomwongoza haipatani na mwongozo wote wa Sheria ya Mungu au Kitabu chote (Biblia), basi, hebu hapo atembee kwa uangalifu akiweka tahadhari, ili asije akanaswa katika mtego wa Ibilisi." - The Advent Herald and Signs of the Times Reporter, Januari 15, 1845. "Mara nyingi mimi nimeupata uthibithisho mwingi wa utauwa uliomo ndani ya mtu kwa kuangalia jicho lake linalong'aa, shavu lake lililolowa kwa machozi na sauti yake inayotoka kwa shida na kuzuia pumzi, kuliko kwa kuyasikiliza makelele yote yanayopigwa na Ulimwengu wa Kikristo."- Bliss, ukurasa wa 282. [GC 396.2; PK Aya ya 15]

Katika siku za Matengenezo ya Kanisa, maadui zake waliwatupia mashtaka ya maovu yote ya ushabiki wa dini usiotumia akili wale wale waliokuwa wakijitahidi

sana kuyapinga mambo hayo. Njia kama hiyo ilifuatwa na wapinzani wa vuguvugu za marejeo pili ya Kristo (Waadventista). Tena wakiwa hawajatosheka na kuwaelezea vibaya na kuyatia chumvi makosa ya wale waliopitiliza kimisimamo, na wasio na kiasi kwa ushabiki wa dini usiotumia akili, walisambaza taarifa mbaya ambazo hazikuwa na mwonekano wa ukweli ndani yake hata kidogo. Watu hawa walisukumwa na ubaguzi na chuki isiyokuwa na sababu, pamoja na kisirani. Amani yao ilivurugwa waliposikia mahubiri kwamba Kristo alikuwa mlangoni. Walihofu sana kwamba huenda inaweza kuwa kweli, lakini walitumainia kwamba haikuwa hivyo, na hiyo ndiyo ilikuwa siri ya vita yao dhidi ya Waadventista, pamoja na imani yao. [GC 397.1; PK Aya ya 16]

**Amani Na Upendo**

Ukweli kwamba wafuasi wachache wa ushupavu wa dini isiyotumia busara walijipenyeza na kuingia katika makundi ya Waadventista, haikuwa sababu tosha ya kuamua kwamba harakati hiyo haikutokana na Mungu kuliko uwepo wa watu kama hao na wadanganyaji ndani ya kanisa katika siku zile za Paulo au siku zile za Luther, kwamba hicho ndiyo kiwe kisingizio cha kuishutumu kazi yao waliyoifanya. Hebu watu wa Mungu na waamke toka usingizini na kuanza kwa bidii kufanya kazi yao ya toba na matengenezo; hebu na wayachunguze Maandiko ili kujifunza Ukweli kama ulivyo katika Yesu; hebu na wajitoe wakfu kikamilifu kwa Mungu, hapo ndipo ushahidi hautakosekana kuonyesha kwamba Shetani yu hai na bado anafanya kazi yake, akiwa yu macho kabisa. Kwa njia zote za udanganyifu zinazowezekana, ataonyesha uwezo wake, akiwaita malaika wote walioanguka dhambini wa milki yake wajikusanye ili waje kumsaidia. [GC 398.1; PK Aya ya 17]

Siyo utangazaji wa marejeo yake Kristo mara ya pili ndio ulisababisha ushupavu wa kidini usiotumia akili pamoja na migawanyiko. Mambo haya yalitokea msimu wa kiangazi wa mwaka 1844 wakati Waadventista walipokuwa katika hali ya kuwa na mashaka na kuchanganyikiwa kuhusu msimamo wao halisi. Utangazaji wa Ujumbe wa Malaika wa Kwanza na kile “kilio cha usiku wa manane” kilikuwa na mwelekeo wa kudhibiti ule ushabiki wa dini usiotumia akili na mifarakano. Wale walioshiriki katika harakati hizi adhimu walipatana na kuwa na amani wao kwa wao; mioyo yao ilijazwa na upendo wa kila mmoja kwa mwingine na wa kila mmoja kwa Yesu, ambaye walitarajia kumwona karibuni. Imani yao moja, tumaini lao la baraka moja, viliwainua juu wasiweze kudhibitiwa na ushawishi uwao wote ule wa kibinadamu, na kwao ikawa ni ngao imara dhidi ya mashambulizi ya Shetani.[GC 398.2; PK Aya ya 18]

“Hata bwana harusi alipokawia kuja, wale wanawali wote walisinzia, wakalala. Usiku wa manane kukawa na kelele: Haya, haya! Bwana harusi anakuja; nendeni kumlaki. Hapo wale wanawali wote wakaamka,

wakazitayarisha taa zao” Mathayo 25:5-7. Katika majira ya joto ya mwaka wa 1844 (Juni mpaka Agosti -Summer), katikati ya wakati ambao ulikuwa umefikiriwa mwanzoni kuwa siku 2300 zingekomea, na wakati wa kupukutisha majani mwaka huo huo, ambapo baadaye iligunduliwa kwamba siku zile zilifika, ila zilirefushwa kwenda mbele, basi ujumbe huu ulitangazwa kwa kutumia maneno yale yale ya Maandiko: “Haya, Bwana arusi Yuaja!” [GC 398.3; PK Aya ya 19]

Kile kilichowaongoza kufanya mabadiliko haya ilikuwa ni kule kuigundua amri ya Artashasta ya kuujenga upya mji wa Yerusalemu, ambayo ndiyo ilichukuliwa kama tarehe ya kuanza kipindi cha siku (miaka) 2300, ambayo ilianza kutekelezwa katika majira ya kupukutisha ya mwaka wa 457 K.K., na siyo mwanzoni mwa mwaka, kama ilivyokuwa imesadikiwa katika siku za nyuma. Kwa kukokotoa kuanzia majira ya kupukutisha majani ya mwaka wa 457 K.K., miaka 2300 iliishia katika majira ya kupukutisha majani ya mwaka wa 1844. (Angalia Nyongeza dokezo la ukurasa wa 329.) [GC 398.4; PK Aya ya 20]

Hoja zilizokuwa zimechukuliwa katika mifano ya Agano la Kale, pia zilielekeza kwenye majira ya kupukutisha majani (Septemba-Novemba) kama wakati ambao tukio lililowakilishwa na “kutakaswa kwa Patakatifu.” lazima lingetokea. Jambo hilo lilielezewa kwa uwazi kabisa kwa kutilia mkazo katika mifano iliyohusu ujio wa Kristo kwa mara ya kwanza kama lilivyokuwa limetimizwa." [GC 399.1; PK Aya ya 21]

Kuchinjwa kwa mwana-kondoo wa Pasaka kulikuwa ni kivuli cha wa kifo Chake Kristo: “Basi jisafisheni mkatoe ile chachu ya kale mpate kuwa donge jipya, kama vile mlivyo hamkutiwa chachu. Kwa maana Pasaka wetu amekwisha kutolewa kuwa sadaka yaani Kristo;” 1 Wakorintho 5:7. Mganda wa malimbuko, ambao wakati wa pasaka ulitikiswa mbele ya Bwana, ulikuwa mfano wa ufufo wa Kristo; Paulo anasema, akiongolea kuhusu ufufuo wa Bwana na watu Wake wote: “Limbuko ni Kristo baadaye walio Wake Kristo, atakapokuja” 1 Wakorintho 15:23. Kama ulivyokuwa ule mganda wa kutikisa, ambao ulikuwa nafaka ya kwanza kukomaa na kukusanywa kabla ya mavuno, ndivyo Kristo alivyo limbuko letu la mavuno ya uzima wa milele yasiyopatikana na mauti, ya waliokombolewa, ambao wakati wa ufufuo ujao watakusanywa katika ghala Yake Bwana. [GC 399.2; PK Aya ya 22]

Mifano hii ilitimizwa, sio tu kwa tukio lenyewe; bali pia kwa wakati wake. Siku ya kumi na nne ya mwezi wa kwanza wa Kiyahudi, siku ile ile na mwezi ule ule ambao kwa karne ndefu kumi na tano (miaka 1500) Mwana-Kondoo Yule wa Pasaka alikuwa akichinjwa, Kristo, akiisha kuila Pasaka pamoja na wanafunzi Wake, aliianzisha sherehe ambayo ilipaswa kuadhimisha kumbukumbu ya kifo Chake Mwenyewe kama “Mwana-Kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya

ulimwengu." Usiku ule ule alikamatwa kwa mikono ya waovu na kusulibiwa na kuuawa. Na kama Yule ambaye mfano wa mganda wa kutikiswa ulimlenga, Bwana wetu alifufuka kutoka katika wafu siku ya tatu, akiwa "limbuko lao waliolala," mfano wa wenye haki wote watakaofufuliwa, ambapo "mwili wetu wa unyonge" utabadilishwa, na upate "kufanana na mwili Wake wa utukufu." Fungu la 20; Wafilipi 3:21. [GC 399.3; PK Aya ya 23]

Kwa njia iyo hiyo mifano inavyohusiana na ujio wa mara ya pili wa Kristo ni lazima itimizwe kwa wakati ule uliotajwa katika huduma ya mifano. Chini ya mfumo wa Musa kutakaswa kwa Patakatifu, au Siku Kuu ya Upatanisho, ilitokea katika siku ya kumi ya mwezi wa saba wa Kiyahudi (Mambo ya Walawi 16:29-34), wakati huu kuhani mkuu, baada ya kufanya upatanisho kwa ajili ya Israeli yote, na kwa njia hiyo kuziondoa dhambi zao kutoka Patakatifu, alijitokeza nje na kuwabariki watu. Kwa hiyo iliaminika kuwa Kristo, Kuhani wetu Mkuu, angetokea kuja kuitakasa dunia kwa njia hii ya kuiangamiza dhambi pamoja na wenye dhambi, na kuwabariki watu Wake waliokuwa wanangojea kupewa hali ya kutokufa (uzima wa milele). Siku ya kumi ya mwezi wa saba, yaani, Siku Kuu ya Upatanisho, wakati wa kutakaswa kwa Patakatifu, ambayo katika mwaka wa 1844 iliangukia katika tarehe ya ishirini na mbili, Oktoba, na ilichukuliwa kwamba utakuwa ndio wakati wa kuja Kwake Bwana. Tarehe hii iliafikiana na uthibithisho ambao ulikwisha kutolewa tayari, kwamba siku zile 2300 zingeishia katika majira yale ya kupukutisha majani (Septemba-Novemba), na hitimisho hilo lilionekana lisilowezwa kuzuilika.[GC 399.4; PK Aya ya 24]

Katika mfano wa Mathayo 25 wakati wa kungoja na kulala usingizi hufuatiwa na kuja Kwake Bwana harusi. Hilo lilikuwa limekubaliana na hoja zilizokuwa zimekwisha kutolewa punde, kutoka sehemu zote mbili--- kutoka katika unabii na kutoka katika mifano. Walikuwa wameshawishika kabisa kuhusu Ukweli wake; na kile "kilio cha usiku wa manane" kilibebwa na kuhubiriwa na maelfu ya walioamini, na ikawa kama mbiu inayopigwa au tangazo la kutoa tahadhari. [GC 400.1; PK Aya ya 25]

Kama wimbi kubwa la tsunami linavyoenea ndivyo vuguvugu la marejeo lilivyoifagia nchi. Kutoka jiji hadi jiji, toka kijiji hata kijiji, na kwenda mpaka kwenye sehemu za mbali sana huko pembezoni mpaka mashambani, mpaka watu wa Mungu waliokuwa wakingojea walipokuwa wameamshwa kikamilifu. Ushupavu wa dini usiotumia akili ulitoweka mbele ya tangazo hili kama umande wa barafu wa alfajiri unavyoyeyuka kabla ya jua kuchomoza. Waamini waliona mashaka yao, kuchanganyikiwa kwao na fadhaa vikiyeyuka, na tumaini na ujasiri vikaichangamsha mioyo yao. Kazi hii ikawa haina misimamo mikali inayopitiliza mipaka, ambayo daima inadhihirishwa wakati wa kunapokuwa na msisimko wa kibinadamu usiotawaliwa na mvuto wa Neno, wala na Roho wa Mungu. Uzoefu huu ulikuwa na tabia inayofanana na nyakati za kujinyenyekeza na kumrudia

Bwana ambazo, zilifuata miongoni mwa Israeli ile ya zamani, baada ya ujumbe wa onyo kutolewa na watumishi Wake. Ujumbe huu ulibeba sifa na tabia zinazoashiria kazi ya Mungu katika kila zama. Furaha inayotokana na misisimko au mihemko tu ilikuwa ndogo sana, na badala yake palikuwa na kujichunguza moyo kwa kina, kuungama dhambi na kuachana na mambo ya ulimwengu huu. Kujiandaa kukutana na Bwana ulikuwa ndio mzigo ulioumiza roho zao. Kulikuwa na maombi ya dhati na yasiyochoka na kujiweka wakfu kikamilifu kwa Mungu.[GC 400.2; PK Aya ya 26]

Miller alisema hivi katika kueleza habari ya kazi ile: "Hakuna onyesho kubwa la shangwe: yaani, mambo yalivyokuwa ni kana kwamba shangwe hiyo ilikuwa imetunzwa kwa ajili ya tukio lijalo, wakati mbingu na dunia yote vitakaposhangilia pamoja kwa furaha isiyoneneka, na ikiwa imejaa utukufu. Hakuna kupiga makelele: hilo pia lilihifadhiwa kwa ajili ya kupiga kelele huko mbinguni. Waimbaji wako kimya: wanasubiri kujiunga na jeshi la malaika, kwaya ya kutoka mbinguni.... Hakuna mgongano wa hisia au maoni: wote wana moyo mmoja na nia moja." - Bliss, ukurasa wa 270, 271. [GC 401.1; PK Aya ya 27]

Mwingine aliyeshiriki katika vuguvugu hilo, alitoa ushuhuda huu: "Kila mahali, kazi ile ilikuwa imeleta kujichunguza moyo kwa kina sana na kujinyenyekesha nafsi mbele za Mungu wa mbinguni juu. Ilisababisha kuyaondoa mapenzi kutoka katika mambo ya ulimwengu huu, kuponya mabishano, mashindano na uhasama/uadui, na kuwafanya watu kuungama makosa yao, kupondeka mioyo mbele za Mungu, na kutoa dua Kwake kwa moyo wa toba, ilihamasisha moyo uliovunjika-vunjika, na kujutia makosa ili kupatiwa msamaha na kukubaliwa Naye. Ilileta kuushusha na kuunyenyekesha moyo na kuilaza nafsi kifudifudi, katika hali tuliyokuwa hatujapata kamwe kuishuhudia. Kama Mungu alivyoagiza kupitia kwa Yoeli, wakati siku ile ya Bwana itakapokuwa imekaribia, kazi hii ilileta uraruaji wa mioyo, na wala si mavazi, na kumgeukia Bwana kwa kufunga na kulia na kuomboleza. Kama Mungu alivyosema kupitia kwa Zekaria, roho ya neema na dua ilimwagwa juu ya watoto Wake; nao wakamwangalia Yeye ambaye walimchoma kwa mikuki, pakawa na maombolezo makuu katika nchi,..... tena wale waliokuwa wakitazamia kumwona Bwana walijitesa kwa kutaabisha nafsi zao mbele Zake." - Bliss, in. Advent Shield na Review, juzuu ya 1 uk. 271 (Januari, 1845). [GC 401.2; PK Aya ya 28]

Katika harakati zote za kidini tangu siku za Mitume, hakuna harakati hata moja iliyokuwa na kiasi kidogo cha udhaifu wa kibinadamu na hila za Shetani chache zaidi ya ile la majira yale ya kupukutisha ya mwaka 1844. Hata sasa, baada ya kupita miaka mingi, wale wote walioshiriki vuguvugu lile na ambao hata sasa bado wamesimama kidete juu ya jukwaa hilo la Ukweli, bado wanauhisi mvuto mtakatifu wa kazi ile iliyobarikiwa na takatifu, nao wanatoa ushaidi wao kwamba lilikuwa vuguvugu la Mungu. [GC 401.3; PK Aya ya 29]

Wakati kelele ya wito ilipopigwa, ikisema, “Haya, Bwana arusi Yuaja; tokeni mwende kumlaki,” wale waliokuwa wakingojea “wakaondoka ... wakatengeneza utambi wa taa zao;” yaani, wakajifunza Neno la Mungu kwa shauku kubwa sana, ambayo ilikuwa haijapata kujulikana kabla yake. Malaika walitumwa kutoka mbinguni kuwaamsha wale waliokuwa wamevunjika moyo na kukatishwa tamaa na kuwaandaa ili waweze kuupokea ujumbe. Kazi hii haikutegemea hekima, wala usomi wa mwanadamu, bali ilikuwa ni kwa nguvu ya Mungu. Hawakuwa watu wenye vipaji vikubwa au talanta kuliko watu wengine wote, bali walikuwa wa kwanza kuusikia na kuutii mwito ule, tena walikuwa watu wanyenyekevu sana ambao walikuwa wamejitoa wakfu sana. Wakulima waliacha mazao yao yakiwa yamesimama mashambani mwao, mafundi walizitupa chini zana zao, na kwa machozi na furaha kuu walitoka kwenda kulitoa lile onyo. Wale waliokuwa wa kwanza kuongoza kazi, walikuwa miongoni mwa watu wa mwisho kujiunga katika vuguvugu hili. Kwa jumla makanisa yote yalifunga milango yao dhidi ya ujumbe huu, na kundi kubwa la wale walioupokea walijiondoa katika ushirika wa makanisa. Kwa uongozi wa Mungu, utangazaji huu uliungana na Ujumbe wa Malaika wa Pili na kuipa nguvu kazi hiyo.[GC 402.1; PK Aya ya 30]

Ujumbe, “Haya, Bwana arusi Yuaja!” haukuwa na suala la kubishania, ingawa uthibitisho wa Maandiko ulikuwa wazi na wa kuhitimisha. Pamoja na ujumbe ilikuwamo nguvu iliyowashinikiza watu kwa kuigusa mioyo yao. Hapakuwa na mashaka yoyote, hapakuwa na maswali yoyote. Katika tukio la Kristo kuingia kwa shangwe na ushindi mjini Yerusalemu, watu waliokuwa wamekusanyika toka katika sehemu zote za nchi ile kuadhimisha sikukuu ile walikusanyika kwenda kwenye Mlima wa Mizeituni, nao walipojiunga na kadamnasi kubwa iliyokuwa imeshonana ikimsindikiza Yesu, waliguswa na hamasa ya saa ile, nao wakasaidia kuvumisha makelele wakisema: “Abarikiwe Yeye ajaye kwa Jina la Bwana!” Mathayo 21:9. Halikadhalika wasioamini waliofurika kwenye mikutano ya Waadventista-- wengine kwasababu ya udadisi wao tu, wengine kwa kusudi la kudhihaki- walihisi nguvu ya ushawishi, ambao iliandamana na ujumbe uliosema: “Haya, Bwana Arusi Yuaja!” [GC 402.2; PK Aya ya 31]

Wakati huo palikuwa na imani iliyoleta majibu kwa maombi yao - imani iliyoheshimiwa kwa kupewa thawabu kuu. Kama manyunyu ya mvua juu ya ardhi iliyo na kiu, Roho yule wa neema aliwashukia watafutaji wale wa dhati na wenye bidii. Wale waliotazamia katika muda mfupi kusimama uso kwa uso na Mkombozi wao, walipata furaha kubwa moyoni isiyoweza kuelezeka. Uweza wa Roho Mtakatifu ulainishao na utiishao (uletao utii), uliuyeyusha moyo wakati Mbaraka Wake uliposhushwa kwa wingi sana juu ya wale waliokuwa waaminifu na wenye imani.[GC 402.3; PK Aya ya 32]

Kwa uangalifu, uaminfu, taadhima na kicho, wale walikuwa wameoupokea ujumbe waliufikia muda ambao walitumaini kukutana na Bwana na Mkombozi

wao. Kila asubuhi walijisikia ya kuwa ulikuwa ni wajibu wao wa kwanza kujipatia uthibithisho wa kukubaliwa kwao na Mungu. Mioyo yao ilikuwa imeunganishwa kwa ukaribu sana, nao waliomba sana wakiwa pamoja na pia kila mmoja alimwombea mwenzake. Mara nyingi walikutana pamoja kwenye maeneo ya faragha ili kuzungumza na Mungu, na sauti ya kuombeana kwao ikapanda juu mbinguni kutoka mashambani na nyikani. Uhakikisho wa kukubaliwa na Mwokozi ulikuwa ni wa muhimu sana kwao kuliko chakula chao cha kila siku; na iwapo wingu lilitia giza akili au mioyo yao, basi, hawakuweza kutulia mpaka lilipofagiliwa mbali. Walipohisi ushuhuda wa neema isameheyo, walitamani sana kumwona Yeye ambaye mioyo yao ilimpenda. [GC 403.1; PK Aya ya 33]

**Wakata Tamaa Tena**

Lakini kwa mara nyingine tena walikabiliwa na kukata tamaa. Wakati huu wa matarajio ya Ujio wa Yesu ulikuja na ukapita, na wala Mwokozi wao hakutokea. Kwa Imani na ujasiri usiotetereka walikuwa wametazamia ujio Wake, na sasa walijisikia vibaya kama alivyohisi Mariamu wakati alipofika kwenye kaburi la Mwokozi na kulikuta liko tupu, ndipo alipopiga kelele na kulia kwa mshangao akisema: "Wamemwondoa Bwana wangu, wala sijui walikomlaza." Yohana 20:13. [GC 403.2; PK Aya ya 34]

Hisia ya kicho na hofu kuu, yaani, woga kwamba ujumbe huu huenda unaweza kuwa wa kweli, kwa kipindi fulani ilikuwa kama kizuizi kwa ulimwengu uliokuwa hauamini. Baada ya muda kupita hofu hii haikutoweka mara moja; mwanzoni hawakuthubutu kuwazomea wale waliokatishwa tamaa kama ni watu walioshindwa; lakini kwa kuwa hakuna dalili zozote za ghadhabu ya Mungu zilizoonekana, walipata nafuu kwa kupona hofu yao na kuendelea tena na kuwagombeza na kuwadhihaki wenzao. Kundi kubwa la wale ambao walikuwa wamedai kuamini ujio wa Bwana wa haraka, walikana imani yao. Wengine ambao walikuwa wamejiamini sana kuhusu tukio hilo, walijeruhiwa mno kutokana na kiburi chao kiasi kwamba walitamani kutoweka ulimwenguni. Kama Yona, alivyotenda, hawa walimlalamikia Mungu na wakaona ni bora kuchagua kifo kuliko kuishi. Wale ambao walikuwa wameweka imani yao juu ya maoni ya wengine na si juu ya Neno la Mungu, walikuwa sasa tayari tena kubadili maoni yao. Watu wenye dhihaka waliwavuta watu dhaifu na waoga kuingia katika safu zao, na hawa wote walijiunga pamoja kutangaza kwamba sasa pasingekuwa na hofu tena au matarajio mengine zaidi. Wakati mahsusi waliouweka ulikuwa umepita, na Bwana alikuwa hajaja, na ulimwengu ungeendelea kubaki vile vile kwa maelfu ya miaka. [GC 403.3; PK Aya ya 35]

Watu walioamini kwa dhati, wanyofu wa moyo, walikuwa wametoa vyote kwa ajili ya Kristo na walikuwa wameshiriki uwepo Wake kuliko wakati mwingine uliopita. Walikuwa kama walivyoamini, walikuwa wametoa onyo lao la mwisho

kwa ulimwengu; na walisubiri muda mfupi kupokelewa katika jamii ya Bwana wao wa mbinguni na malaika Zake, wakawa wamejitenga kwa kiwango kikubwa kutoka katika jamii ya wale ambao hawakupokea ujumbe huo. Kwa matamanio makubwa walikuwa wakiomba hivi "Njoo, Bwana Yesu, na uje upesi." Lakini Bwana hakuja. Na sasa kurudi tena kubeba majukumu mazito ya mahangaiko, masumbufu na mashaka ya maisha na kustahimili kejeli na matusi ya ulimwengu wenye dhihaka, lilikuwa jaribu la kutisha sana la imani na uvumilivu. [GC 404.1; PK Aya ya 36]

Hata hivyo hali hii ya kukatishwa tamaa haikuwa kubwa kama ilivyokuwa kwa wanafunzi wakati wa ujio wa Kristo kwa mara ya kwanza. Yesu Kristo alipopanda punda kwa shangwe kuingia Yerusalemu, wafuasi Wake waliamini kwamba alikuwa karibu kukalia kiti cha enzi cha Daudi na kuwakomboa Israeli kutoka utawala uliowakandamiza. Kwa matumaini makubwa na matazamio yenye furaha walipigana vikumbo wao kwa wao, wakishindana kuonyesha heshima kwa Mfalme wao. Wengi walitandaza mavazi yao ya nje kama zulia katika njia Yake Mwokozi, wengine walitandaza mbele Yake matawi yenye majani ya mitende. Katika shamrashamra yao iliyojaa shauku, waliungana katika shangwe hii: "Hosana kwa Mwana wa Daudi!" Wakati Mafarisayo, wakidhika na kukasirishwa na mlipuko huo wa shangwe, nao walimwomba Yesu awakemee wanafunzi Wake, Naye aliwajibu hivi: "Hawa wakinyamaza, mawe yatapiga kelele mara moja." Luka 19:40. Unabii lazima utimizwe. Wanafunzi walikuwa wakitimiza kusudi la Mungu; lakini walikuwa wakielekea kwenye kukatishwa tamaa sana huko mbele. Hazikupita siku chache kabla hawajashuhudia kifo cha uchungu wa kutisha cha Mwokozi na wakaona akilazwa kaburini. Matarajio yao hayakuwa yametimia hata chembe, na matumaini yao yalikufa pamoja na Yesu. Ni mpaka Bwana wao alipokuwa amefufuka kutoka kaburini kwa ushindi, ndipo waliweza kutambua kwamba yote yalikuwa yametabiriwa na unabii na "ya kwamba ilimpasa Kristo kuteswa, na kufufuka katika wafu." Matendo 17:3. [GC 404.2; PK Aya ya 37]

Miaka mia tano kabla ya hapo, Bwana alikuwa ametangaza hivi kupitia nabii Zekaria: "Furahi sana, Ee binti Sayuni; piga kelele, Ee binti Yerusalemu; tazama, Mfalme wako anakuja kwako; ni Mwenye haki, Naye ana wokovu; ni mnyenyekevu, amepanda punda, naam, mwanapunda, mtoto wa punda." Zekaria 9:9. Kama wanafunzi wangegundua kwamba Kristo alikuwa anaenda kuhukumiwa na kufa, wasingetenda sehemu ya kuutimiza unabii huu namna hiyo.[GC 405.1; PK Aya ya 38]

Hali kadhalika Miller na wenzake walitimiza unabii na kutoa ujumbe ambao Uvuvio ulikuwa umetabiri kwamba ungetolewa kwa ulimwengu, lakini ambao wasingeweza kuutoa kama wangeelewa kikamilifu unabii unaoonyesha kukatishwa tamaa kwao, na ukiwaambia ujumbe mwingine wa kuhubiri kwa mataifa yote kabla marejeo ya Bwana. Ujumbe wa malaika wa kwanza na wa pili

wa imani, ulitolewa kwa wakati sahihi na ulikamilisha kazi ambayo Mungu alikusudia itekelezwe kupitia wao. [GC 405.2; PK Aya ya 39]

Ulimwengu ulikuwa ukitarajia kwamba ikiwa wakati huo ungepita na Kristo asitokee, basi mfumo wote wa Uadventista ungekufa (ungekatiwa tamaa). Ijapokuwa wengi chini ya majaribu makali waliiacha Imani yao, walikuwepo baadhi ya watu waliosimama imara. Matunda ya vuguvugu la marejeo, roho ya unyenyekevu na kujipeleleza moyo, kuuacha ulimwengu na kufanya matengenezo ya maisha, ambavyo viliambatana na kazi hiyo, vilishuhudia kwamba vuguvugu hili lilikuwa ya Mungu. Hawakuthubutu kukataa kwamba nguvu ya Roho Mtakatifu ilikuwa imeshuhudia utangazaji wa ujio wa pili na hawakuweza kugundua kosa lolote katika ukokotoaji wa vipindi vya kiunabii. Wapinzani wao hodari kabisa hawakufaulu kuukosoa mfumo wao wa kutafsiri unabii. Wasingeweza kuafiki pasipo mamlaka ya ushahidi wa Biblia, kuachana na misimamo yao ambayo ilikuwa imefikiwa kwa kujifunza Maandiko kwa bidii kubwa na maombi, kwa akili zilizoangazwa na Roho wa Mungu na mioyo iliyokuwa inawaka kwa nguvu iliyo hai; misimamo ambayo ilikuwa imestahimili ukosoaji makini na upinzani mkali wa waalimu wa dini mashuhuri, na watu wenye hekima ya kidunia na ambayo ilistahimili kwa uimara mkubwa dhidi ya majeshi ya pamoja ya elimu na ufasaha, dhihaka, shutuma na kashfa za watu wenye kuheshimiwa na  na hata jamii ya watu wa hali ya chini. [GC 405.3; PK Aya ya 40]

Ni kweli, kulikuwepo na kukosea kuhusiana na tukio lililotarajiwa, lakini hata hili halikuweza kuitikisa imani yao katika Neno la Mungu. Yona alipotangaza katika mitaa ya Ninawi kwamba ndani ya siku arobaini mji ungeangamizwa, Bwana alikubali kujinyenyekeza kwa Waninawi na kuongeza muda wao wa rehema; pamoja na hayo ujumbe wa Yona ulitumwa na Mungu na Ninawi ilijaribiwa kulingana na mapenzi Yake Bwana. Waadventista waliamini kwamba kwa jinsi kama hiyo Mungu alikuwa amewaongoza kutoa onyo la hukumu. “ujumbe, umeijaribu mioyo ya wote waliousikia,” walisema, “na umeamsha upendo kwa ajili ya kuja Kwake Bwana; au umeleta chuki, inayoeleweka au isiyoeleweka kwa wanadamu, lakini inayojulikana kwa Mungu kuhusu ujio Wake. Ujumbe huu umechora mstari, ..... ili wale ambao watakaoipima mioyo yao wenyewe, wapate kujua ni upande gani wa mstari wangekutwa-- ikiwa Bwana angekuwa amekuja wakati ule-Je, wangesema kwa furaha, ‘Tazama! Huyu Ndiye Mungu wetu tuliyemngoja Naye atatuokoa; au ikiwa wangeiita miamba na milima ipate kuwaangukia na kuwaficha wasiuone uso Wake Yeye aketiye juu ya kiti cha enzi, na ghadhabu ya Mwana-Kondoo. Hivyo ndivyo tunavyoamini, Mungu alikuwa amewajaribu watu Wake, alikuwa ameijaribu imani yao, akawathibitisha na kuona kama wangejikunja kwa hofu katika saa ya kujaribiwa, na kuiacha nafasi ambayo Bwana aliona inafaa kuwaweka; au ikiwa wangeiacha dunia hii na

kulitegemea kwa uthabiti Neno la Mungu." The Advent Herald and Signs of the Times Reporter, juzuu ya 8, No. 14 (Nov 13, 1844). [GC 406.1; PK Aya ya 41]

Hisia za wale ambao bado waliamini kwamba Mungu alikuwa amewaongoza katika uzoefu wao uliopita zimeelezwa katika maneno ya William Miller: "Ikiwa ningekuwa na uwezo wa kuishi maisha yangu tena, nikiwa na ushahidi uleule niliokuwa nao wakati ule, ili kuwa mwaminifu kwa Mungu na mwanadamu, mimi bado ningefanya yale yale niliyofanya" "Ni matumaini yangu kuwa nimeyatakasa mavazi yangu kutoka kwa damu ya roho za watu. Ninahisi kwamba, kwa kadiri ilivyokuwa katika uwezo wangu, nimejiweka huru kutokana na hatia zao zote na hukumu yao." "Ingawa nimevunjika moyo mara mbili," aliandika mtu huyo wa Mungu, "bado sijasononeshwa wala kuvunjika moyo kabisa-- Tumaini langu katika ujio wa Kristo lina nguvu na litadumu na nguvu kama zamani. Nimefanya tu kile ambacho baada ya miaka mingi ya tafakari nzito, nilihisi kuwa ni wajibu wangu adhimu kufanya. Ikiwa nimekosea, imekuwa hivyo kwa upande wa ukarimu, na upendo kwa wanadamu wenzangu, na usadikisho wa wajibu wangu kwa Mungu." "Jambo moja nalolijua, sikuhubiri chochote kile isipokuwa kile tu ambacho nimekiamini; na Mungu amekuwa pamoja nami; Nguvu Zake zimedhihirika katika kazi hiyo, na mema mengi yametokea." "Maelfu mengi, ya watu, kwa mtazamo wa kibinadamu, wamehamasishwa kujifunza Maandiko kwa kuhubiriwa juu ya wakati huo; na kwa njia hiyo, kupitia imani na umwagikaji wa damu ya Kristo, wamepatanishwa na Mungu."— Bliss, ukurasa wa 256, 255, 277, 280, 281. "Sijawahi kutafuta tabasamu za wenye kiburi, wala kutetemeka wakati ulimwengu ulipokunja uso wake. Hata sasa siwezi kununua upendeleo wao, wala sitavuka wajibu ili kuchokoza chuki yao. Sitafuti uhai wangu mikononi mwao, wala sitarudi nyuma kwa woga, natumaini kupoteza uhai wangu, ikiwa Mungu katika uongozi Wake mwema ataamuru hivyo."*—J. White, Maisha ya William. Miller, ukurasa wa 315 *(Ikiwa angekabiliwa na kifo kwa ajili ya imani yake, hangewaomba watesi wake waokoe maisha yake, wala asingeweza kuogopa kufa, ikiwa kifo hicho kilikuwa mapenzi ya Mungu.)[GC 406.2; PK Aya ya 42]

Mungu hakuwaacha watu Wake; Roho Wake bado aliendelea kukaa pamoja na wale ambao hawakuikataa nuru waliyoipokea bila kutafakari au kwa mihemko fulani tu, na kukana hadharani vuguvugu la marejeo: Katika Waraka kwa Waebrania kuna Maneno ya kutia moyo na onyo kwa wale waliojaribiwa, waliongoja wakati wa dharua au janga hili: "Basi msiutupe ujasiri wenu, Kwa maana una thawabu kuu. Maana mnahitaji saburi, ili kwamba mkiisha kuyafanya mapenzi ya Mungu mpate ile ahadi. Kwa kuwa bado kitambo sana, Yeye ajaye atakuja, wala hatakawia. Lakini Mwenye haki Wangu ataishi kwa imani; Naye akisita-sita, roho Yangu haina furaha Naye. Lakini sisi hatumo miongoni mwao wasitao na kupotea, bali tumo miongoni mwa hao na imani ya kutuokoa roho zetu." Waebrania 10:35-39. [GC 407.1; PK Aya ya 43]

Kwamba onyo au agizo hili limeelekezwa kwa kanisa la siku za mwisho ni ushahidi tosha kwamba mausia haya huonyeshwa ukaribu wa ujio wa Bwana: “Kwa maana bado kitambo kidogo, Yeye ajaye atakuja, wala hatakawia.” Na inadokezwa moja kwa moja kwamba kungekuwapo na mwonekano wa kukawia, na ya kwamba Bwana angeonekana kana kwamba anakawia. Maelekezo yaliyotolewa hapa yanahusiana hasa na uzoefu wa Waadventista/Wanamarejeo wa wakati huu. Watu walioonywa hapa walikuwa katika hatari ya kupoteza Imani yao (1Tim 1:19). Walikuwa wamefanya mapenzi ya Mungu kwa kufuata mwongozo wa Roho Wake na Neno Lake; walakini hata hivyo hawakuweza kuelewa kusudi Lake katika uzoefu wao uliopita, wala hawakuweza kutambua njia iliyokuwa mbele yao, nao walijaribiwa kutilia shaka kama kweli Mungu alikuwa akiwaongoza. Wakati huu maneno haya yalikuwa na maana sana kwao: “Sasa mwenye haki ataishi kwa imani.” wakati wa nuru kali ya “kilio cha usiku wa manane” ilipokuwa imeangazia kwenye njia yao, nao walipokuwa wameona unabii ukifunuliwa na utimizwaji wa dalili zilizoashiria kuwa ujio wa Kristo ulikuwa karibu, walikuwa wametembea, kwa kuona kwa macho ya kibinadamu kama hali ya mambo yenyewe yalivyokuwa, lakini sasa, wakiwa wameinamishwa chini kwa matumaini yaliyokatishwa tamaa, wangeweza kuinuka na kusimama tu kwa kumwamini Mungu na kuliamani Neno Lake. Ulimwengu wenye dhihaka ulikuwa ukisema: “Mmedanganywa. Acheni imani yenu, na semeni kwamba vuguvugu la marejeo lilikuwa la Shetani. Lakini Neno la Mungu lilitangaza hivi: lakini “Mtu akisitasita, nafsi Yangu haitakuwa na furaha naye.” Kuikana imani yao hadharani sasa, na kuikataa nguvu ya Roho Mtakatifu iliyoambatana na ujumbe, ingekuwa kurudi nyuma na kuelekea upotevuni. Walitiwa moyo kuwa jasiri na maneno ya Paulo: “Basi msiutupe ujasiri wenu; Mnahitaji saburi, kwa maana bado kitambo kidogo, na Yeye ajaye atakuja, wala hatakawia.” Usalama wao pekee ulikuwa katika kushikilia nuru ambayo tayari walikuwa wameipokea kutoka kwa Mungu, kushikilia sana ahadi Zake, na kuendelea kuyachunguza Maandiko, na kungoja na kukesha kwa subira ili kupokea nuru zaidi. [GC 408.1; PK Aya ya 44]

# SURA YA 23

# PATAKATIFU NI NINI?

**(Siri Za Hekalu La Mungu—Patakatifu Na Patakatifu Pa Patakatifu Ndani Ya Madhabahu)**

Ufupisho: Biblia inatuelezea kuhusu Patakatifu palipojengwa kwa amri ya MUNGU Kwenye Kutoka 25. Huu lilikuwa ni jengo la kustaajabisha na lenye maelezo mengi, mahsusi na nyeti sana ambayo yana maana ya pekee kwetu leo. Hii ilikuwa picha ya wokovu wa mwanadamu iliyoelezwa kwa njia rahisi inayoeleweka kwa akili finyu za mwanadamu. Huduma hii iliyotabiri matukio yajayo kuhusu mpango mkuu wa wokovu kwa ajili ya wanadamu inashangaza sana. Tunahitaji kujifunza kusudi la Patakatifu pa Patakatifu pa mbinguni, katika kitabu cha Waebrania na maana yake katika maisha yetu sasa hivi. Karibu usome kuhusu Patakatifu pa unabii, Jengo la ajabu sana katika ulimwengu wote na huduma ya Masihi kwa niaba yako na yangu ndani yake. Mlango umefunguliwa kwa ajili yetu, nao unaingia kwenye chumba cha enzi cha MUNGU.

Andiko ambalo limekuwa msingi na nguzo kuu ya imani ya marejeo juu ya yote mengine katika imani ya Marejeo/Waadventista lilikuwa ni tamko hili: "Hata nyakati za jioni na asubuhi (miaka) elfu mbili na mia tatu; ndipo Patakatifu patakapotakaswa." Danieli 8:14. Hayo yalikuwa ni Maneno yaliyojulikana sana kwa wote waliokuwa wanauamini ujio wa haraka wa Bwana. Maelfu ya vinywa vya watu waliukariri unabii huo na wakaurudia-rudia tena kama Kaulimbiu yao kuu ya imani. Wote walihisi juu ya matukio yaliyotabiriwa katika Aya hii na ndipo ndani yake kulikuwa na matarajio yao yaliyong'aa sana pamoja na matumaini waliyoyathamini moyoni mwao mno. Siku hizi za kiunabii zilionyeshwa kuwa zitaishia katika majira ya kupukutisha majani (Septemba – Novemba) ya mwaka wa 1844. Wakiwa na msimamo mmoja na Ulimwengu mzima wa Kikristo, Waadventista wa wakati huo waliamini kwamba dunia hii, au sehemu yake fulani, ilikuwa ni Patakatifu. Walielewa kwamba kutakaswa kwa Patakatifu kulikuwa ni kusafisha dunia hii kwa mioto ya siku kuu ya mwisho na ya kwamba tukio hili lingetokea wakati wa ujio wa pili wa Masihi. Ndiyo maana walifikiria hitimisho kuwa Kristo angerudi tena duniani katika mwaka wa 1844. [GC 409.1; PK Aya ya 1]

Lakini wakati huo uliopangwa ukawa umepita, na Bwana akawa hakutokea. Waumini waliamini kwamba Neno la Mungu haliwezi kushindwa wala kukosea; basi, wakaona kwamba huenda tafsiri yao ya unabii, bila shaka ndiyo ilikuwa na makosa; lakini kosa lile lilikuwa wapi? Wengi bila kufikiri walikikata kifundo kile cha utata kwa haraka kwa kukana kuwa siku zile 2300 hazikuishia mwaka wa

1844. Hakuna sababu yoyote iliyoweza kutolewa kwa ajili ya wazo lao hii isipokuwa tu kwamba Kristo alikuwa hajaja kwa wakati ule waliomtarajia. Walijenga hoja kwamba kama siku za kiunabii ziliishia mwaka wa 1844, basi, Kristo angekuwa amekwisha kuja kupatakasa Patakatifu kwa kuisafisha dunia hii kwa moto; na kwamba kwa kuwa alikuwa hajaja, basi, siku zile zilikuwa bado hazijaisha au kufikia mwisho wake. [GC 409.2; PK Aya ya 2]

Kulikubali hitimisho hili kulimaanisha kukanusha ukokotoaji wa awali wa vipindi vya kiunabii. Siku 2300 zilikuwa zimeonekana kwamba zilianza wakati amri ya Artashasta ya kuujenga upya Yerusalemu ilipotekelezwa katika majira ya kupukutisha majani ya mwaka wa 457 K.K. Kwa kuchukua wakati huu kama ndiyo mahali pa kuanzia, basi, kulikuwa na mwafaka kamili wa matukio yote yaliyotabiriwa katika maelezo ya kipindi kilicho katika Danieli 9:25- 27. Majuma yale sitini na tisa, yaani, miaka 483 ya kwanza [7 x 69 = 483] katika kipindi cha miaka 2300, yalipaswa kuiishia wakati wa Masihi, yaani, Mpakwa Mafuta; na ubatizo Wake Kristo na kupakwa mafuta na Roho Mtakatifu katika mwaka wa 27 B.K., vilitimiza kikamilifu kabisa vipengele vyote vya unabii ulioelezwa. Katikati ya juma lile la saba, Masihi alipaswa kukatiliwa mbali (kuuawa kikatili). Miaka mitatu na nusu baada ya ubatizo Wake, Kristo alisulibiwa katika majira ya kuchipua majani (Machi-Mei) ya mwaka wa 31 B.K. (27 + 3 ½ = 30 ½ = 31.) Majuma yale sabini, au miaka 490 (70 x 7 = 490), yalitengwa kwa ajili ya Wayahudi peke yao. Mwishoni mwa kipindi hiki taifa lilitia muhuri kumkataa kabisa Kristo kwa kuwatesa wanafunzi Wake (kama Taifa Takatifu –23:37-39; Lk. 19:41-44), ndipo Mitume walipowageukia Mataifa katika mwaka wa 34 B.K. (Mdo. 13:44-52). Miaka 490 ya kwanza katika ile miaka 2300 ilipokuwa imekwisha wakati ule, miaka 1810 ilikuwa imebaki (2300-490 = 1810). Tangu mwaka wa 34 B.K., miaka 1810 inaishia mwaka 1844 (34+1810=1844). “Ndipo,” akasema malaika, “Patakatifu patakapotakaswa.” Vipimo au mambo yote yahusuyo huu unabii, na vipengele vyake vyote vilivyotangulia vilikuwa vimetimizwa bila kuacha shaka lolote kwa wakati ule ule uliowekwa. [GC 410.1; PK Aya ya 3]

Kutokana na mahesabu haya, mambo yote yalikuwa wazi, tena yaliafikiana (yalipatana), isipokuwa ilionekana kwamba hapakuwa na tukio lolote lililokuwa limetokea katika mwaka wa 1844 ambalo lingetoa jibu la kutosheleza kuhusu kutakaswa kwa Patakatifu. Kukataa kwamba siku hizi ziliishia wakati ule ilikuwa ni kuutosa unabii wote katika mkanganyiko, na kukanusha suala hili zima kwa kukataa misimamo iliyokuwa imethibithishwa kwa utimizo usio na mashaka wa matukio mbali mbali ya unabii. [GC 410.2; PK Aya ya 4]

Lakini basi, ni Mungu Ndiye aliyekuwa amewaongoza watu Wake katika vuguvugu za marejeo ya pili (Kiadventista); nguvu, uweza na utukufu Wake ulikuwa umeambatana na kazi ile, wala Yeye Asingeiruhusu kazi hii iishie katika giza, na kukata tamaa, wala kudhihakiwa kwamba ilikuwa ni msisimko wa uongo

na ushupavu wa dini usiotumia akili. Yeye asingeweza kuruhusu Neno Lake libaki katika mashaka na kutokuwa na mwelekeo. [GC 410.3; PK Aya ya 5]

Ingawa wengi waliachana na ukokotoaji wa awali wa vipindi vya kiunabii na kukataa usahihi wa vuguvugu lililokuwa limejengwa juu yake, wengine hawakuwa tayari kukubali kuvikana vipengele vya imani yao pamoja na uzoefu waliokuwa wameupata, yaani mambo yote yalitegemezwa na ushahidi wa Maandiko pamoja na ushuhuda wa Roho wa Mungu. Walisadiki kabisa kwamba walikuwa wametumia kanuni sahihi na thabiti za kufasiri katika kujifunza kwao unabii, na ya kwamba ilikuwa ni wajibu wao kuzishikilia sana zile Kweli zilizokuwa zimekwishapatikana, na kuendelea na kuwajibika kwa moyo na bidii ile ile ya utafiti wa Biblia. Kwa maombi yao ya dhati na bidii walirejelea tena msimamo wao na kujifunza Maandiko ili kuligundua kosa lao. Kwa kuwa walishindwa kuliona kosa lolote katika ukokotoaji wa vipindi vya kiunabii, waliongozwa kulichunguza kwa ukaribu zaidi somo lile la Patakatifu. [GC 410.4; PK Aya ya 6]

Katika uchunguzi wao waligundua kwamba hapakuwa na ushahidi wowote katika Maandiko ulioliunga mkono wazo lile lililoaminiwa na watu wengi ambalo lilisema kwamba dunia hii ndiyo ilikuwa Patakatifu; ila walipata katika Biblia maelezo kamili juu ya somo la Patakatifu, jinsi palivyo, asili yake, mahali na huduma zake; ushuhuda wa waandishi watakatifu ulikuwa na nuru wazi na ya kutosha kiasi cha kuweza kuliweka suala mbali na maswali yoyote. Mtume Paulo, katika Waraka wake kwa Waebrania, anasema hivi: “Basi hata agano la kwanza lilikuwa na kawaida za ibada, na Patakatifu pake, pa kidunia. Maana hema ilitengenezwa, ile ya kwanza, mlimokuwa na Kinara cha Taa, na Meza, na Mikate ya -Wonyesho; ndipo palipoitwa, Patakatifu. Na nyuma ya pazia la pili, ile hema iitwayo Patakatifu pa Patakatifu, yenye chetezo cha dhahabu, na Sanduku la Agano lililofunikwa kwa dhahabu pande zote, mlimokuwa na kopo la dhahabu lenye ile Mana, na ile Fimbo ya Haruni iliyochipuka, na vile Vibao vya agano (Amri Kumi); na juu yake Makerubi ya utukufu, yakikitia kivuli Kiti cha Rehema.” Waebrania 9:1-5. Waebrania 9:1-5. [GC 411.1; PK Aya ya 7]

Patakatifu ambapo Paulo anaparejelea hapo juu ni ile hema iliyojengwa na Musa kwa amri ya Mungu kama makazi Yake Yeye Aliye juu sana hapa duniani (hema ya kukutania). “Nao na wanifanyie Patakatifu; ili Nipate kukaa kati yao” (Kutoka 25:8), hilo ndilo lilikuwa agizo na mwongozo alilopewa Musa wakati alipokuwa katika Mlimani na Mungu. Wana wa Israeli walikuwa wakisafiri jangwani, na hema lilikuwa limejengwa kwa namna ambayo ingeweza kuhamishwa toka mahali kusimikwa mahali pengine; na bado lilikuwa ni hema kubwa na lenye fahari na utukufu mwingi. Kuta zake zilitengenezwa kwa mbao zilizosimama wima, ambazo zilipakwa dhahabu nyingi na kuchomekwa katika

vitako vya fedha, ambapo paa lake lilitengenezwa kwa mapazia yaliyofuatana moja baada ya jingine, au vifuniko, -vya nje kabisa vikiwa vya ngozi, vya ndani kabisa vilikuwa vya kitani safi na nzuri iliyopambwa kwa michoro ya maumbo ya makerubi. Kando ya ule uwanja wa nje, uliokuwa na madhabahu ya sadaka ya kuteketezwa, hema lenyewe liliundwa na vyumba viwili vilivyoitwa Patakatifu na Patakatifu pa Patakatifu, navyoo vilikuwa vimetenganishwa kwa pazia la gharama, lenye rangi ya kuvutia na linalopendeza sana, au kitenganisho (pazia/shela); pazia lililofanana na lile lilifunga lango la kuingilia katika chumba kile cha kwanza. [GC 411.2; PK Aya ya 7]

Ndani ya mahali Patakatifu palikuwa na kinara cha taa upande wa kusini, pamoja na taa zake saba zilizoangazia hekalu mchana na usiku; upande wa kaskazini ilisimama meza ya mikate ya wonyesho; na mbele ya pazia lililotenganisha Patakatifu na Patakatifu pa Patakatifu palikuwa na madhabahu ya dhahabu ya uvumba, ambapo wingu la harufu nzuri likiwa na maombi ya Israeli lilitokea hapo na kupanda kila siku mbele za Mungu. [GC 412.1; PK Aya ya 8]

Ndani ya Patakatifu Patakatifu lilisimama Sanduku la Agano, sanduku lililotengenezwa kwa mbao za thamani kubwa lililofunikwa kwa kupakwa dhahabu, hifadhi ya mbao mbili za mawe ambazo juu yake Mungu alikuwa ameandika Sheria ya Amri Kumi (Kut. 31:18; Kum. 4:12, 13). Juu ya Sanduku la Agano, kilikuwepo Kiti cha Rehema, kilichofanyika sehemu ya kifuniko cha sanduku lile takatifu, kazi bora sana ya stadi, Makerubi Wawili wakiwa wamewekwa juu yake, mmoja mwisho huu na mwingine mwisho wa pili wa Sanduku la Agano, na wote wawili wakiwa wametengenezwa kwa dhahabu safi pekee. Katika chumba kile uwepo Wake Mungu ulidhihirishwa katika wingu la utukufu katikati ya makerubi hawa wawili (Kut. 25). [GC 412.2; PK Aya ya 9]

**Hekalu La Sulemani**

Baada ya Waebrania kuanza kuishi katika nchi ya Kanaani, hema hili liliachwa na badala yake Hekalu la Sulemani lilitumika, ambalo, japo lilikuwa jengo la kudumu na likichukua eneo kubwa zaidi, lilijengwa kwa uwiano wa vipimo vilivyofanana na vile vya hema la kukutania, nalo liliwekewa samani na mapambo ya aina ile ile. Katika muundo huu, hekalu lilidumu kuwepo - isipokuwa lilibomolewa na kusalia magofu wakati wa Danieli--mpaka wakati wa kuharibiwa kwake na Warumi mnamo mwaka wa 70 BK. (Dan. 7:26, 27; Mt. 24:15). [GC 412.3; PK Aya ya 10]

Hili ndilo hekalu-Patakatifu pekee palipopata kuwepo duniani, ambapo Biblia inatupasha sisi habari zake. Hapo ndipo palipotangazwa na Paulo kuwa Patakatifu pa agano la kwanza. Lakini, je, hivi Agano jipya halina Patakatifu?

(Patakatifu pa mapatano-old covenant, sio vitabu vile vya Agano la Kale, kati ya Mungu na Israeli – (Ebr. 8:8-13; Kut. 19:5-8). [GC 412.4; PK Aya ya 11]

Tukirudi tena katika kitabu cha Waebrania, watu watafutaji wa Ukweli waligundua kwamba uwepo wa Patakatifu pa pili au Patakatifu pa Agano Jipya palikuwa pamedokezwa katika Maneno ya Paulo yaliyokwisha kunukuliwa tayari: "Basi Agano la kwanza lilikuwa pia na maagizo ya huduma takatifu, na hekalu la kidunia." Na matumizi ya Neno hili "hata" au "pia" huashiria kwamba Paulo tayari amepataja Patakatifu hapo awali kabla ya kufika mahali hapo. Wakirudi nyuma, mwanzoni mwa sura ile iliyotangulia, Walisoma Maneno haya: "Basi, katika hayo tunayosema, Neno lililo kuu ndilo hili: Tunaye Kuhani Mkuu wa namna hii, aliyeketi mkono wa kuume wa kiti cha enzi cha Ukuu mbinguni, Mhudumu wa Patakatifu, na wa ile hema ya Kweli, ambayo Bwana aliiweka wala si mwanadamu." Waebrania 8:1, 2. [GC 413.1; PK Aya ya 12]

Hapa pamefunuliwa Patakatifu pa agano jipya. Patakatifu pa agano la kwanza paliwekwa na mwanadamu, yaani, palijengwa na Musa; lakini Patakatifu pa Agano Jipya pamejengwa na Bwana, wala sio mwanadamu. Katika Patakatifu pa dunia, makuhani wa kibinadamu waliendesha huduma zake; hapo, Kristo, Kuhani wetu Mkuu, anahudumu akiwa mkono wa kulia wa Mungu. Patakatifu pa kwanza palikuwa hapa duniani, Patakatifu papili pako mbinguni [GC 413.2; PK Aya ya 13]

Zaidi ya hayo, hema ile iliyojengwa na Musa iliungana kulingana na mfano (Pateni). Bwana alimwelekeza Mungu: "Sawasawa na haya yote nikuonyeshayo, mfano wa maskani, na mfano wa vyombo vyake vyote, ndivyo mtakavyovifanya." Na tena agizo hili lilitolewa kwake, "Nawe angalia ya kwamba uvifanye kama mfano wake, ulioonyeshwa mlimani." Kutoka 25:9, 40. Naye Paulo anasema kwamba hema ile ya kwanza ilikuwa "ndiyo mfano wa wakati huu uliopo sasa; wakati huo sadaka na dhabihu zinatolewa;" ya kwamba Patakatifu pake (vyumba vyote viwili) palikuwa "makala ya mambo yaliyo mbinguni," na ya kwamba makuhani waliotoa zawadi na kafara kulingana na sheria ilivyoagiza walitumika kama "mfano na kivuli cha mambo ya mbinguni," na ya kuwa "Kristo hakuingia katika Patakatifu palipofanyika kwa mikono, ndio mfano wa Patakatifu halisi; bali aliingia mbinguni hasa, aonekane sasa usoni pa Mungu kwa ajili yetu." Waebrania 9:9, 23; 8:5; 9:24. [GC 413.3; PK Aya ya 14]

**Mahali Pa Asilia Pakuu**

Patakatifu pa mbinguni, ambamo Yesu anahudumu kwa ajili yetu, ndipo mahali pakuu halisi,* ambapo Patakatifu palipojengwa na Musa palikuwa nakala yake (Ufu 4 na 5). Mungu aliweka Roho Wake juu ya wajenzi wa hekalu la duniani. Stadi ya sanaa iliyoonyeshwa katika ujenzi wake vilikuwa ni udhihirisho wa hekima ya Mungu. Kuta zake zilikuwa na mwonekano wa rundo la dhahabu, zikiakisi kila upande mwanga wa zile taa saba za kinara cha dhahabu. Meza ya

Mikate ya Wonyesho na Madhabahu ya kufukizia Uvumba, vilimeremeta kama dhahabu iliyosuguliwa sana. Pazia kubwa lililofanya kazi kama dari, lilikuwa limechorwa picha za malaika, kwa rangi ya bluu na ya zambarau, na nyekundu, liliongezea uzuri wa mwonekano wa mahali hapa. Na ng'ambo ya pazia la pili palikuwa na Shekina takatifu, (mng'ao mkali 1 Tim. 6:16), udhihirisho uonekanao wa utukufu wa Mungu, ambao mbele Zake hakuna aliyeweza kuingia na kuwa hai, isipokuwa kuhani mkuu peke yake. (Kut. 25:22) *(ndilo lenyewe haswa, na siyo nakala-the Great Original). [GC 414.1; PK Aya ya 15]

Utukufu usio na mfano wa hema la Patakatifu pa duniani, uliyaonyesha macho ya mwanadamu utukufu wa Hekalu la Mbinguni ambamo Kristo, Mtangulizi wetu anahudumu kwa ajili yetu mbele ya kiti cha enzi cha Mungu. Pale ndipo mahali pa kudumu pa Mfalme wa wafalme, ambapo maelfu mara elfu humtumikia, na kumi elfu mara kumi elfu husimama mbele Zake (Danieli 7:10); Hekalu lile, lililojazwa na utukufu wa kiti cha enzi cha milele, ambamo wale maserafi, walinzi wake wenye kung'aa, wanazifunika nyuso zao kwa kicho wanapomcha/wanapomwabudu Mungu na kuonyesha upendo wao, hapa ndipo lilipo jengo lenye utukufu wa juu sana ambalo linaakisiwa kwa uzuri na utukufu wake kwa uhafifu tu. Pamoja na hayo Ukweli muhimu kuhusu Patakatifu pa mbinguni na kazi kuu inayoendeshwa pale kwa ajili ya ukombozi wa mwanadamu vilifundishwa kupitia Patakatifu pa duniani pamoja na huduma zake. [GC 414.2; PK Aya ya 16]

Sehemu mbili za Patakatifu pa kule mbinguni zimewakilishwa na vyumba viwili katika Patakatifu pa duniani. Wakati Mtume Yohana, alipopewa fursa ya kuona Hekalu la Mungu lililoko mbinguni, akiwa katika maono, aliona pale "taa saba za moto zikiwaka mbele ya kile kiti cha enzi." Ufunuo 4:5. Alimwona malaika "mwenye chetezo cha dhahabu, na akapewa uvumba mwingi, ili autie pamoja na maombi ya watakatifu wote juu ya madhabahu ya dhahabu, iliyo mbele ya kiti cha enzi." Ufunuo 8:3. Hapa ndipo nabii aliruhusiwa kukiona chumba cha kwanza cha Patakatifu mbinguni; naye aliona mle "taa saba za moto" na "madhabahu ya dhahabu," vilivyowakilishwa na "kinara cha taa saba cha dhahabu" na madhabahu ya dhahabu ya kufukizia uvumba katika Patakatifu pa duniani. Tena, "Hekalu la Mungu (lililoko mbinguni) likafunguliwa" (Ufunuo 11:19), kisha akaangalia ndani ya pazia la ndani, yaani, Patakatifu pa Patakatifu. Hapa aliona "Sanduku la Agano Lake," lililowakilishwa na Sanduku takatifu ambalo lilitengenezwa na Musa ili kuihifadhi ndani yake Sheria ya Mungu (Amri Kumi). [GC 414.3; PK Aya ya 17]

Hivyo ndivyo wale waliokuwa wanalichunguza na kujifunza somo hili walivyopata uthibithisho usiopingika wa uwepo wa Patakatifu pa mbinguni. Musa alijenga Patakatifu pa duniani kwa mfano ule alioonyeshwa. Paulo anafundisha

kuwa mfano ule ulikuwa Patakatifu halisi pa mbinguni. Naye Yohana anashuhudia kwamba aliliona kule mbinguni. [GC 415.1; PK Aya ya 18]

Ndani ya hekalu la mbinguni, makazi ya Mungu, Kiti chake cha Enzi kimeimarishwa katika haki na hukumu. Ndani ya Patakatifu Pa patakatifu iko Sheria Yake, mwongozo mkuu wa haki, ambao kwa huo wanadamu wote wanapaswa kupimwa. Sanduku la Agano linalozihifadhi kwa usalama sana mbao mbili za Sheria (Amri Kumi) limefunikwa na Kiti cha Rehema, ambacho mbele yake Kristo anasihi kwa njia ya damu Yake kwa niaba ya mwenye dhambi (anafanya maombezi na kumtetea mwanadamu). Kwa njia hiyo umewakilishwa muungano wa haki (Amri Kumi) na rehema (msamaha) katika mpango wa ukombozi wa mwanadamu. Muungano huo ni hekima ya Mungu isiyo na kikomo ndiyo imeweza kubuni, na nguvu isiyokuwa na kikomo pekee ndiyo ingeweza kuutekeleza; ni muungano unaoijaza mbingu yote na mshangao, na kumwabudu Mungu na kumpenda. Makerubi wa Patakatifu pa duniani, kwa kukiangala kiti cha rehema kwa kicho, huwakilisha shauku kubwa ambayo jeshi la mbinguni huwa nayo wanapoitafakari kazi ya ukombozi. Hiyo ndiyo siri na fumbo la rehema ambalo malaika wanatamani kulichungulia (wanatamani waielewe siri na kitendawili hicho) - kwamba Mungu anaweza kuwa Mwenye haki na wakati huo huo amhesabie haki mwenye dhambi anayetubu na kurejesha upya mahusiano/mawasiliano Yake na wanadamu walioanguka dhambini; kwamba Kristo aliweza kujishusha na kuinama chini sana ili kuwainua watu wasio na idadi kutoka katika shimo refu la uharibifu na kuwavika mavazi yasiyo na doa ya haki Yake Mwenyewe ili apate kuwaunganisha na malaika ambao hawakuwahi kuanguka dhambini kamwe na kuishi daima mbele za Mungu. [GC 415.2; PK Aya ya 19]

**Unabii Mzuri Sana**

Kazi Yake Kristo kama Mwombezi wa mwanadamu imewasilishwa katika ule unabii mzuri sana wa Zekaria unaomhusu Kristo, Yeye ambaye “Jina Lake ni Chipukizi.” Asema hivi huyo nabii: “Naam, Yeye atalijenga hekalu la Bwana; Naye atauchukua huo utukufu; ataketi akimiliki katika kiti cha enzi; na kutakuwa na kuhani katika kiti Chake cha enzi; na shauri la amani litakuwa kati ya hao wawili.” Zekaria 6:12,13. [GC 415.3; PK Aya ya 20]

“Yeye atalijenga hekalu la BWANA.” Kwa kafara (dhabihu) Yake na upatanishi Wake, Kristo Ndiye msingi, tena Ndiye mjenzi wa kanisa la Mungu. Mtume Paulo anamsonda Yeye kidole akimwelezea kuwa Ndiye “Jiwe kuu la Pembeni, katika Yeye jengo lote linaungamanishwa vema na kukua hata liwe hekalu takatifu katika Bwana. Katika Yeye ninyi nanyi,” anasema, “mnajengwa pamoja kuwa maskani ya Mungu katika Roho.” Waefeso 2:20-22. [GC 416.1; PK Aya ya 21]

“Naye atauchukua huo utukufu.” Kwake Kristo kuna utukufu wa ukombozi kwa ajili ya jamii ya wanadamu iliyoanguka dhambini. Katika zama zote za milele, wimbo wa wale walionunuliwa utakuwa ni huu: “Yeye atupendaye na kutuosha dhambi zetu katika damu Yake…….utukufu na ukuu una Yeye hata milele na milele. Amina." Ufunuo 1:5, 6. [GC 416.2; PK Aya ya 22]

Yeye “ataketi na kutawala juu ya kiti Chake cha enzi; Naye atakuwa kuhani katika kiti Chake cha enzi.” (Zekaria 6:13). Kwa sasa hajaketi “juu ya kiti Chake cha enzi cha utukufu Wake;” maana ufalme wa utukufu bado haujawaidia. Ni Mpaka kazi Yake kama Mpatanishi itakapofikia mwisho, ndipo Mungu atampa “kiti cha enzi cha Daudi, baba Yake,” yaani, ufalme ule ambao utakuwa “hauna mwisho,” Luka 1:32, 33. Kama kuhani, Kristo sasa ameketi pamoja na Baba Yake katika kiti Chake cha enzi. Ufunuo 3:21 Juu ya kiti cha enzi na Yule ambaye ni wa milele, Aliye na uwepo Wake Mwenyewe (hakuumbwa), ni Yeye aliyekuwako milele, Ndiye ambaye “ameyachukua masikitiko yetu, amejitwika huzuni zetu,” ambaye “alijaribiwa sawasawa na sisi katika mambo yote, kama tujaribiwavyo, lakini hakutenda dhambi,” ili “aweze kuwasaidia wao wanaojaribiwa.” “Na kama mtu akitenda dhambi tunaye Mwombezi kwa Baba,” Isaya 53:4; Waebrania 4:15; 2:18; 1 Yohana 2:1. Maombezi Yake ni yale ya mwili Wake uliochomwa mikuki, na kutobolewa, na kuvunjika, ya maisha Yake yasiyokuwa na doa. Viganja Vyake vilivyochubuliwa, ubavu Wake uliochomwa na mkuki, nyayo zake zilizoharibiwa-haribiwa, husihi kwa ajili ya mwanadamu aliyeanguka dhambini, ambaye ukombozi Wake ulinunuliwa kwa gharama ya thamani kubwa mno isiyokadirika (1 Pet. 1:18,19). [GC 416.3; PK Aya ya 23]

"Na shauri/ Agano la amani litakuwa kati ya hao wawili." Upendo wa Baba, kadhalika haukuwa pungufu kuliko ule wa Mwanawe, huo umekuwa ni msingi wa wokovu wa jamii ya wanadamu waliopotea. Yesu aliwaambia wanafunzi Wake hivi kabla hajaenda Zake: “Siwaambii ya kwamba Mimi nitawaombea kwa Baba; kwa maana Baba Mwenyewe awapenda ninyi.” Yohana 16:26, 27. Mungu alikuwa “ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu na nafsi Yake.” 2 Wakorintho 5:19. Na katika huduma inayoendelea katika Patakatifu pale pa juu mbinguni, “Shauri la amani li kati ya hao wawili.” “Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee (asiangamie), bali awe na uzima wa milele.”Yohana 3:16. [GC 416.4; PK Aya ya 24]

**Siri Ya Patakatifu Yafumbuliwa**

Swali, Patakatifu ni nini? limejibiwa kikamilifu katika Maandiko bila kuacha shaka lolote. Neno hili “Patakatifu,” kama lilivyotumika katika Biblia, hurejelea, kwanza kabisa, kuhusu lile hema lililojengwa na Musa, kama mfano wa mambo yale ya mbinguni; na, pili, linahusu “Patakatifu halisi au hema la kweli” kule mbinguni, ambalo Patakatifu pa duniani palikuwa panaelekeza au panawakilisha.

Wakati wa kifo Chake Kristo huduma ya kivuli au mfano ilikoma (2:14-17). “Patakatifu halisi au hema la Kweli” la mbinguni ndipo Patakatifu pa agano jipya. Na kwa vile unabii wa Danieli 8:14 umetimizwa katika dhana hii katika kipindi hiki, basi, Patakatifu panapotajwa hapa, hapana budi kuwa ni pale pa agano jipya (new Covenant). Mwishoni mwa siku 2300, mnamo 1844, Patakatifu pa duniani hapakuweko kwa karne nyingi. Kwahiyo unabii huo wa “Hata nyakati za jioni na asubuhi elfu mbili na mia tatu; ndipo Patakatifu patakapotakaswa,” unahusu Patakatifu pa mbinguni bila kuwa na swali lolote. [GC 417.1; PK Aya ya 25]

Lakini swali la muhimu kuliko yote ambalo bado halijajibiwa ni hili: Kutakaswa kwa Patakatifu maana yake ni nini? Kwamba palikuwapo na huduma kama hiyo kuhusiana na Patakatifu pa kidunia inaelezwa katika Maandiko ya Agano la Kale. Lakini je, kunaweza kuwepo na kitu chochote cha kutakaswa mbinguni? Katika Waebrania 9 kutakaswa kwa Patakatifu pote pawili, yaani, pa duniani na pa mbinguni, kumefundishwa kwa uwazi kabisa. “Na katika torati karibu vitu vyote husafishwa kwa damu, na pasipo kumwaga damu hakuna ondoleo. Basi ilikuwa sharti nakala za mambo yaliyo mbinguni zisafishwe kwa hizo, lakini mambo ya mbinguni yenyewe yasafishwe kwa dhabihu zilizo bora kuliko hizo” Waebrania 9:22, ambayo ni damu ya thamani ya Kristo. [GC 417.2; PK Aya ya 26]

**Kutakaswa Pa Patakatifu**

Utakaso, katika huduma zote mbili, ya mfano au kivuli na ile halisi (original), ni sharti ufanyike kwa damu: katika huduma ya awali, kwa damu ya wanyama; katika huduma ya pili, kwa damu Yake Kristo. Paulo anaeleza sababu kwa nini utakaso ni lazima utekelezwe kwa damu ya Kristo, ni kuwa pasipo kumwaga damu hakuna ondoleo la dhambi. Ondoleo la dhambi, au kuziweka mbali dhambi, hiyo ndiyo kazi hasa inayopasa kutekelezwa. Lakini ni kwa jinsi gani dhambi hiyo imeshikamana na Patakatifu pa mbinguni au pa duniani? Jambo hili tunaweza kulielewa kwa kujifunza au kuchunguza huduma ya mfano; kwa maana makuhani waliohudumu duniani, walihudumu kulingana na“mfano na kivuli cha mambo ya mbinguni.” Waebrania 8:5. [GC 417.3; PK Aya ya 27]

Huduma ya Patakatifu pa duniani iligawanyika katika sehemu mbili; makuhani walihudumu kila siku katika mahali Patakatifu, wakati ambapo mara moja kwa mwaka kuhani mkuu alifanya kazi ya pekee ya upatanisho katika Patakatifu pa Patakatifu, kwa ajili ya kutakasa Patakatifu. Siku kwa siku mwenye dhambi alileta sadaka yake penye mlango wa hema, na kwa kuweka mkono wake juu ya kichwa cha mnyama wa sadaka, naye aliziungama dhambi zake, kwa njia hiyo ya mfano, yaani kielelezo, akizihamisha dhambi zake kutoka nafsi yake mwenyewe na kuziweka kwenye kafara asiyekuwa na hatia. Kisha mnyama huyo alichinjwa.

“Na pasipo kumwaga damu,” asema mtume, “hakuna ondoleo la dhambi.” “kwa kuwa uhai wa mwili u katika hiyo damu.” Mambo ya Walawi 17:11. Sheria ya Mungu iliyovunjwa ilidai uhai wa yule mvunjaji wa Sheria uondolewe (Amri Kumi). Damu iliwakilisha uhai ulionyang’anywa wa mwenye dhambi, ambaye hatia yake ilibebeshwa mnyama wa kafara, ilichukuliwa na kuhani mpaka pale Patakatifu naye alinyumiza mbele ya pazia, ambalo nyuma yake lilikuwako Sanduku la Agano lililohifadhi Sheria (Amri Kumi) ndani yake ambayo yule mwenye dhambi alikuwa ameivunja. Kwa sherehe hii, dhambi, kwa njia ya damu, ilihamishwa hadi Patakatifu kwa mfano. Katika kesi fulani fulani damu hiyo haikupelekwa ndani ya Patakatifu; lakini badala yake nyama yake ilipaswa kuliwa na kuhani, kama Musa alivyowaagiza wana wa Haruni, akasema: “Naye Mungu amewapa ninyi ili kuuchukua uovu wa mkutano.” Mambo ya Walawi 10:17. Huduma zote mbili za ibada ya kafara kwa namna ile ile moja ziliashira kuhamishwa kwa dhambi kutoka kwa mwenye dhambi aliyetubu na kuiingiza Patakatifu. [GC 418.1; PK Aya ya 28]

Hiyo ndiyo kazi iliyoendelea, siku kwa siku katika mwaka mzima. Hivyo ndivyo dhambi za Israeli zilivyohamishiwa kutoka kwao kwa njia hiyo na kuingizwa ndani ya Patakatifu, na kazi ya pekee ilikuwa lazima ifanywe ili kuziondoa mbali. Mungu aliagiza kwamba upatanisho ufanywe kwa ajili ya kila kimoja cha vyumba vile vitakatifu. “Naye atafanya upatanisho kwa ajili ya mahali Patakatifu, kwa sababu ya mambo machafu ya wana wa Israeli, na kwa sababu ya makosa yao, naam, kwa ajili ya dhambi zao zote; naye atafanya vile vile kwa ajili ya hema ya kukutania, ikaayo pamoja nao katikati ya machafu yao.” Upatanisho ulipaswa kufanywa pia kwa ajili ya madhabahu, “kuitakasa, ili machafu yote ya wana wa Israeli yaitoke.” Mambo ya Walawi 16:16, 19. [GC 418.2; PK Aya ya 29]

**Mara Moja Kwa Mwaka**

Mara moja kwa mwaka, katika Siku Kuu ya Upatanisho, kuhani (mkuu) aliingia Patakatifu pa Patakatifu kwa ajili ya kupatakasa Patakatifu. Kazi iliyofanyika mle ilikamilisha mzunguko ya huduma wa mwaka mzima wa huduma. Katika siku ya Upatanisho wana-mbuzi wawili waliletwa kwenye mlango wa hema, kisha kura zilipigwa juu yao, “kura moja kwa ajili ya BWANA; na kura ya pili kwa ajili ya Azazeli (Shetani).” Kifungu cha 8. Mbuzi yule aliyeangukiwa na kura kwa ajili ya Bwana alichinjwa kama sadaka ya dhambi kwa ajili ya watu wote. Kisha yule kuhani alitakiwa kuichukua damu yake mpaka ndani ya pazia na kuinyunyiza juu ya Kiti cha Rehema na mbele ya Kiti cha Rehema. Damu ile pia ilipaswa kunyunyizwa juu ya Madhabahu ya kufukizia Uvumba iliyokuwa mbele ya pazia. [GC 419.1; PK Aya ya 30]

“Na Haruni ataweka mikono yake miwili juu ya kichwa cha yule mbuzi aliye hai, na kuungama juu yake uovu wote wa wana wa Israeli, na makosa yao, naam,

dhambi zao zote; naye ataziweka juu ya kichwa chake yule mbuzi, kisha atampeleka aende jangwani kwa mkono wa mtu aliye tayari. Na yule mbuzi atachukua juu yake uovu wao wote, mpaka nchi isiyo na watu; naye atamwacha mbuzi jangwani.” Kifungu cha 21, 22. Mbuzi yule wa Azazeli hakuweza kurudi tena katika kambi ya Israeli, na mtu yule aliyempeleka kule mbali alitakiwa kuoga yeye mwenyewe na kuzifua nguo zake kwa maji kabla ya kurudi kambini. [GC 419.2; PK Aya ya 31]

**Mafundisho Makuu Yafundishwa**

Sherehe yote ya ibada ya kafara ilikusudiwa kuwapa Waisraeli picha ya utakatifu wa Mungu na chuki kubwa aliyo nayo dhidi ya dhambi; na, zaidi ya hayo, kuwaonyesha kwamba wasingeweza kugusana na dhambi bila kunajisika. Kila mtu alitakiwa kujitesa nafsi yake wakati kazi ya upatanisho ilipokuwa ikiendelea. Shuguli zote zilipaswa kuwekwa kando, na kutano lote la Israeli lilipaswa kuitumia siku ile nzima kwa unyenyekevu mwingi na kicho mbele za Mungu, kwa maombi, kufunga, na kujichunguza sana moyoni. [GC 419.3; PK Aya ya 32]

Ukweli muhimu kuhusu upatanisho ulifundishwa kupitia huduma hiyo ya mifano au vivuli. Kafara ilikubaliwa mbadala wa mwenye dhambi- kuchukua mahali pa mwenye dhambi; lakini dhambi yake haikufutwa kwa njia ya damu ya yule mnyama (dhabihu). Kwa ajili hiyo, njia iliwekwa ambayo kwayo dhambi ilihamishiwa ndani ya Patakatifu. Kwa njia ya sadaka ya damu, mwenye dhambi alikiri kwamba Sheria (Amri Kumi) ilikuwa na mamlaka juu yake, alikiri hatia yake ya kuivunja Sheria na kuonyesha shauku yake ya kupata msamaha kwa njia ya imani kwa Mkombozi Yule ajaye; lakini alikuwa bado hajawekwa huru kutokana na hukumu ya Sheria. Katika Siku ya Upatanisho kuhani mkuu, baada ya kupokea sadaka kutoka katika ule mkutano, aliingia Patakatifu pa Patakatifu akiwa na damu ya sadaka hii, kisha aliinyunyiza juu ya Kiti cha Rehema, yaani, juu kabisa ya Sheria ile (juu ya mbao za Amri Kumi), ili kuridhisha madai yake, kisha kwa mujibu w cheo chake kama mpatanishi, alizichukua dhambi zile mwilini mwake mwenyewe na kuziondoa nje ya Patakatifu. Akiwa ameiweka mikono yake juu ya kichwa cha mbuzi wa Azazeli, aliziungama dhambi zote juu yake, hivyo kwa mfano alizihamisha kutoka kwake na kuziweka juu ya yule mbuzi. Kisha mbuzi huyu alizibeba na kuondoka nazo mbali, nazo zilichukuliwa kuwa zilikuwa zimetenganishwambali na watu milele. [GC 420.1; PK Aya ya 33]

Hii ndiyo huduma iliyofanywa “kwa mfano na kivuli cha mambo ya mbinguni” Na kile kilichofanywa kama mfano katika huduma ya Patakatifu pa duniani kinafanywa katika uhalisia wake katika huduma ya Patakatifu pa mbinguni. Baada ya kupaa Kwake, Mwokozi wetu alianza kazi Yake kama Kuhani Mkuu (Ebr.

9:11,12). Asema hivi Paulo: “Kwa sababu Kristo hakuingia katika Patakatifu palipofanyika kwa mikono, ndio mfano wa Patakatifu halisi; bali aliingia mbinguni hasa, aonekane sasa usoni pa Mungu kwa ajili yetu.” Waebrania 9:24. [GC 420.2; PK Aya ya 34]

Huduma ya kuhani ya mwaka mzima katika chumba cha kwanza cha Patakatifu, “ndani ya pazia” ambalo lilikuwa ndio mlango uliotenganisha Patakatifu na uwanja wa nje, huwakilisha kazi ya huduma aliyoianza Kristo mara tu baada ya kupaa Kwake (Ebr. 9:11,12). Ilikuwa ni kazi ya kuhani mkuu katika huduma Yake ya kila siku kuwakilisha damu ya sadaka ya dhambi mbele za Mungu, kadhalika alifukiza uvumba uliopanda juu pamoja na maombi ya Israeli. Hivyo ndivyo Kristo alivyotumia damu Yake kumsihi Baba Yake kwa ajili ya wenye dhambi, na pia kuwasilisha mbele Zake maombi ya wenye dhambi waliotubu yaliyochanganywa pamoja na harufu nzuri na ya thamani ya haki Yake Mwenyewe. Hiyo ndiyo kazi ya huduma iliyofanyika katika chumba kile cha kwanza cha Patakatifu pa mbinguni. [GC 420.3; PK Aya ya 35]

Pale ndiko imani ya wanafunzi Wake Kristo ilikomfuata alipopaa kutoka machoni pao. Hapa ndiko matumaini yao yaliwekwa, “matumaini... tuliyo nayo,” alisema Paulo, “kama nanga ya roho, yenye salama, yenye nguvu, yaingiayo hata mle mlimo ndani ya pazia, alimoingia Yesu kwa ajili yetu, Mtangulizi wetu, amekuwa Kuhani Mkuu hata milele.” “Wala si kwa damu ya mbuzi na ndama, bali kwa damu Yake Mwenyewe aliingia mara moja tu katika Patakatifu, akiisha kupata ukombozi milele.” Waebrania 6:19, 20; 9:12. [GC 421.1; PK Aya ya 36]

Kwa karne kumi na nane (tangu mwaka 31BK hadi mwaka 1844) kazi hiyo ya huduma iliendelea katika chumba cha kwanza cha Patakatifu. Damu ya Kristo iliwaombea waumini waliotubu kwa kusihi, na kuwapatia msamaha na kukubaliwa mbele za Baba, lakini dhambi zao zilikuwa bado zimebaki katika vitabu vya kumbukumbu. Kama ilivyokuwa katika huduma ya mfano palikuwa na kazi ya upatanisho ya kufanya mwishoni mwa mwaka, hivyo kabla ya kazi ya Kristo ya ukombozi haijakamilika, kuna kazi ya upatanisho ya kufanywa kwa ajili ya kuondolewa mbali kwa dhambi ndani ya Patakatifu. Hii ndiyo huduma ambayo ilianza wakati siku 2300 zilipoisha. Wakati huo, kama ilivyotabiriwa na nabii Danieli, Kuhani wetu Mkuu aliingia Patakatifu pa Patakatifu, kufanya sehemu ya mwisho ya kazi Yake kuu takatifu - yaani, kupatakasa Patakatifu. [GC 421.2; PK Aya ya 37]

Kama ilivyokuwa zamani, ambapo dhambi za watu zilivyowekwa kwa imani juu ya dhabihu ya mnyama wa sadaka ya dhambi na kwa njia ya damu Yake, dhambi zilihamishwa kwa mfano ndani ya Patakatifu pa kidunia, hivyo katika agano jipya dhambi za wale wanaotubu huwekwa kwa imani juu ya Kristo na kuhamishwa kiuhalisia kwenda ndani ya Patakatifu, naam, pa madhabahu ya mbinguni. Na kama utakaso wa mfano wa Patakatifu pa duniani ulivyotekelezwa

kwa kuziondoa dhambi ambazo zilikuwa zimepachafua au kupatia unajisi, kadhalika utakaso halisi wa Patakatifu pa mbinguni utatekelezwa kwa kuondoa, au kufuta, dhambi zilizorekodiwa mle. Lakini kabla ya jambo hilo kufanyika, ni lazima pawepo na uchunguzi wa vitabu vya kumbukumbu ili kuamua ni akina nani kwa njia ya toba ya dhambi zao na imani ndani ya Kristo, wanayo haki ya kupewa mafao ya upatanisho Wake. Hivyo utakaso wa Patakatifu unahusisha kazi ya upelelezi - kazi ya hukumu. Kazi hii lazima ifanyike kabla ya ujio Wake Kristo kuwakomboa watu Wake; kwa maana atakapokuja ujira wake utakuwa pamoja Naye mkononi ili kumlipa kila mtu kwa kadiri ya matendo yake. Ufunuo 22:12. [GC 421.3; PK Aya ya 38]

Hivyo wale walioifuata nuru ya Neno lile la unabii waligundua kwamba badala ya Yeye Kristo kuja duniani mwishoni mwa zile siku 2300 katika mwaka ule wa 1844, Kristo aliingia wakati huu ndani ya Patakatifu pa Patakatifu pa hekalu mbinguni ili kufanya kazi Yake ya mwisho ya upatanisho na kujiandaa kwa ajili ya ujio Wake wa pili duniani. [GC 422.1; PK Aya ya 39]

Pia ilionekana kuwa wakati sadaka ya dhambi, yaani mbuzi yule wa Bwana, alimwakilisha Kristo kama Kafara yetu, na kuhani mkuu pia alimwakilisha Kristo kama Mpatanishi wetu, mbuzi wa Azazeli alikuwa mfano wa Shetani, mwasisi wa dhambi, ambaye juu yake dhambi za wale waliotubu kikamilifu zitawekwa hatimaye. Wakati kuhani mkuu, kwa njia ya damu ya sadaka ya dhambi, alipoondoa dhambi kutoka ndani ya hekalu, aliziweka juu ya mbuzi wa Azazeli, ambaye, katika utekelezaji wa hukumu, atapaswa kuibeba ile adhabu. Wakati Kristo, kwa nguvu ya damu Yake Mwenyewe, atakapoziondoa dhambi za watu Wake kutoka ndani ya hekalu la mbinguni mwishoni mwa huduma Yake, ataziweka juu ya Shetani, ambaye, katika utekelezaji wa hukumu, atawajibika kwa ajili ya adhabu ya mwisho kabisa. Mbuzi wa Azazeli alipelekwa mbali katika nchi isiyokaliwa na watu, ili asiweze kamwe kurudi tena katika kutano la wana wa Israeli. Kadhalika Shetani atakafukuzwa milele atoke mbele Zake Mungu, na mbele ya watu Wake, na asionekane tena, atafutiliwa mbali asiwepo kabisa tena katika uangamizaji wa mwisho utakaofanywa dhidi ya dhambi na wenye dhambi (Mal. 4:1-3; Eze. 28:11-19) [GC 422.2; PK Aya ya 40]

# SURA YA 24

# NDANI YA PATAKATIFU PA PATAKATIFU

## (Yesu Kristo Mwombezi Wetu Mbele Za Mungu)

Ufupisho: Somo la Patakatifu ni ufunguo unaofungua Kweli nyingi za Biblia ambazo zimekuwa zikieleweka kidogo. Somo la Patakatifu pa Biblia lilifunua mbele ya macho yao mfumo kamili wa Ukweli ambao ulikuwa umeshikama pamoja, na kuafikiana.

Somo la Patakatifu lilikuwa ufunguo uliofungua fumbo na siri ya kukatishwa tamaa, mnamo mwaka 1844. Ufunguo huu ulifungua mbele ya macho yao mfumo kamili wa Ukweli ambao ulikuwa umeshikama pamoja, na kuafikiana, ukionyesha kwamba mkono wa Mungu ulikuwa umeiongoza vuguvugu hii kuu ya Marejeo (Waadventista) na kuwafunulia wajibu wa sasa, yaani waliowapasa kufanya kwa wakati wao, kwa kuonyesha nafasi na kazi ya watu Wake. Kama vile wanafunzi wa Yesu, baada ya usiku wa huzuni ya kutisha uliojaa uchungu na kukatishwa tamaa, "walivyofurahi walipomwona Bwana," ndivyo wale waliokuwa wamemtazamia kwa imani kurudi Kwake mara ya pili walivyofurahi sasa. Walikuwa wamemtarajia atonekane katika utukufu ili atoe ujira kwa watumishi Wake. Matumaini yao yalipokatishwa tamaa, walishindwa kumwona Yesu, ndipo, kama Mariamu kaburini, walilia wakisema: "Wamemwondoa Bwana wangu, wala mimi sijui walikomweka." Sasa akiwa ndani ya Patakatifu pa Patakatifu waliweza kumwona tena, Kuhani wao Mkuu Mwenye huruma, ambaye hivi karibuni atatokea kama Mfalme na Mkombozi wao. Nuru kutoka katika hekalu iliangaizia wakati uliopita, wakati wa sasa na wakati wa ujao. Walielewa fika kwamba ni Mungu Ndiye aliyekuwa amewaongoza kwa hekima Yake isiyokosea kamwe. Ingawa wao wenyewe, kama ilivyokuwa kwa wanafunzi Wake wa kwanza na wao wenyewe, walikuwa wameshindwa kuuelewa ujumbe ule waliokuwa wameubeba na kuuhubiri, japokuwa ujumbe huu ulikuwa sahihi katika kila kipengele. Katika kuutangaza walikuwa wamelitimiza kusudi la Mungu, na kazi yao waliyofanya haikuwa bure katika Bwana. Wakiwa wamezaliwa "mara ya pili tena katika

tumaini hai," walifurahi sana "kwa furaha isiyoelezeka, yenye utukufu mwingi." [GC 423.1; PK Aya ya 1]

Unabii wa Danieli 8:14, usemao, "Hata nyakati za jioni na asubuhi elfu mbili na mia tatu; ndipo Patakatifu patakapotakaswa," pamoja na Ujumbe wa Malaika wa Kwanza, usemao, "Mcheni Mungu, na kumtukuza, kwa maana saa ya hukumu Yake imekuja," vyote viwili vilielekeza kidole chake kwenye huduma ya Kristo ndani ya Patakatifu pa Patakatifu (Patakatifu sana), yaani, kwenye ile Hukumu ya Upelelezi, na wala sio kwenye marejeo ya Kristo kuja kuwakomboa watu Wake na kuwaangamiza waovu. Kosa halikuwa katika ukokotoaji wa vipindi vya kiunabii, bali lilikuwa katika tukio ambalo lingetokea mwishoni mwa siku 2300. Kwa njia ya kosa hili, waaminio walipata huzuni kwa kukatishwa tamaa, lakini yote yale yaliyotabiriwa katika unabii huu, na yote yale waliyokuwa wanayatarajia ambayo yalikuwa na ushahidi wa Maandiko, yalikuwa yametimia. Wakati ule ule walipokuwa wakiomboleza kwa kupoteza matumaini yao, tukio lilikuwa limetokea, ambalo lilikuwa limetabiriwa katika ujumbe huo, na ambalo lilikuwa ni lazima litimizwe kabla Bwana hajarudi mawinguni, kuja kutoa thawabu watumishi Wake. [GC 424.1; PK Aya ya 2]

Kristo alikuwa amekuja, sio duniani kama wao walivyotarajia, bali Patakatifu pa Patakatifu katika Hekalu la Mungu lililoko mbinguni, kama ilivyokuwa imeonyeshwa mapema katika kivuli chake. Nabii Danieli amemwakilisha Yeye kama Yule anayekuja wakati huu kwa Mzee wa Siku: "Nikaona katika njozi za usiku, na tazama, Mmoja aliye mfano wa mwanadamu akaja pamoja na mawingu ya mbingu"- huko siko kuja duniani, bali kuja kwa - "huyo Mzee wa Siku (Baba), wakamleta karibu Naye." Danieli 7:13. [GC 424.2; PK Aya ya 3]

Ujio Wake huo pia umetabiriwa na nabii Malaki: "Naye Bwana mnayemtafuta atalijilia Hekalu Lake ghafula; naam, Yule Mjumbe wa Agano mnayemfurahia, angalieni, anakuja, asema BWANA wa majeshi." Malaki 3:1. Kuingia Kwake Bwana kwenye hekalu Lake kulikuwa kwa ghafla, kusiko kwa kutarajiwa na watu Wake. Hawa walikuwa hawamtarajii kwenda pale. Walimtazamia aje duniani, "katika mwali wa moto; huku akiwalipiza kisasi wao wasiomjua Mungu, na wao wasioitii Injili." 2 Wathesalonike 1:8. [GC 424.3; PK Aya ya 4]

**Kazi Ya Kujiweka Tayari Ni Ya Lazima**

Lakini watu walikuwa bado hawajawa tayari kumpokea Bwana wao. Bado kulikuwa na kazi maandalizi yaliyopaswa kukamilishwa ndani yao. Nuru ilipaswa kutolewa (tena Ufu. 10:8-11; 11:1), ikiyaelekeza mawazo yao kwenye Hekalu la Mungu lililoko mbinguni; na wakati wakimfuata kwa imani Kuhani wao Mkuu katika huduma Yake pale, basi, majukumu mapya yangefunuliwa kwao. Ujumbe mwingine wa onyo na mafundisho ulipaswa kutolewa kwa kanisa. [GC 424.4; PK Aya ya 5]

Nabii anasema: “Lakini ni nani atakayestahimili siku ya kuja Kwake? Au ni nani atakayesimama atakapoonekana Yeye? Kwa maana Yeye ni mfano wa moto wa mtu asafishaye fedha na kuitakasa, Naye atawatakasa wana wa Lawi atawasafisha kama dhahabu na fedha; nao watamtolea BWANA dhabihu katika haki.” Malaki 3:2,3. Wale watakaoendelea kuishi duniani wakati maombezi ya Kristo katika Patakatifu yatakuwa yamekoma katika hekalu la mbinguni, watasimama mbele za macho ya Mungu Mtakatifu bila kuwa na Mpatanishi/Mwombezi. Mavazi yao yanapaswa yasiwe na doa, tabia zao ni lazima zisafishwe kutokana na dhambi kwa njia ya kunyunyiziwa damu ya Kristo (Law. 16:15,16; Ebr. 9:12-15). Kwa njia ya neema Yake Mungu na juhudi zao binafsi zilizo thabiti, inawapasa wawe washindi katika vita yao dhidi ya uovu (Ufu. 21:7,8). Wakati wa hukumu ya Upelelezi ikiendelea kule mbinguni, wakati dhambi za waaminio wanaotubu zikiondolewa toka hekaluni, ni lazima iwepo kazi maalumu ya utakaso, kazi ya kuziweka mbali dhambi miongoni mwa watu wa Mungu walio juu ya uso wa dunia hii. Kazi hii imewasilishwa kwa uwazi zaidi katika ujumbe wa Ufunuo 14 (wa malaika watatu). [GC 425.1; PK Aya ya 6]

Wakati kazi hiyo itakapokuwa imekamilika, wafuasi wa Kristo watakuwa tayari kwa ajili ya ujio Wake wa pili. “Wakati ule ndipo dhabihu za Yuda na Yerusalemu zitakapopendeza mbele za BWANA, kama katika siku za kale, na kama katika miaka ya zamani.” Malaki 3:4. Hilo ndilo kanisa ambalo wakati wa kuja Kwake Bwana litakuwa ni “Kanisa tukufu, lisilo na hila wala kunyanzi, wala lolote kama hayo.” Waefeso 5:27. Ndipo litaonekana “kama alfajiri, zuri kama mwezi, safi kama jua, wa kutisha kama wenye (jeshi) bendera.” Wimbo Ulio Bora 6:10. [GC 425.2; PK Aya ya 7]

Pamoja na kule kuja Kwake Bwana katika Hekalu Lake, Malaki pia kwa Maneno hayo, anatabiri pia kuja Kwake kwa mara ya pili, kwa ajili ya kutekeleza hukumu: “Nami nitawakaribieni ili kuhukumu; Nami sitasita kutoa ushahidi juu ya wachawi; na juu ya wazinzi, na juu ya waapao kwa uongo; juu ya wamwoneao mwajiriwa, kwa ajili ya mshahara wake, wamwoneao mjane na yatima, na kumpotosha mgeni asipate haki yake, wala hawaniogopi Mimi, asema Bwana wa majeshi.” Malaki 3:5. Yuda anarejelea tukio lile lile anaposema, “Angalia, Bwana Yuaja pamoja na watakatifu Wake maelfu kwa maelfu (Malaika), ili afanye hukumu juu ya watu wote, na kuwaadhibu wote wasiomcha Mungu kati yao kwa ajili ya kazi zao zote za upotevu.” Yuda 14, 15. Ujio huu wa kuja kwa Bwana ndani ya hekalu Lake, ni matukio mawili tofauti kabisa, hayo siyo kitu kimoja, yametenganishwa. [GC 425.3; PK Aya ya 8]

Kuja kwa Kristo kama Kuhani wetu Mkuu katika Patakatifu pa Patakatifu, kwa ajili ya utakas0 wa hekalu kunakotajwa katika Danieli 8:14; na kuja kwa Mwana wa Adamu kwa Mzee wa Siku kama inavyoonyeshwa katika Danieli 7:13; na

kuingia kwa Bwana ndani ya hekalu Lake kulikotabiriwa na Malaki, ni maelezo ya tukio lile lile moja; tena tukio hilo limewakilishwa pia na ujio wa Bwana Arusi kwenye harusi kulikoelezwa na Kristo katika mfano wa wanawali kumi wa Mathayo 25. [GC 426.1; PK Aya ya 9]

Katika majira ya joto (Summer-Juni-Agosti) na ya kupukutisha majani (Septemba-Novemba) ya mwaka wa 1844, tangazo, "Haya Bwana Arusi Yuaja," lilitolewa. Makundi hayo mawili yanayowakilishwa na wanawali wenye hekima na wapumbavu yalikuwa yamejitokeza wakati ule -- kundi la kwanza, ambalo lilitazamia kwa furaha nyingi ujio wake Bwana, nalo lilikuwa likijiandaa kwa bidii kukutana Naye; na kundi jingine ambalo lilikuwa linashawishiwa kwa hofu na kutenda kwa mihemko bila kufikiri, lilikuwa limeridhika na nadharia ya Ukweli, lakini lilipungukiwa na neema ya Mungu. Katika mfano huo, Bwana Arusi alipokuja, "nao waliokuwa tayari wakaingia pamoja Naye arusini." Kuja kwa Bwana Arusi kunakooneshwa hapo kunatokea kabla ya arusi. Arusi huwakilisha upokeaji wa Kristo wa ufalme Wake (Ufu. 19:6, 7). Mji mtakatifu, yaani, Yerusalemu Mpya, ambao ni mji mkuu nao huwakilisha ufalme, nao unaitwa "Bibi-arusi, mke wa Mwana-Kondoo." "Malaika akasema, "Njoo huku. Nitakuonyesha bibi arusi, mke wa Mwana-Kondoo." Malaika akanichukua kwa Roho Mtakatifu mpaka kwenye mlima mkubwa na mrefu. Akanionyesha mji mtakatifu wa Yerusalemu. Mji ulikuwa ukishuka kutoka mbinguni kwa Mwenyezi Mungu." Ufunuo 21:9, 10. Kwa hakika kabisa basi, Bibi-arusi anawakilisha mji mtakatifu, na wanawali wanaotoka kwenda kumlaki Bwana Arusi ni mfano wa kanisa. Katika kitabu cha Ufunuo watu wa Mungu wanasemekana ya kwamba ni wageni walioalikwa katika karamu ya arusi. Ufunuo 19:9. Ikiwa ni wageni hapo, basi hawawezi tena kumwakilisha hapo bibi-arusi pia. Kristo, kama alivyoelezwa na nabii Danieli, atapokea kutoka kwa Mzee wa Siku mbinguni, "mamlaka, na utukufu, na ufalme," yaani, ataipokea, Yerusalemu Mpya, Mji Mkuu wa ufalme Wake, ukiwa "umewekwa tayari kama bibi-arusi aliyekwisha kupambwa kwa mumewe." Danieli 7:14; Ufunuo 21:2. Baada ya Yeye kuupokea ufalme huo, ndipo atakuja katika utukufu Wake kama Mfalme wa wafalme, na Bwana wa mabwana (Ufu. 19:11-16), kwa madhumuni ya kuwakomboa watu Wake, ambao "wataketi pamoja na Ibrahimu, na Isaka, na Yakobo" mezani Pake katika ufalme Wake (Mathayo 8:11; Luka 22:30), kushiriki karamu ya harusi ya Mwana Kondoo. [GC 426.2; PK Aya ya 10]

**Tazama Bwana Yuaja**

Tangazo hili, "Haya, Bwana-arusi Yuaja," lililotolewa katika majira ya joto ya mwaka wa 1844, nalo liliwaongoza maelfu kutarajia ujio wa haraka wa Bwana. Wakati uliopangwa ulipofika Bwana-arusi alikuja, siyo duniani, kama watu walivyotarajia, bali kwa Mzee wa Siku mbinguni, arusini, katika karamu ya

kuupokea ufalme Wake. “Nao waliokuwa tayari wakaingia pamoja Naye arusini; mlango ukafungwa.” Hawakutakiwa kuwako ana kwa ana kimwili kule arusini (sio mbashara); kwa maana inafanyika mbinguni, na wao wakiwa hapa duniani. Wafuasi wa Kristo wanatakiwa kumngojea Bwana wao, atakaporudi kutoka arusini.” Luka 12:36. Lakini inapasa kuielewa kazi Yake, na kisha wamfuate kwa imani anapoingia ndani mbele za Mungu. Ni katika maana hii ndiyo wanaelezwa kwamba wanakwenda arusini. [GC 427.1; PK Aya ya 11]

Katika mfano wa wanawali kumi ni wale waliokuwa na mafuta katika vyombo vyao na taa zao, ndio ambao walienda pamoja Naye arusini. Wale ambao, pamoja na ujuzi wao wa Ukweli kutoka katika Maandiko, pia walikuwa na Roho wa neema ya Mungu, na ambao, katika usiku wao ule mchungu wa majaribu, walikuwa wamengojea kwa uvumilivu wakizichunguza Biblia zao ili wapate nuru iliyo wazi zaidi – hawa ndio waliouona Ukweli kuhusu Patakatifu pa mbinguni na badiliko (kuhama) katika huduma Yake Mwokozi wao, nao kwa imani walimfuata katika kazi Yake ndani ya hekalu la juu mbinguni. Na wale wote ambao wanaukubali Ukweli huo huo kupitia ushuhuda wa Maandiko hayo, wakimfuata Kristo kwa imani anapoingia mbele za Mungu kufanya kazi ya mwisho ya upatanisho, na mwisho wa kazi hiyo apokee ufalme Wake - yote hayo huwakilishwa na kwenda pamoja Naye arusini. [GC 427.2; PK Aya ya 12]

**Kazi Ya Mwisho Katika Upatanisho**

Katika mfano wa Mathayo 22 kielelezo hicho hicho cha arusi kimetumiwa, na Hukumu ya Upelelezi imeoneshwa waziwazi ikiendeshwa kabla ya arusi hiyo. Kabla ya arusi hiyo Mfalme anakuja kuwaona wageni Wake, kuona kama wote wamevaa vazi la arusi, joho lisilo na doa la tabia ambalo limefuliwa na kufanywa jeupe katika damu ya Mwana-Kondoo. Mathayo Mathayo 22:11; Ufunuo 7:14. Yule anayekutwa na mapungufu anatupwa nje, lakini wale wote ambao baada ya kukaguliwa wanaonekana kuwa wamevaa vazi la arusi wanakubaliwa na Mungu na kuhesabiwa kuwa wanastahili kuwa na sehemu katika ufalme Wake na kuketi juu ya kiti Chake cha enzi. Kazi hii ya kuichunguza au kuikagua tabia, yaani, ya kubaini ni akina nani waliojiandaa tayari kuingia katika ufalme huo wa Mungu, ni kazi ya Hukumu ya Upelelezi (Investigative Judgment), yaani, kazi ya mwisho kabisa katika hekalu la mbinguni. [GC 428.1; PK Aya ya 13]

Kazi hiyo ya upelelezi itakapokwisha, wakati kesi za wale waliokiri kwamba ni wa wafuasi Wake Kristo katika zama zote zitakapokuwa zimechunguzwa na kufanyiwa uamuzi, ndipo hapo, na wala sio kabla ya hapo, muda wao wa majaribio (au kipindi cha kupimwa tabia zao) utakapofungwa, na mlango wa rehema utafungwa (nafasi ya kuweza kutubu na kupata msamaha itafungwa). Hivyo kwa sentensi moja fupi tu itasemwa hivi, “Nao waliokuwa tayari wakaingia pamoja Naye arusini; mlango ukafungwa,” tunachukuliwa na kupitishwa chini

kushuka kuja kwetu hadi mwisho wa huduma Yake Mwokozi, yaani, hadi wakati ambapo kazi ile kubwa inayofanywa kwa ajili ya wokovu wa mwanadamu itakapokamilika. [GC 428.2; PK Aya ya 14]

Katika huduma ya hekalu la hapa duniani, ambalo, kama tulivyokwisha kuona, ni kielelezo cha huduma ya mbinguni, wakati kuhani mkuu Siku ile ya Upatanisho alipoingia ndani ya Patakatifu pa Patakatifu, huduma katika chumba cha kwanza (cha Patakatifu) ilisitishwa. Mungu aliamuru akisema: "Wala hapatakuwa na mtu katika hema ya kukutania, wakati aingiapo (kuhani mkuu) ili kufanya upatanisho katika Patakatifu, hata atakapotoka nje." Mambo ya Walawi 16:17. Hivyo Kristo alipoingia ndani ya Patakatifu pa Patakatifu kufanya kazi Yake ya mwisho ya upatanisho, huduma Yake katika chumba cha kwanza ilisitishwa. Lakini huduma Yake katika chumba kile cha kwanza ilipoisha (Patakatifu), huduma Yake katika chumba cha pili ikawa imeanza (Patakatifu pa Patakatifu). Katika huduma ya mfano (typical) kuhani mkuu alipokuwa ameondoka ndani ya Patakatifu Siku ile ya Upatanisho, aliienda mbele za Mungu kupeleka damu ya mnyama wa sadaka ya dhambi kwa niaba ya Waisraeli wote ambao walitubu dhambi zao kwa dhati. Kwa hiyo, Kristo alikuwa amekamilisha sehemu moja tu ya huduma Yake kama Mwombezi wetu, na ili aingie katika sehemu nyingine ya kazi, Naye bado anaendelea kutumia damu Yake kumwomba Baba Yake kwa niaba ya wenye dhambi. [GC 428.3; PK Aya ya 15]

Somo hili halikueleweka kwa Waadventistawa mwaka wa 1844. Baada ya wakati aliotarajiwa kuja Mwokozi kupita, bado waliendelea kuamini kwamba kuja Kwake kulikuwa karibu; walishikilia kwamba walikuwa wamekifikia kilele cha tukio muhimu na la dharura kuliko mambo yote na kwamba kazi ya Kristo kama Mwombezi wa mwanadamu mbele za Mungu ilikuwa imekoma. Kwao ilionekana kana kwamba walikuwa wamefundishwa katika Biblia kwamba muda wa mlango wa rehema wa wanadamu ungefungwa muda mfupi tu kabla ya ujio halisi wa Bwana katika mawingu ya mbinguni. Hili kwao lilionekana kuwa ni dhahiri kutokana na Maandiko yanayoelekeza kidole chake kwa wakati ule wanadamu watakapotafuta, watakapobisha hodi mlango, na kulia nje ya mlango wa rehema, na wala hautafunguka. Na kwao likabaki swali moja kwamba ikiwa tarehe waliyokuwa wametarajia kuja kwa Kristo ingeweza kuwa ni alama ya kuonyesha mwanzo wa kipindi ambacho kingetangulia kuja muda mfupi kabla ya ujio Wake. Wakiwa wamekwishamaliza kulitoa onyo la hukumu iliyokuwa karibu, walihisi kwamba kazi yao kwa ulimwengu ilikuwa imekwisha, nao walipoteza mzigo kwa ajili ya wokovu wa roho za wenye dhambi ambao walikuwa nao moyoni mwao, na wakati huo huo dhihaka zenye ujasiri na kufuru za wale wasiomcha Mungu zilionekana kana kwamba ni ushahidi mwingine ulioonyesha kwamba Roho wa Mungu alikuwa amekwisha kuondolewa kutoka kwa wale walioikataa rehema Yake. Yote haya yalifanya hitimisho katika imani yao

kwamba muda wa rehema ulikuwa umekwisha kwa ajili yao, au, kama wao walivyolileleza wakati ule, “mlango wa rehema ulikuwa umefungwa.” [GC 429.1; PK Aya ya 16]

Lakini nuru kubwa zaidi ilipatikana walipolichunguza suala la Patakatifu. Sasa waliona kwamba walikuwa hawajakosea katika kuamini kwao kwamba mwisho wa siku (miaka) zile 2300 katika mwaka wa 1844 kuliashiria alama ya tukio la dharura, muhimu na lenye upeo mkuu. Japokuwa ilikuwa ni kweli kwamba mlango wa matumaini na rehema ambao kwao kwa karne zile kumi na nane (miaka 1800) watu walikuwa na njia ya kumfikia Mungu kupitia huo na sasa ulikuwa umefungwa, mlango mwingine ulikuwa umefunguliwa, na msamaha wa dhambi ulitolewa kwa wanadamu kwa njia ya maombezi ya Kristo ndani ya Patakatifu pa Patakatifu mbinguni (mlango wa kafara na ukuhani wa binadamu ulifungwa baada ya Kafara ya Yesu). Sehemu moja ya huduma Yake ilikuwa imefungwa, ili kutoa nafasi kwa ajili ya nyingine. Bado palikuwa na “mlango uliofunguliwa” kuelekea katika hekalu la mbinguni, ambapo Kristo alikuwa anahudumu kwa ajili ya mwenye dhambi. [GC 429.2; PK Aya ya 17]

Sasa yakaonekana matumizi ya yale Maneno  ya Kristo katika Ufunuo, yaliyoelekezwa kwa kanisa, na ambayo yanalihusu kanisa la wakati huu: “Haya ndiyo anenayo Yeye aliye mtakatifu, Yeye aliye wa Kweli, aliye na ufunguo wa Daudi, Afunguaye wala hapana afungaye; Naye hufunga wala hapana afunguaye; Nayajua matendo yako; tazama, nimeweka mbele yako mlango uliofunguliwa, wala hapana awezaye kuufunga.” Ufunuo 3:7, 8. [GC 430.1; PK Aya ya 18]

Ni wale ambao kwa imani wanamfuata Yesu  katika kazi yake kubwa ya upatanisho, ndio wanaopokea manufaa au faida ya upatanishi Wake na maombezi anayofanya kwa ajili yao, ambapo wale wanaoikataa nuru ambayo inayoweka wazi huduma Yake hii, basi hao hawanufaishwi nayo. Wayahudi walioikataa nuru iliyotolewa wakati wa ujio wa kwanza wa Kristo, na hivyo wakakataa katakata kumwamini Yeye kama Mwokozi wa ulimwengu, hawakuweza kupokea msamaha unaopatikana kupitia Kwake. Wakati Kristo alipopaa kwenda mbinguni, aliingia ndani ya Patakatifu pa mbinguni kwa njia ya damu Yake Mwenyewe (Ebr. 9:11,12), ili kumwaga mibaraka ya maombezi Yake kwa wanafunzi Wake, Wayahudi waliachwa katika giza nene kabisa wakiendelea na kafara na sadaka zao zisizokuwa na manufaa au maana yo yote. Huduma ya mifano na vivuli ilikuwa imekoma (Mt. 27:50,51; Efe. 2:14-16; Kol. 2:14- 17). Mlango ule ambao ulikuwa wazi, na kwa njia yake wanadamu walikuwa wamepata kumkaribia Mungu hapo awali, sasa haukuwa wazi tena. Wayahudi walikuwa wamekataa kumtafuta Yeye kwa njia ile moja pekee ambayo kwayo angeweza kupatikana kwa wakati ule, yaani, kupitia katika huduma Yake katika Hekalu la mbinguni. Kwa hiyo, hawakuwa na ushirika au mawasiliano yoyote na

Mungu. Kwao mlango ulikuwa umefungwa. Hivyo hawakuwa na maarifa ya kutambua Kristo Ndiye Kafara halisi na Mpatanishi pekee mbele za Mungu; kwa hiyo hawakuweza kupata manufaa ya  upatanisho Wake. [GC 430.2; PK Aya ya 19]

Hali ya Wayahudi wasioamini inaonyesha hali ya wale wasiojali na wasioamini waliomo miongoni mwa wale wanaodai au kujiita ni Wakristo, ambao kwa hiari na kukusudia kwao ni wajinga wa kazi ile anayofanya Kuhani wetu Mkuu Mwenye rehema nyingi (hawataki kujijua kazi hiyo). Katika huduma ya mfano duniani, kuhani mkuu alipoingia Patakatifu pa Patakatifu, Waisraeli wote walitakiwa kukusanyika pamoja na kupazunguka Patakatifu, na kwa kicho na umakini mkubwa kabisa kuzinyenyekeza nafsi zao mbele za Mungu, ili wapate kupokea msamaha wa dhambi zao, na wasije wakakatiliwa mbali (wakafa ghafula) kutoka katika mkutano. Basi ni jambo la muhimu kiasi gani katika huduma hiyo ya Siku ya Upatanisho halisi kwamba imetupasa sisi kuielewa kazi ya Kuhani wetu Mkuu na kujua majukumu gani tunayotakiwa sisi tupate kuyafanya. [GC 430.3; PK Aya ya 20]

Wanadamu hawawezi kuepuka kuadhibiwa kwa kulipuuzia onyo ambalo Mungu kwa rehema Yake amekwisha kuwapatia. Ujumbe ulitumwa kutoka mbinguni kwenda ulimwenguni katika siku  za Nuhu, na wokovu wao ulitegemea namna ambayo wangeutendea ujumbe huo. Kwa kuwa walilikataa onyo lile, Roho wa Mungu aliondolewa kutoka kizazi kile cha wanadamu wenye dhambi (Mwa. 6:3,6-8), nao wakaangamia kwa maji ya Gharika. Wakati wa siku za Ibrahimu, rehema iliacha kusihi kwa ajili ya wakazi wa Sodoma wenye dhambi, na wote, isipokuwa Lutu na mkewe na mabinti zake wawili, waliteketezwa kwa moto ulioshuka chini toka mbinguni. Hivyo ndivyo itavyokuwa katika siku Zake Kristo. Mwana wa Mungu aliwaambia hivi Wayahudi wasioamini wa kizazi kile, akawaambia: “Angalieni, nyumba yenu mmeachiwa hali ya ukiwa” (Hekalu lenu mmeachiwa likiwa tupu bila utukufu wa Mungu). Mathayo 23:38. Akiangalia kushuka zama zote kushuka chini na kuja mpaka siku zetu hizi za mwisho, Mungu  Yule Yule Mwenye Uweza usio na kikomo, anawatangazia wale ambao “hawakukubali kuipenda ile Kweli (Yn. 17:17; Zab. 119:142), wapate kuokolewa,” anasema: “Kwa hiyo Mungu awaletea nguvu ya upotevu, wauamini uongo; ili wahukumiwe wote ambao hawakuiamini Kweli, bali walikuwa wakijifurahisha katika udhalimu” 2 Wathesalonike 2:10-12.* Wanapokataa kabisa mafundisho yale yanayotoka kwenye Neno Lake, Mungu humwondoa Roho Wake na kuwaacha wapate kudanganywa na udanganyifu wanaoupenda *(hazuii). [GC 431.1; PK Aya ya 21]

Lakini Kristo  bado anaendelea kufanya maombezi Yake kwa ajili ya wanadamu, na nuru inatolewa kwa wale wanaoitafuta. Ingawa jambo hili mwanzoni halikueleweka kwa Waadventista wa awali, baadaye liliwekwa wazi

wakati Maandiko yanayofasili msimamo na nafasi yao halisi yalivyoanza kufunguka mbele yao. [GC 431.2; PK Aya ya 22]

Kupita kwa wakati mwaka wa 1844 kulifuatiwa na kipindi cha jaribu kubwa kwa wale ambao bado walibaki kushikilia imani ya Marejeo au Kiadventista. Nafuu yao pekee, kwa kadiri ya nafasi yao sahihi ilivyohusika, ilikuwa ni ile nuru iliyoongoza mawazo yao kuelekea kwenye Patakatifu pa mbinguni. Wengine wakaitupilia mbali imani yao kwa habari ya ukokotoaji wao wa awali wa vipindi vya kiunabii (michoro yao ya chati inavyoonyesha) na kuuhesabu mvuto wenye nguvu wa Roho Mtakatifu ulioambatana na vuguvugu za Marejeo kuwa ulitokana na mawakala wa kibinadamu au wa kishetani. Kundi jingine lilishikilia kwa nguvu sana kwamba ni Bwana aliyekuwa amewaongoza katika uzoefu wa mambo yale yaliyopita ambayo yalikuwa yamewapata katika maisha yao; nao walingoja na kukesha na kuomba ili wapate kuyajua mapenzi ya Mungu, hawa waligundua kwamba Kuhani wao Mkuu zaidi alikuwa ameingia katika hatua nyingine, ili kuanza kazi nyingine ya huduma, nao, wakimfuata kule kwa imani, waliongozwa pia kuona kufungwa kwa kazi ya kanisa, wakati wa mwisho wa wakati. Waliuelewa kwa uwazi zaidi Ujumbe wa Malaika wa Kwanza na Malaika wa Pili, nao walikuwa tayari kulipokea na kulitoa kwa ulimwengu mzima onyo zito na kali la Malaika wa Tatu wa Ufunuo 14. [GC 431.3; PK Aya ya 23]

# SURA YA 25

# SHERIA YA MUNGU ISIYOBADILIKA

**(Marekani Katika Unabii, Alama Ya Mnyama)**

Ufupisho: Mojawapo ya maonyo mazito yaliyowahi kutolewa katika Maandiko yanapatikana katika sura 13 na 14 ya kitabu cha Ufunuo. Alama ya mnyama ni nini? Je, itatolewa lini? Ni nani ataipokea? Na la muhimu zaidi, ni lazima mimi na wewe tufanye nini ili tuepuke kuipokea hii alama au chapa?Hili ni somo la umuhimu mkubwa. Nalo lina mambo nyeti ambayo unapaswa kujua. tunaishi karibu na mwisho wa wakati, na watu wengi wanatambua kwamba mgogoro mkubwa unakaribia kwa kasi.

"Kisha Hekalu la Mungu lililoko mbinguni likafunguliwa, na Sanduku la Agano Lake likaonekana ndani ya hekalu Lake." Ufunuo 11:19. Sanduku la Agano la Mungu liko ndani ya Patakatifu pa Patakatifu, chumba cha pili cha Hekalu. Katika huduma ya hema la duniani, ambalo lilitumika kama "mfano na kivuli cha mambo ya mbinguni," chumba hiki kilifunguliwa tu wakati wa Siku Kuu ya Upatanisho kwa madhumuni ya utakaso wa hema. "Kwa hiyo, tangazo hili lisemalo kwamba Hekalu la Mungu lililoko mbinguni lilifunguliwa mbinguni, na Sanduku la Agano likaonekana, huelekeza kwenye ufunguaji wa Patakatifu pa Patakatifu pa hekalu la mbinguni mwaka 1844, wakati Kristo alipoingia ndani ili kutekeleza kazi Yake ya kukamilisha huduma ya mwisho ya upatanisho. Wale ambao kwa imani walimfuatilia Kuhani wao Mkuu wa mbinguni wakati alipoingia kufanya huduma Yake ya Patakatifu pa Patakatifu (Patakatifu sana), waliliona Sanduku la Agano Lake. Kwa vile walikuwa wamejifunza somo la Patakatifu ndani ya hekalu takatifu na walipata uelewa wa badiliko la huduma ya Mwokozi wao, nao waliona kwamba sasa alikuwa akihudumu mbele ya Sanduku la Agano la

Mungu, akitumia damu Yake iliyomwagika kusihi kwa ajili ya wenye dhambi. [GC 433.1; PK Aya ya 1]

Sanduku la Agano katika hema ya kukutania iliyokuwa duniani lilikuwa kasha tu la kuhifadhia Mbao za mawe ndani yake, ambazo juu yake ziliandikwa amri (kumi) za Sheria ile ya Mungu. Sanduku lile la Agano lilikuwa ni chombo tu cha kutunzia mbao zile za Sheria ya Mungu (Amri Kumi), na ule uwepo wa kanuni au amri hizi za Mungu ulilipa sanduku lile thamani yake na utakatifu wake. Hekalu la Mungu lilipofunguliwa mbinguni, Sanduku la Agano Lake likaonekana mle. Ndani ya Patakatifu pa Patakatifu, yaani, katika Patakatifu pale pa mbinguni, Sheria hiyo ya Mungu (Amri Kumi) imehifadhiwa katika hali ya utakatifu Wake - Sheria (Amri zile Kumi) iliyotangazwa na Mungu Mwenyewe katikati ya radi na ngurumo za Sinai na kuandikwa kwa kidole Chake Mwenyewe juu ya Mbao za Mawe (Kut. 31:18; Kum. Kutoka 20). [GC 433.2; PK Aya ya 2]

Sheria ya Mungu (Amri Kumi) ambayo iko katika Hekalu la mbinguni ndiyo nakala halisi ya sheria ya Mungu (the Great Original), ambayo kanuni zilizoandikwa juu ya mbao za mawe na kunakiliwa na Musa katika vitabu vyake vitano vinavyoita Torati (Pentatuk au Tanakh) ilikuwa ni hati isiyokosea. Wale waliofikia mahali pa kulielewa jambo hili muhimu waliongozwa kwa kuiona tabia Yake takatifu, isiyobadilika ya Sheria ya Mungu (Zab 111:7,8,]. Waliona vizuri zaidi kuliko kabla ya hapo au siku za nyuma, uzito wa Maneno haya ya Mwokozi: “Mpaka mbingu na nchi zitakapoondoka, yodi moja wala nukta moja ya Torati haitaoondoka, hata yote yatimie.” Mathayo 5:18. Sheria ya Mungu (Amri Kumi), kwa kuwa ni ni ufunuo wa mapenzi Yake Mungu, maelezo ya tabia Yake, ni lazima idumu milele, ikiwa “kama shahidi mwaminifu wa mbinguni” Hakuna amri hata moja ambayo imefutwa; hakuna yodi moja, wala nukta moja ambayo imebadilishwa au kufutwa. Asema hivi Mwandishi wa Zaburi: “Ee Bwana, Neno Lako lasimama imara mbinguni hata milele.” “Maagizo Yake yote ni amini, yamethibitika milele na milele.” Zaburi 119:89; 111:7, 8. [GC 434.1; PK Aya ya 3]

Katika ya Amri Kumi (Dekalojia) kuna amri ile ya nne, kama ilivyotangazwa kwa mara yake ya kwanza: “Ikumbuke Siku ya Sabato (Jumamosi) uitakase. Siku sita fanya kazi, utende mambo yako yote; lakini Siku ya Saba ni Sabato YA BWANA, Mungu wako, siku hiyo usifanye kazi yoyote, wewe, wala mwana wako, wala binti yako, wala mtumwa wako, wala mjakazi wako, wala mnyama wako wa kufuga, wala mgeni aliye ndani ya malango yako. Maana, kwa siku sita, BWANA alifanya mbingu, na nchi, na bahari, na vyote vilivyomo, akastarehe Siku ya Saba; kwa hiyo BWANA akaibarikia siku ya Sabato akaitakasa” Kutoka 20:8-11 (Akaitenga kwa matumizi matakatifu ya ibada si kwa Wayahudi bali kwa binadamu wote). [GC 434.2; PK Aya ya 4]

Roho wa Mungu aliigusa sana mioyo ya wale wanafunzi wa Neno Lake. Ushawishi ulijengeka mioyoni mwao kwa umakini kabisa kwamba kwa ujinga wao walikuwa wameivunja kanuni hiyo kwa kutoijali siku hiyo ya mapumziko aliyoiweka Muumbaji wao. Wakaanza kuzichunguza sababu za kuitunza siku ya kwanza ya juma (Jumapili) badala ya kuitunza siku Sabato ambayo Mungu alikuwa ameitakasa (Jumamosi). Hawakuweza kupata ushahidi wowote katika Maandiko ulioonyesha kwamba amri ya nne ilikuwa imefutwa, au kwamba Sabato (Jumamosi) ilikuwa imebadilishwa; mbaraka ulioitakasa siku ya saba (Jumamosi) mara ya kwanza baada ya uumbaji ulikuwa haujapata kuondolewa Naye kamwe. Walikuwa wanatafuta kwa unyofu wa moyo kuyajua na kuyafanya mapenzi ya Mungu (Kutii amri); sasa walipong'amua wenyewe ya kwamba walikuwa wavunjaji/waasi wa Sheria Yake, huzuni iliijaza mioyo yao, nao walionyesha utiifu wao kwa Mungu kwa kuitunza Sabato Yake na kuitakasa Sabato. [GC 434.3; PK Aya ya 5]

## Siri Iliyojificha Nyuma Ya Upinzani Ule

Jitihada nyingi na za dhati zilifanywa ili kuipindua imani yao. Hakuna mtu ambaye angeshindwa kuona kwamba ikiwa hema ya duniani ilikuwa ni mfano au nakala ya hekalu la mbinguni, basi Sheria ile (Amri Kumi) iliyohifadhiwa ndani ya Sanduku la Agano la hema la duniani, ni dhahiri kwamba ilikuwa ni nakala halisi na kamili ya Sheria, iliyo ndani ya Sanduku la Agano kule mbinguni (Ufu. 11:19); na ya kuwa kuukubali kwa imani Ukweli huu uliohusu hema ya mbinguni kulijumuisha kuyatambua na kuyakubali madai ya Sheria ya Mungu na kuwajibika na masharti ya Sabato ya amri ya nne (Jumamosi). Hapa ndipo ilipokuwapo siri ya upinzani wenye uchungu mkali uliodhamiriwa kwa makusudi kabisa dhidi ya ufafanuzi wenye mwafaka wa Maandiko yaliyofunua huduma Yake Kristo katika hekalu la mbinguni. Watu walijitahidi sana kuufunga mlango ambao Mungu alikuwa ameufungua, na kuufungua mlango aliokuwa amekwisha kuufunga. Lakini Yeye "Mwenye kufungua wala hapana afungaye, Naye afunga wala hapana afunguaye," alikuwa amesema: "Tazama, nimekupa mlango uliofunguliwa mbele yako, ambao hapana awezaye kuufunga" Ufunuo 3:7, 8. Kristo alikuwa ameufungua mlango, au huduma ya Patakatifu pa Patakatifu, nuru ilikuwa inang'aa kutoka katika mlango ule uliofunguliwa wa Hekalu la mbinguni, na amri ya nne ilioneshwa ikiwa imejumuishwa katika Sheria ambayo ilikuwa imehifadhiwa mle ndani; kile ambacho Mungu amekianzisha, hakuna mwanadamu ambaye angeweza kukiangusha au kukipindua. [GC 435.1; PK Aya ya 6]

Wale waliokuwa wameipokea nuru kuhusu Upatanisho wa Kristo na uendelevu wa kudumu wa Sheria ya Mungu waligundua kwamba hizo ndizo Kweli zilizokuwa zimewasilishwa katika Ufunuo 14. Vipengele mbali mbali vya ujumbe

wa sura hii huunda onyo lenye sehemu tatu (tazama Kiambatisho) ambalo ni linawaandaa wakazi wa dunia hii kuwa tayari kwa ujio wa pili wa Bwana. Tangazo hili, "Saa ya hukumu Yake imekuja," huelekeza watu kwenye kufunga huduma ya Kristo kwa ajili ya wokovu wa wanadamu (huduma ya mwisho ya kufunga kazi). Linapiga mbiu ya habari za Ukweli ambao ni lazima ziendelee kutangazwa mpaka hapo maombezi ya Mwokozi yatakapokoma, na Yeye atakaporejea ulimwenguni hapa ili kuwachukua watu Wake kwenda nao Kwake. Kazi hiyo ya hukumu iliyoanza mwaka ule wa 1844 ni lazima iendelee mpaka hapo kesi za makundi yote zitakapokuwa zimeamuliwa, walio hai na waliokufa; kwa maana hukumu hiyo itaendelea kuhubiriwa mpaka kufungwa kwa mlango wa rehema kwa wanadamu wote. Ili watu wapate kujiandaa na kuwa tayari kusimama katika hukumu hiyo, ujumbe huu unawaamurisha ukisema "Mcheni Mungu, na kumtukuza," tena "Msujudieni Yeye aliyezifanya mbingu na nchi na bahari na chemchemi za maji" (Ufu. 14:6,7; Kut. 20:8-11) Kumi),... Matokeo ya kukubali kuzipokea Jumbe hizi tatu, yametajwa kwa Maneno haya: "Hapa ndipo penye subira ya watakatifu, hao wazishikao amri za Mungu, na imani ya Yesu" (Ufu. 14:12). Ili kujiandaa tayari kwa ajili ya hukumu hiyo, ni lazima watu waishike Sheria hiyo ya Mungu (Amri Kumi). Sheria hiyo itakuwa ndicho kipimo cha tabia katika hukumu hiyo (Yak. 2:10-13). Mtume Paulo anasema: "Na Wote waliokosa, wenye sheria, watahukumiwa kwa sheria…… katika siku ile Mungu atakapozihukumu siri za wanadamu, kwa Kristo Yesu." Naye anasema kwamba "waitendao sheria watakaohesabiwa haki" (Warumi 2:12-16; Imani ni ya lazima ili kuitii Sheria ya Mungu; kwa maana "pasipo imani haiwezekani kumpendeza." Na "kila tendo lisilotokana na imani ni dhambi." Waebrania 11:6; Warumi 14:23. [GC 435.2; PK Aya ya 7]

Kwa njia ya malaika wa kwanza, wanadamu wanaalikwa'wamche Mungu, na kumtukuza' na kumsujudu Yeye aliye Muumbaji wa mbingu na nchi. Ili kufanya jambo hili, ni lazima waitii Sheria Yake (Amri Zake). Asema hivi mtu mwenye hekima: "Mche Mungu, nawe uzishike amri Zake, maana kwa jumla ndiyo impasayo mtu." Mhubiri 12:13. Bila kuzitii amri Zake hakuna ibada inayoweza kumpendeza Mungu (Mk. 7:6-13; Yak. 2:10-12; 1 Yoh. 2:3-6; Zab. 17:5). "Kwa maana huku ndiko kumpenda Mungu, kwamba tuzishike Amri Zake." "Yeye aligeuzaye sikio lake asiisikie Sheria, Hata sala yake ni chukizo." 1 Yohana 5:3; Mithali 28:9. (Maagizo, Amri, Sheria au Shuhuda Zake- Katika Zaburi 119 yanaonyesha ni kitu kimoja). [GC 436.1; PK Aya ya 8]

### Wito Wa Kumsujudu Muumba Wetu

Wajibu wa kumwabudu Mungu umejengwa juu ya Ukweli kuwa Yeye Ndiye Muumbaji na Kwake uwepo wa wenye uhai wengine wote unamtegemea Yeye. (Viumbe vinawiwa Naye uhai walio nao). Na mahali popote ndani ya Biblia, dai Lake la kupewa kicho na kuabudiwa juu ya miungu ya wapagani,

linapowalisisishwa ushahidi unaotolewa kuunga mkono dai hilo ni uwezo Wake wa Kuumba. “Maana miungu yote ya watu si kitu, Lakini Bwana Ndiye aliyezifanya mbingu.” Zaburi 96:5. “Mtanifananisha na nani, basi, nipate kuwa sawa Naye? Asema Yeye aliye Mtakatifu. Inueni macho yenu juu, mkaone; ni nani aliyeziumba hizi.” “Maana BWANA, aliyeziumba mbingu, asema hivi; Yeye ni Mungu; Ndiye aliyeiumba dunia na kuifanya;... Mimi ni BWANA, wala hapana mwingine.” Isaya 40:25; 26; 45:18. Mwandishi wa Zaburi anasema hivi: “Jueni kwamba Bwana Ndiye Mungu; Ndiye aliyetuumba na sisi tu watu Wake.” “Njoni, tuabudu, tusujudu, Tupige magoti mbele za Bwana aliyetuumba.” Zaburi 100:3; 95:6. Na wenye uhai watakatifu wanaomwabudu Mungu mbinguni wanasema, kama sababu ya Ibada yao kwanini kwamstahili Mungu tu: “Umestahili Wewe, Bwana wetu na Mungu wetu, kuupokea utukufu na heshima na uweza; kwa kuwa Wewe Ndiwe uliyeviumba vitu vyote.” Ufunuo 4:11. [GC 436.2; PK Aya ya 9]

Katika Ufunuo 14, wanadamu wanaitwa kumwabudu Muumbaji; na unabii unatufunulia tabaka la watu ambalo, kama matokeo ya Ujumbe wenye sehemu tatu (zilizofungamanishwa), wanazitunza Amri Kumi za Mungu. Moja ya amri hizi humtaja moja kwa moja Mungu kama Muumbaji (Kutoka 20, Ufu 14:12). Amri ya nne inasema hivi: “Siku ya saba ni Sabato ya BWANA, Mungu wako,... maana, kwa siku sita BWANA alifanya mbingu, na nchi, na bahari, na vyote vilivyomo, akastarehe siku ya saba; kwa hiyo BWANA akaibarikia siku ya Sabato (Jumamosi) akaitakasa.” Kutoka 20:10,11. Kuhusu Sabato, Bwana anasema zaidi kwamba ni “ishara,... mpate kujua ya kuwa Mimi Ndimi BWANA, Mungu wenu.” Ezekieli 20:20. Na sababu iliyotolewa ni kuwa: “Kwani kwa siku sita Bwana alifanya mbingu na nchi, akastarehe kwa siku ya saba na kupumzika.” Kutoka 31:17. [GC 437.1; PK Aya ya 10]

“Umuhimu wa Sabato kama kumbukumbu ya uumbaji ni kuwa inadumisha daima uwepo wa sababu ya Kweli ya ibada kupaswa kutolewa kwa Mungu” - kwa sababu Yeye Ndiye Muumbaji, na sisi tu viumbe Vyake.” Kwa hiyo, Sabato ni msingi kabisa wa ibada ya Mungu, maana inafundisha Kweli hii kuu kwa njia ya kuvuuta moyo sana, na wala hakuna agizo jingine lolote lililowekwa ambalo linaweza kufanya hivyo. Msingi wa Kweli wa ibada ya kumwabudu Mungu, sio tu wa ibada ile inayofanyika katika siku ya saba (Jumamosi), bali wa ibada zote, unapatikana katika kuweka tofauti kati ya Muumbaji na viumbe Wake. Ukweli huu mkuu hauwezi kamwe kupitwa na wakati, na haupaswi kusahauliwa kamwe.” - J. N. Andrews, History of the Sabbath, sura ya 27. Ilikuwa kwa kusudi la kuudumisha Ukweli huu daima mbele ya akili za wanadamu, ndiyo maana Mungu aliiweka Sabato katika Bustani ya Edeni; na kwa kadiri Ukweli kuwa Yeye Ndiye Muumbaji wetu unavyozidi kuendelea kuwa sababu inayoonyesha kwa nini sisi tunapaswa kumwabudu Yeye, ndivyo Sabato itakavyoendelea kuwa ishara na kumbukumbu ya Ukweli huo. Ikiwa Sabato ingelikuwa imetunzwa na watu wote

ulimwenguni, na kwa wakati wote, mawazo na upendo wa wanadamu vingeelekezwa kwa Muumbaji, Yeye Peke Yake Ndiye angekuwa kiini cha kicho na ibada/kuabudiwa, na kamwe kusingekuwapo na mwabudu sanamu, asiyemuamini Mungu, mtu anayemkana Mungu au kafiri. Utunzaji wa Sabato ni ishara ya utii kwa Mungu wa Kweli, "Yeye aliyeziumbaa mbingu na nchi, na bahari, na chemchemi za maji." Maana yake ni kuwa ujumbe unaowaagiza wanadamu kumwabudu Mungu na kuzishika Amri Zake na kutoa kwa njia ya uhakika wito rasmi kwa watu kuishika amri ya nne (Kut. 20:8-11). [GC 437.2; PK Aya ya 11]

Kinyume na wale wanaozishika amri (kumi) za Mungu na kuwa na imani ya Yesu, malaika wa tatu anaelekeza kwenye tabaka jingine la watu, ambalo dhidi ya makosa yao onyo hili zito na la kuogofya linatamkwa: "Mtu awaye yote akimsujudu huyo mnyama na sanamu yake, na kuipokea chapa katika kipaji cha uso wake, au katika mkono wake, yeye naye atakunywa katika mvinyo ya ghadhabu ya Mungu"* Ufunuo 14:9, 10. (Ufunuo ina Maelezo zaidi kwenye mapigo saba). Tafsiri sahihi ya mifano hiyo iliyotumiwa ni ya muhimu ili kuweza kuuelewa ujumbe huu. Ni nini kinachowakilishwa na mnyama, sanamu ya mnyama, chapa (alama) ya mnyama? *("Mtu awaye yote akimsujudu huyo mnyama na sanamu yake, na kuipokea chapa (alama) katika kipaji cha uso wake (katika fikra zake), au katika mkono (uwajibikaji) wake, yeye naye atakunywa katika mvinyo ya ghadhabu ya Mungu") [GC 438.1; PK Aya ya 12]

### Kumtambulisha Joka

Mlolongo wa unabii ambamo mifano hii inapatikana ndani yake unaanzia katika Ufunuo 12, unaanza kwa kumtaja yule joka aliyetafuta kumwangamiza Kristo wakati wa kuzaliwa Kwake. Joka anaelezwa kuwa ni Shetani (Ufunuo 12:9); ndiye aliyemhamasisha Herode kumuua Mwokozi. Lakini kibaraka mkubwa wa Shetani katika kupigana vita dhidi ya Kristo na watu Wake wakati wa karne za kwanza za zama za Ukristo ilikuwa ni himaya ya Kirumi, ambapo ndani yake upagani ulikuwa ndiyo dini yake kuu iliyoenea kote. Hivyo, japokuwa kimsingi Joka anamwakilisha Shetani, katika maana ya pili, huyo (Joka) ni mfano wa Rumi ya Kipagani. [GC 438.2; PK Aya ya 13]

Katika sura ya 13 (mstari wa 1-10) anaelezwa mnyama au ufalme mwingine (Dan. 7:17), aliyekuwa "mfano wa chui," ambaye Joka anampa "nguvu zake na kiti chake cha enzi na mamlaka kubwa." Mfano huo, kama walivyoamini Waprotestanti wengi, huwakilisha Upapa, ambao ulichukua nguvu na mamlaka ya kiti cha enzi na uwezo uliokuwa umeshikiliwa kwanza na Dola ya Rumi ya zamani. Kwa habari ya mnyama huyo mfano wa chui yanatolewa maelezo haya: "Naye akapewa kinywa cha kunena maneno makuu, na makufuru.... Akafunua kinywa chake amtukane Mungu, na kulitukana Jina Lake, na maskani Yake, nao

wakaao mbinguni. Tena akapewa kufanya vita na watakatifu na kuwashinda, akapewa uwezo juu ya kila kabila na jamaa na lugha na taifa." Unabii huu, ambao unakaribia kufanana sana na maelezo ya pembe ndogo ya Danieli 7, bila shaka lolote unazungumzia Upapa. [GC 439.1; PK Aya ya 14]

"Akapewa uwezo wa kufanya kazi yake miezi arobaini na miwili" (fungu la 5). Naye nabii asema hivi, "Nikaona kimoja cha vichwa vyake (watawala wake) kana kwamba kimetiwa jeraha la mauti" (fungu la 3). Na tena asema hivi: "Mtu akichukua mateka, atachukuliwa mateka. Mtu akiua kwa upanga, atauawa kwa upanga" (fungu la 10). Miezi hiyo arobaini na miwili ni sawa na "wakati, na nyakati mbili, na nusu wakati," miaka mitatu na nusu, au siku 1260 za Danieli 7,--* muda ambao upapa ulipewa mamlaka ya kuwatesa watu wa Mungu. Kipindi hichi, kama ilivyokwisha kuelezwa katika Sura zilizotangulia, kilianza na upapa uliposhika hatamu za utawala wa dunia (papal supremacy) katika mwaka wa 538 B.K., nacho kilikoma mwaka ule wa 1798 (1798 – 538 = miaka 1260). Wakati huo papa (Pius wa VI) alichukuliwa mateka na jeshi la Kifaransa, hapo ndipo mamlaka ya kipapa ilipotiwa jeraha lake la mauti – Ufu. 17:18), tena likawa limetimizwa Neno hili lililotabiriwa, "Mtu akichukua mateka atachukuliwa mateka" (fungu la 7 - akiwafunga na kuwaua watakatifu – Dan. 11:32-35) *(Jeshi lililoongozwa na Jenerali Berthier wakati wa Napoleon, lilimteka papa, na upapa ulipoteza uwezo wake wa kuitawala dunia). [GC 439.2; PK Aya ya 15]

**Kutokea Kwa Mamlaka Mpya**

Katika hatua hii mfano mwingine unatambulishwa. Nabii anasema: "Kisha nikaona mnyama mwingine, akipanda juu kutoka katika nchi; naye alikuwa na pembe mbili mfano wa mwana-kondoo." Fungu la 11. Mambo yote mawili, yaani mwonekano wa mnyama huyo na jinsi alivyotokea vinaonyesha kwamba taifa linalowakilishwa naye hapa ni tofauti na yale yaliyoelezwa katika mifano iliyotangulia. Falme kuu zilizowahi kuitawala dunia hii ziliwasilishwa kwa nabii Danieli kama wanyama wawindao, wakatili na wa kutisha (wanaoteka nyara), waliotokea wakati zile "pepo nne za mbinguni zilipovuma kwa nguvu juu ya bahari kubwa." Danieli 7:2. Katika Ufunuo 17 malaika alifafanua kwamba maji yanawakilisha "jamaa na makutano na mataifa na lugha." Ufunuo 17:15. Upepo ni ishara ya mashindano au vita. Pepo nne za mbinguni zinazoshindania juu ya bahari kuu zinawakilisha mandhari za kutisha za mashindano vitani na mapinduzi ambayo kwayo falme hujitwalia mamlaka. [GC 439.3; PK Aya ya 16]

"Lakini mnyama (ufalme) yule mwenye pembe mbili mfano wa mwanakondoo alionekana "akipanda juu kutoka katika nchi." Badala ya kuzipindua mamlaka ya falme zingine na kujiimarisha kimamlaka, taifa lililowakilishwa hapa ni lazima liinuke katika eneo ambalo awali halikuwa na wakazi na lilikua taratibu na kwa amani. Basi, lisingeweza kutokea miongoni mwa mataifa yale yenye msongamano

wa watu na yenye changamoto zilizokuwa zinayakumba kama mataifa ya Ulimwengu ule wa Zamani (Ulaya)---- yaani, lisingetokea katika bahari ya mawimbi iliyochafuka na "jamaa na makutano na mataifa na lugha." Ni lazima litafutwe katika Bara la Magharibi. [GC 440.1; PK Aya ya 17]

Je, ni taifa gani la Ulimwengu Mpya lililokuwa likipanda juu kwa uwezo na kujitwalia mamlaka yake katika mwaka 1798, likitoa matumaini ya kuwa na nguvu na ukuu, na kuvuta umakini wa ulimwengu mzima? Matumizi ya mfano huo hayatuachii tuwe na swali lolote. Taifa moja, na moja tu, hutimiza vipengele vya unabii huu. Unabii unaelekeza kidole chake bila kukosea kwa taifa la Marekani (U.S.A.). Tena na tena wazo hilo, na karibu kwa kutumia Maneno yale yale kabisa ya mwandishi mtakatifu, bila kutambua na mnenaji mahiri na mwanahistoria aliyeelezea kutokea kuinuka na kukua kwa taifa hili. Mnyama alionekana "akipanda juu kutoka katika nchi;" kwa mujibu wa watafsiri, Neno hili "kupanda juu" lililotumika hapo maana yake ikichukuliwa neno kwa neno humaanisha ni "kukua au kuchipua kama mmea." Na, kama tulivyokwisha kuona, taifa hili liliinuka katika eneo ambalo halikuwa limekaliwa na watu siku za nyuma. Mwandishi mmoja mashuhuri, akieleza kuinuka kwa Marekani (U.S.A), anazungumza juu ya "siri ya kupanda kwake juu kutoka mahali pasipokuwa na watu," tena anasema hivi: "Kama mbegu iliyokuwa kimya tulizidi kukua na kuwa himaya." - G. A. Townsend, The New World Compared With the Old, uk. 462. Jarida la Ulaya katika mwaka ule wa 1850 lilizungumzia kuhusu Marekani (U.S.A) kama taifa zuri na la ajabu ambalo lilikuwa "likiinuka," na "katikati ya ukimya wa dunia, likijiongeza nguvu zake na kiburi kila siku." - The Dublin Nation. Edward Evarett - katika hotuba yake fasaha juu ya Wasafiri Waanzilishi wa Taifa hili, alisema: "Si walitafuta mahali pa utulivu, palipojificha, pasipochukiza kwa kutojulikana kwake, na palipo salama kwasababu ya umbali wake, mahali ambapo kanisa dogo la Leyden lingeweza kuufurahia uhuru wa dhamiri? Tazameni maeneo hayo yenye nguvu sana, ambayo kwa ushindi wa amani,... wamezibeba bendera zao za msalaba!" - Speech Delivered at Plymouth, Massachusetts, Dec. 22, 1824, uk. 11. [GC 440.2; PK Aya ya 18]

"Naye alikuwa na pembe mbili mfano wa mwana-kondoo." Pembe mfano wa mwana-kondoo huashiria uchanga, kutokuwa na hatia, na upole, mambo hayo yaliiwakilisha kikamilifu tabia ya taifa la Marekani (U.S.A) wakati lilipowasilishwa mbele ya nabii huyu "likipanda juu" katika mwakawa 1798. Miongoni mwa wakimbizi au wahamiaji Wakristo waliokimbilia uhamishoni Marekani kwa mara ya kwanza na kutafuta hifadhi yao mbali na mateso na unyanyasaji wa wafalme waonevu na viongozi wa dini wasiokuwa na uvumilivu wa dini za wengine, walikuwamo wengi waliodhamiria kuunda serikali yao juu ya msingi mpana wa Uhuru wa kiraia na Uhuru wa dini (kuabudu). Mawazo yao yalipata mpenyo katika Azimio la Uhuru, ambalo linabainisha ukweli mkuu

usemao kwamba “watu wote wameumbwa sawa,” tena wamejaliwa kuwa na haki isiyoweza kuachanika kwao (Isiyoweza kupingika) ya kuwa na “uhai, uhuru, na utafutaji wa furaha yao.” Na Katiba ya Marekani inawathibithishia wananchi uhakika wa kujitawala katika serikali yao wenyewe, ikielekeza kuwa nafasi ya wawakilishi waliochaguliwa kwa kura nyingi, watatunga na kuzisimamia sheria za nchi. Uhuru wa imani ya kidini pia ulitolewa, kila mtu akiruhusiwa kumwabudu Mungu kulingana na misukumo ya dhamiri yake. Kuwa Ujamhuri na Uprotestanti,* ukawa ndizo kanuni za msingi za taifa hilo. Kanuni hizo ndiyo siri ya nguvu na mafanikio yake. Wale waliokandamizwa, walioonewa au walioteswa na kukanyagwa chini katika Ulimwengu wote wa Kikristo wameigeukia nchi hii kwa shauku na matumaini. Mamilioni ya watu walikimbilia fukwe zake, na Marekani (U.S.A) imepanda (imeinuka) juu na kuwa miongoni mwa mataifa yenye nguvu zaidi ya ulimwengu (pembe zile mbili- Republicanism and Protestantism- Ujamhuri na Uprotestanti). [GC 441.1; PK Aya ya 19]

### Tofauti Dhahiri Sana

Lakini yule mnyama (nchi au ufalme) mwenye pembe mbili kama mwana-kondoo “akanena kama joka. Naye atumia uwezo wote wa mnyama yule wa kwanza mbele yake. Naye aifanya dunia na wote wakaao ndani yake wamsujudu mnyama wa kwanza, ambaye jeraha lake la mauti lilipona.... Akiwaambia wale wakaao juu ya nchi kumfanyia sanamu yule mnyama, aliyekuwa na jeraha la mauti naye akaishi.”, aliyekuwa na jeraha la upanga naye akaishi.” Ufunuo 13:11-14. [GC 441.2; PK Aya ya 20]

Zile pembe za mwana-kondoo na sauti ya joka katika mfano huo huonyesha ukinzani mkubwa uliopo kati ya maneno yanayokiriwa kwa mdomo na matendo ya taifa hilo lililowakilishwa kwa njia hiyo. Kule “kunena” kwa taifa hilo ni utendaji wa mamlaka yake ya kutunga sheria (Kibunge) na kimahakama. Kwa utendaji huo, taifa litasema uongo kwa kubadilisha kanuni za uhuru na amani ambazo lilijiwekea kama msingi wa sera yake. Utabiri kwamba litanena “kama joka” na kutumia “uwezo wote wa mnyama yule wa kwanza” hutabiri waziwazi juu ya ujio wa roho ile ya kutovumilia imani ya wengine (intolerance) na mateso, ambayo ilionyeshwa na mataifa yaliyowakilishwa na joka na mnyama yule aliye kama chui. Na usemi huo kwamba mnyama (ufalme) mwenye pembe mbili “aifanya dunia na wote wakaao ndani yake wamsujudie mnyama (mfalme) yule wa kwanza” huashiria kwamba mamlaka ya taifa hili itatumiwa katika kushinikiza kisheria utekelezaji wa jambo fulani la kiibada ambalo litakuwa ni tendo la kusujudia upapa. [GC 442.1; PK Aya ya 21]

**Kutofuata Utaratibu**

Hatua ya tendo hilo itakuwa kinyume kabisa na kanuni za serikali hii, kinyume cha msingi wa taasisi zake huru na zenye uwezo mahiri kiakili, kinyume na maneno yake mazito ya viapo yaliyo katika Azimio la Uhuru na kinyume na Katiba ya Nchi. Waasisi wa taifa hilo walijitahidi kwa busara kuweka kinga dhidi ya kuzitumia mamlaka za kiserikali kuingilia mambo ya kanisa, pamoja na matokeo yake yasiyoepukika - kukosa uvumilivu wa imani ya wengine na mateso. Katiba ya Nchi hiyo imeweka masharti haya, kwamba "Bunge la Marekani (Kongresi) halitatunga sheria yoyote inayohusiana na uanzishaji wa dini, au kupiga marufuku uendeshaji huru wa dini hiyo," na ya kwamba "dini haitakuwa kigezo kwa mtu yeyote kitakachozingatiwa kama sifa ya kushika ofisi au wajibu wowote wenye dhamana ya umma kwenye taifa la Marekani. Ni kwa ukiukwaji tu wa wazi wa maadili unaochukiza wa kinga hizi za thamani, zilizowekwa kwa ajili ya uhuru wa taifa hilo, ndiyo kwawezesha utekelezaji fulani wa kidini kushinikizwa na mamlaka ya kiserikali. Lakini mgogoro au kutofautiana kunaoletwa na ubadilikaji wa tendo hilo hauwezi kuwa mkubwa zaidi kuliko ulivyowakilishwa katika mfano wenyewe. Ni yule mnyama mwenye pembe mbili kama za mwana-kondoo - ambaye kwa mwonekano yuko safi, mpole, na asiye na madhara yoyote - ndiye ambaye ananena kama joka. [GC 442.2; PK Aya ya 22]

"Akiwaambia wakaao juu ya nchi, kumfanyia sanamu yule mnyama." Hapa kuna maelezo ya wazi kuhusu mfumo wa serikali ambao mamlaka yake ya kutunga sheria (Bunge) yako katika mikono ya wananchi (demokrasia), ushahidi huo ni madhubuti kabisa, kwamba Marekani ndilo taifa linalomaanishwa katika unabii huu. [GC 442.3; PK Aya ya 23]

Lakini, je! "sanamu ya mnyama" ni nini? Tena Sanamu hiyo inafanyikaje? Sanamu inafanywa na mnyama mwenye pembe mbili, tena ni sanamu kwa ajili ya mnyama. Pia inaitwa sanamu ya mnyama. Basi kujifunzaili kuelewa sanamu hii ikoje na inafanyikaje ni lazima tujifunze tabia halisi za mnyama mwenyewe - yaani, tujifunze tabia za upapa. [GC 443.1; PK Aya ya 24]

Wakati kanisa la awali lilipochafuka kwa kuiacha injili sahili na kupokea taratibu za mapokeo ya ibada za kipagani (ukafiri) pamoja na desturi zake, lilipoteza Roho na nguvu ya Mungu; na ili lipate kuzitawala dhamiri za watu (liwazuie watu kumwabudu Mungu wanavyotaka), liliomba msaada kuungwa mkono na mamlaka ya kidunia. Matokeo yake yakawa kuzaliwa kwa mfumo wa upapa, mfumo wa kanisa uliotawala mamlaka ya kiserikali na uliotumia mamlaka ya kiserikali kutekeleza makusudi ya kanisa, hasusani kwa ajili ya kupambana na kuuadhibu "uzushi" (Rumi iliyaita mafundisho safi ya Biblia kuwa ni uzushi). Ili Marekani ipate kuifanya sanamu hiyo ya mnyama,* ni lazima mamlaka ya kidini (Uprotestanti wa Marekani) iitawale kabisa serikali ya kiraia kwa namna ambayo

mamlaka ya kiserikali itatumiwa pia na kanisa kutimiza matakwa ya kanisa *(mfumo wa utawala unaofanana na upapa, yaani, mtu mmoja kuvaa kofia mbili – dini na serikali). [GC 443.2; PK Aya ya 25]

"Wakati wowote ule kanisa lilipopata mamlaka ya kiserikali, liliyatumia mamlaka hayo kwa ajili ya kuwaadhibu wale wanaotofautiana na mafundisho yake ya dini (Doctrines). Makanisa ya Kiprotestanti yaliyozifuata nyayo za Rumi kwa njia ya kuungana na mamlaka au serikali za kidunia yamedhihirisha tamaa yao inayofanana na ile ya Rumi ya kudhibiti mipaka ya uhuru wa dhamiri ya mtu (yaani, kumlazimisha mtu kuamini kile tu wanachotaka aamini kinyume na vile dhamiri yake inavyotaka). Mfano wa jambo hilo ulionekana katika yale mateso yaliyoendelea kwa muda mrefu sana dhidi ya watu wanaotofautiana na Kanisa la Kingereza (Anglican Church), yaani, wale waliokataa kukubaliana na mafundisho yake ya dini. Katika kipindi chote cha karne ya kumi na sita na kumi na saba, maelfu ya wachungaji wasiofungamana na upande wowote walilazimishwa kuyakimbia makanisa yao, na wengi wao, wakiwa wachungaji na walei. walikabiliwa na adhabu ya kutozwa faini, kufungwa, kuteswa vibaya sana, na kuuawa kama wafia dini kwa ajili ya Imani yao. [GC 443.3; PK Aya ya 26]

**Uasi Unaongoza Njia**

Ulikuwa ni uasi uliolifanya kanisa (Rumi) kuomba msaada kwa serikali ya kiraia, na jambo hilo liliandaa njia ya uanzilishwaji na ukuzwaji wa upapa - mnyama. Alisema hivi Paulo: "Hapo" "Maana haiji usipokuja kwanza ule ukengeufu,.....akafunuliwa yule mtu wa kuasi." 2 Wathesalonike 2:3." Kwa hiyo, uasi ndani ya kanisa utatayarisha njia ya kuundwa kwa sanamu ya mnyama (Mfumo wa serikali ya Kiprotestanti ya Marekani unaofanana na ule wa upapa – mtu mmoja kuvaa kofia mbili, ya kiraia na kikanisa). [GC 443.4; PK Aya ya 27]

Biblia inaeleza kwamba kabla ya ujio Wake Bwana patakuwa na hali ya kurudi nyuma katika mambo ya kiroho/dini kama ilivyotokea katika karne za kwanza "Siku za mwisho kutakuwako nyakati za hatari. Maana watu watakuwa wenye kujipenda wenyewe, wenye kupenda fedha, wenye kujisifu, wenye kiburi, wenye kutukana, wasiotii wazazi wao, wasio na shukrani, wasio safi, wasiowapenda wa kwao, wasiotaka kufanya suluhu, wasingiziaji, wasiojizuia, wakali; wasiopenda mema, wasaliti, wakaidi, wenye kujivuna, wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu; wenye mfano wa utauwa, lakini wakikana nguvu Zake." 2 Timotheo 3:1-5. "Basi Roho anena waziwazi ya kwamba nyakati za mwisho wengine watajitenga na imani, wakisikiliza roho zidanganyazo, na mafundisho ya mashetani." 1 Timotheo 4:1. Shetani atafanya kazi "kwa uwezo wote, na ishara na ajabu za uongo; na katika madanganyo yote ya udhalimu." Na wale wote ambao "kwa sababu hawakukubali kuipenda ile Kweli, wapate kuokolewa," wataachwa waipokee "nguvu ya upotevu, wauamini uongo." 2 Wathesalonike

2:9-11. Wakati hali hiyo ya uovu au uasi, yaani kutomcha Mungu itakapofikiwa, matokeo yale yale yatafuata kama vile ilivyokuwa katika karne zile za kwana. 2 Wathesalonike 2:9-11. [GC 444.1; PK Aya ya 28]

Tofauti nyingi za imani zinazoonekana katika makanisa ya Kiprotestanti huchukuliwa na wengi kama ndio uthibithisho wa hakika kuwa hakuna jitihada yoyote ya kulazimisha umoja inayoweza kufanyika miongoni mwao (muungano wa makanisa au ecumenism). Lakini, basi, kwa miaka mingi kumekuwapo na wazo lenye nguvu, na tena linaloendelea kukua ndani ya makanisa haya yenye imani ya Kiprotestanti, ambalo linaunga mkono uwepo wa muungano uliojengwa juu ya vipengele vinavyofanana vya mafundisho ya dini yanayokubaliwa na wote. Ili kufanikisha muungano kama huo wa makanisa, mjadala juu ya mada ambazo wote hawakubaliani nazo - haidhuru yawe ni mafundisho ya muhimu kiasi gani kutokana mtazamo wa Biblia – ni lazima uepukwe kwa juhudi zote. [GC 444.2; PK Aya ya 29]

Charles Beecher, katika hubiri lake la mwaka wa 1846, alitangaza kwamba huduma ya "madhehebu ya Waprotestanti Wainjilisti au Evangelical Protestants, sio tu kwamba "yameundwa kuanzia chini kwenda juu kwa kutumia shinikizo kubwa linalotokana na hofu ya kibinadamu tu, bali pia wanaishi, wanatembea, na kupumua katika hali ya mambo machafu au ya kifisadi sana, na kila saa wakiitetea tabia yao kuhusiana na kila madhaifu ya asili yao ili kunyamazisha Ukweli (kuuzima), na kuipigia magoti mamlaka ya uasi. Je, si hivyo ndivyo mambo yalivyokwenda kwa upande wa Rumi? Je, sisi haturudii kuishi maisha yake 'Rumi' tena kwa mara nyingine? Tena, Je! tunaona nini huko mbele yetu hivi sasa? Ni Baraza kuu jingine, linalojumuisha wote! Mkutano mkuu wa ulimwengu! Huu ni Muungano wa wainjilisti, na imani moja ya ulimwengu wote! (Universal creed)" - Hubiri juu ya "The Bible a Sufficient Creed," lililotolewa Fort Wayne, Indiana, Feb. 22, 1846. Wakati lengo hili litakapofikiwa, ndipo, katika jitihada ya kujipatia mfanano, au umoja kamili wa makanisa, itakuwa ni hatua moja tu inayotakikana ili kufikia kwenye matumizi ya nguvu. [GC 444.3; PK Aya ya 30]

Wakati makanisa makubwa yaongozayo Marekani yakiungana juu ya vipengele kama hivyo vya mafundisho ya dini yanayoshikiliwa na wote, yatakapoishawishi serikali ya Marekani kulazimisha utekelezaji wa amri zao na kutegemeza taasisi zao kwa ajili ya uendeshaji wake, hapo ndipo Marekani ya Kiprotestanti itakapokuwa imefanya sanamu ya utawala wa kanisa Rumi (hierakia), na matokeo yasiyoepukika yatafuata mara moja, na hapo ndipo utoaji wa adhabu kali kwa msaada wa serikali ya kiraia kwa wale wanaotofautiana nao utatokea mara moja. [GC 445.1; PK Aya ya 31]

**Mnyama Na Sanamu Yake**

Naye mnyama mwenye pembe mbili "anawafanya wote, wadogo kwa wakubwa, na matajiri kwa maskini, na walio huru kwa watumwa, watiwe chapa katika mkono wao wa kuume, au katika vipaji vya nyuso zao; tena kwamba mtu awaye yote asiweze kununua wala kuuza, isipokuwa ana chapa ile, yaani, jina la mnyama yule, au hesabu ya jina lake." Ufunuo 13:16, 17. Onyo la malaika wa tatu ni hili: "Mtu awaye yote akimsujudu huyo mnyama na sanamu yake, na kuipokea chapa katika kipaji cha uso wake, au katika mkono wake, yeye naye atakunywa katika mvinyo ya ghadhabu ya Mungu." "Mnyama" anayetajwa katika ujumbe huu, ambaye ibada yake inalazimishwa na huyu mnyama mwenye pembe mbili, ni yule mnyama wa kwanza, mnyama anayefanana na chui wa Ufunuo 13--upapa. "Sanamu ya mnyama" huuwakilisha mfumo wa Uprotestanti ulioasi utakaojengeka wakati ule makanisa ya Kiprotestanti yatakapotafuta msaada kutoka kwa mamlaka ya kiserikali kwa ajili ya kusukuma mbele utekelezaji mafundisho yao ya dini. "Alama au Chapa ya Mnyama" Ndiyo bado haijafasiliwa (inangojewa kuonekana kwamba itatokezaje, unabii mwingine ni mpaka utokee ndiyo ujulikane). [GC 445.2; PK Aya ya 32]

Baada ya onyo hilo dhidi ya kumwabudu mnyama (upapa) na sanamu yake (Uprotestanti Ulioasi mafundisho ya Biblia), unabii huo unaeleza hivi: "Hapa ndipo penye subira ya watakatifu, hao wazishikao amri za Mungu, na imani ya Yesu" Kwa kuwa wale wazishikao amri za Mungu wanatofautishwa kwa njia hiyo na wale wanaomsujudu mnyama na sanamu yake na kupokea chapa (alama) yake, basi, ina maana ya kwamba kule kuishika Sheria ya Mungu (Amri Kumi), kwa upande mmoja, na kuivunja, kwa upande mwingine, kutakuwa ndiyo tofauti kati ya wale wanaomwabudu Mungu na wale wanaomwabudu mnyama. [GC 445.3; PK Aya ya 33]

Sifa ya pekee ya mnyama huyo, na hivyo sanamu yake, ni kuzivunja amri za Mungu. Danieli anasema hivi kuhusu PembeNdogo (– Dan. 7:24): "Naye ataazimu kubadili majira na Sheria (za Mungu)." Danieli 7:25. Naye Paulo aliipa jina mamlaka hiyo kuwa ni "mtu wa dhambi au mwana wa uasi" ambaye angejiinua mwenyewe dhidi ya Mungu (2 Wathesalonike 2:4). Unabii huo mmoja unaongezea unabii mwingine na kuukamilisha. Ni kwa kubadili Sheria ya Mungu pekee ndiko kungeufanya upapa uweze kujiinua juu ya Mungu; mtu yeyote ambaye, huku akijua, angeshika amri iliyobadilishwa, angekuwa anatoa heshima kuu isiyo na kifani kwa mamlaka hiyo ambayo ilifanya badiliko hilo. Tendo kama hilo la kutoa utii kwa sheria za kipapa lingekuwa alama ya utii kwa papa badala ya utii kwa Mungu. [GC 446.1; PK Aya ya 34]

Upapa umejaribu kubadili Sheria ya Mungu. Amri ya pili, inayokataza kuabudu sanamu, imeondolewa kabisa kutoka katika Sheria hiyo na amri ya nne imebadilishwa mno ili kuidhinisha utunzaji wa siku ya kwanza ya juma (Jumapili) badala ya siku ya saba (Jumamosi) ya juma kama Sabato. Lakini waumini wa

upapa, wanadai kama sababu ya kuiondoa amri ya pili, kuwa sio ya muhimu, kwa kuwa imejumuishwa katika amri ya kwanza, na ya kwamba wao wanaitoa au kuiufundisha Sheria hiyo (Amri) sawasawa kabisa na Mungu alivyopanga ipate kueleweka kwa watu. Hili sio lile badiliko alilolitabiri nabii (Danieli 7:25). Hapo kuna badiliko la kukusudia kabisa, na kudhamiriwa nalo limewasilishwa hivi: "Naye ataazimu kubadili majira na Sheria" Badiliko lililofanyika katika amri ya nne (Kut. 20:8-11) linatimiza unabii huu kikamilifu. Kwa badiliko hili hapa, mamlaka pekee inayodaiwa kuhusika ni ile ya kanisa. Hapa mamlaka hiyo ya upapa, inajiweka yenyewe waziwazi juu ya Mungu. [GC 446.2; PK Aya ya 35]

**Ishara Ya Uweza Na Uumbaji**

Wakati ambapo watu wanaomwabudu Mungu watatambulishwa haswa, kwa heshima yao kwa kuitunza amri ya nne (Kutoka 20)- kwa kuwa hii ndiyo ishara ya uweza Wake wa uumbaji, tena ni ushuhuda wa madai yake ya majivuno kwa ajili ya kicho, ibada, na heshima kutoka kwa mwanadamu, kumsujudu Yeye, - watu wanaomwabudu au kumsujudu mnyama watatambulishwa kwa juhudi zao halisi za kuichana-chana kabisa kumbukumbu hiyo ya Muumbaji, na kutukuza au kuinua agizo la taasisi ya Rumi (Jumapili). Ilikuwa ni kwa ajili ya Jumapili ambapo upapa ulionesha madai ya kiburi chake *(Tazama Kiambatanisho);* na hitaji la kwanza la msaada wa mamlaka ya kiserikali ilikuwa ni kwa madhumuni ya kulazimisha kwa nguvu utunzaji wa Jumapili kama "Siku ya Bwana." Lakini Biblia inaelekeza kidole chake kwenye siku ya saba (Jumamosi), na wala sio kwenye siku ya kwanza (Jumapili) kama Siku ya Bwana. Kristo alisema: "Basi Mwana wa Adamu Ndiye Bwana wa Sabato pia." Amri ya nne hueleza hivi: " "Siku ya saba ni Sabato ya Bwana." Na kupitia kwa nabii Isaya Bwana anaiita siku hiyo: "Siku ya utakatifu Wangu." Marko 2:28; Isaya 58:13 *(Siyo ya Wayahudi). [GC 446.3; PK Aya ya 36]

Dai linalototolewa mara nyingi sana, lisemalo kwamba Kristo aliibadili Sabato linakanushwa na Maneno Yake Mwenyewe. Katika Hubiri Lake la Mlimani alisema "Msidhani ya kuwa nalikuja kuitangua torati au manabii; la, sikuja kutangua, bali kutimiliza. Kwa maana, amin, nawaambia, Mpaka mbingu na nchi zitakapoondoka, yodi moja wala nukta moja ya torati haitaoondoka, hata yote yatimie. Basi mtu ye yote atakayevunja amri moja katika hizi zilizo ndogo, na kuwafundisha watu hivyo, ataitwa mdogo kabisa katika ufalme wa mbinguni; bali mtu atakayezitenda na kuzifundisha, huyo ataitwa mkubwa katika ufalme wa mbinguni." Matthew 5:17-19. [GC 447.1; PK Aya ya 37]

Ni Ukweli unaokubaliwa na Waprotestanti kwamba Maandiko hayatoi idhini au mamlaka yoyote kwa ajili ya kuibadilisha Sabato. Jambo hilo limeelezwa waziwazi katika Machapisho yaliyotolewa na Chama cha Vijizuu cha Kiamerika (American Tract Society) na Umoja wa Kiamerika wa Shule ya Jumapili

(American Sunday School Union). Mojawapo ya vijitabu au kazi hizi hukiri kwamba {Kuna ukimya kabisa wa Agano Jipya kuhusu amri ya moja kwa moja au iliyo wazi kuhusu Sabato (jumapili), siku ya kwanza ya juma} au kuwapo kwa kanuni mahsusi kuhusu utunzaji wake." - George Elliott, The Abiding Sabbath, uk. 184. [GC 447.2; PK Aya ya 38]

Mwingine anasema: "Mpaka wakati wa kifo Chake Kristo, hakuna badiliko lolote lililowahi kufanywa katika siku hiyo;" tena "kwa kadiri kumbukumbu zinavyoonyesha, wao (Mitume) hawakutoa ... amri yoyote iliyo mahsusi inayoagiza kutupilia mbali Sabato ya siku ya saba (Jumamosi), na kuweka utunzaji wake siku ya kwanza ya juma (Jumapili)." - AE Waffle, The Lord's Day, uk. 186-188. [GC 447.2; PK Aya ya 39]

Wakatoliki wa Rumi wanakiri kwamba badiliko hilo la Sabato (Jumamosi) lilifanywa na kanisa lao, nao wanatangaza kwamba Waprotestanti kwa njia ya kuishika Jumapili wanakiri mamlaka ya kanisa la Rumi. Katika Katekisimu ya Kikatoliki ya Dini ya Kikristo (Catholic Catechism of Christian Religion), ikijibu swali kuhusu siku gani inayopaswa kutunzwa ili kuitii amri ya nne (Kut. 20:8-11), kauli hii imetolewa: "Katika kipindi cha Sheria ya zamani (Amri Kumi), Jumamosi ilikuwa ndiyo siku iliyokuwa imetakaswa; lakini kanisa (la Roma), likielekezwa na Yesu Kristo, na kuongozwa na Roho wa Mungu, limeiweka Jumapili badala ya Jumamosi; kwa hivyo sasa tunaitakasa siku ya kwanza ya juma (Jumapili), na sio siku ya saba ya juma (Jumamosi). Jumapili inamaanisha kwa watu, na sasa ndiyo Siku ya Bwana." [GC 447.4; PK Aya ya 40]

Kama ishara ya mamlaka ya Kanisa Katoliki, waandishi wengi ambao ni waumini wa upapa wanatumia dondoo hili "tendo lenyewe la kuibadili Sabato (Jumamosi) kuwa Jumapili, tendo ambalo Waprotestanti wameliruhusu na kukubaliana nalo;... kwa sababu kwa kuishika Jumapili, wanakiri mamlaka ya kanisa kuamuru Siku kuu, na kuwaamrisha chini ya dhambi." Henry Tuberville, An Abridgment of the Christian Doctrine, uk. 58. Ni nini basi maana ya badiliko hili la Sabato, kama sio ishara au chapa, ya mamlaka ya Kanisa la Rumi - yaani, "Chapa ya Mnyama". [GC 448.1; PK Aya ya 41]

**Madai Makuu Kuliko Yote**

Kanisa hilo la Rumi halijalitupilia mbali dai lake la ukuu kuliko wote; na ulimwengu pamoja na makanisa ya Kiprotestanti unapoikubali sabato iliyoanzishwa na kanisa hilo (Jumapili), na kuikataa Sabato ya Biblia (Jumamosi), kimsingi wanakubaliana kabisa na dai hilo (lisemalo kwamba papa ni mkuu kuliko wote duniani). Wanaweza kudai mamlaka yatokanayo na mapokeo, pamoja na mamlaka ya Mababa (Fathers) kwa ajili ya badiliko hilo; lakini kwa kufanya hivyo wanaipuuzia kanuni ile ya msingi hasa ambayo inawatenga wao mbali na Rumi- - isemayo kwamba, Biblia, na Biblia peke yake, hiyo ndiyo dini ya Waprotestanti."

“Muumini wa mfumo wa upapa anaweza kuwaona hao Waprotestanti kuwa wanajidanganya wenyewe, kwa hiari, na kwa makusudi, kwani wanafumba macho yao kwa kuchagua wenyewe, wasiuone Ukatika suala hili (Eze. 22:26). Harakati inayotaka utunzaji wa Jumapili ulazimishwe kisheria, inavyozidi kupata upendeleo kwa kasi (kwa kukubalika na wengi), mfuasi huyo wa papa anashangilia, akiwa na hakika kuwa hatimaye (Jumapili hiyo) itauleta Ulimwengu wote wa Kiprotestanti kuwa chini ya bendera ya Roma. [GC 448.2; PK Aya ya 42]

Waumini wa Uroma wanatangaza kwamba “utunzaji wa Jumapili unaofanywa na Waprotestanti ni heshima wanayoitoa katika kusujudia mamlaka ya Kanisa Katoliki, wakiwa wanajipinga wenyewe.” - Mgr. Segur, Plain Talk About the Protestantism of Today, uk. 213. Utekelezaji wa ulazimishaji wa utunzaji wa Jumapili kwa upande wa makanisa ya Kiprostestanti ni ulazimishaji watu kuusujudu upapa - yaani, kumwabudu yule mnyama. Wale ambao wanayaelewa madai ya amri ya nne (Kut. 20:8-11), na bado wanachagua kuitunza sabato ya uongo badala ya Sabato ya Kweli, na kwa njia hiyo wanaheshimu mamlaka ya Rumi, ambayo ndiyo pekee yaliamuru kuitunza siku hiyo. Lakini katika tendo lilo hilo la kulazimisha wajibu wa kidini kwa kutumia mamlaka ya serikali ya kiraia, makanisa hayo ya Kiprotestanti kwa upande wao wenyewe watafanya sanamu ya mnyama; kwa hiyo, ulazimishaji wa utunzaji wa Jumapili kisheria katika nchi ya Marekani utakuwa ni ulazimishaji kisheria wa ibada ya mnyama na sanamu yake. [GC 448.3; PK Aya ya 43]

Lakini, basi, Wakristo wa vizazi vilivyopita waliitunza Jumapili wakidhani kwamba kwa kufanya hivyo walikuwa wanaitunza Sabato ile ya Biblia; na tena hata sasa wapo Wakristo wa Kweli katika kila kanisa, ikiwa ni pamoja na jumuia ya kanisa la Roma, ambao kwa moyo wa dhati wanaamini kwamba Jumapili ni Sabato iliyowekwa na Mungu. Mungu anakubali udhati wa kusudi lao litokanalo na unyofu wao wa moyo na uadilifu wa mioyo yao mbele Zake. Lakini ushikaji huo wa Jumapili utakapolazimishwa kwa sheria iliyotungwa na Bunge, na ulimwengu wote utakapokuwa umeangaziwa nuru kuhusu madai ya Sabato ya Kweli inayowafunga watu wote, hapo ndipo yeyote yule atakayeivunja amri hiyo ya Mungu, ili kuitii amri hiyo isiyokuwa na mamlaka ya juu zaidi ya yale ya Roma, atakuwa kwa njia hiyo anauheshimu upapa kuliko Mungu. Atakuwa anaisujudu/anaiheshimu Rumi pamoja na mamlaka inayoshinikiza (utunzaji wa Jumapili) agizo hili ili kulazimisha utunzaji wa siku iliyowekwa na taasisi ya Roma. Mtu huyo anamsujudu mnyama na sanamu yake. Wakati wanadamu watakapoikataa kabisa taasisi ya siku ya Sabato aliyoitangaza Mungu kwamba ni ishara ya mamlaka yake, na badala yake kuiheshimu siku iliyochaguliwa na Rumi kuwa alama ya ukuu wake usio na kifani, watakuwa kwa njia hiyo wameipokea alama ya utii wao kwa Rumi “Alama (Chapa) ya Mnyama” Tena jambo hilo halitakuwa hivyo mpaka suala hilo litakapokuwa limewekwa mbele ya watu wote

wazi, kama ilivyoelezwa, nao watafikishwa mahali pa kuchagua kati ya amri za Mungu na amri za wanadamu, ndipo wale watakaoendelea kuzivunja Amri* hizo za Mungu watakapopokea “Alama ya Mnyama.” *(mnyama ni upapa na sanamu yake ni Uprotestanti ulioasi Amri za Mungu, na Sheria, Shuhuda, Kanuni, Maagizo na Neno Lake) [GC 449.1; PK Aya ya 44]

**Onyo La Malaika Wa Tatu**

Tishio la kuogofya mno lililopata kutolewa dhidi ya wanadamu walio na hali ya kufa,linapatikana katika Ujumbe wa Malaika wa Tatu. Hiyo lazima iwe ni dhambi ya kutisha mno ambayo inasababisha ghadhabu ya Mungu isiyochanganywa na rehema Yake kushuka chini toka mbinguni. Watu hawapaswi kuachwa gizani kuhusu jambo hili la muhimu; onyo dhidi ya dhambi hiyo linapaswa kutolewa kwa ulimwengu mzima kabla ya kupatilizwa na hukumu hizo za Mungu, ili wote wapate kujua kwa nini watateswa kwa hizo hukumu, na hivyo kuwawezesha kupata fursa ya kuzikwepa. Unabii unatangaza kwamba malaika wa kwanza alipaswa kulitoa tangazo lake kwa “kila taifa na kabila na lugha na jamaa” (Ufu. 14:6). Onyo la Malaika wa Tatu (Ufu. 14:9-11), ambalo ni sehemu ujumbe ule ule wenye sehemu tatu, Halipaswi kuenea kwenye eneo dogo kuliko hilo,na hivyo litaaenda kwa “kila taifa na kabila na lugha na jamaa”. Katika unabii huo limewakilishwa kuwa litatangazwa kwa sauti kuu na malaika yule arukaye katikati ya mbingu([Ufu. 14:6; 18:1,2); nalo litakuwa na uwezo wa kuvuta usikivu wa ulimwengu mzima. [GC 449.2; PK Aya ya 45]

Katika shindano hili, Ulimwengu wote wa Kikristo utagawanyika katika matabaka makubwa mawili – wale wazishikao amri za Mungu na imani ya Yesu kwa upande mmoja, na wale wanaomwabudu mnyama na sanamu yake na kupokea chapa (alama) yake kwa upande wa pili. Ijapokuwa kanisa na serikali vitaunganisha uwezo wao ili kuwalazimisha watu kwa kutumia nguvu za dola “wote, wadogo kwa wakubwa, na matajiri kwa maskini, na walio huru kwa watumwa” (Ufunuo 13:16), kupokea “chapa ya mnyama,” hata hivyo, watu wa Mungu hawataipokea. Nabii wa Patmo aliona “wale waliokuwa wamejipatia ushindi wao dhidi ya mnyama, na dhidi ya sanamu yake, na dhidi ya alama yake,* na kwa hesabu ya jina lake, walikuwa wamesimama kandokando ya hiyo bahari ya kioo, wenye vinubi vya Mungu,” nao wakiimba wimbo wa Musa na wimbo wa Mwana-Kondoo. Ufunuo 15:2, 3, (Ufu. 13:18) *(Jumapili). [GC 449.3; PK Aya ya 46]

# SURA YA 26

# WATETEZI WA ILE KWELI

**(Kazi Ya Matengenezo, Kutengenza Palipobomoka,Kurejeshwa Kwa Msingi Isaya 58)**

Ufupisho: Biblia ni hazina ya Kweli zenye thamani. Tushukuru kwamba maarifa hayo ya Mungu yako mbele yetu ili tuyasome na kuyaishi. Katika sura hii tutajifunza sehemu ya mpango wa Mungu wa kurejesha Kweli zilizosahaulika ambazo zinahitajika leo. MUNGU wetu ni Mungu mkuu, tunapojifunza Neno Lake na kumwamini atuongoze, Yeye atatufungulia njia zitakazotupeleka mpaka mji wa Mfalme mkuu, kwenye makao mazuri anayotuandalia.

Kazi ya matengenezo ya Sabato (Jumamosi) itakayotekelezwa katika siku za mwisho ilitabiriwa katika unabii wa Isaya: "Bwana asema hivi, shikeni hukumu, na fanyeni hukumu; kwa maana wokovu Wangu u karibu kuja, na haki Yangu kufunuliwa. Heri mtu afanyaye haya, na mwanadamu ayashikaye; na mwana wa binadamu aishikaye; aishikaye Sabato asiitie unajisi, auzuiaye mkono wake usifanye uovu wowote." "Wana wa wageni, walioambatana na Bwana, ili kumtumikia, na kulipenda Jina la Bwana, na kuwa watumishi Wake, kila mtu aishikaye Sabato asiitie unajisi, na kulishika sana agano Langu; hao nitawaleta hata mlima Wangu mtakatifu, na kuwafurahisha katika nyumba Yangu ya sala." Isaya 56:1, 2, 6, 7. [GC 451.1; PK Aya ya 1]

Maneno haya yanaelezea uhalisia katika zama za Ukristo, kama unavyooneshwa katika muktadha huu: “Bwana Mungu akusanyaye waliofukuzwa na wasiojaliwa katika Israeli asema, Pamoja na hayo nitamkusanyia na wengine, zaidi ya hao walio Wake waliokusanywa” Mstari wa 8. Hapa pametabiriwa kuwa ukusanyaji wa mataifa kwa njia ya injili utafanyika. Na kwa wale wanaoiheshimu Sabato (Jumamosi) mbaraka umetangazwa. Hivyo madai ya utunzaji wa amri ya nne yanadumu kuwepo hata baada ya kusulubishwa, kufufuka na kupaa Kwake Kristo hadi wakati ambapo watumishi Wake watapolazimika kuhubiri kwa mataifa yote ujumbe huo wa habari njema ya furaha.[GC 451.2; PK Aya ya 2]

Bwana anatoa agizo kupitia kwa nabii huyo huyo “Ufunge huo ushuhuda, funga sheria kati ya wanafunzi Wangu.” lsaya 8:16. Muhuri wa Sheria ya Mungu unapatikana katika amri ya nne (Kutoka 20:8-11). Ni amri hii peke yake kati ya zote kumi, ndiyo ambayo huonyesha wazi Jina na Cheo cha Mtoa-Sheria hiyo. Inamtangaza Yeye kuwa Ndiye Muumbaji wa mbingu na dunia na hivyo huonyesha dai Lake la kupewa kuheshimiwa na kuabudiwa juu ya miungu yoyote mingine. Kando na amri hii, hakuna kitu chochote kingine katika Maagizo haya ya Sheria kinachoonyesha ni kwa mamlaka ya nani Amri hizo zimetolewa. Wakati Sabato ilipobadilishwa na mamlaka ya upapa, muhuri uliondolewa kutoka katika sheria hiyo. Wanafunzi wa Yesu wameitwa kuurejesha muhuri huo mahali pake sahihi kwa kuinua Sabato ya amri ya nne inavyostahili kama kumbukumbu ya Muumbaji na ishara ya mamlaka Yake. [GC 451.3; PK Aya ya 3]

“Na waende kwa sheria na kwa ushuhuda.” Ingawa mafundisho na nadharia zinazokinzana zipo nyingi na kuzagaa kila mahali, sheria ya Mungu ndiyo mwongozo usiokosea kamwe, ambapo kwa hiyo maoni yote, mafundisho yote ya dini na nadharia zote zinapaswa zipimwe (kujaribiwa). Nabii anasema hivi: "Ikiwa hawasemi sawasawa na Neno hili, ni kwa sababu hamna nuru ndani yao." Isaya 8:20. [GC au PK 452.1]

Kwa mara nyingine tena, amri hii imetolewa: “Piga kelele, usiache, Paza sauti yako kama tarumbeta; Uwahubiri watu wangu kosa lao, Na nyumba ya Yakobo dhambi zao.” Siyo ulimwengu wa waovu ndiyo unapaswa kukemewa kwa uvunjaji wa sheria (Amri kumi) bali ni wale ambao Bwana anawaita “watu Wangu” ambao inapasa waambiwe makosa yao. Anaendelea kuelezea zaidi kwa kusema “Walakini wanitafuta kila siku; hupenda kujua njia Zangu; kama vile taifa waliotenda haki, wasioacha sheria ya Mungu wao.” Isaya 58:1, 2. Hapa limedhihirishwa tabaka la watu wanaojiona wenyewe kuwa ni wenye haki (waadilifu), na kuonekana kana kwamba wana usongo sana wa kujishugulisha na huduma au kazi ya Mungu; lakini onyo kali na zito la Yule Mchunguzaji wa mioyo linathibitisha kuwa wanazikanyaga amri za Mungu chini ya miguu yao, Mungu anawaona kuwa wao ni wavunjaji wa Amri Zake. (1 Yoh. 2:3,4]). [GC 452.2; PK Aya ya 4]

## Mahali Palipobomoka Katika Ukuta

Hivyo unabii huo unasonda kidole chake kwenye amri ambayo imeachwa "Utaiinua misingi ya vizazi vingi; nawe utaitwa, Mwenye kutengeneza mahali palipobomoka; na, Mwenye kurejeza njia za kukalia, Kama ukigeuza mguu wako usihalifu Sabato, usifanye anasa yako siku ya utakatifu wangu; ukiita Sabato siku ya furaha, na siku takatifu ya Bwana yenye heshima; ukiitukuza, kwa kutokuzifanya njia zako mwenyewe, wala kuyatafuta yakupendezayo, wala kusema maneno yako mwenyewe; ndipo utakapojifurahisha katika Bwana; Nami nitakupandisha mahali pa nchi palipoinuka; nitakulisha urithi wa Yakobo baba yako; kwa maana kinywa cha Bwana kimenena hayo" fungu la Isaya 58:12-14. Unabii huu unahusu wakati wetu pia. Hali ya kubomolewa, ambayo ni upotoshaji wa Sheria ya Mungu ulifanywa wakati Sabato ilipobadilishwa na mamlaka ya Kirumi/Kiroma.* Lakini wakati umewadia ambapo amri hiyo ya Mungu inapaswa irudishwe mahali pake. Mahali pale palibomoka, ni kielelezo kinachosimamia upotoshaji, na lazima parekebishwe/pakarabatiwe, na msingi wa vizazi vingi ni lazima uinuliwe *(Sheria ni Ukuta kutokana na Maandiko). [GC 452.3; PK Aya ya 5]

Ikiwa imetakaswa kwa pumziko na mbaraka wa Muumbaji, Sabato ilitunzwa na Adamu katika hali yake ya kutokuwa na hatia (dhambi) yoyote ndani ya Edeni takatifu; Ilitunzwa na Adamu, aliyeanguka dhambini lakini aliyekuwa ametubu, baada ya kufukuzwa kutoka katika milki yake ya Edeni, iliyomletea raha. Ilitunzwa na wazee wote wa imani, kuanzia kwa Habili hadi Nuhu mwenye haki, hadi kwa Ibrahimu, hadi Yakobo. Wakati wateule walipokuwa utumwani Misri, wengi wakiwa katikati ya ibada ya sanamu iliyoenea kote, walisahau ujuzi wao wa Sheria ya Mungu; lakini Bwana alipowakomboa Israeli alitangaza Sheria Yake (Amri Kumi Sinai) kwa utukufu wa kutisha mno kwa umati uliokusanyika, ili wapate kuyajua mapenzi Yake (Mhu. 12:13; Zab. 40:8] na kumcha na kumtii Yeye milele. [GC 453.1; PK Aya ya 6]

Kutokea siku ile alipotangaza sheria Yake hadi leo hii, maarifa ya Sheria ya Mungu (Amri Kumi) yamehifadhiwa hapa duniani, na Sabato ya amri ya nne imetunzwa Ingawa yule "mtu wa uasi" alifanikiwa kuikanyaga chini ya miguu yake siku hiyo takatifu ya Mungu, lakini hata katika kipindi chake cha kushika ukuu na kutawala (papal supremacy) palikuwako na watu waliokuwa waaminifu ambao walijificha mahali pa siri, walioiheshimu siku hiyo ya Sabato. Tangu wakati wa Matengenezo ya Kanisa, wamekuwepo baadhi ya watu katika kila kizazi waliodumu kuiadhimisha/kuitunza. Ingawa mara nyingi walijikuta katikati ya dhihaka na mateso, ushuhuda wao umedumu kutolewa daima kuhusu uendelevu wa Sheria ya Mungu (Amri Zake) na wajibu mtakatifu wa wanadamu wa kuitunza Sabato hiyo ya uumbaji (Jumamosi). [GC 453.2; PK Aya ya 7]

Ukweli huu, kama ulivyoelezwa katika Ufunuo 14 kuhusiana na "injili ya milele," utalitambulisha Kanisa la Kristo wakati wa kuja Kwake kwa mara ya pili. Kwa kuwa kama matokeo ya ujumbe huo wa sehemu tatu tangazo imetangazwa hivi: "Hapa ndipo penye subira ya watakatifu, hao wazishikao amri za Mungu na imani ya Yesu" (fungu la 12). Na ujumbe huo ndio wa mwisho kutolewa kabla ya kuja kwake Bwana kwa mara ya pili. Mara tu baada ya utangazaji wa ujumbe huo Mwana wa Adamu anaonwa na nabii huyo akija katika utukufu ili kuvuna mavuno ya dunia (Ufu. 14). [GC 453.3; PK Aya ya 8]

**Uzuri Na Mwafaka Kamili Wa Ukweli**

Wale walioipokea nuru kuhusiana na Patakatifu na kutobadilika kamwe kwa Sheria ya Mungu walijawa na furaha na mshangao walipouona uzuri na mwafaka wa mfumo wa Ukweli uliofunuliwa katika ufahamu wao. Walitamani kwamba nuru ya Kweli iliyoonekana kwao kuwa ya thamani mno, ingeweza kugawiwa kwa Wakristo wote-kusambazwa; nao waliamini kabisa kwamba ungeweza kupokelewa kwa furaha. Lakini Kweli zile ambazo zingewafanya wahitilafiane/watofautiane na ulimwengu hazikukaribishwa au kupendwa na wengi waliodai kuwa wafuasi Wake Kristo. Utii wa amri ya nne (Kut. 20:8-11) ulihitaji kafara ambayo walio wengi walirudi kinyumenyume ili wasijihusishe.[GC 454.1; PK Aya ya 9]

*Madai ya Sabato (Jumamosi) yalipowasilishwa, wengi walitoa hoja kufuatana na mtazamo wa kidunia. Wakisema hivi: "Sikuzote sisi tumeitunza Jumapili, baba zetu waliitunza, na watu wengi wema na wacha Mungu walikufa kwa furaha huku wakiwa wanaitunza. ikiwa wao walikuwa sahihi, basi, na sisi tuko sahihi pia. Utunzaji wa Sabato hii mpya (Jumamosi) utatuondoa sisi nje ya maelewano/ mwafaka na ulimwengu, na hivyo tutapoteza mvuto wetu kwa ulimwengu. Hivi lile kundi dogo linaloitunza siku hiyo ya saba (Jumamosi) linaweza kuwa na tumaini la kufanya nini dhidi ya ulimwengu wote unaoendelea kuitunza Jumapili?" Ilikuwa ni kwa hoja zinazofanana na hizo, ndivyo Wayahudi walijitahidi kujihesabia haki kwa kumkataa kwao Kristo. Baba zao walikuwa wakikubaliwa na Mungu kwa kutoa matoleo yao ya sadaka za kuteketezwa za wanyama, basi, kwa nini watoto wasipate wokovu kwa kufuata njia ile ile waliyoipita baba zao? Kwahiyo, katika wakati wa Luther, wafuasi wa upapa walitoa hoja zile zile kwamba Wakristo wa kweli walikuwa wamekufa katika imani ya Kikatoliki, na hivyo dini ile ilikuwa inatosha kwa wokovu. Hoja kama hizo zitajionesha kuwa ni kipingamizi kikubwa dhidi ya uzuiaji wa maendeleo yote ya ukuaji katika imani,utendaji wa maisha ya kidini.

**Wakati Uliowekwa Na Wanadamu Unaoheshimiwa**

Wengi walidai kwamba utunzaji wa Jumapili ulitokana na fundisho lililokuwa kamili na desturi ya kanisa iliyoendelea kujulikana mahali pengi, na iliyodumu karne nyingi. Kinyume cha hoja hii, ilionyeshwa kwamba, Sabato na utunzaji wake vilikuwa vya zamani zaidi na vilivyoenea mahali pote, hata ilikuwa na umri sawa na umri wa dunia yenyewe, na ilikuwa na idhini ya malaika na Mungu pia, wakati misingi ya dunia ilipowekwa, nyota za asubuhi zilipoimba pamoja, na wana wote wa Mungu walipopiga kelele kwa furaha ndipo msingi wa Sabato ulipowekwa, Ayubu 38:6, 7; Mwanzo 2:1-3. Naam, siku hii inadai heshima yetu kihalali kabisa, na haikuanzishwa na mamlaka yoyote ya kibinadamu wala kujengwa juu ya mapokeo ya kibinadamu, ilianzishwa na Mzee wa Siku na kuamriwa kwa Neno Lake la milele. [GC 454.3; PK Aya ya 10]

Wakati usikivu wa watu ulipoitwa kutafakari somo la Matengenezo ya Sabato (Sabbath Reform), wachungaji mashuhuri waliopendwa na wengi walilipotosha Neno la Mungu wakitoa tafsiri kuhusu ushuhuda wa Sabato kwa jinsi ambavyo ingewanyamazisha na kuwatuliza wale waliokuwa wakiuliza maswali ili wapate kujua Ukweli. Na wale ambao hawakuchunguza Maandiko kwa ajili yao wenyewe binafsi, walitosheka kukubaliana na mahitimisho yaliyopatana na matakwa yao. Kwa njia ya mijadala, mabishano, ulaghai, mapokeo ya Mababa, na mamlaka ya kanisa, wengi walijitahidi kuupindua Ukweli. Wale waliokuwa mawakala wa Sabato, walisukumwa kuichunguza Biblia zaidi ili waweze kutetea uhalali wa amri ya nne (Kutoka 20:8-11). Watu duni na wanyenyekevu, walikuwa wamevaa silaha ya Neno la Ukweli pekee yake, walikabiliana na mashambulizi ya watu wenye visomo, ambao, kwa mshangao na hasira, waliona kwamba ustadi wa maneno yao fasaha ya ulaghai, haukufua dafu dhidi ya watu sahili, walio na elimu ndogo, ambao kwa hekima yao isiyopinda-pinda walibobea katika ujuzi wa kina wa Maandiko badala ya werevu ambao kiuhalisia ulikuwa ni udangayifu uliofundishwa mashuleni (au vyuo vya theolojia). [GC 455.1; PK Aya ya 11]

Kwa kukosa kwa ushuhuda wa Biblia uliowaunga mkono hoja zao, wengi waliendelea kwa bidii bila ya kuchoka—wakiwa wamesahau jinsi hoja zile zile zilivyokuwa zimetumiwa dhidi ya Kristo na mitume Wake, wakasisitiza wakisema: “Kwanini watu wetu mashuhuri hawaelewi lolote kuhusu suala hili la Sabato? Lakini ni wachache mno wanaoamini kama ninyi mnavyoamini. Haiwezekani kwamba ninyi ndio muwe sahihi na kwamba wasomi wote ulimwenguni wawe wamekosea.” [GC 455.2; PK Aya ya 12]

Kuzikanusha hoja kama hizo ilihitajika kutumia mafundisho ya Maandiko na historia ya jinsi Bwana alivyowatendea watu Wake katika zama na vizazi vyote. Mungu hufanya kazi kupitia kwa wale wanaoisikia na kuitii sauti Yake (Neno Lake) wale ambao, ikibidi, watasema Ukweli usiokuwa na ladha nzuri kwa watu wengi, wale ambao hawaogopi kukemea dhambi mashuhuri zinazopendwa na watu wengi. Sababu inayomfanya Bwana mara nyingi kutochagua wale wenye

visomo na nyadhifa za juu kuongoza vuguvugu za matengenezo ni kwamba wao wanategemea itikadi zao za dini (creeds), nadharia zao, na mifumo yao ya theolojia, na hufikiria kuwa hawana haja ya kufundishwa na Mungu. Ni wale tu walio na uhusiano binafsi na Chanzo cha Hekima ndiyo wawezao kuelewa na kuyafafanua Maandiko hayo (Dan. 12:10). Watu wale walio na kisomo kidogo tu cha madarasani, mara zingine huitwa kuutangaza Ukweli, si kwa kuwa hawana kisomo, bali ni kwa sababu hawajitegemei wenyewe kiasi cha kutofundishwa na Mungu. Wanajifunza katika shule ya Kristo, kisha ule unyenyekevu na utii wao, unawafanya kuwa wakuu. Katika kuwakabidhi maarifa ya Ukweli Wake, Mungu huwatunukia juu yao heshima, ambayo, kwa kuilinganisha, na hekima na heshima ya kidunia na ukuu wa kibinadamu vinazama na kupwelea sana kwa thamani. [GC 455.3; PK Aya ya 13]

**Kuipa Kisogo Nuru**

Walio wengi miongoni mwa Waadventista waliukataa Ukweli uliouhusu Patakatifu na Sheria ya Mungu (Amri Kumi), na wengi pia waliikana imani yao kuhusiana na vuguvugu la Majilio ya Yesu la 'Waadventista' na kuwa na maoni yasiyopelekana na Neno na Mungu, na yanayokinzana kuhusu unabii uliolihusu vuguvugu lile. Baadhi waliingia katika kosa la kurudia tena na tena tarehe maalumu ya kuja Kwake Kristo. Nuru ambayo sasa ilikuwa inanga'aa juu ya somo la Patakatifu ilipaswa kuwaonyesha kwamba hakuna kipindi chochote cha kiunabii ambacho kilifika hadi wakati wa ujio wa Kristo kwa mara ya pili; kwamba wakati mahususi/kamili wa ujio huu wa Yesu haujatabiriwa. Lakini wakiwa wameiacha nuru, waliendelea kupanga wakati/tarehe baada ya wakati/tarehe kwa ajili ya kuja Kwake Bwana, na mara nyingi walikatishwa tamaa. [GC 456.1; PK Aya ya 14]

Kanisa la Wathesalonike lilipoyapokea mawazo potofu juu ya kuja kwa Kristo, Mtume Paulo aliwashauri kuyapima matumaini na matarajio yao kwa makini kwa kutumia Neno la Mungu. Alirejelea dondoo kutoka katika unabii, ulioyafunua matukio yaliyokuwa hayana budi kutokea kabla ya kuja Kwake Kristo kwa mara ya pili, na alionyesha kwamba hawakuwa na sababu ya msingi ya kutegemea ujio Wake katika siku zao. "Mtu awaye yote asiwadanganye kwa njia yoyote" 2 Wathesalonike 2:3, hayo ni maneno yake ya onyo. Endapo wangeendekeza matarajio yaliyokuwa hayajapata kibali cha Maandiko, basi, wangeongozwa kuendelea kuchukua njia yenye makosa katika matarajio na utendaji wao; kukata tamaa kwa kukosa kuyapata waliyoyatarajia, hali hiyo ingewaanika wazi katika mahali ambapo wale wasioamini wangewadhihaki na kuwazomea, tena wangekuwa katika hatari ya kuvunjika moyo, kisha wangejaribiwa kusalimu amri kwa ukatishwaji tamaa huo na wangejaribiwa kutilia mashaka zile Kweli zilizokuwa muhimu kwa wokovu wao. Onyo na himizo hilo la Mtume kwa

Wathesalonike lina somo la maana ndani yake, kwa watu wanaoishi katika siku hizi za mwisho. Waadventista wengi waliona kwamba ikiwa wasingeweka imani yao juu ya tarehe mahususi ya kuja kwa Bwana wao, basi, wasingeweza kuwa na bidii au ari (motomoto), wala hawangeweza kuwa na bidii katika kazi yao ya maandalizi ya kuwa tayari. Lakini matumaini yao yanaposisimuliwa tena na tena, na kisha wakati wote yanazimwa kwa kukatishwa tamaa, imani yao inapata mshtuko mkali kiasi kwamba wanakaribia kupoteza uwezo wa kuamini Ukweli huu mkuu wa unabii. [GC 456.2; PK Aya ya 15]

Kule kuhubiri wakati mahsusi wa hukumu, katika kuutangaza ujumbe wa malaika wa kwanza, kuliagizwa na Mungu. Ukokotoaji wa vipindi vya kiunabii ambavyo vilikuwa msingi wa ujumbe ule, ukiweka mwisho wa siku zile 2300 (miaka ile) katika kipindi cha kupukutisha majani cha 1844 BK (Septemba-Novemba), unasimama bila kupingwa, yaani hauna dosari. Juhudi zilizorudiwa rudiwa mara kwa mara za kutafuta tarehe nyingine mpya kwa ajili ya mwanzo na mwisho wa vipindi vya kiunabii, na hoja zisizoridhisha zilizotumiwa ili kuunga mkono misimamo hiyo, siyo tu kuwa zilielekeza akili za watu kwenda mbali na Ukweli wa leo, lakini pia zilitupa dharau juu ya juhudi zote za kuelezea unabii. Kwa kadiri upangaji wa muda mahususi wa ujio wa Kristo unavyowekwa mara kwa mara, na kadri unavyofundishwa mahali pengi, ndivyo hali hiyo inavyofaa kwa ufanisi zaidi katika kutimiza makusudi ya Shetani. Baada ya tarehe hiyo kupita, Shetani huchochea dhihaka na dharau dhidi ya mawakala wanaoweka siku hizo mahsusi, na kwa njia hiyo analeta aibu juu ya vuguvugu kuu la ujio wa Kristo la mwaka ya mwaka 1843 na mwaka 1844. Wale wanaozidi kuendelea katika kosa hilo hatimaye wataweka tarehe iliyo mbele mno katika siku sijazo, kwa ujio Wake Kristo. Kwa njia hiyo wataongozwa kupumzika katika usalama bandia, tena wengi hawataachana na madanganyo hayo mpaka wajikute wamechelewa kabisa. [GC 456.2; PK Aya ya 16]

Historia ya Israeli ya zamani ni mfano wa kushangaza wa uzoefu wa siku za nyuma wa jamii ya Waadventista. Mungu aliwaongoza watu Wake waliokuwa katika vuguvugu ya ujio wa pili, kama vile alivyowaongoza wana wa Israeli toka Misri. Katika hali ya kukatishwa tamaa sana, imani yao ilijaribiwa kama imani ya Waebrania ilivyojaribiwa walipofika kwenye Bahari ya Shamu. Ikiwa wangeendelea kuutegemea na kuuamini mkono uliokuwa unaongoza, ambao ulikuwa pamoja nao katika uzoefu wao wa nyuma, basi, wangekuwa wameuona wokovu wa Mungu. Ikiwa watu wote waliokuwa wamehusika katika kazi kwa umoja mnamo mwaka wa 1844, basi wangekuwa wameupokea Ujumbe wa Malaika wa Tatu na kuutangaza kwa uweza wa Roho Mtakatifu, Bwana angelitenda matendo makuu pamoja na juhudi zao. Mafuriko ya nuru yangekuwa yameuangazia ulimwengu wote (Uf 18:1). Miaka mingi iliyopita wakazi wa ulimwengu huu wangekuwa wameonywa, na kazi ya kufunga historiaingekuwa

imekamilika, na Kristo angekuwa amerudi kwa ajili ya ukombozi wa watu Wake. [GC 457.1; PK Aya ya 17]

Haikuwa mapenzi ya Mungu kwamba Israeli watange-tange jangwani kwa miaka arobaini; Bwana alitamani kuwaongoza moja kwa moja hadi nchi ya Kanaani na kuwastawisha huko, na kuwafanya wawe watu watakatifu, na wenye furaha. Ila twaona kuwa “hawakuweza kuingia kwa sababu ya kutokuamini kwao" Waebrania 3:19. Kwa sababu ya kurudi nyuma kwao na uasi wao waliangamia jangwani, na wengine waliinuliwa na kuingia katika Nchi ya Ahadi. Kwa namna hiyo hiyo, hayakuwa mapenzi Yake Mungu kwamba ujio Wake Kristo ucheleweshwe kwa muda mrefu, na watu Wake waendelee kubaki kwa miaka mingi katika ulimwengu huu wenye dhambi na huzuni. Lakini kule kutokuamini kwao kuliwatenga mbali na Mungu. Walipokataa kufanya kazi ile ambayo Yeye alikuwa amewapangia, wengine waliinuliwa na kutangaza ujumbe ule. Kwasababu ya rehema Yake aliyonayo kwa ulimwengu huu (2 Pet. 3:9, 15), Yesu anachelewesha ujio Wake, ili wenye dhambi wapate fursa ya kulisikia onyo hilo na kupata hifadhi ndani Yake kabla ya ghadhabu ya Mungu kumiminwa. (Ufu 16). [GC 458.1; PK Aya ya 18]

Sasa, kama vile ilivyokuwa katika zama zilizopita, kuwasilisha Ukweli unaokemea dhambi na makosa ya wakati huu, kutaamsha upinzani. "Maana kila mtu atendaye mabaya huichukia nuru, wala haji kwenye nuru, matendo yake yasije yakakemewa" Yohana 3:20. Kadiri watu wanapoona kwamba hawawezi kuutetea msimamo au hoja zao kwa kutumia Maandiko, wengi hudhamiria kushikilia hata katika hatari au gharama zozote hoja hizo, na kwa roho ya hiana yenye kuwadhuru wengine, wanashambulia vibaya tabia pamoja na makusudi ya wale wanaosimama imara kuutetea Ukweli usiopendwa na watu wengi. Ni sera hiyo hiyo ambayo imetumiwa katika zama zote. Eliya alitangazwa kuwa mtaabishaji wa Israeli (1 Fal. 18:17), Yeremia aliitwa msaliti, Paulo aliitwa mtu anayelichafua hekalu. Tangu wakati ule hadi leo hii, wale ambao wanachagua kuwa watiifu kwa Ukweli wameshutumiwa kuwa ni wachochezi wa maasi dhidi ya serikali, wazushi, au waleta mifarakano. Watu wengi sana wasio na imani kabisa kiasi cha kutolikubali Neno imara lenye uhakika la unabii, watapokea kwa upesi bila ya kuwa na maswali, mashtaka yatakayotolewa dhidi ya wale wanaothubutu kuzikemea dhambi zile za kimtindo (zinazopendwa na watu). Roho ya aina hiyo itazidi kuongezeka zaidi na zaidi. Tena Biblia inafundisha waziwazi kwamba wakati unakaribia ambapo sheria ya nchi itakinzana vibaya mno na Sheria ya Mungu (Amri Kumi) kiasi kwamba yeyote atakayetaka kuzitii amri zote za Mungu itampasa kwa ujasiri kukabiliana na shutuma na adhabu kama mtenda mabaya au mtu mwovu. [GC 458.2; PK Aya ya 19]

Katika mazingira kama haya, Je, upi ni wajibu wa mjumbe wa Ukweli? Je! ahitimishe kuwa Ukweli huo haufai kuhubiriwa, kwa sababu mara nyingi matokeo

yake ni kuwachochea tu wanadamu kuyakwepa au kuyapinga madai yake? Hapana! Yeye hana sababu nyingine zaidi ya kuficha ushuhuda huo wa Neno la Mungu usitolewe, kama vile ulivyotolewa mapema na Wanamatengenezo, ati kwa sababu tu unaamsha upinzani. Kuikiri imani (Ungamo la imani) kulikofanywa na watakatifu na wafia dini kuliandikwa katika kumbukumbu kwa manufaa ya vizazi vilivyofuata. Mifano ile hai ya utakatifu na uadilifu usioyumba imehifadhiwa na kutufikia sisi, ili kuchochea moyo wa ujasiri kwa wale wanaoitwa sasa ili kusimama kama mashahidi Wake Mungu. Walipokea neema na Ukweli, si kwa ajili yao wenyewe tu, bali kwamba, kupitia kwao, ujuzi wa maarifa ya Mungu upate kuiangazia dunia nzima. Je, Mungu ametoa nuru kwa ajili ya watumishi Wake katika kizazi hiki? Basi ikiwa ni hivyo, inapasa waiachilie nuru hiyo, ili ipate kuuangazia ulimwengu mzima (Isa. 60:1, 2). [GC 459.1; PK Aya ya 20]

Zamani za kale Bwana alimtangazia yule aliyenena kwa Jina Lake kusema: “Nyumba ya Israeli hawatakusikiliza wewe; kwa kuwa hawanisikilizi Mimi.” Hata hivyo, aliendelea kusema: “Nawe utawaambia Maneno Yangu, kwamba watasikia, au kwamba hawataki kusikia.” Ezekieli 3:7; 2:7. Kwa mtumishi wa Mungu wa wakati huu amri hii inatolewa: “Paza sauti yako kama tarumbeta; uwahubiri watu Wangu kosa lao, na nyumba ya Yakobo dhambi zao” (Isa. 58:1). [GC 459.2; PK Aya ya 21]

### Tuko Chini Ya Uwajibikaji Wa Kuogofya

Kwa kadiri fursa zinavyozidi kuongezeka, kila mmoja aliyeipokea nuru ya Ukweli yuko chini ya wajibu ule ule mzito na wa kutisha kama aliokuwa nao nabii Ezekieli, ambaye kwake Neno la Bwana lilimjia, likisema: “Basi wewe, mwanadamu, nimekuweka kuwa mlinzi kwa nyumba ya Israeli; basi ulisikie Neno hili kinywani Mwangu, ukawape maonyo Yangu. Nimwambiapo mtu mbaya, Ewe mtu mbaya, hakika utakufa, nawe husemi Neno la kumwonya mtu huyo, aiache njia yake, mtu mbaya huyo atakufa katika uovu wake, lakini damu yake nitaitaka mkononi mwako. Walakini ukimwonya mtu mbaya kwa sababu ya njia yake, kusudi aiache; wala yeye asiiache; atakufa huyo katika uovu wake, lakini wewe umejiokoa roho yako." Ezekieli 33:7-9 [GC 459.3; PK Aya ya 22]

### Hoja Peke Yake Dhidi Ya Ile Kweli

Kikwazo kikuu dhidi ya mambo yote mawili, yaani, kuupokea na kuutangaza Ukweli, ni kuwa kwa kawaida Ukweli huwa unajumuisha usumbufu na aibu. Hii ndiyo hoja peke yake dhidi ya Ukweli ambao wale wanaoutetea Ukweli hawajapata kukanusha kamwe. Lakini jambo hili haliwazuii wafuasi wa kweli wa Kristo. Hawa hawangojei mpaka hapo Ukweli utakapopendwa na kuwa maarufu kwa watu wengi. Wakiishashawishika kuhusu wajibu wao, basi, wanadhamiria wenyewe kukubali kuubeba msalaba, wakihesabu pamoja na Mtume Paulo kuwa

“dhiki yetu nyepesi iliyo ya muda wa kitambo tu, yatufanyia utukufu wa milele uzidio kuwa mwingi sana;” pamoja na mtu yule zamani, “akihesabu ya kuwa kushutumiwa Kwake Kristo ni utajiri mkuu kuliko hazina za Misri” (za ulimwengu huu mwovu). 2 Wakorintho 4:17; Waebrania 11:26. [GC 460.1; PK Aya ya 23]

Haijalishi taaluma zao ni zipi, ni wale tu wanaoitumikia dunia hii kwa moyo wa dhati, ambao wanatenda kazi kutokana na sera zaidi kuliko kufuata kanuni katika masuala ya dini. Tunapaswa kuchagua Ukweli kwa sababu ni Ukweli, na kuacha matokeo mikononi mwa Mungu. Ulimwengu unapaswa kuwashukuru wale wanaosimama kidete juu ya kanuni, imani, na uthubutu kwa ajili ya matengenezo na mabadiliko makubwa yaliyofanywa Kupitia watu hawa, kazi hiyo ya matengenezo kwa wakati huu haina budi isonge mbele. [GC 460.2; PK Aya ya 24]

Bwana asema hivi: “Nisikilizeni, ninyi mjuao haki, watu ambao mioyoni mwenu mna sheria Yangu; msiogope matukano ya watu, wala msifadhaike kwa sababu ya dhihaka zao. Maana nondo itawala kama vazi, na funza atawala kama sufu; bali haki Yangu itakuwa milele na wokovu wangu hata vizazi vyote" Isaya 51:7, 8. [GC 460.3; PK Aya ya 25]

*Katika kiini chenyewe kabisa cha ile Dekalojia (Amri Kumi Kutoka 20:8-11) kuna amri ya nne, kama ilivyotangazwa awali. Soma ili uielewe vizuri hapa chini “Ikumbuke Siku ya Sabato [Jumamosi] uitakase. Siku sita [kuanzia Jumapili mpaka Ijumaa–Eze. 46:1] fanya kazi, utende mambo yako yote; lakini Siku ya Saba [Jumamosi] ni Sabato YA BWANA, Mungu wako [si ya Wayahudi], siku hiyo usifanye kazi yo yote, wewe, wala mwana wako, wala binti yako, wala mtumwa wako, wala mjakazi wako, wala mnyama wako wa kufuga, wala mgeni aliye ndani ya malango yako. Maana, kwa siku sita [Jumapili hadi Ijumaa–Mwanzo 1:5,8,13,19,23,31], BWANA alifanya mbingu, na nchi, na bahari, na vyote vilivyomo, akastarehe [akapumzika] Siku ya Saba [Jumamosi – Mwa. 2:1-3]; kwa hiyo BWANA akaibarikia siku ya Sabato akaitakasa [akaitenga kwa matumizi matakatifu ya ibada].” Kutoka 20:8-11. Roho wa Mungu aliigusa sana mioyo ya wanafunzi wa Neno Lake. Walisadikishwa kabisa kwamba kwa ujinga wao walikuwa wameivunja amri hiyo kwa kutoijali siku hiyo ya mapumziko aliyoiweka Muumbaji wao. Wakaanza kuzichunguza sababu za kuitunza siku ya kwanza ya juma [Jumapili] badala ya kuitunza siku [Jumamosi] ile aliyoitakasa Mungu. Hawakuweza kupata ushahidi wowote katika Maandiko ulioonyesha kwamba amri ya nne ilikuwa imefutwa, au kwamba Sabato [Jumamosi] ilikuwa imebadilishwa; baraka ile iliyoitakasa siku ya saba [Jumamosi] mara ile ya kwanza ilikuwa haijapata kuondolewa Naye kamwe. Kwa unyofu wao wa moyo walikuwa wakitafuta kuyajua na kuyafanya mapenzi ya Mungu [Amri Kumi]; basi walipong’amua wenyewe ya kwamba walikuwa wavunjaji wa Sheria yake [Amri

Kumi], huzuni ikaijaza mioyo yao, nao wakaonyesha utiifu wao kwa Mungu kwa kuitakasa Sabato [Jumamosi] Yake.

# SURA YA 27

# UAMSHO WA KISASA

**(Funguo za Ufalme)**

Ufupisho: Nini kimetokea kwenye wakati wetu? Huduma ambazo hazihudumii watu ila zinapenda matumbo na maoni yao. Uamsho ambao hauamshi. Ila Uamsho wa zamani ulileta uchunguzi wa kina wa moyo—Lakini nyakati zetu zimebadilika. Udunia unaingia kanisani. Ni nini kimetokea na kwa nini kimetokea?

Mahali popote ambapo Neno la Mungu lilihubiriwa kwa uaminifu, matokeo yaliyofuata yalithibitisha kwamba Neno asili yake ni Mwenyezi Mungu Mwenyewe (mbingu). Roho wa Mungu alifuatanana ujumbe wa watumishi Wake na Neno lilikuwa na nguvu. Wenye dhambi walihisi dhamiri zao zikihuishwa. Yule "Nuru Halisi, imtiayo nuru kila mtu, ajaye katika ulimwengu" aliangazia vyumba vya siri vya mioyo ya watu na mambo yale yaliyofichika ya giza yalianikwa wazi. Usadikisho wa kina uligusa akili na mioyo yao. Walisadikishwa kuhusu dhambi na

haki na hukumu inayokuja. Walipata ufahamu wa haki ya Yehova na waliona hofu ya kutokea Kwake, katika hatia na uchafu wao, mbele ya Mchunguzi wa mioyo yao. Basi, kwa uchungu walipaza sauti wakilia: “Ni nani atakayeniokoa na mwili huu wa mauti?” Msalaba wa Kalvari, pamoja na kafara Yake isiyo na kikomo kwa ajili ya dhambi za wanadamu, ulipofunuliwa kwao, waliona kuwa hakuna kitu kingine isipokuwa haki ya Kristo pekee, kuwa Ndiyo ingetosha kufanya upatanisho wa dhambi zao; haki ya Kristo pekee, ndiyo ingeweza kumpatanisha mwanadamu na Mungu. Kwa imani na unyenyekevu walimpokea Mwana-Kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu. Kwa njia ya damu ya Yesu walipata “ondoleo la dhambi zilizopita.” [GC 461.1; PK Aya ya 1]

Roho hizi zilileta matunda yapasayo toba. Waliamini na kubatizwa na waliinuka na kutembeaa katika upya wa uzima, wakawa viumbe vipya katika Kristo Yesu; wakiachana na maisha yao ya zamani, waliyoishi kwa kufuata tamaa za mwili, waliishi kwa imani ya Mwana wa Mungu wakizifuata nyayo Zake, wakiakisi tabia Yake, na kujitakasa kama Yeye alivyo mtakatifu. Mambo waliyokuwa wakiyachukia awali sasa waliyapenda na mambo waliyoyapenda hapo awali, sasa wanayachukia. Wenye kiburi, wenye kujikweza na kujitumaini wenyewe waligeuka na kuwa wapole na wanyenyekevu wa moyo. Watu wenye ubatili na majivuno na kudharau wengine wakawa watu makini na wasiopenda kujitanguliza mbele au kujionyesha. Watu waliomkufuru Mungu walibadilika na kuwa wacha Mungu, walevi wakaacha vileo, na waasherati wakawa na maisha safi. Mitindo ya ulimwengu iliyokuwa ni ubatili tu, ikawekwa pembeni. Wakristo hawa hawakutafuta “kujipamba kwa nje, yaani, kusuka nywele, na kuvaa dhahabu, na kuvalia mavazi; bali…utu wa moyoni usioonekana, katika mapambo yasiyoharibika; yaani, roho ya upole na utulivu, iliyo ya thamani kuu mbele za Mungu.” 1 Petro 3:3, 4. [GC 461.2; PK Aya ya 2]

Mikutano uamsho ilichochea bidii ya kujichunguza kwa kina katika mioyo na unyenyekevu. Mikutano hiyo ilihusisha miito mizito, na ya dhati kwa mwenye dhambi, kwa kutamani huruma ya upatanisho wa damu ya Kristo. Wanaume kwa wanawake waliomba na kupigana mieleka na Mungu kwa ajili ya wokovu wa roho za watu. Matunda ya mikutano hiyo ya uamsho yalionekana ndani ya watu ambao hawakujikunyata walipotakiwa kujikana nafsi zao na kujitoa kafara, bali walifurahi kwamba walihesabiwa kuwa wanastahili kupata aibu na majaribu kwa ajili ya Kristo. Watu waliona mabadiliko katika maisha ya wale waliokuwa wameliamini Jina la Yesu. Jamii yao ilinufaika kwa mvuto wao. Walikusanya pamoja na Kristo na kupanda kwa Roho, ili wavune uzima wa milele. [GC 462.1; PK Aya ya 3]

Maneno haya yaliwezwa kusemwa juu yao: “Mlihuzunishwa, hata mkatubu.” “Maana huzuni iliyo kwa jinsi ya Mungu hufanya toba iletayo wokovu isiyo na majuto; bali huzuni ya dunia hufanya mauti. Maana, angalieni, kuhuzunishwa

kuko huko kwa jinsi ya Mungu kulitenda bidii kama nini ndani yenu; naam, na kujitetea, naam, na kukasirika, naam, na hofu, naam, na shauku, naam, na kujitahidi, naam, na kisasi! Kwa kila njia mmejionyesha wenyewe kuwa safi katika jambo hilo." 2 Wakorintho 7:9-11. [GC 462.2; PK Aya ya 4]

**Wanahukumiwa Kwa Matunda Yao**

Haya ni matokeo ya kazi ya Roho wa Mungu. Hakuna ushahidi wowote wa toba ya kweli ikiwa toba hiyo haileti matengenezo. Hebu mtu aliyetubu, atimize kiapo au ahadi aliyoitoa, arudishe kile alichowapora watu na kuungama dhambi zake na ampende Mungu pamoja na wanadamu wenzake, hapo ndipo mdhambi huyo anaweza kuwa na hakika kwamba ameipata amani na Mungu. Hayo ndiyo yalikuwa matokeo ambayo katika miaka ya zamani yalifuatana na nyakati za uamsho wa kidini. Watu walipopimwa kwa matunda yao, walijulikana ya kuwa walikuwa wamebarikiwa na Mungu kwa wokovu wa wanadamu uliotendeka pamoja na kuwainua wanadamu kuwa na maisha bora kwa jumla. [GC 462.3; PK Aya ya 5]

Lakini matukio mengi ya uamsho wa siku hizi yameonyesha tofauti kubwa na ule udhihirisho wa neema ya Mungu ambao katika siku za awali uliandamana na kazi iliyofanywa na watumishi wa Mungu. Ni kweli kwamba shauku ya watu wengi huamshwa mahali pote, na wengi wanakiri kuwa wameongoka na wanajishugulisha sana na nyadhifa mbalimbali makanisani; hata hivyo, matokeo yake hayatuthibitishii sisi tupate kuamini ya kwamba pamekuwapo na ukuaji wa dhati wa maisha ya kiroho unaoendana sambamba na ongezeko la waumini wapya. Nuru iliyomulika kwa muda mfupi huzimika, na kuacha giza lililo nene zaidi kuliko ilivyokuwa hapo awali. [GC 463.1; PK Aya ya 6]

Matukio ya uamsho maarufu unaopendwa na watu wengi mara nyingi husisimua mawazo juu ya mambo ya kufikirika lakini yasiyo na uhalisia, ambayo huchochea mihemko na kukidhi upendo wa kitu kipya na cha kustajabisha au kufikirika. Waongofu wanaopatikana kwa namna hiyo hawana hamu ya kusikiliza Kweli za Biblia na huwa na shauku kidogo sana ya ushuhuda wa manabii na mitume. Huduma ya kidini, kama haina kitu fulani cha kusisimua ndani yake au chenye morimori, basi, huwa haina mvuto wowote kwao. Ujumbe wowote unaogusa akili zao kufanya maamuzi yasiyo na harara, haupati itikio lolote ndani yao. Maonyo yaliyo wazi yatokayo katika Neno la Mungu, ambayo yanahusiana moja kwa moja na maslahi yao ya milele, hupuuzwa. [GC 463.2; PK Aya ya 7]

**Wafuasi Wa Kweli Wa Kristo**

Kwa kila roho iliyoongoka kikamilifu, uhusiano wake na Mungu na mambo ya umilele itakuwa mada kuu ya maisha yake. Lakini ni wapi katika makanisa makubwa ya siku hizi, na yanayopendwa na watu, kuna roho ya kujiweka wakfu

kwa Mungu? Waongofu wake hawaachani na kiburi chao na kuupenda ulimwengu. Hawako tayari kujikana nafsi, wala kubeba msalaba na kumfuata Yesu aliye mpole na mnyenyekevu, kuliko ilivyokuwa kabla ya kuongoka kwao. Dini imekuwa mzaha au kichekesho kwa wale wasiomwamini Mungu na wenye kutilia shaka kwa sababu wengi wanaolibeba Jina hilo la dini hawazijui kanuni zake. Nguvu ya utauwa imekaribia kutoweka kabisa katika makanisa yaliyo mengi. Pikiniki (picnic), michezo ya kuigiza makanisani, maonyesho ya kanisa, majumba mazuri, maonyesho binafsi, vimefukuzia mbali mawazo ya watu kumwelekea Mungu. Ardhi, mali, vitu na pilikapilika za kidunia vimerundikana akilini, na maslahi ya umilele hata hayatupiwi macho tena. [GC 463.3; PK Aya ya 8]

Licha ya kuenea kwa maporomoko ya imani na uchaji wa Mungu, bado wapo wafuasi wa Kweli wa Kristo katika makanisa haya. Kabla ya kupatilizwa kwa hukumu za mwisho za Mungu duniani kutakuwa na uamsho wa utauwa sahili kama ule wa zamani ambao haujashuhudiwa tangu nyakati za mitume miongoni mwa watu wa Bwana. Roho na nguvu za Mungu vitamwaga juu ya watoto Wake. Wakati huo wengi watajitenga na makanisa ambayo kuupenda ulimwengu huu kumechukua nafasi ya upendo kwa Mungu na Neno Lake. Wengi, miongoni mwa wachungaji na walei, watapokea kwa furaha Kweli hizo kuu ambazo Mungu ameagizwa zitangazwe wakati huu ili kuwatayarisha watu kwa ajili ya ujio wa pili wa Bwana. Adui wa roho anatamani kuizuia kazi hii; na kabla ya wakati wa vuguvugu kama hilo kufika, atajitahidi kuzuia vuguvugu hilo kwa kuanzisha vuguvugu lake lenye uamsho wa bandia. Katika yale makanisa ambayo anaweza kuyaweka chini ya nguvu zake za udanganyifu, atafanya ionekane kwamba baraka ya pekee ya Mungu imemiminwa kwao; kutakuwepo na udhihirisho wa kile kinachodhaniwa kuwa ni shauku kubwa ya kidini. Watu wengi watafurahia sana kwamba Mungu anatenda kazi ya miujiza/ajabu kwa ajili yao, wakati kazi hiyo inatoka kwa roho nyingine (Shetani). Chini ya mwavuli wa dini, Shetani atajificha na atatafuta kueneza mvuto wake juu ya ulimwengu wa Kikristo. [GC 464.1; PK Aya ya 9]

Katika matukio mengi ya uamsho ambayo yametokea katika kipindi cha nusu karne iliyopita, ushawishi huo huo umekuwa ukifanya kazi, kwa kiwango kikubwa au kidogo, ambacho utadhihirika katika harakati kubwa zaidi za siku zijazo. Kunakuweko msisimko wa hisia, ambao umekuwa na mchanganyiko wa mambo ya Kweli na uongo, ambao umeandaliwa vizuri kwa kusudi la kupotosha watu. Hata hivyo hakuna haja ya hata mtu mmoja kudanganywa. Katika nuru ya Neno la Mungu siyo vigumu kutambua asili ya harakati hizi. Pahali popote pale watu wanapopuuza ushuhuda wa Biblia, na kuziacha zile Kweli zilizo wazi, zinazopima mioyo ya watu, na kutoa hitaji la kujikana nafsi na kuachana na dunia, hapo tunaweza kuwa na uhakika kuwa hizo baraka za Mungu haziwezi kutolewa. Na kwa mwongozo ambao Kristo Mwenyewe aliutoa, "Mtawatambua kwa matunda

yao "Mathayo 7:16), ni dhahiri kuwa harakati hizi siyo kazi ya Roho wa Mungu. [GC 464.2; PK Aya ya 10]

Katika Kweli za Neno Lake, Mungu amejifunua Mwenyewe kwa watu wote; na kwa wote wanaoupokea huko Ukweli, ni kinga dhidi ya madanganyo ya Shetani. Ni kupuuza Ukweli huu ndiyo imepelekea mlango wa maovu kufunguliwa, ambayo sasa yanaenea sana katika ulimwengu wa kidini. Msingi na umuhimu wa sheria ya Mungu kwa kiasi kikubwa vimepotezwa akilini mwa watu. Uelewa potofu kuhusu sifa, uendelevu na ulazima wa ushikaji wa sheria ya Mungu ambao unawafunga watu wote umesababisha mafundisho yenye makosa juu ya uongofu na utakaso na kupelekea kushuka kwa kiwango cha utakatifu/utauwa katika kanisa. Na hii ndiyo siri ya ukosefu wa Roho na nguvu za Mungu katika matukio ya uamsho ya nyakati zetu. [GC 465.1; PK Aya ya 11]

Katika madhehebu mbalimbali, wapo watu wanaoujulikana kwa kumcha Mungu wao, watu mashuhuri kwa uadilifu ambao wanaukiri ila wanautupilia mbali Ukweli huu. Profesa Edwards A. Park, katika kueleza hatari za sasa za kidini, anasema hivi kwa ufasaha: “Chanzo Kimoja cha hatari ni uzembe unaoonekana mimbarini katika kusimamia utekelezaji wa sheria ya Mungu. Katika siku za awali mimbari ilikuwa mwangwi wa sauti ya dhamiri……Wahubiri wetu wengi maarufu waliyapa utukufu wa ajabu mahuburi yao kwa kufuata mfano wa Bwana na kuzipa uzito sheria za Mungu, kanuni Zake, na utisho Wake. Waliirudia misemo miwli ya hekima, kwamba sheria ni nakala ya utakatifu na ukamilifu wa Mungu na kuwa mtu asiyeipenda sheria haipendi injili; kwa kuwa sheria, pamoja na injili, ni kioo kinachoakisi tabia ya Kweli ya Mungu. Jambo hili la hatari linafungua mlango mwingine, ule wa kushindwa kubaini ubaya wa dhambi, ukubwa wake, na madhara yake. Kuna uwiano kati ya kiwango cha uzuri wa kuitii Sheria hiyo ya Mungu na kiwango cha ubaya cha kutoitii.... [GC 465.2; PK Aya ya 12]

“Pamoja na hatari zilizokwishakutajwa kuna hatari ya kuipuuzia haki ya Mungu. Mwelekeo wa mimbari ya leo ni kutenganisha haki ya Mungu kutoka katika wema wa Mungu, kuzamisha chini hadhi ya wema wa Mungu, na kuiona ni kama hisia tu ya kufikirika badala ya kuiinua na kuipa hadhi kuwa kanuni. Ufanunuzi huu wa kitheolojia, wa kutazamia mambo mbalimbali na kuyadadavua, hutenganisha kile ambacho Mungu alikiunganisha pamoja. Je, sheria ya Mungu ni njema au ni mbaya? Ni njema Basi haki ni njema; kwa kuwa kazi yake ni kutekeleza sheria. Kutokana na mazoea ya kudharau wema wa sheria na haki ya Mungu, na kushindwa kubaini kiwango na hasara ya uasi wa binadamu, watu wanajikuta wameteleza kirahisi katika mazoea ya kupuuzia thamani ya neema ambayo imetoa upatanisho kwa ajili ya dhambi zetu.” Hivyo injili inapoteza thamani na umuhimu wake katika akili za watu na haichukui

muda mrefu  wanakuwa tayari kwa vitendo, kuitupilia mbali Biblia yenyewe. [GC 465.3; PK Aya ya 13]

Waalimu wengi wa dini wanadai kwamba Kristo kwa kifo Chake aliitangua sheria na wanadamu tangu hapo hawabanwi na matakwa yake, yaani wako huru. Kuna kundi la watu wengine pia, ambao huiwasilisha sheria kama mzigo mzito na kinyume na utumwa wa sheria, wanawasilisha kwamba uhuru unaopatikana na kufurahiwa chini ya injili, kinyume na ule wa kuwa chini ya sheria hiyo. [GC 466.1; PK Aya ya 14]

Lakini sivyo walivyofanya manabii na mitume, walivyoichukulia Sheria Takatifu (Amri Zake) ya Mungu. Daudi alisema: “Nami nitakwenda panapo nafasi, Kwa kuwa nimejifunza mausia yako.” Zaburi 119:45. Mtume Yakobo, aliyeandika baada ya kifo cha Kristo, anarejelea Sheria hii kuwa ni “sheria ya kifalme” na “sheria kamilifu iliyo ya uhuru.” Yakobo 2:8; 1:25. Naye Yohana wa ufunuo, nusu karne baada ya kusulubishwa kwa Kristo, anatangaza baraka juu yao “wazishikao amri Zake, wawe na amri kuuendea huo mti wa uzima, na kuingia mjini kwa milango yake.” Ufunuo 22:14. [GC 466.2; PK Aya ya 15]

Madai ya kwamba Kristo kwa kifo Chake aliibatilisha sheria ya Baba Yake hayana msingi/mashiko. Kama kungekuwa na uwezekano wa sheria kubadilishwa au kuwekwa pembeni, basi Kristo asingelazimika kufa ili kumwokoa mwanadamu kutoka katika adhabu ya dhambi. Kifo cha Kristo, mbali na kwamba hakikutangua sheria, kinathibithisha kwamba sheria haiwezi kubadilika. Mwana wa Mungu alikuja “Kuitukuza sheria, na kuiadhimisha.” Isaya 42:21. Alisema: “Msidhani ya kuwa nalikuja kuitangua torati; "Mpaka mbingu na nchi zitakapoondoka, yodi moja wala nukta moja ya torati haitaoondoka, hata yote yatimie." Mathayo 5:17, 18. Na kuhusu Yeye Mwenyewe anasema hivi: “Kuyafanya mapenzi Yako, Ee Mungu Wangu, ndiyo furaha Yangu; Naam, sheria Yako imo moyoni Mwangu.” Zaburi 40:8. [GC 466.3; PK Aya ya 16]

**Sheria Hiyo Haibadiliki Kamwe**

Sheria ya Mungu, kwa asili yake yenyewe, yaani kwa jinsi ilivyo, haiwezi kamwe kubadilika. Sheria ni ufunuo wa mapenzi na tabia ya Mwasisi Wake. Mungu ni Upendo na sheria Yake ni Upendo. Kanuni Zake kuu mbili ni upendo kwa Mungu na upendo kwa mwanadamu. "Upendo ni utimilifu wa sheria." Warumi 13:10. Tabia ya Mungu ni Haki na Kweli; na hiyo ndiyo asili ya sheria Yake ilivyo. Mwandishi wa Zaburi anasema hivi: “Na sheria Yako ni Kweli.” “Maana maagizo Yako yote ni ya haki.” Zaburi 119:142, 172. Na mtume Paulo asema: “Basi torati ni takatifu, na ile amri ni takatifu, na ya haki, na njema.” Warumi 7:12. Sheria kama hiyo, kwa kuwa inatoa ufafanuzi wa kile kilichomo kwenye akili na mapenzi ya Mungu, lazima iwe ya kudumu kama alivyo Mwasisi Wake. [GC 467.1; PK Aya ya 17]

Ni kazi ya uongofu na utakaso, ya kuwapatanisha wanadamu na Mungu kwa kuwaleta katika mapatano na kanuni za sheria Yake. Hapo mwanzo mwanadamu aliumbwa kwa mfano wa Mungu. Alikuwa katika mapatano kamili ya asili (nature) na sheria ya Mungu; kanuni za haki zilikuwa zimeandikwa juu ya moyo wake. Lakini dhambi ilimtenga na Muumbaji wake. Hakuweza kuakisi tena sura ya Mungu. Moyo wake ulikuwa katika vita dhidi ya kanuni za sheria ya Mungu. "Kwa kuwa ile nia ya mwili ni uadui juu ya Mungu, kwa maana haitii sheria ya Mungu, wala haiwezi kuitii." Warumi 8:7. Lakini "Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe Pekee," ili mwanadamu apatanishwe na Mungu. Kwa njia ya haki ya Kristo anaweza kurudishwa tena katika mwafaka na Muumba wake. Moyo Wake ni lazima uumbwe upya kwa neema ya Mungu; ni lazima apokee maisha mapya kutoka juu mbinguni. Badiliko hilo ni uzoefu wa kuzaliwa upya, ambao, mtu asipokuwa nao,Yesu anasema, "hawezi kuuona ufalme wa Mungu." [GC 467.2; PK Aya ya 18]

Hatua ya kwanza katika upatanisho na Mungu ni kushawishika na kukiri kuwa ni mwenye dhambi. "Kwa kuwa dhambi ni uasi." "Kwa maana kutambua dhambi huja kwa njia ya sheria." 1 Yohana 3:4; Warumi 3:20. Ili aone hatia yake, mwenye dhambi lazima aipime tabia yake kwa njia ya kiwango kikuu cha Mungu cha haki. Na kioo kinachoonyesha ukamilifu wa tabia ya haki na kumwezesha mwenye dhambi kutambua mapungufu/kasoro zake. [GC 467.3; PK Aya ya 19]

**Huru Mbali Na Hukumu Ya Adhabu**

Sheria inamfunulia mwanadamu dhambi zake, lakini haitoi suluhisho au tiba. Wakati ambapo inaahidi uzima kwa watu watiifu, inatangaza kwamba kifo ni mshahara wa mkosaji. Injili ya Kristo pekee ndiyo inayoweza kumwokoa mwenye dhambi kutokana na hukumu au uchafu wa dhambi. Ni lazima afanye toba kwa Mungu, ambaye sheria Yake imevunjwa; na kuwa na imani katika Kristo na kafara Yake pekee ya upatanisho. Hivyo anapokea "ondoleo la dhambi zilizopita" na kuwa mshirika wa asili ya Uungu. Yeye sasa ni mwana wa Mungu, akiwa amepokea roho ya kuasiliwa,* kufanya mwana, ambapo analia: "Abba, yaani Baba!" [GC 467.4; PK Aya ya 20]

Je, mtu huyo sasa yuko huru kuvunja sheria ya Mungu? Paulo anasema hivi: "Basi Je! Twaibatilisha sheria kwa imani hiyo? Hasha! Kinyume cha hayo twaithibitisha sheria." "Hasha Sisi tulioifia dhambi tutaishije tena katika dhambi?" Naye Yohana anasema hivi: "Kwa maana huku ndiko kumpenda Mungu, kwamba tuzishike amri Zake; wala amri Zake si nzito." Warumi 3:31; 6:2; 1 Yohana 5:3. Katika kuzaliwa mara ya pili moyo unaletwa katika maafikiano na Mungu, kama unavyoletwa katika mapatano na sheria Yake. Wakati badiliko hili kubwa linapotokea ndani ya mwenye dhambi, anakuwa amepita kutoka mautini na kuingia uzimani, kutoka dhambini hadi katika utakatifu, kutoka katika uasi na

makosa au kuvunja sheria hadi kwenye utii na uaminifu. Maisha ya zamani ya kujitenga na Mungu yamekoma; maisha mapya ya upatanisho, imani na upendo, yameanza. Ndipo “haki ya torati na sheria” itatimizwa ndani yetu sisi, tusioenenda kwa kufuata mambo ya mwili, bali mambo ya Roho, Warumi 8:4. Ndipo lugha ya roho ya mtu huyo itakuwa: “Sheria Yako naipenda mno ajabu! Ndiyo kutafakari kwangu mchana kutwa." Zaburi 119:97. [GC 468.1; PK Aya ya 21]

"Sheria ya Bwana ni kamilifu, huiburudisha nafsi."Zaburi 19:7. Bila sheria, wanadamu hawana dhana au uelewa wa haki wa usafi wa maisha na utakatifu wa Mungu au wa hatia yao na uchafu wao. Hawana usadikisho wa Kweli wa dhambi na hawaoni haja ya kutubu. Kwa kutoona hali yao ya kupotea kama wavunjaji wa sheria ya Mungu, hawatambui hitaji lao la damu inayopatanisha ya Kristo. Tumaini la wokovu hupokelewa bila badiliko kubwa la moyo au matengenezo ya maisha. Kwa njia hiyo waongofu wa juu juu ni wengi, na hivyowatu wanaunganishwa au wanajiunga na kanisa ambao kamwe hawajapata kuunganishwa na Kristo. [GC 468.2; PK Aya ya 22]

Nadharia potofu za utakaso, zinazotokana na kupuuzwa au kukataa sheria ya Mungu, zimepata kipaumbele kikubwa katika vuguvugu za kidini za siku hizi. Nadharia hizi zote ni zenye mafundisho ya uongo na ni hatari katika matokeo ya matendo halisi ya kila siku; na ukweli kwamba zinakubaliwa na wengi kwa jumla, zinafanya mafundisho haya kupata fursa na upendeleo, na zinafanya iwe muhimu maradufu kwamba wote wawe na uelewa sahihi wa kile kinachofundishwa na Maandiko juu ya kipengele (pointi) hiki. [GC 469.1; PK Aya ya 23]

**Utakaso Wa Kweli Ni Nini?**

Utakaso wa Kweli ni fundisho la Biblia. Mtume Paulo, katika waraka wake kwa kanisa la Thesalonike: “Maana haya ndiyo mapenzi ya Mungu, kutakaswa kwenu.” Naye anasali hivi: “Mungu wa Amani Mwenyewe awatakase kabisa.” 1 Wathesalonike 4:3; 5:23. Biblia inafundisha waziwazi maana ya utakaso na jinsi unavyopaswa kupatikana. Mwokozi aliwaombea wanafunzi Wake: “Uwatakase kwa ile Kweli: Neno Lako ndiyo Kweli.” Yohana 17:17. Na Paulo anafundisha kwamba waumini wanapaswa “kutakaswa na Roho Mtakatifu.” Warumi 15:16. Kazi ya Roho Mtakatifu ni nini? Yesu aliwaambia wanafunzi Wake hivi: “Yeye atakapokuja, huyo Roho wa Kweli, atawaongoza awatie kwenye Kweli yote.” Yohana 16:13 Warumi 15:16. Na mwandishi wa Zaburi anasema: “Sheria Yako ndiyo Kweli.” Kwa njia ya Neno na Roho wa Mungu kanuni kuu za haki zinazowekwa katika sheria Yake zinafunuliwa kwa wanadamu. Na kwa kuwa sheria ya Mungu ni “takatifu, na ya haki, na njema,” nakala ya ukamilifu wa Mwenyezi Mungu, ina maana kuwa na tabia inayojengwa kwa njia ya kuitii sheria hiyo itakuwa takatifu. Kristo ni mfano mkamilifu wa tabia hiyo. Anasema: “Kama

vile Mimi nilivyozishika amri za Baba Yangu." "Kwa sababu nafanya siku zote yale yampendezayo." Yohana 15:10; 8:29. Wafuasi wa Kristo wanapaswa kuwa kama Yeye kwa neema ya Mungu inawapasa wajenge tabia zinazopatana na kanuni za sheria Yake takatifu. Huu ni utakaso wa Biblia. [GC 469.2; PK Aya ya 24]

**Ni Kwa Njia Ya Imani Peke Yake**

Kazi hii inaweza kutekelezwa tu kwa njia ya imani katika Kristo, kwa uwezo wa Roho wa Mungu anayekaa ndani yao. Paulo anawahimiza hivi waaminio: "utimizeni wokovu wenu wenyewe kwa kuogopa na kutetemeka. Kwa maana Ndiye Mungu atendaye kazi ndani yenu, kunia/kutaka kwenu na kutenda kwenu, kwa kulitimiza kusudi Lake jema." Wafilipi 2:12, 13. Mkristo atahisi misukumo ya dhambi, lakini atadumisha vita vya kuipinga dhambi. Hapa ndipo msaada wa Kristo unapohitajika. Udhaifu wa kibinadamu unaunganana nguvu za Mwenyezi Mungu na imani inapaza sauti ikisema: "Mungu ashukuriwe atupaye kushinda kwa Bwana wetu Yesu Kristo." 1 Wakorintho 15:57. [GC 469.3; PK Aya ya 25]

Maandiko yanaonyesha waziwazi kuwa kazi ya utakaso ni endelevu. Wakati wa uzoefu wa uongofu, mdhambi anapopata amani na Mungu kwa njia ya damu ya upatanisho, maisha ya Ukristo ndiyo tu yanakuwa yameanza. Sasa inampasa "akaze mwendo tu ili aufikilie utimilifu;" akue "hata kufika kwenye cheo cha kimo cha utimilifu wa Kristo." Mtume Paulo anasema hivi: "Nafanya neno hili moja tu, nikiyasahau yaliyo nyuma, nikiyachuchumilia yaliyo mbele; nakaza mwendo, niifikilie mede ya thawabu ya mwito mkuu wa Mungu katika Kristo Yesu. Wafilipi 3:13, 14. Na Petro anaweka mbele yetu hatua ambazo inampasa mtu kuzifuata ili kupata utakaso wa Biblia: "Naam, na kwa sababu iyo hiyo mkijitahidi sana kwa upande wenu, katika imani yenu tieni na wema, na katika wema wenu maarifa, na katika maarifa yenu kiasi, na katika kiasi chenu saburi, na katika saburi yenu utauwa, na katika utauwa wenu upendano wa ndugu, na katika upendano wa ndugu, upendo.....Mkifanya hayo, hamtaanguka kamwe." [GC 470.1; PK Aya ya 26]

Watu wanaopata uzoefu wa utakaso wa Biblia watadhihirisha roho ya unyenyekevu. Kama ilivyokuwa kwa Musa, wamepata kuona udhihirisho wa utukufu wa kutisha na ushangazao wa utakatifu na wanaona kutostahili kwao wakijilinganisha na usafi na ukamilifu ulioinuliwa juu, wa Yeye wa Milele, Yule Asiye na kikomo. [GC 470.2; PK Aya ya 27]

Nabii Danieli alikuwa mfano wa utakaso wa kweli. Maisha yake marefu yalijaa utumishi mwema kwa ajili ya Bwana wake. Alikuwa mtu "aliyependwa sana" (Danieli 10:11) na Mbingu. Badala ya kudai kuwa msafi na mtakatifu, nabii huyu aliyeheshimiwa alijitambulisha kama mmoja wa wana wa Israeli ambao walikuwa wametenda dhambi kweli-kweli alipokuwa akimlilia Mungu kwa niaba ya watu

wake: “Maana hatukutolei maombi yetu kwa sababu ya haki yetu, lakini kwa sababu ya rehema Zako nyingi.” “Tumefanya dhambi, tumetenda maovu." Anasema kuwa: “Nilipokuwa nikisema na kuomba, na kuiungama dhambi yangu, na dhambi ya watu wangu Israeli.” Na wakati wa baadaye Mwana wa Mungu alitokea, ili kumpatia maagizo, Danieli anasema: "Maana uzuri wangu uligeuzwa ndani yangu kuwa uharibifu, wala sikusaziwa nguvu." Danieli 9:18, 15, 20; 10:8. [GC 470.3; PK Aya ya 28]

**Hakuna Kutoa Madai Ya Kujisifu Wenyewe**

Ayubu aliposikia sauti ya Bwana ikitoka katika upepo wa kisulisuli, alisema kwa huzuni: “Najichukia mwenyewe, na kutubu katika mavumbi na majivu." Ayubu 42:6. Wakati Isaya alipouona utukufu wa Bwana na kuwasikia makerubi wakisema, "Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu, ni Bwana wa majeshi" Ndipo akalia Ole wangu! Kwa maana nimepotea (nimekwisha).” Isaya 6: 3, 5. Paulo, baada ya kunyakuliwa hadi katika mbingu ya tatu na kusikia mambo ambayo mwanadamu hakuweza kuyatamka, naye alielezea mwenyewe kuhusu uzoefu wake akajiona kuwa ni “mdogo kuliko aliye mdogo zaidi wa watakatifu wote.” Wakorintho 12:2-4; Waefeso 3:8. Ilikuwa Yohana mpendwa, ambaye aliegemea katika kifua cha Yesu na kuuona utukufu Wake, ambaye alianguka chini kama mtu aliyekufa mbele ya miguu ya malaika Ufunuo 1:17. [GC 471.1; PK Aya ya 29]

Hakutakuwa na kujiinua nafsi, hakuna madai ya kujivuna kwamba hutuna dhambi, kwa wale watu wanaotembea katika kivuli cha msalaba wa Kalwari. Wanatambua kwamba ni dhambi zao ndizo zilizosababisha uchungu uliopasua moyo wa Mwana wa Mungu na wazo hili litawafanya wajishushe. Wale wanaoishi karibu na Yesu wanatambua kwa uwazi zaidi udhaifu na dhambi ya wanadamu na tumaini lao pekee ni katika haki ya Mwokozi aliyesulubiwa na kufufuka. [GC 471.2; PK Aya ya 30]

Utakakaso unaopata umaarufu sasa kwa kasi sana katika ulimwengu wa kidini unabeba pamoja nao roho ya kujikweza na kupuuzia sheria ya Mungu ambayo inaupinga utakaso huo kama jambo geni katika dini ya Biblia. Watetezi wake hufundisha kwamba utakaso huo ni kazi ya kufumba na kufumbua, ambayo kwayo, kwa njia ya imani pekee, wanafikia utakatifu kamili. Kitu unachopaswa kufanya ni "Amini peke yake," wanasema, "na mbaraka huo ni wako." Hakuna juhudi zaidi kwa upande wa mpokeaji wa baraka hizo inayohitajika kufanyika. Kwa wakati huo huo wanakataa mamlaka ya sheria ya Mungu, wakidai kuwa wameachiliwa kutoka katika ulazima wa kushika amri. Lakini inawezekanaje kwa wanadamu kuwa watakatifu, kulingana na mapenzi na tabia ya Mungu, pasipo kuufikia mwafaka kati yao na kanuni (Amri Zake) hizo ambazo ni zinaelezea asili la mapenzi Yake? Kwani hizi kanuni ndizo zinazoonyesha tabia na mapenzi Yake

Mungu, tena hizo kanuni ndizo ambazo zinazoonyesha kile kinachompendeza Mungu [GC 471.3; PK Aya ya 31]

**Dini Rahisi**

Tamaa ya kuwa na dini rahisi isiyohitaji kujitahidi, kujinyima au kujikana nafsi, isiyohitaji kuachana na upumbavu wa dunia, imelifanya fundisho la imani na imani pekee, kuwa fundisho maarufu na linalopendwa sana; lakini Neno la Mungu linasemaje? Mtume Yakobo anasema hivi: "Ndugu zangu, yafaa nini, mtu akisema ya kwamba anayo imani, lakini hana matendo? Je! Ile imani yaweza kumwokoa?....Lakini wataka kujua, wewe mwanadamu usiye kitu, kwamba imani pasipo matendo haizai/imekufa? Je! Baba yetu Ibrahimu hakuhesabiwa kuwa ana haki kwa matendo, hapo alipomtoa Isaka mwanawe juu ya madhabahu? Je, hauoni kwamba imani ile ilitenda kazi pamoja na matendo yake, na ya kwamba imani hiyo ilikamilishwa kwa njia ya matendo yale?.... Mwaona kwamba mwanadamu huhesabiwa kuwa ana haki kwa matendo yake; si kwa imani peke yake." Yakobo 2:14-24. [GC 472.1; PK Aya ya 32]

Ushuhuda wa Neno la Mungu unapinga fundisho hili lenye mtego usiotambulika kirahisi, fundisho la imani bila matendo. Siyo imani inayodai upendeleo wa Mbingu pasipo utii kwa kuzingatia masharti ambayo ni lazima, ili rehema itolewe, ni kulijua Agizo la Mungu na kuamua kwa kiburi kutolitenda na kujidangaya tu (presumption); kwa kuwa imani ya kweli msingi wake ni katika ahadi na maagizo ya Maandiko. [GC 472.2; PK Aya ya 33]

Mtu yeyote asijidanganye kuwa kuna imani ambayo kwayo mtu anaweza kuwa mtakatifu huku kwa uchaguzi wake mwenyewe anavunja moja ya matakwa ya sheria ya Mungu kwa makusudi. Utendaji wa dhambi inayofahamika unanyamazisha sauti inayoshuhudia ya Roho na kuitenganisha roho na Mungu. "Kwa kuwa dhambi ni uasi." Na "kila atendaye dhambi hakumwona Yeye, wala hakumtambua." 1 Yohana 3:6. Ingawa Yohana katika nyaraka zake anaelezea kikamilifu sana juu ya upendo, lakini hasiti kufichua tabia halisi ya lile tabaka linalodai kutakaswa huku wakiishi katika uasi wa sheria ya Mungu. "Yeye asemaye, Nimemjua, wala hazishiki amri Zake, ni mwongo, wala Kweli haimo ndani yake. Lakini yeye alishikaye Neno Lake, katika huyo upendo wa Mungu umekamilika kweli kweli. Katika hili twajua ya kuwa tumo ndani Yake." 1 Yohana 2:4, 5. Hapa kuna kipimo cha imani ya kila mwenye mwili. Hatuwezi kumhesabia mtu yeyote kuwa mtakatifu bila kumleta kwenye kipimo cha kiwango pekee cha Mungu cha utakatifu mbinguni na duniani. Ikiwa wanadamu hawahisi uzito wa sheria ya uadilifu, ikiwa wanazidharau na kuzipuuzia amri za Mwenyezi Mungu, ikiwa wanavunja moja ya amri iliyo ndogo kabisa miongoni mwa amri Zake, na kuwafundisha watu hivyo ili nao wazivunje, watajipotezea

thamani yao mbele za mbingu, nasi tunaweza kujua kwamba madai yao hayana mashiko au msingi wowote. [GC 472.3; PK Aya ya 34]

Kuhusiana na dai la kutokuwa na dhambi; dai hilo lenyewe, ni ushahidi tosha kwamba huyo anayetoa dai hili yuko mbali kabisa na utakatifu. Ni kwa sababu hana uelewa sahihi wa usafi na utakatifu usio na kikomo wa Mungu au hana uelewa sahihi wa jinsi anavyopaswa kuwa yule ambaye atapatana na na tabia Yake Bwana; na kwa sababu hana uelewa sahihi wa usafi na uzuri uliotukuka wa Yesu, basi atakuwa pia hana uelewa sahihi wa madhara na uovu wa dhambi ulivyo, ambapo mwanadamu anaweza kujidhania kuwa yeye ni mtakatifu. Kwa kadiri umbali kati yake na Kristo unavyozidi kuwa mkubwa zaidi, na kwa kadri uelewa wake wa tabia ya Mungu na matakwa Yake Bwana unavyokuwa mdogo zaidi, ndivyo anavyozidi kujiona kuwa yeye ni mwenye haki na mwadilifu machoni pake mwenyewe. [GC 473.1; PK Aya ya 35]

**Dhabihu Iliyo Hai**

Utakaso uliolezwa katika Maandiko hujumuisha utu wote kamili—yaani roho, nafsi na mwili. Paulo alifanya maombezi kwa ajili ya Wathesalonike ili Mungu wa amani Mwenyewe awatakase kabisa; na kuwa nafsi zao na roho zao na miili yao vihifadhiwe wawe "kamili, bila lawama, wakati wa kuja Kwake Bwana wetu Yesu Kristo." Wathesalonike 5:23. Tena aliwaandikia hivi waaminio: "Basi, ndugu zangu, nawasihi, kwa huruma Zake Mungu, itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu, ya kumpendeza Mungu, ndiyo ibada yenu yenye maana." Warumi 12:1. Nyakati za Israeli ya zamani kila sadaka iliyoletwa kama kafara kwa Mungu ilikaguliwa na kupimwa kwa uangalifu mkubwa. Ikiwa kasoro yoyote iligundulika kwa mnyama aliyeletwa, mnyama huyo alikataliwa; kwa maana Mungu alikuwa ameamuru kwamba kafara iwe "bila waa au dosari." Kwa hiyo Wakristo wameagizwa waitoe miili yao, kuwa "dhabihu iliyo hai, takatifu, ya kumpendeza Mungu." Ili kufanya hivyo, nguvu zao zote lazima zitunzwe katika hali bora zaidi kwa kadri inavyowezekana. Kila tendo au mazoea yanayodhoofisha nguvu za kimwili au kiakili humfanya mtu asifae kwa ajili ya utumishi kwa Muumba Wake. Na Je! Mungu atapendezwa na kitu chochote kilicho pungufu ya kiwango tunachoweza kutoa? Kristo alisema: "Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote." Wale wanaompenda Mungu kwa moyo wote watakuwa na matamanio ya kumpatia Yeye utumishi ulio bora kabisa wa maisha yao, nao watakuwa wakitafuta daima kuleta kila nguvu ya maisha yao kupatana na sheria ambazo zitakuza uwezo wao wa kutenda mapenzi Yake. Hawatadhoofisha au kuchafua sadaka ambayo wanaitoa kwa Baba yao wa mbinguni, kwa kuendekeza uchu wa chakula au tamaa ya mwili kama hasira. [GC 473.2; PK Aya ya 36]

Petro anasema: "Jiepusheni na tamaa za mwili, ambazo hupigana na roho." 1 Petro 2:11. Kila dhambi inayotendwa ili kukidhi tamaa hizo mbaya huzitia ganzi

nguvu za fahamu zinazotuwezesha sisi kutenda mambo yote na kuua utambuzi wetu wa kiakili na kiroho, na Neno au Roho wa Mungu huwa na mguso hafifu tu. Paulo anawaandikia Wakorintho, akisema: “na tujitakase nafsi zetu na uchafu wote wa mwili na roho, huku tukitimiza utakatifu katika kumcha Mungu.” 2Wakorintho 7:1. Na pamoja na tunda la Roho “upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, upole”_ anajumuisha “kiasi katika orodha hiyo." Wagalatia 5:22, 23. [GC 474.1; PK Aya ya 37]

Licha ya matamko ya Maneno haya yaliyovuviwa, ni wangapi wanaojiita Wakristo na kisha hudhoofisha nguvu zao katika kutafuta faida au katika ibada ya mitindo; ni wangapi hudhalilisha utu wao wenye sura ya Mungu kwa ulafi, kwa utumiaji wa vileo na anasa zilizokatazwa. Na kanisa, badala ya kukemea mambo haya, mara nyingi huhamasisha uovu kwa kuchochea uchu wa chakula, tamaa ya mapato au kupenda anasa, ili kuijaza hazina ya kanisa, ambayo upendo kwa ajili ya Kristo umeshindwa kuijaza kwa vile ni dhaifu mno na hivyo haukidhi katika kuijaza hazina hiyo. Kama Yesu angeingia katika makanisa ya siku hizi na kuona karamu na shughuli najisi zilizoshonana zikiendelezwa humo kwa jina la dini, je, asingeliwafukuza hao wanajisi wa hekalu, kama alivyowafukuza wabadili fedha kutoka hekaluni? [GC 474.2; PK Aya ya 38]

**Usafi Wa Injili**

Mtume Yakobo anatangaza kuwa hekima ile inayotoka juu “kwanza ni safi.” Endapo angekutana na wale wanaolikiri Jina la thamani la Yesu kwa midomo iliyotiwa unajisi kwa tumbaku, wale ambao pumzi zao na nafsi zao zimechafuliwa na harufu yake mbaya, nao huchafua hewa ya anga na kuwalazimisha wote wanaowazunguka kuvuta ile sumu--ikiwa mtume angekutana na mazoea haya yanayopingana na usafi wa injili, je, si angeikemea na kuiita tabia hii kuwa ya “dunia, ya tamaa ya kimwili, na ya kishetani”? Watumwa hao wa tumbaku, wanadai wamepata mbaraka wa utakaso kamili, nao huzungumza juu ya tumaini lao la mbinguni; lakini Neno la Mungu linatangaza waziwazi kwamba “huko ndani yake hakitaingia kamwe chochote kilicho kinyonge. Ufunuo 21:27.. *(Wakati huu wa miaka ya 1800 wizara za afya za dunia zilikuwa bado hazijagundua madhara ya tumbako na madaktari wengi waliitumia mioshi ya misokoto ya tumbaku kama tiba ya mapafu! Maagizo ya tiba ilikuwa vuta mara tatu kwa siku nk, lakini mtumishi huyu wa Mungu alikuwa ameshapewa maarifa haya) [GC 474.3; PK Aya ya 39]

Au hamjui ya kuwa mwili wenu ni hekalu la Roho Mtakatifu aliye ndani yenu, mliyepewa na Mungu? Wala ninyi si mali yenu wenyewe? Maana mlinunuliwa kwa thamani. Sasa basi, mtukuzeni Mungu katika miili yenu." Yeye ambaye mwili wake ni hekalu la Roho Mtakatifu hatafanywa mtumwa wa tabia mbaya inayomdhuru. Nguvu zake ni mali ya Kristo, ambaye amemnunua kwa gharama ya

damu Yake. Mali yake ni ya Bwana. Anawezaje kuwa hana hatia katika ubaradhifu au kufuja mtaji huu aliopewa kama dhamana kuusimania? Wale wanaojiita Wakristo, kila mwaka hutumia kiasi kikubwa sana cha pesa kununua vitu vya upuuzi, visivyo na manufaa na ambavyo wanaviendekeza japo ni vya kudhuru mwili, wakati roho zinaangamia kwa ajili ya kukosa Neno la uzima. Wanamuibia Mungu zaka na sadaka, huku wakiteketeza juu ya madhabahu ya tamaa zao zinazoangamiza kiasi kikubwa zaidi kuliko wanavyotoa kwa ajili ya kusaidia masikini au kutegemeza injili. Ikiwa wote wanaodai kuwa wafuasi wa Kristo wangetakaswa kweli, mali zao, badala ya kutumiwa kwa ajili ya kuendekeza anasa zisizo za lazima na hata zenye madhara, hizo mali zingegeuzwa na kuwekwa kwenye hazina ya Bwana na Wakristo wangeweza kuweka kielelezo cha kuwa na kiasi, kujikana nafsi, kujitoa kafara na kuwa na kiasi. Ndipo watakuwa nuru ya ulimwengu. [GC 475.1; PK Aya ya 40]

Ulimwengu huu umejitumbukiza katika kuendekeza na kukidhi tamaa zake mbaya bila kujizuia. “Tamaa ya mwili, tamaa ya macho na kiburi cha uzima” vinawatawala watu wengi sana. Lakini wafuasi wa Kristo wana wito mtakatifu zaidi. “Kwa hiyo, Tokeni kati yao, Mkatengwe nao, asema Bwana, Msiguse kitu kilicho kichafu." Katika nuru ya Neno la Mungu tuna haki katika kutangaza kwamba utakaso hauwezi kuwa wa kweli wakati usipofanya kazi hii ya kukataa kabisa utafutaji wa dhambi na anasa za ulimwengu. Huu. [GC 475.2; PK Aya ya 41]

Kwa wale wanaotii masharti, “Tokeni kati yao, mkajitenge, ... wala msiguse kitu kilicho kichafu,” Ahadi ya Mungu ni, “Nami nitawakaribisha. Nitakuwa Baba kwenu, Nanyi mtakuwa Kwangu Wanangu wa kiume na wa kike asema Bwana Mwenyezi.” 2 Wakorintho 6:17, 18. Ni fursa na wajibu wa kila Mkristo kuwa na tajiriba na uzoefu mwingi katika mambo ya Mungu. Yesu anasema “Mimi Ndimi nuru ya ulimwengu.” “Yeye anifuataye hatakwenda gizani kamwe, bali atakuwa na nuru ya uzima." Yohana 8:12." Bali njia ya wenye haki ni kama nuru ing'aayo, Ikizidi kung'aa hata mchana mkamilifu." Mithali 4:18. Kila hatua ya imani na utii huileta nafsi katika mshikamano wa karibu na Nuru ya ulimwengu, ambayo ndani Yake “hakuna giza hata kidogo.” Miale inayong’aa ya Jua la Uadilifu inawamulika watumishi wa Mungu, nao wanapaswa kuakisi miale Yake. Kama vile nyota zinavyotuambia kwamba kuna nuru kubwa mbinguni ambayo kwa utukufu Wake zinafanywa kung'aa, kadhalika Wakristo wanapaswa kudhihirisha kwamba kuna Mungu kwenye kiti cha enzi cha ulimwengu wote ambaye tabia Yake inastahili kupewa sifa na kuigwa. Neema za Roho Wake, usafi na utakatifu wa tabia Yake, vitadhihirika kwa mashahidi Wake. [GC 475.3; PK Aya ya 42]

**Wana Na Binti Za Mungu**

Paulo katika waraka wake kwa Wakolosai anaweka wazi mibaraka tele na mikubwa inayotolewa kwa watoto wa Mungu. Anasema: “Kwa sababu hiyo sisi nasi, tangu siku ile tuliposikia, hatuachi kufanya maombi na dua kwa ajili yenu, ili mjazwe maarifa ya mapenzi Yake katika hekima yote na ufahamu wa rohoni; mwenende kama ulivyo wajibu wenu kwa Bwana, mkimpendeza kabisa; mkizaa matunda kwa kila kazi njema, na kuzidi katika maarifa ya Mungu; mkiwezeshwa kwa uwezo wote, kwa kadiri ya nguvu ya utukufu Wake, mpate kuwa na saburi ya kila namna na uvumilivu pamoja na furaha.” Wakolosai 1:9-11. [GC 476.1; PK Aya ya 43]

Tena anaandika juu ya shauku yake kwamba ndugu zake wa Efeso wapate kuelewa kina cha upendeleo na fursa aliyopewa Mkristo. Naye anafungua mbele yao, kwa lugha iliyo fasaha kabisa na inayobeba mambo yote, nguvu za ajabu na maarifa ambayo wangeweza kuwa nayo kama wana na binti za Yeye Aliye Juu sana. Ilikuwa ni stahiki yao “kuimarishwa kwa uwezo na Roho Wake katika utu wa ndani,” kuwa na “shina na msingi katika upendo,” ili “kufahamu pamoja na watakatifu wote jinsi ulivyo upana, na urefu, na kimo, na kina; na kuujua upendo wa Kristo, upitao maarifa.” Lakini ombi la mtume linafikia kilele cha upendeleo anapoomba kwamba “mpate kutimilika kwa utimilifu wote wa Mungu.” Waefeso 3:16-19. [GC 476.2; PK Aya ya 44]

Hapa panafunuliwa siri ya urefu na upana wa mafanikio ambayo miguu yetu inaweza kuyafikia kwa kupitia njia ya imani katika ahadi za Baba yetu wa mbinguni, tunapotimiza matakwa Yake. Kwa njia ya haki ya Kristo tunayo fursa ya kukiendea kiti cha enzi cha nguvu, isiyokuwa na mipaka. Yeye asiyemwachilia Mwana Wake Mwenyewe, bali alimtoa kwa ajili yetu sisi sote, atakosaje kutukirimia na mambo yote pamoja Naye?" Warumi 8:32. Baba alimtoa Roho Wake bila kipimo kwa Mwana Wake, na sisi pia tunaweza kushiriki ukamilifu Wake. Yesu anasema "basi ikiwa ninyi mlio waovu mnajua kuwapa watoto wenu vipawa vyema, je! Baba aliye mbinguni hatazidi sana kuwapa Roho Mtakatifu hao wamwombao?" Luka 11: 13. "Mkiomba lolote kwa Jina Langu, nitafanya.” "Ombeni, nanyi mtapata; furaha yenu iwe timilifu.” Yohana 14:14; 16:24. [GC 477.1; PK Aya ya 45]

Ijapokuwa maisha ya Mkristo yanatakiwa kuwa na sifa ya unyenyekevu, hayapaswi kuwa ya huzuni na kutojithamini. Ni fursa ya kila mtu kuishi kwa njia ambayo Mungu atamkubali na kumbariki. Kamwe si mapenzi ya Baba yetu wa mbinguni kwamba tuwe chini ya hukumu na giza daima. Hakuna ushahidi wa unyenyekevu wa kweli katika kutembea kwa unyonge huku kichwa kimeinamishwa chini na moyo ukiwa umejazwa na mawazo ya ubinafsi. Tunaweza kumwendea Yesu ili tutakaswe na kusimama mbele ya sheria bila aibu wala hatia. "Sasa, basi, hakuna hukumu ya adhabu juu yao walio katika Kristo Yesu." Warumi 8:1. [GC 477.2; PK Aya ya 46]

Kwa njia ya Yesu wana wa Adamu walioanguka wanakuwa “wana wa Mungu.” "Maana Yeye atakasaye na hao wanaotakaswa wote pia watoka kwa mmoja. Kwa ajili hii haoni haya kuwaita ndugu Zake." Waebrania 2:11. Maisha ya Mkristo yanapaswa kufumbatwa na imani, ushindi na furaha katika Mungu. "Kwa maana kila kitu kilichozaliwa na Mungu huushinda ulimwengu; na huku ndiko kushinda kuushindako ulimwengu, hiyo imani yetu." 1 Yohana 5:4. Mtumishi wa Mungu Nehemia alisema ukweli huu: “furaha ya Bwana ni nguvu zenu." Na Paulo anasema: “Furahini katika Bwana sikuzote; tena nasema, Furahini." “Furahini siku zote. Ombeni bila kukoma. Shukuruni kwa kila jambo; maana hayo ni mapenzi ya Mungu kwenu katika Kristo Yesu.” Wafilipi 4:4; 1 Wathesalonike 5:16-18. [GC 477.3; PK Aya ya 47]

Hayo ndiyo matunda haswa ya uongofu na utakaso wa Biblia; Na ni kwa sababu kanuni kuu za haki zilizotajwa katika sheria ya Mungu hazipendwi sana na ulimwengu wa Kikristo ndiyo maana matunda haya ni nadra sana kuonekana. Ndiyo maana kuna udhihirisho mdogo sana wa kazi hiyo ya kina na yenye uendelevu ya Roho wa Mungu ambayo iliambatana na harakati za uamsho katika miaka ya mwanzo. [GC 478.1; PK Aya ya 48]

Ni kwa kutazama ndiyo tunabadilishwa. Na ikiwa zile kanuni takatifu ambazo ndani yake Mungu amewafunulia watu ukamilifu na utakatifu wa tabia Yake zinapopuuzwa, na akili za watu zikavutwa kutafakari mafundisho na nadharia za kibinadamu, hatupaswi kushtuka kwamba kilichofuatia ni poromoko la utakatifu ulio hai makanisani. Asema Bwana; "Wameniacha Mimi, niliye chemchemi ya maji ya uzima, wamejichimbia mabirika, mabirika yavujayo, yasiyoweza kuweka maji." Yeremia 2:13. [GC 478.2; PK Aya ya 49]

“Heri mtu yule asiyekwenda Katika shauri la wasio haki.... Bali sheria ya Bwana ndiyo impendezayo; na sheria Yake huitafakari mchana na usiku. Naye atakuwa kama mti uliopandwa Kandokando ya vijito vya maji, Uzaao matunda yake kwa majira yake, Wala jani lake halinyauki; Na kila alitendalo litafanikiwa.” Zaburi 1:1-3. Ni pale tu ambapo sheria ya Mungu inaporudishwa kwenye nafasi yake stahiki ndipo kunaweza kuwepo na uamsho wa imani na utauwa wa awali miongoni mwa watu wa Mungu. “Bwana asema hivi, Simameni katika njia kuu, mkaone, mkaulize habari za mapito ya zamani, I wapi njia iliyo njema? Mkaende katika njia hiyo, nanyi mtajipatia raha katika nafsi zenu." Yeremia 6:16. [GC 478.3; PK Aya ya 50]

# SURA YA 28

# KUKABILIANA NA KUMBUKUMBU YA MAISHA

## (Hukumu Ya Upelelezi Kabla Ya Siku Ya Mwisho)

Ufupisho: Ni somo gani lililo na umuhimu zaidi kuliko lile la hukumu. Ni muhimu sana tujifunze yote tuwezayo kuhusu siku hii kuu ambayo inakuja hivi karibuni. Biblia inatuambia mengi sana juu yake. Lini itakuwa,itaendeshwaje, nani atashiriki, vitabu vya kumbukumbu, na Kanuni zitakazotumika kuhukumu. Hukumu ya upelelezi ni mojawapo ya matukio mazito ya historia ya mwanadamu, tukio linalomuhusu kila mmoja wetu. Twabidishwa tujitayarishe kwa siku hiyo.

"Nikatazama" Asema nabii Daniel, hata viti vya enzi vikawekwa, na Mmoja aliye Mzee wa Siku ameketi; mavazi Yake yalikuwa meupe kama theluji, na nywele za kichwa Chake kama sufu safi; Kiti Chake cha enzi kilikuwa miali ya moto, na gurudumu zake moto uwakao. Mto kama wa moto ukatoka ukapita mbele Zake; maelfu elfu wakamtumikia, na elfu kumi mara elfu kumi wakasimama mbele Zake; hukumu ikawekwa, na vitabu vikafunuliwa." Danieli Danieli 7:9, 10. [GC 479.1; PK Aya ya 1]

Hivyo ndivyo nabii Danieli alivyoonyeshwa katika njozi siku hii kuu na ya kutisha, wakati tabia na maisha ya wanadamu yatakapopita na kuchunguzwa mbele ya Jaji Mkuu wa ulimwengu wote (kama mkanda wa video!), na kila mtu atakapolipwa "sawasawa na matendo yake." Mzee huyo wa Siku ni Mungu Baba. Asema Mwandishi wa Zaburi: "Kabla haijazaliwa milima, wala hujaiumba dunia, na tangu milele hata milele Ndiwe Mungu." Zaburi 90:2. Ni Yeye Ndiye Chimbuko la uhai, na Chemchemi ya Sheria yote, ambaye atakayekikalia kiti cha hukumu hiyo (atasimamia kama Mwenyekiti!) Na malaika watakatifu wakiwa wahudumu na mashahidi, idadi yao "elfu kumi mara elfu kumi, na maelfu elfu," wanahudhuria katika Mahakama hii kuu. [GC 479.2; PK Aya ya 2]

"Nikaona katika njozi za usiku, na tazama, Mmoja aliye mfano wa mwanadamu akaja pamoja na mawingu ya mbingu akamkaribia huyo Mzee wa Siku, wakamleta karibu Naye. Naye akapewa mamlaka, na utukufu, na ufalme, ili watu wa kabila zote, na taifa zote, na lugha zote, wamtumikie; mamlaka Yake ni mamlaka ya milele, ambayo hayatapita kamwe, na ufalme usioweza kuangamizwa." Danieli 7:13, 14. ujio wa pili wa Kristo unaoelezwa hapa sio kule kuja Kwake mara ya pili katika dunia hii. Anakuja kwa Mzee wa Siku mbinguni apewe mamlaka, na utukufu, na ufalme, ambao atapewa mwisho wa kazi Yake kama Mpatanishi wetu. Ni ujio huu, ndio uliotabiriwa katika unabii kuwa utatimizwa mwishoni mwa siku 2300 mwaka 1844 na siyo kuja Kwake kwa mara ya pili hapa duniani. Akiwa anasindikizwa na malaika wa mbinguni, Kuhani wetu Mkuu anaingia katika Patakatifu pa Patakatifu na pale anakwenda mbele ya Mungu apate kutenda shuguli Yake ya mwisho ya huduma Yake kwa ajili ya mwanadamu - kufanya kazi ya Hukumu ya Upelelezi na kufanya Upatanisho kwa wote wanaoonekana kuwa wananastahili kupata manufaa Yake (upendeleo Wake, Maslahi yatokanayo na kafara Yake). [GC 479.3; PK Aya ya 3]

Katika huduma ya kivuli mfano ni wale tu waliokuwa wamekuja mbele Zake Mungu wakiungama na kutubu, na ambao dhambi zao kwa njia ya sadaka ya dhambi zilihamishiwa katika chumba cha Patakatifu, ndio ambao walikuwa na sehemu katika huduma ya Siku Kuu ya Upatanisho. Kwa hiyo, katika Siku Kuu ya Upatanisho wa mwisho na Hukumu ya Upelelezi kesi peke yake zitakazoshugulikiwa zitakuwa ni zile tu watu wanaodai kuwa watu wa Mungu. Hukumu ya waovu ni kazi tofauti, na inayojitegemea, nayo inatokea katika kipindi kile cha baadaye. "Kwa maana wakati umefika wa hukumu kuanza katika nyumba ya Mungu; na ikianza kwetu sisi, mwisho wao wasioitii injili ya Mungu utakuwaje?" 1 Petro 4:17. [GC 480.1; PK Aya ya 4]

Vitabu vya kumbukumbu mbinguni, ambavyo ndani yake majina na matendo ya wanadamu huandikwa, vitatumiwa kufanya maamuzi ya hukumu hii. Nabii Danieli anasena "Hukumu ikawekwa, na vitabu vikafunguliwa." Nabii wa Ufunuo, akieleza tukio hilo pia, anongezea hivi: "Na Kitabu kingine kikafunguliwa, ambacho ni cha uzima; na hao wafu wakahukumiwa katika mambo hayo yaliyoandikwa katika vile vitabu, sawasawa na matendo yao." Ufunuo 20:12 [GC 480.2; PK Aya ya 5]

Kitabu cha Uzima kina majina ya wote ambao wamewahi kuingia katika kazi ya utumishi ya Mungu (huduma). Yesu aliwaagiza wanafunzi Wake, alisema: "Furahini kwa sababu majina yenu yameandikwa mbinguni." Luka 10:20. Paulo anazungumza maneno haya kuhusu watenda kazi wenzake waaminifu, "ambao majina yao yamo katika Kitabu cha Uzima." Wafilipi 4:3. Danieli, akiangalia kushuka chini kuja mpaka kwetu "wakati wa taabu, mfano wake haukuwapo tangu lilipoanza kuwapo taifa hata wakati uo huo" anaeleza kwamba watu wa Mungu watakaookolewa, "kila mmoja atakayeonekana ameandikwa katika kitabu kile." Naye Nabii wa Ufunuo Yohana anasema kwamba wataingia katika jiji la Mungu, wale tu ambao majina yao "yameandikwa katika kitabu cha uzima cha Mwana-Kondoo." Danieli 12:1; Ufunuo 21:27. [GC 480.3; PK Aya ya 6]

"Kitabu cha Ukumbusho" ambacho kimeandikwa mbele Zake Mungu, ambamo ndani yake yameandikwa matendo mema ya "hao waliomcha BWANA, na kulitafakari Jina Lake." Malaki 3:16. Maneno yao ya imani, matendo yao ya upendo, huandikwa mbinguni. Nehemia anaielezea habari hiyo anaposema: "Unikumbukie hayo, Ee Mungu wangu…….wala usifute fadhili zangu nilizozitenda kwa ajili ya nyumba ya Mungu wangu." Nehemia 13:14. Katika kitabu hicho cha kumbukumbu cha Mungu kila tendo la haki walilolifanya wanadamu limeandikwa humo nalo hudumu humo milele. Humo kila jaribu lilopingwa, kila uovu walioushinda, kila neno la huruma lilolitamkwa, linaandikwa kwa uaminifu. Na kila tendo la kujitoa kafara, kila teso na huzuni iliyopitiwa kwa ajili Yake Kristo huandikwa humo. Asema hivi Mwandishi wa Zaburi: "Umehesabu kutanga-tanga

kwangu; uyatie machozi yangu katika chupa Yako; Je, hayamo katika kitabu Chako?" Zaburi 56:8. [GC 481.1; PK Aya ya 7]

Pia huko iko Kumbukumbu ya Dhambi za Wanadamu. "Kwa maana Mungu ataleta hukumuni kila kazi, pamoja na kila neno la siri, likiwa jema au likiwa baya." Alisema hivi Mwokozi: "Kila neno lisilo maana watakalolinena wanadamu, watatoa hesabu ya neno hilo siku ya hukumu.": "Kwa maneno yako utahesabiwa haki, na kwa maneno yako utahukumiwa." Mhubiri 12:14; Mathayo 12:36, 37. Makusudi na nia ya siri vinaonekana kwenye kumbukumbu ya kitabu hicho kisichokosea; kwa kuwa Mungu "atayamulikisha yaliyositirika ya giza, na kuyadhihirisha mashauri ya mioyo."1 Kor 4:5. "Tazama, Neno hili limeandikwa mbele Zangu, ... maovu yenu, na maovu ya baba zenu pamoja, asema Bwana." Isaya 65:6, 7. [GC 481.2; PK Aya ya 8]

Kazi ya kila mwanadamu inachunguzwa/inahakikishwa mbele za Mungu, tena inasajiliwa ama kwa uaminifu au kwa kukosa uaminifu. Kando ya kila jina katika vitabu vya mbinguni pameandikwa kwa usahihi wa kutisha kila neno lisilo sahihi, kila tendo la ubinafsi na uchoyo, kila wajibu ambao haukutimizwa, na kila dhambi ya siri, na kila hila au unafiki uliofanywa kwa werevu ili usionekane. Maonyo au makaripio yaliyotumwa na mbingu na kupuuzwa, muda uliopotezwa bure, fursa ambazo hazikufanyiwa kazi, mvuto au ushawishi uliotolewa ukahamasisha wema au ubaya, pamoja na matokeo yake kwa mapana, mambo hayo yote yanasimuliwa katika kumbukumbu zenye tarehe na malaika anayetunza kumbukumbu hizo. [GC 482.1; PK Aya ya 9]

**Kipimo Kinachotumika Katika Hukumu**

Sheria ya Mungu* ndicho kiwango ambacho kitakachotumika kupimia tabia na maisha ya wanadamu katika hukumu. Alisema mtu mwenye hekima: "Hii ndiyo jumla ya maneno; yote yamekwisha sikiwa; Mche Mungu, nawe uzishike amri Zake, maana kwa jumla ndiyo impasayo mtu. Kwa maana Mungu ataleta hukumuni kila kazi." Mhubiri12:13, 14. Mtume Yakobo anawaonya ndugu zake, akisema: "Semeni ninyi, na kutenda kama watu watakaohukumiwa kwa sheria ya uhuru." Yakobo 2:12 *(Amri, Maagizo, Shuhuda, Kanuni, Neno Lake….). [GC 482.2; PK Aya ya 10]

Wale ambao katika hukumu "wanahesabiwa kuwa wamestahili" watakuwa na sehemu katika ufufuo wa wale wenye haki. Yesu alisema: "Lakini wale wahesabiwao kuwa wamestahili kuupata ulimwengu ule, na kule kufufuka katika wafu...... huwa sawasawa na malaika, nao ni wana wa Mungu, kwa vile walivyo wana wa ufufuo" Luka 20:35, 36. Na tena anasema kuwa "wale waliofanya mema" watatoka "kwa ufufuo wa uzima." Yohana 5:29. Wenye haki waliokufa hawatafufuliwa mpaka baada ya hukumu hii kufungwa ambayo kwayo

wamehesabiwa kuwa wanastahili kuupata huo “ufufuo wa uzima. Hivyo basi, hawatakuwepo huko mahakamani kimwili wakati kumbukumbu zao za maisha zinapochunguzwa na kesi zao kuamuliwa. [GC 482.3; PK Aya ya 11]

Yesu atakuwepo pale kama Mtetezi/Wakili wao, akifanya maombezi na kusihi mbele Zake Mungu kwa niaba yao. “Na kama mtu akitenda dhambi tunaye Mwombezi kwa Baba, Yesu Kristo Mwenye haki.” “Kwa sababu Kristo hakuingia katika Patakatifu palipofanyika kwa mikono, ndiyo mfano wa Patakatifu halisi; bali aliingia mbinguni hasa, aonekane sasa usoni pa Mungu kwa ajili yetu.” “Naye, Kwa sababu hii, aweza kuwaokoa kabisa wale wamjiao Mungu kwa Yeye, maana Yu hai siku zote ili awaombee.” Waebrania 9:24; 7:25. [GC 482.4; PK Aya ya 12]

***Kumbukumbu Yafunuliwa**

Vitabu vya kumbukumbu vilifunuliwa katika hukumu hiyo, maisha ya wale wote waliopata kumwamini Yesu huja kuchunguzwa mbele Zake Mungu (bila ya wao kuwapo pale kimwili). Uchunguzi ulifanywa kwa kuanza na wale waliotangulia kwanza kuishi duniani humu (Adamu na Hawa), Wakili wetu anaziwasilisha kesi za kila kizazi baada ya kizazi mbele Yake, na kisha anamalizia na kesi za walio hai. Kila jina linatajwa, kila kesi huchunguzwa kwa umakini wa karibu sana. Majina mengine yanakubaliwa majina mengine yanakataliwa. Ikiwa kuna jina lolote ambalo lina dhambi ambazo hazijatubiwa wala kusamehewa, majina yao yataondolewa katika kitabu cha uzima, na kumbukumbu ya matendo yao mema itafutwa katika kitabu cha Mungu cha ukumbusho. Mungu alitangaza kwa Musa: “Mtu ye yote aliyenitenda dhambi ndiye nitakayemfuta katika kitabu changu.” Kutoka 32:33. Naye nabii Ezekieli anasema: “Bali mwenye haki atakapoghairi, na kuiacha haki yake, na kutenda uovu … Katika matendo yake yote ya haki aliyoyatenda halitakumbukwa hata mojawapo.” Ezekieli 18:24. [GC 483.1; PK Aya ya 13]

Wale wote waliotubu dhambi zao kweli kweli, na kwa imani wakadai damu ya Kristo iwe kafara yao ya upatanisho, wana msamaha ambao umeingizwa mbele ya majina yao katika vitabu vya mbinguni; kwa kuwa wamekuwa washirika wa haki ya Kristo, na tabia zao zimeonekana kuwa zinapatana kabisa na sheria ya Mungu, dhambi zao zitafutwa katika vitabu, nao watahesabiwa kuwa wanastahili kuupata uzima wa milele. Bwana anasema kupitia kwa nabii Isaya: “Mimi, naam, Mimi Ndimi niyafutaye makosa yako kwa ajili Yangu Mwenyewe, wala sitazikumbuka dhambi zako.” Isaya 43:25. Yesu alisema: “Yeye ashindaye atavikwa hivyo mavazi meupe, wala sitalifuta kamwe jina lake katika kitabu cha uzima, Nami nitalikiri jina lake mbele za Baba Yangu, na mbele ya malaika zake.” “Basi, kila mtu atakayenikiri mbele ya watu, Nami nitamkiri mbele za Baba Yangu aliye mbinguni. Bali mtu ye yote atakayenikana mbele ya watu,

Nami nitamkana mbele za Baba Yangu aliye mbinguni." Ufunuo 3:5; Mathayo 10:32,33. [GC 483.2; PK Aya ya 14]

Shauku ya kina inayooneshwa miongoni mwa wanadamu katika maamuzi ya mahakama za kidunia huwakilisha kwa uhafifu tu shauku inayodhihirishwa katika mahakama wa mbinguni wakati majina yaliyoingizwa katika kitabu cha uzima yanapoletwa kupitiwa mbele ya Hakimu wa ulimwengu wote. Mwombezi wetu wa mbinguni (Kiungu) anawasilisha ombi kwamba wale wote walioshinda kwa imani katika damu Yake wasamehewe dhambi zao, kwamba wapate kurejeshwa nyumbani kwao Edeni, na wavikwe taji kama warithi pamoja Naye wa ile "mamlaka ya kwanza." Mika 4:8. Shetani katika juhudi yake yote ya kuidanganya na kuijaribu jamii yetu ya wanadamu alikuwa amekusudia kuharibu mpango wa Mungu wa kumwumba mwanadamu; lakini sasa Kristo anaomba kwamba mpango huu utekelezwe sasa kana kwamba mwanadamu hakuwahi kuanguka kamwe. Anawaombea watu Wake si tu msamaha na kuhesabiwa haki, timilifu na kamili, bali pia kwamba wapate kushiriki sehemu katika utukufu Wake na waketishwe katika kiti Chake cha enzi. [GC 483.2; PK Aya ya 15]

Wakati Yesu akiwaombea wanufaikaji wa neema Yake, Shetani anawashtaki mbele za Mungu kama wakosaji. Mdanganyaji mkuu huyu alitafuta kuwaingiza katika mashaka, kuwafanya wapoteze ujasiri kwa Mungu, kwa kumtilia mashaka, kuwafanya wajitenge mbali na upendo wa Mungu, na wavunje sheria Yake. Sasa anawaonyesha kumbukumbu za maisha yao, kuwaonyesha dosari walizo nazo katika tabia zao, jinsi wasivyofanana na Kristo, jambo ambalo limemwaibisha Mkombozi wao, akiwaonyesha dhambi zote alizowashawishi kuzitenda, na kwa sababu ya dhambi hizi, anadai kwamba wao nira raia wake, yaani wako chini ya ufalme wake. [GC 484.1; PK Aya ya 16]

Yesu hatoi udhuru kwa ajili ya dhambi zao, bali anaonyesha toba na imani yao, na, anadai msamaha kwa ajili yao, ananyosha mikono Yake iliyojeruhiwa mbele za Baba Yake na mbele ya malaika Zake watakatifu, akisema: "Nawajua kwa majina yao. Nimewachora katika viganja vya mikono Yangu. "Dhabihu za Mungu ni roho iliyovunjika; ni moyo uliovunjika na kupondeka, Ee Mungu, hutaudharau." Zaburi 51:17. Na kwa yule mshtaki wa watu Wake anasema: "BWANA na akukemee, Ewe Shetani; naam, BWANA, aliyechagua Yerusalemu, na akukemee; je! hiki si kinga kilichotolewa motoni?" Zekaria 3:2. Kristo aliwavika waaminifu Wake haki Yake Mwenyewe, ili apate kuwawasilisha mbele za Baba Yake wakiwa kama "Kanisa tukufu, lisilo na hila wala kunyanzi wala lolote kama hayo: bali liwe takatifu lisilo na mawaa." Waefeso 5:27. Majina yao yamebaki yakiwa yameandikwa katika kile kitabu cha uzima, na kwa habari kuhusu wao imeandikwa: "Nao watakwenda pamoja Nami hali wamevaa mavazi meupe, kwa kuwa wamestahili." Ufunuo 3:4. [GC 484.2; PK Aya ya 17]

Kwa njia hiyo utimilifu kamili wa ahadi ya agano jipya utatimia: “Maana nitausamehe uovu wao, wala dhambi yao sitaikumbuka tena.” “Katika siku hizo na wakati huo, asema BWANA, uovu wa Israeli utatafutwa, wala uovu hapana; na dhambi za Yuda zitatafutwa, wala hazitaonekana.” Isaya 31:34; 50:20. “Siku hiyo Chipukizi la BWANA litakuwa zuri, lenye utukufu na matunda ya nchi yatakuwa mema sana, na kupendeza, kwa ajili ya Waisraeli wale waliookoka. Tena itakuwa ya kwamba yeye aliyebaki katika Sayuni, na yeye aliyeachwa ndani ya Yerusalemu, ataitwa mtakatifu; yaani, kila mmoja aliyeandikwa miongoni mwa hao walio hai ndani ya Yerusalemu.” Isaya 4:2,3. [GC 485.2; PK Aya ya 18]

Kazi ya hukumu ya upelelezi na utakasaji/ufutaji wa dhambi inapaswa kukoma kabla ya Bwana wetu Yesu kuja mara ya pili. Kwa kuwa watu waliokufa wanapaswa kuhukumiwa kutokana na mambo yale yaliyoandikwa katika vitabu vile, haiwezekani kwamba dhambi za wanadamu hawa zinafutwe mpaka baada ya hukumu hiyo, ambapo kesi zao zinachunguzwa. Lakini Mtume Petro anaeleza waziwazi kwamba dhambi za waamini zitafutwa zitakapokuja “nyakati za kuburudishwa kwa kuwako Kwake Bwana; apate kumtuma Kristo.” Matendo 3:19,20. Wakati wa hukumu ya Upelelezi itakapofungwa, Kristo atakuja, na ujira Wake utakuwa pamoja Naye kumlipa kila mtu kama kazi yake sawasawa na matendo yake. [GC 485.2; PK Aya ya 19]

Katika huduma ya mfano-kivuli ya Patakatifu pa duniani, kuhani mkuu, baada ya kufanya upatanisho kwa ajili ya Israeli, alitoka nje na kuwabariki makutano. Kadhalika Kristo Naye, mwishoni mwa kazi Yake kama Mwombezi, Mpatanishi na Mtetezi, atatokea, ‘pasipo dhambi, kwa hao wamtazamiao kwa wokovu,’ (Waebrania 9:28), kuwabariki watu Wake wanaomngojea kwa kuwapa uzima wa milele. Kama vile kuhani, katika kuiondoa dhambi kutoka katika hema la Patakatifu, aliziungama dhambi juu ya kichwa cha mbuzi wa Azazeli, kadhalika Kristo Naye atakaweka dhambi zote juu ya Shetani, mwasisi na mbunifu wa dhambi. Yule mbuzi wa Azazeli, akiwa amebeba dhambi za Israeli, alipelekwa mbali mpaka katika nchi “isiyo na watu” (Mambo ya Walawi 16:22); kadhalika Shetani naye, akiwa amebeba hatia ya dhambi zote alizosababisha watu wa Mungu kuzitenda, atakafungwa kwa miaka elfu moja katika dunia hii, ambayo kwa wakati huo itakuwa tupu, yaani ukiwa bila watu, na hatimaye atapewa adhabu ya mwisho na kamili ya dhambi zake katika moto utakaowaangamiza waovu wote. Hivyo Mpango Mkuu wa Ukombozi utafikia ukamilifu wake kwa kuiangamiza dhambi kwa mara ya mwisho na wokovu wa wale wote waliokuwa tayari kuachana na uovu. [GC 485.2; PK Aya ya 30]

**Wakati Uliowekwa Ulipofika**

Wakati uliopangwa kwa ajili ya hukumu-- mwisho wa zile siku 2300, mwaka wa 1844-- ilianza kazi ile upelelezi na utakaso wa dhambi- kuzifuta dhambi.

Wote wale ambao wamelwahi kulibeba wenyewe jina la Kristo ni lazima wapitishwe katika uchunguzi huo mkali na wa kina. Makundi yote mawili yaani walio hai na wafu lazima wahukumiwe "katika yale yaliyoandikwa katika vile vitabu, sawasawa na matendo yao." (Uf 20:12) [GC 486.1; PK Aya ya 31]

Dhambi ambazo hazikuungamwa na kuachwa hazitasamehewa, wala kufutwa katika vitabu vya kumbukumbu, bali zitabaki kusimama kama ushahidi dhidi ya mwenye dhambi huyo katika siku ile ya Mungu. Anaweza kuwa alizitenda katika nuru ya mchana au katika giza la usiku; lakini zililikuwa waziwazi na dhahiri mbele Yake Yeye ambaye sisi tunapaswa kuwajibika Kwake (Zab. 139:1 -12). Malaika Zake Mungu walikuwa wakishhudia kila dhambi iliyotendwa, nao wakaisajili katika kumbukumbu zile zisizokosea kamwe. Dhambi inaweza kufichwa, inweza kukanwa, inaweza kufunikwa isipatwe kuonwa na baba, mama, mke, watoto, marafiki na wale tunaoshirikiana nao; hakuna mtu yeyote anayeweza kujua au kushuku uovu wa moyoni mwa mtu isipokuwa mtu huyo anayetenda uovu (mtu feki); lakini hilo liko wazi kabisa mbele ya akili za mbinguni (malaika). Giza la usiku wenye giza nene, usiri wa sanaa zote za hila zilizotumika, halitoshi kulificha wazo hata moja lisiweze kujulikana kwa Yule aliyepo Milele zote. Mungu anayo kumbukumbu sahihi ya kila taarifa isiyo ya haki, au ambayo si sahihi pamoja na kila tendo la uonevu lililofanywa kwa watu. Yeye hadanganywi kwa mwonekano wa nje wa uchaji Mungu au utakatifu. Yeye hafanyi kosa lolote katika kutathmini tabia ya mtu. Wanadamu wanaweza kudanganywa na wale walio  na uovu mioyoni mwao, lakini Mungu anapenya ndani ya vificho vyote vya nje vya kinafiki na kusoma maisha ya ndani. [GC 486.2; PK Aya ya 32]

Wazo hili linatisha kiasi gani! Siku baada ya siku, inapotokomea katika umilele, hubeba mzigo wake wa kumbukumbu za kuandikwa katika vitabu vya mbinguni. Maneno yetu mara tu yanapotamkwa, matendo yetu mara tu yanapotendwa, hayawezi kurudishwa kamwe. Malaika wamekwisha kuyaandika yote mawili, mema na mabaya, katika kumbukumb (Mhu.5:6; 12:14). Mshindi mwenye nguvu vitani na aliye hodari kuliko wote hapa duniani hana uwezo wowote wa kuirudisha au kuifuta kumbukumbu yake hata ya siku moja tu (rewind or delete). Matendo yetu, maneno yetu, hata nia zetu za sirini kabisa zinazotufanya kutenda matendo yetu, mambo hayo yote yana uzito wake katika kuamua hatima ya maisha yetu ya milele kama yatakuwa ya ubaya na huzuni ya wema na faraja. Ingawa sisi huenda tutakuwa tumeyasahau yote, yatatoa ushahidi wake katika kutupatia haki au kutupa hukumu [Gal. 6:3-5; Mdo. 3:19]. [GC 486.3; PK Aya ya 33]

Kama vile alama za usoni zinavyonakiliwa kwa usahihi jinsi zilivyo kwa usahihi usiokosea juu ya bamba lililong'arishwa la mchoraji, kadhalika tabia yetu imenakiliwa kwa uaminifu katika vitabu vya juu mbinguni. Lakini ni hofu ndogo

mno kiasi gani inahisiwa kuhusiana na kumbukumbu yao ambayo inapaswa ikodolewe na macho ya wakazi wa mbinguni! Laiti kama pazia lile linalotenganisha ulimwengu huu unaoonekana na ule usioonekana kwa macho lingeweza kuvutwa nyuma, kisha wana wa wanadamu wapate kumwona yule malaika anayeandika kila neno na kila tendo ambalo ni lazima wakutane nalo tena katika hukumu siku ya mwisho, sijui ni maneno mangapi yanayotamkwa kila siku yangebaki bila kusemwa, na ni matendo mangapi yangebaki bila kutendwa. [GC 487.1; PK Aya ya 34]

Katika hukumu hiyo uchunguzi wa makini utafanywa kuhusiana na jinsi kila talanta/vipawa tulivyopewa vilivyotumika. Je, tunautumiaje mtaji tuliokopeshwa na Mbingu? Je, Bwana atakaporudi atapata iliyo Yake pamoja na faida? (Mt. 25:14-30.) Je, tumeboresha nguvu zile tuliodhaminiwa, yaani, nguvu za mikono yetu na moyo wetu na bongo zetu, kwa ajili ya utukufu Wake Mungu kwa ajili ya kuuletea mibaraka ulimwengu huu? Je, tumeutumiaje muda wetu, kalamu zetu, sauti zetu, pesa zetu, na mvutowetu? Tumemfanyia nini Kristo katika utu wa wale walio maskini, wanaoteseka, yatima, au mjane? (Mt. 25) Mungu ametufanya sisi kuwa walinzi na wahifadhi wa Neno Lake Takatifu; je, tumefanya nini na nuru na Ukweli tuliopewa ili kuwahekimisha wanadamu hata wapate wokovu? (2 Tim. 3:15-17.) Hakuna thamani yoyote ambayo meambatanishwa na madai ya mdomo tu, ya kumkiri Kristo kwa imani tu bila matendo; upendo ule ambao unadhihirishwa kwa vitendo, ndio pekee unahesabiwakuwa wa dhati. Hata hivyo, ni upendo pekee ndio hulifanya tendo lolote liwe na thamani mbele ya macho ya Mbingu. Lolote linalotendwa kutokana na upendo, hata lingeonekana kwa udogo kiasi gani katika makadirio ya wanadamu, linakubaliwa na kupewa thawabu yake na Mungu. [GC 487.2; PK Aya ya 35]

Uchoyo wa wanadamu uliofichika huwekwa wazi, yaani hufuniliwa katika vitabu vya mbinguni. Pale kuna kumbukumbu ya wajibu ambao haukutimizwa kwa wanadamu wenzao, na usahaulifu wa madai ya Mwokozi aliyo nayo juu yao. Kule wataona ni mara ngapi walimpa Shetani wakati wao, mawazo yao, na nguvu zao, vyote hivyo ambavyo ni vilikuwa ni mali Yake Kristo. Kumbukumbu ambazo malaika wanazichukua na kwenda nazo mbinguni ni za kuhuzunisha kiasi gani. Wanadamu ambao ni Viumbe wenye akili nyingi, nao hutangaza kuwa ni wafuasi Wake Kristo, wametumbukia katika shimo la kuchuma mali ya ulimwengu huu na kujifurahisha na anasa za ulimwengu huu. Pesa, wakati, na nguvu hutolewa kafara kwa ajili ya kujionyesha na kuendekeza tamaa ya mambo ya ulimwengu huu; lakini ni muda mchache sana unaotumiwa kwa ajili ya maombi, kwa ajili ya kuchunguza Maandiko, katika kuinyenyekesha nafsi na kuungama dhambi. [GC 487.3; PK Aya ya 36]

Shetani hubuni mbinu zisizo na idadi ili kushikilia akili zetu, ili zisijikite katika kushugulikia kazi ile ambayo tunapaswa kuifahamu vizuri zaidi kuliko jambo jingine lolote. Mlaghai huyo mkuu huyu anachukia Kweli zile kuu zinazodhihirisha wazi kafara ya upatanisho na Mwombezi Mwenye nguvu zote (Ebr 7:25). Anajua kwamba kwa upande wake yeye, kila kitu kinategemea kazi yake ya kuelekeza akili za watu mbali na Yesu na Ukweli Wake. [GC 488.1; PK Aya ya 37]

**Njia Ya Kuufikia Utakatifu**

Wale ambao wanapaswa kuwaeleza wengine manufaa ya upatinisho na pia kujipatia wenyewe manufaa hayo ya kazi ya Mwokozi ya Upatanishi, hawapaswi kuruhusu kitu chochote kuingilia wajibu wao wa kuwa na utakatifu kamili katika kumcha Mungu. Saa zao za thamani, badala ya kuzitumia kwa mambo ya anasa, kujionyesha, au kutafuta mapato, zinapaswa kutumiwa usomaji/Ujifunzaji wa Neno la Kweli kwa moyo wa dhati na bidii na maombi. Somo la Patakatifu (the Sanctuary) na Hukumu ya Upelelezi (the Investigative Judgment) linapaswa lieleweke kikamilifu kwa watu wa Mungu. Wote wanahitaji kuwa na ujuzi wao binafsi wa mahali alipo na kazi anayofanya Kuhani wao Mkuu (Yesu Kristo Ebr. 4:14-16) Vinginevyo, haitawezekana kwao kuifanyia mazoezi imani yao ambayo ni ya muhimu sana kwa wakati huu au kujaza nafasi ile ambayo Mungu amekusudia waijaze. Kila mtu peke yake ana nafsi ya kuiokoa au kuipoteza. Kila mtu anayo kesi inayomngojea katika Mahakama ya Mungu. Kila mtu inampasa kukutana na Jaji Mkuu uso kwa uso (mbashara kwa njia ya kumbukumbu katika vitabu – 2 Kor. 5:10). Kwa hiyo basi, ni jambo la muhimu kiasi gani kwamba, kila mtu aitafakari mara kwa mara mandhari hiyo ya kutisha wakati hukumu itakapokaa na vitabu vitakapofunuliwa, wakati pamoja Danieli, kila mtu peke yake atapaswa kusimama katika kizimba chake mwenyewe, mwisho wa siku au kura yake mwenyewe. (Dan. 7:9,10 na 12:13). [GC 488.2; PK Aya ya 38]

Wale wote ambao wamepokea nuru juu ya masomo haya (Patakatifu na Hukumu ya upelelezi) inawapasa kutoa kwa wengine ushuhuda wao kuhusu Kweli hizi kuu ambazo Mungu amewakabidhi. Patakatifu kwenye hekalu la mbinguni ndiyo kituo mahsusi cha kazi ya Kristo kwa ajili ya wanadamu. Panahusu kila mtu anayeishi anayeishi humu duniani. Panatufunulia sisi wazi mpango wa ukombozi na kutuleta karibu kabisa na mwishowa wakati na kutufunulia suala la ushindi la pambano kati ya haki na dhambi (wema na ubaya). Hili ni suala la muhimu sana, kwamba wote wanapaswa wajifunze masomo haya (mawili) kwa kina na waweze kumjibu kila mtu awaulizaye sababu ya tumaini lililoko ndani yao. [GC 487.3; PK Aya ya 39]

**Maombezi Ya Kristo**

Maombezi ya Kristo kwa ajili ya mwanadamu ndani ya Patakatifu pa hekalu la pale mbinguni ni muhimu sana kwa ajili ya Mpango huo wa Wokovu kama kifo Chake msalabani kilivyo muhimu. Kwa njia ya kifo Chake aliianza kazi ile ambayo baada ya ufufuo Wake alipaa mbinguni kwenda kumalizia (Ebr. 9). Kwa imani sisi tunapaswa kuingia ndani ya pazia, "alimoingia Yesu kwa ajili yetu Mtangulizi wetu." Waebrania 6:20. Mle nuru itokayo katika msalaba wa Kalwari inaakisiwa. Mle ndipo tunaweza kupata uelewa wa wazi zaidi kuhusu siri ya ukombozi (Zab 77:13). Wokovu wa mwanadamu unatekelezwa kwa gharama isiyo na kikomo na mbingu; Kafara ile iliyotolewa inakidhi kabisa madai mapana zaidi ya sheria ya Mungu iliyovunjwa. Yesu amefungua njia ya kuelekea kwenye kiti cha enzi cha Baba, na kwa njia ya upatanisho na maombezi Yake, shauku ya dhati ya wale wote wanaokwenda Kwake kwa imani wanaweza kuwasilishwa kwa Mungu. [GC 489.1; PK Aya ya 40]

"Afichaye dhambi zake hatafanikiwa; bali yeye aziungamaye na kuziacha atapata rehema." Mithali 28:13. Ikiwa wale wanaoficha dhambi zao na kutoa udhuru kwa makosa yao wangeweza kuona jinsi Shetani anavyoshangilia kwa mwenendo wao (mbaya), na jinsi anavyomsuta Kristo pamoja na malaika Zake watakatifu, kwa sababu ya ufichaji na udhuru wao huo, basi wangeharakisha kuungama dhambi zao, na kuziacha. Kupitia dosari katika tabia zetu, Shetani anatenda kazi yake ili kuitawala akili yote, naye anajua vyema kwamba kasoro hizo zikiendekezwa ndani ya mioyo yetu, basi, atafaulu. Kwa hiyo, daima anatafuta kuwahadaa wafuasi wa Kristo, akitumia hila zake zinazofisha kiasi kwamba haiwezekani wao wenyewe kuzishinda. Lakini Yesu anasihi kwa niaba yao haki ile iliyopatikana kwa mikono Yake iliyojeruhiwa, pamoja na mwili Wake uliochubuliwa; naye anawatangazia wale wote ambao wangetaka kumfuata akisema, "Neema Yangu yakutosha." Wakorintho 12:9. "Jitieni nira Yangu, mjifunze Kwangu; kwa kuwa Mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo; nanyi mtapata raha nafsini mwenu. Kwa maana nira Yangu ni laini, na mzigo Wangu ni mwepesi." Mathayo 11:29, 30. Basi, asiwepo mtu yeyote anayefikiria kwamba dosari zake za tabia haziwezi kutibika. Mungu atatoa imani na neema ya kumwezesha kushinda. [GC 489.2; PK Aya ya 41]

Sasa tunaishi katika Siku Kuu ya Upatanisho (at-one-ment). Katika huduma ya mfano katika Patakatifu pale pa duniani, wakati kuhani mkuu alipokuwa akifanya upatanisho kwa ajili ya Israeli, wote walitakiwa kutesa nafsi zao kwa toba na kujinyenyekesha mbele Zake Bwana, ili wasije wakatengwa miongoni mwa watu Wake (Lawi 23). Hali kadhalika, wale wote wanaotaka majina yao yadumu katika Kitabu cha Uzima, wakati wamebakiwa na siku chache tu za muda wao wa rehema, inawapasa sasa kutesa nafsi zao mbele za Mungu kwa kuhuzunikia dhambi zao na kufanya toba ya kweli. Ni lazima kuwepo na kazi ya kujichunguza moyo kwa uaminifu na kina. Roho ya kuyachukulia mambo haya bila umakini au

kirahisi-rahisi kwa kupuuzia na kimchezo-mchezo, inayoendekezwa na watu wengi wanaokiri kwa mdomo kuwa ni wakristo, inapaswa kutupiliwa mbali. Kuna vita kali mbele yetu inayowakabili wote wanaojititahidi kuishinda mielekeo yao ya uovu inayojitahidi kutawala nafsi. Kazi ya kujitayarisha ni kazi ya mtu mmoja mmoja binafsi. Hatuokolewi katika makundi. Usafi wa maisha, ucha Mungu au uadilifu wa mtu mmoja hautaweza kufidia upungufu wa sifa hizi ndani ya mtu mwingine. Ingawa mataifa yote yanapaswa kupita katika hukumu ya Mungu, bado Yeye ataichunguza kesi ya kila mtu mmoja mmoja kwa uyakinifu na kina kana kwamba hakuna kiumbe mwingine yeyote duniani. Kila mmoja ni lazima ajaribiwe na aonekane kuwahana waa, wala kunyanzi, wala kitu chochote cha aina hiyo. [GC 489.3; PK Aya ya 42]

Matukio yale yanayoambatana na kufungwa kwa kazi hiyo ya upatanisho, yaani kazi ya mwisho ni mazito na ya kutisha sana. Maslahi makubwa sana yanahusishwa na kazi hiyo. Hukumu hiyo inaendelea hivi sasa katika Patakatifu pa mbinguni (hekaluni). Kwa miaka mingi (tangu 1844) kazi hiyo imekuwa ikiendelea huko. Hivi karibuni  - hakuna ajuaye ni muda mfupi kiasi gani - hukumu hiyo itahamia kwa kesi za walio hai, yaani watu wanaoishi duniani sasa. Mbele ya uwepo wa kutisha wa Mungu maisha yetu yanapaswa kupelekwa hapo kwaawjil ya uchunguzi (bila ya sisi kuwapo pale kimwili). Wakati huu juu ya nyakati zingine zote, kila mtu anapaswa kulizingatia onyo hili la Mwokozi,:“Angalieni, kesheni, ombeni; kwa kuwa hamjui wakati ule utakapokuwapo.” Marko 13:33. “Walakini usipokesha, nitakuja kama mwivi, wala hutaijua saa nitakayokuja kwako.” Ufunuo 3:3. [GC 490.1; PK Aya ya 43]

**Umilele Wa Watu Wote Utakuwa Umeamuliwa**

Wakati kazi hiyo ya hukumu ya upelelezi itakapofungwa, hatima (umilele) ya wote itakuwa imeamriwaa kwa uzima au mauti. Rehema inafungwamuda mfupi kabla  ya kuonekana kwa Bwana katika mawingu ya mbinguni. Kristo akitazama mbele, anatangaza katika kitabu cha Ufunuo, maneno haya,: “Mwenye kudhulumu na azidi kudhulumu; na mwenye uchafu na azidi kuwa mchafu;na mwenye haki na azidi kufanya haki; na mtakatifu na azidi kutakaswa. Tazama Naja upesi, na ujira Wangu u pamoja Nami, kumlipa kila mtu kama kazi yake ilivyo.” Ufunuo 22:11, 12. [GC 490.2; PK Aya ya 44]

Wenye haki na waovu watakuwa bado wakiishi hapa duniani katika hali ya kufa - watu watakuwa wakipanda na kujenga, wakila na kunywa, wote wakiwa hawana habari kwamba uamuzi wa mwisho usiotenguliwa kuhusu kesi zao umekwisha kukatwa na kutangazwa katika Patakatifu pa mbinguni. Kabla ya Gharika, baada ya Nuhu kuingia ndani ya safina, Mungu alimfungia ndani na kuwafungia nje waovu wasiomcha Mungu; lakini kwa siku saba watu, bila kujua ya kwamba maangamizi yao yalikuwa yamekwisha kupangwa na yasingewezwa

kubadilishwa, waliendelea na maisha yao ya kutokujali kitu, maisha ya kupenda anasa na kuendelea kudhihaki maonyo ya hukumu iliyokuwa ikiwajia mbele yao kwaghafula. Mwokozi asema hivi: “Ndivyo kutakavyokuwa kuja Kwake Mwana wa Adamu.” Mathayo 24:39. Kimya kimya, kama mwizi wa usiku wa manane anayekuja bila kutoa taarifa, saa itafika inayoamua hatima ya kila mmoja ambayo itapanga hatima ya kila mtu, saa ya kuondolewa milele kwa maisha ya kila mwanadamu, yaani, saa ya kuondolewa kwa mara ya mwisho fursa ya rehema Yake kwa mwanadamu mwenye hatia ya dhambi. [GC 491.1; PK Aya ya 45]

“Kesheni basi ... asije akawasili ghafula akawakuta mmelala”, (Marko 13:35,36). Hali hiyo ya hatari sana inawakabili wale ambao wamechoshwa na kukesha, wanageukia vivutio vilivyopo ulimwenguni. Wakati mfanyabiashara amemezwa katika kujishugulisha na kutafuta mapato, wakati mpenda anasa anaendekeza tamaa zake, wakati binti mitindo anapangilia mapambo yake—inawezekana katika saa hiyo Jaji Mkuu wa dunia yote akatangaza hukumu hii: “Umepimwa katika mizani nawe umeonekana kuwa umepunguka.” Danieli 5:27. [GC 491.2; PK Aya ya 45]

# SURA YA 29

# CHIMBUKO LA UOVU

[Dhambi Ilitoka Wapi-Shetani Alikujaje-Kwa Nini Alitupwa Toka Mbinguni]

**(Kwanini Dhambi Na Mateso Viliruhusiwa)**

Ufupisho: Uovu ulianzaje? Kwanini kuna dhambi? Sura hii inajitokeza zaidi katika kitabu hiki kizima kinachohusu zama zote. Soma kisa hiki cha kustaajabisha zaidi--jinsi dhambi ilivyoanza. Ingawa hakuzungukwa na ubinafsi daima, kitu kilitokea. Ni nini kingeweza kumgeuza malaika huyu wa nuru kuwa Shetani na kufanya uovu ndani humo ya mbingu, mbele za Mungu Mwenyewe? Kisa hiki kitakushangaza, wapaswa kukisoma. Kitakuambia ni kwa nini Mungu alilazimika kungojea uovu uive- na wakati ujao mzuri ambao ameuhifadhi kwa watoto Wake……

Kwa akili za watu wengi chimbuko la dhambi au uovu na sababu ya kuwepo kwake ni jambo linalotatanisha sana na kuleta mfadhaiko mkuu. Wanaona matendo mabaya ya uovu, pamoja na matokeo yake ya kutisha yaletayo huzuni, taabu na maangamizi, nao wanahoji inawezekanaje basi haya yote kutokea chini ya utawala Mkuu wa Mwenyezi Mungu, Yule asiye na kikomo katika hekima, nguvu na upendo. Hapo ndipo ilipo siri au lile fumbo ambalo wao hawapati maelezo au ufumbuzi wowote juu yake. Na katika hali yao ya kutokuwa na hakika pamoja na mashaka yao, wanakuwa vipofu wasiweze kuziona zile Kweli zilizofunuliwa kwa uwazi katika Neno la Mungu, ambazo ni za muhimu kwa wokovu wetu. Wapo wale ambao wanajiuliza maswali na kutafuta-tafuta sababu ya uwepo wa dhambi; wanajitahidi sana kufanya utafiti wao juu ya kile ambacho Mungu hajapata kamwe kukifunua; kwa hiyo, hawapati suluhisho lolote la matatizo yao; na kwa watu kama hao wanaochochewa na mashaka, wanachukulia kuukosa ufumbuzi huko kama kisingizio cha kukataa Maneno ya Maandiko Matakatifu. Wengine hata hivyo hawana uelewa wa kutosha kuhusu tatizo hilo kubwa la kuwapo kwa uovu kutokana na ukweli kwamba mapokeo na tafsiri zisizo sahihi vimefunika fundisho la Biblia kuhusu tabia ya Mungu ilivyo hasa, msingi au mfumo wa serikali Yake, na kanuni Zake anazotumia katika kuishughulikia dhambi. [GC 492.1; PK Aya ya 1]

Haiwezekani kabisa kueleza chimbuko la dhambi kwa namna ambayo inawezesha kutoa sababu za kutosheleza kuhusu kuwepo kwake. Hata hivyo bado inawezekana kuelewa kiasi cha kuridhisha kwa mambo haya mawili, chimbuko la dhambi na kuondolewa kwake hatimaye, ili kudhihirisha kwa ukamilifu haki, wema na ukarimu wa Mungu katika kuushughulikia Kwake uovu huo kikamilifu. Hakuna wazo linalofundishwa kwa uwazi zaidi katika Maandiko kuliko wazo kuwa Mungu kwa namna yoyote ile hawajibiki katika kuingia kwa dhambi; kwamba hakuiondoa kiimla au kiholela neema Yake, kwamba hapakuwa dosari yoyote katika Serikali ya Mungu ambayo ingetoa mwanya wa kuinuka kwa uasi. Dhambi ni mvamizi, ambaye hakuna sababu iwezayo kutolewa kwa ajili ya uwepo wake. Ni fumbo, hailezeki, haiwezi kuchunguzwa, kuitolea udhuru ni kuitetea. Kama udhuru wowote kwa ajili ya dhambi ungeweza kupatikana, au sababu yoyote ingeweza kutolewa ya kuwako kwake, basi, ingekoma kuwa dhambi. Fasili yetu ya pekee ya dhambi ni ile iliyotolewa katika Neno la Mungu; yaani dhambi ni "uasi wa sheria;" ni matokeo ya utekelezaji wa kanuni ile inayopingana vita dhidi ya Sheria kuu ya upendo ambayo ndio msingi wa serikali ya Mungu (1 Yoh 3:4). [GC 492.2; PK Aya ya 2]

Kabla ya kuingia kwa uovu palikuwa na amani na furaha katika sayari zote na mbinguni pia. Mambo yote yaliafikiana kikamilifu na mapenzi ya Muumbaji wao. Upendo wao kwa Mungu ulikuwa Juu (Hauna kifani), upendo wa mtu mmoja kwa mwingine ulikuwa hauna upendeleo (haukuwa nusu-nusu). Kristo aliye Neno, Mwana Pekee wa Mungu, alikuwa Mmoja na Baba wa milele,-- Mmoja katika asili, katika tabia, na katika kusudi,-- Mwenye Uhai Pekee katika malimwengu yote ambaye alikuwa na fursa ya kushiriki mashauri na makusudi yote ya Mungu. Kwa njia ya Kristo, Baba alitekeleza uumbaji wa wote wenye uhai walioko mbinguni.... "Kwa kuwa katika Yeye vitu vyote viliumbwa, vilivyo mbinguni na vilivyo juu ya nchi, vinavyoonekana na visivyoonekana; ikiwa ni vitu vya enzi, au usultani, au enzi, au mamlaka; vitu vyote viliumbwa kwa njia Yake, na kwa ajili Yake." Wakolosai 1:16; na kwa Kristo, sawa sawa na vile ilivyokuwa kwa Baba Yake, mbingu yote ilitoa kiapo cha utii. [GC 493.1; PK Aya ya 3]

Sheria ya upendo ikiwa ndiyo msingi wa Serikali ya Mungu, furaha ya viumbe vyote ilitegemea utii wao kamili wa kanuni Zake za haki. Mungu anatamani kupata toka kwa viumbe vyake vyote huduma ya upendo -- ibada na heshima inayotokana na kuithamini, na kuitambua tabia Yake kwa kina kwa kutumia akili zetu. Hafurahishwi na utii unaotolewa Kwake kwa kushurutishwa, tena Yeye huwapa wote uhuru wa kufanya uchaguzi wapendao, ili waweze kumtumikia kwa hiari yao. [GC 493.2; PK Aya ya 4]

**Lusifa Wa Kwanza Miongoni Mwa Makerubi**

Lakini kulikuwa na kiumbe mmoja aliyechagua kuutumia vibaya uhuru huu. Dhambi ilianzia ndani yake huyu ambaye akiwa wa pili baada ya Kristo, alikuwa amepewa heshima kubwa sana na Mungu, naye alikuwa amesimama katika nafasi ya juu sana katika nguvu na Utukufu miongoni mwa wakazi wote wa Mbinguni. Kabla ya kuanguka kwake, Lusifa alikuwa wa kwanza miongoni mwa makerubi wafunikao, akiwa mtakatifu, na safi (asiye na unajisi au waa). "Mwanadamu, umfanyie maombolezo mfalme wa Tiro, umwambie Bwana MUNGU asema hivi: Wewe wakitia Muhuri kipimo, umejaa hekima na ukamilifu wa uzuri. Ulikuwa ndani ya Edeni, bustani ya Mungu; kila jiwe la thamani lilikuwa kifuniko chako, akiki na yakuti manjano, almasi, zabarajadi, shohamu, yaspi, yakuti samawi, zumaridi, baharamani, na dhahabu; kazi ya matari yako na filimbi zako ilikuwa ndani yako; Katika siku ya kuumbwa kwako zilikuwa zimetengenezwa tayari. Wewe ulikuwa Kerubi mwenye kutiwa mafuta afunikaye; Nami nalikuweka hata ukawa juu ya mlima Mtakatifu wa Mungu, umetembea huko na huko kati ya mawe ya moto. Ulikuwa mkamilifu katika njia zako tangu siku ile ulipoumbwa, hata uovu ulipoonekana ndani yako." Ezekieli 28:12-15 [GC 493.3; PK Aya ya 5]

Lusifa alikuwa na uwezekano wa kudumisha fadhila aliyopewa na Mungu, akipendwa na kuheshimiwa na jeshi lote la malaika, akitumia uwezo wake mkuu na bora kuwaletea furaha wengine kuwabariki na kumtukuza Muumbaji wake. Lakini, nabii anasema, “Moyo wako uliinuka kwa sababu ya uzuri wako; umeiharibu hekima yako kwa sababu ya mwangaza wako.” Mstari wa 17. Kidogo kidogo, Lusifa alianza kuendekeza tamaa ya kujikweza mwenyewe. "Basi, kwa hiyo, Bwana MUNGU asema hivi; Kwa kuwa umeweka moyo wako kama moyo wa Mungu;" "Nawe ulisema moyoni mwako,...... Nitapanda mpaka mbinguni, Nitakiinua kiti changu juu kuliko nyota za Mungu; nami nitaketi juu ya mlima wa mkutano, Katika pande za mwisho za kaskazini. Nitapaa kupita vimo vya mawingu, Nitafanana na Yeye Aliye juu." Mstari wa 6, Isaya 14:13, 14. Badala ya kumfanya Mungu aonekane kuwa Ndiye Mkuu kuliko wote katika kupendwa na kuheshimiwa na viumbe Vyake, Lusifa alielekeza nguvu zake kuwashawishi viumbe wa Mungu watoe huduma yao pamoja na utii wao kwake yeye mwenyewe. Naye akitamani sana heshima ambayo Baba wa milele alikuwa amempa Mwana Wake, mkuu huyu wa malaika alitaka sana kujinyakulia mamlaka yale ambayo ilikuwa ni haki Yake Kristo peke yake kuyamiliki na kuyatumia. [GC 494.1; PK Aya ya 6]

Mbingu yote ilikuwa imefurahia kuakisi utukufu wa Muumbaji wao na kuzitangaza sifa Zake. Na wakati Mungu alipoheshimiwa hivyo, hali ilikuwa ya amani na furaha kote. Lakini sauti ya kutokuelewana sasa iliharibu amani na upatanifu wote uliokuwako mbinguni. Kuitumikia na kuiinua juu nafsi, kinyume cha mpango wa Muumbaji, kuliamsha hisia za uovu mioyoni mwa wale ambao walikuwa wameupa kipaumbele utukufu wa Mungu. Mabaraza ya mbinguni

yakamsihi sana Lusifa. Mwana wa Mungu alionyesha mbele yake (Lusifa) ukuu, fadhili, na haki ya Muumbaji, pamoja na utakatifu na tabia ya Sheria Yake ile isiyobadilika (Amri Zake). Mungu Mwenyewe Ndiye aliyekuwa ameuweka utaratibu wa mbinguni; na katika kule kujitenga nao, Lusifa angekuwa anamvunjia heshima Muumbaji wake, na kujiletea maangamizi mwenyewe. Lakini onyo hili lililotolewa kwa upendo na rehema isiyo na kikomo, liliamsha tu roho ya upinzani ndani yake. Lusifa akauachilia wivu wake dhidi ya Kristo kumtawala mpaka ukazidi kuwa mwingi, tena alizidi kunuia zaidi kwa ushupavu. [GC 494.2; PK Aya ya 7]

Kiburi kilichotokana na utukufu wake mwenyewe kilipalilia tamaa ndani yake ya kutaka awe mkubwa kuliko wote. Heshima kuu alizopewa Lusifa hazikuthaminiwa naye kama karama kutoka kwa Mungu, wala hazikumpa matamanio ya kuwa na shukrani yoyote kwa Muumbaji wake. Aliona fahari kubwa na kujitukuza kwa sababu ya mwangaza wake, na cheo chake, naye alitaka kupigania nafasi ya kuwa sawa na Mungu. Alikuwa anapendwa sana na kuheshimiwa na jeshi lote la mbinguni. Malaika walifurahia kutekeleza amri zake, naye alipewa hekima na utukufu kuwapita wengine wote. Lakini Mwana wa Mungu Ndiye alitambuliwa kuwa Mfalme Mwenye enzi kuu mbinguni, hivyo, alikuwa mmoja na Baba Yake katika nguvu na mamlaka. Katika mabaraza yote ya mashauri ya Mungu, Kristo alikuwa mshiriki, lakini Lusifa hakuruhusiwa kuingia na kushiriki katika makusudi ya Kiungu kama Kristo. “Kwa nini Kristo awe Mkuu kuliko wote?” alihoji malaika huyu mwenye nguvu nyingi, “Kwa nini Yeye anaheshimiwa kuliko mimi Lusifa?” [GC 495.1; PK Aya ya 8]

**Manung’uniko Miongoni Mwa Malaika**

Akiwa anaondoka mahali pake ambapo palikuwa karibu sana na uwepo wa Mungu, Lusifa alikwenda kueneza roho ya kutoridhika yaani manung’uniko miongoni mwa malaika. Akifanya kazi yake kwa siri kubwa, kwa kitambo aliweza kuficha kusudi lake halisi chini ya mwonekano wake wa nje wa kuwa na kicho kwa Mungu, alijitahidi sana kuchochea roho ya chuki kuhusu Sheria zile zilizokuwa zinawatawala wale wenye uhai wa mbinguni, akatangaza kwamba ziliweka mipaka/vizuio visivyokuwa vya lazima. Kwa vile tabia zao zilikuwa kwa asili ni takatifu, alisisitiza kwamba malaika wangepaswa kuyatii maagizo ya nia zao wenyewe. Alijitahidi sana kuwavuta kwa kujenga mazingira yaliyowafanya wamwonee huruma ili wapate kushirikiana naye kwa kuwaeleza kwamba Mungu alikuwa hajamtendea yeye haki kwa kumpa Kristo heshima kubwa kiasi kile. Alidai kwamba kwa kule kutaka kwake kugombania madaraka makubwa zaidi pamoja na heshima alikuwa hana lengo la kujiinua nafsi yake, bali alikuwa anatafuta njia kwa ajili ya kuwapatia uhuru wakazi wote wa mbinguni, na ya kwamba kwa njia hiyo wakazi hawa wangeweza kuyafikia maisha ya juu na bora zaidi. [GC 495.2; PK Aya ya 9]

**Rehema Nyingi Za Mungu**

Mungu katika rehema Zake kuu alimvumilia Lusifa kwa muda mrefu. Lusifa hakushushwa cheo chake mara moja kutoka katika nafasi yake ya juu sana wakati ule alipoendekeza roho ya kutoridhika, wala hata wakati alipoanza kuwasilisha madai yake ya uongo mbele za malaika watiifu. Aliachwa na kuendelea kukaa mbinguni kwa muda mrefu. Tena na tena alipewa upendeleo wa msamaha kwa sharti la kutubu na kujisalimisha. Jitihada kama zile toka Kwake Yeye aliye na upendo usio na mwisho, na hekima isiyokuwa na kikomo pekee ndiyo zilikusudiwa kumsadikisha Lusifa kosa lake. Roho ya chuki na kutoridhika ilikuwa haijawahi kujulikana kamwe kule mbinguni-kabla ya hapo. Mwanzoni Lusifa mwenyewe alikuwa hajajua mkondo huo wa mawazo ulikuwa unampeleka wapi kwa taratibu; hakuielewa asili halisi cha hisia zake. Lakini kule kutoridhika kwake kulipothibitika kwake kuwa hakukuwa na msingi wowote, basi, Lusifa alisadiki kwamba alikuwa amekosea, kuwa madai ya Mungu yalikuwa ya haki, na kwamba ilimpasa yeye kukiri mbele ya mbingu yote kuwa madai ya Mungu yalikuwa ya haki, na kuwa ilimpasa ayakubali kama mbingu ilivyoyakubali. Ikiwa yeye angalifanya hivyo, angekuwa amejiokoa yeye mwenyewe pamoja na malaika wengi. Wakati alikuwa bado hajaondoa utii wake wote kwa Mungu. Japokuwa alikuwa amekiacha cheo chake kama Kerubi afunikaye, hata hivyo, kama angetaka kumrudia Mungu, na kuikubali hekima ya Muumbaji wake, na kuridhika kuikalia nafasi ile aliyopewa katika mpango mkuu wa Mungu, angekuwa amerejeshwa katika ofisi yake. Lakini kiburi chake kilimzuia asiweze kunyenyekea au kutii. Aliendelea tu kuutetea msimamo wake kwa bidii bila kukoma, alisimama kidete akisema kwamba yeye hana haja yoyote ya kutubu, kisha alijisalimisha kikamilifu kwa nafsi yake mwenyewe, na kujipanga kujitosa katika pambano kuu dhidi ya Muumbaji wake. [GC 495.3; PK Aya ya 10]

Akiwa na akili yenye uwezo mkubwa, sasa aliielekeza akili hii mahiri katika kupanga mipango kabambe (mastermind), na ubongo sasa ukapindishwa kuelekea katika kufanya udanganyifu, yaani, alijitahidi kuwashawishi malaika waliokuwa chini ya usimamizi wake wamwonee huruma ile wapate kushirikiana naye. Hata ule Ukweli kwamba Kristo alikuwa amemwonya na kumshauri ulipotoshwa naye ili kutimiza hila zake za usaliti (Yn. 8:44). Kutoka katika mbinu yake ya kuyawakilisha vibaya Maneno ya Kristo, yaani upotoshaji, aliingia katika ukwepaji wa kusema Ukweli wote, na hatimaye alisema uongo moja kwa moja, akimtuhumu Mwana wa Mungu kuwa ana mpango wa kumdhalilisha yeye mbele ya wakazi wote wa mbinguni. Kisha alitafuta njia ya kujenga fitina kati yake na malaika watiifu. Wale wote alioshindwa kuwageuza na kuwaleta upande wake kabisa, aliwatuhumu kwamba walikuwa hawajali maslahi ya wenye uhai wa mbinguni. Kazi ile ile aliyokuwa akiifanya yeye mwenyewe, ndiyo aliwatupia

malaika walioendelea kuwa waaminifu kwa Mungu. Ili kuthibithisha mashtaka yake dhidi ya dhuluma za Mungu kwake, aliwakilisha vibaya Maneno na matendo ya Muumbaji wake. Ilikuwa sera yake kuwachanganya mawazo malaika kwa njia ya hoja zake za kichini-chini zilizohusu makusudi ya Mungu kwao. Kila kitu kilichokuwa cha kawaida  au rahisi alikifunika kifuniko cha usiri, na kwa upotoshaji uliorembwa-rembwa, alitia mashaka juu ya maneno ya wazi kabisa ya Yehova. Nafasi yake ya juu, yaani kule kuwa karibu kabisa na utawala wa Mungu, kulimpa nguvu nyingi katika maelezo yake aliyotoa kwao ili kupotosha, ndipo wengi wakashawishika kuungana naye katika maasi yake dhidi ya mamlaka ya Mungu. [GC 496.1; PK Aya ya 11]

**Madanganyo Ya Shetani**

Mungu, katika hekima Yake, alimruhusu Shetani aendelee na kazi yake, mpaka hapo roho ya chuki na kutoridhika itakapokomaa na kuzaa uasi kamili. Lilikuwa ni jambo la muhimu kwamba mipango yake Shetani iendelezwe mpaka ipate kukomaa kikamilifu, ili asili yake na mwelekeo wake halisi vipate  kudhihirika kwa wote. Lusifa, akiwa ni kerubi aliyepakwa mafuta, alikuwa ameinuliwa sana kwa kupewa wadhifa ya juu sana; alipendwa sana na wenye uhai wa mbinguni, na mvuto wake juu yao ulikuwa na nguvu kubwa. Serikali ya Mungu iliwajumuisha siyo tu wakazi wote wa mbinguni, bali pia wakazi wa sayari zingine zote ambazo Mungu alikuwa ameziumba; naye Shetani alidhani ya kuwa ikiwa angefaulu kuwabeba malaika wote wa mbinguni na kuwaingiza katika uasi wake, basi, angefaulu kujitwalia hata sayari zingine. Kwa hila alitoa maelezo ya msimamo wake katika mgogoro kwa ujanja/werevu mwingi, akitumia hila na ulaghai ili kutekeleza malengo yake. Uwezo wake wa kudanganya ulikuwa ni mkubwa sana, na kujifunika kwake kwa vazi la udanganyifu kulimfanya kulifikia lengo lake. Hata malaika waliokuwa watiifu hawakuweza kabisa kuitambua kikamilifu tabia yake au kuona kazi yake ilikuwa inaelekea wapi au kuleta matokeo gani. [GC 497.1; PK Aya ya 12]

Shetani alikuwa amepewa heshima kubwa sana, na matendo yake yote yalikuwa yamevikwa siri na mafumbo, hata ikawa vigumu kwa Mungu kuwafunulia malaika asili halisi ya kazi yake. Bila kufikia katika hatua ya dhambi, isingalionekana kuwa ni kitu kibaya sana kama vile ilivyo. Mpaka wakati huu dhambi haikuwepo katika himaya/ulimwengu wa Mungu, na wenye uhai watakatifu hawakuwa na wazo lolote kuhusu asili yake halisi, wala ubaya wake wa kutisha. Hawakujua matokeo ya kutisha yanayoambatana na kitendo cha kuiweka kando Sheria ya Mungu. Mwanzoni Shetani alikuwa ameificha kazi yake chini ya madai ya juu juu tu, na yasiyo na mashiko ya kujifanya kuwa yeye alikuwa mtiifu kwa Mungu. Alidai kwamba alikuwa anatafuta njia ya kuhamasisha heshima kwa Mungu, uimara wa Serikali Yake, na usitawi wa wakazi wote wa mbinguni. Wakati anaendelea kupandikiza hali ya kutoridhika mioyoni mwa

malaika waliokuwa chini yake, kwa hila na ustadi alikuwa amefanya ionekane kana kwamba alikuwa anatafuta kuiondoa hali ile ya kutoridhika. Wakati alipokuwa anasisitiza kwamba mabadiliko yalikuwa hayana budi kufanyika katika utaratibu na Sheria za serikali ya Mungu, alikuwa na kisingizio kwamba mabadiliko hayo yalikuwa ni ya lazima yawepo ili kuhifadhi maelewano mbinguni. [GC 497.2; PK Aya ya 13]

Katika kushugulika na dhambi, Mungu angeweza kutumia haki na Kweli tu, na ndivyo alifanya, alitumia haki na Kweli pekee (kwa vile hiyo ndiyo tabia Yake, hawezi kutenda dhambi). Shetani angeweza kutumia kile ambacho Mungu asingeweza kutumia - kujipendekeza, na kusifia kwa hila na kutia chumvi kwenye maelezo, udanganyifu, na uongo. Alikuwa ametafuta njia ya kubadilisha Neno la Mungu ili lionekane kuwa ni uongo na kuwasilisha vibaya mpango wa Serikali Yake mbele ya malaika, akidai kwamba Mungu alikuwa hana haki kuwawekea Sheria na Kanuni wakazi wa mbinguni; kwamba katika kuwataka viumbe Wake wajisalimishe Kwake na kumtii Yeye, Mungu alikuwa akitafuta kujiinua Mwenyewe tu. Kwa hiyo, ilikuwa ni lazima idhihirike mbele ya wakazi wote wa mbinguni, na mbele ya sayari zote (Ayu. 1 na 38), kuwa Serikali ya Mungu ilikuwa ya haki, Sheria Yake ilikuwa ni kamilifu. Shetani alikuwa ametengeneza mazingira yaliyoonekana kana kwamba yeye mwenyewe ndiye alikuwa anahenyeka kuuendeleza usitawi wa ulimwengu mzima. Tabia halisi ya mnyang'anyi huyo (tapeli), na lengo lake halisi, ni lazima vieleweke kwa wote. Lazima apewe muda ajifunue mwenyewe kwa kazi zake ovu. [GC 498.1; PK Aya ya 14]

Huyo laghai afichuliwa uhasama uliokuwa umesababishwa na mwenendo wake huko mbinguni, Shetani alidai chanzo chake ni Sheria na Serikali ya Mungu. Alitangaza kwamba maovu yote yalikuwa ni matokeo ya utawala wa Mungu. Alidai kwamba ilikuwa kusudi lake kuziboresha Sheria za Yehova. Kwa ajili hiyo, ilikuwa ni lazima apewe nafasi ili aonyeshe sura ya madai yake, na kuonyesha utendaji wa mabadiliko aliyokuwa amependekeza yafanyike katika Sheria takatifu ya Mungu (Amri za Mungu). Ilikuwa ni lazima kazi yake imhukumu yenyewe. Tangu mwanzo Shetani alikuwa amedai kwamba alikuwa hafanyi uasi wowote. Ulimwengu wote unapaswa kumwona laghai huyo akiwa bila barakoa, yaani akiwa amefichuliwa na kuonekana kwa wazi. [GC au PK 498.2; PK Aya ya 15]

Hata ilipokuwa imeamuliwa kwamba asingeweza kuendelea tena kubaki kule mbinguni, Mungu Mwenye Hekima isiyo na kikomo hakumwangamiza Shetani. Kwa kuwa huduma ya upendo ndiyo tu inayoweza kukubalika kwa Mungu, utii wa viumbe Vyake hauna budi kujengwa na usadikisho wao wenyewe, kuwa Mungu ni Mwenye haki na Mkarimu. Wakazi wa mbinguni na sayari zingine, wakiwa hawajawa tayari kuelewa asili au matokeo ya dhambi, kwa wakati ule

wasingeweza kuona haki na rehema za Mungu katika kumwangamiza Shetani. Endapo angeangamizwa pale pale, basi, wangekuwa wanamtumikia Mungu kwa hofu kuliko kwa upendo. Mvuto wa huyo mdanganyaji (tapeli) usingeweza kuangamizwa kabisa. Uovu ulipaswa kuachwa mpaka ukomae kabisa. Kwa manufaa ya ulimwengu wote katika vizazi vyote, milele yote, Shetani alikuwa hana budi kuachwa ili azidhihirishe kwa ukamilifu kanuni zake, ili shutuma zake dhidi ya Serikali ya Mungu zipate kuonekana katika nuru yake halisi kwa wenye uhai wote walioumbwa, ili haki na rehema ya Mungu pamoja na kutobadilika kwa Sheria yake,vipate kuwekwa wazi na hivyo kundoa shaka milele zote, na pia visihojiwe milele zote. [GC 498.3; PK Aya ya 16]

Uasi wa Shetani ulipaswa uwe fundisho kwa uumbaji wote na sayari zote katika zama zote zijazo, Ushuhuda wa daima wa asili na athari za kutisha za dhambi. Utendaji kazi wa utawala wa Shetani, yaani, madhara yake juu ya wanadamu na malaika, vingeonyesha matokeo ya tunda la kukiuka mamlaka ya Mungu. kwamba kule kuwako kwa Serikali ya Mungu na Sheria Yake isiyobadilika kamwe kumeshikamana na usitawi wa viumbe vyote alivyoviumba. Kwa hiyo, historia ya jaribio hili la kutisha la uasi litakuwa ulinzi/kinga ya daima kwa viumbe vyote vitakatifu vyenye akili, ili kuwazuia wasipate kudanganywa tena kuhusu hali halisi ya asili ya uvunjaji huo wa Sheria Yake (Amri Zake Mungu), na kuwaepusha wasitende dhambi tena kamwe na kupatwa na mateso yatokanayo na adhabu zake. [GC 499.1; PK Aya ya 17]

**Dharau Dhidi Ya Sheria Ya Mungu**

Karibu na mwisho kabisa wa pambano hilo kule mbinguni, mnyang'anyi huyo mkuu aliendelea kujihesabia haki yeye mwenyewe. Ilipotangazwa kwamba yeye pamoja na wafuasi wake wote ni lazima wafukuzwe kutoka kwenye makao yale yenye raha, ndipo kiongozi huyo wa uasi alipoanika kwa ujasiri kabisa dharau yake kwa kiapo cha wazi kabisa dhidi ya Sheria ya Muumbaji wake. Akalirudia tena dai lake alilotoa kwamba malaika hawakuwa na haja yoyote ya kutawaliwa au kuwekewa mipaka, bali ilipaswa wachwe huru kufuata mapenzi yao wenyewe, ambayo yangeweza kuwaongoza vizuri daima. Akazishutumu Amri za Mungu kwamba zilikuwa ni kizuizi cha uhuru wao na alitangaza kwamba lilikuwa ni kusudi lake kuhakikisha anaifutilia mbali Sheria hiyo ya Mungu, kwamba, wakiisha kuwekwa huru na kizuizi hiki cha Sheria, majeshi yote ya mbinguni yataweza kuingia katika hali ya juu zaidi, na ya utukufu zaidi ya maisha. [GC 499.2; PK Aya ya 18]

Kwa nia moja, Shetani na jeshi lake walimrushia Kristo lawama yote kwa uasi wao, wakitangaza kwamba kama wasingekemewa, basi, wasingeweza kamwe kufanya maasi yale waliyoyafanya. Hivyo, wakawa wakaidi, jeuri, na wasumbufu, tayari kupigana vita kutokana na utovu wao wa utii, wakitafuta kuipindua

Serikali ya Mungu bila sababu na bila mafanikio, lakini wakati ule ule wakidai kwa makufuru kwamba wao ndio walikuwa wahanga wasiokuwa na hatia yoyote, wa mamlaka hiyo ya ukandamizaji/uonevu. Mwasi yule mkuu pamoja na wale wote walioshirikiana naye hatimaye walifukuzwa mbinguni (Ufu. 12). [GC 499.3; PK Aya ya 19]

Roho ile ile iliyoanzisha uasi kule mbinguni bado ingali inaendelea kuchochea uasi hapa duniani. Shetani ameendeleza sera yake ile ile ya kushughulika na wanadamu, ambayo aliitumia akiwa na malaika. Roho yake sasa inatawala ndani ya watoto wa kuasi. Kama yeye wanajitahidi sana kuvivunjilia mbali vizuizi* vya Sheria ya Mungu, tena wanawaahidia uhuru kwa njia ya kukikuka kanuni Zake Mungu. Kemeo lo lote dhidi ya dhambi zao (uasi wa kanuni za Mungu),* bado linaamsha roho ile ile ya chuki na upinzani. Wakati ujumbe wa Mungu wa onyo unapoletwa kwao na kuzigusa dhamiri zao, Shetani huwaongoza watu hao wajihesabie haki wenyewe na kuwatafuta watu wengine wa kuwaunga mkono katika njia yao ya dhambi, kwa kuwaonea huruma. Badala ya kuyasahihisha makosa yao, wao wanachochea hasira na chuki kali dhidi ya yule anayewakemea, kana kwamba yeye ndiye aliyekuwa chanzo pekee la tatizo lao. Tangu siku za Habili, mwenye haki, mpaka siku hizi zetu hiyo ndiyo roho iliyokwisha kujidhihirisha kwa wale wanaothubutu kuikemea dhambi. (Amri, Maagizo, Kanuni, Neno la Mungu, na Shuhuda mara nyingi zinatumika kama neno moja-commandments, law, ordinances, statues, Word, testmonies n.k) [GC 500.1; PK Aya ya 20]

Kwa njia ile ile ya kuielezea na kuiwakilisha tabia ya Mungu vibaya, kama vile alivyofanya mbinguni, alipomfanya Mungu aonekanekuwa ni mkali tena ni katili, Shetani alishawishi mwanadamu kutenda dhambi. Na baada ya kufaulu mpaka katika hili, alitangaza kwamba vizuiozi vyote vya Mungu ambavyo vilikuwa si vya haki, navyo ndivyo vimesababisha wanadamu kuanguka dhambini, kama vile vilivyomsababisha yeye kuangukia katika uasi wake mwenyewe mbinguni. [GC 500.2; PK Aya ya 21]

Lakini basi, Yule anayeishi Milele, Yeye Mwenyewe anaitangaza tabia Yake, kwa kusema:"Bwana akapita mbele yake, akatangaza, Bwana, Bwana, Mungu mwingi wa huruma, Mwenye fadhili, Si mwepesi wa hasira, mwingi wa rehema na Kweli; Mwenye kuwaonea huruma watu elfu elfu, Mwenye kusamehe uovu na makosa na dhambi; wala si Mwenye kumhesabia mtu mwovu kuwa hana hatia kamwe; Mwenye kuwapatiliza watoto uovu wa baba zao, na wana wa wana wao pia, hata kizazi cha tatu na cha nne." Kutoka 34:6, 7. [GC 500.3; PK Aya ya 22]

Katika kitendo cha kufukuzwa Shetani kutoka mbinguni, Mungu alitangaza haki Yake na kudumisha heshima ya kiti Chake cha enzi. Lakini wakati mwanadamu alipotenda dhambi, kwa kuyakubali madanganyo ya roho/pepo huyo aliyeasi, Mungu alitoa ushahidi wa upendo Wake kwa kumtoa Mwanawe Pekee afe kwa

ajili ya jamii ya wanadamu iliyoanguka dhambini (Yn. 3:16). Katika upatanisho huu,tabia ya Mungu ilifunuliwa wazi. Hoja ya nguvu ya msalaba huonyesha kwa sayari zote kwamba, kwa vyovyote vile, Serikali ya Mungu isingestahili kutupiwa lawama yoyote kutokana na njia ya dhambi aliyoichagua Lusifa. (Serikali ya Mungu haihusiki na njia ya dhambi ambayo Lusifa alijichagulia mwenyewe, kila mtu ana uchaguzi, ila kama uchaguzi wake unangamiza maisha ya wengine, je, hii itakuwa ni haki kwa wengine?). [GC 500.4; PK Aya ya 23]

Katika shindano kati ya Kristo na Shetani wakati Mwokozi alipokuwa akifanya kazi ya huduma Yake hapa duniani, tabia ya mnyang'anyi/tapeli huyo mkuu yaani Shetani, iliwekwa wazi. Hakuna kitu chochote ambacho kingeweza kumng'oa Shetani kutoka katika upendo ambao malaika wa mbnguni walikuwa nao kwake na wakazi wote waliokuwa watiifu kwa Mungu katika sayari zote kwa ufanisi kama pambano lake la kikatili dhidi ya Mkombozi wa ulimwengu. Ujasiri wa madai yake yenye makufuru kwamba Kristo amsujudu yeye, ujasiri wake uliojaa kiburi wa kumchukua mpaka juu ya kilele cha mlima mrefu sana na juu ya kinara cha hekalu, kusudi lake lenye nia mbaya lilionekana wakati alipomshurutisha ajitupe chini kutoka katika kilele kinacholeta kizunguzungu, uovu wake usiosinzia uliomwinda Kristo kila mahali alipokwenda, ukiichochea mioyo ya makuhani na watu kulikataa pendo Lake, na hatimaye kuwafanya wapige makelele na kusema, "Msulibishe! Msulibishe!" -- mambo hayo yote yaliamsha mshangao mkuu na hasira ya Kiungu ya sayari zote (mwishowe viumbe vyote vilikarishwa kuona tabia yake halisi). [GC 501.1; PK Aya ya 24]

Shetani ndiye aliyeuchochea ulimwengu umkatae Kristo. Mkuu huyo wa uovu alitumia nguvu, hila na mbinu zake zote ili kumwangamiza Yesu; kwa maana aliona kwamba rehema, upendo, huruma, upole na uvumilivu Wake usiochoka, vilikuwa vinaiwakilisha na kuianika tabia ya Mungu mbele ya ulimwengu huu. Shetani alipinga kila dai alilotoa Mwana wa Mungu na kuwatumia watu kama vibaraka wake ili kuyajaza maisha ya Mwokozi na mateso na huzuni. Ule ujanja na uongo wake ambao kwa huo alikuwa amejitahidi kuizuia kazi ya Yesu, chuki aliyoionesha kwa kupitia kwa wana wa kuasi, mashtaka ya kikatili dhidi Yake Kristo, Yeye ambaye maisha Yake yalikuwa na wema usio na mfano, yote hayo yalitokana na roho yake Shetani ya kulipiza kisasi chenye mizizi mirefu. Mioto mikali ya wivu na chuki iliyomiminwa, kijicho na ubaya, ikalipuka pale Kalvari dhidi ya Mwana wa Mungu, wakati mbingu ikiwa inatazama tukio hilo kwa ukimya wenye kutisha mno na mshangao tele. [GC 501.2; PK Aya ya 25]

Wakati Kafara hii kuu ilipokamilishwa (kutolewa), Kristo alipaa juu mbinguni, akikataa kupokea ibada ya malaika mpaka awasilishe ombi hili: "Baba, ulionipa nataka wawe pamoja Nami popote nilipo, wapate na kuutazama utukufu Wangu ulionipa; kwa maana ulinipenda kabla ya kuwekwa msingi ulimwengu" Yohana 17:24. Ndipo kwa upendo na kwa nguvu zisioelezeka, jibu likaja kutoka katika

kiti cha enzi cha Baba: “Na wamsujudu malaika wote wa Mungu.” Waebrania 1:6. Hapakuwa na doa lolote juu ya Yesu. Kudhalilishwa Kwake kukakoma, kafara Yake ilikamilika, Naye akapewa Jina lile lipitalo majina yote (Flp. 2:8 -10). [GC 501.3; PK Aya ya 26]

Sasa hatia ya Shetani ilijitokea wazi bila kuwapo udhuru wowote. Alikuwa ameidhihirisha tabia yake halisi kuwa yeye ni mwongo na mwuaji (Yn. 8:44). Ilionekana wazi ya kwamba roho ile ile aliyokuwa nayo katika kuwatawala wana wa wanadamu ambao walikuwa chini ya mamlaka yake, ndiyo ambayo angeitumia kwao endapo angekuwa ameruhusiwa kuwatawala wakazi wa mbinguni. Alikuwa ametoa madai yake kuwa uvunjaji wa Sheria ya Mungu ungeleta uhuru na kuinuliwa juu; lakini ilionekana kwamba ukiukaji wa sheria huleta vifungo vya utumwa na kushushwa chini, kudhalilishwa, aibu, na hali mbaya ya maisha (Rum. 6:15-23). [GC 502.1; PK Aya ya 27]

Mashtaka ya uongo ya Shetani dhidi ya tabia ya Mungu na Serikali Yake yalionekana katika nuru yake halisi. Alikuwa amemshtaki Mungu kuwa anatafuta tu kujiinua Mwenyewe kwa kutaka viumbe Wake wajisalimishe Kwake na kumtii Yeye, tena alikuwa ametangaza kwamba, wakati Muumbaji anapowaamuru wengine wote wajikane nafsi zao kwa kumtii, Yeye Mwenyewe alikuwa hafanyi zoezi hilo la kujikana nafsi Yake, na wala hakutoa kafara yoyote. Sasa ilionekana wazi kwamba, kwa ajili ya wokovu wa jamii ya wanadamu walioanguka na kutenda dhambi, Mtawala Huyu wa sayari zote, (Mungu) alikuwa ametoa kafara kubwa mno kuliko zote ambazo ni upendo peke yake ungeweza kutoa; Kwa kuwa “Mungu alikuwa ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu na nafsi Yake, asiwahesabie makosa yao; Naye ametia ndani yetu Neno la upatanisho." 2 Wakorintho 5:19. Pia ilionekana wazi kwamba, wakati Lusifa ndiye aliyeufungua mlango na kuiingiza dhambi kutokana na tamaa yake ya kujipatia heshima na uwezo mkuu wa kutawala, Kristo alikuwepo, ili kuiangamiza dhambi, Naye alikuwa amejinyenyekeza Mwenyewe na kuwa mtii hadi mauti ya msalaba. [GC 502.2; PK Aya ya 28]

**Hoja Iliyotolewa Kwa Ajili Ya Mwanadamu**

Mungu alikuwa ameonyesha chuki Yake ya kanuni za uasi. Mbingu yote iliiona haki Yake ikiwa imefunuliwa, katika hukumu ya Shetani na katika ukombozi wa mwanadamu, Lusifa alikuwa ametangaza kwamba, ikiwa Sheria ya Mungu (Amri Zake) haibadiliki, basi na adhabu yake isingeweza kuondolewa, kila mkosaji lazima azuiliwe milele kutoka katika fadhila za Muumbaji, yaani asikubaliwe na Muumbaji tena. Alikuwa amedai kwamba jamii ya binadamu waliotenda dhambi iliwekwa ng’ambo, mbali na wigo wa ukombozi, nao wasingeweza kukombolewa, na kwa sababu hiyo walikuwa mawindo yake halali. Lakini kifo Chake Kristo kilikuwa ni hoja iliyotolewa kwa niaba ya mwanadamu ambayo

isingeweza kushindwa. Adhabu ya Sheria, ilianguka juu yake Yeye Kristo, ambaye alikuwa sawa na Mungu na mwanadamu alipewa uhuru wa kuipokea haki ya Kristo na kwa maisha ya toba na unyenyekevu aweze kupata ushindi, kama vile Mwana wa Mungu alivyopata ushindi dhidi ya nguvu za Shetani. Hivyo Mungu ni Mwenye haki na bado ni Mhesabiaji wa haki wakati huo huo, kwa wale wote wanaomwamini Yesu (Rumi 3:21-26). [GC 502.3; PK Aya ya 29]

Lakini haikuwa kwa ajili ya utekelezaji wa ukombozi wa Mwanadamu tu Kristo alikuja humu duniani kuteseka na kufa. Alikuja "kuitukuza Sheria" na "kuiadhimisha." Sio tu kwa wakazi wa sayari hii pekee yake ndio ambao wanapaswa kuichukulia sheria kama ilivyopaswa kuzingatiwa, bali ilikuwa ni kwa madhumuni ya kuzionyesha kwa wakazi wa sayari zote kwamba Sheria ya Mungu haibadiliki. Ikiwa madai Yake yangeweza kutupiliwa kando, basi Mwana wa Mungu asingekuwa na ulazima wa kupoteza uhai Wake ili kufanya upatanisho wa kuvunjwa kwa Sheria, yaani dhambi. Kifo cha Kristo kinathibitisha kuwa Sheria ya Mungu haibadiliki kamwe (Kutoka 20). Na kafara ambayo upendo usio na kikomo ulilazimisha Baba na Mwana kuitoa, ili wenye dhambi waweze kukombolewa, inaonyesha kwa sayari zote—hakuna kitu chochote ambacho chini ya mpango huu wa upatanisho kingeweza kutosheleza/kukidhi upatanisho—kwamba haki na rehema ndiyo msingi wa Sheria na Serikali ya Mungu. [GC 503.1; PK Aya ya 30]

Katika utekelezaji wa mwisho wa hukumu, itakuja kuonekana kwamba hapakuwa na sababu yoyote ya kuwapo kwa dhambi. Wakati Jaji Mkuu (Mwamuzi) wa dunia yote atakapomwuliza Shetani, "Kwa nini wewe umeniasi na kuninyang'anya Mimi raia wa ufalme Wangu?" Mwanzilishi huyo wa uovu hawezi kutoa kisingizio chochote. Kila kinywa kitafungwa na majeshi yote ya uasi yatakuwa kimya bila ya kuzungumza kwa kutekewa. [GC 503.2; PK Aya ya 31]

Msalaba wa Kalvari wakati ukitangaza Sheria haibadiliki, wakati huo huo unatangaza kwa malimwengu yote kwamba mshahara wa dhambi ni mauti. Katika kilio cha mwisho cha kukata roho kwa Mwokozi, "Imekwisha/tetelestai,"* kengele ya kifo cha Shetani iligongwa. Ile Pambano (vita) kuu lililokuwa limedumu kwa muda mrefu sana liliamuliwa hapo, na hatua ya mwisho ya uondoshaji wa dhambi ulithibitishwa. Mwana wa Mungu alipita katika milango ya kaburi, ili "kwa njia ya mauti amharibu yeye aliyekuwa na nguvu za mauti, yaani, Ibilisi," Waebrania 2:14. Tamaa ya Lusifa ya kujiinua ilimwongoza mahali pa kusema: "Nitakiinua kiti changu juu kuliko nyota za Mungu;....... Nitafanana na Yeye Aliye juu." Mungu anatangaza "Nimekufanya kuwa majivu juu ya nchi....... wala hutakuwapo tena hata milele." Isaya 14:13, 14; Ezekieli 28:18, 19. "Kwa maana, angalieni, siku ile inakuja, inawaka kama tanuru; na watu wote wenye kiburi, nao wote watendao uovu, watakuwa makapi; na siku ile inayokuja

itawateketeza, asema Bwana wa majeshi; hata haitawaachia shina wala tawi." Malaki 4:1. *(Tetelestai Kiebrania). [GC 503.3; PK Aya ya 32]

Sayari zote zitakuwa mashahidi wa asili na athari ya dhambi. Na uondoshaji wake kamili (kufutwa), ambao hapo mwanzo ungeleta hofu kwa malaika na dharau kwa Mungu (kwa kuvunjiwa heshima Yake), sasa utathibitisha upendo Wake na utaiimarisha heshima Yake mbele ya malimwengu yote yaliyo na wenye uhai wanaofurahia kuyatenda mapenzi Yake na ambao mioyoni mwao wanayo Sheria Yake (Amri Zake). Kamwe uovu hautaonekana tena au kuinua kichwa chake tena. Linasema hivi Neno la Mungu: “Mnawaza nini juu ya Bwana? Yeye atakomesha kabisa; mateso hayatainuka mara ya pili." Nahumu 1:9. Sheria ya Mungu, ambayo Shetani aliikashifu kama kongwa la utumwa, itaheshimiwa kama Sheria ya Uhuru. Uumbaji wote uliojaribiwa na kuthibitishwa hautaweza kuyumbishwa kamwe kugeuka tena katika utii wake Kwake Yeye ambaye tabia Yake imedhihirishwa kikamilifu kwa uwazi mbele yao kuwa ni ya upendo wenye kina kisichopimika au kuelezeka, na hekima isiyo na kikomo. [GC 504.1; PK Aya ya 33]

# SURA YA 30

# UADUI KATI YA MWANADAMU NA SHETANI, UNABII WA KWANZA.

## (Adui Mbaya Mno Wa Mwanadamu)

Ufupisho: Shetani hufanya kila kitu ili aweze kutupa kivuli chake cha kuzimu juu yetu na hivyo tusiweze kuona vizuri utukufu na uzuri wa upendo na huruma za Mungu. Lakini Yesu kwa neema Yake ya ajabu atabadilisha mioyo na maisha ya wale wanaomlilia ili wapate nguvu na msaada. Kwa wale wanaotubu kwa unyenyekevu-hakuna kitu kinachozuiliwa watakachohitaji ili kuwa karibu na Yesu wa thamani. Hii ni sura yenye ahadi ya kudai sasa hivi

“Nami nitaweka uadui kati yako na huyo mwanamke, na kati ya uzao wako na uzao wake; huyo utakuponda kichwa, na wewe utamponda kisigino.” Mwanzo 3:15. Hukumu ya Mungu iliyotamkwa dhidi ya Shetani baada ya anguko la mwanadamu ilikuwa ni unabii pia, unaokumbatia zama zote hadi mwisho wa wakati na ukiashiria pambano kuu litahusisha jamii zote za binadamu watakaoishi duniani. [GC 505.1; PK Aya ya 1]

Mungu anatangaza kwa kusema: “Nami nitaweka uadui.” Uadui huu haupokelewi kwa furaha kwa kawaida (hatuufurahii, kwa asili hatupendi tuwe na uadui na Shetani). Mwanadamu alipovunja sheria ya Mungu (Amri Zake), asili yake ilibadilika na kuwa ya uovu (dhambi) na tena alikuwa na upatanifu na Shetani, wala hakupenda kutofautiana naye (Hakuwa na uadui na Shetani). Kwa asili hakuna uadui wowote uliopo kati ya mwanadamu mwenye dhambi na yule mwanzilishi wa dhambi (Shetani). Wote wawili waligeuka na kuwa waovu kupitia uasi (uvunjaji wa Amri za Mungu). Mwasi hatulii kamwe isipokuwa amepata

huruma na kuungwa mkono kwa kuwashawishi wengine kufuata mfano wake. Kwa sababu hii malaika wale walioanguka dhambini huungana na watu waovu katika ushirika huo mbaya, unaokatisha tamaa, na kuhuzunisha. Ikiwa Mungu asingeingilia kati kwa njia ya pekee, Shetani na mwanadamu wangekuwa wameingia katika ubia dhidi ya Mbingu; na badala ya kuwa na uadui dhidi ya Shetani, familia yote ya mwananadamu ingekuwa imeungana kumpinga Mungu. [GC 505.2; PK Aya ya 2]

Shetani alimjaribu mwanadamu kutenda dhambi kama vile alivyosababisha malaika kuasi, ili kwa njia hiyo apate ushirikiano wao katika vita yake dhidi ya Mbingu. Hapakuwa na mfarakano wowote kati yake na malaika walioanguka dhambini kwa suala la chuki yao dhidi ya Kristo; wakati katika vipengele vingine vyote walikuwa hawapatani, walikuwa wameungana bila kutetereka katika kuipinga mamlaka ya  Mtawala wa malimwengu yote. Lakini Shetani aliposikia tangazo la kwamba uadui ungekuwako kati yake na mwanamke, kati ya uzao wake na uzao wa mwanamke, basi, alitambua kwamba juhudi zake za kuharibu asili ya mwanadamu binadamu zingeingiliwa; na kwamba kwa njia fulani mwanadamu angewezeshwa kuupinga nguvu zake. [GC 505.3; PK Aya ya 3]

Uadui wa Shetani dhidi ya uzao wa mwananadamu (human race) unachochewa kwa sababu, kwa njia ya Kristo, wao ni walengwa wa upendo na rehema za Mungu. Yeye anatamani kukwamisha mpango wa Mungu kwa ajili ya ukombozi wa mwanadamu, kumvunjia Mungu heshima Yake kwa njia ya kuiharibu-haribu sura Yake na kuichafua kazi ya mikono Yake; anapendapenda kusababisha huzuni kubwa mbinguni na kuijaza dunia hii kwa maangamizi, huzuni na ukiwa (ole). Naye husonda kidole chake kuelekea kwenye maovu hayo yote na kusema kwamba ni matokeo ya kazi ya Mungu katika kumuumba mwanadamu [GC 506.1; PK Aya ya 4]

**Uadui Kati Ya Mwanadamu Na Shetani**

Ni neema ambayo Kristo anaipandikiza katika roho  ndiyo inaumba ndani ya mwanadamu uadui huo dhidi ya Shetani. Bila ya neema hii inayobadilisha (inayoongoa) mtu tabia yake na nguvu inayoumba upya, mwanadamu angeendelea kuwa mateka wa Shetani, yaani, mtumishi wake aliye tayari daima kutii maagizo ya Shetani anapoamriwa. Lakini kanuni hiyo mpya ikiwa moyoni huumba mgogoro mahali ambapo hadi sasa pamekuwa na amani. Nguvu ambayo Kristo anatoa, inamwezesha mwanadamu kumpinga mtawala huyo katili) na mnyanganyi (tapeli). Yeyote aonekanaye kuichukia dhambi badala ya kuipenda, yeyote azipingaye na kuzishinda tamaa za mwili ambazo zimekuwa zikitawala kabisa ndani yake, anaonyesha utendaji kazi wa kanuni itokayo mbinguni asilimia mia (100%!). [GC 506.2; PK Aya ya 5]

Upinzani uliopo kati ya roho ya Kristo na roho ya Shetani ulionekana kwa namna ya wazi na kustajabisha mno kwa njia ulimwengu huu ulivyompokea Kristo. Haikuwa sana kwa sababu mwonekano wake wa kutokuwa na utajiri wa dunia hii, na fahari yake, au utukufu (umaarufu), ya kwamba ndio maana Wayahudi walishawishiwa kumkataa. Waliona kwamba alikuwa na nguvu ndani Yake ambayo ingefidia zaidi upungufu aliokuwa nao katika hizo faida za nje za kidunia. Lakini usafi na utakatifu Wake Kristo uliamsha chuki ya waovu (wasiomcha Mungu) dhidi Yake. Maisha Yake ya kujikana nafsi na uaminifu usio na dhambi, mambo hayo yakawa ni karipio na suto la daima kwa watu wenye kiburi, na wenye tabia ya uasherati na tamaa za mwili. Jambo hilo ndilo lililoibua uadui na chuki dhidi ya Mwana wa Mungu. Shetani na malaika zake waovu waliungana pamoja na watu waovu. Nguvuzote za uasi zikala njama pamoja dhidi ya Jemedari wa Ukweli. [GC 506.3; PK Aya ya 6]

### Ghadhabu Ya Shetani

Uadui huo huo unaoneshwa dhidi ya wafuasi wa Kristo kama ulivyoonyeshwa dhidi ya Bwana wao. Yeyote anayeiona tabia ya dhambi ilivyo ya kuchukiza, na kwa nguvu itokayo juu anayapinga majaribu yote, bila shaka ataiamsha ghadhabu ya Shetani na ya raia zake. Chuki dhidi ya kanuni safi za Ukweli na kutoa shutuma na mateso dhidi ya watetezi wa Ukweli, vitaendelea kuwepo maadamu dhambi na wenye dhambi wanadumu kuwepo. Wafuasi wa Kristo na watumishi wa Shetani hawawezi kuwa na maafikiano kamwe. Kwazo la msalaba halijabatilika. "Naam, na wote wapendao kuishi maisha ya utauwa katika Kristo Yesu wataudhiwa (watateswa)" 2 Timotheo 3:12. [GC 507.1; PK Aya ya 7]

Mawakala wa wake Shetani wanafanya kazi daima chini ya maelekezo yake ili kuimarisha mamlaka yake na kuujenga ufalme wake kwa kupingana na Serikali ya Mungu. Kwa kusudi hilo, wanajitahidi sana kuwadanganya wafuasi wa Kristo na kuwavuta kwaujanja ili wauache utii wao kwa Kristo. Wao, kama kiongozi wao alivyo, wanayaelewa vibaya, wanayatafsiri vibaya na kuyapotosha Maandiko ili kutimiza lengo lao. Kama vile Shetani alivyojitahidi sana kumtupia lawama yote Mungu, ndivyo vibaraka wake wanavyojitahidi sana kutoa mashitaka ya uongo kwa watu wa Mungu. Roho ile iliyomwua Kristo ndiyo inayowachochea waovu hao ili wapate kuwaangamiza wafuasi Wake Mungu. Mambo hayo yote yalidokezwa mapema katika unabii wa kwanza, uliosema: "Nami nitaweka uadui kati yako na huyo mwanamke, na kati ya uzao wako na uzao wake." Na hali hiyo ya uadui itaendelea hadi mwisho wa wakati. [GC 507.2; PK Aya ya 8]

Shetani huyakusanya majeshi yake yote na kutumbukiza nguvu zake zote katika mapambano hayo. Je! Ni kwanini basi hakutani na upinzani mkubwa zaidi?

Kwa nini askari wa Kristo wamelala usingizi mzito sana na kuwa katika hali ya kutojalikabisa? Ni kwa sababu wanacho kiwango kidogo sana cha mshikamano wa Kweli na Kristo; ni kwa sababu hawana Roho Wake kabisa. Kwao dhambi haina ladha mbaya na wala haiwachukizwi nayo kama vile Bwana wao anavyochukizwa nayo. Hawakabiliani nayo kwa upinzani ulio thabiti na kwa kuazimia kwa kusimama kidete, kama alivyofanya Kristo. Hawautambui ubaya utishao mno na uovu mkuu wa dhambi, tena ni vipofu wasioweza kuona tabia aliyo nayo mfalme wa giza na nguvu zake. Kuna uadui mdogo sana ndani yao dhidi ya Shetani na kazi zake, kwa sababu kuna ujinga mkubwa sana kuhusu nguvu na uovu alio nao na nia yake ya kuwadhuru wanadamu, na eneo pana sana la vita vyake dhidi ya Kristo na kanisa Lake (Ufu. 12:17). Hapo ndipo umati mkubwa sana wa watu wanadanganyika. Wao hawajui kwamba adui yao ni jenerali hodari sana wa vita, ambaye anayatawala mawazo ya malaikawaovu, na ya kwamba anayo mipango yake kabambe iliyokamilika na kukomaa vizuri pamoja na mikakati yenye ustadi wa kupigana vita na Kristo ili kuzuia wokovu wa watu usipatikane. Kwa kawaida miongoni mwa wale wajiitao Wakristo, na hata miongoni mwa wachungaji na wahudumu wanaoihubiri injili, wanamgusia kwa nadra sana Shetani, isipokuwa pengine kumtaja kwa bahati nasibu tu kwenye mimbari. Wanashindwa kuona ushahidi wa utendaji wake (kazi) na mfanikio yake endelevu; wanapuuza maonyo mengi dhidi ya hila yake; wanaonekana kana kwamba ni vipofu ambao macho yao hayaoni kabisa kwamba yupo miongoni mwao. [GC 507.3; PK Aya ya 9]

### Adui Aliye Macho Wakati Wote

Wanadamu wanapokuwa hawana ufahamu wa (wamejiziuka) hila za adui huyo asiyesinzia, yaani ambaye anakesha wakati wote, akifuatilia nyayo zao kila dakika katika ile njia wanayopita. Anajikaribisha bila kualikwa kwa kujipenyeza katika kila idara ya nyumbani, katika kila mtaa wa miji yetu, ndani ya makanisa, katika mabaraza ya kitaifa, katika mabaraza ya sheria na mahakama (au hata Mabunge), akiwafadhaisha watu, akileta mashaka, akidanganya, akibembeleza na kuwatongoza watu, kila mahali akiziangamiza roho na miili ya wanaume, na wanawake, na watoto, akizivunjilia mbali familia, akipanda mbegu za chuki, fitna, ushindani, wivu, malumbano, maasi dhidi ya serikali, na mauaji. Na Ulimwengu wa Kikristo unaonekana kuyaangalia mambo hayo kana kwamba ni Mungu aliyeyapanga, na ya kwamba, basi, ni lazima yaendelee tu kuwako. [GC 508.1; PK Aya ya 10]

### Uadui Kati Ya Mwanadamu Na Shetani

Shetani anajitahidi bila kukomakuwashinda watu wa Mungu kwa kuvivunjilia mbali vizuizi ambavyo vinawatenga na ulimwengu. Israeli ile ya zamani

ilishawishika kutenda dhambi wakati ule walipojiingiza kwa ujasiri kufanya mahusiano harama na wapagani. Kwa njia inayofanana na ile Israeli ya leo wanapotea. “Mungu wa dunia hii (Shetani) amezipofusha fikira zao wasioamini, isiwazukie nuru ya injili ya utukufu Wake Kristo aliye sura Yake Mungu.” 2 Wakorintho 4:4. Wale wote ambao hawajaazimia kuwa wafuasi wa Kristo wenye msimamo wa kweli, hao ni watumishi wa Shetani. Ndani ya moyo usiozaliwa mara ya pili kuna mwelekeo wa kuipenda dhambi, tena umo yamo mazoea ya kuifuga na kuitolea visababu. Katika moyo ule uliofanywa upya, kuna kuichukia dhambi na kuipinga kwa uimana wa kudhamiria kabisa. Wakristo wanapochagua kushirikiana na jamii ya wasiomcha Mungu na wale wasiomwamini Mungu, wanajianika wenyewe katika hatari ya kukabiliwa na majaribu. Shetani hujificha ili asionekane, na kwa kunyatia anawafunika juu ya macho yao kwa barakoa yake ya udanganyifu ili wasione hila na mitego yake. Hawawezi kutambua ya kuwa urafiki kama huo umefanyiwa mikakati yenye ustadi ili kuwaletea madhara; na wakati wote huo wanazidi kupalilia tabia ya kufanana na ulimwengu katika maneno, na matendo yao, nao wanaendelea kugubwika na upofu zaidi na zaidi. [GC 508.2; PK Aya ya 11]

Kuendana na desturi za ulimwengu kwa kuziiga, kunaliongoa kanisa na kulifanya liwe la ulimwengu; kamwe haliwezi kuoongoa ulimwengu na kuuleta kwa Kristo. Kuzoeana na dhambi kutaleta matokeo yasiyoepukika ya kuifanyadhambi ionekane kwetu kuwa haichukizi na haina madhara sana. Yeyote kujichanganya na watumwa wa Shetani hatimaye ataacha kumwogopa bwana wa.* Ikiwa tumo njiani kutekeleza wajibu wetu wa kazi, nasi tunakumbwa na majaribu, kama vile alivyoingizwa Danieli katika nyumba ya mfalme, tunaweza kuwa na uhakika kwamba Mungu atatulinda; ila kama tunajianika wenyewe katika majaribu kwa kuyakaribisha, basi muda si mrefu tutaanguka upesi majaribuni *(Watu wanaposhirikiana na watumishi wa Shetani hofu yao ya Shetani inapungua). [GC 509.1; PK Aya ya 12]

Mjaribu mara nyingi hufanya kazi kwa mafanikio zaidi kupitia wale ambao hawashuku kabisa kwamba wapo chini ya utawala wake. Watu wenye vipaji na elimu wanashabikiwa na kuheshimiwa na watu, kana kwamba sifa hizi zinaweza kuchukua nafasi ya kicho kwa Mungu wao au kuwastahilisha watu hao wawe na haki ya kupata upendeleo au fadhila Zake. Talanta, ustaarabu na utamaduni, zikichukuliwa zenyewe tu kama zilivyo, ni zawadi za Mungu; lakini pindi hizi zinapotumiwa kama mbadala wa uchaji wa Mungu (utauwa) yaani kuziba nafasi ya utakatifu, basi, badala ya kumleta mtu aliye navyo karibu zaidi na Mungu, vinampeleka mbali sana Naye, na hapo ndipo zinapogeuka na kuwa laana na mtego. Kuna wazo linalotawala bongo za watu wengi kwamba yote ambayo yanaonekana kuwa na sura ya adabu, ukarimu, kujistahi, uungwana, ustaarabu au ubora, kwa namna fulani, lazima yawe upande wa Kristo. Kamwe hapajakuwa

na kosa kubwa zaidi ya hili! Sifa hizi (viashiria) zinapaswa kuipamba tabia ya kila Mkristo, kwa kuwa zishinikiza mvuto wenye nguvu kwa watu na kuwaelekeza kwenye kuipenda dini ya Kweli; lakini basi, hizi ni lazima zitolewe wakfu (zisalimishwe kikamilifu) kwa Mungu, kinyume chake, hizo pia zina uwezo wa kuwaelekeza watu kwenye uovu. Watu wengi wenye akili iliyokuzwa na tabia za kupendeza na kuvutia watu, ambao hawawezi kujishusha kwenye kitendo ambacho kwa kawaida kinachukuliwa kuwa kitendo cha ukosefu wa maadili, ni chombo kilichonolewa tu mikononi mwake Shetani. Mvuto wa mtu huyo wenye athari za zilizojificha (siri) na udanganyifu wake, pamoja na mfano wake, humfanya awe adui wa hatari sana kwa kazi ya Kristo kuliko wale ambao ni wajinga* (hawana elimu), na wasiostarabika au wanaoonekana kuwa siyo waungwana (hawajakuza utamaduni wa akili). [GC 509.2; PK Aya ya 13]

Kwa kuwa na bidii katika maombi ya dhati na kumtegemea Mungu, Sulemani alijipatia hekima ambayo iliuvutia ulimwengu na kuufanya umstaajabie na kumsifu. Lakini alipogeuka na kumwacha Yule aliye Chimbuko la nguvu zake, na kusonga mbele akijitegemea mwenyewe, aliangushwa na majaribuni na kuwa mateka wa Shetani. Ndipo nguvu zile za ajabu alizopewa mfalme huyu mwenye hekima kuliko wafalme wote zilimfanya kuwa chombo au wakala tu mwenye ufanisi mkubwa mno kutenda kazi ya adui wa roho watu. [GC 509.3; PK Aya ya 14]

Shetani anapojitahidi daima kuzipofusha akili zao ili wasiuone Ukweli huo, hebu Wakristo wasisahau kamwe kwamba “Kwa maana kushindana kwetu sisi si juu ya damu na nyama; bali ni juu ya falme na mamlaka, juu ya wakuu wa giza hili, juu ya majeshi ya pepo wabaya katika ulimwengu wa roho.” Waefeso 6:12. Onyo hili lililovuviwa na roho wa Mungu linasafiri kwa sauti kubwa kupitia karne nyingi hadi kufika katika wakatietu: “Mwe na kiasi na kukesha; kwa kuwa mshitaki wenu Ibilisi, kama simba angurumaye, huzunguka-zunguka, akitafuta mtu ammeze. 1 Petro 5:8. Vaeni silaha zote za Mungu, mpate kuweza kuzipinga hila za Shetani. Waefeso 6:11. [GC 510.1; PK Aya ya 15]

Tangu siku zile za Adamu mpaka kuzifikia nyakati hizi zetu, adui yetu huyo mkuu amekuwa akiutumia uwezo wake kwa kuwatesa, kuwaoneana kuwaangamiza wanadamu. Kwa sasa anajiandaa kwa kampeni yake ya mwisho dhidi ya kanisa (Ufu. 12:17). Wale wote wanaojitahidi kumfuata na kumtafuta Yesu wataingizwa katika pambano hilo dhidi ya adui huyo asiye na huruma, na asiyepumzika (asiyechoka). Kwa kadiri Mkristo anavyokaribia zaidi kufanana na sura ya Mungu, ndivyo atakavyojiweka mwenyewe kuwa shabaha ya kulengwa na mashambulizi ya Shetani. Wale wote wanaojishughulisha kwa bidii kufanya kazi ya Mungu, wakijitahidi kuyafichua madanganyo ya Ibilisi na kumwasilisha Kristo mbele ya watu (kumhubiri), wataweza kujiunga na ushuhuda wa Paulo, ambao

anazungumza juu ya kumtumikia Bwana kwa unyenyekevu wote wa nia na akili, kwa machozi na majaribu mengi (Mdo. 20). [GC 510.2; PK Aya ya 16]

Shetani alimshambulia Kristo kwa majaribu yake makali sana, na yaliyofichwa na yaliyojaa hila, lakini alishindwa katika kila pambano. Vita vile vilipiganwa na Kristo kwa ajili yetu sisi; ushindi huo umetupa uwezo wa sisi nasi kushinda. Kristo atatoa nguvu kwa wale wote wanaozitafuta sana. Hakuna mtu yeyote ambaye bila idhini yake mwenyewe (bila yeye mwenyewe kukubali) anaweza kushindwa na Shetani. Mjaribu huyo hana mamlaka yoyote ya kuitawala nia ua mapenzi ya mtu au kumlazimisha kutenda dhambi. Yeye anaweza kumfadhaisha au kumtesa mtu sana na kusababisha uchungu, lakini hawezi kumchafua au kumwambukiza uovu wowote. Anaweza kusababisha maumivu makubwa sana, bali hawezi kusababisha uchafu. Ukweli kwamba Kristo ameshinda ungewatia moyo wa ujasiri wafuasi Wake ili wapate kupigana kiume (kwa ujasiri) vita hiyo dhidi ya dhambi na Shetani. [GC 510.3; PK Aya ya 17]

# SURA YA 31

# UTENDAJI WA PEPO WABAYA

### (Malaika Walioanguka Ni Akina Nani?)-Ushindi Katika Kristo.

Ufupisho: Kama Shetani angeweza kumfuta kila Mkristo juu ya uso wa dunia basi angefanya hivyo. Pia kama angeweza kumfutilia mbali kila binadamu angefanya hivyo. Akiwa na malaika wasio na idadi ambao walianguka, na walio tayari kutetekeleza maagizo yake, sisi kwa akili yetu yetu wenyewe, hatufui dafu kwa nguvu na ujanja wake. Lakini ndani ya Kristo kuna nguvu inayohitajika. Hatari yetu iko katika kutotambua nguvu na idadi ya askari wake—na hivyo tukajiona kuwa tuko salama. Hatumwelezi Kristo, muda baada ya muda, msaada tunaohitaji ili atusaidie kwenye pambano hili kali.

Mshikamano uliopo kati ya ulimwengu huu unaoonekana kwa macho na ule usioonekana, huduma wanayotoa malaika za Mungu na utendaji wa wakala wa pepo wachafu (wabaya), mambo haya yamefunuliwa kwa wazi katika Maandiko na yameshikamana pamoja na historia ya mwanadamu kwa namna isiyoweza kutenganishwa. Kuna mwelekeo unaokua wa kutoamini uwepo wa pepo wachafu, na wakati uo huo malaika watakatifu "watumikao wakitumwa kuwahudumu wale watakaourithi wokovu" (Waebrania 1:14) wanachukuliwa na watu wengi kuwa ni

roho za watu waliokufa. Lakini basi, Maandiko hayafundishi tu uwepo wa malaika hao wema na waovu, bali yanatoa uthibitisho usio na shaka kuonyesha kwamba malaika hao si roho za wafu zisizokuwa na miili (zilizotenganisha na mwili). [GC 511.1; PK Aya ya 1]

Kabla ya uumbaji wa mwanadamu, malaika walikuwepo; kwa kuwa wakati misingi ya dunia hii ilipowekwa, "Hapo nyota za asubuhi zilipoimba pamoja, na wana wote wa Mungu walipopiga kelele kwa furaha" Ayubu 38:7. Baada ya anguko la mwanadamu dhambini, malaika walitumwa kuulinda mti wa uzima na jambo hili lilitokea kabla ya mwanadamu yoyote hajafa. Katika asili yao, malaika wako juu kuliko wanadamu, kwa kuwa Mwandishi wa Zaburi anasema kwamba mwanadamu alifanywa "akiwa mdogo punde kuliko malaika; Umemvika taji ya utukufu na heshima;" Zaburi 8:5. [GC 511.2; PK Aya ya 2]

Tumefahamishwa katika Maandiko kuhusu idadi, nguvu na utukufu wa malaika wa mbinguni, kuhusu mshikamano wao na serikali ya Mungu na pia kuhusu uhusiano wao katika kazi ya ukombozi. "Bwana ameweka kiti Chake cha enzi mbinguni; Na ufalme Wake unavitawala vitu vyote." Na, kisha nabii huyo anasema, "Nikasikia sauti ya malaika wengi pande zote za kile kiti cha enzi." Mbele ya uwepo wa Mfalme wa wafalme wanahudumu—"Malaika, walio hodari katika nguvu," "wahudumu Wake, wafanyao mapenzi Yake," "wakiisikiliza sauti ya Neno Lake." Zaburi 103:19-21; Ufunuo 5:11. Elfu kumi mara elfu kumi na maelfu ya maelfu, walikuwa ndiyo wale malaika wa mbinguni aliowaona nabii Danieli. Mtume Paulo aliwataja kama "majeshi ya malaika elfu nyingi (yaani wasiohesabika)." Danieli 7:10; Waebrania 12:22. Kama wajumbe wa Mungu wanatoka, kama "kumulika kwa umeme," (Ezekieli 1:14), ndivyo utukufu wao unavyong'aa (unatia kiwi macho) na ndivyo ilivyo kasi ya urukaji wao. Malaika aliyetokea penye kaburi la Mwokozi, na sura Yake ilikuwa "kama umeme, na mavazi yake meupe kama theluji," ilifanya walinzi kutetemeka kwa hofu nao "wakawa kama wafu." Mathayo 28:3, 4. Wakati Senakeribu, Mwashuru mwenye majivuno mengi, alipomtukana na kumkufuru Mungu na kutishia kuwaangamiza Israeli, "Ikawa usiku uo huo malaika wa Bwana alitoka, akaingia katika kituo cha waashuru, akawapiga watu mia na themanini na tano elfu." Katika tukio hili "Walikatiliwa mbali mashujaa wote, na wakuu, na maakida," kutoka katika jeshi la Senakeribu. "Basi akarudi katika nchi yake akiwa na aibu." 2 Wafalme 19:35; 2 Mambo ya Nyakati 32:21. [GC 511.3; PK Aya ya 3]

Malaika wanatumwa kwenye utume (misheni) wa rehema kwa watoto wa Mungu. Kwa Ibrahimu, walikwenda na ahadi nyingi za baraka; kwenye malango ya Sodoma, walitumwa ili kumwokoa Lutu mwenye haki ili asiangamizwe na moto wa kutisha; kwa Eliya, walitumwa alipokaribia kufa kwa uchovu na njaa katika jangwa; kwa Elisha, walikwenda wakiwa na farasi na magari ya moto na kuuzunguka mji mdogo uliokuwa umezingirwa na maadui zake; kwa Danieli,

walitumwa wakati alipokuwa akitafuta hekima kutoka kwa Mungu katika ikulu ya mfalme mpagani (mtu wa mataifa), au akiwa ameachwa peke yake kuwa mawindo ya simba, nao walikwenda kumwokoa; kwa Petro walitumwa kumwokoa, alipokuwa amehukumiwa kifo katika gereza la Herode; malaika walikwenda kwa wafungwa pale Filipi; walitumwa kwa Paulo na wenzake katika usiku wa tufani baharini; walitumwa kwenda kufungua akili moyo ya Kornelio kuipokea injili; walitumwa kwa Petro na ujumbe wa wokovu kwa mgeni asiye Myahudi (mmataifa)—hivyo malaika watakatifu hao, wamewahudumia watu wa Mungu katika zama zote. [GC 512.1; PK Aya ya 4]

**Ulinzi Wa Malaika**

Malaika mlinzi amepangwa kwa kila mfuasi wa Kristo. Hawa walinzi wa mbinguni huwakinga wenye haki dhidi ya nguvu za yule mwovu. Jambo hili Shetani mwenyewe alilitambua aliposema: "Je! huyo Ayubu yuamcha Bwana bure? Wewe hukumzingira kwa wigo pande zote, pamoja na nyumba yake, na vitu vyote alivyo navyo? Ayubu 1:9, 10. Wakala ambaye anayetumiwa na Mungu kuwalinda watu Wake ameelezwa katika maneno ya Mwimba Zaburi: "Malaika wa Bwana hufanya kituo, akiwazungukia wamchao na kuwaokoa." Zaburi 34:7. Mwokozi alisema hivi, akizungumzia wale wanaomwamini: "Angalieni msidharau mmojawapo wadogo hawa; kwa maana nawaambia ya kwamba malaika wao mbinguni siku zote huutazama uso wa Baba Yangu aliye mbinguni." Mathayo 18:10. Malaika walioteuliwa kuwahudumia watoto wa Mungu, wanayo fursa saa yoyote kufikia uwepo Wake Mwenyezi Mungu. [GC 512.2; PK Aya ya 1]

Hivyo watu wa Mungu, wanapokuwa wameanikwa au kukabiliwa na nguvu za udanganyifu usiokoma, wenye nia ya kuwadhuru, alio nao mfalme wa giza asiyesinzia, wanapewa hakikisho la ulinzi usiokoma wa malaika wa mbinguni. Wala uhakika huo hautolewi bila hitaji. Mungu amewapa watoto Wake ahadi ya neema Yake na Ulinzi Wake kwa sababu kuna mawakala wakubwa wa uovu wenye nguvu nyingi wa kukabiliana/kupambana nao -- mawakala hawa wengi, walionuia haswa, waliojizatiti na wasiochoka daima, nia zao zenye ubaya wa kutisha, pamoja na nguvu zao, hakuna mtu yeyote awezaye kukaa kijinga-jinga tu au ambaye anayepuuza, au kutojua na aweze kuwa salama. [GC 513.1; PK Aya ya 2]

Pepo hawa wabaya, mwanzoni waliumbwa wakiwa hawana dhambi, wakiwa sawa kwa asili, uwezo na utukufu na malaika watakatifu ambao kwa sasa ni wajumbe wa Mungu. Lakini wao kwa kuanguka dhambini, wameungana pamoja katika kusudi la kumvunjia Mungu heshima Mungu na kuwaangaiza wanadamu. Wakiwa wameungana na Shetani katika uasi wake, walitupwa pamoja naye kutoka mbinguni, katika zama zote zilizofuata wameshirikiana naye katika vita vyake dhidi ya mamlaka ya Mungu. Tumeambiwa katika Maandiko juu ya

shirikisho lao pamoja na serikali yao, habari juu ya maagizo yao mbalimbali, juu ya vyeo vyao tofauti na makundi yao mbali mbali, kuhusu akili na hila walizo nazo na kuhusu njama zao mbaya za chuki na zilizokorokotolewa kudhuru amani na furaha ya wanadamu. [GC 513.2; PK Aya ya 3]

Historia ya Agano la Kale inataja hapa na pale juu ya uwepo wao na wakala wao, yaani utendaji wa kazi zao; lakini katika siku zile Kristo alipokuwa hapa duniani pepo wachafu walionyesha nguvu zao kwa njia ya wazi zaidi, kiasi cha kuvuta umakini mkubwa wa watu. Kristo alikuwa ameingia katika mpango uliopangwa kwa ajili ya ukombozi wa mwanadamu na Shetani alidhamiria kuwa jasiri katika kuonyesha haki yake ya kuutawala ulimwengu. Alikuwa amefaulu kuanzisha ibada ya sanamu katika kila sehemu ya dunia isipokuwa ardhi ya Palestina. Katika nchi pekee ambayo haikuwa imejisalimisha kikamilifu chini ya himaya ya mjaribu, Kristo alikuwa amekuja kuwaangazia watu nuru ya mbinguni. Hapa mamlaka mbili zilizoshindana na kupingana zilidai ukuu. Yesu alikuwa akinyoosha mikono Yake ya upendo, akiwaalika wote ambao wangependa kupata msamaha na amani ndani Yake. Majeshi ya giza yalielewa kwamba hayakuwa na utawala usio na ukomo, na yalielewa kwamba ikiwa kazi ya utume wa Kristo ingefaulu, basi utawala wao ungekoma ndani ya muda mfupi. Shetani alikasirika kama simba aliyefungwa minyororo na kwa ujeuri alionyesha waziwazi nguvu zake kwa ukali katika miili na roho za wanadamu. [GC 513.3; PK Aya ya 4]

### Kuwako Kwa Mapepo Na Kazi Yao

Ukweli ule kwamba wanadamu wamekuwa wakipagawa na mapepo wachafu, umeelezwa wazi katika Agano Jipya. Watu walioteseka hivyo, hawakuwa tu na magonjwa yatokanayo na sababu za kawaida. Kristo alikuwa na uelewa kamili wa kile alichokuwa akishughulika nacho na alitambua uwepo wao halisi mahali pale na utendaji wao hawa mawakala wa pepo wabaya. [GC 514.1; PK Aya ya 5]

Mfano wa kushangaza wa idadi yao, nguvu, uovu na nia yao mbaya ya kuwadhuru wanadamu, na pia uwezo na rehema ya Kristo, umetolewa katika maelezo ya Maandiko kuhusu uponywaji wa watu waliopagawa na pepo wachafu katika nchi ya Wagerasi. Wale wendawazimu masikini, walioteswa sana, walivivunja vizuizi vyao vyote vilivyowafunga navyo, wakajifurukuta na kujitupa huku na huko, wakigaragara na kutokwa na povu mdomoni, wakionyesha hasira, walipiga kelele kwa ukali sana, na walilijaza anga kwa kelele zao, waliifanyia miili yao ukatili,, na kuhatarisha wote ambao wangeweza kuwakaribia walipo. Miili yao iliyovuja damu na kuharibika vibaya na akili zilizokuwa zimevurugika kwa kupoteza mwelekeo na fadhaa, mambo hayo yalikuwa ni kituko kilichomfurahisha sana mfalme wa giza. Mmoja wa wale pepo waovu aliyekuwa amempagaa mgonjwa mmoja, alitangaza hivi: “Jina langu ni Legioni, kwa kuwa tu wengi.” Marko5:9. Katika jeshi la Kirumi, legioni lilikuwa jeshi la watu kuanzia

elfu tatu hadi elfu tano.* Majeshi ya Shetani pia yamepangwa katika kombania au vikosi, na kikosi kimoja ambacho wale mapepo walikuwa humo, sehemu yake walikuwa siyo chini ya legioni moja kwa nambari *(wanajeshi 3,000 hadi 5,000). [GC 514.2; PK Aya ya 6]

Kwa amri ya Yesu, mapepo yaliwaaacha wahanga wao, kutoka kwao kulifanya watu hawa wakae kwa utulivu miguuni pa Mwokozi, wakiwa katika hali ya kujitawala wenyewe, wapole, wenye akili timamu, na wasikivu. Lakini mapepo yaliruhusiwa kuliswaga kundi la nguruwe na kulitosa baharini; na mwonekano wa hasara ya wale nguruwe kwa wenyeji wa nchi ya Wagerasi ilizidi mibaraka ambayo Kristo alikuwa ameileta kwao, ndipo yule Mponyaji wa mbinguni aliposihiwa sana aondoke katika mipaka ya nchi yao. Matokeo haya yalikusudiwa na Shetani. Kwa kumtupia Yesu lawama ya hasara waliyopata, alichochea ndani yao hofu za watu zilizojaa uchoyo na ubinafsi na kuwazuia wasipate kuyasikia Maneno Yake. Daima Shetani anawashtaki Wakristo kuwa ndio chimbuko la hasara, balaa, misiba, na mateso, badala ya kuiacha shutuma hiyo idondokee mahali inapostahili--, yaani, juu yake mwenyewe na vibaraka wake. [GC 514.3; PK Aya ya 7]

Lakini makusudi ya Kristo hayakuzuiliwa. Aliwaruhusu pepo wachafu waangamize kundi la nguruwe kama kemeo kwa wale Wayahudi ambao walikuwa wanafuga wanyama najisi kwa ajili ya mapato. ikiwa Kristo asingewazuia hawa pepo, basi wangewatosa baharini, siyo tu nguruwe, bali pia wachungaji na wamiliki wao. Utunzaji wa wachungaji na wamiliki wote wa nguruwe, ulitokana na mamlaka Yake pekee, ambayo ilitumiwa kama rehema kwa ajili ya ukombozi wao. Zaidi ya hapo, tukio hili liliruhusiwa kutendeka ili wanafunzi waweze kushuhudia nguvu za kikatili za Shetani juu ya mwanadamu na mnyama pia. Mwokozi alitamani wafuasi Wake wamwelewe adui ambaye walipaswa kukabiliana naye, ili wasije wakadanganywa na kushindwa na hila zake. Yalikuwa pia mapenzi Yake kwamba watu wa eneo hilo waone uwezo Wake wa kuvunja utumwa wa Shetani na kuwaachilia mateka wake. Na ingawa Yesu mwenyewe aliondoka, watu hawa waliookolewa kwa muujiza wa ajabu sana, walibaki kuzitangaza rehema za Mfadhili wao. [GC 515.1; PK Aya ya 8]

Matukio mengine yanavyofanana na haya, yamerekodiwa katika Maandiko. Binti wa yule mwanamke Myunani, Msirofoinike alikuwa ameteswa sana na pepo ambaye Yesu alimtoa kwa Neno Lake. “Mtu mwenye pepo, kipofu, naye ni bubu; (Mathayo 12:22). Kijana aliyekuwa na pepo bubu “alimtupa motoni na ndani ya maji, amwangamize” (Marko 9:17-27); mtu aliyekuwa kama kichaa, aliyeteswa na “roho ya pepo mchafu” (Luka 4:33-36), alivuruga utulivu wa Sabato katika sinagogi la Kapernaumu—wote hawa waliponywa na Mwokozi Mwenye huruma. Katika kila tukio, Kristo alizungumza na roho mwovu kama nafsi yenye akili, akimwamuru amtoke mhanga wake na asimtese tena. Waabudu wa Kapernaumu,

walipouona uwezo Wake mkuu, “Mshangao ukawashika wote, wakasemezana wakisema, Ni neno gani hili, maana awaamuru pepo wachafu kwa uwezo na nguvu, nao hutoka.” Luka 4:36. [GC 515.2; PK Aya ya 9]

Wale wanaopagawa na pepo kwa kawaida huonekana kuwa katika hali ya mateso makubwa; lakini kuna kesi nyingine zenye utofauti kwa kanuni hii. Kwa ajili ya kupata nguvu zisizo za kawaida, wengine walikubali kukaribisha nguvu za mapepo. Lakini watu hawa hawakuwa na mgogoro na mapepo. Katika kundi hili walikuwepo wale waliokuwa na pepo wa uaguzi, Simoni Magus, Elima mchawi, na yule binti aliyewafuata Paulo na Sila kule Filipi. [GC 516.1; PK Aya ya 10]

Hakuna walio katika hatari kubwa zaidi ya mvuto  wa pepo wabaya kuliko wale ambao licha ya ushahidi tele na wa moja kwa moja wa Maandiko, wanakana uwepo na wakala wa ibilisi na malaika zake. Kwa kadri tunavyokosa ufahamu kwa kupuuzia au kuwa wajinga, na hivyo kudharau hila zao, ndivyo wanavyopata faida isiyofikirika; wengi hufuata mapendekezo yao huku wakidhani wanafuata maagizo ya hekima yao wenyewe. Hii ndiyo sababu, kwa kadri tunavyokaribia mwisho wa wakati, Shetani anafanya kazi kwa nguvu kubwa zaidi kudanganya na kuangamiza, anaeneza kila mahali imani kwamba yeye (Shetani) hayupo. Ni sera yake kujificha na kuzificha mbinu anazotumia kufanya kazi. [GC 516.2; PK Aya ya 11]

Hakuna kitu ambacho mdanganyifu mkuu anachoogopa zaidi kuliko sisi kuzijua mbinu zake. Ili afiche tabia na makusudi yake halisi, amejifanya mwenyewe awasilishwe kwa namna ambayo inawafanya watu wawe na hisia kali zaidi ya kejeli au katuni, na hivyo kufanya watu wamdhihaki na kumdharau. Anafurahishwa sana anapochorwa akiwa na umbo la kuchekesha au kuchukiza, au bovu, nusu mnyama na nusu mwanadamu.* Anafurahi sana anaposikia jina lake likitumiwa katika michezo na dhihaka na wale wanaojiona kuwa wana akili nyingi na ujuzi wa kutosha *(wanamchora kama katuni mwenye mapembe na anabeba ratu, angalia mtandaoni). [GC 516.3; PK Aya ya 12]

Ni kwa sababu amejifunika uso kwa ustadi wa juu na barakoa ya udangayifu kwa stadi ya juu sana, swali linaloulizwa mara nyingi kwa kawaida ni: “Je, kiumbe wa aina hii yupo kweli?” Ni uthibitisho wa mafanikio yake kwamba nadharia zinazotoa uwongo kwa ushuhuda ulio wazi zaidi wa Maandiko zinapokelewa kwa upana sana katika ulimwengu wa kidini. Na ni kwa sababu Shetani anaweza kudhibiti kwa urahisi zaidi akili za wale wasiojua ushawishi wake, kwamba Neno la Mungu linatupa mifano mingi sana ya kazi yake yenye uovu wenye hatari na chuki ya kutisha, likifunua mbele yetu majeshi yake ya siri na hivyo kutuweka tuwe macho dhidi ya mashambulizi yake. [GC 517.1; PK Aya ya 13]

Nguvu na ubaya wa Shetani na jeshi lake hutuweka kwenye hali ya tahadhari na tishio kwa haki kabisa na kutufanya tutafute hifadhi na wokovu katika nguvu kubwa zaidi ya Mkombozi wetu. Tunazithibiti kwa uangalifu nyumba zetu kwa komeo na kufuli ili kulinda mali zetu na maisha yetu kutokana na watu wabaya au waovu; lakini ni mara chache sana huwa tunafikiria juu ya malaika waovu ambao daima wanatafuta mpenyo ili kutufikia na ambao mashambulizi yao kwa nguvu zetu wenyewe hatuna mbinu ya kujilinda dhidi yake. Wakiruhusiwa, wanaweza kukoroga na kupotosha akili zetu, kuharibu na kutesa miili yetu, wanaweza kuharibu mali zetu na kuangamiza maisha yetu. Furaha yao pekee ni kuleta huzuni, taabu na maangamizi. Hali ya kuogofya inawakabili wale wanaopinga madai ya Mungu na kujisalimisha wenyewe kwenye majaribu ya Shetani, mpaka Mungu anaruhusu waachwe chini ya udhibiti wa pepo wabaya. Lakini wale wanaomfuata Kristo daima wako salama chini ya ulinzi Wake. Malaika walio na nguvu nyingi wanatumwa kutoka mbinguni ili kuwalinda. Shetani hawezi kuvunja ukuta wa ulinzi ambao Mungu amewazungushia watu Wake. [GC 517.2; PK Aya ya 14]

# SURA YA 32

# MITEGO YA SHETANI

### (Usitutie Majaribuni)-Kasha La Vifaa Vya Kazi Vya Shetani

Ufupisho: Shetani hutafuta kumnasa kila mtu ambaye anatafuta kuwa Mkristo. Anawanyemelea watoto wao pia. Wengi wanabanwa na mtego wake kila siku kwa kuwa hawajui pilikapilika zake au mikakati yake. Sura hii inaeleza kuhusu kasha la zana za Shetani, kwa kuwa ana mbinu nyingi za kuangamiza roho, na watu wengi hata hawajui kama kasha kama hilo lipo. Ni vyema usome haya kwa makini ili usiminywe na kumalizwa naye. Hapa kuna mitego 65 ya Shetani kwenye kasha lake.

Pambano kuu kati ya Kristo na Shetani, ambalo limeendelea kwa takribani miaka elfu sita, sasa linakaribia kufungwa na mwovu Shetani anaongeza juhudi zake mara mbili ili kuishinda kazi ya Kristo kwa niaba ya mwanadamu na kuwanasa watu katika mitego yake. Kuwashikilia watu gizani na kuwafanya wawe katika hali ya kutotubu hadi upatanisho wa Mwokozi uishe na kusiwepo tena

kafara ya dhambi zao, hilo ndilo lengo lake analojitahidi sana kulifikia. [GC 518.1; PK Aya ya 1]

Kama hakuna jitihada yoyote madhubuti na ya kipekee itakayofanywa kuupinga uwezo wake; wakati hali ya kutojali inapotawala katika kanisa na ulimwenguni, Shetani huwa hana wasiwasi wowote; kwa maana hayuko katika hatari ya kuwapoteza wale anaowaongoza kuwa mateka kwa mapenzi yake. Lakini basi, kipaumbele na umakini unapoelekezwa kwenye mambo ya milele, na watu wanapouliza-uliza, wakisema, "Nifanye nini ili nipate kuokolewa?" Hapo ndipo yeye anapojitupa uwanjani, na kukaa chonjo na huku akitafuta kupambana dhidi ya nguvu ya Kristo na kupinga mvuto wa Roho Mtakatifu. [GC 518.2; PK Aya ya 2]

Maandiko yanaeleza kuwa wakati mmoja, malaika wa Mungu walipokuja kujihudhurisha mbele za Bwana, Shetani naye alikuja miongoni mwao (Ayubu 1:6), si kwa madhumuni ya kusujudu mbele za Mfalme wa Milele, bali kutafura fursa ya kuendeleza na kutimiza mipango yake ya kudhuru na ya uovu dhidi ya wenye haki. Kwa lengo hilo hilo hujihudhurisha katikati ya watu wanapokusanyika pamoja kwa ajili ya kumwabudu Mungu. Ingawa anajificha na hivyo haonekani kwa macho, anafanya kazi yake kwa bidii zake zote ili kutawala mawazo ya watu wanaokuja kuabudu pale. Kama jenerali stadi, anaweka mikakati yake mapema. Anapomwona mjumbe wa Mungu anayachunguza Maandiko, analiona lile somo litakalohubiriwa kwa watu. Ndipo anatumia hila zake zote na akili zake zote kwa kutawala mazingira ili ujumbe ule usiweze kuwafikia watu ambao anawadanganya kuhusu kipengele hicho kinachoandaliwa. Yule anayehitaji mno kulipata onyo hilo atasukumwa na Ibilisi kwenda kufanya miamala ya pilika-pilika zingine ambazo zinataka yeye binafsi awepo pale, au kwa njia nyingine iwayo yote atazuiwa asiweze kuyasikia Maneno yale ambayo kwake yangeweza kuwa ni harufu ya manukato ya uzima iletayo uzima. [GC 518.3; PK Aya ya 3]

Kwa mara nyingine tena, Shetani anawaona watumishi wa Bwana wakiwa wamelemewa na mzigo mzito moyoni mwao kwa sababu ya giza la kiroho linalowafunika watu. Yeye anasikia maombi yao ya dhati yanayotolewa kwa bidii kwa ajili ya kupatiwa neema na nguvu ya Mungu ili kuvunjilia mbali laana ya kutojali, uzembe na uvivu. Ndipo kwa usongo mpya anatumia werevu wake. Anawaletea majaribu watu ili waendekeze uchu wa chakula au wajifurahishe nafsi zao kwa aina zingine za anasa zinazokidhi tamaa zao za mwili bila kujizuia, na kwa njia hiyo anatia ganzi fahamu zao hata washindwe kusikia mambo yale yale ambayo walihitaji mno kuyasikia na kujifunza. [GC 519.1; PK Aya ya 4]

Shetani pia anajua vizuri ya kwamba wale wote ambao anaweza kuwaongoza wapuuze maombi pamoja na kutojali kuyachunguza Maandiko, wataangushwa

kutokana na mashambulizi yake. Kwa hiyo, anabuni kila nyenzo iwezekanayo ili apate kuzichota akili zao. Daima limekuweko kundi la watu fulani wanaodai wacha Mungu, ambao, badala ya kuendelea kufuatilia ili kuujua Ukweli, wao hufanya dini yao iwe kutafuta makosa katika tabia au kosa katika imani ya wale wasiokubaliana nao. Watu hawa ndio wasaidizi wa mkono wa kulia wa Shetani. Washtaki wa ndugu zao, sio wachache, nao daima wanajishughulisha sana kufanya kazi yao hiyo, wakati Mungu anapokuwa kazini na watumishi Wake wanapomwabudu katika kicho cha kweli. Wataweka rangi ya uongo katika maneno na matendo ya wale wanaoipenda na kuitii Kweli. Watawawakilisha watumishi wa Kristo walio dhati, na wenye bidii (motomoto), wanaojikana nafsi zao na kusema kuwa wamedanganywa au ni wadanganyaji. Ni kazi yao kuwakilisha vibaya nia ya kila tendo la kweli na zuri, kusambaza maneno yasiyothibithishwa, yaani kusingiza wengine au kuwachongea, na kuchochea mashaka ndani ya akili za wale wasiokuwa na uzoefu na mambo hayo. Katika kila namna inayoweza kufikiriwa watatafuta kukifanya kile kilicho safi na cha haki kichukuliwe na watu kuwa ni kibaya, kinachukiza na kimejaa hila. [GC 519.2; PK Aya ya 5]

### Kweli Hutakasa

Lakini basi, hakuna haja ya mtu yoyote kudanganywa na watu hao. Inaweza kujulikana kwa urahisi kuwa hawa ni watoto wa nani, ni mfano wa nani wanafuata, na ni kazi ya nani wanayoifanya. "Mtawatambua kwa matunda yao."Mathayo 7:16. Mwenendo wao unafanana na ule wa Shetani, mzushi mwenye sumu, “mshtaki wa ndugu zetu” Ufunuo 12:10. Mlaghai huyu mkuu anao vibaraka wake wengi walio tayari kufundisha fundisho lolote lenye makosa ili kuwanasa watu katika mtego wake (Doctrines—Mafundisho ya uongo kinyume na Biblia) -- uongo na au uzushi huo ulioandaliwa naye vizuri kulingana na ladha ya mambo wanayoyapenda watu pamoja na uwezo wa wale anaotaka kuwaangamiza. Ni mpango wake kuleta kanisani watu wasio na moyo wa dhati na watu ambao hawajaumbwa upya watakaoweza kuchochea mioyo ya watu kuwa na mashaka na kutokuamini, na kuwa kikwazo kwa wote wanaotaka kuiona kazi ya Mungu ikisonga mbele na wao kusonga mbele pamoja nayo. Wengi ambao hawana imani ya Kweli katika Mungu au katika Neno Lake wanazikubali baadhi ya kanuni za Ukweli na wanapitishwa kama Wakristo, na kwa njia hiyo wanawezeshwa kuingiza mafundisho yao yenye makosa kama nguzo za mafundisho ya dini yatokayo katika Maandiko. [GC 519.3; PK Aya ya 6]

Msimamo unaosema kuwa haidhuru ni nini kile ambacho watu wanakiamini ni mojawapo ya madanganyo ya Shetani yanayofanikiwa sana. Yeye anajua kwamba Ukweli ukipokelewa kwa moyo wa kuupenda, yaani kuishi kulingana nao, unautakasa moyo wa mpokeaji; kwa hiyo daima anatafuta kuweka mahali pake

nadharia potovu, hekaya za uongo, yaani, injili nyingine badala ya Ukweli wa Neno la Mungu (Gal. 1:6-9). Tangu mwanzo watumishi wa Mungu wameshindana na waalimu wa uongo, sio tu kama watu wakatili tu, bali pia ni wafundishaji hodari wasiochoka wa mambo mengi ya uongo ambayo yana hatari kwa uhai wa roho ya mtu. Kwa uthabiti na bila woga Eliya, Yeremia, na Paulo waliwapinga bila woga wale waliokuwa wakiwageuza watu kulielekea Neno la Mungu. Ule uhuru unaochukulia imani sahihi ya kidini (Maandiko) kuwa siyo muhimu haukupata kibali kabisa cha watetezi na walinzi watakatifu wa Ukweli. [GC 520.2; PK Aya ya 7]

Tafsiri za Maandiko zisizokuwa dhahiri na za kufikirika, zinazofurahisha-furahisha tu, ambazo ni za kuwazia-wazia tu (fanciful), pamoja na nadharia nyingi zinazokinzana kuhusu imani za dini, ambazo zinapatikana katika Ulimwengu wa Kikristo ni kazi yake adui yetu mkuu anayetaka kuchanganya watu akili, ili wasitambue Ukweli. Na malumbano na migawanyiko inayoonekana miongoni mwa makanisa ya Ulimwengu wa Kikristo inasababishwa kwa kiwango kikubwa na desturi zilizopo za kuyanyumbulisha kwa nguvu Maandiko ili kuiunga mkono nadharia fulani inayopendwa sana na watu wengi. Badala ya kujifunza Neno la Mungu kwa makini na unyenyekevu wa moyo ili kuyajua mapenzi Yake, wengi hutafuta  kugundua kitu fulani cha ajabu, kisichokuwa cha kawaida au kipya (original). [GC 520.3; PK Aya ya 8]

Ili kuweza kuhalalisha mafundisho yao yenye makosa na mazoea yao yasiyokuwa za Kikristo, Baadhi wanachukua mafungu fulani ya Maandiko waliyoyatenga kutoka katika Muktadha husika, (wanatoa ama maneno yaliyotangulia au yale yanayofuata) pengine wakinukuu nusu tu ya fungu moja ili kuthibitisha hoja yao, wakati sehemu iliyobaki ingeonyesha maana iliyo kinyume chake kabisa. Kwa werevu wa nyoka wanajibanza wenyewe kwa uthabiti nyuma ya kauli zisizokuwa na uhusiano au zilizotenganishwa vizuri ila ambazo wao wanazifafanua kulingana na tamaa zao za kimwili. Kwa njia hiyo watu wengi wanalipotosha Neno la Mungu kwa makusudi kabisa. Wengine walio na akili zenye utendaji mkubwa, wana dhana za kufikirika-fikirika sana, mambo  yasiyokuwepo, yasiyo halisi, nao wanaichukua mifano, misemo, alama, namba, na ishara za Maandiko Matakatifu na wanahalalisha ubunifu wao kwa kurejelea  Maaandiko, bila kujali hata kidogo ushuhuda wa Maandiko unaosema kwamba Maandiko daima yanajitafsiri yenyewe (Isa. 28:7- 10, 13, 15, 17-23), halafu wanawasilisha mawazo yao ya ajabu ajabu, na yasiyo na msingi kama ndiyo mafundisho ya Biblia. [GC 521.1; PK Aya ya 9]

**Biblia Nzima Ni Mwongozo Wetu**

Wakati wowote ule, kujifunza au kusoma kwa Maandiko kunapofanyika bila kuwa na roho ya maombi, unyenyekevu, na kufundishika, huo ndio wakati

ambapo aya zilizo wazi na rahisi kabisa, pamoja na zile ngumu, zitaeleweka tofauti kabisa na maana yake halisi. Viongozi wa upapa wanachagua sehemu za Maandiko zinazotimiza vizuri zaidi kusudi lao, na kuzifasiri ili ziwafae wao wenyewe, halafu wanaziwasilisha tafsiri hizi kwa watu, huku wakiwanyima fursa ya kujifunza Biblia na kuelewa Ukweli mtakatifu kwa kuusoma wao wenyewe. Biblia nzima inapaswa kutolewa kwa watu kama inavyosomeka. Ingekuwa heri kwao wasipate kabisa mafundisho yoyote ya Biblia kuliko kupata mafundisho ya Maandiko yaliyowakilishwa vibaya kwa kiasi hicho. [GC 521.2; PK Aya ya 10]

Biblia ilikusudiwa iwe mwongozo kwa wale wote wanaopenda kujua mapenzi ya Muumbaji wao. Mungu aliwapa wanadamu Neno la Kweli la unabii lililo imara zaidi; malaika na hata Kristo Mwenyewe walikuja kumfahamisha Danieli na Yohana mambo ambayo hayana budi kuja upesi. Yale mambo muhimu yanayohusu wokovu wetu hayakuachwa katika hali ya mafumbo au sirini. Hayakufunuliwa kwa namna ambayo ingewaletea watu utata na kumpoteza yule mtafutaji wa dhati wa Ukweli. Bwana alisema hivi kupitia nabii Habakuki: “Iandike njozi hii, ukaifanye iwe wazi, ... ili aisomaye apate kuisoma kama maji Habakuki 2:2. Neno la Mungu liko wazi kwa wote wanaolisoma kwa moyo wa maombi. Kila mtu aliye mwaminifu na wa kweli, atapokea nuru ya Ukweli. “Nuru huangaza wenye haki.” Zaburi 97:11. Na hakuna kanisa linaloweza kukukua katika utakatifu isipokuwa washiriki wake wanautafuta Ukweli kwa dhati na bidii nyingi kama kutafuta hazina iliyofichwa. [GC 521.3; PK Aya ya 11]

**Makelele Ya Uhuru**

Kwa kelele zisemazo “Uhuru” watu wanapofushwa macho wasiweze kuona mbinu za adui yao, wakati yeye siku zote anafanya kazi kwa taratibu na kwa uhakika kwa ajili ya kufanikisha lengo lake. Anapofanikiwa kuondoa Biblia na badala yake akaingiza dhana za kukisia-kisia za wanadamu, hapo ndipo sheria ya Mungu inawekwa pembeni na makanisa hayo yanakuwa chini ya utumwa wa dhambi, huku waabuduo humo wanadai kwamba wapo huru. [GC 522.1; PK Aya ya 12]

Kwa wengi, utafiti wa kisayansi umegeuka na kuwa laana kwao. Mungu ameruhusu mafuriko ya nuru kumwagwa juu ya dunia hii kwa njia ya ugunduzi wa sayansi na sanaa (inajumuisha ufundi na teknolojia nk); lakini basi, hata wale watu wenye uwezo mkubwa wa akili, wasipoweza kuongozwa na Neno la Mungu katika utafiti wao, wanachanganyikiwa mno na kuona mafumbo katika jitihada zao za kuchunguza uhusiano uliopo kati ya sayansi na mafunuo ya Mungu. [GC 522.2; PK Aya ya 13]

Ujuzi wa mwanadamu wa mambo ya kimwili na ya kiroho ni mdogo tu, yaani ni nusu nusu tu na wala siyo kamili; matokeo yake ni kuwa wengi wanashindwa kuyafanya maoni yao kuhusu sayansi yaweze kupatana na kauli za Maandiko.

Wengi wanazipokea nadharia zisizo na uhalisia, dhana za kufikirika, nao hufikiria kuwa mambo haya ndiyo ukweli wa kisayansi, na wanafikiria kwamba Neno la Mungu linapaswa kupimwa kwa mafundisho yao ya "elimu iitwayo sayansi ambayo kwa hakika ni elimu ya uongo." 1 Timotheo 6:20. Muumbaji na kazi Zake (Uumbaji) vipo nje ya ufahamu wao; na kwa sababu hawawezi kuyaeleza mambo hayo kwa kutumia sheria za asili za maumbile (natural laws), basi wao huichukua historia ya Biblia kama taarifa isiyoweza kutegemewa. Wale wanaotilia mashaka kumbukumbu za Agano la Kale na Agano Jipya mara nyingi huenda hatua moja mbele na kutilia mashaka juu ya uwepo Wake Mungu na wanadai vitu vya asili (nature) vina nguvu isiyo na mipaka. Wakiwa wameiacha Nanga yao, basi, wanaachwa kujigonga-gonga huku na kule juu ya miamba ya ukafiri. [GC 522.3; PK Aya ya 14]

Kwa njia hiyo wengi wanajikwaa katika imani na kutongozwa na Ibilisi. Wanadamu wanajaribu sana kuwa na hekima kuliko Muumba wao; falsafa ya kibinadamu imejaribu sana kupekua na kueleza mafumbo na siri ambazo hazitafunuliwa kamwe, milele zote. Ikiwa wanadamu wangeridhika kuchunguza na kujua tu kile alichowafunulia Mungu kumhusu Yeye Mwenyewe na makusudi Yake, basi, wangeona mandhari ya utukufu, nguvu na mamlaka ya Yehova kiasi kwamba wangegundua udogo wao wenyewe nao wangeridhishwa na yale ambayo yamefunuliwa kwa ajili yao, na kwa ajili ya watoto wao (Kum 29:29). [GC 522.4; PK Aya ya 15]

Ni hila za ustadi wa hali ya juu kabisa za Shetani kuwafanya wanadamu watumie akili zao kuendelea kuchunguza na kujaribu kukisia-kisia ili kupata maelezo kuhusiana na mambo ambayo Mungu hajayafunua wazi kwetu na ambayo hakusudii yaeleweke kwetu. Ilikuwa kwasababu hiyo Lusifa alipoteza nafasi yake mbinguni. Alifikia hatua ya kutoridhika kwa sababu siri zote za makusudi ya Mungu hazikufunuliwa kwake, naye akadharau kabisa yale ambayo yalikuwa yamefunuliwa kwake kuhusiana na kazi yake katika cheo chake alichopewa mbinguni. Kwa kuchochea hali ya kutokuridhika katika mioyo ya malaika waliokuwa chini ya uongozi wake, alisababisha anguko lao. Sasa anatafuta kuzijaza akili za wanadamu na roho ile ile na kuwaongoza nao pia wazidharau amri za Mungu zinazoeleweka moja kwa moja. [GC 523.1; PK Aya ya 16]

### Hadithi Za Uongo Zinazopendeza

Watu ambao hawataki kuzikubali Kweli za Biblia zilizo wazi, na zinazochoma moyo, daima hutafuta hekaya zenye kupendeza ambazo zitanyamazisha dhamiri zao zinazowasumbua. Kwa kadri Mafundisho yanayotolewa yanavyozidi kupungua katika mambo ya kiroho, kujikana nafsi, na kujinyenyekesha, ndivyo yanavyozidi kupendwa na kupokelewa kwa wepesi zaidi. Watu hawa wanazishusha vibaya

nguvu zao za kiakili ili wapate kutimiza tamaa zao za mwili. Wakiwa na hekima nyingi katika kiburi chao, na wanapoyachunguza Maandiko wanapungukiwa na roho toba, maombi ya dhati ili wapate mwongozo wa Mungu, kiasi kwamba hawana ngao dhidi ya kurubuniwa. Shetani yuko tayari kukidhi haja za mioyo yao, naye anagawa uongo wake mahali pa ile Kweli. Hivyo ndivyo upapa ulijipatia mamlaka yake juu ya akili za watu; na kwa njia ya kuukataa Ukweli kwasababu unahusisha msalaba, Waprotestanti wanaifuata njia ile ile. Wote wanaolipuuza Neno la Mungu ili wafuate njia rahisi na nafuu na sera ya mwanadamu, kwa lengo la kukwepa kuhitilafiana na ulimwengu, wataachwa wapokee uongo wa kutisha kama mbadala wa Ukweli wa kidini. Kila aina ya fundisho la uongo ambalo linaloweza kufikiriwa, litapokelewa na wale wanauokataa Ukweli kwa makusudi kabisa. Mtu anayetazama kwa hofu kubwa uongo wa Fundisho moja, atakuwa tayari kupokea uongo mwingine kirahisi.* Mtume Paulo, akizungumzia tabaka ambalo "hawakukubali kuipenda ile Kweli, wapate kuokolewa," anasema hivi: "Kwa sababu hiyo Mungu atawaletea nguvu ya udanganyifu, ili wauamini uongo, ili wote wahukumiwe ambao hawakuiamini Kweli, bali walikuwa wakijifurahisha katika udhalimu." 2 Wathesalonike 2:10-12. Basi, tukiwa tunakabiliwa na onyo kama hilo mbele yetu, yatupasa kuwa waangalifu kuhusu fundisho tunalolipokea (Fundisho la imani - Doctrine *Huenda tusidanganywe na fundisho moja la uwongo, na kwa kweli, tunaweza kulitazama Fundisho hilo la uongo kwa mshtuko—lakini fundisho la uwongo jingine litakuja kwetu kirahisi tu, na hilo linalofuata linaweza kutudanganya. Kwa hivyo tunapaswa kuwa macho kila wakati). [GC 523.2; PK Aya ya 17]

**Mafundisho Ya Uongo Ni Hatari**

Miongoni mwa mawakala wanaofanikiwa sana wa mdanganyaji huyu mkuu, ni mafundisho ya udanganyifu na maajabu ya uongo kupitia imani ya kuwasiliana na watu waliokufa—umizimu (Spiritualism). Shetani akijigeuza na kuwa malaika wa nuru, anatandaza wavu wake mahali ambapo hatarajiwi hata kidogo. Ikiwa watu wangejifunza tu kile Kitabu cha Mungu (Biblia) kwa maombi ya dhati ili wapate kulielewa jambo hili, wasingeachwa gizani, nao wasingeweza kupokea mafundisho hayo ya uongo. Lakini kwa kuwa wameukataa Ukweli, wananajikuta wameanguka na kutafunwa kama mawindo ya mafundisho ya udanganyifu. [GC 524.1; PK Aya ya 18]

Uongo mwingine wa hatari jingine ni fundisho linalokana Uungu wa Kristo, likidai kwamba Yeye Hajawahi kuwepo hata kidogo kabla ya kuja Kwake hapa duniani kwa mara ya kwanza. Nadharia hii inapokelewa kwa furaha na kupendwa sana na tabaka kubwa linalodai kuiamini Biblia; lakini linapingana kabisa na kauli zinazoeleweka wazi kabisa alizozitoa Mwokozi wetu kuhusu uhusiano Wake na Baba Yake, tabia Yake ya Kiungu na uwepo Wake kabla ya ujio Wake duniani kwa

mra ya kwanza. Fundisho hili haliwezi kutetewa na mawazo yetu pasipo kuyapotosha Maandiko. Si tu kwamba linashusha uelewa wa mwanadamu kuhusu kazi ya ukombozi, bali pia linaiharibu imani ya watu katika Biblia kama ufunuo kutoka kwa Mungu. Wakati kutoiamini Biblia kunaifanya nadharia au fundisho la kuukana Uungu wa Yesu kuwa hatarishi zaidi, pia hulifanya kuwa na ugumu zaidi kupambana, kwani haliwezi kupingwa kirahisi. Ikiwa watu wanaukataa ushuhuda wa Maandiko yaliyovuviwa kuhusu Uungu wa Kristo, basi ni kazi bure kubishana nao mada hiyo; kwa maana hakuna hoja yoyote inayoweza kutolewa kwao, hata ya mamlaka gani ya mwisho au hitimisho haidhuru iwe ya kuondoa mashaka yote jinsi gani, na kuwafanya wasadiki. "Mtu wa kidunia hapokei mambo ya Roho wa Mungu. Kwake mtu huyo mambo hayo ni upumbavu mtupu; yanapita akili yake; maana yanaweza tu kutambuliwa kwa msaada wa Roho." 1 Wakorintho 2:14. Hakuna mtu yeyote anayeshikilia kosa hili anayeweza kuwa na uelewa wa kweli wa tabia Yake au utume Wake Kristo, au juu ya mpango mkuu wa Mungu kwa ajili ya ukombozi wa mwanadamu. [GC 524.2; PK Aya ya 19]

Bado lipo fundisho jingine lenye makosa na hila, na lenye kupenda kuleta madhara makubwa na ambalo ni gumu kulielezea, nalo ni lile linaloenea kwa kasi lisemalo kwamba Shetani siyo kiumbe halisi mwenye nafsi; kuwa jina hilo hutumika tu katika Maandiko ili kuwakilisha mawazo maovu na machafu, na tamaa mbaya za wanadamu. [GC 524.3; PK Aya ya 20]

Fundisho moja linalotoa mwangwi wake mbali na mahali pengi kutoka kwenye vibweta maarufu vinavyopendwa na wanadamu, ni kuwa ujio wa pili wa Kristo, ni ujio Wake kwa kila mtu wakati mtu anapokufa, hii ni zana ya kuyageuza mawazo ya wanadamu kutoka katika ujio Wake binafsi (ana kwa ana), yaani kimwili, na uso kwa uso, katika mawingu ya mbinguni. Kwa miaka mingi Shetani amekuwa akisema hivi, "Tazama, Yumo katika vyumba vya siri" (Mathayo 24:23-26); na roho nyingi zimepotea kwa kukubali uongo huu. [GC 525.1; PK Aya ya 21]

Tena, kuna hekima ya kidunia inayofundisha kwamba maombi siyo muhimu. Wanasayansi hudai kuwa hakuna jibu halisi kwa maombi; kwamba jambo hili lingekuwa kukiuka sheria ya asilia, muujiza (natural laws),na kuwa miujiza haipo kabisa. Sayari zote wasemavyo wao, zinatawalia na sheria zisizobadilika (fixed), na Mungu Mwenyewe hafanyi chochote kinyume na sheria hizi (nature). Kwa njia hiyo wanamwakilisha Mungu kwamba anabanwa na sheria Zake Mwenyewe-- kana kwamba utendaji wa sheria za Mungu za asili na maumbile (nature) zinaweza kumwondolea uwezo Wake wa Kiungu wa kufanya jambo alitakalo kwa Uhuru (kama Mwenyezi Mungu). Fundisho hilo linapingana na ushuhuda wa Maandiko. Je! miujiza haikufanywa na Kristo na mitume Wake? Mwokozi Yule Yule Mwenye huruma anaishi, Yuko hai leo, kama vile alivyokuwa akitembea na kuonekana miongoni mwa watu watu. Na Yeye Yuko leo tayari

kusikiliza maombi ya imani kama vile alipotembea mbashara kati ya wanadamu. Vitu vya asili (natural) tunavyoviona kwa macho vinashirikiana na vitu vilivyo juu ya vitu vya asili, visivyo vya kawaida kwetu (Supernatural). Ni sehemu ya mpango Wake Mungu, kutupatia sisi kama jibu kwa ombi letu Kwake, lililotolewa kwa imani, kile ambacho Yeye asingeweza kutupatia kama tusingekuwa tumemwomba hivi. [GC 525.2; PK Aya ya 22]

**Alama Za Mipaka Zilizowekwa Na Neno La Mungu**

Kuna idadi isiyoweza kuhesabika ya Mafundisho yenye makosa na mawazo ya kuwazia-wazia au kufikirika yanayoshamiri miongoni mwa makanisa ya ulimwengu wa Kikristo. Haiwezekani kabisa kukadiria matokeo mabaya ya kuiondoa alama moja ya viwango vilivyoweka na Neno la Mungu. Ni wachache mno wanaodiriki kufanya hivyo, ambao wanaachia kulikata Fundisho moja tu la Ukweli. Walio wengi husonga mbele kwa kuendelea kuiweka pembeni kanuni moja ya Ukweli baada ya nyingine, hadi wanafikia mahali pa kuwa makafiri kamili. [GC 525.3; PK Aya ya 23]

Mafundisho potofu yanayotokana na theolojia maarufu inayopendwa na wengi, yamewasukuma watu wengi kuwa watu wa mashaka-mashaka ambao vinginevyo wangeweza kuwa waamini Maandiko. Haiwezekani kwake kukubali mafundisho yanayokasirisha hisia zake kuhusiana na haki, rehema, wema na ukarimu; na kwa kuwa haya yanawakilishwa kama fundisho la Biblia, basi yeye anakataa kupokea kipengele hicho kama Neno la Mungu (Watu wasioenda kanisa wanaweza kuukataa Ukristo kwa sababu wamefundishwa kimakosa Mafundisho ya Biblia, kama vile Jehanamu iwakayo moto milele, kutetea utumwa, n.k—aina ya mafundisho ambayo yanamfanya mtafutaji afikiri kwamba ikiwa mafundisho haya yanawakilisha Ukristo, basi yeye hataki sehemu yake. Mfano mzuri utakuwa pale Mungu alisema taifa la Kanani liangamizwe, na mtu anafikiri kwamba hii si haki, rehema, wema au ukarimu, ila Mungu anajua anashugulika na nani na mengine tusiyojua kwa hekima zetu, mfano mzuri kwangu ni Boko Haram wa Nigeria ambao ni wakatili sana kwa watu wanaomwamini Mungu, na kisha hatima yao yaweza kuamuliwa kuwa kali). [GC 525.4; PK Aya ya 24]

Na hili ndilo lengo ambalo Shetani anajitahidi kulitimiza. Hakuna jambo analolitamani zaidi kuliko kuua kabisa imani na ujasiri wa watu kwa Mungu na kwa Neno Lake. Shetani ni kiongozi wa jeshi kubwa la watu wenye mashaka na anafanya kazi kwa uwezo wake wote alio nao ili kuwadanganya watu na kuwaleta kwenye gwaride lake. Kuwa na mashaka umekuwa mtindo wa maisha. Lipo kundi kubwa ambalo kwao Neno la Mungu hutazamwa kwa mashaka au kushukiwa kwa sababu ile ile kama alivyoangaliwa Mwanzilishi Wake (Masihi)--kwa sababu linaikemea na kuihukumu dhambi. Wale ambao hawako tayari kutii matakwa Yake Mungu, hujitahidi kuipindua mamlaka Yake (Neno). Wanasoma

Biblia au wanayasikiliza mafundisho yake kama yanavyowasilishwa kutoka katika mimbari takatifu, kwa kusudi tu la kutafuta makosa katika Maandiko hayo au mahubiri yenyewe. Si wachache wanaogeuka kuwa makafiri ili kujionyesha kuwa wao wana haki au wanao udhuru wa kujitetea kwa kutotekeleza wajibu wao uwapasao. Wengine huchukua kanuni za kushuku-shuku, yaani kutoamini kutokana na kiburi na uvivu wao. Hupenda mno raha (maisha bwerere) kiasi cha kushindwa kujipatia sifa kwa kufanya jambo lolote linalostahili heshima, ambalo huhitaji wao watumie jitihada na kujikana nafsi zao, wao hulenga kujipatia umaarufu kutoka kwa watu kwamba eti wataonekana ni wenye hekima ya hali ya juu kwa kuweza kuikosoa Biblia. Kuna mengi ambayo akili ya mwanadamu finyu, na yenye mipaka, inakuwa haina uwezo wowote wa kuyafahamu bila kuangaziwa na ile nuru na hekima itokayo kwa Mungu; na kwa njia hiyo wao wanapata kisingizio cha kuyakosoa. Wapo wengi wanaoonekana kana kwamba wanaona kuwa ni sifa njema kusimama upande wa kutoamini, mashaka na ukafiri. Lakini chini ya mwonekano huo wa kuwa wazi, itaonekana ya kwamba watu kama hao wanachochewa na moyo wao wa kujiamini wenyewe pamoja na kiburi walicho nacho. Wengi hufurai wakipata kitu fulani ambacho ni kama kitendawili au jambo la kutatanisha katika Maandiko ambacho kinawaacha watu wamepigwa na butwaa. Wengine mwanzoni wanakosoa na kutoa sababu zao wakisimama upande wenye makosa, kutokana tu na kupenda kwao ubishi. Hawatambui kwamba kwa njia hiyo, wao hujinasa wenyewe katika mtego wa yule mwindaji (Ibilisi). Lakini baada ya wao kueleza wazi mashaka yao, wanajisikia kwamba ni lazima wautetee msimamo wao. Hivyo wanaungana na waovu wasiomcha Mungu na kujifungia wenyewe malango ya paradiso. [GC 526.1; PK Aya ya 25]

**Msingi Imara**

Mungu ametoa ushahidi wa kutosha katika Neno Lake kwa kuonyesha utakatifu wa tabia Yake ya Kiungu katika Neno hilo. Kweli zile kuu zinazohusu ukombozi wetu zimewasilishwa kwa njia inayoeleweka wazi. Kwa msaada wa Roho Mtakatifu, ambaye ameahidiwa kutolewa kwa wote wanaomtafuta kwa dhati na bidii, kila mtu anaweza kuelewa Ukweli huu yeye mwenyewe. Mungu amewapa wanadamu msingi ulio imara wa kuisimika imani yao juu Yake. (Mt. 7:24-27). [GC 526.2; PK Aya ya 26]

Lakini bado akili finyu na zenye kikomo za wanadamu hazitoshi kuweza kuelewa kwa ukamilifu mipango na makusudi ya Yule wa milele, asiye na ukomo. Kamwe hatuwezi kumjua, kumpata au kumwona Mungu kwa kuchunguza (uchunguzi, au utafiti). Tusijaribu kuona kwamba kuna ulazima wa kulifunua lile pazia ambalo limeuficha nyuma utukufu na ukuu Wake Mungu kwa mikono yetu yenye kiburi. Mtume anapaza sauti yake akisema: “Hukumu Zake hazichunguziki, wala njia Zake hazitafutikani!” Warumi 11:33. Tunaweza tu kuelewa jinsi

anavyoshughulika nasi na nia ambayo inamsukuma kufanya hivyo, ili tuweze kutambua upendo Wake usio na mipaka na rehema Zake zilizofungamana na uweza Wake usiokuwa na mipaka. Baba yetu aliyeko mbinguni ameweka utaratibu wa kila kitu kwa hekima na haki Yake, na sisi hatupaswi kuwa na hali ya kutoridhishwa na kutokuwa na imani Naye, bali tujisalimishe Kwake kwa kicho. Yeye atatufunulia sisi makusudi Yake mengi kama ilivyo muhimu (faida) kwetu kuweza kujua, na zaidi ya hapo sisi tunapaswa kuutumainia Mkono Wake ambao una nguvu zisizo na mipaka, na Moyo ambao umesheheni upendo. [GC 527.1; PK Aya ya 27]

Wakati ambapo Mungu ametoa ushahidi wa kutosha kukidhi imani yetu, kamwe hataondoa visingizio vyote vya kutokuamini. Watu wote wanaotafuta ndoana za kuning'iniza mashaka yao watazipata. Na wale wanaokataa katakata kulikubali na kulitii Neno la Mungu ati mpaka kila kikwazo kiwe kimeondolewa, na wala kusiwe tena na nafasi ya kuingiwa na mashaka, kamwe hawataweza kuja nuruni. [GC 527.2; PK Aya ya 28]

Kutomwamini Mungu ni matokeo ya asili ya moyo ambao haujaumbwa upya, ambao una uadui na Mungu. Lakini imani inavuviwa na Roho Mtakatifu, nayo itastawi tu kwa jinsi itakavyopaliliwa moyoni. Hakuna mwanadamu anayeweza kuwa imara katika imani bila kuazimia kwa juhudi za makusudi. Kukosa imani kunaimarika kunapokokewa moto; na ikiwa watu, badala ya kukita kwenye kutafakari ushahidi ambao umetolewa na Mungu ili kuijenga imani yao, wao hujielekeza wenyewe katika kulaumu na kuhoji vitu vidogo vidogo na vya kipuuzi, basi hao wataishia kuona mashaka yao yakizidi kuthibitishwa na kuwa makubwa zaidi na zaidi. [GC 527.3; PK Aya ya 29]

Lakini wale wanaozitilia mashaka ahadi za Mwenyezi Mungu, na wanakosa imani katika ahadi yenye uhakika ya neema Yake, wanamkosea Mungu heshima (wanamwaibisha pia); tena mvuto wao, badala ya kuwavuta wengine kwa Kristo, unakuwa na mwelekeo wa kuwafukuza mbali Naye. Wao ni miti isiyozaa, ambayo inaeneza matawi yake meusi yanayotia giza mbali na katika maeneo mengi, nayo huzuia jua lisiweze kuifikia mimea mingine na kuifanya idhoofike na kisha kufa chini ya kivuli cha baridi yenye kustua. Kazi ya maisha ya watu hawa itajitokeza kama ushahidi wa kudumu dhidi yao. Wanapanda mbegu za kutoamini kwa yale yaliyo wazi, na kumtilia mashaka Mungu, na mbegu hizo zitatoa mavuno yake hatimaye. [GC 527.4; PK Aya ya 30]

Kuna njia moja tu ya kufuata kwa wale ambao wanatamani kwa dhati kuondokana na mashaka yao. Badala ya kuhoji yale yanayoonyesha mashaka yao na kubishana au kulalamika kuhusu yale wasiyoyaelewa ambayo wala hayana umuhimu, hebu na wawekeze umakini wao kwenye nuru ile ambayo wameshaipokea na inayowaangazia tayari, ndipo watapokea nuru kubwa zaidi. Hebu na watimize kila wajibu wao uliowekwa wazi kwa ufahamu wao, nao

watawezeshwa kuelewa na kutekeleza yale ambayo kwa sasa wanayatilia mashaka. [GC 528.1; PK Aya ya 31]

Shetani anaweza kuwasilisha kitu cha bandia (feki) ambacho kinafanana kwa ukaribu sana na Ukweli kiasi cha kuwapotosha wale wanaopenda kudanganywa (au walio tayari kudanganywa), wale wanaotamani kukwepa kujikana nafsi na kujitoa kafara kunakotakiwa na Ukweli wa Neno la Mungu; lakini haiwezekani kabisa kwake Shetani kumshikilia chini ya uwezo wake mtu ambaye anayetamani kwa uadilifu wa moyo kuujua Ukweli, kwa gharama yoyote ile. Kristo ni Kweli na ni “Nuru halisi, amtiaye nuru kila mtu akija katika ulimwenguni.” Yohana 1:9. Roho wa Kweli ametumwa kuwaongoza (kuwatia) watu katika Ukweli wote. Na kwa mamlaka ya Mwana wa Mungu, inatangazwa: “Tafuteni, nanyi mtapata.” "Ikiwa mtu yeyote anataka kufanya mapenzi Yake, atayafahamu mafundisho." Mathayo 7:7; Yohana 7:17. [GC 528.2; PK Aya ya 32]

Wafuasi wa Kristo wanajua kwa udogo tu kuhusiana na njama ambazo Shetani na majeshi yake wanaandaa dhidi yao. Lakini Yeye aketiye mbinguni anatawala na kuzigeuza hila na mbinu hizi zote ili kutimiza mikakati Yake ya kina. Bwana huruhusu watu Wake wapitishwe katika tanuru la moto wa majaribu makali, si kwa sababu Yeye anafurahia maudhi na mateso yao, lakini kwa sababu mchakato huu ni wa muhimu kwa ajili ya kuupata ushindi wao wa mwisho. Kwa utukufu Wake Mwenyewe, Bwana asingeweza kuwakinga dhidi ya majaribu; kwa kuwa kusudi la msingi wa hayo majaribu ni kuwaandaa watu ili wapate kuvipinga vishawishi/ vivutio vyote ving’aavyo vya uovu. [GC 528.3; PK Aya ya 33]

Sio watu waovu wala mashetani wanaoweza kuzuia kazi ya Mungu, au kuwafungia mlango watu Wake wasiwe na uwepo Wake, ikiwa watadhamiria kwa mioyo yenye utiifu, na iliyopondeka kutubu na kuachana na dhambi zao, na kisha kwa imani wadai ahadi Zake. Kila jaribu, kila nguvu ya upinzani, ikiwa ya wazi au ya siri, inaweza kupingwa kwa mafanikio, “si kwa uwezo, wala si kwa nguvu, bali kwa Roho Wangu, asema Bwana wa Majeshi.” Zekaria 4:6. [GC 529.1; PK Aya ya 34]

### Uwezo Alio Nao Mwangamizi

“Kwa kuwa macho ya Bwana huwaelekea wenye haki, Na masikio yake husikiliza maombi yao...” Naye ni nani atakayewadhuru ikiwa ninyi ni wafuasi wa lililo jema?” 1 Petro 3:12, 13. Wakati Balaamu aliposhawishiwa kwa ahadi ya kupewa zawadi za gharama nyingi, alijaribu kuwaloga wana Israeli na kwa kutoa kafara zake kwa Bwana alitaka kuwaletea laana watu Wake Bwana, Roho wa Mungu alimkataza kusema uovu aliotamani sana kuutamka, na Balaamu akalazimishwa kutamka Maneno haya kwa Mshangao: “Nitamlaanije yeye ambaye Mungu hakumlaani? au nimtukaneje yeye ambaye Bwana hakumtukana? "Na nife kifo cha mwenye haki, na mwisho wangu uwe kama wake!" Baada ya kafara

kutolewa tena, nabii asiyemcha Mungu alitangaza: “Tazama, nimepokea amri kubariki, Naye amebariki; na siwezi kuigeuza. Hakuona uovu katika Yakobo, Wala Hakuona ukaidi katika Israeli; Bwana, Mungu wake, Yu pamoja naye, Na sauti ya mfalme i katikati yao.” “Hakika hapana uchawi juu ya Yakobo, wala hapana uganga juu ya Israeli; Lakini hata hivyo, mara ya tatu madhabahu zikajengwa, na Balaamu alijaribu tena kutupa laana. Lakini kutoka katika midomo isiyopenda ya yule nabii, Roho wa Mungu alitangaza mafanikio ya wateule Wake, na kukemea upumbavu na nia mbaya za maaadui zao: “Na abarikiwe kila akubarikiye, na alaaniwe kila akulaaniye.” Hesabu 23:8, 10, 20, 21, 23; 24:9. [GC 529.2; PK Aya ya 35]

Watu wa Israeli kwa wakati huu walikuwa watiifu kwa Mungu; na kwa kadri walivyodumu kutii sheria Yake, hakuna nguvu yoyote duniani au kuzimuni ambayo ingeweza kuwashinda. Lakini laana ambayo Balaamu alilkatazwa kuitamka dhidi ya watu wa Mungu, hatimaye alifaulu kuileta juu yao kwa kuwashawishi na kuwafanya watende dhambi. Walipozivunja amri za Mungu, ndipo walijitenga Naye, nao waliachwa wazionje nguvu za mwangamizaji. [GC 529.3; PK Aya ya 36]

Shetani anatambua fika ya kwamba mtu yule aliye dhaifu kuliko wote ambaye anakaa ndani ya Kristo anayazidi nguvu majeshi yote ya giza, na ya kwamba, kama angejifunua waziwazi kabisa, basi, angekabiliwa na upinzani na kushindwa. Kwa hiyo anajitahidi kuwavuta askari wa msalaba watoke mbali na ngome yao imara, huku akiwa anawavizia pamoja na majeshi yake, akiwa tayari kuwaangamiza wote wanaothubutu kulikanyaga eneo lake. Ni kwa kumtegemea Mungu kwa unyenyekevu tu, na kuzitii amri Zake zote, ndipo sisi tunaweza kuwa salama. [GC 530.1; PK Aya ya 37]

Hakuna mwanadamu aliye salama kwa siku moja au saa moja bila maombi. Muhimu kuliko yote, tunapaswa kumlilia Bwana kwa bidii ili atupe hekima ya kulielewa Neno Lake. Humo zimefichuliwa hila za yule mjaribu, na njia ambazo tunaweza kumpinga kwa mafanikio. Shetani ni bingwa wa kudondoa/kunukuu Maandiko, akiweka tafsiri yake mwenyewe juu ya mafungu ambayo anatarajia kutufanya tujikwae nayo. Sisi tunapaswa kujifunza Biblia kwa unyenyekevu wa moyo, kamwe tusisahau hitaji letu la kumtegemea Mungu. Wakati ambapo inatupasa kuwa macho siku zote dhidi ya hila za Shetani, tunapaswa daima kuomba kwa imani tukisema: "Usitutie majaribuni." [GC 530.2; PK Aya ya 38]

# SURA YA 33

# UDANGANYIFU WA KWANZA MKUU

**(Siri Ya Kupata Uzima Wa Milele)**

Ufupisho: Moja ya udanganyifu wa kushangaza wa wakati wote ulianzishwa na Shetani maelfu ya miaka iliyopita. Inashangaza kwamba ni wachache leo wanautambua udanganyifu huu jinsi ulivyo. Na bado adui anazikamata roho na kuzishikilia sana kwenye wavu wake. Sasa utajifunza jinsi Shetani anavyotumia wafu--kuwakamata walio hai.

Tangu mwanzoni kabisa wa historia ya kuwepo kwa mwanadamu, Shetani alianza juhudi zake za kuidanganya jamii yetu ya kibinadamu (race). Yule aliyechochea uasi mbinguni alitamani kuwaleta wakazi wa dunia hii waungane naye katika vita yake dhidi ya serikali ya Mungu. Adamu na Hawa walikuwa na furaha kamilifu katika kuitii kwao ile Sheria ya Mungu (Amri Zake Kumi),* na Ukweli huu ulikuwa sikuzote ni ushuhuda dhidi ya madai ambayo Shetani alikuwa ameyasisitiza kule mbinguni, kwamba Sheria ya Mungu ilikuwa ni ya ukandamizaji, tena ilikuwa kinyume na maslahi ya viumbe Vyake. Na zaidi ya hayo, kijicho cha Shetani kiliamshwa alipoyaona makao mazuri yaliyokuwa yameandaliwa kwa watu wawili, jozi, mume na mke, waliokuwa hawana dhambi. Akaazimu kusababisha anguko lao, ili, akiisha kuwatenganisha mbali na Mungu, apate kuwaweka chini ya mamlaka yake, kisha apate kuichukua na kuimiliki dunia hii kama yake na kuusimika ufalme wake akipingana na Yeye Aliye juu. [GC 531.1; PK Aya ya 1]

Endapo Shetani angekuwa amejifunua katika tabia yake halisi, angekuwa angepingwa mara moja, kwa kuwa Adamu na Hawa walikuwa wamekwisha kuonywa dhidi ya adui huyo wa hatari; lakini alifanya kazi yake gizani, akilificha kusudi lake ili apate kulitekeleza lengo lake kwa ufanisi zaidi. Akimtumia nyoka kama njia yake, kiumbe ambaye wakati ule alikuwa na mwonekano wa kuvutia sana, Shetani yeye mwenyewe akazungumza na Hawa, akisema: "Ati! Hivi ndivyo alivyosema Mungu, Msile matunda ya miti yote ya bustani?" Mwanzo 3:1. ikiwa Hawa angejizuia asiingie katika majadiliano na yule mjaribu, angekuwa salama; lakini yeye alijitosa ajadiliane naye na ndipo alipoanguka, na akawa mhanga wa hila zake (akanaswa mtegoni). Ni kwa njia hiyo hiyo wengi bado wanatwezwa naye. Wanatilia mashaka na kuhoji matakwa ya Mungu; na badala ya kuzitii amri za Mungu, wao wanazipokea nadharia za kibinadamu, ambazo kimsingi zinaficha mitego ya Shetani. [GC 531.2; PK Aya ya 2]

"Mwanamke akamwambia nyoka, Matunda ya miti ya bustanini twaweza kula; Lakini matunda ya mti ulio katikati ya bustani Mungu amesema, Msiyale wala msiyaguse, msije mkafa. Nyoka akamwambia mwanamke, Hakika hamtakufa. Kwa maana Mungu anajua ya kwamba siku mtakayokula matunda ya mti huo, mtafumbuliwa macho, nanyi mtakuwa kama Mungu, mkijua mema na mabaya." fungu la 2-5. Shetani aliwatangazia kwamba wangekuwa kama Mungu wakiwa na hekima nyingi sana kuliko hapo kwanza na kuwa na uwezo wa kuishi wa hali ya juu zaidi. Hawa akajisalimisha kwa jaribu lile na kuanguka; na kwa kupitia ushawishi wa Hawa, Adamu aliongozwa kutenda dhambi. Waliyakubali maneno ya nyoka, kwamba Mungu hakumaanisha kile alichokisema; walimtilia mashaka Muumbaji wao, tena walimwazia kwamba Yeye alikuwa anawawekea mipaka ya uhuru wao na ya kwamba wao wangeweza kupata hekima kubwa na kuinuliwa juu kwa kuivunja Sheria Yake (Amri). [GC 532.1; PK Aya ya 3]

Lakini Je! Ni jambo gani ambalo Adamu aliligundua baada ya kutenda dhambi yake kuhusu maana ya Maneno “kwa maana siku utakapokula matunda ya mti huo utakufa hakika.” Je, aligundua kile ambacho Shetani alimwongoza kuamini kwamba angeinuliwa na kuingizwa kati maisha ya hali ya juu? Kama kweli ilikuwa ndivyo hivyo, basi, kwa hakika tungeamini kwamba kulikuwa na faida kubwa iliyopatikana kwa kuasi Sheria ya Mungu, yaani kutenda dhambi (Amri Zake), na Shetani angethibitishwa kuwa mfadhili wa jamii ya mwanadamu. Lakini Adamu hakugundua kuwa huu Uongo wa Shetani, ndiyo ilikuwa maana ya sentensi ya hukumu ambayo Mungu aliitoa. Mungu alitangaza kwamba kama adhabu kwa dhambi zake, mwanadamu angepaswa kurudi mavumbini alikotolewa. “Kwa maana u mavumbi wewe, nawe mavumbini utarudi.” Fungu la 19. Maneno yale ya Shetani aliyosema, “mtafumbuliwa macho,” yalionekana kuwa ni ya kweli kwa maana hii moja tu: baada ya Adamu na Hawa kumwasi Mungu, macho yao yalifumbuliwa kutambua upumbavu wao; ni kweli kwamba hawakujua uovu au dhambi ni nini, na walionja tunda chungu la matokeo ya uasi (uvunjaji wa Amri za Mungu). [GC 532.2; PK Aya ya 4]

Katikati ya Edeni ulikuwa mti wa uzima, ambao matunda yake yalikuwa na uwezo wa kuendeleza uhai/uzima wao. Ikiwa Adamu angedumu kuwa mtiifu kwa Mungu, angekuwa ameendelea kufurahia uhuru wake wa kuuendea mti wa uzima na kula matunda yake, naye angeishi milele. Lakini alipotenda dhambi alikatazwa asiuendee mti wa uzima na kula matunda yake, naye alikabiliwa na kifo. Hukumu hiyo ya Mungu isemayo, “U mavumbi wewe, na mavumbini utarudi,” huonyesha kutoweka kabisa kwa uzima (kukoma kwa uhai). [GC 532.3; PK Aya ya 5]

Hali ya kutokufa yaani uzima wa milele, ambayo mwanadamu alikuwa amehidiwa kwa sharti la utii, iliondolewa kwa sababu ya kutenda dhambi (kuivunja Sheria ya Mungu). Lakini Adamu asingeweza kurithisha wazao wake kile ambacho yeye mwenyewe hakuwa nacho; na kulikuwa hakuna tumaini lolote kwa jamii ya wanadamu iliyoanguka, dhambini ikiwa Mungu kwa njia kumtoa Mwanawe kama kafara, asingerudisha hali ya kutokufa karibu nao ili waweze kuipata. Wakati ambapo “mauti iliwafikia watu wote kwa sababu wote wamefanya dhambi," Kristo amebatilisha mauti na “ameufunua uzima na kutokuharibika, kwa ile Injili." Warumi 5:12; 2 Timotheo 1:10. Tena ni kwa njia ya Kristo peke Yake hali ya kutokufa inaweza kupatikana. Yesu alisema hivi: “Amwaminiye Mwana yuna uzima wa milele; asiyemwamini Mwana hataona uzima.” Yohana 3:36. Kila mtu anaweza kumiliki mbaraka huo wa thamani isiyokadirika kama atatimiza masharti yake. Wote “wale ambao kwa saburi katika kutenda mema wanatafuta utukufu na heshima na kutokuharibika,” watapewa “uzima wa milele.” Warumi 2:7. [GC 533.1; PK Aya ya 6]

Mdanganyaji mkuu pekee ndiye aliyemuahidi Adamu uzima katika uasi (kuvunja amri za Mungu). Na tangazo la nyoka kwa Hawa ndani ya Bustani ya Edeni -- “Hakika hamtakufa” -- lilikuwa ndilo hubiri la kwanza lililowahi kuhubiriwa kuhusu hali ya kutokufa kwa roho. Hata hivyo, tangazo hilo, lililojengwa juu ya mamlaka ya Shetani peke yake mwangwi wake unasikika (mahubiri yake yanarudiwa-rudiwa) kutoka katika vibweta vya Ulimwengu wa Kikristo, na kupokelewa kwa utayari na watu wengi sana miongoni mwa wanadamu kama lilivyopokelewa na wazazi wetu wa kwanza. Hukumu ya Mungu isemayo, “Roho itendayo dhambi, ndiyo itakayokufa” (Ezekieli 18:20). Kwao inatafsiriwa kumaanisha: Roho itendayo dhambi, siyo itakayokufa, bali ndiyo itakayoishi milele. Sisi hatuna la kufanya ila kushangaa tu jinsi wanadamu wanavyoweza kupumbazwa akili kwa namna ya ajabu na kufanywa kuyaamini mno maneno haya ya Shetani na kukataaa kuwa na imani kabisa na Maneno ya Mungu. [GC 533.2; PK Aya ya 7]

Ikiwa mwanadamu baada ya anguko lake, angeruhusiwa kuufikia mti wa uzima, basi, angeishi milele; na kwa hivyo dhambi ingefanywa kuwa ya milele. Lakini makerubi na upanga wa moto uliogeuka huku na huko vililinda “njia ya mti wa uzima” Mwanzo 3:24, na wala hakuna hata mmoja katika familia ya Adamu ambaye amewahi kuruhusiwa kupita kizuizi kile na kula tunda linalotoa uzima. Kwa hiyo, hakuna mwenye dhambi yeyote aliye na uzima wa milele ndani yake (Warumi 3:23). [GC 533.3; PK Aya ya 8]

Lakini baada ya Anguko, Shetani aliwaamuru malaika zake wafanye juhudi maalumu za kupandikiza imani ya hali ya kutokufa kwa mwanadamu; kisha, baada ya kuwashawishi wanadamu kulipokea fundisho hili la uongo au kosa, iliwapasa kuwaongoza wanadamu watoe hitimisho lao kwamba mwenye dhambi angeishi katika mateso na huzuni ya milele na milele (Jehanamu). Sasa, mfalme huyu wa giza, akiwa anafanya kazi yake kupitia kwa mawakala wake, anamwakilisha Mungu kuwa ni mtu katili, na dhalimu sana anayelipiza kisasi, tena anatangaza kwamba anawatupa jehanamu wote wasiompendeza Yeye, na kuwafanya wapate kuionja ghadhabu Yake mle; na ya kwamba wanapoendelea kupata maumivu makali sana yasiyoelezeka na huku wakigaragara na kuhangaika katika ndimi za moto wa milele, Muumbaji wao anawaangalia hapo chini walipo na kuridhika. [GC 534.1; PK Aya ya 9]

**Shetani Anamwelezea Mungu Vibaya**

Kwa hiyo adui mkuu anamvika Muumbaji na Mruzuku wa wanadamu, kwa sifa zake mwenyewe. Ukatili ni wa Shetani. Mungu ni pendo (Yn. 8:44, 1 Yoh. 4:8); na vitu vyote alivyoviumba Mungu vilikuwa safi, vyema, vitakatifu, na vyenye kupendeza, mpaka dhambi ilipoingizwa humu duniani na mwasi mkuu wa kwanza. Shetani mwenyewe ndiye adui anayemjaribu mwanadamu atende dhambi, halafu akiweza, ndipo anamwangamiza; tena, yeye anapohakikisha

amefaulu kupata mhanga wake, ndipo anaposhangilia sana kwa ajili ya maangamizi aliyotenda. Endapo angeruhusiwa, angeifutilia mbali jamii yote ya wanadamu katika wavu wake. Isingekuwa ni kule kuingilia kati kwa nguvu za Mungu, hakuna mwana au binti ya Adamu hata mmoja ambaye angeweza kuponyoka. [GC 534.2; PK Aya ya 10]

Siku hizi Shetani anafanya jitihada yake kubwa sana ili kuwashinda wanadamu, kama alivyowashinda wazazi wetu wa kwanza, kwa kuitikisa imani yao (tumaini lao) kwa Muumbaji wao na kuwaongoza kutilia mashaka juu ya hekima ya serikali Yake pamoja na haki ya Sheria Yake (Amri Zake). Shetani na vibaraka wake humwakilisha Mungu kana kwamba ni mbaya sana hata kuliko wao wenyewe walivyo, ili kuhalalisha nia yao mbaya ya kuwadhuru wanadamu pamoja na uasi wao. Mlaghai huyu mkuu anajitahidi sana kuhamishia ukatili wa kutisha wa tabia yake na kuuweka juu ya Baba yetu wa mbinguni, ili aweze kutengeneza hali ya yeye kuonekana kama ndiye aliyetendewa vibaya kwa kufukuzwa toka mbinguni ati kwa sababu yeye hakukubali kumtii gavana dhalimu kama huyo. Anawasilisha mbele ya ulimwengu uhuru ambao wanadamu wangeweza kuufurahia chini ya utawala wake usio na ukali, mwepesi, tofauti na kongwa la utumwa la amri kali sana za Yehova (Kanuni Zake) ambalo Mungu ameliweka kwa nguvu juu yao. Kwa njia hiyo Shetani anafanikiwa kuwashawishi wanadamu na kuwafanya wasimtii Mungu. [GC 534.3; PK Aya ya 11]

### Fundisho La Dini Lilionea Sana

Kinachochukiza na kushtua hisia ya upendo na rehema iliyomo moyoni mwetu, na hata kwa uelewa wetu wa haki, ni Fundisho lile lisemalo kwamba waovu wale waliokufa wakiwa na dhambi zao wanateswa kwa moto na kiberiti katika jehanumu inayoendelea kuwaka moto milele zote; kwamba kwa ajili ya dhambi zao za kipindi kifupi cha maisha yao waliyokuwa nayo hapa duniani, inawapasa kupata mateso wakati wote ambao Mungu atadumu kuwepo. Lakini, fundisho hilo limemekuwa likifundishwa kote duniani, na bado limewekwa miongoni mwa misingi ya imani katika ulimwengu wa Kikristo (Creeds) nyingi za Ulimwengu wa Kikristo. Alisema hivi daktari mmoja msomi wa shahada ya Uchungaji na theolojia (Uzamivu-Doctor of Divinity DD): "Mwonekano wa mateso makali ya jehanum utaongeza sana furaha ya watakatifu milele hata milele. Wanapowaona wengine wenye asili kama ya kwao na waliozaliwa chini ya mazingira yale yale kama yao, wakitumbukizwa katika mateso kama yale, na wao wakiwa wamepewa heshima kubwa, jambo hili litawafanya wao wajue maana ya kwanini wawe na furaha kubwa." Mwingine (mwenye shahada ya dini) alitumia maneno haya: "Wakati amri ya kukataliwa inaendelea kutekelezwa milele na milele juu ya miili inayopokea ghadhabu (vyombo vya ghadhabu), moshi wa maumivu yao utakuwa ukipanda juu milele hata milele na ukionwa na walengwa wa rehema (wale

watakatifu), ambao, badala ya kushiriki mateso ya hawa wenye huzuni na waliokataliwa (mle motoni), watasema, Amina, Haleluya! Bwana na asifiwe!" [GC 535.1; PK Aya ya 12]

Je! Ni wapi, Fundisho hili linapatikana katika kurasa za Neno la Mungu? Je! waliokombolewa mbinguni watapoteza hisia zote za huruma, kujali na sikitiko (hata upendo), na hata wasiwe na hisia za umoja wa ubinadamu wa kawaida walizokuwa nazo hapa duniani? Je, hisia hizo zitaondolewa na kuwa na ubaridi mkavu usiojali kama wa mtu yule asiyejali furaha, wala huzuni, wala maumivu (stoic), au zitakuwa na ukatili usio na huruma wa watu washenzi (wasiostaarabika)?* Hapana, Hapana; haya si mafundisho yatokayo katika Kitabu cha Mwenyezi Mungu. Wale wanaowasilisha maoni yaliyoelezwa katika dondoo hizo zilizotolewa hapo juu huenda wakawa ni wasomi sana na hata kuwa watu walio wanyofu wa moyo, lakini wamepotoshwa na uongo wa Shetani. Anawaongoza wakose kuelewa na kutafsiri vyema kauli nzito na zenye nguvu za Maandiko, akiipa lugha inayoonyesha picha au rangi ya uchungu (kinyume cha upendo), kifo, nia mbaya, chuki na uovu, mambo ambayo ni yake mwenyewe, lakini si ya Muumbaji wetu. "Kama Mimi niishivyo, asema Bwana MUNGU, sikufurahii kufa kwake mtu mwovu; bali aghairi mtu mwovu, na kuiacha njia yake mbaya, akaishi. Ghairini, ghairini, mkaache njia zenu mbaya; mbona mnataka kufa, Enyi nyumba ya Israeli?" Ezekieli 33:11. [GC 535.2; PK Aya ya 13]

Hivi Mungu angepata faida gani ikiwa sisi tungekubali kwamba Yeye anafurahia kushuhudia mateso makali yasiyokoma; kwamba Yeye anatumbuizwa kwa kilio chao cha maumivu makali na yowe za maneno ya laana ya viumbe wale wanaoteswa ambao anawashikilia katika miale ya moto wa jehanamu? Je, sauti hizo za kuchukiza zinaweza kuwa muziki mzuri katika sikio la Upendo wa milele? Kuna hoja inatolewa nao kuwa kupatilizwa kwa maumivu yasiyokoma dhidi ya waovu kungeonyesha chuki ya Mungu dhidi ya dhambi kuwa ni uovu unaoharibu amani na utulivu wa sayari zote. Loo! Hii ni kufuru ya kutisha! Kana kwamba chuki ya Mungu dhidi ya dhambi ndiyo sababu ya mateso hayo yanayoendelezwa. Kwani, kulingana na mafundisho ya wanatheolojia hao, kuendelezwa kwa mateso bila kuwapo tumaini la rehema, kunawafanya wahanga masikini wawe na hasira zaidi na kadri wanavyopofoka na kumwaga hasira yao nje kwa laaana na kufuru, wanazidi kuongeza mzigo wao wa hatia milele hata milele. Utukufu wa Mungu hauongezwi kwa njia hiyo ya kuudumisha na kuuongeza mzigo wa dhambi daima, katika zama zisizo na mwisho (zisizokoma, milele na milele). [GC 536.1; PK Aya ya 14]

**Uovu Ulioletwa Na Uzushi wa Mateso Yasiyokoma**

Ni nje ya uwezo wa akili ya mwanadamu kukadiria uovu ambao umefanywa kwa njia ya fundisho la uongo la mateso yanayoendelea kama adhabu ya milele

na milele. Dini ya Biblia iliyojaa upendo na fadhili, na ikiwa imesheheni tele, inatiwa giza kwa ushirikina huo, na kuvikwa vazi la kuogofya sana. Tunapotafakari jinsi Shetani alivyoipaka rangi za uongo tabia ya Mungu, je, tunaweza kushangaa kuona Muumbaji wetu Mwenye rehema nyingi anavyoogopwa, anavyohofiwa sana, na hata kuchukiwa na watu? Mawazo haya ya kustusha na kutisha mno kumhusu Mungu yaliyosambazwa kote ulimwenguni kutokana na mahubiri yanayotolewa katika mimbari, yamewafanya maelfu, ndiyo, mamilioni wamtilie mashaka Mungu na Neno Lake na wengine wawe makafiri kabisa. [GC 536.2; PK Aya ya 15]

Nadharia hiyo ya mateso yanayoendelea milele kama adhabu ni mojawapo ya mafundisho ya uongo yanayotengeneza mvinyo wa machukizo ya Babeli (dini ya uongo), ambao anawanyweshwa watu wa mataifa yote. Ufunuo14:8; 17:2. Ukweli kwamba wachungaji na wahudumu wa Kristo walilipokea fundisho hili la uongo na kulihubiri kutoka katika vibweta vitakatifu, kwa kweli, ni siri na fumbo la ajabu asiloweza kulielewa mwanadamu. Wao walilipokea kutoka Roma, kama walivyopokea kutoka kwake sabato ya uongo (Jumapili). Ni kweli, limefundishwa na watu wanaoheshimiwa na wema kabisa; lakini nuru juu ya somo hili haikuwa imewafikia wao kama ilivyotufikia sisi (Mithali 4:18). Wao waliwajibika tu kwa nuru ile iliyomulika katika nyakati zao; sisi nasi tunawajibika kwa ajili ya nuru inayomulika katika wakati wetu. Tukiupa kisogo ushuhuda wa Neno la Mungu, na kukubali kuyapokea mafundisho hayo ya uongo, ati kwa sababu baba zetu waliyafundisha, basi, tutakuwa tukiangukia chini ya hukumu iliyotangazwa juu ya Babeli; tutakuwa tunakunywa mvinyo wa ghadhabu ya machukizo yake (uasherati wake, mafundisho yake ya uongo). [GC 536.3; PK Aya ya 16]

Tabaka kubwa la wale ambao kwao fundisho la mateso ya adhabu ya moto wa milele na milele linawachukiza mno, wanaswaga upande mwingine wa kosa lililo kinyume cha lile la kwanza. Hawa wanaona kwamba Maandiko yanamwakilisha Mungu kama Mwenye Uhai, Mwenye upendo na huruma, nao hawawezi kuamini kwamba Yeye atawapeleka viumbe Wake motoni katika jehanamu inayowaka milele hata milele. Lakini wakiwa wanaishikilia imani isemayo kwamba roho kwa asili yake ina uzima wa milele, yaani haifi, nao basi hawaoni njia nyingine yoyote isipokuwa kuhitimisha kuwa wanadamu wote hatimaye wataokolewa. Wengi wanavichukulia vitisho vilivyomo ndani ya Biblia kwamba vimetengenezwa kuwatisha tu wanadamu ili wawe watiifu, na siyo kweli kuwa vitatimizwa kiuhalisi. Kwa hivyo mwenye dhambi anaweza kuishi katika anasa za kibinafsi anavyotaka, huku akipuuzia matakwa (maagizo) ya Mungu, na bado atarajie hatimaye kupokelewa na kukubaliwa Naye. Fundisho kama hilo, lenye kudhania kwa kiburi kujipatia rehema ya Mungu, lakini likipuuza uwepo wa haki ya Mungu, linaufurahisha moyo wa wanadamu unaopenda matendo ya kimwili (ambao

haujazaliwa mara ya pili) na kuwapa moyo wa ujasiri waovu kuendelea katika dhambi zao. [GC 537.1; PK Aya ya 17]

Ili kuonyesha jinsi waaminio katika wokovu wa watu wote duniani wanavyopotosha Maandiko kwa madhumuni ya kuhalalisha mafundisho yao ya dini yanayoziangamiza roho za watu, tunahitaji tu kudondoa kaulizinazotoka midomoni mwao wenyewe kama mfano ili kuithibitisha hoja hii. Kwenye mazishi ya kijana mwanamume asiye na dini, ambaye alikuwa ameuawa papo hapo kwa ajali (ghafla), mchungaji mwenye Imani isemayo Watu Wote Wataokolewa* alichagua kama fungu lake kuu kauli ya Maandiko iliyomhusu Daudi: "Kwa kuwa ametulizwa kwa habari ya Amnoni, kwa maana amekufa." 2 Samueli 13:39 *(Fundisho la kila mtu ataenda mbinguni-Universal Salvation Dogma, mshiriki wake anaitwa Universalist). [GC 537.2; PK Aya ya 18]

"Huwa ninaulizwa mara kwa mara," alisema mhubiri yule, "hatima yao itakuwaje wale wanaoondoka duniani wakiwa wenye dhambi, wanaokufa, pengine wakiwa wamelewa, wakifa wakiwa na madoa mekundu sana katika majoho yao ambayo hayajaondolewa kutokana na uhalifu wa jinai walioutenda, au wakifa kama alivyokufa kijana huyu, wakiwa hawajapata kamwe kuikiri imani au kuwa na uzoefu wowote wa maisha ya kidini. Sisi tunaridhishwa na Maandiko; jibu litokalo katika Maandiko hayo linatatua tatizo hilo la kuogopesha sana. Amnoni alikuwa mwovu kupita kawaida; hakuwa na muda wa kutubu, alileweshwa, na wakati alipokuwa katika hali ya kulewa aliuawa. Daudi alikuwa ni nabii wa Mungu; basi ni lazima atakuwa alijua kama hatima ya mwanawe Amnoni ingekewa mbaya au nzuri katika ulimwengu ujao. Maelezo kutoka moyoni mwake yalikuwa yana ujumbe gani? Alichagua fungu la Maandiko matakatifu lilimlohusu Daudi: "Ametulizwa kwa habari ya Amnoni, kwa maana amekufa." 2 Samweli 13:39. [GC 537.2; PK Aya ya 19]

"Basi, fundisho gani tunaweza kulipata kutokana na lugha hiyo iliyotumika hapo? Je, hiyo haimanishi kwamba mateso yasiyokoma hayakuwa sehemu ya imani yake ya dini? Hivyo ndivyo tuonavyo sisi; tena hapo tunagundua hoja iletayo ushindi katika inayotetea neno lile tunalolikubali sisi ingawa halijathibitika (nadharia/hypothesis), ambalo linapendeza zaidi, lina hekima zaidi, tena lina ukarimu zaidi, ambalo linahusu utakatifu wa watu wote ulimwenguni na Amani mwishowe. Yeye alifarijiwa, alipomwona mwanawe amekufa. Na kwa nini iwe hivyo? Kwa sababu kwa jicho la kiunabii aliweza kuona mbele katika wakati ujao wenye utukufu baadaye na kumwona mwanawe Amnoni akiwa ameepushwa na kuwekwa mbali sana na majaribu yote, akiwa amefunguliwa kutoka kwenye utumwa na kuoshwa uchafu wote wa dhambi zake, na baada ya kufanywa mtakatifu kwa kiwango cha kutosha na kupewa nuru ya kutosha, aliruhusiwa kuingia katika kusanyiko la roho zilizokwisha kupaa juu, zilizokuwa zinafurahia sana. Faraja yake ya pekee, ilikuwa ni kwamba katika

kuondolewa kwake kutoka katika hali yake ya sasa ya dhambi na mateso, mwanawe mpendwa alikuwa amekwenda kule ambako uvuvio wa hali ya juu kabisa wa Roho Mtakatifu ungemulika nuru katika roho yake yenye giza, kule ambako akili yake ingefunguliwa na kupokea hekima ya mbinguni na shangwe tamu itokanayo na upendo usio na kikomo, na kwa njia hiyo kutayarishwa kupewa asili iliyotakaswa ili apate kufurahia pumziko la raha pamoja na kukaa na jamii ya watu wote watakaoirithi mbingu. [GC 538.1; PK Aya ya 20]

Katika mawazo haya sisi ni vyema tuelewe kuwa tunaamini kwamba wokovu wa mbinguni hautegemei kitu cho chote tuwezacho kukifanya sisi katika maisha haya, wala badiliko lolote la moyo kwa wakati huu wa sasa, wala imani ya sasa, au tunavyoikiri sasa kuwa tuna dini.” [GC 538.2; PK Aya ya 21]

Hivyo ndivyo asemavyo yule aliyedai kuwa ni mchungaji/mtumishi Wake Kristo ambaye alikuwa amekariri na kuurudia ule uongo uliosemwa na yule nyoka kule Edeni: “Hakika hamtakufa.” “Siku mtakayokula matunda ya mti huo, mtafumbuliwa macho, nanyi mtakuwa kama Mungu.” Anadai kwamba mwenye dhambi wa kupindukia - mwuaji, mwizi, na mzinzi—baada ya kifo chake, atakuwa ameandaliwa tayari kuingia katika raha ile ya milele (kutokufa). [GC 538.3; PK Aya ya 22]

Na ni kutokea wapi huyu mpotoshaji wa Maandiko anapata hitimisho au uamuzi wake huo? Ni kutoka katika sentensi moja tu inayoeleza kujisalimisha kwa Daudi kwa uongozi wa Mungu. Nafsi yake ilitamani “kutoka kumwendea Absalomu; kwa maana alifarijiwa kuhusiana na habari ya Amnoni, alipoona amekufa." Baada ya maumivu ya majonzi yake yakiwa yamepunguzwa makali kadri muda ulivyozidi kusonga mbele, mawazo yake yalihama kutoka kwa mwanawe aliyekufa na kuelekea kwa mwanawe aliyekuwa hai, aliyekuwa amejifukuza mwenyewe toka nyumbani kwao, akiogopa kuadhibiwa kwa haki kutokana na lile tendo lake baya alilokuwa amelitenda. Tena, wao wanasema kwamba ati huo ndio ushahidi unaoonyesha kwamba Amnoni, mhusika aliyembaka dada yake mwenyewe, na mlevi wa pombe, mara baada ya kifo chake, alichukuliwa mara moja kwenda hadi kwenye makao ya amani na raha ya milele, kutakaswa akiwa kule, na kuandaliwa kuishi katika ushirika wa malaika wasio na dhambi! Hii ni hekaya ya uongo na inayopendeza kweli kweli, ambayo inaridhisha moyo wenye tamaa za kimwili, usio na Roho wa Mungu! (usioongoka)! Hilo ni fundisho la Shetani mwenyewe, nalo linasaidia katika kazi yake kwa ufanisi mkubwa. Je, tushangae kweli kwamba kwa mafundisho kama haya, uovu unazidi kuongezeka? [GC 538.4; PK Aya ya 23]

Njia iliyofuatwa na huyu mwalimu mmoja wa uongo ni mfano wa wengine wengi. Maneno machache ya Maandiko yametenganishwa na muktadha,* ambayo katika hali nyingi ingeonyesha maana yake kuwa kinyume kabisa na tafsiri inayotolewa kuhusu maneno hayo; katika mafungu hayo ya Maandiko ambayo

yamekatwa-katwa, yanapotoshwa na kutumiwa kama uthibitisho wa mafundisho yao ya dini ambayo hayana msingi wowote katika Neno la Mungu. Ushahidi huo uliotolewa ambao umedondolewa ili kuthibitisha kwamba yule Amnoni mwovu, aliyelewa yuko mbinguni ni tafsiri inayopingana moja kwa moja na kauli wazi na chanya ya Maandiko inayoeleweka isemayo kwamba hakuna mlevi yeyote atakayeurithi ufalme wa Mungu. 1Wakorintho 6:10. Ni kwa njia kama hiyo wale wenye mashaka, wasioamini, na wale wenye kushuku Maneno ya Mungu, hugeuza Maneno ya Mungu kuwa uongo. Na watu wengi sana wamedanganyika kutokana na uongo wao na kuwekwa kwenye kitanda cha watoto wachanga kubembea mpaka wanapumbazwa na kusinzia katika kitanda cha usalama wa kimwili *(maneno yaliyotangulia au yanayofuatia). [GC au PK 539.1; PK Aya ya 24]

Endapo ingekuwa ni kweli kuwa roho za wanadamu wote hupita moja kwa moja na kuingia mbinguni wakati wa saa yao ya kufa, basi, tungeweza kutamani kufa kuliko kuishi. Wengi kutokana na fundisho hilo wameongozwa kukatisha maisha yao  Wanapolemewa sana na taabu, mifadhaiko, na kukatishwa tamaa, inaonekana kuwa ni jambo rahisi kwao kuukata uzi wa maisha unaokatika upesi na kupaa kwenda zao kwenye pumziko la raha ya ulimwengu wa milele. [GC 539.2; PK Aya ya 25]

**Ushahidi Wa Mwisho Kabisa**

Mungu ametoa katika Neno Lake uthibitisho wa hakika kwamba atawaadhibu wavunjaji wa sheria Yake (Amri Zake). Wale wanaojidanganya wenyewe kwa kujifariji kuwa Yeye ni mwingi wa rehema hata asiweze kutekeleza haki Yake dhidi ya mwenye dhambi, inabidi tu wautazame msalaba wa Kalvari. Kifo cha Mwana wa Mungu asiyekuwa na doa lolote (dhambi) ni ushuhuda tosha kwamba "mshahara wa dhambi ni mauti," yaani, kwamba kila uvunjaji wa Sheria ya Mungu ni lazima upokee malipo yake ya haki. Kristo asiye na dhambi, alifanyika dhambi kwa ajili ya mwanadamu (2 Kor. 5:21). Alibeba hatia ya dhambi zetu, hata alivumilia kufichwa kwa uso wa Baba Yake mpaka moyo Wake ulipovunjika na uhai Wake kupondwa-pondwa hadi kutoweka. Kafara hiyo yote ilifanywa ili wenye dhambi wapate kukombolewa. Kulikuwa hakuna njia nyingine ambayo kwayo mwanadamu angeweza kuachiliwa huru kutoka katika adhabu ya dhambi. Na kila mtu anayekataa katakata kuwa mshirika wa upatanisho huo uliopatikana kwa gharama kubwa mno kama hiyo, atalazimika kubeba hatia yake mwenyewe, hatia na adhabu yake mwenyewe  kwa kuivunja Sheria ya Mungu (Amri Zake) [GC 539.3; PK Aya ya 26]

Hebu na tuangalie zaidi kile ambacho Biblia inafundisha kuhusu waovu, yaani watu wasiomcha Mungu na wale wasiotubu, ambao yule mtetezi wa nadharia au imani isemayo kwamba'wokovu kwa ulimwengu wote bila kujali hali yao ya kiroho, au kama ni wema na waovu' (Universalist), ambaye kwa picha anatoa,

anawaweka watu wote mbinguni kama malaika watakatifu, wenye furaha. [GC 540.1; PK Aya ya 27]

"Mimi nitampa yeye mwenye kiu, ya chemchemi ya maji ya uzima, bure." Ufunuo 21:6. Ahadi hii ni kwa wale wenye kiu. Hakuna atakayepewa maji, isipokuwa ni wale tu wanaosikia kwamba wanalo hitaji la kunywa maji ya uzima, tena ambao wanayatafuta kwa hasara ya mambo mengine yote. "Yeye ashindaye atayarithi haya, Nami nitakuwa Mungu Wake, Naye atakuwa Mwanangu." fungu la Ufunuo 21:7. Hapa, pia, masharti yamebainishwa wazi, ili kurithi hayo yote, inatupasa tuipinge na kuishinda dhambi. [GC 540.2; PK Aya ya 28]

Bwana anatangaza kupitia kwa nabii Isaya, anasema: “Waambieni wenye haki kuwa watakuwa heri, kwa maaana watakula matunda ya matendo yao.” “Ole wake mtu mbaya (avunjaye Maagizo ya Bwana); shari itakuwa kwake; kwa maana atapewa ijara ya mikono yake.” Isaya 3:10, 11. "Ajapokuwa mwenye dhambi amefanya maovu mara mia, akazidisha siku zake; lakini hata hivyo najua hakika ya kwamba itakuwa heri kwao wamchao Mungu, wenye kicho mbele Zake; walakini haitakuwa heri kwa mwovu." Mhubiri 8:12, 13. Na Paulo naye anashuhudia kwamba mwenye dhambi anajiwekea mwenyewe akiba ya “hasira kwa siku ile ya hasira na ufunuo wa hukumu ya haki ya Mungu, atakayemlipa kila mtu kwa kadiri ya matendo yake;” “dhiki na shida juu ya kila nafsi ya mwanadamu atendaye uovu.” Warumi 2:5, 6, 9. [GC 540.3; PK Aya ya 29]

“Maana neno hili mnalijua hakika, ya kwamba hakuna mwasherati wala mchafu wala mwenye tamaa, ndiye mwabudu sanamu, aliye na urithi katika ufalme wa Kristo na Mungu." Waefeso 5:5. "Tafuteni kwa bidii kuwa na amani na watu wote, na huo utakatifu, ambao hapana mtu atakayemwona Bwana asipokuwa nao;" Waebrania 12:14. "Heri wazifuao nguo zao, wawe na amri kuuendea huo mti wa uzima, na kuingia mjini kwa milango yake. Huko nje wako mbwa, na wachawi, na wazinzi, na wauaji, na hao waabuduo sanamu, na kila mtu apendaye uongo na kuufanya." Ufunuo22:14, 15. [GC 541.1; PK Aya ya 30]

**Tangazo La Tabia Ya Mungu Ilivyo**

Mungu ametoa tamko kwa watu Wake, tabia Yake ilivyo na njia Yake ya kushughulika na dhambi. "Bwana, Bwana, Mungu mwingi wa huruma, Mwenye fadhili, si mwepesi wa hasira, mwingi wa rehema na kweli; Mwenye kuwaonea huruma watu elfu elfu, Mwenye kusamehe uovu na makosa na dhambi; wala si Mwenye kumhesabia mtu mwovu kuwa hana hatia kamwe; Mwenye kuwapatiliza watoto uovu wa baba zao, na wana wa wana wao pia, hata kizazi cha tatu na cha nne." Kutoka 34:6,7 "Wakosaji wataangamizwa pamoja, Wasio haki mwisho wao wataharibiwa." Zaburi 145:20, 37:38. Uwezo na mamlaka ya serikali ya mbinguni vitatumika kukomesha uasi (uvunjaji Amri za Mungu); lakini, hata hivyo, udhihirisho huo wote wa adhabu ya haki au mshahara wa dhambi, utapatana

kikamilifu na tabia ya Mungu ambaye ni Mwenye huruma nyingi, asiyekuwa mwepesi wa hasira, na Mwenye fadhili. [GC 541.2; PK Aya ya 31]

Mungu halazimishi mapenzi, nia au maamuzi ya mtu yeyote. Yeye hafurahii utiifu wa kitumwa, usiotumia akili, wa mtu kulazimishwa kutenda bila kupenda. Anatamani kwamba viumbe vilivyoumbwa kwa mikono Yake wampende kwa sababu Yeye Anastahili kupendwa. Angependa wamtii Yeye kwasababu wametambua kwa kutumia akili zao wenyewe kuwa Mungu ni Mwenye hekima, haki, ukarimu, na fadhila Zake. Na wote walio na uelewa sahihi wa sifa hizi watampenda kwa sababu wanavutwa Kwake kwa kustaajabia na kuvutiwa na sifa Zake. [GC 541.3; PK Aya ya 32]

Kanuni za wema, rehema, na upendo, zilizofundishwa na kuonyeshwa kwa vitendo katika maisha ya Mwokozi wetu, ni nakala, yaani mfano halisi wa mapenzi na tabia Yake Mungu. Kristo alisema kwamba Hakufundisha chochote isipokuwa kile alichopokea kutoka kwa Baba Yake. Kanuni za serikali takatifu ya Mungu, zinapatana kikamilifu na kanuni ya Mwokozi isemayo, “Wapende adui zenu." Mwenyezi Mungu anatekeleza haki juu ya waovu, kwa ajili ya manufaa ya sayari/malimwengu yote (universe), na hata kwa wale ambao hukumu Yake inapatilizwa juu yao ni kwa manufaa yao. Angeweza kuwafanya wawe na furaha ikiwa angeweza kufanya hivyo kwa mujibu wa sheria za serikali Yake na haki/uadilifu wa tabia Yake. Anawazungushia viashiria vya upendo Wake, anawapa fursa ya kujipatia ujuzi wa sheria Yake, na kuwafuatilia kwa kuwapa fursa ya rehema Yake; lakini wanachukia upendo Wake, wanaibatilisha sheria Yake, na kukataa rehema Yake. ijapokuwa wanazipokea zawadi Zake daima, wanamvunjia heshima Mpaji wao; wanamchukia Mungu kwa sababu wanajua kwamba anazichukia dhambi zao. Bwana anavumilia kwa muda mrefu uasi wao wa kukusudia; lakini saa ya mwisho ya kuamua mambo yote hatimaye itafika, ndipo mustakabali wao utakapoamriwa. Je! wakati ukifika, atawakamata hawa waasi na kuwafunga kwa minyororo upande Wake? Je! atawalazimisha kwa kutumia nguvu ili wapate kuyafanya mapenzi yake? [GC 541.4; PK Aya ya 33]

Wale waliokwisha kumchagua Shetani kama kiongozi wao, tena wanatawaliwa na nguvu Yake, hawako tayari kuingia katika uwepo wa Mungu. Kiburi, udanganyifu, uasherati, ukatili, vimejengeka na kuimarishwa katika tabia zao. Je,wanaweza kuingia mbinguni ili wapate kuishi kule milele pamoja na wale waliokuwa wamewadharau, wamewadhihaki, na kuwachukia walipokuwa nao hapa duniani? Kamwe, Ukweli hautakubalika kwa mtu mwongo; unyenyekevu hautamridhisha mwenye tabia ya kujiinua au kujisifu na mwenye kiburi; usafi wa maisha haukubaliki kwa mfisadi; upendo usiobagua, yaani usio na upendeleo hauonekani kumvutia mtu mchoyo/mbinafsi anayejifikiria. Ni chanzo gani cha furaha ambacho mbingu ingeweza kuwapatia wale waliozama katika tija za dunia

hii, na maslahi ya kichoyo, yanayowanufaisha wenyewe tu? [GC 542.1; PK Aya ya 34]

Ikiwa wale ambao maisha yao yote yametumiwa katika uasi dhidi ya Mungu wangeweza kupelekwa kwa ghafla hadi mbinguni na kushuhudia hali ya juu mbinguni, ya utakatifu na ya ukamilifu ambayo iko huko, --kila nafsi ikiwa imejazwa kwa upendo, kila uso uking'aa kwa furaha, muziki unaobubujika kwa sauti za kupendeza haswa za vyombo vya nyuzi (kinubi) ukipanda juu kwa heshima ya Mungu na Mwana-Kondoo, na vijito vya miale ya nuru visivyokoma vikitiririka juu ya wale waliokombolewa kutoka katika uso wa Yeye aketiye juu ya kiti cha enzi,-- Je, wale ambao mioyo yao imejaa chuki dhidi ya Mungu, na dhidhi ya Ukweli na utakatifu, wangeweza kuchanganyika na mkutano huo wa mbinguni na kuungana nao kuimba nyimbo za sifa? Je, wangeweza kuustahimili utukufu wa Mungu na wa Mwana-Kondoo? Hapana, hapana; walishapewa miaka mingi ya majaribio na mlango wa rehema ulikuwa wazi kwao ili waweze kujenga tabia kwa ajili ya mbinguni; lakini hawakufundisha akili yao kupenda usafi wa maisha au utakatifu; hawajawahi kujifunza lugha ya mbinguni, na sasa wamechelewa mno kujifunza. Maisha ya uasi dhidi ya Mungu yamewafanya wasiwe na sifa kabisa kwa ajili ya kuishi mbingu. Usafi wa maisha ya mbinguni, utakatifu wake na amani yake yangekuwa mateso makali kwao (tocha/torture); utukufu wa Mungu ungekuwa moto ulao kwao. Wangetamani sana kutimua mbio kutoka mahali pale patakatifu. Wangekaribisha kifo chao kwa furaha, ili nyuso zao zifichwe na hivyo wasiweze kuuona uso Wake Yeye aliyekufa ili kuwakomboa. Hatima ya waovu imeamriwa kutokana na chaguo lao wenyewe. Kutokwenda kwao mbinguni ni kwa hiari yao wenyewe, na ni haki na rehema ya Mungu. [GC 542.2; PK Aya ya 35]

### Rehema Zake Mungu

Kama maji ya Gharika, mioto ya siku ile kuu ya mwisho, inatangaza hukumu ya Mungu ya mwisho inayoonyesha kwamba waovu hawawezi kuponywa. Hawana mwelekeo wa kujisalimisha chini ya mamlaka ya Mungu. Nia (mapenzi) yao ilitumika na kuzoeshwa katika uasi; na maisha yao yanapokoma, watakuwa wamechelewa tayari kugeuza mkondo wa mawazo yao kuelekea upande ulio kinyume chake, watakuwa wamechelewa sana kugeuka kutoka katika uasi wa Sheria za Mungu na kwenda kwenye utii, kutoka katika chuki yao hadi kwenye upendo. [GC 543.1; PK Aya ya 36]

Katika kuyahifadhi maisha ya Kaini mwuuaji, Mungu aliupa ulimwengu kielelezo cha kile ambacho kingekuwa matokeo ya kumwacha mwenye dhambi aendelee kuishi maisha ya uovu bila kizuizi chochote. Kwa njia ya mvuto wa mafundisho na kielelezo cha Kaini, umati mkubwa wa uzao uliongozwa kuishi maisha ya dhambi, hadi "maovu ya mwanadamu yalipokuwa makubwa duniani"

na “kila kusudi analowaza moyoni mwake lilikuwa baya tu siku zote.” “Dunia ikaharibika mbele za Mungu, na dunia ilikuwa imejaa udhalimu.” Mwanzo 6:5, 11. [GC 543.2; PK Aya ya 37]

Kwa kuuhurumia ulimwengu, Mungu aliwafutilia mbali wakazi wake waovu katika wakati wa Nuhu. Kwa rehema Zake Aliwaangamiza wakazi wafisadi waliokuwa Sodoma. Kwa kupitia nguvu za udanganyifu za Shetani watenda maovu wanaungwa mkono kwa kupata huruma za watu na wanavutia watu (wanashabikiwa kama celebrity), na kwa njia hiyo daima wanawaongoza wengine kufanya uasi. Ilikuwa hivyo katika siku za Kaini na Nuhu, na ilikuwa hivyo katika siku za Ibrahimu na Nuhu na katika siku hizi zetu. Ni kutokana na rehema Yake kwa sayari zote ndiyo maana Mungu hatimaye atawaangamiza kabisa wale wanaoikataa neema Yake. [GC 543.3; PK Aya ya 38]

**Mshahara Wa Dhambi Ni Mauti**

"Mshahara wa dhambi ni mauti bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu Bwana wetu." Warumi 6:23. Wakati uzima ndiyo urithi wa wenye haki, mauti ndiyo mshahara na fungu la waovu. Musa aliwatangazia Israeli: “Nimekuwekea leo mbele yako uzima na mema, na mauti na mabaya.” Kumbukumbu la Torati 30:15. Mauti inayorejelewa katika maandiko haya si ile iliyotamkwa kwa Adamu kwa maana wanadamu wote wanapatwa na adhabu hiyo iliyotokana na kosa lake. Hii basi ni “mauti ya pili.” Ambayo ni kinyume na uzima wa milele (Ufunuo 20). [GC 544.1; PK Aya ya 39]

Kufuatia dhambi yake Adamu, mauti iliwatembelea jamii yote ya wanadamu kupitia urithi. Wote wanashuka kaburini. Na kupitia fursa ya mpango wa wokovu, wote ni lazima wafufuliwe kutoka makaburini mwao. “Kutakuwa na ufufuo wa wafu, wenye haki na wasio haki pia.” "Kwa maana kama katika Adamu wote wanakufa, vivyo hivyo katika Kristo wote watahuishwa." Matendo 24:15; 1 Wakorintho 15:22. Lakini tofauti dhahiri inawekwa baina ya matabaka haya mawili yaliyoletwa. “Wote waliomo makaburini wataisikia sauti Yake, nao watatoka; wale waliofanya mema kwa ufufuo wa uzima, na wale waliotenda mabaya kwa ufufuo wa hukumu.” Yohana 5:28, 29. Wale ambao ‘wamehesabiwa kuwa wanastahili’ ufufuo ule wa uzima ni “heri na watakatifu.” "Juu ya hao mauti ya pili haina nguvu." Ufunuo 20:6. Lakini wale ambao, kwa njia ya msamaha na imani, hawajajipatia msamaha (hawajaziungama dhambi zao), ni lazima wapokee adhabu ya dhambi zao—huo ndio “mshahara wa dhambi.” “Wanapata adhabu inayotofautiana kwa urefu wa muda na ukali wake, “sawasawa na matendo yao,” lakini hatimaye wakiishia katika mauti ya pili (yaani, watakufa wasiweze kufufuliwa tena kamwe). Kwa kuwa haiwezekani kabisa kwa Mungu, kulingana na matakwa ya haki na rehema Yake, kumwokoa mwenye dhambi katika dhambi zake, basi, Mungu hampi maisha ambayo uvunjaji

wake wa Sheria ya Mungu umempokonya, na ambayo yeye mwenyewe amethibitika kuwa hastahili kuwa nayo. Asema hivi mwandishi mmoja aliyevuviwa: “Maana bado kitambo kidogo asiye haki hatakuwapo, utapaangalia mahali pake wala hatakuwapo.” Na mwingine anatangaza hivi: “Nao watakuwa kana kwamba hawakuwako kamwe.” (Zaburi 37:16); “Bado kitambo kidogo asiye haki hatakuwapo; naam, utapafahamu mahali pake, wala hatatokea". Na mwingine anatangaza: "Watakuwa kana kwamba hawakuwapo kamwe." Zaburi 37:10; Obadia 16. Wakiwa wamefunikwa na aibu kwa matendo yao maovu, wanazama katika upotevu usio na matumaini wa milele. [GC 544.2; PK Aya ya 40]

**Kukomeshwa Kwa Dhambi**

Hivyo ndivyo dhambi itakavyokomeshwa kabisa, yaani utakuwa mwisho wake kabisa, pamoja na misiba, taabu na uharibifu uliotokana nayo. Asema hivi Mtunga Zaburi: “Umewakemea mataifa; na kumwangamiza mdhalimu; umelifuta jina lao milele na milele; adui wamekoma na kuachwa ukiwa milele.” Zaburi 9:5, 6. Yohana, katika Ufunuo, akingoja kwa hamu hali ya umilele siku za mbele, anasikia wimbo wa sifa wa ulimwengu wote bila kuharibiwa kwa noti moja kwa kutopatana na zingine. Kila kiumbe mbinguni na duniani alisikika akimtukuza Mungu. Ufunuo 5:13. Wakati huo hakutakuwako na roho hata moja iliyopotea itakayomkufutu Mungu, huku ikigaragara motoni kwa maumivu ya moto usiokoma; hakutakuwa na watu walio waovu ndani ya jehanamu ambao sauti zao nyembamba za mayowe makali, zitatolewa kwa kulia kwa maumivu makali, na kuchanganya vilio vyao na nyimbo za waliokombolewa. [GC 545.1; PK Aya ya 41]

Juu ya kosa la msingi la hali ya asili ya kutokufa, limejengwa fundisho la uongo lisemalo kwamba watu waliokufa wanao ufahamu wa kutambua wakati wa kifo - fundisho la dini, ambalo ni sawa na lile la mateso katika moto wa milele, ambalo liko kinyume na busara na hisia zetu za ubinadamu na mafundisho yaliyomo ndani ya Maandiko. Kwa mujibu wa imani hiyo inayopendwa na watu wengi (mashuhuri), wale waliokombolewa kule mbinguni wanajua kila kitu kinachotokea hapa duniani, hususani habari za maisha ya rafiki zao waliowaacha nyuma. Lakini furaha ingeweza kutoka wapi kwa hao wafu wanaoruka-ruka huko juu, na kuzijua taabu zinazowapata walio hai, na kushuhudia dhambi zinazotendwa na wapendwa wao wenyewe na kuwaona wakikabiliana na huzuni zote, na kukatishwa tamaa kwao kote, na uchungu wote wanaoupata katika maisha haya? Lakini ni kwa jinsi gani linaweza kuwa chanzo cha amani na faraja mbinguni na ingeweza kufurahiwa vipi na wale ambao wanaowazunguka marafiki zao angani juu ya vichwa vyao wakiruka au kuelea juu ya vichwa vya marafiki zao hapa duniani? Tena inachukiza mno jinsi gani, imani ile isemayo kwamba mara tu pumzi inapotoka mwilini, roho ya mtu yule aliyekuwa hataki kutubu inatupwa katika ndimi za moto wa jehanamu? Ni kina kirefu kiasi gani cha

maumivu makali wanacholazimika kutumbukizwa ndani yake wale waliookolewa, wanapowaona marafiki zao wakiingia makaburini mwao bila maandalizi, wakiingia katika mateso na dhambi ya milele! Wengi wamekuwa kama wendawazimu kwa kulitafakari wazo hili linalofadhaisha kwa huzuni. [GC 545.2; PK Aya ya 42]

Maandiko yanasema nini kuhusu mambo haya? Daudi anatangaza kuwa mwanadamu anapokufa hawezi kuwa na ufahamu wowote mautini “Pumzi yake hutoka, huurudia udongo wake; siku hiyo mawazo yake yapotea.” Zaburi 146:4. Sulemani naye anatoa ushuhuda huo huo: “Walio hai wanajua ya kwamba watakufa; lakini wafu hawajui neno lolote.” “Mapenzi yao, na chuki yao, na husuda yao, imepotea yote pamoja; wala hawana sehemu tena milele katika jambo lo lote linalofanyika chini ya jua." "Hakuna kazi, wala shauri, wala maarifa, wala hekima, kuzimu uendako wewe." Mhubiri 9:5, 6, 10. [GC 545.3; PK Aya ya 43]

Wakati maisha ya Hezekia yalirefushwa kutokana na jibu kwa sala yake, mfalme mwenye shukrani alimwimbia Mungu wimbo wa sifa na kwa rehema Zake nyingi kwake. Katika wimbo huu anaeleza sababu inayomfanya yeye afurahi hivyo: “Kaburi haliwezi kukusifu, mauti haiwezi kukuadhimisha: washukao shimoni hawawezi kuitumainia Kweli yako. Aliye hai, ndiye atakayekusifu, kama nifanyavyo leo.” Isaya 38:18, 19. Theolojia maarufu ipendwayo na wengi, inawasilisha kuwa wenye haki waliokufa wako mbinguni, wameingia katika pumziko na raha ile kuu na tena wanamsifu Mungu kwa ndimi zisizoweza kufa; lakini Hezekia hakuweza kuona mustakabali wenye utukufu kama huo mautini Kwa maneno yake anakubaliana na ushuhuda wa mwandishi wa Zaburi: “Katika kifo hakuna kumbukumbu yako; kuzimu ni nani atakayekushukuru?” "Wafu hawamsifu Bwana, wala wote washukao katika kimya." Zaburi 6:5; 115:17. [GC 546.1; PK Aya ya 44]

**Sauti Ya Mitume**

Petro katika Siku ya Pentekoste alitangaza kwamba mzee wa imani Daudi “alikufa akazikwa, na kaburi lake liko kwetu hata leo.” "Kwa maana Daudi hakupanda mbinguni." Matendo 2:29, 34. Ukweli kwamba Daudi angali bado kaburini mwake mpaka siku ya ufufuo unatuthibitishia sisi kwamba wenye haki hawaendi mbinguni wakati wanapokufa. Ni kwa njia ya ufufuo pekee, na kwa njia ya Ukweli kuwa Kristo amefufuka, ndipo Daudi anaweza hatimaye kuketi mkono wa kuume wa Mungu. [GC 546.3; PK Aya ya 45]

Naye Paulo alisema hivi: “Maana kama wafu hawafufuliwi, Kristo Naye hakufufuka. Na kama Kristo hakufufuka, imani yenu ni bure; mngali katika dhambi zenu. Basi hao nao waliolala katika Kristo wamepotea.” Wakorintho

15:16-18. Ikiwa kwa miaka elfu nne (Kuanzia kwa Adamu mpaka kwa Paulo) wale wenye haki walikuwa wanakwenda moja kwa moja mbinguni wakati wa kufa kwao, Paulo angewezaje kusema kwamba kama hakuna ufufuo, basi, “wao nao waliolala katika Kristo wamepotea?” Isingekuwako haja ya ufufuo. Mfia dini Tyndale, akirejelea hali ya wafu, alitangaza hivi: “Nakiri wazi, kwamba mimi siamini kwamba wao wako katika utukufu kamili ambao Kristo anao, au ule walio nao malaika wateule wa Mungu. Mambo hayo mawili si kanuni ya imani yangu; maana kama ingekuwa hivyo, mimi sioni faida ya kuhubiri habari za ufufuo wa mwili maana lingekuwa ni jambo lisilo na maana kabisa.” William Tyndale, Preface to New Testament (toleo la 1534). Imechapishwa tena na British Reformers—Tindal, Frith, Barnes, ukurasa wa 349. [GC 547.1; PK Aya ya 46]

**Kweli Tukufu**

Ni Ukweli usiokanushika kwamba tumaini la kupewa mbaraka wa uzima wa milele (kutokufa) wakati mtu anapokufa limesababisha watu wengi sana kupuuza fundisho la Biblia la ufufuo. Mwelekeo huo uliongelewa habari zake na Dk. Adam Clarke, ambaye alisema hivi: “Fundisho hilo la ufufuo linaonekana kuwa lilifikiriwa sana kuwa lina athari nzito miongoni mwa Wakristo wa awali kuliko linavyofikiriwa sasa! Jambo hilo limetokeaje? Mitume walikuwa wanalisisitiza sikuzote, na kuwahamasisha wafuasi wa Mungu kuwa na bidii, utii, na uchangamfu kupitia fundisho hilo. Lakini wale warithi wao katika siku zetu hizi ni nadra sana hulitaja jambo hilo! (ufufuo) Hivyo ndivyo mitume walivyolihubiri, na Wakristo wa awali waliamini hivyo; kadhalika sisi tukihubiri hivyo, wasikilizaji wetu wataamini hivyo. Hakuna fundisho katika Injili ambalo limepewa mkazo mkubwa kama hilo; na tena hakuna fundisho katika mfumo wa mahubiri ya siku zetu hizi ambalo limepuuzwa zaidi kama hilo!” - Commentary, maelezo juu ya 1 Wakorintho 15, fungu la 3. [GC 547.2; PK Aya ya 47]

Jambo hilo limeendelea kuwepo mpaka Ukweli wenye utukufu wa ufufuo karibu ufichwe na kusahauliwa kabisa na Ulimwengu wa Kikristo. Hivi ndivyo asemavyo mwandishi mmoja mashuhuri wa dini, akitoa maoni yake juu ya maneno ya Paulo katika 1Wathesalonike 4:13-18, anasema hivi: “Kwa makusudi yote ya kila siku yanayoweza kuwekwa katika vitendo, ambayo huleta faraja kwa watu, fundisho hili la dini wa hali iliyobarikiwa ya kutokufa ya wale wenye haki, kwetu linachukua mahali pa fundisho lenye mashaka linalosema juu ya ujio wa mara ya pili wa Bwana. Wakati wa kufa kwetu, Bwana anakuja kwa ajili yetu kutuchukua. Hicho ndicho tunachopaswa kungojea na kukesha kwa ajili yake. Watu waliokufa tayari wameingia kwenye utukufu. Wao hawangojei ile parapanda ya mwisho kwa ajili ya hukumu yao na mibaraka yao.” [GC 547.3; PK Aya ya 48]

## Maneno Ya Faraja Na Tumaini

Lakini karibu na wakati wa kuachana na wanafunzi Wake, Yesu hakuwaambia wanafunzi kwamba wangekwenda Kwake upesi. “Naenda kuwaandalia mahali,” Yesu alisema. “Na nikienda na kuwaandalia mahali, nitakuja tena niwakaribishe Kwangu.” Yohana 14:2, 3. Na Paulo anatuambia, zaidi, kwamba “Bwana Mwenyewe atashuka kutoka mbinguni pamoja na mwaliko, na sauti ya Malaika Mkuu, na parapanda ya Mungu; nao waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza; kisha sisi tulio hai, tuliosalia, tutanyakuliwa pamoja nao katika mawingu, ili tumlaki Bwana hewani; na hivyo tutakuwa pamoja na Bwana milele.” Naye anaongezea: “Farijianeni kwa Maneno haya.” 1Wathesalonike 4:16-18. Tofauti kubwa iliyoje kati ya maneno haya ya faraja na yale ya mchungaji wa nadharia ya ‘hatimaye Watu Wote Wataokolewa, yaani wokovu ni wa watu wote bila ya kujali hali zao za kiroho’ (Universalist) ambaye maneno yake yamenukuliwa katika kurasa zilizotangulia hapo awali! Huyu mchungaji wa pili (mwisho) aliwafariji marafiki waliokuwa wamefiwa kwa kuwapa uhakikisho kwamba, hata yule marehemu angekuwa na dhambi kiasi gani, uhai wake unapotoka baada ya kuvuta pumzi ya mwisho basi yeye angepokelewa kati ya malaika wakati ule ule anapokata roho. Paulo anawaelekeza ndugu zake kwenye wakati wa ujio wa pili wa Bwana siku za usoni, wakati vifungo vya kaburi vitakapovunjiliwa mbali, nao “waliokufa katika Kristo” watapofufuliwa na kupewa uzima wa milele. [GC 548.1; PK Aya ya 49]

Kabla ya mtu yeyote kuingia katika makao yale ya wenye heri, yaani waliobarikiwa, kesi zao lazima zipelelezwe, na tabia zao na matendo yao lazima yapitishwe mbele za Mungu ili kwa ajili ya uchunguzi. Ni lazima wote wahukumiwe sawasawa na mambo yale yaliyoandikwa katika vitabu na kulipwa kulingana na kazi zao zilivyo (Ufunuo 20:12). Hukumu hii haifanyiki wakati mtu anapokufa. Weka usikivu mkubwa kwenye Maneno haya ya Paulo: “Ameweka siku atakayowahukumu walimwengu kwa haki, kwa mtu yule aliyemweka; Naye amewapa watu wote uthabiti wa mambo hayo, kwa kumfufua katika wafu.” Matendo 17:31. Hapa mtume alisema waziwazi kwamba wakati uliowekwa ni muda mahsusi, kwa wakati ule ilikuwa ni muda wa baadaye, ulio mbele, uliokuwa umepangwa kwa ajili ya hukumu ya ulimwengu wote. [GC 548.2; PK Aya ya 50]

Yuda anarejelea wakati huo huo: “Malaika wasioilinda enzi yao wenyewe, bali wakayaacha makao yao yaliyowahusu, amewaweka katika vifungo vya milele chini ya giza kwa hukumu ya siku ile kuu.” na, tena, ananukuu Maneno ya Henoko: “Tazama, Bwana anakuja na maelfu kumi ya watakatifu Wake, ili kutekeleza hukumu juu ya wote.” Yuda 6, 14, 15. Yohana anatangaza kwamba “aliwaona wafu, wadogo kwa wakubwa, wamesimama mbele za Mungu; na vile

vitabu vikafunguliwa:...na hao wafu wakahukumiwa katika mambo hayo yaliyoandikwa katika vile vitabu.” Ufunuo 20:12. [GC 548.3; PK Aya ya 51]

Lakini ikiwa watu waliokufa tayari wanafurahia raha kule mbinguni au wanajiragaza wakihangaika katika ndimi za moto wa jehanamu, pana haja gani tena basi, ya hukumu ya wakati ujao? Mafundisho yaliyomo katika Neno la Mungu kuhusu vipengele hivi muhimu, maana sio siri au mafumbo, wala hayapingani au hayajipingi yenyewe; yanaweza kueleweka kwa watu wa akili za kawaida. Lakini ni mtu gani aliye msema kweli au mtoboa Ukweli, awezaye kuona ama busara au haki katika nadharia hiyo iliyopo sasa? Je, wale wenye haki, baada ya kesi zao kupelelezwa, wakati wa hukumu, watapokea Maneno haya ya pongezi, “Vema, mtumwa mwema na mwaminifu;... ingia katika furaha ya Bwana wako,” wakati wao tayari wamekuwa wakiishi mbele Zake Mungu, huenda kwa zama chungu tele? Je, hivi ni kweli kuwa waovu wanaitwa hukumuni kutoka katika mahali pao pa mateso makali huko jehanumu ili kupokea hukumu yao toka kwa Jaji wa ulimwengu wote, isemayo: “Ondokeni Kwangu, enyi mliolaaniwa, mwende katika moto wa milele”? Mathayo 25:21, 41 (wakati wao tayari walikuwa katika moto huo tangu walipokata roho zao). Lo! ni dhihaka kubwa hiyo! Ni ukosoaji wa aibu sana wa hekima na haki Yake Mungu! [GC 549.1; PK Aya ya 52]

Nadharia hiyo ya roho isiyokufa (hali ya kutokufa kwa roho) ilikuwa ni mojawapo ya yale mafundisho ya uongo ambayo Roma, iliyachukua kutoka kwa wapagani, na kuyaingiza katika dini ya Kikristo (Jumuiya ya Wakristo wote duniani). Martin Luther analifananisha Fundisho hili la kutisha kama “Hadithi za kutisha za mazimwi ambazo ni sehemu ya kilima cha kinyesi cha wanyama cha mbolea kilichomo katika nyaraka za mamlaka ya Kipapa, Roma”* angalia mwisho wa sura—E. Petavel, The Problem of Immortality, ukurasa wa 255. Akitoa ufafanuzi wa Maneno ya Sulemani katika Mhubiri, kwamba wafu hawajui lolote, Mwanamatengenezo huyu asema hivi: “Hapa ni mahali pengine panapothibitisha kwamba wafu hawana....hisia yoyote, Anaendelea kusema kuwa huko hakuna wajibu, hakuna sayansi, hakuna ufahamu, hakuna hekima. Sulemani anahitimisha maneno kwa kusema kwamba watu wote waliokufa wamelala, wala hawahisi au kusikia chochote kabisa. Kwa kuwa wafu wamelala pale, na hawawezi kuhesabu siku wala miaka, lakini watakapoamshwa wataonekana kama wamelala muda usiozidi hata dakika moja (watakapofufuliwa kufumba na kufumbua 1Wakorintho 15:54-56).” Martin Luther, Exposition of Solomon's Book, called Ecclesiastes/Mhubiri, ukurasa wa 152. [GC 549.2; PK Aya ya 53]

Hakuna mahali popote katika Maandiko Matakatifu panapopatikana usemi kwamba wenye haki wanakwenda kupata malipo yao au waovu wanakwenda mahali penye adhabu yao mara baada tu ya kifo. Wazee na manabii hawakutuachia uhakikisho kama huo. Kristo na mitume Wake hawakutoa dokezo lolote kuhusiana na hilo. Biblia inafundisha waziwazi kwamba wafu hawaendi

mbinguni mara tu wanapokufa. Wanaelezwa kwamba wamelala hadi wakati wa ufufuo. 1Wathesalonike 4:14; Ayubu 14:10-12. Siku ile ile kamba ya fedha inapolegea na bakuli la dhahabu kuvunjika (Mhubiri 12:6), mawazo ya mwanadamu hupotea. Washukao kuzimu wamenyamaza, hawajui tena lolote linalofanyika chini ya jua. Ayubu 14:21. Hilo ni pumziko lenye baraka kwa wenye haki waliochoka sana! Kwao wakati unaopita, uwe mrefu au mfupi, kwao ni kitambo tu kwao (kufumba na kufumbua tu). Wanalala usingizi; wataamshwa kwa tarumbeta ya Mungu ili wapokee miili yenye hali ya kutokufa yenye utukufu, kufumba na kufumbua, wakati wa parapanda ya mwisho; "Maana parapanda italia, na wafu watafufuliwa......wasiwe na uharibifu, nasi tutabadilika. Maana sharti huu uharibikao uvae kutokuharibika, nao huu wa kufa uvae kutokufa. Basi huu uharibikao utakapovaa kutokuharibika, na huu wa kufa utakapovaa kutokufa, hapo ndipo litakapokuwa lile Neno lililoandikwa, Mauti imemezwa kwa kushinda." 1Wakorintho 15:52-54. Wanapoamshwa kutoka katika usingizi wao mzito ndipo wanaanza kufikiri papo hapo, wakianzia na wazo lao lile waliloishia nalo wakati wa kufa kwao Hisia yao ya mwisho ilikuwa uchungu wa kifo; wazo lao la mwisho, lilikuwa lile la kuanguka chini ya nguvu za kaburi (kifo). Wanapofufuliwa na kuamka kutoka kaburini, wazo lao la kwanza lenye furaha litasikika kama mwangwi wa kilio cha kushangilia kwa vigelegele kwa ushindi wao: "Ku wapi, Ewe mauti, kushinda kwako? U wapi, Ewe mauti, uchungu wako?" fungu 55. [GC 549.3; PK Aya ya 54]

*"Monstrous fables that form part of the Roman dunghill of decretals."--Hekaya za kutisha za mazimwi, ni visa vya kusisimua vinavyosimuliwa hasa kwa watoto. Visa vyenyewe huwa havina ukweli kwa kuwa ni hadithi za kutunga kwa lengo la kufundisha ama kuburudisha. Kilima cha mavi hapa mwandishi anamaanisha mbolea inayowekwa kurutubisha uovu, uchafu, na mafundisho ya uongo yasiyoendana na Neno la Mungu katika nyaraka za kipapa zilizoandikwa kwa ajili ya kujibu hoja zilizoelekezwa kwake ama kwa kutoa ufafanuzi wa jambo fulani au kufanyika sehemu ya mapokeo ya Kanisa la Kiroma.

*(Siri ya kupata uzima wa milele-Mwandishi katika kitabu hiki anaposema Amri, Sheria, Shuhuda, Neno, Kanuni, Maagizo ya Mungu anamaanisha Amri zile Kumi za Kutoka 20, Soma zaidi Zaburi 119)

# SURA YA 34

# JE! WATU WETU WALIOKUFA (WAFU) WANAWEZA KUSEMA NASI?

### (Dini Ya Umizimu-Hila Kubwa Ya Shetani)

Ufupisho: Kuna uchawi ambao unachukuliwa kuwa ni mtakatifu na wengi. Shetani amewapata watu wengi kupitia njia hii. Sauti zinazungumza na sura zinaonekana na nguvu za uchawi zinaingia moyoni. Wengi huona ni mambo bandia/feki, na hivyo wanapojionea maajabu ya kushangaza yasiyo ya kawaida wanatekewa na kuingia dini hiyo ya umizimu. Inaanza kimchezo-mchezo, ila inakuwa vigumu kutoka humo kwenye imani ya 'mwanadamu ana asili ya kutokufa". Jifunze unavyoweza kujikinga mwenyewe na wale wa karibu nawe na kuepuka kuvutwa kwenye roho hizi za umizimu.

Huduma ya malaika watakatifu, kama ilivyoonyeshwa katika Maandiko, ni Ukweli unaofariji na wenye thamani mno, kwa kila mfuasi wa Kristo. Lakini mafundisho ya Biblia juu mada hii yamefunikwa na kupotoshwa kwa njia ya makosa ya theolojia iliyozoeleka na kupendwa sana na watu wengi. Fundisho lisemalo kwamba mwanadamu ana asili ya kutokufa, ambalo liliazimwa kwanza kutoka Katika falsafa za kipagani, na hatimaye wakati wa giza la uasi mkuu likaingizwa katika imani ya Kikristo, na kuchukua nafasi ya Ukweli unaofundishwa wazi kabisa katika Maandiko, kwamba "wafu hawajui neno lolote." Watu wengi sana wamekuja kuamini kwamba ni roho za watu waliokufa ambazo ni "roho watumikao, wakitumwa kuwahudumia wale watakaourithi wokovu." watu wamefikia kuamini hivyo japokuwa imani hiyo ni kinyume na ushuhuda wa Maandiko kuhusu uwepo wa malaika wa mbinguni, na mshikamano wao na historia ya mwanadamu, kabla ya kifo cha mwanadamu yeyote. [GC 551.1; PK Aya ya 1]

Fundisho lisemalo kwamba mwanadamu anaendelea kuwa na ufahamu wake katika kifo (anapokufa anaendelea kuishi), na hasa imani isemayo kuwa roho za wafu hurudi kuja kuwahudumia wale walio hai, limeandaa njia kwa ajili ya dini ya kisasa ya kuongea na watu waliokufa au mizimu (umizimu-modern spiritualism). Ikiwa watu waliokufa wanaruhusiwa kwenda mbele za uwepo wa Mungu na malaika watakatifu na kupewa uwezo wa kuwa na maarifa makubwa zaidi ya yale waliyokuwa nayo hapo awali, kwa nini basi, wasirudi duniani na kuwaangazia maarifa na kuwafundisha walio hai. Iwapo roho za wafu zinarandaranda au kurukaruka angani au juu ya vichwa vya rafiki zao waliomo duniani humu, kama wafundishavyo wanatheolojia hao mashuhuri wanaopendwa na watu wengi, kwa nini, basi, wasiruhusiwe kuongea nao, na kuwaonya dhidi ya

maovu, ama kuwafariji katika huzuni zao? Inawezekanaje wale wanaoamini kwamba nafsi za wafu zinaendelea kuishi, na kuwa na ufahamu, wakatae kile kinachowajia kama nuru ya Mungu iliyowasilishwa na roho zenye utukufu? (Wale wanaoamini kwamba mtu akifa anaendelea kuishi, wataamini kwamba mawasiliano kutoka kwa wafu ni nuru kutoka mbinguni.) Hapa kuna mfereji unaochukuliwa kama mfereji mtakatifu, ambao Shetani anafanya kazi nao kwa ajili ya kutimiza makusudi yake. Malaika wale walioanguka (mapepo) ambao wanatekeleza maagizo yake, hutokea kwetu kama wajumbe kutoka katika ulimwengu wa roho. Wakati wakidai kwamba wanawaleta watu walio hai katika mawasiliano na wafu, mfalme wa uovu anatumia nguvu zake za uchawi kupumbaza akili zao. [GC 551.2; PK Aya ya 2]

Shetani ana uwezo wa kuleta mbele ya watu mwonekano wa sura ya marafiki zao waliokufa. Mwonekano wa umbile hilo la bandia ni mkamilifu, na igizo pia; sura, mwonekano uliozoeleka, maneno, sauti, lafudhi, na maeneo, vinatokea kwa usahihi wa kushangaza. Wengi hufarijiwa na kuhakikishiwa kwamba wapendwa wao wanafurahia uzuri wa mbinguni na bila hata kushuku hatari, au kuchukua tahadhari, wanatega sikio kwa “roho zidanganyazo na mafundisho ya mashetani.” [GC 552.1; PK Aya ya 3]

Wanapokuwa wameongozwa kuamini kwamba wafu wanarudi kweli ili kuongea nao, Shetani anawezesha wale walioingia kaburini wakiwa hawakujiandaa kiroho waonekane kwao. Wakiwatokea kwa madai kuwa wana furaha mbinguni na hata kushika nyadhifa za juu huko na hivyo kosa linafundishwa na kuenezwa sana kwamba hakuna tofauti iliyopo kati ya wenye haki na waovu. Wageni hao wa kuigiza kutoka katika ulimwengu wa mapepo wakati mwingine hutamka maonyo na tahadhari ambazo huthibitika kuwa sahihi kabisa. Kisha wadanganyifu hawa wanavuta watu na kuaminiwa, nao wanawasilisha mafundisho ambayo yanahafifisha na kudharau Maandiko, ili watu wapoteze imani yao katika Biblia. Wakiwa wanaonekana kupendezwa na kuwaletea mambo mema marafiki zao duniani, wanapenyeza makosa na uongo wa hatari zaidi. Ukweli kwamba wanasema baadhi ya mambo yaliyo kweli na kuwa na uwezo wa kubashiri, wanaweza wakati fulani kutabiri matukio ya wakati ujao, na hiyo inazipa kauli zao kuwa na mwonekano wa kuaminiwa; na mafundisho yao ya uongo yanakubaliwa na watu kwa urahisi na kuaminiwa kwa ukamilifu, yaani bila maswali, kana kwamba ndizo Kweli takatifu sana za Biblia. Sheria ya Mungu inawekwa pembeni, Roho wa neema anadharauliwa na kudhihakiwa, damu ya agano inahesabiwa kuwa kitu kisicho kitakatifu. Pepo wanakana Uungu wa Kristo na hata kumweka Muumbaji kwenye daraja lao wenyewe. Kwa hiyo mwasi mkuu bado anaendelea na vita vyake dhidi ya Mungu, chini ya kichaka cha maficho kipya, vita iliyoanza mbinguni kwa karibu miaka elfu sita yeye ameendelea kuifanya duniani. [GC 552.2; PK Aya ya 4]

## Ishara Zinazozidi Uwezo Wa Kibinadamu

Wengi hujaribu kueleza vitendo hivi vya maonyesho ya pepo ni maigizo ya viini macho tu yanavyofanywa na wahusika. Ingawa ni kweli kwamba matokeo ya hila kama za mazingaombwe mara nyingi zimechukuliwa kama ufunuo wa kweli, huwa kunakuwa pia na maonyesho halisi ya nguvu kubwa zaidi kuliko za mwanadamu wa kawaida (supernatural). Milio ya ajabu ya kugongagonga ambayo imani ya kuwasiliana na wafu au mizimu ya kisasa ilianza nayo, haikuwa matokeo ya ujanja wa binadamu au viini macho, bali ilikuwa ni kazi ya moja kwa moja ya malaika waovu, ambao kwa njia hiyo walianzisha moja ya udanganyifu wenye ufanisi katika kuangamiza roho. Wengi watanaswa kwa kuamini kwamba imani ya kuongea na mizimu ni maigizo ya kibinadamu tu au udanganyifu fulani; watakapokutanishwa uso kwa uso na matukio ambayo watayaona kuwa ni ya ajabu na yanahusisha nguvu zisizo za kibinadamu, watadanganywa na wataongozwa kuyapokea kama nguvu kuu ya Mungu. [GC 553.1; PK Aya ya 5]

Watu hawa hupuuza ushahidi wa Maandiko kuhusiana na maajabu yanayotendwa na mashetani na mawakala wake. Ilikuwa ni kwa msaada wa Shetani kwamba wachawi wa Farao waliwezeshwaa kuigiza kazi ya Mungu. Paulo anathibithisha kwamba kabla wa ujio wa pili wa Kristo kutakuwa na matukio ya nguvu ya kishetani. Kuja kwa Bwana mara ya pili kutatanguliwa na "kutenda kwake Shetani kwa uwezo wote na ishara na ajabu za uongo na katika madanganyo yote ya udhalimu." 2 Wathesalonike 2:9, 10. Na mtume Yohana, akieleza juu ya nguvu ya utendaji miujiza itakayodhihirishwa katika siku za mwisho, anatangaza hivi: "Naye afanya ishara kubwa, hata kufanya moto kushuka kutoka mbinguni uje juu ya nchi mbele ya wanadamu, naye awakosesha wale wakaao juu ya nchi, kwa ishara zile alizopewa kuzifanya mbele ya huyo myama na kudanganya wale wakaao juu ya nchi kupitia miujiza anayoweza kuifanya" Ufunuo 13:13, 14. Hapa sio walaghai wanaotabiriwa kuwa watafanya ishara. Wanadamu wanadanganywa na miujiza ambayo mawakala wa Shetani wana uwezo wa kuitenda na si ambayo wanaigiza au kujifanya kuitenda. [GC 553.2; PK Aya ya 6]

## Mkuu Wa Giza

Mfalme wa giza ambaye kwa muda mrefu sana ameelekeza nguvu zake mahiri za akili kwenye kazi ya udanganyifu, kwa kupandikiza majaribu yake kwa watu wa matabaka na hali zote. Kwa watu wa kisasa, waungwana, wasomi, wenye nidhamu ya maadili, wenye uelewa mpana na utamaduni uliokuzwa vizuri, huwa anawasilisha imani ya kuongea na mizimu katika maboresho ya aina fulani kuchukuliana na akili za wanadamu na hivyo kufaulu kuwavuta wengi kwenye mtego wake. Hekima ambayo inayotolewa na kuwasiliana na mizimu ni ile

iliyoelezwa na mtume Yakobo, "Hekima ya namna hiyo haitoki juu mbinguni; bali ni ya kidunia, ya tabia ya kibinadamu, na ya kishetani." Yakobo 3:15. Hata hivyo, mdanganyifu mkuu huficha jambo hili wakati ambao kuficha kutamsaidia zaidi kufanikisha kusudi lake. Anavutia akili kwa kuwasilisha mwonekano mzuri unaovutia; anafurahisha nafsi kwa mandhari ya kusisimua; na anachota hisia za wanadamu kwa maonyesho yake fasaha ya upendo, huruma, wema na ukarimu. Yeye husisimua fikra kwa mambo ya hali ya juu sana, akiwaongoza wanadamu kuwa na kiburi katika hekima yao wenyewe huku mioyoni mwao wanamdharau Yule aliye wa Milele. Kiumbe huyo mwenye nguvu ambaye aliweza kumchukua Mkombozi wa ulimwengu hadi kwenye kilele cha mlima mrefu sana na kuleta mbele Yake falme zote za dunia na utukufu wa falme hizo, ataleta majaribu yake kwa wanadamu kwa namna ya kupotosha hisia za wale wote ambao hawana ulinzi wa nguvu ya Mungu. [GC 553.3; PK Aya ya 7]

Shetani huwahadaa wanadamu sasa kama alivyomhadaa Hawa katika Edeni kwa kumsifia, kwa kuwasha tamaa ya kupata ujuzi uliokatazwa, kwa kusisimua tamaa ya kujiinua. Ni kupalilia maovu haya kulikosababisha anguko lake na kupitia maovu haya analenga kuongoza maangamizi ya wanadamu. "Nanyi mtakuwa kama Mungu," anatangaza "mkijua mema na mabaya." Mwanzo 3:5. Imani ya kuongea na mizimu inafundisha "kwamba mwanadamu ni kiumbe wa maendeleo; kwamba ni lengo lake tangu kuzaliwa kwake aendelee, hatimaye afikie umilele, hadi Uungu." Na tena: "Kila mtu ataamua na sio mwingine." "Hukumu itakuwa ya haki na sahihi sababu ni hukumu ya nafsi yake mwenyewe...... Kiti cha enzi kimo ndani yako mwenyewe." Alisema mwalimu wa imani ya kuongea na mizimu au wafu, "ufahamu wa kiroho" ulipoamka ndani yake: "Wanadamu wenzangu, wote walikuwa nusu miungu ambao hawajawahi kuanguka." Na mwingine anatangaza: "Kila kiumbe chochote chenye haki na kikamilifu ni Kristo." [GC 554.1; PK Aya ya 8]

Hivyo, badala ya haki na ukamilifu wa Mungu asiye na kikomo, ambaye anapaswa kuabudiwa na kutukuzwa; badala ya haki kamilifu ya sheria yake, kiwango cha kweli cha upeo wa mafanikio ya mwanadamu, Shetani ameweka asili ya mwanadamu mwenyewe, mwanadamu mwenye dhambi na anayekosea kuwa ndiyo lengo pekee la kutukuzwa, kanuni pekee ya hukumu, au kiwango cha tabia. Haya ni maendeleo, ila siyo ya kwenda juu, bali yanayoelekea chini. [GC 554.2; PK Aya ya 9]

**Kwa Kutazama Tunabadilika**

Ni sheria ya kiakili na asili ya kiroho kwamba kwa kutazama tunabadilika. Polepole akili inabadilika na kujizoesha kupatana na mambo iliyoruhusiwa kuyatafakari. Inajiunga na kile ambacho imezoeshwa kukipenda, kukiheshimu na kukihusudu. Kamwe mwanadamu hawezi kuinuka juu zaidi kuliko kiwango chake

cha usafi wa moyo, wema au Ukweli. Ikiwa nafsi au kujipenda mwenyewe ndio kitu cha hali ya juu zaidi kwake, basi, hataweza kuinuka juu zaidi ya kitu ambacho kiko juu ya nafsi yake. Badala yake, ataendelea kuzama chini na chini. Ni neema ya Mungu pekee, ndiyo ina nguvu ya kumwinua mwanadamu. Mwanadamu akiachwa peke yake, njia yake lazima ielekee chini tu. [GC 555.1; PK Aya ya 10]

Kwa wanaojipenda nafsi zao, wanaojifurahisha, wanaojiendekeza, wapenda anasa, na walio na tamaa ya matendo ya mwili, imani ya kuwasiliana na mizimu hujitokeza wazi zaidi kwao, kuliko kwa watu wastaarabu, na wenye visomo zaidi; katika miundo yake mibaya zaidi, yaani isiyo na ustaarabu wanapata mambo yale yanayoafikiana na mielekeo yao. Shetani anasoma kila kiashiria cha udhaifu katika asili ya mwanadamu, anazitambua na kuziwekea alama dhambi ambazo kila mtu ana mwelekeo wa kuzitenda na kisha anahakikisha fursa zinakuwa za kutosha kuhamasisha kuuelekea uovu. Anawajaribu watu kwa kutokuwa na kiasi katika yale ambayo ni halali kwa yenyewe, akiwasababisha kutokuweza kutawala nafsi, kudhoofisha nguvu za kimwili, kiakili na kimaadili. Ameangamiza na anaendelea kuharibu maelfu kwa njia ya ulafi wa chakula na kuendekeza tamaa za mwili na kwa njia hiyo kufanyia ukatili asili/utu wa mwanadamu. Na ili kuhitimsha kazi yake, anatangaza, kupitia mapepo kwamba “Ujuzi wa kweli humuweka mwanadamu juu ya sheria yote; kwamba ‘chochote kile ni sahihi’; “kwamba “Mungu hakikatazi wala hakihukumu” na kwamba “dhambi zote zilizotendwa hazina hatia.” Watu wanapoongozwa kuamini kwamba hamu ndiyo sheria ya juu kabisa, kuwa uhuru ni kibali cha kupuuzia sheria kwamba mwanadamu anawajibika kwa nafsi yake mwenyewe tu, ni nani anayeweza kushangaa kwamba ufisadi na uhalifu vimesheheni kila upande? Watu wengi wanaafikiana na mafundisho ambayo yanayowaacha huru kutii misukumo ya mioyo yao miovu. Uwezo wa kujitawala unaachwa kuburuzwa na tamaa za mwili, nguvu za akili na roho zinawekwa chini ya mamlaka ya mielekeo ya kinyama na Shetani anawanasa kwenye mtego wake maelfu ya wanaodai kuwa wafuasi wa Kristo. [GC 555.2; PK Aya ya 11]

Lakini hakuna haja ya hata mtu mmoja anayelazimika kudanganywa na madai ya uongo ya imani ya kuongea na wafu. Mungu ameupatia ulimwengu nuru ya kutosha ili kuwawezesha kugundua mtego huo. Kama ilivyoonyeshwa tayari, nadharia ambayo inaunda msingi hasa ya imani ya kuongea na wafu iko vitani na kauli za wazi kabisa za Maandiko. Biblia inatangaza kwamba wafu hawajui lolote, kwamba mawazo yao yamepotea; hawana sehemu katika jambo lolote linalofanyika chini ya jua; hawajui lolote kuhusu furaha au huzuni za wale waliokuwa vipenzi vyao sana duniani. [GC 556.1; PK Aya ya 12]

**Mawasiliano Yaliyokatazwa**

Zaidi ya hayo, Mungu amekataza waziwazi mawasiliano yote ya bandia na watu waliokufa. Katika siku za Waebrania palikuwa na tabaka la watu waliodai, kama wafanyavyo leo waumini katika mawasiliano na wafu, kuwa huwa wanaongea na wafu. Lakini "roho za utambuzi," kama walivyoitwa wageni hao kutoka katika ulimwengu mwingine, wanatangazwa na Biblia kuwa "roho za mashetani." (Linganisha Hesabu 25:1-3; Zaburi 106:28; 1 Wakorintho 10:20; Ufunuo 16:14.) Kazi ya kushughulika na pepo ilitajwa kuwa ni chukizo kwa Bwana na ilipigwa marufuku kabisa na adhabu ya mkosaji wa dhambi hii ilikuwa kifo. Mambo ya Walawi 19:31; 20:27. Jina lenyewe la uchawi kwa sasa linachukiwa na kudhrauliwa. Dai la kwamba binadamu wanaweza kufanya mawasiliano na pepo wachafu huchukuliwa kuwa ni hekaya ya Zama za Giza. Lakini imani ya kuongea na wafu, ambayo ina idadi ya waumini mamia ya maelfu, ndiyo, hata mamilioni ambayo imeshaingia katika duru za kisayansi, na kuvamia makanisa na kupata kibali katika vyombo vya kutunga sheria na hata katika ikulu za wafalme, -- udanganyifu huu mkubwa ni uamsho tu wa wachawi katika joho jipya liliokatazwa na kupigwa marufuku tokea wakati wa zamani. [GC 556.2; PK Aya ya 13]

Kama kusingelikuwapo na ushahidi mwingine wa tabia halisi ya imani ya kuongea na wafu, ingetosha tu kwa mkristo kujua kwamba roho za mashetani au mapepo hayatofautishi kati ya haki na dhambi, kati ya wale walio waaminifu na safi miongoni mwa mitume wa Kristo na watumishi wa Shetani walio waovu sana. Kwa kusema wanadamu waovu wapo mbinguni na wameinuliwa huko juu, Shetani anauambia ulimwengu hivi: "Haidhuru mtu awe mwovu kiasi gani; haidhuru ikiwa unamwamini au humwamini Mungu na Biblia. Ishi upendavyo; mbinguni ni nyumbani kwako tu." Waalimu wa imani ya umizimu wanatangaza hivi: "Kila atendaye mabaya ni mwema machoni pa Bwana, Naye huwafurahia watu hao, au, Mungu Mwenye kuhukumu Yuko wapi?" Malaki 2:17. Neno la Mungu linasema hivi: "Ole wao wasemao kwamba uovu ni wema, na kwamba wema ni uovu; watiao giza badala ya nuru, na nuru badala ya giza!" Isaya 5:20. [GC 556.3; PK Aya ya 14]

Mitume, wanapoigizwa na roho hizi zidanganyazo,, wanafanywa kuonekana kama wanapinga yale waliyoaandika kwa maagizo ya Roho Mtakatifu alipokuwa duniani. Wanakanusha chimbuko la Biblia kuwa inatoka kwa Mwenyezi Mungu na kwa njia hiyo wanavunja msingi wa tumaini la Mkristo na kuzima nuru inayofunua njia ya kwenda mbinguni. Shetani anaufanya ulimwengu uamini kwamba Biblia ni riwaya tu, au angalau ni kitabu kinachofaa binadamu walio wachanga, kwamba sasa kichukuliwe kwa wepesi, au kutupiliwa mbali kwa kusema kimepitwa na wakati (zilipendwa). Na kwa kuchukua nafasi ya Neno la Mungu anaonesha utendaji wa imani ya kuongea na wafu. Hapa pana njia ya mawasiliano yaliyo chini ya utawala wake kamili; kwa njia hii anaweza kuufanya ulimwengu uamini

kile atakacho. Kitabu ambacho kitamhukumu yeye na wafuasi wake anakiweka chini ya kivuli, mahali anapotaka kikae; anamfanya Mwokozi wa ulimwengu kuwa mwanadamu wa kawaida. Na kama vile walinzi wa Kirumi waliokuwa wakililinda kaburi la Yesu walivyokuwa wakieneza taarifa za uongo ambazo makuhani na wazee waliwawekea vinywani mwao ili kuthibithisa kutofufuka Kwake Kristo, ndivyo waumini wa imani ya umizimu wanavyojaribu kufanya ionekane kwamba hakuna kitu cha ajabu au miujiza katika asili ya maisha ya Mwokozi wetu. Baada ya kutafuta namna ya kumweka Yesu mahali fulani huko nyuma ya pazia, wanaita usikivu wa watu uende kwenye miujiza yao wenyewe, wakitangaza kwamba hiyo miujiza yao ni mikubwa zaidi kuliko kazi za Kristo. [GC 557.1; PK Aya ya 15]

### Imani Ya Mizimu Yabadilisha Sura Yake

Ni kweli kuwa sasa imani ya kuongea na mizimu inabadilisha muundo wake na kuvificha baadhi ya vipengele vyake vibaya na vinavyochukiza zaidi, kwa kujivika joho la Kikristo. Lakini matamko yake kutoka mimbarani na kupitia vyombo vya habari yamekuwa mbele za umma kwa miaka mingi, na katika mambo haya tabia yake halisi inadhihirika. Mafundisho haya hayawezi kupingwa au kufichwa. [GC 557.2; PK Aya ya 16]

Hata katika muundo wake wa sasa, yamekuwa hayastahili kuvumilika zaidi kuliko ilivyokuwa siku za nyuma, hakika imani ya kuongea na wafu sasa ni ya hatari zaidi, kwa sababu haiko wazi na ina ujanja mwingi na hivyo inakuwa vigumu kuidadavua. Wakati pale mwanzoni mafundisho hayo ya imani ya kuongea na wafu yalimkana Kristo na Biblia, kwa sasa hivi yanadai kumkubali Kristo na Biblia. Lakini Biblia inafasiriwa kwa namna ambayo inaupendeza moyo usiofanywa upya, wakati Ukweli wake bora na muhimu ukifanywa kuwa usio na mashiko au maana yoyote. Upendo unachukuliwa kuwa sifa kuu ya Mungu, lakini unashushwa hadhi na kuwa hisia dhaifu, na hivyo kuweka tofauti ndogo kati ya wema na ubaya. Haki ya Mungu, makemeo Yake kwa dhambi, matakwa ya Sheria Yake takatifu, vyote visionekane machoni pa watu. Watu wanafundishwa kuiona Sheria ya Mungu ya Amri Kumi (Dekalojia) kama barua ambayo haijawafikia watu walioandikiwa, ina anuani isiyo sahihi, na kwamba imepitwa na wakati (dead letter). Hekaya za kupendeza na kuchagamsha zinaroga hisia na kuwaongoza watu kuikataa Biblia kama msingi wa imani yao. Hakika Kristo anakanwa na watu kama alivyokataliwa awali; lakini Shetani amepofusha macho ya watu kiasi kwamba udanganyifu haugunduliwi. [GC 558.1; PK Aya ya 17]

Kuna watu wachache ambao wanao utambuzi kamili kuhusiana na nguvu ya udanganyifu wa imani ya kuongea na wafu na hatari ya kuingia nchi ya mvuto wake. Wengi huichezea na kuinyangua-nyangua ili tu kuridhisha udadisi wao. Hawaamini uhalisia wa jambo hili la sivyo wangejazwa na hofu kwa wazo la

kujisalimisha chini ya utawala wa mapepo. Lakini wanatembea kwenye ardhi iliyokatazwa na mharibifu mkuu hutumia uwezo wake juu yao, dhidi ya nia yao. Ngoja washawishiwe kuzisalimisha akili zao chini ya uongozi wake naye mara moja atawanyakua na kuwafanya kuwa mateka wake. Haiwezekani, kwa nguvu zao wenyewe, kupona kutoka kwa uchawi wake ambao unavuta kama sumaku. Hakuna ufumbuzi wa kutoka kwenye hilo shimo isipokuwa tu nguvu ya Mungu inatolewa kwa kujibu ombi la dhati la imani inayoweza kuziokoa roho hizi zilizonaswa. [GC 558.2; PK Aya ya 18]

Wote wanaoendekeza tabia ya dhambi, au kupalilia kwa makusudi dhambi inayojulikana, wanakaribisha majaribu ya Shetani. Wanajitenga na Mwenyezi Mungu na ulinzi wa Malaika Zake; mwovu anapoleta udanganyifu wake, wanakuwa hawana ulinzi na hivyo huwa mawindo rahisi. Wale wanaojiweka hivyo katika nguvu yake, hawatambui ilivyo, mahali ambapo safari yao itaishia. Baada ya kufanikisha kuwapindua miguu juu na kichwa chini, mjaribu atawatumia kama mawakala wake ili kuwajaribu wengine na kuwaangamiza. [GC 558.3; PK Aya ya 19]

**"Na Waende Kwa Sheria Na Ushuhuda"**

Nabii Isaya asema hivi: "Na watakapokuambia, tafuta habari kwa watu wenye pepo na kwa wachawi, waliao kama ndege na kunong'ona; Je! Haiwapasi watu kutafuta habari kwa Mungu wao? Je! Waende kwa watu waliokufa kwa ajili ya watu walio hai? Na waende kwa sheria na ushuhuda; ikiwa hawasemi sawasawa na Neno hili, bila shaka kwa wao hapana asubuhi." Isaya 8:19, 20. Ikiwa wanadamu wangekuwa tayari kupokea Ukweli ambao umeelezwa wazi kabisa katika Maandiko kuhusu asili ya mwanadamu na hali ya wafu, wangeona katika madai na vioja vya imani ya kuongea na wafu utendaji kazi wa Shetani kwa nguvu na ishara na miujiza ya uongo wake. Lakini badala ya kusalimisha uhuru unaofikiana na moyo usioongoka wa matendo ya kimwili, na kuzikata dhambi wanazozipenda, umati mkubwa wa watu hufumba macho yao wasiione nuru na kusonga mbele katika hiyo nuru licha ya maonyo waliyopewa, wakati Shetani akisuka mitego yake kuwazunguka pande zote, nao wanakuwa mawindo yake rahisi. "Kwa sababu hawakukubali kuipenda ile Kweli, wapate kuokolewa," kwa hiyo "Mungu awaletea nguvu ya upotevu, wauamini uongo." 2 Wathesalonike 2:10, 11. [GC 559.1; PK Aya ya 20]

Watu wanaopinga mafundisho ya imani za kuwasiliana na roho za waliokufa, wanakuwa wakishambulia, sio wanadamu peke yao, bali Shetani na malaika zake. Wameingia katika vita dhidi ya mamlaka, nguvu na roho wachafu katika anga za juu. Shetani hatarudi nyuma hata sentimita moja, isipokuwa anaposukumwa nyuma kwa nguvu ya wajumbe wa mbinguni. Watu wa Mungu wanapaswa kuwa tayari kukabiliana naye kama alivyofanya Mwokozi wetu, kwa

Maneno haya: "Imeandikwa." Shetani anaweza kunukuu Maandiko sasa kama alivyofanya katika siku za Kristo, naye anapotosha mafundisho Yake ili kuunga mkono udanganyifu wake. Wale ambao watasimama katika wakati huu wa hatari lazima waelewe wao wenyewe ushuhuda wa Maandiko. [GC 559.2; PK Aya ya 21]

Wengi watakakutana na roho za mashetani waliojigeuza na kujifanya kuwa ni ndugu, jamaa, marafiki wapendwa waliokufa, wakifundisha mafundisho ya uongo wenye hatari zaidi. Wageni hawa watagusa hisia zetu za huruma nyororo na upendo na watatenda miujiza kuunga mkono madai yao bandia/feki (maigizo ya uongo). Ni lazima tuwe na utayari kusimama imara na kuwapinga kwa Ukweli wa Biblia kwamba wafu hawajui neno lolote na kwamba wale wanaoonekana au kutokea ni roho za mashetani. [GC 560.1; PK Aya ya 22]

Karibuni kabisa mbele yetu kuna "saa ya kujaribiwa iliyo tayari kuujilia ulimwengu wote, kuwajaribu wakaao juu ya nchi." Ufunuo 3:10. Wote wale ambao imani yao haijasimika mizizi kwa uthabiti juu ya Neno la Mungu watadanganywa na watashindwa na adui. Shetani "hufanya kazi kwa madanganyo yote ya udhalimu" ili kuutawala uzao wa wanadamu, na kisha madanganyo yake yataongezeka daima. Lakini anaweza kufikia lengo lake tu, pale watu wanapokubali kwa hiari kujisalimisha kwa majaribu yake. Wale wanaotafuta kwa dhati na bidii ujuzi wa Ukweli na wanajitahidi kutakasa roho zao kwa njia ya utii, wakifanya kila wawezalo ili kujiandaa kwa ajili ya pambano hilo, watajipatia ulinzi wa hakika kutoka kwa Mungu wa Ukweli. "Kwa kuwa umelishika Neno la subira Yangu, Mimi Nami nitakulinda" (fungu la 10), ni ahadi ya Mwokozi. Yeye angeweza kumtuma upesi kila malaika kutoka mbinguni kuwalinda watu Wake wote kuliko kuacha roho moja inayomtumaini Mungu ishindwe na Shetani. [GC 560.2; PK Aya ya 23]

Nabii Isaya anafunua udanganyifu wa kutisha utakaowajia waovu, utaowafanya wajihesabu kuwa salama dhidi ya hukumu za Mungu: "Tumefanya agano na mauti, tumepatana na kuzimu; pigo lifurikalo litakapopita, halitatufikia sisi; kwa maana tumefanya maneno ya uongo kuwa kimbilio letu, tumejificha chini ya maneno yasiyo kweli." Isaya 28:15. Katika tabaka lililoelezewa hapa wamejumuishwa wale ambao katika ukaidi wao wa kutokutubu wanajifariji kwa uhakikisho kwamba hapatakuwa na adhabu kwa mwenye dhambi; kwamba wanadamu wote, haidhuru jinsi walivyo mafisadi, wanatarajia kuinuliwa mbinguni, kuwa kama malaika wa Mungu. Lakini kwa kukazia zaidi bado, kuna wale wanaofanya agano na kifo na makubaliano na kuzimu, wale ambao wanaozikataa zile Kweli ambazo Mbingu imezitoa kama ulinzi kwa wenye haki katika siku ya taabu na kukubali hifadhi ya uongo inayotolewa na Shetani badala yake-- maigizo ya uongo wa imani ya kuongea na watu waliokufa. [GC 560.3; PK Aya ya 24]

Ajabu zaidi inayoshtua kuliko maelezo ni ule upofu wa watu wa kizazi hiki. Maelfu hulikataa Neno la Mungu kama lisilofaa kuaminiwa na kwa ujasiri wao uliojaa ushupavu huyakimbilia madanganyo hayo ya Shetani kwa ari. Wenye mashaka na wenye dhihaka wanaushutumu ubaguzi wenye chuki wa wale wa wale wanaotetea imani ya manabii na mitume na kisha wanachepuka kwenye upotofu wenyewe kwa kudhihaki matamshi mazito ya Maandiko kuhusu Kristo na mpango wa wokovu na adhabu inayokaribia kuwapata wanaoukataa Ukweli. Wanaonyesha rehema kubwa kwa wale walio na ufinyu wa akili, udhaifu na ushirikina kiasi cha kushindwa kukiri madai ya Mungu na kutii maagizo ya Sheria Yake. Wanakuwa na uhakika mkubwa kana kwamba, wamefanya agano na kifo na mapatano na kuzimu -- kana kwamba walikuwa wameweka ngome isiyoweza kupenyeka kati yao wenyewe na adhabu ya Mungu. Hakuna jambo linaloweza kuamsha hofu zao. Wamejisalimisha kikamilifu kwa mjaribu, wameshikamana naye kwa ukaribu sana na kujazwa kabisa na roho yake, kiasi kwamba hawana nguvu, wazo na mwelekeo wa kutoka katika mtego wake. [GC 561.1; PK Aya ya 25]

Shetani kwa muda mrefu amekuwa akijiandaa kwa ajili ya jitihada yake ya mwisho ya kuudanganya ulimwengu. Msingi wa kazi yake ulijengwa katika uhakikisho aliopewa Hawa katika Edeni: "Hakika hamtakufa." "Siku mtakayokula matunda yake, mtafumbuliwa macho, nanyi mtakuwa kama miungu, mkijua mema na mabaya." Mwanzo 3:4, 5. Kidogo kidogo amekuwa akitayarisha njia kwa ajili ya kazi yake ya udanganyifu mkubwa wenye ustadi katika kuanza na kuendelea na imani ya kuongea na wafu. Bado hajafikia kilele cha mafanikio yake; lakini itafikia katika sehemu ya mwisho ya wakati, nabii asema hivi: "Nikaona roho tatu za uchafu zilizofanana na vyura, zikitoka katika vinywa vya yule joka, na katika kinywa cha yule mnyama, na katika kinywa cha yule nabii wa uongo. Hizo ndizo roho za mashetani, zifanyazo ishara, zitokazo na kuwaendea wafalme wa ulimwengu wote kuwakusanya kwa vita ya siku ile kuu ya Mungu mwenyezi." Ufunuo 16:13, 14. Isipokuwa wale tu wanaotunzwa na nguvu za Mungu, kwa njia ya imani katika Neno Lake, ulimwengu wote utatatekwa katika katika wimbi la udanganyifu huu na kuwa wahanga wake. Watu wanabembelezwa kwa haraka na usalama feki/bandia (wa uongo) ambao una hatari ya kufisha, ili hatimaye waamshwe tu na kumwagwa na mvua ya ghadhabu ya Mungu. [GC 561.2; PK Aya ya 26]

Bwana MUNGU asema hivi: "Nami nitafanya hukumu kuwa ndiyo kanuni, na haki kuwa timazi; na mvua ya mawe itachukulia mbali hilo kimbilio la maneno ya uongo, na maji yatapagharikisha mahali pa kujisitiri. Na agano lenu mliloagana na mauti litabatilika, tena mapatano yenu mliyopatana na kuzimu hayatasimama; pigo lifurikalo litakapopita, ndipo ninyi mtakapokanyagwa nalo." Isaya 28:17, 18. [GC au PK 562.1]

*(Savage/barbarians-Washenzi, wakatili, wapagani, wenye unyama katika historia ya enzi za giza, mfano utumwa, au kuua watu kwa Rumi kwenye viwanja kwa kuraruliwa na wanyama, au kutundika watu kwenye msalaba)

# SURA YA 35

# UHURU WA DHAMIRI WATISHIWA

**(Malengo Ya Upapa)**

Ufupisho: Kuna nguvu zinafanya kazi kwa siri kubatilisha imani yetu. Na ni wachache wanalijua jambo hilo. Uhuru wetu wa dhamiri ya kuabudu tutakavyo, wengi huichukulia kirahisi ila vita vilipiganwa kwa karne nyingi ili upatikane, na uhuru huu unaweza kutokomea kirahisi. Hatari iko karibu na Neno la Mungu linalotuambia tusibweteke na kustarehe kana kwamba tumefika, bado tuko katika nchi ya adui, mapambano hayajaisha bado.

Ukatoliki hivi sasa unaangaliwa na Waprotestanti kwa kukubalika, yaani unapendwa zaidi kuliko katika miaka ya nyuma. Katika nchi zile ambazo Ukatoliki hauendelei kukua au hauna ushawishi mkubwa, na viongozi wa kipapa wanachukua hatua za kufanya kazi ya upatanisho ili kuwa na mvuto, kuna hali inayoongezeka ya kutoyajali mafundisho yanayoyatenganisha makanisa yaliyofanya Matengenezo mbali na utawala wa hierakia wa kipapa; maoni hayo yanazidi kupata nguvu nayo yasema kwamba, hata hivyo, hatutofautiani sana katika mambo ya msingi kama ambavyo imekuwa ikidhaniwa, na ya kwamba kule kupunguza kidogo msimamo na kukubaliana mambo fulani kwa upande wetu kutatuwezesha sisi kuwa na maelewano mazuri zaidi na Roma. Palikuwa na wakati ambapo Waprotestanti walithamini sana uhuru wa dhamiri* ambao ulikuwa umenunuliwa kwa gharama kubwa mno. Waliwafundisha watoto wao kuuchukia sana upapa na kushikilia msimamo wao kwamba kutafuta mapatano na Rumi kungekuwa ni kukosa utii kwa Mungu (uasi). Lakini ni tofauti kubwa jinsi gani ya mawazo yanayoletwa sasa! *(uhuru wa kila mtu kumwabudu Mungu wake kama apendavyo mwenyewe) [GC 563.1; PK Aya ya 1]

Watetezi wa upapa wanatangaza kwamba kanisa hilo limekosolewa na kuzungumzwa kwa ubaya jambo ambalo si kweli, na ulimwengu wa Kiprotestanti uko tayari kukubali kauli hii. Wengi wanasisitiza kwamba si haki kulihukumu kanisa la leo (la Rumi) kwa machukizo na upumbavu uliolitambulisha kipindi cha

utawala wake katika karne za kutojua/ujinga na giza. Wanautolea udhuru ukatili wake wa kuogofya mno na kusema kwamba ulisababishwa na ushenzi na unyama (barbarism) uliokuwako nyakati zile, kisha wanatoa madai yao kwamba kutokana na mvuto wa ustaarabu wa, kanisa hilo limebadili mawazo na nia yake. [GC 563.2; PK Aya ya 2]

Je, watu hawa wamesahau madai ya kutokosea kamwe, yaliyotolewa kwa muda wa miaka mia nane na mamlaka hii yenye kiburi? Mbali kabisa na kuachwa, dai hili lilithibitishwa katika karne ya kumi na tisa kwa mkazo mkubwa zaidi kuliko kabla ya hapo awali. Kama Rumi inavyodai kwamba "kanisa halikuwahi kukosea kamwe; wala kwa mujibu wa Maandiko, halitakosea kamwe" (John L. von Mosheim, Institutes of Ecclesiastical History, kitabu cha 3, karne ya 2, sehemu ya 2, sura ya 2, sehemu ya 9, maelezo ya 17), kanisa hili linawezaje kuacha kanuni zilizoiongoza zama zote zilizopita? [GC 564.1; PK Aya ya 3]

Kanisa hilo la kipapa kamwe halitaacha dai lake lisemalo kwamba haliwezi kukosea kamwe. Yote yale ambayo limewahi kufanya katika mateso yake kwa wale wanaoyakataa mafundisho yake ya imani yasiyobadilika, linachukuliwa kuwa sahihi na haki kabisa; na je, halitaweza kuyarudia tena matendo yake yale yale endapo fursa itajitokeza? Hebu ngoja vizuizi vyote vinavyowekwa sasa na serikali za dunia (zisizo za kidini) viondolewe, na kisha Rumi irejeshwe tena katika mamlaka yake ya zamani ya kutawala dunia nzima, ndipo udikteta wake na mateso yake vingefufuka kwa haraka sana. [GC 564.2; PK Aya ya 4]

Mwandishi mmoja mashuhuri anasema hivi kuhusu nia ya utawala huo wa hierakia wa kipapa kuhusu uhuru wa dhamiri, na hatari kubwa zinazoitishia Marekani (U.S.A) kutokana na mafanikio ya sera zake (Rumi): [GC 564.3; PK Aya ya 5]

"Kuna wengi ambao wana mwelekeo wa kutokuwa na hofu yoyote juu ya Ukatoliki wa Rumi katika nchi hii ya Marekani kuwa huo ni ushabiki tu wa dini au chuki zisizo na mashiko au ni utoto mwingi tu (upuuzi tu). Watu kama hao hawaoni kitu chochote katika tabia na mtazamo wa Urumi ambao una uadui mkubwa kwa taasisi zetu huru, au hawaoni kitu chochote kinachoashiria hatari kubwa mno katika kuongezeka kwa nguvu zake. Basi, hebu kwanza tulinganishe baadhi ya kanuni za msingi za serikali yetu na zile za Kanisa Katoliki. [GC 564.4; PK Aya ya 6]

"Katiba ya Nchi ya Marekani inatoa uhakika wa kuweko kwa uhuru wa dhamiri. Hakuna jambo jingine la thamani sana, linalopendwa na la msingi zaidi kuliko hili. Papa Piusi wa Tisa, katika Barua yake ya Utume ya Ensiklika ya Desemba 8, 1854, aliyoituma kwa Maaskofu wote wa kanisa la Rumi, alisema hivi: 'Mafundisho au kauli hizo za dini za kipuuzi na za uongo au maneno hayo ya wendawazimu ya kutetea uhuru wa dhamiri ni moja ya makosa mabaya sana

linaloleta madhara - ni mdudu mharibifu aletaye maradhi, miongoni mwa wote, anayepaswa kuogopwa sana kuliko wengine katika taifa.' Papa huyo huyo, katika Barua yake ya Utume ya Ensiklika kwa Maaskofu mnano Desemba 8, 1864, aliwakemea na kuwalaani 'wale wanaodai uhuru wa dhamiri na uhuru wa ibada ya kidini,' pia 'wale wote waliounga mkono kuwa kanisa halipaswi kutumia nguvu.' [GC 564.5; PK Aya ya 7]

"Mwelekeo wa amani wa Roma katika nchi ya Marekani haumaanishi kuwa Urumi imepata badiliko la moyo wake. Kanisa limekuwa na uvumulivu wa kuwapo kwa dini nyingine za Kikristo kwa kutokuwa na uwezo wa kufanya lolote. Asema hivi Askofu O'Conner: 'Uhuru wa dini unavumiliwa tu mpaka pale ambapo kinyume chake kinatekelezwa bila kuhatirisha Ulimwengu wa Kikatoliki.'... Askofu Mkuu wa St. Louis aliwahi kusema hivi wakati mmoja: 'Uzushi* na kukosa imani ni makosa ya jinai, yaani uhalifu; na katika nchi za Kikristo, kwa mfano, kama katika nchi ya Italia na Hispania, ambako watu wote ni Wakatoliki, na ambako dini ya Kikatoliki ni sehemu muhimu ya sheria za nchi, makosa hayo ya uzushi na kutoamini yanaadhibiwa kama uhalifu mwingine wowote.'..… *(mafundisho ya dini toka katika Biblia yasiyokubaliana na yale ya Rumi mara nyingi huitwa uzushi) [GC 565.1; PK Aya ya 8]

Kila Kadinali, askofu mkuu, na askofu katika Kanisa la Katoliki hula kiapo cha utii kwa papa, ambacho ndani yake hupatikana maneno haya yafuatayo: 'Wazushi, na wale waletao mafarakano, na waasi dhidi ya bwana wetu aliyetajwa (papa), au wafuasi wake waliokwisha kutajwa, mimi nitawatesa na kuwapinga kabisa kwa nguvu zangu zote…"— Yosia Strong, Our Country, sura ya 5, kifungu. 2-4 (Tazama Nyongeza kwa Marejeleo Yaliyosahihishwa.) [GC 565.2; PK Aya ya 9]

Ni kweli kwamba kuna Wakristo wa kweli katika jumuia ya Kanisa Katoliki la Rumi. Maelfu katika kanisa hilo wanamtumikia Mungu kulingana na nuru yote waliyo nayo. Hawaruhusiwi kulisoma Neno Lake Mungu, na kwa sababu hiyo hawautambui Ukweli. [Ilichapishwa mnamo 1888 na 1911. Tazama Kiambatisho.) Hawa hawajapata kamwe kuiona tofauti iliyopo kati ya huduma hai inayotolewa kutoka moyoni kwa dhati na ile ya kurudia- rudia tena taratibu za ibada zilizo tupu pamoja na maadhimisho yake. Mungu anawaangalia kwa sikitiko lililojaa huruma nyororo (upendo), watu hawawaliolelimishwa katika elimu hiyo kama walivyo, katika imani idanganyayo na isiyoridhisha. Atawezesha miale ya nuru kupenya giza nene linalowazunguka. Atawafunulia Ukweli kama unavyopatikana ndani ya Yesu, na bado wengi wao watachukua msimamo wao, na kusimama upande wa watu wa Mungu [Ufu. 18:4; 15:2, 3]. [GC 565.3; PK Aya ya 10]

Lakini hivi sasa Urumi kama mfumo wa dini, haupatani sana na Injili Yake Kristo, sawasawa tu na vile ulivyokuwa katika kipindi cha zamani katika historia yake. Makanisa ya Kiprotestanti yamo katika giza kuu, isipokuwa kama

wangeweza kutambua dalili za nyakati. Kanisa la Rumi linaona kwa mbali sana katika mipango yake na mbinu zake za kiutendaji. Linatumia kila hila kueneza mvuto wake na kuongeza nguvu yake, katika kujiandaa kwa mgogoro mkali sana wa mwisho uliodhamiriwa kuirudia hali ya kuitawala tena dunia, na kuanzisha tena mateso yake (Ufu. 17:6,17, 18), na kutengua/kubomoa yote ambayo uprotestanti umekwisha kufanya. Ukatoliki unaendelea kustawi, kujipatia nguvu na kukubalika kwa kupata upendeleo kila upande. Angalia ongezeko la idadi ya makanisa yake makubwa inavyozidi kuongezeka pamoja na yake makanisa madogo (chapels) katika nchi za Kiprotestanti. Angalia jinsi vyuo vyake vinavyopendwa sana na watu pamoja na umaarufu wa Seminari zake kwa Waprotestanti katika nchi hii ya Marekani. Angalia ukuaji wa taratibu zake za ibada katika nchi ya Uingereza, na mara kwa mara watu hutoroka kutoka katika Kanisa la Uingereza, yaani Anglikana na kujiunga katika safu za Wakatoliki. Mambo hayo yangeamsha wasiwasi ndani ya wote wanaothamini sana kanuni za usafi wa injili. [GC 565.4; PK Aya ya 11]

**Kufanya Maridhiano Na Kuachilia Mambo Fulani**

Waprotestanti wameonyesha urafiki na wamechezacheza na upapa na kuufadhili; wamefanya maridhiano na makubaliano kulegeza misimamo yao ya mafundisho fulani kiasi ambacho wafuasi wa upapa wenyewe wanashangaa wanapooona yameachwa, na tena wanashindwa kuelewa. Watu wanafumba macho yao ili wasipate kuiona tabia halisi ya Urumi na hatari ambazo zinapaswa kuhofiwa utakaposhika hatamu zake za kuitawala dunia hii. Watu wanahitaji kuamshwa usingizini ili wapinge madai ya adui huyu wa hatari ambaye anasonga mbele zaidi dhidi ya uhuru wa kiraia na uhuru wa kidini. [GC 566.1; PK Aya ya 12]

Waprotestanti wengi wanadhani kwamba dini ya Kikatoliki haiwavutii sana watu, na ya kwamba ibada yake imepoa, yaani, ni maadhimisho yasiyo na maana yanayorudiwa kwa mizunguko ya mapokeo ya maneno fulani, tena na tena. Hapa wanakosea. Wakati Urumi imejengwa juu ya msingi wa udanganyifu, huo sio uigizaji usiokuwa wa adabu au uungwana au tabia ya rafu au matusi, wala siyo ibada ya ovyo ovyo tu isiyo na weledi. Huduma ya kidini inayoendeshwa na Kanisa la Rumi ni sherehe inayovutia mno. Sherehe zake zinapambwa vizuri sana na taratibu zake za ibada zenye kicho huyasisimua mawazo ya watu na kuinyamazisha sauti ya busara akilini inayouliza maswali pamoja na sauti ya dhamiri. Jicho hufurahishwa sana. Makanisa yake makubwa ya kifahari, maandamano yake makubwa yanayovutia sana, altare (mimbari) zake za dhahabu, madhabahu zake zilizopambwa kwa vito vya thamani, michoro ya rangi zilizochaguliwa kwa uangalifu mkubwa sana, na sanamu zake maridadi zilizochongwa na kunakshiwa vizuri huwavutia wale wanaopenda uzuri/urembo.

Sikio pia hutekewa. Muziki pale hauna mshindani. Sauti tamu ya kinanda cha ogani chenye sauti nzito na sauti kutoka kwenye matamvua yake, zikichanganyika na sauti zinazoimba za watu wengi huvuma katika mapaa marefu ya kanisa na kati ya nguzo zilizopangwa kwa marefu katika makanisa yake makubwa sana (kathedro) ya jimbo yenye askofu, mambo hayo hayawezi kukosa kuugusa moyo na kuishangaza akili iwe na kicho na heshima kuu. [GC 566.2; PK Aya ya 13]

Utukufu huu, unaoonekana kwa nje, fahari yake, na usherekeaji wake wa nje, mambo hayo ambayo yanadhihaki tu shauku ya moyo ulioumizwa na dhambi na ulio na matamanio ya kutulizwa, ni ushahidi wa ufisadi uliomo ndani yake (kanisa hilo). Dini ya Kristo haihitaji vivutio vyote hivyo ili ipate kukubalika na watu au kuonekana inafaa. Katika nuru inayoangaza kutoka msalabani, Ukristo wa kweli unaonekana kuwa ni safi na wa kupendeza mno kiasi kwamba hakuna mapambo yoyote ya nje yanayowezakuiongeza thamani yake halisi. Ni uzuri wa utakatifu, yaani, ile roho ya upole, ukimya na utulivu, ndiyo ambayo ina thamani mbele za Mungu. [GC 566.3; PK Aya ya 14]

Mwonekano wa nje uliotukuka kwa uzuri au mng'ao si lazima uwe kigezo cha fikra safi, iliyoinuliwa, na yenye ubora. Uelewa wa hali ya juu wa sanaa, uchaguzi na uboreshaji wa ladha nzuri, mara nyingi mambo hayo huwa ndani ya mioyo inayoipenda dunia hii na tamaa za mwili. Mara kwa mara mambo hayo hutumiwa na Shetani kuwaongoza watu wasahau njaa na kiu za roho zao, na kisha washindwe kuona mambo ya wakati ujao, yaani, uzima wa milele, na kumpa kisogo Msaidizi wao wa milele [Mungu], na kuishi kwa ajili ya ulimwengu huu peke yake. [GC 567.1; PK Aya ya 15]

Dini iliyojengwa juu ya mambo yale yanayoonekana kwa nje inavutia sana ule moyo ambao haujaumbwa upya. Fahari na sherehe za ibada ya Kikatoliki zina uwezo wa kuteka akili na kuwaduwaza watu kama zifanyavyo nguvu ya uchawi, nao wengi wanadanganyika kwazo; nao wanakuja kulitazama Kanisa la Rumi kama lango lenyewe halisi la kuingilia mbinguni. Hakuna wasioweza kuathiriwa na mvuto wake, isipokuwa wale tu walioisimika miguu yao kwa uthabiti juu ya msingi wa Ukweli, na ambao mioyo yao imeumbwa upya kwa Roho wa Mungu, watu walio na kinga dhidi ya mvuto wake. Maelfu ambao hawana maarifa ya kumjua Kristo ambayo wanaweza kuyaweka katika vitendo, wataongozwa kukubali maigizo ya utauwa tu pasipokuwa na nguvu zake. Dini kama hiyo ndiyo wanayoipenda watu wengi. [GC 567.2; PK Aya ya 16]

**Kupewa Leseni Ya Kutenda Maovu**

Dai la kanisa la Rumi kwamba lina haki ya kusamehe dhambi humwongoza Mrumi kujisikia kwamba yuko huru kutenda dhambi; tena ibada ile ya kitubio au

maungamo, ambayo bila hiyo msamaha wa dhambi hautolewi, ina mwelekeo pia wa kumpa mtu leseni/uhuru ya kutenda maovu. Yeyote apigaye magoti mbele ya mwanadamu aliyeanguka dhambini, na kuyafunua mawazo yake ya siri pamoja na fikra zilizomo moyoni mwake kwa njia ya maungamo, anajidhalilisha utu wake na kuishusha hadhi ya kila hisia iliyo bora ya nafsi yake. Katika kuzifunua dhambi za maisha yake kwa padri,--ambaye ni mwanadamu mkosaji, mwenye dhambi, na anayekufa, na ambaye mara nyingi anakuwa amenajisiwa kwa mvinyo, uasherati na tamaa zingine za mwili, - huwa anakishusha chini kiwango cha tabia yake, na hatimaye anachafuliwa naye. Mawazo yake juu ya Mungu huwa duni sana, naye humfananisha Mungu na binadamu walioanguka dhambini, kwa maana yule padre anasimama pale kama mwakilishi wa Mungu. Maungamo hayo yanayoshusha hadhi ya mwanadamu huyo anayeungama kwa mwanadamu mwenzake, ndiyo chemchemi ya siri ulikotoka mkondo wa maovu mengi yanayoinajisi dunia hii na kuitayarisha kwa maangamizi yake ya mwisho (makufuru). Hata hivyo, kwake yeye apendaye kuendekeza tamaa zake mbaya za mwili, ni jambo linalopendeza sana kwake kuungama dhambi zake kwa mwanadamu mwenzake kuliko kuufunua moyo wake mbele za Mungu. Ni jambo  linalopendeza kwa silika ya kibinadamu kufanya kitubio kuliko kuachana kabisa na dhambi; ni rahisi sana kuutesa mwili kwa kuvaa magunia na kujimwagia upupu na kujifunga kwa minyororo mizito inayochubua ngozi kuliko kuzisulibisha tamaa mbaya za mwili. Moyo usioongoka uko tayari kubeba kongwa zito kuliko kuinama chini ya nira ya Kristo. [GC 567.3; PK Aya ya 17]

**Mfanano Wa Kushangaza Sana**

Kuna mfanano wa kushangaza sana kati ya Kanisa la Rumi na Kanisa la Wayahudi la wakati wa kuja mara ya kwanza Kristo. Wayahudi kwa siri walikuwa wakiikanyaga chini ya miguu yao kila kanuni ya Sheria ya Mungu, kwa nje walikuwa wakali sana katika kutunza miongozo yake wakizishindilia na mzigo mzito wa amri zao ngumu  na mapokeo yao wenyewe, mambo ambayo yalifanya utii kuwa mchungu na mzigo mzito ulemeao kwa watu. Kama Wayahudi walivyodai kuwa walikuwa wanaiheshimu sana Sheria, ndivyo Warumi wanavyodai kuuheshimu sana msalaba. Wanaitukuza alama ya mateso Yake Kristo (msalaba), wakati wakimkana Yeye katika maisha yao, Yule ambaye msalaba  unamwakilisha. [GC 568.1; PK Aya ya 18]

Waumini wa upapa huweka misalaba kwenye makanisa yao, kwenye altare (madhabahu) zao, na kwenye mavazi yao. Kila mahali panaonekana alama hiyo ya msalaba. Kila mahali msalaba huo unaheshimiwa na kutukuzwa kwa mwonekano wa nje tu. Lakini mafundisho ya Kristo yanazikwa chini ya takataka nyingi za mapokeo yao yasiyo na maana, na tafsiri zao za uongo, na amri zao kali zinazowashurutisha watu kutii (matakwa magumu). Maneno ya Mwokozi kuhusu Wayahudi waliong'ang'ania misimamo mikali ya imani, ambayo  ilipitiliza na

kukosa busara yanawahusu kwa maana yenye uzito mwingi zaidi viongozi wa Kanisa Katoliki la Rumi: “Wao hufunga mizigo mizito na kuwatwika watu mabegani mwao; wasitake wenyewe kuigusa kwa kidole chao.” Mathayo 23:4. Roho hizi adilifu na zenye bidii ya kufanya vizuri yale yote yawapasayo zinawekwa katika hali ya hofu daima, zikiogopa ghadhabu toka kwa Mungu aliyekosewa kwa matendo, wakati wengi miongoni mwa viongozi wakuu wa kanisa wakiishi katika anasa, na kuridhisha uasherati na tamaa zingine za mwili. [GC 568.2; PK Aya ya 19]

Ibada ya sanamu pamoja na masalio ya vitu na mifupa ya watakatifu waliokufa zamani (ushirikina), maombi kwa watakatifu waliokufa zamani, na kumtukuza papa ni mbinu anazotumia Shetani kuivuta mioyo ya watu mbali na Mungu na mbali na Mwanawe. Ili kutekeleza maangamizi yao, anajitahidi sana kuyageuza mawazo yao mbali na Yeye ambaye kwa njia Yake peke yake wanaweza kupata wokovu. Atawaelekeza mawazo yao kwenye kitu kingine chochote kinachoweza kuwekwa badala ya Yeye aliyesema: “Kwangu, ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo, Nami nitawapumzisha.” Mathayo 11:28. [GC 568.3; PK Aya ya 20]

Ni juhudi ya kudumu ya Shetani kuipotosha tabia ya Mungu kwa kuiwasilisha vibaya, asili ya dhambi, na mambo halisi yaliyo hatarini katika hilo pambano kuu. Uongo wake hulegeza uwajibikaji wa watu kwa Sheria ya Mungu (Amri Kumi) na kuwapa idhini ya kutenda dhambi. Wakati huo huo anawafanya kuthamini uelewa potofu juu ya Mungu ili wamwangalie kwa hofu na chuki badala ya kumtazama kwa upendo. Ukatili ambao ni sehemu ya tabia yake mwenyewe anampakazia Muumbaji; ukatili umewekwa katika mifumo mbalimbali ya dini na huonyeshwa katika taratibu zake tofauti za ibada. Hivyo akili za wanadamu hupofushwa, na Shetani anawachukua na kuwafanya mawakala wake ili wapate kumpingaMungu. Kwa uelewa wao potofu kuhusu tabia ya Mungu, mataifa ya kipagani na yasiyo na ustarabu (kishenzi-Barbarism) yaliongozwa kuamini kwamba kutoa kafara za wanadamu ilikuwa ni muhimu ili kupata fadhila ya Mungu; na ukatili huo wa kutisha umeendelezwa chini ya mifumo mbalimbali ya ibada ya sanamu. [GC 569.1; PK Aya ya 22]

Kanisa Katoliki la Rumi likiunganisha mifumo mbalimbali ya ibada za upagani na Ukristo, tena, kama upagani ulivyofanya, likiielezea na kuiwakilisha vibaya tabia ya Mungu, lilikuwa limetumia vitendo vya kikatili na vya kuchukiza ambavyo havikuwa na upungufu wowote kuliko vile (vya wapagani). Katika siku za ukuu wa Rumi ya kidini kushika hatamu zake za utawala wa dunia, palikuwa na zana za kutesea watu vibaya ili kuwashurutisha wayakubali mafundisho yake ya dini. Palikuwa na nguzo ya kuchomea watu moto kwa wale waliokuwa hawawezi kukubaliana na madai yake. Palikuwa na mauaji ya halaiki kwa kiwango cha kutisha ambayo hayataweza kufahamika mpaka yatakapofichuliwa

katika hukumu (walichoma kumbukumbu za ukatili huo). Viongozi wenye hadhi ya juu wa kanisa hilo walichukua mafunzo yao, chini ya bwana wao Shetani, na kubuni njia zilizokuwa na uwezo mkubwa mno wa kuwapatia watu mateso makali sana kwa kadri inavyowezekana bila ya kuuondoa uhai wa mteswaji. Katika matukio mengi, kitendo kile kibaya na cha huzuni sana na kishetani kilirudiwa tena na tena hadi kufikia kiwango ambacho mwanadamu asingewa kustahimili, ndipo mwili uliposalimu amri na mtu huyo akafa, na yule mhasiriwa alishangilia kifo chake kama ndiyo suluhisho na faraja yake tamu. [GC 569.2; PK Aya ya 23]

### Nidhamu Ya Kanisa Hilo

Hiyo ndiyo hatima iliyowapata maadui wa Rumi. Kwa wafuasi wake waaminifu alikuwa anawapa adhabu ya kujichapa wenyewe na mijeledi yenye misumari katika ncha zake (flagellation), kujitesa kwa njaa kali, na kuutesa mwili wao kwa ukali wa kila njia inayofikirika ambayo inaweza kuleta maumivu moyoni mwao. Ili kuweza kujipatia ukubali wa Mbingu, wale waliotubu walikiuka sheria za Mungu kwa njia ya kuzivunja sheria za maumbile yao. Walifundishwa kuvivunjilia mbali vifungo vya kifamilia na ndoa ambavyo Mungu aliviweka ili kumletea mibaraka na kumfurahisha mwanadamu katika kukaa kwake hapa duniani kama mgeni na msafiri. Viwanja vya makanisa hilo vimejaa mamilioni ya makaburi ya wahasiriwa ambao walitumia maisha yao yote kwa kujitahidi bure kutiisha hisia zao za kimwili za asili, yaani walizozaliwa nazo, kutoonyesha mapenzi ambayo yanapaswa kuonyesha kwa watu (natural affections), kulikandamiza kila wazo na hisia ya huruma kwa viumbe wenzao, ati kwamba mambo hayo humchukiza sana Mungu. [GC 569.3; PK Aya ya 24]

Ikiwa sisi tunatamani kuelewa ukatili wa Shetani uliokusudiwa kabisa, ambao ulidhihirishwa kwa mamia ya miaka, sio miongoni mwa wale waliokuwa hawajapata kumsikia Mungu kamwe, bali katika na katikati kabisa ya kiini cha eneo lote la Ulimwengu wa Kikristo, basi, yatupasa tu kuiangalia historia ya Urumi. Kupitia mfumo huo mkubwa wa udanganyifu, mfalme wa uovu (Shetani) analifanikisha kusudi lake la kumkosea Mungu heshima na kumwaibisha Mungu na kumletea mwanadamu maumivu na majanga mazito mno. Nasi kama tunavyoona jinsi anavyofanikiwa kujificha mwenyewe na kutekeleza kazi yake kupitia kwa viongozi hao wa kanisa, ndipo tunaweza kuelewa vizuri kwa nini anaichukia sana Biblia. Ikiwa Kitabu hiki kitasomwa na watu, basi, rehema na upendo wa Mungu vitafunuliwa kwao; itaonekana wazi ya kwamba Yeye haweki juu ya wanadamu mizigo hii mizito ambayo inawalemea sana. Yale yote anayotaka kwao ni moyo uliovunjika na kupondeka, roho ya unyenyekevu, na utii. [GC 570.1; PK Aya ya 25]

### Moyo Wa Mwokozi Uliojaa Upendo

Kristo hatoi mfano wowote katika maisha Yake unaowafanya wanaume na wanawake kujifungia wenyewe katika nyumba za watawa, ili wapate kufaa kwenda kuishi mbinguni. Yeye hakuwahi kufundisha kamwe kwamba upendo na huruma vizuiwe kuonyeshwa kwa watu (vikandamizwe). Moyo Wake Mwokozi wetu ulifurika kwa upendo Wake aliokuwa nao kwa watu. Kwa kadiri mwanadamu anavyokaribia sana kwenye ukamilifu wa uadilifu, hisia zake zinazidi kuwa makini kutambua mambo, na ndivyo mtazamo wake wa kutambua dhambi unavyozidi kuwa na makali zaidi, na ndivyo huruma yake kwa wanaoteseka inavyozidi ya kina zaidi. Papa anadai kwamba yeye ni Badala ya Kristo; lakini, je, tabia yake inafanananaje na ile ya Mwokozi wetu? Je! Kristo aliwahi kujulikana wakati wowote kuwatupa watu gerezani au kuwalaza kwenye kichanja cha kutesea watu kwa kuwavuta viungo vyao vya mwili na kuwaletea mateso makali sana ati kwa kuwa wao walikataa kumsujudia Yeye kwa kumpa heshima kama Mfalme wa mbinguni? Je, sauti Yake ilipata kusikika ikiwahukumu kupata adhabu ya kifo, watu wale ambao walimkataa? Wakati alipopuuzwa na watu wa kijiji cha Samaria, mtume Yohana alijawa na hasira kali, na kuuliza swali hili: “Bwana, wataka tuamuru moto ushuke kutoka mbinguni, uwateketeze, kama Eliya alivyofanya?” Yesu alimtazama kwa huruma mwanafunzi Wake, na kumkemea kwa roho yake ya ukali, akisema: “Mwana wa Adamu hakuja kuziharibu roho za watu; bali kuziokoa.” Luka 9:54, 56. Ni tofauti kubwa kiasi gani kati ya roho aliyoidhihirisha Kristo na ile inayoonyeshwa na yule anayedai kuchukua mahali pa Kristo (Vicar of Christ au Vicarius Filii Dei). [GC 570.2; PK Aya ya 26]

Kanisa la Roma kwa sasa linawakilisha mwonekano mzuri wa haki kwa ulimwengu, likiifunika kumbukumbu ya kuogofya mno ya ukatili wake ilioufanya kwa kukiri na kuomba radhi. Limejivika mavazi yenye mwonekano wa Kristo; lakini halijabadilika hata chembe ndogo. Kila kanuni ya upapa iliyokuwako katika zama zilizopita bado ipo pale pale leo. Mafundisho yake ya dini yaliyobuniwa katika Zama za Giza Kuu (ujinga) bado yanakumbatiwa mpaka sasa. Hebu na asiwepo mtu anayejidanganya mwenyewe. Upapa ambao Waprotestanti hivi sasa wako tayari mno kuuheshimu ni ule ule ulioitawala dunia katika siku za Matengenezo ya Kanisa, wakati watu wa Mungu waliposimama kidete, wakihatirisha maisha yao wenyewe, ili kuuanika nje uovu wake. Kanisa bado lina majivuno na dhana ya kiburi ile ile iliyoikuwa nayo wakati lilipokuwa juu zaidi ya wafalme na wakuu wa nchi mbali mbali,na madai yake ya kujinyakulia mamlaka (ya kidunia) na kujionyesha kuwa yeye ni mtawala juu ya wafalme (au Marais) na wakuu wa nchi mbalimblai, na kudai lina mamlaka na haki zile zile alizo nazo Mwenyezi Mungu. Roho yake haijapungua ukatili na ukandamizaji wake siku hizi kuliko wakati ule alipousagasaga uhuru walio nao wanadamu kwa kuwachinja ovyo watakatifu Wake, Yeye Aliye juu zaidi ya yo yote [Ufu. 17:6, 18]. [GC 571.1; PK Aya ya 27]

Upapa ndio ule ule ambao unabii ulitangaza kwamba ungekuwa, ukengeufu wa nyakati za mwisho. Wathesalonike 2: 3, 4, 7. Ni sehemu ya sera yake kuchukua tabia itakayomwezesha kulitimiza vyema kusudi lake; lakini chini ya mwonekano wake huo unaobadilika-badilika kama kinyonga, kanisa linaficha sumu kali sana isiyobadilika ya nyoka. "Imani haipaswi kumilikiwa na wazushi, wala pamoja na watu wanaoshukiwa kuwa wazushi" (Lenfant, gombo la 1, ukurasa wa 516), Kanisa linatangaza hivyo. Je! Mamlaka hii, ambayo kumbukumbu yake ya miaka elfu moja iliyoandikwa kwa damu ya watakatifu (Ufu. 17:6), sasa iweze kukubaliwa sasa kama sehemu ya Kanisa la Kristo? [GC 571.2; PK Aya ya 28]

**Badiliko Limetokea Katika Uprotestanti**

Dai hili halijatolewa hivi hivi tu bila sababu za msingi katika nchi za Kiprotestanti, kuwa Ukatoliki sasa una tofauti kidogo tu na Uprotestanti kuliko ilivyokuwa katika nyakati za zamani. Kumekuwepo na badiliko ila badiliko hilo haliko katika upapa. Ukatoliki wa leo, kusema kweli unafanana sana na Uprotestanti uliopo sasa, kwa sababu Uprotestanti umeporomoka hadhi na thamani yake mno tangu siku za Wanamatengenezo ya Kanisa. [GC 571.3; PK Aya ya 29]

Makanisa ya Kiprotestanti yalipokuwa yakitafuta kupendwa na kukubaliwa na ulimwengu huu, basi yalifumba macho kwa upendo wa bandia. Hawaoni kitu chochote isipokuwa kuamini wema katika uovu wote, na, kama matokeo yake yasiyoepukika, hatimaye watafikikia kuamini kila kitu ni uovu ambacho ni chema (Isa. 5:20). Badala ya wao kusimama imara na kuitetea imani waliyokabidhiwa watakatifu mara moja tu, wao hivi sasa, kama mambo yalivyo, wanaomba msamaha kwa Rumi kwa maoni yao yasiyo na ukarimu/upendo kwa Kanisa la Kikatoliki, wanaomba msamaha kwake kwa ubaguzi wao wa dini wenye chuki dhidi ya Kanisa Katoliki (waliokuwa nao huko nyuma). [GC 571.4; PK Aya ya 30]

Tabaka kubwa, hata miongoni mwa wale wanaoutazama Urumi bila upendo au kuwaunga mkono, hawatambui hata kidogo hatari inayowakabili kutokana na mamlaka na mvuto wake. Wengi wanasisitiza kwamba giza la kiakili na kimaadili lililokuwako katika kipindi cha Zama za Kati zenye giza, lilichangiza kuleta manufaa katika usambazaji wa mafundisho yake ya dini (dogmas), ushirikina wake, pamoja na ukandamizaji wake, na ya kwamba akili nyingi zinazopatikana nyakati hizi za sasa, uenezaji wa jumla wa maarifa hayo, na ongezeko la uhuru na malengo bora ya kuwafaa wengi katika masuala ya dini kutazuia hali ya kufufuliwa tena kwa roho ya kutovumilia imani ya wengine, na roho ya udikteta na ukatili. Wazo lenyewe linalosema kwamba hali ya mambo kama yale ya mateso na kunyimwa uhuru wa dhamiri itakuwako tena katika zama hizi zenye maarifa mengi huwa linachekwa na watu (maarifa kama teknolojia, sanaa na sayansi). Ni kweli kwamba nuru kubwa, kiakili, kimaadili na kidini, inaangazia

kizazi hiki. Katika kurasa zilizofunguliwa wazi za Neno la Mungu, nuru kutoka mbinguni imeangaza juu ya ulimwengu huu. Lakini ikumbukwe kwamba kadiri nuru kubwa inavyozidi kutolewa kwetu, ndivyo giza nene zaidi linavyozidi kuongezeka kwa wale wanaoipotosha na kuikataa nuru. [GC 572.1; PK Aya ya 31]

**Kujifunza Biblia Kwa Maombi**

Usomaji wa Biblia kwa maombi ungeweza kuwaonyesha Waprotestanti tabia halisi ya upapa na kuwafanya wauchukie sana na kuukwepa huu upapa; lakini wengi ni wenye hekima nyingi katika kiburi chao wenyewe, na kuona kuwa hawana haja ya kunyenyekea na kumtafuta Mungu ili wapate kuongozwa kwenye Ukweli. Ingawa wao wanajivunia wenyewe kwa nuru waliyopata, ni wajinga (si waelewa), hawajui chochote kuhusu Maandiko na uweza wa Mungu. Wao wanachokazania ni kuwa na njia fulani ya kuzinyamazisha dhamiri zao, nao katika kukidhi hitaji hili, wanatafuta mambo ambayo ni ya kiroho kidogo tu, yale ambayo hayawanyekeshi sana. Wanachotamani ni kupata mbinu ya itakayowafanya wamsahau Mungu ambayo itawaliwaza na kuonekana kwao kwamba ni mbinu ya kumkumbuka Mungu. Upapa umejipanga vizuri na mikakati ya kukidhi matakwa hayo yote mawili. Umejiandaa kukidhi matakwa ya matabaka haya mawili ya wanadamu, ukikumbatia karibu ulimwengu mzima - wale wanaotaka kuokolewa kwa njia ya matendo yao mema, na wale ambao wanapenda kuokolewa wakiwa na dhambi zao. Hapa ndipo palipo Siri ya nguvu yake. [GC 572.2; PK Aya ya 32]

Siku ya giza kubwa la kiakili imeonyesha kuwa ndiyo ina msaada kwa mafanikio ya upapa. Hata hivyo pia, bado itakuja kudhihirika kwamba siku ya nuru kubwa ya kiakili ni msaada mkubwa wa mafanikio ya upapa. Katika zama zile zilizopita, watu walipokuwa hawana Neno la Mungu, na bila kujua maarifa ya Ukweli, macho yao yalikuwa yamefungwa kwa kitambaa, na maelfu walinaswa, wasiweze kuuona wavu uliotandazwa kuinasa miguu yao. Katika kizazi hiki wako wengi ambao macho yao yanatiwa kiwi (giza) kwa mng'ao mkali wa mambo ya wanadamu wanayokisia-kisia tu, yaani, "sayansi kama inavyoitwa kwa uongo" (1 Tim. 6:20); hawautambui wavu uliotegwa, wanaingia ndani ya wavu kwa urahisi kana kwamba wamefungwa macho yao na kitambaa. Mungu alipanga kwamba uwezo wa akili ya mwanadamu unachukuliwa kama zawadi kutoka kwa Muumbaji wake na utumiwe katika huduma ya Ukweli na haki; lakini kiburi na kutaka makuu vinapopaliliwa moyoni, na watu wanapozitukuza nadharia zao na kuziweka juu ya Neno la Mungu, hapo ndipo akili zao zinaweza kufanya madhara makubwa kuliko ujinga uwezavyo kufanya. Hivyo basi, sayansi ya uongo ya siku hizi, ambayo inadhoofisha imani ya watu katika Biblia itaonekana kufanikiwa sana katika maandalizi ya njia ya kuupokea upapa, pamoja na sherehe zake za ibada zinazofurahisha, sawasawa tu na jinsi ya wakati uliopita maarifa

yalipozuliwa ili yasipate kuwafikia watu, na hilo likaleta mafaniko makubwa katika kufungua njia ya kujijengea umaarufu wa upapa katika Zama za Giza. [GC 572.3; PK Aya ya 33]

Katika harakati zinazoendelea hivi sasa katika nchi ya Marekani ili kujipatia msaada wa fedha kutoka serikalini kwa ajili ya kuendeshea taasisi zao na kwa matumizi ya kanisa, Waprotestanti wanafuata katika nyayo za upapa. Hapana, ni zaidi sana ya hapo, wao wanaufungua mlango katika nchi ya Kiprotestanti ya Amerika ili upapa upate kushika tena hatamu za ukuu ililioupoteza katika Ulimwengu wa zamani (Ulaya - katika mwaka wa 1798). Na kile kinachozipa uzito mkubwa harakati hizi ni ukweli ule kwamba lengo kuu linalofikiriwa ni kulazimisha utunzaji wa Jumapili kisheria - desturi ambayo ilianzishwa na Rumi, na ambayo Rumi inadai kuwa ni alama ya mamlaka yake (chapa) (Ufu. 13:16,17). Ni roho ya upapa - roho ya kufuata desturi za kidunia, yaani, kuyaheshimu sana mapokeo ya wanadamu kwa hali ya juu zaidi kuliko amri za Mungu – ambayo imepenya na kusambaa katika makanisa ya Kiprotestanti na kuwafanya wafanye kazi ile ile ya kuiinua Jumapili, kazi ambayo upapa ulikwishafanya kabla yao. [GC 573.1; PK Aya ya 34]

### Mamlaka Za Kidunia Kuliunga Mkono Kanisa

Ikiwa msomaji angependa kuelewa mawakala watakaotumiwa katika pambano linalokuja hivi karibuni, basi, hana budi kufuatilia tu kumbukumbu za njia alizozitumia Rumi kwa lengo hilo hilo katika zama zilizopita. Ikiwa anataka kujua jinsi wakereketwa wa upapa na Waprotestanti watakavyoungana kwa pamoja na kuwashughulikia wale wanaokataa mafundisho yao ya dini, hebu na aangalie roho aliyoionyesha Rumi kwa Sabato (Jumamosi) na watetezi wake. [GC 573.2; PK Aya ya 35]

Maagizo ya wafalme, mabaraza makuu, pamoja na amri za kanisa zilizotekelezwa na mamlaka ya serikali za kidunia, zilikuwa ndizo ngazi ambazo ziliwezesha siku kuu za kipagani kufikia nafasi yake ya kuheshimiwa katika Ulimwengu wa Kikristo. Amri ya kwanza iliyolazimisha utunzaji wa Jumapili ilikuwa ni sheria iliyotungwa na Konstantino. (Mwaka 321 BK; Angalia Nyongeza ya maelezo ukurasa wa 53.) Amri hii iliwataka wakazi wa mjini kupumzika ile “siku ya heshima ya jua” (Jumapili), lakini aliwaruhusu watu walioishi nje ya mji au mashambani kuendelea na kazi zao za kilimo. Japokuwa kwa hakika ilikuwa ni sheria ya kipagani kabisa, nayo ilikuwa imelazimishwa na mfalme wa dola Contantine baada ya yeye kuukubali Ukristo kwa jina tu. [GC 574.1; PK Aya ya 36]

### Sikukuu Iliyokubalika Sana

Wakati ambapo mamlaka ya kifalme haikuwa na uwezo wa kusimama kama mbadala wa mamlaka ya Mungu, Eusebius, askofu aliyetafuta kukukubaliwa na kupendwa na wakuu wa dunia, na ambaye alikuwa rafiki yake wa pekee na mwenye kumpaka mafuta kwa chupa ya mgongo Constantine, aliendeleza madai yake kwamba Kristo alikuwa ameihamisha Sabato kwenda Jumapili. Hakutoa ushahidi hata wa fungu moja kutoka katika Maandiko ili kuthibitisha fundisho lake hilo jipya. Eusebius yeye mwenyewe bila kujua anakiri uongo wa madai yake na kusonda kidole kwa waasisi halisi wa mageuzi hayo. "Mambo yote," anasema, "yale yaliyokuwa ni wajibu kufanywa siku ya Sabato (Jumamosi), hayo sisi tumeyahamishia hadi Siku ya Bwana (Jumapili)." —Robert Cox, Sabbath laws and Sabbath Duties, uk. 538, (Sheria za Sabato na Wajibu wa Sabato, ukurasa wa 538). Lakini hoja hiyo ya Jumapili, japokuwa haina mashiko yoyote kama vile ilivyokuwa, ilitumika kuwahamasisha watu katika kuikanyaga chini ya miguu yao, Sabato ya Bwana (Jumamosi). Wale wote waliotaka heshima ya ulimwengu huu waliipokea siku kuu hii [Jumapili] iliyopendwa na watu wengi, nayo ikatokea kuwa maarufu. [GC 574.1; PK Aya ya 37]

Upapa ulipokuwa umejizatiti kabisa, kazi ya kuitukuza Jumapili iliendelea. Kwa muda fulani watu walishughulika na kilimo walipokuwa hawahudhurii makanisani, na siku ya saba (Jumamosi) ilikuwa bado inatunzwa kama Sabato. Lakini mageuzi yalitekelezwa taratibu ila kwa uhakika. Wale waliokuwa katika ofisi takatifu* walikatazwa kupitisha hukumu katika kesi yoyote ya serikali ya kiraia katika siku ya Jumapili. Muda mfupi tu baada ya pale, watu wote, wa kila cheo, waliamriwa kuacha kufanya kazi zao za kawaida Jumapili kwa tishio la kutozwa faini kwa watu huru waliopewa haki ya uraia wa jiji lile, na tishio la maumivu ya viboko kwa watumwa. Baadaye amri ilitolewa iliyosema kwamba matajiri wangeadhibiwa kwa kupoteza nusu ya mali zao, iwe ardhi, nyumba au fedha; na endapo wangeendelea kuwa na shingo ngumu kwa ukaidi, basi, wangefanywa kuwa watumwa. Wale wa madaraja ya chini walilazimika kufukuzwa milele kutoka nchini, na wasionekane tena *(Inquistition/Inkwizisheni au ofisi takatifu-Mahakama ya Kanisa la Rumi). [GC 574.3; PK Aya ya 38]

Miujiza pia ilihusishwa katika masharti ya kuwalazimisha watu kutii. Miongoni mwa maajabu mengine, iliripotiwa kwamba mkulima mmoja alipokuwa anataka kuanza kulima shamba lake kwa plau siku ya Jumapili, alipokuwa akilisafisha jembe lake la kukokotwa kwa ng'ombe kwa kipande cha chuma, chuma kile kiling'ang'ania mkononi mwake, na kwa miaka miwili kilinataa hivyo kiganjani mwake, naye akaenda nacho kila mahali, "aliendelea kujipatia maumivu makali mno kwa aibu yake." —Francis West, Historical and Practical Discourse on the Lord's Day, ukurasa wa 174. [GC 575.1; PK Aya ya 39]

Baadaye papa alitoa maagizo yaliyosema kwamba kila kasisi wa parokia, yaani paroko, anapasa kuwaonya wavunjanji wa Jumapili na kuwataka waende kanisani

na kutoa sala zao, ili wasije wakajiletea balaa au majanga makubwa wao wenyewe pamoja na majirani zao. Baraza la Kanisa likatoa hoja ambayo toka hapo imekuwa ikitumika mahali pengi, hata na Waprotestanti, nayo ni hii, kwa vile watu fulani walikuwa wamepigwa na radi walipokuwa wakifanya kazi siku ya Jumapili, basi, ni lazima Jumapili iwe ni Sabato. "inaonyesha wazi," walisema maaskofu wa papa, "jinsi ambavyo chuki ya Mungu ilivyo kubwa kwasababu wameipuuzia siku hii" (Jumapili). Ndipo wito ukatolewa kwamba mapadri na wachungaji, wafalme na wakuu wa nchi, mawaziri na watu wote waaminifu "wafanye bidii zao zote na kuwa waangalifu kuona kwamba siku hii ya Jumapili inarudishiwa heshima yake tena, na kwa ajili ya kuuletea sifa na heshima Ukristo, itunzwe kwa kicho zaidi siku zijazo."—Thomas Morer, Hotuba katika Majadiliano Sita Juu ya Jina, Dhana, na Maadhimisho ya Siku ya Bwana, uk. 271. (Thomas Morer, Discourse in Six Dialogues on the Name, Notion, and Observation of the Lord's Day, page 271. [GC 575.2; PK Aya ya 40]

Matakamko ya mabaraza yapoonekana kuwa hayatoshelezi, wenye mamlaka ya serikali za kidunia waliombwa kutoa amri ambayo ingetia hofu kubwa katika mioyo ya watu ili kuwalazimisha wajizue wenyewe kufanya kazi siku ya Jumapili. Katika kikao cha Sinodi kilichokaa Rumi, maamuzi yote yaliyotangulia yalithibitishwa kwa nguvu nyingi na kwa uzito zaidi. Pia ziliingizwa katika sheria za kanisa na utekelezaji na mamlaka ya kiraia karibu katika ulimwengu wote unazodai kuwa ni wa Kikristo. (Angalia Heylyn, Historia ya Sabato, seh. 2, sura 5, sek. 7). [GC 575.3; PK Aya ya 41]

Bado kule kukosekana kwa mamlaka ya Maandiko kwa utunzaji wa Jumapili kuliendelea kuleta aibu ambayo haikuwa ndogo kwao. Watu waliuliza uhalali (haki) wa waalimu wao kuliweka pembeni tangazo chanya na lenye nguvu la Yehova, lililosema, "Siku ya saba (Jumamosi) ni Sabato ya BWANA, Mungu wako" [Kut. 20:10], ili wapate kuiheshimu siku ile ya jua (Jumapili). Kuziba shimo hili la upungufu wa ushahidi utokao katika Biblia, mbinu zinginezo zilibid zitumike ili kusawazisha mambo. Mtetezi mmoja mwenye ari ya Jumapili (motomoto), ambaye karibu na mwisho wa karne ya kumi na mbili alikuwa ameyatembelea makanisa ya Uingereza, alipingwa na mashahidi waaminifu wa ile Kweli; na hivyo zile juhudi zake hazikuzaa matunda kabisa, naye ikabidi aondoke nchini kwa kipindi fulani na kuzunguka zunguka kila upande ili apate njia fulani za kuyalazimisha mafundisho yake kwa nguvu. Aliporudi tena nchini, upungufu ule ulizibwa, na katika mikakati yake ya baadaye alipata mafanikio makubwa zaidi. Huui a lileta gombo alilodai kwamba lilikuwa limetoka kwa Mungu mwenyewe, ambalo lilikuwa na amri iliyohitajika kwa ajili ya utunzaji wa Jumapili, gombo hili lilikuwa na vitisho vya kuogofya ili kuwaita hofu wale wasiotii. Hati hii ya thamani -- ikiwa ni ya kughushi kama taasisi yenyewe iliyokuwa inaiunga mkono - ilidaiwa kuwa ilidondoka kutoka mbinguni na ilikutwa Yerusalemu, juu ya altare

(madhabahu) ya Mtakatifu Simeoni, huko Golgotha. Lakini ukweli wenyewe ni kwamba hati hii ilitoka kwenye jumba la kifalme la papa, yaani Ikulu ya Rumi. Ulaghai na kughushi ili kuendeleza mamlaka na mafanikio ya kanisa hilo yamefikiriwa machoni pa utawala huo wa hierakia wa kipapa katika vizazi vyote kuwa ni halali kufanyika. [GC 576.1; PK Aya ya 42]

Gombo hili lilikataza kazi isifanyike kuanzia saa ya tisa, yaani, saa tisa mchana siku ya Jumamosi alasiri, hadi mapambazuko ya jua siku ya Jumatatu; na mamlaka yake yalitangazwa kwamba yalikuwa yamethibitishwa kwa miujiza mingi. Iliripotiwa kwamba watu waliokuwa wakiendelea kufanya kazi zaidi ya ile saa iliyopangwa, walipigwa na ugonjwa wa kupooza kwa kiharusi. Msagishaji unga mwenye mashine ya kusaga nafaka alipojaribu kusaga mahindi yake, aliona, badala ya kutoa unga, lilitoka bubujiko la damu, na gurudumu la mashine likatulia kimya, licha ya maji yenye nguvu kupita kwenye ile mashine ya kusaga. Mwanamke aliyeweka mkate alioukanda ndani ya jiko la oveni la kuokea mikate, aliukuta ukiwa mbichi alipoutoa, ingawa oveni ilikuwa na joto kali sana. Mwingine aliyekuwa amekanda unga wa mikate tayari kuioka kuanzia saa ya tisa lakini akaamua kuiweka hiyo mikate mibichi mpaka Jumatatu asubuhi, aligundua kwamba siku iliyofuata, yaani Jumapili ilikuwa imeiva yenyewe na hivyo mikate hiyo ilikuwa imeokwa kwa uwezo wa Mungu. Mwanaume mmoja aliyeoka mkate baada ya kupita saa tisa siku ya Jumamosi, alipoumega asubuhi iliyofuata alikuta damu inaanza kuchuruzika kwenye mkate. Kwa kutunga au kuzua upuuzi kama huo na ushirikina,watetezi wa Jumapili walijaribu kuweka bidii ili kuonyesha utakatifu wa Jumapili. (Ona Roger de Hoveden, Annals, juzuu ya 2, ukurasa wa 526-530.) [GC 576.2; PK Aya ya 43]

Katika nchi ya Scotland, kama vile ilivyokuwa katika nchi ya Uingereza, heshima kubwa kwa ajili ya Jumapili ilipatikana kwa njia ya kuiunganisha na sehemu ya Sabato ya zamani (Jumamosi). Lakini wakati uliowekwa wa kuiheshimu kama masaa matakatifu, ulitofautiana. Amri toka kwa mfalme wa nchi ya Scotland ilitangaza kwamba "Jumamosi kuanzia saa sita mchana inapaswa kuhesabiwa kuwa ni takatifu," na ya kwamba asiwepo mtu ye yote, kuanzia saa hiyo mpaka Jumatatu alfajiri, atakayejishughulisha na shuguli za kidunia.— Morer, ukurasa wa 290, 291. [GC 577.1; PK Aya ya 44]

Lakini pamoja na juhudi zote zilizofanyika katika kuujenga utakatifu wa Jumapili, wapiga debe wa upapa wenyewe walikiri hadharani uwepo wa mamlaka ya Mungu ya Sabato (Jumamosi), na chimbuko la kibinadamu la siku Jumapili ambayo ilikuwa imewekwa badala ya Sabato ya Jumamosi. Katika karne ya kumi na sita baraza la papa lilitangaza waziwazi: "Wakristo Lazima wote na wakumbuke kwamba siku ya saba (Jumamosi) ilitakaswa na Mungu na ilipokelewa na kutunzwa, sio tu na Wayahudi, bali na wengine wote wanaojifanya kumwabudu Mungu; Japokuwa sisi Wakristo tumeibadilisha Sabato (Jumamosi)

yao kuwa Siku ya Bwana [Jumapili].” - Ibid., ukurasa wa 281, 282. Wale waliokuwa wanaichezea sheria ya Mungu hawakuwa wajinga kuhusiana na tabia ya kazi yao waliyokuwa wakiifanya. Kwa makusudi kabisa walikuwa wakijiinua wenyewe juu ya Mungu [2 Wathes. 2:3, 4]. [GC 577.2; PK Aya ya 45]

**Mfano Wa Kushangaza Mno**

Kielelezo kizuri na cha kushangaza  cha sera iliyotumiwa na Rumi dhidi ya wale wasiokubaliana naye kilionekana katika mateso yaliyoambatana na umwagaji wa damu nyingi ya Wawaldensia (Wawaldo/Hugenots) kwa kipindi kirefu sana, baadhi yao walikuwa wanaitunza Sabato (Jumamosi). Wengine nao waliteswa kwa njia iyo hiyo kwa ajili ya uaminifu wao kwa amri ya nne [Kut. 20:8 -11]. Historia ya makanisa ya Ethiopia na Uhabeshi (Abyssinia) ina maana ya pekee kwetu. Katikati ya giza la utusitusi kwenye Zama za Giza, Wakristo wa Afrika ya Kati hawakuonwa na mtu, tena walisahauliwa na ulimwengu, na kwa karne nyingi walifurahia uhuru wa kuiishi imani yao. Lakini hatimaye Rumi ilipata habari kuhusu uwepo wao kule, ndipo  mfalme wa dola ya Abyssinia alipolaghaiwa kwa muda mfupi mara moja na kumkiri papa kuwa ni mwakilishi wa Kristo, yaani  badala ya Kristo hapa duniani (Vicar of Christ). Maridhiano mengine yalifuata. Amri ilitolewa ikikataza kuitunza Sabato (Jumamosi) chini ya tishio la adhabu kali kwa Wakushi. (Ona Michael Geddes, Church History of Ethiopia, kurasa 311, 312.) Lakini utawala wa kidiketa na ukatili wa kipapa mara ukawa ni nira nzito iliyowaumiza mno, mpaka wale Wahabeshi waliazimu kuitupilia mbali kutoka katika shingo zao. Baada ya mapambano ya kutisha, Warumi walifukuzwa kutoka kwa maeneo yao, na imani ya zamani ikarejeshwa upya. Makanisa haya yakaufurahia tena uhuru wao, wala hawakusahau kamwe fundisho walilokuwa wamejifunza kuhusu madanganyo, ushupavu wa dini usiotumia busara, na mamlaka ya kiimla ya Rumi. Ndani ya milki yao  tulivu na iliyokuwa imejitenga mbali, waliridhika kubaki bila kujulikana na Ulimwengu uliobaki wa Kikristo.[GC 577.3; PK Aya ya 46]

Makanisa ya Afrika yaliitunza Sabato (Jumamosi) kama ilivyotunzwa na kanisa la papa kabla uasi kamili. Wakati walipoitunza siku ya saba (Jumamosi) kwa kuitii amri ya Mungu (Kut. 20:8-11), waliacha kufanya kazi siku ya Jumapili ili kwenda sambamba na  desturi ya kanisa. Ilipojipatia mamlaka ya juu, Roma ilikuwa imeikanyaga chini ya miguu yake Sabato ya Mungu (Jumamosi) ili kuitukuza Jumapili yake; lakini makanisa haya Afrika, yakiwa yamefichwa kwa karibu miaka elfu moja, hayakushiriki katika uasi huo. Yalipowekwa chini ya utawala wa Rumi, yalishurutishwa kuiweka kando Sabato  ya Kweli (Jumamosi) na kuitukuza sabato ya uongo (Jumapili); lakini mara tu walipopata uhuru wao na kujitawala tena walirudi kuitii amri ya nne. (Tazama Kiambatisho.) [GC 578.1; PK Aya ya 47]

Kumbukumbu hizi za nyuma hufunua waziwazi uadui alio nao Rumi na Sabato ya Kweli (Jumamosi) na watetezi wake, na njia zile anazozitumia ili kuiheshimu siku iliyobuniwa naye (Jumapili). Neno la Mungu linafundisha kwamba mandhari hizi zitarudiwa tena wakati Wakatoliki wa Rumi na Waprotestanti watakapoungana pamoja kwa madhumuni ya kuiinua Jumapili. [GC 578.2; PK Aya ya 48]

**Mnyama Mwenye Pembe Mfano Wa Mwana -Kondoo**

Unabii wa Ufunuo 13 hutangaza kwamba mamlaka inayowakilishwa na mnyama mwenye pembe kama za mwana -kondoo (Marekani) itaifanya "dunia na wote wakaao ndani yake" kuusujudia upapa - ambao katika unabii unawakilishwa kwa mfano wa mnyama "mfano wa chui." Yule mnyama mwenye pembe mbili pia atawaambia "wakaao juu ya nchi kumfanyia sanamu yule mnyama" tena, zaidi ya hayo, atawaamrisha wote, "wadogo kwa wakubwa, na matajiri kwa maskini, na walio huru kwa watumwa," wapokee alama ya mnyama. Ufunuo 13:11-16, Imeonyeshwa kwamba nchi ya Marekani (U.S.A) ndiyo mamlaka iliyowakilishwa na mnyama mwenye pembe mbili mfano wa mwana-kondoo, na ya kwamba unabii huo utatimizwa wakati ule Marekani itakapolazimisha uadhimishaji wa siku ya Jumapili kisheria, jambo ambalo Rumi inadai kwamba ni kutambua na kukubali kwa njia ya pekee ukuu wake usio na kifani. Lakini katika huku kuheshimu au kuusujudia upapa, nchi ya Marekani haitakuwa peke yake. Nguvu ya Roma katika nchi ambazo awali zilikiri utawala wake na bado haijaangamizwa. Na unabii huu unatabiri mapema juu ya kurejeshwa tena kwa nguvu yake. "Nikaona kimoja cha vichwa vyake kana kwamba kimetiwa jeraha la mauti, na pigo lake la mauti likapona. Dunia nzima ikamstaajabia yule mnyama na kumfuata (mfalme – Dan. 7:17) na Mstari wa 3. Pigo la jeraha ya mauti linaonyesha anguko la upapa katika mwaka wa 1798. Baada ya anguko lile, asema nabii, "pigo lake la mauti likapona. Dunia yote ikamstaajabia mnyama yule." Paulo anasema waziwazi kuwa "mtu wa kuasi au mtu wa dhambi" ataendelea hadi wakati wa ujio wa pili. 2 Wathesalonike 2:3-8. Mpaka mwisho kabisa wa wakati ataiendeleza kazi yake ya kudanganya. Tena, nabii wa Ufunuo, akiwa anauzunguzia upapa pia, anatangaza hivi "Wote wakaao juu ya nchi watamsujudu, ambao majina yao hayakuandikwa katika kitabu cha uzima." Ufunuo 13:8. Katika Ulimwengu wa Zamani au kale {Ulaya} na Ulimwengu Mpya {Amerika na Australia}, upapa utasujudiwa kwa njia ya heshima itakayotolewa kwa agizo la siku ya Jumapili iliyoiweka, ambayo imejengwa juu ya msingi wa mamlaka ya Kanisa la Kirumi peke yake. [GC 578.3; PK Aya ya 49]

Tangu katikati ya karne ya kumi na tisa, wanafunzi wa unabii katika nchi ya Marekani wamekuwa wakitoa ushuhuda huu kwa ulimwengu. Katika matukio yanayotokea hivi sasa kunaonekana maendeleo ya kasi sana kuelekea kwenye

kutimizwa kwa utabiri huu. Kwa upande wa waalimu wa Kiprotestanti, madai yale yale ya uwepo wa mamlaka ya Mungu katika utunzaji wa Jumapili hutolewa pia na, kutokuwepo kule kule kwa ushahidi kutoka katika Maandiko, kama ilivyokuwa kwa viongozi wale wa kipapa walioghushi miujiza ili kuwezesha kujaza pengo la kutokuweko kwa amri ya Mungu. Dai linalosema kwamba hukumu za Mungu zilikuwa zimepatilizwa juu ya watu kwa kuivunja kwao sabato-ya- Jumapili, litarudiwa tena; tayari limemeanza kusisitizwa. Na harakati hiyo ya ulazimisha wa utunzaji wa Jumapili kwa kutunga sheria inazidi kupata mashiko kwa kasi. [GC 579.1; PK Aya ya 50]

Kanisa la Rumi ni la kushangaza katika werevu na hila zake. Linaweza kusoma mapema kile kitakachokuwa. Linangojea wakati unaofaa, likizingatia kuwa makanisa ya Kiprotestanti yanalisujudia kanisa la Rumi kwa kuikubali sabato yake ya uongo (Jumapili) na kuwa wanajiandaa kuilazimisha kwa kuitungia sheria, yaani, kutumia njia zile zile lililozitumia katika siku zilizopita. Wale wanaoikataa nuru ya Ukweli bado watatafuta msaada kutoka kwa mamlaka hii inayojisema yenyewe kuwa haiwezi kukosea kamwe, ili wapate kuiinua siku hiyo ya Jumapili, iliyowekwa, ambayo chimbuko lake ni kanisa lenyewe. Ni haraka kwa kiasi gani kanisa la Rumi litakuja kutoa msaada kwa Waprotestanti katika kazi hiyo, si jambo gumu kubashiri. Ni nani anayejua vizuri sana kuliko hao viongozi wa kipapa namna ya kuwashughulikia wale wasio watiifu kwa kanisa hilo? [GC 580.1; PK Aya ya 51]

Kanisa Katoliki la Rumi, pamoja na taasisi zake ulimwenguni kote,huunda shirika moja kubwa sana chini ya udhibiti wa jimbo liitwalo Holy see* la papa, likiwa limebuniwa kutekeleza maslahi ya uongozi wa papa. Mamilioni ya waumini wake waochukua sakaramenti, katika kila nchi duniani, wamefundishwa kujichukulia wenyewe kana kwamba wamefungamanishwa katika utii kwa papa. Bila kujali wana utaifa gani au wapo chini ya serikali ipi, wamepewa agizo kuchukulia mamlaka ya kanisa kuwa ndiyo ipo juu ya zingine zote. Ingawa wanaweza kula kiapo cha kuahidi utiifu kwa serikali zao, lakini nyuma ya hicho kiapo, kipo kile kiapo cha utii kwa Rumi, nacho huwaondoa kutoka kwa kila kiapo kilicho kinyume na masilahi ya Rumi (Santa Sede kilatini au holy see)* [GC 580.2; PK Aya ya 52]

Historia inathibithisha juhudi zenye ustadi na hila nyingi zisizokoma, zenye uvumilivu mkubwa wa kujipenyeza lenyewe katika mambo ya serikali za mataifa. Nalo likiisha kujipatia mahali pa kukanyaga mguu wake, basi, linayaendeleza makusudi yake, hata kwa kuwaua wakuu wa nchi na watu. Katika mwaka ule wa 1204, Papa Innocent wa Tatu, alimshurutisha Petro wa Pili, mfalme Arragon, kwa njia ya kumhoji-hoji sana, kutoa kiapo hiki kifuatacho ambacho si cha kawaida: "Mimi, Petro, Mfalme wa Waaragoni, nakiri na kuahidi kwamba nitakuwa mwaminifu daima na mtiifu kwa bwana wangu, Papa Innocent, na kwa Warithi

wake wa kikatoliki watakaokuja baada yake, na kwa Kanisa la Rumi, na kwa uaminifu wangu kuuhifadhi ufalme wangu katika hali ya kumtii yeye, nikiilinda imani hii ya Kikatoliki, na kuwatesa wazushi.” — John Dowling, The History of Romanism, b. 5, sura. 6, sek. 55. Jambo hilo hupatana na madai yahusuyo mamlaka ya kiongozi wa Rumi “kwamba kwake ni halali kuwapindua wafalme wa dola katika kiti chao cha enzi” na “kwamba anaweza kuwafanya watu waache kuwatii watawala wao dhalimu.” - Mosheim, b. 3, senti. 11, sehemu. 2, sura. 2, sek. 9, maelezo 17. (Angalia pia Nyongeza dokezo la ukurasa wa 447.) [GC 580.3; PK Aya ya 53]

Hebu na ikumbukwe kuwa, haya ni majivuno ya kanisa la Rumi nalo haibadiliki kamwe. Kanuni za Gregory VII na Innocent III bado ndizo kanuni za Kanisa Katoliki la Rumi. Na kama lingekuwa na uwezo, lingeweka katika vitendo kwa nguvu nyingi sasa kama ilivyokuwa katika karne zilizopita. Waprotestanti hawajui kikamilfu wanakichofanya wanapopendekeza kukubali misaada ya Rumi katika kazi ya kuiinua Jumapili. Wakati wanajielekeza kutimiza kusudi lao, Rumi inalenga kusimamisha tena mamlaka yake, kurejesha ukuu wake uliopotea. Acha kanuni ianzishwe mara moja katika nchi ya Marekani kwamba kanisa linaweza kutumia au kutawala mamlaka ya serikali au nguvu za dola; kwamba siku kuu au maadhimisho ya kidini yalazimishwe na kutekelezwa na sheria za kiserikali; kwa kifupi, kwamba mamlaka ya kanisa na dola itawale dhamiri, na ushindi wa Rumi katika ya Marekani utakuwa umethibithiswahshwa. [GC 581.1; PK Aya ya 54]

Neno la Mungu limetoa onyo la hatari inayokuja; acha onyo hili lisitiliwe maanani, na ulimwengu wa Kiprotestanti utajifunza kile ambacho ni makusudi halisi ya Rumi, wakati ambao watakakuwa wamechelewa kuuepuka mtego. Kimya kimya kanisa la Rumi linaendelea kukua katika mamlaka yake. Mafundisho yake yanaendelea kueneza mvuto wake katika kumbi za kutunga sheria, katika makanisa, na katika mioyo ya wanadamu. Linaendelea kurundika maghorofa yake marefu na makubwa katika sehemu za siri ambazo mateso yake ya zamani yatarudiwa. Kimya kimya na bila kushukiwa, anaimarisha majeshi yake ili kuendelea malengo yake ili wakati wake wa kutoa pigo ufikapo, awe tayari kupiga. Yote ambayo anatamani ni uwanja wa kuvutia wenye manufaa, na tayari amepewa anachokitamani. Hivi karibuni tutaona na tutahisi kusudi la Uroma ni nini. Yeyote atakayeliamini na kulitii Neno la Mungu basi atagombezwa, na kupokea aibu na mateso. [GC 581.2; PK Aya ya 55]

*Je, neno holy see, au see linamaanisha nini?

Neno Holy See linatokana na neno la Kilatini Sancta Sedes, linalomaanisha "Kiti kitakatifu.” Kiti cha enzi, kinawakilisha nafasi na mamlaka/serikali ya Baba Mtakatifu au askofu, na mahali anapoishi katika eneo la mamlaka yake. Hapa Holy

See inarejelea “kiti cha serikali” cha Kanisa la ulimwengu wote. Kijiografia, kiti hiki cha serikali kiko katika Dayosisi ya Roma.

# SURA YA 36

# PAMBANO LINALOTARAJIWA HIVI KARIBUNI

**(Mgogoro Mkubwa Na Mpango Kabambe Wa Shetani—Amri Zake Au Kanuni Ni Amri Kumi-Kutoka 20)**

Ufupisho: Mungu kamwe halazimishi nia au dhamiri ya mtu, bali shetani hufurahia kufanya yote mawili. na siku za usoni ushurutishaji huu utarudiwa. Makosa yanayogonga kwa jeuri dhidi ya mamlaka ya mbinguni hivi karibuni yataletwa mbele kwa ujasiri- na kupewa msaada wa kuwezeshwa kisheria. Je, wewe na mimi tutakuwa tayari kwa mgogoro wa mwisho ulioelezewa katika kitabu cha Ufunuo? Hapa utajifunza wewe mwenyewe mpango mkuu wa adui.

Tangu mwanzo wa pambano hilo kuu mbinguni limekuwa ni kusudi la Shetani kuipindulia mbali Sheria ya Mungu (Ufunuo 12:7-9, 12, 17). Ilikuwa ni kwa kutimiza kusudi hili ndipo yeye alipojiingiza katika uasi dhidi ya Muumba Wake na ingawa alitupwa nje ya mbinguni ameendelea na vita hiyo hiyo duniani. Kuwahadaa binadamu na hivyo kwa njia hii kuwaongoza kuivunja Sheria ya

Mungu (Amri za Zake), hili ndilo lengo lake ambalo amekuwa akilifukuzia alipate kwa bidii sana. Iwapo hili litatimizwa kwa kutupilia mbali Sheria yote kabisa au kwa kuikataa katakata mojawapo ya kanuni zake dhahiri, matokeo yake hatimaye yatakuwa ni yale yale. Anayejikwaa "katika Neno (amri) moja," anaonyesha dharau kwa sheria yote; mvuto wake na mfano wake viko upande wa uasi yaani kuvunja sheria; na huwa, "amekosa juu ya yote." Yakobo 2:10. [GC 582.1; PK Aya ya 1]

Katika jitihada ya Shetani kutafuta namna ya kuonyesha dharau yake juu sheria za Mungu, Shetani ameyapotosha mafundisho ya dini yaliyomo katika Biblia (Doctrines), na kwa njia hiyo makosa haya yameingizwa katika imani ya maelfu ya wale watu wanaojidai kuyaamini Maandiko. Pambano kuu la mwisho kati ya Ukweli na uongo ni Shindano la mwisho tu la pambano hilo la muda mrefu sana juu ya Sheria ya Mungu (Lilianza mbinguni kwanza Ufu 12). Kuhusu vita hivi ambavyo sasa sisi tunaingia—ni vita kati ya Sheria za wanadamu na Amri (kanuni kumi) za Yehova, kati ya dini ya Biblia na dini ya hekaya za kubuni na mapokeo ya wanadamu. [GC 582.2; PK Aya ya 2]

Mawakala watakaoungana dhidi ya Ukweli na haki katika shindano hili, hivi sasa wamo kazini kikamilifu. Neno Takatifu la Mungu, ambalo limerithishwa kwetu kwa gharama kubwa ya mateso na damu, linathaminiwa kidogo tu. Watu wote wanaweza kuifikia au kuipata Biblia, lakini ni wachache tu ndiyo ambao wanaoikubali kuwa mwongozo wa Maisha yao. Ukafiri umezagaa kote kwa kiasi cha kutisha, sio kwa watu wa mataifa tu, bali ndani ya kanisa pia. Wengi wamefikia hatua ya kuyakana mafundisho ambayo ni nguzo hasa za imani ya Kikristo. Ukweli mkuu wa uumbaji kama ulivyowasilishwa na waandishi waliovuviwa wa Maandiko, anguko la mwanadamu dhambini, upatanisho na uendelevu wa Sheria ya Mungu (umilele), vinakataliwa wazi kabisa kwa vitendo, ama sheria yote au sehemu yake, na sehemu kubwa ya ulimwengu unaodai kuwa ni wa Kikristo. Maelfu wanaojivunia kuwa na hekima na watu walio huru wanaona kuwa ikiwa watakuwa na imani isiyo na mashaka katika Biblia basi huo utakuwa ushahidi dhahiri kwamba wao ni dhaifu; wao wanafikiri kwamba kuyakataa Maandiko ni uthibithisho kwamba wanacho kipaji cha hali ya juu na elimu au usomi uliosheheni na wanajifunza kuilalamikia Biblia kwa mambo madogo madogo yasiyo na msingi, wakinyumbua vipande-vipande hapa na pale, (kuyapinga Maandiko) wanayatafsiri kiroho, kwa kufuata hisia zao zisizovuviwa, na kupotosha kabisa Ukweli muhimu (Hawachukulii kama yalivyo halisi-literal- ila wanasema ni mafumbo au mfano, kiroho tu si kimwili). Wachungaji wengi wanafundisha watu wao, na maprofesa na walimu wengi wa theolojia wanawafundisha wanafunzi wao wakisema kwamba, Sheria ya Mungu imebadilishwa au imefutwa kabisa; na wale watu wanayoyaona kuwa matakwa yake bado ni halali na yana mashiko na nguvu kutiiwa kwa uhalisi wa neno kwa

neno kama yalivyo, hufikiriwa kuwa wanastahili kudhihakiwa au kudharauliwa tu. [GC 582.3; PK Aya ya 3]

Katika kuukataa Ukweli, wanadamu humkataa Mungu, Mwasisi Wake. Katika kuikanyaga chini ya miguu yao Sheria ya Mungu, wanaikataa mamlaka ya Mtoa-Sheria. Ni rahisi kuchonga sanamu ya mafundisho ya uongo na nadharia za uongo kama vile ilivyo rahisi kuchonga au kutengeneza sanamu ya mti au jiwe. Kwa kuwasilisha vibaya sifa za Mungu, Shetani huwaongoza wanadamu kumwelewa Mungu isivyokuwa sahihi, yaani isivyo, maana wana tabia ya uongo kumhusu (isiyo Yake). Kwa walio wengi, sanamu ya kifalsafa imepachikwa kwenye kiti cha enzi mbinguni badala ya Yehova; wakati Mungu Yule aliye Hai, kama anavyofunuliwa katika Neno Lake ndani ya Kristo na katika kazi Zake za uumbaji anaabudiwa na wachache tu. Maelfu wanafanya vitu vya asili au maumbile kuwa miungu yao (nature-wanaabudu uumbaji wa Mungu) na huku wakimkana Mungu wa asili au aliyeumba asili (nature). Japokuwa ni kwa miundo tofauti, ibada ya sanamu imo katika ulimwengu wa Kikristo leo katika uhalisia wake kama ilivyokuwa mongoni mwa Israeli ya kale katika siku zile za Eliya. Mungu wa watu wengi wanajiodai kuwa wana hekima leo, mungu wa wanafalsafa, wa watunzi wa mashairi, wa wanasiasa, wa waandishi wa habari-- yaani mungu wa matabaka ya duru za wanamitindo/fasheni za kisasa, wa vyuo na vyuo vikuu vingi, na hata katika baadhi ya taasisi fulani za kitheolojia-- ni miungu isiyomzidi sana yule Baali, mungu-jua wa Wafoinike. [GC u PK 583.1; PK Aya ya 4]

### Msingi Wa Serikali Zote

Hakuna kosa ambalo lilikubaliwa na ulimwengu wa Kikristo linalogonga kwa ujasiri zaidi mamlaka ya Mbingu, hakuna kosa linalopingana moja kwa moja na sababu za kawaida za busara zinazomwongoza mtu, hakuna lililo na matokeo yenye hatari zaidi kuliko fundisho la kisasa, ambalo limepata umaarufu kwa kuenea kwa kasi sana, kama lile lisemalo kwamba Sheria ya Mungu (Amri Zake) haiwafungi wanadamu tena. Kila taifa linazo sheria zake, ambazo zinapewa heshima na kutiiwa; hakuna serikali ambayo inaweza kudumu ikiwa haina sheria; na je, inawezaje kuingia akilini kwamba Muumbaji wa mbingu na nchi hana sheria ya kutawatawala viumbe Vyake alivyoviumba? Hebu tuseme kwamba hao wachungaji mashuhuri wangeanza kufundisha hadharani kwamba sheria zinazoliongoza taifa lao na kuzilinda haki za raia wake sio za lazima tena (haziwafungi)-- kwamba zilikuwa zinaminya uhuru wa raia na kwa hiyo hazipaswi kutiiwa tena; Je, wanadamu kama hao wangevumiliwa kwa muda gani wakifundisha hivyo kwenye vibweta vyao? Lakini je, ni kosa zito zaidi kupuuza sheria za nchi na za mataifa kuliko kuzikanyaga chini ya miguu yao kanuni* za

Mungu, ambazo ndiyo msingi wa serikali zote? *(Amri/maagizo/shuhuda/Maneno/ Sheria) (Rum 13:1-10, Ebr 10:27-31) [GC 584.1; PK Aya ya 5]

Ingekuwa ni afadhali zaidi kwa mataifa kuzifuta (kuzitangua) sheria zao, na kuwaruhusu watu wafanye kama wapendavyo, kuliko kwa Mtawala wa sayari zote kubatilisha Sheria Yake na kuacha ulimwengu bila kipimo cha kuhukumu mwenye hatia au kumpa haki yule aliye mtiifu Kwake. Je, tungependa kujua matokeo ya kuibatilisha (kuifuta) sheria ya Mungu? Jaribio hilo limekwisha kufanyika. Matukio ya kutisha yalitokea nchini Ufaransa wakati mamlaka inayotawala ilipomkana Mungu kisheria, na kusema Mungu hayuko (ukafiri-atheism) na hivyo ukana-Mungu ulifanywa kuwa mamlaka ya utawala. Wakati huo ilidhihirishwa waziwazi ulimwenguni kwamba kule kuvitupilia mbali vizuizi (wigo) ambavyo Mungu amewevika ni kukubali utawala wa watu madikteka katili kuliko wote. Kipimo hicho cha haki kinapowekwa pembeni (au kiwango), njia inakuwa imefunguliwa wazi kumkaribisha mfalme wa uovu kuimarisha mamlaka yake duniani. [GC 584.2; PK Aya ya 6]

Mahali popote sheria za Mungu zinapokataliwa, dhambi inakoma kwao kuonekana mbaya au haki kuonekana sifa ya kutamaniwa kwao. Wale wanaokataa kujisalimisha chini ya serikali ya Mungu hawafai kabisa kujiongoza wenyewe. Kwa njia ya mafundisho mabaya, yenye madhara, na uovu, roho ya kutotii inapandikizwa katika mioyo ya watoto na vijana, ambao kwa asili hawana uvumilivu wa kutawaliwawa; na hali ya kutofuata sheria (uasi) na kutokuwa na maadili kama uasherati na tamaa mbaya za mwili ndiyo huwa matokeo yake. Wakati wakidhihaki wale walio wepesi kutii matakwa ya Mungu,watu wengi hukubali ulaghai wa Shetani. Huzipatia tamaa zao za mwili usukani kuwaongoza na kutenda matendo ya dhambi ambayo yamesababisha hukumu za Mungu kushuka juu ya watu wa mataifa (wapagani). [GC 584.3; PK Aya ya 7]

**Kuvuna Tufani**

Wale wanaowafundisha watu kuzichukulia kwa wepesi Amri za Mungu, wanapanda mbegu ya uasi ili wavunje matunda ya uasi. Ukiacha kizuizi (wigo) kilichowekwa na Sheria ya Mungu (Amri Zake) kiondolewe kabisa na hakika haitachukua muda mrefu kwa sheria za wanadamu kupuuzwa pia kabisa (kutojaliwa). Kwa kuwa Mungu anakataza matendo yasiyokuwa na uaminifu, kusema uongo, kutamani, na ulaghai, basi, wanadamu wako tayari kuyakanyaga Amri Zake wakisema ni kipingamizi cha ustawi wao wa kidunia; lakini matokeo ya kuondoa kabisa hizi Kanuni Zake Mwenyezi Mungu yangekuwa ya uzito mkubwa vile wasivyotegemea. Ikiwa sheria hizo za nchi hazikuwa za lazima, na wala hazimbani mtu, kwanini kuwe na hofu kwa mtu yoyote kuzivunja hizo sheria? Mali isingekuwa salama tena. Watu wangejitwalia mali za majirani zao kwa jeuri

au mabavu na wale walio na nguvu zaidi wangekuwa matajiri kuliko wote. Uhai wenyewe usingeheshimiwa. Kiapo cha ndoa kisingekuwa imara tena kama ngome takatifu ya kuilinda familia. Yule ambaye ana uwezo au nguvu nyingi, kama angependa, angemchukua mke wa jirani yake kwa jeuri au nguvu. Amri ya tano ingeondolewa pamoja na ya nne (Kutoka 20). Watoto wasingesita kuwaua wazazi wao ikiwa kwa kufanya hivyo wangeweza kupata kile ambacho haja ya mioyo yao miovu ingetaka kukipata. Ulimwengu huu uliostaarabika ungekuwa genge la majambazi na wauaji; na amani, utulivu na furaha vingelitoweka duniani. [GC 585.1; PK Aya ya 8]

Tayari fundisho lisemalo kwamba wanadamu wameachiliwa huru kutoka katika utii wa matakwa ya Mungu limedhoofisha nguvu ya uwajibikaji wao wa kiuadilifu na kufungua milango ya mafuriko ya maovu juu ya ulimwengu huu. Uasi wa sheria, ulevi, uasherati, ubaradhifu, kutokuwa na kiasi kufanikisha kuipindua kabisa serikali ya ya Mungu. Na kazi ile ile ambayo alikuwa akijitahidi kuikamilisha kwa njama za namna hiyo, aliwasingizia malaika wana ufisadi vinaenea juu yetu na kutufagia kama wimbi kubwa sana linalotushinda nguvu (Tsunami). Katika familia zetu, Shetani yuko kazini. Bendera yake inapepea hata katika nyumba zinazodai kuwa ni za Kikristo. Kuna wivu, kushuku wengine vibaya, unafiki, mafarakano, chuki, uadui, malumbano, usaliti wa amana takatifu, uendekezaji wa tamaa mbaya. Mfumo mzima wa kanuni na mafundisho ya kidini ambayo yanapaswa kujenga msingi na mfumo wa jukwaa la maisha ya kijamii, unaonekana kuwa jengo linaloyumbayumba kwa kutaka kuanguka kwa ajili ya mzigo uliolilemea na msingi mbaya unaoshindwa kuhimili shida hiyo, na sasa liko tayari kuanguka chini kwa kishindo na madhara na kuwa gofu tu. Wahalifu na waovu kupindukia, wanapotupwa gerezani kwa sababu ya makosa yao, mara nyingi hupewa zawadi na kushabikiwa kana kwamba walikuwa wamepata ushindi fulani mkubwa unaostahili kuonewa wivu. Habari zao za uhalifu na tabia zinatangazwa sana mbele ya watu na kile walichokifanya. Vyombo vya habari hutangaza maelezo ya kuchukiza ya uovu wao kwa kinagaubaga na hivyo kuwachochea wengine kujifunza mambo haya ya ulaghai, ujambazi na mauaji; naye Shetani hushangilia sana kufaulu kwa mikakati yake ya Kijehanamu. Kupenda uovu kiasi cha kupumbazwa, kutojizuia ukatili wa kuondoa maisha ya wengine, kuongezeka kwa kutisha kwa kutokuwa na kiasi na uovu wa kila aina na kila kiwango, vyapaswa kuwazindua wale wote wamchao Mungu, ili wapate kujiuliza ni nini hasa kinapaswa kufanyika ili kuzuia tsunami ya maovu. [GC 585.2; PK Aya ya 9]

**Matokeo Yasiyoepukika**

Mahakama za sheria zimejaa ufisadi, rushwa na uonevu. Watawala wanasukumwa na tamaa ya mapato na kupenda kujifurahisha katika anasa mbaya za mwili. Kutokuwa na kiasi kumefunika uwezo wa akili za wengi kiasi kwamba

Shetani anakaribia kuwatawala kikamilifu katika kila nyanja. Mfumo wa mahakama, sheria na haki umepotoka, kwani wanahongwa na kulaghaiwa. Ulevi na karamu nyingi za ulevi, ulafi, tamaa, husuda, kukosa uaminifu kwa kila namna, huonekana miongoni mwa wale wanaosimamia utekelezaji wa sheria. "Na haki inasimama mbali sana; maana Kweli imeanguka katika njia kuu, na unyofu hauwezi kuingia." Isaya 59:14. (haki-unyofu). [GC 586.1; PK Aya ya 10]

Uovu na giza la kiroho lililosheheni chini ya himaya ya Rumi, haya yalikuwa ni matokeo ya moja kwa moja yaliyoletwa naye kwa kukandamiza Maandiko; lakini basi ni wapi katika kizazi hiki cha uhuru ambapo panaweza kupatikana chimbuko la ukafiri huu uliozagaa mahali pengi, pamoja na kukataliwa kwa Sheria ya Mungu (Amri Kumi), na ufisadi unaofuata baada ya kuikataa sheria ya Mungu, chini ya nuru kamilifu ya injili katika zama za uhuru wa kidini? Kwa vile sasa Shetani hawezi tena kuutawala ulimwengu kwa kuzuia Maandiko, yeye ameamua kutumia njia nyinginezo ili kutimiza kusudi lake lile lile. Kuharibu imani ya watu kwa Biblia kunamsaidia Shetani kutimiza kusudi lake na kuharibu Biblia yenyewe. Kwa kuleta imani ya kwamba Sheria ya Mungu haina mashiko, yaani haimbani mtu, yeye huwaongoza watu kirahisi na kwa ufanisi kutenda uovu, yaani kuzivunja Amri Zake Mungu kana kwamba walikuwa hawajui kabisa Kanuni Zake. Na kwa wakati huu wa sasa, kama ilivyokuwa katika zama zilizopita, amefanya kazi kupitia kanisa ili kuiendeleza mipango yake hii. Mashirika na taasisi za kidini ya leo yamekataa kusikiliza Ukweli usiopendwa na usiokuwa na maarufu kwa watu wengi, ambao umeelezwa waziwazi katika Maandiko, na ili kuushinda huo Ukweli wameupatia tafsiri zao na kuweka misimamo yao ambayo imepanda na kueneza mbegu za kutilia mashaka Neno la Mungu (skepticism). Wakiling'ang'ania fundisho la uongo la kipapa lisemalo kwamba mwanadamu ana roho kutokufa kamwe na kwamba akifa bado anakuwa na fahamu zakekatika umauti, wamekataa ulinzina kinga ya pekee dhidi ya udanganyifu wa Imani ya umizimu. Fundisho la mateso yanayoendelea milele motoni limewafanya watu wengi wasiweze kuiamini Biblia. Na madai ya amri ya nne yanapoelezwa kwa watu (Kutoka 20:8-11), inagunduliwa kwamba utunzaji wa Sabato wa siku ya saba umeaamriwa na Mungu (Jumamosi); na kama njia yao ya pekee ya kujinasua kutoka katika wajibu huo ambao hawako tayari kuufanya, walimu wengi mashuhuri wanaopendwa, hutangaza kwamba Sheria ya Mungu haimbani mtu tena (hawawajibiki kuitunza). Hivyo wanaitupilia mbali Sheria hiyo pamoja na Sabato (Jumamosi) kwa pamoja. Kadiri kazi ya matengenezo ya Sabato inavyoendelea kupanuka,* kukataliwa huku kwa Sheria ya Mungu ili kuepuka madai ya amri ya nne kutakuwepo kwa watukaribia ulimwenguni mzima. Mafundisho ya viongozi hao wa kidini yamefungua mlango wa ukafiri wa imani ya kuongea na wafu (umizimu) na dharau kwa Sheria takatifu ya Mungu (Amri Kumi); na juu ya viongozi hao unawakalia uwajibikaji wa kuogofya mno kwa ajili

ya uovu uliomo katika ulimwengu wa Kikristo (Yeremia 25:32-37). [GC 586.2; PK Aya ya 11]

Hata hivyo, tabaka hili hili wanadai kuwa ufisadi unaoenea kwa kasi na kwa kiasi kikubwa, unatokana na kunajisi kile kinachoitwa “sabato ya Kikristo” (Jumapili) na kwamba ulazimishaji wa utunzaji wa Jumapili utaweza kuboresha sana maadili ya jamii. Dai hili linasisitizwa zaidi katika nchi ya Marekani, ambako fundisho la Sabato ya Kweli (Jumamosi) limehubiriwa sana kila mahali. Hapa, harakati za kazi ya kiasi kwa jamii, yaani kuwafundisha watu kuacha kunywa vileo, tumbaku nk (temperance movement), ni mojawapo ya matengenezo makubwa na muhimu zaidi yanayojulikana ya kimaadili, na mara nyingi yanaunganishwa na harakati za kuiendeleza Jumapili, na watetezi wa Jumapili wanajiwakilisha wenyewe kama wanaofanya kazi kwa bidii ili kutetea maslahi ya juu zaidi ya jamii; na wale wanaokataa kuungana nao wanalaumiwa kama maadui wa kiasi na matengenezo hayo (Jumapili). Lakini ukweli ni kwamba vuguvugu la kundi hilo linalokusudia kuendelea uongo limeunganishwa na kazi ile ambayo kama ilivyo yenyewe ni nzuri (kuacha ulevi ni vyema), na sio hoja ya kuunga mkono uongo. Tunaweza kuificha sumu kwa kuichanganya na chakula kizuri kinacholeta afya mwilini, lakini kwa kufanya hivyo hatubadilishi asili ya ile sumu yake. Kinyume chake, imefanywa kuwa ya hatari zaidi, kwani kuna uwezekano mkubwa wa sumu kumezwa bila habari au tahadhari. Ni mojawapo ya mbinu za Shetani kuchanganya uongo kwa kiasi kidogo na Ukweli mwingi ili kuupa uongo uwezo wa kukubalika, yaani ili watu waone kwamba ndiyo Ukweli wenyewe. Viongozi wa vuguvugu la Jumapili* wanaweza kuunga mkono matengenezo ambayo watu wanayahitaji (kuacha ulevi), yaani zile kanuni zinazopatana na Biblia; lakini kwa kuwa matengenezo haya, yamechanganywa na takwa ambalo ni kinyume na Sheria ya Mungu (Amri Kumi), watumishi Wake Mungu hawawezi kuungana nao. Hakuna jambo lolote linaloweza kuwahalalisha kwa kuziacha Amri za Mungu na badala yake kutii kanuni zilizowekwa na wanadamu. [GC 587.1; PK Aya ya 12]

Kwa kupitia njia ya mafundisho mawili makuu ya uongo, kutokufa kwa roho (roho isiyoweza kufa kamwe) na utakatifu wa Jumapili, Shetani atawaleta watu chini ya madanganyo yake. Wakati lile la kwanza linajengamsingi wa Imani ya kuongea na wafu, lile la pili linajenga mshikamano wa kuikubali Rumi kwa kuonyesha huruma. Waprotestanti wa nchi ya Marekani watakuwa katika mstari wa mbele kabisa katika kuinyoosha mikono yao kutoka upande mmoja hadi mwingine wa bonde la ufa ili kushikana mikono na Imani ya kuongea na wafu *(umizimu); watanyosha mikono yao juu ya korongo lenye kina kirefu ili kushikana mikono na mamlaka ya Kirumi; na chini ya mvuto wa muungano wa mamlaka tatu (pande tatu au utatu), nchi hii itafuata katika nyayo za Rumi katika kuzikanyaga chini ya miguu yake haki za dhamiri za watu -(Kuzuia watu

wasimwambudu Mungu kama mioyo inavyotaka. *Asia inalo fundisho hili pia la mtu akifa anafufuka kwingine na kuishi-New Age) [GC 588.1; PK Aya ya 13]

Kwa kuwa imani ya umizimu inaigiza kwa ukaribu zaidi Ukristo wa jina tu wa wakati wetu, inakuwa na nguvu kubwa kudanganya na kuwanasa watu mtegoni. Shetani mwenyewe ameongoka, kulingana na hali ya sasa ya mambo. Atajitokeza katika tabia na mwonekano wa malaika wa nuru. Kwa njia ya wakala wa Imani hii ya umizimu, miujiza itatendwa, wagonjwa wataponywa na maajabu mengi yasiyokanushika yatafanywa (Mt 7:21-23, 24:24-28, 2 Kor 11:13-15). Na kama vile mapepo, yaani roho za mashetani watadai wanaiamini imani katika Biblia na kuonyesha heshima yao kwa taasisi za kanisa, kazi zao zitakubalika kama udhihirisho wa nguvu za Mungu (miujiza). [GC 588.2; PK Aya ya 14]

Mstari unaotofautisha kati ya wale watu wanaodai kuwa ni Wakristo na wale wasiomwamini Mungu kwa sasa hauonekani vizuri. Washiriki wa kanisa wanapenda mambo yaleyale ambayo ulimwengu unayapenda na tena wako tayari kujiunga nao, na Shetani amedhamiria kuwaunganisha wote katika jumuiya moja (Ufunuo 16:13, 14) na kwa njia hiyo kuimarisha kazi yake kwa kuwafagilia wote kwenye safu ya imani ya kuongea na wafu (umizimu). Waumini wa mfumo wa upapa wanaojivunia miujiza kama ishara ya hakika ya kanisa la Kweli, watadanganywa kwa urahisi sana na nguvu hiyo itendayo miujiza; na Waprotestanti nao, wakiwa wameitupilia mbali ngao ya Ukweli (Biblia), watadanganywa pia. Wafuasi wa upapa, Waprotestanti na watu wa kidunia wote kwa pamoja wataupokea mfano huo na kuwa na maigizo ya utauwa bila kuwa na nguvu za Mungu, nao wataona katika muungano wao huu vuguvugu kubwa la kuuongoa ulimwengu wote na uingizaji wa kipindi cha miaka miaka elfu moja (milenia) kilichosuburiwa kwa muda mrefu. [GC 588.3; PK Aya ya 15]

Kwa njia ya Imani ya umizimu, Shetani ataonekana kama mfadhili wa jamii ya wanadamu, akiponya magonjwa ya watu na kudai kuwaletea mfumo mpya, ulio bora na wenye utukufu zaidi wa imani ya kidini; lakini wakati huo huo anafanya kazi kama muuaji. Majaribu yake yanaongoza watu wengi kwenda kuangamizwa. Kutokuwa na kiasi kama ulevi huiondoa busara ya kufikiri vizuri kutoka kwenye kiti chake cha enzi, yaani ubongo; hapo ndiyo watu hutaka kujifurahisha na tamaa ya kimwili, anasa migogoro na ndipo umwagaji damu hufuata. Shetani hupenda na kuchangamkia sana vita, kwa kuwa vita husisimua mihemko mibaya zaidi za rohoni kuliko yote na kisha vinawafagia wahanga wote kuingia katika umilele wakiwa na mwelekeo wa kuzama uovuni, katika dhambi zao na umwagaji damu. Ni kusudi lake kuyachochea mataifa kupigana vita wao kwa wao, kwa kuwa kwa njia hii anaweza kuhamisha akili za watu zisijishugulishe na kazi ya maandalizi ili kuweza kusimama katika siku ya Mungu (siku ya hukumu). [GC 589.1; PK Aya ya 16]

**Kudhibiti Maumbile-Ardhi, Maji, Hewa, Moto**

Shetani anafanya kazi yake kupitia vipengele vya asili* pia ili kukusanya mavuno yake ya roho ambazo hazijajiandiaa kikamilifu (wasiojitoa kikamilifu kwa Mungu). Amefanya utafiti wa siri za maabara za asili na anatumia mafunzo yake ya maabara na nguvu zake zote kutawala mambo ya asili kile ambacho Mungu anaruhusu. Aliporuhusiwa kumtesa Ayubu, kwa kasi kubwa kiasi gani aliweza kufagilia mbali makundi yake ya kondoo, ng'ombe, watumishi wake, nyumba yake na Watoto wake. Janga moja likifuata jingine chini ya nukta moja. Mwenyezi Mungu Ndiye anayevilinda viumbe Vyake na kuwazungushia wigo mbali na ya nguvu za huyo mwangamizaji/muuaji. Lakini ulimwengu wetu wa Kikristo umeonyesha dharau kubwa sana kwa Sheria ya Yehova; na Bwana atafanya kile ambacho ameahidi kwamba atafanya-- ataondoa mibaraka Yake toka duniani na kuondoa ulinzi Wake kutoka kwa wale wanaoendelea kuiasi Sheria Yake (Amri Zake), na kuwafundisha na kuwalazimisha wengine kufanya kama wao (Mt 5:17-19). Shetani anawatawala kabisa wale wote ambao hawako chini ya ulinzi wa Mungu. Anawapendelea na kuwafanikisha baadhi ili kuendeleza njama zake mwenyewe na wengine atawaletea matatizo na kuwaongoza watu wengine kuamini kwamba ni Mungu anayewatesa *(vipengele vya asili ni kama matetemeko, mafuriko, uchafuzi angahewa, moto). [GC a 589.2; PK Aya ya 17]

Wakati Shetani ataonekana kwa watu kama mganga mkuu anayeweza kuponya magonjwa yao yote, atawaletea magonjwa na majanga, hadi majiji yenye wakazi wengi yatakapokuwa magofu na ukiwa. Hata sasa yuko kazini. Katika ajali na majanga yanayotokea baharini na nchi kavu, katika mioto mikubwa iteketezayo, katika vimbuga na tufani kali za mvua ya mawe zenye kutisha, katika dhoruba kali, katika mafuriko, upepo mkali, mawimbi ya maji yaliyojaa kupita kiasi wakati wa kupwa kwa maji ya bahari na matetemeko ya ardhi, kila mahali na katika mifumo yake elfu, Shetani anatumia uwezo wake. Yeye anafagia mazao yanayoendelea kukomaa, ndipo njaa, hofu na dhiki hufuata nyuma yake. Anachafua hewa kwa sumu ya kufisha angani na maelfu huangamia kwa tauni. Majanga hayo yataendelea kutokea mara kwa mara na kuleta maafa mengi zaidi. Matukio haya ya maanganizi yatakuwa juu ya wanadamu na anyama pia. "Dunia inaomboleza, inazimia;" "watu wakuu wa dunia..... wanadhoofika. Tena dunia imetiwa unajisi kwa watu wanaoikaa; kwa maana wameziasi Sheria, wameibadli amri, wamelivunja agano la milele" Isaya 24:4, 5 (Kutoka 20). [GC 589.3; PK Aya ya 18]

Na ndipo mdanganyaji mkuu atakapowashawishi wanadamu kwa kuwaambia kwamba wale wanaomtumikia Mungu ndio chimbuko la majanga hayo. Tabaka ambalo limechokoza hasira ya mbingu ndilo litatupia lawama ya matatizo yao yote kwa wale ambao utii wao kwa Amri za Mungu umekuwa ni kemeo la kudumu kwa wakosaji wanaozivunja Amri za Mungu. Itatangazwa kwamba watu hao

wanamkosea Mungu kwa kuivunja sabato ya Jumapili; kuwa dhambi hiyo imeleta majanga ambayo hayatakoma hadi utunzaji wa Jumapili utakapotekelezwa kikamilifu kabisa kwa kuithibiti kisheria; na kwamba wale wanaowasilisha madai ya kuitunza amri ya nne (Kutoka 20:8-11), na kwa njia hiyo kuharibu heshima kuu inayotolewa kwa Jumapili, ndiyo wataabishaji wa watu, nao ndiyo wanazuia urejeshwaji wao kwa upendeleo wa Mungu na mafanikio ya dunia hii (ya muda mfupi). Hilo ndilo shitaka lililoshinikizwa zamani dhidi ya mtumishi wa Mungu, nalo litarudiwa tena, na kwasababu zinazoonekana kuwa za msingi kama zile: "Ikawa, Ahabu alipomwona Eliya, Ahabu akamwambia, Je! Wewe, Ewe mtaabishaji wa Israeli? Naye akajibu, Si mimi niliyewataabisha Israeli; bali ni wewe, na nyumba ya baba yako, kwa kuwa mmeziacha amri za Bwana, nawe umewafuata Mabaali". 1 Wafalme 18:17, 18. Wakati ghadhabu ya watu itakapochochewa kutokana na mashtaka hayo ya uongo dhidi ya mabalozi wa Mungu, watafuata njia inayofanana kabisa na ile ambayo Waisraeli walioasi walivyotafuta kuwaua mabalozi wa Mungu, Eliya alikuwa miongoni mwa waliofuatwa. [GC 590.1; PK Aya ya 19]

**Nguvu Itendayo Miujiza**

Nguvu hiyo itendayo miujiza ya adui ambayo inajidhihirisha kupitia njia ya Imani ya umizimu itaweka mvuto wake wa upinzani dhidi ya wale wanaochagua kumtii Mungu kuliko wanadamu. Mawasiliano kutoka kwa roho za mapepo (mizimu) yatatangaza kwamba Mungu amewatuma kuwahakikishia wapinzani wa Jumapili kuhusu kosa lao, nao hawa pepo watathibitisha kwamba sheria za nchi (serikali) zinapaswa kutiiwa kama Sheria ya Mungu. Wataomboleza na kusikitika kwa ajili ya uovu mkubwa uliopo duniani na kuunga mkono ushuhuda wa waalimu na viongozi wa dini usemao kwamba hali ya mmomonyoko wa maadili umesababishwa na kunajisiwa kwa Jumapili. Hasira kali itachochewa dhidi ya wote wanaokataa kukubali ushuhuda wao. [GC 590.2; PK Aya ya 20]

Sera ya Shetani katika mgogoro huu wa mwisho na watu wa Mungu ndiyo ileile aliyoitumia wakati wa uanzishaji wa ufunguzi wa pambano kuu mbinguni (Ufunuo 12). Alidai kuwa alikuwa anatafuta kuongeza uimara wa nguvu ya serikali ya Mungu, na huku alikuwa akifanya kila juhudi kisirisiri Mungu watiifu, na kuwatwisha lawama. Sera ile ile ya udanganyifu imeitia doa historia ya Kanisa la Rumi. Linaeleza kuwa linafanya kazi yake kama mwakilishi wa Mbinguni. Wakati likitafuta kujiinua juu ya Mungu na kubadili Sheria Yake (Danieli 7:25). Chini ya utawala wa Rumi, wale walioteswa hadi kuuwawa kwa ajili ya uaminifu wao kwa injili, walilaumiwa kama watenda maovu; walitangazwa kwamba walikuwa na ubia na Shetani; na kila njia inayowezekana ilitumika ili kuwapakaza matope ya lawama, dharau na aibu,na kuwafanya waonekane machoni pa watu na hata machoni mwao wenyewe kama ni wahalifu

wabaya kuliko wahalifu wote. Hivyo ndivyo itakuwa hata sasa. Wakati Shetani akitafuta kwa bidii kuwaangamiza wale wanaoiheshimu Sheria ya Mungu, atasababisha washitakiwe kama wavunjaji wa sheria, yaani, kama watu wanaomvunjia Mungu heshima na kuleta hukumu za Mungu juu ya dunia hii. [GC 591.1; PK Aya ya 21]

Kamwe Mungu halazimishi nia au dhamiri ya mtu; lakini juhudi ya Shetani daima—ni kuweza kuwatala wale watu ambao hawezi kuwashawishi kwa njia nyingine —ni kulazimisha kwa ukatili. Kwa njia ya hofu au nguvu hufanya jitihada kuitawala dhamiri na kujipatia nafasi ya yeye mwenyewe kuabudiwa Ili kufanikisha hili lengo, anafanya kazi kupitia mamlaka za kidini na za kiserikali, akiwaongoza kulazimisha sheria za wanadamu kwa kuasi sheria ya Mungu na hivyo kupingana Naye. [GC 591.2; PK Aya ya 22]

Wale wanaoiheshimu Sabato ya Biblia (Jumamosi) watashutumiwa kama maadui wa sheria, utaratibu na utulivu wa nchi, kama waanaovunja vizuizi vya maadili ya jamii na kusababisha uasi dhidi ya serikali, ufisadi na kuleta hukumu ya Mungu hapa chini duniani. Uadilifu wao unaotokana na dhamiri zao utatamkwa kuwa ni ukorofi, ushupavu, ukaidi na dharau kwa wenye mamlaka. Watashutumiwa kwa kukosa uzalendo kwa serikali. Wachungaji wanaokataa uwajibishaji wa Sheria ya Mungu watahubiri kutoka kwenye madhabahu zao wajibu wa utii kwa mamlaka ya serikali za kiraia kuwa ndiyo amri ya Mungu. Katika majengo ya kutunga sheria (Bungeni) na mahakama za kutoa haki, wanaozishika Amri za Mungu watawasilishwa vibaya na kushukiwa vibaya na kuhukumiwa. Tafsiri ya uongo itapakwa kwenye maneno yao; tafsiri mbaya mno itawekwa juu ya nia zao kwa yale wanayotenda. [GC 592.1; PK Aya ya 23]

Makanisa ya Kiprotestanti yanapozikataa hoja hizo za Maandiko zinazoeleweka wazi, ambazo zinaitetea Sheria ya Mungu, yatatamani sana kuwanyamazisha wale ambao imani yao hawawezi kuishinda kwa Biblia. Ingawa wanajifanya wenyewe kuwa vipofu ili macho yao yasiweze kuuona Ukweli, sasa wanapita katika njia ile ambayo itawafikisha kwenye kuwatesa wale watakaokataa kwa uthabiti kufanya kile ambacho ulimwengu uliobaki wa Kikristo unakifanya na kukiri madai ya sabato ya kipapa (Jumapili). [GC 592.2; PK Aya ya 24]

Viongozi wakuu wa kanisa na wa serikali/dola wataungana Pamoja ili kuhonga, kushawishi au kulazimisha kwa nguvu matabaka yote ili yapate kuiheshimu Jumapili. Kukosekana kwa idhini ya mamlaka ya Mungu kutajazwa kwa kutunga sheria zenye ukandamizaji bungeni. Ufisadi wa kisiasa unaua kuipenda haki na kuheshimu Ukweli; na hata katika nchi huru ya Marekani, watawala wake na watunga sheria (wabunge) ili kujipatia ukubali wa umma, watajisalimisha kwa madai yanayopendwa na wengi kwamba iwepo sheria inayolazimisha utunzaji wa Jumapili. Uhuru wa dhamiri ambao umegharimu watu

kafara kubwa mno, hautaweza kuheshimiwa tena. Katika pambano hilo linalokuja hivi karibuni, tutaona maneno ya nabii yakidhihirishwa kwa vitendo: “Joka akamkasirikia yule mwanamke, akaenda zake afanye vita juu ya wazao wake waliosalia, wazishikao amri za Mungu, na kuwa na ushuhuda wa Yesu. Kristo.”* Ufunuo 12:17. [GC 592.3; PK Aya ya 25]

*(Joka ni Shetani, Mwanamke ni Kanisa safi, Amri hizi ni zile kumi za Mungu, na Wazao wake ni Wafuasi ake, Roho ya unabii Ufunuo 19:10, na Ufunuo 12:17)

*Harakati za kutunza Jumapili siku za karibuni imekuwa ikisisitiza kwamba itasaidia mahusiano ya kifamilia, itaongeza afya na kusaidia mazingira (ekolojia) na kupunguza utumiaji wa nishati.

# SURA YA 37

# MAANDIKO NDIYO USALAMA WETU PEKEE

**(Jenga Juu Ya Mwamba)**

Ufupisho: Udanganyifu wa mwisho utatokea hivi karibuni, nao utafanana na Ukweli kiasi kwamba watu watashindwa kutofautisha isipokuwa wanajisomea Biblia zao. Hata hivyo ni wachache sana ambao wanazithamini Biblia zao na

kuzisoma kwa bidii yote, ili kujitayarisha na dhiki inayoujia ulimwengu. Shetani anataka kuwavuta watu kwake ili wasiende kwenye Maandiko, na ni wachache wanajiandaa kufanya upinzani.

**Ulinzi, Usalama Na Kinga Yetu Pekee Ni Maandiko!**

Na waende kwa sheria na ushuhuda; ikiwa hawasemi sawasawa na Neno hili, bila shaka kwa hao hapana asubuhi." Isaya 8:20. Watu wa Mungu wanaelekezwa kuyachukulia Maandiko kuwa ndiyo kinga yao dhidi ya mivuto ya waalimu wa uongo na nguvu ya udanganyifu ya roho wa giza. Shetani anatumia kila mbinu inayowezekana ili kuwazuia watu wasiweze kupata ujuzi wa Biblia; kwa kuwa kauli zake zinazoeleweka wazi zinayafichua madanganyo yake. Katika kila uamsho wa kazi ya Mungu, mfalme huyo wa uovu anaamshwa na kufanya shuguli zake kwa juhudi kubwa zaidi; hivi sasa anatumia juhudi zake zote kwa ajili ya pambano lake la mwisho dhidi ya Kristo na wafuasi Wake. Uongo wake mkuu wa mwisho karibu sana utafunuliwa mbele yetu. Mpinga Kristo atafanya kazi zake za maajabu yake mbele ya macho yetu. Kazi zake za bandia zitafanana na mambo halisi kiasi kwamba haitawezekana kutofautisha kazi hizo au maajabu hayo isipokuwa tu kwa njia ya Maandiko Matakatifu. Kwa njia ya ushuhuda wa Maandiko kila kauli na kila muujiza lazima vipimwe (1 The. 5:19- 22; 1 Yoh. 4:1 - 6; Mt. 7:21- 27; 2 Kor. 11:13-15; Kum. 13:1-5). [GC 593.1; PK Aya ya 1]

Wale watakaojitahidi sana kuzitii amri zote za Mungu watadhihakiwa, watapingwa na kutukanwa. Wataweza kusimama imara kwa uwezo wa Mungu tu. Ili kustahimili jaribu gumu lililo mbele yao, inawapasa wayaelewe mapenzi ya Mungu kama yalivyofunuliwa katika Neno Lake; wanaweza kumheshimu Yeye tu wanapokuwa na uelewa sahihi kuhusu tabia Yake, serikali Yake, na makusudi Yake, na kutenda kulingana nayo. Hakuna watakaoweza kusimama kidete katika pambano kuu la mwisho, isipokuwa wale tu waliouimarisha moyo wao kwa Ukweli za Biblia. Kwa kila mtu mtihani wenye swali hili unapaswa kuja kwenye moyo wake: Je, nimtii Mungu kuliko wanadamu? Saa ya maamuzi ya mwisho wa kila jambo sasa imewadia. Je! miguu yetu imesimikwa juu ya mwamba wa Neno la Mungu lisilobadilika kamwe? Je, tuko tayari kusimama imara katika kuzitetea amri za Mungu pamoja na imani ya Yesu? (Ufu. 14:12.) [GC 593.2; PK Aya ya 2]

Kabla ya kusulubiwa Kwake Mwokozi wetu aliwaeleza wanafunzi Wake kwamba ilikuwa imempasa kuuawa na kufufuka tena kutoka kaburini, na malaika walikuwapo pale ili kuweka alama kwenye akili na mioyo yao kwa maneno haya. Lakini wanafunzi walikuwa wakitarajia ukombozi wa kidunia kutoka katika kongwa la Kirumi, nao hawakuweza kustahimili wazo kuwa Yule ambaye Kwake walikuwa wameyaweka matumaini yao yote angepaswa kufa kifo cha aibu sana. Maneno yale waliyohitaji kuyakumbuka yalitoweka kabisa akilini mwao; na wakati wa kujaribiwa kwao ulipofika, uliwakuta hawajawa tayari. Kifo Chake

Yesu kiliyavunjilia mbali kabisa matumaini yao, na ikawa kana kwamba alikuwa hakuwahi kuwaonya mapema. Kwa hiyo, katika unabii, wakati ujao umefunuliwa mbele yetu kwa wazi kama vile ulivyofunuliwa kwa wanafunzi Wake kupitia Maneno ya Kristo. Matukio yanayofungamana na kufungwa kwa mlango wa rehema na kazi ya kujitayarisha kwa ajili ya wakati wa taabu, yameelezwa kwa uwazi kabisa. Lakini watu wengi sana hawazifahamu Kweli hizi muhimu sawa tu na vile ambavyo zingekuwa hazijapata kamwe kufunuliwa kwao. Shetani yuko macho akihakikisha anaweza kudaka kila mvuto ambao ungeweza kuwahekimisha watu hata wapate wokovu, na wakati wa taabu utawakuta wakiwa hawajajiandaa. [GC 594.1; PK Aya ya 3]

Mungu anapoyatuma maonyo kwa wanadamu yaliyo muhimu sana kiasi kwamba yanawakilishwa kana kwamba yanahubiriwa na malaika watakatifu wanaoruka katikati ya mbingu, Yeye anataka kila mtu aliyepewa uwezo wa kufikiri auzingatie ujumbe huo kwa umakini mkubwa. Hukumu za kutisha zilizotangazwa dhidi ya ibada ya mnyama na sanamu yake (Ufunuo 14:9-11), zinapaswa kuwaongoza wote wajifunze kwa bidii nyingi unabii huo ili kujua alama ya mnyama ni kitu gani, na kwa jinsi gani wanaweza kuikwepa wasiipokee. Lakini sehemu kubwa sana ya watu wanageuza masikio yao wasitake kuisikia Ukweli, nao wanazigeukia hadithi za uongo zinazobuniwa. Mtume Paulo alipoangalia kushuka chini mpaka siku hizi za mwisho, alitangaza akisema: "maana utakuja wakati watakapoyakataa mafundisho yenye uzima." 2 Timotheo 4:3. Wakati huo umefika tayari. Umati mkubwa wa watu hawataki Ukweli wa Biblia kwa sababu unaingilia tamaa zao za moyo wenye dhambi, unaoipenda dunia hii (1 Yoh. 2:15-17), na mahali pake Shetani anawapa uongo wanaoupenda. [GC 594.2; PK Aya ya 4]

**Watu Wanaoitafuta Biblia**

Lakini Mungu atakuwa na watu Wake hapa duniani watakaoitetea na kuidumisha Biblia, na Biblia pekee, kama kiwango cha kupimia mafundisho yote na msingi wa matengenezo yote (daima). Maoni ya wasomi, mahitimisho yote yanayokisiwa-kisiwa tu na sayansi, imani za dini (creeds), au maamuzi ya mabaraza ya makanisa, ambayo ni mengi, tena yanagongana yenyewe kwa yenyewe kama yalivyo makanisa yanayoyawakilisha, sauti ya walio wengi - hakuna hata mojawapo au yote katika hayo ambayo yangefikiriwa kuwa ni ushahidi wa kuunga mkono au kulikataa jambo lolote la imani ya kidini. Kabla ya kulikubali fundisho, agizo, kanuni au amri yoyote, inatupasa kudai tamko lililo wazi lisemalo "Hivi ndivyo asemavyo Bwana" ili kuweza kuunga mkono fundisho hilo au kanuni hiyo. [GC 595.1; PK Aya ya 5]

Daima Shetani anajitahidi kuvuta usikivu wa watu uelekezwe kwa mwanadamu badala ya kuelekezwa kwa Mungu. Anawaongoza watu wawatazame

maaskofu wao, wachungaji wao, maprofesa wa theolojia, kama viongozi wao, badala ya wao wenyewe kuyachunguza Maandiko ili wajifunze na kuuelewa wajibu wao ni upi. Na kwa kuyatawala mawazo ya viongozi hao, Shetani anaweza kuwaongoza watu wengi sana kama atakavyo yeye. [GC 595.2; PK Aya ya 6]

**Maandiko Ni Ulinzi**

Kristo alipokuja duniani kutangaza Maneno ya uzima, watu wa kawaida walimsikiliza kwa furaha; na wengi, hata miongoni mwa makuhani na watawala, walimwamini. Lakini wakuu wa makuhani na viongozi mashuhuri, wa ngazi za juu taifa waliamua kuyalaani na kuyatupilia mbali mafundisho Yake. Ijapokuwa katika juhudi zao zote walijikanyaga wenyewe na kufeli kupata mashtaka yoyote dhidi Yake, ingawa hawakuweza kujizuia wasiusikie mvuto wa uweza na hekima ya Mungu vilivyoambatana na Maneno Yake, hata hivyo, walijifungia wenyewe kwa chuki yao isiyo na sababu; waliukataa ushahidi ulio wazi kabisa ulioonyesha kwamba Yeye Ndiye Masihi, ili wasije wakalazimika kuwa wanafunzi Wake. Wapinzani hawa wa Yesu, walikuwa ni watu ambao watu walikuwa wamefundishwa tangu utotoni kuwaheshimu watu ambao mamlaka yao walikuwa wamezoea kuisujudia na kuitii bila maswali. “Inakuwaje basi,” waliuliza, “kwamba viongozi wetu pamoja na waandishi wetu wasomi wasimwamini Yesu? Je! watu hawa wacha Mungu wasingempokea kama kweli angekuwa ni Kristo?” Ilikuwa kwasababu ya mvuto wa waalimu wa Maandiko kama hawa ndiyo taifa la Kiyahudi liliongozwa kumkataa Mkombozi wao. [GC 595.3; PK Aya ya 7]

Roho iliyowaendesha makuhani na watawala wa nchi bado ingali inadhihirishwa na wengi wanaojidai kuwa wao ni wacha Mungu sana. Wanakataa kuuchunguza ushuhuda wa Maandiko kuhusu zile Kweli maaalum zilizotolewa kwa ajili ya wakati huu. Wanasonda kidole kwenye idadi yao kubwa, utajiri wao, na umaarufu na kupendwa kwao na watu wengi, kisha wanawatazama kwa dharau watetezi wa Ukweli wakisema kuwa ni wachache mno, maskini, tena hawapendwi na watu wengi, pia wanayo imani inayowatenga mbali na ulimwengu. [GC 596.1; PK Aya ya 8]

**Kuitukuza Mamlaka Ya Kibinadamu**

Kristo aliona mpaka mbele, ya kwamba, kule kujinyakulia mamlaka kusikostahili walikokuwa nako Waandishi na Mafarisayo kusingekomeshwa wakati wa kutawanyika Wayahudi katika mataifa mbalimbali. Aliona kwa macho ya kinabii kazi ya kuyatukuza mamlaka ya kibinadamu ili kutawala dhamiri ya watu, jambo ambalo limekuwa laana ya kuogofya mno kwa kanisa, katika zama zote. Na maonyo ya kutisha aliyoyanena dhidi ya Waandishi na Mafarisayo na maonyo Yake kwa watu kwamba wasiwafuate viongozi hawa vipofu (Mt. 15:12-14),

mambo hayo yaliwekwa katika kumbukumbu kama maonyo na mwongozo kwa vizazivya baadaye. [GC 596.2; PK Aya ya 9]

Kanisa la Rumi linawapatia haki ya kufasiri Maandiko viongozi wa dini tu, yaani makasisi na maaskofu nk. Kwa misingi kuwa ni viongozi wa dini peke yao ndiyo wenye uwezo wa kulifafanua. Neno la Mungu, yaani Biblia limeondolewa kwa watu wa kawaida- (walei) hawa wanazuiwa kulisoma. (Angalia maelezo katika Nyongeza 18 mwisho.) Ingawa Matengenezo ya Kanisa yalifanya wote wawe na Maandiko, hata hivyo kanuni ile ile iliyoshikiliwa na Rumi inawazuia watu wengi ndani ya makanisa ya Kiprotestanti kuisoma na kuichunguza kwa undani Biblia wao wenyewe. Wanafundishwa kuyapokea mafundisho yake kama yalivyofasiriwa na kanisa lao; tena wapo maelfu ambao hawathubutu kulipokea Neno lolote, hata kama limefunuliwa kwa uwazi katika Maandiko, ambalo liko kinyume na itikadi yao ya dini (imani) au fundisho lolote lililokwishawekwa na kanisa lao. [GC 596.3; PK Aya ya 10]

Licha ya Biblia kujaa maonyo dhidi ya waalimu wa uongo, wengi kwa njia hiyo wako tayari kuzisalimisha roho zao mikononi mwa viongozi wa kanisa kama vile wachungaji, makasisi na maaskofu wao. Leo hii wapo maelfu wanaojiita kwamba wanayo dini ambao hawawezi kutoa sababu ya imani yao zaidi ya kusema tu kuwa wao wamefundishwa hivyo na viongozi wao wa dini. Wanapita pembeni bila kuyaona mafundisho ya Mwokozi kwa ukaribu na bila kuyatilia makini au kutoyajali kabisa, nao huweka imani yao bila kuwa na maswali katika maneno yanayonenwa na wachungaji wao. Lakini, je, wachungaji hao hawawezi kukosea kamwe? Twawezaje basi, kuziweka amana roho zetu kwenye uongozi wao, isipokuwa kama tunajua kutokana na Neno la Mungu kwamba wao ni wabeba nuru Yake? Ukosefu wa ujasiri wa kimaadili wa kuweza kutembea kando ya njia iliyozoeleka yaani, iliyotembelewa mara nyingi na ulimwengu huwafanya wengi wafuate nyayo za wasomi; na kwa kusita kwao kujibidisha kuchunguza wao wenyewe, na kisha wanajikuta wamenaswa katika minyororo ya mafundisho ya uongo au yenye makosa bila kuwa na matumaini yoyote. Wanaona kwamba Ukweli wa wakati huu unafunuliwa wazi katika Biblia; nao wanaisikia nguvu ya Roho Mtakatifu ikiambatana na utangazaji wake (hiyo Kweli); lakini bado wanaruhusu upinzani wa viongozi wa dini kama wachungaji, makasisi na maaskofu wao, kuwageuza mbali na nuru. Ingawa akili, busara na dhamiri yao vimeshawishika, roho hizi zilizodanganyika hawaziwezi kuthubutu kufikiri zenyewe mawazo yaliyo tofauti na mchungaji wao; na maamuzi yao binafsi kuhusu maslahi yao ya milele, hutolewa mhanga kwenye madhabahu ya kutokuamini, mashaka, kiburi, ubaguzi, na chuki ya mtu mwingine, isiyo na sababu. [GC 596.4; PK Aya ya 11]

**Kamba Laini Za Upendo**

Kuna njia nyingi ambazo Shetani anazitumia kufanya kazi yake kupitia mvuto wa kibinadamu ili kuwafunga barabara kama mateka wake. Anajipatia watu wengi kuja upande wake kwa kuwafunga kwa kamba za hariri za upendo na wale walio maadui wa msalaba wa Kristo. Haijalishi mshikamano huu ni upi, uwe ni upendo wa wazazi kwa watoto wao, uwe ni upendo wa watoto kwa wazazi wao, uwe ni uhusiano kati ya mume na mke, uwe ni uhusiano wa ndugu au uhusiano katika jamii, athari zake ni zile zile; wapinzani wa Ukweli wanatumia nguvu yao ili kutawala dhamiri ya mtu (kumdhibiti mtu asimwabudu Mungu atakavyo yeye mwenyewe), halafu roho zilizoshikwa chini ya utawala wake huwa hazina ujasiri au uhuru wa kutosha ili kuweza kukitii kile wanachokiamini moyoni mwao kuwa ndio wajibu wao unaowapasa kufanya. [GC 597.1; PK Aya ya 12]

Ukweli na utukufu wa Mungu havitenganishwi; haiwezekani kabisa kwetu sisi ambao tuna uwezo wa kuifanya Biblia iwe karibu nasi, tuendelee kumheshimu Mungu kwa kushikilia maoni yenye makosa. Wengi wanadai kwamba haijalishi kile ambacho mtu anakiamini ikiwa maisha yake ni sahihi au yapo sawa tu. Lakini maisha huendeshwa na imani. Ikiwa nuru ya Ukweli iko ndani ya uwezo wetu kuifikia, nasi tunazembea kuboresha fursa tulizonazo za kuisikia Kweli na kuiona nuru, basi, kusema kweli tumeukataa Ukweli kwa makusudi; tumechagua giza kuliko nuru (Yn. 3:19- 21). [GC 597.2; PK Aya ya 13]

**Maandiko Ni Ulinzi**

"Iko njia ionekanayo kuwa sawa machoni pa mtu, lakini mwisho wake ni njia za mauti." Mithali 16:25. Ujinga au kutojua, sio kisingizio cha kupokea mafundisho ya uongo au dhambi, wakati kuna kila nafasi ya kuyajua mapenzi ya Mungu. Mtu mmoja alikuwa anasafiri na akafika mahali ambapo alizikuta barabara kadhaa na ubao ulioeleza kila barabara inakokwenda. Endapo yeye hatakijali kibao kile chenye maelezo, na kuamua kupita barabara yoyote inayoonekana machoni pake, anaweza kuwa na nia njema (udhati) moyoni mwake, lakini uwezekano wake wa kujikuta yuko katika barabara isiyo sahihi ni asilimia mia moja. [GC 597.3; PK Aya ya 14]

**Jukumu La Kwanza Na La Juu Kabisa**

Mungu ametupatia sisi Neno lake ili tuyajue mafundisho Yake na tuelewe sisi wenyewe kile ambacho anakitaka kutoka kwetu. Wakati mwanasheria alipomjia Yesu na kumwuliza swali hili, "Nifanye nini ili niurithi uzima wa milele?" Mwokozi alimwelekeza kwenye Maandiko, akamwambia, "Imeandikwa nini katika torati? Wasomaje? (Lk. 10:25,26.) Ujinga au kutojua hakutoi udhuru kwa mdogo wala mkubwa kwa umri, wala kuwaokoa wasipatwe na adhabu inayowapasa kwa

kuivunja Sheria ya Mungu (Amri Zake); kwa sababu mikononi mwao wanalo wasilisho kamili lenye kuaminika juu ya Sheria na kanuni Zake, na madai Yake. Haitoshi kuwa na nia nzuriau makusudi mema peke yake; haitoshi kufanya kile ambacho mtu anadhani kuwa ni sahihi kwake au kile ambacho mchungaji wake anamwambia kuwa ni sahihi. Wokovu wa roho yake uko hatarini, isitoshe, ni yeye huyo mwenyewe ndiye anayepaswa kuyachunguza Maandiko hayo kwa manufaa yake mwenyewe. Haidhuru imani yake iwe na nguvu kiasi gani, haidhuru ameshawishika au kuwa na imani kiasi gani kwamba mchungaji wake anaujua Ukweli kiasi gani, huo sio msingi wake yeye. Kwani yeye anayo ramani, mwongozo unaomwonyesha kila alama ya njia katika safari yake ya kwenda mbinguni, naye hapaswi kukisia-kisia tu, au kubahatisha katika jambo lolote. [GC 598.1; PK Aya ya 15]

Ni wajibu wetu wa kwanza na wa juu kabisa kwa kila mmoja wetu aliye na akili timamu kujifunza mwenyewe kutoka katika Maandiko na kujua kile ambacho ni Ukweli, na halafu kutembea katika nuru hiyo na kuwatia moyo wengine kufuata mfano wake. inatupasa kujifunza Biblia siku baada ya siku kwa bidii, tukilipima kila wazo na kulilinganisha Andiko na Andiko (Isa. 28:9 -10,13). Kwa msaada wa Mungu inampasa kila mmoja wetu atafakari namna atakavyowajibika katika kujenga maoni yake mwenyewe na katika kutoa na kujibu taarifa zake mwenyewe mbele za Mungu (binafsi) [GC 598.2; PK Aya ya 16]

Ukweli ambao umefunuliwa wazi kabisa katika Biblia umetiliwa mashaka na kuwekwa giza na watu wenye elimu, ambao, huku wakijifanya kuwa wana hekima nyingi, wanawafundisha watu kwamba Maandiko yana maana yenye mafumbo, yenye maana ya siri na ya kiroho au ushirikina wa namna fulani (mystical), ambayo haionekani wazi katika lugha iliyotumiwa. Watu hawa ni waalimu wa uongo. Ilikuwa ni kwa tabaka kama hilo Yesu alisema Maneno haya kwa nguvu: “Kwa kuwa hamyajui maandiko wala uweza wa Mungu.” Marko 12:24. Lugha ya Biblia inapaswa kueleweka kulingana na maana yake iliyopo humo ndani ambayo inaeleweka wazi, isipokuwa pale ambapo ishara imetumiwa, mfano, au kielelezo kama hesabu au umbo fulani vimetumika pale. Kristo ametupa sisi ahadi Yake inayosema: “Mtu akipenda kufanya mapenzi Yake, atajua habari ya yale mafunzo, kwamba yatoka kwa Mungu, au kwamba Mimi nanena kwa nafsi Yangu tu.” Yohana 7:17. Endapo wanadamu wangeielewa Biblia kama inavyosomeka, kama wasingekuwako walimu wa uongo wanaopotosha na kuvuruga akili zao, basi, kazi ingetimizwa ambayo ingelifanya malaika wafurahi na nayo ingeleta katika zizi la Kristo maelfu kwa maelfu ambao sasa wanamangamanga katika makosa: “Mtu akipenda kuyatenda mapenzi Yake Mungu, atajua habari ya yale mafunzo kwamba yatoka kwa Mungu, au kwamba nanena kwa nafsi yangu tu.” Yohana 7:17. [GC 598.3; PK Aya ya 17]

Inatupasa tusishinikize nguvu zetu zote za akili katika kujifunza Maandiko, tena tuupe kazi ufahamu wetu kuelewa kwa kadiri sisi wanadamu wenye hali ya kufa tuwezavyo, ili tupate kuyaelewa mambo yale mazito na ya kina ya Mungu; lakini haitupasi kusahau kwamba roho ya dhati ya yule anayejifunza ni ile roho ya utiifu na unyenyekevu kama mtoto mdogo, hiyo ndiyo roho ya kweli ya mwanafunzi wa Biblia (Mt. 11:29). Matatizo yanayopatikana katika kuyaelewa Maandiko hayawezi kutatuliwa kamwe kwa kutumia njia zile zile zinazotumika katika kujitahidi  kuchambua na kuhitimisha matatizo ya kifalsafa. Kamwe tusiingie katika kujifunza Biblia tukiwa na hali ya kujitegemea wenyewe kama ile wanayoingia nayo wengi katika uwanja wa sayansi, sisi tunapaswa kuingia kwa maombi yenye kumtegemea Mungu na shauku ya dhati ya kujifunza mapenzi Yake. Ni lazima tuje na roho ya unyenyekevu, na roho iliyo tayari kufundishika, ili kupata maarifa kutoka kwa Mwenyezi Mungu, Yeye ambaye ni  MIMI NIKO. Vinginevyo, malaika waovu watatapofusha ubongo wetu sana na kuifanya mioyo yetu kuwa migumu kiasi cha kutoweza kuguswa  na kupokea Ukweli (Mt. 13:19). [GC 599.1; PK Aya ya 18]

Sehemu nyingi za Maandiko ambazo wasomi wanazitangaza kuwa ni mafumbo au siri, au wanaziruka kwa kigezo kuwa hazina maana au umuhimu, zimejaa faraja na mafundisho kwa yule ambaye amepata mafunzo yake katika shule ya Kristo (Mt. 11:29; Lk. 10:39, 42). Sababu moja inayowafanya wanatheolojia wengi kutokuwa na uelewa sahihi au ulio wazi zaidi wa Neno la Mungu ni kwamba hufumba macho yao wasiziangalie zile Kweli ambazo hawataki kuziishi katika mitindo yao ya maisha (Eze. 22:26). Ufahamu wa Ukweli wa Biblia hautegemei sana juu ya uwezo na nguvu ya akili inayotumika katika kufanya utafiti, bali hutegemea zaidi  unyofu wa kusudi, pamoja na matamanio ya dhati yatokayo moyoni ya kuitafuta haki, na kuishi maisha ya utakatifu. [GC 599.2; PK Aya ya 19]

**Atawafundisha Yote**

Kamwe Biblia isijifunzwe bila maombi (haifai). Roho Mtakatifu pekee Ndiye anayetuwezesha sisi tuchomwe mioyo na kuona umuhimu wa mambo yale ambayo ni rahisi kueleweka, au kutuzuia tusianze kupotosha zile Kweli ambazo ni ngumu kwetu kuzielewa (Yn. 16:13). Ni kazi ya ofisi ya malaika wa mbinguni kuuandaa moyo wetu kwa njia ambayo tunaweza kulielewa Neno la Mungu na kisha tuweze kuvutwa na kutekewa na sumaku ya uzuri Wake, kubadilishwa kwa kutii maonyo yake, au kuchangamshwa na kuimarishwa kwa ahadi Zake. Tungeifanya dua ya Mwandishi wa Zaburi kuwa yetu:”Unifumbue macho yangu niyatazame Maajabu yatokayo katika sheria Yako.” Zaburi 119:18. Mara nyingi majaribu yanaonekana kuwa hayawezi kupingika au kuzuilika kwa sababu, kwa njia ya kuzembea katika maombi pamoja na kujifunza Biblia, mtu anayejaribiwa hawezi kuzikumbuka kwa urahisi ahadi za Mungu na kumkabili Shetani kwa

kutumia silaha hizo za Maandiko. Lakini malaika wamewazunguka pande zote wale wanaopenda Maaandiko na wako tayari kuwafundishwa mambo ya Mungu; na wakati watakapokuwa na hitaji/shida kubwa wataweza kuzikumbuka Kweli zile zile ambazo zinahitajika kwa wakati huo. Hivyo: “Wakati adui atakapokuja kama mafuriko, Roho wa Bwana atainua kiwango dhidi yake.” Isaya 59:19. [GC 599.3; PK Aya ya 20]

Yesu aliwaahidi wanafunzi Wake, akisema: “Lakini huyo Msaidizi, huyo Roho Mtakatifu, ambaye Baba atampeleka kwa Jina Langu, atawafundisha yote, na kuwakumbusha yote niliyowaambia.” Yohana 14:26. Lakini mafundisho ya Kristo yanatakiwa yawe yamehifadhiwa mapema katika akili ili Roho wa Mungu aweze kutukumbusha wakati wa hatari. Daudi anasema “Moyoni mwangu nimeliweka Neno Lako, Nisije nikakutenda dhambi.” Zaburi 119:11. [GC 600.1; PK Aya ya 21]

Watu wote wanaothamini maslahi ya milele wanapaswa kuwa macho kujilinda dhidi ya kuvamiwa na nadharia za mashaka kuhusu mambo ya Mungu wasiyoweza kuyathibitisha wenyewe (wachunge kutoamini). Nguzo muhimu za Ukweli zitashambuliwa vibaya. Haiwezekani kabisa kutofikiwa na mafundisho yenye sumu za kufisha, yatokanayo na ukafiri wa kisasa, kejeli na falsafa za udanganyifu. Shetani anayabadilisha-badilisha majaribu kwa kulingana na tabaka zote za watu. Wakati anawashambulia vibaya wale wasiojua kusoma na kuandika kwa kuwatania au kuwakenulia meno kwa kicheko cha dharau, anawakabili wale wenye visomo kwa vipingamizi vya kisayansi na hoja za kifalsafa, mbinu hizi zote zimekorokorotolewa ili kuchochea mashaka au dharau dhidi ya Maandiko. Hata vijana walio na uzoefu mdogo sana wanapenyeza mashaka waliyo nayo juu ya kanuni zile za msingi za Ukristo. Na ukafiri huu wa vijana, japo hauna kina kwa kawaida, bado una mvuto wake. Kwa njia hiyo wengi wanashawishiwa kukejeli imani ya baba zao na kumtendea jeuri Roho wa neema.Waebrania 10:29. Maisha ya watu wengi yaliyotoa mwelekeo wa matumaini kumletea Mungu heshima na kuwa baraka kwa ulimwengu huu yamechafuliwa na pumzi inayonuka vibaya ya ukafiri huo. Wale wote wanaoyatumainia maamuzi yenye majivuno kutokana na hoja za kibinadamu, na wanaweza kuzieleza siri na mafumbo ya Mungu (Kum. 29:29) na kufikia Ukweli bila kupata msaada wa Mwenyezi Mungu, wanajinasa wenyewe katika mtego wa Shetani uliojificha. [GC 600.2; PK Aya ya 22]

Tunaishi katika kipindi cha kutisha sana cha historia ya ulimwengu huu. Hatima ya umati mkubwa wa watu wa dunia ipo karibu sana kuamuliwa. Hali yetu njema ya baadaye na pia wokovu wa watu wengine hutegemea njia ambayo tunaifuata sasa. Tunahitaji kuongozwa na Roho wa Ukweli. Kila mfuasi wa Kristo anapaswa kujihoji kwa dhati: “Bwana, inanipasa mimi nifanye nini?” Tunahitaji kujinyenyekeza wenyewe mbele Zake Bwana kwa kufunga na kusali, na kulitafakari sana Neno Lake, hasa kuhusu matukio ya hukumu. Hivi sasa tunapaswa kutafuta uzoefu wa maisha wenye kina na ulio hai katika mambo ya

Mungu. Hatuna muda wa kupoteza. Matukio ya muhimu sana yanatokea kila mahali kutuzunguka; sisi tuko katika uwanja wa Shetani unaopendeza na kuvutia kwa uchawi wake. Msisinzie, Enyi walinzi na skari wa Mungu; adui anawanyemelea karibu, naye yu tayari kwa dakika yoyote kuwarukia na kuwafanya kitoweo chake endapo mtazembea na kutekewa na usingizi. [GC 601.1; PK Aya ya 23]

Wengi wamedanganyika kuhusu hali yao halisi ilivyo mbele za Mungu. Wanajipongeza wenyewe kwa matendo maovu ambayo hawafanyi, na wanasahau kuorodhesha matendo mema ya kufanya na tabia inayofaa ambayo ambayo Mungu anataka wawe nayo, lakini ambayo wao wamezembea kuwa nayo. Haitoshi tu kwamba wao ni miti katika shamba la Mungu. Wanapaswa kutimiza matarajio Yake kwa kuzaa matunda. Anawawajibisha kwa kushindwa kwao kutekeleza mema yote ambayo walipaswa kuyafanya kwa njia ya neema Yake ambayo ingewatia nguvu. Katika vitabu vya mbinguni wameandikwa kama watu wanaoleta usumbufu mwingi duniani wanailemea bure ardhi au lishe ya udongo. Lakini kesi ya kundi hilo la watu bado si ya kuikatia tamaa kabisa, yaani ina matumaini bado kwa sasa. Kwa wale walioidharau rehema ya Mungu na kuitukana neema Yake, moyo wa upendo unaovumilia kwa muda mrefu bado unawasihi: "Amka wewe uliyelala, fufuka kutoka wafu, naye Kristo atakuangaza." Basi angalieni jinsi mnavyoenenda, ... mkiukomboa wakati kwa maana zamani hizi ni za uovu." Waefeso 5:14-16. [GC 601.2; PK Aya ya 24]

Wakati wa kujaribiwa utakapofika, wale ambao wamelifanya Neno la Mungu kuwa kanuni yao ya maisha watafunuliwa (Ufu. 3:10). Wakati wa majira ya joto hakuna tofauti kubwa inayoonekana kati ya miti ile isiyokauka majani yake mwaka mzima, hata wakati wa baridi na barafu kali, na miti ile mingine; lakini wakati wa majira ya baridi kali na theluji unapoingia, miti ile ambayo majani yake hayakauki, inabaki bila kubadilika, wakati miti mingine inapoteza majani yote*. Hivyo ndivyo wale walio na mioyo ya unafiki, wanaojidai kuwa ni Wakristo wasivyoweza kutofautishwa sasa na Wakristo wa Kweli, lakini wakati upo njiani kabisa ambapo tofauti hiyo itaonekana waziwazi kabisa. Acha upinzani utokee, acha chuki, ubaguzi na ushupavu wa dini usiotumia akili na hali ile ya kukosa uvumilivu kwa imani ya wengine vishike hatamu tena, acha mateso na yaamshwe, ndipo wale walioongoka nusu nusu (Laodikia) na wanafiki watakapoyumba-yumba vibaya sana na kuiacha mbali imani yao; lakini Mkristo wa Kweli atasimama kidete kama mwamba, imani yake ikiwa na nguvu zaidi, na tumaini lake litang'aa zaidi, kuliko katika siku zile za mafanikio yake *(miti ya kijani daima au evergreen kama mipaini na miti ya Krismasi yenyewe daima majani yake ni ya kijani, hata wakati wa theluji na baridi kali sana, wakati huo miti mingine yote hupukutisha majani yake yote). [GC 602.1; PK Aya ya 25]

Mwandishi wa Zaburi anasema hivi: “Maana shuhuda Zako ndizo nizifikirizo.” “Kwa mausia Yako najipatia ufahamu; Kwa hiyo nachukia kila njia ya uongo.” Zaburi 119:99, 104. [GC 602.2; PK Aya ya 26]

Mwenye Heri au “Mwenye furaha ni mtu yule apataye hekima.” “Atakuwa kama mti uliopandwa kando ya maji, uenezao mizizi yake karibu na mto, hautaona joto lijapo, lakini jani lake litakuwa bichi; wala hautahangaika mwaka wa uchache, wala hautaacha kuzaa matunda. Mithali 3:13; Yeremia 17:8. [GC 602.3; PK Aya ya 27]

# SURA YA 38

# UJUMBE NA ONYO LA MWISHO

**(Kwa Ulimwengu Wote)**

Ufupisho: Uwezo wa Shetani kulaghai ni mkubwa sana binadamu anapochagua kubaki mjinga wa maarifa ya Mungu. Katika kila zama kumekuwa na mapambano yaliyoamuliwa ya Ukweli dhidi ya uongo au makosa ya Mafundisho ya Mungu. Lakini aliye mkuu zaidi Yuko mbele tu. Mojawapo ya majanga makubwa zaidi ya enzi zote mbele ni Babeli ya wakati huu, maana imeamuliwa katika maandiko kwamba, dhambi zake zimefika mbinguni na MUNGU amekumbuka maovu yake. Ufunuo 13 inatabiri wakati ulio mbele yetu ambao wale wanaoheshimu Kweli za msingi za Biblia watashutumiwa kuwa adui wa sheria na utaratibu wa nchi. Ni lazima kila mtu binafsi ajue NENO la MUNGU kwa ajili yake mwenyewe, ili aweze kusimama upande wa kuume wa Mungu katika siku hiyo ya Bwana.

"Naliona malaika mwingine, akishuka kutoka mbinguni, mwenye mamlaka kuu; na nchi ikaangazwa kwa utukufu wake. Akalia kwa sauti kuu, akisema, Umeanguka, umeanguka Babeli ule mkuu; umekuwa maskani ya mashetani, na ngome ya kila roho mchafu, na ngome ya kila ndege mchafu mwenye kuchukiza; Kisha nikasikia sauti nyingine kutoka mbinguni, ikisema, Tokeni kwake, enyi watu Wangu, msishiriki dhambi zake, wala msipokee mapigo yake" Ufunuo 18:1, 2, 4. [GC 603.1; PK Aya ya 1]

Andiko hili linaelekeza mbele wakati ambapo tangazo la anguko la Babeli, kama lilivyotolewa na malaika wa pili wa Ufunuo 14 (Fungu la 8), litakaporudiwa, likiwa na nyongeza ya orodha ya matendo ya kifisadi ambayo yamekuwa yakiingia katika mashirika mbalimbali ambayo yanaunda Babeli, kwa kuwa ujumbe huo ulitolewa kwa mara ya kwanza, katika majira ya joto ya mwaka 1844. Hali ya kutisha ya ulimwengu wa kidini imeelezwa hapa. Kwa kila tukio la kuukataa Ukweli, akili za watu wanaohusika zinazidi kutiwa giza na mioyo yao inazidi kuwa mikaidi zaidi mpaka wanajichimbia kwenye ukafiri mgumu zaidi. Kwa kupinga kwa ushupavu na kuyadharau maonyo ambayo Mungu ametoa, wataendelea kukanyaga na miguu yao moja ya kanuni ya Dekalojia (Amri Kumi), mpaka wataanza kuwatesa wale wanaoitakasa amri hiyo, yaani wanayoitunza kama takatifu. Kristo amebatilishwa na kuonekana kwao ni sifuri kwasababu ya dharau iliyowekwa juu ya Neno Lake na watu Wake. Jinsi mafundisho ya umizimu yanavyopokelewa na kukubaliwa na makanisa, kizuizi kilichowekwa juu ya moyo usiozaliwa upya upendao matendo ya mwili kimeondolewa, na kuikiri kwao kuwa mtu wa dini kutakuwa joho la kuficha maovu yaliyopitiliza. Imani katika maonyesho ya kiroho inafungua mlango kwa roho zidanganyazo na mafundisho ya mashetani na kwa njia hiyo mvuto wa malaika hao waovu utahisiwa na kuonekana katika makanisa (yasiyofuata sheria za Mungu). [GC 603.2; PK Aya ya 2]

Kuhusu Babeli, kwa wakati ilivyoonyeshwa katika unabii huu, imeelezwa: "Kwa maana dhambi zake zimefika hata mbinguni, na Mungu amekumbuka

maovu yake." Ufunuo 18:5. Babeli amejaza kikombe cha maovu yake na maangamizi yake yanakaribia kuiangukia. Lakini Mungu bado anao watu Wake katika Babeli na kabla ya kutekelezwa kwa hukumu Zake, watu hao waaminifu ni lazima waitwe watoke nje, ili wasishiriki dhambi zake na "wasipokee mapigo yake." Ndiyo maana kuna vuguvugu linawakilishwa na malaika anayeshuka kutoka mbinguni, akiangazia dunia kwa utukufu wake na akilia kwa nguvu na sauti kuu, akitangaza dhambi za Babeli. Pamoja na ujumbe wake, sauti inayobeba mwito inasikika ikisema: "Tokeni kwake, watu Wangu." Matangazo haya, yakiungana na ujumbe wa malaika wa tatu, huunda onyo la mwisho litakalotolewa kwa wakazi wote wa dunia. (Ufunuo 14:9-12). [GC 604.1; PK Aya ya 3]

Tukio litakaloujia ulimwengu ni la kutisha sana. Mamlaka za dunia, zikiungana kupigana vita dhidi ya amri za Mungu, zitatoa amri kwamba "Wote, wadogo kwa wakubwa, na matajiri kwa maskini, na walio huru kwa watumwa, watiwe chapa katika mkono wao wa kuume, au katika vipaji vya nyuso zao;" Ufunuo 13:16. Wafuate desturi za kanisa kwa kutunza na kutakasa sabato ya uongo (Isiyo kwenye amri za Mungu yaani Jumapili). Wale Wote wanaokataa kutii agizo hilo watahukumiwa kwa adhabu za kiraia yaani mujibu wa sheria za serikali ya nchi na hatimaye watatangazwa kwamba wanastahili kifo. Kwa upande mwingine, sheria ya Mungu inayoagiza mapumziko ya siku ya Muumbaji inadai utii na inatishia hasira dhidi ya wale wote wanaovunja kanuni Zake (soma amri ya nne). [GC 604.2; PK Aya ya 4]

Baada ya agizo hilo kuletwa kwa uwazi mbele ya kila mtu basi mtu yeyote atakayeikanyaga sheria ya Mungu ili kutii maagizo ya mwanadamu anapokea chapa au alama ya mnyama; anakubali ishara ya utii wake kwa mamlaka ambayo anachagua kuitii badala ya Mungu. Onyo kutoka mbinguni ni hili "Mtu awaye yote akimsujudu huyo mnyama na sanamu yake, na kuipokea chapa katika kipaji cha uso wake, au katika mkono wake, yeye naye atakunywa katika mvinyo ya ghadhabu ya Mungu iliyotengenezwa, pasipo kuchanganywa na maji, katika kikombe cha hasira Yake." Ufunuo 14:9, 10. [GC 604.3; PK Aya ya 5]

Lakini hakuna hata mmoja atakayeteswa au kukutana na ghadhabu ya Mungu (soma zaidi kuhusu mapigo saba) mpaka Ukweli utakapofunuliwa na kuingia katika akili yake na dhamiri yake na kisha ukataliwe. Kuna watu wengi ambao hawajawahi kupata fursa ya kusikia Ukweli maalumu wa wakati huu, ulazima wa amri ya nne, na wajibu wao kuitekeleza, haujawasilishwa kamwe mbele yao katika nuru yake halisi ili waelewe. Yeye anayesoma kila moyo na kulipima kusudi na nia ya kila moyo hatamwacha hata mtu mmoja mwenye matamanio ya kujua Ukweli, adanganywe kuhusu masuala ya msingi katika pambano hilo. Amri hiyo haitashinikizwa kwa watu katika hali ya upofu. Kila mtu atapewa nuru ya

kutosha ili apate kufanya uamuzi wake akitumia akili na busara. [GC 605.1; PK Aya ya 6]

### Jaribio Kuu La Utii Wetu

Sabato ndiyo itakuwa kipimo kikuu cha utiifu (uadilifu), kwa kuwa ndicho kipengele cha Ukweli kinachobishaniwa zaidi kuliko vingine vyote (kimepachikwa utata mwingi na watu). Wakati jaribio la mwisho litakapoletwa juu ya wanadamu, ndipo mstari utachorwa unaotofautisha kati ya wale wanaomtumikia Mungu na wale wasiomtumikia Yeye. Wakati ambapo ule utunzaji wa sabato ya uongo kwa kufuata sheria ya serikali ya nchi kinyume na ile amri ya nne (Kutoka 20:8-11), itakuwa ni kiapo cha utii kwa mamlaka iliyo kinyume na Mungu, utunzaji wa Sabato ya Kweli, katika kutii sheria ya Mungu, ni ushahidi wa utii na uaminifu kwa Muumbaji. Wakati tabaka moja, kwa kukubali alama ya kujisalimisha kwa mamlaka za kidunia, wanapokea alama ya mnyama, na tabaka lingine likichagua ishara ya utii kwa mamlaka ya Mungu, wanapokea muhuri wa Mungu. (Ufunuo 13:16,17 na Ufunuo 7:1-4). [GC 605.2; PK Aya ya 7]

Mpaka wakati huu, wale waliowasilisha au kuhubiri Ukweli wa ujumbe wa malaika wa tatu, mara nyingi wamechukuliwa kuwa watu wanaotoa tahadhari za kustua ambazo ni uvumi tu (Ufunuo 14:9-12). Utabiri wao usemao kwamba kukosa uvumilivu wa kidini (kutovumilia itikadi za dini za wengine) kutapata nafasi ya kujizatiti tena katika nchi ya Marekani, kwamba kanisa na serikali vitaungana Pamoja kwa madhumuni ya kuwatesa wale wanaozishika amri za Mungu, umetamkwa kuwa hauna msingi na ni upuuzi mtupu. Imetangazwa kwa ujasiri kwamba nchi hii ya Marekani, haiwezi kamwe kufanya tofauti na vile ilivyofanya zamani—"Marekani imekuwa na itaendelea kuwa mtetezi wa uhuru kidini". Lakini kwa vile hoja ya ulazimishaji wa utunzaji wa Jumapili imezidi kuhamasishwa sana, tukio hilo lililotiliwa mashaka na kutoaminiwa kwa muda mrefu linaonekana linakaribia (lipo njiani) na ujumbe wa malaika wa tatu utaleta matokeo ambayo hayajawahi kuletwa hapo awali. [GC 605.3; PK Aya ya 8]

Katika kila kizazi Mungu ametuma watumishi Wake ili waikemee dhambi, kote ulimwenguni na kanisani. Lakini watu wanapenda kuambiwa mambo laini tu, ila ule Ukweli ulio safi, usioficha makosa au usiopakwa virangi-rangi wao hawaukubali (Isaya 30:8-14). Wanamatengenezo wa kanisa wengi, walipoanza kazi yao, waliazimia kutumia busara nyingi katika kushambulia dhambi za kanisa na taifa, walitumaini kwa kielelezo cha maisha safi ya Kikristo, wangeweza kuwaongoza watu warudi kwenye mafundisho ya Biblia. Lakini Roho wa Mungu akaja juu yao kama alivyokuja kwa Eliya, na kumsukuma kukemea dhambi za mfalme mwovu na watu walioasi; hawakuweza kujizuia kuhubiri Matamko ya wazi ya Biblia--Mafundisho yale makuu ambayo walikuwa wamesitasita

kuyawasilisha. Walisukumwa kutangaza kwa bidii Ukweli licha ya kuwepo kwa hatari ambazo zilitishia roho, Maneno ambayo Bwana aliwapa waliyasema, bila woga wa matokeo au athari, nao watu walilazimishwa kusikia onyo. [GC 606.1; PK Aya ya 9]

**Ujumbe Kutangazwa Kwa Nguvu**

Hivyo ndivyo ujumbe wa malaika wa tatu utakavyotangazwa. Wakati utakapofika kwa ujumbe huo kuhubiriwa kwa nguvu nyingi mno, Bwana atatenda kazi kupitia kwa vyombo Vyake vinyenyekevu, akiongoza akili za wale wanaojiweka wakfu kwa utumishi Wake (kufanya kazi Yake). Watenda kazi watawezeshwa kwa upako wa Roho Wake Mtakatifu, waweze kuwa na sifa za kufaa kwa kuangaziwa Roho Wake, kuliko kutokana na mafunzo ya taasisi za wasomi wenye elimu kubwa. Watu wenye imani na maombi watabidishwa kusonga mbele kwa bidii takatifu, wakitangaza Maneno ambayo Mungu amewapa. Dhambi za Babeli zitawekwa wazi kabisa, matokeo ya kutisha ya kushinikiza utunzaji wa maadhimisho ya kanisa kupitia sheria za kiraia za serikali, uvamizi wa imani ya umizimu (ndani ya kanisa), na maendeleo ya kimya au chini chini lakini ya kasi ya mamlaka ya upapa,-- yote haya yatafichuliwa wazi. Kwa maonyo haya mazito maelfu kwa maelfu watazinduliwa kutoka kwenye usingizi ambao hawajapata kusikia Maneno kama haya, nao watasikiliza. Kwa mshangao watasikia ushuhuda kwamba Babeli ni kanisa lililoanguka kwa sababu ya mafundisho yake yenye makosa na dhambi zake, kwa sababu ya kukataa kwake Ukweli uliotumwa kwake na mbingu. Kadiri watu watakavyokwenda kwa waalimu wao wa awali (walimu wa maandiko au viongozi wa kiroho) na kuuliza kwa shauku, kwamba, Je! mambo haya ndivyo yalivyo? Wachungaji huwasilisha hekaya za uongo, yaani hutabiri na kuhubiri mambo laini, ili kutuliza hofu zao na kuzituliza dhamiri zao zilizoamshwa. Lakini kwa kuwa wengi watakataa kuridhika na mamlaka tu ya wanadamu na kudai wazi "Hivi ndivyo asemavyo Bwana," hapo ndipo wale wahudumu na viongozi wa Neno wa kidini kama walivyokuwa Mafarisayo maarufu wa zamani, watajaa hasira kali kwa kulitiliwa mashaka au kuhojiwa, watakemea ujumbe huo na kusema kwamba unatoka kwa Shetani, kisha watawachochea watu wanaopenda dhambi ili wawatukane na kuwatesa wale wanaoutangaza ujumbe huo. [GC 606.2; PK Aya ya 10]

**Pambano Laenea**

Kadiri pambano hilo linapotapakaa hadi kufika katika maeneo mapya na akili za watu kuvutwa kugundua sheria ya Mungu iliyokanyagwa chini, Ndipo Shetani atakapochachamaa na kufurukuta. Uwezo unaoandamana na ujumbe huo utawatia wenda wazimu wa mbogo wale wanaoupinga. Viongozi wa kidini watatumia nguvu nyingi ambazo zinakaribia kabisa kupita uwezo wao wa kibinadamu ili kuzima nuru hiyo isije ikawamulika washiriki wao. Kwa kutumia

kila njia iliyo katika uwezo wao watajitahidi kuzuia kabisa mjadala wowote juu ya maswali haya nyeti. Kanisa litaomba msaada wa mkono wenye nguvu wa serikali (rungu la dola), na katika kazi hii wafuasi wa upapa na Waprotestanti wataungana kuwa kitu kimoja. Kadiri vuguvugu la utekelezaji sahihi wa ulazimishaji wa mchakato wa uzingatiaji wa sheria Jumapili zinavyozidi kuwa na ujasiri mkubwa zaidi na kuwekewa mikakati iliyodhamiriwa, sheria itatungwa kukata rufaa kwa mamlaka (bungeni) dhidi ya wale wanaotunza amri kumi za Mungu. Watatishiwa kutozwa faini na kupelekwa magerezani na wengine watapewa madaraka makubwa, zawadi, marupurupu au fursa zingine, kama vivutio vya kuwafanya waikane imani yao. Lakini jibu lao lisilobadilika ni: "Tuonyesheni makosa yetu kutoka katika Neno la Mungu"—Watatoa ombi kama lile lililotolewa na Luther (Mwanamatengenezo wa Ujerumani) katika mazingira kama hayo. Watu wanaofikishwa mahakamani kushtakiwa watatoa ushuhuda thabiti wenye nguvu kwa ajili ya kuutetea Ukweli kwa nguvu, na baadhi ya wale wanaousikiliza huu Ukweli wanaongozwa kuchukua uamuzi wa kusimama pamoja na wale wanaotunza amri zote za Mungu. Kwa njia hiyo, nuru itapelekwa mbele ya maelfu ambao kama isingekuwa kwa njia hiyo, wasingepata fursa ya kuujua Ukweli huu. [GC 607.1; PK Aya ya 11]

Utii uliojengwa juu wa Neno la Mungu utachukuliwa kuwa ni uasi. Kwa kupofushwa macho na Shetani, mzazi atatumia ukali na ukatili dhidi ya mtoto aaminiye Ukweli; bwana au bibi (kibaruani au nyumbani) atamkandamiza mtumishi wake anayezishika amri za Mungu. Upendo utatoweka na mafarakano yataingia; watoto watakataliwa, na kunyang'anywa urithi wao na hata kufukuzwa kutoka majumbani mwao. Maneno ya Paulo yatatimizwa Neno kwa Neno: "Naam, na wote wapendao kuishi maisha ya utauwa katika Kristo Yesu wataudhiwa." 2 Timotheo 3:12. Watetezi wa Ukweli watakapokataa kuheshimu sabato-ya-Jumapili, baadhi yao watatupwa gerezani, wengine watafukuzwa nje ya nchi yao na kwenda uhamishoni (wakimbizi), wengine watafanywa kuwa watumwa. Kwa hekima ya kibinadamu haya yote sasa yanaonekana kama vile hayawezekani; lakini Roho wa Mungu anayezuia atakapoondolewa kutoka kwa wanadamu, watu watabaki chini ya mamlaka ya Shetani, ambaye anazichukia kanuni za Mungu, hapo ndipo kutakuwa na matukio ya ajabu. Moyo unaweza kuwa na ukatili wa kutisha wakati hofu ya Mungu na upendo Wake vinapokuwa vimeondolewa. [GC 608.1; PK Aya ya 12]

Wakati dhoruba inapokaribia, tabaka kubwa la wale watu waliopata kuikiri imani katika ujumbe wa malaika wa tatu (waumini kwa jina tu), ila hawakutakaswa kwa kuitii ile Kweli, watauacha msimamo wao na kujiunga na safu ya jeshi la wapinzani (Ufunuo 19:19). Kule kuungana kwao na ulimwengu na kushiriki katika roho ya ulimwengu, kutawafanya waangalie mambo kwa mtizamo wa karibu na huo; wa ulimwengu na wakati jaribu au mtihani unapokuja,

watakuwa wamejiandaa tayari kuchagua upande ulio rahisi, unaopendwa na wengi na maarufu. Watu mashuhuri, wenye talanta au vipaji vya pekee na wazunguzaji wenye hotuba za kupendeza, ambao hapo awali walifurahia Ukweli huo, watatumia mivuto yao kudanganya na kupoteza watu. Wanatokea kuwa maadui wachungu sana kwa ndugu zao wa zamani (waumini wenzao). Wakati watunza-Sabato watakapoletwa mbele ya mahakama ili kujibu maswali kuhusu imani yao, hawa waasi wa imani ndio watakuwa mawakala wazuri zaidi wa Shetani katika kuwawakilisha na kuwashtaki, na kwa kutoa ripoti za uwongo na kuwasingizia kiasi cha kuwachochea watawala dhidi yao. [GC 608.2; PK Aya ya 13]

Katika kipindi hiki cha mateso, imani ya watumishi wa Bwana itajaribiwa. Wakiwa wamekwisha kutoa onyo kwa uaminifu, wanamwangalia Mungu Na Neno Lake pekee. Roho wa Mungu, ameigusa mioyo yao, na amewabidisha kusema. Wakiwa wamesukumwa na bidiii takatifu na nguvu ya Mungu ikiwa juu yao, Wataanza kuingia katika utendaji wa majukumu yao bila kuhofia au kukorokotoa kichwani matokeo ya kuwaambia watu Neno ambalo Bwana atawapa. Hawatajali maslahi au faida za kitambo, wala hawatajali kutafuta heshima yao, sifa zao au maisha yao. Hata hivyo, wakati wa dhoruba ya upinzani na dhihaka itakapowapasukia juu yao, wengine, watalemewa na hofu kuu na mshangao, na kisha watatamka ghafula wakisema: "Ikiwa tungekuwa tumejua mapema matokeo ya maneno yetu, tungekuwa tumenyamaza kimya kabisa." Watazingirwa na dhiki kubwa. Shetani atawashambulia kwa majaribu makali. Kazi ambayo walipewa kuifanya inaonekana kuwazidi uwezo wao kuikamilisha. Wanatishiwa kuuawa. Juhudi iliyowachochea kwanza inatoweka; lakini hawatakuwa na uwezo wa kurudi nyuma. Kisha, wanapojisikia kuwa ni dhaifu na wasio na msaada kutoka kwao wenyewe kabisa, watamkimbilia Yeye Mwenye Nguvu zote ili awape nguvu. Wanakumbuka kwamba Maneno ambayo walinena hayakuwa yao, bali ni Yake Yeye aliyewaagiza watoe onyo. Mungu aliweka Ukweli mioyoni mwao na hawakuweza kujizuia kuutangaza. [GC 608.3; PK Aya ya 14]

Majaribu kama hayo yalishawapata watu wa Mungu katika zama zilizopita. Wycliffe, Huss, Luther, Tyndale, Baxter, Wesley, walisisitiza kwamba mafundisho yote ya dini sharti yapimwe kwa Biblia nao walitangaza kwamba wangekataa kila kitu ambacho Biblia ilikishutumu au kukikataza. Mateso yenye ghadhabu isiyo na huruma na yasiyokoma yalielekezwa dhidi yao kwa hasira kali; hata hivyo hawakuacha kuutangaza Ukweli. Vipindi mbalimblai na tofauti katika historia ya kanisa vina alama na kila kimoja kikiwa na ukuzaji wa Ukweli fulani maalumu (wa kipekee) uliogunduliwa, kukidhi mahitaji ya watu wa Mungu kwa wakati huo. Kila Ukweli mpya ulipenya dhidi ya chuki na upinzani na kusonga mbele; wale waliobarikiwa na nuru ya Ukweli huo waliteswa na kujaribiwa. Bwana anatoa

Ukweli maalumu kwa watu wakati wa dharura, Ni nani wanathubutu kukataa kuutangaza? Anawaagiza watumishi Wake kutangaza mwaliko/wito wa mwisho wa rehema kwa ulimwengu mzima. Hawawezi kukaa kimya, isipokuwa kwa kuhatarisha roho zao. Mabalozi wa Kristo hawapaswi kabisa kufikiria juu ya matokeo ya kutekeleza agizo la Mungu. Ni lazima watekeleze wajibu wao na kuacha mikononi mwa Mungu matokeo. [GC 609.1; PK Aya ya 15]

### Upinzani Wafikia Vilele Vipya

Upinzani unapozidi kuinuka na kufikia kilele cha ukali wake, watumishi wa Mungu wanafadhaika tena; hii ni kwasababu inaonekana ya kuwa wao ndio wamesababisha mgogoro huo mkubwa wenyewe. Lakini dhamira zao na Neno la Mungu vitawathibithishia kuwa wapo katika njia sahihi na japokuwa majaribu yao yanaendelea, wanapewa nguvu kuyastahimili. Shindano linazidi kupamba moto kwa ukali na kusonga karibu sana nao, lakini imani na ujasiri wao huongezeka kukabiliana na dharura illiyopo, ushuhuda wao ni huu: "Hatuwezi kuthubutu kulichezea Neno la Mungu kwa kutumia uongo, na kuigawa sheria Yake takatifu; tukisema sehemu moja ni ya muhimu na nyingine siyo ya ulazima, ili kupata upendeleo wa ulimwengu (ili tupendwe na ulimwengu). Bwana tunayemtumikia aweza kutuokoa. Kristo amezishinda mamlaka za dunia; basi, je, sisi tuuogope ulimwengu huu ambao tayari umekwishashindwa?" (uliokwisha kutekwa nyara tayari). [GC 610.1; PK Aya ya 16]

Mateso katika miundo yake mbalimbali ni mwendelezo wa kanuni ambayo itaendelea kuwapo, maadamu Shetani ataendelea kuwepo na kwa kadri Ukristo utakavyodumu kuwa na nguvu nyingi. Hakuna mtu anayeweza kumtumikia Mungu bila kujiletea upinzani wa majeshi ya giza yaliyo tayari kupigana naye. Malaika waovu watamshambulia vikali, wakiogopa kwamba ushawishi wake utawapokonya mateka wao kutoka katika mikono yao. Watu waovu, ambao wanakemewa na mfano wake wa maisha, wataungana na hao (mapepo) ili kujaribu kumtenga na Mungu wake kwa kuleta majaribu yanayovutia sana. Haya yasipofaulu kumwangusha, ndipo mamlaka yenye nguvu hutumika kumlazimisha muumini afanye kinyume na dhamiri yake. [GC 610.2; PK Aya ya 17]

### Yesu Mwombezi Wa Mwanadamu

Lakini maadamu Yesu anabaki na kuendelea kuwa mwombezi wa mwanadamu katika Patakatifu pa juu mbinguni, nguvu inayozuia ya Roho Mtakatifu itazidi kuigusa mioyo ya watawala pamoja na raia. Bado kwa kiasi fulani nguvu hii inatawala sheria za nchi (serikali). Kama sheria hizi zisingelikuwapo, basi hali ya ulimwengu huu ingekuwa mbaya zaidi kuliko ilivyo sasa. Ingawa wengi wa watawala wetu ni mawakala hai wa Shetani, Mungu pia anao mawakala Wake miongoni mwa watu wakuu wa taifa. Adui huwasukuma watumishi wake kupendekeza hatua ambazo zingeweza kukwamisha kazi ya Mungu; lakini

viongozi wa serikali wanaoheshimwa na watu na kumcha Bwana wanasukumwa na malaika watakatifu wapinge mapendekezo hayo kwa hoja zisizokanushika. Kwa njia hiyo watu wachache tu wanadhibiti mkondo wenye nguvu wa uovu, upinzani wa maadui wa Ukweli utazuiliwa ili Ujumbe wa Malaika wa Tatu uweze kufanya kazi yake. Onyo la mwisho litakapotolewa, litayanasa mawazo ya viongozi hawa wa watu ambao Bwana anafanya kazi kupitia kwao na baadhi yao watalikubali onyo na watasimama pamoja na watu wa Mungu katika kipindi cha wakati wa taabu (Danieli 12:1). [GC 610.3; PK Aya ya 18]

Malaika anayejiunga katika utangazaji wa ujumbe wa Malaika wa Tatu ataiangazia dunia yote kwa utukufu wake (Ufunuo 18:1-4). Kazi hiyo ambayo inaenea ulimwenguni kote, ambayo itafanywa kwa nguvu isiyo ya kawaida (Mvua ya Masika), ndiyo imetabiriwa hapa. Vuguvugu la ujio wa pili la miaka ya mwaka 1840-44 lilikuwa udhihirisho wenye utukufu wa uweza wa Mungu; ujumbe wa Malaika wa Kwanza ulipelekwa kwenye kila kituo cha umishenari ulimwenguni kote na katika baadhi ya nchi palikuweko na shauku kubwa zaidi ya mambo ya kiroho/kidini ambayo imewahi kushuhudiwa katika nchi yoyote tangu siku za Matengenezo ya Kanisa ya karne ya kumi na sita; lakini haya yote yatapitwa kabisa na vuguvugu kuu ambalo litatokea katika kazi ya kulitangaza onyo la mwisho la Malaika wa Tatu. [GC 611.1; PK Aya ya 19]

Kazi hiyo itafanana na ile ya siku ya Pentekoste kama “mvua ya kwanza” (vuli) ilivyotolewa katika kumwagwa kwa Roho Mtakatifu kwa wingi wakati wa ufunguzi wa mwanzo wa kuihubiri injili, ili kusababisha mbegu ya thamani iweze kuchipuka, ndivyo “mvua ya masika” itakavyotolewa wakati wa kufunga kazi ya injili kwa ajili ya kukomaza mavuno. “Nasi na tujue, naam, tukaendelee kumjua Bwana; kutokea Kwake ni yakini kama asubuhi; Naye atatujilia kama mvua, kama mvua ya vuli iinyweshayo nchi.” Hosea 6:3. “Furahini, basi, enyi wana wa Sayuni, mkamfurahie Bwana, Mungu wenu; kwa kuwa Yeye huwapa ninyi mvua ya masika, kwa kipimo cha haki, Naye huwanyeshea mvua, mvua ya masika, na mvua ya vuli, kama kwanza.” Yoeli 2:23. “Itakuwa siku za mwisho, asema Mungu, nitawamwagia watu wote Roho Yangu, na wana wenu na binti zenu watatabiri; na vijana wenu wataona maono; na wazee wenu wataota ndoto.” “Na itakuwa kila atakayeliitia Jina la Bwana ataokolewa.” Matendo ya Mitume 2:17, 21. [GC 611.2; PK Aya ya 20]

Kazi hii kuu ya injili haitafungwa/haitahitimishwa bila kuwa na udhihirisho wa nguvu ya Mungu, uweza wake hautakuwa pungufu kuliko ule ulioonekana wakati wa ufunguzi wake. Unabii ule ambao ulitimizwa katika umwagaji wa mvua ya kwanza (vuli) mwanzoni mwa kufunguliwa kwa kazi hiyo ya injili, utatimizwa tena inapomwagwa mvua ya masika wakati injili itakapokuwa ikifungwa. Hapa ndipo kuna “nyakati za kuburudishwa” (mvua ya masika) ambazo mtume Petro alizitazamia kwa hamu aliposema: “Tubuni basi, mrejee, ili dhambi zenu

zifutwe, zipate kuja nyakati za kuburudishwa kwa kuwako Kwake Bwana; apate kumtuma Kristo Yesu mliyewekewa tangu zamani; ambaye ilimpasa kupokewa mbinguni hata zije zamani za kufanywa upya vitu vyote, zilizonenwa na Mungu kwa kinywa cha manabii Wake watakatifu tokea mwanzo wa ulimwengu." Matendo ya Mitume 3:19, 20. [GC 611.3; PK Aya ya 21]

Watumishi wa Mungu, nyuso zao zikiwa zimeangazwa na kung'arishwa kwa kujiweka wakfu katika kazi ya Mungu, wataharakisha kutoka sehemu moja na kwenda sehemu nyingine ili kuutangaza ujumbe uliotoka mbinguni. Kwa maelfu ya sauti ulimwenguni kote, onyo hilo litatolewa. Miujiza itatendeka, wagonjwa wataponywa, na ishara na maajabu zitafuatana na waaminio. Shetani naye atafanya kazi yake kwa maajabu na ishara za uongo, hata kushusha moto kutoka mbinguni uje mbele ya wanadamu. Ufunuo 13:13. Hivyo ndivyo wakazi wote wa dunia hii watakavyofikishwa mahali watakapochagua upande wao watakaosimama. [GC 612.1; PK Aya ya 22]

Ujumbe utapelekwa sana, siyo kwa mabishano au kutumia hoja, bali kwa mguso wa kina wa Roho wa Mungu. Hoja zimekwishawasilishwa, mbegu zimekwishapandwa na sasa zitachipuka na kuzaa matunda. Machapisho yale yaliyotawanywa na watendakazi wamishenari yamekuwa na mvuto wenye nguvu, ila wengi ambao akili zao zilikuwa zimeguswa walizuiwa wasielewe Ukweli kikamilifu au kuutii Ukweli. Sasa miale ya nuru inapenya kila mahali, Ukweli unaonekana katika uwazi wake, na watoto waaminifu wa Mungu wanakata kamba zilizowafunga na kuwazuia. Mishikamano ya kifamilia, mahusiano ya kanisani, hayana uwezo kabisa wa kuwazuia sasa. Ukweli una thamani kubwa sana kwao kuliko mambo mengine yote. Licha ya mawakala walioungana Pamoja dhidi ya Ukweli, idadi kubwa ya watu watakata shauri kusimama upande wa Bwana. [GC 612.2; PK Aya ya 23]

## SURA YA 39

## WAKATI WA TAABU

### (Mlango Wa Rehema Utakapofungwa)

Ufupisho: Wakati unakuja hivi karibuni ambapo huruma haitakuwepo kwa waovu tena hapa duniani. Kila kesi itakuwa imeamuliwa ama kwa uzima au kwa mauti. Kufungwa mlango wa rehema kupo njiani, na hata kama hatujui ni lini, ishara zinatuonyesha kwamba ni hivi karibuni, Mungu atusaidie kutumia uchaguzi tuliopewa kwa hekima, ili tusiwe nje ya lango la mbinguni.

"Wakati huo Mikaeli atasimama, jemadari mkuu, asimamaye upande wa wana wa watu wako; na kutakuwa na wakati wa taabu, mfano wake haukuwapo tangu lilipoanza kuwapo taifa hata wakati uo huo; na wakati huo watu wako wataokolewa; kila mmoja atakayeonekana ameandikwa katika Kitabu kile." Danieli 12:1. [GC 613.1; PK Aya ya 1]

Wakati Ujumbe wa Malaika wa Tatu utakapofungwa, rehema inakoma kusihi tena kwa wakazi hao wenye hatia wa dunia hii (mlango wa rehema unakuwa umefungwa kwa wale wenye dhambi kutubu). Watu wa Mungu wamekwisha kukamilisha kazi yao. Wamekwisha kupokea "mvua ya masika," yaani "kuburudishwa kwa kuwako Kwake Bwana," na sasa wako tayari kukabiliana na saa ya majaribu inayowakabili mbele yao. Malaika kule mbinguni wanaharakisha kutoka na kuingia mbinguni. Malaika yule anayerudi kutoka duniani anatangaza kuwa kazi yake imekamilika; Mtihani (jaribio) wa mwisho umekwisha kuletwa juu ya ulimwengu mzima na wote wale ambao walidumu kuwa watiifu kwa Sheria (maagizo, Amri, Shuhuda) za Mungu wamekwisha kutiwa ule "muhuri wa Mungu aliye hai." Hapo ndipo Yesu anasitisha huduma Yake ya maombezi, na wakili (upatanisho) katika hekalu la juu Mbinguni. Anainua mkono Wake na kwa sauti kuu anasema, "Imekwisha;" na jeshi lote la malaika wanazivua na kuzishusha taji zao Yesu anapotangaza tangazo hilo la kuogofya sana: "Mwenye kudhulumu na azidi kudhulumu; na mwenye uchafu na azidi kuwa mchafu; na mweye haki na azidi kufanya haki; na mtakatifu na azidi kutakaswa." Ufunuo 22:11. Kesi ya kila mtu imekwisha kuamuliwa, aidha kwa uzima wa milele au kwa mauti. Kristo amekwishafanya upatanisho kwa watu Wake na amezifutilia mbali dhambi zao. Idadi ya raia Wake imekamilika (wafuasi); "ufalme na utawala, na ukuu wa ufalme chini ya mbingu yote," unakaribia mno kukabidhiwa kwa warithi wa

wokovu, na Yesu anaenda kutawala kama Mfalme wa wafalme na Bwana wa mabwana. [GC 613.2; PK Aya ya 2]

Wakati anapotoka katika Patakatifu kwenye madhabahu, giza linawafunika wakazi wa ulimwengu huu. Katika wakati huo wa kuogofya, wale wenye haki wanapaswa kuishi mbele za Mungu mtakatifu bila ya kuwa na mwombezi au mpatanishi. Kizuizi kilichokuwa juu ya waovu kimeondolewa kwao (Roho Mtakatifu) na Shetani anapata utawala kamili kwa wale ambao hawakutubu hata mwisho. Uvumilivu wa Mungu umekoma. Dunia imeikataa rehema Yake, imechukia upendo Wake na kuikanyaga Sheria Yake. Waovu wamevuka mpaka wa muda wao wa rehema; Roho wa Mungu, ambaye amekuwa hasikilizwi daima, hatimaye ameondolewa kabisa kwao. Wakiishi bila wigo wa neema ya Mungu, hawatakuwa na ulinzi wowote dhidi ya yule mwovu. Hapo ndipo Shetani atawatumbukiza wakazi wa dunia katika taabu moja kubwa, na ya mwisho. Malaika wa Mungu wanapoacha kuzuia pepo kali za hasira ya mwanadamu, viashiria vyote vya vita vitaachiliwa huru. Dunia nzima itahusishwa na uharibifu mkali kuliko ule ulioipata Yerusalemu ya zamani za kale. [GC 614.1; PK Aya ya 3]

Ni malaika mmoja ndiye aliyewaangamiza wazaliwa wote wa kwanza wa Misri na kuijaza nchi ya Misri kwa maombolezo. Daudi alipomkosea Mungu kwa kuwahesabu watu, malaika mmoja ndiye aliyesababisha maangamizi yale ya kutisha ambayo kwa hayo dhambi yake ilipatilizwa. Nguvu iyo hiyo itekelezwayo na Malaika watakatifu Mungu anapowaagiza ndiyo itatekelezwa na malaika wale waovu pale Atakapowaruhusu. Yapo majeshi yaliyo tayari sasa yakingojea tu ruhusa ya Mungu ili kufanya maangamizi yao kila mahali. [GC 614.2; PK Aya ya 4]

Wale wanaoiheshimu Sheria ya Mungu (Amri kumi) wamekuwa wakishitakiwa kuwa wao ndiyo wanaoileta hukumu duniani na watachukuliwa kama ndio chanzo cha matetemeko ya asili ya kutisha na upinzani, migogoro na umwagaji damu miongoni mwa watu waijazao dunia hii kwa misiba. Nguvu ile iliyoshikanishwa na hilo onyo la mwisho imechochea moto mihemko mibaya ya waovu; hasira yao imewashwa moto dhidi yao wote walioupokea ujumbe na Shetani atazidi sana kuwachochea kwa nguvu roho ya chuki na kuwatesa watu hao zaidi. [GC 614.3; PK Aya ya 5]

**Uwepo Wake Mungu Waondolewa**

Ule uwepo wa Mungu ulipoondolewa hatimaye kutoka kwa taifa la wayahudi, makuhani na watu hawakulitambua hilo. Ingawa, walikuwa chini ya udhibiti wa Shetani na kuyumbishwa na hasira za kutisha mno na mbaya mno, bado walijichukulia wao kama wateule, watu waliochaguliwa wa Mungu. Huduma katika hekalu iliendelea; kafara zilitolewa juu ya madhabahu zake zilizonajisiwa na kila siku baraka za Mungu zikatamkwa ili ziwepo juu ya watu hawa wenye

hatia ya damu ya Mwana wa Mungu mpendwa, na ambao walikuwa wakitafuta kuwachinja mitume na watendakazi Wake. Kwa hiyo, hukumu ya Patakatifu isiyobatilishwa itakapokuwa imetangazwa na mwisho hatima ya mambo yote ya dunia itakapokuwa haiwezi kubadilishwa milele, wakazi wa dunia hawatalijua jambo hilo. Taratibu mbalimbali za kidini zitaendelea kutekelezwa na wale watu ambao Roho wa Mungu amekwisha kuondolewa kabisa miongoni mwao; na shauku ya kishetani ambayo kwayo mfalme wa uovu atawavuvia kumaliza mipango yake ya uovu na itafanana na bidii (usongo) waliyo nayo watu kwa ajili ya Mungu. [GC 615.1; PK Aya ya 6]

Kwa kuwa Sabato (Jumamosi) itakuwa kipengele kikubwa kimoja maalumu kinachobishaniwa kwenye Ulimwengu wa Kikristo wote na viongozi wa kidini na wa serikali wameunganisha nguvu zao ili kulazimisha utekelezwaji wa utunzwaji wa Jumapili, upingaji endelevu wa kundi dogo linalokataa kukubaliana na matakwa ya wengi utawafanya wachukiwe sana ulimwenguni kote. Itasisitizwa kuwa, wachache wanaoipinga taasisi ya kanisa na sheria ya nchi hawapaswi kuvumiliwa; kwamba ni bora hao wapate kuteswa kuliko mataifa yote kuwa katika machafuko na ukosefu wa sheria. Hoja hiyo hiyo ililetwa na "viongozi wa watu" dhidi ya Kristo karne nyingi zilizopita kupitia Kayafa mwenye hila; "wala hamfikiri ya kwamba, yafaa mtu mmoja afe kwa ajili ya watu, wala lisiangamie taifa zima" Yohana 11:50. Dai hili litaonekana lenye mamlaka; na sheria itawekwa hatimaye dhidi ya wale wanaoiheshimu na kuitunza Sabato ya amri ya nne. Watawashutumu kama watu wanaostahili adhabu kali sana na kuwapatia watu uhuru baada ya muda fulani ili waweze kuwaua. Urumi katika dunia ya kale na Uprotestanti ulioasi katika dunia mpya ya leo vitafanya jitihada moja kuwaelekea wale wanaoshika Maagizo yote za Mungu (Sheria, amri, shuhuda, kanuni, Maandiko, Neno). [GC 615.2; PK Aya ya 7]

Kisha watu wa Mungu watatumbukizwa katika matukio ya dhiki yanaoelezwa na nabii kama wakati wa taabu ya Yakobo. "Maana Bwana asema hivi, Tumesikia sauti ya tetemeko, Na ya hofu, wala si ya amani......na nyuso zote zimegeuka rangi na kupauka. Ole! Maana siku ile ni kuu, hata hapana inayofanana nayo, maana ni wakati wa taabu yake Yakobo; lakini ataokolewa nayo." Yeremia 30:5-7. [GC 616.1; PK Aya ya 8]

**Yakobo Alijawa Na Hofu**

Usiku wa Yakobo wa uchungu mkali akipambana mieleka katika maombi kusudi apate kuokoka kutoka kwa mkono wa Esau (Mwanzo 32:24-30) unawakilisha uzoefu wa Maisha watakoupitia watu wa Mungu katika ule wakati wa taabu (taabu ya Yakobo). Kutokana na udanganyifu alioufanya ili kupata mibaraka ya baba yake iliyoandaliwa kwa ajili ya Esau, Yakobo alikimbia ili kuokoa uhai wake baada ya kupokea vitisho vya kuuwawa kutoka kwa kaka yake.

Baada ya kuwa uhamishoni kama mkimbizi kwa muda mrefu, alirudi kutoka huko, kwa amri ya Mungu, akiwa na wake zake na watoto na mifugo yake katika nchi yake ya asili. Alipofika katika mipaka ya nchi yake, alijawa na wasiwasi kutokana na ujio wa Esau akiwa na mashujaa wa vita kwamba atatokea bila shaka na hasira ya kujilipizia kisasi. Kundi la Yakobo, likiwa bila silaha na bila ulinzi wowote, lilionekana linaelekea kuwa wahanga wasio na msaada dhidi ya ukatili na mauaji. Kujilaumu kuliongeza uzito katika mzigo wa wasiwasi na woga, kwa kuwa dhambi yake ndiyo iliyoleta hatari hii yote. Tumaini lake pekee lilikuwa katika rehema ya Mungu; ulinzi wake pekee lazima uwe ni maombi. Na bado hakuaacha kufanya lolote kwa sehemu yake ili kujipatanisha na kaka yake na kuzuia hatari iliyo mbele yake. Vivyo hivyo pia ndivyo wanavyopaswa kufanya wafuasi wa Kristo wanapoukaribia ule wakati wa taabu, wanapaswa kufanya juhudi ili kujiweka katika nuru halisi mbele za watu, kupooza nguvu ya chuki yao isiyo na sababu na kuzuia hatari yoyote inayotishia uhuru wa dhamiri zao. [GC 616.2; PK Aya ya 9]

### Peke Yake Pamoja Na Mungu

Akiisha kuiondoa familia yake ili isiweze kushuhudia taabu yake, Yakobo anabaki peke yake ili kumuomba Mungu. Anaungama dhambi yake na kwa kushukuru, anakiri rehema ya Mungu kwake na kwa unyenyekevu na aibu nyingi anaomba agano lile lililofanywa na baba zake na ahadi alizopewa katika maono ya usiku pale Betheli na katika nchi ya uhamisho. Janga katika maisha yake limekuja; kila kitu kiko hatarini. Katika giza hili na upweke anaendelea kuomba na kujinyenyekesha mwenyewe mbele za Mungu. Mara kwa ghafla, mkono unawekwa mabegani mwake! Naye anadhani kuwa adui anatafuta uhai wake na kwa nguvu zake zote za kukata tamaa anapambana mieleka na mshambuliaji wake. Panapoanza kupambazuka, huyu mgeni anaingiza nguvu Yake kubwa isiyo ya kibinadamu; kwa mguso Wake tu, mtu shupavu na mwenye maguvu anaonekana kama anapooza na anaanguka kwenye shingo ya mpinzani wake anayestaajabisha, akijiona hana msaada anatoa machozi akiomba. Yakobo sasa anajua kuwa yule ni Malaika wa Agano ambaye amekuwa akipambana Naye (Masihi). Japokuwa amepewa kilema na anaugua kwa maumivu makali, hakuachilia kusudi lake. Kwa muda mrefu amevumilia mahangaiko, majuto na taabu kwa dhambi yake; sasa anataka kuwa na uhakika kuwa dhambi yake imesamehewa. Mgeni Yule wa mbinguni anaonekana kukaribia kuondoka; lakini Yakobo anang'ang'ania Kwake, akimsihi ambariki. Malaika anasihi, "Niache, niende, maana kunapambazuka;" lakini yule mzee wa imani anaendelea kusema kwa nguvu, "Sikuachi, mpaka umenibariki." Je, ni ujasiri, uthabiti na uvumilivu mkubwa kiasi gani unaoonyeshwa hapa! Kama dai 0hili lingetolewa kwa kujivuna na kiburi cha makusudi, basi, Yakobo angeangamizwa mara moja; lakini ombi lake lilikuwa ni uhakikisho wa mtu anayekiri madhaifu yake na kutokufaa kwake,

lakini bado lilionyesha tumaini ya kupata rehema ya Mungu ambaye ni Mtunza-agano. [GC 616.3; PK Aya ya 10]

"Alikuwa na uwezo juu ya malaika akashinda" Hosea 12:4. Kwa njia ya kujinyenyekesha, toba na kujisalimisha nafsi, mtenda dhambi huyu, mkosaji na mwenye mwili unaokufa, alishinda pamoja na Mungu Mtukufu wa mbinguni. Alishikilia sana kwa kutetemeka juu ya ahadi za Mungu, na moyo wa upendo huu usio na kikomo, usingeweza kutupilia mbali kilio cha ombi la mdhambi huyu. Kama ushahidi wa ushindi wake, na faraja ya kutia moyo wengine pia ili wauige mfano wake, jina lake lilibadilishwa kutoka lile ambalo lingemkumbusha juu ya dhambi yake kwenda kwenye lile lililokumbushia ushindi wake. Na Ukweli kwamba Yakobo alishinda na Mungu, ulikuwa ni uhakikisho kwamba angeweza kushinda pamoja na wanadamu pia. Hakuendelea kuwa na hofu ya hasira ya kaka yake tena kwa kuwa Bwana alikuwa Ndiye ngao yake. [GC 617.1; PK Aya ya 11]

Shetani alikuwa amemshitaki Yakobo mbele za Malaika wa Mungu akidai kumwangamiza kwa sababu ya dhambi yake hiyo; alikuwa amekwishamchochea Esau ili aje kijeshi dhidi yake; wakati wa usiku mrefu wa kupambana mieleka wa mzee yule wa imani, Shetani alidhamiria kuiweka ndani yake hatia ya dhambi yake ili kumvunja moyo na avunje msimamo wake wa kumtegemea Mungu. Yakobo alikaribia kabisa kukata tamaa lakini alijua kuwa bila msaada kutoka mbinguni lazima angeliangamia. Alikuwa ameungama kwa dhati dhambi yake kuu na aliiomba rehema ya Mungu. Hakuweza kabisa kugeuzwa kutoka kwa lengo lake, bali akaendelea kumtegemea na kumsihi Malaika juu ya ombi lake kwa kilio cha dhati, kilichojaa uchungu hata akashinda. [GC 618.1; PK Aya ya 12]

**Shetani Dhidi Ya Watu Wa Mungu**

Kama vile ambavyo Shetani alimchochea Esau Kumwendea Yakobo kijeshi na kuwa kinyume naye, ndivyo vile vile atakavyowachochea watu waovu wawaangamize watu wa Mungu wakati wa taabu. Na kama vile alivyomshitaki Yakobo, ndivyo atakavyotoa malalamiko yake ya shitaka dhidi ya wana wa Mungu pia. Anawahesabu watu wa duniani kama raia wake mwenyewe; lakini kuna kundi dogo la wale wazishikao amri za Mungu wanaoukataa ukuu wake. Kama angeweza kuwafutilia mbali wote kutoka duniani, ushindi wake ungekuwa umekamilika. Anaona kwamba Malaika watakatifu wanawalinda na anang'amua kuwa dhambi zao zimekwishasamehewa; lakini yeye hajui kama kesi zao zimekwisha kuamuliwa katika Patakatifu, hekaluni kule juu mbinguni. Anao ujuzi sahihi juu ya dhambi zile ambazo amewajaribu kuzitenda (nao wakazitenda) na anazileta hizi mbele ya Mungu katika namna ya kukoleza chumvi sana, akiwaonesha watu hawa kuwa, kama yeye, wanastahili kuikosa neema ya Mungu. Anatangaza kuwa Mungu hawezi kusamehe dhambi zao katika haki na bado

akamuangamiza yeye na malaika zake. Anadai hao kuwa ni windo lake halali, na hivyo apewe yeye watu hao ili apate kuwaangamiza. [GC 618.2; PK Aya ya 13]

Shetani anapowashitaki watu wa Mungu kulingana na dhambi zao, Bwana anamruhusu awajaribu kwa kiasi kikubwa. Ujasiri wao katika Mungu, Imani yao na uthabiti wao vitajaribiwa vikali sana. Kila wanapotazama maisha yao kule nyuma, matumaini yao yanazama; kwa kuwa katika maisha yao yote wanaona mazuri machache tu waliyoyatenda. Wanajua kwa udhairi kabisa, udhaifu wao na kutokufaa kwao. Shetani anatia bidii kuwatisha kwa kuleta mawazoni mwao kuwa kesi zao hazina tumaini na doa la unajisi wao haliwezi kufutwa kamwe. Anatumaini kwa kufanya hivyo ataivunja imani yao na watasalimu amri kwenye majaribu yake na waache uadilifu wao kwa Mungu. [GC 618.3; PK Aya ya 14]

Japokuwa watu wa Mungu watazungukwa na maadui ambao wamepania kuwaangamiza, lakini bado mateso wanayoyapitia si kitisho cha kuwafanya wayaogope mateso na kutelekeza ile Kweli; bali wana hofu kuwa huenda dhambi zao zote bado hazijaungamwa ipasavyo na kwamba kupitia makosa fulani ndani yao, watashindwa kuuona utimizwaji wa ahadi ya Mwokozi: “Mimi Nami nitakulinda, utoke katika saa ya kujaribiwa iliyo tayari kuujilia ulimwengu wote” Ufunuo 3:10. Ikiwa wangepata uhakika na kuthibithishiwa kusamehewa basi wasingeyumbishwa na maumivu au kifo; lakini kama wangeonekana kutostahili na kupoteza maisha yao kwa sababu ya makosa yao wenyewe, basi Jina takatifu la Mungu lingeweza kutukanwa. [GC 619.1; PK Aya ya 15]

Katika kila upande wanasikia njama za uhaini na wanaona kazi kubwa ya uasi ikiendelea; na ndani yao yanawaka matamanio makubwa, ya uhitaji wa dhati wa roho, kwamba uasi huu mkubwa ukomeshwe na uovu wa hao waovu ufikie kikomo. Lakini wanapomlilia Mungu kukomesha kazi ile ya uasi, wao wenyewe wanapata utambuzi wa makini na kujishuku kuwa hawana nguvu zaidi ya kuyapinga na kuyazuia mawimbi makali ya uovu. Wanajihisi kuwa kama siku zote wangewekeza nguvu zao katika huduma ya Kristo, na kusonga mbele kutoka nguvu hata nguvu, majeshi ya Shetani yangekuwa na nguvu ndogo kiasi cha kutoweza kuwashinda. [GC 619.2; PK Aya ya 16]

Wanazitesa nafsi zao mbele ya Mungu, wakionyesha toba yao za dhambi zao nyingi na kuidai ahadi Yake Mwokozi isemayo: “Au azishike nguvu Zangu, afanye Amani Nami; naam, afanye Amani Nami” Isaya 27:5. Imani yao haichoki kwa sababu maombi yao hayajibiwi kwa haraka. Ingawa wanasumbuka sana kwa kufadhaika, hofu na dhiki, hawakomi katika kusihi na kuomba. Wanaishikilia nguvu ya Mungu kama Yakobo alivyomshikilia Malaika; na lugha ya mioyo yao ni hii: “Sitakuachia usiponibariki.” [GC 619.3; PK Aya ya 17]

Kama Yakobo asingelitubu dhambi yake ya kujichukulia haki ya mzaliwa wa kwanza kwa kutumia udanganyifu, Mungu hangelisikia ombi lake na kuutunza

uzima wake kwa rehema. Kwa hiyo, katika wakati wa taabu, kama watu wa Mungu watakuwa wametunza dhambi zao bila kutubu wakiwa wanateswa kwa woga na maumivu, wangeelemewa sana kwa kushindwa na kukosa ujasiri; Kukata tamaa kungeimaliza imani yao na wasingekuwa na ujasiri wa kumsihi Mungu awaokoe. Japo wanakuwa na uelewa wa kina wa kutofaa na kutostahili kwao, hawana maovu yaliyofichwa yapaswayo kufunuliwa. Dhambi zitakuwa zimetangulia hukumuni na zimefutwa kabisa na hawawezi kuzikumbuka tena. [GC 620.1; PK Aya ya 18]

Shetani anawaongoza wengi kuamini kuwa Mungu hajali kukosa kwao uaminifu katika mambo madogo-madogo ya maisha; lakini Mungu anaonesha katika kushughulika Kwake na Yakobo kuwa kwa namna iwayo yote hatavumilia au kuufumbia macho uovu au kuuidhinisha. Wote wale wanaojaribu kuficha dhambi na kuzitoleta udhuru, na hivyo kuziruhusu ziendelee kuwepo ndani ya vitabu vya mbinguni, zikiwa hazijatubiwa na kusamehewa, watashindwa na Shetani. Kwa kadri wanavyoshika zile nafasi za juu na za kuheshimika, ndivyo wanavyohurumiwa sana mbele za Mungu na ndivyo ushindi wa yule mwovu mkuu unavyokuwa wa uhakika. Wale wanaojikawiza katika maandalizi ya siku ya Mungu (hukumu) hawawezi kuupata muda huo wakati wa taabu au katika wakati wowote ule unaokuja. Hakuna matumaini kwa kesi za watu wote wa namna hii. [GC 620.2; PK Aya ya 19]

Wale wanaojiita Wakristo, ambao wanalifikia pambano la mwisho la kutisha sana wakiwa hawajajiandaa, kwa kukata tamaa kwao, wataungama dhambi zao kwa maneno yenye utungu unaowaka moto, wakati waovu wanashangilia kutokana na dhiki yao ile. Maungamo hayo yana tabia ile ile kama yalivyokuwa yale ya Esau au ya Yuda. Wale wanaoyaungama, wanaomboleza kutokana na matokeo ya makosa yao, bali si kwa sababu ya hatia yake. Hawajisikii kuwa na toba ya kweli, wala hawana chuki dhidi ya uovu. Wanakiri kwamba wametenda dhambi zao kwa kuogopa adhabu tu; lakini, kama yule Farao wa zamani, wangeweza kuurudia uasi wao wa kufuru dhidi ya Mbingu kama hukumu (adhabu) zingeweza kuondolewa kwao. [GC 620.3; PK Aya ya 20]

Historia ya Yakobo pia ni uthibitisho unaoonyesha kwamba Mungu hatawatupa nje wale waliodanganywa na kujaribiwa na kuingizwa katika dhambi, lakini ambao wamemrudia Yeye kwa toba ya kweli. Wakati Shetani anajaribu kuliangamiza kundi hilo, Mungu atawatuma malaika Zake kuwafariji na kuwalinda katika wakati ule wa hatari kubwa. Mashambulio ya Shetani ni makali, tena yamedhamiriwa, madanganyo yake ni ya kutisha sana; lakini jicho la Bwana lipo juu ya watu Wake, na sikio Lake hukisikia kilio chao. Mateso yao ni makubwa, ndimi za moto wa tanuru zinaonekana kana kwamba zi karibu kuwateketeza kabisa; lakini Msafishaji/Mtakasaji huyo atawasafisha, watatoka kama dhahabu iliyosafishwa kwa moto. Upendo wa Mungu kwa watoto Wake

katika kipindi hicho cha majaribu yao makali mno una nguvu, tena umejaa huruma kama katika siku zile za usitawi wao unaong'aa sana kama mwanga wa jua; lakini ni lazima hao wawekwe katika tanuru hilo la moto; tabia yao ya kidunia ni lazima iteketezwe kabisa, ili sura ya Kristo ipate kuakisiwa kikamilifu. [GC 621.1; PK Aya ya 21]

**Imani Inayoweza Kustahimili**

Kipindi hicho cha dhiki na utungu kilicho mbele yetu kitahitaji sisi tuwe na imani inayoweza kustahimili uchovu mwingi, ucheleweshо, na njaa -- imani isiyoweza kuzimia japo ijaribiwe vikali sana. Muda wa majaribio (rehema ya mtihani wa tabia) umetolewa kwa wote ili wapate kujiandaa kwa wakati huo. Yakobo alishinda kwa sababu alikuwa na nia ya kuendelea kushikilia sana na tena alidhamiria kwa nia thabiti. Ushindi wake ni ushahidi unaoonyesha nguvu ya maombi yanayotolewa kwa bidii ambayo hayajui kukata tamaa. Wote watakaozishikilia ahadi za Mungu bila kukata tamaa kama yeye alivyofanya, na kuwa na bidii na ustahimilivu wa dhati kama aliokuwa nao yeye, watashinda kama yeye alivyoshinda. Wale ambao hawataki kujikana nafsi zao, ili waomboleze na kuugua mbele zake, kwa kuomba kwa muda mrefu na kwa bidii, ili kupata mbaraka Wake, hawataupata. Kushindana mweleka na Mungu -- ni wachache mno kiasi gani wanaojua maana yake! Ni wachache mno kiasi gani waliopata kuitoa mioyo yao kumlilia Mungu kwa shauku yenye kina mpaka nguvu zao zote zimefikia mwisho wa kunyumbulika kwake! Mawimbi ya kukata tamaa yanapopita juu ya mwombaji dua, ni wachache mno kiasi gani wanaozing'ang'ania ahadi za Mungu kwa nguvu na kwa imani isiyokubali kushindwa au kukata tamaa! [GC 621.2; PK Aya ya 22]

Wale ambao wanaizoesha imani yao kwa kiwango kidogo mno wakati huu, wapo katika hatari kubwa sana ya kuanguka chini ya nguvu ya madanganyo ya Shetani na chini ya ile amri itakayozilazimisha dhamiri zao. Na hata kama watastahimili mtihani huo, watatumbukizwa katika dhiki kubwa zaidi na utungu katika wakati ule wa taabu, kwa sababu hao hawana mazoea ya kumtumainia Mungu. Mafunzo yale ya imani waliyoyapuuzia, watashurutishwa kujifunza chini ya shinikizo la kutisha sana na la kuvunja moyo. [GC 622.1; PK Aya ya 23]

Muda huu ni wa sisi kujitahidi sana kujielimisha wenyewe kuhusu Mungu kwa njia ya kuzithibithisha ahadi Zake. Malaika wanarekodi kila ombi lililotolewa kwa moyo wa dhati, bidii na imani. Ni bora kwetu sisi tukitupilia mbali kila kitu tunachokiendekeza kufurahisha nafsi zetu, kuliko kupuuzia au kuacha mawasiliano (sala) yetu na Mungu. Umaskini wa kutupwa, kujinyima kwa hali ya juu, pamoja na kibali Chake, ni bora kuliko utajiri, heshima nyingi, raha, na urafiki bila ridhaa hiyo. Ni lazima tuwe na muda wa kusali. Kama tukiyaruhusu

mawazo yetu kujazwa na maslahi/tija na mambo ya dunia hii, basi, Bwana anaweza kutupatia muda huo kwa kutuondoa na kutupeleka mbali na sanamu au miungu yetu ya dhahabu, nyumba zetu, au mashamba yetu yenye rutuba nyingi. [GC 622.2; PK Aya ya 24]

Vijana wasingeshawishika kuingia dhambini kama wangekataa katakata kuingia katika njia nyingine yoyote, isipokuwa ile ambayo kwayo wangeweza kuuomba mbaraka wa Mungu uwajie juu yao. Kama wajumbe wanaolipeleka onyo la mwisho la kutisha sana katika ulimwengu wote, wangeweza kuomba mbaraka wa Mungu, si kwa njia ya ubaridi, unyonge na uvivu, bali kwa bidii na kwa imani, kama vile alivyofanya Yakobo, hapo ndipo wangeona mahali pengi ambapo wangeweza kusema: “Nimeonana na Mungu uso kwa uso, na nafsi yangu imeokoka.” Mwanzo 32:30. Wangehesabiwa na Mbingu kama wana wa Kifalme wakuu, wenye nguvu ya kumshinda Mungu na wanadamu. [GC 622.3; PK Aya ya 25]

“Wakati wa taabu kuliko wowote kuwahi kutokea”, upo karibu kufungua milango yake kwetu; na tutahitaji uzoefu ambao kwa sasa hatunao na ambao wengi ni wavivu kuufanyia bidi kuupata. Mara nyingi ndivyo mambo yalivyo kwamba taabu inaonekana kuwa ni kubwa sana inapotarajiwa kuliko ilivyo hasa inapokuja machoni petu; lakini jambo hilo si Kweli kuhusu hatari ile kubwa iliyo mbele yetu. Maelezo yaliyo wazi kabisa kueleweka hayawezi kutosha kuelezea ukubwa wa mateso hayo. Katika kipindi kile cha dhiki na hatari kubwa (maonjo), kila mtu ni lazima asimame peke yake mbele za Mungu. “Wajapokuwamo ndani yake Nuhu, na Danieli, na Ayubu, kama Mimi niishivyo, asema Bwana MUNGU, hawataokoa wana wala binti; watajiokoa nafsi zao tu kwa haki yao.” Ezekieli 14:20. [GC 622.4; PK Aya ya 26]

Hivi sasa, wakati Kuhani wetu Mkuu anafanya upatanisho kwa ajili yetu, tungejitahidi sana kuwa wakamilifu ndani ya Kristo. Hata kwa wazo moja tu Mwokozi wetu asingeweza kufikishwa mahali ambapo angeanguka chini ya majaribu. Ndani ya mioyo ya wanadamu Shetani anapata kipengele (pointi) fulani ambacho anaweza kujipatia mahali pa kukanyaga mguu wake, yaani, tamaa fulani ya dhambi inayopendwa na na kutunzwa moyoni, ambayo kwayo majaribu yanawekeza nguvu yake. Lakini kuhusu habari Zake mwenyewe, Kristo alitangaza hivi: “Kwa maana yuaja mkuu wa ulimwengu huu, wala hana kitu Kwangu.” Yohana 14:30. Shetani hakuweza kupata kitu hata kimoja ndani ya Mwana wa Mungu ambacho kingemwezesha kupata ushindi dhidi Yake. Alikuwa amezitunza amri za Baba Yake na hakukuwa na dhambi ndani Yake Kristo ambayo Shetani angeitumia kujipatia manufaa au ushindi. Hii ndiyo hali ambayo wote watakaosimama katika wakati wa taabu wanapaswa kukutwa nayo. [GC 623.1; PK Aya ya 27]

Ni katika maisha haya tunayoishi sasa, ndiyo ambapo tunapaswa kuitenga dhambi mbali nasi, kwa njia ya imani katika damu ya upatanisho ya Kristo. Mwokozi wetu wa thamani anatualika ili tupate kushikamana Naye, kuunganisha udhaifu wetu na nguvu Zake, ujinga wetu na hekima Yake, kutokufaa kwetu na kustahili Kwake. Uongozi Wake Mungu ndiyo shule yetu ambayo ndani yake sisi tunatakiwa kujifunza upole na unyenyekevu wa moyo aliokuwa nao Yesu. Daima Bwana anaweka mbele yetu, sio njia ile ambayo sisi tungeichagua, ambayo kwetu inaonekana kana kwamba ni rahisi na yenye kupendeza zaidi, bali malengo yenye makusudi ya Kweli katika maisha yetu. Ni juu yetu sisi kushirikiana na njia zile zinazozitumiwa na Mbingu katika kazi ya kuzigeuza tabia zetu ili zipate kuwa na mfano wa Mungu. Hakuna watu wawezao kuiacha au kuiahirisha kazi hiyo, pasipo kuhatirisha sana roho zao. [GC 623.2; PK Aya ya 28]

Mtume Yohana alisikia sauti kuu mbinguni ikisema: “Ole wa nchi na bahari! Kwa maana yule ibilisi ameshuka kwenu mwenye ghadhabu nyingi, akijua ya kuwa ana wakati mchache tu” Ufunuo 12:12. Matukio ni ya kuogofya mno, yanayosababisha kutolewa kwa tamko hilo la mshangao la sauti hiyo iliyosikika kutoka mbinguni. Ghadhabu ya Shetani inazidi kuongezeka kadiri wakati wake unavyozidi kuwa mfupi, nayo kazi yake ya kuwadanganya na kuwaua watu itafikia kilele chake katika kipindi cha wakati wa taabu. [GC 623.3; PK Aya ya 29]

Matuko yanayopita akili ya mwanadamu yataonekana mbinguni katika muda mfupi ujao, kama ishara ya nguvu ya utendaji wa mapepo yanayofanya miujiza. Roho za mashetani zitatoka na kuwaendea wafalme wa dunia hii na kwenda ulimwenguni kote, ili kuwafunga katika madanganyo yao, na kuwashurutisha kuungana na Shetani katika pambano lake la mwisho dhidi ya serikali ya mbinguni. Kwa njia ya mawakala wake hao, watawala pamoja na raia wote watadanganyika kwa njia ile ile moja. Watu watatokea wakijidai kwamba wao ndio Kristo mwenyewe, na kudai wapewe cheo Chake na kusujudiwa kwa ibada, jambo ambalo anastahili Yule Mkombozi wa ulimwengu peke Yake. Watafanya miujiza ya ajabu ya uponyaji, kisha watadai kwamba wameleta habari za mafunuo kutoka mbinguni ambazo zitakuwa zinapingana na ushuhuda wa Maandiko. [GC 624.1; PK Aya ya 30]

Kama tendo lake la kilele katika drama ya mfululizo wa matukio makuu ya udanganyifu wake, Shetani atakuja mwenyewe akiwa na umbile linalofanana kabisa na lile la Kristo. Kanisa limetangaza kwa muda mrefu sana kwamba linatazamia kumwona Mwokozi akija mara ya pili kuja kutimiza matumaini Yake na yao. Basi huyo Mlaghai mkuu atafanya ionekane kana kwamba Kristo amekuja. Katika sehemu mbalimbali za dunia, Shetani atajionyesha mwenyewe miongoni mwa wanadamu kama kiumbe mwenye utukufu, anayeng’aa kwa mng’ao unaotia macho kiwi, akifanana na maelezo ya umbile la Mwana wa Mungu (Kristo) yaliyotolewa na Yohana katika Ufunuo 1:13-15. Utukufu ule unaomzunguka

(Shetani) pande zote haufanani na kitu chochote ambacho macho ya wanadamu yamepata kukiona. Makelele ya shangwe yanavuma hewani: “Kristo amekuja! Kristo amekuja!” Watu wanaanguka kifudifudi mbele yake na kumsujudu, wakati yeye anainua mikono yake juu na kutamka baraka juu yao, kama vile Kristo alivyowabariki wanafunzi Wake alipokuwa hapa duniani. Sauti yake ni nyororo na tulivu, lakini ikiwa tamu sana kama muziki. Kwa sauti ya upole, yenye huruma, anazihubiri baadhi ya Kweli zile zile za thamani za mbinguni, ambazo Mwokozi alizinena; anaponya magonjwa ya watu, halafu, katika tabia yake ya kumwigiza Kristo, anadai kwamba ameibadili Sabato kuwa Jumapili, naye anawaamuru wote kuitakasa siku hiyo (ya Jumapili) aliyoibariki yeye. Anatangaza kwamba wale wanaoendelea kuitakasa siku ile ya saba (Jumamosi) wanalikufuru jina lake kwa kukataa kuwasikiliza malaika zake aliowatuma kuleta nuru na kweli. Hayo ndiyo madanganyo yake yenye nguvu nyingi sana yanayowashinda nguvu karibu watu wote. Kama vile Wasamaria walivyodanganywa na Simoni Mchawi (Magus), ndivyo kadamnasi ya watu wengi sana, kuanzia aliye mdogo sana mpaka aliye mkubwa kuliko wote, wanasikiliza uchawi huo, na kusema: Hii ni “nguvu kuu ya Mungu.” Matendo 8:10. [GC 624.1; PK Aya ya 31]

Lakini watu wa Mungu hawatapotoshwa. Mafundisho ya kristo huyo wa uongo ambayo hayapatani na Maandiko. Baraka yake inatamkwa juu ya wale wanaomsujudu yule mnyama na sanamu, yake, yaani, kundi lile lile hasa ambalo juu yake Biblia inatangaza kwamba ghadhabu ya Mungu isiyochanganywa na maji itamwagwa. [GC 625.1; PK Aya ya 32]

Tena, zaidi ya hayo, Shetani haruhusiwi kuigiza namna Kristo atakavyokuja mara ya pili. Mwokozi amewaonya watu Wake dhidi ya udanganyifu katika suala hilo, tena ametabiri waziwazi jinsi kuja Kwake mara ya pili kutakavyokuwa. “Kwa maana watatokea makristo wa uongo, na manabii wa uongo, nao watatoa ishara kubwa na maajabu; wapate kuwapoteza, kama yamkini, hata walio wateule. Basi wakiwaambia yuko jangwani, msitoke; yumo nyumbani, msisadiki; kama radi itokeavyo mashariki na kuangaza hata magharibi; ndivyo ujio wa Mwana wa Adamu utakavyokuwa” Mathayo 24:24-27, 31; 25:31; Ufunuo 1:7; 1 Wathesalonike 4:16, 17. Hakuna uwezekano wa kuwalaghai watu juu ya ujio huu wa Masihi kwani utafahamika ulimwenguni kote-- na kushuhudiwa na wote. [GC 625.2; PK Aya ya 33]

Ni wale tu waliokuwa wanafunzi wenye bidii wa Maandiko, walioupokea upendo wa ile Kweli (walioiweka Kweli katika matendo yao) ndio ambao watalindwa kutokana na madanganyo yale yenye nguvu sana yatakayouteka ulimwengu wote. Kwa ushuhuda wa Biblia watamng’amua mdanganyifu huyo aliyejigeuza katika umbile lake la bandia, ili kudanganya watu. Wakati wa kujaribiwa utawajia watu wote. Kwa njia ya chekecheke la majaribu, Mkristo wa Kweli atagundulika. Je, hivi watu wa Mungu siku hizi wamejizatiti kabisa juu ya

Neno Lake kiasi kwamba hawawezi kusalimu amri kwa ushawishi wa hisia zao? Je, katika wakati wa dharua na hatari kama huo, wangeweza kuing'ang'ania Biblia na Biblia peke yake? Shetani, ikiwezekana, atawazuia wasiweze kujitayarisha kusimama katika siku ile. Atayapanga mambo kwa njia ambayo itaifanya njia yao izungushiwe boma, atawanasa kwa hazina za dunia, na kuwafanya wabebe mzigo mzito ulemeao, hata mioyo yao italemewa na masumbufu ya maisha haya na siku ile ya kujaribiwa itaweza kuwajia kama mwizi. [GC 625.3; PK Aya ya 34]

Amri ile iliyotolewa na watawala mbalimbali wa Ulimwengu wa Kikristo dhidi ya wale wanaozishika amri (kumi za Mungu) itaondoa kwao ulinzi wa serikali na kuwaacha mikononi mwa wale wanaotaka kusababisha maangamizi yao, hapo ndipo watu wa Mungu watakapokimbia kutoka katika miji na vijiji na kujiunga pamoja katika makundi makundi, na kuishi mahali pa ukiwa na upweke sana. Wengi watapata kimbilio lao katika ngome za milima. Kama ilivyokuwa kwa Wakristo wa mabonde ya Piedmont, watapafanya mahali pa juu pa dunia kuwa mahekalu yao na watamshukuru Mungu kwa "ngome ya majabali" Isaya 33:16. Lakini wengi kati ya mataifa na makundi yote, wa juu na wa chini, matajiri kwa masikini, weusi kwa weupe, watatupwa katika kifungo cha uonevu na ukatili mkubwa. Wapenzi wa Mungu wanapitia siku za kuchosha na kuchakaza, wakiwa wamefungwa na minyororo, na kufungiwa gerezani, wakihukumiwa kuuawa, na wengine wakiachwa kufa kwa njaa katika magereza ya chini ya ardhi yachukizayo. Hakuna mwandamu aliye tayari kusikia kilio chao kichungu; hakuna aliye tayari kuwasaidia. [GC 626.1; PK Aya ya 35]

Je! Bwana atawasahau watu Wake katika saa hiyo ya kujaribiwa? Je! alimsahau Nuhu wakati ule hukumu Zake zilipopatilizwa juu ya ulimwengu ule uliokuwako kabla ya Gharika? Je! alimsahau Lutu moto uliposhuka chini kutoka mbinguni kuja kuiteketeza miji ile ya tambarare? Je! alimsahau Yusufu alipokuwa amezungukwa pande zote na waabudu sanamu wale wa Misri? Je! alimsahau Eliya wakati wa kiapo cha Yezebeli kilipomtishia maisha yake kwa ajili ya mambo yaliyowapata manabii wa Baali? Je! alimsahau Yeremia katika shimo lenye giza na lenye kukatisha tamaa kwa weusi wake ambalo lilikuwa ni nyumba yake ya kifungo? Je! aliwasahau wale vijana bora watatu katika tanuru la moto? au Danieli katika tundu la simba? [GC 626.2; PK Aya ya 36]

"Sayuni alisema, YEHOVA ameniacha, Bwana amenisahau. Je! Mwanamke aweza kumsahau mtoto wake anyonyae hata asimhurumie mwana wa tumbo lake? Naam, hawa waweza kusahau, lakini Mimi sitakusahau wewe. Tazama, nimekuchora katika vitanga vya mikono Yangu; Isaya 49:14-16. "Kwa maana BWANA wa majeshi asema hivi, ili nitafute utukufu amenituma kwa mataifa waliowateka ninyi; maana yeye awagusaye ninyi aigusa mboni ya jicho Lake" Zekaria 2:8. [GC 626.3; PK Aya ya 37]

Japokuwa maadui wanaweza kuwasukumia gerezani, kuta za magereza ya ardhini haziwezi kukata mawasiliano kati ya roho zao na Kristo. Yeye aonaye kila mapungufu waliyo nayo, alijuaye kila onjo (jaribu chungu), Yu juu ya mamlaka ya serikali zote za dunia hii; na malaika watawajia katika seli zile za upweke wa gereza, wakileta nuru na Amani kutoka mbinguni. Gereza litakuwa kama jumba la kifalme kwao; kwa maana wale walio matajiri wa imani wanaishi mle, na kuta zile za giza zitaangazwa kwa nuru ya mbinguni kama vile ilivyokuwa kwa Paulo na Sila walipokuwa wakiomba na kuimba nyimbo za sifa usiku ule wa manane katika gereza la chini ya ardhi kule Filipi. [GC 627.1; PK Aya ya 38]

Hukumu za Mungu zitamwagwa juu ya wale wanaojaribu kuwatesa na kuwaangamiza watu Wake. Uvumilivu Wake wa muda mrefu dhidi ya waovu unawatia ujasiri wanadamu kuendelea na dhambi zao, lakini adhabu yao hata hivyo, ni ya hakika na ya kutisha kwa sababu ya kucheleweshwa sana. "Maana Bwana ataondoka kama vile katika mlima Perasimu, ataghadhibika kama vile katika bonde la Gibeoni; apate kufanya kazi Yake, kazi Yake ya ajabu (ngeni)" (Strange Act) Isaya 28:21. Kwa Mungu wetu wa rehema kitendo cha kuadhibu ni kigeni Kwake, yaani kisicho cha kawaida, ni cha ajabu Kwake. "Kama Mimi niishivyo, asema Bwana MUNGU, sikufurahii kufa kwake mtu mwovu." Ezekieli 33:11. Bwana ni "mwingi wa huruma, Mwenye fadhili, si mwepesi wa hasira, mwingi wa rehema na Kweli,.....Mwenye kusamehe uovu na makossa na dhambi;" lakini bado "hataiondoa hatia kwa namna iwayo yote."Bwana si mwepesi wa hasira, ana uweza mwingi, wala hatamhesabia mtu mwovu kuwa hana hatia kamwe." Kutoka 34:6, 7; Nahumu 1:3. Kwa vitu vya ajabu na vya kutisha katika haki Mungu ataitetea mamlaka ya sheria Yake iliyokanyagwa chini. Ukali wa malipo ayastahiliyo mkaidi-sheria ya Mungu yanaweza yakapimwa kwa kukawia Kwake Bwana katika kutenda haki. Taifa ambalo analivumilia sana, na hatalipiga hata limejaa kipimo chake cha uovu katika hekima Yake Mungu, litainywea ghadhabu ya Mungu isiyochanganywa na rehema. [GC 627.2; PK Aya ya 39]

Wakati Kristo atakapokoma kufanya kazi Yake ya maombezi katika Patakatifu, ndipo itakapomwagwa ghadhabu Yake isiyochanganywa na maji ambayo imetishiwa dhidi ya wale wote wanaomsujudu yule mnyama na sanamu yake na kuipokea chapa yake (Ufunuo 14:9, 10). Mapigo juu ya Misri, wakati Mungu alipokuwa anakaribia kuwaokoa Israeli, yanafanana kwa tabia yake, na pia hukumu za kutisha zaidi zitakazoenea mahali pengi, ambazo zitaanguka juu ya dunia hii kabla tu ya kuokolewa mara ya mwisho kwa watu wa Mungu. Asema hivi mwandishi wa kitabu kile cha Ufunuo, akiyaelezea mapigo yale ya kuogofya sana: "Pakawa na jipu baya, bovu, juu ya wale watu wenye chapa ya huyo mnyama, na wale wenye kuisujudia sanamu yake." Bahari "ikawa damu kama damu ya mfu, na vitu vyote vyenye roho ya uhai katika bahari vikafa." Na "mito

na chemchemi za maji; zikawa damu." Japo ni ya kutisha mapigo hayo, kama jinsi yalivyo, haki ya Mungu inathibitishwa kikamilifu na waziwazi. Malaika wa Bwana anatangaza, anasema: "Wewe u Mwenye haki,... kwa kuwa umehukumu hivi; kwa kuwa walimwaga damu ya watakatifu na ya manabii, Nawe umewapa damu wainywe; nao wamestahili." Ufunuo 16:2-6. Kwa kitendo chao kile cha kuwapa hukumu ya kifo watu wa Mungu, hakika wamejipatia hatia ya damu yao kana kwamba ilikuwa imemwagwa kwa mikono yao. Vile vile, Kristo aliwatangazia Wayahudi wa siku Zake kwamba walikuwa na hatia ya damu yote ya watakatifu iliyokuwa imemwagwa tangu siku zile za Habili; kwa kuwa walikuwa na roho ile ile na walitafuta kufanya kazi hiyo hiyo na wale wauaji wa manabii. [GC 627.3; PK Aya ya 40]

Katika pigo linalofuata, uwezo unatolewa kwa jua ili lipate "kuwaunguza wanadamu kwa moto. Na wanadamu wakachomwa kwa maunguzo makubwa ya moto mkali." Mistari 8, 9. Hivi ndivyo manabii wanavyoeleza hali ya dunia katika wakati huo wa kuogofya sana: "Nchi inaomboleza;...maana nafaka imeharibika,... miti yote ya mashamba imekauka; kwa maana furaha imekauka katika wanadamu." "Mbegu zinaoza chini ya udongo wake; ghala zimeachwa ukiwa;... Jinsi wanyama wanavyougua! makundi ya ng'ombe yamefadhaika, kwa sababu hawana malisho;... Vijito vya maji vimekauka, na moto umeyateketeza malisho ya nyikani." "Tena nyimbo za hekaluni zitakuwa vilio siku ile, asema Bwana MUNGU; mizoga itakuwa mingi; kila mahali wataitupa, wakinyamaza kimya." Yoeli 1:10-12, 17-20; Amosi 8:3. [GC 628.1; PK Aya ya 41]

Mapigo haya si ya ulimwengu mzima na si kwamba watu wote wa dunia wataangamizwa. Ila yatakuwa ni mateso makali zaidi kuwahi kutokea kwa viumbe. Hukumu zote juu ya wanadamu kabla ya kufungwa kwa mlango wa rehema, zimechanganywa na rehema. Damu ya Yesu inayosihi imemkinga na kumzingira mdhambi ili asipate kipimo kamili cha hatia yake; lakini katika hukumu ya mwisho, ghadhabu inamwagwa pasipo kuchanganywa na rehema. [GC 628.2; PK Aya ya 42]

Katika siku hiyo umati mkubwa (watu wengi) wataitamani rehema ya Mungu ambayo wamekuwa wakiidharau kwa kipindi kirefu. "Angalia, siku zinakuja, asema Bwana Mungu, ambazo nitaleta njaa katika nchi; si njaa ya kukosa chakula, wala kiu ya kukosa maji, bali ya kukosa kuyasikia Maneno ya BWANA. Nao watatanga-tanga toka bahari hata bahari; na kutoka upande wa kaskazi hata upande wa mashariki; watapiga mbio, wakienda huko na huko, kulitafuta Neno la BWANA, wasilione." Amosi 8:11, 12. [GC 629.1; PK Aya ya 43]

Watu wa Mungu pia hawataepuka mateso; lakini wateswapo na kufadhaishwa, wakivumilia makali ya ufukara na kuteseka kwa kukosa chakula, hawataachwa waangamie. Ni kwamba Mungu Yule aliyemjali Eliya hatampita yeyote kati ya watoto Wake waliojitoa nafsi zao. Yeye azihesabuye nywele za vichwa vyao

atawajali na katika wakati wa njaa watashibishwa. Waovu wakiwa wanaangamia kwa njaa na tauni, malaika watawakinga watakatifu na kuwapatia mahitaji yao. Kwa yeye "aendaye kwa haki" kuna ahadi: "atapewa chakula chake; maji yake hayatakoma." "Maskini na wahitaji wanatafuta maji, wala hapana; ndimi zao zimekauka kwa kiu; Mimi BWANA, nitawasikia, Mimi Mungu wa Israeli, sitawaacha." Isaya 33:15, 16; 41:17. [GC 629.2; PK Aya ya 44]

"Maana mtini hautachanua maua, wala mzabibuni hamtakuwa na matunda; Taabu ya mzeituni itakuwa bure, na mashamba hayatatoa chakula; zizini hamtakuwa na kundi, wala vibandani hamtakuwa na kundi la ng'ombe;" lakini wanaomcha Bwana "watamfurahia BWANA" wa wokovu wao. Habakuki 3:17, 18. [GC 629.3; PK Aya ya 45]

"Bwana Ndiye Mlinzi wako; BWANA ni uvuli mkono wako wa kuume. Jua halitakupiga mchana wala mwezi wakati wa usiku. Bwana atakulinda na mabaya yote; atakulinda nafsi yako." "Maana Yeye atakuokoa na mtego wa mwindaji, na katika tauni iharibuyo. Kwa manyoya Yake atakufunika, chini ya mbawa Zake utapata kimbilio; uaminifu Wake ni ngao na kigao. Hutaogopa hofu ya usiku, wala mshale urukao mchana, wala tauni ipitayo gizani, wala maafa yanayotokea mchana, Ijapo watu elfu waanguka ubavuni pako. Naam, kumi elfu mkono wako wa kuume! Hata hivyo hautakukaribia wewe. Ila kwa macho yako utatazama, na kuyaona malipo ya wasio haki. Kwa kuwa Wewe BWANA Ndiwe kimbilio langu; Umemfanya Aliye juu kuwa makao yako. Mabaya hayatakupata wewe, wala tauni haitaikaribia hema yako." Zaburi 121:5-7; 91:3-10. [GC 629.4; PK Aya ya 46]

Lakini katika jicho la kibinadamu itaonekana kuwa watu wa Mungu lazima watie ushuhuda wao kwa muhuri wa damu zao kama ilivyokuwa kwa wafia dini kabla yao. Nao pia wanaanza kuogopa kuwa Mungu kawaacha wateswe na maadui zao. Ni muda wa maumivu yatishayo. Usiku na mchana wanamlilia Mungu awaokoe. Waovu wanafurahi sana na vicheko vya kuwazomea vinasikika: "Imani yenu I wapi sasa?" "Kwa nini Mungu wenu hawaokoi kutoka kwetu kama kweli ninyi ni watu Wake?" Lakini hawa wamngojao wanakumbuka namna Yesu alivyokufa msalabani Kalwari na makuhani wakuu na watawala wakimkejeli: "Aliokoa wengine, hawezi kujiokoa Mwenyewe. Yeye ni mfalme wa Israeli; na ashuke sasa msalabani, nasi tutamwamini." Mathayo 27:42. Kama Yakobo, wote wanapambana mieleka na Mungu. Nyuso zao zinaelezea hangaiko lao la ndani. Kubadika rangi kunaonekana kwenye ngozi ya nyuso zao (rangi inapauka-pale). Lakini hawakomi katika kujipatanisha kwao kwa dhati kupitia maombi. [GC 630.1; PK Aya ya 47]

Laiti kama wanadamu wangekuwa na macho yenye njozi za kimbingu, wangeweza kuona wingu kubwa la makundi ya malaika wenye nguvu kuu wakiwazunguka wale waliolitunza Neno la Mungu kwa uvumilivu wa Kristo. Kwa upole wa huruma kubwa, malaika wameshuhudia na kuiona dhiki yao na

wamesikia maombi yao. Wanasubiri Neno kutoka kwa Mkuu wao ili kuwaondosha katika hatari inayowakabili. Lakini bado wanapaswa kusubiri kwa kitambo kidogo tena. Watu wa Mungu wanapaswa kukinywea kikombe kile na kubatizwa wa ubatizo ule. Kuchelewa huko, kunakowaumiza, ni jibu sahihi zaidi kwa maombi yao. Wanapotazamia kumsubiri kwa imani Bwana kutenda, wanaongozwa kujifunza imani, tumaini na uvumilivu ambavyo wamekuwa wakijizoesha kwa kiasi kidogo sana katika mitindo yao ya maisha ya kidini. Lakini, kwa ajili ya wale wateule, wakati huo wa taabu utafupishwa. “Na Mungu, je! Hatawapatia haki wateule Wake wanaomlilia mchana na usiku? ... Nawaambia atawapatia haki upesi.” Luka 18:7, 8. Mwisho utakuja kwa haraka zaidi ya vile wanadamu wategemeavyo. Ngano itakusanywa na kufungwa katika matita tayari kuwekwa kwenye ghala la Mungu; magugu yatafungwa kama matita ya kuni kwa ajili ya kuangamizwa motoni. [GC 630.2; PK Aya ya 48]

Walinzi wa mbinguni, walio waaminifu kwa wajibu wao, wanaendelea na ulinzi wao. Japokuwa amri ya ulimwengu mzima imeweka muda ambao wazishikao amri kumi watauawa, maadui wao wataihisi hiyo amri na kabla ya muda uliotajwa watajaribu kuwaua. Lakini hakuna anayeweza kuwapita walinzi hawa wenye nguvu wanaomzunguka kila mtu aliye mwaminifu. Wengine katika kukimbia kwao toka mijini na vijijini wanashambuliwa; lakini panga zilizoinuliwa juu yao ili kuwakata zinavunjika na kuanguka chini zikiwa hazina nguvu kabisa kama vile bua. Wengine wanalindwa na malaika katika umbile la wanajeshi. [GC 631.1; PK Aya ya 49]

Katika zama zote, Mungu amekuwa akitenda yote kupitia malaika Zake watakatifu kwa ajili ya kuwaokoa watu Wake. Hawa viumbe wa mbinguni wamekuwa wakihusika sana katika utendaji wa masuala ya wanadamu. Wamekuwa wakionekana katika mavazi yang’aayo kama umeme; wamekuja kama wanadamu katika umbile na mavazi ya wasafiri. Malaika wametokea katika umbile la wanadamu kwa watu wa Mungu. Wamepumzika mwaloni wakati wa adhuhuri, kana kwamba wamechoka sana. Wamekubali kupokea ukarimu waliofanyiwa katika nyumba za wanadamu. Wamekuwa wakifanya kazi yao kama walinzi kwa wasafiri waliokuwa hawana ufahamu. Wamewasha moto katika madhabahu kwa mikono yao wenyewe. Wamefungua milango ya magereza na kuwatoa watumishi wa Bwana. Wakivikwa na utukufu wa Mbinguni, walikuja kulivingirisha jiwe nakulitoa kutoka kwenye kaburi la Mwokozi. [GC 631.2; PK Aya ya 50]

Katika umbile la wanadamu, malaika wamekuwa wakikaa mara kwa mara katika vikao vya wenye haki; na huenda kutembelea katika makusanyiko ya waovu, kama walivyokwenda Sodoma kupata taarifa ya matendo yao, ili kutoa uamuzi kama wamevuka mpaka wa uvumilivu wa Mungu. Mungu anapendezwa na rehema; na kwa ajili ya watu wachache wanaomtumikia kwa unyofu, Yeye

huzuia majanga na kurefusha utulivu miongoni mwa watu wengi. Ni shida mno kwa wale wanaotenda dhambi dhidi ya Mungu kutambua ya kwamba wanawiwa uhai walio nao kutokana na hao waaminifu wachache ambao wao wanafurahia kuwadhihaki na kuwatesa. [GC 631.3; PK Aya ya 51]

Ijapokuwa watawala wa dunia hii hawalijui hilo, lakini katika mabaraza yao malaika wamekuwa wazungumzaji wakuu. Macho ya wananadamu yamewatazama; masikio ya wanadamu yamesikia hoja na miito yao; midomo ya wanadamu imeyapinga mashauri yao na kuyadhihaki mausia yao; mikono ya wanadamu imekumbana nao na kuwafedhehesha kwa kuwatukana na kuwatendea vibaya. Katika kumbi za mabaraza na mahakama ya sheria wajumbe hao wa mbinguni wameonyesha uelewa wao wa ndani wa historia ya mwanadamu; wamejionyesha wenyewe kuwa wanao uwezo bora wa kutetea hoja ya wale wanaoonewa kuliko watetezi wao waliokuwa na uwezo na ufasaha mwingi sana. Wameyavunjilia mbali makusudi mabaya na kuyazuia maovu ambayo yangeweza kuichelewesha sana kazi ya Mungu na kusababisha mateso makubwa kwa watu Wake. Katika saa ile ya mateso na dhiki, "Malaika wa BWANA hufanya kituo, Akiwazungukia wamchao na kuwaokoa." Zaburi 34:7. [GC 632.1; PK Aya ya 52]

Kwa shauku kubwa, watu wa Mungu wanazisubiri ishara za kuja kwa Mfalme wao. Kama vile walinzi walakiwavyo, "Habari gani za usiku.?" Na jibu linatolewa bila kusitasita, "Mchana unakuja na usiku pia" Isaya 21:11, 12. Mwanga unang'aa kwenye mawingu juu ya vilele vya milima. Punde kutakuwa na udhihirisho wa utukufu Wake. Jua la haki linakaribia kuangaza. Umekaribia mchana na usiku --ni mwanzo wa mchana usio na mwisho kwa wenye haki, na kushuka kwa usiku wa milele kwa waovu. [GC 632.2; PK Aya ya 53]

Wale wanaoshindana mweleka kwa kutoa dua zao kwa bidii mbele za Mungu, pazia lile linalowatenga na ulimwengu wa wale wasioonekana kwa macho linaonekana kana kwamba limeondolewa kabisa. Mbingu zinakuwa nyekundu kutokana na kupambazuka kwa siku ile ya milele, na kama wimbo mtamu miongoni mwa nyimbo zile za malaika maneno haya yanaanguka katika sikio lao: "Simameni imara katika utii wenu. Msaada uko njiani." Kristo, Mshindi hodari, anawaonyesha taji ya utukufu wa milele askari Wake waliochoka sana; na sauti Yake inatoka katika milango ile iliyoachwa wazi, ikisema: "Tazama, Mimi ni pamoja nanyi. Msiogope. Mimi nazijua huzuni zenu zote; nimeyachukua masikitiko yenu. Hampigani vita hii dhidi ya maadui ambao hawajajaribiwa. Nimepigana vita hiyo kwa niaba yenu, na katika Jina Langu ninyi ni zaidi ya washindi." [GC 632.3; PK Aya ya 54]

Mwokozi wetu wa thamani ataleta msaada Wake pale tunapouhitaji sana. Njia ya kwenda mbinguni imewekwa safi kwa nyayo Zake. Kila mwiba unaochoma na kuumiza nyayo zetu ulikwishachoma nyayo Zake. Kila msalaba tunaopaswa

kuubeba Yeye amekwisha kuubeba kabla Yetu. Bwana huruhusu mapambano ili kuiandaa mioyo yetu kwa ajili ya Amani. Wakati wa taabu ni jaribio la kutisha kwa watu wa Mungu; ila ndio muda wa kila aaminiye kutazama juu na kwa imani ataona upinde wa ahadi ukimzunguka. [GC 633.1; PK Aya ya 55]

"Nao waliokombolewa na Bwana watarejea, watafika Sayuni wakiimba; furaha ya milele itakuwa juu ya vichwa vyao; watapata shwangwe na furaha; huzuni na kuugua zitakimbia. Mimi, naam, Mimi Ndimi niwafarijiye; wewe u nani hata ukamwogopa mtu atakayekufa, na mwanadamu atakayefanywa kuwa kama majani? Ukamsahau Bwana Mungu Muumba wako, Yeye aliyezitanda mbingu na kuiweka misingi ya dunia; nawe unaogopa daima mchana kutwa kwa sababu ya ghadhabu yake yeye aoneaye, hapo afanyapo tayari kuharibu; nayo I wapi ghadhabu yake aoneaye? Yeye aliyehamishwa na kufungwa atafunguliwa kwa haraka; wala hatakufa na kushuka shimoni, wala chakula chake hakitapunguka. Maana Mimi ni Bwana Mungu wako niichafuaye bahari mawimbi yake yakavuma. Bwana wa majeshi ndilo Jina Lake. Nami nimetia Maneno yangu kinywani mwako, Nami nimekusitiri katika kivuli cha mkono wangu" Isaya 51:11-16. [GC 633.2; PK Aya ya 56]

"Basi, kwa sababu ya hayo, ulisikilize Neno hili, ewe uliyeteswa na kulewa lakini si kwa mvinyo, BWANA, Bwana wako na Mungu wako, awateteaye watu Wake, asema hivi, Tazama nimeondoa mkononi mwako kikombe cha kulevya-levya, hilo bakuli la kikombe cha hasira Yangu; hutavinywea tena; Nami nitakitia mikononi mwao wakutesao; waliokuambia nafsi yako, Inama, tupate kupita; nawe uliufanya mgongo wako kuwa kama nchi, na kama njia, kwa hao wapitao juu yake" Mistari 21-23. [GC 633.3; PK Aya ya 57]

Jicho la Mungu likitazama zama zote, liliona zahama ambayo itawakabili watu Wake, ambayo watu wanapaswa kuipitia wakati ambapo mamlaka ya dunia hii inapojipanga kuwa kinyume nao. Kama mateka wanavyokuwa uhamishoni, nje ya nchi yao, watahofia kifo kutokana na njaa na kuuawa kikatili. Lakini, Yule Aliye Mtakatifu aliyeigawanya bahari ya Shamu mbele ya wana wa Israeli atadhihirisha nguvu Yake na kuwaweka huru, hawatakuwa mateka tena. "Nao watakuwa watu Wangu, asema Bwana wa majeshi; naam, watakuwa hazina Yangu hasa; Mimi nitawaachilia, kama vile mtu amwachiliavyo mwanawe mwenyewe amtumikiaye." Malaki 3:17. Ikiwa damu ya mashahidi waaminifu wa Kristo ingemwagwa wakati huu, isingeweza kuwa kama mbegu iliyopandwa ili kupata mavuno kwa ajili ya Mungu kama ilivyokuwa kipindi cha wafia dini. Uaminifu wao usingekuwa ushahidi kuwashiwishi wengine waukubali Ukweli; kwa kuwa moyo mkaidi umeyarudisha nyuma mawimbi ya rehema, hata hayawezi kabisa kurudi tena. Ikiwa wenye haki wangeachwa wawe mateka kwa maadui zao hata sasa, ingekuwa ni ushindi kwa upande wa mfalme wa giza. Mwandishi wa Zaburi anasema: "Mradi atanisitiri bandani mwake siku ya mabaya, Atanisitiri katika

sitara ya hema yake, Na kuniinua juu ya mwamba" Zaburi 27:5. Kristo alisema hivi "Njoni watu Wangu, ingia wewe ndani ya vyumba vyako, ukafunge mlango nyuma yako ujifiche kitambo kidogo mpaka ghadhabu hii itakapopita. Kwa maana tazama, Bwana anakuja kutoka mahali Pake, ili kuwaadhibu wakaao duniani, kwa sababu ya uovu wao" Isaya 26:20, 21. Wokovu wa wale wote waliousubiri ujio Wake Bwana kwa uvumilivu na wale ambao majina yao yameandikwa katika kitabu cha uzima utakuwa wa utukufu mkubwa kiasi gani! [GC 634.1; PK Aya ya 58]

# SURA YA 40

# WATU WA MUNGU WAKOMBOLEWA

## (Ujio Wa Mfalme)

Ufupisho: Macho ya mbingu yanaangalia dhiki kuu ambayo inakaribia, na katika kilele chake, Mungu ataingilia kati, kitabu cha Ufunuo kina unabii wa kushangaza kuhusu matukio haya. Jifunze wakati huo ambao ulinzi na usalama wa mwanadamu utaondolewa kwa wale wanaomheshimu Mungu na kutakuwa na harakati za kuwaangamiza. Kisha jifunze zaidi kuhusu ule wakati ambao Yesu atarudi kuwachukua wateule Wake. Mnga'o Wake utazidi jua la mchana, atashuka chini ya mawingu, na kila jicho litauona utukufu Wake wa kushangaza.

Wakati ulinzi utokanao na sheria za kibinadamu utakapoondolewa kutoka kwa wale wanaoiheshimu sheria ya Mungu (amri za Mungu), ndipo kutakuwepo na harakati katika nchi mbalimbali kwa wakati ule ule kuwaua. Wakati uliowekwa katika ile amri unapokaribia, watu watafanya njama kwa siri ili kuking'oa kabisa kikundi cha imani wanachokichukia. Itaamuliwa kuwapa pigo moja la uhakika katika usiku mmoja ambalo litainyamazisha kabisa sauti ile inayopinga mafundisho yao, na ambayo inawaonya. [GC 635.1; PK Aya ya 1]

Watu wa Mungu - baadhi wakiwa vifungoni kwenye vyumba vyao vya magereza, wengine wakiwa wamejificha katika mahali pa usalama, siri na upweke katika misitu na milima - wakiwa bado wanaendelea kumlilia Mungu na kuomba ulinzi Wake, wakati ambapo kila upande una makundi ya watu wenye silaha, wakisukumwa na majeshi ya malaika wale waovu, wanajiandaa kufanya kazi yao ya mauaji. Ni katika wakati huu wa uhitaji, katika saa ya kilele cha dharura kwa ajili ya mateso, ndipo Mungu wa Israeli atakapoingilia kati ili kuwaokoa watelule Wake. Asema hivi Bwana; "Mtakuwa na wimbo kama vile wakati wa usiku, ishikwapo sikukuu takatifu, mtakuwa na furaha ya moyo kama

vile mtu aendapo na filimbi katika mlima wa Bwana, aliye Mwamba wa Israeli. Naye Bwana atawasikizisha watu sauti Yake ya utukufu, Naye atawaonyesha jinsi mkono Wake ushukavyo, na ghadhabu ya hasira Yake, na mwako wa moto ulao, pamoja na dhoruba, na tufani, na mvua ya mawe ya barafu." Isaya 30:29, 30…. [GC 635.2; PK Aya ya 2]

Katikati ya kelele za ushindi, dhihaka, na laana, msongamano wa watu waovu unakaribia kuvamia mawindo yake, na tazama giza nene zaidi ya giza la usiku, linaifunika dunia. Ndipo upinde wa mvua unaong'aa kwa utukufu ule utokao kwenye kiti cha enzi cha Mungu unatanda mbinguni na unaonekana kana kwamba unakizunguka kila kikundi cha watu kinachosalia. Umati wa watu wenye hasira unapatwa mshangao wa ghafla. Makelele yao ya dhihaka yanakoma. Walengwa wa hasira zao za uuaji wanasahauliwa. Kwa hisia za hofu, wanakodoa macho yao kuiangalia ishara ya agano la Mungu na wanatamani wakingwe dhidi ya mng'ao Wake mkali unaowazidi nguvu. [GC 635.3; PK Aya ya 3]

Kwa upande wa watu wa Mungu, inasikika sauti iliyo wazi na tamu, ikisema, "Tazameni juu," nao wanapoyainua macho yao juu mbinguni, wanauona upinde wa ahadi. Mawingu meusi yenye ghadhabu yaliyolifunika anga yanatawanyika nao kama Stefano wanatazama juu mbinguni kwa bidii na kuuona utukufu wa Mungu na Mwana wa Adamu wakiwa wameketi juu ya kiti Chake cha enzi. Katika umbile Lake la Kiungu wanazitambua alama za kudhalilishwa Kwake; na kutoka kinywani Mwake wanasikia ombi likiwasilishwa mbele ya Baba Yake na malaika watakatifu: "hao ulionipa nataka wawe pamoja Nami popote nilipo" Yohana 17:24. Tena inasikika sauti tamu kama muziki, nayo ni ya ushindi, inasema: "Hao wanakuja! Hao wanakuja! Ni watakatifu, hawana madhara yoyote, wala hawajanajisiwa. Wamelitunza Neno la subira Yangu; watatembea miongoni mwa malaika; "na midomo iliyopauka, iliyogeuka rangi, na kutetemeka, ya wale ambao wameshikilia sana imani yao, inapaza sauti juu kwa ushindi. [GC 636.1; PK Aya ya 4]

Ni wakati wa usiku wa manane Mungu anapodhihirisha nguvu Zake kwa ajili ya kuwakomboa watu Wake. Jua linajitokeza, likiangaza kwa nguvu zake zote. Ishara na maajabu vinafuatana kwa haraka na kwa mfululizo. Waovu wanayatazama matukio hayo kama video au filamu kwa hofu na mshangao mkubwa, wakati wenye haki wanatazama kwa furaha kuu viashiria hivi vya ukombozi wao. Kila kitu miongoni mwa vitu vya asili vinaonekana kuondoka katika utaratibu wake. Mito inakoma kutiririka. Mawingu meusi na mazito yanainuka juu na kugongana. Katikati ya mbingu yenye giza na ghadhabu ipo nafasi moja iliyo wazi yenye utukufu usioelezeka, ambamo inatoka sauti ya Mungu kama sauti ya maji mengi, ikisema: "Imekwisha kuwa." Ufunuo 16:17. [GC 636.2; PK Aya ya 5]

**Mbingu Na Nchi Kutetemeka**

Sauti hiyo inatetemesha mbingu na nchi, na panatokea tetemeko la ardhi kubwa, “ambalo tangu wanadamu kuwako juu ya nchi hapakuwa namna ile, jinsi lilivyokuwa kubwa tetemeko hilo.” fungu la 17, 18. Anga linaonekana kana kwamba linafunguka na kujifunga. Utukufu ule unaotoka katika kiti cha enzi cha Mungu unaonekana kana kwamba unamulika kupitia anga hilo. Milima inatikisika kama unyasi katika upepo na miamba iliyopasuka na kutawanywa kila upande. Inasikika ngurumo kama tufani inayokuja. Bahari inajipiga-piga kwa kuchafuka. Kunasikika mlio wa sauti kubwa nyembamba kama mayowe ya sauti ya mapepo waliotumwa kufanya maangamizi. Nchi yote inapata kwikwi na kuumuka kama mawimbi ya bahari. Uso wa dunia unataka kupasuka. Misingi yake inaonekana imeanza kupata ufa. Safu za milima zinazama chini. Visiwa vilivyokaliwa na watu vinatoweka. Miji yenye bandari ambayo imekuwa kama Sodoma kwa uovu wake inamezwa na maji yenye hasira. Babeli mkuu umekumbukwa mbele za Mungu, na “kupewa kikombe cha mvinyo ya ghadhabu ya hasira Yake.” Mawe makubwa ya mvua, “kila moja likiwa na uzito kama wa talanta,” yanafanya kazi yao ya uharibifu (talanta= 56Kg). Mafungu la 19, 21. Miji ya dunia yenye kiburi imeshushwa chini. Maeneo ya kifahari ya kifalme, ambayo juu yake watu wakuu wa dunia wametapanya mali na utajiri wao mwingi ili kujitukuza wenyewe, yanaporomoka na kuwa magofu mbele ya macho yao. Kuta za magereza zinapasuka vipande vipande, na watu wa Mungu, ambao walikuwa wameshikiliwa humo kama wafungwa kwa ajili ya imani yao, wanawekwa huru. [GC 636.3; PK Aya ya 6]

Makaburi yanafunguka, na “Tena, wengi wa hao walalao katika mavumbi ya nchi wataamka, wengine wapate uzima wa milele, wengine aibu na kudharauliwa milele” Danieli 12:2. Wale wote ambao wamekufa katika imani ya Ujumbe wa Malaika wa Tatu wataamka kutoka makaburini wakiwa wana utukufu, ili kusikia agano la Mungu la amani analofanya pamoja na wale ambao wameshika sheria Yake (amri za Mungu). “Na hao waliomchoma” (Ufunuo 1:7), wale waliomdharau na kumkejeli Kristo alipokuwa anapata maumivu Yake makali yaliyopelekea kifo Chake, pamoja na wapinzani waliokuwa na jeuri kubwa dhidi ya Kweli Yake na watu Wake, wanafufuliwa ili wapate kumtazama katika utukufu Wake na kuona heshima wanayopewa wale walio waaminifu na watiifu. [GC 637.1; PK Aya ya 7]

Mawingu mazito bado yamelifunika anga; lakini baada ya muda, jua linapenyeza na kuonekana kila baada ya muda fulani, linaonekana kana kwamba ni jicho la Yehova linalolipiza kisasi. Umeme mkali wa radi unaruka kutoka mbinguni na kuifunika dunia kwa blanketi la ndimi za moto. Juu ya ngurumo za radi za kutisha, sauti za kushangaza, mbaya na zisizojulikana, zinatoa hukumu kwa waovu. Maneno yaliyosemwa yalikuwa hayaeleweki kwa wote lakini yanaeleweka kinagaubaga na walimu wa uongo. Wale ambao hapo kitambo

kidogo tu kilichopita walikuwa watu wasiojali, wazembe, wenye kujitapa, wakaidi, na washangiliaji juu ya ukatili wao kwa watu watunzao amri za Mungu, sasa wametindikiwa na mfadhaiko mkubwa na, tena wanatetemeka vibaya kwa hofu. Yowe zao zinasikika juu ya sauti ya vitu vya asili- kama tetemeko, tufani na mawimbi. Mapepo, yaani, mashetani wanakiri Uungu Wake Kristo na kutetemeka mbele ya nguvu Zake Mungu, wakati huo huo wanadamu wanaomba rehema Yake huku wakitembelea magoti na kujidhalilisha kwa kuomba msamaha kutokana na hofu kuu iliyowashika. [GC 637.2; PK Aya ya 8]

**Siku Ya Bwana**

Manabii wa kale walisema, walipoiona katika maono matakatifu siku ya Mungu: "Pigeni kelele za hofu; maana siku ya Bwana i karibu; itanyesha kama maangamizi yatokayo kwa Mwenyezi Mungu." Isaya 13:6. "Ingia ndani ya jabali; ukajifiche mavumbini mbele za utisho wa Bwana, mbele za utukufu wa enzi Yake. Macho ya mwanadamu yaliyoinuka yatashushwa chini, na kiburi cha mwanadamu kitainamishwa, Naye Bwana, Yeye peke Yake, atatukuzwa siku hiyo. Kwa maana kutakuwa siku ya Bwana wa majeshi juu ya watu wote wenye kiburi na majivuno, na juu ya yote yaliyoinuka; nayo yatashushwa chini." "Siku hiyo kila mtu atazitupilia mbali sanamu zake za fedha, na sanamu zake za dhahabu, walizojifanyia ili kuziabudu, kwa fuko na popo; ili aingie ndani ya pango za majabali, na ndani ya tundu za miamba iliyopasuka, mbele za utisho wa Bwana na utukufu wa enzi Yake, atakapoondoka ili aitetemeshe mno dunia." Isaya 2:10-12, 20, 21. [GC 638.1; PK Aya ya 9]

Kupitia uwazi katikati ya mawingu, nyota inamulika na mng'ao wake unaongezeka mara nne ukilinganisha na lile giza lililokuwepo. Inatangaza maneno ya matumaini na furaha kwa wale walio waaminifu, ila inatamka ukali na hasira kwa wavunjaji wa sheria ya Mungu. Wale ambao wameyatoa kafara yote kwa ajili ya Kristo sasa na kujitaabisha, sasa wako salama, wamefichwa katika hema la siri la Yeye aliye juu. Wamekwisha kupewa jaribio mbele ya ulimwengu na mbele ya wale wanaoudharau Ukweli nao wameudhihirisha uadilifu wao Kwake Yeye aliyekufa kwa ajili yao, Badiliko la ajabu limewatokea wale ambao wameshikilia kwa uthabiti uadilifu wao hata walipokabili kifo ana kwa ana. Wamekombolewa ghafla kutoka katika giza na ukatili wa kutisha sana, wa wale wanadamu waliojigeuza kuwa mapepo/mashetani. Nyuso zao, ambazo hapo awali zilikuwa zimepauka na kugeuka rangi, zenye wasiwasi, na zenye huzuni, na kudhoofika, sasa zinang'aa kwa mshangao, imani na upendo. Wanazipaza sauti zao katika wimbo wa ushindi: "Mungu kwetu sisi ni kimbilio na nguvu, Msaada utakaoonekana tele wakati wa mateso, Kwa hiyo hatutaogopa ijapobadilika nchi, Ijapotetemeka milima moyoni mwa bahari. Maji yake yajapovuma na kuumuka,

Ijapopepesuka milima kwa kiburi chake" Zaburi 46:1-3 Zaburi 46:1-3. [GC 638.2; PK Aya ya 10]

Wakati Maneno haya ya dhamana takatifu yanapopanda juu kwenda kwa Mungu, mawingu yanarudi nyuma, kisha mbingu zenye nyota zinaonekana zikiwa na utukufu usioelezeka kwa kulinganishwa na anga jeusi lenye ghadhabu lililo pande zote mbili. Utukufu wa jiji la mbinguni unatiririka kama mkondo wa mwanga katika malango yaliyoachwa wazi. Ndipo unaonekana mkono angani ukiwa umezishikilia mbao mbili za mawe pamoja. Nabii anasema:"Na mbingu zitatangaza haki Yake, Kwa maana Mungu Ndiye aliye hakimu." Zaburi 50:6. Sheria takatifu, haki ya Mungu, ambayo ilitangazwa katikati ya ngurumo na miali ya moto kutoka Sinai kama mwongozo wa maisha yetu, sasa inafunuliwa kwa wanadamu kama kanuni ya hukumu (Yak 2:10-12). Mkono unazifungua hizo mbao, na kisha ndani yake kunaonekana kanuni za Sheria ile ya Amri Kumi, zikiwa zimeandikwa kwa kufuatiliziwa juu yake, kana kwamba kwa kalamu ya moto. Maneno yako wazi sana kiasi kwamba watu wote wanaweza kuyasoma, kumbukumbu ya kila mmoja inaamshwa, giza la ushirikina na uzushi linafutwa kutoka katika kila akili ya mtu, na kisha zile kauli Kumi za Mungu, fupi, na za kina (nyanja zote), zenye mamlaka, zinawasilishwa machoni pa wakazi wote wa dunia. [GC 639.1; PK Aya ya 11]

Haiwezekani kabisa kuelezea utisho mkuu na kukata tamaa kutakakowapata wale ambao wamekanyaga chini ya miguu yao matakwa hayo matakatifu ya Mungu (Amri Kumi Ebr 10:26-31). Ni Bwana Ndiye aliwapa sheria Yake hii; Wangeweza kuzilinganisha tabia zao na hiyo sheria na kujifunza kurekebisha dosari zao wakati bado kuna fursa ya kutubu na kufanya matengenezo; lakini ili kupata ukubali wa ulimwengu, waliziweka pembeni kanuni Zake na kuwafundisha wengine kuzivunja (kuasi). Walijitahidi sana kuwalazimisha watu wa Mungu kuinajisi Sabato Yake, na sasa wanaadhibiwa na sheria hiyo ambayo wameidharau. Kwa uwazi wa kuogofya, wanaona kwamba hawana udhuru wowote, walimchagua yule ambaye walimtumikia na kumwabudu. "Ndipo mtakaporudi, nanyi mtapambanua kati ya wenye haki na waovu, na kati ya yeye amtumikiaye Mungu na yeye asiyemtumikia." Malaki 3:18. [GC 639.2; PK Aya ya 12]

**Matokeo Ya Kukosa Uaminifu**

Maadui wa sheria ya Mungu (Amri Zake), kuanzia wachungaji na kushuka chini hadi kwa yule aliye mdogo kabisa miongoni mwao, sasa wanapata uelewa mpya wa Ukweli na wajibu wao uliowapasa kutenda. Kwa kuchelewa sana wanaona kwamba Sabato ya amri ya nne ndiyo muhuri wa Mungu aliye hai (Kutoka 20:6-11 Ufu 7:1-4). Kwa kuchelewa mno wanagundua asili halisi ya sabato yao ya bandia, sabato ya uongo na msingi walioujenga juu ya mchanga. Wanagundua kwamba

wamekuwa wakipambana dhidhi ya Mungu. Walimu wa dini wameziongoza nafsi upotevuni, na huku wakidai wamekuwa wakiwaongoza kwenye malango ya Paradiso. Ni mpaka siku ya hukumu ya mwisho (katika kutoa hesabu) ndipo utakapojulikana uzito wa wajibu walio nao wanadamu wanaoshika ofisi takatifu na jinsi yalivyo ya kutisha matokeo ya kukosa uaminifu. Ni katika umilele peke yake ndipo tunaweza kukadiria kwa usahihi hasara ya kupotea kwa roho moja. Maangamizi yatakuwa ni ya kuogofya kwake yeye ambaye Mungu atamwambia maneno haya: Ondoka Kwangu, wewe mtumishi mwovu. [GC 640.1; PK Aya ya 13]

Sauti ya Mungu inasikika kutoka mbinguni, ikitangaza siku na saa ya kuja Kwake Yesu, na inawapa watu Wake agano la milele. Kama sauti ya ngurumo ya radi nzito, zaidi ya kengele yenye sauti kubwa, maneno Yake yanabiringika duniani kote. Wasraeli wa Mungu wanasimama kusikiliza na huku wamekodoa macho yao kuelekea juu. Nyuso zao zinaangazwa kwa utukufu Wake, na kung'aa kama uso wa Musa ulivyong'aa aliposhuka kutoka Sinai. Waovu hawawezi kuwaangalia. Na baraka inapotamkwa juu ya wale ambao wamemheshimu Mungu kwa kuitunza na kuitakasa Sabato Yake, kelele kubwa ya ushindi inasikika. [GC 640.2; PK Aya ya 14]

Muda si mrefu, linatokea wingu dogo jeusi kutoka mashariki, takribani nusu ya ukubwa wa kiganja cha mkono wa mtu, ni wingu linalomzunguka Mwokozi na ambalo linaonekana kwa mbali kana kwamba limefunikwa na giza. Watu wa Mungu wanatambua kwamba ile ndiyo ishara ya Mwana wa Adamu. Kwa ukimya uliojaa kicho wanakazia macho wingu linapoendelea kukaribia duniani, likizidi kuwa jepesi na lenye utukufu zaidi, mpaka linakuwa wingu kubwa jeupe, chini yake kuna utukufu kama moto unaoteketeza, na juu yake kuna upinde wa mvua wa agano. Yesu anatokea wakati huu kama mshindi Mkuu Mwenye nguvu. Wakati huu Yeye siyo "Mtu wa Huzuni," anayekuja ili kukinywea kikombe kichungu cha aibu na mateso, Yeye anakuja sasa akiwa mshindi wa mbingu na nchi, kuwahukumu walio hai na waliokufa. "Mwaminifu na wa Kweli," "Naye kwa haki ahuhukumu na kufanya vita." na "na majeshi yaliyo mbinguni" (Ufunuo 19:11, 14) yanamfuata Yeye. Pamoja na nyimbo za mbinguni za kumsifu Mungu, malaika watakatifu wengi, umati mkubwa usiokuwa na idadi, unamsindikiza katika safari Yake. Anga linaonekana kujazwa na maumbo yanayometameta "elfu kumi mara elfu kumi, na maelfu ya maelfu." hakuna kalamu ya binadamu yoyote inayoweza kuonyesha mandhari hiyo; hakuna akili yenye asili ya kufa, ina uwezo wa kuelezea au kuwazia kuhusu utukufu Wake. "Utukufu Wake ulifunika mbingu, nayo dunia ikajaa sifa Yake. Mwangaza Wake ulikuwa kama nuru." Habakuki 3:3, 4. Wakati wingu lile lililo hai linapozidi kukaribia zaidi na zaidi, kila jicho linamwona Huyo Mfalme wa uzima (Kristo). Hakuna taji ya miiba sasa inayoharibu au kujeruhi kichwa hicho kitakatifu; ila kuna taji ambayo ni ya

utukufu, kama utepe hivi, nao unatulia juu ya kipaji cha uso Wake mtakatifu. Uso Wake unang'aa kuliko mng'ao mzuri wa jua la mchana unaotia macho kiwi." "Naye ana Jina limeandikwa katika vazi Lake na paja Lake, MFALME wa wafalme, na BWANA wa mabwana." Ufunuo 19:16. [GC 640.3; PK Aya ya 15]

Mbele ya uwepo Wake "nyuso zote zimegeuka rangi." Wale wakataaji wa rehema ya Mungu, hofu kuu inawaangukia, nayo inawakatisha tamaa milele." "Hata moyo unayeyuka, na magoti yanagongana-gongana; viunoni mwote mna utungu,..... na nyuso za wote zimekuwa nyeupe kwa hofu." Yeremia 30:6; Nahumu 2:10.. Wenye haki wanalia kwa kutetemeka: "Ni nani atakayeweza kusimama?" wimbo wa malaika unasitishwa, na kuna kipindi cha ukimya wa kutisha. Ndipo sauti ya Yesu inasikika, ikisema: "Neema Yangu yakutosha." nyuso za wenye haki zinachangamka, na furaha inaujaza kila moyo. Kisha malaika wanapiga noti iliyo juu zaidi na kuimba tena wanapoendelea kusogea karibu na dunia. [GC 641.1; PK Aya ya 16]

**Mfalme Wa Wafalme Atokezea**

Mfalme wa wafalme anashuka juu ya wingu ambalo limeviringwa kwa moto uwakao, mbingu zinakunjwa pamoja kama ukurasa wa kitabu, dunia inatetemeka mbele Zake, na kila mlima na kisiwa kinahama kutoka mahali pake. "Mungu wetu atakuja wala hatanyamaza, Moto utakula mbele Zake, na tufani yavuma sana ikimzunguka pande zote. Ataziita mbingu zilizo juu, Na nchi pia awahukumu watu Wake." Zaburi 50:3, 4. [GC 641.2; PK Aya ya 17]

"Na wafalme wa dunia, na wakuu, na majemadari, na matajiri, na wenye nguvu, na kila mtumwa, na mwungwana, wakajificha katika pango na chini ya miamba ya milima, wakiiambia milima na miamba, Tuangukieni, tusitirini, mbele za uso Wake Yeye aketiye juu ya kiti cha enzi, na hasira ya Mwana-Kondoo. Kwa maana siku iliyo kuu, ya hasira yao, imekuja; naye ni nani awezaye kusimama?" Ufunuo 6:15-17. [GC 642.1; PK Aya ya 18]

Zile kejeli za dharau zinakoma. Midomo ya waongo inanyamazishwa, na sasa iko kimya. Mgongano wa silaha, msukosuko wa vita, "Maana silaha zote za mtu mwenye silaha wakati wa mshindo, na mavazi yaliyofingirishwa katika damu" (Isaiah 9:5), vinasitishwa. Hakuna kinachosikika sasa isipokuwa sauti ya maombi na sauti ya kilio na maombolezo. Kilio hiki kinalipuka kwa nguvu midomoni mwa wale waliokuwa wakitoa futuhi muda mfupi uliopita: "Siku kuu ya ghadhabu Yake imekuja; naye ni nani atakayeweza kusimama?" Waovu huomba kuzikwa chini ya miamba ya milima kuliko kukutana na uso wa Yeye ambaye wamemdharau na kumkataa. [GC 642.2; PK Aya ya 19]

Sauti ile ipenyajo masikioni mwa wafu, wanaijua. Ni mara ngapi sauti Yake iliyosihi, na ya upole imewaita wapate kutubu. Ni mara ngapi wameisikia sauti hiyo kupitia kwa Rafiki yao, Kaka yao, na Mkombozi wao akiwasihi na akigusa mioyo yao. Kwa wale walioikataa neema Yake, hakuna sauti nyingine iwayo yote ambayo kwao ingetoa shutuma nyingi sana, ambayo ingewalaani sana, kama ile sauti ambayo kwa muda mrefu imekuwa ikitoa wito wa kuwasihi: "Ghairini, ghairini, mkaache njia zenu mbaya; mbona mnataka kufa," Ezekieli 33:11. Oh! Laiti ingekuwa sauti ya mgeni kwao! Yesu anasema "Kwa kuwa nimeita, nanyi mkakataa; Nimeunyosha mkono Wangu, asiangalie mtu; Bali mmebatilisha shauri Langu, Wala hamkutaka maonyo Yangu;" Mithali 1:24, 25. Sauti hiyo inaamsha kumbukumbu ambazo wangetamani kuzifutilia mbali—yaani maonyo yale waliyoyadharau, mialiko ile waliyoikataa, fursa zile nzuri walizozichezea na kuzikejeli. [GC 642.3; PK Aya ya 20]

Hapo wapo wale waliomdhihaki Kristo wakati wa kufedheheshwa Kwake. Kwa nguvu inayowatetemesha yanakuja akilini mwao maneno Yake Yeye Mteswa, wakati, alipokuwa ameagizwa kwa kiapo na kuhani mkuu, aliposema kwa uzito na utulivu: "Tangu sasa mtamwona Mwana wa Adamu ameketi mkono wa kuume wa nguvu, akija juu ya mawingu ya mbinguni." Mathayo 26:64. Sasa wanamwona katika utukufu Wake, na bado watamwona akiwa ameketi mkono wa kuume wa nguvu. [GC 643.1; PK Aya ya 21]

Wapo wale waliodharau dai Lake la kwamba Yeye ni Mwana wa Mungu, sasa hawana la kusema. Yupo yule Herode mwenye majivuno makubwa ambaye alimdhihaki kwa sauti kubwa na ujeuri kuhusiana na cheo Chake cha kifalme na kuwaambia askari-jeshi waliokuwa wanamdhihaki kumvika taji kama mfalme. Hapo wapo wale watu ambao kwa mikono yao miovu waliweka juu ya mwili Wake joho la zambarau, na juu ya paji la uso Wake mtakatifu, taji ya miiba na katika mkono Wake ambao haukuwa na ubishi, ile fimbo ya kifalme ya bandia, na kusujudu mbele zake kama ibada ya dhihaka iliyojaa kufuru. Watu waliompiga na kumtemea mate Yule aliye Mkuu wa uzima, sasa wanageukia mbali kutoka kwenye macho Yake yaliyokazwa juu yao na kupenya mpaka ndani yao, nao wanatafuta kutimua mbio ili waende mbali na uwepo Wake unaowazidi nguvu. Wale walioipigilia misumari kwenye viganja Vyake vya mikono na miguu Yake, Pamoja na yule askari aliyemchoma ubavuni Mwake, wanazitazama alama hizi kwa hofu kuu na majuto makuu. [GC 643.2; PK Aya ya 22]

Kwa uwazi unaoogofya sana, makuhani na watawala wanayakumbuka matukio yale ya Kalvari. Kwa hofu kuu na kutetemeka vibaya sana, wanakumbuka jinsi walivyotikisa vichwa vyao kwa shangwe ya kishetani, wakisema kwa nguvu: "Yeye ni mfalme wa Israeli; na ashuke sasa msalabani, nasi tutamwamini. Amemtegemea Mungu; na amwokoe sasa, kama anamtaka." Mathayo27:42, 43. [GC 643.3; PK Aya ya 23]

Kwa uwazi kabisa wanakumbuka mfano wa Mwokozi wa wakulima waliokataa kumpa bwana wao matunda ya shamba la mizabibu, ambaye waliwadhulumu kwa kuwatendea vibaya watumishi wake na kumwua mwanawe. Pia, wanakumbuka hukumu ambayo wao wenyewe waliitamka kwa bwana wa shamba la mizabibu "atawaangamiza vibaya watu wale watu waovu." Katika dhambi na adhabu ya wale watu wasio waaminifu, makuhani na wazee wanaona njia yao wenyewe waliyoipita na adhabu yao wenyewe ya haki na sasa kunazuka kilio cha uchungu wa kufa. Kwa sauti ya juu kuliko ile kelele ya, "Msulubishe, Msulubishe," ambayo ilivuma katika mitaa ya Yerusalemu, kili cha maombolezo ya kutisha, na kukata tamaa kinazidi kuongezeka, kikisema, "Huyu Ndiye Mwana wa Mungu! Huyu Ndiye Masihi wa Kweli!" Wanatafuta kukimbia kutoka katika uwepo wa Mfalme wa wafalme. Katika mapango ya kina ya ardhi, yaliyotokea kutokana na mpasuko wa ardhi inayogongana yenyewe (tetemeko, majanga ya asili), wanajaribu kujificha bila mafanikio. [GC 643.4; PK Aya ya 24]

**Mungu Awaita Watakatifu Wake**

Katika maisha ya wale wote wanaokataa Ukweli kuna nyakati ambapo dhamira zao huamka, wakati ambapo kumbukumbu za maisha yao ya unafiki inawaumiza vibaya sana na moyo unasumbuliwa sana na majuto yasiyoweza kuwasaida lolote. Lakini hayo ni kitu gani ikilinganishwa na majuto ya siku ile wakati "Hofu yao ifikapo kama tufani, na msiba (wao) ufikapo kama kisulisuli," Mithali 1:27. Wale ambao walimwangamiza Kristo na watu Wake waaminifu sasa wanashuhudia utukufu ulio juu yao. Katikati ya hofu yao ile kuu wanasikia sauti za watakatifu wakiimba na vyombo vya nyuzi (kinubi) kwa furaha wakisema: "Tazama, huyu Ndiye Mungu wetu, Ndiye tuliyemngoja atusaidie;". Mithali 1:27. [GC 644.1; PK Aya ya 25]

Katikati ya kuwayawaya kwa dunia, kumulika kwa umeme, na ngurumo kali za radi, sauti ya Mwana wa Mungu inawaita watakatifu waliolala watoke nje, anayatazama makaburi ya wenye haki, kisha, akiinua mikono Yake mbinguni, anasema kwa nguvu: "Amkeni, amkeni, amkeni, ninyi mlalao mavumbini, nasema tena inukeni!" Katika marefu na mapana ya dunia wafu wataisikia sauti hiyo, na wale wanaoisikia watapata uzima (wenye haki, Yoh 5:25). Na dunia yote itarindima kwa vishindo vya kukanyaga kwa jeshi kubwa sana la kila taifa, kabila, lugha na jamaa. Kutoka katika nyumba ya gereza la mauti, hao wanatoka, wakiwa wamevikwa utukufu ya kutokufa, wakilia: "U wapi, Ewe mauti, kushinda kwako? U wapi, Ewe mauti, uchungu wako?" 1Wakorintho 15:55. Na wenye haki wale walio hai na watakatifu waliofufuka wanaziunganisha sauti zao na kupiga kelele za furaha kwa muda mrefu, na shangwe za ushindi. [GC 644.2; PK Aya ya 26]

Wote wanatoka makaburini mwao wakiwa na kimo kile kile walipoingia makaburini mwao. Adamu, ambaye anasimama kati ya umati ule mkubwa uliofufuliwa, ana kimo kirefu sana na umbo zuri la fahari, kwa urefu yuko chini kidogo tu ya Mwana wa Mungu. Anaonyesha tofauti inayoonekana wazi kwa watu wa vizazi vile vilivyofuata baadaye, katika kipengele hiki kimoja kunaonekana uharibifu mkubwa wa afya wa jamii ya wanadamu. Lakini wote wanatokezea na upya wa nguvu, uchangamfu na afya za ujana wa milele. Hapo mwanzo, mwanadamu aliumbwa kwa sura ya Mungu, si kwa tabia tu, bali kwa umbo na sura. Dhambi ikanyumbua/ikajeruhi sura na kuwa karibu kabisa kuifutilia mbali sura ya Mungu; lakini Kristo alikuja kukirudisha kile kilichokuwa kimepotea. Ataibadilisha miili yetu hii mibovu na minyonge ili ipate kufanana na mwili Wake wa utukufu (Fil 3:21). Umbile hili linalokufa, linaloharibika, lisilo na uzuri wowote, ambalo zamani lilichafuliwa na dhambi, linakuwa kamilifu, zuri sana, na lisiloweza kufa milele. Mawaa na ulemavu wote huachwa mle kaburini. Wakiwa wamerejeshwa kwenye mti wa uzima wa Edeni ile iliyopotea kwa muda mrefu, waliokombolewa wataendelea "kukua" (Malaki 4:2) hadi watakapofikia kwenye kimo kamili cha wanadamu walichokuwa nacho katika utukufu ule wa kwanza kabisa. Viashiria vya mwisho vilivyosalia vya laana ya dhambi vitaondolewa, na waaminifu Wake Kristo wataonekana katika "uzuri wa Bwana Mungu wetu," katika akili na roho na mwili, wakiakisi sura kamilifu ya Bwana wao. Loo! Huu ni ukombozi wa ajabu sana! Uliozungumziwa Habari zake kwa muda mrefu sana, na kutumainiwa kwa muda mrefu, Na kufikiriwa kwa matamanio makubwa, lakini haukuweza kueleweka kwa ukamilifu wake. [GC 644.3; PK Aya ya 27]

**Wanabadilika Kwa Dakika Moja**

Katika kila upande wa gari lile la wingu kuna mabawa, na chini yake kuna magurudumu yaliyo hai; na gari linapopaa kwenda juu, magurudumu yake yanapiga kelele, "Mtakatifu," na mabawa, yanaporuka, yanapaza sauti, Mtakatifu," na msururu wa malaika hupaza sauti, "Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu, Bwana Mungu Mwenyezi" na waliokombolewa wanapaza sauti (kama kiitikio), "Haleluya!" wakati gari linapoondoka na kusonga mbele kuelekea kule Yerusalemu mpya. [GC 645.2; PK Aya ya 28]

Kabla ya kuingia katika Jiji la Mungu, Mwokozi anawapa wafuasi Wake nishani za ushindi na anawavalisha beji za vyeo vya kifalme. Safu ya jeshi linalometameta linasimama katika umbo la mraba ulio na nafasi wazi katikati Yake kumzunguka Mfalme wao, ambaye umbile Lake tukufu huinuka juu ya watakatifu na Malaika Zake kwa urefu, ambaye kipaji Chake cha uso kinaangaza juu yao, kikiwa kimejaa upendo Wake mwanana. Katika jeshi lisilo na idadi la waliokombolewa, kila jicho limekazwa Kwake, kila jicho linatazama utukufu

Wake Yeye ambaye “sura Yake ilikuwa imeharibiwa kuliko wanadamu wote, na umbo Lake kuliko wanadamu.” Juu ya vichwa vya washindi, Yesu kwa mkono Wake wa kuume anaweka taji ya utukufu. Kwa kila mmoja kuna taji, yenye “jina jipya” lake mwenyewe (Ufunuo 2:17), na maandishi, “Mtakatifu kwa Bwana.” Katika kila kiganja cha mkono wa mshindi linawekwa tawi la mtende na kinubi kinachometameta. Kisha, malaika waongozaji wanapiga noti, kila mkono unagusa nyuzi za kinubi ukizicharaza zile nyuzi kwa mguso wa ustadi, unaoamsha muziki mtamu katika aina nyingi za sauti zenye kupendeza. Furaha kuu isiyoneneka inausisimua kila moyo, na kila sauti inainuliwa juu kwa sifa ya shukrani Pamoja na sifa hizi: “Yeye atupendaye na kutuosha dhambi zetu katika damu Yake, na kutufanya kuwa ufalme, na makuhani kwa Mungu, Naye ni Baba Yake; utukufu na ukuu una Yeye hata milele na milele. Amina.” Ufunuo 1:5, 6. [GC 645.3; PK Aya ya 29]

Mbele ya umati uliosongama wa waliokombolewa linaonekana Jiji Takatifu. Yesu anayafungua wazi malango ya lulu, na mataifa yale ambayo yameitunza Kweli na haki Yake yanaingia. Hapo wanaiona Paradiso ya Mungu, nyumba ya Adamu katika hali yake ya kutokuwa na hatia (bustani Isaya 26:2, Mwanzo 2:7-10, 16, Ufunuo 22:1-5). Ndipo sauti hiyo, iliyo bora na tamu kuliko muziki wowote uliopata kusikika kwenye sikio la mwanadamu, inasikika, ikisema: “Pambano lenu limekwisha.” “Njooni, ninyi mliobarikiwa na Baba Yangu, urithini ufalme uliotayarishwa kwa ajili yenu tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu.” [GC 646.1; PK Aya ya 30]

Sasa ndipo linatimia ombi alilolitoa Mwokozi kwa wanafunzi Wake: “Hao ulionipa nataka wawe pamoja Nami popote nilipo.” “Kuwasimamisha mbele ya utukufu wake bila mawaa katika furaha kuu” (Yuda 24), Kristo anawawasilisha kwa Baba Yake wale aliowanunua kwa damu Yake, akitangaza: “Mimi hapa, na watoto ulionipa.” “Wote wale ulionipa nimewatunza.” Lo! ni maajabu yalioje hayo ya upendo ule unaokomboa! Furaha kuu ya saa ile wakati ambapo Baba wa milele, anapowatazama waliokombolewa, atakapoiona sura Yake, mafarakano yaliyosababishwa na dhambi yamefutiliwa mbali, waa la uharibifu likiwa limekwisha ondolewa, na mwanadamu kwa mara nyingine tena anakuwa katika upatanifu na Mungu! [GC 646.2; PK Aya ya 31]

Kwa upendo usioweza kuelezeka, Yesu anawakaribisha waaminifu Wake katika furaha ya Bwana wao. Furaha Yake Mwokozi ni katika kuwaona, katika ufalme Wake wa utukufu, watu ambao wameokolewa kwa uchungu mkali wa mateso yake na kudhalilishwa Kwake pale msalabani. Ndipo waliokombolewa watakuwa washiriki wa furaha Yake, wanapotazama, miongoni mwa waliobarikiwa, wale ambao wameokolewa kwa kupitia maombi yao, jitihada zao, na kuwapenda kwa kujitolea kafara wenyewe. Wanapokusanyika kukizunguka kiti cha enzi cha ajabu

cheupe, furaha isiyoneneka itajaza mioyo yao, watakapowatazama wale ambao walishugulika kuhusu wokovu wao na kuwaleta kwa Kristo, na kuona jinsi yule mmoja alivyoleta wengine, na hao kuwapata wengine zaidi, wote wakiwa wameletwa kwenye bandari ya raha na pumziko, pale pale wataziweka taji zao miguuni Pake Yesu na kumsifu Yeye katika duru ya vipindi vinavyojirudia ambavyo havina mwisho milele hata milele. [GC 647.1; PK Aya ya 32]

**Adamu Wale Wawili Wakutana**

Wale waliokombolewa wanapokaribishwa katika Jiji la Mungu, kunasikika angani sauti ya kelele za kengele za shangwe na kuabudu. Adamu wale wawili wanakaribiana ili wakutane. Mwana wa Mungu anasimama akiwa amenyoosha mikono Yake kumpokea baba wa jamii yetu ya ubinadamu (baba wa dunia!) -- kiumbe yule ambaye Yeye alimuumba, ambaye alimtenda dhambi Muumba Wake na ambaye kwa ajili ya dhambi yake alama zile za kusulubiwa zinabebwa kwenye mwili wa Mwokozi. Adamu anapozitambua alama zile za misumari ile ya ukatili, yeye haanguki kifuani mwa Bwana Wake, lakini kwa unyonge na kujidhili anajitupa miguuni Pake, akisema: “Anastahili, anastahili Mwana-Kondoo aliyechinjwa!” Kwa upole Mwokozi anamwinua na kumwambia atazame tena makazi ya Edeni ambayo aliondolewa muda mrefu sana uliopita (Mwa 3:22-24). [GC 647.2; PK Aya ya 33]

Baada ya kufukuzwa kwake kutoka Edeni, maisha ya Adamu hapa duniani yalijawa na huzuni. Kila jani lililokuwa linanyauka, kila mnyama wa dhabihu aliyechinjwa, kila dosari juu ya uso mzuri wa viumbe vya asili, kila waa juu ya usafi wa maisha ya mwanadamu, ilikuwa ni ukumbusho mpya wa dhambi yake. Uchungu wa majuto ulikuwa wa maumivu ya kutisha alipouona uovu ukiongezeka, na, kama jibu kwa maonyo yake, alikutana na aibu na lawawa zilizotupwa juu yake mwenyewe, akaambiwa kwamba yeye ndiye msababishaji wa dhambi. Kwa unyenyekevu unaostahimili alibeba adhabu ya maasi yake, kwa karibu miaka elfu moja. Kwa uaminifu alitubu dhambi yake na kutumainia wema wa Mwokozi aliyeahidiwa, naye akafa katika tumaini la ufufuo. Mwana wa Mungu alileta ukombozi katika kushindwa na kuanguka kwa mwanadamu; na sasa, kwa kupitia kazi Yake ya upatanisho, Adamu anarudishwa katika Milki yake ya kwanza. [GC 647.3; PK Aya ya 34]

Akiwa amejawa na furaha na shangwe, anaitazama miti ambayo hapo awali ilikuwa ya kupendeza na furaha kwake—miti ile ile ambayo yeye mwenyewe alikuwa amechuma matunda yake katika siku zake za kutokuwa na hatia na alipokuwa na usafi wa maisha na furaha, anaona mizabibu: ambayo mikono yake mwenyewe imeipogoa au kuielekeza pa kutambaa, maua yale yale ambayo hapo awali alikuwa akiyatunza na kuyapenda. Akili yake inapata ufahamu halisi wa mandhari (sura ya nchi) aliyoifahamu kwamba hii Kweli ni Edeni iliyorejeshwa,

na sasa ni yenye kupendeza zaidi kuliko wakati alipofukuzwa humo. Mwokozi anamwongoza hadi kwenye ule mti wa uzima na kuchuma tunda lenye tukufu na kumwagiza ale. Anatazama karibu yake na kuona umati mkubwa wa jamaa yake waliokombolewa, wakisimama katika Paradiso ya Mungu, ndipo anatupa taji yake yenye kumeta-meta chini ya miguu ya Yesu na anaangukia kifuani Pake, na anamkumbatia Mkombozi Wake. Anakigusa kinubi chake cha dhahabu na mapaa yale yenye dari ya juu ya mbinguni yanarudia kwa mwangwi wimbo wa ushindi: "Anastahili, anastahili, anastahili Mwana-Kondoo aliyechinjwa, akaishi tena!" Familia ya Adamu wanaitikia wimbo huo na kutupa taji zao kwenye miguu ya Mwokozi wanapoinama mbele Zake kwa kuabudu. [GC 648.1; PK Aya ya 35]

Muungano huu unashuhudiwa na Malaika waliolia machozi wakati wa anguko la Adamu na kushangilia wakati Yesu, baada ya kufufuka Kwake, alipopaa mbinguni, akiwa amelifungua kaburi kwa ajili ya wote watakaoliamini Jina Lake. Sasa, wanaona kazi Yake ya ukombozi imekamilikana wanaunganisha sauti zao katika kuimba wimbo wa sifa Kwake. [GC 648.2; PK Aya ya 36]

**Wale 144,000!**

Panapo bahari ya fuwele iliyo mbele ya kiti cha enzi, bahari ya kioo iliyoonekana kama imechanganywa na moto, -- inayopendeza na kuvutia sana kwa rangi yake kwa ajili ya utukufu wa Mungu, -- wanakusanyika kundi la wale "waliomshinda yule mnyama na sanamu yake; na juu ya alama yake, na juu ya hesabu ya jina lake."* Pamoja na Mwana-Kondoo juu ya Mlima Sayuni, "wenye vinubi vya Mungu," wanasimama, wale mia na arobaini na nne elfu waliokombolewa kutoka miongoni mwa wanadamu; kisha ikasikika kama sauti ya maji mengi, na kama sauti ya radi kuu, sauti ya wapiga vinubi wakipiga vinubi vyao. Nao wanaimba "wimbo mpya" mbele ya kiti cha enzi, wimbo ambao hakuna mtu awezaye kujifunza isipokuwa wale mia na arobaini na nne elfu, ni wimbo wa Musa na Mwana-Kondoo, wimbo wa ukombozi ambao hakuna yeyote awezaye kuuimba wimbo huu ila wale mia na arobaini na nne elfu wanaoweza kujifunza wimbo huo kwa kuwa ni wimbo wa uzoefu wao--uzoefu wa maisha waliyopambana nayo ambao hakuna kundi lingine lolote limewahi kuwa nao. "Hawa ndio wamfuatao Mwana-Kondoo kila aendako." Hawa, wakiwa wamenyakuliwa kutoka hapa duniani wakachukuliwa miongoni mwa walio hai, wanahesabiwa kama "matunda ya kwanza kwa Mungu na kwa Mwana- Kondoo-malimbuko." Ufunuo 15:2, 3; 14:1-5. "Hawa ndio waliotoka katika dhiki kuu;" wamepitia wakati wa taabu ambao haujawahi kuwapo tangu lilipoanza kuwapo taifa; wamestahimili utungu wa wakati uo huo (Dan 12:1) wa taabu ya Yakobo; wamesimama bila kuwa na mwombezi na mtetezi katika kipindi cha kumwagwa hukumu za mwisho za Mungu. Lakini wameokolewa, kwa maana "wamefua mavazi yao, na kuyafanya meupe katika damu ya Mwana-Kondoo." "na Katika

vinywa vyao haikuonekana hila, kwa maana hawana hatia" mbele Zake Mungu. hapo awali "Kwa hiyo wako mbele ya kiti cha enzi cha Mungu, nao wanamtumikia mchana na usiku katika hekalu Lake; Naye aketiye juu ya kiti cha enzi atakaa kati yao." wameona dunia ikiwa ikiharibiwa kwa njaa, magonjwa, ukiwa na tauni, jua likipewa uwezo wa kuwaunguza wanadamu kwa joto kuu, na wao wenyewe wamevumilia mateso, njaa, na kiu. Lakini, "hawataona njaa tena, wala hawataona kiu tena, wala jua halitawapiga, wala hari iliyo yote wako mbele ya kiti cha enzi cha Mungu, nao wanamtumikia mchana na usiku katika hekalu Lake, na Yeye aketiye katika kiti cha enzi atatanda hema Yake juu yao. Hawataona njaa tena, wala hawataona kiu tena, wala jua halitawapiga, wala hari iliyo yote. Kwa maana huyo Mwana-Kondoo, aliye katikati ya kiti cha enzi, atawachunga, Naye atawaongoza kwenye chemchemi za maji yenye uhai, na Mungu atayafuta machozi yote katika macho yao." Ufunuo 7:14-17. [GC 648.3; PK Aya ya 37]

Katika zama zote, wateule wa Mwokozi wamefundishwa na kulelewa katika shule ya maonjo (kupimwa Imani na kujaribiwa). Walitembea katika njia ile nyembamba duniani (uzoefu mchungu wa Maisha); wametakaswa katika tanuru ya mateso. kwa ajili Yake Yesu wamevumilia upinzani, chuki, na kusingiziwa ili kushushwa hadhi zao. Walimfuata kupitia migogoro mikali sana na kustahimili kujinyima, kujikana nafsi zao na kukabiliwa na hali za kukatisha tamaa. Kutokana na uzoefu wao wenyewe wenye uchungu walijigundua ubaya wa dhambi, nguvu zake, hatia yake, madhara yake na wanaitazama kwa chuki kubwa. Utambuzi wao wa dhabihu isiyo na kifani ambayo ilitolewa kama tiba inawapa unyenyekevu na kujiona si kitu machoni pao wenyewe na kuijaza mioyo yao shukrani na sifa ambazo wale viumbe ambao hawajaanguka kamwe hawawezi kuelewa au kuthamini. Wanapenda zaidi kwa sababu wamesamehewa mno. Wamekuwa washirika wa mateso ya Kristo, hivyo wametayarishwa wafae kushiriki Pamoja Naye utukufu Wake. [GC 649.1; PK Aya ya 38]

Warithi wa Mungu wametoka katika dari za nyumba, vibanda vibovu vya kimasikini, magereza ya chini ya ardhi, majukwaa ya kunyongea watu, milimani, jangwani, kutoka katika mapango ya ardhi, na kutoka katika mapango ya bahari. Wakiwa hapa duniani walikuwa" wahitaji, wakiteswa, wakiudhiwa na kutendewa mabaya" (Ebr. 11:3). Mamilioni miongoni mwao walishuka makaburini wakiwa wamebebeshwa na watu mzigo wa sifa mbaya kwa sababu walikataa kwa uthabiti kukubali madai ya uongo ya Shetani. Kwa mahakama za kibinadamu walihukumiwa kuwa ni wahalifu wabaya zaidi. Lakini sasa "Mungu Ndiye aliye hakimu." Zaburi 50:6. Sasa maamuzi yale yaliyotolewa na wanadamu yanabatilishwa. "Atafuta machozi katika nyuso zote; na aibu ya watu Wake ataiondoa" Isaya 25:8. "Nao watawaita, Watu watakatifu, Waliokombolewa na Bwana;" Yeye amepanga kwamba wao "wapewe taji ya maua badala ya majivu,

mafuta ya furaha badala ya maombolezo, vazi la sifa badala ya roho nzito; wapate kuitwa miti ya haki, iliyopandwa na Bwana, ili atukuzwe." Isaya 62:12; 61:3. Wao si watu wanyonge, walioteswa, ambao wanaoonewa, na kutawanywa kila mahali na kunyanyaswa vibaya. Tangu sasa na kuendelea watakuwa na Bwana milele. Wanasimama mbele ya kiti cha enzi wakiwa wamevaa majoho ya kitajiri kuliko yale waliyopata kuvaa waheshimiwa wakuu mno wa duniani hapa. Wamevalishwa vilemba vya kifalme vyenye utukufu mwingi kuliko vilivyopata kuwekwa juu ya  vipaji vya uso wa wafalme wa kidunia. Siku za uchungu na maombolezo zimekoma milele (zimepitwa na wakati), Mfalme wa utukufu ameyafuta machozi katika nyuso zote; kila chanzo cha huzuni kimeondolewa. Miongoni mwa wale wanaopepea matawi ya mitende, wimbo wa sifa unamiminika, ulio wazi, mtamu, na wenye sauti  zinazochanganyika kwa upatanifu; kila sauti huwa na mkazo inapopokea wimbo huo na chombo cha nyuzi (kinubi), mpaka wimbo huo mkuu wa kumsifu Mungu unavuma katika mapaa ya majumba  ya mbinguni, wakisema: "Wokovu una Mungu wetu aketiye katika kiti cha enzi, na Mwana- Kondoo." na wakaaji wote wa mbinguni huitikia kwa maandishi haya: "Amina: Baraka, utukufu, na hekima, na shukrani, na heshima na nguvu na uweza, kwa Mungu wetu hata milele na milele. Amina." Ufunuo 7:10, 12. [GC 650.1; PK Aya ya 39]

Katika maisha haya tunaweza tu kuanza kidogo kulielewa somo hili kuu la ajabu la ukombozi. Kwa ufahamu wetu finyu wenye ukomo tunaweza kufikiria kwa dhati na bidii kabisa aibu na utukufu, uzima na kifo, haki na rehema, mambo ambayo yanakutana pale msalabani; lakini hata hivyo, pamoja na kuzitanua sana nguvu zetu za akili tunashindwa kuelewa maana yake kamili. Urefu na upana, kina na kimo, cha upendo unaokomboa hueleweka kwa kiwango kidogo tu. Mpango wa wokovu hautaweza kueleweka kikamilifu, hata wakati ule wale waliokombolewa wakapoona kama jinsi wanavyoonwa na kujua kama jinsi wanavyojuliwa; lakini kupitia enzi (vizazi) za milele Ukweli mpya utaendelea kufunuliwa daima, na kuistajabisha akili na kuipa furaha tele. Ingawa huzuni na uchungu na majaribu ya dunia yamekoma na chanzo chake kuondolewa watu wa Mungu daima watakuwa  uelewa ulio wazi akilini mwao wa kujua jinsi wokovu wao ulivyogharimu. [GC 651.1; PK Aya ya 40]

Msalaba wa Kristo utakuwa ndiyo sayansi na wimbo wa waliokombolewa katika milele zote. Ndan ya Kristo aliyetukuzwa watamwona Kristo aliyesulubiwa. Haitasahaulika kamwe kwamba Yeye ambaye uwezo Wake uliumba na kuzitegemeza sayari zisizo na idadi katika milki kubwa sana ya anga Lake lisilo na kikomo, Yule Mpendwa wa Mungu, Yule Mfalme wa mbinguni, Yeye ambaye makerubi na maserafi wanaong'aa wanafurahia, kumcha na kumpenda,--alijinyenyekesha Mwenyewe ili amwinue mwanadamu aliyeanguka dhambini; hadi kubeba hatia na aibu ya dhambi na uso wa Baba Yake kufichwa, mpaka

msiba wa ulimwengu uliopotea ulipopasua moyo Wake na kuponda-ponda maisha Yake juu ya msalaba wa Kalwari. Kwamba Yule Muumbaji wa sayari zote, Mwasisi wa miisho yote, apate kuuweka kando utukufu Wake na kujidhalilisha Mwenyewe kutokana na upendo Wake kwa mwanadamu, daima tendo Lake litasisimua mshangao na kuhamasisha ibada katika sayari zote. Wakati mataifa ya waliokombolewa yanapomtazama Mkombozi wao na kuuona utukufu wa milele wa Baba uking'aa Usoni Mwake; wanapokitazama kiti Chake cha enzi, ambacho kipo tangu milele hata milele, na kujua kwamba ufalme Wake hauna mwisho, wanabubujika kwa wimbo wa shangwe kubwa wa kutukuza wakisema: "Anastahili, anastahili Mwana-Kondoo aliyechinjwa, Naye alitukomboa kwa Mungu kwa njia ya damu Yake ya thamani!" [GC 651.2; PK Aya ya 41]

Siri ya msalaba inafafanua sira na mafumbo mengine yote yasiyoeleweka katika nuru inayobubujika kwenye mkondo unaotoka pale Kalvari, sifa za Mungu ambazo zilikuwa zimetujaza hofu, woga na kicho (kwa kumdhania kwamba ni mkali na mlipiza kisasi) zinaonekana nzuri na tena za kuvutia. Rehema, upole na upendo ule wa mzazi unaonekana unapatana na utakatifu, haki, na mamlaka Yake. Wakati tunautazama utukufu wa kiti Chake cha enzi, kilicho juu na kuinuliwa, twaiona tabia Yake katika udhihirisho wake wa ukarimu mwingi na kuelewa vizuri, kuliko wakati mwingine wowote kabla ya hapo, umuhimu wa Cheo kile kinachoashira upendo, "Baba yetu." [GC 652.1; PK Aya ya 42]

Itakuja kudhihirika kwamba Yeye ambaye hekima Yake haina kikomo hakuweza kubuni mpango mwingine wowote kwa ajili ya wokovu wetu isipokuwa tu kumtoa Mwanawe kafara. Fidia au malipo ya kafara hii ni furaha ya kuijaza dunia kwa viumbe waliokombolewa, watakatifu, wenye furaha na wasiokufa. Matokeo ya pambano la Mwokozi wetu dhidi ya nguvu za giza na furaha ya waliokombolewa, watakatifu wenye furaha, na wasiokufa. Matokeo ya pambano kati ya Mwokozi wetu na nguvu za giza na furaha ya wale waliokombolewa, vitamletea Mungu utukufu milele zote. Na hii ndiyo thamani ya roho ambayo Baba anaridhishwa na gharama iliyolipwa na Kristo Mwenyewe, akitazama matunda ya kafara Yake ile kuu, anaridhika. [GC 652.2; PK Aya ya 43]

*Wale 144,000 Juu ya bahari ya kioo iliyo mbele ya kiti kile cha enzi, yaani, bahari ya kioo iliyochangamana na moto, - ing'aayo sana kwa utukufu wa Mungu, - limekusanyika lile kundi la wale waliopata ushindi dhidi ya mnyama [upapa], na sanamu yake [Uprotestanti ulioasi], na chapa [alama] yake [Jumapili yake], na hesabu ya jina lake [666]. Soma zaidi katika Ufunuo 7, 13, na 14.

# SURA YA 41

# UKIWA WA DUNIA

**(Dunia Yaangamizwa, Na Muda Wa Kufikiri Kwa Makini)**

Ufupisho: Dunia hii inawayawaya tayari kuanguka, na Je, ni nini kitafuatia? Sura hii inazungumzia kuhusu miaka 1000 au milenia ya Ufunuo, Sura ya 20, muda huu hauko mbali. Wakati muda utasimama na Shetani ataanza kulipia uovu wake. Angalia muda huu kama jambo jema la kucheua mambo, kwani Pambano kuu linakaribia kumalizika sana hapa. Soma zaidi Ukweli kuhusu Milenia.

"Kwa maana dhambi zake zimefika hata mbinguni, na Mungu amekumbuka maovu yake.....Katika kikombe kile alichokichanganyisha, mchanganyishieni maradufu. Kwa kadiri alivyojitukuza na kufanya anasa, mpeni maumivu na huzuni kadiri iyo hiyo. Kwa kuwa husema moyoni mwake, Nimeketi malkia, wala si mjane, wala sitaona huzuni kamwe. Kwa sababu hiyo mapigo yake yatakuja

katika siku moja, mauti, na njaa naye atateketezwa kabisa kwa moto. Kwa maana Bwana Mungu aliyemhukumu ni Mwenye nguvu. Na hao wafalme wa nchi, waliozini naye na kufanya anasa pamoja naye, watalia na kumwombolezea... wauonapo moshi wa kuungua kwake; wakisimama mbali kwa hofu ya maumivu yake, wakisema, ole, ole, mji ule ulio na nguvu! Kwa kuwa katika saa moja hukumu yao imekuja." Ufunuo 18:5-10. [GC 653.1; PK Aya ya 1]

"Nao wafanyabiashara wa nchi wamepata mali kwa nguvu za kiburi chake, watasimama mbali, kwa hofu ya maumi yake; wakilia na kuomboleza, Ole, Ole, mji ule mkuu uliovikwa kitani nzuri, na nguo ya rangi ya zambarau, na nguo nyekundu, na kupambwa kwa dhahabu, na kito cha thamani, na lulu kwa kuwa katika saa moja utajiri mwingi namna hii umekuwa ukiwa." Ufunuo 18:11, 3, 15-17. [GC 653.2; PK Aya ya 2]

Hizo ndizo hukumu ambazo zinaiangukia Babeli katika siku ya kupatilizwa kwake kwa ghadhabu ya Mungu. Babeli imekijaza kipimo cha uovu wake; wakati wake umefika; umekomaa* kwa ajili ya kuangamizwa, *(Umeiva) [GC 653.3; PK Aya ya 3]

Wakati sauti ya Mungu inapogeuza kifungo cha watu Wake na kuwaweka huru mateka waliofungwa, kuna kuzinduka kwa namna ya kutisha kwa wale ambao wamepoteza yote katika pambano kuu la maisha lililokuwa likiendelea.Wakati mlango wa rehema ulipoendelea kuwa wazi, walipofushwa na madanganyo Shetani, na walihalalisha njia yao ya dhambi. Walijivunia ubwana-mkubwa wao na kujilinganisha na wale waliokuwa hawakujaliwa sana kimaisha; lakini walikuwa wamejipatia utajiri wao kwa kuivunja sheria ya Mungu (Amri Kumi). Walikuwa wamepuuzia kuwalisha wenye njaa, kuwavisha nguo walio uchi, kutenda kwa haki, na kupenda rehema/huruma. Walikuwa wametafuta kujitukuza na kusujudiwa na viumbe wenzao, sasa wamenyanganywa vyote vilivyowafanya wajione kuwa wakubwa na wanaachwa wakiwa maskini na bila ulinzi. Wanaangalia kwa hofu uangamizaji wa sanamu walizozipa kipaumbele kuliko Muumbaji wao. Waliziuza roho zao ili kupata utajiri wa dunia na anasa zake walizofurahia na wala hawakutafuta kuwa matajiri mbele za Mungu. Matokeo yake ni haya, maisha yao yameishia kushindwa kabisa; anasa zao sasa zimegeuka kuwa uchungu na hazina zao zimekuwa sifuri. Mapato waliyojipatia katika maisha yao yote yanafutiliwa mbali kwa muda wa chini ya nukta (moment). Matajiri wanaomboleza kwa ajili ya kuharibiwa kwa nyumba zao za kifahari, na kutawanywa kwa dhahabu na fedha zao. Lakini maombolezo yao yananyamazishwa kwa hofu kwamba wao wenyewe wanaenda kuangamizwa pamoja na sanamu zao. [GC 654.1; PK Aya ya 4]

Waovu wanajazwa na majuto, sio kwa sababu ya dhambi yao ya kumpuuza Mungu na wanadamu wenzao, bali kwa sababu Mungu ameshinda. Wanaomboleza kwasababu ya matokeo yalivyo; lakini hawatubu uovu wao. Wasingeliacha

kujaribu kutumia kila njia ili waweze kushinda kama wangekuwa na uwezo wa kufanya hivyo. [GC 654.2; PK Aya ya 5]

Ulimwengu unaliona kundi lile lile ambalo walilidhihaki, na kulidharau na kutamani kuliangamiza, likipita bila kudhurika katika ya magonjwa/tauni, tufani na tetemeko la ardhi. Yeye ambaye kwa wavunjaji wa sheria Yake ni moto ulao, kwa watu Wake Yeye ni hema kubwa linalowahifadhi salama. [GC 654.3; PK Aya ya 6]

**Waasi Dhidi Ya Mungu**

Mchungaji ambaye ameusaliti Ukweli ili kupata upendeleo wa wanadamu sasa anatambua mwenendo na athari ya mafundisho yake. Ni dhahiri kwake sasa kwamba jicho la Mwenye kujua yote lilikuwa likimfuatilia alipokuwa anasimama kibwetani, alipokuwa akitembea mitaani, na alipokuwa anajichanganya na watu katika hali mbalimbali za kimaisha. Kila mhemko wa roho, kila mstari ulioandikwa, kila neno lililotamkwa, kila tendo lililowaongoza watu kutulia katika maficho ya uongo, alikuwa akitawanya mbegu; na sasa, katika hali ngumu, akiwa amezungukwa pande zote na watu waliopotea, anayashuhudia kwa macho yake, mavuno ya kazi yake. [GC 654.4; PK Aya ya 7]

Bwana anasema hivi: "kwa maana wameiponya jeraha ya binti ya watu wangu kwa juu-juu tu, wakisema, Amani, amani; wala hapana amani." "Kwa sababu ninyi mumemhuzunisha moyo mwenye haki kwa uongo wenu, ambaye Mimi sikumletea huzuni na kuitia nguvu mikono ya mtu mbaya, hata asigeuke na kuacha njia zake mbaya na hivyo kuokoa maisha yao." Yeremia 8:11; Ezekieli 13:22. [GC 655.1; PK Aya ya 8]

"Ole wao wachungaji wanaoharibu kondoo za malisho Yangu na kuwatawanya! ...angalieni, nitawapatiliza uovu wa matendo yenu; Pigeni yowe, enyi wachungaji, na kulia; na kugaagaa katika majivu, enyi mlio hodari katika kundi; Maana siku za kuuawa kwenu zimetimia kabisa...Nao wachungaji watakuwa hawana njia ya kukimbia, wala walio hodari katika kundi hawataokoka." Yeremia 23:1, 2; 25:34, 35. Pambizo.[GC 655.2; PK Aya ya 9]

Wachungaji na watu wanang'amua kwamba hawakudumisha uhusiano sahihi na Mungu. Wanagundua kwamba wamemwasi Mwasisi wa sheria yote iliyo ya haki na takatifu (Amri Kumi). Kule kuyaweka pembeni Maaagizo ya Mungu kulifungulia maelfu ya chemchemi za uovu, fitna, vita, chuki, na udhalimu, mpaka dunia yote ikawa uwanja mmoja mkubwa sana la mapambano na fitna, shimo moja la taka za ufisadi. Hii ndio picha halisi inayoonekana sasa kwa wale waliokataa Ukweli na kuchagua kuupenda uongo. Hakuna lugha inayoweza kueleza matamanio makubwa sana waliyonayo wasiotii na wasio waaminifu kwa kile walichokipoteza milele ambacho ni--uzima wa milele. Wanadamu wale

ambao waliabudiwa na ulimwengu kwa talanta zao na ufasaha wao, sasa wanayaona mambo haya katika nuru yake halisi. Wanatambua kile walichopoteza kwa uvunjaji wa sheria nao wanaanguka chini ya miguu ya wale ambao uaminifu wao thabiti waliudharau, na kuudhihaki na kukiri kwamba Mungu amewapenda wao. [GC 655.3; PK Aya ya 10]

Watu wanang'amua kuwa wamekwisha kudanganywa. Wanalaumiana wenyewe kwa wenyewe kwa kupelekana katika maangamizi; lakini wote wanaungana kwa pamoja katika kurundika lawama zao chungu juu ya wachungaji wao.... Wachungaji wao waliokosa uaminifu wamewatabiria mambo laini-laini; wamewaongoza wasikilizaji wao kuibatilisha sheria ya Mungu na kuwatesa wale ambao waliitunza katika utakatifu wake. Sasa, katika kukata tamaa kwa uchungu na mfadhaiko, walimu hawa wanakiri mbele ya ulimwengu kwamba kazi yao ilikuwa ya udanganyifu. Umati wa watu unajazwa kwa ghadhabu. Wanalia wakisema, "Tumepotea!", "na ninyi ndiyo mliosababisha kuangamia kwetu;" Kisha wanawageukia wachungaji wao wa uongo. Wale wale waliowahi kuwathamini, kuwapenda, na kuwashabikia, sasa wanatamka laana za kutisha juu yao. Mikono ileile ambayo hapo zamani iliwavika taji za maua za heshima itainuliwa juu kwa ajili ya kuwaangamiza. Mapanga ambayo yalinolewa ili kuwaua watu wa Mungu sasa yanatumiwa kuwaangamiza adui zao. Kila mahali kuna malumbano, vita na umwagaji damu. [GC au PK 655.4; PK Aya ya 11]

"Mshindo utafika hata mwisho wa dunia (kelele); Maana Bwana ana mashindano na mataifa, atawatetea na watu wote wenye mwili; Na waovu atawatoa wauawe kwa upanga; asema Bwana. Yeremia 25:31. Kwa miaka elfu sita pambano kuu limekuwa likiendelea (toka Edeni mpaka leo); Mwana wa Mungu na wajumbe Wake wa mbinguni wamekuwa wakipambana na nguvu za yule mwovu, ili kuonya, kuangazia na kuokoa watoto wa wanadamu. Sasa wote wamekwisha kufanya maamuzi yao; waovu wameungana kikamilifu kabisa na Shetani katika vita vyake dhidi ya Mungu. Wakati umewadia kwa Mungu kuithibitisha mamlaka ya Sheria Yake iliyokanyagwa chini. Sasa pambano siyo la Shetani peke yake bali na wanadamu." Maana Bwana ana mashindano na mataifa," "Na waovu atawatoa wauawe kwa upanga." [GC 656.1; PK Aya ya 12]

Alama ya ukombozi imewekwa kwa wale "wanaougua na kulia kwa ajili ya machukizo yote yanayofanywa." (Muhuri wa Mungu aliye hai Ufu 7:1-4). Sasa anatokea malaika wa kifo, anayewakilishwa katika njozi ya Ezekieli na wale wanaume wenye silaha zenye kuua, ambao walipewa amri: "Waueni kabisa, mzee, na kijana, na msichana, na watoto wachanga, na wanawake; lakini msimkaribie mtu yeyote mwenye hiyo alama; tena anzeni katika Patakatifu Pangu." Nabii anasema hivi: "Basi, wakaanza kwa wazee waliokuwa mbele ya nyumba." Ezekieli 9:1-6. Kazi hiyo ya uangamizaji huanza miongoni mwa wale ambao wamedai kuwa ni walinzi wa kiroho wa watu (wachungaji, mashehe,

marabi n.k). Walinzi hao wa uwongo ndio wa kwanza kuanguka. Hakuna wanaohurumiwa wala kubakizwa. Wanaume, wanawake, wasichana na watoto wadogo wanaangamia kwa pamoja. [GC 656.2; PK Aya ya 13]

“Kwa maana, tazama, Bwana anakuja kutoka mahali Pake, ili kuwaadhibu wakaao duniani, kwa sababu ya uovu wao; ardhi nayo itafunua damu yake, wala haitawafunika tena watu wake waliouawa Isaya 26:21. “Na hii ndiyo tauni, ambayo Bwana atawapiga watu wote waliopigana na Yerusalemu; Nyama yao itaharibika wakiwa wamesimama kwa miguu yao, na macho yao yatatoweka kwenye mashimo yao, na ndimi zao zitatoweka vinywani mwao. Na itakuwa katika siku hiyo, kwamba machafuko makubwa kutoka kwa Bwana yatakuwa kati yao; nao watashika kila mtu mkono wa jirani yake, na mkono wake utainuka juu ya mkono wa jirani yake.” Zekaria 14:12, 13. Katika migogoro yenye wazimu na mihemko inayotokana na hasira zao kali, na umwagaji wa ghadhabu ya Mungu yenye kutisha na isiyochanganywa na rehema (Ufu 16), wakazi waovu wa dunia--makuhani, watawala, na watu matajiri na maskini, watu walio wakuu, na wale wa hali ya chini wanaanguka chini na kufa. “Na hao waliouawa na BWANA siku hiyo watakuwapo toka upande mmoja wa dunia hata upande wa pili wa dunia; hawataliliwa, wala kukusanywa, wala kuzikwa. Yeremia 25:33. [GC 656.3; PK Aya ya 14]

Wakati wa kuja Kwake Kristo kwa mara ya pili, waovu wanafutiliwa mbali kutoka katika uso wa dunia nzima-- wanateketezwa kwa pumzi ya kinywa Chake na kuangamizwa na mng’ao mkali wa utukufu Wake. Kristo anawachukua watu Wake hadi kwenye Jiji la Mungu, na dunia hii inabaki tupu bila wakazi wake. “Tazama, Bwana ameifanya dunia kuwa tupu, na kuifanya kuwa ukiwa, na kuipindua, na kuwatawanya wakaao ndani yake.” “Dunia hii itafanywa tupu kabisa, na kuharibiwa kabisa; amesema Neno hili.” “Kwa maana wameziasi sheria, wameibadili amri, wamelivunja agano la milele; Tena dunia imetiwa unajisi kwa watu wanaoikaa; kwa maana wameziasi sheria, wameibadili amri, wamelivunja agano la milele. Ndiyo sababu laana imeila dunia hii, na hao wanaoikaa wameonekana kuwa na hatia, ndiyo sababu watu wanaoikaa dunia wameteketea….Isaya 24:1, 3, 5, Dunia yote itaonekana kama jangwa tupu. Magofu ya majumba mijini na vijijini yaliyoharibiwa na tetemeko la ardhi, miti iliyong'olewa, mawe yanayokwaruza na kutupwa baharini juu ya nchi kavu au yaliyopasuka kutoka katika ardhi yenyewe, na kusambaa juu ya uso wa dunia yote, wakati mashimo makubwa yanaonyesha alama ya mahali ambapo milima iling’olewa kutoka kwenye misingi yake. [GC 657.2; PK Aya ya 15]

### Kutengwa Kwa Shetani

Sasa ndipo linatokea tukio lililoashiriwa katika huduma nzito ya Siku ya Upatanisho. Wakati huduma katika Patakatifu pa Patakatifu ilipokuwa

imekamilika, na dhambi za Israeli zilipokuwa zimekwisha kuondolewa kutoka Patakatifu kwa njia ya damu ya sadaka ya dhambi, ndipo mbuzi wa Azazeli alipoletwa akiwa hai mbele za Bwana; na mbele ya mkutano kuhani mkuu aliungama "uovu wote wa wana wa Israeli, na makosa yao naam, dhambi zao zote, naye ataziweka juu ya kichwa chake yule mbuzi." Mambo ya Walawi 16:21. Hali kadhalika, wakati kazi ya upatanisho katika Patakatifu pa mbinguni kule mbinguni itakapokuwa imekamilika, ndipo dhambi za watu wa Mungu zitakapowekwa juu ya Shetani mbele Zake Mungu na malaika wa mbinguni na majeshi ya wale waliokombolewa; atatangazwa kuwa ana hatia ya uovu wote ambao aliwawasababisha kuutenda. Na kama mbuzi wa Azazeli alivyopelekwa katika nchi isiyokaliwa na watu, kadhalika Shetani atalazimishwa kukaa katika dunia hii iliyobaki ukiwa, yaani, jangwa lisilokaliwa na watu na lenye kuleta sonona. [GC 658.1; PK Aya ya 16]

Mfunuaji au Mwandishi wa Ufunuo anatabiri kifungo cha Shetani na hali ya dunia ya machafuko na ukiwa ambayo itaipata dunia, na anatangaza kwamba hali hiyo itaendelea kuwa hivyo kwa muda wa miaka elfu moja. Baada ya kuelezea matukio ya marejeo ya pili ya Bwana na kuangamizwa kwa waovu (Ufu 19), unabii huo unaendelea kueleza: "Kisha nikaona malaika akishuka kutoka mbinguni, mwenye ufunguo wa kuzimu na mnyororo mkubwa mkononi mwake. Akamshika yule joka, yule nyoka wa zamani, ambaye ni Ibilisi na Shetani, akamfunga miaka elfu, akamtupa katika kuzimu, akamfunga, akatia muhuri juu yake, asipate kuwadanganya mataifa tena, hata ile miaka elfu itimie; na baada ya hayo yapasa afunguliwe muda mchache" Ufunuo 20:1-3. [GC 658.2; PK Aya ya 17]

Kwamba neno hili "kuzimu" linaiwakilisha dunia katika hali ya kuvurugikiwa au kuchanganyikiwa na giza huthibitishwa na Maandiko mengine kuhusiana na hali ya dunia "hapo mwanzo," rekodi ya Biblia inasema kwamba dunia "ilikuwa ukiwa, tena yenye utupu; na giza lilikuwa juu ya uso wa vilindi vya maji." [Neno la Kiebrania lililotafsiriwa hapa "vilindi" limetafsiriwa katika tafsiri ya Septuagint (Biblia ya Kigiriki) ya Agano la Kale la Kiebrania kwa neno lilelile linalotafsiriwa "katika kuzimu" Katika Ufunuo 20:1-3. Mwanzo 1:2. Unabii unafundisha kuwa hali hiyo itarejeshwa tena, kwenye hali ile, walau kwa kiasi fulani, nabii Yeremia anatangaza hivi: "Naliiangalia nchi, na tazama, ilikuwa ukiwa, haina watu; naliziangalia mbingu, nazo zilikuwa hazina nuru. Naliangalia milima, na tazama, ilitetemeka, na milima yote ilisogea huko na huko. Nikaangalia, na tazama, hapakuwa na mtu hata mmoja, na ndege wote wa angani wamekwenda zao. Nikaangalia, na tazama, shamba lililozaa sana limekuwa ukiwa, na miji yake yote ilikuwa imebomoka." Yeremia 4:23-26. [GC 658.3; PK Aya ya 18]

Hapa ndipo patakuwa nyumbani kwake Shetani pamoja na malaika zake waovu kwa muda wa miaka elfu moja. Akiwa amewekewa mipaka katika dunia (kizuizini), hatakuwa na uwezo wa kuwafikia wakazi wa sayari zingine ili kuwajaribu na kuwasumbua wale ambao hawajawapata kamwe kuanguka dhambini. Ni katika maana hiyo yeye anasemekana kuwa yupo kifungoni: yaani hakuna watu waliobakia, ambao anaweza kutumia uwezo wake juu yao. Ameachanishwa kabisa na kazi ya udanganyifu na uharibifu ambao kwa karne nyingi ilikuwa chanzo pekee cha furaha yake. [GC 659.1; PK Aya ya 19]

Nabii Isaya, akitazama mbele kwa hamu kubwa, wakati ule Shetani atakapopinduliwa kabisa, anapaza sauti hivi kwa mshangao: "Jinsi ulivyoanguka kutoka mbinguni, Ee nyota ya alfajiri, Mwana wa asubuhi! Jinsi ulivyokatwa kabisa, Ewe uliyewaangusha mataifa!... Nawe ulisema moyoni mwako, Nitapanda mpaka mbinguni, Nitakiinua kiti changu juu kuliko nyota za Mungu;... Nitafanana na Yeye Aliye juu. Lakini utashushwa mpaka kuzimu; mpaka pande za mwisho za shimo. Wao wakuonao watakukazia macho, Watakuangalia sana, wakisema, je! Huyu ndiye aliyeitetemesha dunia, huyu ndiye aliyetikisa falme; aliyeufanya ulimwengu kuwa jangwa (ukiwa)." kuiharibu miji yake; Asiyewafungua wafungwa wake waende kwao?" Isaya 14:12-17. [GC 659.2; PK Aya ya 20]

Kwa muda wa miaka elfu sita (kuanzia Edeni mpaka leo), kazi ya uasi wa Shetani imeitetemesha dunia. Alikuwa "ameufanya ulimwengu wote kuwa ukiwa, na kuiharibu miji yake." Tena yeye "hawafungui wafungwa wake waende kwao milele." Kwa miaka elfu sita nyumba yake ya gereza imepokea watu wa Mungu, naye angeendelea kuwaweka mateka milele; lakini Kristo alikuwa amezikata kamba zake na kuwaweka huru wafungwa. [GC 659.3; PK Aya ya 21]

Hata wale waovu sasa wamewekwa nje ya uwezo wa Shetani (wote wamekufa) na yeye akiwa mwenyewe Pamoja na malaika zake waovu wanabaki hapa duniani kuangalia madhara ya laana ambayo imeletwa na dhambi. "Wafalme wa mataifa, nao wote, wamelala katika utukufu, kila mtu katika nyumba yake [kaburini]. Bali wewe umetupwa nje ya kaburi lako kama tawi la kuchukiza... wewe hutaungamanishwa pamoja nao katika mazishi, Kwa maana umeiharibu nchi yako, Umewaua watu wako." Isaya 14:18-20. [GC 660.1; PK Aya ya 22]

Kwa miaka elfu moja, Shetani atatanga-tanga huku na huko katika dunia hii iliyo ukiwa na kuharibika ili kuona matokeo ya maasi yake dhidi ya sheria ya Mungu. Katika kipindi hicho mateso yake ni makali sana. Tangu anguko lake dhambini, maisha yake yaliyojaa hekaheka zisizokoma, yaliondoa muda wa kutafakari na kucheua mambo; lakini sasa amenyang'anywa uwezo wake na ameachiwa fursa ya kutafakari sehemu ambayo aliitenda tangu alipoasi kwa mara ya kwanza dhidi ya serikali ya mbinguni na kutazama mbele kwa

kutetemeka na hofu kuu hadi wakati ujao ambao unatisha, wakati atakapolazimika kuteseka kwa ajili ya uovu wote alioutenda na adhabu atakayoipata kwa ajili ya dhambi alizozosababisha watu kuzitenda. [GC 660.2; PK Aya ya 23]

Kwa watu wa Mungu kifungo cha Shetani kitaleta  furaha na shangwe kuu. Nabii anasema hivi: "Itakuwa katika siku ile BWANA atakapokupumzisha baada ya huzuni yako, na taabu yako, na utumishi mgumu uliotumikishwa ndani yake, ndipo utatunga mithali hii juu ya mfalme wa Babeli [hapa akiwakilisha Shetani], na kusema, Jinsi alivyokoma mwenye kuonea! Jinsi ulivyokoma mji ule wenye jeuri......Bwana amelivunja gongo la  waovu, fimbo ya enzi ya mtawala; aliyepiga mataifa kwa ghadhabu kwa mapigo yasiyokoma, aliyewatawala mataifa kwa hasira, kwa mateso ambayo hapana aliyezuia." Aya 3-6. [GC 660.3; PK Aya ya 24]

Katika kipindi cha miaka elfu moja kinachoingia katikati ya ufufuo wa kwanza na wa pili, hukumu ya waovu itafanyika. Mtume Paulo anaongelea hukumu hii kama tukio linalofuata baada ya marejeo ya mara ya pili ya Kristo. "Msihukumu neno kabla ya wakati wake, hata ajapo Bwana, ambaye atayafichua yaliyositirika ya giza, na kuyadhihirisha mashauri ya mioyo." 1 Wakorintho 4:5. Danieli anaeleza kuwa, wakati Mzee wa Siku alipokuja, "nao watakatifu Wake Aliye juu wakapewa hukumu." Danieli 7:22. Kwa wakati huu wenye haki wanatawala kama wafalme na makuhani wa Mungu. Yohana katika kitabu cha Ufunuo anasema: "Nikaona viti vya enzi, wakaketi juu yake, nao wakapewa hukumu.""Watakuwa makuhani wa Mungu na wa Kristo, na watatawala pamoja Naye miaka elfu." Ufunuo 20:4, 6. Ni wakati huu ambao, ulitabiriwa na Paulo kuwa, "watakatifu watauhukumu ulimwengu." 1 Wakorintho 6:2. Wakiungana pamoja na Kristo wanawahukumu waovu, wakiyalinganisha matendo yao na kitabu cha sheria, yaani, Biblia, na kuamua kila kesi kulingana na matendo yaliyotendwa katika mwili. Ndipo kipimo wanachopaswa cha adhabu ya wale waovu waovu kinapangwa, kulingana na matendo yao; na kinaandikwa mbele ya majina yao katika Kitabu cha Mauti. [GC 660.4; PK Aya ya 25]

Shetani na malaika zake waovu wanahukumiwa na Kristo pamoja watu Wake. Paulo anasema: "Hamjui ya kuwa mtawahukumu malaika? Mstari wa 3."Na, malaika ambao hawakuridhika na cheo chao, wakayaacha makao yao ya asili, Mungu amewafunga gizani kwa minyororo ya milele wahukumiwe Siku ile kuu." Yuda 6. [GC 661.1; PK Aya ya 26]

Mwishoni mwa miaka ile elfu ufufuo wa pili unatokea. Ndipo waovu watakapofufuliwa kutoka kwa wafu na kutokea mbele za Mungu kwa ajili ya utekelezaji wa "hukumu iliyoandikwa." Hivyo Yohana mfunuaji au mwandishi wa Ufunuo, baada ya kueleza Habari ya ufufuo wa wenye haki, anasema hivi: "Hao wafu waliosalia, hawakuwa hai, hata itimie ile miaka elfu." (waovu wote

waliouawa Yesu alipokuja mara ya pili hawakufufuliwa) Ufunuo 20:5 Naye Isaya anatangaza, kuhusu waovu hao: "Watakusanywa pamoja, kama wakusanywavyo wafungwa shimoni, na kufungwa gerezani, na baada ya siku nyingi watajiliwa." Isaya 24:22. [GC 661.2; PK Aya ya 27]

*Neno la Kiebrania lililotafsiriwa hapa kama "vilindi vya maji" limetolewa katika tafsiri ya Kigiriki iliyofanywa na watu Sabini (Septuagint) kutoka katika Agano la Kale la Kiebrania kwa neno lile lile lililotafsiriwa kama "kuzimu" au "shimo la kuzimu" katika Ufunuo 20:1-3 (linganisha na Ufu. 9:1,2).

# SURA YA 42

# MWISHO WA PAMBANO

## (Hatimaye Ushindi Wa Upendo Wa Mungu Wapatikana)

Ufupisho: Hapa kuna pambano ambalo lilitayarishwa lakini halikufanyika. Historia ya Shetani na kiti cha enzi cha Mungu na mbingu yenye uzuri wa ajabu. Mwisho wa dhambi unaelezewa hapa, jambo ambalo linatupa matamanio kuwa mbinguni. Hazina zote za mbinguni na sayari zote zitakuwa wazi kwetu ili tujifunze, kutakuwa hakuna kifo, maumivu, shida wala machozi, tutakuwa na furaha na hekima ambayo wale viumbe wasioanguka wanayo. Hii ni historia ya mbingu mpya ambayo sote tunatamani tuwemo humo, na tumepewa uchaguzi kuingia humo!

Mwishoni mwa miaka elfu moja, Kristo anarudi tena duniani. Anaandamana na msafara wa jeshi la waliokombolewa na kufuatiwa na msururu wa malaika. Anaposhuka kwa utukufu na ukuu wa kutisha na kushangaza, Naye anawaamuru waovu waliokufa wainuke kutoka makaburini ili kupokea adhabu yao. Kutoka makaburini, linatokezea jeshi kubwa lisiloweza kuhesabika kama vile mchanga wa bahari. Tofauti iliyoje ukiwalinganisha na wale waliofufuliwa kwenye ufufuo wa kwanza! Wenye haki walikuwa wamevikwa ujana wenye uzuri na hali ya kutokufa. Waovu watakuwa na viashiria vya magonjwa na hali ya kifo. [GC 662.1; PK Aya ya 1]

Kila jicho katika umati huo mkubwa wa watu linageuka ili kujionea utukufu wa Mwana wa Mungu. Kwa sauti moja majeshi ya waovu yanapaza sauti na kutamka: "Huyu Ndiye Amebarikiwa, Yeye ajaye kwa Jina la Bwana!" Siyo upendo kwa ajili ya Yesu ndiyo unaohamasisha tamko hili. Nguvu ya Ukweli inayakamua maneno haya kwa nguvu ili yatoke katika midomo isiyo na utayari wa kukiri. Jinsi ambavyo waovu waliingia makaburini mwao, ndivyo wanavyotoka wakiwa na uadui uleule dhidi ya Kristo na roho ile ile ya uasi dhidi Yake. Hawapewi rehema nyingine mpya ili warekebishe kasoro za maisha yao yaliyopita. Hakuna lolote la maana ambalo lingeweza kubadilika kwa kupewa rehema hiyo. Maisha yao ya uasi hayakulainisha mioyo yao. Muda wa pili wa rehema hata ungetolewa kwao, ungetumika kama ulivyotumika ule wa kwanza kwa kukwepa matakwa ya Mungu na kuchochea sumu ya uasi dhidi Yake. [GC 662.2; PK Aya ya 2]

Kristo anashuka juu ya Mlima wa Mizeituni, mahali ambapo, baada ya kufufuka Kwake, Yeye alipaa kutokea hapo, na ndipo mahali malaika walirudia kutangaza ahadi ya kurudi Kwake. Nabii anasema hivi: "Bwana Mungu wangu atakuja, na watakatifu wote pamoja Naye." "Na miguu Yake itasimama siku hiyo juu ya Mlima wa Mizeituni, unaoelekea Yerusalemu upande wa mashariki, na Mlima wa Mizeituni utapasuka katikati Yake, …na kutakuwa na bonde kubwa sana." "Na Bwana atakuwa mfalme juu ya dunia yote; siku hiyo kutakuwa na Bwana mmoja, na Jina Lake moja." Zekaria 14:5, 4, 9. Wakati Yerusalemu Mpya, katika utukufu wake mwingi wenye kumeta-meta, unaposhuka kutoka mbinguni, na kutua juu ya mahali palipotakaswa/pamesafishwa na kuandaliwa kuupokea, Naye Kristo, pamoja na watu Wake na malaika, wanauingia Mji Mtakatifu. [GC 662.3; PK Aya ya 3]

### Shambulio La Mwisho Dhidi Ya Mungu

Sasa Shetani anajiandaa kwa ajili ya pambano lake kuu la mwisho kwa ajili ya ukuu. Alipokuwa amenyang'anywa uwezo wake na kuachishwa kazi yake ya udanganyifu, mfalme wa uovu akiwa na wakati mgumu na kuzimia moyo na

uchovu; lakini waovu waliokufa wanapofufuliwa naye anakiuona umati mkubwa wa watu wakiwa upande wake, matumaini yake yatafufuka, naye anadhamiria kutoacha pambano hilo kuu. Atayakusanya majeshi ya wote waliopotea chini ya bendera yake na kupitia kwao atajibidisha kutekeleza mikakati yake. Waovu ni mateka wa Shetani. Katika kumkataa Kristo wamekubali utawala wa kiongozi huyo aliyeasi. Waasi wako tayari kupokea mapendekezo yake na kufanya maagizo yake. Hata hivyo, akiwa na msimamo wake, ujanja na hila zake za awali, hataki kukiri kuwa yeye ni Shetani. Anadai kuwa yeye ni mfalme ambaye ndiye mmiliki halali wa ulimwengu ambaye urithi wake umeporwa kutoka kwake kinyume cha sheria. Anajionyesha kwa raia wake waliodanganyika kuwa yeye ndiye mkombozi, akiwahakikishia kwamba nguvu zake ndiyo zimewatoa katika makaburi yao na kwamba yuko karibu kuwaokoa kutoka katika utawala wa kikatili, ulio mbaya zaidi. Uwepo wa Kristo ukiwa umeondolewa, Shetani anafanya maajabu ili kuunga mkono madai yake. Anawafanya dhaifu kuwa na nguvu na anavuvia wote na roho na nguvu zake mwenyewe. Anapendekeza kuwaongoza ili kuikabili kambi ya watakatifu na kuuteka na kuumiliki Mji wa Mungu. Kwa shangwe na furaha yake ya kikatili na kishetani anaonyesha mamilioni ya watu wasio na idadi ambao wamefufuliwa kutoka kwa wafu na kutangaza kwamba kama kiongozi wao anaweza kulipindua jiji hilo na kurudisha kiti chake cha enzi na ufalme wake. [GC 663.1; PK Aya ya 4]

Katika umati huo mkubwa ulioshonana, kuna kundi kubwa la watu wa kizazi kilichoishi kwa muda mrefu kabla ya gharika; majitu marefu na yenye akili nyingi, ambayo, yalipojisalimisha chini ya uongozi wa malaika walioanguka, walimwaga ujuzi, stadi na maarifa yao yote katika kujiinua wenyewe; watu ambao kazi zao za ajabu katika sanaa ziliufanya ulimwengu kuabudu fikra na akili zao nyingi (genius), lakini ambao ukatili na uvumbuzi wao wenye uovu, vilitia dunia uchafu/unajisi na kuharibu-haribu vibaya sura ya Mungu,na kumfanya Mungu awafutilie mbali kutoka katika uso wa kazi ya uumbaji Wake. Kuna wafalme na majenerali wa vita walioteka nyara na kushinda mataifa, watu mashujaa ambao kamwe hawakuwahi kushindwa katika vita yoyote, wapiganaji wenye kiburi na matamanio ya kupigana ili kupata ukuu, na ushindi, hawa walisababisha falme kutetemeka kila walipozikaribia. Mautini hawa hawakupoteza uzoefu wao. Wanapotoka kaburini, wanauanza tena mkondo wa mawazo yao pale ulipokomea walipoacha kupumua. Wanachochewa na shauku ile ile ya kushinda katika vita iliyowatawala walipofariki. [GC 664.1; PK Aya ya 5]

Shetani anashauriana na malaika zake, na kisha anashauriana na washindaji na watu wenye nguvu na hodari. Wanatathmini nguvu na idadi iliyoko upande wao na kutangaza kwamba jeshi lililo ndani ya mji ni dogo ukilinganisha na jeshi lao, na kuwa wanaweza kulishinda. Wanaweka mipango yao ya kuteka na kumiliki utajiri na utukufu uliomo Yerusalemu Mpya. Wote mara moja wanaanza

kujiandaa kwa vita. Mafundi stadi wanaunda zana za vita. Viongozi wa kijeshi mashuhuri na waliotukuka kwa mafanikio yao, wanapanga umati wa watu wanaopenda vita katika kombania na migawanyo mbali mbali. [GC 664.2; PK Aya ya 6]

Hatimaye amri ya kusonga mbele inatolewa, na jeshi la idadi isiyohesabika inasonga mbele-- jeshi ambalo halijawahi kukusanywa kamwe na washindi wa kidunia, jeshi ambalo ni muunganiko wa majeshi ya zama zote tangu vita ya kwanza ilivyopiganwa duniani, jeshi hili halina mfanano na lingine ambalo limeweahi kuwepo duniani. Shetani, mpiganaji hodari na mwenye nguvu zaidi, anaongoza msafara wa kivita na malaika zake na wanaunganisha majeshi yao kwa ajili ya pambano hili la mwisho. Wafalme na wapiganaji wamo katika msafara wa gari moshi lake, na umati unafuatana nao katika kombania nyingi, kila moja ikiwa chini ya kiongozi wake aliyeteuliwa. Kwa umahiri wa kijeshi, safu za wanajeshi walioshonana zinasonga mbele juu ya uso wa ardhi uliopasukapasuka na usio na usawa, kuna miinuko na mabonde, wakilielekea jiji la Mungu. Kwa amri ya Yesu, malango ya Yerusalemu Mpya yanafungwa, na majeshi ya Shetani yanalizingira jiji hilo na kujitayarisha kwa ajili ya kuanza mashambulizi. [GC 664.3; PK Aya ya 7]

**Kristo Atokea**

Sasa Kristo anatokea tena na anaonekana mbele ya maadui Zake. Juu kabisa ya mji, juu ya msingi wa dhahabu iliyosafishwa na kung'aa sana, kuna kiti cha enzi, kilicho juu na kilichoinuliwa sana. Juu ya kiti hiki cha enzi ameketi Mwana wa Mungu na waliomzunguka ni raia wa ufalme Wake. Hakuna lugha inayoweza kuelezea, wala kalamu inayoweza kuuandika uzito wa mambo haya, utukufu na ukuu wa Kristo. Utukufu wa Baba wa Milele unamfunika Mwanawe. Utukufu wa uwepo Wake unaujaza Mji wa Mungu, na unatiririka nje ya malango ya mji, na kufurika dunia nzima kwa mng'ao Wake. [GC 665.1; PK Aya ya 8]

Karibu kabisa na kiti cha enzi ni wale ambao hapo awali walikuwa motomoto katika kufanya kazi ya Shetani, lakini ambao waliopolewa kwa kasi na kutolewa nje kama kijinga kutoka kwenye moto, hawa walimfuata Mwokozi wao kwa ibada na uchaji Mungu wenye bidii. Wanaofuata ni wale waliokamilisha tabia za Kikristo katikati ya udanganyifu na ukafiri, wale walioiheshimu sheria ya Mungu wakati ulimwengu wa Kikristo ulipoitangaza kuwa haina mashiko (imebatilishwa), na mamilioni ya watu wa zama zote, ambao waliuawa kwa ajili ya imani yao. Na kwa mbali zaidi ya hapo ni "mkutano mkubwa, ambao hapana mtu awezaye kuuhesabu, watu wa kila taifa, na kabila, na jamaa, na lugha,... mbele ya kiti cha enzi, na mbele ya Mwana-Kondoo, wamevikwa mavazi meupe, na mitende mikononi mwao." Ufunuo7:9. Vita yao imekwisha, ushindi wao umepatikana. Wamekimbia mbio katika shindano na kupokea tuzo zao. Tawi la mitende lililo

mikononi mwao ni nsishara ya ushindi wao, mavazi yao meupe ni nembo ya haki isiyo na mawaa ya Kristo ambayo ni yao sasa. [GC 665.2; PK Aya ya 9]

Waliokombolewa wanapaza sauti wakiimba wimbo wa sifa ambao unatoa mwangwi na kujirudia tena na tena kutoa mwangwi kupitia katika anga la mbinguni huko juu, wakisema: “Wokovu una Mungu wetu aketiye juu ya kiti cha enzi, na Mwana-Kondoo.” (fungu la 10). Na malaika na maserafi wanaunganisha sauti zao katika ibada ya sifa kwa heshima kuu. Baada ya wale waliokombolewa kuiona nguvu na ubaya mkuu wa Shetani, wamethibithisha, kuliko wakati mwingine wowote, kwamba hakuna nguvu yoyote isipokuwa ile ya Kristo tu ndiyo ambayo ingeweza kuwasaidia watu wapate ushindi. Katika umati huo wote unaong'aa hakuna wa kujitapa na kujichukulia sifa mwenyewe kuhusiana na wokovu, kwamba alishinda kwa nguvu na wema wake wenyewe. Hakuna chochote kinachotajwa kuhusiana na kile ambacho wamekifanya au jinsi walivyoteseka; lakini maudhui ya kila wimbo, wazo kuu linalojitokeza katika kila wimbo, ni: Wokovu una Mungu wetu na Mwana-Kondoo. [GC 665.3; PK Aya ya 10]

**Hukumu Yatamkwa Dhidi Ya Waasi**

Mbele ya wakazi wa duniani na mbinguni, waliokusanyika pamoja kushuhudia, kutawazwa kwa mara ya mwisho kwa Mwana wa Mungu kunafanyika. Na sasa, akiwa amekabidhiwa uweza na nguvu ya mamlaka ya juu kabisa, Mfalme wa wafalme anatangaza hukumu juu ya waasi wa serikali Yake na anatekeleza haki juu ya wale wote walioivunja sheria Yake na kuwatesa watu Wake. Nabii wa Mungu anasema, “Kisha nikaona kiti cha enzi kikubwa cheupe, na Yule aketiye juu Yake. Dunia na mbingu vikatoweka mbele ya macho Yake, na havikuonekana tena. Kisha nikawaona watu wakubwa na wadogo, wamesimama mbele ya kiti cha enzi, na vitabu vikafunguliwa. Halafu kitabu kingine, yaani kitabu cha uzima, kikafunguliwa pia. Wafu wakahukumiwa kadiri ya matendo yao, kama ilivyoandikwa ndani ya vitabu hivyo. Ufunuo 20:11, 12. [GC 666.1; PK Aya ya 11]

Mara tu vitabu vya kumbukumbu vinapofunguliwa, na jicho la Yesu linapowatazama wale waovu, wanatambua na kuikumbuka kila dhambi waliyowahi kuitenda. Wanatambua pale ambapo miguu yao ilijikwaa na kutoka katika njia ya maisha ya usafi na utakatifu kwa kutenda dhambi, jinsi ambavyo kiburi na uasi viliwafikisha katika uvunjaji wa sheria ya Mungu. Majaribu ya kushawishi ya tamaa za mwili ambayo waliyaendekeza kwa kujiingiza katika dhambi, baraka za Mungu zilizotumiwa vibaya, wajumbe wa Mungu waliodharauliwa, maonyo ya Mungu yaliyokataliwa, mawimbi ya rehema waliyoyarudisha nyuma na moyo mkaidi, usiotubu, yote yanaonekana kana kwamba yameandikwa kwa herufi za moto. [GC 666.2; PK Aya ya 12]

**Msalaba Juu Ya Kiti Cha Enzi**

Juu ya kiti cha enzi unafunuliwa msalaba; na kama onyesho la filamu/video la mfululizo wa matukio, zinatokea mandhari za majaribu na anguko la Adamu, na hatua zinazofuatana katika mpango mkuu wa ukombozi. Kuzaliwa kwa Mwokozi katika mazingira ya kimasikini; Maisha Yake ya awali ya usahili, unyenyekevu na utiifu; Ubatizo Wake katika mto Yordani; mfungo na majaribu nyikani; Huduma Yake kwa kadamnasi, kuwafunulia wanadamu mibaraka ya mbinguni yenye thamani kubwa; siku zilizosheheni matendo ya upendo na rehema, mikesha ya sala usiku katika upweke na faragha ya milima; njama za husuda za kutafuta kumdhuru, hila, chuki na uovu ambazo zilikuwa kama malipo kwa fadhila Zake; uchungu wa kutisha ajabu na siri katika Gethsemane chini ya uzito wa mzigo unaokandamiza wa dhambi za ulimwengu mzima; kusalitiwa Kwake mikononi mwa genge la wauaji; matukio ya kutisha katika usiku ule wa hofu—mfungwa asiye na ubishi, aliyekimbiwa na wanafunzi aliowapenda mno, akikokotwa kwa jeuri na ufidhuli katika mitaa ya Yerusalemu; Mwana wa Mungu akioneshwa mbele ya Anasi huku watu wakishangilia sana, akipandishwa kizimbani ili kushitakiwa katika jumba la kuhani mkuu, katika ukumbi wa hukumu wa Pilato, mbele ya Herode mwoga na katili, akidhihakiwa, akitukanwa, akiteswa na kuhukumiwa kufa—yote hayo yanaonyeshwa waziwazi. (Panorama)-matukio yanapitishwa kama mkanda wa video waziwazi kila mtu ashuhudie Ukweli) [GC 666.3; PK Aya ya 13]

Na sasa kabla ya umati wa watu unaoyumba-yumba zinafunuliwa mandhari za mwisho-- Mtesekaji mvumilivu akikanyaga kuelekea njia inayokwenda Kalvari; Mkuu na Mfalme wa mbinguni akining'inia juu ya msalaba; makuhani wenye kiburi na umati wa watu wenye kejeli za ovyo wakimzomea katika uchungu Wake mkali uliomfanya akate roho; giza lisilo la kawaida; nchi iliyotetemeshwa na kisha kufumuka, miamba iliyopasuka, makaburi yaliyofunguka, yakiashiria wakati ambapo Mkombozi wa ulimwengu alitoa uhai Wake. [GC 667.1; PK Aya ya 14]

Tamasha na tukio la kutisha linatokea kama lilivyokuwa. Shetani, malaika zake na wafuasi wake hawana uwezo wa kugeuka wasione picha ya kazi yao wenyewe au (kugeuza mambo yaliyotokea). Kila muhusika au muigizaji anakumbuka sehemu ambayo aliyoitenda. Herode, aliyewaua wana wa Bethlehemu wasio na hatia ili kumwangamiza Mfalme wa Israeli; Herodia, ambaye moyo wake wenye hatia inakaa damu ya Yohana Mbatizaji; Pilato mtu aliyekuwa anatumikia wakati au nafsi yake tu; askari waliomdhihaki; makuhani, watawala na umati wenye wazimu kwa hasira uliopaza sauti, "Damu Yake na iwe juu yetu, na juu ya watoto wetu!" wote wanauona ukubwa wa hatia yao. Wanatafuta kujificha bila mafanikio kutoka kwenye utukufu wa uso Wake Mungu, unaong'aa zaidi ya utukufu wa jua, huku waliokombolewa wakitupa taji zao miguuni pa Mwokozi wao, wakisema: "Alikufa kwa ajili yangu mimi!" [GC 667.2; PK Aya ya 15]

Miongoni mwa umati huo wa waliokombolewa kuna mitume wa Kristo, Paulo shujaa, Petro mwenye bidii, Yohana mpendwa na mwenye upendo na ndugu zao wenye mioyo ya kweli, pamoja na jeshi kubwa la wafia dini; wakati nje ya kuta (za Yerusalemu), wakiwa na kila jambo baya, chafu, linalonuka na la kuchukiza, kuna wale ambao waliwatesa, waliwafunga, na kuwaua. Yupo Nero, zimwi kubwa la ukatili na uovu, akitazama furaha ya kuinuliwa kwa wale aliowatesa huko nyuma, ambao katika uchungu wao mwingi alipata furaha ya kishetani. Mama yake yupo pale akishuhudia matokeo ya kazi yake mwenyewe; kuona jinsi tabia yake mbaya ilivyopitishwa kama urithi kwa mwanawe, harara na mihemko aliyochochea na kukuza kwa ushawishi na mfano wake, vimezaa matunda katika uhalifu uliosababisha ulimwengu kutetemeka. [GC 667.3; PK Aya ya 16]

Kuna mapadri na makasisi wa kipapa, walijiodai kuwa mabalozi wa Kristo, lakini walitumia chanja ya kutesea watu, na kuwaweka kwenye magereza ya chini ya ardhi, na kuwachoma moto kwenye mlingoti ili wapate kuzitawala dhamiri za watu wa Mungu. Kuna mapapa wenye kiburi waliojiinua juu ya Mungu na kuazimu kubadili sheria za Yeye Aliye Juu Zaidi. Wale waliojifanya kuwa mababa wa kanisa wanatakiwa kutoa hesabu yao kwa Mungu ambayo wangetamani kuachiliwa huru wasiitoe, bali wasamehewe. Kwa kuchelewa sana wanagundua kwamba Yeye Mwenye kujua mambo yote ana wivu juu ya sheria Yake na kwamba hawezi kumhesabia yoyote anayeivunja kuwa hana hatia, kwa vyovyote vile. Wanajifunza sasa kwamba Kristo alijali maslahi ya watu Wake wanaoteseka; na wanahisi nguvu kubwa ya maneno Yake Mwenyewe: "Kadiri mlivyomtendea mmojawapo wa hao ndugu Zangu walio wadogo, mlinitendea Mimi. Mathayo 25:40. [GC 668.1; PK Aya ya 17]

Ulimwengu wote mwovu unasimama mbele ya kizimba cha mahakama ya Mungu kwa shtaka la uhaini mkubwa dhidi ya serikali ya mbinguni. Hawana wa kuwatetea kesi yao; hawana udhuru; na hukumu ya mauti ya milele inatamkwa dhidi yao. [GC 668.2; PK Aya ya 18]

Sasa inakuwa dhahiri kwa wote kwamba mshahara wa dhambi sio uhuru bora na uzima wa milele, bali utumwa, uharibifu na kifo. Waovu wanayaona yale waliyoyapoteza kwa maisha yao ya uasi. Uzito wa milele, na utukufu upitao tunu yote, walioudharau ulipoletwa kwao lakini unatamanika jinsi gani sasa unapoonekana machoni pao. "Haya yote," mtu aliyepotea italia na kuendelea kusema, "huenda ningekuwa nayo; lakini nilichagua kuweka mambo haya mbali nami. Lo! Kupumbazwa kwa ajabu huku! Nimepoteza amani, furaha na heshima na badala yake nimejichagulia umasikini, udhaifu, sifa mbaya, dharau na kukata tamaa." Wote wanaona kwamba kutengwa na mbingu ni haki kabisa. Kwa mtindo wao wa maisha wamekuwa wakitangaza: "Hatumtaki Mtu huyu (Yesu) atawale juu yetu." [GC 668.3; PK Aya ya 19]

Kama watu walio katika maono na mshtuko, waovu wanamwona Mwana wa Mungu akitawazwa kwa kuvikwa taji. Wanaona mikononi Mwake mbao mbili za sheria ya Mungu (Amri Kumi), sheria ambazo wamezidharau na kuzivunja. Wanashuhudia mlipuko wa mshangao, furaha ya ajabu kuu, na ibada kutoka kwa wale waliookolewa; na wakati wimbi la nyimbo tamu linafunika umati mkubwa nje ya jiji, wote kwa sauti moja wanashangilia kwa sauti kuu, "Ni makuu na ya ajabu matendo Yako, Bwana Mungu Mwenyezi; ni za haki na Kweli njia Zako, Ee Mfalme wa watakatifu" (Ufunuo 15:3); nao wakianguka kifudifudi, wanamwabudu Mfalme wa uzima. [GC 668.4; PK Aya ya 20]

**Hatimaye Shetani Ashindwa**

Shetani anaonekana kana kwamba amepooza kwa kiharusi anapoutazama utukufu na ukuu wa Kristo. Yeye ambaye hapo awali alikuwa kerubi afunikaye anakumbuka ni wapi aliaponguka. Serafi anayeng'aa, "mwana wa asubuhi amebadilika kiasi gani, amefedheheshwa kwa kushuka chini kiasi gani! Kutoka kwenye baraza ambalo awali alikuwa ameheshimiwa, ameondolewa milele zote. Anamwona mwingine sasa akisimama karibu na Baba, akifunika utukufu Wake. Ameona taji likiwekwa juu ya kichwa cha Kristo na malaika wa kimo kirefu na mwonekano wenye utukufu mwingi, na anatambua fika kwamba cheo kilicho juu cha malaika huyu kilikuwa kiwe chake. [GC 669.1; PK Aya ya 21]

Kumbukumbu zinamrudisha hadi makazi yake, wakati alipokuwa hana hatia, mwenye usafi wa moyo, amani na kuridhika, hivi vilikuwa vyake hadi alipojiingiza katika kuendekeza manun'guniko dhidi ya Mungu, na kumwonea wivu Kristo. Mashtaka yake, uasi wake, udanganyifu wake ili kupata huruma na kuungwa mkono na malaika, kudumu kwake katika ukaidi, na kutofanya jitihada yoyote kunusuru kile alichokipoteza kwa kutubu wakati Mungu alikuwa tayari kumsamehe-- yote hayo yanakuja kwa uwazi mbele yake. Anarejelea kazi yake miongoni mwa wanadamu na matokeo yake, uadui wa mwanadamu dhidi ya wanadamu wenzake, uharibifu wa kutisha wa maisha, kuinuka na kuanguka kwa falme, kupinduliwa kwa viti vya enzi, mfululizo mrefu wa ghasia, migogoro na mapinduzi. Anakumbuka juhudi zake zisizochoka katika kupinga kazi ya Kristo na kumdidimiza mwanadamu chini zaidi na zaidi. Anaona kwamba njama zake za kuzimu hazijaweza kuwaangamiza wale ambao wameweka tumaini lao kwa Yesu. Shetani anapoutazama ufalme wake, matunda ya taabu yake, anaona tu kufeli na kuangamizwa. Amewaongoza makutano kuamini kwamba Mji wa Mungu ni windo rahisi kutekwa; lakini anajua kuwa huu ni uwongo. Tena na tena, katika maendeleo ya pambano hilo kuu, ameshindwa na kulazimishwa kusalimu amri. Anajua vizuri sana mamlaka na uwezo wa Mungu wa milele. [GC 669.2; PK Aya ya 22]

**Laghai Mkuu Afichuliwa**

Kusudi la mwasi mkuu daima limekuwa kujihesabia haki na kuonesha kwamba serikali ya Mungu ndiyo inahusika na uasi huo. Amepindisha nguvu zote za akili yake bora kwenye mwelekeo huo ili kufikia lengo hili. Amefanya kazi kwa makusudi na kwa mikakati iliyopangiliwa na kujipatia mafanikio ya kushangaza, akiongoza umati mkubwa wa watu kukubali maelezo yake kuhusu pambano kuu ambalo limekuwa likiendelea kwa muda mrefu. Kwa maelfu ya miaka ya vita hii kuu, mkuu huyu wa njama za uovu, ameweka uwongo wake ndiyo iwe tafsiri ya Ukweli. Lakini wakati umefika sasa ambapo hatimaye uasi utashindwa na historia na tabia ya Shetani itafichuliwa na kuanikwa wazi. Katika jitihada yake kuu ya mwisho ya kumng'oa Kristo katika kiti cha enzi, kuwaangamiza watu Wake na kuumiliki Mji wa Mungu. Mdanganyifu mkuu amefichuliwa kikamilifu (barakoa yake imetolewa). Wale ambao wameungana naye wanaona kushindwa kabisa kwa misheni yake. Wafuasi wa Kristo na malaika wale watiifu wanaona kwa ukamilifu mikakati yake dhidi ya serikali ya Mungu. Yeye ndiye anachukiwa na wote wenye wenye uhai kwenye malimwengu yote (sayari zote). [GC 670.1; PK Aya ya 23]

Shetani anaona kwamba uasi wake wa hiari umemfanya asifae kuwa mkazi wa mbinguni. Amezifanyia nguvu zake mazoezi ya kupigana na Mungu; usafi wa maisha, amani na maelewano ya mbinguni vingekuwa kwake mateso makuu. Mashtaka yake dhidi ya rehema na haki ya Mungu sasa yamenyamazishwa kabisa. Aibu ambayo amejitahidi kumpakaza Yehova sasa inamrudia mwenyewe kikamilifu. Na sasa Shetani anainama chini na anakiri haki ya hukumu yake. [GC 670.2; PK Aya ya 24]

"Ni nani asiyekucha, Ee Bwana, na kulitukuza Jina Lako? kwa kuwa Wewe peke Yako u Mtakatifu; kwa maana mataifa yote watakuja na kusujudu mbele Zako; kwa kuwa matendo Yako ya haki yamekwisha kufunuliwa." Fungu la 4. Kila suala kuhusu Ukweli na uongo katika pambano kuu lililodumu kwa muda mrefu sasa litakuwa limewekwa wazi. Matokeo ya uasi, matunda ya kuweka pembeni amri za Mungu, yamewekwa wazi na kuonekana mbele ya akili za viumbe vyote. Utendaji kazi wa utawala wa Shetani kinyume cha serikali ya Mungu umewekwa wazi kwa malimwengu yote. Kazi alizozitenda Shetani zimemhukumu mwenyewe. Hekima ya Mungu, haki Yake na wema Wake vimethibitishwa kikamilifu. Inadhihirika kuwa mipango Yake yote aliyoifanya katika pambano hilo kuu, ilikuwa imefanywa kwa heshima na manufaa ya wema wa milele wa watu Wake na maslahi ya sayari zote ambazo Ameziumba. "Matendo Yako yote yatakusifu, Ee Bwana; na watakatifu Wako watakubariki." Zaburi 145:10. Historia ya dhambi itasimama ikidumu milele zote kama ushahidi kwamba uwepo wa sheria ya Mungu umefungamana na furaha ya viumbe vyote alivyoviumba. Ukweli wote wa mambo ukiwa unaonekana kwa uhakika kuhusiana na pambano hilo kuu, sayari zote zinazoishi waaminifu na ile inayoishi waasi, kwa nia moja

wanatangaza: “Njia Zako ni za haki na za Kweli, Ee Mfalme wa watakatifu.” (Sheria ya Mungu-inajumuisha Amri Kumi). [GC 670.3; PK Aya ya 25]

Mbele ya macho ya sayari zote (Universe) imewasilishwa kwa uwazi dhabihu kuu iliyotolewa na Baba na Mwana kwa niaba ya mwanadamu. Saa imewadia ambapo Kristo anachukua nafasi Yake ya haki na kutukuzwa juu ya falme na nguvu na kila jina linalotajwa. Ilikuwa ni kwa ajili ya furaha iliyowekwa mbele Yake-- Kwamba Apate kuwaingiza watu wengi kwenye utukufu—ndiyo maana alistahimili msalaba na kuidharau aibu. Na kwa kadri aibu na huzuni ilivyokuwa kubwa ndiyo jinsi ile furaha ilivyokuwa kubwa zaidi, na utukufu ulivyokuwa mwingi zaidi. Yeye anawaangalia wale waliokombolewa, wakiwa wameumbwa upya katika sura Yake, kila moyo ukiwa na chapa kamilifu ya sura ya Mungu, kila uso ukiakisi mfano wa Mfalme wao. Anaona ndani yao matokeo ya taabu ya nafsi Yake na anaridhika. Kisha, kwa sauti inayosikika kwa wote katika kutano lililokusanyika la wenye haki na waovu, Yeye anatangaza: “Tazama, thamani ya damu Yangu! Kwa ajili ya hawa niliteseka, kwa ajili ya hawa nilikufa, ili waweze kuishi pamoja Nami mbashara milele hata milele.” Na wimbo wa sifa unapanda juu kutoka kwa wale waliovaa mavazi meupe katika kiti cha enzi: “Astahili Mwana-Kondoo aliyechinjwa kuupokea uweza na utajiri na hekima na nguvu na heshima na utukufu na baraka. Ufunuo 5:12. [GC 671.1; PK Aya ya 26]

**Mwisho Wa Waovu Utakaowaletea Maangamizi**

Licha ya kuwa Shetani amelazimishwa kukiri haki ya Mungu na kusujudu kwa ukuu wa Kristo, tabia yake inabaki bila badiliko lolote. Roho ya uasi, kama mkondo wa maji yenye nguvu, inafurika tena. Akiwa amejazwa na wazimu, anaazimu kutosalimu amri kwa pambano hilo kuu. Wakati umefika wa pambano la mwisho la kufa na kupona dhidi ya Mfalme wa mbinguni. Anakimbilia katikati ya raia wake na anajaribu kuwachochea kwa ghadhabu yake mwenyewe na kuwahamasisha waingie vitani papo hapo. Lakini kati ya mamilioni wote wasiohesabika ambao amewashawishi katika kuasi, hakuna hata mmoja anayetambua ukuu wake. Mamlaka yake imefikia mwisho wake. Waovu wamejazwa na chuki ile ile dhidi ya Mungu inayomchochea Shetani; lakini wanaona kwamba suala lao halina tumaini, kwamba hawawezi kumshinda Yehova. Hasira yao inawaka dhidi ya Shetani na wale ambao wamekuwa vibaraka wake katika udanganyifu, kwa ghadhabu ya mashetani wanawageukia na kuwashambulia. [GC 671.2; PK Aya ya 27]

Bwana anasema: “Kwa kuwa umeweka moyo wako kama moyo wa Mungu; basi tazama, nitaleta wageni juu yako, watu wa mataifa wenye kutisha; nao watafuta panga zao juu ya uzuri wa hekima yako, nao watachafua mwangaza wako. Watakushusha hata shimoni.” “Nimekuangamiza, Ewe kerubi ufunikaye, utoke katika mawe hayo ya moto. Nimekutupa chini, nimekulaza mbele ya wafalme,

wapate kukutazama. Nimekufanya kuwa majivu juu ya nchi, machoni pa watu wote wakutazamao.... Umekuwa kitu cha kutisha, wala hutakuwapo tena hata milele." Ezekieli 28:6-8, 16-19. [GC 672.1; PK Aya ya 28]

"Maana silaha zote za mtu mwenye silaha wakati wa mshindo, na mavazi yaliyofingirishwa katika damu, yatakuwa tayari kuteketezwa, yatakuwa kuni za kutiwa motoni." "Maana BWANA ana ghadhabu juu ya mataifa yote, na hasira kali juu ya jeshi lao lote; amewaangamiza kabisa, amewatoa waende kuchinjwa." "Awanyeshee wasio haki mitego, Moto na kiberiti na upepo wa hari, Na viwe fungu la kikombe chao." Isaya 9:5; 34:2; Zaburi 11:6. Moto unashuka kutoka kwa Mungu mbinguni. Dunia inapasuka pasuka vipande. Silaha zilizofichwa katika vilindi vyake zinatoka nje. Miale ya moto inayoteketeza inalipuka kutoka kila uwazi wa mpasuko wa shimo ardhini. Miamba yenyewe inawaka moto. Siku imefika ambayo inaunguza kama tanuru. Na vitu vyote vya asili vinayeyuka kwa moto mkali na kufumuliwa, na nchi na kazi zilizomo ndani yake zitateketea. Malaki 4:1; 2 Petro 3:10. Uso wa dunia unaonekana kama donge moja la volkano linaloyeyuka-- ziwa kubwa la moto linachemka. Umefika wakati wa hukumu na kuangamizwa kwa watu wasiomcha Mungu "siku ya kisasi cha BWANA, mwaka wa malipo, ili kumshindania Sayuni." Isaya 34:8.[GC 672.2; PK Aya ya 29]

Waovu wanapokea malipo yao duniani hapa hapa. Mithali 11:31. "Watakuwa makapi; na siku ile inayokuja itawateketeza, asema BWANA wa majeshi. Malaki 4:1. Wengine wanaangamizwa kwa muda mfupi sana, na wengine wanateseka siku nyingi. Wote wanaadhibiwa "kulingana na matendo yao." Dhambi za wenye haki zikiwa zimehamishiwa kwa Shetani, anateswa si kwa ajili ya uasi wake tu, bali kwa ajili ya dhambi zote ambazo amewasababisha watu wa Mungu kuzitenda. Adhabu yake inapaswa kuwa kubwa zaidi kuliko ya wale aliowadanganya. Baada ya wote walioanguka kwa madanganyo yake kuangamia, yeye bado ataendelea kuishi na kuteseka. Katika miali ya moto unaosafisha, waovu hatimaye wanaangamizwa, shina na tawi--Shetani ndiye shina, wafuasi wake ni matawi. Adhabu kamili ya kuvunjwa sheria itakuwa imetekelezwa; madai ya haki yaliyovunjwa yatakuwa yametimizwa; na ndipo mbingu na nchi zitakapokuwa zikitazama hayo, zinaitangaza haki ya Yehova. [GC 673.1; PK Aya ya 30]

Kazi ya Shetani ya uharibifu imekomeshwa milele. Kwa miaka elfu sita ametekeleza mapenzi yake, akiijaza dunia taabu, misiba na kusababisha huzuni katika sayari zote.* Uumbaji wote umeugua kwa kulia na kuteseka pamoja kwa kutaabika kwa maumivu. Sasa viumbe vya Mungu vimekombolewa milele kutoka katika uwepo wake na majaribu yake. "Dunia yote inastarehe na kutulia; Hata wenye haki "huanzilisha kuimba." Isaya 14:7. Basi kelele za sifa na ushindi zitapanda juu kutoka kwa kila sayari ya wale waliokuwa watiifu"Sauti ya

makutano mengi," "sauti ya maji mengi, na kama sauti ya radi yenye nguvu," inasikika, ikisema: "Haleluya; kwa kuwa Bwana Mungu wetu, Mwenyezi, amemiliki." Ufunuo 19:6 *(kutoka dhambi kuingia mpaka leo ni takribani miaka elfu sita, elfu nne kabla ya Yesu Kuzaliwa na elfu mbili baada, anza kuhesabu toka miaka ya Adamu). [GC 673.2; PK Aya ya 31]

Wakati dunia itakapokuwa imefunikwa na moto wa maangamizi, wenye haki wanaishi salama katika Mji ule Mtakatifu. Juu ya wale ambao walikuwa na sehemu katika ufufuo wa kwanza, mauti ya pili haina nguvu. Ingawa Mungu kwa waovu ni moto ulao, Yeye ni jua na ngao kwa watu Wake. Ufunuo 20:6; Zaburi 84:11. [GC 673.3; PK Aya ya 32]

"Nikaona mbingu mpya na nchi mpya; kwa maana mbingu za kwanza na nchi ya kwanza zimekwisha kupita." Ufunuo 21:1. Moto utateketeza waovu na kuisafisha dunia. Kila kiashiria cha laana kinafutiliwa mbali. Hakuna moto wa kuzimu au jehanamu utakaoendelea kuwaka milele na milele ambao utaweka kumbukumbu ya matokeo ya kutisha ya dhambi mbele ya wale waliokombolewa. [GC 674.1; PK Aya ya 33]

**Kumbukumbu Za Kusulibiwa Kwake**

Kumbukumbu moja tu pekee ndiyo itasalia: Mkombozi wetu daima atabaki kuwa na alama za kusulubishwa Kwake. Juu ya kichwa Chake kilichojeruhiwa, ubavuni Mwake, na kwenye mikono na miguu Yake, ndizo alama pekee za kazi ya kikatili iliyotendwa na dhambi. Asema nabii, akimtazama Kristo katika utukufu Wake: "Yeye alikuwa na miale ing'aayo ikitoka ubavuni Mwake; Habakuki 3:4. Ubavu ule uliotobolewa kwa mkuki, pale ilibobubujika ile chemchemi nyekundu ya damu ambayo ilimpatanisha mwanadamu na Mungu-- pale ndio pana utukufu Wake Mwokozi, pale ndipo "ulipofichwa uweza Wake." "Uweza Hodari wa kuokoa," kwa njia ya dhabihu Yake hii ya ukombozi, alikuwa na nguvu ya kutekeleza haki juu ya wale walioidharau neema na rehema ya Mungu. Na alama za mateso na kudhalilishwa Kwake ndiyo heshima Yake kuu kuliko vyote; Milele hata milele majeraha ya Kalvari yataonyesha sifa Yake na kutangaza uweza Wake. [GC 674.2; PK Aya ya 34]

"Ee mnara wa kundi, kilima cha binti Sayuni, utajiliwa; naam, mamlaka ya kwanza yatakuja, ufalme wa binti Yerusalemu." Mika 4:8. Wakati umefika ambao watu watakatifu wamekuwa wakiutazamia kwa hamu kubwa tangu upanga wa moto ulipowazuia jozi ya wanadamu, yaani wenzi wa kwanza kutoka Edeni, mume na mke, Adamu na Hawa, kwa ajili ya "ukombozi wa milki Yake iliyonunuliwa." Waefeso 1:14. Dunia ambayo hapo awali alikabidhiwa mwanadamu kama ufalme wake, na ikasalitiwa na mwanadamu kwa kukosa uaminifu kwake, na kuwekwa mikononi mwa Shetani na kushikiliwa kwa muda

mrefu na adui mkuu, imerejeshwa kwa ule Mpango Mkuu wa ukombozi. Yote ambayo yalipotezwa na dhambi yamerejeshwa. “Bwana asema hivi... Yeye aliyeiumba dunia na kuifanya; Ndiye aliyeifanya imara; hakuiumba ukiwa, aliiumba ili ikaliwe na watu.” Isaya 45:18. Kusudi la awali la Mungu katika uumbaji wa dunia linatimizwa inapofanywa kuwa makao ya milele ya waliokombolewa. “Wenye haki watairithi nchi, nao watakaa humo milele.” Zaburi 37:29. [GC 674.3; PK Aya ya 35]

Hofu ya kuufanya urithi wa milele kuwa unahusisha tu vitu vinavyoonekana kwa macho au mali, umesababisha watu wengi kupunguza bidii au usongo wa kusimulia kuhusu urithi ule wa wakati ujao, yaani Paradiso, kwani wengi wameona kwa kuvisimulia wataonekana kama vile wana uroho wa vitu (materialistic), jambo hili limewaongoza wengi kuzisimulia Kweli za vitu hivyo vya mbinguni katika nyanja ya kiroho tu, wakati ambapo kuna vitu halisi katika makao hayo, ambavyo watu wanapaswa kuwa na matamanio navyo. (Mbinguni ni nchi halisi na si tu hali fulani ya kihisia). Kristo aliwahakikishia wanafunzi Wake kwamba alikwenda kuwaandalia makao katika nyumba ya Baba Yake. Watu wanaoyakubali mafundisho ya Neno la Mungu hawatakuwa wajinga kabisa kiasi cha kutoelewa kuhusu makao ya mbinguni. Na bado, “Mambo ambayo jicho halikuyaona, wala sikio halikuyasikia, wala hayakuingia katika moyo wa mwanadamu, mambo ambayo Mungu aliwaandalia wampendao.” 1 Wakorintho 2:9. Lugha ya mwanadamu haitoshi kuelezea zawadi ya wenye haki. Itaeleweka tu kwa wale watakaoiona. Hakuna akili finyu yenye ukomo inayoweza kufahamu utukufu wa Paradiso ya Mungu. [GC 674.4; PK Aya ya 36]

**Nchi Ya Waliookolewa**

Katika Biblia urithi wa waliookolewa unaitwa “nchi.” Waebrania 11:14-16. Hapo Mchungaji wa mbinguni analiongoza kundi Lake kwenye chemchemi ya maji ya uzima (maji hai). Mti wa uzima utazaa matunda yake kila mwezi na majani ya mti huo ni kwa ajili ya kuwahudumia/kuwaponya mataifa. Pale kuna vijito vinavyotiririka daima maji yang’aayo kama bilauri na kando yake kuna miti inayoyumbayumba ikitupa vivuli vyake juu ya njia zilizotayarishwa kwa ajili ya waliokombolewa na Bwana. Mle tambarare zilizotapakaa kila mahali, zinainuka na kutuna kuwa vilima vizuri sana, na milima ya Mungu itainua vilele vyake upande wa nyuma. Katika mbuga hizo za amani, kando ya vijito hivyo vya maji vilivyo hai, watu wa Mungu, ambao wamekuwa wakisafiri kwa muda mrefu sana, wapitaji wanaomangamanga na kutangatanga, watapata makao. [GC 675.1; PK Aya ya 37]

“Watu wangu watakaa katika kao la amani; na katika maskani zilizo salama na katika mahali pa kupumzikia penye utulivu.” “Jeuri haitasikiwa tena katika nchi yako, ukiwa na uharibifu hazitakuwa mipakani mwako; Bali utaziita kuta zako,

Wokovu, Na malango yako, Sifa." "Nao watajenga nyumba, na kukaa ndani yake; watapanda mizabibu na kula matunda yake. Hawatajenga, akakaa mtu mwingine ndani yake; hawatapanda, akala mtu mwingine;... Wateule Wangu wataifurahia kazi ya mikono yao muda wa siku nyingi." Isaya 32:18; 60:18; Isaya 65:21, 22. [GC 675.2; PK Aya ya 38]

Huko, "nyika na mahali palipo ukiwa patafurahi; jangwa litashangilia, na kuchanua maua kama waridi." "Badala ya michongoma utamea msunobari, na badala ya mbigili, mhadesi." "Mbwa-mwitu atakaa pamoja na mwana- kondoo, na chui atalala pamoja na mwana-mbuzi; ... na mtoto mdogo atawaongoza." "Hawatadhuru wala hawataharibu katika mlima Wangu wote mtakatifu," asema Bwana. Isaya 35:1; 55:13; Isaya 11:6, 9. [GC 675.3; PK Aya ya 39]

Maumivu hayawezi kuwepo katika angahewa ya mbinguni. Machozi hayatakuweko kamwe tena, wala hakuna misafara ya mazishi, hakuna alama au beji za maombolezo kama nguo za matanga au jeneza. "Mauti haitakuwapo tena; wala maombolezo, wala kilio; ... kwa kuwa mambo ya kwanza yamekwisha kupita." "Wala hapana mwenyeji atakayesema, mimi ni mgonjwa; watu wakaao humo watasamehewa uovu wao." Ufunuo 21:4; Isaya 33:24. [GC 676.1; PK Aya ya 40]

Pale kuna Yerusalemu Mpya, jiji kuu la dunia mpya iliyojaa utukufu mwingi, "taji ya uzuri katika mkono wa Bwana, na kilemba cha kifalme mkononi mwa Mungu wako." "Na mwangaza wake ulikuwa mfano wa kito chenye thamani nyingi, kama kito cha yaspi, safi kama bilauri." "Na mataifa watatembea katika nuru Yake. Na wafalme wa nchi huleta utukufu wao ndani yake." Asema Bwana: "Nitaufurahia Yerusalemu, nitawaonea shangwe watu Wangu." "Maskani ya Mungu ni pamoja na wanadamu, Naye atafanya maskani Yake pamoja nao, nao watakuwa watu Wake, Naye Mungu Mwenyewe atakuwa pamoja nao." Isaya 62:3; Ufunuo 21:11, 24; Isaya 65:19; Ufunuo 21:3. [GC 676.2; PK Aya ya 41]

Katika Jiji la Mungu "hakutakuwa na usiku." Hakuna atakayehitaji au kutamani kupumzika. Hakutakuwa na uchovu katika kufanya mapenzi ya Mungu na kulisifu Jina Lake. Daima tutahisi nguvu za upya wa asubuhi na tutakuwa mbali na kuishiwa nguvu mwishoni mwa siku. "Wala hawana haja ya taa, wala ya nuru ya jua; kwa kuwa Bwana Mungu huwatia nuru." Ufunuo 22:5. Nafasi ya jua linalodhuru, itachukuliwa na mng'ao usioumiza macho, wala kutia macho kiwi kwa uangavu wake, hata hivyo ambao unapita mbali mno mwangaza wa majira ya saa sita mchana. Utukufu wa Mungu na wa Mwana—Kondoo unafurika na kuujaza Mji Mtakatifu kwa nuru isiyozimika au kufifia. Waliokombolewa wanatembea katika utukufu usio na jua wa mchana, usio na kikomo-wa milele. [GC 676.3; PK Aya ya 42]

**Ushindi Wa Upendo Wa Mungu**

Pale waliokombolewa watajua, kama vile wanavyojulikana (watatambuana na kujuana kabisa kwa sura kama hapa duniani). Mapenzi, upendo na huruma ambazo Mungu Mwenyewe amezipanda ndani ya moyo wa kila mtu, kule zitapata matumizi ya kweli kwa vitendo na utamu na uzuri wake wote. Ushirika na mawasiliano safi pamoja na viumbe hai na watakatifu, maisha ya kijamii yenye mwafaka/upatanifu pamoja na malaika waliobarikiwa na waaminifu wa zama/vizazi vyote ambao wamefua mavazi yao na kuyafanya kuwa meupe katika damu ya Mwana-Kondoo, vifungo vile vitakatifu ambavyo vinawafunga pamoja Yeye "ambaye kwa Jina Lake Ubaba wote wa mbinguni na duniani unaitwa-familia yote ya mbinguni na duniani" (Waefeso 3:15)--- hivi vyote husaidia kuunda furaha ya waliokombolewa.[GC 677.1; PK Aya ya 43]

Pale, akili zisizoweza kusahau wala kufa zitatafakari kwa furaha isiyo na kikomo maajabu ya nguvu na uweza Wake wa uumbaji, siri na mafumbo ya upendo na ukombozi. Hakutakuwa na adui katili, mdanganyifu atakayewajaribu watu ili wamsahau Mungu. Pale kila kitivo, shuguli au uwezo wa kutenda vitaendelezwa, kila uwezo wa kujifunza au kuendelea mbele utaongezwa. Upatikanaji wa maarifa hautaichosha akili au kumaliza nguvu ya mwili. Huko shuguli muhimu zaidi zitaendelezwa, matamanio bora ya vilele vya juu yatatimizwa, pia matamanio ya kufanya mambo makuu ya hali ya juu yatatimizwa; na bado vitatokea vilele vipya vya kupanda na kushinda, maajabu mapya ya kufurahia, kustaajabishwa nayo na kupendezwa nayo, Kweli mpya za kujifunza, vitu vipya vitakavyohitaji tutumie nguvu za akili, roho na mwili. [GC 677.2; PK Aya ya 44]

Hazina zote za sayari zote zitakuwa wazi kwa ajili ya watu wa Mungu waliokombolewa kujifunza, kutafiti na kugundua. Wakiwa hawajazuiliwa na mwili huu unaokufa wa duniani hapa, wataruka kwa mabawa bila kuchoka hadi kwenye sayari zile za mbali sana-- sayari zilizotetemeka, kwa huzuni kali wakati wa tukio la msiba wa laana kwa binadamu na kurindima kwa nyimbo za furaha kwa ajili ya habari za mtu mmoja mwenye dhambi aliyekombolewa (1 Kor. 15:53; Ayu. 1:6-8; 2:1-3; 38:4, 7, Luka 15:7,10). Kwa furaha isiyoelezeka watoto wa duniani wanashiriki katika furaha na hekima ya viumbe ambao kamwe hawakuanguka dhambini. Wanashiriki hazina za ujuzi, maarifa na ufahamu unaopatikana kupitia zama nyingi kwa kutafakari kazi ya uumbaji wa mikono ya Mungu. Kwa macho yasiyofifia au kuwa na mipaka ya upeo wa macho, wanauoana utukufu wa uumbaji-- mifumo ya jua na nyota na mifumo ya sayari, yote katika mpangilio wake wa awali uliowekwa kukizunguka kiti cha enzi cha Mungu. Juu ya vitu vyote, tangu kile kilicho kidogo sana hadi vile vile vilivyo vikubwa zaidi, Jina la Muumbaji limeandikwa, na vyote vinadhihirisha utajiri wa nguvu Zake hayo yanapoonyeshwa kwao. [GC 677.3; PK Aya ya 45]

Na ile miaka itakavyokuwa ikiendelea kusonga mbele katika umilele, italeta ufunuo mkubwa na wenye utukufu kumhusu Mungu na Kristo kwa wingi zaidi. Kwa kuwa uelewa ni endelevu, kadhalika basi ndivyo maarifa yatakavyozidi kuongezeka, na ndivyo upendo, kicho, heshima na furaha vitakavyongezeka. Kwa kadiri watu wanavyoendelea kumwelewa zaidi Mungu, ndivyo watakavyozidi kuitamani na kuipenda zaidi tabia Yake. Yesu alipofungua mbele yao utajiri wa ukombozi na mafanikio ya kustaajabisha katika pambano kuu na Shetani, mioyo ya waliokombolewa ilisisimka kwa kujitoa wakfu na kumpenda zaidi, nao kwa shangwe kuu zaidi watavicharaza vinubi vyao vya dhahabu; na elfu kumi mara elfu kumi na maelfu ya maelfu ya sauti zitaungana pamoja ili kuvumisha pambio litakalofumuka kwa sifa yenye kibwagizo chenye nguvu. [GC 678.1; PK Aya ya 46]

"Na kila kiumbe kilichoko mbinguni na juu ya nchi na chini ya nchi na juu ya bahari, na vitu vyote vilivyomo ndani yake, nalivisikia, vikisema, Baraka na heshima na utukufu na uweza una Yeye aketiye juu ya kiti cha enzi, na Yeye Mwana-Kondoo, hata milele na milele." Ufunuo 5:13. [GC 678.2; PK Aya ya 47]

Pambano kuu limekwisha. Dhambi na wenye dhambi havipo tena. Ulimwengu na sayari zake zote uko safi. Mdundo mmoja tu wa maelewano na furaha ndio unapiga katika uumbaji Wake wote ulio mpana sana. Kutoka Kwake Yeye aliyeumba vyote, hububujika uhai, uzima, nuru na furaha, katika ufalme Wake wote, katika anga na milki yote isiyo na kikomo au mipaka. Kuanzia kwenye ile chembe ndogo kabisa ya atomu hadi kwenye ulimwengu mkubwa zaidi, vitu vyote, vyenye uhai (vyenye seli) na visivyo na uhai (vyenye atomu), katika uzuri wao usiofunikwa na kivuli chochote na furaha yao iliyo kamilifu kabisa, vinatangaza kwamba MUNGU NI PENDO. (1Yohana 4:8!). [GC 678.3; PK Aya ya 48]

# Kiambatanisho

**Nukuu za Jumla**

Masahihisho au maelezo yaliyofanywa na Wadhamini wa E. G. White Novemba 19, 1956 na Desemba 6, 1979.

Sura ya 3; Aya ya 5. **VYEO**.—Katika kifungu cha maelezo kilichoingizwa katika Kanuni za Kanisa Katoliki (Catholic Canonical Law, au *Corpus Juris Canonici*), Papa Inosenti wa Tatu (Pope Innocent III) alitangaza kwamba Papa wa Roma ni "mwakilishi duniani, siyo wa wanadamu, bali wa Mungu mwenyewe hapa duniani (Vicegerent);" na katika maelezo yaliyoongezwa baadaye kwenye sehemu hiyo inaelezwa kwamba hiyo ni kwa sababu yeye ni wakala wa Kristo, ambaye ni "Mungu kamili na mwanadamu kamili." Angalia katika *Decretales Domini Gregorii Papae IX (Amri za Bwana [Yehova] Papa Gregori wa Tisa), liber 1, de translatione Episcoporum (juu ya makabidhiano ya Maaskofu*), kichwa cha makala Na. 7, sura ya 3; Corpus Juris Canonici (Kanuni za Kanisa Katoliki) (toleo la 2 la Laiputsiki [Leipzig] la mwaka wa 1881), safu ya 99; (toleo la Paris la mwaka 1612), tom. 2, Decretales, safu ya 205. Nyaraka zilizo na matakamko haya zilikusanywa na Gratian, aliyekuwa anafundisha katika Chuo Kikuu cha Bologna karibu na mwaka wa 1140. Kazi yake iliongezwa na kuhaririwa upya na Papa Gregori wa Tisa katika toleo jipya lililotoka mwaka 1234. Nyaraka zingine zilionekana katika miaka iliyofuata toka wakati hata wakati pamoja na Extravagantes [mkusanyo wa nyaraka na amri zilizotolewa na matamko ya kanisa kupitia mapapa katika nyakati mbalimbali ziliingizwa katika Kanuni ya Kanisa], zilizoongezwa karibu na mwisho wa karne ya kumi na tano. Zote hizo, pamoja na Decretum [amri za Mapapa] alizokusanya Gratian, zilichapishwa katika *Corpus Juris Canonici* (Kanuni za Kanisa Katoliki) za mwaka 1582. Papa Pius wa Kumi aliidhinisha kuwekwa kwa amri hizo za mapapa katika Kanuni za Kanisa mnamo mwaka 1904 na kanuni ile iliyotengenezwa ilianza kutumika rasmi mwaka 1918.

Kwa ajili ya cheo hiki cha "Lord God the Pope" (Bwana Mungu Papa) angalia maelezo yake katika nyaraka za ziada-Extravagantes za Papa Yohane wa Ishirini na Mbili (Pope John XXII), Kichwa cha makala Na. 14, sura ya 4, *Declaramus*. Katika toleo lile la Antwerp la *Extravagantes*, la mwaka 1584, maneno haya *"Dominum Deum nostrum Papam"* (Bwana Mungu wetu Papa) yanatokea katika safu ya 153. Katika toleo la Parisi la mwaka 1612, yanatokea katika safu ya 140. Katika matoleo kadhaa yaliyochapishwa tangu mwaka 1612 neno hili "*Deum*" (Mungu) limeondolewa.

Sura ya 3; Aya ya 9. **KUTOWEZA KUKOSEA KAMWE** (Infallibility)—Kuhusu fundisho hili la kutoweza kukosea kamwe kama lilivyotangazwa katika kikao cha

Baraza la Vatikani cha mwaka 1870-71, angalia Philip Schaff *Creeds of Christendom*, (Itikadi au Kanuni za Imani za Ulimwengu wa Kikristo), juzuu ya 2, *Dogmatic Decrees of the Vatican Council* (Kanuni za Mafundisho ya Dini zilizotolewa na Baraza la Vatikani), kurasa za 234-271, ambazo ndani yake, maneno ya Kilatini na ya Kiingereza yametumika. Kwa mjadala wake angalia, kwa mtazamo wa Kanisa Katoliki la Roma, katika *The Catholic Encyclopedia* (Ensaiklopedia ya Kikatoliki), juzuu ya 7, makala - "Kutoweza Kukosea Kamwe," iliyoandikwa na Patrick J. Toner, uk. 790. James Cardinal Gibbons, *The Faith of Our Fathers* (Imani ya Mababa zetu) (Baltimore: John Murphy Company, toleo la 110 la mwaka 1917), sura ya 7 na ya 11. Kwa ukinzani [upingaji] uliotoka katika Kanisa Katoliki la Roma dhidi ya fundisho hili lisemalo kwamba Papa hawezi kukosea kamwe, angalia kitabu cha Johann Joseph Ignaz von Dollinger (jina lake la utani ni "Janus") kiitwacho *The Pope and the Council* (Papa na Baraza) (New York: Charles Scribner's Sons, 1869); na kitabu cha W. J. Sparrow Simpson, kiitwacho *Roman Catholic Opposition to Papal Infallibility* (Ukinzani wa Wakatoliki wa Roma dhidi ya Kutoweza Kukosea Kamwe kwa Papa) (London: John Murray, 1909). Kwa mtazamo usio wa Kiroma, angalia kitabu cha George Salmon, cha *Infallibility of the Church* (Kutoweza Kukosea Kamwe Kwa Kanisa) (London: John Murray, toleo lililofanyiwa masahihisho la 1914).

Sura ya 3; Aya ya 12. **KUABUDU SANAMU**.—"Ibada ya Sanamu ..... ilikuwa ni mojawapo ya mambo ya upotovu katika Ukristo yaliyoteleza na kuingia kwa kunyatia na karibu bila kutambuliwa kabisa au kuonwa. Upotovu huu haukujitokeza mara moja, kama ulivyofanya uzushi mwingine [mafundisho ya uongo ya kutokukosea kamwe kwa Papa], maana kwa hali kama hiyo ungekuwa umekosolewa na kukemewa kwa uakli: lakini ukiwa umeanza kwa kujificha chini ya vazi zuri, basi polepole, desturi au tendo moja baada ya jingine likaingizwa taratibu kuhusiana na ibada hiyo, hata kanisa likawa limezama kabisa katika ibada ya sanamu, si tu bila kukabiliwa na upinzani wenye nguvu, lakini pasipo kutolewa malalamiko yoyote yenye nguvu ya kulipinga jambo hilo; na hatimaye jitihada ilipofanywa kuung'oa kabisa, uovu huo ulionekana ya kuwa ulikuwa umeotesha mizizi yake chini sana kiasi kwamba haukuweza kuondoka.... Jambo hilo chimbuko lake kwa kufuatilia linahusiana na mwelekeo wa ibada ya sanamu ulio ndani ya moyo wa mwanadamu na mwelekeo wake wa kukitumikia kiumbe kuliko Muumbaji.....

"Sanamu na picha ziliingizwa kanisani kwa mara ya kwanza, si kwa kusudi la kuabudiwa, lakini kuwa badala ya vitabu au vielelezo vya kuwafundishia wale waliokuwa hawawezi kusoma au kuamsha moyo wa kumcha Mungu ndani ya watu wengine. Ni kwa kiasi gani sanamu hizo zilikidhi kusudi hili, bado ni jambo la kutiliwa mashaka; lakini, hata tukikubali kwamba jambo hilo lilikuwa hivyo kwa muda mfupi, mara moja lingekoma kuwa hivyo, tena ilikuja kugunduliwa

kwamba picha na sanamu zilizoingizwa kanisani zilitia giza kuliko nuru ndani ya mioyo ya wale waliokuwa wajinga, ziliishusha chini ibada, kuliko kuiinua juu ibada ya yule aabuduye. Kwa hali yoyote ile vile zilivyokuwa zimekusudiwa kuyaelekeza mawazo ya watu kwenda kwa Mungu, haikufanyika na badala yake zikawageuza mbali Naye na kuwafanya waabudu vitu vilivyotengenezwa na watu." - J. Mendham, *The Seventh General Council, the Second of Nicaea* (Baraza Kuu la Saba, la Pili katika Nisea), utangulizi, ukurasa wa iii-vi.

Kwa kumbukumbu za mkutano na maamuzi ya Baraza la Pili la Nisea, 787 B.K., lililokuwa limeitishwa ili kuimarisha ibada ya sanamu, angalia Baronius, *Ecclesiastical Annals* (Kumbukumbu za Kihistoria za Kanisa); Ed. Stillingfleet, Defense of the Discourse Concerning the Idolatry Practiced in the Church of Rome (Utetezi wa Hotuba inayohusu Ibada ya Sanamu inayoendeshwa katika Kanisa la Roma) (London, 1686); *A Select Library of Nicene and Post-Nicene Fathers* (Mfululizo wa Vitabu vilivyochaguliwa vya Mababa wa Nisea [au Nikene] na wale waliokuja Baada ya Nisea), mfululizo wa pili, gombo la 14, kurasa za 521-587 (New York, 1900); Charles J. Hefele, *A History of the Councils of the Church, From the Original Documents* (Historia ya Mabaraza ya Kanisa Kutoka katika Hati Asilia), kitabu cha 18, sura ya 1, sehemu za 332 na 333; sura ya 2, sehemu za 345 hadi 352 (Toleo la T. and T. Clark la 1896), juzuu ya 5, kurasa za 260 hadi 304, 342 hadi 372.

Sura ya 3; Aya ya 16. **SHERIA YA JUMAPILI YA KONSTANTINO**.—Amri iliyotolewa na mfalme wa dola Konstantino (Constantine) tarehe saba Machi, 321 B.K., kuhusu siku ya kupumzika na kuacha kufanya kazi, inasomeka hivi:

"Majaji wote na watu wote wanaokaa mijini, pamoja na mafundi stadi wote watalazimika kupumzika katika Siku ya heshima ya Jua [Jumapili]. Watu wale wa mashambani hata hivyo, wanaweza kuendelea kwa uhuru kushughulika na kazi zao za kulima mashamba, kwa sababu inatokea mara kwa mara kwamba hakuna siku zingine zaidi zinazofaa kwa upandaji wa mbegu wa nafaka, katika mistari iliyochimbwa au kupanda mizabibu katika mifereji iliyochimbwa. Ili kwamba majaliwa yanayotolewa na Mungu wa mbinguni yasije yakapotea bure kwa kukosa nafasi ya muda huo mfupi." - Joseph Cullen Ayer, *A Source Book for Ancient Church History* (Kitabu cha Marejeo cha Historia ya zamani ya Kanisa) (New York: Charles Scribner's Son, 1913), sehemu Kuu ya Pili, pitio la 1, sura ya 1, sehemu ya 59g, kurasa za 284 hadi 285.

Hati Asilia ya Kilatini imo katika kitabu cha *Codex Justinian* (Mkusanyo wa Sheria na Kanuni za Wafalme wa Dola ya Roma ulioamriwa na Yustiniani), mfululizo wa kitabu cha 3, kichwa cha 12, msamiati wa 3. Sheria hiyo imetolewa kwa Kilatini na kwa Kiingereza katika tafsiri iliyo katika kitabu cha Philip Schaff cha *History of the Christian Church* (Historia ya Kanisa la Kikristo), juzuu ya 3, kipindi cha 3, sura ya

7, sehemu ya 75, uk. 380, maelezo yaliyo chini Na. 1; na katika kitabu cha James A. Hessey cha *Bampton Lectures, Sunday* (Hotuba za Bamputoni, Jumapili), hotuba ya 3, aya ya 1, toleo la 3; lililochapishwa na Murray mwaka wa 1866, uk. 58. Angalia majadiliano katika kitabu cha Schaff kilichotajwa hapo juu; na katika kitabu cha Albert Henry Newman, *A Manual of Church History* (Kitabu cha Mwongozo cha Historia ya Kanisa) (Philadelphia: The American Baptist Publication Society, kilichochapishwa mwaka 1933), toleo lililofanyiwa masahihisho, juzuu ya 1, kurasa za 305 hadi 307; na katika kitabu cha Leroy E. Froom, *The Prophetic Faith of Our Fathers* (Imani Iliyojengwa juu ya Unabii ya Mababa Zetu) (Washington, D.C.: Review and HeraldPublishing Association; 1950), juzuu ya 1, kurasa za 376-381.

Sura ya 3; Aya ya 20. **TAREHE ZA KIUNABII**.—Kanuni muhimu katika kutafsiri unabii kuhusiana na unabii unaohusu wakati ni kanuni ya mwaka mmoja kwa siku moja, ambayo chini yake siku moja ya wakati wa unabii inahesabika kama mwaka mmoja wa kawaida wa wakati wa historia. Kabla ya wana wa Israeli kuingia katika nchi ya Kanaani waliwatuma wapelelezi 12 kuichunguza. Wapelelezi walikuwa kule kwa siku arobaini, nao waliporudi, Waebrania wakiwa wameingiwa na hofu kuu kutokana na taarifa yao, walikataa kupanda na kwenda kuikalia nchi ya Ahadi. Matokeo yake yakawa ni hukumu ambayo Bwana aliitoa kwao: "Kwa hesabu ya siku mlizoipeleleza nchi, yaani, siku arobaini kila siku kuhesabiwa mwaka, mtayachukua maovu yenu, ndiyo miaka arobaini." Hesabu 14:34. Njia kama hiyo ya kuhesabu wakati ujao inaonyeshwa kupitia nabii Ezekieli. Miaka arobaini ya adhabu kwa ajili ya maovu iliingoja ufalme wa Yuda. Bwana Alisema kupitia nabii: "utalala kwa ubavu wako wa kuume, nawe utauchukua uovu wa nyumba ya Yuda; siku arobaini, Ezekieli 4:6. Kanuni hii ya siku moja kuwakilisha mwaka ina matumizi muhimu katika kufasiri wakati wa unabii wa "jioni na asubuhi elfu mbili na mia tatu" (Danieli 8:14,) pamoja na kipindi cha siku 1260, kinachoonyeshwa kwa namna mbalimbali kama "wakati, na nyakati mbili, na nusu wakati" (Danieli 7:25), "miezi arobaini na miwili" (Ufunuo 11:2; 13:5), na "siku elfu na mia mbili na sitini" (Ufunuo 11:3; 12:6).

Sura ya 3; Aya ya 24. **MAANDIKO YALIYOGHUSHIWA**.—Miongoni mwa hati ambazo kwa wakati huu wa sasa zinakubaliwa na watu wote kuwa ni za kughushi [za bandia], ni "Donation of Contantine (Mchango wa Konstantino) pamoja na zile za Pseudo-Isdorian Decretals (Mkusanyo wa Amri za Mapapa wa Isidori wa Uongo). "Mchango wa Konstantino" Donation of Contantine ni jina linalotumika kutokana na mapokeo, kuanzia sehemu ya mwisho ya Zama za Kati, kutajwa kwa hati inayodaiwa kwamba iliandikwa na Konstantino Mkuu na kupelekwa kwa Papa Sylvester wa Kwanza, ambayo inapatikana kwanza katika muswada wa Parisian (*Codex lat.* 2777 Mkusanyo wa Amri za Wafalme wa Dola ya Roma kwa Kilatini), ambayo huenda iliandikwa mwanzoni mwa karne ya tisa. Tangu karne ya kumi na moja hati hiyo imetumika kama hoja yenye nguvu inayoyaunga mkono madai ya

upapa na matokeo yake ni kwamba kuanzia karne ya kumi na mbili imekuwa kiini cha kubishaniwa sana. Kwa wakati huo huo, kwa kuufanya upapa ufikiriwe kuwa kipindi cha katikati cha dola  Dola ya Kirumi ya awali na Dola ya Roma ya Zama za Kati [kuanzia 1100 hadi 1500] na kwa njia hiyo kuweka msingi wa kinadharia wa kuviunganisha vipindi hivyo viwili bila kukatika kwa kuendelea kuzipokea sheria za serikali ya Kiroma katika Zama za Kati, ushawishi wake si mdogo katika historia ya ulimwengu." *The New Schaff- Herzog Encyclopedia of Religious Knowledge* (Ensaiklopidia Mpya ya Maarifa ya Kidini ya Shafu Hertsoko), juzuu ya 3, makala: Mchango wa Konstantino kwa Papa, ukurasa wa 484 na 485.

Nadharia hiyo ya kihistoria iliyokuzwa kwa njia ya "Donation au mchango" imejadiliwa kikamilifu katika kitabu cha Henry E. Cardinal Manning, kiitwacho *The Temporal Power of the Vicar of Jesus Christ* (Mamlaka ya Kidunia ya Yule Aliye Badala ya Yesu Kristo yaani, Papa), London, 1862. Hoja kuhusu michango  zilikuwa ni za aina ya kisomi zaidi na uwezekano wa kughushi haukutajwa mpaka ulipotokea uhakiki wa historia katika karne ya kumi na tano. Nikolasi wa Kusa (Nicholas of Cusa) alikuwa mtu wa kwanza aliyetoa hitimisho lake kwamba Konstantino alikuwa hajapata kamwe kutoa tolea kama lile. Lorenzo Valla wa Italia alionyesha kwa wazi kabisa uongo wa hati ile ya michango katika mwaka 1450. Angalia kitabu cha Christopher B. Coleman cha *Treatise of Lorenzo Valla on the Donation of Constantine* (Makala ya Lorenzo Valla juu ya Mchango wa Konstantino) (New York, 1927). Walakini, kwa karne moja zaidi imani juu ya uhalali wa ule "Mchango wa Konstantino" pamoja na Mkusanyo ule wa Uongo wa Amri za Mapapa (*False Decretals*) ilidumishwa. Kwa mfano, Martini Luther mara ya kwanza alizikubali amri za mapapa, lakini katika muda mfupi alimwambia Eki (Eck): "Mimi nina mashaka na  matamko haya;" na kwa Spalatin, alisema: "Yeye [papa] katika amri zake anaharibu na kumsulibisha Kristo, yaani, anaisulibisha ile Kweli."

Inadaiwa kuwa imekwisha kuthibitishwa kwamba waraka wa mchango ni (1) hati ya kughushi [ya uongo], (2) Ni kazi ya mtu fulani mmoja au ya kipindi fulani kimoja, (3) yule aliyeghushi maandiko hayo amezitumia nyaraka au hati za zamani zaidi, (4) kughushi huko kulitokea karibu na mwaka wa 752 na 778. Kwa upande wa Wakatoliki, wao walikwisha kuachilia mbali kutetea uhalali wa hati hiyo pamoja na Baronius katika kitabu chake cha *Ecclesiastical Annals* (Kumbukumbu za Kihistoria za Kanisa), katika mwaka wa 1592. Pata ushauri mzuri kabisa wa maelezo ya K. Zeumer [Tsoima] katika kitabu chake cha *Festgabe fur Rudolf von Gneist* (Toleo la Sikukuu kwa ajili ya Rudolfu wa Ginaisti] (Berlin, 1888). Kimetafsiriwa katika Makala (*Treatise*) ya Coleman, kilichorejelewa hapo juu, na katika kitabu cha Ernest F. Henderson cha *Select Historical Documents of the Middle Ages* (Hati Teule za Kihistoria za Zama za Kati) (New York, 1892), uk. 319; Briefwechset (Toleo la Vaima [Weimer]), kurasa za 141 na 161. Angalia pia *The New Schaff-Herzog Encyclopedia*

*of Religious Knowledge* (Ensaiklopidia Mpya ya Maarifa ya Kidini ya Shafu-Heretsoko) (1950), juzuu ya 3, uk. 484; kitabu cha F. Gregorovio (Gregorovius) cha *Rome in the Middle Ages* (Roma katika Zama za Kati), juzuu ya 2, uk. 329; na kitabu cha Johann Joseph Ignaz von Dollinger kiitwacho *Fables Respecting the Popes of the Middle Ages* (Visa vifupi Vinavyowahusu Mapapa wa Zama za Kati) (London, 1871).

"Maandishi ya Uongo" yaliyotajwa katika maandiko haya yanajumuisha pia ule Mkusanyo wa Amri za Mapapa wa Isdore-wa- Uongo (Pseudo-Isdorian Decretals), pamoja na maandiko mengine ya kughushi. Mkusanyo wa hizo Amri za Mapapa wa Isdore -za-Kugushi ni nyaraka fulani za uongo zinazosemekana kwamba zilitolewa na mapapa wa awali kuanzia kwa Clement (mwaka wa 100 B.K.) Mpaka Gergory mkuu (600 BK), zilizoingizwa katika mkusanyo wa amri hizo wa karne ya tisa unaodaiwa kwamba ulifanywa na "Isdore Merikatori" (Mercator). Jina hilo la Pseudo-Isdorian Decretals limekuwa likitumika tangu kuzuka kwa ukosoaji wa maandiko (criticism) katika karne ya kumi na tano.

Huyo Isdore-wa-Uongo alichukua kama msingi wa maandiko yake ya kughushi mkusanyo wa kanuni halali za kanisa zilizoitwa Hispana Gallica Augustodunensis, kwa njia hiyo akipunguza hatari ya kugunduliwa kwake, kwa sababu mkusanyo ule wa kanuni za kanisa ulifanywa na watu wengi kwa kuongeza mambo mapya katika yale ya zamani. Kwa njia hiyo kughushi kwake maandiko yale kulifichwa na kusionekane wazi zaidi kulipochanganywa na Maandishi ya kweli. Uongo wa maandiko ya kubuni tu ya Isidore wa Pseudo-Isidore sasa unajulikana bila kuwa na ubishi wowote, uhakikisho upo kutokana na ushahidi uliomo ndani yake, utafiti katika vyanzo vyake, mbinu zilizotumika na ukweli kwamba maandiko hayo yalikuwa hayajulikani kabisa kabla ya mwaka 852. Wanahistoria wanaafikiana kwamba mwaka wa 850 au 851 ulikuwa ndio mwaka uliodhaniwa kukamilisha kazi ya mkusanyo huo wa maandiko ya kughushi, kwa sababu hati hiyo inatajwa kwa mara ya kwanza katika kitabu cha Admonitio cha mkusanyo wa sheria kilichotolewa na Baraza la makasisi wa kanisa la Quiercy '*Admonitio of the capitulary of Quiercy*,' katika mwaka wa 857.

Mtunzi wa nyaraka hizi za kughushi [za uongo] hajulikani. Uwezekano upo kwamba zilitoka kwenye chama kipya cha kanisa cha wakereketwa kilichoundwa pale Rheims, Ufaransa katika karne ya tisa. Inakubalika kwamba Askofu Hincmar wa Rheims aliutumia mkusanyo huo wa matamko haya ya mapapa wakati wa kumwondoa madarakani Rothad Swaso ambaye aliupeleka Roma mkusanyo wa amri za mapapa katika mwaka wa 864 na kuyaweka mbele ya Papa Nicholas I.

Miongoni mwa wale walioyapinga maandiko yale ya kughushi walikuwamo akina Nicholas wa Cusa (1401- 1464), Charles Dumoulin (1500-1566) na George Cassender (1513-1564). Ushahidi usiopingika kabisa wa uongo wa matamko hayo ya kughushi ulitolewa na David Blondel, mnamo mwaka 1628. [GC 683.1]

Toleo la mapema limetolewa katika kitabu cha Migne Patrolgia Latina, CXXX. kwa ajili ya mswada wa zamani sana (uliandikwa kwa mkono), ambao ni bora kuliko zote, angalia kitabu cha P. Hinschius, cha *Decretales PseudoIsdorianae at Capitula Angilramni* (Leipzig, 1863). Tafuta ushauri katika *The NewSchaff-Herzog Encyclopedia of Religious Knowledge* (Ensaiklopidia Mpya ya Maarifa ya Kidini ya Shafu-Heretsoko) (1950), gombo la 9, kurasa za 343-345. Angalia pia kitabu cha H. H. Milman cha *Latin Christianity* (Ukristo wa Kilatini) (juzuu ziko 9), juzuu ya 3; kitabu cha Johann Joseph Ignaz von Dollinger kiitwacho *The Pope and the Council* (Papa na Baraza) (1869); na kitabu cha Kenneth Scott Latourette kiitwacho *A History of the Expansion of Christianity* (Historia ya Kuenea Kwa Ukristo) (1939), juzuu ya 3; *The Catholic Encyclopedia* (Ensaiklopidia ya Kikatoliki), juzuu ya 5, makala: "Mkusanyo wa Uongo wa Amri za Mapapa" (False Decretals) na makala ya Fournier yenye kichwa cha "Etudes sure les Fausses Decretals" (Utafiti juu ya Mkusanyo wa uongo wa Amri za Mapapa) ambayo inapatikana katika kitabu cha *Revue d'Historique Ecclesiastique* (Uhakiki wa [au Marejeo ya] Historia ya Kanisa), (Louvain) juzuu ya 7 (1906), na juzuu ya 8 (1907).

Sura ya 3, Aya ya 28. **AMRI YA HILDEBRAND** (Gregori Wa 7).—Kwa toleo asilia la Kilatini angalia kitabu cha Baronio cha *Annales Ecclesiastici* (Kumbukumbu za Historia ya Kanisa), ann. 1076, juzuu ya 17, kurasa za 405 na 406 za kitabu kilichochapishwa Parisi mwaka wa 1869; na kitabu cha *Monumenta Germaniae Historica Selecta*, juzuu ya 3, uk. 17. Kwa tafsiri yake ya Kiingereza angalia kitabu cha Frederic A. Ogg cha *Source Book of Medieval History* (Kitabu cha Marejeo cha Historia ya Zama za Kati) (New York: Charles Scribner's Sons, 1905), sehemu ya 3, kifungu cha 65, kurasa za 136 hadi 139.

Kwa mjadala juu ya msingi wa Amri hiyo (ya Hildebrand), angalia kitabu cha James Brice, *The Holy Roman Empire* (Dola Takatifu ya Kiroma), toleo lililofanyiwa masahihisho, sura ya 10; na kitabu cha James W. Thompson na Edgar N. Johnson cha *Introduction to Medieval Europe* (Kitabu cha Msingi cha Historia ya Ulaya ya Zama za Kati), mwaka 300-1500, kurasa za 377-380.[GC 683.4]

Sura ya 3, Aya ya 28. **TOHARANI** (Purgatory).—Dkt. Joseph Faa Di Bruno anafasili neno toharani kwa maneno haya: Toharani ni hali ya kuteseka baada ya maisha haya kukoma, ambapo roho zinashikiliwa kizuizini pale kwa muda fulani baada ya kuondoka katika maisha haya, baada ya dhambi zao za kufisha kuondolewa mawaa na hatia yake na kusamehewa mateso yale ya milele ambayo zilistahili kuyapata; lakini kuhusiana na hizi dhambi zao bado wanalo deni la kulipa kwa kuteswa au kupata adhabu ya kimwili kwa muda mfupi; sawasawa na roho zinazoondoka katika maisha haya zikiwa zina hatia ya kutenda dhambi ndogo ndogo." *Catholic Belief* (Imani ya Kikatoliki) (toleo la mwaka 1884;

lililoidhinishwa kusomwa na watu wote [imprimatur] na Askofu Mkuu wa New York), ukurasa 196.

Angalia pia kitabu cha K. R. Hagenbach cha *Compendium of the History of Doctrines* (Ufupisho wa Historia ya Mafundisho ya Dini) (Toleo la T. and T. Clark), gombo la 1, kurasa za 234-237, 405, 408; juzuu ya 2, kurasa za 135-150,308,309; kitabu cha Charles Elliott cha *Delineation of Roman Catholicism* (Maelezo ya Kinagaubaga ya Ukatoliki wa Roma), kitabu cha 2, sura ya 12; na *The Catholic Encyclopedia* (Ensaiklopidia ya Kikatoliki), juzuu ya 12, makala: “Toharani.” [GC 683.6]

Sura ya 3, Aya ya 29. **VYETI VYA MSAMAHA WA DHAMBI** (Indulgences).—Kwa maelezo ya kina ya historia ya fundisho hili la vyeti vya msamaha wa dhambi, angalia kitabu cha Mandell Creighton, kiitwacho *A History of the Papacy From the Great Schism to the Sack of Rome* (Historia ya Upapa Kuanzia Mfarakano Mkuu mpaka Kuangamizwa kwa Roma) (London: Longmans, Green and Co., 1911), juzuu ya 5, kurasa za 54-64,71; Makala ya W. H. Kenti ya “Indulgences” (Vyeti vya Msamaha wa Dhambi) katika *The Catholic Encyclopedia* (Ensaiklopidia ya Kikatoliki), juzuu ya 7, ukurasa wa 783-789; Kitabu cha H. C. Lea, kiitwacho *A History of Auricular Confession and Indulgences in the Latin Church* (Historia ya Maungamo Yanayosikilizwa kwa Masikio na Vyeti vya Msamaha wa Dhambi katika Kanisa la Kilatini [Roma]) (Philadelphia: Lea Brothers and Co., 1896); kitabu cha Thomas M. Lindsay, kiitwacho A History of the Reformation (Historia ya Matengenezo ya Kanisa) (New York; Charles Scribner’s Sons, 1917), juzuu ya 1, kurasa za 216-227; kitabu cha Albert Henry Newman, kiitwacho *A Manual of Church History* (Kitabu cha Mwongozo wa Historia ya Kanisa) (Philadelphia: The American Baptist Publication Society, 1953), juzuu ya 2, ukurasa wa 53,54,62; Kitabu cha Leopold Ranke, kiitwacho *History of the Refornation in Germany* (Historia ya Matengenezo ya Kanisa Ujerumani) (toleo la 2 la London; 1845), lilitafsiriwa na Sarah Austin, juzuu ya 1, kurasa za 331,335-337,343- 346; Kitabu cha Preserved Smith, kiitwacho *The Age of the Reformation* (Kipindi cha Matengenezo ya Kanisa) (New York: Henry Holt and Company, 1920), kurasa za 23-25,66.

Kwa utendaji wake wa bidii wa fundisho hilo la Vyeti vya Msamaha wa Dhambi katika kipindi cha Matengenezo ya Kanisa, angalia mada iliyotolewa na Dk. H. C. Lea, yenye kichwa cha “Indulgences in Spain (Vyeti vya Msamaha wa Dhambi nchini Hispania) iliyochapishwa katika *Papers of the American Society of Church History* (Mada za Chama cha Amerika cha Historia ya Kanisa), juzuu ya 1, kurasa za 129-171.

Kwa habari ya faida ya mwanga wa historia unaosaidia kulimulika suala hilo, Dk. Lea anasema hivi katika aya yake ya kwanza: “Ikiwa haijasumbuliwa na mashindano [malumbano] yaliyopamba moto kati ya Luther na Dk. Eck na

Silvester Prierias, nchi ya Hispania kwa utulivu iliendelea kuzifuata njia za zamani zilizokuwa zimekanyagwa sana, nayo inatupatia nyaraka/hati rasmi zisizoweza kupingwa, na ambazo zinatuwezesha sisi kulichunguza suala hilo katika nuru safi ya historia."

Sura ya 3, Aya ya 30. **MISA** (The Mass).—Kwa fundisho wa Misa kama lilivyowekwa katika Baraza la Trenti, angalia *The Canons and Decrees of the Council of Trent* (Kanuni za Kanisa na Amri zilizotolewa na Baraza la Trent) katika kitabu cha Philip Schaff, kiitwacho *Creeds of Christendom* (Itikadi za Dini za Ulimwengu wa Kikristo), juzuu ya 2, kurasa za 126-139, ambamo maelezo yote mawili, kwa Kilatini na Kiingereza, yametolewa. Angalia pia kitabu cha H. G. Shroeder, kiitwacho Canons and Decrees of the Council of Trent (Kanuni za Kanisa na Amri zilizotolewa na Baraza la Trenti) (St. Louis, Missouri: B. Herder, 1941). [GC 684.2]

Kwa mjadala juu ya Misa, angalia *The Catholic Encyclopedia* (Ensaiklopidia ya Kikatoliki), juzuu ya 5, makala: "Ekaristi," iliyoandikwa na Joseph Pohle, ukurasa 572 ff.; kitabu cha Nikolaus Gihr cha *Holy Sacrifice of the Mass, Dogmatically, Liturgically, Ascetically Explained* (Kafara Takatifu ya Misa, Imeelezwa Kiimani, Kiliturujia, na kwa Kujinyima raha na anasa za mwili), toleo la 12, (St. Louis, Missouri: B. Herder, 1937); kitabu cha Josef Andreas Jungmann cha *The Mass of the Roman Rite, Its Origins and Development* (Misa ya Taratibu za ibada ya Kiroma, Chanzo chake na Maendeleo yake), imetafsiriwa na Francis A. Brunner kutoka katika lugha ya Kijerumani) (New York: Benziger Bros., 1951). Kwa mtazamo usio kuwa wa Kikatoliki, angalia kitabu cha John Calvin, *Institutes of the Christian Religion* (Mambo Yaliyoanzishwa na Dini ya Kikristo), kitabu cha 4, sura ya 17,18; na kitabu cha Edward Bouverie Pusey, kiitwacho *The Doctrine of the Real Presence* (Fundisho la Dini la Kuwapo Kabisa Kwa Mwili wa Kristo) (Oxford, England: John H. Parker, 1855).

Sura ya 4, Aya ya 10. **SABATO MIONGONI MWA WAALDENSIA**.—Kuna waandishi wanaodai kwamba Wawaldensia walikuwa na desturi yao iliyoenea kote ya kuitunza Sabato ya Siku ya Saba [Jumamosi]. Dhana hiyo ilitoka katika vyanzo ambavyo Kilatini cha awali kinaeleza kwamba Wawaldensia walikuwa wakiitunza *dies dominicalis*, au Siku ya Bwana (Jumapili), lakini katika jambo hilo kutokana na desturi inayoanzia wakati ule wa Matengenezo ya Kanisa, neno hili "Jumapili" lilikuwa likitafsiriwa "Sabato."

Lakini ushahidi wa kihistoria upo wa kuwako kwa utunzaji wa aina fulani wa Sabato ya Siku ya Saba [Jumamosi] miongoni mwa Wawaldensia. Taarifa ya Mahakama au baraza la Kanisa Katoliki [Inquisition/Inkwizisheni], ambayo mbele yake waliletwa baadhi ya Wawaldensia wa Moravia, katikati ya karne ya kumi na tano, inatangaza kwamba miongoni mwa Wawaldensia "sio wachache kwa kweli

wanaoadhimisha Sabato [Jumamosi] pamoja na Wayahudi." - Johann Joseph Ignaz von Dollinger, *Beitrage zur Sektengeshichte des Mittelalters* (Taarifa Juu ya Historia ya Vikundi Vya Dini vya Zama za Kati), Munich, 1890, Sehemu ya Pili; uk. 661. Hapana shaka lo lote kwamba chanzo hicho kinadokeza utunzaji huo wa Sabato ya Siku ya Saba [Jumamosi].

Sura ya 4, Aya ya 11. **TAFSIRI ZA BIBLIA KWA WAWALDENSIA**.—Kuhusiana na ugunduzi wa hivi karibuni wa maandiko ya mkono Kiwaldensia (miswada), angalia makala ya M. Esposito, "Sur quelques manuscrits de l'anchienne litterature des Vaudois du Piedmont," (Juu ya maandiko mbalimbali ya mkono ya zamani ya Waaldensia wa Pyemo, katika kitabu cha *Revue d'Historique Ecclesiastique* (Marejeo ya Historia ya Kanisa) (Louvain, 1951), uk. 130 ff., Makala ya F. Jostes, iitwayo "Die Waldenserbibeln" (Biblia ya Kiwaaldensia), katika kitabu cha *Historisches Jahrbuch* (Kitabu cha Historia Chenye Taarifa za Mwaka), 1894; kitabu cha D. Lortsch cha *Histoire de la Bible en France* (Historia ya Biblia katika Ufaransa), (Paris, 1910), sura ya 10.

Kitabu kilichokubaliwa na wasomi kuwa ni bora sana ambacho kiliandikwa na mmojawapo wa Wawaldensia wageni (barbs) ni kile cha Jean Leger, kiitwacho *Histoire Generale des Eglises Evengeliques des Vallees de Piedmont* (Historia ya Kawaida ya Makanisa ya Kiinjili katika Mabonde ya Pyemo) (Leyden, 1669), ambacho kiliandikwa katika kipindi cha mateso makali, nacho kina taarifa pamoja na michoro toka kwa mtu aliyekuwapo wakati mambo yale yanatokea-mbashara.

Kwa maandishi haya yenye maneno halisi ya Kiwaaldensia, angalia kitabu cha A. DeStefano, cha Civilta Medioevale (1944); na *Riformatori ed eretici nel medioeve* (Palermo, 1938); kitabu cha J. D. Bounous, cha *The Waldensian Patois of Pramol* (Nashville, 1936); na kitabu cha A. Dondaine cha *Archivum Fratrum Praedicatorum* (1946).

Kwa ajili ya historia ya Wawaldensia, baadhi ya kazi za vitabu vya hivi karibuni zaidi vinavyoaminika ni hivi: E. Comba, *History of the Waldenses in Italy* (Historia ya Waldensia katika Italia) (angalia toleo la baadaye la Kiitaliano lililochapishwa kule Torre Pellice, 1934); E. Gebhart, *Mystics and Heretics* (Vikundi Vyenye Dini za Siri na Wazushi) (Boston, 1927); G. Gonnet, *Il Valdismo Medioevale, Prolegomeni* (Torre Pellice, 1935); na Jalla, *Histoire des Vaudois et leurs colonies* (Historia ya Wavodwa [Waldensia] na makazi yao) (Torre Pellice, 1935).

Sura ya 4, Aya ya 43. **HUKUMU DHIDI YA WAWALDENSIA**.—Sehemu kubwa sana ya maandishi halisi ya amri ya kipapa iliyotolewa na Inoccent wa Nane katika mwaka ule wa 1487 dhidi ya Wawaldensia (Nakala yake Asilia ambayo imo katika maktaba ya Chuo Kikuu cha Cambridge imetolewa katika tafsiri ya

Kiingereza katika kitabu cha John Dowling cha History of Romanism (Historia ya Uroma) (toleo la mwaka 1871), kitabu cha 6, sura ya 5, sehemu ya 62.

Sura ya 5, Aya ya 12. **WYCLIFFE.**—Mwandishi wa historia anagundua kwamba jina hilo la Wycliffe linaandikwa kwa namna mbalimbali za kuliandika. kwa ajili ya mjadala kamili, angalia kitabu cha J. Dahmus, kiitwacho *The Prosecution of John Wycliffe* (Kushtakiwa kwa John Wyclif) (New Haven: Yale University Press, 1952), uk. 7. [GC 685.6] Uk. 85, Amri za Papa (bulla/fahali)

Sura ya 5, Aya ya 19. **KUTOWEZA KUKOSEA KAMWE** (Infallibility).—Kwa maandiko asilia ya amri za mapapa zilizotolewa dhidi ya Wycliffe pamoja na tafsiri yake ya Kiingereza, angalia kitabu cha J. Dahmus cha *The Prosecution of John Wyclyf* (Kushtakiwa kwa John Wyclif) (New Haven: Yale University Press, 1952) kurasa za 35-49; pia kitabu cha John Foxe cha *Acts and Monuments of the Church* (Sheria na Kumbukumbu za Kanisa) (London: Pratt Townsend, 1870), juzuu ya 3, kurasa za 4-13.

Kwa muhtasari wa amri hizo za papa zilizotumwa kwa Askofu Mkuu wa Canterbury, kwa Mfalme Edward, na kwa Mkuu wa Chuo Kikuu cha Oxford, angalia kitabu cha Merle d'Aubigne, kiitwacho *The History of the Reformation in the Sixteenth Century* (Historia ya Matengenezo ya Kanisa katika Karne ya Kumi na Sita) (London: Blackie and Son, 1885), juzuu ya 4, sehemu ya 7, uk. 93; kitabu cha August Neander cha *General History of the Christian Church* (Historia ya Kawaida ya Kanisa la Kikristo) (Boston: Crocker nad Brester, 1862), juzuu ya 5, kurasa za 146, 147; kitabu cha George Sargeant, kiitwacho *History of the Christian Church* (Historia ya Kanisa la Kikristo) (Dallas: Frederick Publishing House, 1948), uk. 323; kitabu cha Gotthard V. Lechler, kiitwacho John Wycliffe and His English Precursors (London: The Religious Tract Society, 1878), kurasa za 162- 164; kitabu cha Philip Schaff cha *History of the Christian Church* (Historia ya Kanisa la Kikristo) (New York: Charles Scribner's Sons, 1915), juzuu ya 5, sehemu ya 2, uk. 317.

Sura ya 6, Aya ya 19. **BARAZA LA KONSTANSI** (Council Of Constance).—Chanzo kikuu cha habari za Baraza la Konstansi ni kitabu cha Richendal Ulrich kiitwacho *Das Concilium so zu Constanz gehalten ist worden* (Baraza Lililofanywa pale Konstansi) (Augsburg, 1483, Incun.). Utafiti wa kuvutia sana wa hivi karibuni wa maandiko hayo, ambayo yamejengwa juu ya msingi wa "Aulendorf Codex," umo katika mkusanyo wa Spencer katika Maktaba ya Umma ya New York, ulichapishwa na Karl Kup, *Ulrich von Richental's Chronicle of the Council of Constance* (New York, 1936). Tazama pia toleo la H. Finke, linaloitwa *Acta Concilii Constanciensis* (1896), juzuu ya 1; Hefele, *Conciliengeshichte* (Habari za Baraza - juzuu 9), juzuu ya 6, 7; L. Mirbt, *Quellen zur Geschichte des Papstuums* (1934); Milman, *Latin Christianity* (Ukristo wa

Kilatini), juzuu ya 7, kurasa za 426-524; Pastor, *The History of the Popes* (Historia ya Mapapa) (juzuu 34), juzuu ya 1, uk. 197 ff.

Vitabu vilivyochapishwa karibuni zaidi juu ya Baraza hilo ni K. Zahringer, *Das Kardinal Kollegium auf dem Konstanzer Konzil* (Munster, 1935); Th. F. Grogau, *The conciliar Theory as it Manifested Itself at the Council of Constance* (Nadharia ya Baraza kama Ilivyojidhihirisha katika Baraza la Konstansi) (Washington, 1949); Fred A. Kremple, *Cultural Aspects of the Council of Constance and Basel* (Vipengele vya Utamaduni vya Baraza la Konstansi na Bazeli) (Ann Arbor, 1955); John Patrick McGowan, *d'Ailly and the Council of Constance* (Washington: Catholic University, 1936).

Kwa habari za John Huss, angalia John Hus, *Letters*, 1904; E. J. Kitts, *Pope John XXIII and Master John Hus* (Papa Yohane wa 23 na bwana John Hus) (London, 1910); D. S. Schaff, John Hus (1915); Schwarze, John Hus (1915); na Matthew Spinka, *John Hus and the Czech Reform* (1941).

Sura ya 12, Aya ya 66. **UJESUTI** (Jesuitism).—Kwa maelezo kuhusu chanzo, kanuni, na makusudi ya "Chama cha Yesu" (Society of Jesus au Jesuits), kama ilivyoelezwa kwa muhtasari na wanachama wa jumuiya au Chama hiki, angalia kazi [kitabu] yenye kichwa hiki *Concerning Jesuits* (Habari Kuhusu Majesuti), ambayo imehaririwa na Mchg. John Gerard, S. J., na kuchapishwa kule London, 1902 na Catholic Truth Society. Katika kazi hiyo inasemekana kwamba, msukumo hasa wa shirika zima la Chama hicho ni roho ya kuwa na utii kamili: 'Hebu kila mmoja,' anaandika Mt. Ignatio (St. Ignatius), 'na ajishawishi mwenyewe ya kwamba wale wanaoishi chini ya utii wanapaswa kujiruhusu wenyewe kusukumwa na kuongozwa na maongozi ya Kimungu kupitia kwa wakuu wao, kana kwamba wao ni maiti au mwili uliokufa, unaojiachia mwenyewe kuchukuliwa na kupelekwa kokote na kutendewa kwa njia iwayo yote ile, au kama fimbo ya mzee inayomsaidia yule anayeshika mkononi mwake kwa njia yoyote ile atakayo yeye.'

"Kujisalimisha kikamilifu huko kunawezeshwa na nia yake kulingana na madhumuni yake, nako kunapakutelekezwa mara moja,' anaendelea kusema mwasisi wake ... 'kwa furaha na ustahimilivu;... aliye mtii kidini anatekeleza kwa furaha kile ambacho wakuu wake walichomwamini kukifanya kwa faragha kwa faida ya wote, akifanya hivyo akiwa hapo, basi yeye ana hakika kwamba anapatana kwa kikamilifu na Mapenzi ya Mungu." - the Comtesse R. de Courson, katika kitabu cha *Concerning Jesuits*, ukurasa wa 6.

Angalia pia kitabu cha L. E. Dupin, *A Compendious History of the Church* (Ufupisho Kamili wa Historia ya Kanisa), karne ya 16, sura ya 33 (London, 1713, juzuu ya 4, kurasa za 132-135); Mosheim, *Ecclesiastical History* (Historia ya Kanisa), karne ya 16, kifungu cha 3, sehemu ya 1, sura ya 1, aya ya 10 (pamoja na maelezo yake); *The*

*Encyclopedia Britannica* (Ensaiklopidia Britanika), (toleo la 9), Makala: “Majesuti;” C. Paroissen, *The Principles of Jesuits, Developed in a Collection of Extracts From Their Own Authors* (Kanuni za Majesuti, zimefafanuliwa kutokana na Mkusanyo wa Madondoo kutoka kwa Waandishi wao wenyewe) (London, 1860, toleo la mapema zaidi lilitokea mwaka 1839); W. C. Cartwright, *The Jesuits, Their Constitution and Teaching* (Majesuti, Muundo na Mafundisho Yao) (London, 1876); E. L. Taunton, *The History of the Jesuits in England* (Historia ya Majesuti Uingereza), (London, 1901).

Angalia pia kitabu cha H. Boehmer, *The Jesuits* (Majesuti) (tafsiri kutoka katika lugha ya Kijerumani, Philadelphia, Castle Press, 1928); E. Goethein, *Ignatius Loyola and the Gegen-reformation* (Ignatio Loyola na Upingaji wa Matengenezo ya Kanisa) (Halle, 1895); T. Campbell, *The Jesuits* (Majesuti), 1534-1921 (New York, 1922)

Sura ya 12, Aya ya 68. **BARAZA LA UCHUNGUZI AU MAHAKAMA YA KANISA** (Inquisition).—Kwa mtazamo wa Kikatoliki, angalia *The Catholic Encyclopedia* (Ensaiklopidia ya Kikatoliki), juzuu ya 8, makala: “Inquisition” au “Mahakama ya Kanisa Katoliki,” iliyoandikwa na Joseph Blotzer, ukurasa 22 ff.; na E. Vacandard, *The Inquisition: A Critical and Historical Study of the Coercive Power of the Church* (Inquisition: Utafiti Uliohakikiwa wa Kihistoria wa Uwezo wa Kanisa wa Kutumia mamlaka yake) (New York: Longmans, Green and Company, 1908).]

Kwa mtazamo wa Wakatoliki wa Kianglikana, angalia kitabu cha Hoffman Nickerson, *The Inquisition: A Political and Military Study of its Establishment* (Inquisition: Utafiti wa Kisiasa na Kijeshi wa Kuanzishwa Kwake). Kwa mtazamo usio wa Kikatoliki, angalia kitabu cha Philip Van Limborch, History of the Inquisition Henry Charles Lea, *A History of the Inquisition of the Middle Ages* (Historia ya Inkwizisheni ya Zama za Kati), juzuu 3; *A History of the Inquisition in Spain* (Historia ya Inkwizisheni kule Hispania), juzuu ya 4, na *The Inquisition in the Spanish Dependencies* (Inquisition katika Makoloni ya Wahispania); na H. S. Tuberville, *Medieval Heresy and the Inquisition* (Uzushi wa Zama za Kati na Inquisition) (London: C. Lockwood and Son, 1920 - mtazamo wa usuluhishi).

Sura ya 15, Aya ya 2. **SABABU ZILIZOLETA MAPINDUZI YA UFARANSA**.—Kuhusu matokeo yenye athari nyingi ya kuikataa Biblia na Dini ya Biblia yaliyowapata watu wa Ufaransa, angalia kitabu cha H. von Sybel, *History of the French Revolution* (Historia ya Mapinduzi ya Ufaransa), kitabu cha 5, sura ya 1, aya ya 3-7; Henry Thomas Buckle, *History of Civilization in England* (Historia ya Ustaarabu Uingereza), sura ya 8, 12, 14 (New York, 1895, juzuu ya 1, kurasa za 364-366, 369-371, 437, 540, 541, 550); Blackwood’s Magazine (Jarida/Gazeti la Blackwood), juzuu 34, Na. 215 (Novemba, 1833), uk. 739; J. G. Lorimer, *An Historical Sketch of the Protestant Church in France* (Muhtasari wa Historia ya Kanisa la Kiprotestanti katika nchi ya Ufaransa), sura ya 8, aya ya 6, 7.

Sura ya 15, Aya ya 8. **JUHUDI ZA KUIKANDAMIZA [KUIFICHA] NA KUIANGAMIZA BIBLIA.**—Baraza la Tulusi (Council of Toulouse) lililokutana karibu na wakati wa vita vya msalaba au vita takatifu (crusade) dhidi ya Waalbigensia (Albigenses), liliamuru hivi: "Tunapiga marufuku walei [waumini wa kawaida] kumiliki nakala za Agano la Kale na Agano Jipya..... Tunawakataza kwa nguvu na ukali wote wasiwe na vitabu hivyo vilivyotajwa hapo juu katika lugha yao mashuhuri na inayopendwa na wote." "Mabwana (malodi) wa Wilaya kwa makini watawatafuta kwa uangalifu wazushi katika makazi yao, mashimo, na misituni, na hata katika maficho yao chini ya ardhi yataharibiwa kabisa." - *Council of Tolosanum, Pope Gregory IX, Anno. Chr.* 1229. Kanuni ya Kanisa ya 14 na ya 2. Baraza hilo lilikaa wakati wa vita vitakatifu vya msalaba dhidi ya Waalbigensia.

"Mdudu huyo mharibifu sana [Biblia] alikuwa amejitandaza na kujiimarisha kiasi kwamba watu wengine walikuwa wamejichagulia makasisi wao wenyewe, na hata baadhi ya wainjilisti ambao waliipotosha na kuiharibu Kweli ya injili na kujitengenezea injili mpya kwa ajili ya makusudi yao wenyewe.... (wao wanajua kwamba) kuhubiri na kuifafanua Biblia kumekatazwa kabisa kwa waumini walei wa kanisa." - *Acts of Inquisition* (Sheria za Inquisition), Philip Van Limborch, *History of the Inquisition* (Historia ya Inquisition), sura ya 8.

Baraza la Tarragona, 1234 lilipitisha kwamba: "Hakuna mtu ye yote awezaye kumiliki Agano la Kale na Agano Jipya katika lugha ya Kirumi (Kitaliano, Kireno, Kihispania), na endapo mtu ye yote anayo, basi, ni lazima amkabidhi askofu wa eneo lake katika muda wa siku nane baada ya kutangazwa kwa amri hii, ili yapate kuchomwa moto na kama yeye ni mchungaji au kasisi au mlei, ili asije akashukiwa hivyo, isipokuwa asafishwe kwa kuondolewa shuku yote kwake." - D. Lortsch, *Histoire de la Bible en France* (Historia ya Biblia katika Nchi ya Ufaransa), 1910, uk. 14.

Katika Baraza la Constance, mwaka wa 1415, Wyclif, alihukumiwa hata baada ya kufa kwake, na Arundel, askofu mkuu wa Canterbury, kuwa ni "mtu msumbufu na mfidhuli, mwenye ugonjwa mbaya sana wa uzushi, aliyegundua tafsiri mpya ya Maandiko katika lugha yake aliyozaliwa nayo."

Upinzani dhidi ya Biblia uliofanywa na Kanisa Katoliki la Roma umeendelea katika karne nyingi, nao ulizidishwa sana wakati ule wa kuanzishwa kwa Vyama Vya Biblia. Tarehe 8 Desemba, 1866, Papa Piusi wa Tisa, katika waraka wake wa utume *Quanta Cura*, alitoa muhtasari wa makosa nane tofauti. Chini ya kichwa cha habari IV tunaikuta orodha hii: "Ujamaa, Ukomunisti, Vyama vya Siri, Vyama vya Biblia.... Wadudu waharibifu kama hawa ni lazima waangamizwe kwa kila njia iwezekanayo." [GC 688.3]

Sura ya 15, Aya ya 34. **UTAWALA WA VITISHO** (Reign Of Terror).—Kwa utangulizi mfupi wa kuaminika wa Historia ya Mapinduzi ya Ufaransa, angalia kitabu cha L. Gershoy cha *The French Revolution* (Mapinduzi ya Ufaransa) (1932); G. Lefebvre, *The Coming of the French Revolution* (Kuja kwa Mapinduzi ya Ufaransa) (Princeton, 1947); na H. von Sybel, *History of the French Revolution* (Historia ya Mapinduzi ya Ufaransa) (1869), juzuu 4.

Gazeti la Moniteur Officiel lilikuwa ndilo gazeti la serikali wakati wa Mapinduzi yale, nalo ni chanzo cha msingi kilichojaa taarifa ya mambo ya kweli kuhusu hatua zilizochukuliwa na Mabunge, maandishi kamili ya hati, n.k. Limechapishwa tena. Tazama pia kitabu cha A. Aulard cha Christianity and the French Revolution (Ukristo na Mapinduzi ya Ufaransa) (London, 1927), ambamo taarifa za maandishi zinaendelezwa hadi kupita mwaka 1802 ni uchunguzi wa kuvutia; W. H. Jervis, *The Gallican Church and the Revolution* (Kanisa la Kifaransa na Mapinduzi) (London, 1882), ni kazi makini [kitabu] iliyoandikwa na Mwanglikana, lakini kinatoa upendeleo kwa Ukatoliki.

Kuhusu uhusiano wa kanisa na serikali katika nchi ya Ufaransa katika kipindi kile cha Mapinduzi, angalia kitabu cha Henry H. Walsh, *The Concordate of 1801: A Study of Nationalism in Relation to Church and State* (Mapatano ya mwaka 1801: Uchunguzi wa Uzalendo kuhusu uhusiano kati ya Kanisa na Serikali) (New York, 1933); Charles Ledre, *L'Eglise de France souls la Revolution* (Kanisa la Ufaransa dhidi ya Mapinduzi) (Paris, 1949).

Baadhi ya utafiti uliofanywa katika kipindi kile kile kuhusu umuhimu wa kidini wa Mapinduzi ni pamoja na ule wa G. Chais de Sourcesol, *Le Livre des Manifestes* (Kitabu cha Manifesto au Sera) (Avignon, 1800), ambacho ndani yake mwandishi alijitahidi kuthibitisha sababu za mgorogoro, na umuhimu wake wa kidini, n.k.; James Bicheno, *The Signs of the Times* (Dalili za Nyakati) (London, 1794); James Winthrop, *A Systematic Arrangement of Several Scripture Prophecies Relating to Antichrist; With Their Application to the Course of History* (Mpangilio unaofuatana kwa Utaratibu wa Unabii kadhaa wa Maandiko Kumhusu Mpinga Kristo; Pamoja na Matumizi yake katika Mkondo wa Historia) (Boston, 1795); na Lathrop, *The Prophecy of Daniel Relating to the Time of the End* (Unabii wa Danieli Kuhusiana na Wakati wa Mwisho) (Springfield, Massachusetts, 1811).

Kwa ajili ya Kanisa wakati ule wa Mapinduzi, angalia kitabu cha W. M. Sloan, *The French Revolution and Religious Reform* (Mapinduzi ya Ufaransa na Matengenezo ya Kidini) (1901); P. F. La Gorce, *Histoire Religieuse de la Revolution* (Historia ya Kidini Wakati wa Mapinduzi) (Paris, 1909).

Kuhusu mahusiano na upapa, angalia kitabu cha G. Bourgin, *La France et Rome de* 1788-1797 (Ufaransa na Roma ya miaka ya 1788-1797) (Paris, 1808), imetokana na mafaili ya siri katika Vatikani; A. Latreille, *L'Eglise Catholique et la Revolution* (Kanisa Katoliki na Mapinduzi) (Paris, 1950), habari ya kuvutia hasa ni juu ya Papa Pius VI na mgogoro wa Kidini, 1775-1799.

Kuhusu Waprotestanti wakati ule wa Mapinduzi, angalia (toleo la) Pressense, *The Reign of Terror* (Utawala wa Vitisho) (Cincinnati, 1869).

Sura ya 15, Aya ya 42. **WANANCHI WALIO WENGI NA MATABAKA YA WATU WANAOPENDELEWA KWA FURSA**.—Kuhusu hali ya maisha ya jamii zilizokuwako katika nchi ya Ufaransa kabla ya kipindi kile cha Mapinduzi, angalia kitabu cha H. Von Holst, *Lowell Lectures on the French Revolution* (Hotuba za Lowell juu ya Mapinduzi ya Ufaransa), Hotuba ya 1; pia angalia kitabu cha Taine, *Ancien Regime* (Serikali ya Zamani), na cha A. Young, *Travels in France* (Safari katika Nchi ya Ufaransa).

Sura ya 15, Aya ya 50. **ULIPIZAJI WA KISASI**.—kwa ajili ya maelezo ya kinagaubaga kuhusu tabia ya kulipiza kisasi ya Mapinduzi ya Ufaransa, angalia kitabu cha Thos. H. Gill, *The Papal Drama* (Vioja Vya Upapa), kitabu cha 10, na kitabu cha Edmond De Pressense, *The Church and the French Revolution* (Kanisa na Mapinduzi ya Ufaransa), kitabu cha 3, sura ya 1.

Sura ya 15, Aya ya 51. **UKATILI MBAYA MNO WA UTAWALA WA VITISHO**.—Angalia kitabu cha M. A. Thiers, *History of the French Revolution* (Historia ya Mapinduzi ya Ufaransa), juzuu ya 3, kurasa za 42-44,62- 74,106, (New York, 1890, imetafsiriwa na F. Shorberl); kitabu cha F. A. Mignet, *History of the French Revolution* (Historia ya Mapinduzi ya Ufaransa), sura ya 9, aya ya 1 (Bohn, 1894); kitabu cha A. Alison, *History of Europe* (Historia ya Ulaya), 1789-1815, juzuu ya 1, sura ya 14 (New York, 1872, juzuu ya 1, kurasa za 293- 312).

Sura ya 15, Aya ya 59. **UENEZAJI WA MAANDIKO**.—Katika mwaka 1804, kwa mujibu wa Bwana William Canton wa Chama cha Biblia cha Uingereza na Nchi za Kigeni (British and Foreign Bible Society), anasema, "Biblia zote zilizopo sasa ulimwenguni, katika muswada au zilizochapishwa, ukihesabu kila tafsiri katika kila nchi, hazikuwa zaidi ya milioni nne.... lugha mbalimbali ambazo zilitumika kwa hizi Biblia milioni hizo nne, ikiwa pamoja na lugha za zamani za Moeso-Gothic za Ulfilas na Kianglo-Saksoni cha Bede, zimeandikwa katika kumbukumbu kuwa zinafikia takribani lugha hamsini." - *What is the Bible Society?* (Chama cha Biblia Ni Nini?), toleo lililofanyiwa masahihisho, 1904, 23.

Chama cha Biblia cha Amerika kilitoa taarifa ya Biblia zilizotawanywa 481, 149, 365 kwa kipindi kinachoanzia 1816 hadi 1955, ukijumuisha Agano la kale na sehemu za Agano Jipya katika ulimwengu wote. Kwa idadi hii waweza kuongeza

zaidi ya Biblia au sehemu za Maandiko zaidi ya 600,000,000 zilizotawanywa na Chama cha biblia cha Uingereza. Maandiko, kamili au kwa sehemu sehemu, yamechapishwa katika lugha 1,092 kufikia mwaka wa 1955 pekee chama cha Biblia cha Amerika kilisambaza jumla ya Biblia, Agano la Kale na Agano Jipya, na sehemu za Agano la Kale na Agano Jipya 23, 819, 733 ulimwenguni kote.

Sura ya 15, Aya ya 60. **MISHENI KATIKA NCHI ZA NG'AMBO**.—Kazi za Umishenari za Kanisa la awali la Kikristo hazijarudiwa tena mpaka katika siku za sasa. Zilikuwa zimekufa kabisa kufikia mwaka wa 1000BK, tena zilifuatiwa na mapambano ya kijeshi katika Vita zile za msalaba au zilitwa vita takatifu (Crusades). Kipindi kile cha Matengenezo ya kanisa kiliona kazi ndogo mno za kimishenari katika nchi za kigeni, isipokuwa kwa upande wa Majesuti wa awali. Uamsho wa utauwa zalisha wamishenari wachache tu. Kazi ya Kanisa la Moraviani katika karne ya kumi na nane ilikuwa ni ya kusifika, na palikuwa na vyama fulani vichache vya Kimishonari vilivyoundwa na Waingereza kufanya kazi katika makoloni yao kule Amerika Kaskazini. Lakini kufufuka tena kukubwa kwa shughuli za kimishonari kunaanzia mnamo mwaka wa 1800BK, "wakati wa mwisho." Danieli 12:4. Katika mwaka wa 1792 kiliundwa Chama cha Kamishenari cha Kibaptisti, ambacho kilimtuma Carey kwenda India. Katika mwaka wa 1795 Chama cha Kimishonari cha London kilianzishwa, na chama kingine katika mwaka wa 1799 ambacho katika mwaka wa 1812 kilibadilisha jina na kuwa Chama cha Wamishenari cha Kanisa (CMS). Muda mfupi baadaye Chama cha Kimishonari cha Wesley kiliundwa. Nchini Marekani Bodi ya Makamishna wa Amerika wa Misheni katika Nchi za ng'ambo au kigeni kwenye nchi hizi, iliundwa mwaka ule wa 1812, na Adoniram Judson alitumwa katika mwaka ule kwenda Calcutta. Alijijenga kule Burma mwaka uliofuata. Katika mwaka wa 1814 Umoja wa Misheni wa Kibaptisti wa Amerika uliundwa. Bodi ya Presibyterian ya Misheni katika Nchi za Mbali iliundwa mwaka 1837.

"Katika mwaka wa 1800 B.K.,... idadi kubwa mno ya Wakristo ilikuwa ya watoto au vitukuu vya wale waliokuwa wameongolewa kabla ya mwaka wa 1500 B.K..... Sasa, katika karne ya kumi na tisa kulitokea uongezekaji wa Ukristo na kusambaa tena. Hakuna mabara mengi au nchi kubwa ambazo zilikuwa zimepenywa kwa mara ya kwanza katika karne tatu zile zilizotangulia. Jambo hilo lingekuwa haliwezekani, kwa sababu katika nchi zile kubwa zaidi za dunia, ukiacha Australia na miongoni mwa maeneo yote yenye ustaarabu wa Kikristo wa hali ya juu, Ukristo ulikuwa umekwisha kuingizwa kabla ya mwaka wa 1800. Kilichotokea sasa ilikuwa ni kule kujipatia maeneo mapya ya kuotesha mizizi, na miongoni mwa watu waliokuwa tayari wamefikiwa, upanuzi wenye eneo kubwa lisilowahi kutokea kutoka katika maeneo mapya na yale ya zamani zaidi, na kuingia kwa Ukristo kwa watu wengi katika nchi kubwa kama hizo, na visiwa,

pamoja na mataifa na makabila yaliyokuwa hayajapata kuguswa kabla ya hapo....

"Uenezaji wa Ukristo katika karne ya kumi na tisa, kimsingi kuliwezeshwa kutokana na mbubujiko mpya wa maisha ya kidini utokanao na msukumo wa Kikristo.... Kamwe haujapata kuwako wakati wowote unaolingana na huo, ambao msukumo huo wa Kikristo ulipata kuanzisha harakati [makundi] nyingi mno. Ukristo ulikuwa haujapata kamwe kuleta mabadiliko makubwa mno juu ya watu wa Ulaya Magharibi kama kipindi hicho. Ilikuwa ni kutokana na nguvu hiyo kubwa viliweza kuibuka Vyama vya Kimishonari ambavyo katika karne ile ya kumi na tisa vilisaidia kwa nguvu kuongeza wingi wa watu waliomwamini Bwana pamoja na mvuto wa Ukristo." Kenneth Scott Latourette, *A History of the Expansion of Christianity* (Historia ya Kuenea kwa Ukristo), juzuu ya IV, *The Great Century* A..D. 1800-A..D.1914 (Karne Kuu 1800 B.K. – 1914 B.K.) (New York: Harper & Brothers, 1941), kurasa 2-4.

Sura ya 18, Aya ya 25. **TAREHE ZA UNABII**.—Kulingana na hesabu za Kiyahudi, mwezi ule wa tano (Ab) wa mwaka wa saba wa utawala wa Artashasta ulianzia Julai 23 hadi Agosti 21, 457 K.K. Baada ya kufika kwake Ezra kule Yerusalemu katika majira ya kupukutisha (autumn) ya mwaka ule, amri ya mfalme huyo ilianza kutekelezwa. Kwa uhakika wa mwaka huo wa 457 K.K. kwamba ulikuwa ni mwaka wa saba wa Artashasta, angalia kitabu cha S. H. Horn and L. H. Wood, *The Chronology of Ezra* [691] 7 (Taratibu za Miaka ya Ezra 7) (Washington, D.C.: Review and Herald Publishing Assn., 1953); kitabu cha E. G. Kraeling, *The Brooklyn Museum Aramaic Papyri* (Jumba la Makumbusho la Bruklini la juzuu ya Kiaramu) (New Haven or London, 1953), kurasa 191-193; kitabu cha The Seventh-day Adventist Bible Commentary (Kitabu cha Ufafanuzi wa Biblia cha Waadventista Wasabato) (Washington, D.C.: Review and Herald Publishing Assn., 1954), juzuu ya 3, kurasa za 97-110.

Sura ya 18, Aya ya 30. **KUANGUKA KWA DOLA YA UTURUKI** (Ottoman Empire).—Athari za Uturuki ya Kiislamu dhidi ya Ulaya baada ya kuanguka kwa Konstantinopo (Constantinople) mwaka ule wa 1453 zilikuwa kali sana kama ulivyokuwa ushindi wa Waarabu wale Waislamu (Saracens) ulioleta maafa mengi dhidi ya Dola ya Mashariki ya Waroma katika kipindi cha karne moja na nusu baada ya kifo cha Muhammad. Katika kipindi chote cha Matengenezo ya Kanisa, Uturuki ilikuwa tishio la kudumu katika milango ya mashariki ya Ulimwengu wa Kikristo wa Ulaya; maandiko ya Wanamatengenezo wa Kanisa yamejaa shutuma nyingi dhidi ya mamlaka ile ya Kituruki. Tangu wakati ule waandishi wa Kikristo wamejihusisha na sehemu inayoihusu Uturuki katika matukio ya siku zijazo ya ulimwengu huu, na wafafanuzi wa unabii wameiona mamlaka hiyo ya Uturuki na kudhoofika kwake ya kuwa imetabiriwa katika Maandiko.

Kwa sura inayofuata, chini ya unabii ule wa "saa, siku, mwezi, mwaka" kama sehemu ya ile baragumu ya sita, Josiah Litch alifanya mahesabu yake na kuutumia unabii huo wa wakati, kuonyesha kwamba uhuru wa Uturuki ungekoma katika mwezi ule wa Agosti, 1840. Mtazamo wa Litch unaweza kuonekana kwa kirefu katika makala yake yenye kichwa cha *The Probability of the Second Coming of Christ About A.D. 1843* (Uwezekano wa Kuja Kwa Kristo Mara ya Pili Mnamo mwaka wa 1843 B.K.) (iliyochapishwa mwezi Juni, 1838); *An Address to the Clergy* (Hotuba kwa Wachungaji na Maaskofu) iliyochapishwa katika majira yale ya kuchipua (Spring) ya mwaka wa 1840; toleo la pili, pamoja na kumbukumbu za kuunga mkono usahihi wa ma hesabu yaliyofanywa kwanza kuhusu kipindi cha unabii ule kilichofikia kwenye anguko la Dola ya Uturuki, lilichapishwa mwaka 1841; na makala yake iliyo katika gazeti la Signs of the Times and Expositor of Prophecy [Dalili za Nyakati na Mfafanuzi wa Unabii], la Agosti 1, 1840. Angalia pia makala yake katika gazeti la Signs of the Times and Expositor of Prophecy [Dalili za Nyakati na Mfafanuzi wa Unabii], la Feb. 1, 1841; na kitabu cha J. N. Loughborough cha *The Great Advent Movement* (Kundi Kuu la Waadventista) (toleo la 1905), ukurasa wa 129-132. Kitabu cha Uriah Smith cha *Thoughts on Daniel and the Revelation* (Tafakuri juu ya Danieli na Ufunuo) (toleo lililofanyiwa masahihisho la mwaka 1944, huongelea juu ya mpangilio wa wakati wa unabii huo katika kurasa zake za 506-517.

Kwa historia ya mapema ya Dola ya Uturuki, na kudhoofika kwa Mamlaka hiyo ya Uturuki, angalia pia kitabu cha William Miller, *The Ottoman Empire and Its Successors* (Dola ya Uturuki na Watawala Waliofuata), 1801- 1927 (Cambridge, England: University Press, 1936); kitabu cha George G. S. Eversley, *The Turkish Empire From 1288 to 1914* (Dola ya Kituruki Kuanzia Mwaka 1288 hadi 1914) (London: T. Fisher Unwin, Ltd., toleo la pili, 1923); kitabu cha Joseph von Hammer-Purgstall, *Geschichte des Osmannischen Reiches* (Historia ya Dola ya Uturuki) (Pesth: C. A. Hartleben, toleo la 2, 1834-36), juzuu 4; kitabu cha Herbert A. Gibbons, *Foundation of the Ottoman Empire* (Kuanzishwa Kwa Dola ya Uturuki), 1300-1403 (Oxford: University Press, 1916); kitabu cha Arnold J. Toynbee and Kenneth B. Kirkwood, Turkey (Uturuki) (London, 1926).

Sura ya 18, Aya ya 63. **KUIZUIA BIBLIA KWA WATU**.—Msomaji atatambua kwamba maneno ya juzuu hii yaliandikwa kabla ya Mtaguso wa Pili wa Vatikani, ambao kwa namna fulani sera zake zimebadilishwa kuhusu usomaji wa Biblia.

Kwa karne nyingi, mtazamo wa Kanisa Katoliki la Roma kuhusu Uenezwaji wa Maandiko Matakatifu katika matoleo ya lugha za makabila tofauti ya waumini inaonyesha kuwa mbaya. Tazama kwa mfano G. P. Fisher, *The Reformation*, Ch. 15, kifungu. 16 (1873 ed., ukurasa wa 530-532); J. Kardinali Gibbons, *Faith of Our*

*Fathers* (Imani ya Baba Zetu), sura ya. 8 (toleo la 49, 1897), ukurasa wa 98-117; John Dowling, Historia ya Urumi, b. 7, sura. 2, sek. 14; na b. 9, sura. 3, sekunde. 24-27 (1871 ed., ukurasa wa 491-496, 621-625); L. F. Bungener, *Historia ya Baraza la Trent*, ukurasa wa 101-110 (2d Edinburgh ed., 1853, iliyotafsiriwa na D. D. Scott); G. H. Putnam, *Vitabu na Waandishi Wao Wakati wa Enzi za Kati*, juz. 1, sehemu. 2, sura. 2, kifungu. 49, 54-56. Angalia pia Fahirisi ya Vitabu Vilivyokatazwa (Vatican Polyglot Press, 1930), uk. IX, X; Timothy Hurley, *A Commentary on the Present Index Legistlation* (New York: Benziger Brothers, 1908), uk. 71; *Tafsiri ya The Great Encyclical Letters of Leo XIII* (New York: Benziger Brothers, 1903), p. 413.

Lakini katika miaka ya hivi karibuni mabadiliko makubwa  chanya yametokea katika suala hili. Kwa upande mmoja, kanisa limeidhinisha matoleo ya Biblia kadhaa yaliyotayarishwa kwa msingi wa lugha asilia; kwa upande mwingine, imeendeleza Mafundisho ya Maandiko Matakatifu kwa njia ya usambazaji wa bure na taasisi za Biblia. Kanisa, hata hivyo, linaendelea kujiwekea haki ya pekee ya kuifasiri Biblia kulingana na mapokeo yake, na hivyo kuhalalisha mafundisho yale ambayo hayapatani na Mafundisho ya Biblia.

Sura ya 20, Aya ya 47. **MAVAZI YA KUVAA WAKATI WA KUPAA** (Ascension Robes).—Kisa kile kisemacho kwamba Waadventista walishona mavazi ya kuvaa wakati wa kupaa "ili kumlaki Bwana hewani," kilibuniwa na wale waliotaka kuyashutumu mahubiri ya Waadventista. Kisa hicho kilienezwa kwa bidii nyingi sana kiasi kwamba wengi walikisadiki, lakini uchunguzi wa makini ulithibitisha uongo wa kisa hicho. Kwa miaka mingi zawadi nono ilitolewa kwa yule atakayetoa ushahidi kuonyesha mfano mmoja kama ule uliopata kutokea, lakini hakuna ushahidi wo wote uliotolewa. Hakuna hata mmoja miongoni mwa wale waliopenda kuona kuja kwake Mwokozi, ambao wangekuwa wajinga mno wa mafundisho ya Maandiko kiasi cha kudhani kwamba mavazi ambayo wangeweza kuyashona yangehitajika kwa tukio hilo. Vazi pekee ambalo watakatifu watalihitaji ili kumlaki Bwana ni vazi la haki Yake Kristo. Tazama Isaya 61:10; Ufunuo 19:8.

Kwa ukanushaji kamili wa kisa hicho kisichokuwa cha kweli kuhusu mavazi ya kuvaa wakati wa kupaa, angalia kitabu cha Francis D. Nichol, *Midnight Cry* (Kilio cha Usiku wa Manane) (Washington, D.C.: Review and Herald Publishing Assn., 1944), sura ya 25-27, pamoja na Nyongeza zake H-J. Angalia pia kitabu cha Leroy Edwin Froom, *Prophetic Faith of Our Fathers* (Imani ya Unabii ya Baba Zetu) (Washington, D.C.: Review and Herald Publishing Assn., 1954), juzuu ya 4, kurasa 822-826.

Sura ya 20, Aya ya 48. **MPANGILIO WA MIAKA YA UNABII**.—Dk. George Bush, profesa wa Kiebrania na maandiko ya Mashariki katika Chuo Kikuu cha Mji wa

New York, katika barua aliyomwandikia William Miller, ambayo ilichapishwa katika magazeti ya *Advent Herald (Mbiu ya Marejeo yake Kristo) na Signs of the Times Reporter* (Mtoa Habari wa Dalili za Nyakati), Boston, Machi 6 na 13, 1844, alitoa maelezo yake fulani ya maana kukiri usahihi wa mahesabu yake aliyoyafanya kuhusu kipindi kile cha unabii. Dk. Bush aliandika hivi: "Wala ubishi hauwezi kutolewa kwako, wewe mwenyewe au kwa rafiki zako, kama ninavyoona mimi, kwamba mmetumia wakati mwingi na fikra zenu kujifunza mfuatano wa miaka ya unabii, tena mmejitahidi sana kuweka tarehe za mwanzo na za mwisho za vipindi vyake vikuu. Kama vipindi hivyo vimetolewa hasa na Roho Mtakatifu katika vitabu vya unabii, basi, bila shaka, ilikuwa kwa kusudi kwamba vipate kuchunguzwa, na labda, mwisho wake, vipate kueleweka kikamilifu; wala hakuna mtu ye yote atakayeshtakiwa kuwa na upumbavu wa makusudi ambaye kwa kicho anajitahidi kufanya hivyo.... Kwa kuchukua siku moja kama Neno linalotumika kiunabii kwa mwaka mmoja, mimi naamini mmeungwa mkono kwa uchambuzi wa mafungu ulio wa busara kabisa, tena mmeimarishwa kwa majina yenye sifa ya Mede, Sir Isaac Newton, Askofu Newton, Kirby, Scott, Keith, na jeshi la wengine ambao kwa muda mrefu uliopita wamefikia hitimisho la msingi kama lenu juu ya kichwa hiki. Wote hao wanakubaliana kwamba vipindi vile vikuu vilivyotajwa na Danieli na Yohana, ni kweli vinafikia mwisho wake mnamo kizazi hiki cha ulimwengu na ingekuwa ni mantiki ya ajabu ambayo ingekuhukumu wewe kuwa mzushi kwa kuyashikilia maoni yale yale yanayojitokeza yenyewe kwa wazi mno katika matangazo ya wajuzi hao mashuhuri wa mambo ya Mungu." "Matokeo yako uliyoyapata katika nyanja hii ya uchunguzi hayanishangazi mimi kuwa yako nje ya njia yenyewe kiasi cha kuathiri mambo yoyote ya maana ya ile Kweli au wajibu." "Kosa lako, ninavyofahamu mimi, linaelekea upande mwingine zaidi ya ule wa mpangilio wa miaka. "Umekosea kabisa kwa habari ya aina ya mambo yenyewe yanayopaswa kutokea wakati vipindi vile vitakapokuwa vimekwisha. Hiki ndicho kichwa na uso wa kosa la ufafanuzi wako." Angalia pia kitabu cha Leroy Edwin Froom, *Prophetic Faith of Our Fathers* (Imani ya Kinabii ya Baba Zetu) (Washington, D.C.: Review and Herald Publishing Assn., 1950), juzuu ya 1, sura ya 1, 2.

Sura ya 27, Aya ya 7. **UJUMBE WENYE SEHEMU TATU**.—Ufunuo 14:6, 7 hutabiri kutangazwa kwa ujumbe wa Malaika wa kwanza. Kisha nabii anaendelea kusema: "Malaika mwingine akafuata, akisema, Umeanguka, umeanguka Babeli.... na malaika wa tatu akawafuata." Neno lililotumika hapa lisemalo "akawafuata" lina maana ya "kwenda pamoja nao," "kumfuata mmoja," "kwenda pamoja Naye." Tazama kitabu cha Henry George Liddell and Robert Scott, *Greek English Lexicon* (Msamiati au Kamusi ya Kigiriki-Kiingereza) (Oxford: Clarendon Press, 1940), juzuu ya 1, uk. 52. Pia linamaanisha "kusindikiza/kufuatana na." Angalia kitabu cha George Abbot-Smith, *A Manual of*

*Greek Lexicon of the New Testament* (Kitabu cha Mwongozo wa Msamiati wa Kigiriki cha Agano Jipya) (Edinburgh: T. and T. Clark, 1950), ukurasa 17. Ni neno lile lile lililotumika katika Marko 5:24, "Yesu akaenda pamoja naye; na watu wengi wakamfuata, wakamsonga." Pia inatumika kwa wale waliokombolewa mia moja arobaini na nne elfu, Ufunuo 14:4, ambapo inasemwa, "hawa ndio wale wanaomfuata Mwana-Kondoo kila aendako." Katika sehemu zote hizi mbili ni dhahiri kwamba wazo linalokusudiwa kutolewa ni lile la "kwenda pamoja," "kufuatana na." Kwa hivyo ndani ya 1 Wakorintho 10:4, ambapo tunasoma juu ya wana wa Israeli kwamba "wakaunywea ule Mwamba wa kiroho uliowafuata," neno "walifuata" limetafsiriwa kutoka katika neno lile lile la Kigiriki na ukingo wa kitabu, "uliokwenda pamoja nao." Kutoka katika hili tunajifunza kuwa wazo katika Ufunuo 14:8, 9 si tu kwamba malaika wa pili na yule wa tatu walimfuata yule wa kwanza kwa kufuata wakati, bali kwamba walikwenda pamoja naye. Jumbe hizo tatu ni ujumbe mmoja tu wenye sehemu tatu. Ni jumbe tatu tu kwa utaratibu wa kutokea kwao. Lakini Baada ya kuinuka, jumbe hizo zinaenda sambamba na hazitenganishiki.

Sura ya 27, Aya ya 36. **UKUU KULIKO WATU WOTE KWA MAASKOFU WA ROMA** (Supremacy Of The Bishops Of Rome).—Kwa matukio makuu yaliyosababisha kujinyakulia ukuu kuliko watu wote kwa wale maaskofu [mapapa] wa Roma, angalia kitabu cha Robert Francis Cardinal Bellarmine, *Power of the Popes in Temporal Affairs* (Mamlaka ya Mapapa katika Mambo ya Kidunia) (tafsiri ya Kiingereza iko katika Maktaba ya Bunge la Marekani, Washington, D.C.); kitabu cha Henry Edward Cardinal Manning, *The Temporal Power of the Vicar of Jesus Christ* (Mamlaka ya Kidunia ya Yule Aliye Badala ya Yesu Kristo) (London: Burns and Lambert, toleo la 2, 1862); na kitabu cha James Cardinal Gibbons, *Faith of Our Fathers* (Imani ya Mababa Zetu) (Baltimore: John Murphy Co., toleo la 110, 1917), sura ya 5,9,10,12. Kwa waandishi wa Kiprotestanti, angalia kitabu cha Trevor Gervase Jalland, *The Church and the Papacy* (Kanisa na Upapa) (London: Society for Promoting Christian Knowledge, 1944, a Bampton Lecture, Hotuba ya Bamputon); na kitabu cha Richard Frederick Littledale, *Petrine Claims* (Madai ya Kipetro) (London: Society for Promoting Christian Knowledge, 1899). Kwa vyanzo vinavyotokana na karne zile za mwanzo kuhusu nadharia hiyo ya Kipetro, angalia kitabu cha James T. Shotwell and Louise Ropes Loomis, *The See of Peter* (Jimbo la Petro) (New York: Columbia University Press, 1927). Kwa "Mchango wa Konstantino wa uongo" (Donation of Psudo-Costantine), angalia kitabu cha Christopher B. Coleman, *The Treatise of Lorenzo Valla on the Donation of Constantine* (Makala ya Lorenzo Valla juu ya Mchango wa Konstantino), ambayo imetumia maneno yote ya Kilatini, na uhakiki kamili wa hati hiyo, pamoja na tasinifu yake.

Sura ya 35, Aya ya 9. **NUKUU KUTOKA KWA JOSIAH STRONG**.—Katika toleo lake la kwanza la kitabu cha *Our Country*, Yosia Strong, bila kupata vyanzo vya msingi, alirejelea kimakosa taarifa zilizohusishwa na Papa Pius IX. Rejea sahihi ya nukuu ya kwanza ni barua ya Papa Gregory XVI ya Agosti 15, 1832.

Aya husika imenukuliwa kwa ukamilifu hapa: Uhuru wa Dhamiri “Njia hii ya aibu ya kutojali inatoa upenyo wa pendekezo hilo la kipuuzi na potovu ambalo linadai kwamba uhuru wa dhamiri lazima udumishwe kwa kila mtu. Inaeneza uharibifu katika mambo matakatifu na ya kiraia, ingawa wengine hurudia tena na tena kwa ufidhuli mkubwa kwamba dini hupata faida fulani kutokana nayo. 'Lakini kifo cha nafsi ni kibaya zaidi kuliko uhuru wa makosa,' kama Augustine alivyozoeleka kusema. Vizuizi vyote vinapoondolewa ambavyo kwa hivyo watu wanawekwa kwenye njia nyembamba ya Ukweli, asili yao, ambayo tayari ina mwelekeo wa uovu, inawasukuma kwenye uharibifu. Ndipo kwa kweli ‘shimo lisilo na mwisho’ linafunguliwa ambalo kutoka humo Yohana aliona moshi ukipanda juu ambao ulifunika jua na kutoka humo nzige wakatoka na kuangamiza dunia. Hapo ndipo inakuja mabadiliko ya akili, upotofu wa vijana, kubeza mambo matakatifu na sheria takatifu, kwa maneno mengine, tauni yenye kufisha zaidi katika taifa kuliko sehemu yoyote. Uzoefu unaonesha, hata tangu nyakati za kale, kwamba majiji yaliyojulikana kwa utajiri, utawala, na utukufu yaliangamia kwa sababu ya uovu huo mmoja, yaani, uhuru usio na kiasi wa maoni, uhuru wa kusema na tamaa ya mambo mapya.” Kama ilivyochapishwa katika Claudia Carlen., Ihm, *The Papal Encyclicals*, 1740-1878 (Ann Arbor, Michigan: The Pierian Press, 1990) 1:238.

Nukuu ya pili inapaswa kutajwa kwa Papa Pius IX *Syllabus of Errors*, iliyoambatana na barua yake ya ensiklika ya Desemba 8, 1864. Miongoni mwa makosa 80 yaliyolaaniwa ni pamoja na: “24. Kanisa halina uwezo wa kutumia nguvu, wala halina nguvu za muda, za moja kwa moja au zisizo za moja kwa moja. Barua ya Kitume 'Ad Apostolicae,' Agosti 22, 1851.” “78. Kwa hiyo imeamuliwa kwa hekima na sheria, katika baadhi ya nchi za Kikatoliki, kwamba watu wanaokuja kukaa humo watafurahia utendaji wa hadharani wa ibada yao ya pekee. Allocution 'acerbissimum,' Septemba 27, 1852. “79. Zaidi ya hayo, ni uongo kwamba uhuru wa kiraia wa kila aina ya ibada na uwezo kamili, unaotolewa kwa wote, wa kudhihirisha waziwazi na hadharani maoni yoyote na mawazo yoyote, huchangia kwa urahisi zaidi kuharibu maadili na akili za watu na kueneza hali ya kutojali. Allocution 'Nunquam Fore,' Desemba 15, 1856.”Kama ilivyochapishwa katika Anne *The papal Encyclicals in their Historical Context* (New York: Wana wa GP Putnam, 1956), 146, 152.

Ikumbukwe pia kwamba kiapo cha utii kwa papa, kilichonukuliwa katika aya ya mwisho ya dondoo kutoka kwa Strong, kilikuwa kiapo cha askofu, si kiapo cha

makadinali.

Sura ya 35, Aya ya 10. **KANISA LA ETHIOPIA NA SABATO**.—Hadi miaka ya hivi karibuni Kanisa la Coptic la Ethiopia lilishika Sabato ya siku ya saba. Waethiopia pia waliitunza Jumapili, siku ya kwanza ya juma, katika historia yao yote kama Wakristo. Siku hizi ziliadhimishwa kwa ibada maalumu katika makanisa. Utunzaji wa Sabato ya siku ya saba, hata hivyo, umekoma katika Ethiopia ya kisasa. Kwa masimulizi ya watu waliojionea kwa macho siku hizi za kidini nchini Ethiopia, tazama Pero Gomes de Teixeira, *The Discovery of Abyssinia by the Por- Tugues* mnamo 1520 (imetafsiriwa kwa Kiingereza huko London: British Museum, 1938), uk. 79; Padre Francisco Alvarez, *Narrative of the Portuguese Embassy to Abyssinia During the Years 1520-1527*, zipo katika kumbukumbu za Jumuiya ya Hakluyt (London, 1881), juz. 64, ukurasa wa 22-49; Michael Russell, *Nubia na Abyssinia* (Tukimnukuu Padre Lobo, Mmisionari Mkatoliki nchini Ethiopia mwaka wa 1622) (New York: Harper & Brothers, 1837), uk. 226-229; S. Giacomo Baratti, *The Travels into the Remote Countries of Abyssinia* (London: Benjamin Billingsley, 1670), ukurasa wa 134-137; Job Ludolphus, *A new History for Ethiopia* (London: S. Smith, 1682), ukurasa wa 234-357; Samuel Gobat, *Journal of Three Years Residensei Abyssinia* (New York: Mhariri wa 1850), ukurasa wa 55-58, 83- 98. Kwa vitabu vingine vinavyogusia swali hili, tazama Petro Heylyn, *History of the Sabbath*, 2d ed., 1636, juzuu ya. 2, ukurasa wa 198-200; Arthur P. Stanley, (New York: Wana wa Charles Scribner, 1882), hotuba ya 1, par. 1; CF Rey, *Romance of the Portuguese in Abyssinia* (London: FH na G. Witherley, 1929), uk 59, 253-297.

## Hoja Muhimu Za Kitabu Cha Pambano Kuu

[Mwongozo Wa Hoja Za Kujifunzia Kitabu Cha Pambano Kuu.]

Kitabu cha Pambano Kuu ni muhimu sana kwa kila mwanadamu wakati huu tunaoishi, maana kwenye ulimwengu wa utandawazi sote tunasikia ghasia, machafuko na tetesi nyingi kila kukicha. Kwa vile ni kitabu nyeti na kirefu, Kisome na Maswali haya kila sura, nayo yatakusaidia kurahisisha uelewaji wa mada zilizomo ndani.

**Sura ya 1 - Kuangamizwa kwa Yerusalemu**

1. Jifunze hali na tukio la huzuni na maombolezo ya uchungu ya Yesu juu ya Yerusalemu. Ni kwa sababu zipi watu waliona kuwa ni jambo la ajabu mji kuangamizwa na watazamaji wakashindwa kuwajibika? 17:1, 2 [15:1, 2] GC-SG 5.1

2. Je, Yesu alikuwa na sababu ya kusikitika Alipokabiliana na Gethsemane na Kalwari? Ni jambo gani lililoongoza kwenye huzuni Yake kuu? 18:1 [16:1] GC-SG 5.2

Angalia.—Tunapofikiria nyakati za majaribu zilizo mbele ya watu wa Mungu, je, hangaiko letu kuu zaidi liwe kuhusu magumu na majaribu yetu wenyewe, au kwa ajili ya hatima ya wale wasiotubu? Tukifuata mfano wa Yesu wa kufikiria nafsi zilizopotea, je tutadhihirishaje kwamba mzigo huu wa waliopotea upo maishani mwetu? GC-SG 5.3

3. Tafakari juu ya huruma na upendo wa Mungu kwa watu Wake katika kushughulika Kwake nao zamani na katika utume wa upendo wa Kristo kwao. Kariri: "Mawimbi ya rehema, yaliyorudishwa na mioyo hiyo migumu, yalirudi kwenye wimbi lenye nguvu la huruma, na upendo usioelezeka." 20:2 [19:3] GC-SG 5.4

4. Ni nini kilichowafanya manabii walie? Maoni ya Yesu kuhusu wakati ujao yalilinganishwaje na matazamio yao— (1) kuhusu wakati uliofichwa uliohusika, (2) kuhusu umati wa watu waliohusika, (3) kuhusu uovu wao, (4) kuhusu ukali wa hukumu? 21:1; 22:1; 36:2 [21:1; 22:1; 39:2] GC-SG 5.5

5. Linganisha dhambi kuu ya Wayahudi na ile ya ulimwengu wa Kikristo wa baadaye. 22:2 [22:2] GC-SG 5.6

6. Ni unabii gani wa Mika ambao ungetimizwa kuhusiana na mtazamo wa Wayahudi na kuharibiwa kwa jiji lao? Je, ulitimizwaje? 26:2; 27:2 [27:2; 28:1] GC-SG 6.1

7. Ni mazingira gani yaliyofanya iwezekane kwa wafuasi wa Kristo kutoroka kutoka Yerusalemu wakiwa hai? Je, walipata wapi mahali pa usalama? 30:2; cf. 37:2 [31:1; cf. 41:1] GC-SG 6.2

8. Kama inavyoonyeshwa katika kushughulika kwa Mungu na Israeli, hebu tuwe na mtazamo wa kuona kwamba Mungu hutumia mali za mbinguni ili kuwashawishi wanadamu waukubali wokovu. 20:3; 22:1; 28:1 [19:4; 22:1; 29:1] GC-SG 6.3

9. Kuna wakati wanadamu hatimaye watamkataa Mungu bila kurudi nyuma, na kumchagua Shetani kuwa mtawala wao. Je Shetani ni bosi wa namna gani? Jaribu kuonyesha kwamba uharibifu wa Yerusalemu na taifa la Kiyahudi ulikuwa tokeo la asili la kutotubu kwao. Je, kanuni hii inatumikaje kwa wakati wetu wenyewe? 35:3 [38:2] GC-SG 6.4

10. Je, tunawiwa na nani kwa ajili ya amani na ulinzi wetu? Ni nini kinachoweza kusababisha uondoaji wa ulinzi huu, na matokeo yake yatakuwa wapi? 36:1 [39:1] GC-SG 6.5

11. Ni hali gani zitakuwepo hadi wakati wa kufungwa kwa rehema? 38:1 [41:2] GC-SG 6.6

**Sura ya 2 - Mateso Katika Karne za Mapema**

1. Katika kutabiri matukio ya watu Wake hadi mwisho wa wakati, je, Yesu alitoa vishawishi au vizawadi vya udanganyifu ili kuwaongoza wanadamu kuukubali Ukristo? Ni awamu gani ya uzoefu wao aliisisitizia hasa? 39:1 [43:1] GC-SG 7.1

Angalia.-Je, ni kweli kwamba Uhalisia wa utabiri wa Yesu kuhusu matukio ya kujaribu ambayo kanisa Lake lingepitia imetoa ushawishi wenye nguvu katika kuwaimarisha waamini katika pambano lao na nguvu za uovu. GC-SG 7.2

2. Nini ilikuwa siri ya ujasiri na ustahimilivu wa waadilifu katikati ya mateso ya kutisha chini ya upagani? 41:1, 41:2 [45:1, 2]GC-SG 7.3

3. Ni kwa njia gani mateso yalithibitika kuwa baraka—(1) kwa ajili ya Ukweli, (2) kwa ajili ya uzoefu wa muumini mmoja-mmoja, (3) kwa kanisa kama mwili wa Bwana? 41:3; 41:1 [45:3; 47:2] GC-SG 7.4

Kumbuka.-Ukuaji wa ajabu wa kanisa chini ya hali hizi mbaya ni ushahidi tosha wa roho ya ajabu ya bidii na kimishenari kati ya washiriki wa kawaida. GC-SG 7.5

4. Alipobadilisha mkakati wake dhidi ya kanisa, Shetani alitenda kwa ufanisi zaidi kwa kutumia uharibifu wake kwa kuwaongoza washiriki wake kwenye mapatano au maridhiano (compromise). Washiriki waliongezeka kwa idadi, lakini kwa gharama kubwa kwani hawakuwa na uhai wa kiroho. 42:2; 43:1 [46:2; 47:2] GC-SG 7.6

Kumbuka.-Tunaona katika ulimwengu wa kidini leo mwelekeo maarufu na unaopendwa na wengi kuelekea mapatano kwa gharama ya kusalimisha zile Kweli muhimu. GC-SG 7.7

5. Tunapaswa kuwa na mtazamo gani kuelekea mwelekeo wa siku hizi wa kuridhiana au kufikia mwafaka na huku kunaendelea kuwa na makosa katika mafundisho muhimu ya imani (Doctrines)? 46:1 [50:4] GC-SG 7.8

6. Waasi wa imani walitenda sehemu gani katika vita vyao dhidi ya Mafundisho ya Kristo? 45:1 [50:1] (Kwa matumizi ya kanuni hiyohiyo katika wakati wetu angalia ukurasa wa 608, fungu la 2, je, umeelewa nini) [608:2-681:1] GC-SG 7.9

7. Maneno ya Yesu, “sikuja kuleta amani, bali upanga,” yanawezaje kupatana na cheo Chake kama, “Mfalme wa Amani”? 46:2, 3 [51:1, 2] GC-SG 7.10

8. Angalia jinsi Mungu anavyoshughulika na wenye haki na waovu, katika kuwaruhusu waionyeshe au waianike wazi tabia yao ya kweli kwa kuionyesha kwa ulimwengu na, hivyo kuhitimisha haki ya uamuzi Wake kuhusu wao. 48:1, 2 [52:2, 53:1] GC-SG 8.1

9. Je, Ukweli wa kwamba leo hakuna mateso makali dhidi ya kanisa unapaswa kuchukuliwa kuwa ni jambo la kuridhika nalo sana? Ni uzoefu gani wa watu wa Mungu utakaoamsha upya mateso? 48:3 [53:2] GC-SG 8.2

**Sura ya 3 – Zama Za Ukengeufu**

1. Katika Ufuatiliaji wa kila kuzaliwa upya, ama kwa mtu binafsi au kwa kanisa, kuna kufuatiliwa na hatari ya kuzorota. Historia ya mzozo juu ya maisha ya wanadamu imewahi kuwa kama ile ya Israeli, kama inavyosemwa katika Waamuzi 2:7-19. Mazungumzo hayo pia ni ya kweli, kwamba katika saa ya giza kuu la kiroho, Mungu huwasha nuru mpya ili kuliangazia giza hilo. GC-SG 9.1

2. Linganisha hatua za ukengeufu wa mtu binafsi na zile za ukengeufu wa kanisa la kwanza. Hatua za michepuko ya kwanza ilikuwa vigumu sana kuonekana. 49:2 [55:2] tunapaswa kujilinda kwa uangalifu kiasi gani dhidi ya mwanzo wa maridhiano au kukubalina ili kulinda amani, ambako kunaelekea kushusha kiwango cha muundo mkamilifu wa Mungu: GC-SG 9.2

3. Shetani anatambua nguvu za Neno la Mungu, “Mchunguzi wa makosa.” 51:3 [57:3] Wakati wowote na popote ambapo Shetani hawezi kuwazuia watu wasiwe na Maandiko, ni kwa njia gani anafanya kazi kuwazuia watu wasipate nguvu au uweza wao walioahidiwa na Bwana?Angalia msukumo wa sentensi ya kilele, mwishoni mwa sura hii, na ulinganishe na 526:1 na 595:2 [597:3 na 671:2] GC-SG 9.3

4. Wayahudi walikuwa na dhana gani ya uongo kuhusu Sabato, na dhani hii iliongoza kwenye nini? 52:2 [58:3]. Je, jambo hili linapendekeza ulazima wa kutilia maanani kwa bidii njia ambazo kwazo utunzaji wa Sabato unaweza kufanywa kuwa Shangwe na furaha, kama inavyoonyeshwa katika Isaya 58:13? GC-SG 9.4

5. “Madai yenye upinzani ya ukafiri na Ukristo yaliunganishwa kwa njia gani”? 53:1, 2 [59:1, 2] Angalia jinsi mambo yaleyale yanavyofanya kazi leo. 573:1 [647:1] GC-SG 9.5

**Sura ya 4 – Waldenses (ibada)**

1. Kama motisha ya kuchunguza kwa kina na kwa subira Ukweli wa kihistoria kuhusu Wawaldensi, angalia sentensi ya kumalizia sura hiyo. Kazi waliyoianza itamalizwa kwa utukufu na wale wanaochukua kazi baada yao. GC-SG 10.1

2. “Mwanzoni mwa karne ya saba Ulaya ya Kikristo ilikuwa imefikia kiwango cha chini sana kiakili. . . . Ni nchini Uingereza na Ireland tu ....... na katika majiji machache ya Italia, ndiyo kulikuwa na jambo lolote la matokeo ya elimu ya kale ya Kiroma.”—“History of Education,” Ellwood P. Cubberley, p. 127. Fikiria uhusiano wa ukweli huu na taarifa ya historia 62:3 [70:3] Elimu inapoandamana na akili ni msadaa kwa Ukristo wa UKweli. Ufisadi katika Ukristo ulihusishwa na upungufu mkubwa wa kujifunza. Kwa hiyo katika matengenezo ya Ukristo, elimu ya Kweli inarejeshwa. GC-SG 10.2

3. Tunapokabiliana na maswala ya majaribio na mitihani mbele, ni vyema kutambua mafunzo ya wazazi kwa watoto na elimu iliyotolewa kwa vijana, na jinsi inavyowatayarisha kwa ajili ya ujasiri na uaminifu chini ya mateso. 67:1-3 [76:1-3] GC-SG 10.3

4. Ni motisha gani iliyoongoza vijana kuhudhuria katika baadhi ya vyuo vikuu vya Italia na Ufaransa? Nini ilikuwa siri ya uimara wao? Ni kazi gani iliyokuwa mbele zaidi akilini mwao wakiwa huko? Je, walikuwa viongozi, au waliongozwa mbali na kanuni zao? “Shuhuda,” Vol. V, ukurasa wa 583, 584. 69:3 hadi 70:1 [78:3 hadi 79:1] GC-SG 10.4

5. Ni wazo gani lililowaletea utambuzi wa wajibu wao mzito wa kuacha nuru yao iangaze? 70:2 [79:2] GC-SG 10.5

6. Ni suala gani kuu lililotofautisha wale walio wa kweli na waasi wa imani? 73:1. Ni mahali gani fundisho la “haki kwa imani” linapaswa kuchukua nafasi katika uzoefu wetu, na kazi zetu? 73:5 [81:3] GC-SG 10.6

**Sura ya 5 - John Wycliffe [1324-1384]**

1. Kariri 94:2 [105:2] au sehemu muhimu ya Aya. GC-SG 11.1

Angalia.—“Kufafanusha kwa Maneno Yako kwatia nuru.” Zaburi 119:130 Ilikuwa baada ya kuondolewa kwa Biblia kutoka kwa watu wa kawaida, na uwekaji wa mamlaka ya kibinadamu badala ya ile ya Neno la Mungu, ndipo ulimwengu ulipoingia katika Enzi za Giza. Tunaanza sasa kufuatilia urejeshwaji wa Kitabu Kikuu na nuru iliyofuata, ambayo ilikuwa endelevu, na ikiendelea kuongezeka katika mng’ao hadi Matengenezo makubwa, katika kisa cha Wycliffe, mwandishi anatukumbusha kwamba nguvu na juhudi zake zilikuwa kama matokeo ya Maandiko Matakatifu GC-SG 11.2

2. Je, kazi ya Wycliffe ilidhoofishwa au kuimarishwa na elimu yake huru? (liberal education) Toa sababu nyingi za hitimisho lako kwa kadiri unavyoweza

kupata, ukibainisha hasa 80:2; 81:1; 84:3; 87:2 [90:3; 91:2; 95:3; 98:2] GC-SG 11.3

Angalia.—Wanafunzi ambao Yesu aliwaita wengi wao walikuwa watu wenye elimu ndogo. Tunafanya vyema kukumbuka kila mara kwamba nguvu za Roho Mtakatifu zikiwa juu ya watu waliojitoa wakfu, na wanyenyekevu, itakuwa ni bora zaidi kwa Mungu kuliko kujifunza tu wenyewe. GC-SG 11.4

3. Ni sifa gani tunazopata kwa Wycliffe ambazo zilichangia mafanikio yake ya ajabu kama kiongozi? 81:2; 94:1 [91:3; 105:1] GC-SG 11.5

4. Taja mafundisho mawili ya imani yaliyotiliwa mkazo kwenye Uprotestanti? 89:1; 93:3 [100:1; 104:3] GC-SG 11.6

5. Wycliffe alikuwa na vyeo gani rasmi? 82:1; 84:3; 85:2 [93:1; 95:3; 96:2] GC-SG 11.7

6. Maandamano yake ya kwanza yalielekezwa dhidi ya dhuluma gani mbili? 82:1, 2 [93:1, 2] GC-SG 11.8

7. Wycliffe alipangaje "harakati ya watu wa kawaida," na kwa mafanikio gani? 87:2; 88:3; 89:1 [98:1; 99:3; 100:1] GC-SG 11.9

8. Ni katika vipindi gani viwili, ambapo kifo cha mtu mashuhuri kilimwokoa katika nyakati za hatari? 85:3; 86:1 [96:3; 97:1] GC-SG 12.1

9. Wycliffe aliitwa mbele ya mahakama zipi nne, na matokeo yake yalikuwa nini katika kila kipindi? 85:3; 89:3; 90:3 [96:3; 100:3; 101:2] GC-SG 12.2

10. Kilele cha kazi ya Wycliffe kilikuwa nini na nini ilikuwa silaha yake yenye matunda zaidi dhidi ya makosa? 88:1, 2 [99:1, 2] GC-SG 12.3

11. Je, mustakabali wa vuguvugu nchini Uingereza lililoanza chini ya uongozi wake ulikuwa upi? 94:3; 95:2 [106:1, 2] GC-SG 12.4

Kumbuka.—Masomo yenye faida kwa kazi yetu wenyewe yanaweza kutolewa kutokana na ushawishi wa machapisho yaliyotolewa na Wycliffe. Ni kwa jinsi gani ushuhuda wake ulisambazwa kwa haraka na kwa upana zaidi. GC-SG 12.5

**Sura ya 6 - Huss [1373-1415]**

1. Ni maendeleo gani ambayo injili ilikuwa imefanya huko Bohemia, na ni matatizo gani injili ilikumbana nayo kabla ya siku za John Huss? 97:1, 2 [109:1; 110:1] GC-SG 13.1

Kumbuka.-Fahali/bulla au amri ya papa Gregory VII aliyetajwa katika maandishi yaliyotolewa mwaka wa 1079 AD GC-SG 13.2

2. Kutawanywa kwa waumini kwa mateso au uonevu mara kwa mara kumebarikiwa na mbingu katika kueneza nuru. Matendo 11:19-21. Hili linaonyeshwa katika historia iliyorekodiwa katika sura hii. 97:1; 100:3 [109:1, 112:2] GC-SG 13.3

3. Wycliffe alitoka familia ya watu wa hali ya juu kimaisha na hakuwa na matatizo ya kifedha kukabiliana na kujipatia elimu. Wakati Huss anatupa mfano wa kijana aliyetoka katika nyumba ya watu maskini. Wote wawili, hata hivyo, walijituma kwa bidii kujifunza, na wote wawili walikuwa vielelezo vyema katika usafi wa maisha yao. 98:1, 2 [110:2, 3] GC-SG 13.4

4. Huss alichagua kufuata wito gani, na alishika nyadhifa zipi? 98:2; 99:1 [110:3; 111:1] GC-SG 13.5

5. Ni maandalizi gani yaliyoongoza kwenye kuenea kwa maandishi ya Wycliffe hadi Bohemia? 99:2, 3 [111:2, 3] GC-SG 13.6

6. Ni nini Huss alitambua kuwa hitaji kuu zaidi la kusanyiko ambalo aliitwa kulihudumia? 99:1 [111:1] GC-SG 13.7

7. Ni tukio gani linaloonyesha uwezo wa elimu ya maono? 99:3; 100:1 [111:3; 112:1] GC-SG 13.8

8. Ni hali gani zilizoongoza kwenye kuwekwa kwa Prague chini ya amri ya papa? Ni masharti gani yalikuwepo kwa kizuizi kama hicho? 100:3; 104:1 [112:3; 113:1] GC-SG 14.1

9. Ni kanuni gani zinazopaswa kutuongoza ikiwa tunaitwa kuchagua kati ya shauri la Kristo linalopatikana katika Yohana 10:12, 13 na lile lipatikanalo katika Mathayo 21:23? 101:2 [113:2] Rejelea Maandiko yaliyotangulia katika “Fahirisi ya maandiko na Masomo ya Maandishi ya Ellen G. White,” ukurasa wa 45, 58. GC-SG 14.2

Kumbuka.-”Ni lazima nifuate maagizo au kanuni gani kati ya mawili haya? Kati ya mapendekezo haya mawili yanayokinzana, ni lipi ninalopaswa kutii? . . . siwezi kusema.” Ndivyo alivyoandika Huss. (Bonnechose, Vol. I, p. 86). GC-SG 14.3

10. Ni uamuzi gani wa mwisho wa Huss katika jambo hilo, na mwenendo wake ulithibitishaje uhakikisho huu, “Hatuwezi kufanya Neno lolote kinyume cha ile Kweli, ila kwa ajili ya Kweli”? GC-SG 14.4

11. Taja sababu mbili kuu za kuita Baraza la Constance, 1414-18? 104:2, 3 [117:2, 3] GC-SG 14.5

12. Zingatia hoja za mkataba kati ya John XXXIII, mshtaki, na Huss, mshtakiwa. 104:3; 106:2 [117:3; 119:3] GC-SG 14.6

13. Tunapata mambo gani kuhusu zawadi ya unabii katika sura hii? 97:1; 108:1 [110:1; 122:1] "Huss alipata maono na ndoto za kiunabii."— Bonnechose, juzuu ya 5. II, uk. 24. GC-SG 14.7

14. Tukizingatia hali yao mbaya gerezani hapo awali, je, ujasiri na uchangamfu wa akili ya Huss na Jerome unaweza kuhesabiwa kama jambo la kawaida? 107:2; 112:2, 3 [121:2; 127:2, 3] GC-SG 14.8

15. Ni nini matokeo ya papo kwa hapo katika Bohemia baada ya kuuawa kwa Huss? 115:3 [131:3] GC-SG 15.1

16. Ni mafanikio gani yaliyohudhuria jitihada za majeshi ya Sigismund dhidi ya watetezi wa Bohemia wa kanuni za uhuru wa kidini? 117:2 [133:2] GC-SG 15.2

17. Ni jinsi gani lile jambo ambalo halikuweza kutimizwa kwa nguvu, lilitekelezwa kwa kutumia diplomasia? 118:1 [134:1] GC-SG 15.3

18. "United Brethren" walikuwa nani? Uvutano wao ulikuwa nini katika kudumisha Ukweli? 119:1-3 [135:1-3] GC-SG 15.4

**Sura ya 7 - Kujitenga kwa Luther kutoka Roma** (mgawanyiko kutoka Roma)

1. Wakati unaozungumziwa katika sura hii ni tangu kuzaliwa kwa Luther, mwaka wa 1483, hadi amri ya papa ya mwisho (fahali au bulla), ikimtenga na kanisa, iliyotolewa na papa mwaka wa 1520. GC-SG 16.1

2. Hiki ni kielelezo cha uwezo ambao vijana waliowekwa wakfu wanaweza kuwa nao, kumbuka kwamba akiwa na miaka kumi na nne Luther aliingia Magdeburg; na akiwa na miaka kumi na nane alianza masomo huko Erfurt; akiwa na miaka ishirini aligundua Biblia ya Kilatini. Apokuwa na miaka ishirini na miwili aliingia kwenye monasteri yaani nyumba ya utawa, na alitawazwa kuwa kasisi akiwa na miaka ishirini na nne. GC-SG 16.2

Mwaka uliofuata alipata wito wa kuwa profesa katika chuo kikuu. Alianza kuhubiri akiwa na miaka ishirini na sita. Safari yake iliyo kwenye kumbukumbu ya kwenda Rumi ilifanywa akiwa na umri wa miaka ishirini na saba. Alikuwa na umri wa miaka thelathini na tano, alipotangaza hadharani hoja au matamko yake tisini na tano (95) dhidi ya vyeti vya msamaha. Miaka miwili baadaye alitengwa na kanisa, yaani alifukuzwa. GC-SG 16.3

3. Kuna nini cha kupongezwa, na nini cha kujiuliza, kuhusu mazoezi ya wazazi wa Martin akiwa mvulana mdogo? 120:3-121:1 [137:3-138:1] GC-SG 16.4

4. Katika kuchanganua sifa za kibinafsi zilizomtia alama Luther, kariri sentensi ya pili ya sura, na kumbuka rejelea hizi 121:3-122:2; 123:1 [138:4-139:1; 140:3] GC-SG 16.5

5. Kama ilivyokuwa kwa Sauli mtesaji watu, vivyo hivyo kwa Luther— bidii ya uangalifu sana ambayo ilitia alama kila wakati katika makosa, ilimfanya awe na uwezo katika utumishi wa Mungu wakati nuru ilipoangaza ndani ya nafsi yake. Fuatilia kupitia kisa cha mwangaza uliopenya akili yake taratibu. (cf. Wafilipi 3:5-9; Wagalatia 1:14) 123:1, 2; 124:2; 128:3; 139:2; 143:1 [140:2, 3; 141:2; 147:2; 160:1; 164:1] GC-SG 16.6

6. Ingawa Luther ameonekana mara kwa mara kuwa mstari wa mbele, wengine walitumiwa na Mungu kutenda kama washauri wenye hekima pia, wasaidizi wa kiroho, au walinzi. 123:3; 134:2; 147:3; 138:3; 140:2 [141:1; 154:2; 158:2; 159:2; 160:4]. Kama kielelezo cha jinsi Mungu alivyotumia watu ambao walikuwa wanakwenda kinyume na kupitiliza kiasi, mwenendo huu baada ya wongofu uliwafanya wasaidie kazi Yake kwa mvuto mkubwa, angalia "Maandiko ya Awali," 224:1, 2. GC-SG 16.7

7. Luther alikuwa na mtazamo gani kuhusu suala la elimu ya Kikristo? 125:2; 132:2; 139:1; 140:5 [143:2; 152:1; 159:4; 161:3 ] GC-SG 17.1

8. Ni uthibitisho gani unaweza kupatikana kuhusu harakati kubwa ya walei kwa niaba ya zile Kweli mpya zilizopatikana? 133:1; 139:1-3; 141:1 [152:3; 159:4-160:2; 161:4] GC-SG 17.2

9. Wycliffe na Luther walilindwa kwa namna ya ajabu katika kazi yao. Huss na Jerome waliuawa kama mashahidi au wafia dini mapema katika kazi yao. Kifo cha wengine, maisha ya ujasiri ya wengine, vilichangia vile vile makusudi ya Mungu. Haikujalisha kama mwanamatengenezo alitoa maisha yake au la, kinachojalisha ni kwamba kila mmoja alijitoa moyo wake kwa Mungu na kuwa tayari kwa ajili ya uhai au kifo. (Wafilipi 1:20) 134:3; 137:3; 140:1; 141:2 [154:3; 158:2; 160:3; 162:1] GC-SG 17.3

10. Hata Luther wakati fulani alitatizwa na mashaka juu ya kazi yake. Je alishindaje Mashaka haya? 143:1 [164:1]. GC-SG 17.4

11. Ni masomo gani ya kivitendo yanayotolewa katika sehemu hii ya utume wa Luther, katika kuonyesha hali zinazolingana na wakati wetu wenyewe? 143:3-144:1 [165:1, 2] GC-SG 17.5

**Sura ya 8 Luther Mbele ya Diet (1521)**

1. Dola ya Ujerumani ya kipindi hiki ilikuwa ni shirikisho la majimbo, ambayo Saxony ilikuwa moja wao. Mteule wa Saxony anaweza kulinganishwa na gavana wa mojawapo ya Jimbo letu. GC-SG 18.1

2. Ni kwa ajili gani Baraza liliitwa, Baraza ni Diet kijerumani, (diet of Worms ni Baraza lililofanyika mjini Worms) mkusanyiko, uliitishwa kwa kusudi gani katika 1521? Ni swali gani lililokuwa la hatima kubwa zaidi kuliko yote? Ni tabaka gani za watu zilizounda wanachama wa baraza? 145:2 [168:1] GC-SG 18.2

3. Suala la kwanza kati ya pande pinzani lilikuwa Luther aje kwenye Baraza la Worms au asije. Ni sababu gani zilizomfanya mjumbe wa papa kupinga kuja kwake, na kwa nini Luther na marafiki zake walifanya juu chini ili kuhakikisha kwamba angekuja barazani? Nani alishinda katika mzozo wa kwanza kuhusu suala hili? 146:1-2 [168:1-169:1] GC-SG 18.3

4. Alipopewa nafasi ya kumtuhumu Luther wakati hayupo, Aleander alijijipingaje mwenyewe? 147:1 [169:2] GC-SG 18.4

5. Baada ya kumshawishi mfalme wa Himaya kumruhusu kuwasilisha hoja yake mbele ya kikao, ni kwa mambo gani mawili Aleander aliwasilisha rufaa yake dhidi ya Luther? (1.) 148:1 [170:1]; (2. 148:2 [170:2] Ni somo gani kwa wakati wetu linaloweza kutolewa kutokana na njia hii ya mashambulizi? 148:3, 4 [170:3-171:1] GC-SG 18.5

6. Wengi walikuwa dhidi ya Luther, ni nani aliyetumiwa na Mungu kuelekeza mawazo ya kusanyiko kutoka kwake Luther hadi kwenye manyanyaso ya Roma? Je, hotuba yake ilikuwa na matokeo gani? 149:2,3; 150:2,3 [171:2-172:1; 172:3,4] GC-SG 18.6

7. Malaika wa Mungu walitenda sehemu gani katika tukio au drama hii? 150:2 [172:3] GC-SG 19.1

8. Marafiki wa Luther kule Wittenberg na njiani kuelekea Worms walikuwa na ushauri gani? Je, jibu la Luther kwa maombi yao lilikuwa nini? 150:5-151:2; 153:1,2 [173:1-3; 175:2,3] GC-SG 19.2

9. Ni njama gani ya hila iliyofanywa ili kumshawishi Luther aache kusudi lake? 153:2 [175:3] Kama Luther angekubali mwaliko huu angalicheleweshwa hadi wakati ambapo hati yake ya uhakikisho wa ulinzi ingeisha siku, hata kama angefaulu kulifikia baraza. GC-SG 19.3

10. Katika pambano na Roma, kuonekana kwa Luther mbele ya baraza Worms kulikuwa na umuhimu gani? 155:1 [177:3] GC-SG 19.4

11. Je, alitumiaje wakati wa mapumziko, na matokeo yalikuwa nini kwake mwenyewe? 156:2-157:2 [179:2- 180:2] GC-SG 19.5

12. Aligawanya maandishi yake katika sehemu gani tatu? Je, kauli yake ilikuwa nini kuhusu kila moja ya sehemu hizo mbele ya baraza la Worms? 158:3 [181:2] GC-SG 19.6

13. Ni maneno gani ya kukumbukwa yaliyomalizia hotuba yake? 160:2 [182:4] GC-SG 19.7

14. Ushawishi wa Luther wenye ujasiri kwa ajili ya ile Kweli ulikuwa mkubwa kwa kadiri gani? 166:3 [189:2] GC-SG 20.1

15. Ni masharti gani ya amri ya mfalme wa himaya yalionekana kufanya kazi ya Matengenezo ya Kidini kuwa bila tumaini? 167:3 [191:2] GC-SG 20.2

16. Ni kwa jinsi gani mwaka wa kutengwa kwa Luther kwa kulazimishwa ulitimiza mengi zaidi kwa ajili ya ile Kweli kuliko wakati angekuwa na uhuru wake? 168:1-3 [191:3-192:2] GC-SG 20.

**Sura ya 9 - Mwanamatengenezo wa Uswisi**

1. Wycliffe, Huss na Jerome, Luther walionekana kufuatana kama Wanamatengenezo. Karne moja na nusu ilifunikwa kwa kazi yao, hadi Diet of Worms (Baraza kwenye mji wa Worms). Zwingle alikuwa rika la Luther, na walifanya kazi katika kipindi kimoja ingawa yeye alikuwa kiongozi, alikuwa ni mmoja tu kati ya watu kadhaa waliotokea katika majimbo ya Uswisi, na akisukumwa na Roho Yule Yule wa Mungu kuchukua nafasi kama viongozi katika vuguvugu kuu la Matengenezo. GC-SG 21.1

2. "Katika Ujerumani kanuni ya kifalme ilitawala; na katika Uswisi demokrasia. Huko Ujerumani Matengenezo ya Kanisa yalilazimika kupambana na walichotaka wakuu; na huko nchini Uswizi, walilazimika kupambana kinyume cha matakwa ya watu. Kusanyiko la watu ambalo huchukuliwa kwa kupindishwa kirahisi zaidi kuliko mtu mmoja, pia uharakisha mambo katika uamuzi. Ushindi juu ya upapa, ambao uligharimu miaka mingi ya mapambano nje hata ya nchi za Rhine, ulihitaji kwa upande huu miezi michache na nyakati nyingine siku chache tu."—D'Aubigne b. 8, Ch. 1. GC-SG 21.2

3. Je, ni sifa gani mbili muhimu za watu ambao Mungu anaweza kuwatumia katika utumishi Wake? Kwa nini Mungu anajipatia watu wenye ushawishi na mafunzo au wenye sifa hizi kwa nadra sana? 171:9 [195:1] GC-SG 21.3

4. Je, jamaa wa Zwingle aliyezeeka na aliyekuwa mnyenyekevu alisaidiaje kuumba akili ya Zwingle alipokuwa mtoto? 171:2, [196:1] GC-SG 21.4

5. Je, Zwingle alipelekwa mahali gani kwa ajili ya elimu, na kwa nini anakumbukwa? 172:1-2 [196:2-3] GC-SG 21.5

6. Zwingle aliwiwa na nani kwa miale ya kwanza ya nuru yenye ufanisi mkubwa, na chanzo cha nuru hiyo kilikuwa nini? 173:1 [197:1] GC-SG 21.6

7. Ni mawazo gani yenye msaada kuhusu ujifunzwaji wa Maandiko unaoweza kupatikana kutokana na kisa cha Zwingle? 173:2-174:1 [197:2-198:1] GC-SG 21.7

8. Ni sehemu gani iliyoonekana katika Matengenezo Makubwa ya Kidini na mwamko wa Ujio wa pili wa Yesu Pili ambayo ilitoa uthibitisho wa mwongozo wa Bwana katika kila hatua mojawapo? 174:2; 140:3; 212:1-3; 357:1 [198:2; 161:1; 244:1-3; 409:1] GC-SG 22.1

9. Kazi ya Zwingle huko Einsiedeln iliathirije msaada wa kifedha? 174:3-175:3 [198:3-199:3] GC-SG 22.2

10. Alipoitwa kwenye kanisa kubwa yaani Kathedro kule Zurich, Zwingle alijihusishaje maagizo yaliyotolewa na wale waliomwalika? 176:3-4 [200:2-201:2] GC-SG 22.3

11. Ni nani aliyekuwa msimamizi mkuu wa vyeti vya msamaha kule Uswisi, na ambaye alikuwa mtu mwenye tabia ya tamaa ya pesa, naye alipata mafanikio gani huko Zurich? 178:4-179:1 [203:2-3] GC-SG 22.4

12. Je, Zwingle aliwajibuje wawakilishi wawili wa manaibu kutoka kwa askofu wa Constance mbele ya Baraza la Zurich, na mtazamo wa Baraza ulikuwaje? 180:3-181:2 [205:1-2] GC-SG 22.5

13. Kwa nini Zwingle hakuonekana kutetea kazi katika mabishano ya Baden? Je, kwa kutokuwepo kwake, alifanyaje ushawishi wake uhisiwe huko? Tofautisha mwonekano wa Oecolampadius na Eck kwenye mjadala, pia tofauti za rufaa zao? Na Matokeo ya majadiliano yao yalikuwa nini? 182:1-184:2 [207:3-209:3] GC-SG 22.6

**Sura ya 10 - Maendeleo ya Mageuzi nchini Ujerumani**

1. Je, kutoweka kwa Luther kulisaidia au kulizuia kazi ya Matengenezo ya Kanisa? 185:3 [212:1] mGC-SG 23.1

2. Je, Melancthon alikuwa na mtazamo gani awali kuhusu madai ya baadhi ya watu waliosema wana karama ya unabii? Je, kuna wale ambao walikuwa waaminifu kweli, ila waliodanganywa na harakati hizo? Je, ni vipimo gani ambavyo dai kama hilo linaweza kuonyeshwa kwamba ni la kweli (kipimo cha nabii wa kweli)? 186:1-187:3; 190:3, 4 [212:2-214:2; 217:2, 3] GC-SG 23.2

3. Je, Ushabiki usiotumia akili au unaopitiliza ulikomeshwaje hatimaye? 190:2 [217:1] GC-SG 23.3

4. Wakati Luther alitetea kanuni za uhuru wa kidini, yeye alitamka nini? 189:4-190:1 [216:2-4] GC-SG 23.4

5. Ni nini kinachosemwa kuwa "mojawapo ya mbinu zenye mafanikio zaidi za Shetani za kutupa masuto juu ya Usafi na Ukweli? 193:1 [221:1] GC-SG 23.5

6. Katika baadhi kile kinachoitwa "vuguvugu la Matengenezo" ya siku za leo tunaona udhihirisho wa sifa zile zile za alama ya kazi ya Thomas Munzer na wenzake. Zingatia yafuatayo: Wakiwa wenye nia ya kutaka Matengenezo; wakiwa na tamaa ya kutaka makuu na nafasi ya ushawishi; walidai kuona miongoni mwa viongozi udhihirisho wa "aina ya upapa;" walidai kuwa "tume ya Kimungu ya kuanzisha Matengenezo ya kweli;" kazi zake zilitawaliwa na hisia; zilifurahisha "tamaa ya wanadamu kwa kupenda mambo ya kustaajabisha;" walikataa utaratibu katika ibada ya hadhara; waliwatukana viongozi waliowapinga; walikata rufaa na kupata huruma kwa madai ya kutendewa isivyo haki; walitoa madai makubwa kuhusiana na utakatifu na utakaso. 191:1-193:1 [217:4-221:2] GC-SG 23.6

7. "Ingawa sifa kuu inatolewa kwa haki kwa viongozi wa Matengenezo ya Kanisa, bado kilele cha mafanikio na hali ya kiroho bora katika vuguvugu hiyo ilifikiwa wakati jeshi la walei wa safu zote" wakiwa na Maandiko na fasihi zilizojaa ujumbe wakienda kila mahali wakihubiri Neno. 195:2 [224:2] Linganisha harakati hii na ile iliyofafanuliwa katika "Testimonies," Vol. 9, uk. 126. GC-SG 23.7

**Sura ya 11 - Maandamano ya Wakuu**

1. Mtawala aliyekuwa akiyumba-yumba, yaani Charles wa Tano, alikuwa ameamua kusaidia Matengenezo ya Kidini kwa muda, na majeshi yake yalikuwa yameingia Rumi na kuliteka jiji hilo, katika Mei 1527. Kufuatia hayo, majeshi ya Ufaransa yalikuwa yakimsukuma sana, naye akafikiri ili kuimarisha nafasi yake, basi ni bora aende kutafuta tena urafiki na Rumi. Ilikuwa wakati huu baraza la Diet of Spiers ya 1529 liliitishwa. GC-SG 24.1

2. Wakati wa mwingiliano wa amani na uhuru wa kidini, vuguvugu la Matengenezo lilikuwa limeungana, na utaratibu wa kanisa ulikuwa umeanzishwa. GC-SG 24.2

3. Inaweza kuonyeshwaje kwamba Waturuki, Wafaransa, na hata Papa walisaidia kazi ya Matengenezo huko Ujerumani? 197:2 [227:2] Taz. Ufu. 12:15,16. GC-SG 24.3

4. Je! Matakwa ya pande  mbili kwenye mzozo wa Baraza/Diet yalikuwa mo nini, na ni mapatano gani yaliyopendekezwa? 199:1, 2 [229:2, 3] GC-SG 24.4

5. Mapatano haya yangeweza kukubaliwa kwa hoja zipi zenye kusadikika? Ni kanuni gani za Ukweli ambazo zingesalimishwa kwa hilo?199:4-200:1 [230:1, 2 GC-SG 24.5

6. Katika mtihani wa mwisho wa nguvu, ni chama gani kilikuwa kimependwa na wengi? 201:2 [231:2] GC-SG 24.6

7. Walio wachache walikata rufaa kwa nani? 202:2 [232:3] GC-SG 24.7

8. Maandamano hayo kwa Baraza yalielekezwa dhidi ya dhuluma gani mbili? 202:4-203:4 [233:1-234:2] GC-SG 25.1

9. Ni kwa njia gani uzoefu wa Wanamatengenezo hawa umekuwa somo kwa wakati wetu? 204:2 [235:1] GC-SG 25.2

10. Tuna kielelezo gani kuhusu nguvu za muziki? 206:1 [236:2] GC-SG 25.3

11. "Ungamo la Imani" lililosomwa katika Baraza au kusanyiko gani hatimaye? 205:4; 207:1 [236:1; 238:1] GC-SG 25.4

12. Je, Luther alihusika na damu iliyotiririka katika mapigano kati ya Serikali ya Ujerumani na maadui wa Matengenezo ya Kanisa? 209:1-3 [240:1-3] GC-SG 25.5

**Sura ya 12 - Matengenezo ya Ufaransa**

1.Baada ya miaka ya vita na umwagaji damu, katika jaribio lake la kukomesha Matengenezo ya Kidini katika Ujerumani kwa nguvu ya silaha, Je, Charles wa Tano hatimaye alilazimishwa kutoa nini? Alimalizaje siku zake? 211:1 [243:1] GC-SG 26.1

2. Roho wa Mungu anaweza kuwatumia kama chombo Chake vijana wa miaka ishirini kama Luther, au mzee wa miaka sabini, kama LeFevre. Kila mmoja wao alikuwa ameonyesha bidii yenye kuonekana kwa macho katika kutafuta kupata kibali cha Mungu kwa matendo yenye kustahili sifa. Kila mmoja aliacha historia katika kipindi chake cha kazi nyingi muhimu kutoka pale Biblia ilipogunduliwa. Kila mmoja alikuwa mwalimu katika chuo kikuu mashuhuri, na kwa kipawa cha kufundisha aliwapitishia wanafunzi wake nuru tukufu ya Ukweli ambayo ilichukua mahali pa jitihada zake za awali za kupata wokovu kwa matendo. GC-SG 26.2

3.Ni kwa kusudi gani LeFevre alikuja kujifunza Maandiko, na alipata nini humo? 212:2 [244:3] GC-SG 26.3

4. Ni mwanafunzi gani alikuwa mtu wa kwanza kabisa katika kukubali na kufundisha imani mpya? Uzoefu wake wa mapema ulikuwa nini? 213:2 [245:2] GC-SG 26.4

5. Ni watu gani mashuhuri waliokuwa miongoni mwa wale walioathiriwa na mafundisho ya Farel na LeFevre? 214:2 [246:2] GC-SG 26.5

6. Kanisa la kwanza la Kiprotestanti lilianzishwa wapi katika nchi ya Ufaransa, na ni mabadiliko gani ambayo yalifanywa katika jumuiya hiyo? 214:3-215:1 [246:3-247:1] GC-SG 26.6

7. Ni mtu gani msomi wa Ufaransa aliyesemekana kuwa ndiye "Luther wa pili"? Je, alimshuhudiaje Kristo katika maisha na kifo? 215:3-218:4 [247:3-250:4] GC-SG 26.7

8. Je, mateso yaliendelezaje tena kazi ya injili? 219:1, 2 [251:1, 2] GC-SG 27.1

9. Je, watu wawili walichangia kwa njia gani tofauti katika kuongoka kwa Calvin? 220:1-3 [252:1-3] GC-SG 27.2

10. Linganisha hekima na ufanisi wa kuendeleza Ukweli kwa "mabishano ya kitheolojia" na kwa kazi tulivu ya nyumba hadi nyumba. 221:4-222:1 [253:4-255:1]
GC-SG 27.3

11. Ni hali gani zilizowezesha kuhubiriwa waziwazi kwa kanuni za Kiprotestanti katika jiji la Paris? Jambo hili liliwezekana kwa muda gani? 222:2-223:1 [254:2-255:1] GC-SG 27.4

12. Eleza kazi ya mwisho ya Calvin huko Ufaransa? Alienda mahali gani? 223:2-224:2 [255:2-256:2] Tukio la kazi yake kuu lilikuwa nini? 236:2 [269:1] GC-SG 27.5

13. Ni "harakati gani yenye bidii lakini ilikuwa haifai" nayo ilileta matokeo mabaya kwa Waprotestanti nchini Ufaransa? 224:3; 227:3 [256:3; 260:2] GC-SG 27.6

14. Ufaransa ililipa gharama gani ya kutisha kwa ajili ya "kukataa kwake zawadi ya mbinguni"? 230:2, 3 [263:2, 3] GC-SG 27.7

15. Baada ya Farel kushindwa kupanda injili huko Geneva, ni chombo gani kinyenyekevu ambacho Mungu alikitumia? 232:2, 3 [265:2-266:1] GC-SG 28.1

16. Ni vuguvugu gani iliyotokea wakati huu ili kutetea kazi ya Roma? Ni katika njia zipi waliwaigiza Wanamatengenezo? Je, ni baadhi ya njia gani zilizochangia mafanikio yao? 234:2-235:2 [267:2-268:2] GC-SG 28.2

## Sura ya 13 - Uholanzi na Skandinavia

1. Kanuni za Kiprotestanti zilipata kuingia Uholanzi mapema kiasi gani, na kwa njia gani? 237:1 [271:1] GC-SG 29.1

2. Matamko kuhusu wamisionari wa Kiwaldensia [238:1; 239:1 (272:1; 273:1)] yanapaswa kuunganishwa na yale yaliyotokea awali, hasa [71:1 (80:2)] Matunda ya kazi ya vijana yaliyoonekana karne nyingi baadaye miongoni mwa warithi wao waliopokea injili moja kwa moja kutoka kwao. GC-SG 29.2

3. Kwa nini mateso ya wafuasi wa Luther katika nchi ya Uholanzi yalikuwa makali zaidi kuliko Ujerumani? Je, Ukweli kwamba waamini waliteswa mahali pamoja, huku kukiwa na uhuru katika sehemu nyingine, ilimaanisha kwamba injili ilizuiliwa katika sehemu moja zaidi kuliko ile nyingine? 293:3 [274:1] GC-SG 29.3

4. Ni nani aliyekuwa Mwanamatengenezo aliyeongoza kazi Uholanzi? Aliongozwaje kujifunza Maandiko? Je, alikuwa na sifa gani za kielimu? Kazi zake zilikuwa nini, na alishuhudia kwa muda gani? 238:3-239:2 [272:1-273:2] GC-SG 29.4

5. Ni sifa gani alizokuwa na Tausen alipokuwa mtoto, ambazo zilizoongoza kwenye fursa adimu ya elimu? Ni kizuizi gani kiliwekwa katika uchaguzi wake wa shule? Hatimaye aliongozwaje kwenda Wittenberg, na je, jambo hili lilikuwa na hatari gani kulifanya? Aliporudi Denmark, alianza kazi yake wapi? Je, jitihada za kunyamazisha ushuhuda wake zilikuwa na matokeo gani? 241:1-3 [275:3-276:2] GC-SG 29.5

6. Kaka wawili walioongoza Matengenezo ya Kanisa katika Uswidi, walipata wapi kuzoefu wao? Je, Walifanana katika jambo gani, na walitofautianaje katika tabia? Ni fursa gani nzuri ilijitokeza kwao kwa kutoa ushuhuda mbele ya wakuu wa Sweden, na matokeo yake, yalikuwa nini? 242:2-244:1 [276:3-279:1]GC-SG 29.6

7. Je, elimu na ushawishi wa viongozi na walimu wa Matengenezo vilisaidiaje mafanikio? Je, ni sifa gani muhimu zilizowatia alama wote? 243:3 [278:2] GC-SG 29.7

8. Kukubali kwake Uprotestanti kulikuwa na matokeo gani kwenye historia ya Sweden siku za mbeleni, (1.) kuhusu nguvu ya taifa, (2.) kuhusu hatima ya mataifa mengine? 244:2 [279:2] GC-SG 29.8

## Sura ya 14 - Wanamatengenezo wa Kiingereza wa Baadaye

1. Ni masharti gani yaliyopunguza manufaa ya tafsiri ya Biblia ya Wycliffe katika lugha ya Kiingereza, (1.) kuhusiana na usahihi wa maandishi, (2.) kuhusiana na kuenezwa kwake? Ni mchango gani muhimu uliotolewa na Erasmus? 245:1 [281:1]
GC-SG 30.1

2. Usomaji wa makini wa paragrafu hii hautazua maswali kuhusu uwezekano wa makosa mazito katika maandishi yaliyomo kwenye Maandiko. Kasoro katika toleo la Biblia ya Wycliffe ilitokana na kutofanya kazi yake kutoka kwenye lugha asilia, bali kutokana na tafsiri mbovu ya lugha ya Kilatini. Tangu wakati huo, miswada mingi ya zamani imegunduliwa na kutafsiriwa kutoka katika maandishi hayo za awali za Kiebrania na Kigiriki. GC-SG 30.2

3. Tyndale alitoa sababu zipi za busara za walei kumiliki Maandiko? Ni kusudi gani lililoundwa katika akili yake kufanya jambo hili liwezekane? Ni chini ya vizuizi gani alilazimika kufanya kazi hii? Agano lake Jipya lilichapishwa wapi, nalo liliingiaje Uingereza? Askofu wa Durham alisaidiaje jambo hilo bila kujua? 246:2-247:1 [282:2-283:3] GC-SG 30.3

4. Ni watu gani walioishi wakati mmoja naTyndale waliotetea Ukweli, na kuongeza maarifa ya Mungu na kulikuza Neno? Kulingana na Latimer, ni nani aliyekuwa askofu mwenye bidii zaidi katika Uingereza yote, na alifanya kazi vipi? Je, utabiri wa mwisho wa Latimer ulikuwa upi? 248:1-249:1 [284:2- 285:1] GC-SG 30.4

5. Mahali hapa ambapo nakala nyingi za Biblia ya Tyndale zilichomwa hadharani, sasa kuna British and Foreign Bible House, yaani Chama cha Biblia cha Uingereza na nchi zingine za ng'ambo. GC-SG 30.5

6. Ni ushawishi gani wa awali gani uliosaidia Scotland kudumisha uhuru wake kwa muda mrefu kuliko Uingereza? Mwenge wa Ukweli uliwashwaje tena katika ufalme wa kaskazini? 249:2-4 [285:2-286:2] GC-SG 30.6

7. Ni nani aliyekuwa kiongozi mkuu wa Matengenezo ya kanisa Scotland? Je, Alifasirije amri ya Mungu katika kuwatii watawala wao? Ni shauri gani la hekima alilotoa ili kuwaongoza wale waliochanganyikiwa kwa sababu ya tofauti za imani miongoni mwa viongozi wa kiroho? Uongozi wake huko Scotland ulikuwa na ufanisi kiasi gani? 250:2-251:3 [287:1-288:3] GC-SG 30.7

8. Katika uanziswaji wa Uprotestanti huko Uingereza, ni kanuni gani potovu za upapa zilibakizwa? Matokeo yalikuwa nini kwa wapinzani? Ni kitabu gani cha kulitiliwa umakini ambacho kilichotolewa na mfia-dini kwa ajili ya imani yake, akiwa gerezani? Ni vitabu gani vingine vinne vilivyojitokeza ambavyo vilikuwa na nuru ya kiroho? 251:4-252:3 [288:4-290:2] GC-SG 31.1

9. Je, hali ya kiroho ya Uingereza ilikuwaje karne moja baadaye? Ni Wanamatengenezo gani walioinuka wakati huo? Je! Charles Wesley aliongozwaje kutambua ubatili wa kazi zake mwenyewe kwa wokovu? 253:1-3 [290:3-291:1] Wesley aliabudu wapi kwanza? 253:1-254:2 [290:3-291:3] GC-SG 31.2

10. Je, maisha ya Kikristo thabiti ya Wamoravian yalimshawishije John Wesley? 254:3-256:1 [292:1-293:2] GC-SG 31.3

11. Je, matokeo ya wasiwasi wa Wesley kuhusu nuru ya neema ya Mungu yalikuwa yapi? Ni kwa msingi gani tofauti sasa alidumisha kazi zake nzuri za zamani? Ni nini kilipelekea jina la "Wamethodisti"? 256:1-4 [293:2-294:1] GC-SG 31.4

12. Je, Whitefield, Wesley na wenzao walizisawazishaje tofauti ndogo katika mafundisho kati yao? 257:3 [295:1] GC-SG 31.5

13. Je, kuna visa vingapi vya ulinzi wa Mungu dhidi ya ghasia za magenge ya watu ambavyo Wesley alivirekodi? Je, ni viongozi peke yao ndiyo waliteswa? Je, walikuwa na ulinzi kutoka serikalini? 258:1-259:2 [295:2-296:2] GC-SG 31.6

14. Wesley alipambana na makosa gani mawili maarufu, naye alileta hoja gani dhidi yao? Je, makosa kama haya yameenea leo? 260:2-264:1 [297:1-301:1] GC-SG 31.7

15. Ni mafanikio gani ya ajabu yaliyonufaisha kazi ya Wesley wakati wa uhai wake? Ni nini kinachoweza kusemwa juu ya ushawishi wake zaidi ya kile kilichoonekana? Kariri sentensi ya kumalizia. GC-SG 31.8

**Sura ya 15 - Biblia na Mapinduzi ya Ufaransa**

1. Ni nini umuhimu wa matamko yafuatayo, yanayopatikana katika unabii wa Ufu. ll:2-11: "mji mtakatifu"; "miezi arobaini na miwili" 266:2, 3 [304:3, 4] "mashahidi wawili" 267:1 [305:2] "tabiri . . . kuvikwa nguo za magunia" 267:2; 269:1 [307:1; 307:2] "mnyama kutoka kuzimu" 268:3 [306:3] "mji mkuu" 269:2 [307:2] "mizoga . . . siku tatu na nusu" 273:2-274:2; 287:1 [312:3-313:2; 328:1] GC-SG 32.1

2. Ni onyo gani linalotolewa dhidi ya kupotosha maana iliyo wazi ya Maandiko? 268:1, 2 [306:1, 2] GC-SG 32.2

3. "Misri" na "Sodoma" husimama kwa dhambi gani maalum? 269:2, 3 [307:2, 3]
GC-SG 32.3

4. Ni matabaka gani mawili ya Wakristo ambayo yalitoa ushahidi kwa ajili ya Kristo, na hao walitesekaje kwa ajili ya imani yao? 271:2; 273:1 [309:2-312:1] GC-SG 32.4

5. Katika “vita dhidi ya Mungu” huko Ufaransa, ni hatua gani zilizochukuliwa dhidi ya ibada ya hadharani? Biblia? Sabato? Sakramenti za ubatizo, Komunio, na ndoa? kutambuliwa kwa Mungu? Ni nini kilichukuliwa kama mbadala wa kuabudiwa au wa ibada, na kiliwekwaje kwa mtu binafsi? 273:3-276:3 [312:3-316:3] GC-SG 32.5

6. Je, kanisa linawezaje kuonyesha kwamba limewajibika kwa kuzorota kwa uhuru wa kidini, na pia limekuwa kwenye upande wa Serikali katika kukandamiza uhuru wa dhamiri wa raia? 276:4-277:2 [316:4-317:2] GC-SG 32.6

7. Je, mateso ya Wahuguenoti yalichangiaje umaskini na umasikini wa nchi? 278:1-279:2 [318:1-319:1] GC-SG 33.1

8. Ni tofauti gani zinazotolewa kati ya matakaba yanayopendelewa na wakulima maskini, na ni nini zilikuwa sababu za hali hiyo? Je matokeo yalithibitishaje kuwa kinyume cha yale yaliyotarajiwa? 279:4-281:3 [319:3-321:3] GC-SG 33.2

9. Ilipofika wakati wa watu wa kawaida kujipatia nguvu serikalini, Je, walitumiaje mamlaka yao vibaya? 282:1-284:1 [322:1-324:2] GC-SG 33.3

10. Ni kosa gani la kufisha na ambalo bado linawajibika kwa ukatili, huzuni, udhalilishaji na taabu katika ulimwengu huu? 285:2-286:1 [326:2-327:1] GC-SG 33.4

11. Ni harakati gani mbili zilizoanzishwa na Mungu wakati huu, ili kuzuia mipango ya Shetani ambayo ilionekana kama imefaulu, na kuufunulia ulimwengu kanuni Zake Mwenyewe za upendo na uhuru? 287:2-288:3 [328:1-329:4] GC-SG 33.5

12. Katika sura hii tuna onyesho la uhalisia/ukweli kwamba nguvu mbaya za Shetani zimezuiliwa na Roho wa Mungu, na ni pale tu wanadamu wanapochagua kwa makusudi kumfuata yule mwovu, ndipo ulinzi huu unapoondolewa hapo. Ukweli huu bado unaonyeshwa wazi zaidi leo. Tazama 265:1; 274:2; 282:2; 285:4-286:1 [303:1; 313:2; 322:2; 326:4-327:1] GC-SG 33.6

**Sura ya 16 - Mababa wa Imani Wasafiri/Wahujaji**

1. Suala la hekima ya “mapatano au Maridhiano” liliwagawanyaje Wanamatengenezo wa Kiingereza? Hoja ya kubishania kuhusu kuunga mkono au kupinga ilikuwa nini? Kanisa lenye mamlaka nchini lilijaribuje kusuluhisha

pambano hilo, na matokeo yalikuwa ni nini kwa walio wachache? 289:1-290:2 [331:1-332:2] GC-SG 34.1

2. Ni katika roho gani Mahujaji na Wasafiri wa imani walikubali magumu ya uhamishoni, na “mateso na kufukuzwa nchini” vilifunguaje “njia ya uhuru” kwao? (pilgrims) 290:3-291:2 [333:1-3] GC-SG 34.2

3. Ni kanuni gani muhimu ya Uprotestanti, iliwekwa ndani katika Agano la Wapuritani, iliyosisitizwa na Mchungaji John Robinson? Je, kukosa kuitambua kanuni hii kunawezaje kuonyeshwa kuwa ndiyo sababu ya madhehebu mengi leo? 291;3-292:2 [333:4-334:3] GC-SG 34.3

4. Ni kanuni gani za uhuru wa dhamiri au uhuru wa kidini ambazo kwa muda fulani zilikiukwa na mababa na wasafiri na makasisi wahujaji? Ni nani aliyekuwa wa kwanza kusisitiza uhuru kamili wa dhamiri ya mtu binafsi? Je, Alifafanuaje majukumu ya hakimu? Ni kwa kutumia maneno gani alipinga kulazimisha watu kuhudhuria kanisa? 292:3-294:2 [335:1-336:2] GC-SG 34.4

5. Je, kampeni ya uhuru wa kidini/dhamiri ilisaidia au kuzuia kufukuzwa kwa Roger Williams? 294:2-295:1 [337:1-3] GC-SG 34.5

6. Ni kanuni gani ya Katiba ya Marekani ambayo mwanadamu amepewa na Mungu kwa asili na, na kwa hivyo, iko juu ya akili ya mwanadamu kuigusa? 295:3 [338:2] GC-SG 34.6

7. Kupata makazi katika Ulimwengu Mpya na hali ya mazingira yake, viliathiriwaje na ofa ya Wakristo walioteswa katika nchi zote duniani kupewa hifadhi huko? 296:1-4 [338:3-339:3] GC-SG 34.7

8. Ni nini hutokea wakati kanisa linapofaulu kupata Upendeleo maalum katika serikali? 297:1 [341:1] GC-SG 34.8

9. Ni kwa njia gani Uprotestanti umerudia historia ya kanisa wakati wa karne za kwanza? Kwa kuwa Shetani ameshindwa tena kuufuta Ukweli kupitia mateso, amefanyaje sasa ili kupotosha makanisa yaliyoanzishwa na Wanamatengenezo? 297:3-298:2 [340:2-341:2] Taz. 42:2, 3 [46:3-47:1] GC-SG 34.9

**Sura ya 17—Wapiga Mbiu Wa Majira Ya Mapambazuko**

1. Orodhesha wahusika wa Agano waliotabiri kuja kwa Kristo, pamoja na matukio yanayohusiana nayo. Ni nani kati yao aliyesisitiza hukumu? Ufufuo? furaha kuu ya waliokombolewa? utukufu wa kuja kwa Bwana, na matukio halisi kuonekana katika maumbile ya asili? 299:1-300:3 [343:1-344:3] GC-SG 35.1

2. Ni Maneno gani chanya ya Kristo yanayoongeza uhakika kwenye tumaini la kurudi Kwake mara ya pili? Nani ataandamana Naye? 301:1 [345:1] GC-SG 35.2

3. Kupitia Malaika, Paulo na Yohana, ni ushuhuda gani unaotolewa kuhusu jinsi Yesu atakavyokuja? 301:2 [345:2] GC-SG 35.3

4. Je, kuja kwa Kristo kunahusianaje na urejeshwaji wa kile kilichopotea wakati wa anguko la mwanadamu? 301:3-302:1 [345:3-346:1] GC-SG 35.4

5. Ni matukio gani ya pekee ambayo yameleta hamu kubwa ya kurudi kwa Kristo miongoni mwa wafuasi Wake? 302:2-4 [346:2-4] GC-SG 35.5

6. Wanamatengenezo walishangiliwaje katika kazi yao na "tumaini lenye baraka?" 303:1-4 [347:1-4] GC-SG 35.6

7. Ni nini kilichokuwa cha kwanza kabisa kati ya "ishara" zilizoahidiwa za kukaribia kwa mwisho wa wakati? 304:1-305:2 [348:2-350:1] GC-SG 35.7

8. Onyesha kwamba ile siku ya giza ya mwaka 1780 ilitimiza unabii kuhusu wakati wa mwisho? Je, ilitambuliwa na wengi walioiona kuwa imetimiza unabii hususani wa Maandiko? 306:1-308:1 [350:2-354:1] GC-SG 36.1

9. Hali ya kiroho ya kanisa ilikuwaje wakati ishara za kuja kwa Kristo zilipoanza kuonekana? Onyesha kwamba hili pia lilikuwa somo la unabii? 309:1 [354:3-355:1] GC-SG 36.2

10. Ni sehemu gani za kiunabii kuhusiana na "siku ya Bwana" zinazoleta kwetu mwito wenye nguvu wa kuamka kutoka katika uchovu wa kiroho? 310:1-311:1 [355:2-356:3] GC-SG 36.3

11. Ni ujumbe gani wa onyo uliopaswa kutolewa wakati huo, nao ulitolewa na tabaka gani la wanadamu? 311:2-312:3 [356:4-357:4] GC-SG 36.4

12. Ni watu wa Mungu wangapi waliokuwa wakimtazamia Kristo, wakati wa kuja Kwake mara ya kwanza? Je, viongozi wa kidini walikuwa na mtazamo gani wakati huo kwa unabii wa kuja Kwake? Ni makundi gani ya watu yalichaguliwa kutangaza kuzaliwa kwa Yesu? Je, kuna masomo gani katika uzoefu huu kwa wakati wetu tunaoishi leo? 313:1-316:1 [358:1-361:2] GC-SG 36.5

**Sura ya 18 - Mwanamatengenezo wa Marekani**

1. Ni sifa gani kitabia na ni hali gani ya maisha vilimstahilisha William Miller kuwa kiongozi mkuu wa kiroho? 317:1, 2 [363:1, 2] GC-SG 37.1

2. Kumbuka: Deism, pamoja na imani hii ya kuwa na ufahamu katika Mungu kama Ndiye sababu kuu ya ulimwengu kuwepo, katika wajibu wa wanadamu kumheshimu Yeye kwa maisha ya wema, na katika Fundisho la imani la thawabu au adhabu, iliikataa Biblia kama ufunuo wa Mwenyezi Mungu. Imani hii Ilishikilia

kwamba akili ya mwanadamu pekee ilitosha kuanzisha dini na kuwezesha maadili mema yatekelezwe, Kadiri kupingana kwake yenyewe kulivyodhihirika, vuguvugu hilo lilidumu kwa muda mfupi, na wafuasi wake ama walirudi kwenye Ukristo wa awali wa Biblia, au wakawa watu wasioamwamini Mungu, au wakana Mungu. GC-SG 37.2

3. Miller aliongozwa na hoja gani zenye kupatana na za busara katika kumkubali Kristo kuwa Mwokozi wake na kuyapenda Maandiko kwa bidii/usongo? Ni changamoto gani iliyomfanya ajifunze Biblia kwa dhati na bidii? 318:2-319:3 [364:2-365:2] GC-SG 37.3

4. Ni njia gani za kujifunza Biblia zilizochangia nuru akilini mwake? Ni vitabu gani vilivyopuuzwa ambavyo yeye alivisoma, na je, alifikia hitimisho gani? 320:1, 2 [366:1, 2] GC-SG 37.4

5. Fundisho la milenia ya muda lilipata mahali gani katika mafundisho ya Kikristo, na likawa na matokeo gani mabaya? Ni Kweli zipi kuhusu matukio yanayohusiana na ujio wa pili wa Kristo ambazo Miller alizigundua tena? 321:1-323:1 [367:1-369:1] GC-SG 37.5

6. Kumbuka: Daniel Whitby (1638-1726), mwanatheolojia mashuhuri wa Uingereza, na ambaye aliandika vitabu vingi vya hali ya kutatanisha, alikuwa wa kwanza kuweka wazi maoni ya kwamba Milenia haikuwa "utawala wa watu waliofufuliwa kutoka kwa wafu, lakini ustawi wa kanisa kwa utukufu kwa miaka elfu moja baada ya kuongolewa kwa Wayahudi,"- "Paraphrase and Commentary of the New Testament," 1703, Vol. II, 7th ed., p. 687. GC-SG 37.6. GC-SG 37.6

7. Miller aliongozwaje kutafuta unabii ambao unaweza kuonyesha nyakati zinazohusiana na siku za mwisho? Ni unabii gani hasa ulionekana kwake kufunua wakati wa Ujio wa pili wa Yesu? 323:2-324:3 [369:2-370:2] GC-SG 37.7

8. Kumbuka: Kama msaada wa kuweka akilini maelezo ya zile siku 2300, itakuwa msaada kwa msomaji kuunda, kwa matumizi yake mwenyewe, chati yenye mfululizo wa matukio yanayoufuatana kutokana na tarehe (Kronolojia au chati ya wendo) (Chronological chart) 326:1-329:2 [371:3] -375:2] GC-SG 38.1

9. Ni miaka mingapi ilipita toka Miller aanze kuchunguza/kujifunza Biblia hadi alipotoa tangazo lake la kwanza la imani hadharani? Kipindi hiki kimegawanywa katika mgawanyiko gani? 329:2-330:2 [376:2-379:2] GC-SG 38.2

10. Alianza kazi yake ya umma akiwa na ulemavu gani, kuhusiana na umri, uzoefu, na ujasiri? Alipataje miadi ya kuhubiri? Je, makanisa wakati huu yalijihusisha vipi na kazi na mafundisho yake? Alisaidiwa vipi kifedha? 331:2-332:2 [380:2-381:3] GC-SG 38.3

11. Unabii wa aina gani mbili ulitimizwa wakati wa mahubiri ya Miller yaliyotoa msukumo uliojitokeza wazi kwenye vuguvugu ya Ujio wa Pili wa Yesu? 333:1-335:1 [382:1-384:4] GC-SG 38.4

12. Kazi yake ilipingwaje na wachungaji maarufu waliopendwa na watu, watu wasiomwogopa Mungu, na baadaye, viongozi wa kanisa? Miller alitoa mwito gani unaofaa kwa makanisa? 335:3-337:2; 340:2 [385:2-387:2; 390:2] GC-SG 38.5

13. Ni mambo gani yanaweza kulinganisha kati ya siku za Nuhu na siku za mwisho? 337:3-339:1 [387:3-388:3] GC-SG 38.6

14. Ni nini kinachoonyeshwa katika kisa cha mtu anayedai kuwa yeye ni Mkristo na kisha hatamani kuja kwa Kristo mawinguni kwa mara ya pili?
339:2-340:1 [338:4-389:2] GC-SG 38.7

15. Kwa nini Shetani anajitahidi kuwazuia watu wasijifunze kitabu cha Ufunuo, Je, amefanikiwa kwa kiasi gani? 341:2-342:1 [391:1-4] GC-SG 38.8

**Sura ya 19 - Nuru Yapenya Gizani**

1. Ni kielelezo gani kinachojitokeza na kinachotolewa kuhusu Ukweli kwamba wanadamu ambao Mungu huwatumia kama vyombo Vyake kufanya kazi maalum, mara nyingi huwa na mawazo pungufu kuhusiana na makusudi Yake? 344:2, 3 [394:2, 3] GC-SG 39.1

2. Kando na mapungufu ya asili ya akili ya mwanadamu, ni hali gani ambayo mara nyingi imesababisha kushindwa, hata na watumishi wa Mungu katika kuelewa jumbe Zake? 345:1 [395:1] GC-SG 39.2

3. Angalia ulinganifu ufuatao katika uzoefu wa wanafunzi na wale ambao, kabla ya 1844, walihubiri ujumbe wa Ujio wa Pili wa Masihi: (1.) Kufanana kwa ujumbe; (2.) Kuhusu sehemu mbili za kipindi kimoja cha unabii; (3.) Akili zilizopofushwa na makosa ya muda mrefu; (4.) Ingawa ni sahihi kwa wakati wa kiunabii, kutoelewa asili ya tukio yaani kuanza kazi ya Hukumu mbinguni; (5.) Alitimiza Mapenzi ya Mungu; (6) Kukata tamaa; (7) Mungu aliwafunga macho ili mema zaidi yatokee; (8.) Kupitia maombi na kujifunza, waliongozwa kwenye nuru na ufahamu/uelewa. 345:1 - 352:3 [395:1-403:3] GC-SG 39.3

4. Ni kwa njia gani ujumbe wa Kuja kwa Yesu mara ya pili na mtihani wa kukatishwa tamaa vililitakasa kanisa? 353:1-354:2 [404:1-405:1] GC-SG 39.4

**Sura ya 20 - Mwamko Mkuu wa Kidini**

1. Changanua ujumbe wa Malaika wa kwanza wa Ufunuo 14:6, 7, ukionyesha tabia tukufu ya kazi hiyo, kasi yake na mapana katika harakati zake ulimwenguni, na wakati unapofika. 355:1-356:2 [407:1-408:3] GC-SG 40.1

2. Kuinuka kwa vuguvugu la Majilio ya Yesu kunafananaje na wakati wa matengenezo makubwa kwa namna inayoonyesha asili ya Bwana ndani ya yote mawili? 357:1 [409:1] GC-SG 40.2

3. Ni Myahudi gani aliyeongoka na kusafiri kama mtangazaji wa kwanza wa ujumbe wa Ujio wa Yesu katika nchi nyingi za Ulaya, Afrika na Asia? Ni hatua gani zilizoashiria maendeleo yake kutoka kwenye Dini ya Kiyahudi hadi Uprotestanti? 357:2-358:1 [409:2-410:2] GC-SG 40.3

4. Aliongozwa kufuata maoni gani kuhusu matukio yanayohusiana na kuja kwa Kristo, na kukokotoa kwake kulilinganaje na kule kwa William Miller? Alikutanaje na wale walionukuu Mathayo 24:36, kwa kuonyesha kwamba wakati wa ujio wa Pili wa Yesu haungeweza kujulikana? 359:1-3 [411:1-3] GC-SG 40.4

5. Ni miaka mingapi Wolff alitumia katika safari zake? Je, ni ufahamu gani alipewa na John Quincy Adams? Alifanya kazi katika nchi gani na kati ya watu gani? Ni miongoni mwa watu gani alihubiri imani ya ujio wa pili wa Kristo? 360:2-361:1 [412:2-414:1] GC-SG 40.5

6. Ujumbe ulihubiriwa mapema kiasi gani huko Uingereza? Vuguvugu za huko zilitofautiana kwa namna gani na zile za Marekani? Jinsi gani Uingereza iliathiriwa na vuguvugu hiyo? 362:2 [414:3] GC-SG 40.6

7. Tambua na fuatilia ushawishi wa Lacunza, Bengel, Gaussen. Je, mpango wa kufikia wazazi kupitia watoto unastahili kufanyiwa kazi leo? 363:1-366:1 [415:1-418:1] GC-SG 40.7

8. Watu waliposhindwa au walipokatazwa kuhubiri, Mungu alitumia njia gani (1.) katika nyua za hekalu la Yerusalemu, katika siku za Kristo (2.) katika nchi za Skandinavia? Na Kutangaza ujumbe wa Ujio wa Yesu kwa mara ya pili 366:2-367:2 [418:2-419:3] GC-SG 41.1

9. Je, kazi ya wachungaji na walei ilikuwa na nguvu gani katika tangazo lenye nguvu la ujio wa Yesu huko Amerika? 368:2 [420:2] GC-SG 41.2

10. Je, yatupasa tusome ujumbe wa Ujio wa Yesu kama historia tu, au kama tukio lililoahidiwa wakati ujao lenye ujumbe wenye matokeo mazito? 369:1-3; cf. 611:1-612:2 [421:1-422:2; cf. 690:1-691:3] GC-SG 41.3

11. Ni Maneno gani ya Kristo yaliyotumiwa vibaya na bado yanatumiwa kupinga tamko Lake lingine lililo wazi? Je, ushuhuda wa Paulo ni upi kuhusu jambo hili? 370:1-372:1 [423:1-424:2] GC-SG 41.4

12. Kwa nini kukataliwa kwa ujumbe huo kulikuwa kukataa kwa makusudi nuru ya Mwenyezi Mungu, wakati ambapo kama tujuavyo sasa, Miller na wenzake

kuna kitu ambacho walikikosea? Ni nia gani isiyofaa iliyowafanya wengi kuukubali ujumbe huo? Je, hao waliathiriwaje na hali hiyo ya kukata tamaa? 373:3-374:2 [427:1-3] \GC-SG 41.5

**Sura ya 21 - Onyo Lakataliwa**

1. Miller alikuwa na mtazamo gani kuhusu uanzishaji wa madhehebu mapya ya kidini? Je, tangazo la ujumbe wa majilio liliathirije ukuaji wa makanisa? 375:1, 2 [429:1, 2] GC-SG 42.1

2. Ni hali gani iliyobadilika na iliyosababisha kutengwa kwa Waadventista wengi kutoka kwa makanisa yao ya zamani? 376:1 [430:1] GC-SG 42.2

3. Hali ya kiroho ya makanisa ingeathiriwaje kimantiki kufukuzwa au kujiondoa kwa washiriki wale waliopenda ujio wa Kristo? Ni ushuhuda gani wa kisasa unaothibitisha viashiria vya kuporomoka kwa "ghafla na alama" katika maisha ya kiroho? 376:2-377:2 [430:2-451:2] GC-SG 42.3

4. Ni matokeo gani yenye kuhuzunisha yanayofuata kukataa kwa makusudi Kweli ya Biblia? Kanuni hii ilionyeshwaje kwa Wayahudi katika siku za Kristo, na tangu wakati huo? 377:3-378:2 [431:3-432:2] GC-SG 42.4

5. Ujumbe wa Malaika wa kwanza ulikuwa na mpango gani, na wale walioukubali walipata matokeo gani yenye baraka? 379:1-3 [433:1-3] GC-SG 42.5

6. Ni sababu zipi zilizopelekea chuki ya jumla na kutoamini ujumbe wa majilio? Je, kukataliwa kwake kulihusisha nini? 380:1, 2 [434:1, 2] GC-SG 42.6

7. Neno "Babeli" kama linavyotumiwa katika kitabu cha Ufunuo linaonyeshwaje kuwa Ishara au alama ya kanisa lisilokuwa na uaminifu? na ni Maandiko gani yanayolitambulisha kanisa hili na Rumi? 381:1-382:3 [434:3-436:2] GC-SG 42.7

8. "Mabinti" ni nani, na ni mambo gani ya hakika yanayoonyesha kwamba wao ndio hasa wanaotajwa katika ujumbe wa malaika wa pili? 382:3-385:1 [436:3-439:1] GC-SG 43.1

9. Viwango vya sasa vya makanisa maarufu vinalinganishwaje na maadili ya waanzilishi wao? 385:2-388:1 [439:2-442:3] GC-SG 43.2

10. Ni nini kinachofananishwa na "divai"? Ni kwa jinsi gani Biblia inaweza kuzuiwa kwa njia ya hila kama jinsi ambavyo inaweza kuzuiwa kwa Amri? 388:2-389:1 [443:1-3] GC-SG 43.3

11. Kuna uhusiano gani kati ya tangazo la anguko la Babeli katika Ufunuo 14:8 na katika sura ya 18:4, 5? Kutokana na hali kama zilivyoendelea katika nusu

karne tangu hili lilipoandikwa, Je, jambo hili linathibitisha kuhusu utabiri uliotolewa wakati huo? 389:2, 3 [444:1, 2] GC-SG 43.4

12. Tunapokaribia upeo wa uasi wa imani wa leo, ni maoni gani yenye matumaini yanayotolewa ili kutia moyo utendaji wa kimishenari? 390:2, 3 [445:1, 2] GC-SG 43.5

**Sura ya 22—Unabii Watimizwa**

1. Ni mafungu gani vya Maandiko yalileta faraja kwa waamini waliokatishwa tamaa, walipoendelea kutafuta nuru zaidi? 391:1-394:1 [447:1-451:2] GC-SG 44.1

2. Adui wa nafsi alijaribuje kuleta shutuma juu ya harakati hiyo kipindi cha “wakati wa kungojea”? 395:1-396:2 [452:1-453:2] GC-SG 44.2

3. Ni matukio gani ya wakati uliopita yanayoonyesha kwamba wakati Bwana anapoendeleza mbele vuguvugu lenye nguvu, watu wenye kupitiliza kwa ushupavu usio na busara, wanaweza kutazamiwa kujiunganisha na vuguvuvu hilo? 397:1-398:2 [454:1-455:2] GC-SG 44.3

4. Ni uvumbuzi gani katika Maandiko ulioongoza wengi kutazamia mwisho wa siku 2300 kwenye vuli ya 1844? Je, Wakati wa ugunduzi wao, ulilipaje tangazo hilo jina la “kilio cha usiku wa manane”? 398:3, 4; 400:1 [455:2, 3; 457:1] GC-SG 44.4

5. Je, Uchunguzi wa siku kuu za majira ya kuchipua majani, na uhusiano wa kifo na ufufuo Wake Kristo vilionyeshaje tarehe ya 22 Oktoba 1844? 399:1-4 [456:1-4] GC-SG 44.5

6. Je, vuguvugu la “kilio cha usiku wa manane” zililinganishwaje na vuguvugu la awali za nguvu za kiroho, na utendaji wa kimishenari? 400:2-403:1 [457:2-459:3] GC-SG 44.6

7. Kufuatilia hali hii ya pili ya kukatishwa tamaa, ni tabaka gani tatu za wafuasi waliokataa kuwa na uhusiano na vuguvugu la Waadventista? 403:3 [460:2] GC-SG 45.1

8. Rudia uzoefu sawia wa wanafunzi na wale waliotangaza ujio wa pili wa Bwana wakati wa Miller (351:1, 2 [402:1, 2], na uangalie mambo ya kufanana yaliyokuzwa zaidi katika kukatishwa tamaa kwao. 404:1-405:2 [460:3-462:1] GC-SG 45.2

9. Ni mafungu gani ya Maandiko ndiyo yaliyowasaidia wale waliokatishwa tamaa kupata kitia-moyo na uhakikisho zaidi kwa ajili ya wakati ujao? 407:1-408:1 [464:1, 2] GC-SG 45.3

**Sura ya 23 - Patakatifu ni nini?**

1. Je, Miller na wenzake peke yao ndio waliohusika katika kutoelewa maana ya "Patakatifu" kama inavyotumiwa katika Danieli 8:14, ambayo iliongoza kwenye kutakaswa kwake kutazamwa kuwa kunahusishwa na ujio wa Pili wa Yesu? 409:1 [467:1] GC-SG 46.1

2. Umuhimu wa uhalisia huu haupaswi kupuuzwa. Kwa sababu ya kosa hilo, wakosoaji wa vuguvugu hilo wanadai kwamba upinzani dhidi yake ulihalalishwa na ulimwengu wa Kikristo. Lakini ukweli huu unabakia kwamba mashambulizi dhidi ya msimamo wa Miller yalikuwa kwa misingi mingine, ambayo haikuwa ya Kimaandiko, na kwamba hakuna hata mmoja wa wapinzani wake aliyeona au kutaja dhana hii potofu ya kimsingi. Katika majaliwa Yake Mungu aliacha ugunduzi wa Ukweli wa Patakatifu uunde msingi wa ujumbe utakaotangazwa kwa ulimwengu na kanisa la masalio. GC-SG 46.2

3. Waumini wa Ujio wa Yesu baada ya kukatishwa tamaa, waligawanywaje katika makundi mawili yenye mawazo tofauti kuhusiana na uzoefu wao na nyakati za unabii? Wale walioongozwa kujifunza hili na ambao bado waliamini kwamba Mungu alikuwa amewaongoza waliishia kufanya nini? 409:2-410:3 [468:1-469:1] GC-SG 46.3

4. Mawazo yao yalielekezwa kwa nyaraka gani ya Agano Jipya? Ni uthibitisho gani waliuona  kule mbinguni kama ndiyo mahali halisi pa mfano, wa Patakatifu pa duniani? 411:1-413:3; 417:1 [469:2-471:4; 475:1]. GC-SG 46.4

5. Danieli na Yohana waliona sehemu gani za hekalu la mbinguni na huduma zake katika njozi? 414:2, 3 [472:2, 3] GC-SG 46.5

6. Kupitia funzo la Patakatifu, wanafunzi wa Biblia waliongozwaje kwenye dhana mpya za utakatifu wa Sheria ya Mungu? 415:2 [473:2]  GC-SG 46.6

7. Ni unabii gani wa Agano la Kale unaoelekeza kwa Kristo kama kuhani mwombezi wetu katika Patakatifu pa mbinguni? 415:3-416:4 [473:3-474:3] GC-SG 46.7

8. Ni nini kilitumika kutakasa katika  huduma ya Patakatifu? Ni Andiko gani linaloonyesha kwamba hata mbinguni, kuna hitaji la "kutakasa"? Ni kwa njia gani mbili dhambi zilihamishwa kutoka kwa mwenye dhambi aliyetubu hadi Patakatifu pa duniani? 417:2-418:1 [475:2.-476:1]  GC-SG 47.1

9. Hilo ndilo lilikuwa kusudi la ibada maalum katika siku ya upatanisho. Damu ya dhabihu gani ililetwa katika mahali Patakatifu pa Patakatifu? Baada ya yote kutakaswa, yote yaliyokuwa yanahusu Patakatifu, ni tabia gani kilifanywa na

dhambi ambazo zilikuwa zimeungamwa katika mwaka huo? 418:2-420:1 [476:2-479:1] GC-SG 47.2

10. Wengine wamehoji kwamba damu inawezaje kutumika kutia unajisi na kutakasa wakati huo huo? Hili litaonekana kuwa linawezekana pale itakapobainika kuwa damu ya dhabihu ya dhambi ilikuwa kwa njia ya uhamisho wa dhambi, iliyotiwa unajisi. Hakuna dhambi iliyoungamwa juu ya kichwa cha mbuzi siku ya upatanisho. Inachukua dhabihu zote mbili kumwakilisha Kristo kama mbeba dhambi (mchukua-dhambi), na Kristo kama Yeye Asiye na dhambi. Kwa sababu uovu haukuonekana ndani Yake, hivyo Yeye Aweza kuwatakasa wote na uchafu wote. GC-SG 47.3

11. Kristo aliingia lini kufanya kazi Yake kama Kuhani Mkuu, na ni wakati gani unashughulika na huduma Yake katika chumba cha kwanza? 420:2-421:2 [479:2-480:2] GC-SG 47.4

12. Ushahidi zaidi wa Kimaandiko unapatikana kwa ajili ya kuanza kwa huduma na kazi ya Kristo baada ya kupaa Kwake katika (1) unabii wa kupakwa mafuta kwa “Mtakatifu zaidi” katika kipindi cha majuma sabini (Danieli 9:24), neno la Kiebrania hapa hurejelea tu “kitu” kitakatifu, kamwe si mtu; (2) ulazima wa Kristo kuwa mmoja wa jamii ya ubinadamu Ambaye angewawakilisha, na hivyo kuwa na “huruma” inayohitajika—kuwa na hisia ya huruma kwa wenzake; (Waebrania 4:15-5:2); (3) utoaji wa dhabihu lazima utangulie huduma ya damu (Waebrania 8:3); (4) Kristo alifanywa kuwa Kuhani Mkuu kwa kiapo cha Baba (Waebrania 4:5); na kiapo hicho kilikuwa “baada ya torati,” (Waebrania 7:28). GC-SG 47.5

13. Palikuwa na mapazia mawili katika Patakatifu. Musa anayatofautisha kwa kuita la kwanza kama “linaloning’inia” (Ebr. Masak) na la pili kama “pazia” (Ebr. paroketh). Hata hivyo yote mawili yalitundikwa kwa namna ileile, nayo yalitengenezwa kwa malighafi ileile, na kutumikia kusudi lilelile, kama mlango. Paulo katika Waebrania haonyeshi tofauti kwa kutumia Neno tofauti, lakini anaporejelea pazia la ndani analiita “pazia la pili,” Waebrania 9:3. Hakuwezi kuwa na la pili bila la kwanza, na si jambo lisilo na mantiki kuelewa kwamba katika Waebrania 6:20, anarejelea pazia la kwanza, badala ya lile la pili. Ufahamu huu unaleta fungu hili kupatana na Maandiko mengine, na lilikuwa hitimisho lililofikiwa na waanzilishi waliokatishwa tamaa miaka arobaini na au 1844, na ambalo lilithibitishwa na Roho wa unabii. GC-SG 47.6

14. Ni nuru gani zaidi iliyoonekana kuhusiana na kutakaswa kwa Patakatifu na matukio ya wakati ujao kama yalipofananishwa na “mbuzi wa Azazeli”? 421:3-422:2 [480:3-481:2] GC-SG 47.7

**Sura ya 24 - Katika Patakatifu pa Patakatifu**

1. Je, nuru kutoka kwa "Patakatifu" ilielezeaje hali ya kuvunjika moyo ya 1844? Ni maandiko gani mawili, yote yakiwa mashuhuri katika vuguvugu hilo, yalipatikana kuwa yanafanana kwa maana? 423:1-424:1 [483:1-484:1] GC-SG 48.1

2. "Kuja kwa Kristo" kuna maana gani zaidi ya ujio Wake wa pili duniani ulioonekana na nabii Danieli na Malaki? Kufuatia ujio huu, ni kazi gani ya utakaso wa Kanisa iliyoonekana na Malaki, ikifuatiwa na Ujio wa Pili na utekelezaji wa hukumu? 424:2-426:1 [484:2-486:2] GC-SG 48.2

3. Kwa mwanga zaidi juu ya mfano wa wanawali wenye busara na wapumbavu, ni wakati gani ilionekana kwamba kilio cha usiku wa manane kilitolewa? Ni makundi gani mawili ya mabikira yalizungumziwa wakati huo? Ni nini kinachowakilishwa na ujio wa Bwana-arusi? Ndoa? Karamu ya Harusi? Bibi harusi? Wageni? Kurudi kutoka kwenye harusi? 426:3-427:1 [486:3-487:1] GC-SG 48.3

4. Ni kundi gani la waumini lililoingia pamoja na Kristo kwenye -harusi/ndoa? Ni katika mfano gani Yesu alifundisha kwamba kungekuwa na uchunguzi au kupimwa kwa wageni wanaoingia, lakini kabla ya ndoa halisi? Je, ni nini kitaashiria kufungwa kwa mlango wa rehema? 427:2-428:2 [487:2-489:2] GC-SG 48.4

5. Katika kipindi cha mpito, kabla ya kazi ya Patakatifu kueleweka, ni nini kiliaminika kuwa na maana ya kufungwa kwa mlango katika mfano wa wanawali kumi? Ni Andiko gani sasa linalofunua kuhusu "mlango uliofunguliwa"? 429:1-430:1 [490:1-491:1] GC-SG 48.5

6. Ni ulinganifu gani unaotolewa kati ya Wayahudi walioikataa nuru ambayo ingewaongoza kuona huduma ya Yesu katika Patakatifu pa Patakatifu pa kimbingu, na wale ambao hawakujua kwa hiari kuingia Kwake katika Patakatifu pa Patakatifu sana katika mwaka wa 1844? 430:2-431:2 [492:1-493:1] GC-SG 48.6

7. Mungu hangeweza kuwaongoza watu Wake kwa kasi zaidi ya vile ambayo waliweza kufuatilia kwa akili zao, kwani akili zao ziliangaziwa na Roho Mtakatifu walipojifunza Neno kwa bidii na kwa maombi. Wangeweza tu kufuata hatua moja baada ya nyingine katika nuru endelevu na hiki kilikuwa ni kipindi cha miaka michache, kati ya kukatishwa tamaa hadi kufikia uendelezaji kamili wa mafundisho ya msingi ambayo sasa yanashikiliwa na Waadventista Wasabato. Kipindi hiki na matokeo ya subira na imani yao yanawekwa wazi, tofauti na wale waliokana imani yao katika uongozi wa Mungu kwenye Vuguvugu la ujio wa Bwana. 431:3 [493:3] GC-SG 48.7

## Sura ya 25 - Sheria ya Mungu Isiyobadilika

1. Yohana alitangaza nini kingeonekana wakati hekalu la Mungu litakapofunguliwa mbinguni? Je, hili linapaswa kufanyika wakati gani? Je, kukubalika kwa Sabato na Waadventista watafutao Ukweli kulitimizaje unabii huu? 433:1-434:3 [495:1-497:1] GC-SG 49.1

2. Ni sababu gani iliyofichika inayopinga Kweli ambayo ilifunua huduma ya Kristo katika Patakatifu pa Patakatifu? 435:1 [697:2] GC-SG 49.2

3. Je, watu gani walitayarishwa kwa ajili ya kuja kwa Kristo kupitia ujumbe wenye sehemu tatu wa Ufunuo 14 wana sifa gani? Je, ujumbe wa kwanza unaonyeshwaje kuwa ni wito wa kuzishika Amri za Mungu? Ni Amri gani iliyokazia kwamba Mungu ni Muumba? Utunzaji wa Sabato ulimwenguni pote ungewezaje kuulinda ulimwengu dhidi ya ibada ya sanamu na Kumkana Mungu (upagani)? 435:2-437:2 [498:1-499:2] GC-SG 49.3

4. Ni nini kinachofananishwa na joka wa Ufunuo 12? Mnyama anayefanana na chui wa sura ya 13? Ni wakati gani mnyama aliye kama mwana-kondoo analetwa na kutambulishwa? Ni mambo gani mawili ambayo mwisho hutofautiana na yale yanayotangulia, na wanyama aliowaona Danieli? 438:2-440:1 [500:3-502:2] GC-SG 49.4

5. Marekani inaonyeshwaje (1) Kuhusiana na wakati, (2) Namna inavyoinuka, (3) Mahali ilipo, (4) Zile pembe mbili? 440:2-441:1 [502:3-503:1] GC-SG 49.5

6. Ni tofauti gani yenye kuonekana wazi kwa mnyama anapoonekana kwanza akipanda juu, na katika matamko yake ya baadaye? Je, kuna dokezo gani muhimu kuhusu nafasi ambayo Marekani itatenda katika siku za mwisho? Linganisha Ufunuo 5:12 na 12:9. 441:2-443:1 [505:1-506:1] GC-SG 49.6

7. Ni nini kililifanya kanisa la awali kutafuta kuungwa mkono na mamlaka ya kidunia? Kwa hiyo, ni kanisa gani lililoanzishwa, na lilitumiaje mamlaka ya kiraia? 443:2-4 [506:2-4] GC-SG 49.7

8. Ni hali gani za mapema zilizotangulia muungano wa kanisa na serikali? Ni maandiko gani yanayoonyesha kwamba hali kama hizo katika makanisa ya leo zitakuja na matokeo kama hayo? 443:5-444:1 [506:5-507:1] GC-SG 50.1

9. Makanisa ya Kiprotestanti ya aina mbambali yanaweza kuungana katika hali gani ili kushawishi Serikali kutunga sheria kwa niaba yao? Je, Serikali itakapokubali madai yao, matokeo yatakuwa nini? 444:2-445:1 [507:2-508:1] GC-SG 50.2

10. Ujumbe wa Malaika wa tatu unaonyeshwaje kuwa onyo dhidi ya kukubali madai ya "mnyama" au "sanamu" yake? Je, ni dhahiri kwa jinsi gani kwamba dai hili ni kinyume na amri za Mungu? 445:2-446:1 [508:2-509:3] GC-SG 50.3

11. Ni Amri gani ambayo imebadilishwa kwa kudhamiria? Katika nuru ya ujumbe wa kwanza, kwa nini amri hii ni ya muhimu sana? 446:1-3 [509:1-3] GC-SG 50.4

12. Ni maneno gani ya Kristo yanayokanusha madai kwamba Yeye aliibadilisha Sabato? Ni nini dai la Kanisa Katoliki kuhusu badiliko hilo, na Je, washiriki wa Uroma huonaje kukubali kwa Waprotestanti badiliko hilo? 447:1-448:3 [510:1-512:1] GC-SG 50.5 (Angalia rejelea mwisho kabisa wa Kitabu)

13. Watu watapokea "alama ya mnyama" wakati gani na chini ya hali gani? Je, kunaweza kuwa na msimamo wa kutofungamana na upande wowote katika toleo la mwisho wa amri hii (neutral)? 449:1-450:1 [512:2-513:2] GC-SG 50.6

**Sura ya 26 - Kazi ya Matengenezo**

1. Ni unabii gani katika Isaya unaoahidi baraka kwa watunza Sabato wasio Wayahudi? Muktadha unaonyeshaje kwamba ahadi hii inatumika katika siku za mwisho? 451:1, 2 [515:1, 2] GC-SG 51.1

2. Je, ni kwa jinsi gani Sheria itatiwa muhuri miongoni mwa wanafunzi wa Mungu, kama maandalizi ya kumtafuta? (Isaya 8:17) 452:1, 2 [516:1, 2] GC-SG 51.2

3. Nabii Isaya anawakaripia watu wa Mungu wapi kwa kuacha agizo Lake? Je, agizo hilo linafafanuliwaje? Ni baraka gani inayotamkwa juu ya wale wanaoirejesha? 452:3, 4 [516:3-517:1] GC-SG 51.3

4. Je, kumewahi kuwa na wakati ambapo hapakuwa na watunza Sabato duniani? Ni nini kimekuwa sehemu ya maisha yao mara kwa mara? 453:1, 2 [517:2, 3] GC-SG 51.4

5. Wahubiri wa Matengenezo ya Sabato walipowasilisha mada hii, ni vipingamizi gani viwili vya kawaida vilivyotolewa na watu? 454:1-3 [519:2-520:1] GC-SG 51.5

6. Je, kukataliwa kwa jumla kwa nuru kwenye Patakatifu kulihusishaje kundi la Waadventista kupanga tarehe hususani za Ujio wa Yesu? Je, kutoa tarehe kamili ya wakati wa ujio wa Yesu kunasaidiaje makusudi ya Shetani? 456:1-457:1 [521:1-522:1] GC-SG 51.6

7. Ni kwa njia gani uzoefu wa Waadventista waliofuata 1844 ulikuwa sawa na ule wa Israeli kule Kadesh-barnea? 457:2-458:1 [522:2-523:1] GC-SG 52.1

8. Roho ya kutovumilia imani za wengine itabebwa na wapinzani hadi kufikia kilele kipi? Je, upinzani au mateso ni kisingizio cha kukataa ujumbe wa Mungu? 458:2-459:2 [523:2-524:2] GC-SG 52.2

9. Ni wangapi wameitwa kwenye jukumu zito la kuwa walinzi? Ni hoja gani pekee isiyoweza kupingwa dhidi ya Ukweli? 459:3-460:2 [524:3-525:2] 10. Kariri Isaya 51:7, 8. GC-SG 52.3

**Sura ya 27 - Uamsho wa Kisasa**

1. Ni alama gani za uongofu wa kweli daima zimefuata mahubiri ya uaminifu ya Neno la Mungu? 461:1-528:3 [527:1-528:3] GC-SG 53.1

2. Je, uamsho maarufu au bandia hulinganishwaje na uamsho wa kweli wa kiroho, kuhusu (1) wito unaofanywa; (2) matokeo katika maisha ya waongofu; (3) kudumu kwa kazi ya neema? 463:1-3 [529:1-3] GC-SG 53.2

3. Kwa kutazamia uamsho na nguvu za pentekoste zilizoahidiwa miongoni mwa watu wa Mungu, Shetani anafanyaje kazi kuwadanganya wale ambao wakati huo wataitwa watoke Babeli? 464:1 [530:1] GC-SG 53.3

4. Mkristo ana ulinzi gani dhidi ya udanganyifu kwa maonyesho bandia ya nguvu za Roho Mtakatifu? 464:2 [530:2] GC-SG 53.4

5. Ni mafundisho gani maarufu, na ambayo yanapendwa na watu lakini yana hatari na huwajibika kuleta viwango vya chini vya utauwa kwa sababu ya makosa yahusuyo utakaso wa kweli? Ni hatari gani inayofanana na hiyo na iliyotambuliwa na Prof. Edward Parks? 465:1-3 [531:1-3] GC-SG 53.5

6. Ni Maandiko gani yanapinga fundisho kwamba Kristo alibatilisha Sheria, au kwamba kuna mgongano kati ya Sheria na injili? 466:1-467:1 [532:1-4] GC-SG 53.6

7. Je, dhambi imeleta mabadiliko gani ndani ya moyo wa mwanadamu katika mtazamo wake kuelekea Sheria ya Mungu? Je, ni sehemu gani muhimu ambayo Sheria hufanya kwa wongofu? Je! Injili inaongeza vipi kile ambacho Sheria haiwezi kufanya? 467:2-468:1 [533:1-4] GC-SG 53.7

8. Je, ni nini sababu ya kuongezeka kwa uongofu wa juu juu? (Laodikia) 533:2 [534:1] GC-SG 53.8

9. Fafanua utakaso wa Biblia. Je, yule aliyetakaswa atakuwa huru kutokana na majaribu? Je, kazi ya utakaso ni ya papo hapo? Ni katika njia zipi tatu za uwongo kuna tofauti zinazoonekana katika maisha ya Musa, Danieli, Ayubu, Isaya, na Paulo? 469:3-471:3 [535:1-537:1] GC-SG 53.9

10. Mtazamo gani kati ya Uhusiano wa imani na matendo ni mambo ya dhana za kufikirika tu? Ni nini matokeo ya kuipenda na kuitunza dhambi tunayoijua? Je, madai ya kutokuwa na dhambi ni ushahidi wa nini? 472:1-473:1 [537:2-538:2] GC-SG 53.10

11. Je, ni utendaji gani unaohusu utakaso? Ni mazoea gani ya kawaida yaliyo kati ya "tamaa za mwili zipiganazo na nafsi"? 473:2-475:2 [538:3-540:3] GC-SG 53.11

12. Mkristo anaweza kufikia viwango vya juu kwa kiasi gani? Ni mpango gani ambao Mungu ameufanya ili kufanya tukio hili liwezekane? 475:3-477:1 [541:1-542:2] GC-SG 53.12

13. Furaha inayo sehemu gani katika uzoefu wa Mkristo? Ni ahadi zipi na uzoefu ambao utayatafanya maisha yake yawe yenye furaha? Kwa nini matunda haya ya utakaso yanaonekana kwa nadra sana? 477:2-478:3 [542:3-543:3] GC-SG 53.1

**Sura ya 28 - Hukumu ya Upelelezi**

1. Katika maono ya Danieli ya Hukumu ni nani Ndiye alikuwa msimamizi? Mashahidi ni akina nani? Ni kumbukumbu gani zinatumika? Nani analetwa kama Wakili wa mwanadamu? Ni nini alipewa mwishoni mwa kazi Yake kama Mpatanishi? Tukio hili liko wapi, na saa ngapi? 479:1-3 [545:1-546:1] GC-SG 54.1

2. Katika aina na mfano, ni kesi gani zinazozingatiwa wakati wa Siku kuu ya Upatanisho? Ni aina gani ya vitabu vinatumiwa, na je, sisi tunajua nini kuhusu utunzaji wa kumbukumbu? 480:1-482:1 [546:2-547:3] GC-SG 54.2

3. Maisha ya wanadamu yanahukumiwa kwa kipimo gani? Je! Ni malipo gani wanapewa wale wanaopatikana kuwa wanastahili? Mtenda dhambi aliyetubu anawakilishwa na nani? 482:1-3 [548:2-4] GC-SG 54.3

4. Kazi ya uchunguzi inafanywa kwa ukamilifu/kina kwa kadiri gani katika mahakama ya mbinguni? Je, ni lini dhambi za wanadamu husamehewa? GC-SG 54.4

Je, dhambi zinafutwa lini? Ni nini kinachosemwa katika Ezekieli kuhusu haki ya wale waliorudi nyuma na wasiotubu? 483:1, 2 [549:1, 2] GC-SG 54.5

5. Hatua ya mwisho ya kufutwa kwa dhambi iliyoungamwa na kusamehewa ina sharti la kuendelea kuwa mwaminifu na hii inafunzwa waziwazi na Kristo katika mfano wa mtumishi asiye na huruma. Angalia Mathayo 18:23-25. GC-SG 54.6

6. Je, Yesu, kama Wakili wetu, anafanya maombezi kiasi gani kwa niaba ya wateja Wake? Ni mashtaka gani ambayo yanayotolewa na mshtaki wa watu wa Mungu, na yanashugulikiwaje? Ni masharti gani ya ahadi ya Agano jipya yatatimizwa kikamilifu? 483:3-485:1 [549:3-551:1] GC-SG 54.7

7. Ni sababu gani zimetolewa kuhusu "kwa nini Hukumu ya uchunguzi na kufutwa kwa dhambi lazima vitendeke kabla ya ujio wa Pili Bwana? Ni nani basi anayewajibika kwa hatia ya dhambi za wenye haki? Kwa nini hii ni haki? 485:2, 3 [551:2, 3] GC-SG 54.8

8. Nini yatakuwa matokeo ya mtu anayethamini dhambi ambazo hazijaacha? Mwenendo wetu ungeathiriwaje ikiwa sikuzote tungezingatia matukio ya hukumu? Ni maswali gani yanapendekezwa kwa kila mmoja wetu katika kujichunguza mioyo yetu wenyewe? 486:1-487:3 [552:1-553:3] GC-SG 55.1

9. Kwa nini ni muhimu masomo ya Patakatifu na hukumu ya uchunguzi lazima yaeleweke kwa undani? Je, kazi ya Kristo kama mtetezi/mwombezi Kristo na kifo Chake inalinganishwaje katika umuhimu? 488:2-489:1 [554:1-3] GC-SG 55.2

10. Shetani ana mpango gani kuzuia jitihada za Kristo za kuwapatanisha watenda-dhambi? 488:1, 489:2 [554:1, 555:1] GC-SG 55.3

11. Waisraeli waliamriwa kwa jinsi gani waadhimishe siku ya upatanisho? Je, hii inatupendekezea mafundisho gani katika siku hizi? Je, hukumu ya uchunguzi inahusiana vipi na kufungwa kwa mlango wa rehema? 489:3-491:2. [556:1-557:3] GC-SG 55.4

**Sura ya 29 - Chimbuko la Dhambi**

1. Uwepo wa dhambi na uovu unaleta maswali gani kuhusu tabia ya Mungu? Dhambi ni nini? Je, ni jinsi gani Mungu anathibitishwa kwamba hana hatia kutokana na shitaka la kuwajibika kwa uwepo wa dhambi? 492:1, 2 [559:1-560:1] GC-SG 56.1

2. Amani na furaha katika sayari zote inategemea nini? Ni kanuni gani inapaswa kutawala utii wa viumbe vyote? 493:1, 2 [560:2, 3] GC-SG 56.2

3. Eleza nafasi ya asili ya yule ambaye dhambi ilianzia kwake. Je, mwanzo wa kuasi kwake ulikuwa nini? Je, alienda mbali kiasi gani? Je, ni jitihada gani zilizofanywa ili kumrejesha, na matokeo yake yalikuwa nini? 493:3-494:2 [561:1-3] GC-SG 56.3

4. Nia na malengo ya Lusifa yalikuwa yapi? Je, haya malengo yalijificha vipi, na kwa uwasilishaji potofu alitafutaje kupata huruma kwa ajili ya matamanio yake ya ukuu? 495:2, 3 [562:2, 3] GC-SG 56.4

5. Je, alipewa kipindi gani cha rehema, na ni ofa gani zilizotolewa kwake? Akiwa amejitoa kikamilifu kwa uasi, alichukua hatua gani zaidi kuhalalisha mwenendo wake mwovu? 495:3-496:1 [562:1, 2] GC-SG 56.5

6. Kwa nini Mungu aliruhusu uasi uendelee kwa muda mrefu bila kuzuiwa? 497:1-498:2 [564:1-565:2] GC-SG 56.6

7. Onyesha jinsi Mungu alivyoshughulika na dhambi inavyopaswa na kwamba jambo hilo likawa ulinzi wa daima kwa dhambi kurudiwa tena mahali popote pale, katika sayari zote. 498:3-499:1 [565:3-566:1] GC-SG 56.7

8. Shetani na malaika zake walitoa mashtaka gani zaidi walipohukumiwa kufukuzwa kutoka mbinguni? Shetani alitangaza kusudi gani baada ya hapo? 499:2, 3 [566:2-567:1] GC-SG 56.8

9. Ni kwa mambo gani Uasi uliofanyika duniani, unafanana na uasi wa mbinguni? 500:1-3 [567:2-4] GC-SG 56.9

10. Ni hoja gani ndiyo yenye nguvu zaidi dhidi ya mashtaka ya Shetani? Ni lini tabia yake ilifichuliwa kikamilifu? Kristo alifunuliwaje kwa njia tofauti na Shetani? 500:4-502:3 (567:4-570:1] GC-SG 56.10

11. Je, kifo cha Kristo kinaonyeshaje kutobadilika kwa sheria ya Mungu? 503:1 [570:2] GC-SG 56.11

12. Mungu hatimaye atahesabiwa kuwa ana haki gani katika kutekeleza hukumu juu ya dhambi? Tunapewa uhakikisho gani kuhusu furaha ya wakati ujao? 503:2-504:1 [571:1-3] GC-SG 56.12

**Sura ya 30 - Uadui kati ya Mwanadamu na Shetani**

1. Je, uelewa wa wanadamu ulikuwa wa kiasi gani kuhusiana na tamko la Mungu kwamba ataweka uadui kati ya uzao wa mwanamke na Shetani? Kama ahadi hii isingelikuwepo, ni uhusiano gani ungekuwepo kati ya Shetani na wote wanaokubali majaribu yake? 505:1-3 [573:1-574:1] GC-SG 57.1

2. Ni nini sababu ya uadui wa Shetani dhidi ya jamii ya wanadamu, na uadui huo unaonyeshwaje? Je, ni kwa jinsi gani ya pekee uadui huu umepandwa kwa mwanadamu dhidi ya Shetani? 506:2, 3 [574:2, 3] GC-SG 57.2

3. Ni nini ilikuwa siri ya uadui uliooneshwa wazi na Wayahudi dhidi ya Yesu? Na uadui dhidi ya wafuasi Wake uliodhihirishwa na wale wenye dhambi? 506:3-507:2 [574:4-575:2] GC-SG 57.3

4. Je, Shetani anafaidika kwa vipi watu wakiwa wajinga na wasipoamini uwepo wake na hila zake? 507:2-508:1 [575:3-577:1] GC-SG 57.4

5. Je, kuna tofauti gani kati ya moyo ambao haujazaliwa upya na moyo uliofanywa upya? Ni njia gani kwa kawaida hukaribisha majaribu? 508:2-509:1 [577:2-578:1] GC-SG 57.5

6. Je, kuwa na talanta, elimu na utamaduni vinapaswa kudharauliwa na Mkristo mnyenyekevu? Je, watu wenye talanta, elimu, na uungwana, wanawezaje kutumiwa na Shetani kuwa mtego kwa wengine? Ni mfano gani unaotolewa wa hatari wa kupotosha mamlaka haya? 509:2, 3 [578:2, 3] GC-SG 57.6

7. Shetani amekuwa akijitayarisha kwa suala gani? Ni uhakikisho gani unaotolewa kwa ajili ya kututia moyo katika mzozo wa mwisho? 510:1-3 [579:1-3] GC-SG 57.7

**Sura ya 31 - Wakala wa Pepo Wabaya**

1. Ni nini ushahidi wa kuwepo kwa malaika kabla ya kuumbwa kwa mwanadamu? Inasemekana nini juu ya idadi yao? Ni mifano gani iliyorekodiwa kuhusu nguvu zao? 511:1-3 [581:1-582:1] GC-SG 58.1

2. Walitumwa kwa nani wakiwa na ujumbe wa rehema? 512:1 [582:2] GC-SG 58.2

3. Je, sisi Tunajua nini kuhusu huduma ya malaika watulindao? 512:2 [583:1] GC-SG 58.3

4. Kwa nini neema na ulinzi huo unahitajika kwa watoto wa Mungu? 513:1 [583:2] GC-SG 58.4

5. Ni nini chanzo cha roho waovu, au malaika waovu? Ni katika kipindi gani hasa walikuwa wana shuguli nyingi, na kwa nini? 513:2,3 [583:3-584:1] GC-SG 58.5

6. Eleza jinsi Kristo alivyokutana na "jeshi" la hawa pepo wabaya. Ni faida gani zilizotokana na mzozo huu? 514:1-515:1 [584:2-585:2] GC-SG 58.6

7. Ni katika kipindi gani kingine ambapo Kristo alileta ukombozi kwa wale waliokuwa chini ya nguvu za roho wachafu? 515:2 [585:3] GC-SG 59.1

8. Ni visa gani vinavyoonyesha kwamba wale waliopagawa na roho waovu siyo mara zote huteseka? 516:1 [586:1] GC-SG 59.2

9. Ni kundi gani la watu ndilo ambalo lipo katika hatari kubwa zaidi kuhusiana na mawakala wa pepo wabaya? 516:2-517:1 [586:2-587:1] GC-SG 59.3

10. Ni ahadi gani zenye thamani na za hakika zinazotolewa kwa ajili ya wa wafuasi wa Kristo? 517:2 [587:2] GC-SG 59.4

**Sura ya 32 - Mitego ya Shetani**

1. Ni nini kusudi kuu la Shetani analolinuia wakati pambano linapokaribia mwisho? Je, anahangaika kuhusu nani zaidi? 518:1, 2 [589:1, 2] GC-SG 60.1

2. Je, anaweka mipango gani ili kuharibu jitihada za watumishi wa Mungu? 518:3-519:1 [590:1,2;] GC-SG 60.2

3. Je, washitaki wa ndugu au watafuta-makosa ya wenzao hutimizaje kusudi la Shetani? Ni wakati gani wanakuwa na bidii zaidi? 519:2, 3 [590:3-591:1] GC-SG 60.3

4. Shetani anapangaje kutambulisha uzushi miongoni mwa washiriki wa kanisa kutoka ndani? Ni katika fundisho gani maarufu la uhuru (Kiliberali) kuna hatari kubwa? Kwa nini? 520:1, 2 [591:2, 3] GC-SG 60.4

5. Ni nia gani mbaya katika kujifunza Maandiko ndiyo ambayo imesababisha mafarakano na kuchanganyikiwa? Ni kwa namna gani mafungu ya Biblia mara kwa mara yanafasiriwa vibaya? 520:3-521:1 [591:4-592:1] GC-SG 60.5

6. Ni katika mazingira gani kujifunza Biblia ni hatari? Ni nini matokeo ya kukataa kujifunza sehemu fulani za Maandiko? 521:2 [592:2] GC-SG 60.6

7. Ni sehemu gani za Biblia zilizo wazi sana kiasi kwamba zinaweza kueleweka kwa wote? Moyo ulio na uaminifu unapewa matumaini gani katika kujifunza Biblia? 521:3; 526:2; 528:2 [592:3; 598:1; 599:5] GC-SG 61.1

8. Je, "kuwa huru" kunachangiaje uasi wa sheria? Je, utafiti wa sayansi umesadiaje kutilia mashaka Mambo ya Mungu? Je, kuna ukinzani wa kweli kati ya sayansi na Biblia? 522:1-4 [593:1-4] GC-SG 61.2

9. Je, mtazamo wetu unapaswa kuwa upi kuhusu siri au mafumbo ya Biblia ambayo bado hayajafunuliwa kwetu,sisi wenye akili zenye ukomo? 523:1; 527:1,2 [594:1; 598:2-599:1] GC-SG 61.3

10. Ni kundi gani la wasomaji wa Biblia ambao 'hawana ngao dhidi ya udanganyifu'? 523:2 [595-1] GC-SG 61.4

11. Orodhesha makosa matano ya kawaida, pamoja na sababu kwa nini haya ni hatari. 524:1-525:2 [595:2-596:4] GC-SG 61.5

12. Ni hatima gani huwapata watu wanaokataa kwa makusudi kanuni moja ya Ukweli? Ni sababu gani inayosadikiwa ambayo makafiri wengi wanayo kwa ajili ya kutoamini kwao? 525:3, 4 [597:1, 2] GC-SG 61.6

13. Watu wengine wanaongozwaje kwenye ukafiri kwa mtizamo wao wenyewe? (Makundi manne) 526:1 [597:3] GC-SG 62.1

14. Ni sababu gani hasa ndiyo inachangia kutomwamini Mungu? Ni nini kinachohitajika ili kudumisha imani inayookoa? 527:3-528:1 [599:2 - 4] GC-SG 62.2

15. Kwa nini Mungu hawakingi watu Wake dhidi ya vishawishi vya Shetani? Je mtu anaweza kushinda majaribu au vishawishi kwa ufanisi mkubwa-SG 62.3

16. Ni wakati gani ambapo Israeli ilikuwa salama kutokana na jaribio la Balaamu kuwalaani, na ni nini kilichosababisha kuanguka kwao? 528:3-530:2 [600:1-601:3] GC-SG 62.

**Sura ya 33 - Udanganyifu Mkuu wa Kwanza**

1. Ni nia gani iliyomwongoza Shetani kuwashawishi wazazi wetu wa kwanza? Je, Hawa angewezaje kuepuka hila zake? Ni tumaini gani la uongo alilowekewa ambalo lilimfanya akubali kushindwa? 531:1-532:1 [603:1-604:2] GC-SG 63.1

2. Je, matokeo ya kutomtii Mungu yalithibitishaje uhakikisho wa Shetani kuwa ni wa uongo? 532:2, 3 [604:2-605:1] GC-SG 63.2

3. Ni nini kilipotezwa kwa kutenda dhambi, na kinawezaje kupatikana au kurudishwa tena? 533:1 [605:1] GC-SG 63.3

4. Je, theolojia maarufu na inayopendwa inarudiaje maneno ya mjaribu katika Edeni? Ni kwa jinsi gani Shetani ametumia hilo katika kuichafua tabia ya Mungu? 533:2-536:3 [605:3-608:3] GC-SG 63.4

5. Ni kwa jinsi gani watu wanasukumwa kinyume kabisa na fundisho lenye kuchukiza la mateso ya milele? (watu wote wataokolewa) Ni kielelezo gani kinatolewa katika upotoshaji kwa kutumia Aya moja tu katika kufundisha udanganyifu au kosa hili? 537:1-539:1 [609:1-611:1] GC-SG 63.5

6. Ni mafundisho gani yenye makosa ambayo yamesababisha watu wengi kujiua? Ni maandiko gani yanafundisha wazi kwamba watenda dhambi wasiotubu hawataurithi ufalme wa Mungu? 539:2-541:2 [611:2-613:1] GC-SG 63.6

7. Kwa nini utumishi unaochochewa na hofu ya Mungu mwenye kulipiza kisasi hauwezi kukubaliwa Naye? 541:3, 4 [613:2, 3] GC-SG 63.7

8. Inawezaje kuonyeshwa kwamba ni haki na rehema kwa Mungu kuwatenga watenda-dhambi wasiotubu kutoka mbinguni? 542:1-543:3 [614:1-615:3] GC-SG 64.1

9. Je, kifo cha pili kinatofautishwaje na kile cha kwanza (1) Kuhusiana na wakati, (2)Urefu wa muda wake? 544:1-545:1 [615:4-616:1] GC-SG 64.2

10. Nadharia ya mtu kuwa na ufahamu anapokuwa amekufa yaweza kuonyeshwaje kuwa ni fundisho lenyekuchukiza katika madokezo yale yahusuyo waadilifu na wasio waadilifu pia? Je, ushuhuda wa Maandiko ni upi kuhusiana na hili? 545:2-546:3 [616:2-618:2] GC-SG 64.3

11. Ni maoni gani kuhusu imani ya watu wengi kuhusu hali ya kifo ambayo Tyndale na Dakt. Adam Clark walitoa? Je, fundisho hili la ufufuo linabatilishwa vipi? 547:1-3 [618:3-619:1] GC-SG 64.4

12. Maandiko yanaelekeza ni wakati gani waadilifu wataingia katika furaha ya mbinguni? Ni nini lazima kitangulie, utoaji wa thawabu au adhabu? 548:1-549:1 [619:2-620:2] GC-SG 64.5

13. Fundisho la kutokufa kwa mwanadamu lilipataje njia yake katika kanisa la Kikristo? Mafundisho ya Luther yalikuwa yapi kuhusiana na swali hilo? 549:2 [620:3] GC-SG 64.6

14. Je, kifo na ufufuo wa wenye haki vinahusianaje? Je, mpango wa Mungu kwao unaweza kuboreshwa? 449:1 [621:1] GC-SG 64.7

**Sura ya 34 - Umizimu au Imani ya Kuwasiliana na Wafu au Wafu Bado Wako Hai au Mbinguni.**

1. Kanuni ya msingi ya Kuwasiliana na wafu au umizimu ni ipi? Hili ni hitimisho la kimantiki la dhana ipi ya uongo? 551:1, 2 [623:1, 2] GC-SG 65.1

2. Ni maonyesho gani yanayoonekana kwa mambo ama ya kimwili au kiakili, yanayoonekana kuunga mkono madai ya Umizimu? Haya yanapokubaliwa ni udanganyifu gani wa kutisha hufuata? 552:1, 2 [624:1, 2] GC-SG 65.2

3. Houdini alidai kwamba angeweza kwa urahisi, kuiga matukio yoyote ya kuwasiliana na wale waliokufa, na aliamini kwamba yote haya yalikuwa ya ulaghai. Dini zetu za kiafrika zina mengi ya kuzungumza na watu waliokufa na hasa mababu pia. Sir Oliver Lodge alishikilia kuwa alikuwa amewasiliana kabisa na mwanawe aliyefariki. Ukweli uko wapi, kulingana na Maandiko, na kulingana na uhalisia ambao watu wameuona kwa macho? 553:1, 2 [625:1, 2] GC-SG 65.3

4. Ni wito gani wa kupendeza unaotolewa kwa watu waliostaarabika na waliosafishwa, kuhusiana na maendeleo yao ya wakati ujao? Je, maendeleo haya ya kufikirika yanaonyeshwaje kuwa yanapeleka watu chini badala ya kwenda juu? 553:3-555:2 [627:1-628:2] GC-SG 65.4

5. Ni mafundisho gani kupitia “roho za wale waliokufa au mapepo” yanawapendeza watu wenye kujifurahisha wenyewe na wale walio na tamaa za kimwili? 555:3 [628:3] GC-SG 65.5

6. Ni matamko gani yaliyo wazi katika Biblia, ambayo yangeaminiwa, yangekuwa ulinzi dhidi ya madanganyo ya kuwasiliana na wafu? Je, tuna ushahidi gani leo kwamba kujishugulisha na kuzungumza na wafu si mambo mapya bali ya zamani sana? 556:1, 2 [629:1, 2] GC-SG 65.6

7. Ni mafundisho gani ambayo yamekuja kupitia “umizimu” yanayodhoofisha kanuni za msingi za mpango wa wokovu? 556:3-557:2 [629:3-630:2] GC-SG 65.7

8. Je, Umizimu wa siku za leo una hatari zaidi kuliko hapo awali? 558:1 [631:1] GC-SG 65.8

9. Ni hatari gani zinazotokana kuchunguza madai ya harakati hii ya udanganyifu? Mkristo wa kweli atakutana na udanganyifu huu kwa jinsi gani? 558:2-559:2 [632:1-633:1] GC-SG 65.9

10. Ni majaribu gani yenye nguvu kwa imani yetu katika Neno la Mungu ambayo huenda yakatujia sisi binafsi tunapoingia kwa undani au kikamilifu zaidi katika “saa ya kujaribiwa”? Ni msaada gani ungetumwa, ikiwa ni lazima, kwa ajili ya ulinzi wetu? 560:1, 2 [633:2, 3] GC-SG 65.10

11. Ni nini ufafanuzi wa hasira ya mataifa na kujitayarisha kwa vita kwa ulimwengu mzima? Ni wangapi hatimaye watapatikana katika safu za umizimu, wakiwasiliana na roho za watu waliokufa? 561:1-562:2 [634:2-635:1] GC-SG 65.11

## Sura ya 35 - Malengo ya Upapa

1. Je harakati "huru" katika makanisa ya Kiprotestanti zimeathirije uhusiano wao na Ukatoliki wa Kiroma? Je, kuna sababu za msingi tunaposema kwamba kanisa la Kiroma lina uvumilivu zaidi moyoni sasa kuliko zama za giza? 563:1-565:2; 571:1-4 [637:1-639:2; 645:1-4] GC-SG 66.1

2. Tunapaswaje kutofautisha kati ya mshiriki mmoja binafsi na kanisa la Kiroma na mfumo wa lenyewe? Kusudi kuu la Kanisa ni nini na ni kipi kinachoweza kuonekana ambacho kinatuonyesha mafanikio kuelekea lengo hili? 567:2, GC-SG 66.2

3. Ni mambo gani yahusuyo ibada ndiyo ambayo huvuta hisia za mwanadamu? Je, mambo haya yanawezaje kuwa mbadala wa ibada ya Kweli ya moyo? 566:2-567:2 [640:2-641:2] GC-SG 66.3

4. Je, vipengele gani vina mambo ya machukizo katika fundisho la ungamo? 567:3 [641:3] GC-SG 66.4

5. Ni mfanano gani unaotolewa kati ya Kanisa la Roma na kanisa la Kiyahudi katika siku za Kristo? 568:1-3 [642:4-3] GC-SG 66.5

6. Je, ni kipengele gani cha tabia yake mwenyewe ambacho Shetani amewaongoza wanadamu kufikiri kwamba hii ni sifa ya Mungu? Dhana hii isiyo ya kweli juu ya Mungu iliongozaje kwenye vitendo vya ukatili miongoni mwa wapagani? Ni kwa njia zipi jambo hil ilimedhihirishwa wazo, katika Kanisa Katoliki la Roma? 569:1-570:2 [643:1-644:2] GC-SG 66.6

7. Kwa nini kuongezeka kwa nuru na ujuzi zaidi wakati wetu si sababu ya kutuhakikishia kwamba siku za ushirikina, ujinga na kutovumilia imani za wengine si habari ya zamani tu? 572:1-3 [646:1-3] GC-SG 66.7

8. Ni kwa njia gani Waprotestanti wamefuata nyayo za Roma? Sheria ya Jumapili ya kwanza ilitungwa lini, na ni nani waliopewa udhuru wa masharti yake? 573:1-574:1 [647:1-648:1] GC-SG 66.8

9. Fuatilia hatua zaidi zilizochukuliwa katika kuinuliwa kwa utunzaji wa Jumapili? 574:2-577:1 [648:2-651:1] GC-SG 66.9

10. Je, tuna ushahidi gani kwamba badiliko la Sabato kutoka Jumamosi na kwenda Jumapili kilikuwa ni kitendo cha kudhamiria cha kanisa ambacho hakikuwa na mamlaka ya Maandiko? Je, utunzaji wa Sabato Ethiopia unatuonyeshaje kuwa Sabato ilitunzwa kwa karne nyingi baada ya Kristo? 577:2-578:1 [651:2-659:1] GC-SG 66.10

11. Ni maandiko gani yanayotabiri kufufuliwa kwa sheria ya kuabudu na kuitunza Jumapili na kuleta mateso ulimwenguni pote? 578:2-579:1 [652:2-653:1] GC-SG 66.11

12. Je, Roma inangoja hatua ipi ili kuanzisha mamlaka yake Marekani? Je, inajiandaa kwa namna gani kwa ajili ya fursa hiyo? 580:1-581:2 [654:1-652:2] GC-SG 66.12

**Sura ya 36 - Mgogoro Ujao**

1. Ni suala gani kuu la pambano la muda mrefu kati ya Kristo na Shetani ndilo mada kuu ya pambano la mwisho? Ni dhana gani zinazoshikiliwa na watu wengi

nazo ndizo zinawarundika kwenye upande usiofaa? 582:1-583:1 [657:1-658:2] GC-SG 67.1

2. Kwa nini fundisho kwamba Sheria ya Mungu haina mashiko tena juu ya mwanadamu (1) linapingana na ubongo wa mtu, (2) Je, lina matokeo ya hatari gani? 584:1-585:1 [659:1-660:2] GC-SG 67.2

3. Ni maovu gani ya siku hizi ambayo yanaonekana kuwa ni tokeo la kimantiki ya fundisho ya kwamba wanadamu wameachiliwa huru wasiitii Sheria ya Mungu? 585:2-586:1 [660:3-661:1] GC-SG 67.3

4. Wakati wowote au popote pale ambapo Biblia haiwezi kunyamazishwa tena, na uhuru wa dini unakuwepo, Shetani hutafutaje kutekeleza yale ambayo alitimiza hapo awali kupitia ujinga wa Maandiko na mateso kwa ajili ya kutokuwa na uhuru wa dini? Kuikataa Kweli inayohusu Amri ya Nne ya Sabato kumeongozaje kwenye uasi-Sheria? 586:2 [661:2] GC-SG 67.4

5. Ni sababu gani inayotolewa kuhusu kushamiri kwa uovu na baadhi ya walimu wenye kusema wameokolewa kwa neema na hivyo Sheria ya Mungu haina haja ya kuitiiwa, ni nini hawa wanachopendekezewa kama dawa ya uovu? Je, mtazamo wetu kuhusu matengenezo ya afya na kiasi unapaswa kuwa upi? 587:1 [662:1] GC-SG 67.5

"Kila matengenezo ya kweli yana nafasi yake katika kazi ya ujumbe wa Malaika wa tatu. Hasa matengenezo ya kiasi yanahitaji umakini wetu na pia tunapaswa kuyaunga mkono. "Muungano wa Wanawake wa Kiasi, kwa Wakristo ni shirika ambalo juhudi zake za kueneza kanuni za kiasi tunaweza kuunganisha moyo wetu wote na hiyo. Nuru imetolewa kwangu kwamba hatupaswi kusimama pembeni yao, ijapokuwa hatupaswi kutelekeza kanuni kwa upande wetu, kadiri inavyowezekana tunapaswa kuungana nao katika kufanya kazi kwa ajili ya matengenezo ya afya na kiasi."—" Testimonies for the church," Vol. 6, uk. 110; "Counsel For Health," uk. 436. GC-SG 67.

6. Dini zinazodai kuwa za Kikristo zitaungana juu ya makosa gani mawili ya kimsingi? Ni muungano gani wa pande tatu utakaotokeza, na nini itakuwa ishara? 588:1 [663:1] Ona pia " Testimonies for the Church," Juz. 5, uk. 451. GC-SG 67.7

7. Ni sehemu gani inayotendwa na Imani ya Umizimu katika kufanikisha muungano wa Uprotestanti na Ukatoliki? 588:2-589:1 [663:2-664:1] GC-SG 67.8

8. Shetani anahusika kwa upana gani kuhusiana na matetemeko ya ardhi na majanga mengine ya asili? Kwa nini haya yanaongezeka idadi na ukali? Ni sababu gani ya uongo itatolewa kuhusu maovu haya? 589:2-590:1 [664:2-665:2] GC-SG 67.9

9. Je, hasira itaamshwaje dhidi ya watunza-Sabato, kupitia Umizimu? Ni mbinu gani zilizotumiwa na Shetani mwanzoni mwa pambano kuu dhidi ya Mungu ambazo zitarudiwa dhidi ya masalio? 590:2-591:1 [666:1, 2] GC-SG 67.10

10. Tofautisha mbinu za kupata utii anazozitumia Mungu na anazozitumia mwovu. Hili litawaathirije wale ambao hawawezi kushawishiwa kumwasi Mungu? 591:2-592:3 [666:3-667:3] GC-SG 67.11

**Sura ya 37 Maandiko ni Kinga na Usalama**

1. Ni mazingira gani katika siku za mwisho yanayofanya kujifunza Neno la Mungu kuwa muhimu zaidi kuliko wakati mwingine wowote? 593:1, 2 [669:1-670:1] GC-SG 68.1

2. Kwa nini wanafunzi hawakuwa tayari kwa ajili ya kifo cha Kristo? Je, sisi tunapata somo gani kwa jambo hili? Je, umati wa watu utajihusisha kwa namna gani na ujumbe wa mwisho? 594:1-595:1 [670:1-671:1] GC-SG 68.2

3. Je, Shetani amewatumia kwa namna gani viongozi wa dini ili wasiweze kuchunguza Neno la Mungu? Kristo alifundishaje wajibu wa mtu binafsi katika kuyachunguza Maandiko? 595:2-596:4 [671:2-672:4] GC-SG 68.3

4. Ni wakati gani ujinga hauna kinga dhidi ya adhabu ya dhambi? Je, ni kwa kiwango gani wanadamu wanawajibika kwa ujuzi wa Neno la Mungu? 597:2-598:2 [674:1-675:1] GC-SG 68.4

5. Ni kanuni gani ya ufasiri wa Biblia ndiyo ambayo ingemzuia mtu kutoka kwenye udanganyifu mbaya? Ni kwa roho gani mtanziko au kutoeleweka kwa Maandiko kunapaswa kushughulikiwa? Ni jambo gani lililo muhimu zaidi kuliko uwezo wa akili? 599:1, 2 [675:3-676:1] GC-SG 68.5

6. Mwanafunzi mwenye roho ya maombi kwa Mungu anaweza kutarajia kupokea nini? Ni ahadi gani ya Kristo ambayo ndiyo sharti la kuhifadhi Neno la Mungu akilini? 599:3-600:1 [676:1, 2] GC-SG 68.6

7. Angalia sababu zinginezo za kujifunza Biblia kwa bidii na kina: (1) kama ulinzi dhidi ya ukafiri ulioenea; (2) kama matayarisho ya moyo ili kufaulu mtihani wa hukumu; (3) kuhamasisha kuzaa matunda katika maisha; (4) kuimarisha nafsi kwa nyakati za mateso. 600:2-602:1 [678:1-679:1] GC-SG 68.7

8. Ni Furaha gani itakuja kwa mtu anayepata hekima ya Kweli katika Neno la Mungu? 602:2, 3 [679:2, 3] GC-SG 68.8

**Sura ya 38 - Onyo la Mwisho:**

1. Ujumbe wa Ufu. 18:1-4 una uhusiano gani na ujumbe wa awali kama huo unaopatikana katika sura ya 14:6, 7? 603:1-604:1; 611:1 [681:1-682:1; 690:1] GC-SG 69.1

2. Je, ulimwengu utaletwa kwenye suala gani la kuogofya. Ni nani pekee atakayepokea alama ya mnyama hatimaye? 604:2-605:2 [682:2-683:3] GC-SG 69.2

3. Je, msukosuko wa sheria ya Jumapili utatoaje nguvu ya ziada kwa Jumbe zenye sehemu tatu? 605:3 [683:4] GC-SG 69.3

4. Je, mtazamo wa wanamatengenezo kwa wenye dhambi hubadilikaje mara kwa mara, Roho wa Mungu anapowamiliki? Ni maovu gani matatu yatafichuliwa katika onyo la mwisho? Matokeo gani yanafuata? Je, mateso yataathirije uenezaji wa ujumbe? 606:1-607:1 [685:1-686:1] GC-SG 69.4

5. Je imani ya watumishi wa Mungu itajaribiwa katika njia zipi? Ni nani atakayekuwa mchungu zaidi katika kupinga Ukweli? 608:1-3 [686:2-687:2] GC-SG 69.5

6. Je, ni usisitizaji wa jaribu gani muhimu kuhusu ile Kweli ndilo umefanya upinzani utokee sikuzote? Onyesha kwamba urejeshwaji wa Ukweli wa awali limekuwa jambo endelevu-hatua kwa hatua. Ni nini kinachowawezesha watumishi wa Mungu kuvumilia mateso yanayozidi kuongezeka? 609:1-610:1 [688:1, 2] GC-SG 70.1

7. Je, tunapaswa kutegemea kukomeshwa kwa mateso kabla ya kazi ya Mungu kukamilika? Mungu ametumiaje viongozi wa serikali kuzuia nguvu za uovu? Je, baadhi ya viongozi hawa watazadiwa kwa namna gani? 610:2, 3 [689:1, 2] GC-SG 70.2

8. Ni Maandiko gani yaliyoanza kutimizwa siku ya Pentekoste, na ambayo yanatoa hakikisho la uwezo mkuu wa Roho Mtakatifu katika kuimalizia kazi? 611:2, 3 [690:2-691:1] GC-SG 70.3

9. Ni kwa njia gani ya ajabu Mungu ataimaliza kazi Yake? 612:1, 2 [691:2, 3] GC-SG 70.4

**Sura ya 39 - Wakati wa Taabu**

1. Je, kusimama kwa Mikaeli kunamaanisha nini kwa (1) wenye hatia; (2) watu wa Mungu; (3) Malaika wa mbinguni; (4) Kristo? GC-SG 71.1

2. Je, nguvu zisizozuiliwa za Shetani zitadhihirikaje? 613:1-614:1 [693:1-694:1] Je, Malaika waovu wamekuwa wakingoja ruhusa ya kufanya nini? Je, kuondolewa kwa Roho wa Mungu azuiaye kutakuwa na matokeo gani kwa nguvu zinazokinzana? Je, Watunza Sabato wataonekanaje kwa watu wa dunia? Ni amri gani itatolewa dhidi yao? 614:2-615:2 [694:2-695:2] GC-SG 71.2

3. Ni muda gani ambao Yakobo alikuwa na uchungu mzito katika usiku ule aliopigana mieleka na Bwana? Huku akimtumaini Mungu pekee, alikuwa amefanya nini kwa ajili yake mwenyewe? Je, tunapata somo gani katika mweleka huu leo? 616:1, 2 [697:1,2] GC-SG 71.3

4. Kuna mambo gani mengine yanayofanana ambayo yalimpata Yakobo wakati wa taabu yake na ambayo pia yatawapata watu wa Mungu wakati wa taabu siku za mwisho? 616:3-619:1 [697:3-700:1] GC-SG 71.4

5. Ni tukio gani la kujikosoa, kujidharau na kujishutumu ambalo litaongeza dhiki ya watakatifu? Je, watakuwa wamefanya nini ambacho kitazuia imani yao kushindwa? 619:2-620:1 [700:2-701:1] GC-SG 71.5

6. Kukubali udanganyifu gani wa Shetani kutathibitika kuwa hatari kwa wengi? Kwa nini Mungu hawezi kusamehe dhambi zinazoungamwa wakati wa taabu? Je, kujaribiwa kwa imani yao kutatenda nini kwa watoto wa Mungu? 620:2-621:1 [701:2-4] GC-SG 71.6

7. Je, watu wa Mungu wanapaswa kujiandaa kwa namna gani kwa ajili ya wakati wa taabu? Ni masomo gani ambayo tumejifunza hapo awali ambayo yanaweza kupunguza majaribu ya wakati huo? Je, ni mtazamo gani ambao ungewaepusha vijana kuepuka kuwa upande wa dhambi? 621:2-622:3 [702:1-703:2] GC-SG 71.7

8. Ni nini kitakachowazuia wengi wasijiandae inavyopaswa? Nini ilikuwa siri ya uwezo wa Kristo kuishi juu ya dhambi? Ni msaada gani umeahidiwa kwa kila mtu anayejitahidi kushinda? 622:4-623:2 [703:3-704:1] GC-SG 72.1

9. Ni kwa njia gani Imani ya Mizimu itaonyesha nguvu zake sasa? Ni tukio gani litatendeka kileleni mwa tamthilia ya udanganyifu? Kwa nini hakuna hata mmoja wa watu wa Mungu atakayepotoshwa katika janga hili? 624:1-625:3 [704:3-706:1] GC-SG 72.2

10. Ni matukio gani tofauti yenye majaribu mazito ambayo sasa yanakuja kwa watunza-Amri? Ni mawazo gani yatawaletea faraja na uhakikisho? 626:1-627:1 [706:2-707:3] GC-SG 72.3

11. "Tendo geni" kwa Mungu ni lipi? Ulimwengu umekuwa na hatia ya uhalifu gani ambao ni wa kutisha sana? Ni nini kinachotofautisha hukumu za mwisho na

zile za nyakati zote zilizopita? 627:2-629:1 [707:4-710:2] Isaya 28:21. GC-SG 72.4

12. Mungu atatoa majaliwa gani kwa ajili ya mahitaji ya kimwili ya watu Wake? Malaika wa mbinguni watatenda sehemu gani katika kuwalinda watu Wake Mungu? 629:2-631:1 [710:3-712:2] GC-SG 72.5

13. Ni kwa namna gani Malaika wametenda kwa niaba ya watu wa Mungu nyakati zilizopita? 631:2-632:1 [712:3-713:2] GC-SG 72.6

14. Walinzi watawatiaje moyo wenzao ambao wanateseka nao pamoja? Ni uhakikisho gani utakaotoka mbinguni? Katika nyakati zilizopita Mungu ameruhusu watakatifu Wake wengi wateseke na hata kufia imani: kwa nini sasa watalindwa katika tukio la mwisho? 632:2-633:1 [713:3-715:1] GC-SG 72.7

**Sura ya 40 - Watu wa Mungu Wakombolewa**

1. Ni chini ya mazingira gani nyeti ambapo ukombozi wa ghafula huja kwa watu wa Mungu? Waovu wanakamatwa kwa matukio gani ya ajabu? 635:1-3 [717:1-718:1] GC-SG 73.1

2. Ni uzoefu gani wenye furaha unaowapata watu wa Mungu wakati huu? 636:1 [718:2] GC-SG 73.2

3. Je, uwepo wa Mungu duniani una matokeo gani? 636:2-637:1 [718:3-719:1] GC-SG 73.3

4. Ni nani watakaofufuliwa kutoka makaburini ili kumwona Kristo akitokea? 637:2 [719:2] GC-SG 73.4

5. Ni nini kitakachowapata waovu waliokuwa karibu kuwaangamiza watakatifu? 637:3-638:1 [720:1, 2] GC-SG 73.5

6. Ni tukio gani zaidi tukufu litakalowajia watakatifu? Ni nini kitakachofunuliwa kwa macho ya wote? Je, watu wote wataona nini kuhusu Sabato? 639:1-640:1 [721:1-722:1] GC-SG 73.6

7. Watoto wa Mungu wanajulishwa nini sasa? Ni nini kinachotokea na kuonwa na wote toka mbinguni? Kunakuwa na athari gani kwa kila tabaka la watazamaji? 640:3-642:3 [722:3-724:2] GC-SG 73.7

8. Ni kumbukumbu gani, pamoja na majuto yasiyoelezeka, yatakayoamshwa wakati waovu wanaposikia sauti ya Mungu? 642:3-644:1 [724:3-726:1] GC-SG 73.8

9. Ni tofauti gani kubwa inayoonekana kati ya watakatifu waliofufuka? Je, wote wanaweza kutazamia nini? 644:1, 2 [726:2, 3] GC-SG 74.1

10. Ni mabadiliko gani huja kwa wenye haki walio hai? Je, Gari la mawingu ambalo watu watapanda nalo kwenda mbinguni linaundwa na nini? Je, ni sherehe gani hufanyika kabla hawajaingia pale Jijini? 645:1-3 [727:1-3] GC-SG 74.2

11. Ni nini kinachoonekana wakati malango ya jiji yanapofunguliwa? 646:1 [728:1] GC-SG 74.3

"Wakati wimbi la uovu lilipoenea ulimwenguni, na uovu wa wanadamu ukaleta hatima ya kuangamizwa kwao kwa gharika ya maji, Mkono ulioiumba dunia na kupanda mimea humo Edeni uliiondoa bustani hiyo duniani. Lakini katika urejeshwaji wake wa mwisho, kutakapokuwa na 'mbingu mpya na nchi mpya,' itarejeshwa ikiwa imepambwa kwa utukufu zaidi kuliko hapo mwanzo."—" Patriarchs and Prophets," uk. 62. GC-SG 74.4

12. Je, watakatifu watauchukuliaje ule mwaliko unaosema, "Ingia katika furaha ya Mola wako Mlezi"? 646:2-647:1 [728:2,3] GC-SG 74.5

13. Je, Adamu anaongezaje Furaha ya Malaika na ya wale waliokombolewa, anapokutana na Mwokozi? 647:1-648:2 [729:1-730:1] GC-SG 74.6

14. Ni tukio gani zaidi linalotendeka juu ya bahari ya fuwele? Watakatifu wamepitia uzoefu gani ambao unawastahilisha kuimba "wimbo mpya"? 648:3-650:1 [730:2-731:2] GC-SG 74.7

15. Msalaba wa Kristo utatazamwaje katika vizazi vyote? Je, ni siri na mafumbo gani yataendelea kufunuliwa katika nuru yake? 651:1-652:2 [732:1-733:2] GC-SG 74.8

**Sura ya 41 - Ukiwa wa Dunia**

1. Ni Hukumu gani zimetabiriwa kwa Babeli? 653:1-3 [735:1-736:1] GC-SG 75.1

2. Ni majuto gani ya kutisha ambayo sasa yanawakumba wale waliokataa rehema ya Mungu? Je, hili linatofautiana vipi na toba kwa ajili ya dhambi? 654:1, 2 [736:2,3] GC-SG 75.2

3. Wachungaji wa uwongo wanaadhibiwa kwa namna gani hasa? 654:4-655:4 [737:1-738:1] GC-SG 75.3

4. Pambano la miaka elfu sita linapofikia upeo wake, ni nani wanaojumuishwa pamoja na Shetani na wafuasi wake waasi? Je, ni matokeo gani yatakuwa kwao? 656:1-657:2 [738:2-739:2] GC-SG 75.4

5. Dunia itabakia katika hali gani? "Shimo lisilo na mwisho" ni nini? Na Shetani 'amefungwa' kwa maana gani? 658:3-660:2 [740:1-742:2] GC-SG 75.5

6. Ni kazi gani maalum ya watakatifu itakayokuwa katika kipindi cha miaka elfu moja? Je, mwisho wa kipindi hiki nini kitatokea? 660:4-661:2 [742:4-743:2] GC-SG 75.6

**Sura ya 42 - Pambano Lakwisha**

1. Waovu wanapoinuliwa mwishoni mwa ile miaka elfu moja, ni tukio gani linaloyakumba macho yao? Je, Wanasemaje? Kwa nini wasiwe na rehema ya pili? Yerusalemu Mpya unatua na kutulia wapi? 662:1-3 [745:1-746:1] GC-SG 76.1

2. Wakati huu Shetani anatumaini kutimiza nini? Ni kwa madai gani ya udanganyifu anajenga imani ya wafuasi wake kumsadiki yeye? Ni hali gani zinazoonekana kutoa tumaini kwa jitihada zao? 663:1-664:2 [646:2-647:1] GC-SG 76.2

3. Majeshi ya waovu yanapozunguka jiji, ni mandhari gani ya utukufu inaonekana kwao? Ni nani kati ya waliokombolewa walio karibu zaidi na kiti cha enzi? Ni mzigo gani ulio moyoni kwenye wimbo wa wale waliokombolewa? 664:3-665:3 [747:3-748:3] GC-SG 76.3

4. Ni Sherehe gani hufanyika mbele ya macho ya wote? Kabla ya kutekelezwa kwa Hukumu juu ya waovu, wanawezeshwaje kutambua kwamba hukumu yao ni ya haki? 666:1, 2 [749:1,2] GC-SG 76.4

5. Ni matukio gani ya kuvutia ambayo sasa yako katika panorama au video? Kila muigizaji atasaidiwaje kwenye dhamira yake kuona matokeo ya mwenendo wake mbaya? 666:3-667:1 [749:3-751:2] GC-SG 76.5

6. Je, waovu watafikiri nini kuhusu kukataa kwao kuipokea injili walipopewa ofa? Je!Watalazimishwa kukiri nini kutoka kwa midomo yao? 668:3, 4 [751:3,4] GC-SG 76.6

7. Shetani anakumbuka mambo gani anapotazama filamu au video za matukio hayo? 669:1, 2 [752:1,2] GC-SG 76.7

8. Shetani anatazamwa namna gani sasa, yaani uongo wake unapofichuliwa? Je, analazimishwa kufanya nini mwishowe? 670:1, 2 [753:1,2] GC-SG 77.1

9. Viumbe vyote katika ulimwengu wote mzima viko tayari kutangaza nini sasa? Kristo anatoa tangazo gani kuhusu waliokombolewa, na wimbo wao wa mwitikio ni upi? 670:3-671:1 [753:3-754:1] GC-SG 77.2

10. Shetani anaonyesha kwa njia gani kwamba tabia yake haijabadilika? Wafuasi wake wanaitikiaje jaribio lake la mwisho analowaongoza kutenda? 671:1 [754:2] GC-SG 77.3

11. Ni kwa njia gani Dhambi na watenda-dhambi wataangamizwa hatimaye? Ni nini uzoefu wa watakatifu wakati wa uharibifu huu? 672:1-673:2 [755:1-756:3] GC-SG 77.4

12. Ni kazi gani mbili zinazotimizwa kwa moto kutoka mbinguni? Ni ukumbusho gani mmoja tu wa dhambi utakaobaki? Je, kazi ya urejeshwaji wa kile kilichopotea sasa imekamilika kwa kiasi gani? 674:1-3 [757:1-3] GC-SG 77.5

13. Urithi wa watakatifu ni nini? Ni uzoefu gani wa kidunia utakaokuwa haupo? Watakatifu watatumiaje wakati wao mbinguni? 674:4-678:2 [758:1-762:2] GC-SG 77.6

14. Ni Ukweli gani mkuu kuhusu tabia ya Mungu ambao sasa utakuwa umethibitishwa milele katika sayari zote au Uumbaji wote? 678:3 [762:3] GC-SG 77.7

## Chapter 26 Supplement: The Weekly Cycle

The writings of historians, the records of chronographers, the language of earth, the calendar of time, and the existence of the Jewish race—all testify to the fact that the weekly cycle on our calendars today is the same as in earlier centuries—going bak to the time of Christ, to Moses and beyond.

In the beginning, God gave us the weekly seven-day cycle, with the Sabbath as the last day. That pattern has never been changed. The seventh-day of the week today is the true bible Sabbath. Our seventh day is the Sabbath which Jesus kept; it was the Sabbath in the time of Moses when the Ten Commandments were written down. Historians and scientist all agree that this is true.

If there had been any change in the weekly cycle, between the time of Creation and the time of Moses, a correction would have been made when the Ten Commandments were given to the Hebrews. From that time on, down to the present, there have always been Jews to testify as to the true Sabbath. It is the same seventh day of the week which is on our calendars. While all the other ancient races are now intermingled, the Jews have been kept separate so they could testify to the fact that our seventh day is the Bible Sabbath.

The yearly cyle has been changed. In 1562, the length of the year was changed to include the leap year. This changeover resulted in October 1582 having only 21 days! But each week remained the same seven days in lenghth. Thursday, October 4, was followed by Friday, October 15. God has divinely protect the weekly cyle down through the ages. If he had not done this, it would be impossible to keep the Sabbath holy, as He has commanded. But, because he has, we have no excuse not to. The Seventh day is Sabbath. Sunday is the First day; the day called “ Saturday” In English language is the Sabbath.

However in 108 languages of mankind, the Seventh day is called “The Sabbath!” Did you know that? Dr. William Mead Jones of London prepared a chart proving this. (A copy of this chart can be obtained for free by Harvest Time

books, google their contact). Ask for the Chart of the week (BS 28-29). English is one of the few major languages in which the Seventh Day is not called “the Sabbath”.

Here are Eight examples: Hebrew-Shabbath/Greek-Sabbaton/Swahili-Sabato/Latin-Subbatum/Arabic-Assabit/Russian-Subbota/Italian-Sabbato/Spanish-Sabado/

“By calculating the eclipses, it can be proved that no time has been lost and the creatin days were seven, Divided into 24 hours each.”—Dr Hinkley, The watchman, July 1926. (Hinkley was a well known astronomer)

“The human race never lost the septenary (seven days) sequence of week days and that the Sabbath of thse latter times comes down to us from Adam, thought the ages, without a single lapse”-- Dr Totten, Professor of Astronomy at Yale University.

“Seven has been the ancient and honored number among the nations of the earth, they have measured their time by weeks from the beginning. The origin of this was the Sabbath of God, as Moses has given the reason for it in his writings.” Dr Lyman Coleman.

“There has been no change in our calendar in past centuries that has affected in any way the cycle of the week.—James Robertson, Director Amrican Ephemeris, Navy Department, U.S, Naval Observatory, Washington, D.C, March 12, 1932.

“It can be said with assurance that not a day has been lost since Creation, and all the calendar changes notwithstanding, there has been no break in the weekly cycle.”—Dr Frank Jeffries, Fellow of the Royal Astronomical Society and Research Director of the Royal Observatory, Greenwich, England.

It is remarkable how complete is the Biblical and historical corroborating the fact that the Bible and Sabbath was given to us by God of heaven. Let us keep the Sabbath that Jesus kept-Luke 4:16. He worshipped on the Bible Sabbath, and never told us to stop keeping it. Noone else int Bible said to either. The seventh day is the Sabbath, for GOD NEVER CHANGED IT!

For a copy of the 256 page book, Beyond Picairn, explaining in remarkable detail about the Bible Sabbath, write to Harvest time book, is is an extremely readable book.

**CATHOLIC SPEAKS**

“Sunday is a Catholic institution, and its claim to observance can be defended only on Catholic principles…..From the beginning to the end of Scriptures, there is not a single passage that warrants the transfer of weekly public worship from the last day of the week to the first.”—Catholi Press, Sydney, Australia, August, 1900.

“Protestantism, in discarding the authority of the [Roman Catholic] Church, has no good reason for its Sunday theory, and ought logically to keep Saturday as the Sabbath.”—John Gilmary Shea, in the American Catholic Quarterly Review, January 1883.

“It is well to remind the Presbyterians, Baptists, Methodists, and all other Christians that the Bible does not support them anywhere in their observance of Sunday. Sunday is an institution of the Roman Catholic Church, and those who observe the day observe a commandment of the Catholic Church.”—Priest Brady, in an address, reported in the Elizabeth, N.J. News of March 18, 1903.

“**Ques**.—Have you any other way of proving that the [Catholic] Church has power to institute festivals of precept [to command holy days]?

“**Answer**.—Had she not such power, she could not have done that in which all modern religionists agree with her: She could not have substituted the observance of Sunday, the first day of the week, for the observance of Saturday, the seventh day, a change for which there is no Scriptural authority.”—Stephen Keenan, Doctrinal Catechism, p. 176.

“Reason and common sense demand the acceptance of one or the other of these two alternatives: either Protestantism and the keeping holy of Saturday or Catholicity and the keeping holy of Sunday. Compromise is impossible.”—The Catholic Mirror, December 23, 1893.

“God simply gave His [Catholic] Church the power to set aside whatever day or days she would deem suitable as Holy Days. The Church chose Sunday, the first day of the week, and in the course of time added other days, as holy days.”—Vincent J. Kelly, Forbidden Sunday and Feast-Day Occupations, p. 2.

“Protestants……accept Sunday rather than Saturday as the day for public worship after the Catholic Church made the change . … But the Protestant mind does not seem to realize that in accepting the Bible, in observing the Sunday, they are accepting the authority of the spokesman for the church, the Pope.”—Our Sunday Visitor, February 5, 1950.

“We hold upon this earth the place of God Almighty.”—Pope Leo XIII, in an Encyclical Letter, dated June 20, 1894.

“Not the Creator of Universe, in Genesis 2:1-3,—but the Catholic Church “can claim the honor of having granted man a pause to his work every seven days.”—S.C. Mosna, Storia della Domenica, 1969, pp. 366-367.

“The Pope is not only the representative of Jesus Christ, but he is Jesus Christ, hidden under veil of flesh.”—The Catholic National, July 1895.

“If Protestants would follow the Bible, they should worship God on the Sabbath Day. In keeping the Sunday they are following a law of the Catholic Church.”—Albert Smith, Chancellor of the Archdiocese of Baltimore, replying for the Cardinal, in a letter dated February 10, 1920.

“We define that the Holy Apostolic See (the Vatican) and the Roman Pontiff hold the primacy over the whole world.”—A Decree of the Council of Trent, quoted in Philippe Labbe and Gabriel Cossart, “The Most Holy Councils,” col. 1167.

“It was the Catholic Church which, by the authority of Jesus Christ, has transferred this rest [from the Bible Sabbath] to the Sunday . . Thus the observance of Sunday by the Protestants is an homage they pay, in spite of themselves, to the authority of the [Catholic] Church.”—Monsignor Louis Segur, Plain Talk about the Protestantism of Today, p. 213.

“We observe Sunday instead of Saturday because the Catholic Church transferred the solemnity from Saturday to Sunday.”—Peter Geiermann, CSSR, A Doctrinal Catechism, 1957 edition, p. 50.

“We Catholics, then, have precisely the same authority for keeping Sunday holy instead of Saturday as we have for every other article of our creed, namely, the authority of the Church . . whereas you who are Protestants have really no authority for it whatever; for there is no authority for it [Sunday sacredness] in the Bible, and you will not allow that there can be authority for it anywhere else.”—The Brotherhood of St. Paul, “The Clifton tracts,” Volume 4, tract 4, p. 15.

“The Church changed the observance of the Sabbath to Sunday by right of the divine, infallible authority given to her by her founder, Jesus Christ. The Protestant, claiming the Bible to be the only guide of faith, has no warrant for observing Sunday. In this matter the Seventh-day Adventist is the only consistent Protestant.”—The Catholic Universe Bulletin, August 14, 1942, p. 4.

The Bible is your only safe guide. Jesus can help you obey it. Trust God’s Word more than man’s traditions.

**THE PROTESTANTISM SPEAKS OUT**

**BAPTIST**: “There was and is a command to keep holy the Sabbath day,: but that Sabbath day was not Sunday. It will however be readily said, and with some show of triumph, that the Sabbath was transferred from the seventh to the first day of the week, with all its duties, privileges and sanctions. Earnestly desiring information on this subject, which I have studied for many years, I ask, where can the record of such a transaction be found? Not in the New Testament—absolutely not. There is no scriptural evidence of the change of the Sabbath institution from the seventh to the first day of the week.”—Dr. E.T. Hiscox, author of the Baptist Manual.

**CONGREGATIONALIST**: “It is quite clear that however rigidly or devot-: edly we may spend Sunday, we are not keeping the Sabbath . . The Sabbath was founded on a specific divine command. We can plead no such command for the observance of Sunday . . There is not a single line in the New Testament to suggest that we incur any penalty by violating the supposed sanctity of Sunday.”—Dr. R.W. Dale, The Ten Commandments, pp. 106-107.

**PROTESTANT EPISCOPAL**: “The day is now changed from the seventh AL: to the first day . . but as we meet with no Scriptural direction for the change, we may conclude it was done by the authority of the church.”—“The Protestant Episcopal Explanation of the Catechism.

**BAPTIST**: “The Scriptures nowhere call the first day of the week the: Sabbath . . There is no Scriptural authority for so doing, nor of course, any Scriptural obligation.”—The Watchman.

**PRESBYTERIAN**: **YTERIAN**: “There is no word, no hint in the New Testament about YTERIAN: abstaining from work on Sunday. The observance of Ash Wednesday, or Lent, stands exactly on the same footing as the observance of Sunday. Into the rest of Sunday no Divine Law enters.”—Canon Eyton, Ten Commandments.

**ANGLICAN**: **ANGLICAN**: “And where are we told in the Scriptures that we are to ANGLICAN: keep the first day at all? We are commanded to keep the seventh; but we are nowhere commanded to keep the first day.”—Isaac Williams, Plain Sermons on the Catechism, pp. 334, 336.

**METHODIST**: “It is true that there is no positive command for infant: baptism. Nor is there any for keeping holy the first day of the week. Many believe that Christ changed the Sabbath. But, from His own words, we see that He came for no such purpose. Those who believe that Jesus changed the Sabbath base it only on a supposition.”—Amos Binney, Theological Compendium, pp. 180-181.

**EPISCOPALIAN**: "We have made the change from the seventh to the ALIAN: first day, from Saturday to Sunday, on the authority of the one holy, catholic, apostolic church of Christ."—Bishop Seymour, Why We Keep Sunday.

**SOUTHERN BAPTIST**: "The sacred name of the seventh day is Sab-: bath. This fact is too clear to require argument [Exodus 20:10, quoted] . . On this point the plain teaching of the Word has been admitted in all ages . . Not once did the disciples apply the Sabbath law to the first day of the week,—that folly was left for a later age, nor did they pretend that the first day supplanted the seventh."—Joseph Judson Taylor, The Sabbatic Question, pp. 14-17, 41.

**AMERICAN CONGREGATIONALIST**: "The current notion, that Christ and: His apostles authoritatively substituted the first day for the seventh, is absolutely without any authority in the New Testament."—Dr. Lyman Abbot, Christian Union, June 26, 1890.

**CHRISTIAN CHURCH: CHRISTIAN CHURCH**: "Now there is no testimony in all the oracles of CHRISTIAN CHURCH: heaven that the Sabbath is changed, or that the Lord's Day came in the room of it."—Alexander Campbell, Reporter, October 8, 1921.

**DISCIPLES OF CHRIST**: "There is no direct Scriptural authority for des-: ignating the first day 'the Lord's Day.'"—Dr. D.H. Lucas, Christian Oracle, January 23, 1890.

**BAPTIST**: "To me it seems unaccountable that Jesus, during three years': discussion with His disciples, often conversing upon the Sabbath question, discussing it in some of its various aspects, freeing it from its false [Jewish traditional] glosses, never alluded to any transference of the day; also, no such thing was intimated. Nor, so far as we know, did the Spirit, which was given to bring to their remembrance all things whatsoever that He had said unto them, deal with this question. Nor yet did the inspired apostles, in preaching the gospel, founding churches, counseling and instructing those founded, discuss or approach the subject.

"Of course I quite well know that Sunday did come into use in early Christian history as a religious day, as we learn from the Christian Fathers and other sources. But what a pity that it comes branded with the mark of paganism, and christened with the name of the sun god, then adopted and sanctified by the Papal apostasy, and bequeathed as a sacred legacy to Protestantism."—Dr. E.T. Hiscox, report of his sermon at the Baptist Minister's Convention, New York Examiner, November 16, 1893